# Mafundisho juu ya Biblia

# AGANO JIPYA

## MATAYO – MATENDO

## Maelezo ya
## Maandiko Matakatifu
## kwa Waamini

**Mwandishi : William MacDonald**

~~~~~~

**Mtengenezaji wa Maneno ya Mbele: Arthur Farstad**

Everyday Publications Inc.
Port Colborne, ON L3K 6A6
Canada
~~~~~~

Traduit de l'anglais
par G. I. Harlow, 2011
avec collaboration de M. et J. Wolcott

Copyright © 2012
par Everyday Publications, Inc.
310 Killaly Street West
Port Colborne, ON L3K 6A6
Canada

ISBN 978-0-88873-157-9

*Imprimé aux Etats-Unis d'Amérique*

# Fahirisi


Majina ya Vitabu vya Agano Jipya 4
Utangulizi wa Mwandishi 5
Namna gani kitabu hiki kiliandikwa 5
MLANGO KWA AGANO JIPYA 6
MLANGO KWA VITABU VYA HABARI NJEMA 8
**Matayo** **11**
Mafundisho juu ya Ufalme wa Mbinguni 19
Mafundisho juu ya Habari Njema 26
Mafundisho juu ya Mwamini na Sheria 30
Mafundisho juu ya Kuachana na Kuoa tena 33
Mafundisho juu ya Kufunga Chakula 38
Mafundisho juu ya Sabato 65
**Marko** **145**
**Luka** **211**
**Yoane** **325**
**Matendo** **453**
Mafundisho juu ya Maombi ndani ya Kitabu cha Matendo 460
Mafundisho juu ya Kanisa Nyumbani 471
Mafundisho juu ya Mkristo na Serikali 481
Mafundisho juu ya Ubatizo wa Mwamini 491
Mafundisho juu ya Utumishi wa Kila Mwamini kanisani 493
Mafundisho juu ya Utaratibu wa Kueneza Habari Njema 512
Mafundisho juu ya haki ya Kanisa Kujitawala Yenyewe 517
Mafundisho juu ya Maongozi ya Mungu 519
Maongozi juu ya Maajabu 521
Mafundisho juu ya Habari Njema ikihubiriwa kwa pahali namna namna 527
Mafundisho juu ya Habari za Kitabu cha Matendo 556

# Majina ya Vitabu vya Biblia

## Vitabu vya Agano Jipya

| Jina | Ufupisho |
|---|---|
| Matayo | Mt. |
| Marko | Mk. |
| Luka | Lk. |
| Yoane | Yn. |
| Matendo | Mdo. |
| Waroma | Rom. |
| 1 Wakorinto | 1 Kor. |
| 2 Wakorinto | 2 Kor. |
| Wagalatia | Gal. |
| Waefeso | Efe. |
| Wafilipi | Flp. |
| Wakolosayi | Kol. |
| 1 Watesalonika | 1 Tes. |
| 2 Watesalonika | 2 Tes. |
| 1 Timoteo | 1 Tim. |
| 2 Timoteo | 2 Tim. |
| Tito | Tit. |
| Filemono | Flm. |
| Waebrania | Ebr. |
| Yakobo | Yak. |
| 1 Petro | 1 Pet. |
| 2 Petro | 2 Pet. |
| 1 Yoane | 1 Yn. |
| 2 Yoane | 2 Yn. |
| 3 Yoane | 3 Yn. |
| Yuda | Yud. |
| Ufunuo | Ufu. |

## Vitabu vya Agano la Kale

| Jina | Ufupisho |
|---|---|
| Mwanzo | Mwa. |
| Kutoka | Kut. |
| Walawi | Law. |
| Hesabu | Hes. |
| Kumbukumbu la Torati | Tor. |
| Yosua | Yos. |
| Waamuzi | Amu. |
| Ruta | Rut. |
| 1 Samweli | 1 Sam. |
| 2 Samweli | 2 Sam. |
| 1 Wafalme | 1 Fal. |
| 2 Wafalme | 2 Fal. |
| 1 Mambo ya Siku | 1 Sik. |
| 2 Mambo ya Siku | 2 Sik. |
| Ezra | Ezr. |
| Nehemia | Neh. |
| Esiteri | Est. |
| Yobu | Yob. |
| Zaburi | Zab. |
| Mezali | Mez. |
| Mhubiri | Mhu. |
| Wimbo wa Solomono | Wim. |
| Isaya | Isa. |
| Yeremia | Yer. |
| Maombolezo | Omb. |
| Ezekieli | Eze. |
| Danieli | Dan. |
| Hosea | Hos. |
| Yoeli | Yoe. |
| Amosi | Amo. |
| Obadia | Oba. |
| Yona | Yon. |
| Mika | Mik. |
| Nahumu | Nah. |
| Habakuki | Hab. |
| Zefania | Zef. |
| Hagai | Hag. |
| Zekaria | Zek. |
| Malaki | Mal. |

# UTANGULIZI WA MWANDISHI

Kusudi la Kitabu hiki cha *Mafundisho juu ya Biblia kwa Waamini* ni kusaidia Mkristo kujifunza Biblia na kuendelea kujuana na Maandiko Matakatifu. Lakini hakuna kitabu cha Mafundisho kinachoweza kukomboa faida ya Biblia yenyewe. Kinaweza kueleza tu maana yake na kusaidia msomaji kufahamu maneno anayosoma yeye mwenyewe ndani ya Maandiko Matakatifu. Ninaamini kabisa ya kwamba Mkristo ye yote anayedumu kusoma na kujifunza Neno la Mungu anaweza kugeuka "mfanya kazi asiyeona haya, akifasiri vema neno la kweli" (2 Tim. 2:15).

Lakini kujua tu maneno ya Biblia hakutoshi. Ni lazima kwa msomaji kutii mafundisho yake ndani ya maisha yake ya kila siku. Kwa sababu hii mwandishi wa kitabu hiki cha Mafundisho anajaribu sana kuonyesha namna gani msomaji anaweza kuwa *mtendaji* wa Neno la Mungu, si *msikiaji* tu.

Msomaji akisoma kitabu hiki cha Mafundisho peke yake, pasipo Biblia, kitabu hiki hakitamsaidia, lakini kitageuka mtego kwake. Kitakuwa na faida tu kama kikiongeza hamu yake kutafuta Maandiko yeye mwenyewe na kutii maagizo ya Bwana.

Ninaomba Roho Mtakatifu, aliyeongoza kuandika kwa Biblia, afungue na kutia nuru nia ya msomaji wakati anapojitoa kwa neno hili zuri zaidi – kujua Mungu kwa njia ya Neno lake.

## Namna gani kitabu hiki kiliandikwa

Vitabu vingi vimeandikwa kueleza maana ya Biblia kwa njia mbalimbali, na kwa makusudi mbalimbali. Vingine vinaieleza kila neno moja moja, na vingine vinaieleza sura kwa sura.

Maelezo ya vitabu vingine hayapatani na maana ya kweli ya Neno la Mungu.

Ndani ya kitabu hiki cha **"Mafundisho ya Biblia"** kusudi la mwandishi William MacDonald ni

1. kueleza maana ya Biblia waziwazi, hata maneno yale yaliyo ngumu kufahamu.
2. kuongoza msomaji kujuana na kupendana na Bwana Yesu Kristo sana, na kugeuka *mfuata na mtumishi* wake mwaminifu.

**Unaweza kutumika na kitabu hiki kwa njia mbalimbali.**

1. Unaweza *kusoma nusu nusu* ya mafundisho ndani ya sura mbalimbali na kuonja utamu wake bila kufuata utaratibu fulani.

2. Labda wakati unaposoma Neno la Mungu, unakuta *mashairi magumu* ambayo yanakushinda kabisa kufahamu. Maelezo ndani ya kitabu hiki yatakusaidia sana.

3. *Elimu ya dini* – labda unataka kujua mafundisho ya Biblia juu ya neno fulani, kama sabato, ubatizo, haki ya Mungu. Ndani ya Tafsiri kwa ukurasa 3 utaona mafundisho juu ya maneno 17 ya namna hii.

4. *Kitabu fulani katika Biblia* – Labda watu wa kanisa lako, au katika Ecole du dimanche wamechagua kujifunza barua moja ya Agano Jipya pamoja. Utapata faida kubwa kwa roho yako na kuweza kusaidia watu wengine vilevile kama ukijifunza kila juma mbele ya kusanyiko lenu mafundisho yanayopatikana ndani ya kitabu hiki.

5. *Kitabu kizima* – Kwa mwisho ingepasa kila Mkristo kusoma Biblia nzima. Utakutana na mashairi magumu mara kwa mara, lakini kitabu hiki cha Mafundisho kitakusaidia sana kuyafahamu.

# MLANGO KWA AGANO JIPYA

*"Maandiko haya ya Agano Jipya yana faida kubwa kupita ufahamu wetu, kwa maneno ya historia, na roho. Kristo wa Unabii wa Agano la Kale anageuka Kristo wa Historia ndani ya vitabu vya Habari Njema; Kristo wa Uzoevu wa Maisha ndani ya Barua za Agano Jipya; na Kristo ndani ya Utukufu ndani ya Ufunuo."*

## I. Jina la "Agano Jipya"

Mbele ya kujiingiza kabisa ndani ya kujifunza habari za kitabu hiki, ni vizuri tuwaze kwanza juu ya maneno mengine ya Kitabu hiki Kitakatifu tunachoita "Agano Jipya."

Kweli kitabu hiki ni mapatano, ndiyo *agano* la Mungu na watu wake.

Kinaitwa Agano *Jipya* kuonyesha kwamba ni namna nyingine na Agano la Kale, ndilo Agano la zamani.

Mungu aliongoza kuandika Maagano mbili yote, na kwa sababu hii yana faida kwa Wakristo wote. Lakini hatushangai kuona kwamba mwamini wa Kristo anageuka kupita kwa sehemu ile ya Biblia inayopasha zaidi juu ya Bwana na kanisa lake, na inayofundisha namna gani anataka wanafunzi wake kuishi.

Augustine alionyesha vizuri ya kwamba

Agano Jipya lilifichwa ndani ya
Agano la Zamani;
Agano la Zamani linafunuliwa
ndani ya Agano Jipya.

## II. Kanuni ya Agano Jipya

Neno hili *kanun*i ni tafsiri ya *kanon* kwa Kiyunani. Ni kama kipimo cha maneno. Kanuni ya Agano Jipya ndiyo mkusanyo wa vitabu vilivyoandikwa kwa maongezi ya Mungu. Tunaweza kujua kama inafaa kwa *vitabu hivi tu* kuwa ndani ya kanuni, au kwamba inapasa vitabu hivi vyote 27 kuwa sehemu yake? Kulikuwa na maneno mengine yaliyoandikwa na Wakristo kwa wakati ule (hata maandiko ya mafundisho ya uwongo). Namna gani tunaweza kujua kwamba maandiko yale 27 yanafaa kuwa ndani ya kanuni?

Tunasikia mara nyingi ya kwamba kuna baraza ya kanisa karibu na 400 A.D. waliokusanya majina ya vitabu ndani ya kanuni. Lakini vitabu hivi vilikuwa *sehemu ya kanuni* mara moja nyuma ya kuandikwa. Wanafunzi wenye kuogopa Mungu na wenye ufahamu walitambua maandiko matakatifu mara moja, kama Petro alivyotambua maandiko ya Paulo (2 Pet. 3:15, 16). Lakini hawakupatana juu ya vitabu vingine (Yuda, 2 na 3 Yoane, kwa mfano) kwa wakati.

Kwa kawaida, kama kitabu kiliandikwa na mtume, kama Matayo, Petro, Yoane, au Paulo, au mmoja wa wale waliotumika pamoja na mitume, hakuna shaka ya kwamba kilikuwa sehemu ya kanuni.

Baraza waliotambua kanuni yetu waliyakinisha maneno yaliyokwisha *kukubaliwa* na watu kwa miaka mingi sana. Baraza hawakukusanya orodha ya *vitabu vilivyoandikwa na maongozi ya Mungu,* lakini waliandika orodha ya *majina ya vitabu vilivyoandikwa kwa maongozi ya Mungu.*

## III. Waandishi

Mwandishi wa Agano Jipya ni Mungu Roho Mtakatifu. Ni yeye aliyeongoza

Matayo, Marko, Luka, Yoane, Paulo, Yakobo, Petro, na mwandishi wa Waebrania tusiyejua jina lake. Lakini liliandikwa na watu hawa vilevile. Haifai kusema kwamba kwa sehemu liliandikwa na watu, na kwa sehemu na Mungu. Njia nzuri zaidi kueleza neno hili ni kusema ni maandiko ya Mungu na watu pamoja kwa saa moja. Roho Mtakatifu alizuiza waandishi wa binadamu kuandika maneno yasiyo kweli. Hivi maandiko yao ya kwanza yalikuwa bila makosa wala upungufu.

Kwa kutusaidia kufahamu neno hili, tunaweza kusawanisha Neno (Biblia iliyoandikwa na Mungu pamoja na watu), na Neno Hai – ndiye Bwana wetu Yesu Kristo. Yeye si mtu kwa sehemu, na Mungu kwa sehemu. Yeye ni Mungu mkamilifu, pamoja na mtu mkamilifu. Kwa sababu ya uungu wake haikuwezekana kwaye kuanguka au kufanya zambi hata kidogo.

## IV. Tarehe

Karibu miaka elfu moja ilihitajiwa kuandika Agano la Kale (karibu 1400–400 av. J.C.). Agano Jipya liliandikwa ndani ya muda wa miaka 50 tu (50–100 A.D.)

Namna vitabu vinavyofuatana katika Agano Jipya ni vizuri sana kwa kanisa kwa kila wakati. Vinaanza na habari za maisha ya Kristo, vinaendelea na habari za kanisa, na mafundisho kwa kanisa, na mwishoni vinafunua habari za kuja za kanisa, na za dunia. Lakini vitabu hivi havikuandikwa kwa utaratibu huu. Viliandikwa kwa wakati vilipohitajiwa. Tunafikiri vitabu vya kwanza viliandikwa kwa makanisa yaliyosimamishwa kwanza, ndizo Barua ya Yakobo, kwa Wagalatia, na kwa Watesalonika, na viliandikwa karibu na mwaka 96 A.D.

Vitabu vya Habari Njema vilifuata, kwanza Matayo, au labda Marko, nyuma yake Luka, kisha Yoane. Kitabu cha mwisho ni Ufunuo, karibu na mwisho wa miaka mia moja ya kwanza A.D.

## V. Muhtasari

Vitabu vya Agano Jipya vinaweza kujumlishwa hivi:

*Vitabu vya historia*
- Vitabu vine vya Habari Njema
- Matendo

*Vitabu vya Barua*
- Barua za Paulo
- Barua nyingine

*Kitabu cha mwisho*
- Ufunuo

Mkristo anayefahamu mafundisho ya vitabu hivi vizuri "ametengenezwa kabisa kwa kila tendo jema" (2 Tim. 3:17).

Tunaomba kitabu hiki kiweze kusaidia waamini wengi kuwa watumishi wa faida kubwa kwa Bwana.

## VI. Lugha

Agano Jipya liliandikwa kwa namna ya Kiyunani ambayo Wayunani walitumika nayo kila siku. Kiliitwa *koine* vilevile. Kwa njia ya majeshi ya Alesanduro, mfalme mkubwa, watu wa inchi nyingi nyingine walisema lugha hii.

# MLANGO KWA VITABU VYA HABARI NJEMA

*"Vitabu vya Habari Njema ni Malimbuko ya maandiko yote."* – Origen

## I. Vitabu vyetu vitukufu vya Habari Njema

Vitabu hivi ni namna nyingine na vitabu vyote vingine vilivyoandikwa. Ndani yao ni habari za maisha ya watu wengine, mezali juu ya mambo mbalimbali, na sehemu za hotuba nyingi za Bwana wetu, na mazungumuzo yake na watu.

Walimu wengine wa uwongo waliandika vitabu ambavyo waliita habari njema, na kufundisha maneno yasiyokuwa kweli. Lakini kwa karibu miaka elfu mbili Wakristo wa kweli wametambua vitabu vilivyoandikwa na Matayo, Marko, Luka, na Yoane tu, kuwa sehemu ya Maandiko Matakatifu.

## II. Mifano Mine

Wakristo wengi wanafikiri mifano ya vitabu vine vya Habari Njema minalingana na mifano mine ya vitabu vya Ezekieli na Ufunuo. Mifano hii ndiyo simba, ngombe ndume (au ndama ya ngombe), mwanamume na tai. Simba inatufikirisha Habari Njema ya Matayo, ndiyo Habari Njema ya Simba ya Yuda. Ngombe ndume ni nyama ya kubeba mizigo na kutumika kazi, na inatufikirisha Marko, Habari Njema ya Mtumishi. Mwanamume anatufikirisha sana Luka, Habari Njema ya Mwana wa Watu. Ndani ya kitabu kimoja cha mafundisho tunasoma kwamba tai ni "mfano wa Yoane, mwenye mawazo ya mbingu na roho."[1]

## III. Wasomaji namna ine

Elezo zuri zaidi la neno hili ni ya kwamba kwa njia ya vitabu hivi vine vya Habari Njema, Roho Mtakatifu alijaribu kusema na roho za watu namna ine. Namna hizi ine za watu wanaishi kwa wakati wa sasa vilevile.

Watu wote wanakubali kwamba Matayo aliandika zaidi kwa Wayuda. Alitaja mashairi au sehemu za mashairi toka Agano la Kale. Hotuba zake, na kizazi chake zinatufikirisha vivyo hivyo.

Ni kama Marko alikuwa katika mji mkubwa wa ufalme, ndio Roma, wakati alipoandika Habari Njema yake. Hivi aliandika zaidi kwa Waroma, na kwa milioni za watu wanaofanana nao wanaopenda matendo kupita mawazo. Hivi ndani ya Habari Njema yake tunasoma juu ya maajabu mengi na mifano michache. Hakuna habari za kizazi ndani ya Habari Njema hii, kwani Waroma hawakuweza kuweka roho juu ya kizazi Kiyuda cha Mtumishi.

Inaonekana wazi kwamba Luka aliandika kwa Wayunani na kwa Waroma, wengi waliopenda picha na maandiko ya Wayunani.

Inabaki Yoane. Habari Njema yake iliandikwa kwa watu wote. Ndani yake kuna maneno ya kusaidia kila mtu. Inatangaza njia ya wokovu kwa wasioamini, na mafundisho ya ndani ndani ya imani ya Wakristo.

## IV. Mifano mine mingine

Kuna mifano mitamu mine mingine ndani ya Agano la Kale ya maneno yanayopatana na mifano ya vitabu vine vya Habari Njema.

"Tawi" ni jina la Bwana wetu ndani ya mashairi haya:

"… Daudi TAWI … Mfalme" (Yer. 23:5,6)

"Mtumwa … TAWI" (Zek. 3:8)

" … Mtu … TAWI" (Zek. 6:12)

"Tawi la BWANA (Yehova) (Isa. 4:2)

Kuna "Tazama" ine vile vile ndani ya Agano la Kale zinazopatana kabisa na vitabu vya Habari Njema:

"Tazama, mfalme wako" (Zek. 9:9).

"Tazama, mtumishi wangu" (Isa. 42:1)

"Tazama, mtu" (Zek. 6:12)

"Tazameni Mungu wenu" (Isa. 40:9).

Rangi ine za nguo ndani ya hema ya Agano la Kale, na maana yao zinatufikirisha Bwana wetu kwa njia ine:

*Zambarau*, ndiyo rangi ya *Matayo,* Habari Njema ya Mfalme, kama tunavyoona ndani ya Amu. 8:26.

*Nyekundu* ni rangi watu waliyopata zamani kwa njia ya kuponda namna moja ya kidudu. Inatufikirisha Marko, Habari Njema ya mtumwa, "mdudu wala si mtu" (Zab. 22:6).

*Meupe* inasema juu ya matendo ya haki ya watakatifu (Ufu. 19:8). Habari Njema ya *Luka* inaonyesha wazi sana utu mkamilifu wa Kristo.

*Samawi* inatufikirisha rangi ya mbingu tunayoona na macho (Kut. 24:10), mfano mzuri sana wa uungu wa Kristo ndani ya Habari Njema ya Yoane.

## V. Utaratibu na Maana

Maneno tunayosoma ndani ya Habari Njema hayakuandikwa kila mara kufuatana na namna yalivyotokea. Vizuri tukumbuke ya kwamba Roho Mtakatifu alichagua kufunga na kuandika habari za mafundisho fulani pamoja.

Neno hili linatusaidia kufahamu kwa sababu gani maandiko ya Habari Njema tatu yanafuatana ndani ya habari nyingi, lakini habari zao ni mbalimbali kidogo juu ya maisha na masemo ya Bwana wetu mara nyingine. Habari Njema ya Yoane ni namna nyingine na Matayo, Marko na Luka, kwa sababu Yoane hakutaka kuandika tena habari zilizokwisha kuandikwa na waandishi wale wengine. Maandiko yake ni zaidi juu ya mafundisho ya roho.

## VI. Sababu ya tofauti katika Habari Njema za Matayo, Marko na Luka

Kwa sababu gani maneno mengine yanayoandikwa ndani ya vitabu hivi ni sawasawa kabisa, lakini kwa maneno mengine maandiko yao ni mbalimbali? Neno hili halifazaishi wala kusumbusha waamini wa kweli. Kuna watu wengi waliotoa maelezo mbalimbali kwa neno hili, lakini hakuna msingi ndani ya Maandiko Matakatifu kwa maelezo yao yasiyopatana na kweli ya Mungu mara nyingine.

Jibu zuri zaidi ndilo masemo ya Bwana Yesu mwenyewe ndani ya Yoane 14:26: "Lakini Msaidizi, Roho Mtakatifu, ambaye Baba atatuma kwa jina langu, yeye atawafundisha ninyi yote, na kuwakumbusha ninyi yote ambayo niliwaambia ninyi."

Ni Roho Mtakatifu aliyeongoza kuandika kwa habari za mwanzo wa Luka (Lk. 1:1), naye alifunua kweli nyingine, ona 1 Kor. 2:13).

Hivi tukikuta habari zilizoandikwa na waandishi wa vitabu vya Habari Njema si sawasawa kila mara, vizuri tufahamu kwamba kuna sababu kwa neno hili. Kwa mfano ndani ya Matayo, Habari Njema iliyokuwa zaidi kwa Wayuda, watu wawili waliponyeshwa (mpofu na mwenye pepo) kwani sheria iliagiza washuhuda kuwa wawili au watatu. Marko na Luka waliandika juu ya kuponyeshwa kwa mtu yule aliyeonekana, ndiye mpofu Baratimayo.

Kufanana kwa mashairi mengine kuna maana na mafundisho makubwa.

Ni kama Luka 6:20-23 ni karibu sana sawa na hotuba ya Yesu mlimani katika Matayo 5, lakini kwa Luka 6:17 Bwana alikuwa ameshuka kwa pahali pa uwanda. Sifa za heri kwa Matayo zinaonyesha tabia njema ya wenyeji kamili wa ufalme, lakini ndani ya Luka tunaona zaidi maisha na mwenendo wa wanafunzi wa Kristo.

Luka 6:40 na Matayo 10:24 yanafanana sana, lakini ndani ya Matayo, Yesu

ndiye Mwalimu na sisi ni wanafunzi wake. Ndani ya Luka, mwenye kufanya wanafunzi ni mwalimu, na yule ambaye anamfundisha ni mwanafunzi wake. Matayo 7:22 ni juu ya utumishi kwa Mfalme. Luka 13:25-27 ni juu ya ushirika pamoja na Bwana.

Luka 15:4-7 ni mashitaki makali ya Wafarisayo, lakini Matayo 18:12,13 yanaonyesha mapendo ya Mungu kwa watoto.

Wakati waamini tu walipokuwa pamoja na Yoane Mbatizaji, Yoane alisema, "Atawabatiza ninyi na Roho Mtakatifu" (Mk. 1:8; Yn. 1:33). Wakati kulipokuwa na wasioamini, na zaidi Wafarisayo, pamoja na waamini, alisema, "Atawabatiza ninyi na Roho Mtakatifu na kwa moto" (ubatizo wa hukumu) (Mt. 3:11; Lk. 3:16).

Hivi hakuna mabishano hata kama habari nyingine namna hii ni mbalimbali kidogo. Ni mbalimbali na kusudi, na yanasaidia mwamini kukaa kuwaza sana juu ya Maneno Matakatifu ya Mungu.

# HABARI NJEMA KAMA ALIVYOANDIKA
# MATAYO

## Utangulizi

*Habari Njema kama ilivyoandikwa na Matayo, ndiyo mwingilio mzuri sana kwa Agano Jipya toka Agano la Kale.*

### I. Nafasi ya pekee katika Kanuni

Habari Njema ya Matayo inakutanisha Agano la Kale na Agano Jipya. Shairi la kwanza linaturudisha kwa baba mzee wa watu wa Mungu katika Agano la Kale, ndiye Abrahamu, na kwa mfalme *mkubwa* wa kwanza wa Israeli, ndiye Daudi. Inataja mashairi mengi ya Maandiko Matakatifu yaliyoandikwa kwa Kiebrania, nayo ni kitabu kilichowekwa kwanza ndani ya Agano Jipya. Kwa sababu ya maneno haya Matayo ndipo pahali pazuri kuanza kujulisha watu wa dunia habari za Kristo.

Kwa miaka mingi Habari Njema ya Matayo ilikuwa kwa pahali pa kwanza, mbele ya Marko, Luka na Yoane, kwa sababu watu waliamini *iliandikwa* kwanza. Vilevile namna habari zilivyoandikwa na Matayo zinafuatana vizuri, na hivi zinafaa kwa kusoma kanisani. Kwa sababu hii watu walipenda Matayo kupita Habari Njema nyingine, lakini watu walipenda Yoane sana vilevile.

Si neno la lazima kuamini ya kwamba Habari Njema ya Matayo iliandikwa kwanza. Lakini zaidi ya Wakristo wa kwanza walikuwa Wayuda, ndio watu wengi sana. Ingekuwa akili njema kusaidia mahitaji ya roho ya Wakristo hawa kwanza.

### II. Mwandishi

Ilionekana wazi kwa watu wote zamani ya kwamba Matayo, mtoza kodi, aliyeitwa Lawi vilevile, aliandika Habari Njema ya kwanza.

Waandishi wengine wa zamani, ndio Justin Martyr, Dionysius wa Korinto, Teofilo wa Antiokia, na Athenagoras, wa Atene walifikiri vivyo.

Labda Matayo alihubiri kwa miaka kumi na mitano katika Palestine, kisha alikwenda kuhubiri Habari Njema katika inchi nyingine. Labda ndani ya mwaka 45 A.D. aliachia Wayuda waliokwisha kuamini Yesu mwandiko wa upesi wa Habari Njema yake (au hotuba za Yesu tu), na kwa wakati wa nyuma alitimiza maandiko haya kwa watu wote.

Namna Habari Njema hii ilivyoandikwa inashuhudu ya kwamba iliandikwa na Myuda mwenye kupenda Mungu na Agano la Kale, na aliyekuwa mwandishi mzuri. Akiwa mwenye kutumikia Waroma angejua lugha yao na alijua lugha ya watu wake vilevile, ndiyo Kiaramaic. Ndani ya Habari Njema hii tunasoma habari za hesabu, mifano juu ya mali, vivyo hivyo, mambo yaliyokuwa kazi ya kila siku kwa mtoza kodi.

Hata hivi walimu wengi kwa wakati wa sasa wanafikiri, kwa sababu mbalimbali, ya kwamba Habari Njema ya

Marko iliandikwa kwanza, si Matayo.

### III. Tarehe

Kama ni kweli ya kwamba Matayo aliandika mwandiko wa upesi wa Habari Njema yake (au hotuba za Yesu tu) kwa lugha ya Kiaramaic kwa 45 A.D. (miaka 15 nyuma ya kurudi mbinguni kwa Yesu) wenye elimu wanafikiri kwamba alitimiza maandiko haya kwa watu wote kwa lugha ya Kiyunani kwa mwaka 50 au 55 A.D., au hata nyuma kupita.

### IV. Msingi na Jambo Kubwa

Matayo alikuwa kijana wakati Yesu alipomwita. Alikuwa Myuda na alijifunza na kufanya kazi ya mtoza kodi, lakini aliacha vyote kufuata Kristo. Kwa sababu hii alibarikiwa kwa njia ya kugeuka mmoja wa mitume kumi na wawili. Baraka nyingine ndiyo hii: alichaguliwa kuandika Habari Njema hii ambayo wenye elimu wanafikiri ni Habari Njema ya kwanza. Inaaminiwa vilevile ya kwamba Matayo na Lawi ni mtu mmoja (Marko 2:14; Luka 5:27).

Ndani ya Habari Njema yake Matayo anaonyesha ya kwamba Yesu ndiye Masiya wa Israeli, ambaye watu walimngojea kwa miaka mingi sana, na ya kwamba yeye peke yake ana haki ya kukaa juu ya kiti cha kifalme cha Daudi.

Si kusudi la kitabu hiki kuandika habari za maisha mazima ya Yesu. Kinaanza na kizazi cha Kristo na miaka yake ya kwanza, halafu kinapita kwa mwanzo wa utumishi wake wakati alipokuwa na miaka karibu makumi tatu. Matayo aliongozwa na Roho Mtakatifu kuchagua habari zile za maisha na utumishi wa Mwokozi ambazo zinamwonyesha kuwa *Mpakaliwa* wa Mungu (ndiyo maana ya *Masiya* na *Kristo*). Kitabu chenyewe kinaendelea

---

## HABARI YALIYOMO


| | | |
|---|---|---|
| 1. | KIZAZI NA KUZALIWA KWA MASIYA-MFALME | (Sura 1) |
| 2. | MIAKA YA KWANZA YA MASIYA-MFALME | (Sura 2) |
| 3. | MATAYARISHO KWA UTUMISHI WA MASIYA NA MWANZO WA UTUMISHI WAKE | (Sura 3, 4) |
| 4. | KUSIMAMISHWA KWA UTARATIBU WA UFALME | (Sura 5–7) |
| 5. | MAAJABU YA UWEZO NA NEEMA YA MASIYA NA MAWAZO YA WATU JUU YAO | (8:1–9:34) |
| 6. | MITUME YA MASIYA-MFALME WANATUMWA KWA ISRAELI | (9:35–10:42) |
| 7. | KUONGEZEKA KWA UADUI NA KUKATALIKA | (Sura 11, 12) |
| 8. | MFALME ANATANGAZA MWANZO WA UFALME WA NAMNA NYINGINE, KWA WAKATI TU, KWA SABABU YA KUKATALIWA NA ISRAELI | (Sura 13) |
| 9. | NEEMA YA MASIYA HAIPUNGUKI LAKINI UADUI WA WATU UNAONGEZEKA | (14:1–16:12) |
| 10. | MFALME ANATAYARISHA WANAFUNZI WAKE | (16:13–17:27 |
| 11. | MFALME ANAFUNDISHA WANAFUNZI WAKE | (Sura 18–20) |
| 12. | KUONYESHWA NA KUKATALIWA KWA MFALME | (Sura 21–23) |
| 13. | HOTUBA KWA MLIMA WA MZEITUNI | (Sura 24, 25) |
| 14. | MAUMIVU NA MAUTI YA MFALME | (Sura 26, 27) |
| 15. | KUSHINDA KWA MFALME | (Sura 28) |

hata habari za hukumu, mauti, maziko, ufufuko na kurudi kwa Bwana Yesu mbinguni, habari ambazo zilizo msingi kwa wokovu wa watu. Ni kwa sababu hii kitabu hiki kinaitwa Habari Njema – si kwa sababu kinafundisha namna gani wenye zambi wanaweza kupata wokovu, lakini kwa sababu kinaonyesha kazi ya Kristo kama zabihu kwa zambi, kwa njia yake inawezekana kwa wenye zambi kupata wokovu.

Kusudi la kitabu hiki cha *Maelezo ya Agano Jipya kwa Waamini* si kutafsiri kila neno, lakini kuamsha ndani ya mwamini hamu kutafuta Maandiko yeye mwenyewe, na zaidi ya yote hamu kubwa kwa kurudi kwa Mfalme.

# Maelezo

## 1. KIZAZI NA KUZALIWA KWA MASIYA-MFALME (Sura 1)

### 1. Kizazi cha Yesu Kristo (1:1-17)

Labda wasomaji wengine wangefazaika kwa sababu gani Matayo alianza kitabu chake na kizazi, ndiyo majina tu. Faida yao nini?

Tufahamu basi ya kwamba kizazi hiki kinahitajiwa kabisa kwani ni msingi wa habari zote zinazofuata. Kilihitajiwa kuonyesha ya kwamba Yesu ni mzao wa Daudi kwa njia ya sheria kwa kuweza kuhakikisha ya kwamba yeye ni Masiya-Mfalme wa Israeli. Hivi Matayo alianza maandiko yake na kushuhudu ya kwamba Yesu alikuwa mriti wa haki wa kiti cha kifalme cha Daudi.

Kizazi hiki kinaonyesha wazazi wa Yesu *Mfalme* wa Israeli kwa njia ya sheria; kizazi ndani ya Luka kinaonyesha wazazi wake kama *Mwana* wa Daudi. Kizazi cha Matayo kinaonyesha wazazi wa Yesu Mfalme kwa njia ya Solomono; ndani ya Luka tunaona Daudi kama mzazi wa mwana mwingine, ndiye Natani. Kizazi katika Matayo kinakwisha na Yosefu ambaye *alilea na kufanya Yesu mwana wake;* ndani ya Luka 3 tunaona Yesu kama Mwana *aliyezaliwa* kweli na Maria.

Miaka elfu moja mbele Mungu alifanya agano na Daudi, bila masharti, ya kwamba atampa ufalme ambao utaendelea milele, na wazao kutawala daima (Zaburi 89:4, 36, 37). Agano hili limetimizwa sasa ndani ya Kristo. Yeye ni mriti, kwa sheria, wa kiti cha kifalme cha Daudi kwa njia ya Yosefu, na mzao kabisa wa Daudi kwa njia ya Maria. Kwa sababu yeye ni hai milele ufalme wake utaendelea kwa milele, naye atatawala kwa milele kama Mwana mkubwa zaidi wa Daudi.

**1:1-15** Mwanzo wa shairi 1, **"Kitabu cha kizazi cha Kristo, Mwana wa Daudi, Mwana wa Abrahamu,"** unafanana na mwanzo wa Mwanzo 5:1: "Hiki ni kitabu cha vizazi vya Adamu." Mwanzo kinatupasha juu ya Adamu ya kwanza; Matayo kinatupasha juu ya Adamu ya mwisho. Adamu wa kwanza alikuwa mwanzo wa muumbo wa kwanza, ya dunia hii; Kristo ni mwanzo wa muumbo wa mwisho, wa roho.

Neno kubwa la Habari Njema hii ni **Yesu Kristo**. Jina la **Yesu** linamwonyesha kama Yehova-Mwokozi; na **Kristo** ("Mpakaliwa") kama Masiya wa Israeli ambaye walikuwa wamengoja kufika kwake kwa muda mrefu. **Mwana wa Daudi** linatufikirisha kazi zake mbili kama Masiya na Mfalme katika Agano la Kale. **Mwana wa Abrahamu** linasema juu ya Bwana wetu kama Yule atakayetimiza mwishoni ahadi zilizofanywa kwa mwenye kuanza taifa la Waebrania.

Kuna sehemu tatu kwa kizazi chenyewe: toka Abrahamu kufika Yese, toka Daudi kufika Yosia, na toka Yekonia kufika Yosefu. Sehemu ya kwanza inafika hata maisha ya Daudi; sehemu ya pili inapasha juu ya muda wa ufalme; sehemu ya tatu inachunga majina ya wazao wa mfalme kwa wakati wa muda wa uhamisho (av. J.-C. 586 na nyuma yake vilevile).

Ndani ya mashairi haya tunaona majina ya wanawake wane: **Tamari, Rahaba, Ruta** na Batiseba (**yule mke wa Uria**). Hili ndilo neno la kushangaza, kwa sababu haikuwa desturi kuingiza majina ya wanawake ndani ya vizazi. Zaidi ya ile wawili wa wanawake walikuwa makahaba (Tamari na Rahaba), mmoja wao alitenda uzini (Batiseba), na wawili walikuwa watu wa Mataifa (Rahaba na Ruta). Labda kwa njia ya kuingiza majina yao ndani ya kizazi hiki tunaweza kuona, kama kwa maficho, ya kwamba kuja kwa Kristo kutaleta wokovu kwa wenye zambi, neema kwa Mataifa, na ya kwamba ndani ya Kristo tofauti ya kabila na hali ya kuwa mume au mke haiko tena.

Tuone vilevile jina la mfalme **Yekonia**. Ndani ya Yeremia 22:30 Mungu alilaani mtu huyu:

> Bwana anasema hivi:
> "Andikeni habari za mtu huyu
> kwamba hana watoto,
> mtu asiyesitawi siku zake zote;
> maana hapana mtu katika wazao
> wake atakayesitawiwa,
> akikaa katika kiti cha ufalme cha
> Daudi,
> na kutawala tena katika Yuda."

Kama Yesu angalikuwa mwana wa *hakika* wa Yosefu, angalikuwa chini ya laana hili vilevile. Lakini ilikuwa lazima kwaye kuwa mwana wa Yosefu kwa njia ya sheria kusudi awe mwenye kuriti haki ya ufalme wa Daudi. Neno hili liliwezekana kwa njia ya ajabu ya kuzaliwa kwake na bikira Maria. Hivi Yesu alikuwa mriti *kwa sheria* wa kiti cha ufalme kwa njia ya Yosefu. Alikuwa Mwana *wa hakika* wa Daudi kwa njia ya Maria. Laana ya Yekonia haikuwa juu ya Maria na watoto wake kwa sababu hakuwa mzao wa Yekonia.

**1:16** Kwa njia ya Kiyunani tunafahamu kwamba **"aliyezaa"** inasema juu ya Maria, si juu ya Yosefu.

Kuna maneno mengine yaliyo nguvu kufahamu ndani ya mashairi haya:

**1:17** Matayo anasema waziwazi ya kwamba kuna sehemu tatu ndani ya kizazi hiki, na kila sehemu ina vizazi **kumi na ine** ndani yake. Lakini tunafahamu kwa njia ya Agano la Kale ya kwamba hakutaja majina yote. Kwa mfano, katikati ya Yoramu na Uzia (sh.8): Ahaziah, Yoasi, na Amazia walitawala kama wafalme vilevile (ona 2 Fal. 8–14; 2 Sik. 21–25).

Ni kama vizazi vya Matayo na Luka vinapitana wakitaja majina mawili, Saltieli na Zerubali (Matayo 1:12,13; Luka 3:27). Ni nguvu kufahamu kwa sababu gani vizazi vya Yosefu na Maria vinaungana hivi, lakini nyuma yake vinatengana tena. Na zaidi ya ile vitabu hivi viwili vya Habari Njema vinataja, kama Ezra 3:2, Zerubali kuwa mwana wa Saltieli, lakini ndani ya 1 Sik. 3:19 tunasoma kwamba Zerubali alikuwa mwana wa Pedaya.

Neno lingine ambalo linatufazaisha ni ya kwamba ndani ya Matayo kuna vizazi 27 toka Daudi kufika Yesu, lakini ndani ya Luka kuna vizazi 42. Hata kama waandishi hawa wawili wanaandika habari za vizazi vya watu mbalimbali, ni nguvu kufahamu kwa sababu gani hesabu ya vizazi ni mbalimbali hivi.

Basi inapasa msomaji wa Biblia kufikiri nini juu ya maneno haya? Kwanza, msingi wetu ni ya kwamba Biblia nzima ni Neno la Mungu. Maandiko yake yote yameongozwa na Yeye tu. Hivi hakuna

makosa ndani yake hata kidogo. Mengi ya maandiko yake yanashinda ufahamu wetu kwani yanatoka kwa Mungu.

Hivi tunaona ya kwamba tunashindwa kufahamu maneno mengine kwa sababu tuko watu wa kujua nusu tu, si kwa sababu maandiko mengine ya Biblia si kweli. Ingepasa maneno haya kutusukuma kutafuta Maandiko sana kwa kupata majibu. "Ni utukufu wa Mungu kuficha neno, lakini utukufu wa wafalme ni kutafuta neno" (Mez. 25:2).

Hata kama wenye elimu wametafuta maneno haya sana, hawakuweza kuonyesha ya kwamba maneno yaliyoandikwa ndani ya Biblia si kweli. Kuna maelezo ya akili kwa maneno haya yote yasiyopatana kwa mafikiri yetu, na maelezo haya yana maana ya faida kwa roho.

**B. Yesu Kristo amezaliwa na Maria (1:18-25)**

**1:18 Kuzaliwa kwa Yesu Kristo** kulikuwa namna nyingine na kuzaliwa kwa watu wote wengine ndani ya kizazi hiki. Pale tuliona tena na tena: "Fulani akazaa fulani," lakini sasa tunasoma juu ya kuzaliwa kwa mtoto asiyekuwa na baba. Lilikuwa shauri kwa Maria kuwa mke wa Yosefu, lakini hawajaoana bado. Kwa wakati wa Agano Jipya mume na mke walipatana kuoana, lakini hawakutimiza ndoa hii kwanza. Waliweza kuvunja mapatano haya ya kuoana kwa njia ya kuachana tu. Hata kama mume na mke waliopatana kuoana hawakukaa kwanza pamoja kufika siku ya ndoa yao, uzini kwa muda ule ulikuwa zambi mbaya sana uliostahili azabu ya mauti.

Ndani ya muda huu wa kupatana kuoa, bikira Maria alipata mimba kwa **Roho Mtakatifu; ajabu sana.** Malaika alijulisha Maria habari hizi mbele: "Roho Mtakatifu atakuja juu yako, na nguvu zake Mungu aliye juu zitakutulia kivuli" (Luka 1:35). Lakini bila shaka watu walianza kuwa na shaka juu ya Maria wakati mimba yake ilipoanza kuonekana. Tangu zamani watu hawajaona bikira akipata mimba. Wakati watu walipoona mke asiyeolewa akipata mimba, walifikiri neno moja tu, ndilo mke huyu alikuwa amezini.

**1:19** Hata **Yosefu** hakujua kwanza maana ya kweli ya mimba ya Maria. Aliweza kuwa na uchungu rohoni kwa sababu ilionekana kwamba Maria hakuwa mwaminifu kwake; na vilevile watu waliweza kufikiri Yosefu mwenyewe alikuwa amezini naye! Lakini Yosefu alipenda Maria na kwa sababu alitaka haki ifanywe, alifanya shauri kuvunja mapatano yao ya ndoa kwa siri. Alitaka kuepuka haya mbele ya watu.

**1:20** Wakati mtu huyu mpole alipofanya shauri kuchunga Maria asipate haya mbele ya watu, **malaika ya Bwana alitokea kwake katika ndoto akimwita "Yosefu, mwana wa Daudi."** Bila shaka malaika alimwita na jina hili kumkumbusha ya kwamba yeye mwenyewe alikuwa mzao wa mfalme Daudi, na kutayarisha mafikiri yake kwa kutokea kwa Mfalme-Masiya wa Israeli. Haifai kwa Yosefu kuwa na shaka juu ya kuoa **Maria**. Mimba yake ilikuwa ya **Roho Mtakatifu.**

**1:21** Halafu malaika alimwonyesha kama Mtoto atakayezaliwa atakuwa kijana au msichana, na jina lake na kazi yake. Maria atazaa **Mwana**. Ataitwa **YESU** (maana yake "Yehova ni wokovu" au "Yehova, Mwokozi"). Kupatana na jina lake, **ataokoa watu wake toka zambi zao**. Mtoto huyu alikuwa Yehova mwenyewe, akifikia dunia kwa wakati kuokoa watu toka azabu ya zambi, toka uwezo wa zambi, na mwishoni toka hata ukaribu wa zambi.

**1:22** Wakati Matayo alipoandika maneno haya alifahamu kwamba kuanza saa ile Mungu atatendea watu wa dunia namna nyingine. Unabii ambao Isaya alitoa zamani juu ya Masiya yalitimizwa kwa njia ya Mtoto wa Maria: **Maneno**

**haya yote yamekuwa litimie neno lililosemwa na Bwana kwa nabii.** Matayo aliamini kwamba alikuwa Mungu aliyesema maneno haya kwa njia ya Isaya miaka 700 au zaidi mbele ya kuzaliwa kwa Kristo.

**1:23** Unabii huu kwa Isaya 7:14 ulionyesha kwamba kuzaliwa kwa Mtoto huyu kutakuwa namna nyingine (Tazama, bikira atachukua mimba"), mtoto atakuwa kijana ("naye atazaa mwana"), na jina la mtoto ("nao watamwita jina lake Emanueli"). Matayo alieleza kwamba maana ya **Emanueli** ni **Mungu pamoja nasi**. Hatusomi kwamba Kristo aliitwa na jina hili wakati alipokuwa duniani; aliitwa "Yesu" tu kila mara. Lakini maana ya jina hili *Yesu* (ona maelezo juu ya sh.21) lina maana ya **Mungu pamoja nas**i. Labda Kristo ataitwa Emanueli wakati atakapokuja mara ya pili.

**1:24** Kwa sababu ya masemo ya malaika Yosefu hakuachana na Maria. Alikaa pamoja naye kufika saa ya kuzaliwa kwa Yesu, kisha alimwoa.

**1:25** Watu wengine wanafundisha ya kwamba Maria alikuwa bikira kwa maisha yake mazima, lakini shairi hili linaonyesha kwamba mafundisho yale si kweli hata kidogo. Kuna mashairi mengine yanayoonyesha kwamba Maria alizaa watoto kwa njia ya Yosefu, ndiyo Matayo 12:46; 13:55,56; Marko 6:3; Yoane 7:3,5; Matendo 1:14; 1 Wakorinto 9:5; na Wagalatia 1:19.

Wakati Yosefu alipooa Maria kuwa mke wake, alifanya Mtoto wa Maria kuwa mwana wake vilevile. Neno hili liligeuza Yesu mriti, kwa njia ya sheria, wa kiti cha ufalme wa Daudi. Akitii masemo ya malaika **aliita jina la** Mtoto mchanga **Yesu.**

Hivi Masiya-Mfalme alizaliwa. Yule aliye tangu milele, mwenye uwezo wote, aligeuka mtoto mchanga. Bwana wa utukufu alificha utukufu wake ndani ya mwili wa mtu, na katika yeye "utimilifu wote wa Mungu ukakaa kwa mwili" (Kol. 2:9).

## 2. MIAKA YA KWANZA YA MASIYA-MFALME (Sura 2)

### A. Waakili wanakuja kuabudu Mfalme (2:1-12)

**2:1,2** Ni nyepesi kufazaika juu ya namna matukio yalivyofuatana wakati wa kuzaliwa kwa Kristo. Ni kama shairi 1 linaonyesha kwamba Herode alijaribu kuua Yesu wakati Yosefu na Maria walipokuwa kwanza ndani ya nyumba ya kulisha ngombe, lakini habari tunazosoma ndani ya mashairi mengi mengine yanaonyesha kwamba miaka miwili ilikuwa imepita. Ndani ya shairi 11 Matayo anasema kwamba waakili waliona Yesu ndani ya nyumba. Agizo la Herode kuua watoto wasiokuwa na miaka miwili kwanza linaonyesha vilevile kwamba alitoa agizo hili nyuma ya wakati fulani tu.

**Herode** Mkuu huyu alikuwa mzao wa Esau, na kama wazao wote wa Esau alikuwa adui ya Wayuda. Aligeuka na kushika dini ya Wayuda, lakini labda hakufanya hivi na roho ya kweli lakini kusaidia utawala wake tu. **Waakili toka mashariki** walifika karibu na mwisho wa utawala wake kutafuta **Mfalme wa Wayuda**. Labda wanaume hawa walikuwa makuhani wapagano walioabudu viumbe. Kwa sababu ya akili yao na uwezo wao wa kutabiri, walichaguliwa mara nyingi kusaidia wafalme. Hatujui pahali gani walipokaa kwa mashariki, kama walikuwa watu wengapi, na kama walisafiri kwa muda gani.

**Nyota** ile **katika mashariki** iliwafahamisha kwamba mfalme alikuwa amezaliwa, nao walikuja kumwabudu. Inawezekana kwamba walijuana na unabii katika Agano la Kale juu ya kuja kwa Masiya. Labda walisikia habari za unabii wa Balama kwamba Nyota ata-

toka katika Yakobo (Hes. 24:17) na waliunganisha habari hizi na unabii wa majuma makumi saba yaliyoonyesha wakati Kristo atakapokuja mara ya kwanza (Dan. 9:24,25). Lakini zaidi tunafikiri alikuwa Mungu ambaye aliwajulisha habari hizi.

Wenye elimu wamejaribu kueleza kuonekana kwa nyota hii. Lakini kuhamahama kwa nyota hii kulikuwa namna nyingine na desturi za nyota. Ilitangulia waakili na kuwaongoza toka Yerusalema hata nyumba pahali Yesu alipokuwa (sh.9). Halafu ilibaki palepale. Lilikuwa ajabu tu.

**2:3 Wakati mfalme Herode aliposikia habari** za kuzaliwa kwa mtoto atakayekuwa mfalme wa Wayuda ali**fazaika** sana. Mtoto namna hii angeweza kuwa hatari kwa utawala wake juu ya Wayuda. Watu wa **Yerusalema pia** walifazaika vilevile. Ingalipasa watu wa mji kupokea habari hizi na furaha, lakini waliogopa zitakasirisha watawala wao Waroma ambao walichukia.

**2:4-6** Herode alikutanisha viongozi vya dini Wayuda kuulizana nao **pahali gani Kristo atakapozaliwa.** Wakubwa wa makuhani walikuwa kuhani mkubwa na wana wake (na labda watu wengine wa jamaa yake). Waandishi wa watu walikuwa wafundi wa Sheria ya Musa. Walichunga na kufundisha sheria na walifanya kazi ya waamuzi. Makuhani na waandishi walitaja Mika 5:2 mara moja, ndilo shairi lililoonyesha kwamba Betelehemu wa Yudea ndipo pahali Mfalme atakapozaliwa. Katika Mika 5:2 kwa Agano la Kale pahali pale panaitwa Betelehemu-Efurata. Kulikuwa na miji mingine katika Palestina iliyoitwa Betelehemu, na jina hili linaonyesha wazi kwamba Betelehemu huu ulikuwa katika wilaya ya Efurata ndani ya mipaka ya makabila ya Yuda.

**2:7,8 Mfalme Herode aliita waakili kwa siri** kuuliza **saa gani nyota ilionekana kwanza.** Akiwaita kwa siri ilifunua kusudi lake baya: Alihitaji kujua neno hili ili aweze kufahamu kama Mtoto gani ndiye Kristo. Akitaka kuficha kusudi lake **alituma** waakili kutafuta habari hizi na kumjulisha wakati walipokwisha kuzipata.

**2:9** Wakati waakili waliposhika njia, **nyota ambayo waliona kwa mashariki mbele** ilionekana tena. Neno hili linaonyesha kwamba nyota ile haikuwaongoza kwa safari yao nzima toka mashariki. Lakini sasa iliwaongoza na kuwafikisha kwa nyumba **pahali Mtoto alipokuwa.**

**2:10 Waakili walifurahi sana wakati walipoona nyota**. Watu hawa wa Mataifa walitafuta Kristo na bidii; Herode alifanya shauri kumwua; makuhani na waandishi hawakufikiri kwanza sana juu yake; watu wa Yerusalema walifazaika. Habari hizi zote zinaonyesha kwa ufupi namna gani Masiya atapokewa duniani.

**2:11** Wakati waakili walipoingia nyumba waliona **Mtoto pamoja na Maria, mama yake. Wakaanguka, wakamwabudu** na kumtolea **zawad**i za bei kubwa za zahabu, uvumba na manemane. Ona ya kwamba waliona Yesu pamoja na mama yake. Ilikuwa desturi kutaja mama kwanza na mtoto nyuma yake, lakini Mtoto huyu alikuwa namna nyingine, na ilipasa kumpa pahali pa kwanza. Ona vilevile mashairi 13,14, 20,21. Waakili waliabudu Yesu, *si* Maria wala Yosefu. (Matayo hakutaja Yosefu hapa, na nyuma kidogo jina lake halikuonekana tena ndani ya maandiko ya Habari Njema.) Ni Yesu anayestahili kupokea sifa na kuabudu, si Maria au Yosefu.

Hazina waakili walizoleta zina maana kubwa. **Zahabu** ni mfano wa uungu na utukufu; inatufikirisha ukamilifu wa kungaa kwake aliye Mungu. **Uvumba** ni marasi au harufu tamu; unatukumbusha

maisha yake matamu na bila zambi. **Manemane** ni majani machungu. Yanasema juu ya maumivu yake wakati atakapobeba azabu kwa zambi za dunia. Watu hawa wa Mataifa wakileta zawadi wanatukumbusha maneno ya Isaya katika 60:6. Isaya alitabiri kwamba Mataifa watafikia Masiya na zawadi, lakini alitaja zahabu na uvumba tu: "... wataleta zahabu na uvumba; na watatangaza sifa ya Bwana." Kwa nini Isaya hakutaja manemane? Kwa sababu alikuwa akisema juu ya kuja kwa pili kwa Kristo – na uwezo na utukufu. Hatateswa kwa wakati ule, hivi Isaya hakutaja manemane. Lakini Matayo alitaja manemane kwa sababu aliandika juu ya kuja kwa Kristo mara ya kwanza. Ndani ya Matayo tunasoma juu ya mateso ya Kristo; mashairi haya katika Isaya yanaonyesha utukufu wake kwa wakati wa kuja.

**2:12** Waakili walitii maonyo waliyopewa katika ndoto wasirudi karibu na Herode, wakafuata njia nyingine kurudi kwao. Hakuna mtu anayekutana na Kristo na roho ya kweli atakayerudi bila kugeuka namna nyingine. Kukutana naye kunageuza maneno yote ya maisha yetu.

### B. Yosefu, Maria, na Yesu wanakimbia kwa Misri (2:13-15)

**2:13,14** Tangu utoto wake Bwana wetu alikuwa katika hatari. Ni wazi ya kwamba alizaliwa kusudi afe – kwa saa iliyochaguliwa na Mungu. Hakuna mtu anayeishi akifanya mapenzi ya Mungu anayeweza kufa mbele ya kumaliza kazi yake. **Malaika ya Bwana** alisema na **Yosefu katika ndoto akimbilie Misri** pamoja na Yesu na mama yake kwa sababu Herode alikuwa tayari kutafuta mtoto aweze kumwua. Hivi Yosefu na jamaa yake waligeuka wakimbizi. Hatujui kama walikaa miaka mingapi katika Misri. Wakati Herode alipokufa waliweza kurudi tena kwao.

**2:15** Hivi unabii mwingine katika Agano la Kale ulitimizwa na kupata maana mpya. Mungu alikuwa amesema **kwa njia ya nabii** Hosea, **"niliita mwana wangu toka Misri**" (Hos. 11:1). Wakati unabii huu ulipotolewa kwanza, ulikuwa juu ya kuponyeshwa kwa Israeli toka utumwa kwa Misri. Lakini ulikuwa na maana nyingine vilevile – kuponyeshwa kwa Kristo na kurudi kwake kwa Israeli toka Misri.

Wakati Bwana atakaporudi duniani kutawala katika haki Misri itakuwa moja ya inchi zitakazoshiriki ndani ya baraka za utawala wa Kristo kwa miaka elfu moja (Isa. 19:21-25; Zef. 3:9,10; Zab. 68:31). Kwa sababu gani taifa hili waliokuwa adui wa Israeli tangu zamani watabarikiwa hivi? Labda ni kama alama ya asante ya Mungu kwa sababu lilikuwa kimbilio kwa Bwana Yesu?

### C. Herode anaua watoto wadogo katika Betelehemu (2:16-18)

**2:16** Wakati waakili wasiporudi **Herode** alifahamu kwamba alikuwa **amedanganywa** nao na hakuweza kutimiza shauri lake kuvumbua pahali Mfalme kijana alipokuwa. Na gazabu iliyokosa akili aliagiza watoto waume wote wasiokuwa bado na miaka miwili katika Betelehemu na kando kando kuuawa. Hatujui kama watoto wangapi walikufa. Mwandishi mmoja alifikiri walikuwa karibu makumi mbili na sita.

**2:17,18** Kilio kilichofuata uuaji wa watoto kilitimiza masemo ya **nabii Yeremia:**

"Sauti ilisikiwa katika Rama,
Kilio na maombolezo mengi,
Rakeli akililia watoto wake,
Asitake kufarijiwa,
kwa sababu hawako." (Yer. 31:15)

Ndani ya unabii huu **Rakeli** ni mfano wa Israeli wenye huzuni. Rakeli alizikwa katika Rama (karibu na Betelehemu, pahali watoto walipouawa). Wakati wazazi waliofiwa watoto walipopita

kaburi lake, ni kama Rakeli alikuwa akitoa **machozi** pamoja nao. Na Herode alijipatia aibu tu.

**D. Yosefu, Maria na Yesu wanakaa katika Nazareti (2:19-23)**

Nyuma ya mauti ya Herode **malaika ya Bwana** alimwambia **Yosefu** kwamba waliweza kurudi sasa na salama. Wakati Yosefu alipofikia **inchi ya Israeli** na kusikia kwamba mwana wa Herode, ndiye **Arkelao** alikuwa amekomboa baba yake kama mfalme wa Yudea, aliogopa kufika kule. Akikwisha kuonywa na Mungu katika **ndoto** walisafiri kwenda kwa **upande wa Galilaya** kwa kaskazini, wakapanga katika **Nazareti**.

Mara ya ine ndani ya sura hii Matayo alitukumbusha ya kwamba maneno yaliyotabiriwa zamani yalikuwa yakitimizwa. Hakutaja majina ya manabii hawa, lakini alisema kwamba walitabiri Masiya **ataitwa Mnazareti.** Kwa wakati ule mji na wenyeji wa Nazareti hawakuwa na heshima katikati ya watu wengine, na jina la Mnazareti lilikuwa jina la kuzarau. Hivi Natanaeli aliuliza, "Kitu kizuri kinaweza kutoka Nazareti?" (Yn.1:46). Hakuna shairi ndani ya Agano la Kale linalotaja jina hili wazi, lakini ndani ya Isaya 53:3 tunasoma ya kwamba "amezarauliwa na kukataliwa na watu." Shairi lingine linasema kwamba atakuwa mdudu, wala si mtu, laumu ya watu na mwenye kuzarauliwa nao (Zab. 22:6). Hivi hata kama manabii hawakutaja jina la Mnazareti, hii ilikuwa maana ya unabii wao.

Ni neno la kushangaza ya kwamba wakati Mungu mwenyezi alipofika duniani, alipewa jina la laumu. Ni heshima kwa wafuata wake kushiriki ndani ya laumu lake (Ebr. 13:13).

**3. MATAYARISHO KWA UTUMISHI WA MASIYA NA MWANZO WA UTUMISHI HUU (Sura 3,4)**

**A. Yoane Mbatizaji alitayarisha njia (3:1-12)**

Nyuma ya sura 2 na mbele ya sura 3 kulikuwa muda wa miaka 28 au 29. Matayo hakuandika juu ya maneno yaliyotokea ndani ya muda huu. Yesu alikuwa katika Nazareti kwa wakati ule akijitayarisha kwa kazi yake kubwa. Hakufanya maajabu ndani ya miaka ile, lakini alipendeza Mungu Baba yake sana (Mt. 3:17). Sura 3 inatufikisha kwa mwanzo wa kazi yake katikati ya watu.

**3:1,2** Yoane Mbatizaji alizaliwa miezi sita mbele ya Yesu, mtoto wa ndugu ya mama yake (ona Luka 1:26,36). Alitokea katikati ya watu kama mtangulizi wa Mfalme wa Israeli. Alihubiri katika **jangwa la Yudea** – inchi ya kukauka iliyoenea toka Yerusalema kufika Yorodani. Habari kubwa za mahubiri yake zilikuwa, **"Tubuni, kwa sababu ufalme wa mbinguni umekaribia!"** Mfalme atatokea nyuma kidogo, lakini atakataa kutawala watu waliofungana na zambi zao. Lazima wageuze mwenendo wao na kukiri na kuacha zambi zao. Mungu alikuwa akiwaita kutoka katika ufalme wa giza na kuingia ufalme wa mbinguni.


**UFALME WA MBINGUNI**

Ndani ya shairi 2 tunaona maneno haya "ufalme wa mbinguni" mara ya kwanza. Tutayaona mara 32 ndani ya Habari Njema hii. Haiwezekani kwa mtu kufahamu Habari Njema ya Matayo vizuri bila kufahamu maana ya maneno haya, hivi tutajaribu kueleza.

Ufalme wa Mungu ndipo pahali watu wanapokubali utawala wa Mungu. Neno hili "mbingu" linasema juu ya Mungu. Tunaona neno hili katika Danieli 4:25, pahali Danieli aliposema "Aliye juu anatawala katika ufalme wa watu." Ndani ya shairi linalofuata alisema ya kwamba "mbingu" zinatawala. Ufalme wa mbinguni ni pahali po pote watu wanaponyenyekea utawala wa Mungu.

Tunaweza kusawanisha ufalme wa

mbinguni na sanduku miwili. Ndani ya sanduku kubwa watu wote wanakiri kwamba wanajua Mungu ni Mtawala mwenyezi. Ndani ya sanduku ndogo iliyo ndani ya ile kubwa ni watu wale tu waliookolewa kweli kweli na kukiri ya kwamba wao ni wafuata wake kabisa. Tunaona neno hili ndani ya mfano wa mpandaji mbegu (Mt.13:3-9), mfano wa mbegu ya haradali (Mt. 13:31,32), na wa chachu (Mt.13:33). Watu wale tu waliozaliwa tena kweli kwa njia ya kuamini Bwana Yesu Kristo wanaweza kuingia ndani ya sanduku mdogo (Mt. 18:3).



Wakati tunapoangalia mashairi yote ndani ya Biblia juu ya ufalme pamoja tunaona kwamba unaendelea kwa hatua tano katika historia.

Kwanza kulikuwa na *unabii* juu ya ufalme ndani ya Agano la Kale. Danieli alitabiri ya kwamba Mungu atasimamisha ufalme usioharibiwa kamwe wala kushindwa na taifa lingine (Dan. 2:44). Aliona mbele vilevile ya kwamba Kristo atakuja kutawala dunia nzima (Dan. 7:13,14; ona vilevile Yer. 23:5,6).

Kwa hatua ya pili Yoane Mbatizaji, Yesu, na mitume kumi na wawili walihubiri juu ya ufalme, wakisema juu yake kwamba *ulikuwa karibu* (Mt. 3:2; 4:17; 10:7). Ndani ya Matayo 12:28, Yesu alisema "... mimi kwa Roho ya Mungu nikitoa pepo wachafu, ufalme wa Mungu umekwisha kuwafikia ninyi." Katika Luka 17:21 alisema, "ufalme wa Mungu ni ndani yenu" au katikati yenu. Ufalme ulikuwa pale kwani Mfalme mwenyewe alikuwa pale. Tutaona nyuma kwamba mara nyingine unaitwa ufalme wa Mungu na mara nyingine ufalme wa mbinguni.

Hatua ya tatu ndiyo ufalme kwa *muda wa kati*. Nyuma ya kukataliwa na taifa la Israeli Mfalme alirudia mbingu. Lakini ufalme uko hata wakati wa sasa, ndani ya mioyo ya wote ambao wanaheshimu Kristo kama Mfalme wao, pamoja na mafundisho yote aliyotoa juu ya Mlima. Mifano ya Matayo 13 inafundisha juu ya muda huu.

Hatua ya ine ya ufalme ni kuonekana kwake, au *ufunuo* wake, wakati wa utawala wa Kristo duniani kwa miaka elfu moja. Tunaona mfano wa neno hili wakati sura ya Yesu ilipogeuzwa juu ya mlima, naye alionekana katika utukufu wake kwa wakati wa utawala wake kwa wakati wa kuja (Mt. 17:1-8). Yesu alifikiri juu ya hatua hii katika Matayo 8:11 wakati aliposema "… wengi watakuja toka mashariki na toka mangaribi, na wataketi pamoja na Abrahamu na Isaka na Yakobo katika ufalme wa mbinguni."

Hatua ya mwisho ni ufalme *wa milele*. Tunasoma juu yake ndani ya 2 Petro 1:11, ". . . ufalme wa milele wa Bwana wetu, Mwokozi Yesu Kristo."

Maneno haya "ufalme wa mbinguni" ni ndani ya Habari Njema ya Matayo tu, lakini "ufalme wa Mungu" ni ndani ya Habari Njema zote ine. Maneno yanayosemwa juu ya ufalme wa mbinguni yanasemwa juu ya ufalme wa Mungu vilevile. Kwa mfano, ndani ya Matayo 19:23 Yesu alisema itakuwa nguvu kwa mtajiri kuingia ufalme wa *mbinguni.* Marko (10:23) na Luka (18:24) vilevile waliandika kwamba Yesu alisema hivi juu ya ufalme wa *Mungu.* (Ona vilevile Mt. 19:24.)

Tulisema mbele ya kwamba ufalme wa mbinguni unaonekana kwa macho,

lakini ni kitu cha ndani, cha hakika na roho vilevile. Ni vivyo hivyo na ufalme wa Mungu. Tunaona neno hili ndani ya mifano ya mpandaji mbegu (Lk. 8:4-10), mbegu ya haradali (Lk.13:18,19), na chachu (Lk. 13:20,21). Wale tu wanaozaliwa tena kweli wanaweza kuingia ufalme wa Mungu kwa roho na kweli (Yn. 3:3,5).

Neno moja lingine kwa kumaliza mafundisho haya: ufalme na kanisa si neno moja. Ufalme ulianza wakati Kristo alipoanza kazi yake katikati ya watu. Kanisa lilianza siku ya Pentekote (Matendo 2). Ufalme utaendelea kufika wakati dunia itakapoharibiwa; kanisa litaendelea kufika wakati Kristo atakapotoka mbinguni kupeleka waamini wote kwake mbinguni (1 Tes. 4:13-18). Kanisa litarudi pamoja na Kristo kama bibi-arusi yake wakati atakapokuja mara ya pili. Kwa wakati wa sasa watu walio ndani ya mviringo mdogo ulio ndani ya ule mkubwa ni ndani ya kanisa vilevile. ❖

**3:3** Tuendelee sasa na mafundisho ya Matayo 3. Ona ya kwamba Isaya alitoa unabii miaka mia saba mbele juu ya kazi ya Yoane kutayarisha njia kwa Bwana:

> "Sauti ya mtu anayelia katika
> jangwa,
> Tengenezeni njia ya Bwana,
> Nyosheni mapito katika jangwa
> kwa Mungu wetu!" (40:3).

Yoane alikuwa **sauti** ile. Taifa la Israeli lilikuwa kama **jangwa** ya kukauka kwa maneno ya roho, bila matunda. Yoane aliita watu **kutayarisha njia ya Bwana** kwa njia ya kutubu zambi zao na kuziacha, na **kunyolosha njia yake** kwa njia ya kuondosha toka maisha yao vitu vyote vilivyoweza kuzuiza Bwana asitawale katika mambo yote.

**3:4** Yoane alivaa vazi la singa za ngamia namna watu waliotumika porini walilovaa, na alikuwa na mkaba wa ngozi vilevile. Lilifanana na mavazi ya Elia (2 Waf.1:8) na labda Wayuda waamini walitambua kwamba utumishi wa Yoane ulifanana na ule wa Elia (Mal. 4:5; Lk 1:17; Mt. 11:14; 17:10-12). Yoane alikula **nzige na asali ya pori,** ndicho chakula masikini cha mtu anayeweka roho kabisa juu ya kazi yake tu na kusahau maneno watu wengine wanayofurahia.

Bila shaka kukutana na Yoane Mbatizaji kulichokoza damiri za watu sana. Alikuwa mtu asiyeweka roho juu ya vitu watu wengine wanavyotamania. Aliishi kwa maneno ya roho tu, na tunafikiri neno hili lilifahamisha watu wengine umasikini wa roho zao wenyewe, na lilikuwa kemeo la kukata roho zao juu ya mapendo yao kwa vitu vya dunia.

**3:5, 6** Watu wengi walitoka **Yerusalema, Yudea yote**, na inchi zote karibu na Yorodani kumsikia. Wengine walipokea mahubiri yake vizuri, wakabatizwa naye katika Yorodani, na kwa njia hii walionyesha kwamba walikuwa tayari kupokea na kutii Mfalme ambaye alikuwa karibu kufika.

**3:7 Wafarisayo na Wasadukayo** walifika kusikia mahubiri ya Yoane vilevile, lakini Yoane alifahamu kwamba hawakufanya hivi na roho ya kweli. Alitambua hali ya roho za **Wafarisayo**, roho za hila. Walitenda kama watu walioheshimu sheria sana, lakini ndani ya roho zao walikuwa waovu, wadanganyifu na wenye hila, wakifikiri wao ni wenye haki kabisa. **Wasadukayo** walikuwa jamii iliyoheshimiwa na watu, wenye mashaka kwa maneno ya roho, waliokana kweli nyingine kabisa, kama ufufuko wa mwili, malaika, kweli ya kwamba roho ya mtu inaishi kwa milele, na azabu ya milele. Hivi Yoane aliita Wafarisayo na Wasadukayo **uzao wa nyoka** waliotenda kama wenye kutaka **kuepuka hasira itakayokuja,** lakini wasiotubu kweli.

**3:8** Aliwaita kuhakikisha kama walitubu kweli kwa njia ya kuzaa **matunda yanayofaa na toba**. Mwalimu mmoja,

ndiye J.R. Miller, aliandika kwamba toba "inayoonekana kwa njia ya huzuni na woga na kutoa machozi machache tu ni bure. Lazima tuachane na zambi tunazokiri na kuanza kutembea katika haki na utakatifu."

**3:9** Ilipasa Wayuda kuacha kufikiri watafika mbinguni kwa sababu walikuwa wazao wa **Abrahamu**. Neema ya wokovu haipitishwi kwa njia ya kuzaa mwilini. Ingalikuwa nyepesi kwa Mungu kugeuza **mawe** katika Yorodani kuwa **watoto** wa Abrahamu, kupita kwa Wafarisayo na Wasadukayo kuokolewa.

**3:10** Kwa njia ya kusema kwamba **shoka limekwisha kuwekwa katika shina la miti,** Yoane alijulisha wasikiaji wake kwamba hukumu ya Mungu ilikuwa karibu kuanza. Kufika kwa Kristo kutapima watu wote. Wale wasiozaa matunda wataharibiwa kama mti usiozaa matunda mazuri … **unakatwa na kutupwa katika moto.**

**3:11,12** Ndani ya mashairi 7-10 Yoane alisema na Wafarisayo na Wasadukayo tu (ona shairi 7), lakini ni kama sasa alisema na watu wote, ndio wenye imani ya kweli na wale waliokosa imani. Alieleza tofauti kati ya utumishi wake na ule wa Masiya atakayetokea nyuma kidogo. Yoane alibatiza **kwa maji hata toba**, lakini **maj**i haya hayakuweza kusafisha roho ya mtu; hata mtu **akitubu na roho ya kweli**, ubatizo huu haukuweza kumpatia wokovu. Yoane alifahamu kwamba utumishi wake ulikuwa utumishi wa kutayarisha tu watu kwa kuja kwa Bwana. Masiya atakuwa mkubwa kupita na **mwenye uwezo mkubwa kupita** Yoane. Atastahili kupita, kazi yake itagusa watu wengi kupita, maana atabatiza … **kwa Roho Mtakatifu na kwa moto.**

Ubatizo **kwa Roho Mtakatifu** ni mbali na ubatizo kwa **moto.** Ubatizo wa kwanza ndio ubatizo wa baraka; ule wa pili ni ubatizo wa hukumu. Ubatizo wa Roho Mtakatifu ulitokea kwa Pentekote; ule wa hukumu utatokea kwa wakati wa kuja. Ubatizo wa kwanza ni kwa waamini wote wa kweli wa Bwana Yesu; ule wa pili utapata wasioamini wote. Ubatizo wa kwanza utakuwa alama wa kuonekana kwa Waisraeli waliokuwa wametubu kweli rohoni; ule wa pili utakuwa kwa Wafarisayo, Wasadukayo, na wote wasiotubu na roho ya kweli.

Watu wengine wanafundisha kwamba ubatizo kwa Roho Mtakatifu na ubatizo kwa moto ni neno moja. Wanafikiri ubatizo kwa moto unasema juu ya ndimi za moto zilizoonekana wakati Roho Mtakatifu alipotolewa siku ya Pentekote. Tukisoma shairi 12 hatufikiri mafundisho haya ni kweli.

Mara moja nyuma ya kusema juu ya ubatizo wa moto, Yoane alisema juu ya hukumu. Alisema juu ya Bwana kama mwenye kushika **pepeto** mkononi na akitupa nafaka juu kwa upepo. **Ngano** (ndio waamini wa kweli) inaanguka chini mara moja kwa udongo na **kupelekwa katika gala. Makanda** (wasioamini) yanabebwa na upepo kwa mwendo mdogo tu mbele ya kukusanywa na **kuteketezwa kwa moto usiozimika.** Moto ndani ya shairi 12 unasema juu ya hukumu, na shairi hili likiwa kama sehemu ya shairi 11, tunafikiri ubatizo wa moto ndio ubatizo wa hukumu.

### B. Yoane Mbatizaji anabatiza Yesu (3:13-17)

**3:13** Yesu alitembea karibu km. 96 **toka Galilaya** kufikia upande wa chini wa mto **Yorodani** aweze **kubatizwa** na Yoane. Tendo hili lilionyesha kwamba ubatizo ulikuwa neno kubwa kwa mafikiri yake na ungepasa ubatizo kuwa na maana kubwa kwa wafuata wake kwa wakati wa sasa.

**3:14,15** **Yoane** alijua kwamba Yesu hakuhitaji kutubu, kwani hakuwa na zambi. Hakutaka kumbatiza, akisema ingepasa Yesu kumbatiza yeye. Yesu

hakubisha neno hili lakini aliomba Yoane tena kumbatiza **kutimiza haki yote**. Alifikiri ni taratibu kwa yeye kushiriki kwa njia hii na Waisraeli wenye kupenda Mungu waliokuwa wakifika kupokea ubatizo wa toba.

Lakini ubatizo huu ulikuwa na maana kubwa kupita kwa Yesu. Ulikuwa mfano kwake wa namna atatimiza madai nzima ya haki ya Mungu juu ya zambi za watu. Kuingia maji ya ubatizo kulikuwa mfano wa hukumu ya Mungu kwa Kalvari. Kutoka kwake katika maji kulikuwa mfano wa ufufuko wake. Kwa njia ya mauti, kuzikwa na kufufuliwa atatimiza haki yote ya Mungu na kutayarisha njia ya haki kwa wenye zambi kuweza kuhesabiwa haki.

**3:16,17** Mara moja nyuma ya **kutoka katika maji,** Yesu aliona **Roho ya Mungu akishuka kama hua, akikuja juu yake.** Katika Agano la Kale vitu viliwekwa kwa Mungu kwa kazi fulani kwa njia ya kuvipakaa na "mafuta matakatifu ya kupakaa" (Kutoka 30:25-30). Vivyo hivyo Yesu alipakaliwa na Roho Mtakatifu kama Masiya.

Mungu Baba, Mungu Mwana na Roho Mtakatifu wote walishiriki ndani ya tukio hili takatifu. **Mwana mpendwa** alikuwa pale, **Roho** Mtakatifu kwa mfano wa **hua** alikuwa pale, na **sauti** ya Baba ilisikiwa **toka mbinguni** akibariki Yesu, akitaja shairi la Maandiko Matakatifu **"Wewe ni Mwana wangu** (Zaburi 2:7) . . . **nafsi yangu inapendezwa naye"** (Isaya 42:1). Baba alisema mara tatu toka mbinguni kuonyesha furaha na ukubali wa Mwana wake asiyekuwa na kifani; hapa, na kwa Matayo 17:5 na Yoane 12:28.

### C. Yesu anajaribiwa na Shetani (4:1-11)

**4:1** Labda tunashangaa wakati tunapoona **Roho akiongoza Yesu** jangwani kujaribiwa na Shetani. Majaribu haya yalihitajiwa kuhakikisha ya kwamba alikuwa mwema, na alifaa kabisa kwa kazi aliyofika kufanya duniani. Adamu wa kwanza alionyesha kwamba hakufaa kuwa na mamlaka wakati alipokutana na adui katika shamba la Edeni. Hapa Adamu wa pili alikutana na adui huyu vilevile na alimshinda.

Habari hizi za majaribu ya Bwana wetu ni siri kubwa. Tukiuliza kama angaliweza kufanya zambi, na tunajibu "Hapana", halafu tunafazaika kwa njia gani lingekuwa jaribu la hakika kama asipoweza kuangushwa nalo. Kama tukijibu "Ndiyo", inatupasa kuuliza, "Namna gani Mungu katika mwili anaweza kufanya zambi?"

Ni sharti kabisa kwa sisi kukumbuka kwamba Yesu Kristo ni Mungu, na ya kwamba Mungu hawezi kufanya zambi. Ndiyo, yeye ni mtu vilevile, lakini hakuna neno ndani ya Biblia kuonyesha kwamba aliweza kufanya zambi kama mtu. Waandishi wa Agano Jipya waliandika kwamba Kristo hakuwa na zambi. Paulo aliandika kusema kwamba "hakujua zambi" (2 Kor. 5:21); Petro alisema "hakutenda zambi" (1 Pet. 2:22); na Yoane alisema, "zambi si ndani yake" (1 Yn. 3:5).

Kama sisi watu, Yesu aliweza kujaribiwa *toka nje.* Shetani alifika kwake na kumjaribu kufanya maneno yasiyopatana na mapenzi ya Mungu. Lakini hakuwa kama sisi kwa sababu hakuweza kujaribiwa toka *ndani ya roho yake* – hakuwa na tamaa. Na vilevile hakuna neno ndani ya roho yake lililoweza kukubali ushawishi wa Shetani (Yn. 14:30).

Hata kama Yesu hakuweza kufanya zambi, majaribu haya yalikuwa majaribu ya hakika. Lakini hata akijaribiwa kufanya zambi, haikuwezekana kwaye kushindwa nayo. Aliweza kufanya tu kama alivyoona Baba kufanya (Yoane 5:19), na hakuona Baba kamwe akifanya zambi. Yesu hakuweza kufanya neno peke yake mwenyewe (Yn. 5:30), na isingaliwezekana kamwe kwa Baba kumpa ruhusa kufanya zambi.

Kusudi la majaribu halikuwa kuona kama atafanya zambi, lakini kuhakikisha ya kwamba hata akikutana na majaribu makubwa sana aliweza kutii Neno la Mungu tu.

**4:2, 3** Nyuma ya kushinda kwa **siku makumi ine muchana na usiku** bila chakula, Yesu **akaona njaa**. (Hesabu hii **'makumi ine'** inaonekana mara na mara ndani ya Maandiko pamoja na mapimo au majaribu.) Basi neno hili lilimpa **mjaribu** (ndiye Shetani) njia kusema na Yesu kutumika na uwezo wake wa ajabu kugeuza **mawe** ya jangwa kuwa **mkate.** Alisema naye, **"Kama ukiwa Mwana wa Mungu …"** Maana ya "Kama" si kuonyesha shaka, lakini "*Kwa sababu* wewe ni Mwana wa Mungu." Mjaribu alikuwa akikumbuka masemo ya Mungu Baba kwa Yesu saa ya ubatizo wake, "Huyu ni Mwana wangu, mpendwa wangu," na alisema na Yesu kutumika na uwezo huu kusaidia njaa yake.

Lakini kwa Yesu kutumika na uwezo wake wa Mungu kumaliza njaa yake ya mwili kungalikuwa kuasi Mungu. Masemo ya Shetani hapa yanatufikirisha masemo yake katika Mwanzo 3:6 ("ulikuwa mzuri kwa chakula"). Kwa mawazo ya Yoane majaribu haya yanasawanishwa na "tamaa ya mwili" (1 Yn. 2:16). Na kwa sisi watu wa sasa ni majaribu kuishi kwa anasa na usitawi, badala ya kutafuta kwanza ufalme wa Mungu na haki yake.

**4:4** Yesu **alijibu** jaribu hili kwa njia ya kutaja Neno la Mungu. Bwana wetu ni mfano kwetu ya kwamba *si* lazima kwa sisi kuishi, lakini *ni* lazima kwa sisi kutii Mungu. Neno kubwa zaidi kwa maisha yetu *si* kujipatia mkate, lakini ni **kutii kila neno la Mungu**. Mungu Baba hakusema na Mwana wake kugeuza mawe kuwa mikate. Hivi Bwana hakufanya neno hili kwa kutaka kwake mwenyewe na kutii Shetani. Si neno kama njaa yake ilikuwa kali sana.

**4:5,6** Jaribu la pili lilikuwa kwa **mnara wa hekalu** kwa Yerusalema. **Shetani** alisukuma Yesu **kujitupa chini** kama ono la kushangaza kwa watu ya kwamba yeye ndiye Mwana wa Mungu. Alitaja ahadi ya Mungu katika Zaburi 91:11,12 kuchunga Masiya.

Kujitupa chini toka mnara wa hekalu bila kuumia kungalikuwa ajabu kabisa. Kwa njia hii Yesu angaliweza kuonyesha kwamba alikuwa Masiya, na kujipatia utukufu bila mateso. Angaliweza kufikia kiti cha ufalme bila kufa msalabani kwanza. Lakini kufanya hivi hakukuwa mapenzi ya Mungu. Yoane alita jaribu hili "kiburi cha uzima" (1 Yn. 2:16). Linafanana na "mti wa kutamaaniwa" katika shamba la Edeni (Mwa. 3:6). Lilifanana na jaribu la pili la Shetani kwa Yesu kwani lilikuwa njia kujipatia utukufu bila kutii kutaka kwa Mungu. Ndani ya maisha yetu ya sasa tunajaribiwa kujipatia heshima kama watu wa maneno ya Mungu bila kushiriki ndani ya mateso ya Kristo. Tunajitafutia mambo makubwa, lakini kwa wakati wa taabu na matata tunakimbia. Tunajaribu Mungu wakati tunapojitukuza wenyewe na kuona kutaka kwake bure.

**4:7 Yesu** alijibu tena kwa njia ya kusema **"Tena imeandikwa, 'Usijaribu Bwana, Mungu wako'"** (ona Tor. 6:16). Mungu alikuwa ameahidi kuchunga Masiya *kama* akitii mapenzi yake ndani ya maisha yake. Kuzania Mungu atafanya hivi kama asipotii ni kujaribu Mungu. Kwa wakati wa kutimia Yesu atafunuliwa kama Masiya, lakini ilimpasa kusulibishwa kwanza. Sharti mazabahu ya zabihu itangulie kiti cha kifalme. Lazima taji ya miiba itangulie taji ya utukufu. Yesu alikusudi kungojea wakati uliochaguliwa na Mungu na kutimiza mapenzi yake.

**4:8,9** Kwa jaribu la tatu **Shetani alipeleka Yesu hata mlima mrefu sana, akamwonyesha falme zote za ulimwengu**. Alisema na Yesu atampa

hizi zote kama Yesu **akimwabudu.** Jaribu hili lilikuwa juu ya **kuabudu**, tendo la roho, lakini kwa njia hii Shetani alijaribu kusukuma Yesu kujikamatia utawala wa dunia kama mfalme kwa njia ya kuabudu Shetani. Zawabu kwa kufanya hivi, **falme zote za ulimwengu,** inatufikirisha "tamaa ya macho" (1 Yn. 2:16).

Ndiyo, kwa njia nyingine falme za ulimwengu ni mali ya Shetani kwa wakati wa sasa. Katika 2 Kor. 4:4 anaitwa "mungu wa dunia hii", na Yoane anatuambia kwamba "dunia yote pia inakaa katika yule mwovu" (1 Yn. 5:19). Wakati wa kuja kwa pili kwa Yesu kama Mfalme wa wafalme (Ufu.19:16), "Ufalme wa dunia" utageuka ufalme wa Bwana (Ufu. 11:15). Yesu hatageuza shauri la Mungu na hataabudu Shetani kamwe!

Jaribu hili linatuonya sisi watu wa sasa juu ya maneno mawili: 1) Haifai tubadilishe uzima na baraka zetu zote za roho kwa utukufu wa dunia hii iliyo kwa wakati mdogo tu; na 2) tusiabudu na kutumikia kiumbe kwa pahali pa Mwumba.

**4:10** Mara ya tatu Yesu alishinda majaribu kwa njia ya kutaja shairi toka Agano la Kale, **"Uabudu Bwana Mungu wako, umtumikie yeye peke yake."** Kuabudu, na utumishi ulio tunda la kuabudu, ni kwa Mungu peke yake. Kuabudu Shetani ni kusema yeye ni Mungu.

**4:11 Shetani aliacha** Yesu wakati Yesu alipomaliza kushinda majaribu yake yote. Katika Isaya 59:19 tunasoma, "Wakati adui atakapoingia kama garika, Roho ya Bwana atanyanyua bendera juu yake." Ni faraja tamu sana kwa watu wa Mungu wakati wa mateso!

Tunasoma **malaika wakakuja, wakamtumikia,** lakini hakuna elezo juu ya maneno haya. Tunafikiri walimletea vyakula ambavyo alikataa mbele, saa ya majaribu yake.

Majaribu ya Yesu yanatufundisha kwamba Shetani anaweza kushindana na watu wanaotawaliwa na Roho Mtakatifu, lakini hana uwezo kushinda wale ambao wanashindana naye na Neno la Mungu.

**D. Yesu anaanza utumishi wake katika Galilaya (4:12-17)**

Hatusomi hapa juu ya utumishi wa Bwana Yesu ulioendelea kwa karibu mwaka mmoja katika Yudea (ona Yoane 1–4); nyuma ya wakati wa Matayo 4:11 na mbele ya 4:12. Nyuma ya kuandika juu ya majaribu ya Shetani, Matayo aliendelea mara moja kuandika juu ya utumishi wa Yesu katika Galilaya.

**4:12 Wakati Yesu aliposikia kwamba Yoane amefungwa,** alifahamu ya kuwa neno hili lilikuwa kama alama ya kukataliwa kwake mwenyewe. Ni kama wakati watu walipokataa mwenye kutangulia mfalme, walikuwa wakikataa Mfalme mwenyewe. Lakini si woga ambao ulimsukuma kwenda kwa upande wa kaskazini **kwa Galilaya**. Galilaya ilikuwa katikati ya ufalme wa Herode – ndiye Herode aliyefunga Yoane gerezani sasa tu. Kwa njia ya kuhama kwa Galilaya alionyesha kwamba Habari Njema itafikia Mataifa kwa sababu Wayuda walimkataa.

**4:13** Yesu alikaa katika **Nazareti** kufika wakati watu wa mji walipojaribu kumwua kwa sababu alihubiri Habari Njema kwa Mataifa (ona Luka 4:16-30). Kisha alihama kukaa kwa Kapernaumu kando ya bahari ya Galilaya, pahali watu wa makabila ya **Zebuluni na Nafutali** walipokaa zamani.

**4:14-16** Kuhama kwa Yesu kukaa kwa Galilaya kulitimiza unabii wa **Isaya** 9:1,2. Watu wa **Mataifa** hawa, wajinga, na wenye kuamini mambo ya uchawi, waliokaa katika **Galilaya,** waliona **nuru kubwa** – ndiye Kristo, **Nuru** ya dunia.

**4:17 Kutoka** wakati ule **Yesu** aliendelea kuhubiri habari Yoane alizohubiri mbele: **"Tubuni; kwa maana**

**ufalme wa mbinguni umekaribia."** Aliita watu kujitayarisha kwa roho na mwenendo wao kwa kuja kwa ufalme wake. Ufalme ulikuwa karibu, maana Mfalme mwenyewe alikuwa palepale.

**E. Yesu anaita wavuvi wane (4:18-22)**

**4:18,19** Hii ni mara ya pili Yesu aliyoita **Petro na Anderea**. Ndani ya Yoane 1:35-42 waliitwa kupata wokovu; sasa Yesu aliwaita kumtumikia. Mara ya kwanza walikuwa katika Yudea; sasa walikuwa katika Galilaya. Petro na Anderea **walikuwa wavuvi,** lakini Yesu aliwaita kuwa **wavuvi wa watu**. Kazi yao ilikuwa **kufuata** Kristo; ilikuwa kazi yake kuwageuza **kuwa** wavuvi wa faida. Neno lililohitajiwa kwa Petro na Anderea halikuwa kufuata Yesu kwa mwenendo wa mwili tu, lakini kumwiga kwa tabia ya roho. Namna walivyokuwa rohoni mwao lilikuwa neno kubwa kupita maneno waliyosema au kufanya. Kwa njia ya kufuata Kristo mwanafunzi alijifunza kwenda pahali samaki walipokuwa, kutumika na chambo kilichohitajiwa, kuvumilia masumbuko na taabu, kuwa na saburi, na kukaa kwa maficho.

**4:20** Petro na Anderea walisikia na kutii mwito wa Yesu **mara moja**. Kwa imani **waliacha mikila yao,** na walijitoa **kufuata** Yesu na mapendo na bidii.

**4:21,22** Nyuma yake Yesu aliita **Yakobo na Yoane**, nao vilevile walimfuata mara moja. Hawakuacha chombo yao tu, ndiyo njia kujipatia mali kwa mahitaji yao, lakini waliacha **baba yao** vilevile. Kwa njia hii walionyesha kwamba kufuata Bwana ni neno kubwa kupita jamaa, na rafiki, na watu wa dunia.

Kwa njia ya kutii mwito wa Yesu, wavuvi hawa walikuwa na sehemu kubwa ndani ya kazi ya kuhubiri Habari Njema kwa watu wa dunia. Kama wangalifungana na mikila yao, tusingalisikia habari zao kamwe. Ni neno kubwa sana kufuata Kristo kama Bwana wa maisha yetu.

**F. Yesu aliponyesha watu wengi (4:23-25)**

Utumishi wa Bwana Yesu ulikuwa na sehemu tatu: Alifundisha Neno la Mungu **katika masunagogi**; alihubiri **Habari Njema ya ufalme**; na aliponyesha wagonjwa. Kusudi moja la maajabu ya kuponyesha watu lilikuwa kuhakikisha kwamba yeye ni kweli Mwana wa Mungu (Ebr. 2:3,4). Ndani ya Matayo 5–7 tunapata mfano wa mafundisho yake, na sura 8–9 zinapasha habari za maajabu yake.

**4:23** Ndani ya shairi hili **Habari Njema** linatajwa mara ya kwanza katika Agano Jipya. Ni "habari njema za wokovu." Ndani ya kila muda tangu kuumbwa kwa dunia kumekuwa Habari Njema moja tu, njia moja tu ya wokovu.

### HABARI NJEMA

Habari Njema ilianza ndani ya neema ya Mungu (Efe.2:8), maana yake Mungu analeta uzima wa milele bila bei kwa watu wasiostahili hata kidogo kupokea.

Msingi wa Habari Njema ni kazi ya Kristo msalabani (1 Kor. 15:1-4). Mwokozi wetu alitimiza haki yote ya Mungu, na kwa sababu hii Mungu anawezeshwa kuhesabia haki wenye zambi wanaoamini. Waamini wa Agano la Kale walihesabiwa haki kwa njia ya Kristo hata kama kwa wakati ule hajakufa bado. Labda hawakujua maneno mengi juu ya Masiya, lakini Mungu alijua – naye aliwahesabia faida ya kazi ya Kristo hata mbele ya kufika kwake duniani kulipa bei ya zambi zao. Kwa sisi watu wa sasa, kazi hii imekwisha.

Watu wanapokea Habari Njema kwa njia ya imani tu (Efe. 2:8). Katika Agano la Kale watu waliokolewa kwa njia ya kuamini maneno Mungu aliyokwisha

kuwaambia. Kwa wakati wa sasa watu wanaokolewa kwa njia ya kuamini ushuhuda wa Mungu juu ya Mwana wake kama njia ya pekee ya wokovu (1 Yn. 5:11,12). Kifiko cha Habari Njema ni mbingu. Pamoja na watakatifu wa Agano la Kale sisi vilevile tuna tumaini la kuishi mbinguni kwa milele (Ebr. 11:10, 14-16; 2 Kor. 5:6-10).

Kuna Habari Njema moja tu, lakini ni mbalimbali kidogo kwa njia nyingine, kwa muda mbalimbali. Tuwaze juu ya Habari Njema ya ufalme na Habari Njema ya neema ya Mungu. Habari Njema ya ufalme inaagiza: "Tubu na pokea Masiya; halafu utaweza kuingia ufalme wake wakati utakaposimamishwa duniani." Habari Njema ya neema inasema: "Tubu na pokea Kristo; halafu utanyanyuliwa kukutana naye na kukaa pamoja naye kwa milele." Ni Habari Njema moja tu – lakini inasimamishwa kwa njia mbalimbali kupatana na kusudi la Mungu kwa wakati wa muda mbalimbali.

Wakati Yesu alipohubiri Habari Njema ya ufalme, alitangaza habari za kuja kwake kama Mfalme kwa Wayuda, na alionyesha nini ilihitajiwa kwa watu kuweza kuingia ndani ya ufalme wake. ❖

**4:24,25** Habari za Yesu zilienea katika **Suria nzima**, ndiyo inchi kwa upande wa kaskazini-mashariki wa Israeli. **Wagonjwa wote** na **wenye pepo wachafu** na **wenye kupooza** walisaidiwa na kuponyeshwa naye. Watu wengi walifika kwake toka **Galilaya, Dekapoli** (ndiyo miji kumi ya Mataifa iliyofungana pamoja kwa upande wa kaskazini-mashariki wa Palestina), **Yerusalema, Yudea,** na inchi kwa mashariki ya **Yorodani.** Watu walishangaa sana juu ya habari zilizotoka Galilaya!

## 4. KUSIMAMISHWA KWA UTARATIBU WA UFALME (Sura 5–7)

Hotuba hii ya Bwana Yesu iliwekwa karibu na mwanzo wa Agano Jipya na kusudi la kuonyesha ukubwa wa mafundisho haya. Ndani yake Mfalme alionyesha tabia ya roho na ya mwenendo wa wafuata wake.

Hotuba hii **si mafundisho** juu ya njia ya wokovu na **si** kwa wasioamini. Bwana Yesu aliitoa kwa wanafunzi wake (5:1,2), na ndani yake Bwana aliwafundisha utaratibu na sheria na maagizo ambayo alitaka watu wa ufalme wake kutawaliwa nayo. Ilikuwa kwa watu wote – wa zamani, sasa, na kwa wakati wa kuja – wanaonyenyekea Kristo kama Mfalme wao. Wakati Kristo alipokuwa duniani, mafundisho haya yalikuwa zaidi kwa wanafunzi wake. Sasa, wakati Bwana wetu anapotawala mbinguni, ni kwa watu wote ambao wanamtukuza mioyoni mwao kama mfalme wao. Mwishoni, ni mafundisho kwa mwenendo wa wafuata wa Kristo kwa wakati wa Mateso Makubwa na kwa wakati atakapotawala duniani.

Ni kama hotuba hii ni zaidi kwa Wayuda na inataja Baraza (5:22), mazabahu (5:23,24), na Yerusalema (5:35), lakini haifai kusema kwamba ni kwa waamini wa Israeli tu, wa zamani na wa wakati wa kuja. Ni kwa watu wote wa kila wakati wanaopokea na kunyenyekea Yesu Kristo kama Mfalme.

### A. Sifa za heri (5:1-12)

**5:1,2** Hotuba hii inaanza na sifa za heri, au baraka. Zinaonyesha maneno ambayo yanapaswa kuonekana ndani ya wenyeji wazuri wa ufalme wa Kristo. Maneno haya ni mbali kabisa na yale ambayo watu wa dunia wanasifu.

**5:3** Baraka ya kwanza ni kwa wale walio **masikini wa roho**. Hawakuzaliwa hivi, lakini walichagua kuwa hivi kwa njia ya kujitawala wenyewe. Ni wale wanaojua uzaifu wao kwa maneno ya roho, na wanaotegemea uwezo mkubwa wa Mungu kusaidia mahitaji ya roho

zao. **Ufalme wa mbinguni ni wao,** lakini kujitegemea mwenyewe na kujitukuza mwenyewe ni zambi ndani ya ufalme wa mbinguni.

**5:4 Wenye huzuni ni heri;** watafarijiwa siku nyingine. Shairi hili halisemi juu ya huzuni watu wanazopataga duniani kama ugonjwa au kufiwa kwa ndugu. Linasema juu ya huzuni tunayoshiriki na Bwana Yesu kwa sababu ya taabu na zambi za dunia. Hivi si huzuni kwa sababu ya zambi zetu wenyewe tu, lakini kwa sababu ya hali mbaya sana ya dunia hii; huzuni kwa sababu ya wale wanaokataa Mwokozi na hukumu inayongojea wale wanaokataa rehema yake. Wenye huzuni kwa sababu ya maneno haya **watafarijiwa** kwa wakati wa kuja wakati Mungu "atapungusa kila chozi katika macho yao" (Ufu. 21:4). Waamini wanapata huzuni yao yote wakati walipo hai hapa duniani; kwa wasioamini huzuni hii ni kama kionjo cha mbele cha taabu kubwa ambayo inawangojea kwa milele.

**5:5** Heri ya tatu ni kwa **wenye upole; maana watariti inchi.** Labda kwa njia ya tabia yao ya zambi watu hawa walikuwa wenye kunungunika, watu wakali na wenye kiburi, lakini wakati walipopokea Kristo walikusudi kufanana naye, na kwa njia ya kumfuata waligeuka wapole na wanyenyekevu wa moyo (Mt. 11:29). **Wenye upole** si wazaifu, lakini ni wenye kukubali pahali pao pa chini; wasiojisimamia wenyewe, lakini walio tayari kusimamia Mungu au kulinda watu wengine.

Wenye upole *hawariti* inchi *sasa*; zaidi wanariti shutumu na kutwaliwa vitu vyao. Lakini **watariti inchi** kweli wakati Kristo, Mfalme, atakapotawala kwa miaka elfu moja na salama na usitawi.

**5:6** Kuna heri vilevile kwa **wenye njaa na kiu kwa haki:** njaa yao itashibishwa. Watu hawa wana njaa kubwa sana **kwa haki** ndani ya maisha yao wenyewe; wanataka kuona haki na kweli na uaminifu ndani ya watu ambao wanakaa katikati yao, na ndani ya kanisa. Hamu yao **itashibishwa** wakati ufalme wa Kristo utakaposimamishwa, na haki itatawala na uovu utakapokombolewa na maisha na mwenendo wa haki.

**5:7** Ndani ya ufalme wa Bwana wetu **wenye rehema watabarikiwa … kwa sababu watapata rehema**. Kuwa na **rehema** ni kutenda rehema kwa njia ya kutokuazibu wale wanaostahili kuazibiwa; ni vilevile kusaidia wenye mahitaji ambao hawawezi kujisaidia wenyewe. Mungu alikuwa na rehema wakati asipotuacha sisi kuhukumiwa kama tulivyostahili kwa sababu ya zambi zetu, na kwa njia ya kututendea mema kwa njia ya kazi ya Kristo msalabani. Tunaiga Mungu wakati tunapohurumia watu wengine.

Wenye rehema **watapata rehema.** Yesu hakusema hapa juu ya rehema ya wokovu ya Mungu kwa mwenye zambi; mtu halazimishwi kuwa na rehema yeye mwenyewe kusudi apate rehema ile – ni zawadi. Anasema hapa juu ya **rehema** tunayohitaji kila siku kutuwezesha kuishi kwa Bwana, na kwa wakati wa kuja vilevile saa kazi ya kila mtu itakaponekana na kufunuliwa (1 Kor. 3:12-15). Siku ile mtu asiyekuwa mwenye rehema hatapokea rehema; maana yake zawabu zake zitapunguka.

**5:8** Kuna ahadi kwa **wenye moyo safi** ya kwamba **wataona Mungu**. Mwenye moyo safi ni mtu aliye mtakatifu rohoni na ndani ya mafikiri yake, mwenye damiri safi. Maneno haya **'wataona Mungu'** yanaweza kuwa na maana mbalimbali: 1. **Wenye moyo safi wanaona Mungu** sasa kwa njia ya Neno lake na Roho Mtakatifu. 2. Mara nyingine Bwana anajifunua kwao kwa njia ya ajabu au ono. 3. **Wataona Mungu**

wakati watakapoona Yesu saa atakapokuja tena. 4. **Wataona Mungu** kwa wakati wa milele.

**5:9** Kuna heri kwa **wenye kufanya salama: maana wataitwa wana wa Mungu**. Mungu hasemi hapa juu ya watu wenye tabia ya salama, au wanaopenda kukaa na salama. Anasema juu ya watu wanaojaribu kusaidia watu wengine kukaa na salama. Mara nyingi sisi watu tunataka kuangalia na macho tu saa watu wengine wanapogombana. Mungu anataka tusaidie watu wale kupatana tena na kukaa na salama, hata kama kwa njia ya kufanya hivi sisi wenyewe tunalaumiwa na kutukanwa.

**Wenye kufanya salama** wanaitwa **wana wa Mungu**. Hii si namna gani mtu ana*geuka* mwana wa Mungu – anaweza kugeuka mwana wa Mungu kwa njia ya kupokea Yesu Kristo kama Mwokozi wake tu (Yn. 1:12). Waamini wakijaribu kuleta salama katikati ya watu, wana*onyesha* kwamba wao ni **wana wa Mungu,** na siku nyingine Mungu ataonyesha wazi kwamba wao ni watu wa jamaa yake.

**5:10** Kuna heri vilevile kwa wale **wanaoteswa**, si kwa mabaya ambayo walitenda, lakini **kwa sababu ya haki**. **Ufalme wa mbinguni** ni kwa wale wanaotenda haki. Mwenendo wao wa haki unashitaki na kuhukumu wazalimu wa dunia na kuamsha uadui wao. Watu wanachukia mwenye maisha ya haki, kwa sababu mwenendo wake wa haki unafunua uzalimu wao wenyewe.

**5:11** Heri hii inafanana na ile ndani ya shairi 10. Lakini ndani ya shairi 10 mateso yalikuwa kwa sababu ya **haki;** hapa ndani ya shairi 11 ni kwa ajili ya **Kristo**. Bwana alijua ya kwamba wafuata wake watateswa kwa sababu ya ushirika wao naye. Na kweli tangu kufa kwa Kristo watu wa dunia wametesa, kufunga gerezani, na kuua wafuata wa Yesu.

**5:12** Ni heshima kupata mateso kwa ajili ya Kristo, neno ambalo ingetufurahisha. Kuna **zawabu kubwa** kwa wale wanaoshiriki na **manabii** ndani ya mateso yao. Wale watumishi wa Mungu kwa wakati wa Agano la Kale walisimama imara kwa Mungu, si neno kama walipata mateso. Wote wanaoiga uhodari na uaminifu wao kwa wakati wa sasa watatukuzwa pamoja nao kwa wakati wa kuja.

Mashairi 3-12 ya sura hii yanatuonyesha namna gani kuwa mfuata na mwenyeji mzuri ndani ya ufalme wa Kristo. Ona *haki* (sh.6), *salama* (sh.9), na *furaha* (sh.12). Labda Paulo alikumbuka mashairi haya wakati alipoandika, "Kwa maana ufalme wa Mungu si kula na kunywa, lakini haki, na salama, na furaha katika Roho Mtakatifu" (Rom. 14:17).

### B. Waamini ni chumvi na nuru (5:13-16)

**5:13** Bwana Yesu alisawanisha wanafunzi na **chumvi.** Kwa watu wa dunia kazi ya chumvi ni kuzuiza vyakula visioze; inaleta kiu kwa mtu, na inaongeza utamu wa vyakula. Vivyo hivyo wafuata wa Yesu wanazuiza uovu usizidi duniani, na wanaamsha ndani ya roho za watu wengine hamu kuishi maisha ya haki tuliyosoma juu yake ndani ya mashairi yaliyotangulia.

Lakini nini itatokea **kama chumvi ikiharibika**? Nini itaweza kurudisha utamu wake wa mbele? Haiwezekani kurudisha utamu wake. Haina faida kwa kazi yo yote tena, ila kutupwa njiani na kukanyagwa na watu.

Mwanafunzi wa Yesu ana kazi kubwa moja, ndiyo: kuwa **chumvi ya dunia** kwa njia ya kutii mafundisho ya Bwana Yesu ndani ya mashairi 3-10 ya hotuba hii Bwana Yesu aliyotoa mlimani, na katika hotuba yake nzima. Kama maneno haya hayaonekani ndani

ya maisha yake, watu wataona ushuhuda wake bure na kuukanyaga na miguu. Watu wa dunia wanazarau mwamini asiyejitoa mzima kwa Bwana.

**5:14** Yesu anaita Wakristo kuwa **nuru ya ulimwengu** vilevile. Alijiita mwenyewe "nuru ya dunia" (Yn. 8:12; 12:35,36,46). Nuru inatoka kwa Yesu, na Wakristo wanarudisha nuru yenyewe. Ni kazi yao kungaa kwa yeye namna mwezi unavyorudisha utukufu wa jua.

Mkristo ni kama mji **juu ya mlima;** watu wote kando kando wanaweza kuuona, na unangaa katika giza. Nuru ya wale wanaotii mafundisho ya Bwana ndani ya maisha yao **haiwezi kufichwa** vilevile.

**5:15,16** Watu **hawawashi taa na kuiweka chini ya kitunga**. Wanaiwasha na kuiweka juu ya **kinara** ili **nuru yake iweze kungaa kusaidia watu wote nyumbani**. Bwana hakutaka tuchunge mafundisho yake kujisaidia wenyewe tu, lakini tuweze kuyashiriki na watu wengine. Inatupasa **kuacha nuru yetu kungaa** mbele ya watu, **waone matendo yetu mazuri, watukuze Baba yetu aliye mbinguni**. Kristo akionekana ndani ya maisha yetu, maisha yetu yana ushuhuda wa uwezo kwa Bwana kupita masemo yetu.

### C. Kristo alitimiza sheria (5:17-20)

**5:17,18** Zaidi ya viongozi wakubwa walioleta maasi duniani katika miaka inayopita waliharibu utaratibu wa utawala wa inchi, lakini Bwana Yesu hakufanya hivi. Alisimamia sheria ya Musa akisema na nguvu kwamba ni lazima kwa maneno yake yote kutimizwa. Yesu hakufika kuharibu **torati au manabii**, lakini kuyatimiliza. Alisema kwamba yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka kufika saa zote zitakapotimizwa. **Yodi** na **nukta** ni herufi ndogo zaidi za alfabeti ya Kiebrania. Yesu aliamini ya kwamba kuandikwa kwa kila herufi ya Biblia, hata zile zilizo ndogo zaidi, ziliongozwa na Mungu na zina maana.

Tuone vilevile ya kwamba Yesu *hakusema* ya kuwa torati *haitapita kamwe.* Alisema ya kwamba haitapita **mbele ya kutimia kwa maneno yake yote.**

### MWAMINI NA SHERIA

Mungu alitoa sheria kwa taifa la Israeli kwa njia ya Musa. Sheria nzima ni ndani ya Kutoka 20–31, Walawi, na Torati, lakini maneno yake makubwa yanajumlishwa ndani ya Amri Kumi.

Mungu hakuleta sheria kama njia ya wokovu (Mdo. 13:39; Rom. 3:20a; Gal. 2:16,21; 3:11); kusudi lake lilikuwa kufahamisha watu kwamba wao ni wenye zambi (Rom. 3:20b; 5:20; 7:7; 1 Kor. 15:56; Gal. 3:19) na kisha kuwakokota karibu na Mungu kupokea wokovu wake wa neema. Mungu aliitoa kwa taifa la Israeli, lakini mafundisho yake yana faida kwa watu katika kila muda (Rom. 2:14,15). Mungu alipima Israeli na Sheria, kama mfano wa taifa zima la watu wa dunia, na hatia ya Israeli ilihakikisha hatia ya ulimwengu mzima (Rom. 3:19).

Sehemu ya sheria ilikuwa azabu ya mauti (Gal. 3:10), na mtu akiasi moja la maagizo yake ni kama anaasi yote (Yak. 2:10). Watu waliasi sheria, hivi walikuwa chini ya laana ya mauti. Lakini Mungu ni haki na mtakatifu, na ilikuwa lazima kwa azabu hii ilipwe. Ni kwa sababu hii Yesu alikuja duniani: kulipa azabu hii na mauti yake. Alikufa kwa pahali pa wenye kuvunja sheria, lakini yeye mwenyewe hakuwa na zambi. Hivi Habari Njema haikupindua sheria, lakini iliisimamia na kuonyesha kwamba Bwana Yesu alitimiza maneno yote pia yaliyohitajiwa na sheria, kwa njia ya maisha na mauti yake kukomboa watu.

Hivi mtu akiamini Yesu, yeye si chini ya sheria tena; yeye ni chini ya neema (Rom. 6:14). Yeye ni mfu kwa maneno

ya sheria kwa sababu ya kazi ya Kristo. Ilipasa azabu ya sheria kulipwa mara moja tu, na kwa sababu Kristo aliilipa, hakuna hitaji kwa mwamini kuilipa tena. Kwa sababu hii sheria haikuwa na uwezo tena kama mbele kwa mwamini (2 Kor. 3:7-11). Sheria ilikuwa mwalimu kufika wakati Kristo alipokuja na kuleta wokovu, kisha mwalimu huyu hakuhitajiwa tena (Gal. 3:24,25).

Lakini hata Mkristo si chini ya sheria tena, si kusema yeye ni bila sheria. Anafungwa na kamba iliyo na nguvu kupita sheria kwani yeye ni chini ya sheria ya Kristo (1 Kor. 9:21). Hasukumwi ndani ya mwenendo wake na woga wa azabu, lakini na hamu kubwa kupendeza Mwokozi wake. Kristo amegeuka mfano wake (Yn. 13:15; 15:12; Efe. 5:1,2; 1 Yn. 2:6; 3:16).

Waamini wengi wanauliza kama ni lazima kwao kutii Amri Kumi. Ni kweli ya kwamba maagizo mengine ya sheria ni kwa wakati wa sasa na hata daima vilevile. Ni zambi katika muda wo wote kuiba, kutamani au kuua. Tisa za Amri Kumi zinatajwa ndani ya Agano Jipya. Hazitajwi pamoja na hatari ya azabu, lakini kufundisha watu wa Mungu katika haki (2 Tim. 3:16b). Moja tu za amri kumi haitajwi ndani ya Agano Jipya, ndiyo ile juu ya kushika sabato. Wakristo *hawaagizwi kamwe* kushika sabato (ndiyo siku ya saba ya juma).

Lakini utumishi wa sheria kwa wasioamini haukwishi. "Lakini tunajua sheria ni njema, kama mtu akiitumia kwa njia ya sheria" (1 Tim. 1:8). Kazi yake ni kufahamisha mtu zambi zake na kumwongoza kutubu. Lakini kazi ya sheria si kwa watu wanaokwisha kuokolewa: "sheria haifanywi kwa mtu wa haki" (1 Tim. 1:9).

Haki ambayo inahitajiwa na sheria inatimizwa ndani ya wale wasiotembea kufuata maneno ya mwili lakini maneno ya Roho (Rom. 8:4). Na maagizo ya Bwana wetu ndani ya hotuba mlimani ni hata magumu kupita ile ya sheria. Kwa mfano, sheria iliagiza, "Usiue"; Yesu aliagiza, "Usichukie." Hivi hotuba mlimani haisimamii tu Sheria na Manabii lakini iliongeza ufahamu wetu wa maana yao. ❖

**5:19** Bwana Yesu alijua mbele ya kwamba watu watajaribu kupunguza uwezo wa maagizo ya Mungu, na kueleza maana yao kwa akili ya binadamu. Lakini mtu ye yote "**anayevunja amri moja** katika hizi na **kufundisha** watu hivyo, **ataitwa mdogo kabisa katika ufalme wa mbinguni.**" Tunashangaa kwamba watu wa namna hii wana ruhusa kuingia ufalme wa mbinguni – lakini tunakumbuka ya kwamba *tunaingia ufalme* kwa njia ya kuamini Kristo. Cheo cha mtu *ndani* ya ufalme ni kwa kipimo cha kutii na uaminifu wake hapa duniani. Mtu yule anayetii sheria ya ufalme **ataitwa mkubwa katika ufalme wa mbingini.**

**5:20** Kwa kuingia ufalme, lazima **haki** yetu ipite **haki ya Wafarisayo na waandishi** (waliokuwa na kawaida za dini tu kusafisha watu kwa upande wa inje, wa kuonekana tu, bila kusafisha roho zao). Mungu anakubali utimilifu mmoja tu, ndio ule ambao anahesabia watu wale wanaopokea Mwana wake kuwa Mwokozi wao (2 Kor. 5:21). Na wale wanaoamini Kristo na imani ya kweli watakuwa na mwenendo wa haki vilevile, kupatana na mafundisho ya Yesu ndani ya hotuba yake mlimani.

### D. Yesu anaonya watu juu ya kasirani (5:21-26)

**5:21** Wayuda walioishi wakati Yesu alipokuwa duniani walijua kwamba uuaji ulikatazwa na Mungu na ya kwamba mwuaji alipaswa kuhukumiwa. Ilikuwa hivi hata wakati Mungu asipotoa sheria bado (Mwa. 9:6), na nyuma

iligeuka sehemu ya sheria (Kut. 20:13; Tor. 5:17). Wakati Yesu aliposema, **"Lakini mimi ninawaambia ninyi,"** alionyesha kwamba aliongeza mafundisho haya juu ya uuaji. Mtu hakuweza kujivuna tena kwa sababu hakuua mtu mwingine kamwe. Sasa Yesu alisema, "Ndani ya ufalme wangu haifai kwa mtu hata *kuwaza* juu ya kuua mtu mwingine." Halafu aliendelea kuonyesha namna tatu za kasirani zisiyo za haki.

**5:22** Kwanza alisema juu ya mtu **anayekasirikia ndugu yake bila sababu.** Inawezekana kwa mtu huyu kuhukumiwa. Zaidi ya watu wanafikiri wana sababu nzuri kwa kasirani yao, lakini kuna ruhusa kwa kasirani tu juu ya neno linalopunguza heshima ya Mungu, au wakati mtu mwingine anapotendewa mabaya. Haifai kamwe kwa sisi kuwa na kasirani kwa sababu ya mabaya ambayo sisi tulitendewa.

Zambi ya kuzarau ndugu ni hata kubwa kupita. Kwa wakati wa Yesu watu walitumika na neno **'Raka'** (neno la kiaramaik, maana yake "mtu bure"), ndiyo matukano na zarau. Iliwezekana kwa wale waliotumika na neno hili kuhukumiwa na **Baraza** – ndiyo hukumu kubwa zaidi inchini.

Mwishoni, Yesu alikataza watu kuita mtu **'mpumbavu'** kwa kasirani bila sababu**.** Maana ya neno hili si mwenye kukosa akili tu, lakini ukosefu wa akili *wa roho.* Ni kama mwenye kutumika na neno hili angetaka mtu huyu kufa. Kwa wakati wa sasa tunasikia watu wakisema, "Mungu akulaani milele." Ni kama anataka mtu yule kupotea kwa milele. Yesu anasema kwamba mtu akitoa laana namna hii anastahili Gehena ya moto. Ilikuwa desturi kwa maiti za watu waliouawa kwa sababu ya zambi zao kutupwa ndani ya shimo la jalala lililowaka kwa moto inje ya Yerusalema lililoitwa Bonde la Hinomu au Gehena. Lilikuwa mfano wa moto wa Hadeze usiozimika kamwe.

Ukali wa masemo haya ya Mwokozi unaonekana wazi. Alifundisha ya kwamba ndani ya masemo namna hii ni mbegu za uuaji, na hamu ya wenye kuyatumia kutenda uuaji. Ona ya kwamba kipimo cha azabu kwa maneno haya kinaongezeka: *hukumu, baraza,* na *moto wa milele.* Katika ufalme Bwana ataazibu zambi kwa kipimo cha ukubwa wao.

**5:23, 24** Mtu akiumiza roho ya mtu mwingine kwa njia ya kasirani au njia yo yote nyingine, si faida kwa yeye kuleta sadaka kwa Mungu, kwani sadaka hii haiwezi kumpendeza. Lazima mtu huyu aliyeumiza mwingine atengeneze kwanza mabaya aliyotenda. Halafu Mungu atakubali kupokea sadaka yake.

Hata kama maneno haya yaliandikwa kwanza kwa Wayuda, yana maana kwa watu wa sasa vilevile. Waza juu ya mafundisho ya Paulo juu ya karamu ya ukumbusho katika 1 Wakorinto 11. Mungu hawezi kupokea kuabudu kwa mwamini asiye na upatano na mwamini mwingine.

**5:25,26** Ndani ya mashairi haya Bwana anakataza waamini wasiwe na roho ya kutaka kushitaki mwamini mwingine mbele ya mwamuzi, na anawaonya juu ya kutokubali kosa lao wenyewe. Ni vizuri kupita watengeneze magomvi yao mbio na kuepuka kushitakiana mbele ya mwamuzi, ili wao wawili wasipate hasara. Mafundisho ya mfano huu ni wazi. Kubali kosa lako mbio na tengeneza neno lenyewe mara moja. Usipofanya hivi, kosa lako litageuka neno kubwa sana na itakupasa kutoa mali ya kutosha kutengeneza neno lenyewe, na zaidi ya ile malipo ya azabu vilevile. Hivi haifai kuwa na haraka kufikisha mashitaki yako mbele ya mwamuzi.

**E. Yesu anahukumu uzini (5:27-30)**

**5:27,28** Sheria ya Musa ilikataza uzini waziwazi (Kut. 20:14; Tor. 5:18). Inawezekana kwa mtu kujivuna kwa sababu hakuzini kamwe, na hata hivi kuwa mwenye "macho yanayojaa uzini" (2 Pet. 2:14). Hata kama mwenendo wake mbele ya watu ni safi, mawazo yake si safi hata kidogo naye anakaa kuwaza juu ya uzini. Hivi Yesu alionya wanafunzi wake kwamba usafi wa matendo tu hautoshi; sharti wawe safi rohoni vilevile. Sheria ilikataza watu kutenda uzini; Yesu alikataza hata hamu ya uzini rohoni: **Kila mtu anayetazama mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake.** Zambi inaanza ndani ya nia yetu, na kama tukikaa kufikiri juu yake, zambi hii ya roho itageuka tendo wazi baadaye.

**5:29, 30** Inatupasa kuweka roho kabisa kutawala mawazo yetu yawe safi. Hivi Yesu alifundisha kama kiungo cho chote cha mwili kikituingiza ndani ya zambi, ingekuwa vizuri kukata kiungo hiki tusipoteze roho yetu kwa milele. Maana ya masemo haya ya Yesu ilikuwa kweli ya kwamba inatupasa kukata kiungo cha mwili wetu *kama ikihitajiwa*? Ndiyo, lakini tushukuru Mungu kwa sababu neno hili *halihitajiwi kamwe* kwani Roho Mtakatifu anawezesha waamini kuishi maisha matakatifu. Lakini sharti mwamini *atake* kuishi maisha safi.

**F. Yesu analaumu kuachana (5:31, 32)**

**5:31** Kwa wakati wa sheria ya Agano la Kale kuachana kulikubaliwa, ona Tor. 24:1-4. Shairi 31 halisemi juu ya mwanamke aliyetenda uzini (azabu ya mzini ilikuwa mauti, ona Tor. 22:22). Lakini linasema juu ya kuachana kwa sababu mume na mke hawakupendana wala kupatana.

**5:32** Lakini ndani ya ufalme wa Kristo **kila mtu anayeacha mke wake, isipokuwa kwa habari za uasherati, anamfanya kuwa mzini**. Si kusema kwamba ni lazima kwa mwanamke kugeuka mzini, lakini kwa sababu anakosa mtu kumchunga sasa, analazimishwa kukaa na mwanamume mwingine, na kwa hivi anageuka mzini. Zaidi ya ile, mwanamume **anayeoa mwanamke aliyeachwa anatenda uzini.**

Ni nguvu sana kueleza maneno yote juu ya kuachana, hivi tutajaribu kueleza kwa ufupi maneno ambayo tunaamini Biblia inafundisha juu ya neno hili.

### KUACHANA NA KUOA TENA

Halikuwa kusudi la Mungu kamwe kwa watu kuachana. Alitaka mwanamume mmoja na mwanamke mmoja kuoana na kukaa pamoja daima, hata siku ya kufa (Rom. 7:2,3). Yesu alionyesha neno hili wazi kwa Wafarisayo kwa njia ya kuonyesha utaratibu wa Mungu saa ya kuumbwa kwa dunia. (Mt. 19:4-6).

Mungu anachukia kuachana (Mal. 2:16), maana kuachana kusikopatana na Neno lake. Hachukii kila namna ya kuachana kwa sababu alisema yeye mwenyewe aliachana na Israeli (Yer. 3:8). Alifanya hivi kwa sababu taifa la Israeli walikuwa wamemwacha na kuanza kuabudu sanamu. Taifa halikuwa aminifu kwake.

Katika Matayo 5:31,32 na 19:9 Yesu alifundisha ya kwamba kuachana kulikatazwa isipokuwa kama au mume au mke alikuwa ametenda uzini (sababu hii haikutajwa ndani ya Marko 10:11,12 na Luka 16:18).

Labda Marko na Luka hawakutaja sababu hii kwa sababu hawakuandika maneno yote Bwana aliyosema juu ya neno hili. Hivi, hata kama halikuwa kusudi la Mungu kwa watu kuachana, kunakubaliwa wakati mume au mke alipokuwa mzinifu, na Yesu ali*ruhusu* waachane hata kama hakuwa*agiza* kufanya hivi.

Walimu wengine wanafikiri mafundisho ya 1 Korinto 7:12-16 ni ya kwamba kuachana kunakubaliwa wakati mwamini anapoachwa na msiyeamini. Paulo alisema yule aliyeachwa "si mfungwa katika maneno kama haya." Mwandishi wa kitabu hiki anaamini kwamba msiyeamini akiondoka na kwenda kukaa na mtu mwingine, kuachana kwa mtu aliyeachwa kunakubaliwa tu kama msiyeamini alitenda uzini.

Watu wengine wanafundisha ya kwamba kuna ruhusa kwa watu kuachana, lakini hakuna ruhusa kwa mtu asiyezini kuoa tena. Lakini Agano Jipya linafundisha kwamba yule asiyekuwa na hatia ana ruhusa kuoa tena.

Ulizo lingine ni juu ya wale walioachana mbele ya kuokolewa. Ni wazi ya kwamba zambi za watu walioasi maagizo ya Mungu na kuachana na kuoa tena mbele ya kuokolewa zimesamehewa (kwa mfano ona 1 Kor. 6:11 pahali Paulo alipotaja uzini kama moja ya zambi ambazo waamini wa Korinto walizotenda mbele ya kuokolewa.) Zambi waamini walizotenda mbele ya kuokolewa hazizuizi waamini kushiriki katika kanisa.

Ulizo lililo gumu kupita ndilo hili: Wakristo walioachana kwa sababu ya neno lisilokubaliwa na Biblia, na halafu walioa tena. Ni vizuri kuwapokea tena katika ushirika wa kanisa pahali wanapokaa? Kama watu hawa wakiishi pamoja katika uasherati, ingewapasa kukiri zambi yao na kuacha kukaa pamoja. Ni nguvu kutambua mapenzi ya Mungu ndani ya maneno ya namna hii yanayoweza kuzaa mabaya makubwa kupita, labda kuacha wanawake na watoto bila nyumba wala vyakula.

Mwandishi wa kitabu hiki anaamini ya kwamba Wakristo walioachana na kuoa tena kwa njia isiyopatana na Maandiko wanaweza kutubu zambi yao na roho ya kweli, na kurudishwa kwa ushirika wa kanisa tena. Ni kama kwa maneno haya ya kuachana ni lazima kwa wazee wa kanisa kuangalia maneno ya kila mtu mmoja mmoja na kuyahukumu kupatana na Neno la Mungu. Kama azabu ikihitajiwa mara nyingine, lazima wote wanyenyekee maagizo ya wazee.

❖

### G. Yesu anahukumu viapo (5:33-37)

**5:33-36** Kulikuwa na mashairi machache ndani ya Sheria ya Agano la Kale kukataza watu kutoa viapo **vya uwongo** kwa jina la Mungu (Law. 19:12; Hes. 30:2; Tor. 23:21. Maana ya kuapa kwa jina la Mungu ni ya kwamba Mungu ni mshuhuda kwamba unasema kweli. Wayuda walijaribu kuepuka kutoa kiapo cha uwongo kwa jina la Mungu kwa njia ya kuapa kwa **mbingu**, **dunia, Yerusalema**, au kwa **kichwa** chao.

Yesu alihukumu hila ya kuepuka uwezo wa sheria namna hii na alikataza namna zote za kutoa viapo, hata ndani ya masemo yetu. Ulikuwa udanganyifu, na haikuwa na faida kujaribu kuepuka kutoa kiapo kwa jina la Mungu kwa njia ya kukomboa jina lake na neno lingine. Kuapa kwa **mbingu** ni kuapa kwa **kiti cha ufalme** wake. Kuapa kwa **dunia** kunakatazwa kwa sababu ni **kiti cha kuweka miguu yake**. Kuapa kwa **Yerusalema** ni kuapa kwa mji wa Mfalme mkubwa. Hata kutoa kiapo kwa **kichwa** chako ni vibaya kwani ni Mungu ambaye alikiumba.

**5:37** Mkristo hahitaji kutoa kiapo. Kama akisema **Ndiyo**, ingepasa maana yake kuwa **Ndiyo**. Na akisema **Siyo**, inapasa maana yake kuwa **Siyo**. Kutumika na masemo ya nguvu kupita haya ni kama kukubali kwamba **yule mwovu**, ndiye Shetani, anatawala maisha yetu. Hakuna matukio ndani ya maisha ya Mkristo ambayo yanampa Mkristo ruhusa kutoa kiapo cha uwongo.

Mashairi haya yanakataza vilevile udanganyifu wo wote. Lakini hayakatazi Mkristo kutoa kiapo kwa baraza ya hukumu. Yesu mwenyewe alitoa kiapo mbele ya kuhani mkubwa (Mt. 26:63-65). Paulo alitoa kiapo na kutaja Mungu kama mshuhuda wake kwamba maneno aliyoandika yalikuwa kweli (2 Kor. 1:23; Gal. 1:20).

### H. Kuongeza wema (5:38-42)

**5:38** Sheria ilisema,“Jicho kwa jicho, jino kwa jino” (Kut. 21:24; Law. 24:20; Tor. 19:21). Lilikuwa agizo la ajabu, na vilevile liliweka mpaka kwa kipimo cha azabu yenyewe. Haikufaa azabu kuwa kubwa kupita zambi yenyewe. Katika Agano la Kale, ni serikali iliyokuwa na amri kutoa azabu yenyewe, si mtu mmoja mmoja.

**5:39-41** Haki Yesu aliyosimamisha ilipita haki ya Agano la Kale, na aliondosha kabisa ruhusa ya kujilipiza kisasi. Alionyeshea wanafunzi wake ya kwamba mbele walikuwa na ruhusa kwa njia ya sheria kujilipiza kisasi, lakini sasa, kwa neema, inawezekana kwao kutendewa mabaya na watu bila kujitafutia malipo. Yesu alifundisha wafuata wake kwamba haifai washindane na **mtu mvovu**. Mtu akiwapiga shavu la kuume, **wamgeuzie la pili vilevile.** Na mtu akimshitaki na kutaka kukamata **kanzu** yake (vazi la ndani), amruhusu kukamata **joho** yake (ndilo vazi la kufunika mwili inje kwa wakati wa usiku) vilevile. Mtu wa serikali akiwalazimisha kubeba vitu vyake **kilomètre moja**, wakae tayari kuvibeba kwa **kilomètres mbili**.

**5:42** Agizo la mwisho Yesu alilotoa kwa wakati huu lilikuwa nguvu zaidi. **Mpa ambaye anakuomba, naye anayetaka kukopa kwako, usimgeukie.** Sisi watu tunaweka roho sana juu ya vitu na mali yetu ambayo tulijipatia, na hatutaki kugawanya nayo hata kidogo. Lakini kama tungeweka roho juu ya hazina mbinguni, na kukubali kukaa na vitu tunayo*hitaji* tu hapa duniani, vyakula na mavazi, kama tungekuwa tayari kutii agizo hili la Bwana. Ndiyo, agizo hili linawaza juu ya kusaidia watu walio na mahitaji ya kweli, na mara nyingine ni nguvu kutambua kama hitaji lo lote ndilo hitaji la kweli, lakini kuanguka na kusaidia mtu asiye na hitaji la kweli ni vizuri kupita kukosa kusaidia mtu aliye na taabu kabisa.

Kwa sisi watu wa dunia haiwezekani kutii agizo hili la Bwana. Watu wale tu wanaotawaliwa na Roho Mtakatifu wanaweza kuishi maisha namna hii ya kujikana wenyewe. Kwa njia ya kuruhusu Mwokozi tu kuishi maisha yake ndani ya mwamini, itawezekana kwa mwamini huyu kurudisha mema kwa uovu (sh.39) na uzalimu (sh.40), na masumbuo (sh.41). Hii ndiyo maana ya ku*ongeza mema.*

### I. Penda adui zako (5:43-48)

**5:43** Mafundisho haya juu ya haki yanaongeza juu ya yale Bwana aliyotoa ndani ya shairi 42. Sheria ilifundisha Waisraeli **kupenda jirani** zao (Law. 19:18). Hata kama hawakukatazwa wazi **wasichukie adui** zao, neno hili lilikuwa sehemu ya agizo la kupenda jirani zao. Shairi hili lilijumlisha mafundisho ya Agano la Kale juu ya wale waliotesa watu wa Mungu (ona Zab. 139:21,22), ndio uadui wa haki kwa adui za Mungu.

**5:44-47** Lakini sasa Yesu anatangaza ya kwamba inatupasa **kupenda adui** zetu na **kuombea wale ambao wanatutesa.** ***Tunaagizwa*** kupenda, hivi tunaona kwamba ni neno tunalofanya na kutaka kwetu, si kwa sababu tuna*sikia* mapendo rohoni mwetu namna ya mapendo tuliyo nayo kwa watu wa jamaa yetu. Si desturi yetu sisi watu kupenda adui zetu, lakini inawezekana kwa neema ya Mungu kwa wenye maisha ya uzima wa milele.

Hatutapokea zawabu kama tukipenda watu wale ambao wanatupenda sisi; Yesu alisema ya kwamba hata watoza kodi wasioamini wanafanya hivi! Hatuhitaji uwezo toka juu kwa mapendo ya namna hii. Ni vivyo hivyo na kusalimiana na kupendana na **ndugu tu**, maana jamaa na rafiki zetu. Wasioamini wanaweza kufanya hivi. Kama haki na mapendo yetu si makubwa kupita yale ya dunia, ushuhuda wetu kwa Bwana utakosa uwezo hapa duniani.

Yesu alisema ilipasa kutendea mema wale ambao waliwatendea mabaya, ili waweze kuwa **wana wa Baba yao aliye mbinguni.** Hakusema kwamba hii ndiyo njia kwa watu *kugeuka* wana wa Mungu, lakini ya kwamba kwa njia hii tuna*onyesha* kwamba tuko watoto wa Mungu. Mungu hana upendeleo kwa watu **waovu au mema** (maana wote wanapata faida sawasawa ya **jua na mvua**) na ingetupasa sisi kutendea watu wote sawasawa, kwa neema na haki.

**5:48** Bwana Yesu anamaliza mashairi haya na onyo hili: **Basi muwe wakamilifu, kama Baba yenu mbinguni alivyo mkamilifu**. Maana ya neno hili **kamilifu** hapa haiko kuwa bila zambi. Ndani ya mashairi tuliyosoma sasa tu tuliona kwamba kuwa kamilifu ni kupenda wale ambao wanatuchukia, kuombea wale ambao wanatutesa, na kutendea watu wote mema, bila upendeleo kwa rafiki ama adui. Ukamilifu namna hii unawezesha Mkristo kuiga Mungu kwa njia ya kuonyeshea watu wote baraka bila tofauti.

### J. Kutoa na roho ya kweli (6:1-4)

**6:1** Ndani ya sehemu ya kwanza ya sura hii Yesu alifundisha juu ya maneno matatu ndani ya maisha ya mwamini: kutoa zawadi (mash.1-4), maombi (mash. 5-15), na kufunga (mash.16-18). Tunaona neno hili **Baba** mara kumi ndani ya mashairi haya 18, nalo linatusaidia kuyafahamu. Sharti matendo yetu ya haki yafanywe kwa ukubali wa Mungu, si wa watu.

Alianza sehemu hii ya hotuba hii na maonyo tusifanye **wema** wetu mbele ya watu wafikiri tuko watu wa Mungu kabisa. Kama kusudi letu ndilo kuheshimiwa na watu, hii ndiyo **zawabu** yetu. Hatutapokea nyingine kwani Mungu hatoi zawabu kwa udanganyifu.

**6:2** Ni nguvu kwa sisi kufahamu kwamba wadanganyifu watajaribu kukokota macho ya watu juu yao wenyewe kwa njia ya kutoa zawadi zao wazi **ndani ya masunagogi** au kwa watu **masikini njiani**. Bwana alisema neno fupi tu juu ya matendo namna hii: **"Wamekwisha kupata zawabu yao"** (maana yake, zawabu yao ndiyo heshima wanayopata hapa duniani; hawatapokea zawabu nyingine).

**6:3,4** Mfuata wa Kristo akitoa **zawadi,** inampasa kufanya hivi kwa **siri**. Ndiyo, kwa siri kabisa. Hivi Yesu alisema na wanafunzi wake kwa mfano, **"mkono wako wa kushoto usijue mkono wako wa kuume unalofanya."** Alitaka wafahamu kwamba sharti zawadi zao ziwe kwa **Baba**, si kwa kupatia mwenye kuzitoa heshima.

Mashairi haya hayafundishi ya kwamba lazima zawadi zetu zote zitolewe kwa siri bila kuonyesha jina la mwenye kuzitoa, lakini yanahukumu wale wanaotoa zawadi kwa kujipatia wenyewe heshima mbele ya watu.

### K. Maombi na roho ya kweli (6:5-8)

**6:5** Halafu Yesu alionya wanafunzi wake wasiwe na udanganyifu **wakati wanapoomba**. Haifai wasimame kuomba pahali watu waweze kuwaona na kufikiri wao ni wenye kupenda Mungu sana. Kama wakiomba kwa kuonekana kwa watu tu, hii ndiyo **zawabu** yao – hawatapokea nyingine.

**6:6** Ndani ya mashairi 5 na 7 Yesu alisema juu ya watu kupita mmoja –

"*mu*napoomba … *mu*kiomba", lakini ndani ya shairi 6 alisema na mtu *mmoja mmoja* – "Lakini *wewe*…". Alionyesha hitaji kwa kila mtu peke yake kufika mbele ya Mungu na kumwomba kwa **siri** (**"katika chumba chako cha ndani, na ukikwisha kufunga mlango wako**"). Mungu atajibu maombi namna hii.

Lakini shairi hili halikatazi watu kukutana pamoja kwa maombi. Waamini walifanya hivi kwa mwanzo wa kanisa, (Mdo. 2:42; 12:12; 13:3; 14:23; 20:36). Neno kubwa si *pahali* gani tunapoomba, lakini *kwa sababu gan*i tunaomba; kuonekana mbele ya watu, au kusikiwa na Mungu.

**6:7** Sharti tuepuke kusema maneno bure **mara kwa mara**. Wasioamini wanaombaga hivi, lakini desturi hii haifurahishi Mungu, na hatawasikia kwa sababu ya masemo mengi. Anataka tumwombe na roho ya kweli.

**6:8 Baba yetu anajua mahitaji yetu** hata **wakati tusipomwomba bado.** Kwa sababu gani basi inatupasa kuomba? Kwa sababu kwa njia ya maombi tunakubali hitaji letu, na ya kwamba tunamtegemea yeye tu kwa maneno yote. Ni msingi wa ushirika wetu na Mungu. Na vilevile Mungu anafanya maneno kwa sababu ya maombi (Yak. 4:2d).

**I. Mfano wa ombi (6:9-15)**

**6:9** Watu wengine wanaita mash. 9-13 "Maombi ya Bwana," lakini inatupasa kukumbuka ya kwamba Bwana hakuomba ombi hili yeye mwenyewe hata mara moja. Lilikuwa mfano tu kuongoza wanafunzi wake ndani ya maombi yao. Haikupewa kusudi wajifunze maneno ya ombi hili na nia, na kuyasema tena na tena.

**Baba yetu uliye mbinguni.** Sharti tuombe kwa Mungu Baba. Kwa njia hii tunaonyesha kwamba yeye ni mwenye enzi juu ya ulimwengu mzima.

**Jina lako litukuzwe**. Inatupasa kuanza maombi yetu na kuabudu, tukitoa sifa na heshima kwake anayestahili kuzipokea.

**6:10 Ufalme wako uje**. Nyuma ya kuabudu Mungu, inatupasa kuomba kwa maendeleo ya maneno na kazi yake hapa mpaka siku wakati Mwokozi-Mungu wetu, Bwana Yesu Kristo, atakaposimamisha ufalme wake duniani na kutawala na haki.

**Mapenzi yako yatimizwe.** Wakati tunapoomba neno hili, tunakubali kwamba Mungu anajua maneno gani ni mema zaidi, na ya kwamba tunaacha kufanya mapenzi yetu na tunanyenyekea mapenzi yake. Na tunaonyesha hamu yetu kubwa kuona watu wote wakikubali kutaka kwake duniani pote.

**Hapa duniani kama mbinguni**. Ombi hili linajumlisha mambo yote matatu ya mbele: Hata sasa **mbinguni** Mungu anapokea kuabudu, anatawala juu ya yote, na mapenzi yake yanafanywa. Ombi letu ni kwa maneno haya kutimizwa **duniani** kama **mbinguni.**

**6:11 Utupe leo chakula chetu cha kila siku.** Nyuma ya kuweka mapenzi ya Mungu kwanza tuna ruhusa kutaja mahitaji yetu wenyewe. Tunaonyesha kwamba ni lazima kwetu kutegemea Mungu kwa chakula chetu cha kila siku, cha mwili na cha roho.

**6:12 Utusamehe deni zetu, kama sisi vilevile tunavyosamehe wadeni wetu**. Usamehe huu si usamehe wa zambi zetu (tunapokea usamehe huu kwa njia ya kuamini Mwana wa Mungu tu). Ni usamehe wa baba unaoweza kutengeneza upatano wetu na Mungu Baba wetu tena. Kama waamini wakikataa kusamehe wale ambao wanawakosea, namna gani wanaweza kufikiri wanaweza kuwa na upatano mzuri na Baba yao ambaye amewasamehe zambi zao zote?

**6:13 Na usitulete katika majaribu.** Labda unafikiri ombi hili linakana

Yakobo 1:13 linalosema kwamba Mungu hawezi kujaribu mtu na maovu. Lakini Mungu anaacha watu wake kujaribiwa mara nyingine. Ombi hili linaonyesha kwamba tunafahamu hatuwezi kushinda majaribu kwa njia ya uwezo wetu wenyewe; tutaweza kushinda kwa njia ya kutegemea Mungu na uwezo wake tu.

**Lakini utuokoe toka yule mwovu.** Hili ndilo ombi la watu wote wanaotaka sana kulindwa kila siku toka zambi kwa uwezo wa Mungu.

**Kwa maana ufalme, na uwezo, na utukufu ni wako kwa milele. Amina.** Hata kama maneno haya yakikosa ndani ya miigo mingi ya zamani, ni njia nzuri kuonyesha kwamba msingi wa pekee kwa maombi yetu ni Mungu mwenyewe.

**6:14, 15** Mashairi haya si sehemu ya ombi hili, lakini yanaongeza mafundisho juu ya usamehe ndani ya shairi 12.

### M. Mafundisho ya Yesu juu ya kufunga chakula (6:16-18)

**6:16** Namna ya tatu ya udanganyifu kwa maneno ya dini ambayo Yesu alihamakia ni juu ya kufunga chakula. Wadanganyifu hawa walijaribu kuonekana kama wenye **kufunga** kwa njia ya kuwa na huzuni usoni, mwili wa kukonda, vivi hivi. Lakini Yesu anasema ni bure kujaribu **kuonekana** kama watu watakatifu.

**6:17, 18** Ingepasa waamini wa kweli kufunga kwa siri, bila kuacha neno hili kuonekana kwa macho ya watu. Kusudi la **kupakaa kichwa na mafuta na kunawa uso** ni kuonekana namna tunavyoonekana kila siku. Inatosha kwa Mungu **Baba** kujua kwamba unafunga, na **zawabu** yake ni vizuri kupita ukubali wa watu.

#### KUFUNGA CHAKULA

Watu wanafunga chakula kwa sababu mbalimbali. Labda wanafanya hivi na kusudi, au kwa sababu wanalazimishwa kufunga (kama kwa Mdo. 27:33 au 2 Kor. 11:27). Ndani ya Agano Jipya tunaona kufunga pamoja na maombolezo (Mt. 9:14,15) na maombi (Lk 2:37; Mdo. 14:23). Wenye kufunga pamoja na maombi wanaonyesha kwa njia hii ya kwamba wanatafuta na bidii kujua mapenzi ya Mungu.

Kufunga chakula hakusaidii mtu kupata wokovu, wala kumpa mwamini ukubali na baraka kupita mbele ya Mungu. Siku moja Mfarisayo mmoja alijisifu kwa sababu alifunga chakula mara mbili kila juma, lakini neno hili halikumpatia haki ambayo alitafuta (Lk 18:12,14). Lakini wakati Mkristo anapofunga kwa kupendeza Mungu na kutambua kutaka kwake, Mungu anaona hamu yake kumpendeza na anampa zawabu. Hakuna agizo ndani ya Agano Jipya kwa Wakristo kufunga chakula, lakini tunaona kwamba ni neno zuri kwani kuna ahadi ya zawabu. Kufunga chakula kunaweza kutusaidia kutambua mapenzi ya Mungu kwa wakati wa matata, na kunatusaidia kujitawala mwenyewe. Inapasa mtu kufunga peke yake mbele ya Mungu tu na kusudi la kumpendeza yeye. Haina faida kama tukisukumwa kufunga kwa kuonana mbele ya watu. ❖

### N. Kujiwekea hazina mbinguni (6:19-21)

Mashairi haya ni mengine ya mafundisho magumu zaidi ya Bwana wetu, na mafundisho ambayo watu hawaweki roho juu yao mara nyingi. Baki la sura hii ni juu ya kuweza kukaa pasipo hofu na mashaka kwa wakati wa kuja.

**6:19,20** Mafundisho ya Yesu ndani ya mashairi 19-21 yanashindana kabisa na mawazo ya watu juu ya namna gani kujipatia mali ya kutosha kwa mahitaji yao kwa wakati wa kuja. Wakati Bwana anaposema, **"Musijiwekee hazina du-**

**niani"** anaonyesha kwamba vitu vya dunia haviwezi kuwapatia salama kwa wakati wa kuja. Vitu vyo vyote vya **dunia** vinaweza kuharibiwa na tufani au mvua (**nondo au kutu**), au mwizi anaweza kuviiba. Mali yo yote isiyoweza kupotea au kuharibika ni kazi unayofanya kwa Kristo sasa na inayoandikwa mbinguni. Ni hazina yako mbingini itakayopata zawabu kwa wakati wa kuja.

**6:21** Msingi wa mafundisho haya magumu ni huu: **"pahali hazina yako iko, pahali moyo wako utakapokuwa vilevile."** Mali yako ikiwa ndani ya sanduku katika banki, mawazo yako yatakuwa pale vilevile. Mafundisho haya yanatulazimisha kujaribu kufahamu maana ya masemo ya Bwana Yesu na kujiuliza, "nitafanya nini na hazina yangu ya dunia?"

### O. Taa ya mwili (6:22,23)

Yesu alifahamu kwamba itakuwa nguvu sana kwa wanafunzi wake kufahamu namna gani wataweza kutii mafundisho haya juu ya kuweza kukaa na salama juu ya mahitaji yao kwa wakati wa kuja. Hivi alitumika na jicho kwa mfano wa kuona kwa roho. Alisema **jicho ni taa ya mwili**. Kwa njia ya jicho tunapata nuru na tunaweza kuona. **Jicho likiwa safi, mwili wako wote** utajaa nuru. **Lakini jicho lako likiwa baya,** hutaweza kuona vizuri, na kwa pahali pa nuru kuna **giza**.

Hii ndiyo maana ya mashairi haya: Mtu mwenye jicho safi ndiye aliye na makusudi safi, anayeweka roho juu ya maneno ya Mungu tu, na anayepokea na kutii mafundisho ya Kristo. Maisha yake yote yanaangazwa na nuru. Anaamini masemo ya Yesu, anaachana na mali ya dunia, anajiwekea hazina mbinguni, na anafahamu ya kwamba kwa njia hii tu anaweza kukaa bila woga na mashaka. Lakini jicho baya ndilo jicho la yule anayejaribu kubaki na mali yake ya dunia hii pamoja na kuweka hazina mbinguni vilevile. Hafahamu namna gani anaweza kutii mafundisho haya ya Yesu – roho yake ni giza.

Halafu Yesu anaongeza kusema: **nuru iliyo ndani yako ikiwa giza, ni giza kubwa sana!** Au kusema, ukijua Kristo anakukataza kutegemea mali ya dunia, lakini ukikaa kufanya hivi, halafu mafundisho haya usiyotii yanageuka giza kwako – upofu mkubwa wa roho kwa maneno ya mali ya dunia.

### P. Huwezi kutumikia Mungu na mali (6:24)

Kueleza mafundisho haya Bwana Yesu alitumika na mfano wa **bwana wa kazi** na watumwa. **Hakuna mtu anayeweza kutumikia bwana wawili.** Bila shaka atakuwa na heshima na uaminifu kwa **mmoja** kupita mwingine. Ni vivyo hivyo na **Mungu na mali.** Ni lazima kwa sisi kuchagua kama tutaweka Mungu kwanza katika maisha yetu, au kama tutaweka vitu vya dunia, vitu vya sasa kwanza, na kukataa kutawaliwa na Mungu.

### Q. Usiwe na mashaka (6:25-34)

**6:25** Ndani ya mashairi haya Yesu anaonyesha tena ya kwamba tunajaribiwa kusumbuka sana juu ya vyakula na mavazi, na kusahau kusudi la kweli la Mungu kwa maisha yetu. Watu hawasumbuki zaidi juu ya mahitaji yao ya *leo* lakini juu ya yale nyuma ya muda wa miaka makumi mbili au makumi tatu. Ni zambi kusumbuka juu ya mahitaji yetu kwa wakati wa kuja, kwani kufanya hivi ni kukana kwamba Mungu ni mwenye mapendo, hekima na uwezo. Kusumbuka hivi kunaonyesha kwamba tunakana mapendo ya Mungu na ya kwamba anaweka roho juu ya mahitaji yetu. Ni kama tunasema Mungu hafahamu maneno anayofanya, na ya kwamba anakosa uwezo kutupatia vitu tunavyohitaji.

Masumbuko namna hii yanatusukuma kutumika na roho na nguvu yote kujipatia mali ya kutosha kwa mahitaji yetu kwa wakati wa kuja. Miaka yetu inapita mbio, na tunafikia mwisho wa uzima wetu bila kutimiza kusudi la Mungu kwa maisha yetu. Mungu hakutuumba kwa sura yake ili tule vyakula tu. Tuko hapa tuweze kumpenda, kumwabudu na kumtumikia na kusimamia kazi yake hapa duniani. Mungu anakusudi kwa miili yetu kuwa watumishi wetu, si bwana wetu.

**6:26 Ndege za anga** ni mfano wa namna Mungu anavyolinda viumbe vyake. Vinatufundisha kwamba ni bure kabisa kwa sisi kusumbuka. Ndege hawapandi vyakula wala hawavuni, lakini Mungu anawalisha. Kwa macho yake watu ni damani kuliko ndege, hivi tunaweza kujua kabisa ya kwamba Mungu atatupatia vyote tunavyohitaji.

Lakini shairi hili halifundishi kwamba hatuhitaji kutumika kazi kutupatia vitu tunavyohitaji kwa wakati wa sasa. Paulo anatukumbusha kwamba "kama mtu hataki kufanya kazi, basi asile chakula" (2 Tes. 3:10). Na haifai tufikiri kwamba ni vibaya kwa mlimaji shamba kupanda mbegu na kuvuna. Kazi hii inahitajiwa kumpatia vitu anavyohitaji sasa. Lakini Yesu anatukataza kuzidisha magala ya nafaka kwa mahitaji yetu kwa wakati wa kuja (alikataza neno hili vilevile ndani ya habari za tajiri mpumbavu katika Luka 12:16-21).

**6:27** Kusumbuka juu ya mahitaji ya wakati wa kuja ni kuaibisha Mungu, na haina faida kabisa. Bwana Yesu alisema neno hili waziwazi wakati aliposema, **"Nani katikati yenu akisumbuka anaweza kuongeza kimo cha mwili wake mkono mmoja?"** Mtu mfupi hawezi kujifanyiza kuwa mrefu kupita. Kujivimbishia mali yote tutakayohitaji kwa wakati wa kuja ni neno lisilowezekana kwa wakati wa sasa vilevile.

**6:28-30** Bwana aliendelea kuonyesha upumbavu wa kusumbuka kwamba hatutakuwa na mavazi ya kutosha kwa wakati wa kuja. **Maua ya shamba hayafanyi kazi, wala hayasokoti**, lakini mapambo yao yanapita mapambo ya mavazi ya kifalme ya mfalme Solomono. Kama Mungu akiweza kuleta mavazi ya mapambo namna hii kwa maua ya shamba yanayodumu kwa muda mfupi tu mbele ya kuharibika, bila shaka atalinda watu wake ambao wanamwabudu na kumtumikia.

**6:31, 32** Hivi haifai kwetu kupoteza maisha yetu tukitafuta vyakula, vinyweo na mavazi tutakayohitaji kwa wakati wa kuja. **Mataifa** wasiookolewa wanasumbuka sana kujivimbishia maneno haya kama ndiyo maneno makubwa ya pekee ya maisha ya sasa. Lakini neno hili halifai kwa Wakristo walio na **Baba mbinguni anayejua** mahitaji yao.

Kusudi la Wakristo likiwa kujipatia mali sasa kwa mahitaji yao yote kwa wakati wa kuja, ingepasa watumike na saa zao zote kujivimbishia mali. Hawawezi kujua kamwe kama wamepata mali ya kutosha, kwani maneno mbalimbali kama ugonjwa na vita, yanaweza kupunguza faida ya mali ambayo walijiwekea. Kama wakiishi hivi, Mungu angeibwa faida ya utumishi wao. Aliumba wanaume na wanawake kwa sura yake, na kuwaokoa, lakini wangeishi bila salama hapa duniani kwa pahali pa kuishi kwa maneno yaliyo na faida kwa milele.

**6:33** Hivi Bwana anafanya mapatano na watu wake. Ni kama anasema nasi, "Kama wewe ukiweka Mungu na maneno yake kwanza ndani ya maisha yako, ninaahidi kukupa vyote unavyohitaji. **Ukitafuta kwanza ufalme wa Mungu na haki yake,** halafu hutakosa kamwe vitu unavyohitaji sasa."

**6:34** Ni kazi ya mwamini kuishi kwa Bwana, akimtegemea na imani isiyo-

tikisika kwamba atampatia vyote atakavyohitaji. Kazi ya mshahara ni kwa mahitaji ya maisha ya leo leo. Mali tunavyopata kwa njia ya kazi hii, na isiyohitajiwa kwa mahitaji ya kila siku ni kwa kazi ya Bwana. Tunaagizwa kuishi kwa siku ya leo tu bila kusumbukia mahitaji ya kesho, kwani **kesho itajisumbukia yenyewe.**

### R. Usihukumu (7:1-6)

Mashairi haya juu ya kuhukumu yanafuata mara moja mafundisho ya Bwana juu ya mali ya dunia. Kwa nini? Kwa sababu ni nyepesi kwa Wakristo walioacha vyote kufuata Yesu kuhukumu Wakristo wenye mali nyingi. Na vivyo hivyo ni nyepesi kwa Wakristo wenye mali wanaoweka roho juu ya kuweka akiba kwa mahitaji ya jamaa yao kwa wakati wa kuja, kupunguza ukali wa agizo la Bwana Yesu kwa mwisho wa sura 6. Hakuna mtu hata mmoja anayeishi kabisa kwa imani, hivi hukumu namna hii haifai.

Kuna maneno mengine ambayo tunakatazwa kuhukumu: Haifai tuhukumu makusudi ya watu, maana kwa sababu gani wanafanya hivi au hivi. Mungu tu anayajua; sisi tunakatazwa kuhukumu maneno tunayoweza kuona kwa macho tu (Yn. 7:24; Yak. 2:1-4). Haifai tuhukumu wenye zamiri zaifu wanaoogopa kufanya maneno mengine yasiyo mabaya (Rom. 14:1-5). Haifai tuhukumu utumishi wa Mkristo mwingine (1 Kor. 4:1-5); na haifai tuhukumu Mkristo mwenzetu kwa njia ya kusema maneno mabaya juu yake (Yak. 4:11,12).

**7:1** Mara nyingine watu hawafahamu maana ya kweli ya maneno haya ya Yesu, na wanafikiri inapasa kukataza kila namna ya hukumu na wanasema **"Musihukumu ili musihukumiwe."** Lakini Yesu hafundishi kwamba inatupasa kuacha kutumika na akili tuliyopewa kutambua uzuri na ubaya wa maneno. Ndani ya Agano Jipya tunasoma tena na tena juu ya kuhukumiwa kwa haki kwa matendo au mafundisho ya watu wengine. Na kwa mambo mengine Wakristo wanaagizwa kukata maneno, kuonyesha nini iliyo mema au mabaya, au nini ni mema au mema zaidi. Waza juu ya mambo kama haya:

1. Magomvi yakitokea katikati ya waamini, inapasa maneno haya kuhukumiwa na watu wa kanisa (1 Kor. 6:1-8).
2. Sharti kanisa lihukumu zambi kubwa za watu wa kanisa hili, na kutenda namna Maandiko yanavyoagiza (Mt. 18:17; 1 Kor. 5:9-13).
3. Waamini wanaagizwa kujaribu mafundisho ya walimu na wahubiri kuona kama yakipatana na Neno la Mungu (Mt. 7:15-20; 1 Kor. 14:29; 1 Yn. 4:1).
4. Inapasa Wakristo kutii agizo la Paulo ndani ya 2 Kor. 6:14 na kutambua kama watu fulani ni waamini wa kweli.
5. Inapasa watu wa kanisa kutambua wanaume gani katikati yao wanastahili kufanya kazi ya wazee na watumishi (1 Tim. 3:1-13).
6. Inatupasa kutambua watu gani hawakai kwa utaratibu; wanyonge au walio zaifu, vivi hivi, na kuwatendea namna tunavyofundishwa ndani ya Biblia (kwa mfano ona 1 Tes. 5:14).

**7:2** Yesu alionya ya kwamba watu watahukumiwa kwa namna wanavyohukumu watu wengine. "Kwa kuwa **hukumu ambayo munahukumu ndiyo mutahukumiwa."** Tunaona neno hili ndani ya kupanda na kuvuna katika maneno ya maisha yetu ya kila siku. Ona Marko 4:24 na Luka 6:38.

**7:3-5** Yesu alionyesha desturi ya watu kuona kuanguka au uzaifu kidogo ndani ya mtu mwingine bila kufahamu kwamba wao wanaanguka kwa njia hii vilevile. Alizidisha na kusudi ukubwa

wa kosa hili kwa njia ya kusema juu ya mtu anayeona **kitakataka** ndani ya **jicho** la ndugu yake, bila kufahamu kwamba yeye ana **boriti** ndani ya jicho lake mwenyewe. Ni udanganyifu kwa sisi kuwaza tunaweza kusaidia mtu mwingine kushinda kosa fulani ndani ya maisha yake kama tukishikwa na kosa kubwa kupita lake sisi wenyewe. Sharti tutengeneze makosa yetu wenyewe kwanza, mbele ya kuhukumu makosa ndani ya maisha ya watu wengine.

**7:6** Shairi hili linahakikisha ya kwamba Bwana Yesu hakukataza *kila* namna ya hukumu. Alisema na wanafunzi wake ya kwamba haifai **kuwapa imbwa** kilicho kitakatifu wala **kutupa lulu mbele ya nguruwe.** Kwa wakati wa sheria ya Musa imbwa na nguruwe zilikuwa nyama wachafu, na ndani ya shairi hili ni mfano wa watu waovu. Wakati tunapokutana na watu waovu wanaozarau kweli ya Mungu kabisa na kupokea mahubiri yetu na matukano na jeuri, si lazima kwetu kukaa kuwahubiri Habari Njema. Kukaa kufanya hivi kunaongeza hukumu yao.

Tunahitaji ufahamu toka Roho Mtakatifu kutambua watu wa namna hii. Labda ni kwa sababu hii Bwana Yesu anaendelea na kutoa mafundisho juu ya maombi, tuweze kuomba kupewa hekima.

### S. Kaa kuomba, kutafuta, kupiga mlango (7:7-12)

**7:7,8** Tukifikiri kwamba tunaweza kutii mafundisho ya hotuba hii kwa nguvu yetu wenyewe, hatujafahamu bado ya kwamba namna ya maisha haya ambayo Bwana anataka tuishi si namna ya maisha ya dunia. Akili na uwezo kwa kuishi maisha ya namna hii zinaweza kutoka juu tu. Hivi mashairi haya yanatuita **kuomba** na kukaa kuomba, **kutafuta** na kukaa kutafuta, **kupiga mlango** na kukaa kupiga mlango. Wakristo wote wanaodumu katika maombi na roho ya kweli watapewa hekima na uwezo.

Ukisoma mashairi haya peke yao, labda utafikiri yanafundisha kwamba unaweza kupokea kitu cho chote unachoomba. Neno hili si kweli hata kidogo. Sharti tuyafahamu pamoja na mashairi yaliyotangulia, na pamoja na kukumbuka mafundisho ya Biblia nzima juu ya maombi. Kwa mfano, ndani ya Zaburi 66:18 tunaona ya kwamba haifai kwa mwenye kuomba kuwa na zambi ndani ya maisha yake ambayo hayakiri. Sharti Mkristo aombe na imani (Yak. 1:6-8), na lazima maombi yake yapatane na mapenzi ya Mungu (1 Yn. 5:14). Sharti tudumu katika maombi (Lk. 18:1-8), na roho ya kweli (Ebr. 10:22a).

**7:9-10** Hivi maneno haya yote yakitimizwa ndani ya maisha ya Mkristo, anaweza kujua kabisa kwamba Mungu atasikia na kujibu maombi yake, kwa sababu yeye ni Baba yetu. Tunajua kwamba hapa duniani mwana **akiomba baba kumpa mkate**, **baba hatampa jiwe**. Na mtoto akiomba **samaki, hatampa nyoka.** Hakuna baba ya dunia ambaye atampa mwana wake kitu ambacho kitamwumiza.

**7:11** Basi hata wazazi wa dunia wakijibu maombi ya watoto wao kwa njia ya kuwapa yaliyo mema kupita, **zaidi sana Baba yetu aliye mbinguni** atafanya vivyo.

**7:12** Baba yetu akiwa mwenye kutuolea vitu vyema, ingetupasa sisi kumwiga kwa njia ya kutendea watu wengine mema. Tunaweza kupima faida ya matendo yetu kwa njia ya kujiuliza kama tungefurahi kwa watu kututendea sisi vivyo hivyo.

Yesu alisema kwamba kufanya hivi ni **torati na manabii,** maana kunatimiza mafundisho ya roho ya **sheria** ya Musa na maandiko ya **manabii** ya Israeli. Haki iliyoagizwa ndani ya Agano la Kale inatimizwa ndani ya waamini wa sasa

wanaotembea kufuata maneno ya Roho (Rom. 8:4). Kama waamini wote wangetii shairi hili, mambo mengi yangetengenea ndani ya jamaa zetu, makanisa yetu, na hata ndani ya serikali duniani.

**T. Njia inayosonga (7:13,14)**

Bwana anaonyesha sasa ya kwamba mlango ni **mwembamba** sana na njia ya kufuata Bwana **inasonga,** maana yake ni **nguvu**. Lakini wale wanaofuata mafundisho yake na uaminifu watajuana na **uzima** wa baraka. Lakini kuna **mlango mpana** vilevile – maisha ya anasa na ya kujipendeza mwenyewe. Mwisho wa maisha ya namna hii ni upotevu. Mafundisho ya mashairi haya si juu ya kupoteza uzima wa milele, lakini juu ya kukosa kutimiza kusudi la Mungu kwa maisha yetu hapa duniani.

Inawezekana kutumika na mashairi haya kwa kuhubiri Habari Njema vilevile. Yanaonyesha njia mbili zinazofika kwa pahali mbalimbali. Mlango mpana na njia pana zinafikisha watu hata upotevu (Mez.16:25). Mlango mwembamba na njia inayosonga inawafikisha hata uzima. Yesu ni mlango (Yn. 10:9) na njia (Yn. 14:6). Ni *mfano* mzuri wa Habari Njema, lakini *mafundisho* ya mashairi haya ni kwa waamini. Yesu anasema ya kwamba watahitaji imani kwa kumfuata, na kujitawala wenyewe, na kuvumilia taabu. Lakini hata hivi maisha haya magumu ni maisha ya faida. Ukichagua njia nyepesi utakuwa na rafiki wengi, lakini utakosa kupokea baraka kubwa zaidi ambayo Mungu amekutayarishia.

**U. Mutawatambua kwa njia ya matunda yao (7:15-20)**

**7:15** Kila pahali watu wanapofundishwa kujitoa mzima kufuata Bwana, **manabii ya uwongo** wanaonekana vilevile, wanaosema ni vizuri kuingia kwa mlango mpana na kuchagua njia nyepesi kabisa. Wanakiri kwamba wanasema maneno ya Mungu wakivaa mavazi ya kondoo na kuonekana kama waamini wa kweli, lakini rohoni wao ni imbwa wakali za mwitu. Maana yake, wao ni wasioamini waovu wanaoteka waamini wasiokomea kwanza wala kusimama imara.

**7:16-18** Mashairi haya yanatufundisha namna gani tunaweza kutambua manabii ya uwongo: **mutawatambua kwa njia ya matunda yao**. Maisha yao ya uasherati na mafundisho yao ya kuharibu yanaonyesha kweli ya roho zao. Miiba haiwezi kuzaa zabibu, na mibaruti haizai tini. Neno hili ni kweli katika mapando ya dunia na ni kweli kwa maneno ya roho vilevile. Sharti tupime mwenendo na mafundisho ya wale wanaosema wako wasemaji kwa ajili ya Mungu. "Kama hawasemi sawasawa na neno hili kweli hakuna asubui kwao" (Isa. 8:20).

**7:19,20** Mwisho wa manabii wa uwongo ni **kutupwa katika moto**. Hukumu ya walimu wa uwongo "ni uharibifu usiokawia" (2 Pet. 2:1). Inawezekana kuwatambua kwa njia ya matunda yao.

**V. Sikuwajua ninyi (7:21-23)**

**7:21** Bwana Yesu anaendelea kusema sharti tukae na ange kwa watu wanaokiri kuwa waamini wa Yesu, lakini wasiookolewa kamwe. **Si kila mtu** anayeita Yesu **"Bwana, Bwana," atakayeingia ufalme wa mbinguni**. Wale tu wanaofanya **mapenzi ya Mungu** wataingia ufalme. Neno la kwanza, ukitaka kufanya mapenzi ya Mungu, ni kuamini Bwana Yesu (Yn. 6:29).

**7:22, 23** Siku ya hukumu wakati wasioamini watakaposimama mbele ya Kristo (Ufu. 20:11-15) **watu wengi** watamkumbusha kwamba **walitabiri,** au **kutoa pepo wachafu**, au kufanya **matendo mengi ya uwezo** – yote kwa jina lake, lakini masemo yao yatakuwa bure. Yesu atawaambia kwamba hakuwajua

kamwe.

Mashairi haya yanaonyesha kwamba si maajabu yote yanafanywa na Yesu, na ya kwamba si watenda wote wa maajabu ni wafuata wa Bwana. Ajabu ndilo tendo linalotendwa kwa uwezo mkubwa kupita uwezo wa mtu. Uwezo huu unaweza kutoka kwa Mungu au Shetani. Shetani anaweza kuwapa watumishi wake uwezo kutoa pepo wachafu kwa muda mdogo kufikirisha watu kwamba ajabu hili linatoka kwa Mungu. Hatengi ufalme wake kushindana nao wenyewe wakati anapofanya hivi, lakini anatayarisha njia kwa kazi hata kubwa kuliko kwa pepo wachafu kwa wakati wa kuja.

**W. Jenga juu ya Mwamba (7:24-29)**

**7:24,25** Yesu anamaliza hotuba yake na mfano kuonyesha kwamba kutii ndilo neno kubwa sana. Haitoshi kusikia tu masemo haya – lazima tuyatii vilevile. Mwanafunzi **anayesikia** na **kutii** maagizo ya Bwana ni kama **mwenye akili anayejenga nyumba yake juu ya mwamba**. Nyumba yake (ndiyo maisha yake) ina msingi wa nguvu, na wakati inapopigwa na **mvua na tufani**, haitaangushwa.

**7:26,27** Mtu **anayesikia masemo** ya Yesu **bila kuyatii** ni kama **mpumbavu anayejenga nyumba yake juu ya mchanga**. Mtu huyu hataweza kusimama imara kwa wakati wa taabu na mambo magumu. Wakati wa kunyesha kwa **mvua** pamoja na **tufani,** nyumba yake itaanguka, kwa sababu ilikosa msingi wa nguvu.

Kama mtu akiishi na kutii maagizo ya Yesu ndani ya hotuba hii, ataitwa mpumbavu na watu wa dunia, lakini Yesu anamwita **mwenye akili.** Watu wa dunia wanafikiri mwenye akili ndiye anayeishi kujifurahisha kwa wakati wa sasa tu. Yesu anamwita mpumbavu. Tunaweza kutumika na habari za mwenye akili na mpumbavu kama mfano wa Habari Njema. Mwenye akili anaweka tumaini lake lote ndani ya Mwamba, ndiye Kristo, na kumtumainia yeye tu kama Bwana na Mwokozi. Mpumbavu anakataa kutubu na kupokea Yesu kama tumaini la pekee kwa kupata wokovu. Lakini zaidi mashairi haya ni maonyo kwa maisha ya kila siku ya Wakristo.

**7:28,29** Basi Bwana Yesu **alimaliza** hotuba yake, na **wasikiaji wake walishangaa** kabisa kwa mafundisho yake. Walitambua tofauti katikati ya mafundisho ya Yesu na yale ya waandishi. Bwana alisema na amri; masemo ya waandishi yalikosa uwezo.

## 5. MAAJABU YA UWEZO NA NEEMA YA MASIYA, NA MAWAZO YA WATU JUU YAO (8:1 – 9:34)

Ndani ya sura 8-12 Bwana Yesu alionyesha waziwazi ya kwamba yeye ndiye Masiya ambaye manabii walitabiri juu yake. Kwa mfano Isaya alitabiri kwamba Masiya atafungua macho ya vipofu na masikio ya viziwi, ataponyesha viwete na kuwezesha bubu kuimba (35:5,6). Kwa njia ya kufanya maneno haya yote Yesu alihakikisha kwamba alikuwa Masiya wa Israeli. Kama Waisraeli wangalisoma Maandiko Matakatifu wangalifahamu yeye ndiye Kristo.

Habari ndani ya 8:1 – 9:34 si habari za kazi zote Bwana alizofanya. Ni habari fulani zilizochaguliwa na Roho Mtakatifu kuonyesha maneno fulani ya maisha ya Mwokozi, kama:

1. Amri zote za Kristo juu ya magonjwa, pepo wachafu, mauti, na viumbe vya ulimwengu kama tufani, na mawimbi.
2. Amri yake kutawala kabisa maneno yote ya maisha ya wafuata wake.
3. Kuongezeka kwa kukatalika kwa Yesu na taifa la Israeli, zaidi na viongozi vyao kwa maneno ya dini.
4. Watu mmoja mmoja wa Mataifa

wakipokea Mwokozi.

**A. Uwezo juu ya ukoma (8:1-4)**

**8:1** Hata kama mafundisho ya Yesu yalikuwa magumu, yalikokota watu kwake kumsikiliza, na tunasoma kwamba **makutano makubwa** yalimfuata.

**8:2** Mkoma mmoja alipiga magoti mbele ya Bwana na kumsihi kumponyesha. Mkoma aliamini kabisa ya kwamba Bwana aliweza kumponyesha, na Bwana haoni imani ya kweli ya mtu ye yote bure kamwe. Ukoma ni mfano wa zambi kwani ni ugonjwa mbaya sana unaoharibu viungo vya mtu, na unaoweza kupitishwa kwa watu wengine. Ukoma ni namna namna; hakuna dawa kuponyesha ukoma namna nyingine.

**8:3** Haikufaa kugusa mkoma. Myuda aliyegusa mkoma alichafuwa kwa maneno ya dini, maana hakuweza kuabudu pamoja na Wayuda wengine. Lakini Bwana Yesu **aligusa** mkoma yule, akasema naye "usafishwe," na **ukoma** wake ulisafishwa **mara moja**. Mwokozi wetu ana uwezo kutusafisha toka zambi, na kuwezesha mtu aliyesafishwa kuwa mwabudaji.

**8:4** Hii ni mara ya kwanza tunayosoma ndani ya Habari Njema ya Matayo ya kwamba Yesu **alikataza watu kupasha habari za ajabu** waliyotendewa au maneno waliyoona (ona vilevile 9:30; 12:16; 17;9; Marko 5:43; 7:36; 8:26). Tunafikiri alifanya hivi kwa sababu watu wengi walitaka kumfanyiza mfalme ili kuponyeshwa toka utawala wa Waroma. Na alijua taifa la Israeli walikuwa hawajatubu bado, hawatataka kuongozwa naye kwa maneno ya Mungu, na vilevile ilikuwa lazima aende msalaba kwanza.

Kwa wakati wa sheria ya Musa **kuhani** alikuwa na kazi ya mganga vilevile. Wakati mkoma aliposafishwa ilimpasa kuleta sadaka na kutokea mbele ya kuhani, aliyeweza kutangaza kwamba mkoma ni safi (Law. 14:4-6). Bila shaka mkoma mmoja mmoja tu alisafishwa. Lilikuwa tukio la kushangaza sana, na lingalipasa kusukuma kuhani kutafuta kama Masiya, ambaye walimngojea tangu miaka mingi, alikuwa ametokea. Lakini hakufanya hivi. Yesu aliagiza mkoma kutii sheria ndani ya neno hili.

Maana kwa maneno ya roho ni wazi. Masiya alikuwa ametokea na uwezo kuponyesha taifa la Israeli toka ugonjwa wake wa zambi. Alifanya ajabu hili kuhakikisha kwamba yeye ndiye Masiya, lakini Waisraeli hawajakuwa tayari bado kwa Mwokozi wao.

**B. Uwezo juu ya ugonjwa wa kupooza (8:5-13)**

**8:5,6** Imani ya **akida** Mtaifa huyu ilikuwa namna nyingine na kutokuamini kwa Wayuda. Hata kama taifa la Israeli walikataa kupokea Mfalme wao, atapokewa na watu wazarauliwa wa wapagano. Akida huyu la Waroma alikuwa juu ya watu karibu mia moja katika au karibu na Kapernaumu. **Alifikia** Yesu kumwomba kuponyesha **mtumishi** wake aliyeteswa sana na ugonjwa wa kupooza. Lilikuwa ajabu kuona roho ya huruma namna hii ya akida – zaidi ya maakida walikosa huruma kwa watumishi wao.

**8:7-9** Wakati **Yesu** aliposema atafika kwake kuponyesha mtumishi mgonjwa tunaona ya kwamba **akida** alikuwa na imani kubwa kweli. Alisema maneno kama haya: "Sistahili kukupokea nyumbani mwangu. Na vilevile neno hili halihitajiwi kwani unaweza kumponyesha kwa njia ya kusema **neno** tu. Ninafahamu kama kuwa na **amri** ni nini. Wakubwa wangu wananiagiza maneno, nami ninatolea maagizo kwa watumishi wangu. Watumishi wangu wananitii mara moja. Masemo yako yatakuwa na uwezo mkubwa zaidi kuponyesha mtumishi wangu!"

**8:10-12** Yesu **alishangaa** juu ya imani ya akida. Tunasoma mara mbili tu juu

ya Yesu akishangaa. Alishangaa vilevile juu ya kutokuamini kwa Wayuda (Mk. 6:6). **Hakukuta imani kubwa** namna hii mbele katikati ya watu wachaguliwa wa Mungu, ndilo taifa la Israeli. Neno hili lilimsukuma kusema ya kwamba kwa wakati wa kuja watu wengi wa Mataifa toka pahali mbalimbali duniani watafikia ufalme wake na kufurahishwa na ushirika na watu wakubwa wa zamani wa Wayuda kama Abrahamu, Isaka na Yakobo. Lakini **wana wa ufalme** watatupwa katika **giza la inje** pahali kutakapokuwa kulia na kusaga **meno. Wana wa ufalme** ndio wale waliozaliwa Wayuda, waliosema kwamba Mungu ni Mfalme, lakini wasiozaliwa tena kweli. Vivyo hivyo kwa wakati wa sasa watoto wengi wanaobarikiwa kwa njia ya kuwa na wazazi Wakristo, watapotea katika hadeze kwa sababu wanakataa Kristo, lakini wapagano wasiobarikiwa hivi watafurahishwa na utukufu wa milele mbinguni kwa sababu waliamini Habari Njema.

**8:13 Yesu akamwambia akida: "Kwenda zako; iwe kwako kama ulivyoamini."** Zawabu ya imani ni kwa kipimo cha imani. **Mtumishi wake akapona** saa ile ile, hata kama Yesu hakuwa pahali penyewe. Neno hili ni mfano wa kazi ya Kristo kwa wakati wa sasa; akisaidia watu wa Mataifa wanaofungwa na ugonjwa wa zambi, hata wakati yeye si hapa katika mwili.

### C. Uwezo juu ya homa (8:14,15)

Wakati Yesu alipoingia nyumba ya Petro, alikuta mama ya mke wake ni mgonjwa na alishikwa na homa. Aligusa mkono wake, na homa yake ilimwondokea mara moja. Homa inaacha mgonjwa na uzaifu kwanza, lakini mwanamke huyu alikuwa na afya na nguvu mara moja, hata aliweza kutoka kitanda na kutumikia Bwana mara moja – njia nzuri kuonyesha asante yake kwa neno ambalo Mwokozi alimfanyia. Ingetupasa sisi kumwiga, na wakati tunapokwisha kuponyeshwa toka ugonjwa kumtumikia na bidii mpya.

### D. Uwezo juu ya pepo wachafu na magonjwa namna namna (8:16, 17)

**Mangaribi**, kwa mwisho wa sabato (ona Marko 1:21-34), watu **wengi** walimzunguka, pamoja na **wengi** waliokaaliwa na kutawaliwa na pepo wachafu. Mara nyingine watu wale wenye pepo walikuwa na akili na nguvu zaidi; mara nyingi waliteswa. Mara nyingine matendo yao yalifanana na matendo ya wazimu, lakini hawakuwa wazimu. Yesu **akatoa pepo wachafu kwa neno lake.**

**Aliponyesha vilevile wote waliokuwa na magonjwa,** akitimiza unabii wa Isaya 53:4, **"Kweli amechukua taabu zetu, na amebeba huzuni zetu."** Hapa Roho Mtakatifu alitumika na unabii huu kusema juu ya kazi ya Mwokozi wetu kuponyesha wagonjwa duniani, *si* juu ya kazi yake msalabani.

Kufika sasa ndani ya sura hii tumeona maajabu mane:

1. Kuponyeshwa kwa mkoma Myuda, Kristo akiwa palepale.
2. Kuponyeshwa kwa mtumishi wa akida, pasipo Kristo akiwa pahali penyewe.
3. Kuponyeshwa kwa mama ya mke wa Petro, Yesu akiwa pamoja nao nyumbani.
4. Kuponyeshwa kwa wagonjwa na wenye pepo wachafu wote, Yesu akiwa pamoja nao.

### E. Ajabu la kukataliwa na watu (8:18-22)

Tumeona amri ya Kristo juu ya gonjwa na pepo wachafu. Sasa tunaona wanaume na wanawake wakishindana naye – ajabu la kukataliwa na watu.

**8:18-20** Wakati **Yesu** alipokuwa tayari kuvuka Bahari ya Galilaya toka

Kapernaumu kwa upande wa mashariki, mwandishi mmoja mwenye kujitegemea mwenyewe alikwendea Bwana, akamwambia kwamba atamfuata pahali po pote atakapokwenda. Bwana alimjibu lazima afahamu bei ya ahadi hii, ndiyo maisha ya kujikania mwenyewe, **"Mbweha wana pango, na ndege za anga wana vioto; lakini Mwana wa watu hana pahali pa kulalisha kichwa chake."** Kwa muda wa utumishi wake katikati ya watu Bwana Yesu hakuwa na nyumba. Ndiyo, kulikuwa na watu ambao walimpokea na furaha nyumbani mwao na hakukosa pahali pa kulala. Lakini kwa maneno ya roho hakuweza kupata raha ya kweli na ya kudumu hapa duniani. Alikuwa na kazi ambayo ilimpasa kutimiza mbele ya kustarehe. Ni vivyo hivyo na wafuata wake; dunia hii si pahali pa raha yao, na haifai kuwa pahali pao kustarehe.

**8:21** Mwingine wa wanafunzi wake alimwambia Bwana kwamba alikuwa tayari kumfuata, lakini kulikuwa na neno lingine ambalo alitaka kufanya kwanza. Alisema, **"Bwana, uniruhusu kwanza kuzika baba yangu."** Hatujui kama baba huyu alikuwa amekufa au alikuwa kwanza hai. Mtu huyu aliweka mapenzi yake mwenyewe mbele ya mapenzi ya Bwana, hivi alisema "Uniruhusu kwanza," maana yake **"Bwana … mimi kwanza."** Si vibaya kwa mtu kutayarisha maziko ya baba yake, lakini tendo hili linageuka kuwa baya wakati tunapoliweka mbele ya mwito wa Mwokozi.

**8:22** Yesu alimjibu kwamba kazi yake ya kwanza ni "**kunifuata Mimi**." Vizuri watu wale **walio wafu rohoni wazike wale waliokuwa wamekufa mwilini**. Msiyeamini anaweza kufanya kazi namna ile, lakini kuna kazi ambayo *wewe tu* unaweza kufanya. Tumika na nguvu yako yote kwa maneno yaliyo na faida kwa milele. Usipoteze maisha yako ukitenda maneno bure." Hatusomi kama watu hawa wawili walifanya nini nyuma ya kusikia maonyo ya Bwana, lakini ni kama waliacha kufuata Bwana, na walichagua kukaa vizuri hapa duniani. Mbele ya kuwahukumu, vizuri tupime roho zetu wenyewe kuona kama sisi ni tayari kufuata na kutii Yesu kwa njia hizi mbili.

### F. Amri juu ya tufani na mawimbi (8:23-27)

Bahari ya Galilaya ilijulikana kwa sababu ya tufani zilizotokea gafula toka bonde la Yorodani kwa upande wa kaskazini. Kwa wakati wa tufani namna hii ni hatari kabisa kwa wabaharia.

Mara hii Yesu alikuwa akivuka bahari toka pwani ya mangaribi kwenda pwani ya mashariki. Alikuwa akilala usingizi ndani ya chombo wakati upepo ulipoanza kuvuma. Wanafunzi waliogopa sana, wakamwamusha toka usingizi na kumsihi kuwasaidia. Nyuma ya kuwahamakia kwa sababu ya imani yao ndogo Bwana **alihamakia pepo na bahari**; ilikuwa **kimya kubwa**. Watu **walishangaa** sana wakati walipoona hata pepo na mawimbi yakitii Bwana. Hawakufahamu hata kidogo ya kwamba Mwumba na Mwenye kutegemeza ulimwengu mzima alikuwa ndani ya chombo pamoja nao siku ile!

Wafuata wote wa Bwana watakutana na tufani ndani ya maisha yao wakati na wakati. Mara nyingine inaonekana sawasawa mawimbi yatatuzamisha. Ni faraja kubwa kukumbuka ya kwamba Bwana wetu Yesu ni ndani ya chombo pamoja nasi. Hakuna mwingine anayeweza kutuliza tufani kama Yeye.

### G. Yesu anaponyesha watu wawili wenye pepo wachafu (8:28-34)

**8:28 Inchi ya Wagerase** ilikuwa kwa upande wa mashariki wa Bahari ya Galilaya. Wakati Yesu alipofika kule, alikutana na watu wawili wenye nguvu

sana waliokaaliwa na pepo wachafu. Walikaa ndani ya **makaburi** na walikuwa **wakali** sana hata ilikuwa hatari kwa watu kusafiri kule.

**8:29-31** Wakati Yesu alipokaribia pahali pale, pepo wachafu walilalamika, **"Tuna nini nawe, Yesu, wewe Mwana wa Mungu? Wewe umekuja hapa kutesa mbele ya wakati?"** Walijua kama Yesu alikuwa nani na ya kwamba mwishoni atawaharibu. Wakifikiri Yesu atawaagiza kutoka watu wale, waliomba ruhusa kuingia **kundi la nguruwe waliokuwa wakikula** karibu na pahali penyewe.

**8:32** Yesu alikubali neno waliloomba. Tunauliza kwa sababu gani Bwana Mwenye Enzi atakubali neno pepo wachafu waliloomba? Kwa kutusaidia kufahamu sababu gani alifanya hivi, tukumbuke maneno mawili: 1) Pepo wanataka kukaa ndani ya kiumbe chenye uzima.Wanataka kukaa ndani ya miili ya watu; au, kama neno hili haliwezekani, ndani ya nyama au viumbe vingine. 2) Kila mara kusudi la pepo wachafu ni kuharibu. Kama Yesu angaliagiza pepo wachafu kuondokea tu watu wale kama wangalikuwa hatari kwa watu wengine waliokaa katika inchi ile. Wakati Yesu alipowaruhusu kuingia nguruwe aliwazuiza wasiingie wanaume na wanawake, lakini waharibu nyama tu. Saa kwa Bwana kuharibu pepo wachafu wale kabisa ilikuwa haijafika bado. Halafu mara moja pepo wachafu walipoingia nguruwe, **kundi zima walitelemuka mbio chini ya genge hata baharini**, wakakufa ndani ya maji.

Habari hizi zinaonyesha kwamba kusudi kubwa la pepo wachafu ni kuharibu. Ni neno la kuogofya kuona kwamba pepo wachafu wengi walizohitajiwa kuharibu nguruwe elfu mbili ziliweza kukaa ndani ya wanaume wawili (Mk. 5:13).

**8:33,34** Wachungaji wa kundi la nguruwe walikimbia na kupasha habari za maneno yaliyotokea.Watu wote wa mji walitoka kukutana na Yesu, wakamsihi aondokee inchi yao. Tangu wakati ule watu wameshitaki Yesu juu ya uharibifu bure wa kundi la nguruwe wale, na wamemwomba kuwaondokea kwa sababu kwa mafikiri ya Yesu uzima wa watu unapita uzima wa nyama. Kama Wagerase hawa walikuwa Wayuda, waliasi sheria ya Musa wakati walipokuwa na makundi ya nguruwe. Lakini hata kama wasipokuwa Wayuda, hukumu yao ndiyo ya kwamba kwa macho yao kundi la nguruwe lilikuwa na faida kupita kuponyeshwa kwa wanaume wale wawili toka utawala wa pepo wachafu.

**H. Uwezo kusamehe zambi (9:1-8)**

**9:1** Wakati Mwokozi alipokataliwa na Wagerase, alivuka bahari ya Galilaya tena na kufikia Kapernaumu uliokuwa **mji wake mwenyewe** tangu siku watu wa Nazareti walipojaribu kumwua (Lk. 4:29-31). Katika mji huu alitenda mengine ya maajabu yake ya uwezo zaidi.

**9:2** Wanaume wane walifika kwake wakileta mtu **mwenye kupooza** juu ya kitanda. Ndani ya Marko tunasoma ya kwamba kwa sababu ya ukubwa wa makutano iliwapasa kutoboa dari ya nyumba ili waweze kushusha mgonjwa na kumfikisha mbele ya Yesu (Mk. 2:1-12). Wakati Yesu alipoona **imani yao** alisema na mwenye kupooza, **"Mwana wangu, uwe na furaha; zambi zako zimesamehewa."** Ona ya kwamba aliona imani *yao*. Watu wale walisukumwa na imani kuleta mgonjwa karibu na Yesu, na mgonjwa mwenyewe aliamini kwamba Yesu ataweza kumponyesha. Halafu neno la kwanza Bwana alilosema naye, lilikuwa **"zambi zako zimesamehewa."** Mganga mkubwa alisaidia hitaji lake la roho kwanza, mbele ya kuponyesha mwili. Tunge-

penda kuuliza kama mara nyingine Kristo aliponyesha mwili wa mtu bila kuokoa roho vilevile. Hatujui.

**9:3-5** Wakati **wengine wa waandishi** waliposikia Yesu akisema zambi za mgonjwa zimesamehewa, walimshitaki **moyoni mwao** na kukufuru. Walijua Mungu tu anaweza kusamehe zambi – nao hawakuwa tayari kukubali kwamba Yesu ni Mungu! Bwana Yesu anayejua maneno yote alijua mawazo yao, akawahamakia juu ya mafikiri yao maovu, na kuwauliza, Nini ni **nyepesi kusema, "Zambi zako zimesamehewa" au kusema, "Simama utembee"?** Hakuna tofauti kwa ku*sema* hivi, lakini neno gani ni nyepesi kupita ku*fanya*? Maneno haya mawili yote hayawezekani kwa watu, lakini halionekani kwa macho kama mtu amesamehewa zambi zake kweli, lakini watu wanaweza kuona mara moja kwamba mtu aliponyeshwa mwilini.

**9:6,7** Kuonyesha kwa waandishi ya kwamba ana uwezo **duniani kusamehe zambi** (na ya kwamba iliwapasa kumheshimu namna walivyoheshimu Mungu) alifanya ajabu waliloweza kuona na macho. Akigeuka **kwa mwenye kupooza** alisema, **"Simama, unyanyue kitanda chako, ukaende kwa nyumba yako."**

**9:8** Wakati makutano walipomwona akitembea na kitanda chake waliogopa wakifahamu kwamba Yesu si mtu tu, na **walitukuza Mungu** ambaye aliwapa **watu amri namna hii.** Lakini hawakufahamu hata kidogo maana ya ajabu hili. Kusudi la kuponyeshwa kwa mwenye kupooza, neno ambalo lilionekana kwa macho, lilikuwa kuhakikisha kwamba zambi za mtu huyu zilikuwa zimesamehewa, ndilo ajabu lisiloonekana kwa macho. Maneno haya yangalipasa kuwafahamisha kwamba kusudi la neno walilokwisha kuona halikuwa kuwaonyeshea Mungu akiwapa watu amri, lakini ya kwamba Mungu alikuwa katikati yao, ndiye Bwana Yesu Kristo mwenyewe. Lakini hawakufahamu.

Na maneno tutakayosoma nyuma yanaonyesha kwamba kutokuamini na kuchukia kwa waandishi kuliongezeka.

### I. Yesu anaita Matayo mtoza kodi (9:9-13)

**9:9** Halafu Matayo, na unyenyekevu, aliandika namna Bwana alivyomwita yeye. Watoza kodi walichukiwa sana na Wayuda wenzao kwa sababu hawakutenda kwa haki, lakini walibebeshea watu mzigo mkubwa sana wa kodi, na zaidi kwa sababu walitumikia Waroma waliotawala Wayuda. Wakati **Yesu alipopita** pahali pa kupokea kodi, **alisema** na Matayo, **"Unifuate."** Matayo alitii agizo hili mara moja. **"Akaondoka na kumfuata."** Wakati alipofanya hivi, aliacha kazi ya udanganyifu na aligeuka mara moja mwanafunzi wa Yesu. Alipoteza kazi ya mshahara mwema lakini alipata uaminifu. Na zaidi ya yote aligeuka mmoja wa wanafunzi kumi na wawili wa Yesu na alipewa heshima ya kuandika Habari Njema ile inayoitwa na jina lake.

**9:10** Karamu hii ilitayarishwa na Matayo kuheshimu Yesu (Lk. 5 :29). Kwa njia hii alikiri mbele ya watu waliotumika pamoja naye ya kwamba Kristo ni Mwokozi wake. Wageni wake walikuwa **watoza kodi** kama yeye, na wengine walioitwa **wenye zambi** vilevile.

**9:11 Wakati Wafarisayo walipoona** Yesu akikula pamoja na watu ovyo namna hii, walifikia wanafunzi wake na kumshitaki juu ya neno hili … nabii wa haki atakula kweli pamoja na **wenye zambi**?

**9:12** Yesu alisikia masemo yao, akajibu, **"Wenye afya hawahitaji mganga, lakini wenye ugonjwa tu."** Wafarisayo walifikiri walikuwa na afya njema

ya roho, na hawakuwa tayari kukiri kwamba walihitaji Yesu. (Lakini walikuwa wagonjwa sana rohoni na walihitaji kuponyeshwa!) Watoza kodi na wenye zambi walikuwa tayari kukubali hali yao ya roho, na kutafuta Kristo na neema yake ya kuokoa. Hivi mashitaki ya Wafarisayo yalikuwa kweli! Yesu alikula pamoja na wenye zambi kweli. Na kama angalikula pamoja na Wafarisayo, mashitaki haya yangalikuwa vivyo hivyo, labda hata kupita. Kama Yesu asingekula pamoja na wenye zambi katika dunia hii, kama angekula peke yake tu wakati wote. Lakini tukumbuke ya kwamba hata wakati alipokula pamoja na wenye zambi hakushiriki ndani ya zambi zao na kuharibu ushuhuda wake, lakini aliita watu kutembea katika kweli na utakatifu.

**9:13** Ndiyo, Wafarisayo walitii kawaida ya dini ya Wayuda karibu karibu, lakini mioyo yao ilikuwa baridi, na walikosa rehema. Hivi Yesu aliwaagiza kujifundisha maana ya agizo la Mungu (toka Hosea 6:6), **"Ninataka rehema, wala si sadaka."** Alikuwa Mungu aliyesimamisha kawaida ya sadaka zamani, lakini hakukusudi kwa kawaida hii kukomboa haki rohoni. Hafurahi juu ya sadaka bila utawa wa roho wa mwenye kuzitoa. Wafarisayo walikuwa wakianguka kwa neno hili. Walitii kila agizo dogo la sheria, lakini hawakuwa na huruma kwa wale waliohitaji kusaidiwa rohoni. Walifungana tu na watu waliojihesabu wenyewe kuwa wenye haki kama wao.

Basi Bwana aliwaambia waziwazi, **"Sikuja kuita wenye haki, lakini wenye zambi kutubu."** Yeye mwenyewe alitimiza kabisa kutaka kwa Mungu kwa rehema pamoja na sadaka. Tungeweza kusema kwamba hakuna watu wenye haki duniani, hivi alifika kuita watu wote **kutubu**. Lakini hapa tunaona kwamba mwito wake ni kwa watu wale tu ambao wanakubali kwamba wao ni wenye zambi. Hawezi kusaidia wale wanaofikiri wao ni wenye haki wasiohitaji kutubu – kama Wafarisayo.

**J. Maulizo juu ya kufunga (9:14-17)**

**9:14** Ni kama kwa wakati huu **Yoane Mbatizaji** alikuwa amefungwa gerezani, na wanafunzi wake **walifikia** Yesu na ulizo. Wao wenyewe walifunga chakula mara nyingi, **lakini wanafunzi wa Yesu hawakufunga**. Kwa nini?

**9:15** Bwana Yesu alitumika na mfano kujibu ulizo lao. Yeye mwenyewe alikuwa **bwana arusi** na wanafunzi walikuwa wageni kwa karamu ya arusi. **Wakati yeye alipokuwa kwanza pamoja nao**, hawakuhitaji kufunga chakula kama alama ya maombolezo. Lakini nyuma ya wakati **ataondolewa kwao;** kwa wakati ule wanafunzi wake **watafunga chakula**. Ali*ondolewa* kwao kweli – kwa njia ya mauti na kuzikwa, na tangu aliporudi tena mbinguni mwili wake haukuwa pamoja nao tena. Bwana Yesu haku*agiza* watu kufunga, lakini masemo yake yanaonyesha kwamba ali*kubali* tendo hili kwa wale wanaongojea kurudi kwa Bwana-arusi.

**9:16** Halafu Yesu alionyesha ya kwamba kuja kwa Yoane kulimaliza muda wa sheria; na kutangaza mwanzo wa muda mwingine, muda wa neema. Alionyesha vilevile ya kwamba haiwezekani kuchanganya maneno haya. Kuchanganya neema na sheria ni kama kutumika na kiraka cha **nguo mpya** kisichopunguka bado kwa njia ya kukivua, kwa kutengeneza mapasuko ya **vazi la zamani**. Wakati mtu atakapovua vazi hili, kiraka kipya kitapunguka na kupasula vazi la zamani hata kupita mbele.

**9:17** Machanganyiko haya yanaweza kusawanishwa vilevile na kuweka mvinyo mpya ndani ya viriba vya zamani. Kuchachuka kwa mvinyo mpya kuta-

haribu viriba vya zamani vilivyopoteza hali ya kunyumbuka. Uzima na uhuru wa Habari Njema zinaharibu utaratibu na kawaida ya sheria. Muda wa Habari Njema ulianza kawaida mpya kabisa. Haifai hata kidogo kuchanganya sheria na Habari Njema.

### K. Uwezo kuponyesha mwenye ugonjwa usioponyeka, na kufufua mfu (9:18-26)

**9:18, 19** Angali Yesu alipokuwa akifundisha juu ya muda wa Habari Njema ukikomboa ule wa sheria, **mtawala** mmoja wa sunagogi alimfikia na huzuni kubwa. **Binti** yake alikuwa **amekufa sasa** tu naye alipiga magoti mbele ya Yesu na kumwomba kumfufua. Haikuwa desturi kwa mtawala wa sunagogi kufanya hivi; zaidi ya viongozi vya Wayuda wangaliogopa kuzarauliwa na wenzao kama wakifanya hivi. **Yesu** alitambua imani ya mtu huyu, akashika njia pamoja na wanafunzi kwendea nyumba ya mtawala.

**9:20** Lakini walikutana na kizuizo kingine. Mara hii kilikuwa **mwanamke** aliyekuwa ameteswa na kutoka damu kwa miaka kumi na miwili. Yesu hakuchukizwa kamwe na vizuizo namna hii; alikaa tayari wakati wote kusaidia watu ambao walimfikia na masumbuko yao.

**9:21, 22** Wanganga hawakuweza kusaidia mwanamke huyu, na hali yake ilizidi kuwa mbaya (Mk. 5:26). Katika taabu yake aliona Yesu aliyezungukwa na watu wengi. Kwa sababu aliamini Yesu ataweza kumponyesha, alipita polepole katika makutano, **akagusa** upindo wa **vazi lake.** Bwana Yesu anajua kila mara wale walio na imani. Aligeuka kumtazama, akasema ameponyeshwa; mara moja **mwanamke alikuwa na afya tena,** mara ya kwanza tangu miaka kumi na miwili.

**9:23, 24** Halafu Yesu alishika njia tena kwendea nyumba ya mtawala mwenye binti aliyekufa. Wakati Yesu alipofikia nyumba yenyewe, watu wenye kazi ya kuomboleza walikuwa wakifanya kelele. Yesu aliagiza waondoshwe wote chumbani pamoja na kusema ya kwamba msichana hakufa lakini alilala. Zaidi ya walimu wa Biblia wanafikiri Bwana Yesu alitumika hapa na neno hili *kulala* kama mfano wa mauti. Lakini wengine wanasema alikuwa na hali ya kuzimia. Hawakani ya kwamba Yesu angaliweza kumfufua kama angalikuwa amekufa kweli, lakini ya kwamba Yesu, akiwa mwenye haki, asingalisema alifufua msichana kama asingalikuwa mfu. Mwalimu mmoja, Sir Robert Anderson alifikiri hivi. Alisema kwamba baba na watu wengine wote walisema msichana alikufa, lakini **Yesu** alisema **hakufa.**

**9:25, 26** Halafu Yesu alishika mkono wake, na ajabu lilifanyikana – msichana alisimama. Habari za ajabu hili zilienea mbio katika inchi ile yote.

### L. Uwezo kuponyesha upofu (9:27-31)

**9:27, 28** Wakati **Yesu alipopita** toka kule, **vipofu wawili walimfuata** wakimsihi kuponyesha macho yao waweze kuona. Hata kama watu hawa hawakuweza kuona na macho yao ya mwili, walikuwa na ufahamu kabisa kwa maneno ya roho. Wakati walipoita Yesu **Mwana wa Daudi**, walimtambua kuwa Masiya na Mfalme wa haki wa Israeli ambaye watu walingojea kufika kwake tangu miaka mingi. Wakati Yesu alipopima imani yao kwa njia ya kuwauliza kama waliamini ya kwamba **ataweza kufanya hivi,** walimjibu mara moja: "Ndiyo, Bwana."

**9:29,30** Halafu Mganga mkubwa **aligusa macho yao** na kuwaambia kwamba kwa sababu ya imani yao wataweza kuona tena. Na kweli walipata kuona tena mara moja.

Watu wanasemaga, "Tukiona tuna-

weza kuamini." Mungu anasema, "Kuamini ni kuona." Yesu alisema na Marata, "Sikukuambia kama ukiamini utaona utukufu wa Mungu?" (Yn. 11:40). Mwandishi wa kitabu cha Waebrania aliandika, "Kwa imani tunafahamu …" (11:3). Mtume Yoane aliandika, "Ninawaandikia ninyi wenye kuamini … ili mujue …" (1 Yn. 5:13). Mungu hapendezwi kama tukitaka kuona ajabu mbele ya kuamini. Anataka tumwamini kwa sababu yeye ni Mungu.

Kwa sababu gani Yesu **aliagiza na nguvu** wale waliokwisha kuponyeshwa wasitangazie watu wengine habari za kuponyeshwa kwao? Ndani ya mafundisho juu ya 8:4 tulionyesha kwamba labda hakutaka watu kujua habari za ajabu hili saa ile kwa sababu hakutaka kuamsha hamu ndani ya roho zao kumfanyiza Mfalme mbele ya wakati uliochaguliwa na Mungu. Watu hawakuwa na roho ya toba kwanza, naye hakuweza kutawala juu yao kufika wakati walipozaliwa tena. Vilevile machafuko katikati ya watu kusimamia Yesu yangalileta kisasi na hukumu kali sana ya serikali ya Waroma kwa Wayuda. Na vilevile ilikuwa lazima kwa Bwana Yesu kusulibishwa mbele ya kuweza kutawala kama Mfalme. Neno lo lote lililoweza kumzuiza kwenda Kalvari lilikuwa mbali na shauri la Mungu tangu zamani.

**9:31** Lakini roho za watu hawa waliopata kuona tena zilijaa asante na furaha kubwa, hata **walieneza habari** za ajabu hili katika inchi ile yote. Hata tukijaribiwa kuwaheshimu kwa ushuhuda wao, tufahamu kwamba waliasi agizo la Bwana kabisa. Hata roho ya asante si sababu kwa kuasi Bwana.

### M. Uwezo kuwezesha bubu kusema (9:32-34)

**9:32** Kwanza Yesu alimpa mfu uzima; nyuma yake aliwezesha vipofu kuona, na sasa anawezesha bubu kusema. Tunaweza kusawanisha namna maneno haya yanavyofuatana na yale yanayotokea ndani ya maisha ya mwamini: kwanza amepata *uzima mpya,* nyuma yake *ufahamu* wa maneno ya Mungu, kisha uwezo *kushuhudia* Bwana.

Roho mchafu alikuwa ametesa mtu huyu hata hakuweza kusema. Mtu mmoja alimhurumia na kumleta karibu na Yesu. Mungu abariki watu wale wanaofikisha watu wengine karibu na Bwana Yesu!

**9:33** Yesu **alitoa pepo mchafu** na **mara moja bubu aliweza kusema!** Tunafikiri maneno ya kwanza aliyosema yalikuwa maneno ya sifa na kuabudu na ushuhuda kwa Bwana ambaye alimponyesha kwa neema yake. Watu walishangaa wakati walipoona neno hili na walikiri kwamba watu hawakuona maajabu namna hii mbele katika **Israeli**.

**9:34** **Lakini Wafarisayo** walisema Yesu alikuwa akitoa pepo wachafu kwa mkubwa wa pepo wachafu. Kwa Matayo 12:32, masemo haya yaliitwa zambi isiyoweza kusamehewa. Kusema maajabu Yesu aliyofanya kwa uwezo wa Roho Mtakatifu yalifanywa kwa uwezo wa Shetani kulikuwa kutukana Roho Mtakatifu. Hivi wakati watu wengine walipokuwa wakibarikiwa na Kristo na kuponyeshwa naye, Wafarisayo walikaa wafu kwa roho, wasioweza kuona wala kusema.

## 6. MITUME YA MASIYA-MFALME WANATUMWA KWA ISRAELI (9:35 – 10:42)

### A. Hitaji kwa wavunaji (9:35-38)

**9:35** Shairi hili linaanza safari ya tatu ya **Yesu** kuzunguka katika **miji na vijiji** vya Galilaya kuhubiri Habari Njema ya **ufalme**, maana yake ya kwamba alikuwa Mfalme wa Israeli, na kama taifa hili likitubu na kumpokea,

atatawala juu yao. Biblia haitujulishi kama nini ingalitokea kama wangalimpokea kweli kwa wakati huu. Tunajua tu ya kwamba ingalipasa Yesu kufa ili Mungu aweze kutenda kwa haki na kuhesabia haki wenye zambi wa nyakati zote.

Wakati Kristo alipofundisha na kuhubiri, aliponyesha namna zote za magonjwa vilevile. Masiya alifanya hivi wakati alipotokea mara ya kwanza na neema na unyenyekevu. Maajabu yatakuwa alama ya kuja kwake mara ya pili vilevile, wakati atakapokuja tena na uwezo na utukufu mkubwa (ona Ebr. 6:5 "nguvu za dunia inayokuja").

**9:36** Wakati Kristo alipotazama **makutano**, wenye kutaabishwa na bila kusaidiwa, aliwaona kama **kondoo** waliokosa **mchungaji,** na aliwahurumia sana. Ingekuwa vizuri kwa sisi vilevile kuwa na mzigo mkubwa kwa roho za watu walio katika hatari ya kufa katika zambi zao. Tukae kuomba wakati wote tuweze kuwaona na huruma na mapendo namna Bwana wetu anavyowaona.

**9:37** Mavuno makubwa yalikuwa tayari kukusanywa, lakini **watenda kazi walikuwa wachache**. Ni vivyo hivyo hata leo. Hesabu ya watenda kazi haitoshi kwa kazi inayohitaji kufanywa.

**9:38** Bwana Yesu alisema na wanafunzi kuomba **Bwana wa mavuno kutuma watenda kazi kwa mavuno yake**. Ona ya kwamba hitaji kwa watenda kazi si mwito wa Bwana kuwa wafanya kazi. Haifai watenda kazi *kwenda* kufika wakati wanapo*tumwa*.

Yesu hakusema wazi hapa kama **Bwana wa mavuno** ni nani. Walimu wengine wanafikiri ni Roho Mtakatifu. Ndani ya 10:5 Bwana Yesu mwenyewe alituma wanafunzi, hivi ni wazi ya kwamba inatupasa kumwomba Yeye juu ya hitaji hili kubwa la kuleta Habari Njema kwa dunia nzima.

**B. Mitume kumi na wawili wanaitwa (10:1-4)**

**10:1** Ndani ya shairi la mwisho la sura 9 Bwana alisema na wanafunzi wake kuomba ili hesabu ya watenda kazi iweze kuongezeka. Kwa kuomba hivi na roho ya kweli iliwapasa kuwa tayari kwenda wao wenyewe. Basi sasa tunaona Bwana akiita **mitume yake kumi na wawili.** Alikuwa amewachagua mbele, lakini sasa aliwaita kuhubiri Habari Njema kwa taifa la Israeli. Pamoja na kuwaita, aliwapa amri vilevile kutoa pepo wachafu na kuponyesha namna zote za ugonjwa. Tunaona hapa wazi kwamba Bwana alikuwa namna nyingine na watu. Kulikuwa na watu walioweza kufanya maajabu, lakini hakuna mtu aliyempa mtu mwingine uwezo huu kamwe.

**10:2-4** Hawa ndio **mitume kumi na wawili:**

1. **Simoni, anayeitwa Petro**. Alikuwa na roho ya haraka, mwenye bidii kutenda bila kufikiri, mwenye moyo wa mapendo, aliyepewa zawadi kuwa mwongozi wa watu.
2. **Anderea, ndugu yake**. Yoane Mbatizaji alimfikisha kwa Yesu (Yn. 1:36, 40), naye alileta ndugu yake Petro kwake. Kazi yake ilikuwa kufikisha watu wengine kwa Yesu.
3. **Yakobo,** mwana wa Zebedayo, aliyeuawa na Herode (Mdo. 12:2) – alikuwa wa kwanza wa wale kumi na wawili aliyeuawa kwa sababu ya imani yake.
4. **Yoane, ndugu yake.** Alikuwa mwana wa Zebedayo vilevile na aliitwa mwanafunzi aliyependwa na Yesu. Ndiye aliyeandika Habari Njema ya Ine, Barua tatu, na kitabu cha Ufunuo.
5. **Filipo**, mtu wa Betesaida aliyeleta ndugu yake Natanaeli karibu na Yesu. Si Filipo mwenye kuhubiri Habari Njema ambaye tunasoma

habari zake ndani ya kitabu cha Matendo.

6. **Bartolomayo**. Walimu wa Neno la Mungu wanafikiri alikuwa Nataneli, Mwisraeli ndani yake Yesu hakukuta hila (Yn. 1:47).
7. **Tomasi**, aliyeitwa "Pacha". Watu walimwita "Tomasi mwenye shaka," lakini alitoa ushuhuda wa kutukuza Kristo sana (Yn. 20:28).
8. **Matayo.** Mbele alikuwa mtoza kodi, lakini aligeuka mwandishi wa Habari Njema hii.
9. **Yakobo, mwana wa Alufayo**. Hatujui habari nyingine juu yake.
10. **Tadeo**. Aliitwa Yuda, mwana wa Yakobo, vilevile (Luka 6:16). Masemo yake ya pekee ambayo tuliyo nayo ni katika Yoane 14:22.
11. **Simoni Mkanana**, aliyeitwa Zelote katika Luka (6:15).
12. **Yuda Iskariota**, aliyetoa Bwana wetu kwa adui.

Tunafikiri mitume walikuwa na umri wa karibu miaka 20 kufika 30 kwa wakati ule. Walikuwa wakifanya kazi mbalimbali, si wenye akili au hekima zaidi, lakini kwa sababu ya kukaa pamoja na Yesu waligeuka wenye faida kubwa kwa kazi yake.

### C. Mitume wanatumwa kwa Israeli (10:5 -33)

**10:5, 6** Baki la sura hii ni maagizo ya Yesu juu ya safari hii ya kuhubiri kwa **nyumba ya Israeli**. Ni mbali na maagizo yake saa alipotuma watu 70 kwa wakati wa nyuma (Lk. 10:1), na agizo lake kubwa kwa Matayo 28:19,20. Maagizo ndani ya sura 10 yalikuwa kwa **safari hii tu** kutangaza kwamba **ufalme wa mbinguni** ulikuwa karibu. Bwana aliondosha mengine ya maagizo haya nyuma (Lk. 22:35,36).

Kwanza aliwaagiza *kama watakwendea watu gani*. Aliwakataza kufikia watu wa **Mataifa** na **Wasamaria** waliokuwa machanganyiko ya watu wa makabila mbalimbali, na waliochukiwa na Wayuda. Mara hii iliwapasa kuhubiri kwa **kondoo wapotevu wa nyumba ya Israeli** tu.

**10:7** *Habari* watakazotangaza ndizo ya kwamba **ufalme wa mbinguni ni karibu.** Kama taifa la Israeli wakikataa habari zenyewe, hawatakuwa na uzuru, kwa sababu walitangaziwa habari hizi waziwazi. Ufalme ulikuwa umewakaribia kwa njia ya kufika kwa Mfalme mwenyewe. Ilipasa Israeli kuchagua kama watampokea au kumkataa.

**10:8** Kwa kuhakikisha kweli ya habari zao walipewa uwezo **kuponyesha wagonjwa, kusafisha wakoma, kufufua wafu** na **kutoa pepo wachafu.** Wayuda waliomba alama (1 Kor. 1:22) hivi Mungu mwenye neema aliwapa alama.

Waombe kupewa *mshahara* kwa kazi yao? Sivyo. Wao wenyewe walikuwa wamepokea baraka nyingi bila bei na iliwapasa kuleta baraka kwa watu wengine vivyo hivyo.

**10:9,10** Hawakuhitaji ku*tayarisha vitu* watakavyohitaji kwa safari yao. Walikuwa Waisraeli wakihubiri kwa Waisraeli na mtenda kazi anastahili posho yake. Hivi hawakuhitaji kwenda na **zahabu na feza na chuma wala mfuko kwa vyakula, wala kanzu mbili, wala viatu, wala gongo**. Wakiwa na viatu na gongo mbele, hawakuhitaji kupeleka vingine (Mk. 6:8). Watapewa kila siku vitu watakavyohitaji.

**10:11** Basi wata*lala wapi*? Wakati walipoingia mji fulani itawapasa kutafuta **mtu ambaye atawapokea** kama wanafunzi wa Bwana na kupokea habari zao. Wakikutana na mtu wa namna hii, wakae nyumbani mwake kwa muda mzima watakaokuwa katika mji ule. Wakiona nyumba nzuri kupita, haifai wahame kule.

**10:12-14** Kama **wakipokewa vizuri nyumbani fulani,** ilipasa wanafunzi ku-

**salimu** jamaa ya nyumba na kupokea ukarimu wao na adabu. Lakini kama nyumba ikikataa kupokea wajumbe wa Bwana haikuwa sharti kwao kuomba **salama** ya Mungu kuwa juu yao, wala baraka ya Mungu kuwa juu ya jamaa yenyewe. Zaidi ya ile iliwapasa kuonyesha kasirani ya Mungu kwa njia ya kunguta **mavumbi** ya miguu yao. Jamaa wakikataa kupokea watumishi wa Bwana walikuwa wakimkataa yeye.

**10:15** Bwana alisema vile kwamba **siku ya hukumu,** azabu yao itakuwa kubwa kupita ile ya watu waovu wa **Sodomo na Gomora**. Neno hili linaonyesha kwamba watu katika Gehena watapokea azabu ya kipimo mbalimbali; kama sivyo, namna gani itakuwa **kuvumilika kuliko** kwa watu wengine?

**10:16** Ndani ya mashairi yanayofuata Yesu anafundisha *namna gani inawapasa kutenda wakati wanapoteswa.* Watakuwa kama **kondoo katikati ya imbwa za mwitu** wakizungukwa na watu wakali wanaoweka roho sana juu ya kuwaharibu. Iliwapasa kuwa wenye **akili kama nyoka**, maana yake wasifanye neno ambalo litakasirisha adui bure au kuwapa adui njia kuwatega kufanya maneno yasiyofaa. Na inawapasa kuwa **wapole kama hua,** wenye haki na imani ya kweli.

**10:17** Wakae na ange kwa Wayuda wasioamini ambao watawakokota mbele ya mabaraza na kuwapiga **ndani ya masunagogi yao**. Watapata matata kwa mikono ya serikali na watu wa dini.

**10:18** Watapelekwa mbele ya **watawala na wafalme** kwa ajili ya Kristo. Lakini mashauri ya Mungu yatashinda makusudi maovu ya watu. Kwa saa inapoonekana kwamba wanashindwa kabisa watapewa heshima kubwa ya kuweza kushuhudia Kristo mbele ya watawala na **Mataifa**. Mungu atageuza maneno yote kuwa mema.

**10:19, 20** Hawatahitaji kutayarisha mbele maneno watakayosema wakati watakaposhitakiwa. Saa yenyewe **Roho Mtakatifu** wa Mungu atawapa akili kusema maneno yatakayotukuza Kristo, na kukologa mawazo ya washitaki wao. Lakini wakati wa kueleza maana ya shairi 19 inatupasa kuepuka kuanguka, kwa njia mbili. 1. Shairi hili halifundishi kwamba mhubiri hahitaji kuweka saa kutayarisha mafundisho yake mbele. 2. Tusifikiri mafundisho ya shairi hili si kwa wakati wa sasa. Sharti mhubiri kungojea Mungu katika maombi kumwongoza kutayarisha mafundisho yanayofaa kwa wasikiaji wake kwa wakati ule. Lakini kwa wakati wa hatari ya gafula, waamini wote wanaweza kutegemea ahadi ya Mungu kuwawezesha kusema na akili toka kwake kwa ajili ya Roho wa Baba yao.

**10:21** Yesu alijulisha wanafunzi wake mbele ya kwamba watatendewa kwa hila na kutolewa kwa mikono ya adui. Ndugu atashitaki ndugu yake. Baba atatoa mtoto wake. Watoto watashitaki wazazi wao na kuwatoa kusudi wauawe.

J.C. Macaulay alisema,

> Mtumishi asifikiri atatendewa vizuri na adui kupita Bwana Yesu mwenyewe. Dunia hii ilikuwa na msalaba tu kwa Yesu; wafuata wake wasifikiri watakaa katika utajiri; watu wa dunia wakimwekea taji ya miiba; sisi wafuata wake tusifikiri tutapokea taji ya maua … Lakini tuangalie ili watu wa dunia watuchukie kweli “kwa ajili ya Kristo,” si kwa sababu ya uovu ndani yetu na matendo yasiyo ushuhuda mzuri wa Kristo Bwana wetu.[1]

**10:22, 23** Wanafunzi **watachukiwa na wote** – si na kila mtu mmoja mmoja, lakini na makabila na mataifa yote, **“lakini yeye anayevumilia hata mwisho ndiye ataokolewa.”** Tukisoma shairi hili moja peke yake tungeweza kufikiri kwamba mtu ataweza kujipatia wokovu kwa njia ya kuvumilia bila

kuacha. Tunajua kwamba hili si maana yake ya kweli, kwa sababu tunasoma tena na tena ndani ya Maandiko kwamba wokovu ni zawadi ya neema ya Mungu, ambayo tunapokea kwa njia ya imani (Efe. 2:8,9). Na vilevile maana yake haiko kwamba wale wanaofuata Kristo na uaminifu hata mwisho hawatauawa – tulisoma sasa tu ya kwamba wanafunzi waaminifu wengine watauawa kwa sababu ya imani yao. Maana ya shairi hili ni kwamba wale wanaodumu kuvumilia mateso wanaonyesha kwamba wao ni waamini wa kweli. Tunaona semo hili katika Matayo 24:13, pahali tunaposoma juu ya baki aminifu la Wayuda wanaokataa kuacha kufuata Bwana Yesu. Uvumilivu wao unaonyesha kwamba wao ni wanafunzi wa kweli.

Katika Biblia mara nyingine mashairi juu ya unabii yanageuka toka wakati wa sasa kwa wakati wa kuja. Yanatimizwa sasa kwa sehemu tu, lakini yatatimizwa kabisa kwa wakati wa kuja. Kwa mfano, kwa mashairi mengine kuna habari juu ya kuja kwa kwanza na kwa pili kwa Bwana pamoja, bila maelezo (Isa.52:14, 15; Mika 5:2-4). Ndani ya mashairi 22 na 23 Bwana Yesu alitoa unabii namna hii. Alipasha wanafunzi kwamba watapata mateso kwa ajili yake, tena ni sawasawa anafikiri juu yao kama mifano ya Wayuda waaminifu kwa wakati wa Mateso Makubwa. Nyuma ya kusema juu ya taabu ya Wakristo wa kwanza, aliruka mbele kwa waamini karibu na kuja kwake kwa pili.

Sehemu ya kwanza ya shairi 23 ingeweza kusema juu ya wanafunzi kumi na wawili. Lakini **"wakati watakapowatesa ninyi katika mji huu, kimbieni kwa mji mwingine …"** Haikuwa lazima kwao kuvumilia ukali wa adui zao kama wakiwa na njia ya haki kukimbia. Si vibaya kukimbia hatari – lakini haifai kukimbia madaraka.

Mwisho ya shairi 23 unapasha juu ya siku zinazotangulia kuja kwa Kristo kutawala: **"… hamutamaliza miji ya Israeli hata Mwana wa watu atakapokuja."** Maneno haya si juu ya safari ya wanafunzi kumi na wawili, kwa sababu Mwana wa watu alikuwa amefika. Walimu wengine wanafikiri linasema juu ya uharibifu wa Yerusalema miaka 70 A.D., lakini ni nguvu kukubali kwamba uharibifu ule mkubwa unaitwa "kuja kwa Mwana wa watu." Ni nyepesi kupita kuamini kwamba tunasoma hapa juu ya kuja kwa pili kwa Bwana. Kwa muda wa Mateso Makubwa ndugu za Kristo, Wayuda waaminifu watakwenda kutangaza habari njema ya ufalme. Watateswa na kufukuzwa. Wakati wasipofikia miji yote ya Israeli bado, Bwana Yesu atakuja kuhukumu adui zake na kusimamisha ufalme wake.

Labda unafikiri kwamba shairi 23 na Matayo 24:14 hayapatani. Hapa katika shairi 23 tunasoma kwamba **hawatafikia miji yote ya Israeli mbele ya kuja kwa Mwana wa watu.** Ndani ya Matayo 24:14 tunasoma kwamba Habari Njema ya ufalme itahubiriwa kwa mataifa yote hata kama haihubiriwi kwa kila mtu mmoja mmoja. Watu watashindana sana na habari hizi, na wajumbe wake watateswa sana na kuzuizwa wasihubiri katika Israeli. Hivi Habari Njema ya ufalme haitafikia miji yote ya Israeli.

**10:24,25** Wanafunzi watafazaika tena na tena kwa sababu gani itawapasa kuvumilia mateso haya yote. Kama Yesu ni Masiya, kwa sababu gani wafuata wake watateswa kwa pahali pa kutawala? Ndani ya mashairi 24 na 25 Bwana Yesu alijibu ulizo lao hata wakati wasipoliuliza waziwazi bado. Anawakumbusha kwamba wao walikuwa wanafunzi, na yeye alikuwa Mwalimu wao. Wao walikuwa watumishi, lakini yeye alikuwa Bwana wao. Inapasa mwanafunzi kufuata Mwalimu wake, si kuwa mkubwa kupita yeye. Na mtumishi asizani atatendewa vizuri kupita Bwana wake. Watu wakiita Bwana mheshimiwa wa nyumba na jina la "Belzebuli" ('bwana wa mainzi') ndiyo

mungu wa watu wa Ekuroni, na jina lililotumiwa na Wayuda kwa Shetani, watazarau watu wa nyumba hata kupita. Inapasa mwanafunzi wa kweli kushiriki ndani ya kukataliwa kwa Bwana wake.

**10:26,27** Bwana alikataza wanafunzi mara tatu kuogopa (mash.26, 28,31). Kwanza, **haifai waogope,** hata wakati ilipoonekana kwamba adui zao watashinda; kwani kwa wakati wa kuja maneno ya Mungu yaliyotabiriwa mbele **yatatimizwa yote**. Kufika wakati ule ni kama Habari Njema **ilifunikwa,** na mafundisho ya Bwana **yalifichwa.** Lakini nyuma kidogo itapasa wanafunzi kutangaza Habari Njema wazi na ukaramisu.

**10:28** Neno la pili, **haifai wanafunzi kuogopa** gazabu ya watu na kuuawa nao. Neno baya zaidi watu wanaloweza kufanya ni **kuua mwili**. Kuuawa si neno baya zaidi linaloweza kupata Mkristo. Kufa kunatufikisha karibu na Kristo, ndilo neno zuri kuliko yote. Kunatufungua toka zambi, huzuni, mateso na mauti, na kunatufikisha hata utukufu wa milele. Kabisa kabisa neno baya zaidi ambalo watu wanaloweza kutenda ni neno zuri zaidi kwa mtoto wa Mungu.

Haifai wanafunzi kuogopa watu, lakini inapasa wawe na **woga pamoja na heshima kwa Mungu, na waogope yeye anayeweza kuharibu nafsi na mwili vilevile katika Gehena**. Hii ndiyo hasara kubwa zaidi – kutengwa na Mungu, na Kristo, na tumaini. Haiwezekani kupima ukubwa wa hasara ile, na ingepasa watu kuweka roho sana kuepuka mauti ya milele.

Shairi 28 linatukumbusha maneno yaliyoandikwa juu ya jiwe la ukumbusho kwa kaburi la mtumishi wa Bwana mwenye kujulikana, ndiye John Knox: "Hapa analala mtu aliyeogopa Mungu sana sana, hata hakuogopa uso wa mtu ye yote."

**10:29** Katikati ya majaribu makali sana wanafunzi waliweza kutegemea Mungu kuwalinda. Bwana Yesu alitumika na mfano wa ndege mdogo sana kufundisha neno hili. **Ndege wadogo wawili namna hii waliuzwa kwa sengi mbili** tu, lakini Mungu Baba anajua wakati kila mmoja anapokufa.

**10:30, 31** Mungu yule anayeweka roho juu ya kufa kwa kila ndege mdogo anahesabu vilevile nyole zote za kichwa za watoto wake wote mmoja mmoja. Neno hili linaonyesha ya kwamba watu wake wana **faida kubwa zaidi** kwake kupita **ndege wengi**, hivi wataogopa kwa sababu gani?

**10:32** Tukijua maneno haya, ni akili njema kwa wanafunzi wa Kristo kum**kiri** bila woga **mbele ya watu**. Watapata zawabu mbinguni kwa haya na laumu wanayopata sasa kwa sababu ya ushuhuda wao saa Bwana Yesu atakapokiri majina yao **mbele ya Baba yake.** Kukiri Kristo hapa ni kujitoa kwake na kumnyenyekea kama Bwana na Mwokozi, na kuonyesha neno hili ndani ya mwenendo na masemo yetu. Zaidi ya wanafunzi walikufa kwa sababu ya ushuhuda wao kwa Kristo.

**10:33** Wale wanaokana Kristo duniani watakanwa vilevile **mbele ya Mungu mbinguni**. Maana ya kukana Kristo hapa ni kukataa kujitoa kwake na kutawaliwa naye kwa wakati wa sasa. Kwa namna ya maisha yao mbele ya watu, watu hawa wanasema kwa Bwana, "Sikukujua kamwe …" Kwa mwisho wa maisha yao watasikia Bwana akisema nao, "Sikukujua kamwe." Bwana hakusema hapa juu ya mtu ambaye kwa wakati wa taabu kubwa anamkana kwa muda mfupi, kama Petro, lakini juu ya watu ambao wanamkana kabisa siku zote hata mwisho wa maisha yao.

### D. Si salama lakini upanga (10:34-39)

**10:34** Masemo haya ya Bwana yanaonyesha *matunda* ya kuja kwa Bwana. Hayaonyeshi *kusudi* la kuja kwake. Alisema kwamba **hakuja kuleta salama duniani lakini upanga.** Lakini Bwana alikuja kufanya salama (Efe.

2:14-17); alikuja ili ulimwengu uokolewe naye (Yn. 3:17).

**10:35-37** Lakini wakati watu walipogeuka wafuata wake, watu wa jamaa zao waliwageukia. Mwana asiyeamini atashindana na baba ambaye alikwisha kupokea Mwokozi, mama Mkristo atapata matata kwa mkono wa binti asiyeamini. Mama mwamini ya bwana wa nyumba atachukiwa na mke wa bwana wa nyumba. Hivi mara nyingi inapasa mwamini kuchagua au Kristo au jamaa. Haifai kamwe kuruhusu mapendo kwa ndugu zetu katika jamaa kutuzuiza tusifuate Bwana na roho moja. Lazima Mwokozi aheshimiwe kupita baba au mama, mwana au binti. Bei moja ya kufuata Bwana ni magomvi na uadui wa watu wa jamaa yetu wenyewe. Mara nyingine uadui huu ni mchungu kupita ule tunaopata kwa mikono ya watu wa dunia.

**10:38** Lakini kuna neno moja linalotaka kuibia Kristo pahali pa kwanza ndani ya maisha ya mwamini – ndiyo mapendo kwa uzima wake wenyewe. Hivi Yesu aliongeza, **"Naye asiyechukua msalaba wake na kunifuata hanistahili."** Msalaba ndio mti kwa kusulibisha mtu. Maana ya kuchukua msalaba na kufuata Kristo ni kujitoa na roho yote kuishi kwa yeye tu, na hata mauti si bei kubwa kupita kipimo. Si wanafunzi wote watakaoitwa kutoa uzima wao, lakini wote wanaitwa kuweka Kristo kwa pahali pa kwanza, juu kupita mambo yote katika maisha yao.

**10:39** Sharti mapendo ya Kristo yashinde hamu yetu ya mwanadamu kuchunga uzima wetu wenyewe. "**Naye anayeona uzima wake ataupoteza; naye anayepoteza uzima wake kwa ajili ya Kristo atauona."** Tunajaribiwa kuepuka maumivu na hasara ya kujitoa kuishi kwa Kristo tu. Lakini kuishi tukijipendeza wenyewe ndiyo njia ya kupoteza faida ya maisha yetu kabisa. Maisha ya faida zaidi ndiyo maisha ya utumishi kwa Kristo. Mtu yule **anayepoteza uzima wake** kwa njia ya kujitoa mzima kwa kutumikia Kristo ataona kwamba huu ndio uzima **wa faida zaidi.**

### E. Kikombe cha maji baridi (10:40-42)

**10:40** Si watu wote watakaokataa habari za wanafunzi. Watu wengine watawatambua kuwa wajumbe wa Masiya na kuwapokea vizuri. Wanafunzi watakosa njia kuonyesha asante yao kwa mema wanayotendewa, lakini hawahitaji kusumbuka juu ya neno hili. Mema yote watu wanayotendea watumishi wa Bwana wanayatenda kwa Bwana mwenyewe na watapewa zawadi.

Kupokea mwanafunzi wa Kristo ni kama kupokea Kristo mwenyewe, na kupokea Kristo ni sawasawa na kupokea Baba ambaye alimtuma, kwani yule anayetumwa ni kwa pahali pake ambaye alimtuma.

**10:41** Mtu ye yote **anayepokea nabii** kwa sababu yeye ni **nabii atapokea zawabu ya nabii.** Ona mawazo ya A.T. Pierson:

> Wayuda walihesabu manabii kuwa wakubwa zaidi kwani, hata wafalme walitawala kwa jina la BWANA na makuhani walifanya kazi yao kwa jina la BWANA, nabii aliyetoka kwa BWANA alifundisha kuhani na mfalme vilevile. Kristo alisema kama ukipokea tu nabii kwa sababu yeye ni nabii na kumsaidia, utapokea zawadi kipimo kimoja na zawadi ambayo nabii yule atapokea. Kumbuka neno hili wakati unaposikiliza mhubiri! Usifikiri rohoni mwako, 'mtu huyu hajui kusema vizuri'. *Ukimsaidia* kusema kwa ajili ya Mungu, utashiriki ndani ya zawabu yake; lakini kama, kwa sababu ya roho yako mbaya, itakuwa nguvu kupita kwaye kutimiza kazi ambayo alipewa na Mungu, wewe mwenyewe utapoteza zawabu yako. Ni vizuri sana kusaidia mtu anayejaribu kutenda yaliyo mema. Haifai uangalie mavazi yake (kama ni mazuri au ya kupasukapasuka), namna anavyosimama na kutenda, au sauti yake; lakini ujiulize mwenyewe, "Ma-

> fundisho haya toka Mungu ni kwa mimi? Mtu huyu ni nabii wa Mungu kwa roho yangu?" Kama ni hivi, umpokee, heshimu mafundisho yake na kazi yake, na pokea sehemu ya zawabu yake.[2]

Mtu yule **anayepokea mwenye haki** kwa sababu yeye ni **mwenye haki, atapokea zawabu ya mwenye haki**. Mara nyingi watu wanaohukumu mtu mwingine juu ya kuonekana kwa mwili, au hesabu ya mali yake, hawafahamu kwamba chini ya maneno haya ya kuonekana kwa macho kuna mwenye roho safi na njema. Namna tunavyotendea mwanafunzi mnyenyekevu namna hii tunatendea Bwana mwenyewe.

**10:42** Bwana anaona kila tendo jema linalotendwa kwa wanafunzi wake, na atatoa zawabu hata kwa **kikombe cha maji** tu ambacho tunaletea **mwanafunzi** kwa sababu yeye ni mfuata wa Bwana.

Hivi Bwana alimaliza agizo lake kwa mitume 12 kwa njia ya kuwapa kazi ya heshima kubwa. Ndiyo, watu watashindana nao, watawakataa, kuwahukumu, kuwafunga gerezani, na hata kuwaua. Lakini wasisahau kamwe ya kuwa walikuwa wajumbe wa Mfalme, na ya kwamba walipewa heshima kubwa kumsimamia kwa njia ya masemo na matendo yao.

## 7. KUONGEZEKA KWA UADUI NA KUKATALIKA (Sura 11, 12)

### A. Yoane Mbatizaji alifungwa (11:1-19)

**11:1** Nyuma ya kutuma wanafunzi wake kumi na wawili kwa nyumba ya Israeli kwa wakati huu, Yesu **"akaondoka kule kufundisha na kuhubiri katika miji yao**, ndiyo miji ya Galilaya, pahali wanafunzi walipokaa mbele.

**11:2,3** Kwa wakati huu Yoane alikuwa amefungwa na Herode. Alishushwa moyo na kusikia upekee, na alianza kuwa na shaka rohoni. Kama Yesu alikuwa Masiya kweli, kwa sababu gani aliacha mtangulizi wake kukaa gerezani? Kama inavyotokea kwa watu wengi wengine wa Mungu, imani ya Yoane ilipunguka kwa muda mfupi. Hivi **alituma wawili wa wanafunzi wake** kuuliza Yesu kama yeye ni kweli yule ambaye manabii walitabiri atakuja, au kama iliwapasa kukaa kutazamia kufika kwa Mpakaliwa.

**11:4, 5 Yesu alijibu** Yoane ya kwamba alikuwa akifanya maajabu yaliyotabiriwa kwamba yatafanywa na Masiya: **vipofu wanapata kuona** (Isa. 35:5); **viwete wanatembea** (Isa 35:6); **wakoma wanasafishwa** (Isa. 53:4; Mt. 8:16,17); **viziwi wanasikia** (Isa 35:5); **wafu wanafufuliw**a (neno hili halikutabiriwa juu ya Masiya; lilikuwa kubwa kupita maajabu yale yaliyotabiriwa). Yesu alikumbusha Yoane vilevile kwamba **masikini** walihubiriwa **Habari Njema**, kama ilivyotabiriwa juu ya Masiya ndani ya Isaya 61:1. Wengi wa viongozi kwa maneno ya dini wanaweka roho juu ya watu wa kujulikana na watajiri. Masiya alileta habari njema kwa watu **masikini**.

**11:6** Halafu Mwokozi aliongeza, **"Abarikiwe yeye asiyechukizwa nami."** Mtu mwingine akisema hivi tungefikiri ni mtu wa kujisifu sana, lakini Yesu akisema hivi, maneno haya yanaonyesha tu ukamilifu wa roho yake. Masiya hakufika kama jemadari mkubwa wa jeshi la askari lakini kama seremala mnyenyekevu. Upole na unyenyekevu zake hazikupatana na maneno watu waliyofikiri wataona ndani ya Masiya mwenye uwezo. Watu walioongozwa na mawazo ya dunia waliweza kuwa na shaka wakati aliposema yeye ni Mfalme, lakini Mungu atabariki watu wenye ufahamu wa roho waliotambua Yesu wa Nazareti kuwa Masiya ambaye atakuja.

Haifai tufikiri Yesu alihamakia Yoane

Mbatizaji ndani ya shairi 6. Imani ya kila mwamini inapunguka mara nyingine na inahitaji kupatishwa nguvu tena. Neno hili ni mbali na mtu anayeangushwa kabisa na kukana kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu. Tukijumlisha habari zote za maisha ya Yoane tunaona kwamba alikuwa mtu mwaminifu na mwenye kudumu kwa njia ya Mungu.

**11:7, 8** Mara moja nyuma ya **kuondoka** kwa wanafunzi wa Yoane na masemo ya kusaidia na kutuliza roho yake, Yesu alianza kusema na **makutano** na kusifu Yoane Mbatizaji sana. Hawa walikuwa watu waliokwenda jangwani mbele wakati Yoane alipohubiri. Walikwenda kwa sababu gani? Kuona mtu zaifu **aliyetikiswa** kwa **upepo** kama nyasi na mawazo mbalimbali ya watu? Sivyo! Yoane alikuwa mhubiri mhodari, aliyesukumwa na zamiri yake kuhubiri, aliyekuwa tayari kuteswa na kufa zaidi ya kunyamaza au kusema uwongo. Walikuwa **wametoka kuona** mfuasi wa mfalme mwenye kukaa katika anasa na kuvaa mavazi ya mapambo nyumbani mwa mtawala? Sivyo, hata kidogo. Yoane alikuwa mtu wa Mungu asiyejipamba mwenyewe, aliyeishi maisha ya kujinyima mwenyewe, maisha yaliyokuwa kemeo kwa watu waliopenda sana mambo ya anasa ya dunia.

**11:9** Walikuwa wametoka kuona nabii? Ndiyo, Yoane alikuwa nabii. Alikuwa nabii mkubwa kupita manabii wote. Bwana hakusema hapa kwamba alikuwa mkubwa kupita kwa njia ya tabia yake au uwezo wake wa masemo, lakini alikuwa mkubwa kupita kwa sababu alikuwa mtangulizi wa Masiya-Mfalme.

**11:10** Neno hili linaonekana wazi ndani ya shairi 10; Yoane alitimiza unabii wa Malaki (3:1) – **mjumbe** atakayetangulia Bwana na **kutayarisha** watu kwa kuja kwake. Watu wengine walikuwa wametabiri vilevile kwamba Kristo atakuja, lakini alikuwa Yoane aliyechaguliwa kutangaza kwamba alikuwa amefika.

**11:11** Maneno haya, **"aliye mdogo katika ufalme wa mbinguni ni mkubwa kupita yeye"** yanahakikisha kwamba Yesu alisema juu ya kazi ya heshima ambayo Yoane alipewa, ndiyo kutayarisha njia kwa kuja kwa Masiya. Hakusema juu ya tabia yake njema. Labda mtu **"aliye mdogo katika ufalme wa mbinguni"** hana tabia njema kupita Yoane, lakini ni mwenye mapendeleo makubwa kupita yeye. Kuwa mwenyeji wa ufalme ni heshima **kubwa kupita** kuwa mwenye kutangaza kufika kwa ufalme. Ilikuwa heshima kubwa kwa Yoane kutayarisha njia kwa Bwana, lakini alikufa mbele ya kufurahishwa na baraka za ufalme.

**11:12** Tangu mwanzo wa utumishi wa Yoane kufika wakati alipofungwa gerezani **ufalme wa mbinguni** ulikuwa umevumilia **ukali.** Wafarisayo na waandishi walikuwa wameshindana sana na ufalme. Herode vilevile alishiriki nao kwa njia ya kufunga mtangulizi wake.

**"… na watu wakali wanaukamata kwa nguvu."** Semo hili linaweza kuelezwa kwa njia mbili. Adui za ufalme walijaribu sana kuukamata kusudi waweze kuuharibu. Namna walivyokataa Yoane ilikuwa mfano wa namna watakataa Mfalme mwenyewe na ufalme wake. Lakini labda semo hili linasema juu ya watu wale waliokuwa tayari kwa kufika kwa Mfalme na waliotaka sana kuingia ndani ya ufalme. Hii ndiyo maana kwa Luka 16:16, "Torati na manabii zilikuwa hata Yoane. Tangu wakati ule Habari Njema inahubiriwa na kila mtu anajiingiza kwa nguvu kule." Hapa tunaona ufalme kama mji unaozungukwa na adui vitani, na watu wa namna zote wakijaribu kuuingia.

Maelezo haya yote mawili yanaonyesha kwamba mahubiri ya Yoane yalifanya kazi kubwa na kali katikati ya watu, na kuzaa matunda yaliyoenea pahali mbalimbali.

**11:13 "Kwa sababu manabii yote na sheria walitabiri mpaka wakati wa Yoane."** Kitabu kizima kuanza na Mwanzo kufika Malaki kilitabiri kwamba Masiya atakuja. Wakati Yoane alipotokea hakutabiri kwamba Masiya atakuja, lakini kwamba alikwisha kuja, na ya kwamba unabii wote juu ya kuja kwake mara ya kwanza ulikuwa umetimia.

**11:14** Malaki alikuwa ametabiri kwamba Elia atatangulia Masiya (Mal. 4:5,6). Kama watu **wangalikubali** kupokea Yesu kama Masiya, Yoane angalikuwa kama **Elia**. Katika Yoane 1:21 Yoane alisema wazi kwamba hakuwa Elia aliyefufuliwa. Lakini kwa Luka 1:17 alitangulia Kristo mwenye roho na nguvu za Elia.

**11:15** Watu wengine hawakufurahia utumishi wa Yoane wala kufahamu maana ya utumishi wake. Hivi Bwana alisema, **"Mwenye masikio ya kusikia, asikie!"** Maana yake, angalia vizuri ili maana ya maneno unayosikia isikupitie. Ikiwa Yoane alitimiza unabii juu ya Elia, Yesu alikuwa Masiya! Hivi kwa njia ya kusimamia Yoane Mbatizaji, Yesu alihakikisha tena kwamba yeye ni Kristo.

**11:16, 17** Lakini **kizazi** waliosikia masemo yake na kubarikiwa kwa njia ya kuona na macho yao kufika kwa Masiya-Mfalme wao, hawakuwa na hamu kupokea Yoane au Kristo. Ilikuwa nguvu kufahamu roho zao. Yesu aliwasawanisha na watoto wenye roho ya kugeukageuka wakiketi kwa soko wasiofurahia kitu cho chote. Rafiki zao wakiwapigia filimbi waweze ku**cheza,** walikataa. Walikataa ku**omboleza** vilevile wakati rafiki zao walipoiga maziko.

**11:18,19 Yoane** alikataa anasa ya mwili katika maisha yake na **alijinyima** vitu vya kufurahisha mwili, hivi Wayuda walisema ana pepo mchafu. **Mwana wa watu** alifika katikati yao akikula namna watu wote wanavyokula, lakini neno hili halikuwafurahisha vilevile. Walisema yeye ni **mlafi** na mlevi, **rafiki ya watoza kodi na wenye zamb**i. Yesu hakula au kunywa kamwe kupita kipimo. Alikuwa **rafiki ya watoza kodi na wenye zambi** kweli, lakini si kwa njia wao waliyofikiri. Alikuwa rafiki ya wenye zambi kusudi aweze kuwaokoa toka zambi zao, lakini hakushiriki kamwe ndani ya zambi zao.

**"Na hekima inapata haki yake kwa kazi zake."** Bwana Yesu ndiye Hekima (1 Kor.1:30). Hata wasioamini wakisema maneno mabaya juu yake, na hata zaidi ya Wayuda wakikataa kuamini kwamba yeye ni Masiya-Mfalme, maajabu yake na kazi alizofanya ndani ya roho za wanafunzi wake yalihakikisha ya kwamba yeye ni Masiya.

### B. Ole kwa miji ya Galilaya isiyotubu (11:20-24)

**11:20** Baraka kubwa inaleta kazi kubwa vilevile. Miji ya Korazini, Betesaida na Kapernaumu ilibarikiwa kupita yote mingine. Mwana wa Mungu katika mwili alitembea katika njia zao zenye mavumbi. Alifundisha watu wao na kufanya zaidi ya **maajabu yake ya uwezo** ndani yao. Lakini hata kama walipewa ushuhuda mkubwa huu, walikaa na ukaidi na walikataa kutubu. Hatushangai kwamba Bwana alitangaza hukumu kubwa sana juu yao.

**11:21** Alianza na **Korazini** na **Betesaida.** Watu wa miji hii walisikia Mungu-Mwokozi wao akiwasihi na neema kumpokea, lakini walimkataa. Mawazo yake yaligeuka kwa watu wa **Tiro na Sidona** waliohukumiwa na Mungu kwa sababu walikwamana na kuabudu sanamu na uovu. Kama watu wa miji ile wangalipewa njia kuona maajabu ya Yesu, wangalijinyenyekeza

na kutubu kabisa. Hivi **siku ya hukumu** Korazini na Betesaida watahukumiwa kupita **Tiro na Sidona.**

**11:22** Maneno haya **"Itakuwa kuvumilika kwa Tiro na Sidona siku ya hukumu kupita ninyi"** yanaonyesha kwamba kutakuwa na vipimo mbalimbali vya hukumu katika Hadeze, kama vile kutakuwa na zawabu za vipimo mbalimbali mbinguni (1 Kor. 3:12-15). Zambi moja tu inafikisha mtu kwa Hadeze, ndiyo zambi ya kukataa kujinyenyekeza na kupokea Yesu Kristo (Yoane 3:36b). Lakini kule atateswa kwa kipimo cha baraka alizokataa na zambi alizofanya.

**11:23, 24** Miji michache tu ilibarikiwa kama Kapernaumu. Uligeuka mji wa Yesu wakati watu wa Nazareti walipokwisha kumkataa (9:1; ona Mk. 2:1-12). Alifanya pale mengine ya maajabu yake ya kushangaza zaidi yaliyohakikisha kabisa kwamba yeye ni Masiya. Kama watu wa Sodomo, wenye zambi sana, wangaliweza kuona maajabu haya, wangalitubu na kuachiliwa. Watu wa Kapernaumu walibarikiwa hata kupita. Ingaliwapasa kutubu na kupokea Mwokozi na furaha, lakini hawakufanya hivi. Zambi za mwili za watu wa Sodomo zilikuwa kubwa, lakini hakuna zambi iliyo kubwa kupita zambi ya kukataa Mwana mtakatifu wa Mungu. Hivi hukumu ya Sodomo itakuwa ndogo kupita ile ya Kapernaumu. Kapernaumu umepandishwa hata **mbinguni** kwa sababu ya baraka uliyopewa lakini **utashushwa hata Hadeze** kwa hukumu. Kama neno hili ni kweli kwa Kapernaumu, ni kweli hata kupita kwa inchi zenye Biblia nyingi, na pahali Habari Njema inapohubiriwa kwa njia nyingi, na watu hawana uzuru kukataa Mwokozi.

Wakati Bwana Yesu alipokuwa duniani kulikuwa na miji mine ya kujulikana katika Galilaya: Korazini, Betesaida, Kapernaumu, na Tiberia. Yesu alitangaza ole juu yao yote ila Tiberia. Mwisho wake nini? Korazini na Betesaida iliangamizwa pia na hatujui kabisa kwa wakati wa sasa pahali iliposimama. Pahali pa Kapernaumu hapajulikani wazi vilevile. Lakini mji wa Tiberia unasimama hata sasa. Maneno haya yanatimiza unabii na kuonyesha kwamba Mwokozi anajua maneno yote, na kuandika kwa Biblia kuliongozwa na Mungu.

### C. Mwokozi alitenda nini kwa sababu ya kukataliwa (11:25-30)?

**11:25, 26** Miji ile mitatu ya Galilaya haikutambua wala kupenda Kristo wa Mungu. Alijua ya kwamba kwa wakati wa kuja atakataliwa na watu wengi zaidi. Ugumu wa mioyo yao ulimsukuma kutenda nini? Alikuwa na roho ya uchungu na vita? Sivyo. Alisifu na kushukuru Mungu kwa sababu hakuna neno lililoweza kuzuiza kutimizwa kwa makusudi yake. **"Ninakushukuru, Ee Baba, Bwana wa mbingu na dunia, kwa kuwa ulificha mambo haya kwa wenye hekima na akili, na uliyafunua kwa watoto wachanga."**

Vizuri tufahamu kwamba maana ya masemo ya Yesu haikuwa kuonyesha kwamba Yesu alifurahi juu ya hukumu itakayopata miji hii ya Galilaya. Na vilevile ya kwamba Mungu hakunyimia wenye hekima na akili nuru.

Miji ile ilikuwa na njia tena na tena kukaribisha Bwana Yesu. Walikataa na kusudi kumnyenyekea. Wakati walipokataa nuru yake, Mungu aliwanyimia nuru. Lakini mashauri ya Mungu yatatimizwa. Kama wenye hekima wakikataa kuamini Bwana Yesu, Mungu atamfunua kwa watu wanyenyekevu wasio na heshima. Anashibisha wenye njaa na vitu vyema; wenye mali amewaondosha mikono mitupu (Lk. 1:53).

Wale wanaofikiri wao ni wenye

hekima nyingi sana, na hawahitaji Kristo watapigwa na upofu wa roho. Lakini atajifunua kwa wale wanaokubali kwamba wanakosa akili kwani "ndani yake hazina zote za hekima na kujua zinafichwa" (Kol. 2:3). Yesu alishukuru Baba kwa sababu hata kama watu wengine wakikataa kumpokea, atapokewa na wengine. Hata wakati kutokuamini kwa watu kulipozidi alifarijiwa wakati alipokumbuka mashauri na makusudi ya Mungu yatatimizwa.

**11:27 Kristo alipewa vitu vyote na Baba yake**. Kwa mtu mwingine kusema hivi ingekuwa kiburi, lakini kwa Bwana Yesu yalikuwa masemo ya kweli. Uadui wa watu ulikuwa ukiongezeka kwa wakati ule, na haikuonekana kwamba Kristo alikuwa na amri yote, lakini ilikuwa hivi kweli. Maneno ya maisha yake yalitokea kufuatana na kutaka kwa Mungu na mwishoni atashinda na utukufu. **"Hakuna mtu anayejua Mwana ila Baba."** Namna ya Kristo ni siri kwa sisi. Hatuwezi kufahamu hata kidogo namna utu na uungu zinaweza kufungamana ndani ya Mmoja. Kwa mfano waza juu ya maneno ya mauti. Mungu hawezi kufa. Lakini Yesu ni Mungu na Yesu alikufa. Lakini haiwezekani kutenga tabia yake ya Mungu na mtu. Tunaweza kumjua na kumpenda na kumtumainia, lakini Mungu Baba tu anaweza kumjua na kumfahamu kabisa.

**"Hakuna mtu anayejua Baba ila Mwana, naye Mwana anapendezwa kumfunulia kwake."** Inatushinda sisi watu kufahamu Baba vilevile. Mungu tu anaweza kufahamu Mungu. Mtu wa dunia hawezi kumjua kwa akili na nguvu yake mwenyewe. Lakini Bwana Yesu anaweza, naye anafunua Baba kwa wale ambao anawachagua. Mtu ye yote anayejua Mwana anajua Baba vilevile (Yn. 14:7).

Lakini nyuma ya kusema maneno haya yote kujaribu kueleza shairi 27, tunakiri ya kwamba kweli hizi zote zinapita akili yetu. Tunaona nusu nusu, kama katika kioo. Hata mbinguni hatutafahamu kabisa ukubwa wa Mungu wetu, wala siri ya Mwana wa Mungu kutwaa utu. Wakati tunaposoma kwamba Baba anafunuliwa kwa wale tu wanaochaguliwa na Mwana, labda tunajaribiwa kufikiri kwamba watu wachache tu wanachaguliwa, kama kwa upendeleo, lakini shairi linalofuata linaonyesha kwamba neno hili si kweli. Ndani ya shairi 28 Bwana anaita watu wote wenye kusumbuka na kubeba mizigo mizito kufika kwake kupata pumziko. Tunaona kwamba watu wale ambao Bwana anachagua kufunua Baba ndio wale ambao wanamwamini kuwa Bwana na Mwokozi. Tuone vilevile kwamba Bwana alitoa mwito huu wa huruma na mapendo nyuma ya kukataliwa na miji ile ya Galilaya iliyobarikiwa zaidi. Kuchukia na ukaidi wa watu hazikuweza kuzima mapendo na neema yake.

**11:28 Kujeni**. Maana ya kuja ni kuamini (Mdo. 16:31); kupokea (Yn. 1:12); kula (Yn. 6:35); kunywa (Yn. 7:37), kuangalia (Isa. 45:22); kukiri (1 Yn. 4:2); kusikia (Yn. 5:24,25); kuingia mlango (Yn. 10:9); kufungua mlango (Ufu. 3:20) ; kugusa upindo wa vazi lake (Mt. 9:20,21), na kupokea zawadi ya uzima wa milele kwa njia ya Kristo Bwana wetu (Rom. 6:23).

**kwangu.** Si kwa dini au mafundisho ya mhubiri fulani, lakini kwa Kristo aliye hai. Wokovu ni ndani ya Kristo. Wale waliopokea Kristo wameokolewa kabisa.

**ninyi wote munaosumbuka na wenye mizigo mizito**. Mtu akitaka kufika kwa Yesu na roho ya kweli, inampasa kukubali kwamba anabeba mzigo wa zambi. Wale tu wanaokubali kwamba wao ni wapotevu wanaweza kuokolewa. Sharti mtu atubu kwa Mungu

kwanza mbele ya kuamini Bwana Yesu Kristo.

**nami nitawapumzisha ninyi**. Ona ya kwamba **pumziko** ni zawadi. Hatustahili kulipokea wala kutumika kazi kulipata. Ni *pumziko la wokovu* tunalopata wakati tunapofahamu kwamba Kristo alitimiza kazi ya ukombozi kwa Kalvari. Ni *pumziko la damiri* wakati tunapofahamu kwamba azabu kwa zambi zetu zote ililipwa na ya kwamba Mungu hataomba malipo mara ya pili.

**11:29** Ndani ya mashairi 29 na 30 mwito wa Yesu unageuka mwito kwa utumishi.

**Tieni nira yangu juu yenu**. Maana yake ni kunyenyekea kutaka kwake, kutoa maisha yetu mazima kutawaliwa naye (Rom. 12:1,2).

**na mufundishwe nami.** Wakati tunapokubali utawala wa Bwana juu ya kila sehemu ya maisha yetu, anatufundisha kuwa wafuata wa faida.

**kwa sababu mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo.** Mwalimu wa kweli si mkali na mwenye kiburi kama Wafarisayo, lakini ni mpole na **mnyenyekevu**. Wale wanaopokea nira yake watajifunza kukamata pahali pa chini zaidi.

**mutapata raha kwa nafsi zenu.** Hasemi hapa juu ya raha ya damiri, lakini raha ya moyo inayopatikana kwa njia ya kukamata pahali pa chini zaidi mbele ya Mungu na watu. Ni raha mtu anayosikia ndani ya utumishi wake kwa Kristo wakati anapoacha kujitafutia mwenyewe ukubwa na utukufu.

**11:30 "Kwa maana nira yangu ni laini, na mzigo wangu ni mwepesi."** Ndiyo, nira yake ni mbali na mizigo ya Wafarisayo. Yesu alisema juu yao, "Maana wanafunga mizigo mizito iliyo michungu kwa kuvumilia kwa mabega ya watu, lakini wao hawataki kuigusa hata na vidole vyao" (Mt. 23:4). Nira ya Yesu ni laini, haiumizi ngozi.

**Mzigo** wake ni **mwepesi**. Si kusema kwamba Wakristo hawapati matata na huzuni, lakini hawahitaji kuzibeba peke yao. Tunafungwa nira pamoja na Bwana Yesu, naye anatupa sisi neema ya kutosha kwa kila wakati wa hitaji. Kumtumikia Yesu si utumwa lakini uhuru wa kweli.

J. H. Jowett anasema,

> Mara nyingi waamini wanaanguka kwa sababu wanajaribu kubeba mzigo wa maisha yao peke yao. Halikuwa kusudi la Mungu kamwe kwa mtu kubeba mzigo wake peke yake. Nira ina nafasi kwa shingo mbili na Bwana mwenyewe anataka kuingia moja ya nafasi hizi. Anataka kushiriki mizigo yetu na kila kazi ngumu. Mkristo anashinda na kupata salama rohoni wakati anapoacha kujaribu kufanya kazi peke yake, na anajinyenyekeza na kupokea "nira" ya Bwana wake .

### D. Yesu ni Bwana wa Sabato (12:1-8)

**12:1** Sura hii inapasha juu ya kuongezeka kwa kukataa na uadui na hila ya Wafarisayo. Maulizo juu ya kushika sabato yalifunua neno hili wazi.

Siku ile ya sabato, **Yesu** na wanafunzi wake walikuwa **wakipita katika mashamba ya nafaka**. **Wanafunzi wake wakaanza kuvunja masuke, wakakula**. Sheria ilikubali wakamate nafaka ya shamba la jirani yao lakini hawakuwa na ruhusa kutumika na mundu (Tor. 23:25) kukata nafaka.

**12:2** Lakini **Wafarisayo** walisema walikuwa wakiasi sheria ya **sabato**. Hatusomi neno hili waziwazi, lakini tunafikiri walishitaki wanafunzi juu ya kuvuna (kuvunja nafaka); kupura na kupepeta nafaka (kutenga nafaka na kapi).

**12:3, 4** Yesu alijibu mashitaki yao ya kuchekesha kwa njia ya kuwakumbusha neno lililotokea katika maisha ya **Daudi**. Siku moja wakati Daudi alipokimbia Saulo, yeye na watu wake walikuwa jangwani na **walikula mikate ya onye-**

**sho** isiyokuwa halali kwao kula; ilikuwa kwa makuhani tu. Daudi wala watu waliokuwa pamoja naye walikuwa makuhani, lakini Mungu hakuwahamakia kwa sababu ya kufanya hivi. Kwa nini?

Halikuwa kusudi kamwe kwa sheria ya Mungu kuwa taabu kwa watu wake waaminifu. Daudi hakuwa mkimbizi kwa sababu ya zambi ambayo alikuwa ametenda. Taifa la Israeli lenye zambi lilimkataa. Kama yeye angalipewa nafasi ambayo alistahili kupokea, yeye na wafuata wake wasingalikula mikate ya onyesho. Kwa sababu kulikuwa na zambi katika Israeli, Mungu alikubali tendo hili lisilofaa.

Habari hizi zilikuwa mfano wazi wa taifa la Israeli kwa wakati ule. Bwana Yesu alikuwa Mfalme wa Israeli, lakini taifa hili halikukubali atawale juu yao. Kama angalikubaliwa kuwa Mtwala wao, kama wafuata wake wasingalilazimishwa kula hivi siku ya sabato au siku yo yote nyingine. Bwana hakukemea wanafunzi wake, kwa sababu hawakufanya neno baya.

**12:5** Bwana Yesu alikumbusha Wafarisayo ya kwamba **makuhani wanakufuru siku ya sabato** kwa njia ya kuchinja nyama za sadaka na kutimiza kazi nyingine za utumishi wao (Hes. 28:9,10), lakini **hawakuwa na kosa** kwa sababu walikuwa wakifanya kazi ya Mungu.

**12:6** Wafarisayo walijua kwamba makuhani walitumika kazi kila sabato hekaluni bila kulichafua. Kwa sababu gani walishitaki wanafunzi juu ya kufanya neno walilofanya mbele ya Mmoja **aliyekuwa mkubwa kupita hekalu**?

**12:7** Wafarisayo hawakufahamu kamwe mapendo ya Mungu. Katika Hosea 6:6 Mungu alisema, **"Ninataka rehema, hapana zabihu."** Mungu anaheshimu huruma kuliko desturi za dini. Angetaka kuona watu wake wakivunja masuke ya ngano na kula kupunguza njaa yao, kupita kujitaabisha kwa njia ya kushika sheria ya sabato katika kila neno dogo. Kama Wafarisayo wangalifahamu neno hili wasingalihukumu wanafunzi. Lakini waliweka roho juu ya kushika sheria ndogo ndogo za kuonekana mbele ya watu, kuliko kuwaza juu ya kusaidia mahitaji yao.

**12:8** Halafu Mwokozi alisema vilevile, **"Mwana wa watu ni Bwana wa sabato."** Alikuwa yeye aliyesimamisha sheria zamani, hivi aliweza kuifasiri vizuri.

Mbele ya kuendelea na habari za Yesu akiponyesha mwenye mkono wa kupooza, tuone maneno mengine juu ya sabato.

### MAFUNDISHO JUU YA SABATO

Siku ya sabato ilikuwa siku ya saba tangu zamani na neno hili halitageuka kamwe.

Mungu alipumzika siku ya saba nyuma ya kushinda siku sita akiumba dunia (Mwa. 2:2). Hakuagiza watu kushika sabato kwa wakati ule; lakini labda alikusudi kwa watu kuiga utaratibu wa kustarehe siku moja ndani ya saba kwa wakati ule.

Taifa la Israeli waliagizwa kushika sabato saa Mungu alipowatolea Amri Kumi (Kut. 20:8-11). Sheria ya sabato ilikuwa namna nyingine na sheria tisa nyingine. Ilikuwa juu ya kawaida ya dini, lakini sheria tisa nyingine zilikuwa juu ya usafi wa mwenendo. Kulikuwa na sababu moja tu iliyokataza watu kutumika kazi siku ya sabato, ndilo agizo la Bwana. Sheria tisa nyingine zilikuwa juu ya maneno yaliyokuwa mabaya.

Sheria iliyokataza watu kutumika kazi haikuwa kamwe juu ya kazi kwa Mungu (Mt. 12:5), kazi za lazima (Mt. 12:3,4), au kazi za rehema (Mt. 12:11,12). Tisa za sheria hizi ni katika Agano Jipya vilevile, lakini si kama she-

ria lakini kama mafundisho kwa Wakristo kwa wakati huu wa neema. Sheria moja tu haikutajwa tena, ndiyo sheria juu ya kushika sabato. Wakristo hawakuagizwa kamwe kushika sabato. Lakini Paulo alionyesha kwamba haifai kuhukumu Mkristo kwa sababu hakushika sabato (Kol. 2:16).

Siku kubwa ya Wakristo ndiyo siku ya kwanza ya juma. Bwana Yesu alifufuka toka wafu siku ile (Yn. 20:1) kuhakikisha kwamba kazi ya ukombozi ilimalizwa na kukubaliwa na Mungu. Siku ya kwanza mbili za nyuma Bwana alikutana na wanafunzi wake (Yn. 20:19,26). Waamini waliletewa Roho Mtakatifu siku ya kwanza ya juma (Mdo. 2:1; ona vile Law. 23:15,16). Wanafunzi wa kwanza walikutana siku ile kuvunja mkate, kutangaza kufa kwa Bwana (Mdo. 20:7). Ni siku iliyowekwa na Mungu kwa Wakristo kutoa mali kwa kazi ya Bwana (1 Kor. 16:1,2).

Sabato ilikuwa kwa mwisho wa juma la kazi. Kwa mwanzo wa juma, siku ya Bwana, waamini walijua kwamba kazi ya ukombozi ilikwisha. Sabato ilikuwa ukumbusho wa kuumba kwa dunia; siku ya Bwana inafungamana na viumbe vipya. Siku ya sabato ilikuwa siku ya lazima; Siku ya Bwana ni siku ya mapendeleo.

Wakristo hawashiki siku ya Bwana kwa kupata wokovu au utakatifu au kwa sababu wanaogopa azabu. Wanaichunga kwa sababu ya mapendo yao kwa Bwana ambaye alijitoa kwa ajili yao. Siku ile hatufungwi na kazi zetu za kila siku, hivi tuna saa nzuri kwa kuabudu na kutumikia Kristo.

Haifai kusema sabato imegeuzwa kuwa siku ya Bwana. Sabato itakaa kuwa siku ya saba ya juma, na Siku ya Bwana ni siku ya kwanza ya juma. Sabato ni kivuli; mwili ni wa Kristo (Kol. 2:16,17). Ufufuko wa Kristo ulikuwa mwanzo wa mambo mapya, na Siku ya Bwana inaonyesha mwanzo ule.

Akiwa Myuda mwaminifu aliyeishi kwa wakati wa sheria, Yesu alishika sabato. Kama Bwana wa sabato aliifungua toka kawaida na maagizo yasiyofaa tena. ❖

### E. Yesu anaponyesha siku ya sabato (12:9-14)

**12:9** Toka mashamba ya nafaka **Yesu akaingia sunagogi**. Luka anatujulisha kwamba waandishi na Wafarisayo walikuwa pale kuona kama wataweza kupata njia kumshitaki (Luka 6:6,7).

**12:10** Katika sunagogi alikuwa mtu **mwenye mkono wa kupooza** – Wafarisayo hawakuweza kumsaidia! Kufika sasa waliona mtu yule bure, lakini sasa walifikiri kwamba labda mtu huyu ataweza kuwasaidia kutega Yesu. Walijua kwamba Mwokozi alikuwa tayari saa zote kusaidia wenye taabu mwilini. Kama akiponyesha mtu huyu siku ya sabato, tendo hili litakuwa kosa ambalo waliweza kuazibu. Hivi waliuliza, **"Ni halali kuponyesha siku ya sabato?"**

**12:11** Mwokozi aliwajibu kwa njia ya kuwauliza kama mmoja wa **kondoo zao** akianguka **shimoni,** watamwondosha kule siku ya **sabato**? Ndiyo, watamwondosha, na labda watasema hili ni tendo la rehema. Lakini wangekumbuka vilevile faida ya kondoo hii kwa njia ya mali, na hawatataka kupata hasara ya mali, hata siku ya sabato.

**12:12** Bwana wetu aliwakumbusha kwamba damani ya mtu inapita mbali **damani ya kondoo**. Kama ni vizuri kurehemu nyama, ni vizuri zaidi kutendea mtu huyu **mema siku ya sabato**!

**12:13,14** Nyuma ya kuonyesha choyo ya Wafarisayo wazi, aliponyesha mkono wa kupooza. Mtu mwenyewe alionyesha **imani** yake wakati alipotii agizo la Bwana na **kunyolosha mkono** wake. **Ukapona kabisa kama mkono wake mwingine.** Tungefikiri Wafarisa-

yo wangefurahi kwa sababu mtu huyu ambaye hawakuweza wala kutaka kusaidia alipona. Sivyo! Walikasirikia Yesu sana, wakatoka na kufanya shauri namna gani wataweza kumwua. Kama wao wangalikuwa na mkono wa kupooza kama wangalifurahi sana kuponyeshwa siku yo yote ya juma!

**F. Kuponyeshwa kwa watu wote (12:15-21)**

**12:15, 16 Wakati Yesu alipofahamu** mawazo ya adui zake, **akaondoka** kule, akakwenda pahali pengine. Lakini pahali po pote alipokwenda kulikuwa na makutano makubwa, na pahali pote wagonjwa walipokusanyika **aliwaponyesha wote**. Lakini aliwakataza wasitangaze habari za maajabu aliyofanya kuwaponyesha, si kwa sababu aliogopa hatari, lakini kwa sababu hakutaka watu wa kugeukageuka kumheshimu kama kiongozi mkuu cha maasi. Lazima orodha ya Mungu itimizwe. Kutakuwa maasi kwa saa iliyowekwa mbele na Mungu, si kwa njia ya kumwangika kwa damu ya Waroma, lakini kwa sababu ya kumwangika kwa damu yake mwenyewe.

**12:17,18** Utumishi wake wa neema ulitimiza unabii wa **Isaya** 41:9; 42:1-4. **Nabii** aliona Masiya kama Mshindaji mpole. Alionyesha Yesu kama **Mtumishi aliyechaguliwa** na BWANA, **Mpendwa aliyependeza** nafsi ya Mungu sana. **Mungu atamwekea Roho** yake, ndio unabii uliotimizwa kwa wakati wa ubatizo wa Yesu. Na utumishi wake haukuwa kwa inchi ya Israeli tu lakini kwa inchi nyingi nyingine. **Atatoa hukumu kwa mataifa**. Neno hili litaongezeka kwa kipimo ambacho watu wa Israeli walimkataa.

**12:19** Isaya alitabiri vilevile ya kwamba Masiya hatashindana, wala mtu hatasikia **sauti yake njiani**. Ni kusema hatakuwa mwenye kuamsha roho za watu na kuongoza makutano kushindana na serikali.

**12:20** Hatavunja **unyasi uliopondwa,** wala hatazima **utambi unaotoka moshi**. Hatakanyaga watu walioondolewa mali, na wasiokuwa na kitu. Atasaidia na kupatisha nguvu wenye roho za kuvunjika na wanaoteswa. Atasaidia na kuongeza vilevile imani ndogo ya wengine. Utumishi wake utaendelea kufika wakati atakapoleta **hukumu mpaka kushinda**. Atakaa kusaidia wengine na mapendo na unyenyekevu, si neno kama watu wakimchukia na kukosa kuwa na asante.

**12:21 Na kwa jina lake Mataifa watatumaini**. Ndani ya Isaya 42:4 imeandikwa: "Na visanga vitangoja sheria yake," lakini maana yake ni moja. Visanga ndivyo Mataifa. Ni mfano kwamba wanangojea utawala wake ili waweze kuwa watumishi wake waaminifu.

**G. Zambi isiyoweza kusamehewa (12:22-32)**

**12:22-24** Wakati Yesu alipoponyesha mtu mwenye pepo mchafu aliyekuwa kipofu na bubu, watu walianza kufikiri labda Yesu ni kweli **Mwana wa Daudi**, Masiya ya Israeli. Neno hili liliamsha gazabu rohoni mwa Wafarisayo. Iliwashinda kuacha watu kusema neno jema juu ya Yesu, na walionyesha hasira yao kwa njia ya kusema ajabu hili lilifanywa kwa uwezo wa **Belzebuli, mkubwa wa pepo wachafu.** Hukumu hii ya kuogofya ilikuwa mara ya kwanza waliyoshitaki Bwana Yesu wazi kusema uwezo wake ulitoka kwa pepo wachafu.

**12:25, 26 Yesu alitambua mafikiri yao,** akaendelea kuonyesha upumbavu wa mawazo ya namna hii. Alionyesha kwamba hakuna **ufalme, mji, au nyumba inayotengwa** juu yake yenyewe inayoweza kusimama na kusitawi. Kama Yesu angalitoa pepo wachafu wa Shetani kwa uwezo wa Shetani, Shetani **angalishindana na yeye mwenyewe.**

**12:27** Na Yesu alikuwa na jibu lingine la nguvu kwa Wafarisayo. Wengine wa watu walioshiriki nao walisema walikuwa na uwezo kutoa wapepo wachafu. Yesu hakukubali wala kubisha neno hili, lakini alionyesha kwamba **yeye** (Yesu) **akitoa pepo wachafu kwa Belzebuli,** halafu watu wale walikuwa wakifanya vivyo hivyo. Wafarisayo wasingalikubali kamwe neno hili, lakini hawakuweza kulibisha vilevile. Watu wale ambao walishiriki nao wangaliwahukumu kufikiri kwamba walikuwa watenda kazi ya Shetani.

**12:28** Lakini Yesu alikuwa akitoa pepo wachafu kwa Roho Mtakatifu. Aliishi maisha yake mazima hapa duniani kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Alikuwa Masiya aliyejazwa Roho Mtakatifu ambaye Isaya alitabiri habari zake (Isa. 11:2; 42:1; 61:1-3. Hivi alisema na Wafarisayo, **"… kama mimi kwa Roho ya Mungu nikitoa pepo wachafu, ufalme wa Mungu umekwisha kuwafikia ninyi."** Bila shaka tangazo hili lingeponda roho za Wafarisayo. Walijivuna juu ya kujua maneno ya Mungu, lakini **ufalme wa Mungu ulikuwa umewafikia** kwa sababu Mfalme alikuwa katikati yao, nao hawakutambua neno hili!

**12:29** Bwana Yesu hakutumika pamoja na Shetani hata kidogo, lakini alimshinda. Alionyesha neno hili kwa njia ya habari za **mtu mwenye nguvu**. **Mwenye nguvu** ndiye Shetani. **Nyumba** yake ni pahali anapotawala. **Vitu** vyake ndivyo pepo wachafu. Ni Yesu anayefunga **mwenye nguvu**, anaingia **nyumbani** mwake na kunyanganya **vitu vyake**. Kufungwa kwa Shetani kutafanyikana sehemu sehemu kwa wakati mbalimbali. Kulianza wakati wa utumishi wa Kristo katikati ya watu. Kufa na ufufuko wa Kristo zilihakikisha kwamba Shetani atafungwa kweli. Utaonekana wazi kupita kwa wakati Mfalme atakapotawala kwa miaka elfu moja (Ufu. 20:2). Kutakuwa kweli kwa milele wakati atakapotupwa ndani ya ziwa la moto (Ufu. 20:10). Hatuoni sasa kwamba Shetani amefungwa, naye ana uwezo wengi, lakini ni kwa muda mfupi tu mbele ya kuangamizwa kwake kwa milele.

**12:30** Halafu Yesu alisema, **"Mtu asiye pamoja nami ni juu yangu, naye asiyeokota pamoja nami anasambaza."** Masemo mabaya ya Wafarisayo yalionyesha kwamba hawakuwa **pamoja** na Bwana; hivi walikuwa **juu** yake, ndio adui zake. Kwa njia ya kukataa kukusanya mavuno pamoja naye walisambaza nafaka. Walikuwa wameshitaki Yesu kusema alitoa pepo wachafu kwa uwezo wa Shetani, lakini wao wenyewe walikuwa watumishi wa Shetani, na walikuwa wakizuiza kazi ya Mungu.

Ndani ya Marko 9:40, Yesu alisema, "… **asiye juu yetu ni upande wetu**." Ni kama masemo haya hayapatani hata kidogo na masemo yake katika Matayo 12:30. Kwa kutusaidia kufahamu neno hili, vizuri tuone ya kwamba shairi katika Matayo ni juu ya *wokovu*. Au mtu ni pamoja na Yesu, au yeye ni juu yake, maana anashindana naye. Hakuna nafasi ya katikati. Marko 9:40 ni juu ya *utumishi*. Hata kama wanafunzi wa Yesu wanashiriki ndani ya makanisa mbalimbali yasiyopatana yote kwa mafundisho yao, neno kubwa ndilo hili: Kama mtu hashindani na Kristo, yeye ni upande wake na inastahili kumheshimu.

**12:31,32** Mashairi haya ni mashairi makubwa ndani ya maisha ya Yesu, na namna anavyotendea viongozi vya Israeli. Aliwashitaki kusema walifanya zambi isiyoweza kusamehewa, ndiyo kutukana Roho Mtakatifu, maana walikuwa wamesema Yesu alifanya maajabu yake kwa uwezo wa Shetani, si

kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Ni kama waliita Roho Mtakatifu Belzebuli, mkubwa wa pepo wachafu.

Kuna usamehe kwa namna nyingine za **zambi na matukano**. Hata mtu anayesema maneno mabaya juu ya Mwana wa watu anaweza kusamehewa. Lakini kutukana Roho Mtakatifu ni zambi isiyoweza kusamehewa, wala katika **ulimwengu wa sasa**, wala katika **ule unaokuja**. Wakati Yesu aliposema juu ya **ulimwengu wa sasa** alisema juu ya muda alipohubiri duniani. Labda haiwezekani kufanya zambi ile isiyoweza kusamehewa sasa, kwa sababu Yesu si hapa katika mwili akifanya maajabu kwa saa hii.

Zambi isiyoweza kusamehewa si sawasawa na zambi ya kukataa kuamini Habari Njema. Inawezekana kwa mtu kukataa kupokea Mwokozi kwa miaka mingi, kisha kutubu, kuamini na kuokolewa. (Lakini akikufa bila kuamini hatasamehewa.)

Na kurudi nyuma si zambi isiyoweza kusamehewa. Inawezekana kwa mwamini kwenda mbali na Bwana, lakini akitubu anaweza kurudishwa tena karibu na Mungu na kwa ushirika wa jamaa ya Mungu.

### H. Mti unajulikana kwa namna ya matunda yake (12:33-37)

**12:33** Ingalipasa hata Wafarisayo kukubali kwamba Bwana alikuwa ametenda mema wakati alipotoa pepo wachafu, lakini walimshitaki kusema alikuwa mwovu. Hapa Bwana alionyesha kwamba maneno haya hayapatani. Anawakumbusha kwamba **mti mzuri** unazaa **matunda mazuri** na mti mbaya anazaa matunda mabaya. Matunda ya utumishi wa Yesu yalikuwa mazuri. Alikuwa ameponyesha wagonjwa, wapofu, waziwi, na wabubu, alitoa pepo wachafu na kufufua wafu. Mti mwovu uliweza kuzaa matunda mazuri namna hii? Haiwezekani hata kidogo! Kwa nini basi walizidi kumkataa?

**12:34, 35** Kwa sababu walikuwa **kizazi cha nyoka**. Masemo yao mabaya yalitoka mioyo yao miovu. Wenye moyo mwema watatoa masemo mema na ya neema na haki; ndani ya mioyo miovu itatoka matukano na uchungu.

**12:36** Yesu alionya wasikiaji wake (na sisi vilevile) ya kwamba **watatoa hesabu ya kila neno bure** wanalosema. Maneno watu wanayosema yanaonyesha hali ya roho zao, na ni msingi wa hukumu au ondoleo ya hukumu yao. Bila shaka hukumu ya Wafarisayo itakuwa kubwa kwa sababu ya maneno mabaya sana waliyosema juu ya Mwana mtakatifu wa Mungu!

**12:37 "Kwani kwa masemo yako utahesabiwa haki, na kwa masemo yako utahukumiwa."** Kwa mwamini azabu kwa masemo bure ililipwa kwa njia ya mauti ya Kristo; lakini kama hakiri na kupata usamehe kwa masemo namna hii, yatapunguza zawabu atakayopokea kwa kiti cha hukumu cha Kristo.

### I. Alama ya Nabii Yona (12:38-42)

**12:38** Bwana Yesu alikuwa amefanya maajabu mengi. Lakini hata hivi **waandishi na Wafarisayo** walikuwa na ukaramisu kumwomba kuwatolea **alama** lingine. Kusudi lao lilikuwa kusema kama Yesu angeweza kuhakikisha ya kuwa yeye ni kweli Masiya, wao wenyewe *wangemwamini!* Haikuwa nguvu kutambua udanganyifu wao. Wataamini kweli kama wakiona alama nyingine? Mungu hapendezwi hata kidogo wakati tunapoomba kupewa maalama kutusaidia kuamini. Yesu alisema na Tomasi, "Heri wale wasioona, lakini wameamini" (Yn. 20:29). Mungu anataka tuamini mbele ya kuona.

**12:39** Bwana aliwaita **kizazi kibaya na chenye uzini.** Walikuwa **wabaya** kwa sababu walitaka kuona alama na walifunga macho yao na kusudi wasione

Masiya yao, na walikuwa **wazini** kwa sababu hawakuwa waaminifu kwa Mungu wao. Mungu Mwumba wao, ndiye Mungu na mtu pamoja, alikuwa akisimama katikati yao na kusema nao, na hata hivi walikuwa na ujasiri kumwomba kuwapa alama.

**12:40** Aliwaambia wazi kwamba hawatapewa **alama ila alama ya nabii Yona,** ndilo mfano wa mauti yake mwenyewe, kuzikwa na kufufuliwa kwake (Yon. 1:17; 2:10). Ufufuko wake toka wafu utakuwa alama ya mwisho ya utumishi wake kwa taifa la Israeli.

**Kama Yona alivyokuwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la samaki mkubwa,** vivyo hivyo Bwana wetu alitabiri kwamba atakuwa **siku tatu mchana na usiku** katika kaburi. Watu wanafikiri kwamba Yesu alizikwa siku ya tano na alifufuliwa siku ya kwanza ya juma. Basi namna gani aliweza kuwa kaburini siku tatu mchana na usiku? Kwa sababu Wayuda walihesabu hata sehemu ya mchana au usiku kuwa siku moja nzima.

**12:41** Yesu alionyesha hatia ya viongozi vya Wayuda kwa njia ya kutaja habari za watu wa Mataifa **wa Ninawe**, na za **malkia** ya Sheba toka kusini. Watu wa Ninawe hawakubarikiwa kama Wayuda lakini **walitubu** na huzuni kubwa wakati waliposikia mahubiri ya nabii mkimbizi huyu, ndiye **Yona**. **Siku ya hukumu** watasimama na kuhukumu watu walioishi wakati Yesu alipokuwa duniani, kwa sababu walikataa kupokea yule aliyekuwa **mkubwa kupita Yona**, ndiye Mwana wa Mungu mwenyewe.

**12:42** Yesu aliendelea kupasha habari za **malkia** ya Seba, mtaifa, aliyefanya safari ndefu sana toka kusini, safari ngumu iliyohitaji mali nyingi, kusemezana na Solomono. Wayuda kwa wakati wa Yesu hawakuhitaji kusafiri hata kidogo kuona Yesu. Yeye alikuwa amesafiri toka mbinguni kufikia pahali pao na kuwa Masiya-Mfalme wao, lakini hawakumpokea Yeye **anayepita Solomono sana kwa utukufu.** Malkia huyu Mtaifa atawahukumu siku ya hukumu kwa kutenda hivi.

Ndani ya sura hii tumeona kwamba Yesu ni mkubwa kupita *hekalu* (sh. 6); *Yona* (sh.41), na mkubwa kupita *Solomono* (sh.42). Yeye ni mkubwa kupita wote!

### J. Pepo mchafu anarudi (12:43-45)

**12:43,44** Halafu Yesu alionyesha kwa njia ya mfano historia ya taifa la Israeli wasioamini kwa wakati wa zamani, wa sasa na wakati wa kuja. **Mtu** huyu ni mfano wa taifa la Wayuda. **Pepo mchafu** ni mfano wa zambi ya kuabudu sanamu iliyofunga taifa hili tangu wakati walipokuwa watumwa katika Misri kufika wakati walipogeuka watumwa kwa Babeli. Waliacha kuabudu sanamu kwa wakati walipokuwa katika Babeli na ilikuwa sawasawa pepo mchafu ilikuwa **imetoka mtu**. Tangu wakati walipokuwa watumwa kwa Babeli kufika sasa Wayuda hawakuabudu sanamu. Wao ni kama nyumba iliyo **tupu, inayokwisha kufagiwa na kupambwa.**

Miaka kupita 1900 imepita tangu Mwokozi alijaribu kuingia nyumba tupu ile. Yeye tu alikuwa na ruhusa kukaa ndani yake kwani yeye tu alikuwa Bwana wa nyumba, lakini watu walizidi kukataa kumpa njia kuingia. Ndiyo, walikuwa wameacha kuabudu sanamu, lakini walikataa kuabudu Mungu wa kweli vilevile.

Nyumba **tupu** ni mfano wa roho ya mtu iliyo tupu bila Mwokozi. Haitoshi kwa mtu kutengeneza mwenendo wake tu; ni lazima apokee Mwokozi.

**12:45** Kwa wakati wa kuja, roho ya kuabudu sanamu atarudia nyumba ile, **pamoja na pepo wengine saba, waovu kuliko** yeye mwenyewe. Hesabu hii

*saba* inasema juu ya ukamilifu au utimilifu, hivi tunafikiri huu ndio mfano wa kuongezeka na kuzidi kabisa kwa kuabudu sanamu. Unatazamia wakati wa Mateso, saa taifa lililokwisha kuacha Mungu watakapoabudu mpinga Kristo. Kuinama mbele ya mtu yule wa kuasi ni namna ya kuabudu sanamu mbaya kupita yote tangu zamani. Hivi **hali ya mwisho ya mtu huyu ni mbaya kupita ya kwanza.** Waisraeli wasioamini watateswa sana na hukumu za kuogofya za Mateso Makubwa na taabu yao itapita sana maumivu yao katika Babeli. Sehemu ya Israeli walioabudu sanamu itaharibiwa kabisa wakati Kristo atakapokuja mara ya pili.

**"Ndivyo itakavyokuwa kwa kizazi kibaya hiki."** Taifa lile lililokufuru Kristo wakati Mwana wa Mungu alipokuja mara ya kwanza litateswa na hukumu kali sana wakati atakapokuja mara ya pili.

### K. Mama na ndugu za Yesu (12:46-50)

Mashairi haya yanapasha habari za kufika kwa mama na ndugu za Yesu kusemezana naye. Walifika kwa sababu gani? Ndani ya Marko 3:21, 31-35 tunaona ya kwamba wengine wa rafiki za Yesu walifikiri amepotewa akili, na walitaka jamaa yake kumwondosha kule bila kelele. Ona vile Yoane 7:5. Wakati Yesu alipoambiwa kwamba **mama na ndugu zake walikuwa inje na walitaka kusemezana naye,** aliuliza, **"Nani aliye mama yangu na ndugu zangu?"** Halafu akigeuka kwa **wanafunzi wake,** alisema, **"Mtu ye yote atakayefanya mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni, yeye ni ndugu yangu, na ndugu yangu mke, na mama yangu."**

Tangazo hili lina maana kubwa. Linaonyesha kwamba kuanza saa ile Yesu aligeuza namna alivyotendea Israeli. Maria na wana wake walikuwa mfano wa Israeli, jamaa ya Yesu kwa njia ya damu. Kufika wakati ule utumishi wake ulikuwa zaidi kwa kondoo wapotevu wa nyumba ya Israeli. Lakini ilikuwa imeonekana wazi kwamba watu wake hawatampokea. Kwa pahali pa kunyenyekea Masiya yao, Wafarisayo walimshitaki kusema alitawaliwa na Shetani.

Hivi sasa ndani ya sura hii tunaona Yesu akitangaza kawaida mpya. Ndiyo, atakaa kusihi watu wa Israeli na roho ya huruma kurudi kwa Mungu, lakini kuanza sasa atageuka kwa Mataifa vilevile, kwani watu wa inchi yake mwenyewe walimkataa. Wayuda *na* Mataifa, kama wakitii Mungu wataweza kufika karibu naye kwa kupata wokovu.

Mbele ya kuacha mashairi haya tuone maneno mawili juu ya mama ya Yesu. Tunasoma ya kwamba hakuwa na heshima kupita watu wengine ambao aliwapa njia kufika karibu naye.

Na vilevile mashairi haya yanakana mafundisho ya watu kwamba Maria alikuwa bikira daima. Wana wake walikuwa pamoja naye, ndio ndugu za Bwana wetu kwa njia ya mama yao. Soma mashairi haya: Zab. 69:8; Mt. 13:55; Mk. 3:31,32; 6:3; Yn. 7:3,5; Mdo. 1:14; 1 Kor. 9:5; Gal. 1:19.

## 8. MFALME ANATANGAZA MWANZO WA UFALME WA NAMNA NYINGINE, KWA WAKATI TU, KWA SABABU YA KUKATALIKA NA ISRAELI (Sura 13)

### Mifano ya Ufalme

Tumefikia wakati wa mabadiliko katika Habari Njema ya Matayo. Bwana alikuwa ameonyesha kwamba kuanza sasa ataweka roho zaidi juu ya hali ya *roho* ya mtu. Neno kubwa si tena kama mtu alizaliwa Myuda kwa njia ya damu ya mwili, lakini kama amechagua kutii

Mungu, Baba. Kwa njia ya kukataa Mfalme waandishi na Wafarisayo walikataa ufalme. Sasa kwa njia ya mifano Bwana Yesu alionyesha kwa ufupi kama ufalme utakuwa namna gani kwa muda unaofuata kukataliwa kwa Yesu, na wakati wa mwisho saa atakapofunuliwa kama Mfalme wa wafalme na Bwana wa wabwana. Sita ya mifano hii inaanza na masemo haya: "Ufalme wa Mungu umefanana …"

Tujikumbushe kwanza maneno tuliyoona ndani ya sura 3 ya Matayo. Mungu anatawala katika ufalme wa mbinguni. Neno hili linaonekana kwa njia mbili. (1) Watu wengine wanaonyesha kwa kinywa, kwa ku*onekana* tu, kwamba wanakubali utawala wa Mungu; na (2) watu wengine wana*ingia* ufalme kwa njia ya kuzaliwa tena. Ufalme wa Mungu unaonekana kwa muda tano: (1) unabii juu yake katika Agano la Kale; (2) "umekaribia," maana Mfalme alikuwa palepale; (3) kwa muda wakati watu wake wanapomfuata nyuma ya kukataliwa kwa Mfalme duniani na kurudi kwake mbinguni; (4) kuonekana kwa ufalme wakati wa utawala kwa miaka elfu moja; na (5) ufalme wa mwisho, wa milele. Kila shairi ndani ya Biblia linalosema juu ya ufalme ni ndani ya mmoja wa nyakati hizi. Ndani ya sura 13 tunasoma juu ya muda wa tatu, ndio muda wa waamini wa kweli tangu Pentekote kufika saa Bwana Yesu atakaporudi tena kuwapeleka mbinguni (ndilo kanisa). Lakini ufalme na kanisa si neno moja kwa njia nyingine.

Basi tuendelee kusema juu ya mifano hii.

### A. Mfano wa mpandaji mbegu (13:1-9)

**13:1 Yesu akatoka nyumbani** pahali alipoponyesha mwenye pepo mchafu, **akaketi kando ya bahari** ya Galilaya. Walimu wengine wanaona nyumba kama mfano wa taifa la Israeli, na bahari kama mfano wa Mataifa. Hivi kuhama kwake kando ya bahari ni mfano wa kugeuka kwa Bwana toka Israeli; kwa muda huu ufalme utahubiriwa kwa mataifa.

**13:2** Kwa sababu **makutano makubwa walikusanyika kwa pwani aliingia ndani ya chombo** kufundisha watu kwa njia ya **mifano**. Mfano ndio habari zenye maana na mafundisho kusaidia roho na mwenendo wa watu. Mifano ambayo tutasoma habari zao sasa inatujulisha juu ya ufalme kwa muda toka kuja kwa Bwana mara ya kwanza na kuja kwake mara ya pili.

Mifano mine ya kwanza ilikuwa kwa makutano; mifano mitatu ya mwisho ilikuwa kwa wanafunzi tu. Bwana alieleza maana ya mifano miwili ya kwanza na mfano wa mwisho kwa wanafunzi wake na aliacha wanafunzi (na sisi) kutambua maana ya ile mingine wao wenyewe.

**13:3** Mfano wa kwanza ni juu ya mpandaji aliyepanda mbegu ndani ya namna ine za udongo. Mavuno hayakuwa sawasawa kila mara.

**13:4-8**

1. Mbegu zilizoanguka njiani kwa **udongo mgumu** zilikuliwa na ndege.
2. Mbegu zilizoanguka pahali udongo nusu tu ulifunika mawe ziliota mbio bila kuwa na misingi; basi mapando **yalichomwa na jua na kukauka.**
3. Nyingine zilianguka kwa udongo uliokuwa na **miiba**, nazo hazikuweza kuota vizuri kwa sababu ya **miiba.**
4. Nyingine zilianguka juu ya **udongo mzuri**. Mbegu hizi ziliota vizuri na kukomea na **kuzaa matunda, nyingine mia, nyingine makumi sita, na nyingine makumi tatu.**

**13:9** Yesu alimaliza habari za mfano huu na agizo hili, **"Mwenye masikio asikie!"** Mfano huu ulikuwa na habari kubwa kwa makutano, na habari nyingine

kwa wanafunzi. Waweke roho sana juu ya maana ya masemo yake.

Bwana yeye mwenyewe alieleza maana ya mfano huu nyuma, ndani ya mashairi 18-23.

**B. Kusudi la mifano (13:10-17)**

**13:10** Wanafunzi walifazaika kwa sababu gani Bwana **alisema** na watu kwa njia ya **mifano**, wakamwomba kuwaelezea kusudi lake.

**13:11** Ndani ya jibu lake, Bwana aligawa watu kwa mafungu mawili. Zaidi ya Waisraeli walikuwa wakimkataa hata kama neno hili halikutimia kufika saa aliposulibishwa. Watu hawa hawatakuwa na ruhusa kufahamu **siri za ufalme wa mbinguni**, lakini wanafunzi wake wa kweli watasaidiwa kuzifahamu.

Siri ndani ya Agano Jipya ni neno watu wasilojua mpaka lilipofunuliwa na Mungu. **Siri za ufalme** zilikuwa maneno ya kweli juu ya ufalme yasiyojulikana mpaka muda ule ulioanza nyuma ya kurudi kwa Bwana mbinguni. Ndiyo, kufika wakati ule habari ya kwamba kutakuwa na ufalme kwa muda wa kuja hazikujulikana.

**13:12** Kwa nini Bwana alificha siri hizi kwa makutano na alizifunua kwa wanafunzi wake? Hili ndilo kusudi lake: **"Kwa maana mtu mwenye kitu atapewa, naye atazidishwa tele; lakini yeye asiye na kitu, ataondolewa hata kitu kile alicho nacho."** Wanafunzi walikuwa na imani, hivi kipimo cha imani yao kitaongezwa. Walikuwa wamepokea nuru, hivi wataongezewa nuru nyingine. Lakini taifa la Israeli walikuwa wamekataa Nuru ya dunia, hivi hawatapewa nuru nyingine, na watapotewa nuru ile nusu ambayo walikuwa nayo.

**13:13** Hivi tunaona kwamba watu waki*chagua* upofu wa roho, watahukumiwa kuwa wapofu. Mwalimu mmoja alisema, "Hawakupenda kweli, hivi hawakupewa nuru ya kweli." Walisema waliona, maana kwamba walijuana na kweli ya Mungu, lakini Kweli, ndiye Bwana Yesu, alisimama mbele yao, nao walikataa kabisa kumwona. Walisema walisikia Neno la Mungu, lakini Neno la Mungu mwenye uzima alisimama katikati yao na walikataa kumtii. Walikataa kufahamu kweli ya ajabu ya kwamba Mungu kwa mwili wa mtu alikuwa katikati yao, hivi uwezo wa kufahamu uliondolewa kwao.

**13:14, 15** Maisha yao yalitimiza unabii wa Isaya 6:9,10. Mioyo ya watu wa Israeli **haikuona tena vizuri** na **masikio** yao hayakutambua sauti ya Mungu. Walichagua **kukataa kuona na macho** yao. Walijua kama wakiona, kusikia, kufahamu na kutubu, Mungu atawaponyesha. Lakini walikataa kusaidiwa naye. Hivi hii ndiyo azabu yao: **watasikia** lakini **hawatafahamu**, na **wataona** bila **kutambua.**

**13:16,17** Wanafunzi walibarikiwa sana kwa sababu waliona maneno watu wasiyoona mbele. Manabii na watu wenye haki wa Agano la Kale walitaka sana kuwa hai wakati wa kuja kwa Masiya, lakini hawakupewa baraka hii. Wanafunzi walikuwa heri kuishi kwa wakati ule, kuona Masiya na maajabu aliyofanya, na kusikia mafundisho yake bora sana.

**C. Elezo la mfano wa mpandaji mbegu (13:18-23)**

**13:18** Baada ya kueleza kwa sababu gani alisema na mifano Bwana aliendelea kueleza mfano wa udongo namna ine. Hakusema wazi kama **mpandaji** mbegu alikuwa nani, lakini tunajua kwamba alisema juu yake mwenyewe (sh.37) au juu ya wale wanaohubiri habari za ufalme. Anasema mbegu ni neno la ufalme (sh.19). Udongo ndio wale wanaosikia mahubiri.

**13:19** Udongo wa nguvu karibu na njia unasema juu ya wale wanaokataa kupokea mahubiri. Wanasikia Habari Njema lakini **hawaifahamu** – si kwa sa-

babu *hawawezi*, lakini kwa sababu hawataki. Ndege ni mfano wa Shetani. **Ananyanganya** mbegu toka mioyo ya wasikiaji. Anatumika pamoja nao ndani ya njia ambayo walichagua, njia ya kutozaa matunda. Wafarisayo walikuwa wasikiaji namna hii.

**13:20, 21** Wakati Yesu aliposema juu ya pahali pa miamba alifikiri miamba iliyofunikwa na udongo nusu. Ni mfano wa watu wanaosikia na kupokea neno **na furaha.** Labda mpandaji atafurahi kuona mahubiri yake yakizaa matunda. Lakini nyuma kidogo anajifunza ya kwamba si vizuri kwa wasikiaji kupokea mahubiri na furaha nyingi. Lazima wafahamu kwanza kwamba wao ni wenye zambi, wawe na huzuni juu ya zambi zao na kuzikiri. Udongo nusu ni mfano wa mtu mwenye imani ndogo asiye na mizizi. Wakati imani yake inapopimwa na jua kali la **taabu au mateso**, anafikiri maneno haya si faida, na anaachana na kukiri na kutii Kristo.

**13:22** Udongo wenye miiba ni mfano wa watu wanaosikia na kupokea neno nusu nusu tu. Kwa wakati wanaonekana kama wafuata wazuri wa ufalme, lakini nyuma kidogo **masumbuko ya duni**a na udanganyifu wa **mali** unasonga neno na hawazai matunda. Mwandishi mmoja, jina lake Lang, anaeleza tukio hili na mfano huu:

> Mwana mmoja alisikia Neno la Mungu kwa ujana wake, lakini alivutwa kabisa na kazi ya biashara ya baba yake. Nyuma kidogo ilimpasa kuchagua kama atapendeza Bwana wake au baba yake. Hivi kulikuwa na miiba ndani ya udongo ule wakati mbegu ilipopandwa, na miiba ile iliota, ndiyo mfano wa masumbuko ya dunia na udanganyifu wa mali. Halafu mwana alinyenyekea kutaka kwa baba yake na kujitoa kwa biashara yao. Aliendelea vizuri na kugeuka kiongozi cha kazi yao. Lakini nyuma ya miaka mingi alifahamu kwamba hakuweka roho juu ya maneno ya Mungu. Alikuwa karibu kuacha kazi ya biashara na kujitoa kupita kwa kazi ya Bwana. Lakini Mungu hazihakiwi. Mtu huyu alikufa gafula nyuma ya miezi michache tu. Aliacha mali nyingi, lakini alikuwa amepoteza maisha yake bila kuzaa matunda kwa Bwana. Miiba ilikuwa imesonga neno, naye hakuzaa matunda. [3]

**13:23 Udongo mzuri** ni mfano wa mwamini wa kweli. **Anasikia neno** na kulipokea na **kulifahamu** kwa njia ya kutii maneno anayosikia. Hata kama waamini hawa hawazai wote matunda kwa kipimo kimoja, wao wote wanaonyesha kwa njia ya matunda yao kwamba wana uzima toka Mungu. Tunafikiri kwamba **matunda** hapa ni zaidi matunda ya roho (Gal. 5:22,23), si watu tunaopata kwa Kristo.Wakati tunapoona neno hili *tunda* ndani ya Agano Jipya, linasema karibu kila mara juu ya matunda ya Roho.

Mfano huu ulionya makutano juu ya hatari ya kusikia Neno la Mungu bila kulitii. Ulikuwa maonyo kwa watu kupokea Neno na roho ya kweli, na kuhakikisha neno hili kwa njia ya kuzaa matunda kwa Mungu. Na ulitayarisha wanafunzi wa wakati ule na wakati wa kuja wasilegee rohoni kama watu wachache tu wa wale wanaosikia mahubiri yao wakiokolewa kweli. Unawazuiza wasidanganywe kufikiri kwamba dunia nzima itaokolewa kwa njia ya kuenea kwa Habari Njema. Kuna maonyo vilevile kwa wafuata waaminifu wa Bwana wakae na ange kwa adui watatu wa Habari Njema: (1) Shetani (ndege – yule mwovu); (2) mwili (ukali wa kuchoma kwa jua – taabu au mateso); na (3) dunia (miiba – masumbuko ya dunia na mapendo ya mali).

Mwishoni alionyeshea wanafunzi wake faida kubwa sana ya kujitoa kusaidia roho za watu. Makumi tatu ni faida ya 3000%; makumi sita ni 6000%,

na mia moja ni 10.000%. Ndiyo, haiwezekani kupima kipimo cha matunda ya maisha ya mtu mmoja anayeokolewa. Mwalimu wa watoto wa école du dimanche asiyejulikana alidumu kufundisha mtoto mmoja, jina lake Dwight L. Moody, na kumfikisha kwa Mwokozi. Moody aliendelea katika imani, na kwa mahubiri yake watu wengi waliamini Kristo. Na waamini wale walileta watu wengi wengine karibu na Mwokozi. Mwalimu mmoja wa école du dimanche alianza kazi hii kubwa isiyokwisha kamwe!

### D. Mfano wa magugu katikati ya ngano (13:24-30)

Mfano wa udongo namna ine ulionyesha wazi kwamba watu wengine ndani ya ufalme wa mbinguni ni waamini wanaoheshimu mfalme kwa midomo tu, na wengine, wale wa namna ya ine ya udongo, ni wafuata wa kweli.

**13:24-26** Mfano wa pili, ule wa magugu na ngano, unaonyesha ufalme kwa njia hizi mbili vilevile. Ngano ni waamini wa kweli. Magugu ni watu wanaokiri na midomo tu kwamba wao ni watu wa Mungu. Yesu alisawanisha ufalme na **mtu aliyepanda mbegu njema ndani ya shamba lake; lakini wakati watu walipolala usingizi, adui yake alikuja na kupanda magugu katikati ya ngano.** Mwalimu mmoja, jina lake Unger, anasema magugu haya ni majani ya sumu yanayoonekana kama ngano saa yanapoota pamoja na ngano. Kwa wakati wa kukomea tu yanajulikana kuwa majani ya sumu na inakuwa nyepesi kuyatenga na ngano. [4]

**13:27, 28** Wakati **watumishi** walipoona magugu katikati ya ngano waliuliza mwenye nyumba kama neno hili liliwezekana namna gani. Mwenye nyumba alifahamu mara moja kwamba ilikuwa kazi ya **adui**. **Watumishi** walikuwa tayari kuondosha magugu mara moja.

**13:29, 30 Lakini** mwenye shamba aliwaagiza kungoja kwanza **kufika wakati wa mavuno**. Saa ile wavunaji watatenga ngano na magugu.Watakusanya ngano na kuiweka kwa gala ya mwenye shamba, na watachoma magugu.

Kwa nini mwenye shamba aliagiza watumishi kungoja kwanza? Kwa sababu mashina ya ngano na magugu yanafungana pamoja udongoni hata ni nguvu sana kuondosha magugu bila kuondosha ngano vilevile.

Bwana alieleza maana ya mfano huu ndani ya mashairi 37-43.

### E. Mfano wa mbegu ya haradali (13:31,32)

Mwokozi aliendelea kusawanisha **ufalme** na **mbegu ya haradali** aliyosema ni ndogo kupita **mbegu** zote ambazo wasikiaji walijuana nazo. Wakati mtu alipopanda moja ya mbegu hizi, iliota na kugeuka **mti** mkubwa sana hata ndege ziliweza kupanga katika matawi yake.

Mbegu hii ni mfano wa ufalme uliokuwa kidogo sana kwa mwanzo wake. Saa ile ulikuwa safi kwa sababu ya mateso ya adui. Lakini nyuma ya wakati ulikubaliwa na kusaidiwa na serikali na halafu uliongezeka sana. Halafu ndege za anga zilikuja na kupanga ndani yake. Neno linalotumiwa hapa kwa ndege ndilo lile tuliloona ndani ya shairi 4. Yesu alieleza kwamba ndege hawa ni mfano wa yule mwovu (sh.19). Ufalme uligeuka pahali pa kupanga kwa Shetani na watumishi wake. Kwa wakati wa sasa dini nyingine ambazo zinaitwa na jina la Kristo, lakini zinazokana kwamba yeye ni Mungu, zinachanganyana ndani yake.

Hivi Bwana alionya wanafunzi wake mbele ya kwamba wakati asipokuwa pamoja nao, ukubwa wa ufalme utaongezeka sana. Haifai wadanganywe na neno hili na kufikiri ni baraka ya Mungu. Hata kama mbegu ile ndogo ya haradali

iliota kuwa mti mkubwa, mti huu ulikuwa "makao ya mashetani na boma la kila pepo mchafu, na boma la kila ndege mchafu mwenye kuchukiza" (Ufu. 18:2).

**F. Mfano wa chachu (13:33)**

Halafu Bwana Yesu alisawanisha **ufalme na chachu ambayo mwanamke alitwaa na kuificha ndani ya vipimo vitatu vya unga hata ukachachwa wote**. Watu wanasema kwamba unga ni mfano wa dunia na chachu ni mfano wa Habari Njema itakayohubiriwa pahali pote duniani mpaka wakati watu wote wanapookolewa. Maelezo haya hayapatani na Maandiko Matakatifu, wala na historia, wala na matukio ya wakati wa sasa.

Chachu ni mfano wa uovu kila mara ndani ya Biblia. Watu walifahamu neno hili wakati Mungu alipowaagiza kuondosha chachu ndani ya nyumba zao (Kut. 12:15). Mtu akikula chakula chenye chachu ndani ya muda wa siku ya kwanza kufika siku ya saba ya Siku Kubwa ya Mkate Usiotiwa Chachu, aliondoshwa katika Israeli. Yesu alisema na wasikiaji kukaa na ange kwa chachu ya Wafarisayo na Wasadukayo (Mt. 16:6,12), na chachu ya Herode (Mk. 8:15). Ndani ya 1 Wakorinto 5:6-8 chachu inaitwa uovu na ubaya, na kwa Wagalatia 5:9 maana yake ni mafundisho mabaya. Hivi tunaona kwamba chachu ni mfano wa mafundisho au mwenendo mbaya.

Hivi ndani ya mfano huu Bwana aliwaonya juu ya kuenea kwa uovu ndani ya **ufalme wa mbinguni.** Mfano wa mbegu ya haradali unaonyesha kuonekana kwa *inje* kwa uovu wa ufalme; mfano huu wa chachu unaonyesha kuoza ambako kutaenea *ndani* ya ufalme.

Tunaamini ya kwamba ndani ya mfano huu **ung**a inasema juu ya chakula cha watu wa Mungu kinachopatikana ndani ya Biblia. **Chachu** ni mafundisho mabaya. **Mwanamke** ndiye nabii mke wa uwongo anayefundisha na kudanganya (Ufu. 2:20). Tunaona ya kwamba ndani ya miaka inayopita dini za uwongo zilianzwa tena na tena na wanawake. Wanawake wanakatazwa kufundisha ndani ya kanisa (1 Kor. 14:34; 1 Tim. 2:12), lakini wengine wanaasi agizo hili na wanachanganya chakula cha watu wa Mungu na mafundisho yasiyopatana na mafundisho ya Biblia.

**G. Yesu alitimiza unabii wakati alipotumika na mifano (13:34, 35)**

Yesu alisema mifano mine ya kwanza kwa **makutano.** Kutumika na namna hii ya mafundisho kulitimiza unabii wa Asafu ndani ya Zaburi 78:2, ya kwamba Masiya atasema kwa njia ya **mezali** mafumbo yaliyokuwa **siri tangu misingi ya dunia.** Maneno haya yaliyofichwa mbele yalionyeshwa wazi sasa.

**H. Elezo la mfano wa magugu (13:36-43)**

**13:36** Bwana alisema maneno yaliyobaki ya hotuba yake kwa wanafunzi wake, **nyumbani.** Labda **wanafunzi** hapa ni mfano wa baki lenye imani la taifa la Israeli. Kusoma juu ya nyumba tena kunatukumbusha kwamba Mungu hakukataa kwa milele watu wake ambao aliwajua tangu zamani (Rom. 11:2).

**13:37** Wakati Yesu alipoeleza mfano huu alisema yeye mwenyewe ni mpandaji mbegu. Alipanda mbegu sana wakati alipokuwa hapa duniani na anakaa kufanya hivi hata sasa kwa njia ya watumishi wake.

**13:38** Shamba ndilo dunia. Tufahamu vizuri ya kwamba shamba *si kanisa,* lakini dunia. **Mbegu njema** ni **wana wa ufalme.** Labda ni wazo la kuchekesha kufikiri juu ya watu wenye uzima wakipandwa ndani ya udongo. Lakini wazo hili ni ya kwamba wana hawa wa ufalme walipandwa duniani. Wakati wa utumishi wake duniani Bwana Yesu ali-

panda duniani wanafunzi wake waaminifu wa ufalme. **Magugu ni wana wa yule mwovu**. Shetani ana mwigo kwa kila neno la kweli la Mungu. Anapanda duniani wale wanaoonekana, na kusema, na kufanana, na wanafunzi kwa njia ya mwenendo wao. Lakini hawako wafuata wa kweli wa Mfalme.

**13:39** Adui ni Shetani, ndiye adui ya Mungu na ya watu wote wa Mungu. **Mavuno ni mwisho wa dunia,** ndio mwisho wa muda wakati Yesu Kristo atakaporudi na uwezo na utukufu, kutawala kama Mfalme. Bwana hasemi hapa juu ya mwisho wa muda wa kanisa. Kuingiza kanisa hapa kunatia wasiwasi tu kwa nia za watu.

**13:40-42** Wavunaji ndio malaika (ona Ufu. 14:14-20). Kwa muda wa sasa wa ufalme, ngano na magugu hayatengwi, lakini yanaota pamoja. Lakini wakati Kristo atakapokuja mara ya pili, malaika watakusanya vitu vyote vinavyokwaza, nao wanaotenda uovu na **kuwatupa ndani ya tanuru ya moto,** pahali watakapolia na kusaga meno.

**13:43** Wenye haki wa ufalme walio duniani kwa wakati wa Mateso makubwa wataingia **ufalme wa Baba yao** kufurahi na **kungaa kama jua** katika utawala wa Kristo wa miaka elfu moja. Halafu Yesu alisema tena, **"Mwenye masikio ya kusikia, asikie!"**

Watu wengine wanaanguka na kufikiri mfano huu unawapa njia kuleta ruhusa kwa wasioamini kukaa ndani ya kanisa la Wakristo kwa pahali fulani. Sharti tukumbuke kwamba shamba ndilo dunia, si kanisa. Makanisa ya pahali fulani yanaagizwa kuondosha katikati yao wenye kutenda zambi fulani (1 Kor. 5:9-13. Mfano huu unafundisha kwamba kwa wakati wa siri kutakuwa na waamini wa kweli ndani ya ufalme pamoja na miigo, kufika mwisho wa muda huu. Kisha watumishi wa Mungu wataweka mbali wale wasio waamini wa kweli kwa kuhukumiwa, na wale wanaobaki watafurahi ndani ya utawala wa utukufu wa Kristo duniani.

### I. Mfano wa hazina inayofichwa (13:44)

Mifano yote tuliyosoma kufika sasa ilionyesha kwamba kutakuwa na uzuri na ubaya, watu wema na wabaya ndani ya ufalme. Mifano miwili inayofuata inaonyesha kwamba kutakuwa na wenye haki namna mbili: (1) Wayuda walio waamini kwa muda wa mbele na nyuma ya Kanisa; (2) Wayuda waamini na waamini wa Mataifa kwa muda wa sasa.

Ndani ya mfano wa **hazina** Yesu anasawanisha **ufalme** na **hazina inayofichwa ndani ya shamba**. **Mtu** anaona hazina hii, anaifunika, kisha na furaha kubwa **anauza vyote alivyo navyo na kununua shamba lile.**

Tunafikiri **mtu** ndani ya mfano huu ni Bwana Yesu mwenyewe. (Yeye alikuwa mtu ndani ya mfano wa ngano na magugu, sh.37.) **Hazina** ni mfano wa baki la Wayuda waamini kwa wakati wa utumishi wa Yesu duniani na nyuma ya kwenda kwa kanisa mbinguni (ona Zab. 135:4 pahali Israeli linapoitwa mali yake mwenyewe). Wanafichwa shambani, maana wanasambazwa duniani na hawajulikani ila kwa Mungu mwenyewe. Yesu alivumbua hazina hii, kisha alikwenda msalabani na kujitoa mzima kwa kununua dunia (2 Kor. 5:19; 1 Yn. 2:2) pahali hazina inapofichwa. Waisraeli wakombolewa wataondoshwa katika pahali walipofichwa wakati Mwokozi atakapotoka Sayuni na kusimamisha Ufalme wake kama Masiya.

Mara nyingine watu wanasema mashairi haya ni mfano wa mwenye zambi akiacha vyote kwa kupata hazina kubwa zaidi, ndiyo Kristo. Elezo hili halipatani na mafundisho ya neema, ya kwamba wokovu ni pasipo bei (Isa. 55:1; Efe. 2:8,9).

### J. Mfano wa lulu ya bei ya damani (13:45,46)

**Ufalme** unasawanishwa vilevile na **mfanya biashara anayetafuta lulu nzuri.** Wakati anapokuta lulu ya bei ya damani, anatoa vyote alivyo na anainunua. Wengine wanafikiri lulu hii ni Mwokozi. Sivyo. Tukumbuke kwamba mwenye zambi halazimishwi kuuza vyote na halazimishwi kununua Kristo.

Tunafikiri **mfanya biashara** ni Bwana Yesu mwenyewe. **Lulu ya bei kubwa** ni kanisa. Kwa Kalvari aliuza vyote kununua lulu hii. Lulu inafanywa ndani ya chaza inayoteswa na kitu kidogo, kama mbegu ya mchanga. Vivyo hivyo kanisa lilifanyika kwa njia ya kutobolewa na kuumizwa kwa mwili wa Mwokozi.

Ndani ya mfano wa hazina ufalme unasawanishwa na hazina yenyewe. Hapa ufalme hausawanishwi na lulu lakini na mfanya biashara. Sababu ya tofauti hii ni nini?

Mfano wa mbele ni zaidi juu ya hazina – ndiyo taifa la Israeli wakombolewa. Walitolewa ufalme kwanza, na kwa wakati wa kuja zaidi ya watu ndani ya ufalme watakuwa Wayuda.

Tulisema mbele ya kwamba kanisa na ufalme si neno moja. Wote walio ndani ya kanisa ni ndani ya ufalme (kwa muda wa sasa), lakini si watu wote walio ndani ya ufalme ni ndani ya kanisa. *Kanisa halitakuwa sehemu ya ufalme kwa wakati wa kuja lakini litatawala pamoja na Kristo juu ya dunia inayofanywa mpya.* Mfano wa pili ni zaidi juu ya Mfalme mwenyewe na bei kubwa sana aliyolipa kujipatia bibi arusi atakayeshiriki katika utukufu wake siku ya ufunuo wake.

Kama lulu ilivyotoka baharini, vivyo hivyo kanisa (mara nyingine linaitwa bibi arusi Mtaifa wa Kristo) linatoka zaidi katika mataifa, hata kama wengine ndani yake ni Wayuda. Ndani ya Matendo 15:14 Yakobo alionyesha kwamba hili ndilo kusudi kubwa la Mungu kwa wakati wa sasa.

### K. Mfano wa mkila (13:47-50)

**13:47,48** Ndani ya mfano wa mwisho ambao Bwana Yesu alitoa kwa wakati ule **ufalme** unasawanishwa na tunga au **mkila unaotupwa baharini na kukusanya samaki za kila namna.** Wavuvi wanatenga samaki, wanachunga samaki njema vyomboni na kutupa nyingine.

**13:49, 50** Bwana wetu alieleza mfano huu na kusema ni kwa **wakati wa mwisho**, ndio mwisho wa muda wa Mateso. Ni wakati wa Kuja kwa Pili kwa Kristo. Wavuvi ndio **malaika**. Samaki wema ni wenye haki, ndio watu waliookolewa, wa Wayuda na Mataifa. Samaki wabaya ni waovu, maana wasioamini wa mataifa yote. Wanatengwa, kama tulivyoona ndani ya mfano wa ngano na magugu (mash. 30, 39-43). Wenye haki wanaingia ufalme wa Baba yao, lakini waovu wanatupwa katika pahali pa moto kutakapokuwa **kulia na kusaga meno**. Lakini hii si hukumu ya mwisho, lakini hukumu kwa *mwanzo* wa utawala wa Kristo kwa miaka elfu moja; hukumu ya *mwisho* itakuwa kwa mwisho wa muda ule wa miaka elfu moja (Ufu. 20:7-15).

Gaebelein anaeleza mashairi haya hivi:

> Mkila unashushwa ndani ya bahari. Tuliona mbele kwamba bahari ni mfano wa mataifa. Mfano ni juu ya kuhubiri kwa habari njema ya milele kwa wakati wa Mateso Makubwa (Ufu. 14:6,7). Wenye kutenga wema na wabaya ni malaika. Maneno haya yote hayasemi juu ya wakati wa sasa wala juu ya kanisa, lakini ni kwa wakati ufalme ni karibu kusimamishwa. Ndani ya kitabu cha Ufunuo tunaona kwamba malaika watakuwa na kazi kwa wakati ule. Waovu watatupwa ndani ya tanuru ya moto, na

wenye haki watakaa duniani kwa ufalme wa miaka elfu moja. [5]

### L. Hazina ya Kweli (13:51,52)

**13:51** Nyuma ya kumaliza mafundisho ya mifano, Bwana aliuliza wanafunzi wake kama **walifahamu** maneno haya. Wakajibu, **"Ndiyo."** Labda jibu lao linatushangaza, na hata kuamsha wivu ndani ya roho zetu kwani kuna maneno mengine tusiyofahamu kwanza vizuri.

**13:52** Lakini kwa sababu wao walifahamu, iliwapasa kushiriki mafundisho haya na watu wengine. Inapasa wanafunzi kuwa mifereji ya maji ya uzima, si kuyachunga kwa wao wenyewe tu. Walikuwa wametayarishwa kwa **ufalme wa mbinguni**, maana yake walikuwa walimu na wenye kutafsiri kweli. Walikuwa kama **mwenye nyumba anayetoa katika hazina yake vitu vipya na vitu vya zamani.** Ndani ya Agano la Kale kulikuwa na hazina kubwa ya **kweli za kale.** Ndani ya mafundisho ya mifano ya Kristo walikuwa wamepokea mafundisho **mapya** kabisa, na iliwapasa sasa kupitisha kweli hii ya utukufu kwa watu wengine.

### M. Yesu anakataliwa kwa Nazareti (13:53-58)

**13:53-56** Nyuma ya **kumaliza mafundisho yake kwa njia ya mifano** hii, Yesu aliondokea pwani ya Galilaya, akakwendea Nazareti mara ya mwisho. Wakati **alipofundisha ndani ya sunagogi lao** watu **walishangaa juu ya hekima yake** na habari za maajabu yake. Watu wa Nazareti walimjua kama **mwana wa seremala** tu. Walijua **mama yake alikuwa Maria … na ndugu zake Yakobo na Yosefu na Simoni na Yuda … na ndugu zake wanawake** – walikuwa pale Nazareti hata saa ile. Waliuliza namna gani mtu wa mji wao aliweza kufanya maneno ya namna hii? Hawakujaribu kufahamu lakini walifungana na ujinga wao.

**13:57, 58 Wakachukizwa naye.** Neno hili lilisukuma **Yesu** kusema ya kwamba **nabii** hakosi kupata heshima ila katika inchi yake mwenyewe. Kutokuamini kwa watu wa Nazareti kulizuiza kazi ya Mwokozi naye aliponyesha watu wachache tu pale (ona Marko 6:5). Si kwa sababu *hakuweza* kuponyesha watu pale; uovu wa watu hauwezi kuzuiza uwezo wa Mungu. Lakini kwa njia ya kazi hii angalileta baraka kwa watu wasiotaka kubarikiwa, na angalisaidia watu wasiofahamu kwamba walikuwa na hitaji, na kuponyesha watu ambao hawakutaka kusikia kwamba walikuwa na ugonjwa.

## 9. NEEMA YA MASIYA HAIPUNGUKI, LAKINI UADUI WA WATU UNAONGEZEKA (14:1–16:12)

### A. Yoane Mbatizaji anakatiwa kichwa 14:1-12

**14:1, 2 Herode mfalme** alisikia habari za utumishi wa Yesu. Herode huyu alikuwa mwana wa Herode Mkuu na aliitwa vilevile Herode Antipa. Ni yeye aliyeagiza Yoane Mbatizaji kuuawa. Wakati aliposikia habari za maajabu yaliyofanywa na Yesu, zamiri yake ilianza kumchokoza. Alisema na watumishi wake kwamba "Huyu ni **Yoane** Mbatizaji; amefufuka **toka wafu,** na kwa hivi nguvu hizi zinatenda kazi ndani yake."

**14:3** Ndani ya mashairi 3-12 Matayo anarudi kuonyesha habari na sababu ya kufa kwa Yoane.

**14:4, 5** Herode alikuwa ameacha mke wake na alikuwa akikaa katika uzini pamoja na **Herodia, mke wa ndugu yake Filipo.** Yoane, akiwa nabii wa Mungu, hakuweza kuona neno hili bure. Na hasira na uhodari alihamakia Herode juu ya uovu wake.

Mfalme alikasirika sana sana na alitaka kumwua, lakini aliogopa kwa sa-

babu watu waliona Yoane **kuwa nabii**, na uuaji wake uliweza kuamsha machafuko katikati yao. Hivi alituliza gazabu yake kwa wakati, kwa njia ya kufunga Yoane gerezani.

**14:6-11** Siku ya ukumbusho wa kuzaliwa kwa Herode, binti ya Herodia, alicheza mbele ya watu na kupendeza mfalme sana, hata mfalme aliahidi kumpa kitu cho chote alichotaka. Mama wake mwovu alimsukuma kuomba kupewa **kichwa cha Yoane Mbatizaji … juu ya sahani!** Kwa wakati ule gazabu ya Herode juu ya Yoane ilikuwa imepunguka; labda rohoni mwake alimheshimu kwa haki na uhodari wake. Alihuzunishwa juu ya kitu msichana alichoomba, lakini alifikiri ni lazima kwake kutimiza ahadi yake, na Yoane **alikatiwa kichwa.**

**14:12** Wanafunzi wa Yoane walikuja kuchukua **maiti** yake na kuizika na heshima; **wakakwenda kumwambia Yesu.** Hakuna pahali pazuri kupita wangaliweza kwenda na huzuni yao, nao ni mfano mzuri kwa sisi wakati sisi tunapoteswa na kupata maumivu na huzuni – tupeleke mizigo yetu yote kwake (1 Pet. 5:7).

Lakini Herode alikaa kukumbuka tendo hili ovu, na wakati aliposikia juu ya maajabu ya Yesu, habari za Yoane Mbatizaji zilirudi kumchokoza.

### B. Kukulishwa kwa watu elfu tano (14:13-21)

**14:13,14 Wakati Yesu aliposikia** ya kwamba habari za maajabu yake zilisumbusha Herode, aliingia **chombo na kwenda** kwa pahali pasipo watu karibu na bahari ya Galilaya. Tunajua hakufanya hivi kwa sababu ya woga; alijua hakuna neno ambalo liliweza kumpata mbele ya kutimia kwa wakati wake. Labda sababu moja ilikuwa kwa wanafunzi wake waliorudi sasa tu toka safari yao ya kuhubiri, saa kwa kupumzika. Ona Marko 6:30; Luka 9:10.

Lakini makutano toka miji walimfuata **wakitembea na miguu**. Walikuwa pale pale wakati alipotoka chombo. Neno hili halikuchokoza Bwana wetu mwenye huruma, akaanza mara moja **kuponyesha wagonjwa wao.**

**14:15** Wakati **mangaribi** ilipokuja, **wanafunzi wake** walianza kusumbuka na kuogopa matata itatokea. Watu walikuwa wengi sana nao walikosa chakula. Hivi waliomba Bwana kuruhusu makutano waende kwa **vijiji** kujinunulia **chakula**. Hawakujuana kwanza na roho ya Kristo wala kutambua uwezo wake!

**14:16-18** Bwana alijibu kusema kwamba watu hawakuhitaji kuondoka. Kwa nini watamwondokea yeye anayefungua mkono wake kusaidia mahitaji ya kila kiumbe? Halafu aliwashitusha kabisa wakati aliposema, **"Ninyi muwape chakula."** Wao walishe makutano haya makubwa? Walikuwa na **mikate mitano na samaki mbili tu.** Walisahau kwamba walikuwa na Yesu vilevile. Na roho ya upole Mwokozi alisema nao, **"Muzilete kwangu."** Hii ilikuwa kazi yao.

**14:19-21** Waza juu ya Bwana akisema na **makutano kuketi katika majani**. **Alitwaa mikate mitano na samaki mbili**, alileta asante, **alivunja** mikate na **kuwapa wanafunzi** kugawa kwa watu. Kulikuwa na chakula cha kutosha kwa watu wote. Na wakati watu **wote** walipokwisha kushiba, wanafunzi waliokota vipande vilivyobaki na kujaza **vitunga kumi na viwili.** Kulibaki chakula kupita kile Bwana alichokuwa nacho kwa mwanzo. Ndiyo, kulikuwa na kitunga kimoja kwa kila mwanafunzi aliyekosa imani. Na watu wengi sana walikuwa wamelishwa, labda 10.000 au 15.000 (wanaume 5000 pamoja na wanawake na watoto).

Ajabu hili lina mafundisho kwa wanafunzi wa kila wakati. Makutano wenye njaa wanatuzunguka wakati wote. Na kwa kila wakati kuna watumishi wa-

chache wa Mungu wasio na vitu vya kutosha kuwasaidia ndani ya kazi yao. Na Mwokozi mwenye huruma ni pale wakati wote. Wakati wanafunzi ni tayari kumpa vyote walivyo navyo, hata ni vidogo sana, anavizidisha kulisha elfu za watu. Tofauti ndiyo hii: **Wanaume wale elfu tano** waliokulishwa kwa Galilaya walishibishwa kwa wakati mfupi tu; wale wanaoshibisha njaa ya roho yao na Kristo aliye hai wanashibishwa kwa milele (ona Yn. 6:35).

### C. Yesu anatembea juu ya bahari (14:22-33)

Ajabu la kulisha watu elfu tano liliaminisha wanafunzi ya kwamba Yule ambaye walimfuata aliweza kuwapa vyote walivyohitaji. Sasa walijifunza ya kwamba aliweza kuwachunga na kuwapa uwezo vilevile.

**14:22, 23** Wakati **Yesu** alipokuwa **akiagana** na makutano, aliagiza **wanafunzi** wake **kuingia chombo** na **kwenda ngambo** ya bahari. Kisha alipanda kilima kuomba na **alikuwa peke yake** wakati usiku ulipoingia.

**14:24-27 Chombo kilikuwa katikati ya bahari sasa,** na upepo ulivuma na kuwataabisha. Yesu aliona hatari yao, na **kwa zamu ya ine ya usiku** (katikati ya saa tisa na saa kumi na mbili ya usiku) **alifika karibu nao akitembea juu ya bahari**. Wanafunzi waliogopa sana wakifikiri alikuwa **pepo**, lakini Yesu alisema nao mara moja, **"Muwe na furaha; ni mimi; musiogope."**

Mara nyingi ni vivyo hivyo ndani ya maisha yetu. Tunafazaishwa na kutaabishwa na kukosa tumaini. Ni kama Bwana ni mbali sana. Lakini saa hii yote anatuombea. Wakati ni kama mambo yote ni giza, yeye ni karibu. Hata saa hii mara nyingi hatumtambui na tunashindwa na woga kabisa. Halafu tunasikia sauti yake ikitufariji, na tunakumbuka ya kwamba hata mawimbi ambayo yalituogopesha sana ni chini ya miguu yake.

**14:28** Wakati **Petro** aliposikia sauti ile ambayo alijua na kupenda sana, roho yake ilifurika na mapendo na alisema, **"Bwana, ikiwa wewe, uniamuru nifike kwako juu ya maji."** Masemo haya yanaonyesha kwamba aliamini Bwana kabisa. Petro alifahamu kwamba pamoja na kutoa agizo, Bwana Yesu anatoa vilevile uwezo kutii agizo hili.

**14:29-33** Mara moja wakati Yesu aliposema, **"Kuja," … Petro** alitoka chomboni, akaanza kwenda kufika karibu naye. Wakati alipoweka macho yake juu ya Yesu, aliweza kufanya neno lisilowezekana kwa watu, lakini mara moja wakati alipoanza kufikiri juu ya **upepo** alianza kuzama, akalalamika na woga mkubwa, **"Bwana, uniponyeshe."** Bwana alinyolosha mkono wake, akamshika, akamhamakia na huruma juu ya **udogo** wa **imani yake,** akamfikisha kwa chombo. **Upepo ulikoma** mara moja wakati Yesu alipoingia chombo. Wanafunzi waliokuwa chomboni wakashangaa sana na kumwabudu wakisema: **"Kweli wewe ni Mwana wa Mungu."**

Maisha ya Mkristo ni kama kutembea juu ya maji, ndiyo neno lisilowezekana kwa watu. Yanawezekana kwa uwezo wa Roho Mtakatifu tu. Tungali tunaondosha macho yetu juu ya mambo yote mengine na kuyaweka juu ya Yesu tu (Ebr.12:2), tunaweza kuishi maisha yasiyowezekana kwa watu wa dunia. Lakini dakika tunapoanza kujifikiri wenyewe na maneno yetu, tunaanza kuzama. Halafu inatupasa kusihi Kristo kuturudisha karibu naye na kutuwezesha tena kwa kazi yake.

### D. Yesu anaponyesha wagonjwa kwa Genezareti (14:34-36)

Chombo kilifikia **Genezareti**, kwa upande wa kaskazini-mangaribi wa bahari ya Galilaya. Wakati watu walipoona Yesu, wakatuma habari katika inchi yote

kandokando, wakaleta kwake **wote waliokuwa na magonjwa ili waguse pindo la vazi lake tu; na wote ambao waliligusa waliponyeshwa.** Hivi waganga wa inchi ile waliweza kupumzika kwa wakati; watu wote walikuwa wamepona kwa sababu ya kufika kwa Mganga Mkubwa!

**E. Uchafu toka ndani (15:1-20)**

Ndani ya sura za kwanza za Habari Njema yake Matayo maandiko yake hayafuatani kwa namna yalivyotokea. Lakini kuanza na sura 14 hata kufika mwisho wa Habari Njema yake yanafuatana kwa utaratibu.

Ndani ya sura 15 tunasoma kwanza juu ya Wafarisayo na waandishi wakigombana, na mabishano yao (mash. 1-20). Maneno haya yalitazamia kukataliwa kwa Masiya na taifa la Israeli. Nyuma yake tunasoma juu ya imani ya mwanamke Mkanana (mash. 21-28), ndio mfano wa Habari Njema ikihubiriwa kwa Mataifa kwa muda wa sasa. Na mwishoni habari za makutano makubwa wakiponyeshwa (mash. 29-31) na watu 4000 wakikulishwa (mash. 32-39) zinatazamia muda wa kuja wa utawala wa miaka elfu moja wakati watu wote watakapokuwa wenye afya na watasitawi.

**15:1,2 Waandishi na Wafarisayo** waliendelea kujaribu kutega Mwokozi. Walituma wengine **toka Yerusalema** na kushitaki **wanafunzi** wake juu ya uchafu kwa sababu walikula chakula **bila kunawa kwanza mikono** yao. Wakikosa kufanya hivi waliasi **desturi ya wazee.**

Kwa kufahamu tukio hili vizuri, sharti tufahamu maana ya masemo ya Wafarisayo juu ya kunawa. Katika Agano la Kale kunawa kulikuwa sehemu ya kawaida ya kuabudu. Kwa mfano, mtu akigusa maiti, au akikula chakula fulani, hakuwa safi, maana hakustahili kuabudu Mungu. Mbele ya kuweza kukaribia Mungu tena, ilimpasa kusafishwa kwa njia ya kutii kawaida fulani.

Lakini wazee walikuwa wameongeza maagizo mengine juu ya namna gani kusafishwa. Kwa mfano, walisema ya kwamba mbele ya kula chakula ilikuwa lazima kwa Myuda kunawa mikono hata kisigino cha mkono. Kama alitoka sokoni ilimpasa kuoga mwili mzima. Hivi Wafarisayo walishitaki wanafunzi kwa sababu hawakutimiza maagizo haya madogo yote ya desturi za wazee.

**15:3-6** Bwana Yesu aliwakumbusha kwamba *wao* walikuwa wakiasi **amri ya Mungu**, si **desturi ya wazee** tu. Sheria ya Mungu iliagiza watu **kuheshimu** wazazi wao, pamoja na kuwasaidia na mali kama ikihitajiwa, lakini waandishi na Wafarisayo (na watu wengi wengine) hawakutoa mali kusaidia wazazi wao wazee. Hivi walitayarisha njia kuepuka hitaji la kufanya hivi. Wakati **baba au mama** walipowaomba kuwasaidia, walihitaji kusema maneno kama haya tu: "Mali yo yote ambayo ninayo na ningaliweza kutoa kukusaidia imetolewa **kwa Mungu**, hivi siwezi kukusaidia nayo." Nyuma ya kusema hivi kwa upotovu hawakuhitaji kusaidia wazazi wao tena, hata kama Neno **la Mungu** liliwaagiza kufanya hivi.

**15:7-9** Kwa njia ya masemo yao ya udanganyifu walitimiza unabii wa **Isaya** 29:13. Waliheshimu Mungu **na midomo yao, lakini mioyo yao ilikuwa mbali naye**. Kuabudu kwao kulikuwa bure kwa sababu waliheshimu na kuweka desturi zao mbele ya Neno la Mungu.

**15:10,11** Akiita **makutano** kwake, Yesu alitangaza neno kubwa sana. Alisema **si kitu kinachoingia kinywani kinachofanyiza mtu mchafu, lakini kitu kinachotoka**. Ni nguvu kwa sisi kutambua ukubwa wa maana ya tangazo hili. Ndani ya kitabu cha Walawi Wayuda walifundishwa ya kwamba vitu vingine vilivyoingia kinywani *vilifanyiza mtu mchafu.* Wayuda walikatazwa kula nyama ye yote asiyecheua na ku-

gauwa kwato. Walikatazwa kula samaki waliokosa mapezi na magamba. Mungu alitoa mafundisho mengi kuonyesha vyakula gani ni vichafu.

Tena sasa Yeye aliyetoa sheria alitayarisha njia kwa kuondoshwa kwa kawaida hii yote ya uchafu kwa maneno ya dini. Alisema vyakula wanafunzi walivyokula bila kunawa mikono havikuwachafua. Lakini udanganyifu wa moyo wa waandishi na Wafarisayo ulichafua watu wale kabisa.

**15:12-14** Wakati **wanafunzi wa Yesu** walipofika na habari ya kwamba **Wafarisayo walichukizwa** na mashitaki haya, Yesu aliwasawanisha na mbegu zisizopandwa na Mungu. Walikuwa magugu, si ngano. Mwishoni wao na mafundisho yao yataondoshwa, maana yake wataharibiwa. Halafu aliongeza, **"Muwaache; wao ni viongozi vipofu wa vipofu."** Walisema walikuwa wenye amri kwa maneno ya roho, lakini walikuwa **vipofu** kwa maneno ya Mungu, na watu ambao waliongoza walikuwa vipofu vilevile, nao wote **wataanguka ndani ya shimo.**

**15:15** Bila shaka wanafunzi walishangaa wakati waliposikia Bwana Yesu akigeuza maneno yote ambayo walijifunza mbele juu ya vyakula vilivyokuwa safi au vichafu. Habari hizi zilikuwa kama **mfano** kwao, na Petro alimwomba kuzieleza.

**15:16, 17** Kwanza Bwana alishangaa kwa sababu walikuwa hawajafahamu maneno haya bado. Halafu aliendelea kueleza kwamba uchafu wa hakika ni uchafu wa roho, si wa mwili. Chakula watu wanachokula si safi au kichafu. Hakuna kitu kilicho safi au kichafu; ni namna tunavyotumika nacho iliyo vibaya. Chakula **kinachoingia kinywa cha mtu kinapita kwa tumbo** lake, na sehemu yake isiyo na faida kwa mwili wake **kinatupwa** kwa choo. Chakula kina kazi kwa mwili tu na hakigusi hali ya roho. Leo tunajua kwamba "kila kiumbe cha Mungu ni kizuri, wala hakuna cha kukataliwa kama kikipokewa kwa asante; kwa sababu hivi kimetakaswa kwa Neno la Mungu na kwa kuomba" (1 Tim. 4:4,5). Ndiyo, mashairi haya si juu ya mapando yenye sumu, lakini juu ya mapando Mungu aliyotayarisha kuwa vyakula vya watu. Haya yote ni mema na tunaweza kuyakula pamoja na kushukuru.

**15:18** Basi kama vyakula visivyotuchafua, **ndivyo** nini vilivyo vichafu? Yesu alijibu, **"… vitu vinavyotoka kinywani mwa mtu vinatoka moyoni; navyo vinafanyiza mtu mchafu." Moyo** hapa si kiungo kinachotembeza damu mwilini mwetu, lakini tabia ya mtu inayoonekana kwa njia ya mawazo, masemo na matendo machafu.

**15:19, 20** Maneno mengine yanayochafua mtu ndiyo **mawazo mabaya, uuaji, uasherati, uzini, wizi, ushuhuda wa uwongo, matukano** (maana ya neno hili kwa Kiyunani ni kusema masemo maovu juu ya watu wengine vilevile).

Wafarisayo na waandishi waliweka roho sana juu ya kutii kawaida ya kunawa mikono, lakini roho zao zilichafuwa kabisa na hawakuweka roho juu ya maneno ya haki yaliyo ya faida. Walishitaki wanafunzi kwa sababu hawakutii desturi za wazee zisiyoagizwa na Mungu. Lakini hawakuogopa kufanya shauri kuua Mwana wa Mungu, pamoja na kutenda zambi zote zinazotajwa ndani ya shairi 19.

### F. Mtaifa anabarikiwa kwa sababu ya imani yake (15:21-28)

**15:21, 22 Yesu** aliondokea pahali pale, **akakwenda kando pande za Tiro na Sidona,** kwa pwani ya Bahari ya Méditerranée. Ni kama hii ni mara ya pekee kwa muda wa utumishi wake katikati ya watu Bwana alipokuwa inje ya inchi ya Wayuda. Hapa kwa inchi ya Foinike, mwanamke wa Kanana ali-

mwomba kuponyesha **binti** yake mwenye **pepo mchafu.**

Inatupasa kufahamu kwamba mwanamke huyu hakuwa Myuda, lakini Mtaifa. Alikuwa mzazi wa Wakanana, taifa ovu ambao Mungu alikusudi kuharibu, lakini kwa sababu ya uasi wa Waisraeli wengine wa Wakanana walipona wakati Waisraeli walipokamata inchi ya Kanana, wakiongozwa na Yosua. Akiwa Mtaifa, hakubarikiwa kama watu wachaguliwa wa Mungu hapa duniani. Alikuwa mgeni, bila tumaini kwa Mungu wala Masiya yake.

Mwanamke aliita Yesu **Bwana, Mwana wa Daudi,** kama Wayuda walivyofanya wakati waliposema juu ya Masiya. Hata kama Yesu *alikuwa kweli* **Mwana wa Daudi,** neno hili halikumpa mtu wa Mataifa ruhusa kumkaribia. Kwa sababu hii Bwana hakumjibu mara moja.

**15:23 Wanafunzi wake walimwomba kufukuza mwanamke huyu** kwa sababu alikuwa akipiga kelele nyuma yao. Lakini Bwana alimwona kama mfano mzuri wa imani, chombo ndani yake neema yake itaonekana wazi. Lakini kwanza Bwana alihitaji kujaribu na kupatisha imani yake nguvu.

**15:24, 25** Alikumbusha mwanamke kwamba alitumwa kwa **kondoo wapotevu wa Israeli,** si kwa Mataifa, na si kwa Wakanana. Jibu hili halikufazaisha mwanamke. Aliacha kumwita *Mwana wa Daudi,* na alimwabudu akisema, **"Bwana, unisaidie!"** Kama asipoweza kumkaribia kama Myuda anavyoweza kukaribia Masiya, aliweza kuja kama kiumbe kwa Mwumba wake.

**15:26** Akikaa kupima kuona kama mwanamke alikuwa na imani ya kweli, Yesu alisema naye kwamba **si vizuri** kwa yeye kuacha kulisha watoto wa Wayuda kwa kuweza kuleta chakula kwa **imbwa** za Mataifa. Kwa masikio yetu haya ni masemo makali, lakini kusudi lake halikuwa kumwumiza, lakini kumsaidia. *Alikuwa Mtaifa kweli* na kwa macho ya Wayuda watu wa Mataifa walikuwa kama imbwa zikizungukazunguka njia za mji zikitafuta makombo ya chakula. Lakini maana ya neno ambalo Yesu alitumika nalo hapa ni **imbwa ndogo,** ndiyo nyama rafiki. Mwanamke atakubali kweli kwamba hakustahili kupokea hata baraka ndogo toka Bwana?

**15:27** Ndiyo! Alikubali masemo yake yote. Alikubali kwamba alikuwa Mtaifa asiyestahili kupokea rehema, mapendo na neema. Ni kama alisema: "Unasema haki; mimi ni mmoja wa wale **imbwa ndogo** tu chini ya meza. Lakini ninaona kwamba mara nyingine **makombo ya chakula** yanaanguka **chini toka meza**. Utaruhusu kwa mimi kupata mengine ya makombo haya? Sistahili kwa wewe kuponyesha binti yangu, lakini ninakusihi kufanya hivi kwa mmoja wa viumbe vyako asiyestahili."

**15:28** Yesu alimsifu kwa **imani** yake **kubwa.** Watoto wale wasioamini hawakuwa na hamu kwa vyakula, lakini mwanamke huyu ambaye alijiita "imbwa ndogo" alitaka sana kuvipokea. Hakuamini bure; binti yake aliponyeshwa **mara moja**. Bwana aliponyesha binti Mtaifa huyu toka mbali. Neno hili linatufikirisha utumishi wake kwa wakati wa sasa kwa mkono wa Mungu, akileta kuponyeshwa kwa roho kwa Mataifa kwa muda huu wakati watu wake wa zamani wanapowekwa kando.

### G. Yesu anaponyesha makutano makubwa (15:29-31)

Ndani ya Marko 7:31 tunajifunza kwamba Bwana aliondokea Tiro, akasafiri kwenda kwa upande wa kaskazini hata Sidona, halafu aligeuka kwenda mashariki hata Yorodani, na kwa kusini mpaka Dekapoli. Pale, karibu na Bahari ya Galilaya, aliponyesha **vipofu, mabubu, vilema** na wengine wengi. Watu

walishangaa sana na **kutukuza Mungu wa Israeli**. Tunafikiri zaidi ya watu hawa walikuwa Mataifa waliofahamu kwamba Yesu na wanafunzi wake walikuwa Wayuda. Wakafahamu vizuri kwamba **Mungu wa Israeli** alikuwa akitumika katikati yao.

### H. Watu elfu ine wanakulishwa (15:32-39)

**15:32** Wasomaji wasioweka roho sana juu ya maneno wanayosoma wanafikiri Maandiko yanaanguka hapa na kupasha habari za kulishwa kwa watu 5000 mara ya pili. Sivyo. Habari hizi ni mbali na habari za kukulishwa kwa watu 5000 tulizosoma mbele.

Wakati **makutano** walipokwisha kushinda pamoja na Bwana kwa siku tatu, vyakula vyao vilikwisha, lakini Bwana hakuwaruhusu kwenda kwao na njaa, wasizimie **njiani.**

**15:33, 34 Wanafunzi wake** walisumbuka tena namna gani watu hawa wote waliweza kulishwa; mara hii walikuwa na mikate saba na samaki wadogo wachache.

**15:35, 36** Kama Bwana alivyofanya mbele wakati alipokulisha watu 5000 aliagiza makutano kuketi, **akashukuru Mungu, akavunja** mikate na samaki **na kuwapa wanafunzi wake kugawa** kwa watu. Bwana anataka wanafunzi wake kufanya kazi wanayoweza kufanya wao wenyewe; kisha yeye anafanya ile wasiyoweza kufanya.

**15:37-39** Wakati watu walipokwisha **kushiba, vitunga vikubwa saba vilibaki** vikijaa vyakula. **Wanaume karibu elfu ine walikulishwa, pamoja na wanawake na watoto.**

Ndani ya sura 16 (mash. 8-12) tutaona kwamba hesabu hizi ya maajabu mawili ya kulisha watu zilikuwa na maana kubwa. Nyuma ya kuruhusu makutano kwenda kwao Bwana wetu aliingia chombo kwenda kwa **Magadani**, kwa pwani ya mangaribi ya bahari ya Galilaya.

### I. Chachu ya Wafarisayo na Wasadukayo (16:1-12)

**16:1** Tangu zamani **Wafarisayo na Wasadukayo** hawakupatana hata kidogo kwa maneno ya dini, na waliamini maneno mbalimbali. Lakini sasa uadui wao kwa Bwana Yesu uliwafunga pamoja na hamu ya kujaribu kutega Mwokozi. Kwa kumjaribu **walimwomba** kuonyesha **alama toka mbingu**. Hatufahamu kusudi lao vizuri wakati walipoomba neno hili. Yesu alikuwa amefanya maajabu yake yote duniani. Ataweza kufanya maajabu mbinguni vilevile?

**16:2, 3 Aliwajibu** na masemo juu ya mbingu (anga). Wakati mbingu (anga) zilipoonekana **nyekundu mangaribi**, walitabiri kwamba itakuwa **nzuri** kesho yake. Lakini wakati mbingu (anga) **zilipoonekana nyekundu asubui**, mvua na tufani zitafuata siku ile. Walikuwa na akili nyingi kutambua kuonekana kwa mbingu, lakini iliwashinda kutambua **alama za nyakati.**[6]

**Alama** hizi zilikuwa nini? Nabii, ndiye Yoane Mbatizaji, alitangaza kwamba Masiya alikuwa amefika. Maajabu ambayo yalitabiriwa mbele kwamba Masiya atafanya – maneno yasiyofanywa na mtu ye yote mwingine – yalifanywa mbele ya macho yao. Alama nyingine ilikuwa kukataliwa kwa Masiya na Wayuda, na mwanzo wa kuhubiriwa kwa Habari Njema kwa Mataifa. Lakini maneno haya yote yaliyotokea kwelikweli yalikuwa bure kwa macho yao.

**16:4** Masiya mwenyewe alisimama katikati yao, lakini hata hivi walitaka kupewa alama. Neno hili lilionyesha kwamba walikuwa **kizazi kibaya cha uzini wa roho.** Hawatapewa alama ila **alama ya nabii Yona**. Kama ilivyoelezwa ndani ya mafundisho juu ya Matayo 12:39, alama hii ni ya kwamba

Mungu atamfufua toka wafu. Itakuwa alama ya hukumu ya wote wanaokataa kupiga magoti mbele yake aliye Mtawala wa halali.

Makutano haya ya Yesu na Wayuda hawa yalikwisha na maneno ya kuogofya: **"Akawaacha, akakwenda zake."** Ole wao wanaoachwa na Kristo!

**16:5, 6** Wakati **wanafunzi** wa Bwana walipofika karibu naye tena kwa upande wa **mashariki** wa ziwa, **walikuwa wamesahau kuchukua chakula**. Hivi wakati Yesu alipowasalimu na kusema kukaa na ange **wajichunge wenyewe kwa chachu ya Wafarisayo na Wasadukayo,** walifikiri aliwakataza wasinunue vyakula toka viongozi hawa. Walifikiri chakula cha mwili tu, si chakula cha roho.

**16:7-10** Walikaa kusumbuka juu ya ukosefu wa vyakula, hata kama Bwana aliyekulisha watu 5000 na 4000 sasa tu alikuwa pamoja nao. Hivi aliwakumbusha habari hizi tena, na tunaona kwamba wakati kulipokuwa na *mikate mitano na samaki wawili tu,* alikulisha watu 5000, na vyakula vilivyobaki vilijaza vitunga kumi na viwili. Wakati alipokulisha watu 4000 na vyakula kupita, vyakula vilivyobaki vilijaza vitunga saba tu. Tukiweka vitu na mali nusu tuliyo nayo mikononi mwake anaweza kuzidisha vyote na kufanya kazi kubwa nayo.

Mwandishi alitumika na maneno yenye maana mbalimbali kwa **'vitunga.'** Ni kama vitunga vilivyotumiwa kwa wakati wa kulisha watu 4000 vilikuwa vikubwa kuliko vile vilivyotumiwa kwa wakati wa kulisha watu 5000.[7] Si neno. Mafundisho makubwa kwa sisi hapa ni haya: Kwa nini tutasumbuka juu ya njaa na mahitaji wakati tunapoungana na Yule aliye mwenye mali na uwezo wote?

**16:11,12** Wakati Bwana aliposema juu ya **chachu ya Wafarisayo na Wasadukayo** hakusema juu ya mkate, lakini juu ya ubaya wa mafundisho na mwenendo wao. Kwa Luka 12:1 chachu iliitwa udanganyifu. Walisema walitii maagizo madogo madogo ya sheria, utii wa kuonekana mbele ya watu tu, lakini ndani ya roho zao walikuwa waovu kabisa.

Chachu cha Wasadukayo ilikuwa kufuata akili ya binadamu. Kama watu wengi kwa wakati wa sasa, walikana maneno mengi, wakisema hakuna malaika na roho, hakuna ufufuko wa mwili, hakuna maisha ya milele, na hakuna azabu ya milele. Chachu hii ya mashaka, kama isipozuizwa, itaongezeka na kuenea katikati ya watu kama chachu ndani ya unga.

## 10. MFALME ANATAYARISHA WANAFUNZI WAKE (16:13–17:27)

### A. Kukiri kwa Petro (16:13-20)

**16:13, 14 Kaisaria-Filipi** ulikuwa karibu km 40 toka bahari ya Galilaya kwa upande wa kaskazini na km 8 toka Yorodani kwa upande wa mashariki. Wakati Yesu alipofikia pande za mji huu na vijiji kando kando (ona Marko 8:27), neno moja kubwa na lenye maana kabisa lilitokea. Kufika wakati ule Bwana alikuwa akiongoza wanafunzi wake kufahamu vizuri kama yeye ni nani. Nyuma ya kumaliza kazi hii aliweka roho yake juu ya kwendea msalaba.

Alianza na kuuliza **wanafunzi wake** kama watu walifikiri yeye ni nani. Walileta majibu mbalimbali, kama **Yoane Mbatizaji, Elia, Yeremia**, au **mmoja wa manabii**. Watu walifikiri Yesu ni mmoja wao tu. Mtu mwema, lakini si mwema zaidi. Mkubwa lakini si mkubwa zaidi. Nabii mmoja lakini si Nabii aliye mkubwa kupita wote. Sifa hii haikutosha hata kidogo. Kama alikuwa mtu tu alikuwa mdanganyi kwa sababu alisema yeye ni sawa na Mungu Baba.

**16:15, 16** Halafu aliuliza wanafunzi wake kama wao walifikiri yeye ni **nani**.

**Simoni Petro** alikiri neno kubwa sana; akasema, **"Wewe ni Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai."** Ni kusema yeye ni Masiya wa Israeli na Mungu Mwana.

**16:17,18** Bwana alibariki **Simoni,** mwana wa **Yona.** Mvuvi huyu wa samaki hakufahamu neno hili kwa akili yake mwenyewe; **lilifunuliwa** kwake na Mungu **Baba**. Lakini Mwana wa Mungu alikuwa na neno kubwa kusema na Petro vilevile. Hivi Yesu aliongeza, **"Nami ninakuambia, Wewe ni Petro, na juu ya mwamba huu nitajenga kanisa langu, wala milango ya Hadeze haitalishinda."** Watu wamebishana sana juu ya maana ya shairi hili, kupita juu ya mashairi yote mengine ya Habari Njema. Wanauliza, "**Mwamba** huu ni nani, au nini?" Kwa Kiyunani maneno kwa *petro* na *mwamba* yanafanana, lakini yana maana mbalimbali. Maana ya neno la kwanza, *petros*, ni jiwe lisilofungana na udongo; maana ya neno la pili, *petra*, ni mwamba mkubwa wa nguvu. Hivi maneno Yesu aliyosema ndiyo haya: **"… wewe ni Petro** (jiwe), **na juu ya mwamba huu nitajenga kanisa langu."** Hakusema atajenga kanisa lake juu ya jiwe, lakini juu ya mwamba.

Basi kama Petro si mwamba, mwamba huu ni nini? Kama tukiangalia karibu karibu maneno yanayotangulia na kufuata mashairi haya, ni wazi kwamba mwamba ndio tendo la kukiri la Petro ya kwamba Kristo ni Mwana wa Mungu aliye hai, ndiyo kweli juu yake kanisa linajengwa. Katika Waefeso 2:20 tunajifunza kwamba kanisa linajengwa juu ya Yesu Kristo, jiwe kubwa la pembeni. Sehemu la shairi hili linasema tumejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii. Tufahamu kwamba msingi huu si mitume wenyewe. Ni msingi uliowekwa ndani ya mafundisho yao juu ya Bwana Yesu Kristo.

Kristo anaitwa Mwamba ndani ya 1 Kor. 10:4. Haya ndiyo maelezo ya mwalimu mmoja, ndiye Morgan:

> Kumbuka kwamba Yesu alikuwa akisema na Wayuda. Ndani ya Maandiko Matakatifu kwa Kiebrania neno hili *mwamba* halitumiwi kamwe kusema juu ya mtu. Kila mara linalotumiwa linasema juu ya Mungu. Hivi hapa katika Kaisaria Filipi Kanisa halijengwi juu ya Petro. Yesu alichagua vizuri maneno aliyotumika nayo ndani ya masemo yake. Alitumika na mfano wao wa zamani kwa Kiebrania, ndio mwamba, unaosema juu ya Mungu kila mara, akasema: "Juu ya Mungu mwenyewe – Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai – nitajenga kanisa langu." [8]

Petro hakusema kamwe juu yake mwenyewe kama msingi wa kanisa. Alisema mara mbili juu ya Kristo kama Jiwe (Mdo. 4:11,12; 1 Pet. 2:4-8), lakini katika mashairi yale jiwe linasema juu ya jiwe kubwa la pembeni, si juu ya msingi.

**"Nitajenga kanisa langu."** Hii ndiyo mara ya kwanza tunayosoma juu ya **kanisa** ndani ya Biblia. Kanisa halikuwa kwa wakati wa Agano la Kale. Halikuwa vilevile wakati Yesu aliposema maneno haya. Lilianzwa siku ya Pentekote, na watu wanaoamini Kristo kweli ni ndani yake, Wayuda na watu wa Mataifa. Linajulikana vilevile kama mwili na bibi arusi ya Kristo.

Tunashangaa kusoma juu ya kanisa hapa ndani ya Habari Njema ya Matayo, ndipo pahali tunaposoma zaidi juu ya Israeli na ufalme. Lakini Wayuda walikuwa wamekataa Kristo, na halafu muda wa kanisa lilianza na litaendelea kufika wakati kanisa litakapopelekwa mbinguni. Nyuma yake Mungu ataendelea kutumika na taifa la Israeli.

**"Milango ya Hadeze haitalishinda."** Tunaweza kufahamu maneno haya kwa njia mbili. Kwanza tunaweza kufikiri juu ya **milango ya Hadeze** *ikishindwa*

ndani ya vita yote kuharibu kanisa – kanisa litashinda. Au tunaweza kufikiri juu ya kanisa lenyewe likishindana na adui zake na *kuwashinda.* Hata ukikubali elezo gani, uwezo wa mauti utashindwa wakati waamini walio hai watakapopelekwa mbinguni na waamini waliokwisha kufa watakapofufuliwa.

**16:19 "Nitakupa wewe funguo za ufalme"** si kusema kwamba Petro atakuwa na amri kuruhusu watu kuingia mbinguni. Maneno haya ni juu ya **ufalme wa mbinguni** *duniani,* ndiyo watu wote wanaokiri kuwa wenye kutii Mfalme, wote wanaokiri kuwa Wakristo. **Funguo** zinatufikirisha njia ya kuingia. Tunafikiri hapa ni funguo zinazotajwa kwa Mt 28:19 – kufanya wanafunzi, ubatizo na mafundisho. (Ubatizo haukuhitajiwa kwa wokovu lakini kwa njia ya kubatizwa watu wanakiri wazi mbele ya watu wengine kwamba wao ni wafuata wa Mfalme.) Petro alitumika na funguo hizi mara ya kwanza kwa Pentekote. Si Petro tu aliyepewa funguo hizi, lakini alizipokea kama wakili wa wanafunzi wote. (Ona Matayo 18:18 pahali wao wote walipopewa ahadi hii.)

**"Lo lote utakalofunga duniani litafungwa mbinguni; na lo lote utakalofungua duniani, litafunguliwa mbinguni."** Watu wengine wanatumika na shairi hili na shairi lingine namna hii, ndilo Yoane 20:23, kufundisha ya kwamba Petro na wale ambao walimkomboa nyuma ya mauti yake walipewa amri kusamehe zambi. Tunajua neno hili si kweli; kwani Mungu tu anaweza kusamehe zambi.

Kuna njia mbili kufahamu shairi hili. Labda mitume walipewa uwezo kufunga na kufungua ambao sisi hatukuwa nao wakati wa sasa. Kwa mfano Petro alifunga zambi za Anania na Safira juu yao na waliazibiwa na mauti palepale (Mdo. 5:1-10), lakini Paulo alifungua mtu aliyehukumiwa, toka matunda ya zambi zake wakati alipokwisha kutubu (2 Kor. 2:10).

Au labda maana yake ni ya kwamba mitume walifunga au kufungua duniani yaliyokwisha kufungwa au kufunguliwa mbele mbinguni. Kama mwalimu Ryrie anavyosema, "Maneno yote ya kufunga na kufungua yanafanywa mbele mbinguni, si na mitume, lakini ni mitume ambao wanajulisha watu maneno haya."

Maana ya pekee ya shairi hili kwa wakati wa sasa ni ya kwamba mtu akiamini Kristo kweli na kumpokea kuwa Bwana na Mwokozi wake, Mkristo anaweza *kutangaza* kwamba zambi zake zimesamehewa. Na wakati mtu anapokataa kupokea Mwokozi, Mkristo anaweza kusema kwamba zambi zake hazisamehewi.

**16:20** Halafu Bwana Yesu aliagiza **wanafunzi wake** tena **wasimwambie mtu** ya kwamba yeye ni Masiya. Kwa sababu ya kutokuamini kwa Israeli kujulisha watu neno hili saa ile kungaliweza kusukuma watu kujaribu kumfanyiza mfalme mbele ya wakati uliowekwa na Mungu, na Waroma wangalihukumu machafuko namna hii na ukali mkubwa.

### B. Matayarisho ya wanafunzi kwa mauti na ufufuko wa Kristo (16:21-23)

**16:21** Wanafunzi walikuwa wamefahamu sasa kwamba Yesu ni Masiya, Mwana wa Mungu aliye hai, na walikuwa tayari kusikia tangazo la kwanza la mauti na ufufuko wake. Walijua makusudi yake yatatimizwa, na kwamba walikuwa pamoja na Mshindaji. Hivi walikuwa tayari kwa tangazo la Bwana ya kuwa **imempasa kwenda Yerusalema,** na **kupata mateso mengi** kwa wazee na wakubwa wa makuhani na waandishi na **kuuawa, na kufufuliwa siku ya tatu.**

**16:22** Petro alikuwa na uchungu wakati alipofikiri juu ya Bwana wake

akitendewa mabaya haya. Alianza kumkemea, **"Iwe mbali nawe, Bwana; neno hili halitatokea juu yako kamwe!"**

**16:23** Lakini Bwana Yesu alimkemea juu ya masemo haya. Alikuwa amefikia duniani kusudi afe kwa wenye zambi. Neno lo lote ambalo lilimzuiza asitimize kusudi hili halikupatana na kutaka kwa Mungu. Hivi alisema na Petro, **"Kwenda nyuma yangu, Shetani; kwani wewe ni jiwe la kukwaza kwangu, kwani huwazi maneno yaliyo ya Mungu, lakini maneno yaliyo ya watu."** Wakati Yesu alipoita Petro **Shetani**, hakutaka kusema Petro alikaaliwa au kutawaliwa na Shetani. Maana ya maneno haya ndiyo kwamba Shetani angaliweza kusema maneno namna hii. Kwa njia ya masemo yake Petro aligeuka kizuizo kwa Mwokozi.

Kila Mkristo anaitwa kuchukua msalaba wake na kufuata Bwana Yesu, lakini wakati tunapokutana na msalaba, tunasikia sauti ndogo ndani ya roho zetu ikisema, "Iwe mbali nawe! Ujiokoe mwenyewe." Au labda ndugu zetu wapenzi wanajaribu kutuzuiza tusitii Bwana. Kwa wakati namna hii inatupasa sisi vilevile kusema, "Kwenda nyuma yangu, Shetani, kwani wewe ni jiwe la kukwaza kwangu."

### C. Matayarisho kwa kuwa mfuasi wa kweli (16:24-28)

**16:24** Sasa Bwana Yesu alionyesha wazi maana ya kuwa mfuasi wake: ni kujikataa mwenyewe, kubeba msalaba, na kumfuata. **Kujikataa** mwenyewe ni mbali na kujikana mwenyewe. Ni kujitoa kabisa kutawaliwa na Bwana bila kubaki na ruhusa yo yote sisi wenyewe. **Kuchukua msalaba** ni kuwa tayari kubeba haya, maumivu, hata mauti kwa ajili ya Bwana; ni kujihesabu mfu kwa kwa kujipendeza, zambi, na dunia. **Kumfuata** ni kuishi namna yeye alivyoishi, ndiyo maisha ya unyenyekevu, umasikini, huruma, mapendo, neema na matendo mema yote mengine.

**16:25** Bwana alijua kwamba kutakuwa na mazuizo kwa watu wasijitoe mzima kumfuata na kutawaliwa naye. Neno la kwanza ndilo hili: Tunajaribiwa **kuepuka** masumbuko, maumivu, upekee au hasara. Neno la pili ndilo utajiri. Juu ya neno la kwanza Yesu anaonya wale wanaoishi kwa faida yao wenyewe ya kwamba roho zao hazitajuana na utimilifu kamwe, lakini wale wanaojitoa mzima kwa Bwana, watafahamu kwamba haya ndiyo maisha ya faida kabisa.

**16:26** Jaribu la pili, ndilo kujivimbisha mali, ni upumbavu. Yesu alisema, "Fikiri ya kwamba **mtu** anaendelea vizuri sana ndani ya kazi yake hata **dunia nzima** inageuka mali yake. Kazi hii ya upumbavu itamaliza saa na nguvu yake yote na hatatimiza kusudi kubwa la maisha yake. Ni faida gani kujipatia mali ile yote, kisha kufa na kuiacha yote duniani na kushinda milele na mikono bure?" Mtu ni hapa duniani kwa kazi kubwa kupita kazi ya kujivimbishia mali. Anaitwa kusimamia maneno ya Mfalme wake. Kama asipotimiza neno hili anapoteza faida yote ya maisha yake.

**16:27** Sasa Bwana anakumbusha watu wake kwamba **utukufu** unafuata mateso. Anatazama mbele kwa wakati atakapokuja duniani mara ya pili **pamoja na malaika,** na katika **utukufu wa kupita wote wa Baba yake. Saa ile atatoa zawabu** kwa wale walioishi kwa yeye. Kama tukitaka kuwa na maisha ya faida, sharti tutazamie wakati ule wa kuja, na kufahamu mambo gani yatakuwa ya faida zaidi kwa wakati ule, kisha kuweka roho kabisa kuishi kwa mambo yale.

**16:28** Halafu alifanya tangazo la kushitusha sana. Alisema **wengine waliosimama** pale pamoja naye **hawatakufa** mbele ya kumwona **akikuja**

**katika ufalme wake**. Basi wanafunzi wale wote wamekufa, lakini Kristo hajakuja kwanza katika uwezo na utukufu kusimamisha ufalme wake. Mashairi 1-8 ya sura 17 yatatusaidia kufahamu tangazo hili. Yanapasha habari za maneno yaliyotokea juu ya mlima wakati Bwana alipogeuzwa sura, na Petro, Yakobo na Yoane walipoweza kuona Kristo katika utukufu wa ufalme wake hata mbele ya wakati neno hili litakapotokea.

Tunaweza kufikiri juu ya kugeuzwa sura ya Kristo kama mfano wa ufalme wake kwa wakati wa kuja. Petro aliandika juu yake kama "uwezo na kuja kwa Bwana wetu Yesu Kristo" (2 Pet. 1:16). Uwezo na kuja kwa Bwana Yesu zinasema juu ya kuja kwake mara ya pili. Na Yoane aliandika juu ya tukio hili mlimani wakati aliposema "… tukatazama utukufu, utukufu kama wa Mwana pekee akitoka kwa Baba" (Yn. 1:14). Kristo alikuja mara ya kwanza katika aibu; atakuja mara ya pili katika utukufu. Hivi tangazo juu ya mlima lilitimizwa; Petro, Yakobo na Yoane waliona Mwana wa watu, si kama mtu mnyenyekevu wa Nazareti, lakini kama Mfalme mtukufu.

### D. Matayarisho ya wanafunzi kwa utukufu: Bwana anageuzwa sura (17:1-8)

**17:1,2** **Siku sita** nyuma ya tukio kwa Kaisaria Filipi, **Yesu alipeleka Petro, Yakobo na Yoane kwa mlima mrefu** katika Galilaya. Luka alisema ilikuwa nyuma ya "karibu siku nane" (Lk 9:28). Alihesabu siku iliyotangulia na siku iliyofuata tukio hili.

Ni kama Petro, Yakobo na Yoane walikuwa karibu na Mwokozi kupita wanafunzi wengine, na walipewa heshima ya kuona kugeuzwa kwa sura yake. Kufika wakati ule utukufu wake ulifichwa ndani ya mwili wa binadamu. Lakini sasa **uso wake** na **mavazi yake** yalingaa **kama jua,** na kuonyesha uungu wake, kama wingu la utukufu (Shekina) katika Agano la Kale lililokuwa mfano ya kwamba Mungu alikuwa pale. Maneno haya yalionyesha mbele kama itakuwa namna gani wakati Bwana Yesu atakaporudi kusimamisha ufalme wake. Saa ile hataonekana tena kama Mwana-Kondoo ya zabihu, lakini kama Simba ya kabila la Yuda. Wote ambao watamwona watamtambua mara moja kama Mungu Mwana, Mfalme wa wafalme na Bwana wa wabwana.

**17:3** Musa na Elia walitokea juu ya mlima na kusemezana juu ya mauti yake iliyokaribia kwa Yerusalema (Lk 9:30, 31). Labda Musa na Elia ni mifano ya watakatifu wa Agano la Kale. Au tunaweza kufikiri juu ya Musa kama mfano wa Sheria, na Elia kama mfano wa Manabii; hivi tunaweza kuona sehemu hizi mbili za Agano la Kale zikitazama mbele kwa mateso ya Kristo na utukufu utakaofuata. Au tunaweza kufikiri kwamba Musa, aliyekwenda mbinguni kwa njia ya mauti, ni mfano wa wote ambao watafufuliwa toka wafu kuingia muda wa utawala wa Kristo kwa miaka elfu moja; lakini Elia aliyepelekwa mbinguni bila kufa, ni mfano wa wale watakaofikia ufalme bila kufa.

Labda wanafunzi, Petro, Yakobo na Yoane ni mfano wa watakatifu wa Agano Jipya. Au wao ni mfano wa baki aminifu la Wayuda watakaokuwa hai wakati wa kuja kwa Kristo mara ya pili, na kuingia ufalme pamoja naye.

Makutano kwa upande wa chini wa mlima (sh.14, sawanisha na Luka 9:37) yamesawanishwa na Mataifa watakaoshiriki ndani ya baraka za utawala wa Kristo kwa miaka elfu moja.

**17:4,5** Roho ya **Petro** iliamshwa kabisa na tukio hili. Akitaka kuzuiza utukufu huu usiondoke, alisema bila kufikiri, kwamba ingekuwa vizuri asimamishe **hema tatu** – **moja kwa Yesu, moja kwa Musa na moja kwa Elia.** Ilikuwa vizuri kwa yeye kuweka Yesu

kwa pahali pa kwanza, lakini alianguka kwa sababu hakumweka juu kupita wale wengine. Yesu hakuwa sawasawa na Musa na Elia, lakini yeye ni Bwana wa wote. Kwa kuwafundisha neno hili, Mungu Baba aliwafunika wote na **wingu** lililongaa, akatangaza, **"Huyu ni Mwana wangu, mpendwa wangu, ambaye ninapendezwa naye; sikieni yeye."** Katika Ufalme, Kristo atakuwa juu ya wote, Mfalme mwenye amri kwa maneno yote. Angepasa kuwa hivi ndani ya mioyo ya wafuata wake kwa wakati wa sasa vilevile.

**17:6-8 Wanafunzi** walishitushwa kabisa wakati waliposikia sauti ile, **wakaanguka kifudifudi**. Lakini Yesu alisema nao wasimame na **wasiogope.** Wakati waliposimama **hawakuona mtu ila Yesu peke yake**. Itakuwa vivyo hivyo katika Ufalme – Bwana Yesu atatukuzwa kupita yote pale.

**E. Juu ya mtangulizi (17:9-13)**

**17:9** Wakati walipokuwa **wakishuka mlima, Yesu aliamuru wanafunz**i wasiseme neno juu ya tukio hili kufika wakati **atakapofufuka toka wafu.** Wayuda walitaka sana kuponyeshwa toka utawala wa Roma na wangalipokea Yesu kuwaokoa toka *Roma*, lakini hawakutaka awe Mwokozi wao toka *zambi*. Walikuwa wamekataa Masiya yao, na haikuwa faida kuwaambia habari za ono hili la utukufu wa Masiya. Nyuma ya ufufuko wake habari hizi zitatangazwa pahali pote duniani.

**17:10-13** Wanafunzi walikuwa wamepewa sasa tu ono la Kristo akikuja na uwezo na utukufu kwa wakati wa kuja. Lakini mtangulizi wake alikuwa hajatokea bado. Malaki alikuwa ametabiri mbele ya kwamba **inapasa Elia kuja kwanza** (Mal. 4:5, 6). Hivi **wanafunzi waliuliza** Yesu juu ya neno hili. Bwana alikubali kwamba **ilipasa Elia kuja kwanza** kutengeneza maneno, lakini alieleza kwamba **Elia alikuwa amefika**. Alikuwa akisema juu ya **Yoane Mbatizaji** (ona sh.13). Yoane hakuwa Elia (Yn.1:21), lakini alikuja kama "mwenye roho na nguvu za Elia" (Lk. 1:17). Kama Israeli wangalipokea Yoane na mahubiri yake, angalitimiza maneno yaliyotabiriwa juu ya Elia (Mt. 11:14). Lakini taifa la Israeli hawakutambua maana kubwa ya kazi ya Yoane, wakamtendea namna waliyotaka. Mauti ya Yoane yalionyesha namna watakavyotendea Mwana wa watu. Walikataa mtangulizi, watakataa Mfalme vilevile. Wakati Yesu alipoeleza neno hili, wanafunzi walifahamu kwamba alikuwa akisema juu ya **Yoane Mbatizaji.**

Ni kama kweli mbele ya kuja kwa Kristo mara ya pili kutakuwa na nabii mmoja atakayetayarisha Israeli kwa Mfalme atakayekuja. Hatuwezi kujua sasa kama atakuwa Elia yeye mwenyewe au mtu mwingine mwenye utumishi namna yake.

**F. Matayarisho kwa utumishi kwa njia ya maombi na kufunga (17:14-21)**

Maisha yetu si furaha siku zote. Nyuma ya saa ndogo za ushirika mtamu pamoja na Bwana na kufurahishwa sana rohoni zinafuata saa na siku za masumbuko na kazi nyingi, na inatupasa kuondokea pahali pale pa baraka na kurudi tena kukutana na mahitaji ya watu.

**17:14,15** Wakati walipokwisha kushuka mlima, baba mmoja mwenye kusumbuka sana aliwangoja. **Alipiga magoti mbele yake** na kumsihi sana kusaidia mtoto wake aliyeteswa sana na pepo mchafu. Mwana huyu aliteswa na **kifafa** na mara nyingine ugonjwa huu ulimtupa ndani ya **moto na mara nyingi ulimwangusha ndani ya maji**. Alikuwa mfano wa namna Shetani anavyotesa watu na ukali sana.

**17:16** Baba wa mtoto alikuwa amefikia wanafunzi kupata kusaidia, lakini hawakuweza kusaidia mtoto.

**17:17 "Ee kizazi kisichoamini na kikaidi, nitakaa nanyi hata wakati gani? Nitachukuliana nanyi hata wakati gani?"** Bwana Yesu alisema maneno haya na wanafunzi. Hawakuwa na imani kuponyesha mtoto mwenye kifafa. Walikuwa sawasawa na Wayuda wengi kwa wakati ule, wakaidi na bila imani.

**17:18** Wakati walipoleta mwenye kifafa karibu na Yesu, **Yesu alihamakia pepo, mgonjwa aliponyeshwa** mara moja.

**17:19,20 Wanafunz**i walifazaika kwa sababu gani walikosa uwezo kuponyesha mtoto, wakauliza Yesu juu ya neno hili. Aliwajibu na neno moja tu: **kutokuamini.** Kama wangalikuwa na **imani** hata ndogo, **kipimo cha mbegu ya haradali** (mbegu ndogo zaidi), wangaliweza kuagiza **mlima** kutupwa baharini na neno hili litafanyikana. Lakini inatupasa kufahamu ya kwamba sharti msingi wa imani ya kweli uwe agizo au ahadi ya Mungu, si kutaka kwetu kufanya tendo la kushangaza watu tu, tendo la kiburi. Lakini kama Mungu akiongoza mwamini kwa njia fulani au kumwagiza kufanya neno fulani, Mkristo huyu anaweza kuamini kabisa ya kwamba hata mambo makubwa na magumu yataondoshwa kwa njia ya ajabu. Hakuna neno lisilowezekana kwa wenye imani.

**17:21 "Namna hii haiwezi kutoka isipokuwa kwa kuomba na kufunga."** Shairi hili linakosa ndani ya matafsiri ya Biblia kwa lugha nyingine kwa wakati wa sasa, lakini ni ndani ya mengi ya maandiko ya zamani.

### G. Wanafunzi wanatayarishwa kwa uhaini wa Mwokozi (17:22, 23)

Tena, bila mshindo wa matarumbeta, Bwana Yesu alipasha wanafunzi wake kwamba atauawa. Lakini tena aliongeza ya kwamba **siku ya tatu atafufuliwa.** Kama asipowaambia habari za mauti yake mbele kama bila shaka wangalifazaishwa kupita kipimo siku ya kuuawa kwake. Hawakufikiri Masiya wao atakufa na haya na maumivu.

Walihuzunishwa sana kwa sababu atawaondokea na kwa sababu atauawa. Walisikia habari hizi wakati alipowaambia maneno haya, lakini ni kama hawakusikia ahadi yake ya kwamba atafufuliwa tena.

### H. Petro na Bwana wake wanalipa kodi (17:24-27)

**17:24, 25** Katika **Kapernaumu** watoza **kodi kwa hekalu** waliuliza Petro kama **Mwalimu** wake alilipa nusu ya shekeli kwa mahitaji na kazi ya hekalu. Petro alijibu, "**Analipa**." Labda hakutaka Bwana wake kupata haya.

Maneno yaliyotokea wakati Petro aliporudi nyumbani yanaonyesha kwamba Bwana anajua maneno yote. Wakati Petro asipopata njia bado kusema neno, Yesu **alimwuliza: "Unafikiri nini, Simoni? Wafalme wa dunia wanatwaa kodi au ushuru kwa watu gani? kwa wana wao au kwa wageni?"** Inapasa kufahamu ulizo hili kwa njia ya kufahamu desturi za wakati ule. Mtawala alilipiza watu wa inchi yake kodi kusaidia kazi ya ufalme wake na mahitaji ya jamaa yake mwenyewe. Hakulipiza watu wa jamaa yake kodi. Kwa wakati wa sasa serikali inalipiza watu wote kodi, hata mtawala na jamaa yake.

**17:26** Petro alijibu vizuri kusema watawala walilipiza **wageni** kodi. Halafu Yesu alionyesha kwamba **wana ni huru**. Basi hekalu lilikuwa nyumba ya Mungu. Kwa Yesu, Mwana wa Mungu, kulipa kodi kusaidia hekalu hili kungekuwa kujilipia mwenyewe kodi.

**17:27** Lakini Yesu hakutaka kuchukiza watu bure, hivi alikubali kulipa kodi. Lakini atapata mali yenyewe

wapi? Hatusomi hata mara moja kwamba Yesu alibeba mali yeye mwenyewe. Alituma Petro kwa **bahari** ya Galilaya na kutwaa samaki ya kwanza iliyokuja. Ndani ya kinywa cha samaki ile atapata **shekeli** moja – mali ya kutosha kwa kulipa kodi kwa Petro na kwa yeye mwenyewe.

Ajabu hili lilionyesha wazi ya kwamba Kristo alijua maneno yote. Alijua samaki gani ya samaki zote baharini ilikuwa na shekeli ndani ya kinywa chake, pahali samaki hii ilipokuwa, na ya kwamba itakuwa samaki ya kwanza Petro atakayopata.

Yesu alilipa kodi hii kwa sababu hakutaka kuumiza roho za watu. Sisi waamini si chini ya sheria tena, lakini tukumbuke zamiri za watu wengine, na tusifanye neno ambalo litawakwalisha.

## 11. MFALME ANAFUNDISHA WANAFUNZI WAKE (Sura 18–20)

### A. Juu ya unyenyekevu (18:1-6)

Sura 18 imeitwa hotuba juu ya ukubwa na usamehe. Inaonyesha namna gani inapasa wafuata wa Kristo Mfalme kutenda.

**18:1** Wanafunzi walifikiri kwamba ufalme wa mbinguni ni muda wa salama na usitawi. Sasa walitamani kuwa na mahali pa heshima ndani yake. Roho hii ya kujitafutia faida na heshima iliwasukuma kuuliza, **"Nani basi aliye mkubwa katika ufalme wa mbinguni?"**

**18:2, 3** Yesu alijibu ulizo lao kwa njia ya kuweka **mtoto mdogo** katikati yao, na kusema ya kwamba inapasa watu **kugeuka kuwa kama watoto wadogo kuingia ufalme wa mbinguni.** Alikuwa akisema juu ya ufalme rohoni mwetu; ya kuwa inapasa mwamini wa kweli kuacha kujitafutia ukubwa, na kwamba sharti akamate pahali pa unyenyekevu kama mtoto mdogo. Inampasa kukiri zambi zake na kutokustahili kwake na kupokea Kristo, ndiye tumaini lake la pekee. Sharti mwamini awe na roho namna hii hata mwisho wa maisha yake. Yesu hakuonyesha kwamba wanafunzi wake hawakuzaliwa tena. Wao wote, ila Yuda, walikuwa na imani ya kweli na walikuwa wamehesabiwa haki. Lakini walikuwa hawayakaliwa na Roho Mtakatifu, hivi walikosa uwezo kuwa na *unyenyekevu* wa kweli, uwezo sisi watu wa sasa tulio nao (lakini tusiotumia namna inavyopasa). Na vilevile ilipasa wageuke, maana iliwapasa kugeuza mawazo yao yasiyo taratibu yapatane na ufalme.

**18:4** Mtu mkubwa zaidi katika ufalme wa mbinguni ndiye **anayejinyenyekeza kama mtoto mdogo**. Ni wazi ya kwamba kawaida na damani ya ufalme ni mbalimbali kabisa na zile za dunia. Ni lazima kwetu kugeuza kabisa namna tunavyofikiri kupatana na mawazo ya Kristo (ona Flp. 2:5-8).

**18:5** Hapa Bwana aligeuka toka mtoto wa mwili kusema juu ya mtoto wa **roho**. Mtu ye yote akipokea mmoja wa wanafunzi wake wanyenyekevu **kwa jina lake** ni kama alipokea Bwana mwenyewe; zawabu yenyewe itakuwa sawasawa. Kitu cho chote tunachotenda kwa mwanafunzi wa Yesu tunafanya kwa Bwana wake.

**18:6** Lakini ye yote anayeshawishi mwamini kufanya zambi anajipatia hukumu kubwa sana. **Inafaa afungiwe shingoni jiwe kubwa la kusagia, apate kuzama** kilindini mwa bahari. (Jiwe kubwa la kusagia linalotajwa hapa lilihitaji nyama kulizungusha; mtu aliweza kuzungusha jiwe dogo na mkono). Ni vibaya kujikosea mwenyewe; ni vibaya zaidi kuingiza mwamini mwingine ndani ya zambi na kuharibu usafi wake, kuchafua nia yake na kuharibu heshima yake. Ingekuwa vizuri kuuawa wewe

mwenyewe kupita kuharibu usafi na utawa wa mtu mwingine!

**B. Juu ya mambo ya kukosesha (18:7-14)**

**18:7** Yesu aliendelea kueleza ya kwamba bila shaka **mambo ya kukosesha** yatafika. **Dunia**, mwili, na Shetani wanafungana pamoja kushawishi na kuangusha watu. Lakini kama mtu akigeuka mwenye kuendesha mambo maovu yale, atakuwa na hatia kubwa. Hivi Mwokozi alionya watu kujihukumu wenyewe na ukali, ili wasikwalishe mtoto mwingine wa Mungu.

**18:8, 9 Mkono** au **mguu** au **jicho** likikukosesha, vizuri kujitaabisha na kuondosha viungo hivi kupita kuviacha kuharibu kazi ya Mungu ndani ya maisha ya mtu mwingine. Ni **afazali kuingia katika uzima** bila viungo vingine au bila uwezo kuona, kuliko kuwa na mikono au miguu miwili kutupwa katika moto wa milele. Bwana wetu hakusema ya kwamba kutakuwa na miili mingine mbinguni bila viungo vingine, lakini alisema juu ya hali ya mwili wa mwamini wakati anapoondokea uzima wa sasa na kuingia ule wa nyuma. Bila shaka mwili wa ufufuko utakuwa mtimilifu na mkamilifu.

**18:10** Halafu Mwana wa Mungu alitoa maonyo wasizarau **mmoja wa wale wadogo,** au watoto au mtu ye yote wa ufalme wa Mungu. Kuonyesha ukubwa wa maonyo haya aliongeza ya kwamba mbinguni **malaika zao** ni siku zote mbele ya Mungu, wakitazama **uso** wake. Tunafikiri **malaika** hawa ni malaika walinzi (ona vilevile Ebr. 1:14).

**18:11** Shairi hili linakosa ndani ya tafsiri nyingine lakini linajumlisha vizuri mafundisho ya mashairi ambayo yanalitangulia.

**18:12, 13** Mchungaji mwenye huruma analinda na kuokoa wadogo hawa vile vile. Kama hata mmoja wa kondoo mia moja akipotea, anaacha kondoo 99 na anatafuta kondoo yule mmoja kufika wakati anapompata. Ingepasa furaha ya Mchungaji wakati anapopata kondoo mmoja aliyepotea kutufundisha kuheshimu na kutambua damani ya wadogo wake.

**18:14** Si malaika wala Mchungaji tu, lakini Mungu **Baba** anaweka roho juu yao. Hataki **hata mmoja** wa wadogo hawa **kupotea.** Basi kama malaika, Bwana Yesu na Mungu Baba wakiweka roho juu yao, haifai kwa sisi kuwazarau kamwe, hata kama wakionekana kama watu bure wasiopendeza.

**C. Namna gani kutendea wakosayi (18:15-20)**

Baki la sura hii ni juu ya magomvi katikati ya watu kanisani, na hitaji la usamehe bila kipimo.

**18:15** Sasa tunapata mafundisho namna gani inapasa Mkristo kutenda kama mwamini mwingine akimkosea. Kwanza inapasa Wakristo hawa wawili wajaribu kutengeneza maneno haya wao wawili tu peke yao. Kama yule aliyeumiza ndugu yake akikubali kosa lake, ndugu wale wanapatanishwa tena. Lakini mara nyingi hatutendi hivi. Tunasemasema na watu wengine juu ya maneno haya na habari zinaenea mbio katikati ya watu na magomvi yao yanaongezeka. Tukumbuke kwamba neno la kwanza ambalo inatupasa kufanya ni **"kwenda umwonyeshe kosa lake wewe naye peke yenu."**

**18:16** Kama ndugu yule ambaye alikosa akikataa kusikiliza, inapasa ndugu mmoja au wawili waende pamoja nawe kujaribu kumfahamisha kosa lake. Neno hili linaonyesha kwamba ni vibaya sana kwa yeye kukataa kutubu. Na vilevile ndugu wale wengine ni washuhuda kwani Maandiko yanaagiza ya kwamba **"katika vinywa vya wa-**

**shuhuda wawili au watatu kila neno lisimamishwe".** (Tor. 19:15) Lakini mara nyingi watu hawatii agizo hili ya kwamba sharti mwenye kushitaki ndugu yake juu ya neno fulani awe na washuhuda wawili au watatu, na kuasi agizo hili kunaleta matata nyingi sana kanisani. Kwa maneno haya baraza za hukumu za watu wa dunia wanatenda na haki kupita makanisa ya Wakristo mara nyingi.

**18:17** Kama yule aliyeshitakiwa akikaa kukataa kukiri kosa lake na kuomba usamehe, inapasa kuleta neno hili mbele ya kanisa. Sharti kanisa la pahali pale lisikie na kukata maneno haya, si baraza ya hukumu ya serikali. Mkristo anakatazwa kushitaki mwamini mwingine mbele ya waamuzi wa dunia (1 Kor. 6:1-8).

Kama mtendaji mabaya akikataa kukubali kosa lake mbele ya kanisa, inapasa awe kwao kama **mtu wa mataifa na mtoza kodi**, maana yake yeye hahesabiwi kuwa mtu wa kanisa hili tena. Hata akiwa ndani ya kanisa lililo mwili wa Kristo, haishi kama Mkristo, hivi hawezi kushiriki ndani ya baraka na upatano wa kanisa la pahali pale tena. Ni neno kubwa na linatoa mwamini kwa Shetani kwa wakati "ili mwili uharibiwe, hata roho yake iokolewe katika siku ya Bwana Yesu" (1 Kor. 5:5). Kusudi la kufanya hivi ni kumfahamisha ubaya wa tendo lake na kumsukuma kukiri zambi yake. Kufika siku anapofanya hivi inapasa waamini wengine kumtenda kwa adabu lakini wamwonyeshe vilevile ya kwamba hawakubali zambi yake na hawana upatano naye kama mbele na namna walivyo nao na waamini wengine. Lakini wakati matendo yake yanapoonyesha kwamba ametubu kweli waamini wasikawe kumpokea tena katikati yao.

**18:18** Shairi hili linafungana na maneno ambayo yanayatangulia. Wakati kanisa na maombi na wakitii neno la Mungu wanapohukumu mwamini na azabu, tendo lao linakubaliwa mbinguni. Wakati mtu yule aliyehukumiwa hivi anapokwisha kutubu na kukiri zambi yake, kanisa wanamrudisha tena katikati yao, na Mungu anakubali tendo lao vilevile (ona Yn. 20:23).

**18:19** Labda unauliza kama ikipasa kanisa kuwa na watu wengapi ndani yake mbele ya kuweza kuhukumu (kufunga na kufungua) namna hii? Waamini **wawili** wanaweza kuleta maneno namna hii mbele ya Mungu ndani ya maombi wakijua kwamba Mungu anasikia maombi yao. Shairi hili ni ahadi ya kwamba Mungu atajibu maombi mengine vilevile, lakini zaidi ni kwa maneno haya ya mwamini anayeanguka. Wakati waamini wanapoomba juu ya maneno mengine, sharti maombi yao yapatane na mafundisho yote mengine juu ya maombi. Kwa mfano,

1) Sharti maombi yao yapatane na mapenzi ya Mungu (1 Yn. 5:14,15).
2) Waombe na imani (Yak.1:6-8).
3) Waombe na roho ya kweli (Ebr. 10:22a).

**18:20** Shairi hili ni zaidi juu ya kusanyiko la Wakristo wa kanisa wanaojaribu kupatanisha Wakristo wawili waliogawanyika kwa sababu ya zambi fulani. Lakini mafundisho haya ni kweli kwa makusanyiko yote ya waamini pahali Kristo ni katikati.

Maana ya "kwa jina langu" ni kwa amri yake, tukikubali kwamba Yeye ni Bwana wa yote, na tukitii Neno lake. Hakuna chama cha Wakristo wanaoweza kusema ya kwamba wao tu wanakutana kwa jina lake; kama ingalikuwa hivi Bwana angaliweza kuwa pamoja na sehemu ndogo tu ya mwili wake hapa duniani. Pahali po pote **wawili au watatu wanapokutana** wakizunguka Bwana na Mwokozi wao, yeye ni **pale katikati yao**.

**D. Juu ya usamehe bila kipako (18:21-35)**

**18:21,22** Halafu **Petro** aliuliza Bwana kama ikimpasa kusamehe **mara ngapi** ndugu Mkristo ambaye anamkosea. Labda alifikiri angekuwa na roho ya neema kabisa kama akimsamehe mara **saba**. Lakini Yesu alijibu "**si mara saba …lakini hata makumi saba mara saba.**" Hataki tufikiri kwamba inatupasa kusamehe mara 490; hesabu hii ilikuwa mfano tu kusema "bila kipimo."

Labda unafikiri, "Kwa nini inapasa kufuata utaratibu huu? Kwa nini inatupasa kufikia mwenye kukosa peke yake kwanza, nyuma yake pamoja na mtu mmoja au watu wawili wengine, na nyuma yake kumleta yeye na maneno yake mbele ya kanisa? Kwa sababu gani siwezi kumsamehe mara moja na kumaliza neno lenyewe?"

Ni kwa sababu usamehe una sehemu tatu:

1. Wakati ndugu mmoja anaponikosea inanipasa kumsamehe mara moja *moyoni mwangu* (Efe. 4:32). Nikifanya hivi sitakuwa na roho ya uchungu na kutosamehe na ninaacha neno lenyewe kwa mikono *yake.*
2. Hata kama ninakwisha kumsamehe moyoni mwangu, simjulishi mara moja kwamba amesamehewa. Si haki kumsamehe mbele ya watu wote kufika wakati anapokwisha kutubu. Hivi inanipasa kufika karibu naye na kumhamakia na roho ya mapendo, nikitaraji kwamba neno hili litamsukuma kukiri zambi yake (Lk. 17:3).
3. Wakati anapokiri zambi yake na kuomba usamehe ninamwambia mara moja kwamba amesamehewa (Lk. 17:4).

**18:23** Halafu Yesu alitumika na mfano wa **ufalme wa mbinguni** kuonya wasikiaji wake waliokwisha kusamehewa wao wenyewe juu ya hatari ya kuwa na roho ya kutokusamehe.

**18:24-27** Mfano huu ni juu ya mfalme asiyetaka watu kukaa na deni karibu naye. Mtumishi wake mmoja alikuwa na deni ya talanta elfu moja asiyoweza kulipa, hivi bwana wake aliagiza yeye pamoja na jamaa yake wauzwe kuwa watumwa kwa kumaliza deni hii. Mtumishi alisumbuka sana, akasihi bwana wake kuwa na saburi na kungoja kwanza na aliahidi **kulipa** deni **nzima** polepole.

Kama watu wengi wenye deni mtu huyu alifikiri ataweza kulipa deni yake nzima kama akiwa na saa tu (sh. 26). Mapato ya inchi ya Galilaya ya mwaka mzima yalikuwa talanta 300 tu, lakini mtu huyu alikuwa na deni ya talanta 10,000! Kwa njia ya kutaja hesabu hizi wazi Bwana alitaka kushitusha wasikiaji waweze kusikiliza vizuri, na kuwaonyeshea deni yao kubwa sana karibu na Mungu. Martin Luther alisema sisi sote ni waombaji masikini mbele yake. Hakuna njia kwa sisi kulipa deni yetu. (Mafundisho ya Notes Bibliques.)

Wakati **bwana** alipoona roho ya toba ya **mtumwa** wake, alimsamehe deni hii nzima ya talanta 10,000. Lilikuwa tendo la neema kubwa, si ya haki ya sheria.

**18:28-30** Basi mtumwa mwingine alikuwa na deni ya dinari mia moja na mtumwa yule aliyesamehewa deni kubwa sana. Mtumwa yule alikataa kumsamehe deni hii, akamshika shingoni na kumwagiza kulipa deni yake nzima mara moja, akamtupa gerezani kufika wakati atakapomaliza kulipa deni yake. Neno hili halikuwezekana kwa sababu hakuwa na njia kufanya kazi wakati alipokuwa gerezani!

**18:31-34** **Watumishi** wenzake walikasirika sana juu ya maneno haya,

wakamwambia **bwana wao**. Na yule bwana alikasirikia sana mtumwa aliyesamehewa deni kubwa sana na aliyekataa kusamehe deni ndogo ya mtumishi mwenzake, akamrudisha kwa wasimamizi wa gereza kutaabishwa kufika atakapomaliza deni yake.

**18:35** Mafundisho ya mfano huu ni wazi. Mfalme ndiye Mungu. Watumishi wake wote walikuwa na deni kubwa sana ya zambi wasiyoweza kulipa. Kwa sababu ya neema na huruma yake kubwa ya ajabu Bwana alilipa deni yao na kuwasamehe kabisa. Halafu labda Mkristo mmoja anatendea Mkristo mwingine mabaya. Mkristo yule anamwuliza juu ya tendo lake na Mkristo aliyekosa anaomba usamehe. Lakini mwamini aliyekosewa anakataa kumsamehe. Yeye mwenyewe alikuwa amesamehewa deni kubwa sana, lakini anakataa kusamehe mwamini mwenzake deni ndogo. Mfalme ataona tendo lake bure? Sivyo; atamwazibu hapa duniani, na kwa wakati atakaposimama mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo atapata hasara kali.

### E. Juu ya ndoa, kuachana, na kukaa bila kuoa (19:1-12)

**19:1,2** Nyuma ya kumaliza kazi yake katika Galilaya Bwana aligeuka kwa kusini kwenda Yerusalema. Ni kama alipita kwa Perea, kwa upande wa mashariki wa Yorodani. Matayo aliita sehemu ile ya inchi **mipaka ya Yudea ngambo ya Yorodani.** Tunasoma juu ya utumishi wake katika Perea toka 19:1 kufika 20:16 au 20:28; haionekani wazi wakati gani alipovuka Yorodani kuingia Yudea tena.

**19:3** Tunafikiri makutano waliofuata Yesu kusudi waponyeshwe walijulisha Wafarisayo pahali Bwana alipokuwa. Kama imbwa kali za mwitu walimzunguka waweze kumtega ndani ya masemo yake. Walimwuliza kama sheria ilikubali watu kuachana kwa sababu yo yote. Hata akijibu neno gani, jibu lake litakasirisha wengine wa Wayuda. Wengine walifikiri kuachana kulikubaliwa kwa sababu yo yote; wengine walikuwa na mawazo makali juu ya neno hili.

**19:4-6** Bwana wetu alieleza ya kwamba kwa mwanzo Mungu alikubali kwa mwanamume kuwa na mke hai mmoja tu. Mungu yule aliyeumba **mume na mke** aliagiza ndoa ikomboe nyumba ya wazazi. Alisema vilevile ya kwamba ndani ya ndoa watu wawili wanafunganishwa kuwa moja. Mungu hakutaka matendo au amri zo zote za watu kuharibu umoja huu.

**19:7** Wafarisayo walifikiri masemo ya Bwana hayakupatana hata kidogo na Agano la Kale. Walimkumbusha kwamba **Musa** alitayarisha njia kwa watu kuachana. Mume aliweza kumpa mke wake barua tu, kisha kumfukuza toka nyumbani mwake (Tor. 24:1-4).

**19:8** Yesu alikubali kwamba **Musa aliruhusu** mwanamume kuacha mke wake, lakini tendo hili halikuwa neno zuri zaidi Mungu alilokusudi kwa watu. Kwa sababu Waisraeli walikuwa wamerudi nyuma kwa maneno ya Mungu **"Musa kwa sababu ya ugumu wa mioyo yenu aliwapa ninyi ruhusa kuondosha wake wenu, lakini tangu mwanzo haikuwa hivi."** Neno kamili Mungu alilotaka lilikuwa kwa watu kukaa pamoja bila kuachana. Lakini mara nyingine Mungu *anakubali* maneno *yasiyoongozwa* naye.

**19:9** Kisha Bwana alisema na amri ya kwamba kuanza sasa ukubali wa kuachana umekwisha. Kutakuwa na sababu moja tu itakayokubaliwa kwa kuachana, ndiyo uasherati. Kama watu wakiachana kwa sababu nyingine yo yote, kisha kuoa tena, wanatenda **uzini.**

Hata kama Bwana hakusema neno hili wazi, ni kama wakati watu walipokwisha kuachana kwa sababu ya uzini, yule asiyetenda uzini ana ruhusa kuoa tena.

Walimu wengine wa Biblia wanafikiri mafundisho haya ni juu ya uasherati mbele ya ndoa tu linalofunuliwa nyuma ya ndoa (ona Tor. 22:13-21). Wengine wanafikiri ni juu ya utaratibu wa ndoa ya Wayuda tu, na kwa sababu hii sababu moja iliyokubaliwa kwa kuachana inatajwa hapa katika Matayo tu, ndiyo Habari Njema iliyoandikwa zaidi kwa Wayuda.

Ona Matayo 5:31,32 kwa mafundisho mengine juu ya uzini.

**19:10 Wanafunzi** walishituka kabisa juu ya mafundisho haya, wakasema kama kuna ruhusa kwa neno hili moja tu kwa kuachana, **vizuri watu wasioe** kusudi wasikose nyuma ya ndoa. Lakini kukaa bila kuoa lisingaliwazuiza wasianguke bila ndoa.

**19:11** Hivi Mwokozi aliwakumbusha ya kwamba si watu wote wanaoweza kukaa bila kuoa; ni wale tu wanaopewa uwezo na neema toka Mungu kufanya hivi. Maana ya masemo haya, **"Si watu wote wanaoweza kupokea neno hili, ila wale waliopewa"** si kusema ya kwamba watu wote hawawezi kufahamu mafundisho yanayofuata, lakini ya kwamba hawawezi kuishi maisha safi bila kuoa isipokuwa wanaitwa kuishi maisha namna hii.

**19:12** Bwana Yesu alieleza kwamba kuna namna tatu za matowashi. Wengine ni matowashi kwa sababu walizaliwa bila uwezo wa kuzaa watoto. Wengine ni matowashi kwa sababu watu wengine waliwafanyiza matowashi. Lakini Yesu alifikiri zaidi wale ambao walijifanya wenyewe matowashi kwa ajili ya ufalme wa mbinguni. Wanaume hawa wangaliweza kuoa, lakini kwa ajili ya Mfalme na ufalme wake, wanachagua kukaa bila kuoa ili waweze kujitoa yote kwa kazi ya Bwana bila kuzuizwa na maneno mengine. Paulo aliandika nyuma, "Yeye asiyeoa anasumbuka juu ya maneno ya Bwana – namna gani apate kupendeza Bwana" (1 Kor. 7:32). Wanakaa bila kuoa kwa sababu wao wenyewe wanachagua kukaa hivi, si kwa sababu ya uzaifu mwilini mwao.

Si watu wote wanaoweza kuishi maisha namna hii; ni wale tu wanaowezeshwa na Mungu: "Kila mtu ana zawadi yake mwenyewe kutoka kwa Mungu, huyu hivi na yule hivi" (1 Kor. 7:7).

**F. Juu ya watoto (19:13-15)**

Habari za watoto zinafuata mara moja hotuba hii juu ya kuachana (ona vilevile Marko 10:1-16); mara nyingi ni watoto wanaotaabishwa zaidi wakati wazazi wao wanapoachana.

Wazazi walileta **watoto wao wadogo** kwa Yesu ili Mwalimu-Mchungaji awabariki. **Wanafunzi** walichukizwa na neno hili na **walikemea** wazazi. Lakini Yesu alitoa jibu hili tamu sana: **"Acheni watoto wadogo waje kwangu wala musiwazuize; kwa sababu ufalme wa mbinguni ni wao."**

Jibu hili linatufundisha maneno makubwa. Kwanza, watumishi wa Mungu wafahamu kwamba ni faida kubwa kupata watoto kwa Kristo wakati nia zao ni kwanza wazi kupokea Neno la Mungu. Neno la pili ndilo hili: Watoto wakitaka kukiri kwamba wanaamini Bwana Yesu, inapasa kuwasaidia ndani ya neno hili, si kuwazuiza. Hatujui kama mfu aliye kijana zaidi katika Hadeze ana miaka mingapi. Mtoto akitaka kweli kuamini na kupokea wokovu haifai kumwambia kwamba inampasa kungoja kwanza kupata nguvu. Lakini haifai vilevile kumsukuma kukiri Kristo. Si lazima kwa watoto kuwa watu wa kukomea kwanza, lakini ni sharti kwa watu wazima kugeuka kama watoto wadogo (Mt. 18:3,4; Mk. 10:15).

Neno la tatu ndilo hili: Watu wanauliza nini inatokea kama watoto wakikufa mbele ya wakati wanapohesabiwa kuwa watu wakubwa? Yesu alisema

**"... ufalme wa mbinguni ni wao."** Ingepasa jibu hili kusaidia roho za wazazi waliokufiwa watoto wadogo.

Watu wengine wanataja mashairi haya kuonyesha kwamba inapasa watoto wadogo kubatizwa kuwafanyiza viungu vya Kristo na wariti wa ufalme. Lakini tukisoma mashairi haya polepole tunaona kwamba wazazi walileta watoto kwa Yesu, si kwa pahali pa kupata ubatizo. Yanaonyesha vilevile kwamba watoto walikuwa wariti wa ufalme hata mbele. Na hatusomi juu ya maji ya ubatizo hata kidogo.

**G. Juu ya mali. Mwenye mali nyingi (19:16-26)**

**19:16** Tulikuwa tumeona ya kwamba ufalme wa mbinguni ni wa watoto wadogo, lakini sasa tutaona ya kwamba ni nguvu sana kwa watu wazima kuingia ndani yake.

Mtu mwenye mali nyingi alifika karibu na Bwana na ulizo. Akiita Bwana **"Mwalimu mwema"** alimwuliza kama ikimpasa **kufanya** nini **kupata uzima wa milele**. Ulizo lake lilionyesha kwamba alikuwa mjinga kabisa. Hakujua kama Yesu alikuwa nani wala njia ya wokovu. Aliita Yesu **"Mwalimu"**, akimweka pahali pamoja na watu wakubwa wengine. Na alisema juu ya kupata **uzima wa milele** sawasawa ni deni, si zawadi.

**19:17** Bwana Yesu alimpima juu ya maneno haya mawili. Wakati alipouliza, **"Kwa sababu gani unaniuliza juu ya maneno mema? Ni mmoja aliye mwema, ndiye Mungu,"** Yesu hakukana ya kwamba yeye mwenyewe ni Mungu, lakini alimpa mtu huyu njia kusema, "Kwa sababu wewe ni mwema – wewe ni Mungu."

Na kwa kumpima juu ya njia ya wokovu Yesu alisema, **"lakini kama ukitaka kuingia katika uzima, ushike amri."** Mwokozi hakutaka kufikirisha watu ya kwamba mtu anaweza kuokolewa kwa njia ya kushika amri. Sivyo, lakini alitumika na sheria kuonyeshea mtu yule kwamba yeye ni mwenye zambi. Mtu huyu alikaa kufikiri kwamba ataweza kuingia ufalme kwa njia ya ku*tenda*. Basi, ashike amri ambayo ilimwambia nini ilimpasa kufanya.

**19:18-20** Bwana wetu alitaja maagizo matano juu ya namna gani kutendea wenzetu, akimaliza na **"Penda jirani yako kama wewe mwenyewe."** Mtu huyu hakufahamu kwamba alijipenda mwenyewe zaidi, akajibu na kiburi ya kwamba **ametii** amri hizi zote.

**19:21** Halafu kwa njia ya kusema naye **kuuza** vitu vyake vyote na **kutoa** mali yenyewe kusaidia watu **masikini,** kisha **aje na kumfuata**, Bwana alionyesha ya kwamba mtu huyu hakupenda jirani yake kwa kipimo alichojipenda mwenyewe.

Maana ya masemo haya ya Bwana haikuwa ya kwamba mtu huyu angaliokolewa kwa njia ya kuuza vitu vyake na kuleta mali yenyewe kwa watu masikini. Kuna njia moja tu kupata wokovu, ndiyo kuamini Bwana Yesu.

Lakini mtu akitaka kuokolewa, sharti akiri ya kwamba amekosa na kupungukia utakatifu wa maagizo ya Mungu. Tajiri hakuwa tayari kushiriki mali yake na wenye mahitaji, na neno hili lilionyesha kwamba hakupenda jirani yake kwa kipimo alichojipenda mwenyewe. Ingalimpasa kusema, "Bwana, kama hili ndilo neno linalohitajiwa, ninafahamu kwamba mimi ni mwenye zambi na siwezi kujiponyesha mwenyewe. Hivi ninakuomba uweze kuniokoa kwa neema yako." Kama angalifanya hivi angalipata wokovu.

**19:22** Lakini hakufanya hivi; **akakwenda zake na huzuni.**

**19:23, 24** Tendo lake lilisukuma **Yesu** kusema kwamba **ni nguvu kwa tajiri**

**kuingia ufalme wa mbinguni**. Ni nyepesi kwa mali kugeuka sanamu kwetu. Ni nguvu kwa mtu kuwa na mali bila kuitegemea. Bwana wetu alisema **"ni neno jepesi kwa ngamia kupita katika tundu la sindano kuliko tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu."**

Ni wazi ya kwamba ngamia hawezi kupita katika tundu la sindano! Wengine wanasema "tundu la sindano" ndilo mlango mdogo katika lango la mji. Ilikuwa nguvu kwa ngamia kupita kwa mlango huu mdogo, lakini iliwezekana kama ikipiga magoti. Lakini neno linalotumiwa kwa "sindano" katika Luka ni sindano ambalo wanganga wanatumika nalo wakati inapowapasa kupasua na kushona mwili wa mtu. Bwana hakusema juu ya neno lililo nguvu, lakini juu ya neno *lisilowezekana*. Kwa ubinadamu *haiwezekani* kwa tajiri kuokolewa.

**19:25 Wanafunzi walishangaa** sana juu ya masemo haya ya Bwana wao. Walikuwa Wayuda walioishi kwa wakati wa sheria ya Musa. Kwa njia ya sheria hii Mungu aliahidi usitawi kwa watu ambao walimtii. Kama watu wanaobarikiwa hivi na Mungu hawawezi kuokolewa, basi watu gani *wanaweza* kupata wokovu?

**19:26** Bwana alijibu akisema, "**Kwa watu haiwezekani, lakini kwa Mungu maneno yote yanawezekana."** Kwa binadamu **haiwezekani** kwa mtu ye yote kuokolewa; Mungu tu anaweza kuokoa roho ya mtu. Lakini ni nguvu kwa tajiri kujitoa kuishi kwa Kristo, kupita kwa mtu masikini kujitoa kwa Bwana, na kwa sababu hii watajiri wachache tu wanaokolewa. Ni nguvu sana kwao kuacha kutegemea mali yao kwa mahitaji yao na kuamini Mwokozi tu ambaye hawawezi kuona na macho. Mungu tu anaweza kugeuza roho yao hivi.

Wahubiri na walimu wengi wanaongeza kusema hapa kwamba si vibaya kwa Wakristo kuwa na mali nyingi. Lakini Bwana alikuwa ameonyesha sasa tu ya kwamba mali ni kikwazo kwa mtu asifikie baraka ya milele. Hivi ni neno la kushangaza kwa walimu kutumika na mashairi haya kuruhusu watu kujivimbishia hazina hapa duniani. Na ni nguvu kufahamu namna gani Mkristo anaweza kushikamana na mali yake wakati anapozungukwa na mahitaji makubwa pahali pote, wakati anapokumbuka kwamba kurudi kwa Bwana ni karibu, na ya kwamba Bwana amekataza watu waziwazi wasijiwekee hazina duniani. Kujivimbishia mali hapa duniani kunaonyesha wazi kwamba hatupendi jirani yetu kama sisi wenyewe.

**H. Juu ya zawabu kwa wenye kujitoa kuishi kwa Bwana (19:27-30)**

**19:27 Petro** alifahamu mafundisho haya ya Bwana na ya kwamba alisema "Acha vyote na unifuate Mimi." Akikumbuka kwamba yeye na wanafunzi wengine walikuwa wamefanya hivi, aliuliza, "**Sisi tutapata nini basi?**" Tabia ya zamani ya Petro ilionekana tena. Ni neno ambalo inatupasa sisi sote kuepuka ndani ya maisha yetu. Ni kama alikuwa akipigania bei na Bwana.

**19:28, 29** Bwana alisema na Petro ya kwamba atapokea zawabu kwa maneno yote aliyofanya kwa yeye. Mitume kumi na wawili watapewa pahali pa amri kwa wakati wa ufalme wa miaka elfu moja. Maana ya **ulimwengu mpya** ndiyo utawala wa Kristo duniani kwa wakati wa kuja **"wakati Mwana wa watu atakapoketi juu ya kiti cha utukufu wake."** Kwa wakati ule mitume kumi na wawili **wataketi juu ya viti vya ufalme kumi na viwili, wakihukumu makabila kumi na mawili ya Israeli**. Katika Agano Jipya zawadi zinaungana na kazi ya utawala katika muda wa utawala wa miaka elfu moja (ona Luka 19:17,19). Bwana ana*toa* zawadi kwa kiti cha hukumu cha Kristo, lakini zita*onekana*

wakati Bwana atakaporudia dunia kutawala.

Kwa maneno ya waamini wengine Yesu aliongeza ya kwamba kila mtu **aliyeacha nyumba, au ndugu, au ndugu wake, au baba, au mama, au watoto, au mashamba, kwa ajili** yake **atapewa mara mia, na atariti uzima wa milele.** Kwa wakati wa sasa wanabarikiwa na ushirika na waamini pahali pote duniani, unaokomboa hata kupita kipimo ushirika wao na ndugu na rafiki walioacha. Wanaacha nyumba yao moja, lakini wanapokewa na mapendo ndani ya nyumba za Wakristo mia moja. Na kwa pahali pa mashamba na mali waliyoacha kwa ajili ya Bwana, watapokea baraka kubwa za roho.

Zawabu kwa waamini wote kwa wakati wa kuja ni **uzima wa milele.** Si kusema kwamba tunaweza kujipatia uzima wa milele kwa njia ya kujikana wenyewe na kuacha vyote. Uzima wa milele ni zawadi, na hatuwezi kufanya kitu kwa kuupata au kuustahili. Maana ya maneno haya ni ya kwamba zawabu ya wale walioacha vyote kwa kufuata Bwana ni kupewa uwezo mkubwa kupita kufurahia uzima wa milele. Waamini wote watakuwa na uzima ule, lakini wengine wataufurahia kupita wenzao.

**19:30** Bwana alimaliza mafundisho haya kwa njia ya kuonya wasikiaji wake wasifikiri faida yao wenyewe ndani ya kazi yao kwa Bwana. Alisema na Petro ya kwamba atapokea zawabu kwa neno lo lote alilofanya kwa yeye, lakini akae na ange asifikiri faida yake mwenyewe ndani ya kazi hii kwa sababu **wengi walio wa mwisho watakuwa wa kwanza; nao walio wa kwanza watakuwa wa mwisho.** Tutaona neno hili ndani ya mfano kwa mwanzo wa sura 20. Labda masemo haya ya Bwana ni maonyo vilevile kwamba haitoshi ku*anza* kumfuata vizuri. Neno kubwa ndilo ku*maliza* utumishi wetu na uaminifu.

Mbele ya kuacha sura hii tuone ya kwamba ndani ya mashairi 23 na 24 "ufalme wa mbinguni" na "ufalme wa Mungu" yana maana moja. Hivi tunafahamu ya kwamba hakuna tofauti kati yao.

**I. Juu ya zawabu za walimaji shambani mwa mizabibu (20:1-16).**

**20:1,2** Mfano huu unaendelea na hotuba juu ya zawabu kwa mwisho wa sura 19. Unaonyesha kwamba wanafunzi wote watapokea zawabu, lakini ukubwa wa zawadi zao ni vipimo mbalimbali kupatana na hali ya roho ambayo walitumikia Bwana nayo.

Mfano ni juu ya **mwenye mashamba aliyetoka asubui mapema kutafuta watenda kazi** kutumika ndani ya **shamba lake la mizabibu**. Watu hawa walipatana kumtumikia kwa siku moja kwa mshahara wa **dinari moja**, ndiyo hesabu nzuri kwa wakati ule. Tuseme walianza kazi kwa saa kumi na mbili ya usiku.

**20:3,4** Kwa saa tatu ya mchana mwenye shamba alikuta watu wengine waliokosa kazi kwa **pahali pa soko**. Mara hii hawakupatana juu ya mshahara. Walikwenda kutumika shambani mwake wakiamini tu kwamba atawapa **iliyo haki.**

**20:5-7** Saa sita na saa tisa mwenye shamba alituma watu wengine kwa shamba lake akiahidi kuwapa mshahara wa haki. Saa kumi na moja alikuta watu wengine waliokosa kazi. Hawakuwa wavivu; walitaka kutumika lakini iliwashinda kupata kazi. Basi mwenye shamba aliwatuma kwa **shamba lake la mizabibu** bila kusema neno juu ya mshahara.

Ona ya kwamba watu wa kwanza walikwenda kutumika nyuma ya kupatana juu ya mshahara; watu wale wote wengine waliacha neno la mshahara wao kwa mikono ya mwenye shamba.

**20:8** Kwa wakati wa mangaribi mwenye shamba aliagiza msimamizi

wake kulipa watu wa kazi, akianza na **watu wa mwisho** hata **watu wa kwanza.** (Kwa njia hii watu wa kwanza waliona mali ambayo watu wengine walipokea.)

**20:9-12** Watu wa kazi wale wote walipokea mshahara kipimo kimoja, ndio dinari moja. Watu walioanza kazi saa kumi na mbili ya usiku walifikiri watapokea kupita wale waliotumika saa nusu tu, lakini sivyo – wao vilevile walipokea dinari moja. Watu wa kwanza walikuwa na uchungu rohoni; walikuwa wametumika mchana mzima na **kuvumilia jua kali.**

**20:13,14** Jibu la mwenye shamba kwa mmoja wao linaonyesha mafundisho makubwa ya mfano huu kwa sisi. Kwanza alisema, **"Rafiki, sikutendei mabaya; hukupatana nami kwa dinari moja? Chukua iliyo yako na kwenda zako; ninapenda kumpa huyu wa mwisho sawa na wewe.**" Mtu wa kwanza alipatana na mwenye shamba kupokea dinari moja kwa kazi ya mchana mmoja na alipewa mshahara huu. Wengine wote walitegemea roho ya neema ya mwenye shamba na walipokea neema. Neema ni nzuri kupita haki. Ni vizuri kupita kuacha Bwana kutuchagulia zawabu zetu bila kupigania bei naye.

**20:15** Halafu mwenye shamba alisema, **"Si halali yangu kufanya navyo vilivyo vyangu namna ninavyotaka?"** Ni mafundisho wazi kwa sisi ya kwamba Mungu ni mwenye enzi. Anaweza kufanya namna anavyotaka. Na maneno anayotaka ni mazuri na haki kila mara. Mwenye shamba aliongeza, **"Au jicho lako limekuwa baya kwa sababu mimi ni mwema?"** Ulizo hili linaonyesha kwamba sisi watu tunajifikiri zaidi wenyewe. Watu walioanza kazi asubui mapema walipokea mshahara waliostahili kupata, lakini walikuwa na wivu kwa sababu wengine walioanza kazi nyuma walipewa mshahara ule vilevile. Labda sisi vilevile tunafikiri neno hili si haki. Habari hizi zinatufundisha basi ya kwamba katika ufalme wa mbinguni inatupasa kugeuza kabisa namna tunavyofikiri. Lazima tuachane na roho yetu ya choyo na kuanza kufikiri namna Bwana wetu anavyofikiri.

Mwenye shamba alijua watu hawa wote walihitaji mali, hivi aliwalipa kwa kipimo cha mahitaji yao, si cha choyo chao. Hakuna mtu aliyepokea kidogo kupita mshahara aliostahili kupokea, lakini wao wote walipokea kutosha kwa mahitaji yao na ya jamaa zao. Wakati tunapokaa kusoma na kujifunza mfano huu tunafahamu ya kwamba habari hizi si haki tu, lakini ni za kupendeza sana. Ingalipasa wale walioanza kazi asubui mapema kufikiri juu ya neno hili kama zawabu nyingine, ndiyo kuweza kutumikia bwana mwema namna hii mchana mzima.

**20:16** Yesu alimaliza mfano huu na maneno haya, **"Vivyo hivyo wa mwisho watakuwa wa kwanza, na wa kwanza watakuwa wa mwisho"** (ona Mt.19:30). Kutakuwa na mishangao siku ile wakati Bwana atakapotolea watu zawabu. Watu wengine walio*fikiri* watakuwa kwanza watakuwa kwa mwisho kwa sababu walitumikia Bwana wakisukumwa na roho ya kiburi na tamaa ya kupata heshima. Wengine ambao walimtumikia wakisukumwa na shukrani na mapendo wataheshimiwa sana.

**J. Juu ya mauti na ufufuko wake (20:17-19)**

Inaonekana sawasawa Bwana alikuwa akiondokea Perea sasa na kupita kwa Yeriko kwa safari yao **kwenda Yerusalema** (ona sh. 29). Mara moja tena **alikusanya wanafunzi kumi na wawili peke yao** na kuwaelezea nini itatokea wakati watakapofikia Yerusalema. Atatiwa mikononi mwa **wakubwa wa makuhani na waandishi** (alikuwa akisema kwa maficho juu ya tendo la hila la Yuda). Viongozi wa Wayuda wata-

mhukumu kufa, lakini kwa sababu hawakuwa na ruhusa kufanya hivi wao wenyewe, walimtia kwa mikono ya **Mataifa** (ndio Waroma). Atazarauliwa, kupigwa na kusulibishwa. – **Atafufuliwa tena siku ya tatu.**

### K. Juu ya cheo katika ufalme (20:20-28)

Ni huzuni kuona ndani ya mashairi yanayofuata tabia ya kujifikiri wenyewe ya wanafunzi. Mara moja nyuma ya kusikia mara ya tatu juu ya taabu na kufa kwa Bwana wao, wanafunzi walifikiri utukufu wao wenyewe kupita mateso yake.

> Mara ya kwanza Kristo aliyotabiri kwamba atateswa, Petro alisema neno hili halitatokea (Mt. 16:22). Wakati aliposema juu ya mateso yake mara ya pili, wanafunzi waliuliza mara moja kama nani atakayekuwa mkubwa zaidi katika ufalme. Halafu sasa, nyuma ya tangazo la tatu la kufa kwake, Yakobo na Yoane waliomba neno kubwa kwake. Hawakuweka roho hata kidogo juu ya habari ya kwamba matata ilikuwa karibu kutokea, wakafikiri tu juu ya ahadi ya utukufu kwa wakati wa kuja. Walifikiri juu ya ufalme kama neno la wakati wa dunia tu. *(Ligue pour la Lecture de la Bible)*

**20:20, 21 Mama ya** Yakobo na Yoane alifikia Bwana na **kuomba** wana wake waweze kuketi pamoja na Bwana katika **ufalme wake**, mmoja kwa upande wake wa kuume na mwingine kwa kushoto. Ilikuwa vizuri kwa yeye kutaka wana wake kuwa karibu na Yesu, na ya kwamba hakuacha kuamini kwamba Bwana atakuja tena kutawala. Lakini hakufahamu kwa utaratibu gani watu watapewa heshima namna hii katika ufalme.

Marko alisema Yakobo na Yoane waliomba neno hili wao wenyewe (Mk. 10:35); labda mama yao aliwaongoza kufanya hivi, au labda wao wote watatu pamoja walifika karibu na Bwana. Hakuna mabishano.

**20:22 Yesu aliwajibu** wazi ya kwamba hawakufahamu neno waliloomba. Walitaka taji mbele ya msalaba, kiti cha ufalme bila mazabahu ya zabihu, utukufu bila mateso ambayo yanautangulia. Hivi aliwauliza, **"Munaweza kunywa kikombe nitakachokunywa?" Kikombe** hiki kilikuwa nini? Bwana alikuwa amepasha juu yake sasa tu ndani ya mashairi 18 na 19, ndicho mateso na kufa kwake.

Yakobo na Yoane walisema wataweza kushiriki mateso yake, lakini labda kutaka kwao kulipita ufahamu wao.

**20:23** Yesu aliwaambia ya kwamba hakika **watakunywa** ya **kikombe** chake. Yakobo atauawa kwa sababu ya imani yake, na Yoane atafukuzwa kukaa kwa kisanga kilichoitwa Patemo.

Halafu Yesu alieleza kwamba hakuwa na ruhusa kugawia watu nafasi katika ufalme; **Baba** yake aliwekea watu nafasi kwa sababu fulani. Ni kama wanafunzi hawa walifikiri ya kwamba walikaa karibu na Kristo kupita wanafunzi wengine, hivi watakuwa na nafasi ya heshima kupita katika ufalme. Lakini Mungu alikuwa amefanya shauri zamani watu gani watapewa nafasi hizi za heshima kwa mkono wake wa kuume na kwa kushoto, ndio watu wale walioteswa kwa ajili yake. Hivi heshima kubwa zaidi katika ufalme si kwa Wakristo wengine wa wakati wa mwanzo wa kanisa tu, lakini hata kwa Wakristo wa wakati wa sasa – kwa sababu ya mateso wanayopata kwa ajili yake.

**20:24 Wanafunzi kumi wengine walikasirikia** wana wa Zebedayo kwa sababu waliomba neno hili. Labda wao wenyewe walitaka kupewa pahali pale pa heshima, na walichukizwa kwa sababu Yakobo na Yoane walipaomba kwanza!

**20:25-27** Maneno haya yalimpa

Bwana Yesu njia kutoa mafundisho makubwa juu ya ufalme wake. **Mataifa** wanafikiri ukubwa ni kuwa na amri na uwezo kutawala watu wengine. Ndani ya ufalme wa Kristo ukubwa unaonekana kwa njia ya kutumikia wengine. Lazima yule anayetaka kuwa mkubwa ageuke **mtumishi**, **naye anayetakakuwa wa kwanza** awe **mtumwa.**

**20:28 Mwana wa watu** ndiye mfano mkamilifu wa mtumishi mnyenyekevu namna hii. Hakufika duniani **kutumikiwa lakini kutumikia, na kutoa uzima wake uwe ukombozi kwa watu wengi.** Alifika duniani kwa kusudi hili tu: **kutumikia** na **kuto**a. Ni neno la kushangaza kuwaza juu ya Bwana mtukufu akijinyenyekeza kuzaliwa katika sanduku ya kulisha nyama, na kufa juu ya msalaba. Ukubwa wake ulionekana kwa njia ya kipimo kikubwa cha unyenyekevu. Ingepasa kuwa vivyo hivyo ndani ya maisha yetu vilevile.

Alitoa uzima wake kuwa **ukombozi kwa watu wengi.** Mauti yake ilitosha kuondosha zambi zote za dunia. Lakini ina faida kwa watu wale tu ambao wanampokea kuwa Bwana na Mwokozi wao. Umefanya hivi?

### L. Vipofu wawili wanaponyeshwa (20:29-34)

**20:29,30** Sasa Yesu alikuwa amevuka Yorodani, akafika **Yeriko**. Wakati alipokuwa akitoka mji, **vipofu wawili** walipaza sauti, **"Bwana, uturehemu, wewe Mwana wa Daudi!"** Walimwita **"Mwana wa Daud**i," hivi tunafahamu kwamba hata wakiwa vipofu mwilini, kwa roho zao walitambua kwamba Yesu alikuwa Masiya. Labda wao ni mfano wa baki wenye imani la Israeli wapofu ambao watampokea kama Kristo wakati atakaporudi kutawala (Isa. 35:5; 42:7; Rom. 11:25-26; 2 Kor. 3:16; Ufu. 1:7).

**20:31-34** Makutano walijaribu kuwanyamazisha, lakini **wakazidi kupaza sauti.** Wakati Yesu alipowauliza kama walitaka nini, walikuwa na jibu lao tayari: **"Bwana, macho yetu yafunguliwe."** Wakati sisi tunapoomba, mara nyingi hatutaji wazi neno tunalotaka, lakini vipofu hawa hawakufanana nasi. Walitaja wazi neno walilotaka, na Bwana alijibu ombi lao. **"Yesu akawahurumia, akagusa macho yao; mara moja wakapata kuona, wakamfuata."**

Habari tunazosoma ndani ya Marko 10:46-52 na Luka 18:35-43 na 19:1 ni mbali kidogo na habari hizi katika Matayo. Katika Matayo tunasoma juu ya vipofu *wawili*; katika Marko na Luka kuna *mmoja* tu. Labda Marko na Luka walitaja kipofu mwenye kujulikana tu, ndiye Baratimayo, na Matayo, aliyeandika zaidi kwa Wayuda, alitaja *wawili* kama ushuhuda wa hakika (2 Kor. 13:1). Katika Matayo na Marko tunasoma kwamba neno hili lilitokea wakati Yesu alipoondokea Yeriko; katika Luka iliandikwa kwamba alikuwa akikaribia mji. Kulikuwa na miji miwili iliyoitwa Yeriko, Yeriko ya zamani na Yeriko mpya, na inawezekana kwamba ajabu hili lilifanywa wakati Yesu alipokuwa akiondoka Yeriko mmoja na kuingia mwingine.

## 12. KUONYESHWA NA KUKATALIWA KWA MFALME (Sura 21–23)

### A. Mwingilio na shangwe (21:1-11)

**21:1-3** Akipanda toka Yeriko Yesu alifikia upande wa mashariki wa **mlima wa Mizeituni,** pahali pa Betania na **Betifage**. Toka pale alizunguka kusini wa mlima, alishuka kwa Bonde la Yosafati, akavuka kijito Kiduroni na kupanda kwenda **Yerusalema.**

Alituma **wanafunzi wawili** kwa Betania akijua kwamba **watakuta punda amefungwa na mwana-punda pamo-**

**ja naye.** Aliwaagiza kufungua nyama hawa na **kuwaleta** kwa Yesu. Watu wakiwauliza juu ya tendo hili, waeleze kwamba **Bwana** aliwahitaji. Halafu mwenye nyama atakubali waende nao. Labda mtu huyu alijua Yesu na alimwambia mbele kwamba alikuwa tayari kumsaidia. Au tukio hili linaonyesha kwamba Bwana Yesu anajua maneno yote na alikuwa na amri yote. Kila neno lilitokea namna Yesu alivyowajulisha mbele.

**21:4, 5** Maneno haya yalitimiza unabii wa Isaya na Zekaria:

> **"Mumwambie binti ya Sayuni,**
> **Tazama, mfalme wako anakuja kwako,**
> **Mpole naye amepanda punda,**
> **Na mwana-punda, mtoto wa punda."**

**21:6 Wanafunzi** waliweka mavazi yao juu ya punda, kisha Yesu aliketi juu ya mwana-punda (Mk. 11:7), akakaribia Yerusalema.

Kwa njia ya kuingia Yerusalema hivi, Bwana Yesu alionyesha wazi, na kusudi, ya kwamba yeye ndiye Masiya. Mwalimu Lange alionyesha:

> Alitimiza na kusudi unabii ambao watu wote wa wakati wake walieleza kuwa unabii juu ya Masiya. Mbele alifikiri kwamba kutangaza wazi ya kuwa yeye ni Mwana wa Mungu kulikuwa hatari, lakini sasa hakuweza kunyamaza juu ya neno hili tena … Hivi kutoka saa ile watu hawakuweza kusema kamwe kwamba hakuonyesha wazi ya kuwa yeye ndiye Masiya. Wakati wa kuja watu wa Yerusalema walishitakiwa juu ya kuua Masiya, lakini hawakuweza kusema ya kwamba hakuonyesha neno hili wazi kwa watu wote. [9]

**21:7,8** Bwana aliingia mji akitembea juu ya zulia ya **mavazi** na **matawi** ya mitende akisikia sifa na mashukuru ya watu. Kwa saa ndogo, basi walimkiri kuwa Mfalme.

**21:9 Makutano** wakapaza sauti … **"Hosana kwa Mwana wa Daudi; mbarikiwa anayekuja kwa jina la Bwana."** Hili ni maneno toka Zaburi 118:25-26 yanayosema wazi juu ya kuja kwa Masiya. Zamani maana ya **Hosana** ilikuwa "okoa sasa"; labda watu walifikiri, "Utuokoe toka Waroma ambao wanatutaabisha." Nyuma, maana yake iligeuka semo la gafula la sifa. Masemo haya, **"Mwana wa Daudi"** na **"Mbarikiwa yeye anayekuja kwa jina la Bwana,"** yanaonyesha wazi kwamba watu walimtambua kuwa Masiya. Yeye ndiye Mbarikiwa anayekuja na amri toka Yehova kufanya mapenzi yake.

Marko aliongeza maneno haya juu ya sifa na malalamiko ya makutano: "Ubarikiwe ufalme wa baba yetu Daudi unaokuja kwa jina la Bwana" (Mk. 11:10). Yanaonyesha kwamba watu walifikiri ufalme ulikuwa karibu kusimamishwa na Kristo akiketi juu ya kiti cha ufalme cha Daudi. Wakati makutano walipolalamika, **"Hosana juu mbinguni,"** waliita mbingu kufungana na dunia kusifu Masiya, na labda walimwita kuwaokoa toka juu mbinguni.

Marko aliandika kwa 11:11 kwamba nyuma ya kufikia Yerusalema Yesu alikwendea kiwanja cha hekalu, lakini hakuingia ndani. Lilikusudiwa kuwa nyumba ya Mungu lakini Yesu hakulifurahia kwa sababu makuhani na watu walikataa kumheshimu. Nyuma ya kutazama pande zote kwa saa nusu alikwenda Betania pamoja na wanafunzi kumi na wawili. Ilikuwa mangaribi siku ya kwanza ya juma.

**21:10,11** Lakini **mjini** watu walifazaika sana kama yeye ni nani. Wakati walipouliza waliambiwa kwamba alikuwa **Yesu, nabii toka Nazareti ya Galilaya.** Ni kama watu wachache tu walifahamu yeye ni Masiya. Mbele ya mwisho wa juma lile makutano ya

kugeukageuka watalalamika, "Asulibiwe! Asulibiwe!"

### B. Kusafishwa kwa hekalu (21:12, 13)

**21:12** Kwa mwanzo wa utumishi wake katikati ya watu Yesu alifukuza wote waliofanya biashara hekaluni (Yn. 2:13-16). Lakini nyuma kidogo, kwa kiwanja cha hekaku, watu walianza tena kujaribu kujipatia faida kwa njia ya kuuza na kununua kwa bei kubwa nyama na ndege zilizohitajiwa kwa sadaka. **Wabadilisha feza** walibadilisha mali ya wasafiri toka inchi nyingine kwa vipande vya nusu ya shekeli iliyopasa wanaume Wayuda kulipa kama kodi kwa hekalu. Sasa wakati alipokuwa akikaribia mwisho wa utumishi wake **Yesu alifukuza tena** wote ambao walijipatia faida kwa njia ya maneno ya Mungu.

**21:13** Akitaja sehemu za mashairi toka Isaya na Yeremia alihukumu maneno haya yote kuwa makufuru. Akitaja sehemu ya Isaya 56:7, alikumbusha watu kwamba Mungu alikusudi nyumba yake kuwa **nyumba ya maombi,** lakini walikuwa wameifanya pango la **wanyanganyi** (Yer. 7:11).

Hili lilikuwa tendo la kwanza la Bwana nyuma ya kuingia Yerusalema, na kwa njia yake alionyesha wazi kwamba alikuwa Bwana wa hekalu.

Habari hizi zinatufundisha maneno makubwa mawili. Tunahitaji uwezo wa Bwana ndani ya makanisa yetu kuyasafisha na kuondosha maneno yote kama karamu, kuuza vitu, na njia mbalimbali kupata mali kwa kanisa. Ndani ya maisha yetu wenyewe, tunahitaji Bwana kusafisha siku zote miili yetu iliyo mahekalu ya Roho Mtakatifu.

### C. Hasira ya makuhani na waandishi (21:14-17)

**21:14** Kisha tunaona Bwana wetu akiponyesha **vipofu na viwete** kwa kiwanja cha hekalu. Ni kama pahali po pote alipokwenda, wenye mahitaji walivutwa kwake, naye hakuwaruhusu kwenda zao kamwe bila kuwasaidia kwanza.

**21:15,16** Lakini adui zake, ndio **wakubwa wa makuhani na waandishi,** walikuwa wakitazama na walikasirika sana wakati waliposikia watoto wakisifu Yesu kama **Mwana wa Daudi.**

Walimwambia, **"Husikii maneno hawa wanayosema?"** Ni kama walifikiri atakataza watoto wasimsifu kama Masiya! Kama Yesu asingalikuwa Masiya, hii ingalikuwa saa nzuri kwa yeye kusema hivi wazi. Lakini jibu lake lilionyesha kwamba ilikuwa vizuri kwa watoto kumsifu. Alitaja Zaburi 8:2, **"Toka vinywa vya watoto wachanga nao wanaonyonya umepata sifa ya kutimia."** Kama makuhani na waandishi waliozani wao ni wenye hekima hawakumsifu kama Masiya, halafu Bwana atapata sifa toka vinywa vya watoto wadogo. Mara nyingi ufahamu wa maneno ya roho wa watoto wadogo ni mkubwa kupita umri wao, na masemo yao ya imani na mapendo yanatukuza Bwana zaidi.

**21:17** Yesu aliacha viongozi vya dini kuwaza juu ya kweli hii, akaondoka hekaluni na kurudia **Betania** kushinda usiku pale.

### D. Mtini usiozaa matunda (21:18-22)

**21:18,19** Wakati Bwana aliporudia Yerusalema **asubu**i, aliona **mtini** kando ya njia, na alitaraji matunda yake yatasaidia kupunguza njaa yake. Lakini mtini **ulikuwa na majani tu**, hivi alisema, **"Yasipatikane matunda kwako tangu leo hata milele." Mtini ule ulikauka** mara moja.

Kwa Marko 11:12-14 tunasoma kwamba haukuwa wakati wa tini. Tunge-

weza kufikiri kwamba Bwana alikasirika mbio na bila akili. Tunajua neno hili si kweli, hivi tunaweza kueleza tukio hili namna gani?

Mitini ndani ya inchi zile ilizaa matunda yanayoweza kuliwa hata mbele ya kuonekana kwa majani. Yalitangulia mavuno yatakayofuata. Kama hakuna matunda yale ya kwanza, neno hili lilionyesha ya kwamba hakutakuwa na mavuno nyuma.

Hili ni ajabu la pekee Kristo alilotenda lililotukana kwa pahali pa kubariki, kuharibu kwa pahali pa kurudisha uzima. Watu wengine wanafazaika juu ya neno hili. Ni kwa sababu hawajuani sana na Kristo kwanza. Yeye ni Mungu, mwenye enzi wa ulimwengu. Mengine ya maneno anayofanya ni siri kwetu, lakini tunajua kwamba anatenda kwa haki kila mara. Hapa Bwana alijua kwamba mtini hautazaa matunda kamwe, na alitenda kama mlimaji anayeondosha mti usiozaa toka shamba lake.

Hata wale wanaofazaika juu ya Bwana akilaani mtini wanakubali kwamba tendo hili lina maana nyingine vilevile. Ni mfano wa namna alivyopokewa katika Yerusalema na furaha nyingi sasa tu. Kama mzabibu na mzeituni, mtini ni mfano wa taifa la Israeli. Wakati Yesu alipotokea katikati yao alikuta majani tu, kukiri kwa kinywa tu bila matunda kwa Mungu. Yesu alikuwa na hamu kwa matunda ya kweli toka taifa hili.

Kwa sababu matunda ya kwanza yalikosa, alijua watu hawa wasioamini hawatazaa matunda nyuma vilevile, hivi alilaani mtini. Ni mfano wa hukumu itakayopata taifa kwa mwaka 70 A.D.

Tukumbuke ya kuwa taifa la Israeli *lisiloamini* halitazaa matunda kamwe, lakini wengine katikati yao, ndilo *baki,* watarudi karibu na Masiya nyuma ya kupelekwa kwa kanisa mbinguni. Watamzalia matunda kwa wakati wa Mateso na katika utawala wake kwa miaka elfu moja.

Mashairi haya yana mafundisho vile vile kwa watu wa kila wakati, wanaosema maneno makubwa na kinywa ambayo hawatimizi katika mwenendo wao.

**21:20-22** Wakati **wanafunzi** waliposhangaa sana juu ya kukauka mbio kwa mtini, Bwana aliwaambia kwamba waliweza kufanya maajabu makubwa kupita hili kama wakiwa na **imani.** Kwa maana, wangeweza kusema na mlima, **“Uondoshwe na kutupwa katika bahari,”** na neno hili lingefanyika. **“Na vitu vyote mutakavyoomba katika maombi, kama mukiamini mutapokea.”**

Inatupasa kueleza tena ya kwamba sharti tufahamu maombi haya kwa ‘vitu vyote’ tukikumbuka mafundisho yote mengine ndani ya Biblia juu ya maombi. Maana ya shairi 22 haiko ya kwamba Mkristo ye yote anaweza kuomba Mungu kwa kitu cho chote anachotaka na kukipokea. Sharti maombi yake yapatane na mafundisho yote katika Biblia juu ya maombi.

### E. Yesu anaulizwa juu ya amri yake (21:23-27)

**21:23** Wakati Yesu **alipoingia** kiwanja inje ya **hekalu**, **wakubwa wa makuhani na wazee** walimwuliza nani ambaye alimpa **amri** kufundisha, kufanya maajabu, na kusafisha hekalu. Walitaraji kumtega, si neno kama akitoa jibu gani. Kama akisema ana amri kwa sababu yeye ni Mwana wa Mungu, wangemshitaki na ukufuru. Kama akisema watu walimpa amri, wangesema amri hii ni bure. Akisema amri yake ilitoka kwa Mungu, watabishana na jibu lake. Walijihesabu wenyewe wachungaji wa dini, waliojifunza kazi hii, na waliowekwa na watu kuongoza watu ndani ya maneno ya dini. Yesu hakujifunza darasani na

hakupokea ruhusa wala amri toka watawala wa Waisraeli. Maulizo yao yalionyesha wivu wao wa Yesu aliyekuwa mwenye uwezo na amri toka mbinguni.

**21:24, 25** Bwana alikuwa tayari kuwaelezea amri yake kama wakikubali kujibu ulizo lake moja. “Ubatizo wa Yoane **ulitoka mbingu au kwa watu**?” Maana ya **ubatizo** wa Yoane ndiyo utumishi wa Yoane. Hivi Bwana aliuliza kama nani alimpa Yoane ruhusa kwa kazi yake? Watu au Mungu? Jibu la ulizo hili ni wazi: Yoane alikuwa ametumwa na Mungu. Alipewa uwezo *toka Mungu,* si ruhusa *toka watu*.

Makuhani na wazee watasema nini basi? Watakubali kwamba Yoane alitumwa na Mungu? Yoane aliongoza watu kuja kwa Yesu Masiya. Kama amri ya Yoane ilitoka kwa Mungu, kwa sababu gani hawakutubu na **kuamini Kristo?**

**21:26** Lakini wakisema Yoane hakutumwa na Mungu, watu watacheka jibu lao, kwa sababu zaidi yao waliamini kwamba **Yoane** alikuwa **nabii** aliyetumwa na Mungu. Kama wakijibu vizuri na kusema Yoane alitumwa na Mungu, itawapasa kujibu ulizo lao wenyewe: Yesu alikuwa Masiya ambaye Yoane alitangulia.

**21:27** Basi walikataa kujibu, wakisema hawajui pahali gani Yoane alipopata uwezo wake. Halafu Yesu alisema, **“Wala mimi siwaambii ninyi kwa amri gani ninafanya maneno haya.”** Kwa nini atawaambia neno walilokwisha kujua na wasilotaka kukubali?

### F. Mfano wa wana wawili (21:28-32)

**21:28-30** Mfano huu ni kemeo kali kwa wakubwa wa makuhani na wazee kwa sababu hawakutii mwito wa Yoane kutubu zambi zao na kuamini. Ni mfano juu ya **mtu** mmoja aliyekuwa na **wana wawili**. Aliwaomba **kutumika** ndani ya **shamba lake la mizabibu**. Mmoja wao alikataa kwenda kwanza, lakini nyuma aligeuka akakwenda. Wa pili alikubali kwenda, lakini hakwenda.

**21:31, 32** Wakati Yesu alipouliza **nani** wa wana wawili **alifanya mapenzi** ya **baba yake**, viongozi vya dini walijihukumu wenyewe kwa njia ya kusema mara moja bila kufikiri, **“Wa kwanza.”**

Halafu Bwana alionyesha maana ya mfano huu. **Watoza kodi na makahaba** walikuwa kama yule mwana wa kwanza. Hawakutii Yoane Mbatizaji mara moja, lakini kwa wakati wa nyuma wengi wao walitubu na kuamini Yesu. Viongozi wa watu kwa maneno ya dini walikuwa kama mwana wa pili. Walitenda sawasawa walikubali mahubiri ya Yoane, lakini hawakukiri zambi zao wala kuamini Mwokozi. Hivi wale waliojulikana kuwa wenye zambi kabisa waliingia ufalme wa Mungu, lakini viongozi vya dini waliotegemea haki yao wenyewe walibaki inje. Ni vivyo hivyo leo. Wale walio wenye zambi kabisa wanapokea Habari Njema mbio kupita watu wanaoonekana kuwa watu wa dini bila kuwa na imani ya kweli.

**“Yoane alikuja kwenu kwa njia ya haki,”** maana yake kwamba alikuja akihubiri ya kuwa watu wanahitaji haki kwa njia ya toba na imani.

### G. Mfano wa walimaji waovu wa shamba la mizabibu (21:33-46)

**21:33-39** Bwana Yesu aliendelea kufundisha juu ya kuwa na amri kwa njia ya kupasha **mfano** wa **mtu mmoja mwenye nyumba aliyepanda shamba la mizabibu, na kulizunguka na boma la miti,** akachimba **shimo la kukamua matunda** ndani yake, … akajenga **mnara** na kupangisha **walimaji**, **akakwenda safari** katika **inchi** nyingine. **Wakati wa matunda … alituma watumishi karibu na walimaji** waweze kupokea se-

hemu yake ya mavuno, lakini **walimaji walipiga mmoja wao, waliua mwingine, na walitupia wa tatu mawe.** Wakati **alipotuma watumishi wengine,** waliwatendea vivyo hivyo. Mara ya tatu alituma **mwana wake mwenyewe**, akifikiri **watamheshimu** yeye. Lakini walimaji, wakijua kwamba huyu alikuwa **mriti, walimwua** wakikusudi kutwaa **uriti wake.**

**21:40, 41** Halafu Bwana aliuliza makuhani na wazee kama mwenye shamba **atafanyia walimaji hawa** nini. Wakamwambia, **"Ataangamiza vibaya wale watu wabaya, na atapangisha walimaji wengine katika shamba lile la mizabibu, ambao watampa matunda yake kwa wakati wao."**

Si nguvu kuonyesha maana ya mfano huu. Mungu ndiye mwenye shamba, Israeli ni shamba la mizabibu (Zab. 80:8; Isa. 5:1-7; Yer. 2:21). Boma la miti ni sheria ya Musa iliyotenga Israeli na Mataifa na kuwachunga kuwa taifa kwa Bwana tu. Shimo la kukamua matunda ndani yake linatufikirisha matunda ambayo ingalipasa Israeli kuzaa kwa Mungu. Mnara unatukumbusha namna Bwana anavyolinda watu wake. Walimaji ndio wakubwa wa makuhani na waandishi.

Mungu alituma watumishi wake manabii tena na tena karibu na Waisraeli akitafuta ndani ya shamba hili la mizabibu matunda ya ushirika, utakatifu na mapendo. Lakini watu walitesa manabii na kuua wengine katikati yao. Mwishoni Mungu alituma Mwana wake, akisema, "Wataheshimu mwana wangu" (sh. 37). Makuhani walisema, "Huyu ni mriti." Walikubali katikati yao kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu (hata kama walikataa kweli hii mbele ya watu) na kwa njia hii walijibu ulizo lao juu ya amri yake. Alikuwa mwenye amri kwa sababu alikuwa Mwana wa Mungu.

Ndani ya mfano walisema "Huyu ni mriti. Kujeni tumwue na kutwaa uriti wake" (sh.38). Kwa hakika walisema, "Kama tukimwacha hivi, watu wote watamwamini, na Waroma watakuja na kuondoa pahali petu na taifa letu vilevile" (Yn. 11:48). Basi walimkataa, walimtupa inje na kumsulibisha.

**21:42** Wakati Mwokozi alipouliza kama mwenye shamba la mizabibu atafanya nini, jibu lao liliwahukumu, kama anaonyesha ndani ya mashairi 42 na 43. Alisema maneno toka Zaburi 118:22, **"Jiwe wajengaji walilokataa limekuwa kichwa cha pembe. Neno hili limetoka kwa Bwana nalo ni ajabu machoni mwetu."** Wakati Kristo, Jiwe, alipotokea mbele ya wajengaji – viongozi vya Israeli, nafasi haikupatikana kwaye ndani ya ramani ya majengo yao. Walimweka kando kama jiwe lisilo na faida. Lakini nyuma ya mauti yake alifufuliwa toka wafu na kupewa pahali pa juu zaidi ndani ya jengo la Mungu: "Mungu alimtukuza sana na kumpa jina lililo juu ya kila jina …" (Flp. 2:9).

**21:43** Halafu Yesu alitangaza waziwazi ya kwamba Israeli **wataondolewa ufalme wa Mungu, nao utaletwa kwa taifa lingine, wenye kuzaa matunda yake.** Na ilitokea hivi. Israeli wamewekwa kando kama watu wachaguliwa wa Mungu, na kuhukumiwa na upofu. Mioyo ya watu wa taifa waliokataa Masiya wao ilitiwa ugumu. Unabii kwamba **ufalme utaletwa kwa taifa lingine wenye kuzaa matunda yake** unaelezwa kuwa: (1) kanisa la waamini Wayuda na watu wa Mataifa walioamini – "taifa takatifu, watu walio mali ya Mungu mwenyewe" (1 Pet. 2:9); au (2) sehemu ya Israeli watakaokuwa waamini hai kwa wakati Bwana atakapokuja mara ya pili. Waisraeli wakombolewa watazaa matunda kwa Mungu.

**21:44 "Naye anayeanguka juu ya jiwe hili atavunjikavunjika; na kila mtu ambaye litamwangukia, litamsagasaga."** Ndani ya sehemu ya kwanza ya shairi hili, **jiwe** ni chini kwa udongo; ndani ya sehemu ya pili, linashuka chini toka juu. Maneno haya yanatufikirisha kuja mbili kwa Kristo. Wakati alipokuja mara ya kwanza, viongozi vya Wayuda walikwaa kwa sababu yake na kuvunjika vipande vipande. Wakati atakapokuja tena, atashuka na hukumu, akisambaza adui zake kama vumbi.

**21:45,46** Wakubwa wa makuhani na Wafarisayo walifahamu kwamba **mifano** hii ilikuwa zaidi jibu kwa ulizo lao juu ya amri ya Kristo. Walitaka sana kumkamata saa ile ile, lakini **waliogopa makutano, ambao waliheshimu** Yesu kama **nabii**.

### H. Mfano wa karamu ya arusi (22:1-14)

**22:1-6** Yesu alikuwa na maneno mengine kusema na wakubwa wa makuhani na Wafarisayo. Ndani ya mfano wa **karamu** ya arusi alionyesha tena ya kwamba taifa barikiwa la Israeli watawekwa kando, na mataifa wazarauliwa watapokewa kama wageni kwa meza yake. Alisawanisha **ufalme wa mbinguni** na **mfalme aliyetayarisha karamu ya arusi kwa mwana wake**. Kwanza, alituma watumishi kujulisha na kuita watu mmoja mmoja, lakini wale walioitwa walikataa kufika. Nyuma yake alitangaza ya kwamba karamu ilikuwa tayari. Watu wengine waliizarau, wengine walikuwa na kazi nyingi ya mashamba na kazi ya biashahara, na wengine **walikamata** na nguvu watumishi waliotumwa na mfalme, waliwatendea vibaya na **kuwaua**.

**22:7-10** Mfalme **alikasirika** sana na **kuharibu wauaji wale na kuteketeza mji wao.** Hakuita tena wale walioitwa mbele, lakini aliita mtu ye yote aliyetaka kufika aje. Mara hii viti vyote vilijazwa na watu ndani ya **chumba kikubwa cha arusi.**

**22:11-13** Lakini mmoja wa **wageni** hakuvaa **vazi la arusi**. Wakati mfalme alipomwuliza juu ya neno hili, **hakuwa na neno la kusema**. Mfalme aliagiza atupwe katika giza la inje; **kutakuwa kulia na kusaga meno.** Watumwa hawa ndani ya shairi 13 ni mbali na watumwa ndani ya shairi 3.

**22:14** Bwana alimaliza mfano huu na maneno haya, **"Kwani wao wanaoitwa ni wengi, lakini wale wanaochaguliwa ni wachache."**

Hii ndiyo maana ya mfano huu: Mfalme ndiye Mungu, na mwana wake ni Bwana Yesu. Karamu ya arusi inatufikirisha furaha ya ufalme wa mbingu. Mfano huu ni zaidi juu ya kuwekwa kando kwa Israeli – si juu ya mwito wa kanisa, wala hali ya kanisa kwa wakati wa kuja.

Watumishi wa kwanza waliotumwa kuita watu kwa karamu ni mfano wa Yoane Mbatizaji na mitume kumi na wawili walioita Israeli kwa karamu ya arusi. Lakini taifa la Israeli "walikataa kuja" (sh.3). Neno hili lilionekana wazi wakati waliposulibisha Kristo.

Nyuma yake alitangaza ya kwamba karamu ilikuwa tayari. Tangazo hili linatufikirisha kutangazwa kwa Habari Njema kwa Wayuda katika Matendo. Watu wengine walitendea vibaya watumishi waliotumwa na mfalme. Zaidi ya mitume waliuawa kwa sababu ya imani yao.

Mfalme alikasirikia Israeli, akatuma "majeshi yake," maana yake Tito, mfalme Mroma na majeshi yake, kuangamiza Yerusalema na kuua zaidi ya wenyeji wake kwa mwaka 70 A.D. Yaliitwa "majeshi yake" kwa sababu Mungu alitumika nao kuazibu Israeli. Walikuwa majeshi yake hata kama hawakumjua.

Sasa taifa la Israeli linawekwa kando, na Habari Njema inahubiriwa kwa Mataifa, "waovu na wazuri," ndio namna namna (Mdo. 13:45,46; 28:28). Lakini imani ya kila mtu anayekuja inapimwa. Mtu huyu aliyekosa vazi la arusi alisema yeye ni tayari kwa ufalme, lakini hakuvalishwa na haki ya Mungu kwa njia ya Bwana Yesu Kristo (2 Kor. 5:21). Kama mwalimu Ryrie alivyo-onyesha, ilikuwa desturi kwa wakati ule kusaidia wageni na vazi la arusi kama walikosa vazi la kufaa. Lakini mtu huyu hakupokea vazi lenyewe. Bila Kristo, hakuwa na neno la kusema wakati alipo-ulizwa kwa nini alifikiri alistahili ku-ingia ufalme (Rom. 3:19). Alihukumwa na kutupwa katika giza la inje, pahali pa kulia na kusaga meno. Kulia kuna-tukumbusha mateso ya Gehena. Watu wengine wanafikiri kusaga meno ni mfano kwamba wale walio katika Gehena wataendelea na roho ya ku-chukia na kuasi Mungu. Kama ni hivi, maneno haya yanaonyesha kwamba moto wa Gehena hautakasi roho zao, kama watu wengine wanavyofundisha, ndiyo mafundisho ya uwongo.

Shairi 14 linasema juu ya mfano mzima, si juu ya mtu huyu aliyekosa vazi la arusi tu. **Wao wanaoitwa ni wengi,** maana yake Habari Njema inahubiriwa kwa watu wengi. **Lakini wale wanaochaguliwa ni wachache.** Wengine wanakataa mwito mwenyewe. Wengine wa wale ambao wanaupokea wanaonekana nyuma kwamba hawaku-amini kweli. Wote wanaoitika Habari Njema wanachaguliwa. Mtu anaweza kufahamu kwa njia moja tu kama alicha-guliwa. Ni kujua kama aliitika mwito wa Bwana Yesu, na anamfuata. Mwalimu mmoja (Jennings) alisema: "Wote wana-itwa kushiriki ndani ya karamu, lakini si kila mtu anayeamini kwamba Mwenye Kutayarisha Karamu atampatia vazi linalohitajiwa kwa karamu yenyewe."

**I. Kutoa kwa Kaisari na kwa Mungu (22:15-22)**

Ndani ya sura 22 wajumbe namna tatu za watu walitumwa kutega Mwana wa Mungu.

**22:15,16** Kwanza **Wafarisayo** na **Waherode** walifika karibu naye. Wa-farisayo na Waherode walichukiana, lakini walipatana kwa muda mfupi sasa kwa sababu wao wote walichukia Mwokozi. Walikusudi kusukuma Kristo kusema neno ambalo litamwingiza ndani ya matata na serikali na watu. Walijua kwamba Wayuda walikuwa na mawazo mbalimbali juu ya kutawaliwa na Kaisari. Wengine hawakutaka hata kidogo kunyenyekea mtawala mtaifa. Wengine, kama Waherode, hawakufikiri neno hili ni vibaya sana.

**22:17** Kwanza walisifu Bwana na hila juu ya usafi wake wa roho na juu ya roho yake ya kweli na uhodari wake. Kisha walimwuliza, **"Ni halali kumpa Kaisari kodi, au sivyo?"**

Kama Yesu angalijibu, "Hapana," angaliongeza uadui wa Waherode, na vilevile watu wangalimshitaki juu ya kuasi serikali ya Waroma. Wafarisayo wangalimshitaki mara moja kwa seri-kali. Kama angalijibu, "Ndiyo," wengi wa Wayuda wasio na cheo – watu tu, wangaliacha kumfuata. Ni watu wale waliozuiza viongozi kufika saa ile wasimwue.

**22:18,19** Yesu aliwashitaki wazi kuwa **wadanganyifu** waliojaribu kumtega. Halafu alisema nao kumwonyesha di-nari, ndiyo feza iliyotumiwa kulipa kodi kwa serikali ya Waroma. Kila mara Wayuda waliyoona mfano na jina la Kaisari juu ya feza hii walikumbushwa kwamba iliwapasa kulipa kodi kwa Mataifa ambao waliwatawala. Ingali-pasa dinari kuwakumbusha ya kwamba walikuwa watumwa wa Waroma kwa sababu ya zambi zao. Kama wasingali-kwenda mbali na BWANA kama wasi-

ngalilazimishwa kulipa kodi kwa Kaisari.

**22:20, 21** Yesu aliwauliza, **"Mfano huu ni wa nani, na anwani hii?"** Ilikuwa lazima kwao kujibu, "Ni ya **Kaisari.**" Halafu Bwana aliwaagiza, **"Lipeni Kaisari yaliyo ya Kaisari, na Mungu yaliyo ya Mungu."**

Ulizo la Wafarisayo halikutimiza kusudi lao. Walitaka kutega Yesu juu ya kulipa kodi kwa Kaisari, lakini Yesu alionyesha kwamba walikuwa wamekosa kulipia Mungu kodi. Hata kama walichukia kulipa kodi kwa Kaisari walifanya hivi, lakini walikuwa wamekosa kutii maagizo ya Mungu kwa maisha yao. Basi Yule aliyesimama mbele yao alikuwa "chapa ya nafsi" ya Mungu mwenyewe (Ebr. 1:3), lakini hawakumpa heshima ambayo alistahili kupokea.

Jibu la Yesu linaonyesha ya kwamba mwamini ni mwenyeji wa inchi mbili. Ni lazima kwake kutii serikali ya inchi yake duniani na kulipa kodi yake. Haifai kwake kusema maneno mabaya juu ya watawala wa inchi yake wala kuwaangamiza. Anaagizwa kuombea watawala wake. Na kama mwenyeji wa mbingu, inampasa kutii Mungu. Kama maagizo ya watawala wake ni mbali na yale ya Mungu, inampasa kutii Mungu (Mdo. 5:29).

Wakati sisi watu tunapotaja shairi 21 wengi wetu tunaweka roho sana juu ya kulipa Kaisari, lakini si juu ya kutii Mungu – ndilo kosa ambalo Yesu alihamakia Wafarisayo juu yake!

**22:22 Wakati** Wafarisayo **waliposikia** jibu hili walifahamu kwamba walishindwa. Walishangaa, wakakwenda zao.

### J. Wasadukayo na fumbo lao juu ya ufufuko (22:23-33)

**22:23, 24** Tuliona mbele kwamba Wasadukayo walikuwa walimu wasioamini kwamba miili ya watu itafufuliwa nyuma ya kufa kwao. Na hawakuamini ya kwamba kuna malaika na maajabu. Hesabu ya maneno waliyokataa kuamini ilipita hesabu ya maneno waliyokubali.

Wasadukayo wengine **walifika karibu na Yesu** na habari za kuchekesha juu ya ufufuko. Walimkumbusha sheria moja juu ya ndoa (Tor. 25:5). Sheria hii iliagiza kwamba Mwisraeli akikufa bila kuzaa **watoto**, **ilipasa ndugu yake mume kuoa** mjane wake kuchunga jina la jamaa hii, na uriti wake ubaki ndani ya jamaa ile vilevile.

**22:25-28** Fumbo lao lilikuwa juu ya mwanamke aliyekufiwa mume wake, kisha aliolewa kwa mmoja wa ndugu za mume. Ndugu huyu ya pili alikufa vilevile, hivi alioa ndugu ya tatu, vivi hivi, kufika ndugu yake ya saba. Mwishoni **mwanamke alikufa** vilevile. Halafu Wasadukayo waliendelea na ulizo lao ambalo walifikiri litahayarisha Bwana aliye ufufuko na uzima (Yn. 11:25): **"Basi katika ufufuko atakuwa mke wa nani katika wale saba? Maana wao wote walikuwa naye."**

**22:29** Walifikiri mafundisho juu ya ufufuko ni ngumu kufahamu, hivi ufufuko si neno la kweli. Yesu alijibu kusema kwamba mafundisho haya hayakuwa ngumu, lakini wao walikuwa wajinga kwa sababu hawakujua **maandiko** wala **uwezo wa Mungu**.

**Hawakujua Maandiko**. Biblia haifundishi ya kwamba watu wataoana mbinguni kama hapa duniani. Wanaume watakaa kuonekana kama wanaume na wanawake kama wanawake, lakini watakuwa kama malaika wasiooa wala kuolewa.

Na hawakujua **uwezo wa Mungu**. Huyu aliyeumba watu toka mavumbi aliweza vilevile kufufua mavumbi ya wale waliokufa na kuyafanyiza tena kuwa na miili ya utukufu.

**22:30-32** Halafu Bwana alionyesha mfano toka Maandiko ya kwamba ufufuko ni neno la sharti. Katika Kutoka 3:6

Mungu alijiita mwenyewe **Mungu wa Abrahamu, … Isaka, na … Yakobo.** Na Yesu alionyesha kwamba **"Mungu si Mungu wa wafu, lakini wa walio hai."** Mungu alifanya maagano na watu hawa, lakini walikufa mbele ya kutimizwa kwa maagano haya. Basi namna gani Mungu aliweza kusema juu yake mwenyewe kama Mungu wa wanaume hawa watatu wenye maiti kaburini? Namna gani Huyu asiyeweza kukosa kutimiza ahadi zake ataweza kutimiza zile ambazo alitolea watu hawa waliokwisha kufa? Kuna jibu moja tu, kwa njia ya ufufuko.

**22:33** Wakati **makutano** haya waliposikia **mafundisho yake walishangaa sana;** nasi tunashangaa vivyo hivyo!

**K. Amri iliyo kubwa (22:34-40)**

**22:34-36 Wakati Wafarisayo waliposikia** kwamba Yesu alikuwa **amenyamazisha** adui zao **Wasadukayo,** walifika kusemana na Yesu. Mtu yule aliyesema kwa ajili yao alikuwa **mwana sheria**, akaomba Yesu kuonyesha katika torati amri gani iliyo kubwa.

**22:37, 38** Na maarifa mengi Bwana Yesu alijumlisha deni ya mtu kwa Mungu kwa njia ya **amri iliyo kubwa: "Upende Bwana Mungu wako na moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote."** Marko aliongeza "na kwa nguvu zako zote" (Mk. 12:30). Ni kusema kwamba deni ya kwanza ya mtu ni kupenda Mungu na roho yake nzima, maana yake na moyo na nia na nguvu yake yote.

**22:39-40** Yesu aliendelea kuonyesha deni ya pili ya mtu ni **kupenda jirani yake** kwa kipimo anachojipenda mwenyewe. Inatupasa kuwaza mara nyingi juu ya maneno haya, **"Penda jirani yako kama wewe mwenyewe."** Tufikiri na kukumbuka ya kwamba tunajipenda wenyewe sana, na tunafanya maneno mengi kujisaidia wenyewe, ili tuweze kukaa vizuri na bila shida. Halafu tufikiri kama ingekuwa namna gani kwa sisi kuonyeshea jirani yetu mapendo makubwa namna hii! Si desturi ya watu wa dunia kufanya hivi. Inawezekana kwa wale tu waliozaliwa tena, na kwa wale wanaoacha Kristo kutumika nao kufanya hivi.

**L. Mwana wa Daudi ni Bwana wa Daudi (22:41-46)**

**22:41,42 Wakati Wafarisayo walipokuwa wakishangaa kwanza** juu ya jibu la Yesu kwa mwana sheria, Yeye aliwauliza neno gumu. **"Munafikiri nini juu ya Kristo? Yeye ni Mwana wa nani?"**

Zaidi ya Wafarisayo hawakuamini kwamba Yesu alikuwa Kristo; wakakaa kungojea kuja kwa Masiya. Hivi Yesu hakuwauliza, "Munafikiri nini juu yangu?" lakini kama Masiya atakuwa Mwana wa nani wakati atakapotokea.

Walijibu vizuri ya kwamba atakuwa mzao wa **Daudi**.

**22:43,44** Halafu Bwana Yesu alitaja Zaburi 110:1 pahali Daudi aliposema, **"BWANA alimwambia Bwana wangu, 'Uketi kwa mkono wangu wa kuume, hata ninapoweka adui zako chini ya miguu yako.'"** "BWANA" wa kwanza ndiye Mungu Baba, na Bwana wa pili ndiye Masiya. Hivi Daudi alisema juu ya Masiya kama Bwana wake.

**22:45** Halafu Yesu aliwauliza, **"Basi Daudi akimwita Bwana, yeye ni mwana wake namna gani?"** Jibu la ulizo hili ndilo ya kwamba Masiya ni Bwana wa Daudi na Mwana wake vilevile – yeye ni Mungu na Mtu. Kama Mungu alikuwa Bwana wa Daudi; kama Mtu alikuwa Mwana wa Daudi.

Kama Wafarisayo wangalikuwa na roho tayari kupokea mafundisho, kama wangalifahamu kwamba Yesu alikuwa Masiya – Mwana wa Daudi kwa njia ya Maria, na Mwana wa Mungu, kama masemo, mwenendo na maajabu yalivyoonyesha.

**22:46** Lakini walikataa kufahamu maneno haya. Walishindwa kabisa na hekima yake na waliacha kujaribu kumtega na maulizo. Kutoka saa ile walikusudi kujaribu kumwondosha kwa njia nyingine, ndiyo *jeuri.*

### M. Maonyo juu ya masemo yasiyopatana na mwenendo (23:1-12)

**23:1-4** Kwa mwanzo wa sura hii Mwokozi alionya makutano na **wanafunzi wake** wakae na ange kwa masemo ya **waandishi na Wafarisayo**. Viongozi hawa waliketi katika kiti cha Musa, maana walifundisha sheria ya Musa. Mara nyingi mafundisho yao yalikuwa mazuri, lakini hayakupatana na matendo yao. Masemo yao hayakupatana na mwenendo wao. Hivi Yesu alisema, **"… Maneno yote ambayo wanawaambia ninyi kutenda, muyashike na kuyatenda, lakini musitende kwa mfano wa matendo yao; kwa maana wanasema, lakini hawatendi."**

Wafarisayo waliagiza watu kufanya mambo magumu, lakini hawakuwasaidia kuyafanya.

**23:5** Walitimiza kawaida ya dini kusudi watazamwe na watu, si na roho ya kweli kutaka kupendeza Mungu. Ni kwa sababu hii walitumia hirizi. Wakati Mungu alipoagiza Israeli kufunga maneno yake kama alama juu ya mikono yao na kama pindo katikati ya macho yao (Kut. 13:9, 16; Tor. 6:8; 11:18), alikusudi wakumbuke sheria wakati wote na kuongozwa nayo ndani ya matendo yao. Wakati Yesu alipokuwa duniani watu hawakukumbuka tena maana ya roho ya hirizi hizi, hata kama walitii agizo hili katika miili yao. Walifunga sehemu za Maandiko ndani ya sanduku ndogo za ngozi na kuzifunga kwa paji la nyuso yao au mikono yao. Hawakuweka roho juu ya kutii sheria, lakini kwa njia ya kuvaa hirizi hizi zilizokuwa kubwa kupita kipimo walionekana kama watu watakatifu kabisa. Sheria iliagiza watu kuvaa vishada vya rangi ya samawi katika mapindo ya mavazi yao (Hes. 15:37-41; Tor. 22:12). Kazi ya vishada hivi ilikuwa kuwakumbusha ya kwamba walikuwa watu namna nyingine, na ya kwamba iliwapasa kutengwa na mataifa mengine kwa njia ya mwenendo wao. Wafarisayo hawakufikiri juu ya mafundisho ya roho ya vitu hivi hata kama walikaa kufanya vishada hivi virefu kupita.

**23:6-8** Walionyesha kiburi yao kwa njia ya kuketi kwa pahali pa mbele **kwa karamu** na **katika masunagogi.** Walifurahi kwa watu **kuwasalimu kwa pahali pa soko** na kuitwa **Rabi** (maana yake "mwalimu").

**23:9,10** Halafu Bwana alionya wanafunzi wake tena juu ya kuita watu na majina yanayofaa kwa Mungu tu. Aliwakataza kuitwa rabi kwa sababu tuna **Mwalimu mmoja, ndiye Kristo**. Na haifai kuita mtu ye yote **baba** kwani Mungu ni **Baba** yetu.

Maana ya masemo haya ya Mokozi ni wazi. Katika ufalme wa mbinguni waamini wote ni sawasawa, bila wengine kuitwa na majina ya kuwaheshimu kupita wengine. Lakini kwa wakati wa sasa watu wengine wanaheshimwa na majina mbalimbali, kama Révérend, Père, Docteur (maana yake mwalimu katika kiroma), vivi hivi. Maonyo haya ni kwa maneno ya *roho*, si kwa utaratibu wa watu hapa duniani. Si vibaya kwa mtoto kuita mtu "Baba" yake, au kwa mgonjwa kuita mtu "Mganga." Kwa dunia hii ya sasa inatupasa kuwapa "wote haki zao … mwenye kustahili heshima, heshima" (Rom. 13:7).

**23:11,12** Hapa tunaona tena ya kwamba ufalme wa mbinguni ni namna nyingine kabisa na falme za dunia. Yesu alisema, **"Yeye aliye mkubwa katikati yenu atakuwa mtumishi wenu. Naye anayejitukuza mwenyewe, atanyenyekezwa; naye anayejinyenyekeza,**

**atatukuzwa."** Wale walio wakubwa kweli wanajinyenyekeza kutumikia wengine. Wafarisayo ambao wanajitukuza wenyewe watashushwa. Wafuata wa kweli ambao wanajinyenyekeza watatukuzwa nyuma.

**N. Waandishi na Wafarisayo wanalaumiwa (23:13-36)**

Bwana Yesu alitangaza ole nane kwa wadanganyifu wa wakati ule. Ole hizi si "malaana," lakini zinaonyesha huzuni ya Bwana kwa sababu ya mwisho wao wa taabu.

**23:13 Ole** ya kwanza ilikuwa kwa sababu walikataa wao wenyewe kuingia **ufalme,** na waliweka roho juu ya kuzuiza watu wengine **wasiuingie**. Mara nyingi viongozi vya watu kwa maneno ya dini ni wenye kushindana na nguvu zaidi na Habari Njema ya wokovu. Wanaweza kuwa na roho nzuri ya uvumilivu kwa neno lo lote ila habari njema ya wokovu. Watu wa dunia hawataki kupokea neema ya Mungu, na hawataki Mungu kuonyesha neema kwa watu wengine.

**23:14** Ole ya pili ilikemea wale ambao walijikamatia **nyumba za wajane** na kuficha matendo yao maovu kwa njia ya **maombi marefu**. Hata kwa wakati wa sasa viongozi vya dini za uwongo wanasukuma wajane wazee, waamini wasiofahamu vizuri, kutoa nyumba na vitu vyao kwa "kanisa." Wadanganyifu namna hii **watapata hukumu iliyo kubwa zaidi.**

**23:15** Ole ya tatu ilikuwa kwa wenye bidii sana kwa neno lisilo jema. Wanasumbuka sana kufanya mtu mmoja kuwa mgeuzi, lakini wakati walipokwisha **kumpata** wanamfundisha kuwa mwovu **mara mbili** zaidi kuliko wao wenyewe. Kwa wakati wa sasa wafuata wa dini ya uwongo ni tayari kufikia nyumba 700 kupata mfuata mmoja mwingine kwa dini yao, lakini mwisho wa masumbuko yao ni mtu mwovu kabisa.

**23:16-22** Kemeo la ine la Bwana lilikuwa juu ya namna walitumika na akili yao kwa udanganyifu. Walikuwa wamesimamisha utaratibu kuepuka kulipa mali ambayo waliapa kutoa. Kwa mfano, walifundisha ya kwamba ukiapa kwa **hekalu**, si lazima kwako kulipa, lakini ukiapa kwa **zahabu ya hekalu,** sharti utimize kiapo chako. Walisema ya kwamba ukiapa kwa zawadi juu ya mazabahu, lazima utimize kiapo hiki, lakini hukuhitaji kutimiza kiapo kwa mazabahu yasiyo na zawadi juu yake. Hivi kwa macho yao zahabu ilikuwa na damani kupita Mungu (hekalu lilikuwa nyumba ya Mungu), na zawadi juu ya mazabahu (mali namna yo yote) ilikuwa na damani kupita mazabahu. Waliweka roho juu ya mambo ya dunia kupita mambo ya roho. Waliweka roho juu ya kupokea (zawadi) kupita juu ya kutoa (mazabahu yalikuwa pahali pa kutoa).

Akiita wasikiaji wake **viongozi wapofu** Yesu alionyesha udanganyifu wao wazi. Zahabu ya hekalu ilikuwa na damani tu kwa sababu ilikuwa sehemu ya nyumba ya Mungu. Ilikuwa mazabahu tu iliyoleta damani kwa zawadi juu yake. Watu wanaofikiri zahabu yenyewe ni kitu cha damani ni wapofu; inapata damani tu wakati inapotumiwa kwa utukufu wa Mungu. Zawadi zinazoletwa na kusudi la tamaa ya mwili ni bure; zile zinazoletwa kwa jina la Bwana zina damani ya milele.

Viapo vyo vyote vya Wafarisayo vilitolewa kwa sababu ya Mungu, na vilikuwa lazima kwao kutimiza viapo hivi. Haiwezekani kwa mtu kuepuka neno hili kwa njia ya kutumika na akili yake ya udanganyifu. Ni sharti kabisa kwa watu kutimiza viapo na ahadi.

**23:23, 24** Ole ya **tano** ilikuwa juu ya matendo ya kawaida ya dini yasiyotoka kwa roho. **Waandishi na Wafarisayo**

waliweka roho sana juu ya kutolea Bwana zaka ya mboga ndogo walizopanda mashambani mwao. Yesu hakuwahukumu juu ya kutii Mungu ndani ya maneno haya madogo, lakini aliwakemea na ukali kwa sababu hawakutendea watu wengine kwa **haki, rehema,** na imani. Alitumika na mfano wa kuchuja **imbu** na kumeza **ngamia** kuonyesha kwamba ni kitu cha kuchekesha kuweka roho sana juu ya maneno yale madogo na neno baya sana kuona bure zambi kubwa kama udanganyifu na hila na ukali, na choyo.

**23:25, 26 Ole** ya sita ilikuwa juu ya bidii ya Wafarisayo kujaribu kuonekana kama watu wa kufuata dini kabisa na wenye mwenendo safi, lakini mioyo yao ilijaa na desturi ya **kulipiza watu kwa jeuri** na **kujipendelea wenyewe. Sharti wasafishe kwanza ndani ya kikombe na sahani,** maana wasafishe mioyo yao na toba na imani. Nyuma yake, na kwa njia hii moja tu, watakuwa wenye mwenendo wa kukubaliwa. Sisi watu tunataka sana watu watuone kama watu wema, lakini Mungu anaangalia roho zetu, kama roho zetu ni safi na njema mbele yake. Anataka kweli moyoni (Zab. 51:6).

**23:27,28 Ole** ya saba ni juu ya kuonekana kwa inje vilevile. Ole ya sita ilikuwa kemeo kali juu ya kuficha tamaa ya mali, lakini ole ya saba inahukumu kuficha **udanganyifu na uovu.**

Makaburi yalipakaliwa pembe ili Wayuda wasiyaguse bila kusudi, na kuchafuwa kwa dini yao. Yesu alisawanisha waandishi na Wafarisayo na **makaburi yaliyopakaliwa pembe** yaliyoonekana safi inje, lakini yaliyojaa mifupa ya wafu. Watu walifikiri watatakaswa kwa njia ya kuwa pamoja na viongozi hawa wa dini, lakini walichafuwa rohoni kwa sababu ya udanganyifu na uovu wao.

**23:29, 30 Ole** ya mwisho ilikuwa kwa **waandishi na Wafarisayo** waliotenda sawasawa waliheshimu **manabii** wa Agano la Kale kwa njia ya kujenga au kutengeneza **makaburi** yao na kupamba nguzo za ukumbusho zao. Ndani ya hotuba zao juu ya manabii walisema **wasingalishiriki** na wazazi wao wakati walipoua **manabii**.

**23:31** Yesu alisema nao, **"Hivi munajishuhudia wenyewe ya kwamba ninyi ni wana wao walioua manabii."** Lakini walishuhudu neno hili namna gani? Ni kama shairi 30 linaonyesha kwamba walijitenga na baba zao walioua manabii. Kwanza, walikubali kwamba baba zao (ambao waliwazaa) walimwanga damu ya manabii. Lakini Yesu alitumika na neno hili **wana** na maana ya watu wenye tabia namna yao. Alijua ya kwamba hata saa ile walipopamba makaburi ya manabii walifanya shauri namna watakavyomwua yeye. Neno la pili, wakati walipoonyesha heshima namna hii kwa manabii waliokwisha kufa, ni kama walisema, "Tunapenda manabii waliokufa tu." Kwa njia hii walikuwa wana wa baba zao vilevile.

**23:32** Halafu Bwana wetu aliongeza, **"Jazeni basi kipimo cha baba zenu."** Baba zao walikuwa wamejaza kikombe cha uuaji nusu kwa njia ya kuua manabii. Bado kidogo waandishi na Wafarisayo watakijaza tele kwa njia ya kuua Bwana Yesu na wafuata wake, na hivi kufikisha kwa mwisho wa kuogofya kabisa kazi ambayo baba zao walianza.

**23:33** Saa ile Kristo wa Mungu alisema maneno haya ya kushitusha kabisa, **"Ninyi nyoka, ninyi wana wa majoka, mutakimbia hukumu ya Gehena namna gani?"** Mungu wa mapendo katika mwili wa mtu anaweza kusema maneno makali namna hii? Ndiyo, kwa sababu inapasa mapendo ya kweli kuwa haki na takatifu vilevile. Yesu si mtengenezaji zaifu anayejuana

na mapendo tu. Ni lazima kwa mwenye mapendo kuwa mwenye haki vilevile.

Ni neno la kuogopesha kukumbuka kwamba maneno haya makali ya hukumu yalisemwa kwa viongozi wa dini, si kwa walevi na waovu. Kwa wakati wa sasa Wakristo wengine wana-fungana na kushiriki na adui za msalaba wa Kristo, na inatupasa kukumbuka mfano wa Yesu, na maneno Yehu aliyo-sema na Yehosafati, "Imekupasa ku-saidia waovu, na kuwapenda wenye kuchukia BWANA?" (2 Mam. 19:2).

**23:34, 35** Pamoja na kufahamu kwa-mba yeye mwenyewe atauawa Yesu ali-waambia waandishi na Wafarisayo wazi kwamba wataua wengine wa wajumbe ambao atatuma – **manabii na watu wenye akili na waandishi**. Wengine watakaoepuka mauti watawapiga katika **masunagogi,** na kuwafukuza **mji kwa mji**. Kwa njia hii viongozi wa dini wata-jivimbishia hatia ya uuaji wa watu wa Mungu wote tangu zamani. Juu yao itakuwa **damu yote ya haki iliyo-mwangika duniani, toka damu ya Abeli, mwenye haki, … hata … damu ya Zekaria**. Habari za kufa kwake zi-liandikwa kwa 2 Mam. 24:20,21, kitabu cha mwisho ndani ya Biblia kwa Kiebra-nia. (Huyu si Zekaria aliyeandika kitabu cha Zekaria katika Agano la Kale.)

**23:36** Hatia ya miaka yote iliyopita itakuwa juu ya **kizazi** au taifa ambacho Kristo alisema nao, kama kufunga pamoja kumwangika kwa damu ya watu wote waliouawa bila kustahili kufa, na uuaji wa Mwokozi asiyekuwa na kosa. Hukumu kali sana itapata taifa lile waliochukia Masiya wao bila sababu, na kumfunga juu ya msalaba wa mvunja sheria.

### O. Maombolezo ya Yesu juu ya Yerusalema (23:37-39)

**23:37** Ona ya kwamba sura hii, ina-yojaa na matangazo ya ole ya Bwana Yesu kupita karibu sura zote nyingine, inakwisha na machozi yake! Nyuma ya kushitaki Wafarisayo na uchungu sana, alitaja jina la **Yerusalema** mara mbili ndani ya maombolezo yake na huzuni kubwa kwa sababu mji ule ulikuwa umepoteza njia yake ya wokovu. Watu wa mji ule walikuwa wameua **manabii** na kutupia wajumbe wa Mungu mawe, lakini Bwana alipenda mji huu hata hivi. Alitaka mara nyingi kukusanya watoto wake kwake – **kama vile kuku ana-vyokusanya watoto wake** chini ya mabawa yake … **lakini hawakutaka.**

**23:38** Bwana alimaliza maombolezo yake na kusema, **"Tazameni, nyumba yenu imeachwa kwenu tupu."** Neno hili "nyumba" hapa linasema kwanza juu ya hekalu, lakini labda linasema juu ya mji wa Yerusalema na taifa la Israeli vilevile. Kutakuwa na muda wa hesabu fulani ya miaka nyuma ya mauti ya Kristo na kuja kwake mara ya pili. Kwa muda ule Waisraeli wasioamini hawa-tamwona (nyuma ya ufufuko wake waamini tu walimwona).

**23:39** Shairi 39 linatazamia kuja kwake kwa pili wakati Waisraeli we-ngine watakapompokea kama Masiya-Mfalme wao na kusema, **"Amebari-kiwa anayekuja kwa jina la Bwana."**

Wauaji wa Kristo hawatakuwa na njia kuokolewa. Alisema na Yerusa-lema, na wenyeji wa mji, na kwa taifa la Israeli zima. Nyuma ya kufa kwake wenyeji wa Yerusalema hawatamwona tena kufika wakati watakapomtazama ambaye walimchoma, na watamwo-mbolezea kama mtu anavyoombolezea mwana wake mzaliwa pekee (Zek. 12:10). Kwa Wayuda maombolezo kwa mwana mzaliwa wa pekee ni machungu kupita yote.

## 13. HOTUBA KWA MLIMA WA MIZEITUNI (Sura 24, 25)

Hotubu hii ni unabii juu ya muda wa Mateso na kuja kwa pili kwa Bwana. Ni zaidi juu ya taifa la Israeli, katika

Palestina. Tunasoma "wale walio katika Yudea wakimbie kwa milima" (Mt. 24:16); "Ombeni ili kukimbia kwenu kusiwe ... siku ya sabato" (Mt. 24:20). "Wachaguliwa" (Mt. 24:22) ndio *wachaguliwa Wayuda,* si kanisa. Hatusomi juu ya kanisa ndani ya unabii huu, wala ndani ya mifano ya hotuba hii.

**A. Yesu anatabiri kwamba hekalu litaharibiwa (24:1, 2)**

Tunasoma kwanza ya kwamba **Yesu akatoka hekaluni, akakwenda zake** – ndizo habari za maana kabisa wakati tunapokumbuka maneno yake ya mwisho ya sura 23, "… nyumba yenu imeachwa kwenu tupu." Yanatufikirisha maneno ya Ezekieli juu ya kuondoka kwa utukufu toka hekalu (Eze. 9:3; 10:4; 11:23).

Wanafunzi walitaka Bwana kusifu mapambo ya hekalu pamoja nao. Waliwaza zaidi juu ya maneno ya dunia yatakayopita, si na maneno ya milele. Yesu aliwajulisha kwamba jengo hili litaharibiwa kabisa na **halitabaki jiwe juu ya jiwe pasipo kubomolewa**. Tito, mtawala wa Roma, alijaribu sana kuponyesha hekalu, lakini askari zake waliliteketeza na kutimiza unabii wa Yesu. Wakati moto ulipoyeyusha zahabu, iliingia katikati ya mawe. Kwa kuipata ilipasa askari kuondosha kila jiwe, kama Bwana wetu alivyotabiri. Hukumu hii ilitukia kwa mwaka 70 A.D. wakati Waroma, wakiongozwa na Tito, walipoharibu Yerusalema.

**B. Sehemu ya kwanza ya Mateso (24:3-14)**

**24:3** Wakati Yesu alipokwisha kwendea **Mlima wa Mizeituni, wanafunzi wakamkwendea peke yao** na maulizo matatu:

1. **Maneno haya yote yatakuwa wakati gani**; maana kuharibiwa kwa hekalu?
2. **Alama ya kuja kwake** itakuwa **nini**, maana tukio gani lisilo la dunia litatangulia kurudi kwake duniani na kusimamisha ufalme wake?
3. Alama ya **mwisho wa dunia** itakuwa nini; maana nini itatangaza mwisho wa muda unaotangulia utawala wake wa utukufu? (Ulizo la pili na la tatu ni karibu sawasawa.)

Sharti tukae kukumbuka kwamba wanafunzi hawa Wayuda walifikiri zaidi juu ya muda wa utukufu wa Masiya duniani. Hawakufikiri juu ya Kristo akifika kwa kanisa; walijua nusu tu juu ya neno lile. Walitazamia kuja kwake na uwezo na utukufu kuharibu adui zake na kutawala dunia.

Bwana hakujibu ulizo lao la kwanza peke yake. Ni kama alisema juu ya uharibifu wa Yerusalema kwa 70 A.D. (ona Lk 21:20-24) pamoja na uharibifu mwingine wa namna hii kwa wakati wa nyuma. Wakati tunapojifunza maneno ya unabii, tunaona Bwana akipita toka kutimia kwa unabii fulani kwa sehemu, duniani, kufika kutimizwa kwake kabisa kwa wakati wa mwisho.

Majibu kwa maulizo ya pili na ya tatu ni ndani ya mash 4-44 ya sura hii. Mashairi haya yanasema juu ya miaka saba, ndiyo muda wa Mateso yatakayotangulia kuja kwa Kristo na utukufu. Tunasoma juu ya miaka mitatu na nusu ya kwanza ndani ya mashairi 4-14. Miaka mitatu na nusu ya mwisho inayoitwa vile Mateso Makubwa na Wakati wa Taabu ya Yakobo (Yer. 30:7) utakuwa wakati wa taabu kubwa kupita taabu yote duniani tangu zamani.

Taabu namna nyingi ndani ya sehemu ya kwanza ya Mateso zimekuwa duniani tangu zamani, lakini zitakuwa nyingi kupita kwa sehemu ya kwanza ya Mateso. Bwana Yesu alisema na Wakristo wa kanisa kwamba watakuwa na mateso (Yn. 16:33), lakini mateso haya ni namna nyingine na Mateso yataka-

yomwangwa juu ya dunia hii iliyokataa Mwana wa Mungu.

Tunaamini kwamba kanisa litaondoshwa duniani (1 Tes. 4:13-18) mbele ya mwanzo wa siku ya gazabu ya Mungu (1 Tes. 1:10; 5:9; 2 Tes. 2:1-12; Ufu. 3:10).

**24:4, 5** Kwa sehemu ya kwanza ya Mateso, masiya za uwongo wengi watatokea watakaoweza kudanganya watu wengi. Hata sasa kuna watu wengi wenye mafundisho ya uwongo, lakini watu hawa si wale wa muda wa Mateso. Viongozi wa dini za uwongo kwa wakati ule watakuwa Wayuda wanaojitaja **Kristo.**

**24:6,7** Kutakuwa na **vita na matetesi ya vita. Taifa litapigana na taifa, na ufalme kupigana na ufalme.** Tunaona nusu ya maneno haya sasa, lakini itakuwa nyingi zaidi. Kunabaki neno moja tu litakalotimizwa mbele ya wakati ule, ndilo kupelekwa kwa kanisa mbinguni (Yn. 14:1-6; 1 Kor. 15:51-57). Nyuma ya kuondoshwa kwa kanisa duniani, mateso haya yote yataonekana mbio. Kutakuwa na **njaa na matetemeko ya inchi kwa pahali mbalimbali.** Hata kwa wakati wa sasa watawala wa dunia wanaogopa njaa kubwa duniani kwa sababu ya kuongezeka kwa hesabu ya watu duniani, na ukosefu wa vyakula utaongezeka kwa sababu ya vita.

**Matetemeko ya inchi** kwa wakati wa sasa hayatimizi unabii wa Bwana juu ya matetemeko kwa wakati wa kuja.

**24:8** Shairi 8 linaonyesha kwamba wakati huu ni **mwanzo wa uchungu**.

**24:9,10** Waamini waaminifu watatabishwa sana kwa muda huu wa Mateso. Wote walio waaminifu kwa Bwana watachukiwa sana na mataifa. Watahukumiwa ndani ya baraza za dini na za serikali (Mk. 13:9), lakini wengi watauawa kwa sababu wanakataa kuacha imani yao. Ndiyo, Wakristo wameteswa hivi tangu zamani, lakini ni kama hapa tunasoma zaidi juu ya mateso ya waamini Wayuda 144,000 watakaotumikia Bwana kwa wakati ule.

Wengi wataacha imani yao, kwa kuepuka maumivu na mauti. Ndugu zao watapasha habari za imani yao kwa viongozi wa inchi, na **kuwatoa** kwa watesaji wakali.

**24:11 Manabii wengi wa uwongo watasimama** na **kudanganya** watu wengi. Manabii hawa si wamasiya wa uwongo kwa shairi 5. Tunaweza kuwatambua kwa njia mbili: **Manabii wa uwongo** wanasema wao ni wanenaji kwa Mungu, lakini mambo wanayotabiri hayafanyikani mara nyingine, na mafundisho yao yanaondosha watu karibu na Mungu wa kweli. Kusoma hapa juu ya *manabii* wa uwongo kunaonyesha kwamba Mateso haya ni zaidi kwa Wayuda. ***Manabii* wa uwongo** ni wa taifa la Israeli; katika kanisa hatari inatoka ***walimu* wa uwongo** (2 Pet. 2:1).

**24:12** Kwa sababu ya kuzidi kwa uovu, watu hawatapendana kama mbele. Mapendo ya watu wengi yatapoa.

**24:13 "Lakini mwenye kuvumilia hata mwisho ataokolewa."** Maana ya shairi hili si kwamba roho za watu zitaokolewa kwa sababu ya kuvumilia taabu. Tunaona tena na tena ndani ya Biblia kwamba wokovu ni zawadi toka Mungu wa neema, ya kwamba tunaipokea kwa imani ndani ya kufa kwa Kristo kwa ajili yetu, na ufufuko wake. Na maana yake si ya kwamba wale wanaovumilia wataepuka taabu mwilini; tumesoma mbele ya kwamba waamini wengi watauawa kwa sababu ya imani yao (sh.9). Shairi lenyewe linaonyesha ya kwamba wale wanaosimama imara, bila kuacha imani yao, wataponyeshwa wakati Kristo atakapokuja mara ya pili. Watu wasifikiri kwamba wataweza kuepuka hatari kwa njia ya kuacha imani. Watu wenye imani ya kweli tu **wataokolewa.** Hata ikiwezekana kwa

imani yao kupunguka mara nyingine, imani ya kweli inadumu daima..

**24:14** Kwa wakati huu, **Habari Njema ya ufalme** itahubiriwa duniani pote **kama ushuhuda kwa mataifa yote.** Kama ilielezwa ndani ya mafundisho juu ya Matayo 4:23, **Habari Njema ya ufalme** ni habari nzuri kwamba Kristo atakuja kusimamisha **ufalme** wake duniani, na wale ambao wanampokea kwa njia ya imani kwa wakati wa Mateso watafurahi ndani ya baraka ya utawala wake wa miaka elfu moja.

Watu wengi wanafikiri shairi 14 linaonyesha ya kwamba Kristo hawezi kurudi kwa kanisa lake kwanza kwa sababu kuna makabila mengi yasiyosikia Habari Njema bado. Mawazo haya si sawa. Shairi hili linasema juu ya Kristo akikuja *pamoja na* watakatifu wake, si *kwa* watakatifu wake. Na ni juu ya habari njema ya *ufalme*, si juu ya habari njema ya *neema ya Mungu* (ona mafundisho juu ya Mt. 4:23).

Matukio tunayosoma habari zao ndani ya mashairi 3-14 yanatufikirisha Ufunuo 6:1-11. Yule anayepanda farasi *mweupe* – **masiya ya uwongo**; mpandaji wa farasi *mwekundu* – **vita**; mpandaji wa farasi *mweusi* – **njaa**; mpandaji wa farasi ya *rangi kama nyeupe* – **tauni** au **mauti.** Nafsi chini ya mazabahu ni wale waliouawa kwa sababu ya imani yao. Matukio katika Ufunuo 6:12-17 yanafungana na yale katika Matayo 24:19-31.

### C. Mateso Makubwa (24:15-28)

**24:15** Shairi hili linatufikisha kwa mwisho wa sehemu ya kwanza ya Mateso. Tunajua neno hili kwa njia ya kulisoma pamoja na Danieli 9:27. Danieli alitabiri ya kwamba katikati ya juma la 70 (maana yake kwa mwisho wa miaka mitatu na nusu) sanamu, ndilo chukizo la uharibifu, itasimamishwa katika pahali patakatifu, ndipo hekalu katika Yerusalema. Watu wote wataagizwa kuabudu sanamu hii ya kuchukiza sana. Azabu kwa watu wanaokataa kufanya hivi itakuwa mauti (Ufu. 13:15).

**“Basi wakati munapoona chukizo la uharibifu lililosemwa na Danieli nabii, likisimama kwa pahali patakatifu (yeye anayesoma afahamu).”** Kusimamishwa kwa sanamu hii kutakuwa alama kwa wale wanaojua Neno la Mungu ya kwamba Mateso Makubwa yameanza. Ona ya kwamba Bwana anataka wale **wanaosoma** unabii huu **kuufahamu.**

**24:16 Wale walio katika Yudea wakimbie kwa milima.** Kama wakibaki karibu na Yerusalema watajulikana mbio kwa sababu ya kukataa kuinama mbele ya sanamu.

**24:17-19** Na sharti wakimbie na haraka. Mtu akiketi **juu ya dari ya nyumba,** aache vitu vyake vyote nyumbani asiuawe saa anapojaribu kuvifunga kwenda navyo. Mwanamume akitumika **shambani** asirudi kukamata **mavazi** yake pahali alipoyaacha. Itakuwa nguvu zaidi kwa **wanawake wenye mimba** na **wenye kunyonyesha** watoto kukimbia.

**24:20** Lazima waamini **waombe** hatari hii isitokee wakati wa **baridi** wakati kusafiri ni hatari sana, au siku ya **sabato** wakati sheria inapokataza watu kufanya safari ndefu ya kuwawezesha kutoka pahali pa hatari (Kut.16:29).

**24:21 “Kwa sababu yatakuwa mateso makubwa, kama hayajatokea namna yake tangu mwanzo wa ulimwengu hata sasa, wala hayatakuwa kamwe.”** Katika mia za miaka inayopita watu wamepatwa na mateso na mauaji namna namna, lakini unabii wa shairi 21 unaonyesha wazi kwamba mateso ya shairi hili ni kwa wakati wa kuja, kwani yatakwisha na kuja kwa pili kwa Kristo.

**24:22** Mateso haya yatakuwa maku-

bwa zaidi na **kama siku zile zisingalifupizwa**, kama asingeokolewa mtu ye yote. Maana yake haiwezi kuwa ya kwamba urefu wa Mateso Makubwa (unaosemwa kuwa miaka mitatu na nusu) utafupishwa. Tunafikiri ya kwamba Mungu atafanya ajabu kufupisha saa za mchana, ndizo saa wakati vita na uuaji zinapozidi. **Kwa ajili ya wachaguliwa** (maana wale walioamini Yesu) Bwana atafanyiza usiku na giza kuanza mbele ya wakati wao.

**24:23-26** Kuna maonyo mengine ndani ya mashairi 23 na 24 juu ya masiya wa **uwongo na manabii wa uwongo**. Kwa wakati wa hatari habari zitaenea ya kwamba Masiya ni pahali fulani kwa maficho. Habari namna hii zinaweza kuwa mtego kwa watu wanaotazamia Kristo na roho ya kweli na mapendo. Hivi Bwana anaonya wanafunzi wote wasiamini habari kwamba ametokea kwa maficho na kwa pahali pa maficho. Hata wale wanaofanya maajabu si watu wa Mungu kila mara; labda wanafanya maajabu haya kwa uwezo wa Shetani. Mwenye uasi katika 2 Tes. 2:9-10 atapewa uwezo toka Shetani kufanya maajabu.

**24:27** Kufika kwa Kristo kutakuwa wazi na kwa gafula, mbele ya macho ya watu wote. Kutakuwa kama **umeme** unaoonekana mara moja na wazi kwa watu wote.

**24:28** Uovu wote utahukumiwa sana kwa wakati ule. **"Kwa maana pahali maiti inapolala, pahali tai watakapokusanyika." Maiti** ndiyo mfano wa dini za kiyahudi, Ukristo, na kawaida wa dunia nzima zinazofungana kukana na kushindana na Mungu na Kristo. **Tai** ni mfano wa hukumu za Mungu kwa wakati wa kuja kwa Masiya.

**D. Kuja kwa pili (24:29-31)**

**24:29** Kwa mwisho wa Mateso Makubwa kutakuwa na matukio ya kuogofya kabisa mbinguni. **Jua litatiwa giza,** na kwa sababu mwezi unarudisha tu nuru ya jua, **mwezi** vilevile hautatoa nuru. Nyota zitaondoka kwa njia zao, na maneno haya yote yatageuza nyakati za jua na baridi duniani, na kujaa na kupunguka kwa mawimbi baharini.

**24:30 "Halafu alama ya Mwana wa watu itaonekana mbinguni."** Hatujulishwi wazi kama **alama** hii ni nini. Kulikuwa na alama mbinguni wakati alipokuja mara ya kwanza – nyota. Labda nyota ya ajabu itatangaza kuja kwake mara ya pili vilevile. Watu wengine wanafikiri kwamba **Mwana wa watu** mwenyewe ndiye **alama** hii. Itaonekana wazi kwa saa yenyewe. Mataifa yote ya dunia wataomboleza – bila shaka kwa sababu walimkataa mbele. Lakini makabila 12 ya Israeli watamboleza zaidi. "… nao watamtazama ambaye walimchoma; watamwombolezea kama mtu anavyoomboleza mwana wake mzaliwa pekee, na wataona uchungu juu yake, kama mtu anavyoona uchungu kwa mwana wake mzaliwa pekee" (Zek. 12:10).

Halafu **"wataona Mwana wa watu akikuja katika mawingu ya mbingu pamoja na uwezo na utukufu mkubwa."** Ono la ajabu kabisa! Yule ambaye walimtemea mate na kumsulibisha anashuhudiwa kuwa Bwana wa uzima na utukufu. Yesu, mpole na mnyenyekevu, ataonekana kuwa Yehova mwenyewe. Mwana-kondoo aliyejitoa kwa zambi ya ulimwengu atashuka kama Simba mshindaji. Mseremala mzarauliwa wa Nazareti atakuja kama Mfalme wa wafalme na Bwana wa wabwana. Magari yake yatakuwa mawingu ya mbingu. Atakuja na uwezo na utukufu wa kifalme – dakika ambayo viumbe vyote vimengojea na kuugua na uchungu kwa maelfu ya miaka.

**24:31** Wakati atakaposhuka **atatuma malaika** pahali pote duniani **kukusanya**

**wachaguliwa wake**, Waisraeli walioamini, kwa inchi ya Palestina. Watakuja toka pande zote za dunia kukaribisha Masiya wao, na kufurahi wakati wa utawala wake wa utukufu.

**E. Mfano wa mtini (24:32-35)**

**24:32 "Basi mujifundishe mfano huu wa mtini."** Bwana wetu alitumika tena na mapando kutoa mafundisho kwa roho zetu. Wakati matawi ya mtini **yanapochipuka na kutoa majani** yake, munajua wakati wa jua kali ni karibu. Tumeona kwamba mtini ni mfano wa Israeli (21:18-22). Ni kama Israeli limelala usingizi kwa mia za miaka, bila serikali, bila inchi, hekalu au makuhani. Watu wake wamesambazwa duniani pote.

Halafu, katika 1948 A.D., Israeli liligeuka taifa lenye inchi, serikali, mali, vivi hivi. Lakini kwa maneno ya roho wangali tasa na baridi, bila matunda kwa Mungu. Lakini kama taifa la dunia tungeweza kusema matawi yake yana**chipuka**.

**24:33 "Nanyi vilevile wakati munapoona maneno haya yote, mujue ya kuwa yeye ni karibu, hata kwa milango."** Israeli likisimama kama taifa tena linaonyesha kwamba mwanzo wa Mateso ni karibu, na ya kwamba Bwana mwenyewe ni karibu, **hata kwa milango!**

Kama utawala wa Kristo ni karibu hivi, kuondoshwa kwa kanisa toka dunia ni karibu zaidi. Tukiona hata sasa vivuli vya matukio yatakayotangulia kuonekana kwake katika utukufu, tunajua sehemu ya kwanza ya *Parousia* (maana Kuja kwake) ni karibu zaidi (1 Tes. 4:13-18).

**24:34** Nyuma ya kusema juu ya mtini, Yesu aliongeza, **"Kweli ninawaambia ninyi, kizazi hiki hakitapita hata maneno haya yote yatakapotimia."** Maana ya **"kizazi hiki"** si watu walioishi wakati Kristo alipokuwa duniani; wao wote wamekufa, lakini maneno ya sura 24 hayatukia bado. Basi maana ya **"kizazi hiki"** ni nini? Maneno haya yanaweza kuelezwa kwa njia mbili:

F.W. Grant na walimu wengine wanafikiri ya kwamba "kizazi kinachoona mwanzo wa maneno haya wataona mwisho wake vilevile." Watu wale wale wanaoona Israeli likisimama kama taifa tena (au wanaoona mwanzo wa Mateso), wataona Bwana Yesu akikuja katika mawingu ya mbingu kutawala.[10]

Elezo la pili ndilo hili: Maana ya **"kizazi"** ni taifa. Hii ndiyo maana ya neno hili katika Kiyunani, watu wa jamaa moja (Mt. 12:45; 23:35-36). Hivi Yesu alitabiri ya kwamba taifa la Wayuda litaishi na kuona kutimia kwa maneno haya yote. Ni ajabu kuona kusimama kwa taifa la Israeli hata nyuma ya taabu na mateso makali sana.

Lakini kwa wakati wa Yesu, "kizazi hiki" kilikuwa taifa waliokaa kukataa kukubali kwamba yeye ndiye Masiya. Ni kama Yesu alitabiri kwamba taifa la Israeli watakaa kukataa Kristo kufika kuja kwake kwa pili. Halafu maasi yote yatashindwa, na wale tu wanaokubali kunyenyekea utawala wake watapona na kuingia utawala wake wa miaka elfu moja.

**24:35** Yesu alionyesha wazi ya kwamba bila shaka mambo yote aliyotabiri yatatimizwa wakati aliposema **mbingu na dunia zitapita** lakini **maneno** yake **hayatapita kabisa**. Wakati aliposema juu ya kupita kwa **mbingu** alifikiri juu ya mbingu tunazoona na macho – mwezi na nyota na mawingu – si juu ya mbingu lililo kao la Mungu (2 Kor. 12:2-4). Tunasoma juu ya kutoweka kwa mbingu na dunia katika 2 Pet. 3:10-13 na tena kwa Ufu. 20:11.

### F. Siku na saa hazijulikani (24:36-44)

**24:36 Hakuna mtu** anayejua **siku** wala **saa** za kuja kwa pili kwa Kristo, hata **malaika walio mbinguni … ila Baba peke yake."** Hivi haifai kutaja tarehe fulani wakati Kristo atakapokuja, au kuamini tarehe zinazotajwa na watu wengine. Hatushangai kwa sababu malaika hawajui – wao ni viumbe tu na hawajui maneno yote.

Hata kama wale wanaoishi mbele ya kurudi kwa Kristo hawatajua *sik*u wala *saa*, ni kama wale wanaojuana na unabii wanaweza kujua *mwaka* wa kurudi kwake. Kwa mfano, watajua atakuja karibu miaka mitatu na nusu nyuma ya kusimamishwa kwa sanamu katika hekalu (Dan. 9:27; ona vilevile Dan. 7:25; 12:7,11; Ufu. 11:2, 3; 12:14; 13:5).

**24:37-39** Lakini zaidi ya watu hawataweka roho juu ya neno hili, kama kwa **siku za Noa**. Hata kama uovu ulizidi sana mbele ya garika, hili si neno Bwana alilofikiri hapa zaidi. Watu walikula, walikunywa, **walioa na kuolewa**; waliendelea kuishi sawasawa watu watakaoishi milele. Walipewa maonyo ya kwamba garika itakuja, lakini walikaa kuishi sawasawa garika halitaweza kuwagusa. Halafu wakati garika ilipokuja kweli, hawakuwa tayari, na hawakukimbilia pahali pa pekee walipoweza kukaa bila hatari. Itakuwa vivyo hivyo wakati Kristo atakaporudi. Wale tu walio ndani ya Kristo, safina ya amani, wataokolewa.

**24:40,41 Watu wawili watakuwa shambani; mmoja atatwaliwa** kwa hukumu, na **mmoja ataachwa** kuingia utawala wa miaka elfu moja. **Wanawake wawili watakuwa wakisaga;** mmoja ataondoshwa kwa hukumu; wa pili atafurahishwa na baraka za utawala wa Kristo. (Mara nyingi watu wanataja mash. 40 na 41 kuonya wasioamini na kuwakumbusha juu ya kurudi kwa Kristo kupeleka waamini wote mbinguni na kuacha wasioamini duniani kwa hukumu. Neno hili ni vizuri, lakini wakati tunapokumbuka mashairi yanayotangulia na yale yanayofuata, tunafahamu mash. 40 na 41 ni zaidi juu ya kuja kwa Kristo kutawala.)

**24:42-44** Kwa sababu watu hawajui siku wala saa ya kuja kwa Bwana, inawapasa kukaa **kuangalia**. Mtu akijua kwamba mwizi ataingia nyumba yake atakuwa tayari, hata kama hajui saa gani atakapokuja. Mwana wa watu atakuja wakati zaidi ya watu wasipozani hata kidogo kwamba atafika. Hivi inapasa watu wake kuwa tayari kila dakika kwa kuja kwake.

### G. Mfano wa watumwa wenye akili na watumwa wabaya (24:45-51)

**24:45-47** Kwa mwisho wa sura hii Bwana anaonyesha kwamba matendo ya **mtumwa** wakati Bwana asiporudi bado yanaonyesha namna ya roho yake. Ingepasa watumwa wote kulisha watu wa nyumba kwa saa ya chakula. Lakini si watu wote wanaokiri kuwa watumwa wa Kristo ni watumwa wa kweli.

Wakati Bwana atakapokuja atakuta **mtumwa mwenye akili** akilinda watu wa Mungu. Atapewa kazi kubwa na ya heshima katika ufalme. **Bwana atamweka juu ya vitu vyake vyote.**

**24:48-51 Mtumwa mbaya** ni mfano wa mtu asiye mwamini wa kweli na asiyefikiri juu ya kurudi kwa bwana wake. **Anaanza kupiga watumishi wenzake, na kula na kunywa pamoja na walevi.** Matendo haya yanaonyesha kwamba yeye si tayari kwa ufalme. Wakati mfalme atakapofika atamwazibu na **kumwekea fungu lake pamoja na wadanganyifu,** pahali watu wanapolia na kusaga meno.

Mashairi haya ni mfano wa kurudi wa Kristo kwa dunia kama Masiya-Mfalme. Lakini yanatufikirisha kuja kwa Bwana kwa Kanisa vilevile. Wengi wa watu

wanaokiri kuwa Wakristo wanaonyesha kwa njia ya uadui wao kwa watu wa Mungu, na kwa njia ya urafiki wao na watu waovu, ya kwamba hawatazamii kurudi kwa Kristo. Kwa watu wale kurudi kwake kutakuwa hukumu, si baraka.

### H. Mfano wa mabikira kumi (25:1-13)

**25:1-5** Neno la kwanza la sura hii, **Halafu**, linaonyesha kwamba habari hizi zinaendelea na zile za sura 24, na kutufahamisha kwamba zinatangulia wakati wa kurudi wa Mfalme duniani. Yesu anasawanisha **ufalme wa mbinguni** kwa wakati ule na **mabikira kumi waliotwaa taa zao na kwenda kukutana na Bwana arusi. Watano walikuwa wenye akili** na walikuwa na **mafuta kwa taa zao;** wengine walikosa mafuta. Wakati walipokuwa wakingoja kufika kwa Bwana arusi wao wote walishindwa na usingizi.

Mabikira watano **wenye akili** ni mfano wa wanafunzi wa kweli wa Kristo kwa wakati wa Mateso. **Taa** zinasema juu ya kukiri Kristo, na **mafuta** ni mfano wa Roho Mtakatifu. Mabikira **wapumbavu** ni wale wanaokiri kutumainia kuja kwa Masiya lakini hawakuokolewa kweli, na hivi Roho Mtakatifu si ndani yao. **Bwana arusi** ni Kristo, Mfalme; kukawa kwake ni mfano wa muda nyuma ya kuja kwake kwa Kanisa na kufika kwake duniani kama Mfalme. Mabikira wote **walilala**, ndilo neno linaloonyesha kwamba wao wote walionekana karibu sawasawa.

**25:6** Saa sita ya usiku kulikuwa na tangazo kwamba **bwana arusi alikuwa akikaribia**. Ndani ya sura 24 tulisoma ya kwamba kutakuwa na matukio ya kuogofya kwa wakati ule.

**25:7-9 Mabikira waliamka na kutengeneza taa zao**. Wao wote walitaka kuonekana tayari kwa kuja kwake. Mabikira wapumbavu walikosa mafuta kwa taa zao, na waliomba mabikira wenye akili kuwapa nusu ya mafuta yao, lakini wenye akili walikataa, wakasema nao waende **kununua** mafuta kwa mahitaji yao. Inaonekana sawasawa wenye akili walijifikiri wenyewe tu, lakini kwa maneno ya roho hakuna mtu anayeweza kugawa Roho Mtakatifu kwa mtu mwingine. Haiwezekani kununua Roho Mtakatifu, lakini kwa pahali pengine Biblia inatumika na mfano wa kununua wokovu pasipo feza na pasipo bei (Isa. 55:1).

**25:10-12 Wakati mabikira wapumbavu walipokwenda** kununua mafuta, bwana arusi alifika. Tafsiri mbili za zamani za Biblia [Syriac na Vulgate] zinasema alikuja *pamoja na bibi arusi yake.* Na kweli Bwana Yesu atarudi nyuma ya karamu ya arusi pamoja na bibi arusi yake, ndilo kanisa (1 Tes. 3:13). (Arusi itakuwa mbinguni [Efe. 5:27] nyuma ya kupelekwa kwa kanisa mbinguni.) Baki la waamini waaminifu wa muda wa Mateso wataingia karamu ya arusi pamoja naye. Karamu ya arusi ni mfano mzuri wa furaha na baraka ya ufalme wa Kristo duniani. Mabikira wenye akili **waliingia pamoja naye kwa arusi; mlango ukafungwa**. Saa imepita kwa mtu mwingine kuingia ufalme. Wakati **mabikira wengine walipofika** na kuomba kuingia, bwana arusi alisema hawajui – neno linalohakikisha kwamba hawakuzaliwa tena.

**25:13** Bwana Yesu alisema mafundisho ya maneno haya ndiyo ya kwamba inatupasa **kuangalia**, kwa sababu hatujui **siku** wala **saa** atakapokuja. Inapasa waamini kukaa na kuishi kila siku na kila saa tayari kwa kuja kwake.

### I. Mfano wa talanta (25:14-30)

**25:14-18** Mfano huu unaonyesha vilevile ya kwamba wakati Bwana atakaporudi atakuta watumishi wazuri na wabaya. Ni habari ya **mtu mmoja** aliyekutanisha watumwa wake na kumpa **kila mtu** hesabu fulani ya mali

yake, **kwa kadiri ya uwezo wa mtumwa mwenyewe**. Mtumwa mmoja alipewa **talanta tano,** mwingine talanta **mbili**, na wa tatu talanta **moja**. Waliagizwa kutumika na mali hii kupatia bwana wao faida. Kisha mtu huyu alikwenda safari ndefu. Mtumwa mwenye **talanta tano** alifanya biashara nazo, akapata **talanta tano nyingine**. Yule mwenye talanta **mbil**i alifanya vivyo hivyo na alipata **talanta mbili nyingine** kwa njia ya kazi yake. Lakini mwenye talanta **moja alichimba udongo na kuzika talanta yake**.

Ni nyepesi kuona kwamba Kristo ndiye bwana aliyekwenda safari ndefu, ndiyo mfano wa muda unaogawa kuja kwake kwa kwanza na kwa pili. Watumwa wale watatu ndio Waisraeli wanaoishi kwa wakati wa Mateso, wenye kazi ya kusimamia faida ya Bwana wao aliye kwanza mbali. Wanapewa kazi kwa kadiri ya uwezo wao.

**25:19-23 Nyuma ya siku nyingi bwana … akarudi na kufanya hesabu na watumwa wake** – ndio mfano wa kuja kwake kwa pili. Mtumwa wa kwanza na wa pili walipokea sifa sawasawa: **"Vema, mtumwa mwema na mwaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa vitu vichache, nitakuweka juu ya vitu vingi; ingia katika furaha ya bwana wako."** Hawakupimwa kwa hesabu ya faida waliyopatia bwana wao, lakini kwa kipimo cha masumbuko yao kumpatia faida. Walijitoa kabisa kwa kazi hii, nao ni mfano wa waamini wa kweli na zawabu yao, ndiyo baraka za ufalme wa Masiya.

**25:24,25** Mtumwa wa tatu alitoa uzuru tu na kutukana bwana wake. Alimshitaki kuwa mtu mgumu, **aliyevuna pahali asipopanda,** na **kukusanya pahali asiposambaza mbegu.** Alitoa uzuru akisema alificha **talanta** yake katika udongo kwa sababu aliogopa bwana wake. Bila shaka mtumwa huyu alikuwa msiyeamini; hakuna mtumwa wa kweli angefikiri maneno namna hii juu ya bwana wake.

**25:26, 27** Bwana wake alimkemea na kusema yeye ni **mbaya na mlegevu.** Akiwa na mawazo namna hii juu ya bwana wake, kwa nini **hakuweka feza yake kwa wabadilisha** feza kwa kupata faida? Vizuri tufahamu kwamba ndani ya shairi 26 bwana hakukubali shitaki la mtumwa wake. Alikuwa akisema, "Ukifikiri mimi ni bwana namna hii, mawazo haya yangalipasa kukusukuma kutumika kazi kupata faida na talanta hii. Masemo yako si uzuru, lakini yanakuhukumu."

**25:28, 29** Kama mtu huyu angalipata talanta moja nyingine, kama angalipokea sifa kama watumwa wale wengine. Basi **talanta ile moja iliondoshwa kwake** na kuletwa kwa mwenye **talanta kumi.** Neno hili linatimiza sheria moja kwa maneno ya roho, sheria isiyoweza kubadilika: **"Mwenye kitu atapewa, naye atazidishwa tele; lakini yeye asiye na kitu ataondolewa hata kitu kile alicho nacho."** Wale wanaotaka kuishi kwa utukufu wa Mungu watapewa uwezo kufanya hivi. Wakitumikia Bwana kwa kipimo gani, watapewa uwezo kufanya hata kupita kwaye. Lakini kama tusipotumika na nguvu na zawadi ambazo Mungu alitupa sisi, tutazipoteza kwa sababu ya uvivu.

**Wabadilisha feza** ndani ya shairi 27 wanatufikirisha ya kwamba tusipoweza kutumika sisi wenyewe na mali yetu kwa Bwana, inatupasa kuitia mikononi mwa wale *watakaoweza* kuitumia kwa kazi yake. Wabadilisha feza hapa ni mfano wa wahubiri wa Habari Njema, wale wanaochapa Biblia na vitabu vya mafundisho kueleza maana yake, wenye kutangaza Habari Njema kwa radio, vivi hivi. Haifai hata kidogo kwa waamini kuacha mali yao kulala bure.

**25:30 Mtumwa yule asiye na faida** alitupwa inje – hakuweza kuingia ufalme.

Alishiriki ndani ya maumivu ya wapotevu. Hakuhukumiwa kwa sababu hakutumika na talanta yake kwa Bwana, lakini ukosefu wake wa matendo mema ulionyesha kwamba hakuamini Bwana na kuzaliwa tena.

**J. Mfalme anahukumu mataifa (25:31-46)**

**25:31** Mashairi yanayofuata ni juu ya Hukumu cha Mataifa. Hukumu hii ni mbali na Kiti cha Hukumu cha Kristo na Hukumu cha Kiti cha Ufalme Kikubwa Cheupe.

Kwa Kiti cha Hukumu cha Kristo, kilicho kwa waamini tu na kinachofuata kupelekwa kwa kanisa mbinguni, Kristo ataangalia kazi ya kila mwamini na kutoa zawabu (Rom. 14:10; 1 Kor. 3:11-15; 2 Kor. 5:9,10). Hukumu cha Kiti cha Ufalme Kikubwa Cheupe itatukia nyuma ya utawala wa Kristo kwa miaka elfu moja. Wafu waovu wasioamini Kristo watahukumiwa na kutupwa katika Ziwa la Moto (Ufu. 20:11-15).

Hukumu ya Mataifa itakuwa duniani nyuma ya kufika kwa Kristo duniani kutawala, kama tunavyoona wazi ndani ya shairi 31: **"Wakati Mwana wa watu atakapokuja katika utukufu wake, na malaika yote pamoja naye."** Tunafikiri pahali penyewe patakuwa bonde la Yosafati (Yoeli 3:2). Mataifa watahukumiwa juu ya namna walivyotendea ndugu Wayuda za Kristo kwa wakati wa Mateso (Yoe. 3:1,2; 3:12-14; Mt. 25:31-46).

**25:32** Neno lenye maana ambayo inatupasa kuona hapa ni namna tatu ya watu: **kondoo, mbuzi**, na **ndugu za Kristo.** Namna mbili za kwanza wa watu ambao Kristo anahukumu ni watu wa Mataifa wanaoishi kwa muda wa Mateso. Namna ya tatu ndio ndugu Wayuda waaminifu wa Kristo, wanaokataa kukana jina lake kwa wakati wa Mateso, hata kama wakiteswa sana.

**25:33-40** Mfalme anaweka **kondoo kwa mkono wake wa kuume, lakini mbuzi kwa mkono wake wa kushoto.** Halafu anaita kondoo kuingia **ufalme wake** wa utukufu **waliotengenezewa tangu kuumbwa kwa ulimwengu.** Kwa sababu gani? Kwa sababu walimkulisha wakati alipokuwa na **njaa**, **walimkunywesha** wakati alipokuwa na **kiu**, walimkaribisha wakati alipokuwa **mgen**i, **walimvalisha** wakati alipokosa nguo, **walimfikia** wakati alipokuwa na **ugonjwa**, na walikwenda **kumwona gerezani**. Kondoo **wenye haki** wanafazaika kwa wakati gani walitendea Mfalme mema haya; hakuwa duniani kwa wakati wao walipokuwa hai. Anaeleza ya kwamba wakionyesha mapendo na urafiki kwa **mmoja wa ndugu zake, walio wadogo,** walimwonyeshea yeye urafiki na mapendo yale**.** Tendo jema lo lote linalofanywa kwa mmoja wa wanafunzi wake litapokea zawabu kama tendo lililofanywa kwa Mfalme mwenyewe.

**25:41-45** Halafu mbuzi wazalimu wanaagizwa **kuondoka karibu naye** na **kwenda kwa moto wa milele uliotengenezwa kwa Shetani na malaika zake,** kwa sababu hawakumlinda kwa wakati ule wa kuogopesha unaoitwa Taabu ya Yakobo. Wakati wanapotoa uzuru kusema hawakumwona kamwe atawakumbusha ya kwamba wakati wasipoweka roho juu ya kusaidia wafuata wake walikuwa wakimwona yeye mwenyewe bure.

**25:46** Hivi mbuzi **wanakwenda kuingia katika azabu ya milele, lakini** kondoo **wataingia uzima wa milele.** Habari hizi zinatufazaisha kwa njia mbili. Kwanza inaonekana sawasawa mataifa *mazima* wanaokolewa au kupotea. Na neno la pili ambalo linatufazaisha ni ya kwamba kondoo wanaokolewa kwa sababu ya matendo yao mema, na mbuzi wanahukumiwa kwa

sababu ya kukosa kutenda mema. Tukumbuke basi ya kwamba mara nyingine Mungu *anatendea* mataifa mazima maneno fulani. Ndani ya Agano la Kale tunasoma tena na tena juu ya mataifa walioazibiwa kwa sababu ya zambi yao (Isa. 10:12-19; 47:5-15; Eze. 25:6,7; Amo. 1:3,6,9,11,13; 2:1,4,6; Oba. 10; Zek. 14:1-5). Hivi si nguvu kuamini ya kwamba mataifa watakaa kuazibiwa na Mungu. Si kusema ya kwamba kila mtu mmoja mmoja wa taifa lile ataazibiwa, lakini Mungu atatendea kwa haki mataifa mazima, na watu mmoja mmoja vilevile.

Watu wengine wanafazaika namna gani itawezekana kwa mataifa mazima kukutanishwa mbele ya Bwana katika Palestina. Labda inatupasa kufikiri ya kwamba wajumbe wa mataifa au cheo fulani za watu watakutanishwa kwa hukumu.

Sharti tufahamu vilevile ya kwamba haifai kutumika na mashairi haya kufundisha kwamba tunaokolewa kwa njia ya kutenda mema. Biblia inafundisha wazi kwamba wokovu ni kwa njia ya imani, si kwa njia ya matendo (Efe. 2:8,9). Lakini Biblia inafundisha wazi vilevile ya kwamba imani ya kweli inazaa matendo mema. Kama mtu asipofanya kazi njema, neno hili linaonyesha kwamba hakuzaliwa tena. Hivi inatupasa kufahamu ya kuwa watu wa Mataifa hawaokolewi kwa sababu ya kusaidia baki la Wayuda, lakini ya kwamba matendo haya mema yanaonyesha mapendo yao kwa Bwana.

Sharti tutaje maneno matatu mengine. Tumesoma kwamba ufalme ulitengenezwa kwa wenye haki tangu kuumbwa kwa ulimwengu (sh.34), lakini moto wa milele ulitengenezwa kwa Shetani na malaika zake (sh.41). Mungu anataka kubariki watu; Gehena haikutayarishwa kwa watu. Lakini watu wakichagua kukataa kupokea uzima, wanachagua mauti.

Neno la pili ndilo hili: Bwana Yesu alisema juu ya moto wa "milele" (sh.41), azabu ya "milele" (sh.46), na uzima wa "milele" (sh.46). Kulikuwa na neno moja tu kuonyesha maana ya "milele." Bwana Yesu alifundisha juu ya uzima wa milele, na azabu ya milele. Na kwa 1 Tim. 1:17 tunasoma kwamba Mungu ni wa milele vilevile.

Neno la tatu ndilo hili: Hukumu ya Mataifa inatukumbusha tena umoja wa Kristo na watu wake; neno lo lote ambalo linagusa watu wake linamgusa yeye vilevile. Hivi tunaweza kumwonyeshea yeye wema na mapendo yetu kwa njia ya kutendea watu wake mema.

## 14. MAUMIVU NA MAUTI YA MFALME (Sura 26, 27)

### A. Shauri la kuua Yesu (26:1-5)

**26:1,2** Sasa Bwana wetu alijulisha wanafunzi tena (mara ya ine na ya mwisho ndani ya Matayo) ya kwamba itampasa kufa (Mt. 16:21; 17:23; 20:18). Ni kama tangazo lake lilifunga Pasaka na kusulibishwa kwake pamoja: **"Munajua ya kama nyuma ya siku mbili Pasaka inakuja, na Mwana wa watu atatolewa asulibiwe."** Mwaka huu Pasaka itatimizwa. Mwana-Kondoo wa Pasaka amefika nyuma ya miaka ile yote, na atauawa nyuma kidogo.

**26:3-5** Hata saa alipokuwa akisema maneno haya, **wakubwa wa makuhani, waandishi,** na **wazee** walikuwa wamekutana kwa **kiwanja cha Kayafa**, **kuhani mkubwa**, kufanya shauri. Walitaka kufunga Yesu kwa siri na kumwua, lakini hawakufikiri ni akili njema kufanya hivi kwa **wakati** wa siku kubwa ya **Pasaka**, kwani waliogopa kusulibishwa kwake kutaleta machafuko makubwa katikati ya watu. Inatushinda kufahamu namna gani viongozi vya Israeli kwa maneno ya dini walikuwa viongozi ndani ya shauri la

kuua Masiya wao. Ingaliwapasa kuwa watu wa kwanza kumtambua na kumfanya mfalme. Sivyo; walikuwa viongozi vya adui zake.

### B. Yesu anapakaliwa mafuta kwa Betania (26:6-13)

**26:6,7** Nyuma ya habari za kuumiza roho za uovu za makuhani na Yuda, mashairi haya matamu yanasaidia roho sana. **Wakati Yesu alipokuwa kwa Betania, katika nyumba ya Simoni mkoma, mwanamke mmoja akamkwendea, mwenye chupa cha marasi ya bei ya damani sana, akaimwanga juu ya kichwa chake**. Bei kubwa ya zabihu yake inaonyesha ukubwa wa mapendo yake kwa Bwana Yesu.

**26:8,9 Wanafunzi wake**, na zaidi Yuda (Yn. 12:4-5) walifikiri tendo lake **lilipoteza mali nyingi** bure. Walifikiri ingalikuwa vizuri kupita kuitoa kusaidia **wamasikini**.

**26:10-12** Yesu alionyesha kwamba mawazo yao hayakuwa mazuri. Mwanamke huyu hakupoteza mali bure, lakini tendo lake lilikuwa zuri na la kupendeza sana. Zaidi ya ile, alilitenda kwa saa iliyofaa kabisa. Tunaweza kusaidia wamasikini wakati wo wote, lakini saa moja tu ndani ya historia nzima ya dunia Mwokozi aliweza kupakaliwa kumtayarisha kwa maziko yake. Saa ile ilikuwa imefika, na ni kama **mwanamke** mmoja tu aliamini masemo ya Bwana juu ya kufa kwake, na alifahamu kwamba asipotolea Bwana zawadi yake kubwa sasa, hatapata njia kufanya hivi kamwe. Na kweli wanawake waliokusudi kupakaa mwili wake nyuma ya kuzikwa kwake walizuizwa na ufufuko wake (Mk. 16:1-6).

**26:13** Bwana Yesu alisifu tendo lake la mapendo litakalokumbukwa kwa milele akisema, **"Kweli ninawaambia ninyi, Pahali po pote Habari Njema hii itakapohubiriwa katika dunia nzima, tendo hili ambalo alitenda mwanamke huyu litatajwa kwa ukumbusho wake."** Tendo lo lote la kuabudu kweli linajaza viwanja vya mbingu na harufu tamu, na Bwana hatalisahau kamwe.

### C. Udanganyifu wa Yuda (26:14-16)

**26:14-15 Halafu mmoja wa wale kumi na wawili** – mmoja wa wanafunzi waliokaa pamoja na Bwana Yesu, aliyesafiri pamoja naye, kuona maajabu aliyofanya, kusikia mafundisho yake mazuri kupita yote, na kuona ajabu la maisha yake bila zambi – ambaye Yesu aliweza kuita "rafiki yangu ya karibu … aliyekula chakula changu" (Zab. 41:9) – ni yeye aliyenyanyulia Mwana wa Mungu kisigino chake. **Yuda Iskariota alifikia wakubwa wa makuhani** na kupatana kuuzisha Bwana wake kwa **vipande makumi tatu vya feza**. Makuhani walimpa mali hii nusu mara moja.

Sawanisha watu hawa wawili, ndio mwanamke na Yuda. Kweli mwanamke huyu aliyefika kupakaa Yesu na marasi nyumbani mwa Simoni aliheshimu Mwokozi sana sana. Yuda alimwona bure.

**26:16** Basi yule aliyetendewa mema tu na Yesu alitoka kutimiza sehemu yake ya mapatano yale mabaya sana.

### D. Pasaka ya mwisho (26:17-25)

**26:17** Ilikuwa **siku ya kwanza ya mikate pasipo chachu**, saa Wayuda walipoondosha chachu yote nyumbani mwao. Waza juu ya mafikiri yaliyojaza nia ya Bwana wakati alipotuma **wanafunzi** kwa Yerusalema **kufanya matayarisho** kwa **Pasaka**. Kila sehemu ya karamu ile itakuwa na maana kubwa.

**26:18-20** Yesu alituma wanafunzi kutafuta **mtu fulani** (hatuambiwi jina lake, labda kuepuka hatari) ambaye atawafikisha kwa **nyumba** iliyochaguliwa. Yesu alijua maneno yote juu ya watu mmoja mmoja, pahali walipo-

kuwa, na kama walikuwa tayari kumsaidia. Ona maneno yake, **"Mwalimu anasema, 'Wakati wangu ni karibu; kwako nitafanya Pasaka pamoja na wanafunzi wangu.'"** Alitazamia kukaribia kwa mauti yake na utulivu, na alitayarisha vyote kwa karamu na roho ya neema. Ilikuwa heshima kubwa kwa mtu huyu kuweza kukopesha nyumba yake kwa Pasaka hii ya mwisho!

**26:21-24** Wakati walipokuwa wakikula Yesu aliwashitusha na tangazo ya kwamba **mmoja** wa wale kumi na wawili **atamtoa kwa mikono ya adui**. Wanafunzi walihuzunishwa sana, wakamwuliza mmoja mmoja, **"Ni mimi, Bwana?"** Wakati wao wote ila Yuda walipokwisha kuuliza hivi, Yesu aliwaambia kwamba ni yeye **anayechovya** pamoja naye **katika sahani**. Halafu Bwana alivunja kipande cha mkate, akakitia ndani ya sahani yenye nyama, na kumpa Yuda (Yn. 13:26) – alama ya mapendo na urafiki. Aliwakumbusha ya kwamba ilikuwa sharti kwaye kusulibishwa, lakini neno hili halikuondosha hatia ya yule aliyekusudi kumtoa kwa mikono ya adui. **Ingalikuwa heri** kwake kama **asingalizaliwa.** Yuda alifanya shauri kuuza Mwokozi, naye atahukumiwa kwa zambi hii.

**26:25** Wakati Yuda alipouliza wazi kama ni yeye, Yesu alijibu, "Wewe umesema."

### E. Karamu ya Ukumbusho ya kwanza (26:26-29)

Ndani ya Yoane 13:30 tunasoma ya kwamba wakati Yuda alipokwisha kupokea mkate alitoka mara moja, na ulikuwa usiku. Hivi tunafikiri hakuwa pamoja na Bwana na wanafunzi wengine wakati wa karamu ya ukumbusho ya kwanza (si watu wote wanaokubali mawazo haya).

**26:26** Nyuma ya kula Pasaka yake ya mwisho, Mwokozi alisimamisha karamu tunayoita sasa Karamu ya Ukumbusho. Mkate na mvinyo zilikuwa tayari mezani, kwani zilikuwa sehemu ya Pasaka mbele, na Yesu aliwapa maana mpya sasa. Kwanza **alitwaa mkate, aliubariki na kuuvunja**. **Wakati alipowapa wanafunzi** wake alisema nao, **"Twaeni, mule, huu ni mwili wangu."** Saa yenyewe alikuwa hajatoa mwili wake msalabani, hivi ni wazi ya kwamba alisema juu ya mkate kama mfano wa mwili wake.

**26:27,28** Ni vivyo hivyo na **kikombe**; kikombe kilikuwa mfano wa kinyweo kilichokuwa ndani yake, ndicho mvinyo iliyokuwa mfano wa **damu ya agano jipya**. Agano **jipya**, agano la neema bila masharti, litathibitishwa na **damu** yake ya damani ambayo ataimwanga kwa wengi kwa usamehe wa zambi. Damu yake ilitosha kusamehe zambi za watu wote. Lakini hapa tunasoma kwamba **ilimwangika kwa ajili ya wengi,** maana yake *inafaa* kuondosha zambi za wale tu wanaoamini.

**26:29** Halafu Mwokozi alikumbusha wanafunzi wake kwamba **hatakunywa matunda ya mizabibu** tena pamoja nao **kufika wakati** atakaporudi duniani kutawala. Kwa wakati ule mvinyo itakuwa na maana mpya; itasema juu ya furaha na baraka ya **ufalme wa Baba** yake.

Watu wengine wanauliza kama ikitupasa kuwa na mkate wenye chachu au bila chachu, na mvinyo inayochachuka kwa karamu ya ukumbusho. Bila shaka Bwana alitumika na mkate usiochachwa na mvinyo iliyochachuka (mvinyo *yote* ilichachuka kwa wakati ule). Wale wanaosema mkate wenye chachu unaharibu mfano wa Mwili wa Kristo (kwani chachu ni mfano wa zambi) wakumbuke kwamba ni vivyo hivyo na kuchachuka kwa mvinyo. Ni huzuni kubwa kama tukiwaza sana sana juu ya *vitu hivi* hata tunakosa kuona *Bwana*

*mwenyewe.* Paulo alisema kwamba neno kubwa si mkate wenyewe, lakini maana yake ya roho. “Kwa sababu Kristo, Pasaka yetu, amekwisha kutolewa kwa ajili yetu; basi, tufanye karamu, si kwa chachu ya zamani, wala kwa chachu ya uovu na ubaya, lakini kwa mkate usiochachwa, ndio moyo safi na kweli.” (1 Kor. 5:7,8). Neno kubwa si chachu ndani ya *mkate* lakini chachu (ndiyo zambi) ndani ya *maisha yetu*!

### F. Wanafunzi wenye kujitumainia wenyewe (26:30-35)

**26:30** Nyuma ya karamu ya ukumbusho, Bwana na wanafunzi wake waliimba **wimbo** (labda moja ya zaburi 113-118). Kisha walitoka Yerusalema, wakavuka kijito Kiduroni na kupanda mlima wa Mizeituni hata shamba la Getesemane.

**26:31** Bwana Yesu alikuwa amejulisha wanafunzi wake tena na tena habari za maneno yatakayotokea. Sasa aliwaambia waziwazi ya kwamba wao wote watamwacha **usiku ule.** Watashindwa na woga wakati watakapoona askari na makutano wakikaribia kukamata Yesu. Wakitaka kuponyesha maisha yao wenyewe wataacha Bwana wao. Unabii wa Zekaria utatimizwa, ndio “Piga mchungaji na kondoo watasambazwa” (Zek. 13:7).

**26:32** Lakini hakuwaacha bila tumaini. Hata wao wakiwa na haya kwa sababu ya ushirika wao naye, Yeye hatawaacha kamwe. Nyuma ya ufufuko wake atakutana nao katika **Galilaya.** Kweli yeye ni Rafiki ya ajabu ambaye hatatupungukia kamwe!

**26:33, 34** Petro, bila kufikiri, alisema na Bwana hata wote wakimwacha, yeye hatafanya hivi **kamwe**. Lakini Yesu aligeuza “kamwe” kuwa “**usiku huu … mara tatu.**” Mbele ya kuwika kwa **jogoo**, Petro atakana Bwana wake **mara tatu.**

**26:35** **Petro** alikaa kusema alikuwa tayari **kufa** pamoja na Kristo kwa pahali pa **kumkana**. **Wanafunzi wote** walisema vivi hivi, na roho ya kweli; hawakufahamu uzaifu wa mioyo yao.

### G. Maumivu kwa Getesemane (26:36-46)

Wakati tunaposoma mashairi haya tunafahamu kwamba kweli ni habari takatifu kabisa.

**26:36-38** Nyuma ya kuingia **Getesemane** (maana ya jina hili ni shinikizo la zeituni), **Yesu** alisema na wanane wa **wanafunzi** wake kumi na mmoja kuketi pale saa yeye alipokwenda kuomba, na alitwaa **Petro na wana wawili wa Zebedayo** kwenda pamoja naye. Labda wanafunzi hawa waliweza kushiriki kupita wengine ndani ya maumivu makubwa ya roho ya Mwokozi?

**Akaanza kuhuzunika na kufazaika sana.** Alijulisha Petro, Yakobo na Yoane wazi kwamba **roho yake ilikuwa na huzuni sana, hata kufa**. Bila shaka yalikuwa machukizo makubwa ya tabia yake takatifu wakati alipotazamia kugeuka zabihu ya zambi kwa sisi. Sisi tulio wenye zambi hatuwezi kufahamu hata kidogo taabu kubwa ya Huyu, asiyekuwa na zambi, kufanywa zambi kwa ajili yetu (2 Kor. 5:21).

**26:39** Hatushangai kumwona akiacha wale wanafunzi watatu na **kwenda mbele kidogo.** Hakuna mtu aliyeweza kushiriki ndani ya taabu yake wala kuomba ombi lake, **“Ee Baba yangu, kama ikiwezekana kikombe hiki kinipitie; lakini si kama ninavyotaka mimi, lakini kama wewe unavyotaka.”**

Ukifikiri maombi haya yanaonyesha ya kwamba Bwana alitaka kurudi nyuma, kumbuka masemo yake katika Yoane 12:27, 28, “Sasa roho yangu inafazaika; nami nitasema nini? Baba,

uniokoe kwa saa hii. Lakini ni kwa sababu hii nimefika kwa saa hii. Baba, utukuze jina lako." Hivi wakati alipoomba **kikombe kimpitie** *hakuomba* kuponyeshwa asife msalabani. Hili lilikuwa kusudi kwa kufika kwake duniani!

Ombi hili linatufundisha neno kubwa. Yesu aliomba Baba yake kama kulikuwa na njia nyingine kuokoa wenye zambi bila kufa kwake msalabani, afunue njia hii sasa. Lakini alitaka ijulikane wazi kwamba hakutaka neno lo lote lisilopatana na mapenzi ya Baba yake.

Jibu la ombi hili lilikuwa nini? Jibu halikuwa! Mbingu zilikuwa kimya! Neno hili linatufahamisha kwamba hakuna njia nyingine kwa Mungu kuhesabia wenye zambi haki ila kwa Kristo, asiyekuwa na zambi, kufa kuwa Mkombozi wetu.

**26:40, 41** Wakati alipofika karibu na **wanafunzi** wake **aliwakuta wakilala.** Walikuwa na **roho tayari**, lakini **miili** yao ilikuwa **zaifu**. Hatuwezi kuwahukumu wakati tunapowaza juu ya maisha yetu. Mara nyingi tunashindwa na usingizi wakati tunapoomba; mara ngapi tunaanza kufikiri juu ya mambo mengine wakati inapotupasa kuangalia. Mara ngapi inapasa Bwana kusema nasi kama alivyosema na Petro, **"Hamukuweza kuangalia pamoja nami saa moja? Angalieni na kuomba, musiingie katika majaribu."**

**26:42 Akakwenda tena mara ya pili,** akinyenyekea mapenzi ya Baba. Atakunywa kikombe cha maumivu na mauti yote pia.

Hakuweza kushiriki na wengine ndani ya maombi yake. Alikuwa amefundisha wanafunzi kuomba, aliomba kwa masikio yao, lakini hakuomba kamwe *pamoja* nao. Alikuwa namna nyingine na watu wengine wote, na kwa sababu hii hawakuweza kushiriki naye ndani ya maombi yake.

**26:43-45** Wakati alipofikia wanafunzi wake mara ya pili, walikuwa **wakilala tena**. Vivyo hivyo mara ya tatu. Aliomba, nao walilala. Halafu alisema nao, **"Laleni sasa na kupumzika; tazama, saa imekaribia na Mwana wa watu ametolewa mikononi mwa wenye zambi."**

**26:46** Saa ya kuangalia pamoja naye ndani ya maombi yake ilikuwa imepita. Waliweza kusikia mhaini akikaribia. Yesu akasema, **"Simameni, twendeni",** – si kukimbia, lakini kukutana na adui uso kwa uso.

Mbele ya kuondokea shamba lile, tusimame kwanza kusikia mara moja tena kuugua kwake, kuwaza juu ya huzuni yake, na kumshukuru na mioyo yetu yote.

### H. Yesu anatolewa kwa hila, na kufungwa kwa Getesemane (26:47-56)

Kutolewa kwa Mwokozi asiyekuwa na zambi na mmoja wa viumbe vyake ni tukio ambalo hatutaweza kufahamu kamwe. Hakuna njia kueleza tendo baya kupita yote la Yuda, isipokuwa tunakumbuka upotovu wa binadamu.

**26:47** Wakati Yesu alipokuwa **akisema** kwa wanafunzi kumi na mmoja, **Yuda** alifika na makutano makubwa na **panga na magongo**. Hatufikiri Yuda alikusudi wafike na vitu hivi vya vita; hakuona Mwokozi hata mara moja akipiga vita au kushindana na adui. Labda wakubwa wa makuhani na wazee waliagiza watu wafike navyo kusudi Yesu asiwe na njia kukimbia.

**26:48** Yuda atatumika na busu kuonyesha nani ndiye Yesu. Alama hii iliyo alama ya mapendo duniani pote, itachafuwa kabisa.

**26:49** Wakati Yuda alipokaribia Yesu, alisema naye, **"Salamu, Rabi!,"** kisha **alimbusu**. Kuna maneno mbalimbali mawili ndani ya mashairi haya yana-

yotafsiriwa *busu*. La kwanza, ndani ya shairi 48, ni neno ambalo watu walitumia karibu kila mara. Lakini maana ya neno la pili lililotafsiriwa *busu* ndani ya shairi 49, ni kubusu *sana sana.*

**26:50** Na utulivu wote Yesu alisema naye, **"Rafiki, fanya neno ulilokuja kufanya."** Bila shaka kuitwa *rafiki* kulichokoza roho ya Yuda! Halafu watu wakakuja, wakakamata Bwana Yesu mara moja.

**26:51** Mmoja wa wanafunzi (alikuwa Petro, Yn. 18:10) **akafuta upanga wake,** akapiga mtumwa wa kuhani mkubwa na **kukata sikio** lake. Hatufikiri lilikuwa kusudi la Petro kukata sikio lake tu; bila shaka alikusudi kumwua mara moja, lakini Mungu alizuiza neno hili.

**26:52** Utukufu wa Bwana Yesu ulionekana wazi hapa. Kwanza alihamakia Petro, akamwagiza: **"Rudisha upanga wako pahali pake; kwani wote wanaoshika upanga wataharibiwa kwa upanga."** Ndani ya ufalme wa Kristo hakuna kushinda kwa njia ya **kutumika na vitu vya mwili.** Adui za ufalme wanatumika na panga, na mwishoni watashindwa. Silaha ya Mkristo ni maombi, neno la Mungu, na kuishi maisha yanayojazwa na Roho Mtakatifu.

Halafu mganga Luka anatujulisha kwamba Yesu, akitenda kwa neema, aliponyesha sikio la Malko – hili ndilo jina la mtumwa mwenyewe (Lk. 22:51; Yn. 18:10). Alipenda wale ambao walimchukia, na kutendea mema wale ambao walitaka kumwua.

**26:53, 54** Kama Yesu angalitaka kushindana na makutano kama asingalihitaji kutegemea upanga mdogo wa Petro. Dakika ile ile angaliweza kuomba na kutumwa **zaidi ya majeshi kumi na mawili ya malaika** (kutoka 36.000 kufika 72.000). Lakini neno hili lingalizuiza shauri la Mungu lisitimizwe. Ilikuwa lazima kwa unabii katika **Maandiko** juu ya kutolewa kwa Kristo kwa adui, mateso yake, kusulibishwa kwake, na ufufuko wake **kutimizwa.**

**26:55** Halafu Yesu alikumbusha makutano kwamba ilikuwa pumbavu kwao kutokea kumkamata na silaha. Hawakumwona hata mara moja ndani ya maisha yake mazima akitumika na silaha. Alifundisha watu **hekaluni kila siku,** na ingalikuwa nyepesi kumkamata saa ile. Kwa sababu gani walifika sasa na **panga na magongo**?

**26:56** Lakini Mwokozi alifahamu kwamba uovu wa watu ulikuwa ukitimiza shauri la Mungu. **"Maneno haya yote yamekuja ili maandiko ya manabii yatimizwe."** Basi wanafunzi walifahamu kwamba hakuna njia kwa Bwana wao kuokolewa, nao **"wote wakamwacha, wakakimbia"** na woga mkubwa. Tukumbuke kwamba hawakukaaliwa bado na Roho Mtakatifu kama sisi.

### I. Yesu mbele ya Kayafa (26:57-68)

**26:57** Bwana Yesu alihukumiwa na viongozi vya dini vya Wayuda na serikali ya Waroma vilevile. Tukisoma habari hizi ndani ya Habari Njema ine zote pamoja tunaona kwamba alifikishwa mara tatu mbele ya viongozi vya Wayuda, na mara tatu mbele ya serikali ya Waroma. Ndani ya Yoane tunasoma kwamba alifikishwa kwanza kwa baba ya mke wa Kayafa, ndiye Ana. Matayo alianza na habari za sehemu ya pili ya hukumu yake mbele ya watu wa dini, nyumbani mwa **Kayafa, kuhani mkubwa.** Watu wa Baraza **walikuwa wamekutana** pale. Ilikuwa desturi kuwapa watu walioshitakiwa njia kujisimamia wenyewe, lakini viongozi hawa wa dini, wakitenda kwa haraka, hawakufanya hivi (Isa. 53:8), na walifunga njia kwa yeye kuhukumiwa kwa haki.

Usiku ule Wafarisayo, Wasadukayo,

**waandishi** na **wazee**, ndio watu wa Baraza, waliona bure kabisa amri zao wenyewe kwa makusanyiko namna hii. Walikatazwa kukutana usiku au kwa siku kubwa zo zote za Wayuda. Hawakuwa na ruhusa kutoa rushwa kupata washuhuda wa uwongo. Ilikuwa sharti kwa usiku mmoja kupita mbele ya kuua mtu aliyehukumiwa kufa. Na sharti viongozi wakutane kwa pahali fulani hekaluni kwa hukumu zao ziweze kutimizwa. Lakini wakitaka sana sana kuondoa Yesu mbio katikati yao, hawakusita kuvunja sheria zao wenyewe.

**26:58** Mwamuzi wa kusanyiko hili alikuwa Kayafa. Ni kama watu wa Baraza walikuwa waamuzi na washitaki vilevile mara hii, neno lisilopatana na utaratibu wao. Yesu alikuwa mshitakiwa. Na **Petro** aliangalia – toka mbali kidogo; **akaketi pamoja na watumishi aone mwisho.**

**26:59-61** Ilikuwa nguvu kwa viongozi hawa Wayuda kupata watu kushuhudia Yesu **maneno yasiyokuwa kweli.** Mwishoni **washuhuda wa uwongo wawili** walipatikana, waliopotoa maneno Yesu aliyosema mwenyewe: “Vunjeni hekalu hili nami nitalisimamisha kwa siku tatu” (Yn. 2:19-21). Washuhuda hawa walisema Yesu alitangaza kwamba **ataharibu hekalu** katika Yerusalema na kulijenga tena. Lakini Yesu alikuwa amesema juu ya mauti yake mwenyewe na ufufuko wake. Sasa Wayuda walitaja unabii huu kama sababu kwa kumwua.

**26:62-63** Bwana Yesu alisikia mashitaki haya yote, lakini hakusema neno: “kama kondoo anavyonyamaza mbele yao wanaokata manyoya yake, hakufungua kinywa chake” (Isa. 53:7). Neno hili lilikasirisha kuhani mkubwa, akajaribu kusukuma Mwokozi kusema neno, lakini yeye hakufungua kinywa chake. Halafu kuhani mkubwa alisema naye, **“Ninakuapiza kwa Mungu aliye hai, utuambie kama wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu!”** Sheria ya Musa ililazimisha Myuda kutoa ushuhuda kama kuhani mkubwa akimwagiza kufanya hivi (Law. 5:1).

**26:64** Akiwa Myuda aliyetii sheria, Yesu alijibu, **“Wewe umesema.”** Na kuonyesha kwamba kweli yeye ni Masiya, aliongeza, **“Lakini ninawaambia ninyi, Tangu sasa mutaona Mwana wa watu akiketi kwa mkono wa kuume wa uwezo, na akikuja juu ya mawingu ya mbingu.”** Hii ndiyo maana ya maneno aliyosema, “Mimi ni Kristo, Mwana wa Mungu, kama (wewe Kayafa) ulivyosema. Kwa wakati wa sasa utukufu wangu unafichwa ndani ya mwili wa mtu; ninaonekana kama watu wengine. Unaniona kwa wakati wa aibu yangu lakini kwa wakati wa kuja ninyi (ndio Wayuda watakaokuwa hai wakati Kristo atakapotokea na utukufu) mutaniona kama mwenye kutukuzwa, sawasawa na Mungu ndani ya maneno yote, nikiketi kwa mkono wake wa kuume na nikikuja na mawingu ya mbingu.” Watafahamu bila shaka kwamba yeye ni Mwana wa Mungu.

Lenski aliandika kwamba watu wengine wanasema, “Yesu hakujiita kamwe ‘Mwana wa Mungu.’ Hapa (katika shairi 64) alitoa *kiapo* kwamba yeye ndiye Mwana wa Mungu.”[11]

**26:65-67** Kayafa alifahamu maana ya masemo ya Yesu. Alikuwa ametaja tu unabii wa Danieli juu ya Masiya, “Nikaona katika maono ya usiku, na tazama, pamoja na mawingu ya mbingu alikuja mmoja aliye mfano wa mwana wa watu, akakaribia huyu mzee wa siku, wakamleta karibu naye.” (Dan. 7:13). Kuhani mkubwa alifahamu kwamba Yesu alikuwa akisema yeye ni sawasawa na Mungu (ona Yn. 5:18). **Alipasua mavazi yake** ya ukuhani, ndiyo alama kuonyesha kwamba Yesu alikuwa amekufuru. Aliuliza watu wa baraza kama

Yesu alikuwa na kosa. Wao wote walijibu, **"Anastahili kufa."**

**26:68** Sehemu ya pili ya hukumu ya mshitakiwa ilikwisha, na waamuzi wake walimpiga na kumtemea mate, kisha walimzihaki na kusema naye atumike na uwezo wake kama **Kristo** kutaja wale ambao walimtendea jeuri. Matendo ya waamuzi haya yalikuwa ya kuchukiza kabisa.

### J. Petro anakana Yesu na kulia kwa uchungu (26:69-75)

**26:69-72** Saa ya taabu kubwa zaidi ilikuwa imefikia Petro. Wakati alipoketi **inje katika kiwanja**, kijakazi mmoja akakuja na kusema na Petro kwamba alikuwa pamoja na Yesu mbele. Petro alibisha maneno yake na ukali akisema, **"Sijui maneno unayosema."** Alitoka **inje hata baraza,** labda na kusudi watu wasikae kumtambua kama mmoja wa wafuata wa Yesu, lakini **kijakazi mwingine** alisema naye wazi mbele ya watu kwamba alikuwa mmoja wa wale waliokuwa **pamoja na Yesu wa Nazareti**. Mara hii Petro alikana na kiapo kwamba hajui **mtu huyu**. **"Mtu huyu"** alikuwa Bwana wake.

**26:73,74 Nyuma kidogo** watu waliosimama pale walikuja na kumwambia, **"Hakika wewe ni mmoja wao; kwa sababu hata usemi wako unaonyesha hivi."** Mara hii Petro alikana masemo yao na kulaani na kuapa, **"Sijui mtu huyu!"** Na saa ile ile **jogoo aliwika.**

**26:75** Kuwika kwa jogoo asubui mapema kulichoma roho ya Petro, akakumbuka maneno Bwana aliyosema, **akatoka inje, akalia kwa uchungu.**

Habari tunazosoma ndani ya vitabu vya Habari Njema ine ni mbalimbali kidogo. Ndani ya Matayo, Luka, na Yoane, tunasoma kwamba Yesu alisema, "Mbele ya kuwika jogoo, utanikana mara tatu" (Mt. 26:34; ona vilevile Lk. 22:34; Yn. 13:38). Ndani ya Marko 14:30 alisema, "… mbele ya kuwika jogoo mara mbili utanikana mara tatu."

Labda jogoo kuliko moja iliwika siku ile, moja katikati ya usiku na moja kwa mapambazuko. Na vilevile labda vitabu vya Habari Njema vinapasha kwamba Petro alikana Bwana wake mara sita. Alikana Kristo mbele ya (1) kijakazi (Mt. 26:69-70; Mk. 14:66-68); (2) kijakazi mwingine (Mt. 26:71,72; Mk. 14:69,70); (3) watu waliosimama pale (Mt. 26:73,74; Mk.14:70,71); (4) mtu mmoja (Lk. 22:58); (5) mtu mwingine (Lk. 22:59,60); (6) mtumishi wa kuhani mkubwa (Yn. 18:26,27). Tunaamini ya kwamba mtu huyu wa mwisho alikuwa mbali na wale wengine ambao walimtangulia, kwa sababu alisema, "Sikukuona katika shamba pamoja naye?" Hatusomi kwamba wengine walisema hivi.

### K. Hukumu asubui mbele ya Baraza (27:1, 2)

Sehemu ya tatu ya hukumu mbele ya viongozi vya dini ilikuwa mbele ya wakubwa wa makuhani na wazee wa watu **asubui.** Sheria yao ilikataza hukumu ya mshitakiwa kumalizwa mbele ya kupita kwa usiku mmoja isipokuwa mshitakiwa aliachiliwa. Haikuwa taratibu kuhukumu watu usiku. Wakubwa walikusanyika asubui kusudi hukumu yao ionekane kuwa taratibu kwa maneno ya sheria.

Wayuda walitawaliwa na Waroma na hawakuwa na ruhusa kuhukumu mtu kufa bila ukubali wao. Hivi sasa viongozi Wayuda walifikisha Yesu kwa haraka mbele ya **Pontio Pilato**, ndiye **liwali** ya Waroma. Walichukia Waroma sana lakini walichukia Yesu kupita. Ni kama machukio yao ya Yesu yanapatanisha hata watu wanaochukiana sana.

### L. Majuto na mauti ya Yuda ( 27:3-10)

**27:3,4 Yuda** alikuwa amefahamu sasa zambi yake kubwa ya **kutoa damu isiyo**

**na kosa,** na alitaka kurudisha mali yenyewe kwa **wakubwa wa makuhani na wazee**. Lakini watu wale waliofurahi kupatana naye, walikataa kushiriki ndani ya maneno haya tena. Ndiyo, Yuda **alijuta**, lakini majuto yake hayakuwa toba ya kweli inayoleta wokovu. Alihuzunishwa juu ya ubaya aliotenda, lakini hakuwa tayari kupokea Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wake.

**27:5** Akikata tamaa, Yuda **akatupa vipande vya feza katika pahali patakatifu,** pahali makuhani tu walipokuwa na ruhusa kwenda, akatoka na kujiua. Tukisoma shairi hili pamoja na Matendo 1:18, ni kama alijitundika juu ya mti, kamba au tawi la mti lilivunjika, na mwili wake ulianguka chini, ukipasuka, na matumbo yake yote yalitoka.

**27:6 Wakubwa wa makuhani** walifikiri haifai kuweka mali hii ndani ya **sanduku ya hazina** hekaluni kwa sababu ilikuwa **bei ya damu,** lakini wao ndio wenye hatia ya kulipa mali hii kusudi Masiya atolewe kwao. Ni kama hawakuweka roho juu ya neno hili. Kama Bwana alivyosema mbele, walisafisha upande wa inje wa kikombe, lakini ndani kilijaa na udanganyifu, hila na uuaji.

**27:7-10** Walitumika na mali hii kununua **shamba la mfinyanzi** kuwa pahali pa maziko ya wageni wa mataifa wasiokuwa safi, waweze kuzikwa. Hawakujua kwamba watu wengi sana wa Mataifa wataingia inchi yao na kunyunyizia njia za mji damu. Ni **shamba la damu** hata sasa kwa taifa lile lenye hatia.

Bila kufahamu, wakubwa wa makuhani walitimiza unabii wa Zekaria ya kwamba watatumika na mali hii kununua shamba la mfinyanzi (Zek. 11:12,13).

Matayo alisema maneno haya yalitimiza unabii wa **Yeremia**, lakini ni wazi kwamba unabii huu ulitoka kitabu cha Zekaria. Tunafikiri Matayo alisoma toka gombo refu la maandiko katika Kiebrania lililoanza na Yeremia.

### M. Yesu anasimama mbele ya Pilato mara ya kwanza (27:11-14)

Wayuda walishitaki na kuhukumu Yesu juu ya maneno ya *dini*, lakini waamuzi Waroma waliona mashitaki juu ya dini bure. Wayuda walijua neno hili, hivi wakati walipofikisha Yesu mbele ya Pilato walimshitaki juu ya maneno ya serikali (Luka 23:2). Walisema: 1) alikuwa mtu wa hatari kwa ufalme wa Roma; 2) alikataza watu wasilipe kodi, na kwa njia hii alipunguza kusitawi kwa ufalme; 3) alisema yeye ni mfalme, ndilo neno lililoweza kuhatarisha uwezo na cheo ya mfalme.

Ndani ya Habari Njema ya Matayo tunaona Pilato akiuliza Yesu juu ya shitaki la tatu. Wakati alipomwuliza kama yeye ni **Mfalme wa Wayuda**, Yesu alijibu, "**Wewe unasema**." Wakati viongozi vya Wayuda waliposikia jibu lake walitoa mashitaki mabaya sana na masingizio machafu. Yesu hakujibu hata moja la mashitaki yao, na Pilato **alishangaa sana.** Labda hakuona kamwe mshitakiwa akikaa kimya kwa wakati wa kushitakiwa na ukali namna hii.

### N. Yesu au Baraba? (27:15-26)

**27:15-18** Ilikuwa desturi ya Waroma kutuliza roho za Wayuda kwa njia ya **kufungua mfungwa** Myuda mmoja kwa wakati wa Pasaka. Mfungwa mmoja aliyeweza kufunguliwa alikuwa Baraba, aliyekuwa ametenda fitina na uuaji (Mk. 15:7). Alikuwa mwasi wa utawala wa Waroma, hivi bila shaka alipendwa na Wayuda wenzake. Hivi wakati Pilato alipouliza kama walitaka **Yesu** au **Baraba** kufunguliwa, walichagua Baraba. Pilato hakushangaa juu ya neno hili kwani alijua wakubwa wa makuhani walikuwa wameshawishi watu kuchagua hivi, kwa sababu ya uwivu.

**27:19** Maendeleo ya hukumu yalisimamishwa kwanza wakati mjumbe wa **mke** wa Pilato alipofika na habari kwaye. Alisukuma mume wake asishiriki ndani ya hukumu ya Yesu kwa sababu ya **ndoto** mbaya ambayo alikuwa nayo **juu ya Yesu**.

**27:20-23 Wakubwa wa makuhani na wazee** walikuwa wakisukuma watu kwa siri kuomba kwa **Baraba** kufunguliwa na kwa mauti ya Yesu. Hivi wakati **Pilato** alipouliza watu tena kama walitaka nani kufunguliwa, walilia mwuaji afunguliwe. Halafu Pilato aliuliza, **"Basi, nitafanya nini na Yesu anayeitwa Kristo?"** Wao wote na sauti moja walilalamika auawe. Ilishinda Pilato kufahamu jibu lao. Kwa nini atasulibishwa? Alikuwa ametenda mabaya gani? Lakini hakuweza kugeuza mafikiri na machafuko yao. Walikaa kulalamika, **"Asulibiwe."**

**27:24 Pilato** alifahamu kwamba hakuna njia kugeuza roho za watu, na fujo lilikuwa limeanza. Hivi **alinawa mikono yake** mbele ya makutano akisema hana kosa katika **damu** ya Mshitakiwa huyu. Lakini maji hayataweza kamwe kuzima hatia kubwa ya Pilato na ukosefu wa haki wa hukumu yake.

**27:25** Makutano, kama wenye wazimu wasioweka roho juu ya hatia, walikuwa tayari kubeba matunda ya zambi ile kubwa. Wakalalamika, **"Damu yake iwe juu yetu na juu ya watoto wetu!"** Na tangu wakati ule Waisraeli wameteswa sana sana kwa njia mbalimbali, wakitaabishwa kwa sababu ya hatia yao kubwa sana ya damu ya Masiya ambaye walimkataa. Na muda wa mateso makubwa zaidi ni kwanza mbele yao – wakati wa kuogopesha wa Taabu ya Yakobo – miaka saba ya taabu kupita yote. Tunasoma habari zao katika Matayo 24 na Ufunuo 6–19. Laana hii haitaondoshwa kufika wakati watakapokiri kwamba Yesu ambaye walimkataa ni kweli Masiya-Mfalme wao.

**27:26** Pilato **akafungulia** makutano **Baraba,** na roho ya Baraba imetawala dunia tangu siku ile, na Mfalme wa haki anakataliwa hata sasa. Halafu, kama ilivyokuwa desturi, Mshitakiwa alipigwa mijeledi. Walifunga vipande vya chuma vikali sana ndani ya fimbo hii ya ngozi, na kupiga mgongo wa Yesu nayo. Mwili wake ulipasuliwa mpaka damu ilivuja sana. Hakuna neno lingine lililobaki sasa kwa liwali yule zaifu kufanya, ila kumtoa kwa askari **asulibishwe.**

### O. Askari wanazihaki Yesu (27:27-31)

**27:27,28 Askari za liwali wakachukua Yesu** kwa nyumba kubwa ya liwali, **wakakusanya kwake kikosi kizima** – mia za watu. Inatushinda kuwaza na kufahamu maneno yaliyofuata. Wale askari wakali na waovu walitendea Mwumba wao na Mwenye kutegemeza ulimwengu haya na aibu kupita kusema. **Walimwondolea mavazi yake na kumvika na nguo nyekundu**, mwigo wa vazi la mfalme. Lakini vazi hili linatufikirisha neno kubwa. Rangi ya nyekundu inasema juu ya zambi (Isa. 1:18), na ninapenda kufikiri kwamba vazi lile ni mfano wa zambi zangu zikiwekwa juu ya Yesu ili vazi la haki ya Mungu liweze kuwekwa juu yangu (2 Kor. 5:21).

**27:29, 30** Wakasokota **taji ya miiba** na kuisukuma **juu ya kichwa chake** na nguvu. Wao walitenda hivi kama michezo iliyokosa adabu, lakini sisi tunajua kwamba alivaa *taji ya miiba* ili sisi tuweze kuvaa *taji ya utukufu.* Walimzarau kama Mfalme wa Zambi; sisi tunamwabudu kama Mwokozi wa wenye zambi.

Wakampa **tete** vilevile – mwigo wa zihaka wa fimbo ya mfalme. Hawakujua kwamba yule ambaye alishika tete hii ndiye anayetawala ulimwengu mzima.

Walipiga magoti **mbele yake** na kumwita **Mfalme wa Wayuda.** Zaidi ya

ile **walitemea mate** Mtu mkamilifu wa pekee, **wakakamata fimbo** ambayo walimpa mbele, **wakampiga kichwani** nayo.

Yesu alivumilia maneno haya yote na saburi; hakusema neno. "Maana kumbukeni sana yeye aliyevumilia mabishano makubwa namna hii ya wenye zambi juu yake, kusudi musipate kuchoka wala kulegea katika nafsi zenu" (Ebr. 12:3).

**27:31** Mwishoni **walimvika mavazi yake mwenyewe tena, wakamchukua inje kwa kumsulibisha.**

**P. Kusulibishwa kwa Mfalme (27:32-44)**

**27:32** Bwana wetu **alibeba msalaba** wake kwa sehemu ya kwanza ya njia (Yn. 19:17). Nyuma yake askari **walilazimisha** mtu mmoja jina lake **Simon**i (toka **Kurene** kwa upande wa kaskazini wa Afrique) kuubeba. Watu wengine wanafikiri Simoni alikuwa Myuda, au mtu wa Afrique. Neno kubwa ndilo hili: alipewa heshima kubwa ya kubeba msalaba wa Yesu.

**27:33 Golgota** ni neno kwa lugha ya Kiaramaic kwa "mfupa wa kichwa." Labda pahali pale palifanana na mfupa wa kichwa au paliitwa na jina hili kwa sababu watu waliuawa pale. Hatujui kabisa kama pahali penyewe palikuwa wapi.

**27:34** Mbele ya kufunga Yesu juu ya msalaba na misumari askari walimtolea mvinyo iliyochanganyika na nyongo, kama ilivyokuwa desturi kufanya kwa wavunja sheria waliohukumiwa kufa kupunguza maumivu yao, lakini Yesu alikataa kuipokea. Ilikuwa lazima kwa yeye kubeba mzigo mzima wa zambi za watu bila kitu kupunguza ufahamu au maumivu yake.

**27:35** Matayo aliandika maneno machache tu juu ya kusulibishwa kwake: "… wakati **walipokwisha kumsulibisha**" – hatutaweza kufahamu maana ya maneno haya kwa milele.

Kama ilivyotabiriwa katika Zaburi 22:18, **askari waligawa mavazi yake wakipiga kura.** Yalikuwa mali yake yote hapa duniani.

**27:36** Askari hawa walikuwa mfano wa watu wanyonge wa dunia. Hawakufahamu hata kidogo maneno makubwa yaliyokuwa yakitokea. Kama wangalifahamu kama wasingali*keti* na **kumlinda**; wangali*piga magoti* na **kumwabudu.**

**27:37 Juu ya kichwa** cha Kristo walikuwa wameandika maneno haya, **"HUYU NI YESU MFALME WA WAYUDA."** Maneno haya ni mbalimbali kidogo ndani ya Habari Njema ine. Marko aliandika "Mfalme wa Wayuda" (Mk. 15:26); Luka: "Huyu ni Mfalme wa Wayuda" (Luka 23:38); na Yoane: "Yesu Mnazareti, Mfalme wa Wayuda" (Yn. 19:19). Wakubwa wa makuhani walinungunika juu ya maandiko haya, lakini Pilato alikataa kuyageuza; yalikuwa kweli, na wazi kwa watu kusoma – kwa Kiebrania, Kiroma na kwa Kiyunani (Yn.19:19-22).

**27:38 Wanyanganyi wawili** walisulibishwa pamoja na Mwana wa Mungu asiyekuwa na zambi, mmoja kwa upande wake wa kuume na mwingine kwa upande wa kushoto. Neno hili lilitimiza unabii wa Isaya miaka 700 mbele ya kwamba atahesabiwa pamoja na wale wenye kukosa (Isa. 53:12). Kwanza wanyanganyi wawili wote walimtukana (sh.44), lakini nyuma kidogo mmoja wao alitubu na aliokolewa; nyuma ya saa chache alikuwa pamoja na Kristo katika Paradiso (Lk. 23:42,43).

**27:39,40** Msalaba unafunua mapendo ya Mungu, lakini unafunua vilevile upotovu wa watu. Wale waliopita njiani walisimama kwa saa ndogo kuzarau Mchungaji saa alipokuwa akikufia kondoo: **"Wewe mwenye kuvunja he-**

**kalu na kulijenga tena katika siku tatu, ujiokoe mwenyewe; kama ukiwa Mwana wa Mungu, shuka msalabani."** Ni namna ya masemo ya wasioamini hata kwa wakati wa sasa. Wanasema, "Tuone kwanza na macho, halafu tutaamini." "Shuka msalabani – au kusema, ukiondosha uchungu wa msalaba tutaamini." William Booth alisema, "Walisema kama angalishuka toka msalaba wangaliamini; sisi tunaamini kwa sababu hakushuka!"

**27:41-44 Wakubwa wa makuhani, waandishi na wazee** waliongeza, bila kufahamu maana ya maneno yao, "**Aliokoa wengine; hawezi kujiokoa yeye mwenyewe."** Walisema hivi kwa kumzarau, lakini sisi tunajua walisema kweli. Asingaliweza kuokoa watu kama angalijiokoa mwenyewe. Na ni kweli ndani ya maisha yetu vilevile. Hatuwezi kuleta watu kwa Kristo bila kujitoa wenyewe kwa kazi hii.

Viongozi vya watu kwa maneno ya dini walimzarau kwa sababu alisema yeye ni **Mfalme wa Israeli** na **Mwana wa Mungu,** na hata **wanyanganyi** walishiriki ndani ya matukano yao ya Mungu.

### Q. Saa tatu ya giza (27:45-50)

**27:45** Maumivu na haya yote Bwana Yesu aliyopokea toka mikono ya watu yalikuwa nusu wakati yanaposawanishwa na taabu kubwa ambayo ilimpata sasa. **Toka saa sita** (ya mchana) **kufika saa tisa giza lilikuwa juu ya inchi yote ya Palestina** na ndani ya roho yake takatifu vilevile. Kwa muda ule alibeba laana linayopita ufahamu la zambi zetu. Ndani ya saa zile tatu alibeba maumivu yote ya Gehena ya moto sisi tuliyopaswa kupata, gazabu ya Mungu kwa makosa yetu yote. Tunaweza kufahamu nusu tu. Inatushinda kabisa kujua taabu, maumivu, na uchungu wote aliobeba kutimiza hukumu ya haki ya Mungu kwa zambi zetu. Tunajua tu ya kwamba ndani ya saa zile tatu alilipa bei kubwa kwa deni ya zambi, na kutimiza kazi iliyohitajiwa kwa ukombozi wa watu.

**27:46** Karibu na saa tisa **alipaza sauti kubwa akisema, "Mungu wangu, Mungu wangu, kwa nini umeniacha?"** Jibu kwa ulizo hili ni ndani ya Zaburi 22:3, "… wewe ni mtakatifu … wewe unayeketi juu ya sifa za Israeli." Kwa sababu Mungu ni mtakatifu, hawezi kuona zambi bure. Ni lazima kwake kuiazibu. Bwana Yesu hakuwa na zambi hata moja, lakini alibeba yeye mwenyewe hatia ya zambi zetu. Wakati Mungu, kama Mwamuzi, alipoangalia na kuona zambi zetu juu ya Mkombozi wetu asiyekuwa na zambi aliachana na Mwana wa mapendo yake. Kuachwa hivi na Mungu kuliumiza roho ya Mwana wake sana.

**27:47,48** Wakati Yesu alipolia, **"Eloi, Eloi … ," wengine waliosimama karibu walisema ... anaita Elia**. Hatujui kama walisema hivi na kuzarau au kwa sababu walifikiri kweli alikuwa akiita Elia. Mmoja wao alijaza **sifongo siki,** akamkunywesha. Zaburi 69:21 linaonyesha kwamba neno hili halikuwa tendo la huruma, lakini kusudi lake lilikuwa kuongeza maumivu yake.

**27:49** Watu walingoja **kuona kama Elia** atakuja kweli kumwokoa. Lakini huu haukuwa wakati kwa kutokea kwa Elia (Mal. 4:5); lakini kwa kufa kwa Yesu.

**27:50** Wakati Yesu **alipotoa sauti kubwa tena, alitoa roho yake.** Alitoa sauti **kubwa** kuonyesha kwamba alikufa akiwa mwenye nguvu, si katika uzaifu. Na kwa njia ya **kutoa roho yake yeye mwenyewe** mauti yake ilikuwa mbali na mauti ya watu wote wengine. Sisi tunakufa kwa sababu ni lazima kwetu kufa; Yeye alikufa kwa sababu alichagua kufa. Alikuwa amesema, "Ninatoa uzima wangu, ili niutwae tena. Hakuna mtu anayeuondoa

kwangu, lakini mimi mwenyewe ninautoa. Nina uwezo kuutoa, na nina uwezo kuutwaa tena." (Yn. 10:17,18).

**R. Pazia linapasuka (27:51-54)**

**27:51** Kwa wakati alipotoa roho, pazia zito la nguo lililogawa vyumba vikubwa viwili hekaluni lilipasuliwa na Mkono usioonekana **toka juu hata chini**. Kufika wakati ule **pazia** lilizuiza watu wote, ila kuhani mkubwa, kuingia Pahali Patakatifu sana, ndipo kao la Mungu, na hata yeye alikuwa na ruhusa kuingia mara moja tu katika mwaka mmoja.

Ndani ya kitabu cha Waebrania tunajifunza kwamba pazia lilikuwa mfano wa mwili wa Yesu. Kupasuliwa kwake kulikuwa mfano wa kutolewa kwa mwili wa Yesu kwa njia ya kufa kwake. Kwa njia ya mauti yake, sisi tuna "uhodari wa kuingia Pahali Patakatifu kwa damu ya Yesu, njia ile aliyoanza kwa ajili yetu, mpya, na hai, katika pazia, ndio mwili wake" (Ebr. 10:19,20). Sasa kila mwamini – masikini au tajiri – ana ruhusa kuingia mbele ya Mungu wakati wo wote kwa maombi na sifa. Lakini tusisahau kamwe kwamba baraka hii ilinunuliwa kwasi kwa bei kubwa sana, ndiyo damu ya Yesu.

Mauti ya Mwana wa Mungu yalizaa mapinduzi makubwa inchini. Kulikuwa na tetemeko la inchi **lililopasua mawe** makubwa na **kufungua makaburi** mengi.

**27:52, 53** Ona ya kwamba **nyuma** ya **ufufuko** wa Yesu wale waliokuwa ndani ya makaburi haya **walifufuliwa na kwenda Yerusalema** na **kuonekana kwa watu wengi.** Hatusomi ndani ya Biblia kwamba watu hawa waliofufuliwa walikufa tena au kama walikwenda mbinguni pamoja na Bwana Yesu.

**27:54** Mapinduzi ya inchi yaliaminisha **akida Mroma** na watu wake kwamba Yesu **alikuwa Mwana wa Mungu. Akida** aliamini nini? Alikiri kwamba Yesu ni Bwana na Mwokozi *wake*? Au alikubali tu ya kwamba Yesu ni mkubwa kupita mwanadamu? Hatuwezi kujua. Masemo yake yanaonyesha staajabu yake, na ufahamu, kwamba mapinduzi ya inchi yalifungana na mauti ya Yesu, si na mauti ya watu wale wawili waliosulibishwa pamoja naye.

**S. Wanawake waaminifu (27:55, 56)**

Matayo alitaja **wanawake** waaminifu waliotumikia Bwana, na **kumfuata** kwa safari ndefu **toka Galilaya** kufikia Yerusalema. **Maria Magdalene, Maria mama ya Yakobo na Yose,** na Salome, mke wa Zebedayo, walikuwa pale. Walipenda Bwana wao sana sana, bila woga, na walibaki pamoja na Kristo wakati wanafunzi wanaume walipokimbia!

**T. Maziko ndani ya kaburi la Yosefu (27:57-61)**

**27:57,58 Yosefu wa Arimatea, tajiri**, na mmoja wa watu wa Baraza hakushiriki nao wakati walipotoa Yesu kwa Pilato (Lk. 23:51). Kufika saa hii alikuwa **mfuata** wa Yesu kwa siri, lakini sasa **alifikia Pilato** na uhodari kuomba ruhusa kuzika Bwana wake. Bila shaka Pilato alishituka, na Wayuda wa Baraza walikasirika, wakati mmoja wao aliposimamia Yesu, msulibiwa, wazi mbele ya watu. Ni kama siku ile Yosefu alijizika mwenyewe kwa maneno ya kupata mali, heshima ya watu, na kwa maneno ya dini, wakati alipozika mwili wa Yesu. Tendo hili lilimtenga daima na viongozi walioua Bwana Yesu.

**27:59,60** Pilato alimpa ruhusa, na Yosefu alifunga **mwili** na mapendo ndani ya **nguo safi ya kitani** na kuweka **ndani ya kaburi lake** mwenyewe, **kaburi jipya lililochongwa toka mawe**. Kaburi lilifungwa na jiwe **kubwa** ambalo Yosefu alifingirisha kusimama ndani ya shimo refu mbele yake.

Mia za miaka mbele Isaya alitabiri, “Wakamfanyia kaburi pamoja na waovu; na pamoja na matajiri katika kufa kwake” (Isa. 53:9). Bila shaka adui zake walikusudi kutupa mwili wake ndani ya bonde la Hinomu uteketezwe kwa moto pamoja na yalala au kuliwa na imbwa za mwitu. Lakini Mungu alitimiza kusudi lake mwenyewe na alitumika na Yosefu kuzika mwili wake *pamoja na matajiri.*

**27:61** Halafu Yosefu alikwenda zake, lakini **Maria Magdalene** na mama ya Yakobo na Yose walibaki na kuketi **mbele ya kaburi** kulilinda.

### U. Kaburi linalindwa (27:62-66)

**27:62-64** Siku ya kwanza ya Pasaka iliyoitwa **siku ya Matengenezo,** ilikuwa siku Bwana Yesu aliposulibishwa. **Kesho yake wakubwa wa makuhani na Wafarisayo** hawakuwa na salama rohoni. Wakikumbuka maneno Yesu aliyosema mbele juu ya kufufuka, waliomba Pilato kuweka walinzi kuchunga kaburi kusudi **wanafunzi wake** wasiibe mwili wake na kuwaambia watu kwamba alikuwa amefufuka. Walifikiri **udanganyifu ule** ungalikuwa **mkubwa kupita ule wa kwanza**, maana yake habari za ufufuko wake zingekuwa mbaya kupita kusema yeye ni Masiya na Mwana wa Mungu.

**27:65,66** Pilato aliwajibu **“Muna askari walinzi; kwendeni mulilinde kwa kadiri munavyoweza.**” Labda walikuwa wamepewa walinzi, au Pilato alikubali neno waliloomba. Labda Pilato alicheka kidogo rohoni mwake wakati aliposema, **“mulilinde kwa kadiri munavyoweza?”** Wayuda walipima sana. Walitia mhuri juu ya jiwe na kuweka walinzi, lakini maneno haya hayakutosha, na Mungu alishinda makusudi maovu ya watu na kuhakikisha hata kupita mbele kwamba Mfalme alifufuka kweli.

## 15. KUSHINDA KWA MFALME (Sura 28)

### A. Kaburi tupu, na Bwana aliyefufuliwa (28:1-10)

**28:1-4** Siku ya kwanza ya juma, mbele ya mapambazuko, wanawake wawili waliotwa Maria **walifika kuona kaburi.** Wakati walipofika kulikuwa na tetemeko kubwa la inchi. **Malaika** … **alishuka toka mbinguni, akakuja kufingirisha jiwe** toka mlango na **kuketi juu yake. Walinzi Waroma** waliogopeshwa sana wakati walipoona kungaa kwa rangi nyeupe ya kiumbe huyu, wakazimia.

**28:5, 6** Malaika alijulisha **wanawake** kwamba hawakuhitaji kuogopa. Yule ambaye walimtafuta alikuwa **amefufuka,** kama alivyoahidi. **“Kujeni mwone pahali Bwana alipolala.”** Jiwe lilikuwa limeondoshwa, si kwa kuleta njia kwa Bwana kutoka, lakini kuonyeshea wanawake kwamba alikuwa amefufuka.

**28:7-10** Kisha malaika alisema na wanawake **kwenda mbio** kujulisha **wanafunzi wake** habari hizi za utukufu. Bwana alikuwa hai tena na atakutana nao katika **Galilaya**. Wakati walipokuwa wakikwenda kuwaambia wanafunzi, Bwana Yesu Mwenyewe alikutana nao na kuwasalimu na neno moja, ndilo **“Salamu.”** Walianguka kwa **miguu** yake na kumwabudu. Halafu aliwaagiza kujulisha wanafunzi kwamba watamwona kwa **Galilaya.**

### B. Askari wanapewa rushwa waseme uwongo (28:11-15)

**28:11** Nyuma kidogo **wengine wa** askari wenye haya walifikia **wakubwa wa makuhani** kuwajulisha habari za neno lililotokea na ya kwamba hawakutimiza kazi yao vizuri. Kaburi lilikuwa wazi!

**28:12,13** Bila shaka viongozi vya dini walishikwa na hofu kubwa. Wakubwa wa makuhani walikusanyika pamoja na wazee kufanya shauri kama

watafanya nini juu ya neno hili. Wakikata tamaa, walitoa rushwa kwa **askari** kupasha watu habari zisizowezekana, ya kwamba **wanafunzi waliiba** mwili wa Yesu wakati askari **walipolala.**

Elezo hili linafungua maulizo mengi mengine ndani ya nia zetu. Kwa nini askari walilala wakati ilipowapasa kuangalia? Namna gani wanafunzi waliweza kufingirisha jiwe na kuliweka kando la mlango bila kuamsha askari? Namna gani askari wote walishikwa na usingizi kwa saa moja? Kama walilala usingizi, namna gani walijua wanafunzi waliiba mwili wa Yesu? Habari hizi zisingalikuwa kweli, kwa sababu gani ilipasa kutoa rushwa kwa askari waweze kuzisambaza? Kama wanafunzi wangaliiba mwili, kwa nini walishinda kwanza na kazi ya kuondosha sanda na kukunja kitambaa cha kichwa? (Lk. 24:12; Yn. 20:6,7).

**28:14** Habari hizi ambazo askari walilipwa kutangaza ziliwaingiza ndani ya hatari, kwani hukumu ya sheria ya Waroma kwa askari aliyelala saa ilipompasa kuangalia ilikuwa mauti. Hivi ilipasa viongozi vya Wayuda kuahidi kusaidia askari hawa kama habari hizi **zikisikiwa na liwali Mroma.**

Watu wa Baraza walikuwa wakijifunza ya kwamba wakisema uwongo mmoja itawapasa kusimamisha uwongo huu na uwongo mwingine, na mwingine na mwingine …

**28:15 Wayuda** wengi **hata sasa** wanaamini hadizi hii, na watu wa Mataifa vilevile. Wilbur Smith anajumlisha mbili za hadizi hizi:

> 1. Wanawake hawakufikia kaburi la Yesu, lakini la mtu mwingine. Fikiri kwanza juu ya elezo hili: Ukitaka kufikia kaburi la mpenzi wako, utaanguka kweli na kufikia kaburi la mtu mwingine? Na vilevile hili lilikuwa shamba la Yosefu wa Arimatea, si pahali pa kuzika watu wo wote. Makaburi mengine hayakuwa pale.
>
> Na waza juu ya Simoni Petro na Yoane, wavuvi na wenye nguvu – wao vilevile wangalikwendea kaburi lingine na kulikuta wazi? Na kukuta malaika pale ambaye aliwaambia, "Yeye si hapa. Amefufuka. Kujeni mwone pahali Bwana alipolala." Unafikiri malaika alikwendea kaburi lingine vilevile, si lile la Yesu? Mawazo haya ya waelimu wengine, yanakosa akili!
>
> 2. Watu wengine wanafikiri kwamba Yesu hakufa kweli, lakini alizimia tu, na nyuma ya wakati aliamshwa tena na kutoka kaburi. Lakini jiwe kubwa lilikuwa limefingirishwa mbele ya lango la kaburi lililotiwa mihuri ya serikali ya Roma. Hakuna mtu ndani ya kaburi lile aliyeweza kuondosha jiwe lile na kutoka.

Maneno yaliyotokea kwa wakati ule yanahakikisha kwamba Bwana Yesu alifufuka. Alitokea hai kwa wanafunzi wake tena na tena:

1. Kwa Maria Magdalene (Mk. 16:9-11).
2. Kwa wanawake (Mt. 28:8-10).
3. Kwa Petro (Lk. 24:34).
4. Kwa wanafunzi wawili kwa njia kwenda Emau (Lk. 24:13-32).
5. Kwa wanafunzi, bila Tomasi (Yn. 20:19-25).
6. Kwa wanafunzi, pamoja na Tomasi (Yn. 20:26-31).
7. Kwa wanafunzi saba kando ya bahari ya Galilaya (Yn. 21).
8. Kwa waamini kupita 500 (1 Kor. 15:7).
9. Kwa Yakobo (1 Kor. 15:7).
10. Kwa wanafunzi juu ya mlima wa Mizeituni (Mdo. 1:3-12).

Moja la mawe makubwa la msingi wa imani la Wakristo lisiloweza kutikisika ni matukio ya historia yanayohakikisha ufufuko wake. Tunaweza kusimama imara juu ya msingi huu na kupigania imani yetu, kwani hata kama watu wengine wanasema kwa-

mba si kweli, hawawezi kuhakikisha neno hili.

**C. Amri kubwa (28:16-20)**

**28:16,17** Katika **Galilaya** Bwana Yesu, nyuma ya ufufuko wake, alitokea **wanafunzi** wake juu ya mlima mmoja. Tunasoma juu ya habari hizi katika Marko 16:15-18 na 1 Wakor. 15:6 vilevile. Lilikuwa kusanyiko la ajabu kabisa! Mateso yake yalikwisha kwa milele. Kwa sababu alikuwa hai, wao vilevile watakuwa hai. Alisimama mbele yao ndani ya mwili wake wa utukufu. Waliabudu Bwana hai, Bwana wa mapendo – hata hivi wengine walikuwa na shaka.

**28:18** Halafu Bwana alieleza kwamba **amepewa mamlaka yote mbinguni na duniani**. Ndiyo, alikuwa na amri yote tangu zamani. Lakini hapa alisema juu ya amri yake kama Kichwa cha muumbo mpya. Tangu mauti na ufufuko wake alikuwa na amri kuleta uzima wa milele kwa wote ambao Mungu alimpa (Yn. 17:2). Alikuwa na uwezo kama mzaliwa wa kwanza wa muumbo wote. Lakini sasa alikuwa amemaliza kazi ya ukombozi, na alikuwa na amri kama mzaliwa wa kwanza kutoka wafu – "ili apate kuwa wa kwanza katika yote" (Kol. 1:15,18).

**28:19,20** Kama Kichwa cha muumbo mpya alitoa Amri Kubwa, agizo kwa waamini wote kwa muda wa sasa wa ufalme – ndio muda katikati ya kukataliwa kwa Mfalme na kuja kwake kwa pili.

Amri hii ina maagizo matatu:

1. **"Kwendeni basi mukafanye mataifa yote wanafunzi."** Si kusema ya kwamba watu wote wa dunia wataokolewa. Kwa njia ya kuhubiri Habari Njema wanafunzi waone watu wengine wakigeuka wafuata wa Mwokozi – toka kila taifa, kabila, na lugha.
2. Waliagizwa **"kuwabatiza kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu."** Ni kazi ya wajumbe wa Kristo kufundisha waamini wa sasa maana ya ubatizo, na ya kwamba hili ndilo agizo ambalo inawapasa kutii. Kwa njia ya kubatizwa, mwamini wa sasa anakiri mbele ya watu kwamba sasa Mungu ni Baba yake, Yesu Kristo ni Bwana na Mwokozi wake na Roho Mtakatifu anakaa ndani yake na kumpa uwezo na kumfundisha. **Jina** ndani ya shairi 19 ni moja lakini linasema juu ya **Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu** pamoja. Linaonyesha umoja wa Mungu.
3. Na **"mukiwafundisha kushika maneno yote ambayo niliwaamuru ninyi."** Amri hii si kuhubiri Habari Njema tu; haitoshi kuongoza watu kuamini na kuokolewa tu, na halafu kuwaacha peke yao kujaribu kuishi kwa Bwana. Ni lazima kuwafundisha *kutii* maagizo ya Kristo ndani ya Agano Jipya. Sharti mwanafunzi ageuke kufanana na Bwana wake, lakini neno hili linawezekana tu kwa njia ya kujifunza, na kunyenyekea Neno la Mungu.

Halafu Bwana aliongeza ahadi tamu ya kwamba atakuwa pamoja na wanafunzi wake siku zote, hata **kutimia kwa nyakati**. Hawatakwenda kuhubiri peke yao bila Msaidizi. Ndani ya utumishi na masafari yao yote Mwana wa Mungu atakuwa pamoja nao.

Tunasoma neno hili "yote" juu ya maneno mane ya Amri Kubwa: **amri yote; mataifa yote; maneno yote; siku zote**.

Hivi kitabu hiki cha Habari Njema kinakwisha na amri na faraja toka Bwana wetu wa utukufu. Karibu miaka elfu mbili imepita tangu aliposema maneno haya, nayo ni amri yake kwa sisi watu wa sasa vilevile. Lakini hata sasa hatujamaliza kazi kubwa ambayo alituagiza!

Tunafanya nini kutimiza amri yake ya mwisho?

## NOTES

[1] (10:21) J. C. Macaulay, *Obedient Unto Death*: Devotional Studies in John's Gospel, II:59.

[2] (10:41) Arthur T. Pierson, *"The Work of Christ for the Believer,"* The Ministry of Keswick, First Series, p. 114.

[3] (13:22) G. H. Lang, *The Parabolic Teaching of Scripture,* p. 68.

[4] (13:24–26) Merrill F. Unger, Unger's Bible Dictionary, p. 1145.

[5] (13:49,50) Gaebelein, *Matthew,* p. 302.

[6] (16:2,3) Of course, these weather indications are valid for Israel, not North America or Great Britain!

[7] (16:7–10) The twelve kophinoi of the 5,000 may have held less than the seven spurides of the 4,000.

[8] (16:17,18) G. Campbell Morgan, *The Gospel According to Matthew,* p. 211.

[9] (21:6) J. P. Lange, *A Commentary on the Holy Scriptures,* 25 Vols., pagination unknown.

[10] (24:34) F. W. Grant, *"Matthew," Numerical Bible, The Gospels,* p. 230.

[11] (26:64) R. C. H. Lenski, *The Interpretation of St. Matthew's Gospel,* p. 1064.

## BIBLIOGRAPHIE

Gaebelein, A. C. *The Gospel of Matthew.* New York: Loizeaux Bros., 1910.

Kelly, William. *Lectures on Matthew.* New York: Loizeaux Bros., 1911.

Lenski, R. C. H. *The Interpretation of Saint Matthew's Gospel.* Minneapolis: Augsburg Publishing House, 1933.

Macaulay, J. C. *Behold Your King.* Chicago: The Moody Bible Institute, 1982.

Morgan, G. Campbell. *The Gospel According to Matthew.* New York: Fleming H. Revell Company, 1929.

Pettingill, W. L. *Simple Studies in Matthew.* Harrisburg: Fred Kelker, 1910.

Tasker, R. V. G. *The Gospel According to St. Matthew, TBC*. Grand Rapids: Wm. B. Eerdmans Publishing Company, 1961.

Thomas, W. H. Griffith. *Outline Studies in Matthew.* Grand Rapids: Wm. B. Eerdmans Publishing Company, 1961.

Weston, H. G. *Matthew, the Genesis of the New Testament.* Philadelphia: American Baptist Publication Society, n.d.

# HABARI NJEMA KAMA ALIVYOANDIKA
# MARKO

## Utangulizi

*"Habari Njema ya Marko inaamsha ndani ya msomaji Mkristo hamu kutumikia na kuiga Bwana wake."* – August Van Ryn

### I. Nafasi ya pekee katika Kanuni

Habari Njema ya Marko ni fupi kupita vitabu vingine vya Habari Njema na karibu 90% (sehemu 90 ya mia moja) ya maneno aliyoandika ni ndani ya Matayo, au Luka, au ndani ya vitabu hivi viwili vyote. Ikiwa hivi, kwa sababu gani tunahitaji kitabu hiki?

Kitabu hiki cha Habari Njema kinasaidia sana waamini wa sasa kwa sababu ni fupi sana na kiliandikwa bila kutumika na masemo ya ndani ndani. Mara nyingi ni kitabu cha kwanza cha Biblia ambacho wahubiri wa Habari Njema wanatafsiri kwa lugha ya watu ambao hawakuisikia mbele.

Ndiyo, namna kitabu hiki kilivyoandikwa ilikuwa faida zaidi kwa Waroma, na hata kwa watu wa sasa vilevile wanaofanana nao, – lakini *maneno yaliyoandikwa ndani* yake ni bora sana vilevile.

Hata kama Marko aliandika zaidi maneno yaliyoandikwa ndani ya Matayo na Luka, aliandika habari chache nyingine vilevile tusiyosoma ndani ya vitabu vingine vya Habari Njema. Kwa mfano aliandika namna Yesu alivyotazama wanafunzi, namna alivyokasirika, na namna alivyowatangulia kwa njia kwenda Yerusalema. Bila shaka alipata habari hizi karibu na Petro, kwani alifungana sana na Petro kwa mwisho wa maisha yake. Watu wa zamani walifikiri (na tunawaza walifikiri vizuri) ya kwamba Habari Njema ya Marko ni zaidi maneno Petro aliyokumbuka, na kwa sababu hii mwandishi aliona na macho yake mwenyewe zaidi ya maneno haya aliyoandika.

Watu wengi wanafikiri ya kwamba Marko ndiye kijana aliyekimbia wichi (14:51), na ni kama kwa njia hii alitia kitabu hiki mkono wake, bila kuandika jina lake wazi. (Wakati vitabu vya Habari Njema vilipoandikwa kwanza havikuwa na anwani.) Basi Marko alikaa kwa Yerusalema, na hakuna sababu kuandika habari hizi ndogo kama kijana huyu asipofungana na Habari Njema hii. Hivi tunafikiri mawazo ya watu kwamba alikuwa Marko ni kweli.

### II. Mwandishi

Zaidi ya walimu wanakubali mawazo ya watu wote walioishi kwa mwanzo wa kanisa, ya kwamba Habari Njema ya pili iliandikwa na Yoane Marko. Alikuwa mwana wa Maria wa Yerusalema. Maria huyu alikuwa na nyumba mjini, na Wakristo wa kwanza walikutana pale.

*Watu wa inchi nyingine* walishuhudia

neno hili vilevile kwa wakati wa mwanzo. Papias (aliyeishi karibu na miaka 110 A.D.) alitaja Yoane Mzee (tunafikiri alikuwa Mtume Yoane, lakini labda alikuwa mwanafunzi mwingine kwa wakati wa mwanzo) kusema ya kwamba Marko, mwenzi wa Petro, aliandika. Neno hili lilikubaliwa na Justin Martyr, Irenaeus, Tertullian, Clement wa Alexandria, Origen, na *Matangulizi ya Anti–Marcionite*.

Kuna maneno mengine machache *ndani ya kitabu* yanayohakikisha ya kwamba kiliandikwa na Marko. Hata ni maneno nusu tu, yanapatana na maneno Wakristo wa wakati wa mwanzo waliyoamini.

Inaonekana wazi ya kwamba mwandishi alijuana sana na inchi ya Palestina, zaidi na Yerusalema. (Anatupasha maneno kupita yale tunayosoma ndani ya vitabu vingine vya Habari Njema juu ya chumba cha juu – hatuwezi kushangaa juu ya neno hili kama ni pahali alipokaa kwa ujana wake!) Tunaona masemo ya Aramaic (ndiyo lugha ya Palestina), na wasomaji walifahamu desturi za Wayuda. Maneno yake yaliandikwa na mwandishi hai na yanatufikirisha ya kwamba alikuwa mwenzi wa mtu aliyeona maneno haya na macho yake mwenyewe. Umbo la kitabu linafuatana na hotuba ya Petro katika Matendo 10.

Kwa sababu watu walifikiri Marko alikuwa kwa Roma wakati alipoandika Habari Njema yake alitumika na maneno mengi ya kiroma, kupita yale ndani ya vitabu vingine vya habari njema, maneno kama *akida, dinari, legioni,* na *praitorio.*

Katika Agano Jipya mwandishi wa kitabu hiki cha Habari Njema anaitwa na jina lake la Mataifa (Kiroma), ndilo Marko, mara kumi; na mara tatu na jina lake la Wayuda na Mataifa pamoja, ndilo Yoane Marko. Marko alikuwa "mtumishi," kwanza wa Paulo, nyuma yake wa mjomba wake Barnaba, na mwishoni wa Petro mbele ya kufa kwake. Kwa sababu hii ni kama alikuwa ametayarishwa kuandika Habari Njema ya Mtumishi Mkamilifu.

## III. Tarehe

Walimu wenye kuamini Biblia wanashindwa kutaja tarehe fulani kama tarehe wakati Habari Njema ya Marko ilipoandikwa. Wanapatana juu ya neno moja tu, ndilo hili: Iliandikwa mbele ya kuharibiwa kwa Yerusalema.

Lakini mawazo ya walimu hawapatani juu ya wakati gani Marko aliandika mahubiri ya Petro juu ya maisha ya Bwana wetu, *mbele* ya kufa kwa Petro, mbele ya 64-68 A.D, au *nyuma ya kufa kwake.*

Kama Marko ni kweli Habari Njema ya kwanza iliyoandikwa (zaidi ya walimu wanafikiri hivi sasa) lazima iliandikwa karibu na mwanzo hata Luka aliweza kutumika na maandiko ya Marko. Walimu wengine wanafikiri iliandikwa karibu na mwaka 51 A.D., lakini ni kama ilikuwa zaidi kwa miaka 57-60 A.D.

## IV. Msingi na Jambo Kubwa

Ndani ya Habari Njema hii tunapata habari za ajabu za Mtumishi Mkamilifu wa Mungu, Bwana wetu wa ajabu Yesu Kristo. Ni habari za mmoja aliyeacha kuonekana na utukufu ambao alikuwa nao mbinguni, na alitwaa namna ya Mtumwa hapa duniani (Flp. 2:7). Ni habari za ajabu, zisizo na kifani, za Mmoja "asiyekuja kutumikiwa ila kutumika na kutoa uzima wake uwe ukombozi wa wengi" (Marko 10:45).

Habari Njema hii inangaa na utukufu wakati tunapokumbuka ya kwamba Mtumishi huyu mkamilifu ni Mwana wa Mungu mwenyewe, na ya kwamba alikuwa tayari kufunga kiuno chake na kitambaa cha mtumwa na kugeuka Mtu-

mishi wa watu. Hapa tunaona Mwana wa Mungu aliyeshika mwili wa mtu na kuishi kama Mtu hapa duniani. Alitegemea na kutii Baba wake na kufanya mapenzi yake ndani ya maneno yote. Kazi zake zote za uwezo zilifanywa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.

Mwandishi, ndiye Yoane Marko, alikuwa mtumishi wa Bwana aliyeanza vizuri. Alishindwa kwa wakati (Matendo 15:38), kisha alirudishwa tena kuwa mtumishi wa faida (2 Timoteo 4:11).

Habari zinafuatana mbio mbio ndani ya maandiko ya Marko. Anaweka roho juu ya matendo ya Bwana kupita juu ya masemo yake, na aliandika juu ya maajabu kumi na tisa lakini juu ya mifano mine tu.

Wakati tunaposoma Habari Njema hii, tutatafuta majibu kwa maulizo matatu: (1) Inasema nini? (2) Maana yake nini? (3) Kuna mafundisho gani kwa mimi ndani ya habari hizi? Habari Njema hii ni kitabu cha faida nyingi kwa wote wanaotaka kuwa *watumishi waaminifu wa kweli wa Bwana Yesu.*

## HABARI YALIYOMO

| | |
|---|---|
| 1. KUTAYARISHWA KWA MTUMISHI | (1:1-13) |
| 2. MWANZO WA KAZI YA MTUMISHI KATIKA GALILAYA | (1:14–3:12) |
| 3. MWITO WA MTUMISHI NA MAFUNDISHO YAKE KWA WANAFUNZI WAKE | (3:13–8:38) |
| 4. SAFARI YA MTUMISHI KWENDA YERUSALEMA | (Sura 9, 10) |
| 5. KAZI YA MTUMISHI KATIKA YERUSALEMA | (Sura 11, 12) |
| 6. HOTUBA YA MTUMISHI KWA MLIMA WA MIZEITUNI | (Sura 13) |
| 7. MAUMIVU NA MAUTI YA MTUMISHI | (Sura 14, 15) |
| 8. KUSHINDA KWA MTUMISHI | (Sura 16) |

# Maelezo

## 1. KUTAYARISHWA KWA MTUMISHI (1:1-13)

### A. Mtangulizi wa Mtumishi anatayarisha njia (1:1-8)

**1:1** Jambo kubwa la Marko ni habari njema juu ya **Yesu Kristo, Mwana wa Mungu.** Kusudi la Marko ni kuonyesha Bwana Yesu kama mtumishi, na kwa sababu hii hakuanza na kutaja wazazi wa Mwokozi Yesu, lakini na habari za utumishi wake. Habari hizi zilitangazwa na Yoane Mbatizaji, mjumbe wa habari njema.

**1:2,3** Malaki na Isaya walitabiri ya kwamba **mjumbe** atatangulia Masiya kuita watu kukaa tayari kwa kufika kwake, kwa maneno ya matendo na roho zao (Mal. 3:1; Isa. 40:3). Yoane Mbatizaji alitimiza unabii huu. Alikuwa **"mjumbe, ... sauti ... akilia jangwani."**

**1:4** Alitangaza kwa watu ya kwamba sharti watubu (kugeuza mafikiri yao na kuachana na zambi zao) kusudi wapate **usamehe wa zambi.** Bila kufanya hivi hawataweza kupokea Bwana. Watu watakatifu tu wanaweza kutambua uzuri wa Mwana Mtakatifu wa Mungu.

**1:5** Wakati wasikiaji wa Yoane Mbatizaji walipotubu kweli, aliwabatiza kuonyesha wazi mbele ya watu ya kwamba waligeuka kabisa. Ubatizo uliwatenga kabisa na makundi ya taifa la Israeli waliokuwa wameacha Bwana. Uliwawezesha kufungana na baki la watu waliokuwa tayari kupokea Kristo. Ni kama shairi 5 linaonyesha kwamba watu wote walipokea mahubiri ya Yoane. Sivyo. Kwa mwanzo watu wengi sana walikwenda mbio kwa jangwa kusikia mhubiri huyu wa uwezo, lakini zaidi yao hawakukiri na kuacha zambi zao na roho ya kweli. Neno hili lilionekana wazi nyuma ya wakati.

**1:6** **Yoane** alikuwa mtu wa namna gani? Kwa wakati wa sasa tungesema alikuwa mtu aliyeshikilia sana na maneno ya dini, mtu mtawa aliyejaribu kuwa mwema na kuepuka sana na maovu, kwa kujinyima anasa za mwili. Alikaa zaidi jangwani. Kama Elia, alivaa mavazi hafifu, ya kukwaruza. Vyakula vyake vilitosha kwa mahitaji ya mwili wake kukaa na nguvu, lakini havikuwa vya kupendeza. Aliweka roho zaidi juu ya kazi ya utukufu ya kutangaza habari za Kristo, na hakuweka roho juu ya maneno mengine. Labda angaliweza kuwa tajiri, lakini alichagua umasikini. Hivi alikuwa mtangulizi wa kufaa wa Yule asiyekuwa na pahali pa kulalisha kichwa chake. Maneno haya yanatufundisha ya kwamba inapasa watumishi wote wa Bwana kuishi maisha yasiyo na anasa.

**1:7** Alihubiri juu ya ukuu na ubora wa Bwana Yesu. Alisema Yesu alikuwa na uwezo na wema na utumishi mkubwa sana. Yoane alifikiri ya kwamba hakustahili kuinama na **kufungua kamba ya viatu** vya Mwokozi – ndiyo kazi ya mtumwa. Mahubiri ya mwenye kujaa Roho Mtakatifu yanatukuza Bwana Yesu, na yananyenyekeza mhubiri mwenyewe.

**1:8** Yoane alibatiza na **maji.** Ubatizo huu ulikuwa alama ulioonekana kwa macho, lakini haukugeuza maisha ya mtu. Yesu **atawabatiza** na **Roho Mtakatifu**; ubatizo huu utawajaza na uwezo mkubwa wa roho (Matendo 1:8). Na vilevile utaingiza waamini wote ndani ya kanisa, ndio mwili wa Kristo (1 Kor. 12:13).

### B. Mtangulizi anabatiza Mtumishi (1:9-11)

**1:9** Tumefika kwa mwisho wa muda wa miaka 30, ndani yake hakuna habari za maisha ya Mtumishi. Bwana Yesu alikuwa tayari sasa kuanza kazi yake katikati ya watu. Alianza na safari ya kilomètres karibu 96 **toka Nazareti** kufikia mto **Yorodani** karibu na Yeriko. **Yoane alimbatiza** pale. Ndiyo, Bwana Yesu hakuwa na toba, kwa sababu hakuwa na zambi ambayo ilimpasa kukiri. Kwa Bwana Yesu ubatizo huu ulikuwa mfano wa ubatizo wake hata kufa kwa Kalvari kwa wakati wa kuja, na ufufuko wake toka mauti. Hivi mara moja kwa mwanzo wa utumishi wake katikati ya watu kuna mfano ulioonyesha mbele msalaba na kaburi tupu.

**1:10, 11** Mara moja wakati alipotoka maji **aliona mbingu zinapasuka na Roho Mtakatifu akishuka juu yake kama hua. Sauti** ya Mungu Baba ilisikiwa ikikiri Yesu ni **Mwana wake mpendwa.**

Hakuna saa ndani ya maisha ya Bwana wetu wakati asipojazwa **Roho** Mtakatifu. Lakini sasa Roho Mtakatifu alikuja **juu yake**, akimpakaa mafuta na kumpa uwezo kumtayarisha kwa miaka mitatu ya kazi itakayofuata. Uwezo wa Roho Mtakatifu ni neno la lazima kwa mtumishi wa Mungu. Inawezekana kwa mtu kujifunza sana na kuwa mwenye akili nyingi, lakini bila uwezo wa Roho Mtakatifu utumishi wake unakosa uwezo na hauna faida. Lazima nijiulize, "Roho Mtakatifu amenipa mimi uwezo kwa kazi ya Bwana?"

### C. Mtumishi anajaribiwa na Shetani (1:12,13)

Mtumishi wa Yehova alijaribiwa na Shetani **jangwani** kwa **siku makumi ine. Roho** ya Mungu alimwongoza kukutana na Shetani – si kuona kama atafanya zambi, lakini kuhakikisha ya kwamba hakuweza kufanya zambi. Kama Yesu angaliweza kufanya zambi wakati alipokuwa Mtu hapa duniani, namna gani tunaweza kujua hakika ya kwamba hataweza kufanya zambi sasa kama Mtu mbinguni?

Kwa nini Marko anasema Yesu alikuwa **pamoja na nyama**? Nyama hawa waliwezeshwa na Shetani kujaribu kuharibu Bwana? Au walikuwa wapole mbele ya Mwumba wao? Tunaweza kuuliza tu – hatujui jibu lenyewe.

**Malaika walimtumikia** kwa mwisho wa siku zile makumi ine (ona Mt. 4:11); kwa wakati alipojaribiwa hakula chakula (Lk. 4:2).

Haiwezekani kwa mwamini kuepuka majaribu. Yatakuwa makubwa zaidi kwa kipimo cha ukaribu wake na Bwana katika mwenendo wake. Shetani haweki roho juu ya kukwalisha Wakristo wa jina tu wasio na imani ya kweli, lakini anajaribu sana kuangusha wale wanaopiga vita kwa maneno ya roho na kushinda. Si zambi kwa Mkristo kujaribiwa, lakini ni zambi kuacha majaribu haya kum*shinda.* Hatuwezi kushinda majaribu kwa nguvu yetu wenyewe, lakini Roho Mtakatifu anayekaa ndani ya mwamini anamwezesha kushinda tabia yake ya zambi.

## 2. MWANZO WA KAZI YA MTUMISHI KATIKA GALILAYA (1:14–3:12)

### A. Mtumishi anaanza kazi yake (1:14,15)

Marko hakuandika juu ya utumishi wa Bwana katika Yudea (ona Yoane 1:1–4:54) lakini alianza mara moja kuandika juu ya utumishi wake mkubwa katika Galilaya, ulioendelea kwa muda wa mwaka mmoja na miezi tisa (1:14–9:50). Nyuma yake aliandika kidogo juu ya sehemu ya nyuma ya utumishi wake kwa Perea (10:1-45) mbele ya kuendelea na habari za juma lake la mwisho katika Yerusalema.

| AJABU | WOKOVU TOKA |
|---|---|
| 1. Kuponyeshwa kwa mtu mwenye upepo mchafu (1:23-26). | 1. Uchafu wa zambi. |
| 2. Kuponyeshwa kwa mama ya mke wa Simoni (1:29-31). | 2. Wasiwasi na utukutu wa zambi. |
| 3. Kuponyeshwa kwa mkoma (1:40-45). | 3. Machukio makubwa ya zambi. |
| 4. Kuponyeshwa kwa mwenye kupooza (2:1-12). | 4. Ukosefu wa msaada kwa sababu ya zambi. |
| 5. Kuponyeshwa kwa mtu mwenye mkono wa kupooza (3:1-5). | 5. Ukosefu wa faida kwa sababu ya zambi. |
| 6. Wokovu wa mwenye pepo mchafu (5:1-20). | 6. Taabu, ukali, na maogofya ya zambi. |
| 7. Mwanamke mwenye kutoka damu (5:25-34) | 7. Uwezo wa zambi kupunguza nguvu ya uzima. |
| 8. Kufufuliwa kwa binti ya Yairo toka mauti (5:21-24; 35-43). | 8. Mauti ya roho kwa sababu ya zambi. |
| 9. Kuponyeshwa kwa binti ya mwanamke wa Sirofoinike (7:24-30). | 9. Utumwa wa zambi na Shetani. |
| 10. Kuponyeshwa kwa kiziwi asiyeweza kusema vizuri (7:31-37). | 10. Ukosefu kusikia Neno la Mungu na kusema juu ya maneno ya roho. |
| 11. Kuponyeshwa kwa kipofu (8:22-26). | 11. Upofu kwa nuru ya Habari Njema. |
| 12. Kuponyeshwa kwa kijana mwenye pepo bubu (9:14-29). | 12. Ukali wa utawala wa Shetani. |
| 13. Kuponyeshwa kwa Baratimayo, ndiye kipofu (10:46-52). | 13. Hali ya upofu na umasikini kwa sababu ya zambi. |

**Yesu alipita hata Galilaya** akihubiri Habari Njema ya **ufalme wa Mungu**. Alitangaza ya kwamba:

1. **Wakati umetimia.** Ndani ya oroza ya wakati tarehe ilichaguliwa kwa kuonekana kwa Mfalme katikati ya watu. Siku ile ilikuwa imefika sasa.
2. **Ufalme wa Mungu ni karibu;** Mfalme alikuwa pale na kuwapa taifa la Israeli njia kupokea ufalme ule. **Ufalme** ulikuwa **karibu** kwa sababu Mfalme alikuwa ametokea katikati ya watu.
3. Watu waliitwa **kutubu na kuamini Habari Njema.** Kwa kustahili kuingia ufalme iliwapasa kuachana na zambi zao kabisa, na kuamini habari njema juu ya Bwana Yesu.

**B. Wavuvi wane wanaitwa (1:16-20)**

**1:16-18 Wakati Yesu alipotembea kwa pwani ya Bahari ya Galilaya** aliona **Simoni na Anderea** waliokuwa wakivua samaki. Alikutana nao mbele na walikuwa wamegeuka wanafunzi wake kwa mwanzo wa utumishi wake (Yoane 1:40,41). Sasa aliwaita kuwa pamoja naye, na aliahidi kuwafanyiza **wavuvi wa watu**. Waliachana mara moja na kazi yao ya kujipatia mali, wakafuata Yesu. Walitii bila kukawa, na roho moja, tayari kuachana na mambo yaliyokuwa faida kwao.

Kuvua samaki ni kazi ya fundi; ni vivyo hivyo na kazi ya kuleta watu kwa Bwana.

1. Inahitaji *saburi*. Mara nyingi inapasa kungoja kwa saa ndefu.
2. Inahitaji *akili* kutumika vizuri na vyambo na nyavu.
3. Kunahitaji kuwa na *ufahamu,* na kujua kwenda pahali samaki walipo.
4. Inahitaji *kudumu.* Mvuvi mzuri halegei mbio.
5. Inahitaji *kimya.* Ni vizuri kujificha mwenyewe na kuepuka msukosuko.

Tunageuka **wavuvi wa watu** kwa

njia ya kufuata Kristo. Kwa kipimo tunavyofanana naye tutaweza kupata watu wengine kwaye. Kazi yetu ni **kumfuata**; halafu yeye ataangalia kazi ya kuvuta watu kwake.

**1:19,20** Nyuma kidogo, Bwana Yesu alikutana na **Yakobo** na **Yoane**, wana wa **Zebedayo,** waliokuwa **wakitengeneza mikila yao**. Wakati **alipowaita** waliagana na **baba yao**, wakakwenda **kufuata** Bwana.

Hata sasa Kristo anaita watu kuacha vyote na kumfuata yeye (Luka 14:33). Haifai waruhusu mali au wazazi kuwazuiza wasitii mwito wake.

### C. Pepo mchafu anafukuzwa (1:21-28)

Mashairi 21-34 yanaonyesha namna Bwana alivyoishi siku kwa siku. Maajabu mengi yalifanyikana wakati Mganga Mkubwa alipoponyesha wenye pepo wachafu na wagonjwa.

Maajabu ya kuponyesha ya Mwokozi yanaonyesha namna anavyofungua watu toka matunda ya zambi. Ona ramani kwa ukurasa 150.

Hata kama mhubiri wa Habari Njema kwa wakati wa sasa haitwi kufanya maajabu kuponyesha miili ya watu inampasa saa zote kusaidia magonjwa yao ya roho. Labda haya ni maajabu makubwa kupita Bwana Yesu aliyosema juu yao kwa Yoane 14:12: "Yeye ambaye ananiamini mimi, kazi ninazofanya, yeye atazifanya vilevile; na atafanya *kazi* kubwa kuliko hizi."

**1:21,22** Lakini sasa turudi kwa habari za Marko. Kwa **Kapernaumu,** Yesu alikuwa **ameingia sunagogi** na alianza kufundisha **siku ya sabato.** Watu walitambua ya kwamba hakuwa namna ya walimu wengine. Masemo yake yalikuwa na uwezo, si kama masemo ya **waandishi** waliokaa kusemasema tu kama mashine. Maneno aliyosema yalikuwa mishale toka Mwenyezi Mungu. Mafundisho yake yalilazimisha watu kusikiliza, kujihukumu wenyewe na kutengeneza maneno yao. Waandishi walifundisha tu maneno ya dini watu waliyosikia mbele. Mafundisho ya Bwana Yesu yalikuwa ya hakika. Aliweza kusema maneno haya kwa sababu mwenendo wake ulifuatana na mafundisho yake.

Sharti kila mwalimu wa Neno la Mungu aseme na amri au anyamaze. Mwandishi wa Zaburi alisema, "Ninaamini, kwa maana nitasema" (Zab. 116:10). Paulo alitaja shairi hili ndani ya 2 Kor. 4:13. Walisema maneno haya kwa sababu waliyasadiki kabisa.

**1:23** **Ndani ya sunagog**i lao siku ile kulikuwa na mtu mmoja aliyekaaliwa na pepo mbaya. Anaitwa hapa **pepo mchafu.** Kwa mawazo yetu maana yake ni ya kwamba roho huyu alichafua mtu mwenyewe mwilini au rohoni. Haifai tufikiri kwamba kukaaliwa na pepo mchafu na kuwa wazimu ni neno moja. Ni maneno mbalimbali kabisa. Mwenye pepo mchafu anakaaliwa na roho mchafu. Mara nyingi watu hawa wanaweza kufanya matendo ya uwezo watu wengine wasiyoweza kutenda, na mara nyingi wanageuka wenye jeuri na watukanaji saa wanaposikia habari za Bwana Yesu Kristo na kazi aliyofanya.

**1:24** Ona ya kwamba roho mchafu alitambua **Yesu,** na alisema yeye ni mtu wa Nazareti na **Mtakatifu wa Mungu**. Ona vilevile ya kwamba mara nyingine alisema kama mtu mmoja, na mara nyingine kama watu wengi: **"Tuna nini nawe? … Umekuja hapa kutuangamiza sisi? … Ninatambua wewe ni nani …"** Kwanza pepo mchafu alisema kama mwenye kufungana na mtu yule; kisha alisema kwa yeye mwenyewe.

**1:25,26** **Yesu** alikataa kupokea ushuhuda wa pepo mchafu, hata kama alisema kweli. Aliagiza pepo mchafu **kunyamaza,** kisha alimwagiza **kutoka**

ndani ya mtu huyu. Bila shaka lilikuwa neno la kushangaza kuona mtu yule **akitetemeshwa na kifafa,** na kusikia kilio cha kutia hofu cha pepo mchafu wakati alipotoka ndani ya mtu huyu ambaye alimtesa.

**1:27,28** Ajabu hili lilishangaza watu sana. Hawakuona mbele mtu akitokesha pepo mchafu kwa njia ya kusema neno tu. Walifazaika kama labda neno hili lilikuwa mwanzo wa dini na mafundisho mapya? Habari za ajabu hili **zikatangazwa sasa hivi pahali po pote katika … Galilaya.** Mbele ya kuacha mashairi haya, tuwaze juu ya maneno matatu:

1. Ni kama kufika kwa Kristo duniani mara ya kwanza kuliamsha pepo wachafu kufanya kazi nyingi duniani.
2. Uwezo wa Kristo ulioshinda roho wabaya hawa ni mfano kuonyesha ya kwamba Kristo atashinda kabisa Shetani na wajumbe wake wote kwa wakati wa mwisho.
3. Pahali gani Mungu anapotumika, Shetani anashindana naye. Wote wanaoanza kutumikia Bwana wajue tu ya kwamba atashindana nao ndani ya kila neno wanalojaribu kufanya. "Kwa maana kushindana kwetu si juu ya damu na nyama, lakini juu ya falme na mamlaka, juu ya watawala wa ulimwengu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika pahali pa mbingu" (Efe. 6:12).

### D. Mama ya mke wa Petro anaponyeshwa (1:29-31)

"Mara moja" ni usemi unaoonekana tena na tena ndani ya Habari Njema ya Marko, na unafaa kabisa kwa Habari Njema hii inayoonyesha Bwana Yesu kama mtumishi.

**1:29, 30** Toka **sunagogi** Bwana wetu alikwendea nyumba ya Simoni. Wakati alipofika, **mara moja** alisikia ya kwamba mama ya mke wa **Simoni alilala na homa**. Ndani ya shairi 30 tunaona watu wa nyumba **wakimpasha habari hizi mara moja.** Hawakukawa mbele ya kujulisha Mganga mahitaji yake.

**1:31** Bila kusema neno Bwana Yesu **akamshika mkono** na kumsaidia kusimama. Mwanamke aliponyeshwa **mara moja**. Ni desturi kwa homa kuacha mgonjwa na uzaifu wa mwili. Mara hii Bwana hakuponyesha homa yake tu, lakini alimpa nguvu mwilini mara moja aweze kutumikia. **"Akawatumikia."** J.R. Miller anasema:

> Ingepasa kila mgonjwa anayeponyeshwa kwa njia ya ajabu, au bila ajabu, kutoa mara moja kwa utumishi wa Mungu uzima aliorudishiwa tena. . . . Watu wengi wana hamu kufanya kazi kubwa kwa Kristo. Wanawaza juu ya kazi fulani nzuri sana, lakini wanaacha kupita bure maneno yale yale ambayo Kristo anataka wafanye kwaye. Utumishi wa kweli kwa Kristo ni kwanza kufanya vizuri kazi yetu ya kila siku.[1]

Ona ya kuwa kila mara Mwokozi aliyoponyesha mtu alifanya hivi kwa njia mbalimbali. Neno hili linatukumbusha ya kwamba watu wanaookolewa toka zambi zao wanafika kwa Mwokozi kwa njia mbalimbali. Inatupasa kufundisha na kuongoza kila mtu peke yake kwa namna ya mahitaji yake wenyewe.

Ndiyo, Petro alikuwa na mama ya mke. Neno hili linaonyesha ya kwamba makuhani wa wakati ule walioa wake. Mafundisho ya kwamba haifai kwa kuhani kuwa na mke ni mawazo ya watu tu. Hayafundishwi ndani ya Neno la Mungu, na yanazaa mabaya mengi.

### E. Kuponyesha watu kwa wakati wa mangaribi (1:32-34)

Habari za kufika kwa Mwokozi zilikuwa zimeenea saa ya mchana. Lakini ilikuwa siku ya sabato na watu waliogopa kufikisha wenye hitaji kwake. Halafu wakati wa mangaribi, **saa jua**

**lilipokwisha kushuka** na sabato ilipokwisha, watu wengi sana walifikia mlango wa nyumba ya Petro. Ni pale **wagonjwa na wenye pepo** walipoponyeshwa kwa uwezo ule unaofungua watu toka kila namna ya zambi.

**F. Mahubiri katika Galilaya (1:35-39)**

**1:35** Yesu **aliamka asubui mapema sana, mbele ya mchana,** na **alikwenda pahali** alipoweza kukaa peke yake bila kizuizo, na kushinda na maombi. Mtumishi wa Yehova alifungua sikio lake kila asubui kupokea maagizo kwa siku ile toka Mungu Baba (Isa. 50:4,5). Kama Bwana Yesu alisikia hitaji katika roho yake kwa saa hii kushinda kimya mbele ya Baba asubui mapema, ingetupasa sisi kufanya vivyo hivyo! Ona vilevile ya kwamba **aliomba** kwa saa ilipokuwa nguvu kwaye kufanya hivi. Aliamka **saa nyingi mbele ya mchana**. Haifai maombi kuwa kitu tunachofanya wakati sisi tunapotaka kufanya hivi, lakini saa fulani tunapojitoa kufanya hivi hata kama ni saa iliyo nguvu kwa sisi kuomba. Labda ni kwa sababu tusipofanya hivi utumishi wetu unakosa uwezo mara nyingi.

**1:36,37** Saa Simoni na wengine walipoamka asubui watu wengi walikuwa wamekutana tena inje ya nyumba. Wanafunzi walikwenda kumwambia Bwana ya kwamba hesabu ya watu ambao walimfuata ilikaa kuongezeka.

**1:38** Lakini Bwana hakurudia mji, lakini alipeleka wanafunzi kwa vijiji vya karibu, akieleza ya kwamba ilikuwa lazima kwa yeye **kuhubiri pale vilevile**. Kwa nini hakurudia Kapernaumu?

1. Alikuwa ameshinda sasa tu kwa maombi na kusikia nini ambayo Mungu alitaka afanye siku ile.
2. Alifahamu ya kwamba furaha ya watu katika Kapernaumu ilikuwa ya juu juu tu. Mwokozi hakuvuta kamwe mafungo makubwa ya watu karibu naye. Aliona ndani ya mioyo ya watu na kujua mawazo yao ya kweli.
3. Alijua hatari ya hali ya kupendwa na watu na alifundisha wanafunzi wake kwa njia ya matendo yake mwenyewe kukaa na ange wakati watu walipowasifu.
4. Aliepuka kila mara kupokea sifa ya watu ambayo ingaliweza kumtukuza *mbele* ya kufa kwake.
5. Aliweka roho zaidi juu ya kuhubiri Neno la Mungu. Ndiyo maajabu ya kuponyesha yalipunguza taabu ya watu, lakini kusudi lao lilikuwa vilevile kupata masikio ya watu kusikia mafundisho yake.

**1:39** Hivi Yesu alipita pahali pote katika Galilaya akifikia masunagogi na kuhubiri na kutoa pepo wachafu. Mahubiri na matendo yake yalipatana. Alisema pamoja na kufanya. Ona ya kwamba mara nyingi alitoa pepo wachafu ndani ya masunagogi. Labda makanisa mengine kwa wakati wa sasa yanafuatana na masunagogi?

**G. Mkoma anasafishwa (1:40-45)**

Habari hizi za **mkoma** ni mfano mzuri kutufundisha namna ya maombi ambayo Mungu anajibu:

1. Aliomba kwa moyo – **akisihi Bwana**, kama mwenye kukata tamaa.
2. Alikuwa na adabu – **akipiga magoti mbele ya Bwana.**
3. Alikuwa na unyenyekevu na roho ya kutii– **"kama ukitaka."**
4. Alikuwa na imani – **"unaweza."**
5. Alionyesha hitaji lake – **"kunisafisha."**
6. Aliomba kwa neno fulani moja – hakuomba Bwana "unibariki", lakini **"unisafishe."**
7. Aliomba kusaidia kwa hitaji *lake* mwenyewe – **"kunisafisha."**
8. Ombi lake lilikuwa fupi – maneno mane tu.

Ona neno lililotokea sasa!

**Yesu alimhurumia.** Tusisome maneno haya kamwe bila furaha kubwa na roho ya asante.

**Akanyosha mkono wake.** Ni neno la kushangaza. Mkono wa Mungu ukinyoshwa kujibu ombi la mtu mnyenyekevu na mwenye imani.

**Alimgusa.** Kwa wakati wa sheria mtu alichafuwa mbele ya Mungu wakati alipogusa mkoma. Na vilevile aliweza kupata ukoma yeye mwenyewe. Lakini Mwana Mtakatifu wa Mungu alijifanya mmoja nao na kushiriki na taabu ya watu na alitawanya maangamizi ya zambi bila kuchafuwa nazo yeye mwenyewe.

Hivi alisema, **"Ninataka."** Hamu yake kutuponyesha inapita hamu yetu kuponyeshwa. Kisha alisema, **"Safishwa."** Mara moja ngozi ya mkoma ilikuwa laini na safi.

Alikataza mtu huyu kutangaza habari za kuponyeshwa kwake mbele ya kufikia **kuhani** na kutoa zabihu iliyoagizwa na sheria (Lawi 14:2ff). Kwa njia ya agizo hili Bwana alipima kwanza utii wa mtu huyu ambaye alimponyesha. Alifanya neno aliloagizwa? Sivyo; alitangaza habari za kuponyeshwa kwake, na kwa njia hii alizuiza kazi ya Bwana (sh.45). Kwa njia ya agizo hili Bwana alipima vilevile utambuzi wa kuhani. Atafahamu ya kwamba Masiya ambaye walingojea kwa muda mrefu alikuwa amefika, na kutenda maajabu haya kuponyesha watu? Kama akifanana na taifa la Israeli, hatafahamu neno hili.

**Halafu tunaona Bwana akiondokea tena** makundi ya watu na kwenda kuhubiri **katika jangwa.** Hakupima usitawi wa kazi kwa njia ya hesabu ya watu ambao walimfikia.

### H. Mwenye kupooza anaponyeshwa (2:1-12)

**2:1-4** Muda mfupi nyuma ya **kuingia** kwa Bwana **katika Kapernaumu … watu wengi walifika na kuzunguka** nyumba pahali alipokuwa. Habari za kufika kwake zilikuwa zimeenea mbio katikati ya watu nao walitaka kuona Mtendaji maajabu huyu akifanya maajabu. Kila mara Mungu anapotumika na uwezo watu wanavutwa kutazama. Mwokozi **alihubiri Neno la Mungu na uaminifu kwa watu** hawa waliokusanyika kwa mlango. Kwa upande wa nyuma wa makutano kulikuwa mtu **mwenye ugonjwa wa kupooza mmoja aliyebebwa na watu wane** juu ya kitanda. Watu wengi waliokuwa pale walimzuiza asifike karibu na Yesu. Kuna vizuizo karibu kila mara tunapojaribu kuleta watu wengine kwa Yesu. Lakini wabebaji wale wane walipata njia. Walipanda madaraja yaliyokuwa inje ya nyumba, **wakatoboa** nusu ya **dari,** wakashusha **mwenye kupooza** chini – labda kulikuwa na kiwanja katikati ya nyumba kilichozungukwa na vyumba – wakamfikisha karibu na Mwana wa Mungu. Mtu mmoja aliwapa rafiki hawa wane majina. Aliita mmoja wao *Huruma*, mwingine *Shirika*, mwingine *Akili ya kutunga*, na wa ine *Kudumu*. Ingetupasa sisi sote kujaribu kuwa rafiki namna hii.

**2:5 Yesu** akiona **imani yao … alisema na mtu mwenye kupooza, "Mwana, zambi zako zinasamehewa."** Kwa sababu gani alisema hivi? Mtu huyu alikuwa pale kwa sababu ya ugonjwa wake wa kupooza, si kwa sababu ya zambi zake, sivyo? Ndiyo, lakini Yesu hakufikiri maneno ya kuonekana kwa macho tu, lakini hali ya roho vilevile. Hataponyesha mwili tu bila kukumbuka hitaji la nafsi. Hatasaidia neno lililo kwa wakati tu bila kusaidia hali ya kudumu milele ya roho. Hivi alisema, **"Zambi zako zinasamehewa."** Lilikuwa tangazo la ajabu kabisa. Sasa hivi – hapa duniani – **zambi** za mtu huyu **zilisamehewa.** Hakuhitaji

kungojea Siku ya Hukumu. Aliweza kujua kabisa saa ile ile ya kwamba amesamehewa. Ni vivyo hivyo na kila mtu anayeamini Bwana Yesu.

**2:6,7 Waandishi** walitambua mbio maana ya neno Bwana alilosema. Walijua mafundisho ya Biblia ya kutosha hata walifahamu ya kwamba **Mungu tu anaweza kusamehe zambi.** Mtu ye yote aliyesema anaweza kusamehe zambi alikuwa akijitaja kuwa Mungu. Ni kweli, lakini kwa pahali pa kukiri ya kwamba Bwana Yesu ni Mungu, walimshitaki mioyoni mwao juu ya **kukufuru**.

**2:8, 9** Yesu alijua mawazo yao, ndilo neno lililohakikisha ya kwamba alikuwa na uwezo usiokuwa wa dunia. "**Nini inapita nyepesi?** Au kusema kwa mwenye kupooza: Zambi zako zimesamehewa, au ya kwamba ameponyeshwa?" Ni nyepesi ku*sema* maneno haya mawili yote. Lakini haiwezekani kwa mtu wa dunia ku*fanya* maneno haya yote mawili.

**2:10-12** Bwana alikuwa amesema ya kwamba zambi za mtu huyu zilikuwa zimesamehewa. Ndiyo, lakini zilisamehewa kweli kweli? Waandishi hawakuweza ku*ona* zambi za mtu huyu, hivi walikataa kuamini. Kwa kuonyesha ya kwamba zambi za mtu huyu zilisamehewa kweli, Mwokozi alifanya neno waandishi waliloweza kuona. Alisema na mtu mwenye kupooza kusimama, kubeba kitanda chake cha matete, na **kutembea**. Mtu mwenyewe alitii mara moja. Watu **walishangaa**. **Hawajaona mbele kamwe neno namna hii.** Lakini waandishi hawakuamini hata ushuhuda mkubwa sana namna hii. Inatupasa sisi wenyewe kuchagua kuamini, lakini watu hawa walichagua kukataa kuamini.

### I. Mwito wa Lawi (2:13-17)

**2:13,14** Wakati Bwana Yesu alipokuwa akifundisha **kando ya bahari** aliona **Lawi** akilipiza watu kodi. Tunajua Lawi ni jina lingine kwa Matayo, Myuda, aliyeandika Habari Njema ya kwanza kwa wakati wa nyuma. Kazi yake haikuwa namna ya kazi Wayuda waliyofanyaga kwani alilipiza watu kodi kwa serikali ya Waroma waliyozarau! Watu wa namna hii hawakuheshimiwa kwani mara nyingi hawakutenda kwa haki – ndiyo, walizarauliwa pamoja na makahaba, na watu wabaya sana. Hata hivi tunaheshimu Lawi kwa sababu wakati aliposikia mwito wa Kristo, aliacha maneno yake mwenyewe mara moja, **akamfuata**. Ingetupasa sisi sote kufanana naye na kutii Bwana mara moja bila kuwa na mashaka. Labda kwa wakati wenyewe tunafikiri kufanya hivi ni kama zabihu kubwa, lakini nyuma, kwa wakati wa milele, hatutafikiri juu yake hivi hata kidogo. Mhubiri wa Habari Njema aliyeuawa kwa sababu ya imani yake, jina lake Jim Elliot, alisema, "Mtu si mpumbavu anayetoa vitu ambavyo hawezi kubaki navyo, badala ya kupata kitu ambacho hakiwezi kumpotelea kamwe."

**2:15** Karamu ilitayarishwa **nyumbani mwa Lawi** ili rafiki zake waweze kukutana na Bwana Yesu. Zaidi ya rafiki zake walikuwa watu kama yeye – **wenye kulipiza kodi na wenye zambi**. Aliita Yesu kufika kwa karamu na Yesu alikubali kuwa pale pamoja nao.

**2:16 Waandishi na Wafarisayo** walifikiri walikuwa wamepata Yesu akitenda neno lisilofaa. Hawakufikia Bwana mwenyewe kumwuliza juu ya neno hili, lakini walifikia **wanafunzi** wake na kujaribu kupunguza heshima yao kwa Bwana wao. **Kwa sababu gani** Bwana wao alikula na kunywa pamoja na **watoza kodi na wenye zambi?**

**2:17 Yesu alisikia ulizo lao,** akawakumbusha ya kwamba wenye afya hawahitaji mganga, lakini wagonjwa tu. Waandishi walifikiri walikuwa wenye **afya njema,** hivi hawakufahamu ya

kwamba walihitaji Mganga Mkubwa. Watu wa kulipiza kodi na wenye zambi walikubali zambi zao na ya kwamba walihitaji kusaidiwa. Yesu alifika kuita wenye zambi namna yao – si wale waliofikiri wao ni watu wenye haki.

Kuna mafundisho hapa kwa sisi sote. Haifai tufungane na kushirikiana na Wakristo tu, lakini kuonyesha urafiki kwa wasioamini na wazalimu vilevile ili kutafuta njia kuwapasha habari za Bwana na Mwokozi wetu. Lakini sharti tukae na ange vilevile tusifanye neno lo lote linaloweza kupunguza ushuhuda wetu mwema mbele ya watu, au kuacha wasioamini kutuingiza ndani ya njia zao za zambi. Sharti sisi tuwaongoze kwa njia njema itakayosaidia mahitaji yao ya roho. Ndiyo, tungependa zaidi kukaa mbali na dunia hii mbovu, lakini Yesu hakufanya hivi, na haifai wafuata wake kufanya hivi.

Waandishi walifikiri wataharibu sifa njema ya Bwana Yesu kwa njia ya kumwita rafiki ya wenye zambi. Walikusudi kumzarau, lakini kabisa kabisa walimsifu. Wakombolewa wote wanakiri na furaha ya kwamba yeye ni rafiki ya wenye zambi, na watampenda kwa milele kwa sababu ya neno hili.

### J. Mabishano juu ya kufunga chakula (2:18-22)

**2:18** Ilikuwa desturi ya **wanafunzi wa Yoane Mbatizaji na wa Wafarisayo kufunga chakula** kama sehemu ya kuabudu kwao. Ndani ya Agano la Kale kufunga kulikuwa alama ya huzuni kubwa. Lakini zaidi ya *maana* yake kwa wakati ule ilikuwa imepotea, na watu walifunga kwa kawaida ya dini tu. Waliona kwamba **wanafunzi** wa Yesu **hawakufunga**, na labda walikuwa na wivu kidogo mioyoni mwao wakati walipouliza Bwana kueleza neno hili.

**2:19, 20** Ndani ya jibu lake alisawanisha wanafunzi na wenzi wa **bwana arusi**. Yeye mwenyewe alikuwa Bwana Arusi. Wakati yeye alipokuwa pamoja nao kwanza, hawakuonyesha huzuni. Lakini **siku zitakuja** wakati bwana arusi **atakapoondoshwa kwao; katika siku zile** watakuwa na sababu **kufunga chakula**.

**2:21** Aliongeza mara moja mifano miwili kuonyesha ya kwamba wakati huu wa sasa haukupatana na ule wa mbele. Ndani ya mfano wa kwanza kulikuwa na kipande cha **nguo** kisichopunguzwa kwanza kwa njia ya kukivua. Kama kikitumiwa kutengeneza **nguo ya zamani** iliyopasuka, bila shaka kitapunguka na nguo ya zamani iliyo zaifu kupita itapasuka tena kwa pahali nguo mpya inaposhonwa. Yesu alikuwa akisawanisha muda wa zamani na nguo ya zamani. Halikuwa kusudi kamwe kwa Ukristo kutengeneza dini ya kiyahudi. Ulikuwa jambo jipya. Huzuni ya muda wa mbele watu waliyoonyesha kwa njia ya kufunga sharti ikombolewe na furaha ya muda mpya.

**2:22** Mfano wa pili ulikuwa juu ya **mvinyo mpya** ndani ya **viriba vya ngozi ya zamani.** Vile viriba vya zamani havikuweza kunyoloshwa tena. **Mvinyo mpya** ikiwekwa ndani yao, kuchachuka kwake kutapasua vile viriba vya zamani. **Mvinyo mpya** ni mfano wa furaha na uwezo wa imani ya Ukristo. **Viriba vya zamani** ni mfano wa desturi na utaratibu wa dini ya kiyahudi. Mvinyo mpya inahitaji viriba vipya. Haikufaa kufunga wafuata wa Yoane na Wafarisayo na utumwa wa kufunga chakula na huzuni, kama ilivyokuwa desturi zamani. Sharti furaha na mchemko wa uzima mpya zipate njia kuonekana. Tangu mwanzo Ukristo ulitaabishwa na wale waliotaka kuchanganya na mafundisho ya sheria. Bwana Yesu alifundisha ya kwamba maneno haya mawili hayapatani. Sheria na neema zinashindana.

**K. Mabishano juu ya Sabato (2:23-28)**

**2:23, 24** Maneno haya ni mfano wa shindano la maneno Yesu aliyofundisha sasa tu juu ya mafundisho ya dini ya kiyahudi na uhuru wa Habari Njema.

Wakati **alipopita katika mashamba ya ngano siku ya sabato wanafunzi wake** walichuma masuke ya **ngano** wapate kula. Lakini kwa mafundisho ya wazee tendo hili halikufaa kwa siku ya sabato kwani lilikuwa kama "kuvuna" na labda hata kama "kupura" (kwa njia ya kufikicha ngano ndani ya mikono yao kuondosha miganda)!

**2:25, 26** Bwana aliwajibu na neno lililotokea katika Agano la Kale. **Daudi,** hata kama alipakaliwa kuwa mfalme, alikuwa amekataliwa. Kwa pahali pa kutawala, watu walimwinda kama kwale. Siku moja wakati vyakula vyake vilipokwisha, **alikwendea nyumba ya Mungu na alitwaa ya mikate ya onyesho** kujikulisha, pamoja na watu wake. Makuhani tu walikuwa na ruhusa kula mkate wa onyesho, lakini Mungu hakuhamakia Daudi juu ya tendo hili. Kwa nini? Kwa sababu maneno mengi katika Israeli hayakuwa taratibu. Wakati Daudi asipopewa njia kutawala namna ilivyompasa kufanya, Mungu alimruhusu kufanya maneno yasiyokubaliwa na sheria.

Ilikuwa vivyo hivyo na Bwana Yesu. Alikuwa amepakaliwa mafuta, lakini hakutawala kwanza. Hitaji la wanafunzi kuchuma masuke ya ngano wakati walipokuwa kwa safari lilionyesha ya kwamba maneno katika Israeli hayakuwa taratibu. Ingalipasa Wafarisayo kuwapokea nyumbani mwao kama wageni wao, si kuwashitaki.

Kama Daudi aliyeasi sheria kwa njia ya kula mikate ya onyesho na hakuhamakiwa na Mungu, zaidi sana wanafunzi, walioasi maagizo ya wazee tu, hawakuwa na hatia.

Shairi 26 linasema ya kwamba Daudi **alikula mikate ya onyesho** wakati **Abiatari alipokuwa kuhani mkubwa.** Ndani ya 1 Samweli 21:1 tunasoma Ahimeleki alikuwa kuhani kwa wakati ule. Abiatari alikuwa baba yake. Labda heshima ya kuhani mkubwa kwa Daudi ilimsukuma kukubali tendo hili lisilopatana na sheria.

**2:27, 28** Bwana wetu alimaliza hotuba yake kwa njia ya kukumbusha Wafarisayo ya kwamba **sabato** ilisimamishwa na Mungu kusaidia watu, si kama utumwa. Aliongeza kusema ya kwamba **Mwana wa watu ndiye Bwana wa sabato vilevile** – ni yeye ambaye aliisimamisha. Hivi alikuwa na amri kuchagua nini ilikubaliwa siku ile, na nini ilikatazwa. Kusudi la sabato halikuwa kamwe kukataza watu kufanya kazi za lazima au za rehema kusaidia watu wengine. Wakristo hawalazimishwi kushika sabato. Agizo la kushika siku ya sabato lilikuwa kwa taifa la Israeli. Siku ya Bwana, ndiyo siku ya kwanza ya juma, inawekwa kwa Ukristo kuwa mbali na siku nyingine za juma. Lakini siku ile haifungwi na maagizo na makatazo mengi. Ni siku wakati waamini hawafungwi na kazi ya mishahara, lakini wanaweza kuabudu Bwana, kumtumikia na kulisha roho zao na Neno la Mungu. Hatuulizi kama neno fulani linakatazwa siku ya Bwana, lakini, "Namna gani ninaweza kutumika na siku hii kwa utukufu wa Mungu, kwa baraka ya jirani yangu, na kwa kusaidia roho yangu mwenyewe?"

**L. Mtumishi anaponyesha siku ya sabato (3:1-6)**

**3:1, 2** Neno lingine lilitokea siku ya sabato. Wakati Yesu **alipokuwa akiingia sunagogi,** alikutana na **mtu mwenye mkono wa kupooza. Ataponyesha mtu huyu siku ya sabato?** Kama akifanya hivi, Wafarisayo watakuwa na njia kumshitaki. Kweli? Walifikiri hivi. Waza juu ya unafiki na hila yao. Hawakuweza kusaidia mtu yule, na

walichukizwa na mtu ye yote aliyeweza kufanya hivi. Walitafuta njia kuhukumu Bwana wa uzima. Kama akiponyesha mtu **siku ya sabato,** watamrukia kama kundi la imbwa za mwitu wanavyorukia na kuua nyama mkali.

**3:3,4** Bwana alisema na **mwenye mkono wa kupooza kusimama mbele.** Watu wote waliangalia karibu karibu kuona kama atafanya nini. Halafu **alisema** na Wafarisayo, **"Inafaa kufanya mema siku ya sabato au kufanya mabaya, kuponyesha au kuua?"** Ulizo lake lilifunua uovu wa Wafarisayo. Walifikiri ilikuwa vibaya kwa Yesu kufanya ajabu na kuponyesha siku ya sabato, lakini haikuwa zambi kwa Wafarisayo kufanya shauri siku ya sabato kumwua!

**3:5** Hatushangai kuona ya kwamba hawakujibu! Nyuma ya kungoja kwa muda mfupi, Mwokozi aliagiza mgonjwa **kunyolosha mkono wake**. Wakati alipofanya hivi, mkono wake ulipata nguvu tena, na kuwa na kipimo chake cha mbele, na vikunjo vyake vilipotea.

**3:6** Ilishinda **Wafarisayo** kubaki pale na kuona maneno mengine! **Walitoka** sunagogi, walitafuta **Waherode,** adui zao tangu zamani, na **kufanya shauri kuua** Yesu. Ilikuwa kwanza siku ya sabato. Herode alikuwa mwenye kuagiza mauti ya Yoane Mbatizaji. Labda wafuasi wake wataweza kuua Yesu. Wafarisayo walitumaini iwe hivi.

### M. Makutano makubwa wanasonga Mtumishi (3:7-12)

**3:7-10** Yesu alitoka sunagogi, **akakwendea bahari ya Galilaya.** Ndani ya Biblia bahari ni mfano wa Mataifa mara nyingi. Hivi labda tendo hili lilionyesha ya kwamba aliacha Wayuda na aligeuka kwa Mataifa. **Makutano makubwa** walikusanyika, si **toka Galilaya** tu, lakini toka inchi nyingine za mbali vilevile. Watu walikuwa wengi sana, hata Yesu aliomba kupewa **chombo kidogo** kusudi aweze kwenda mbali kidogo na pwani ili watu waliofika kuponyeshwa wasimsonge na kumwumiza.

**3:11,12** Wakati **pepo wachafu** katika makutano walipolalamika ya kwamba yeye ni **Mwana wa Mungu, aliwakataza sana** wasiseme hivi. Tuliona mbele ya kwamba hakukubali ushuhuda wa pepo wachafu. Hakubisha ya kwamba alikuwa Mwana wa Mungu, lakini yeye mwenyewe alichagua kwa wakati gani na namna gani neno hili litafunuliwa kwa watu. Yesu alikuwa na uwezo kuponyesha watu, lakini maajabu haya yalifanywa tu kwa watu wale waliofika kwake kusaidiwa naye. Ni vivyo hivyo na wokovu. Uwezo wake unatosha kuokoa watu wote, lakini wale tu ambao wanamwamini wanaokolewa.

Utumishi wa Bwana unafundisha ya kwamba mahitaji ya watu tunayoona pande zote *si* mwito wa Mungu kwa sisi kila mara. Mahitaji yalikuwa pahali pote. Yesu alitii maongozi ya Mungu Baba ambayo yalimwonyesha pahali gani na wakati gani ilipompasa kumtumikia. Sharti sisi tufanye vivyo hivyo.

## 3. MWITO WA MTUMISHI, NA MAFUNDISHO YAKE KWA MITUME YAKE (3:13 – 8:38)

### A. Mitume kumi na wawili walichaguliwa (3:13-19)

**3:13-18** Kwa kueneza Habari Njema pahali pote duniani Yesu alichagua mitume **kumi na wawili.** Watu wale hawakuwa watu wa uwezo au akili kupita watu wengine; waligeuka watu wa kujulikana tu kwa sababu walifuata Yesu.

Walikuwa vijana. James E. Stewart aliandika maneno haya mazuri sana juu ya ujana wa mitume:

> Ukristo ulianzwa na vijana … Tunafikiri zaidi ya mitume hawakufikia miaka makumi tatu kwanza wakati walipokwenda kufuata Yesu. Haifai tusahau kamwe ya kwamba Yesu

> mwenyewe alianza utumishi wake na "umande wa ujana" juu yake (Zaburi 110:3 – alitaja shairi hili juu yake mwenyewe kwanza, na nyuma lilitajwa na Wakristo wa kwanza. Walikumbuka Bwana Yesu hivi wakati walipoandika picha juu ya viambaza mapangoni pahali walipofichama na adui zao (Catacombs). Picha hizi hazionyeshi Bwana kama mzee, mwenye maumivu na kuchoka, lakini kama mchungaji kondoo kijana vilimani kwa wakati wa asubui … Yesu tu alifahamu kabisa roho za vijana, furaha na tumaini na ukarimu wao, vita zilizopigwa ndani ya roho zao na majaribu … Wakati tunapojifunza habari za mitume hawa kumi na wawili tunawaona wakifuata mwongozi wao kwa njia wasiyojua mbele, bila kufahamu kabisa kama alikuwa nani, na kwa sababu gani walimfuata na pahali gani alipowaongoza kwenda. Tunafikiri walizarauliwa na rafiki zao, na mara nyingine walikuwa na shaka ndani ya roho zao wenyewe na hamu kujitenga na maneno haya yote, lakini hata hivi walifungana naye na kumfuata. Vizuri tuingiliwe na hamu yao kufuata Yesu vivyo hivyo." [2]

Yesu aliita wanafunzi hawa kwa makusudi matatu: (1) **wawe pamoja naye**; (2) **aweze kuwatuma kuhubiri**; na (3) **wawe na uwezo kuponyesha wagonjwa na kutoa pepo wachafu.**

Kwanza walihitaji saa kujifunza, kutayarishwa peke yao mbele ya kusimama mbele ya watu wengine na kuhubiri. Huu ndio msingi wa utumishi. Lazima tukae **pamoja na Bwana** mbele ya kwenda kama wajumbe wa Mungu.

Kisha walitumwa **kuhubiri**. Mahubiri ya Neno la Mungu ndiyo msingi wa matangazo ya Habari Njema kwa watu. Ni neno kubwa kupita yote mengine.

Mwishoni walipewa **uwezo** usio wa dunia hii. Kuweza kutoa pepo wachafu kutahakikisha kwa watu ya kwamba Mungu alikuwa akisema kwa njia ya mitume. Kuandika kwa Biblia nzima hakumalizwa bado saa ile. Maajabu yalihakikisha ya kwamba wale ambao waliyatenda walikuwa kweli wajumbe wa Mungu. Kwa wakati wa sasa watu wana Neno zima la Mungu na ni sharti kwao kuliamini *bila* maajabu kulihakikisha.

**3:19** Mmoja wa mitume anajulikana kupita wengine, ndiye **Yuda Iskariota**. Ni siri tusiyoweza kufahamu, namna gani mmoja aliyechaguliwa kuwa mtume aliweza kugeuka na kutoa Bwana wetu kwa adui zake. Moja la maneno yanayoumiza roho ya mtumishi wa Mungu zaidi ni kuona mwamini aliyeanza vizuri na kujitoa sana kufuata Bwana, akirudi nyuma na kugeuzia Mwokozi mgongo na kushikamana tena na maneno ya dunia ambayo ilimsulibisha.

Mitume kumi na mmoja walifuata Bwana na uaminifu, na kwa njia yao alipindua dunia. Watu wengine walizaliwa tena kwa njia ya mahubiri yao, na halafu waamini wale wapya walihubiri vilevile, na wengine walizaliwa na kuendelea kuhubiri Habari Njema, na tunaweza kusema ya kwamba hata sisi sote ni tunda la utumishi wao. Haiwezekani kujua kama watu wengapi na wa pahali gani wanageuka Wakristo kwa sababu ya mwenendo na mahubiri yetu ya Habari Njema.

### B. Zambi isiyoweza kusamehewa (3:20-30)

**3:20, 21** Yesu alirudi toka mlima pahali alipokuwa ameita wanafunzi wake, akakwendea nyumba moja katika Galilaya. **Makutano makubwa** ya watu walikusanyika hata yeye na mitume hawakupata saa kula chakula. **Watu wa jamaa yake** walifikiri **alikuwa mwenye wazimu**, wakajaribu kumwondosha pale. Bila shaka walipata haya kwa sababu ya mtu huyu mwenye bidii kubwa kwa Mungu ndani ya jamaa yao.

J.R. Miller aliandika:

> Waliweza kueleza bidii yake kubwa kwa njia ya kusema alikuwa mwenye wazimu tu. Watu wanasema maneno namna hii kwa wakati wa sasa vilevile, saa mfuata wa Kristo anaposahau faida yake mwenyewe ndani ya bidii yake kufuata Bwana wake. Watu wanasema, "Yeye ni mwenye wazimu!" Wanafikiri kila mtu anayewaka kwa Bwana, na kujitoa kupita Wakristo wengine kumtumikia, ni mwenye wazimu.
>
> Hii ni namna nzuri ya wazimu. Ni huzuni kwa sababu tunaiona mara moja moja tu. Kama waamini wengi zaidi wangalikuwa na wazimu namna hii kama hesabu ya watu wanaokufa bila wokovu ingalipunguka; kama wahubiri wa Habari Njema inchini nyingine wasingalikosa mali kuendelesha kazi yao, kama waamini wasingalinyamaza kimya kwa muda mrefu saa wanapokutana kwa maombi; kama walimu wa watoto katika école du dimanche wasingalikuwa wachache tu. Ingekuwa vizuri kama Wakristo wote wangekuwa wenye wazimu namna hii kama Bwana wao, au kama Paulo. Ni wazimu mbaya zaidi kukaa bila huruma kwa wapotevu na bila kujaribu kuwasaidia. Ndiyo, ni nyepesi kukaa na roho baridi bila kusumbuka juu ya hali ya roho ya wapotevu, lakini tuko wachungaji wa ndugu zetu (Mwanzo 4:9), na ni zambi mbaya zaidi kukaa bila kusumbuka juu ya wokovu wao wa milele.[3]

Ndiyo, kila mara watu wanafikiri mwenye kuwaka kwa Mungu ni mwenye wazimu. Kwa kipimo tunachofanana na Kristo, sisi vilevile tutahuzunishwa kwa sababu watu wa jamaa yetu na rafiki zetu hawatufahamu. Tukiweka roho juu ya kujivimbishia mali nyingi, watu watatusifu. Tukiwa na bidii sana kwa maneno ya kufuata Kristo, watatuzarau.

**3:22 Waandishi** hawakufikiri Yesu alikuwa na wazimu. Walimshitaki juu ya kutoa pepo wachafu kwa uwezo wa **Belzebuli, mkubwa wa pepo wachafu**. Maana ya jina hili "**Belzebuli**" ni "bwana wa mainzi ya mavi" au "bwana wa uchafu". Yalikuwa matukano machafu kabisa!

**3:23** Yesu alionyesha kwanza uwongo wa mashitaki yao, lakini nyuma alitangaza hukumu juu ya watu wale ambao waliyafanya. Kama akitoa pepo wachafu kwa njia ya Belzebuli, halafu Shetani angalishindana na yeye mwenyewe, na kuzuiza makusudi yake mwenyewe. Kusudi la Shetani lilikuwa kutawala watu kwa njia ya pepo wachafu, si kuwafungua toka uwezo wa pepo wachafu.

**3:24-26 Ufalme, au nyumba, au mtu anayetengwa juu yake mwenyewe** hatashinda. Kukaa kuishi kunawezekana kwa njia ya kufungana pamoja, si kwa njia ya kushindana.

**3:27** Hivi mashitaki ya waandishi hayakuwa ya akili. Ndiyo, maneno ambayo Bwana Yesu alikuwa akifanya yalishindana na maneno waandishi waliyosema. Maajabu yake yalionyesha ku*shindwa* kwa Shetani, si *uwezo* wake. Hii ndiyo maana ya neno Mwokozi aliyosema, **"Mtu hawezi kuingia ndani ya nyumba ya mwenye nguvu, na kunyanganya mali yake pasipo kufunga kwanza yule mwenye nguvu, na nyuma kunyanganya vitu vya nyumba yake."**

Shetani ndiye **mwenye nguvu, nyumba** ndiyo ufalme wake; yeye ndiye mungu wa muda huu wa sasa. **Mali yake** ndiyo watu ambao anatawala. Yesu ndiye anayefunga Shetani na kunyanganya vilivyo **nyumbani** mwake. Wakati Kristo atakapokuja tena Shetani atafungwa na kutupwa ndani ya shimo pasipo mwisho kwa miaka elfu moja (Ufu. 20:3). Kazi ya Bwana kutoa pepo wachafu hapa duniani ilikuwa kama

utabiri wa wakati atakapofunga Shetani kabisa.

**3:28-30** Ndani ya mashairi 28-30 Bwana alitangaza hukumu juu ya waandishi waliokwisha kutenda zambi isiyoweza kusamehewa. Walishitaki Yesu juu ya kutoa pepo wachafu kwa uwezo wa pepo wachafu, lakini Yesu aliwatoa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, hivi ni kama waliita Roho Mtakatifu pepo mchafu. Ni matukano **juu ya Roho Mtakatifu**. Zambi za namna **zote** zinaweza **kusamehewa**, lakini hakuna usamehe kwa zambi hii. Ni zambi ya **milele.**

Watu wanaweza kufanya zambi hii kwa wakati wa sasa? Labda hawawezi. Ni zambi watu waliyofanya kwa wakati Yesu alipokuwa duniani akifanya maajabu. Yeye si duniani leo katika mwili akitoa pepo wachafu, hivi haiwezekani kutukana Roho Mtakatifu sasa. Watu wanaofikiri wametenda zambi isiyoweza kusamehewa hawakuifanya. Kwa njia ya kusumbuka juu ya neno hili wanaonyesha ya kwamba hawakutukana Roho Mtakatifu.

### C. Mama na ndugu za kweli za Mtumishi (3:31-35)

Maria, **mama** ya Yesu alikuja pamoja na **ndugu zake** kusemezana naye. Makutano yaliwazuiza wasifike karibu naye, hivi walituma habari karibu naye kusema walimngojea **inje.** Wakati mjumbe alipomwambia Yesu ya kwamba **mama na ndugu zake** walitaka kumwona, **alitazama** watu ambao walimzunguka pande zote, akasema **mama yake na ndugu zake ndio watu wo wote wanaofanya mapenzi ya Mungu.**

Habari hizi zinatufundisha maneno haya:

1. Masemo ya Bwana Yesu yalikemea watu wanaoabudu Maria. Bwana aliheshimu mama yake ya dunia, lakini alisema ya kwamba maneno ya roho yanashinda yale ya mwili. Kufanya mapenzi ya Mungu ilikuwa heshima kubwa kwa Maria, kupita kuwa mama ya Yesu.
2. Watu wengine kwa wakati wa sasa wanafundisha ya kwamba Maria alikuwa bikira la daima, lakini masemo ya Yesu yanaonyesha ya kwamba alikuwa na ndugu. Ndiyo, Yesu alikuwa mzaliwa wa kwanza wa Maria, lakini alizaa wana na binti wengine nyuma yake (Ona Mt. 13:55; Mk. 6:3; Yn. 2:12; 7:3, 5,10; Mdo 1:14; 1 Kor. 9:5; Gal. 1:19. Ona vilevile Zab. 69:8.)
3. Yesu aliweka maneno ya Mungu mbele ya undugu wa dunia. Anasema na wafuata wake hata sasa "Kama mtu akikuja kwangu, asipochukia baba yake, na mama, na mke, na watoto, na ndugu zake waume na wake, hata uzima wake pia, hawezi kuwa mwanafunzi wangu" (Lk. 14:26).
4. Mashairi haya yanaonyesha ya kwamba waamini wana ushirika wa karibu na Wakristo wenzao kupita ushirika na ndugu zao wasioamini.
5. Mwishoni yanaonyesha ya kwamba Yesu anafikiri kufanya mapenzi ya Mungu ni neno kubwa zaidi. Neno hili linatimizwa ndani ya maisha yako? Mimi ni mama au ndugu yake?

### D. Mfano wa mpandaji mbegu (4:1-20)

**4:1,2** Halafu Yesu **alianza tena kufundisha kando ya bahari**. Kwa sababu ya makutano ilimpasa kuingia **chombo** tena kwa kuhubiri karibu na pwani. **Aliwafundisha** tena maneno ya Mungu akiyaeleza kwa njia ya vitu vya dunia ambavyo vilimzunguka, kama shamba, mbegu, ndege, vivi hivi, ndivyo vitu ambavyo sisi sote tunaweza kuona.

**4:3,4** Mfano huu ni juu ya **mwenye**

**kupanda mbegu, mbegu yenyewe,** na udongo. Udongo **kando ya njia** ulikuwa nguvu zaidi na mbegu hazikuwa na njia kuingia na kuota. Basi **ndege walikuja** wakazimeza.

**4:5,6** Kulikuwa na udongo nusu tu juu ya **pahali pa mwamba**. Haukutosha kwa mbegu kuingiza mizizi chini sana.

**4:7** Udongo wa miiba ulikuwa na vijiti vya miiba vilivyosonga mbegu hata hazikupata jua na mvua, na zilizuizwa zisizae matunda.

**4:8,9** **Udongo mzuri** ulikuwa pahali pazuri kwa mbegu kuweza kukua. Mbegu **nyingine** zilizaa **makumi tatu**, nyingine **makumi sita**, na nyingine **mia moja**.

**4:10-12** Wakati wanafunzi walipokuwa **peke yao** pamoja na Bwana, **walimwuliza** kwa sababu gani alitumika na mifano saa ya kufundisha. Alieleza ya kwamba wale tu waliokuwa na roho tayari walipewa ruhusa **kujua siri ya ufalme wa Mungu. Siri** ndani ya Agano Jipya ndiyo kweli watu wasiyojua kufika wakati ule, kweli inayofunuliwa na Mungu tu. **Siri ya ufalme wa Mungu** ndiyo ya kwamba:

1. Bwana Yesu alikataliwa na watu wakati alipojionyesha kuwa Mfalme wa Israeli.
2. Muda fulani utapita mbele ya kusimamishwa kwa ufalme hapa duniani.
3. Kufika wakati ule, utakuwa ufalme wa roho tu. Watu wote wanaokiri ya kwamba Kristo ni Mfalme, watakuwa ndani ya ufalme ule, hata kama Mfalme mwenyewe hatakuwa duniani saa ile.
4. Neno la Mungu litapandwa kwa muda ule na kuzaa matunda kwa vipimo mbalimbali. Watu wengine watazaliwa tena kweli kweli, lakini wengine watakuwa waamini wa kinywa tu. Wote wanaokiri kuwa Wakristo watakuwa ndani ya ufalme unaoonekana, lakini waamini wa kweli tu wataingia ufalme wa kweli, wa roho.

Mashairi 11 na 12 yanaeleza kwa sababu gani tumepewa kweli hii kwa njia ya mifano. Mungu anafunua siri zake za ndani kwa wenye moyo tayari, wale watakaopokea kweli yake na kuitii, lakini anaficha na kusudi, kweli kwa wale wanaokataa nuru waliyopewa. Yesu anaita watu wale **"walio inje."** Labda msomaji anayesoma maneno haya mbio mbio tu atafikiri maneno ya shairi 12 ni makali, **"ili wakitazama, watazame, wasione, na wakisikia, wasikie, wasifahamu, wasije wakageuka na kusamehewa."**

Lakini sharti tukumbuke ya kwamba watu hawa walikuwa wamebarikiwa sana. Mwana wa Mungu alikuwa amefundisha katikati yao, na kutenda maajabu mengi mbele ya macho yao. Kwa pahali pa kukiri kwamba yeye ni Masiya ya kweli, walimkataa hata saa ile. Kwa sababu walikuwa wamekataa Nuru ya ulimwengu, watanyimiwa tangu saa ile nuru ya mafundisho yake. Wataona maajabu yake, lakini hawatafahamu maana yao kwa njia ya roho; watasikia maneno yake, bila kutambua mafundisho yao ya ndani.

Inawezekana kwa watu kusikia Habari Njema mara ya mwisho. Inawezekana kwa mtu kuendelea kufanya zambi mpaka mwisho siku ya neema katika maisha yake, kisha hakuna njia tena kwa yeye kuokolewa. Kuna wanaume na wanawake waliokataa Mwokozi na wasiopata njia tena kamwe kutubu na kupata usamehe. Labda wanasikia Habari Njema, lakini masikio yao na mioyo yao yamegeuka magumu na hawafahamu. Watu wanasemaga, "Kuna taraja kwa mtu angali ana uzima," lakini Biblia inasema juu ya wengine walio na uzima mwilini, lakini

hakuna tumaini kwamba watatubu siku nyingine. Kwa mfano ona Ebr. 6:4-6.

**4:13** Akigeuka na kusema tena juu ya mfano wa mpandaji mbegu, Bwana Yesu aliuliza kama walifikiri **watafahamu mifano** iliyo migumu kupita huu namna gani, kama wakishindwa kufahamu **mfano** huu usiokuwa nguvu.

**4:14** Mwokozi hakusema kama **mpandaji mbegu** ni nani. Labda ni yeye mwenyewe, au wale ambao wanahubiri kama wajumbe wake. Alisema ya kwamba mbegu ni **Neno.**

**4:15-20** Udongo namna namna ni mfano wa mioyo ya watu na kwa kipimo gani wanapokea Neno:

**Udongo kando ya njia** (sh.15). Moyo wa mtu huyu ni mgumu sana. Anakataa kupokea Mwokozi na roho ya ukaidi kabisa. Ndege ni mfano wa **Shetani** anayeondoa mbegu ya Neno la Mungu. Habari alizosikia hazigusi msikiaji kwa wakati ule na kwa wakati wa nyuma vilevile.

**Pahali pa mwamba** (mash. 16,17). Mtu huyu anapokea **Neno** na furaha kwa sababu mhubiri analihubiri na uwezo kabisa. Anakiri ya kwamba anaamini Kristo, lakini imani yake ni ukubali wa kichwa na nia tu. Hajitoi kabisa kwa Bwana. Anapokea Neno **kwa furaha;** laiti angalilipokea na roho ya toba ya kweli. Ni kama anafuata Bwana vizuri kwa wakati, lakini saa **anapopata taabu na mateso** kwa sababu ya kufuata Bwana, anafikiri bei ya kumfuata ni kubwa zaidi na anaacha. Anakiri kuwa Mkristo wakati ni neno zuri kwa macho ya watu, lakini mateso yanafunua ya kwamba hakuamini na roho ya kweli.

**Udongo wenye miiba** (mash.18,19). Inaonekana ya kwamba watu hawa wanaanza vizuri vilevile. Wanaonekana kuwa waamini wa kweli. Lakini nyuma kidogo wanaanza kufikiri zaidi juu ya kazi ya dunia na masumbuko yake, na tamaa ya kujivimbishia mali. Hamu yao kwa maneno ya roho inapunguka, na nyuma kidogo hawasemi tena kwamba wao ni Wakristo.

**Udongo mzuri** (sh.20). Watu hawa wanapokea **Neno** na roho ya kweli, si neno kama bei ya kufanya hivi (taabu, mateso) ni nini. Watu hawa wanazaliwa tena kweli kweli, nao ni wafuata waaminifu wa Kristo, Mfalme. Maneno ya dunia, tabia ya mwili, wala Shetani hayawezi kuwaondosha karibu na Bwana.

Lakini hata wale wanaopokea Neno na roho ya kweli wanazaa matunda kwa vipimo mbalimbali, wengine **makumi tatu**, wengine **makumi sita,** na wengine **mia moja.** Sababu ya vipimo hivi mbalimbali ni nini**?** Mtu anayezaa matunda mengi zaidi ndiye anayetii Neno la Mungu mara moja, bila kuulizauliza juu ya maagizo yake, na anatii na furaha.

**E. Madaraka ya wasikiaji (4:21-25)**

**4:21** **Taa** ni mfano wa kweli Bwana alizojulisha wanafunzi wake. Walikatazwa kuficha kweli hizi **chini ya kitunga au kitanda,** lakini Bwana aliwaagiza kuzionyesha wazi kwa watu. Labda **kitunga** ni mfano wa kazi ya dunia tunayoacha kuiba saa inayopasa kuweka kwa maneno ya Mungu. Labda **kitanda** ni mfano wa uvivu. Maneno haya yote yanashindana na mahubiri ya Habari Njema.

**4:22** Yesu alisema na makutano kwa njia ya mifano. Kweli ile aliyofundisha **ilifichwa**. Alikusudi kwa wanafunzi kueleza kweli hizi kwa wale waliokuwa tayari kuzipokea. Labda maana ya shairi 22 ni ya kwamba inapasa wanafunzi kutumika wakikumbuka ya kwamba kwa wakati wa kuja maneno yote yatafunuliwa wazi. Saa ile itaonekana wazi kama waliweka roho juu ya kazi ya biashara na mambo ya anasa kuliko ushuhuda wao kwa Mwokozi.

**4:23** Maonyo ya Yesu, **“Mwenye**

**masikio ya kusikia asikie"** yanaonyesha uzito wa mafundisho haya.

**4:24** Halafu Mwokozi aliongeza maonyo mazito mengine: **"Angalieni maneno munayosikia."** Nikisikia agizo toka Neno la Mungu bila kulitii mimi mwenyewe, siwezi kulifundisha kwa watu wengine. Mafundisho ya mhubiri yana uwezo kama wasikiaji wakiweza kuona kweli anayofundisha ndani ya maisha na mwenendo wake mwenyewe.

Kwa kipimo tunachoshiriki kweli ya Mungu na watu wengine, kwa kipimo kile na zaidi sisi wenyewe tunabarikiwa. Mwalimu anayetayarisha mafundisho kwa wanafunzi anapata baraka kubwa kupita wanafunzi wenyewe. Na zawabu ambayo atapata kwa wakati wa kuja itapita mbali masumbuko yake madogo.

**4:25** Kila mara tunapopokea kweli mpya, na kuacha kweli hii kugeuka sehemu ya maisha yetu, tutapewa kweli nyingine tena. Lakini kama tusipoacha kweli hii kugusa na kugeuza maisha yetu, tutapoteza faida ya kweli tulizopewa mbele vilevile.

### F. Mfano wa mbegu inayoota kwa siri (4:26-29)

Mfano huu unaandikwa ndani ya Marko tu. Unaweza kuelezwa kwa njia mbili, au zaidi. **Mtu** mwenyewe ni mfano wa Bwana Yesu akitupa **mbegu** juu ya udongo wakati wa utumishi wake katikati ya watu, kisha akirudi mbinguni. Mbegu inaanza kuota – kama kwa siri na bila kuonekana sana, lakini bila shaka inaota. Kwa mwanzo ule mdogo yanatoka mavuno makubwa ya waamini wa kweli. **Wakati mbegu zinapokomea … zitapelekwa** kwa gala ya mbingu.

Au, labda kusudi la mfano huu lilikuwa kupatisha roho za wanafunzi nguvu. Kazi yao ilikuwa kupanda **mbegu**. Waliweza **kulala usingizi usiku na kuamka tena asubui,** wakijua ya kwamba Neno la Mungu halitakufa bure, lakini litatimiza makusudi yake. Kwa njia ya siri tusiyoweza kufahamu, bila nguvu na akili ya mtu, Neno la Mungu linafanya kazi yake ndani ya mioyo ya watu, na kuzaa matunda kwa Mungu. Mtu anapanda na kutia maji, lakini ni Mungu anayekuza mbegu. Lakini shairi 29 halipatani kabisa na elezo hili. Mungu tu anaweza kutuma **mundu** kwa wakati wa **mavuno**. Lakini ndani ya mfano huu mtu yule anayepanda mbegu **anatuma mundu** vilevile wakati mbegu zinapokomea.

### G. Mfano wa mbegu ya haradali (4:30-34)

**4:30-32** Mfano huu unaonyesha kukua na kuongezeka kwa **ufalme** toka mwanzo mdogo sana kama **mbegu ya haradali,** na kugeuka mti mkubwa wa kutosha kwa **ndege** kupanga ndani ya matawi yake. Kwa wakati wa mwanzo wake ufalme ulikuwa na watu wachache tu walioteswa na watu wengine. Nyuma ya wakati uligeuka dini ya serikali. Ulionekana vizuri, lakini wengi wa wafuata wake waliheshimu Mfalme kwa kinywa tu bila kuokolewa kweli. Mwandishi mmoja alisema:

> Kanisa liliendelea vizuri wakati wa mateso. Lakini wakati mateso na maumivu haya yalipokombolewa na sifa na heshima, lilipoa na halikuendelea mbele tena. Kanisa lilisaidiwa na kupatishwa nguvu wakati waamini walipofungwa kuwa vyakula kwa simba, kupita wakati lilipopata sifa na heshima.

Hivi mti wa haradali ni mfano wa Ukristo, ndio watu wanao*jitaja* Wakristo. Matawi ya mti huu yamegeuka pahali pa kila namna ya walimu wa uwongo kukaa chini ya kivuli chake. Huu ndio ufalme unaoonekana kwa macho sasa.

**4:33,34** Mashairi haya yanatuonyesha namna gani inatupasa kufundisha wengine. Yesu alifundisha

watu **kwa kadiri walivyoweza kusikia.** Aliongeza juu ya maneno waliyokwisha kujifunza mbele, akiacha saa ya kutosha kwa mafundisho yale kuingia kabisa rohoni mwao. Alijua kipimo cha ufahamu wa wasikiaji wake, na hakuwafundisha kupita maneno ambayo waliweza kupokea rohoni mwao. (Ona vilevile Yoane 16:12; 1 Kor. 3:2; Ebr. 5:12.)

Alileta zaidi ya mafundisho yake kwa njia ya mifano, lakini **alieleza** maana yao kwa **wanafunzi wake** wakati walipokuwa peke yao. Anaongeza nuru kwa wale ambao wana hamu ya kweli kuipokea.

**H. Upepo na mawimbi yanatumikia Mtumishi (4:35-41)**

**4:35-37 Siku ile ile**, saa ya **mangaribi,** Yesu na wanafunzi wake walianza kuvuka Bahari ya Galilaya kwenda kwa pwani yake ya mashariki. Hawakutayarisha maneno mbele kwa safari hii. **Vyombo vidogo vingine** viliwafuata. Gafula kulikuwa na **zoruba kubwa ya upepo. Mawimbi** makubwa yalitaka kufunika **chombo.**

**4:38-41** Yesu alikuwa akilala kwa **upande wa nyuma** wa chombo. Wanafunzi, wakijaa woga, **walimwamsha**, na kumhamikia kwa sababu ni kama hakuweka roho juu ya hatari kubwa ambayo iliwapata. Bwana **akaamka, akahamakia upepo** na mawimbi, ikakuwa **kimya** mara moja. Kisha Yesu alihamakia wanafunzi kwa sababu waliogopa na kukosa imani. Ajabu hili liliwashangaza sana. Ndiyo, walijua ya kwamba Yesu ni Mungu, lakini hata hivi walistaajabu juu ya uwezo wa Huyu aliyetawala hata zoruba na machafuko ya bahari.

Tukio hili linaonyesha utu na uungu wa Bwana Yesu. Alilala usingizi kwa upande wa nyuma ya chombo; neno hili lilionyesha utu wake. Alisema neno, na bahari ilitulia – alama ya uungu wake.

Linaonyesha uwezo wake juu ya ulimwengu na viumbe ndani yake, kama vile maajabu yake ya mbele yalivyoonyesha uwezo wake juu ya magonjwa na pepo wachafu.

Mwishoni, linaamsha hamu ndani ya roho zetu kufika kwake ndani ya masumbuko na machafuko yote ambayo tunakutana nayo, tukijua ya kwamba chombo hakiwezi kuzama wakati yeye ni ndani yake.

**I. Mwenye wazimu wa Wagerase aliponyeshwa (5:1-20)**

**5:1-5 Inchi ya Wagerase** ilikuwa kwa upande wa mashariki wa bahari ya Galilaya. Pale Yesu alikutana na mtu mwenye nguvu na ukali zaidi aliyetawaliwa na pepo, mwenye kuogopesha watu kando kando. Iliwashinda kabisa kumfunga. Aliishi pahali pa **makaburi** na vilimani, akipiga makelele wakati wote na **kujikata kwa mawe**.

**5:6-13** Wakati mwenye pepo **alipoona Yesu**, alitenda kwanza na adabu, lakini nyuma alinungunika na uchungu. Ni neno la kuogopesha kabisa kuona mtu akiabudu, akiomba na akiamini, lakini ndani ya roho yake ni kama kuna mtu mwingine anayejaa vita, chuki, na woga, pamoja na hamu kufunguliwa toka utumwa wa maneno haya, lakini hata hivi akifungamana nayo.

Hatujui kabisa kama maneno haya yalifuatana namna gani, lakini tunawaza labda ilikuwa hivi:

1. Mwenye pepo alitendea Bwana Yesu na heshima kwanza (sh.6).
2. Yesu aliagiza **pepo mchafu kutoka** ndani yake (sh.8).
3. Pepo, akisema ndani ya mtu mwenyewe, alikiri kwamba Yesu alikuwa nani, akauliza nini ilimpa ruhusa kujiingiliza ndani ya maneno yake, na alisihi Yesu na kiapo kuacha kumtesa (sh.7).
4. Yesu **aliuliza jina** la mtu mwe-

nyewe. Lilikuwa **Legioni**, maana yake pepo wachafu mengi walikaa ndani yake (sh.9). Neno hili halikani shairi 2, pahali tunaposoma alikuwa na roho mchafu (mmoja).

5. Labda alikuwa mnenaji wa pepo wachafu aliyesihi ruhusa kwa pepo **kuingia kundi la nguruwe** (mash.10-12).
6. Alipewa ruhusa na halafu nguruwe **elfu mbili** walishuka mlima mbio na **kuzama baharini** (sh.13).

Watu wameshitaki Bwana mara nyingi juu ya kuharibu nguruwe wale. Tukumbuke maneno haya:

1. Yesu hakuwaharibu; alitoa ruhusa tu waharibiwe. Waliharibiwa kwa uwezo wa Shetani.
2. Hatusomi ya kwamba wenye nguruwe walimshitaki. Labda walikuwa Wayuda na walikatazwa kufuga nguruwe.
3. Damani ya roho ya mtu huyu ilipita bei ya nguruwe zote duniani.
4. Tungalijua maneno yote ambayo Yesu alijua tungalitenda kama yeye.

**5:14-17** Watu walioona uharibifu wa nguruwe walikimbia **kwa mji** na habari hizi. Watu wengi walikwenda kuona nini ilitokea, wakakuta mtu aliyekuwa na pepo wachafu mbele **akiketi** kwa miguu ya Yesu **akivaa nguo, na mwenye akili tena**. Basi watu **waliogopa**. Mtu mmoja alisema waliogopa wakati Yesu alipotuliza zoruba na mawimbi ya bahari, na sasa waliogopa wakati alipotuliza vita ndani ya roho ya mtu. Watu walioona na macho yao maneno haya yakitokea walipasha habari hizi zote kwa wale waliofika sasa tu. Habari hizi ziliwashinda; wakasihi Bwana **kuondoka katika mipaka yao**. Lilikuwa neno hili, si uharibifu wa nguruwe, lililo neno la kuchukiza roho zetu zaidi. Kristo alikuwa mgeni mwenye bei kubwa zaidi.

Mwalimu mmoja alisema, "Hata sasa watu wengi sana wasioweza kuhesabiwa wanataka Kristo kukaa mbali nao, kwani wanaogopa ya kwamba kupatana naye kutakuwa hasara kwao kwa njia ya mali au urafiki wa watu. Wakijaribu kuponyesha mali yao wanapoteza roho zao."

**5:18-20** Wakati Yesu alipokuwa karibu kwenda zake ndani ya **chombo**, mtu aliyeponyeshwa **alimsihi** kumruhusu kwenda pamoja naye. Ombi lake lilikuwa ombi zuri. Lilionyesha ya kwamba alizaliwa tena kweli, lakini Yesu alimwagiza kurudi kwa **nyumba yake** kama mshuhuda hai wa uwezo na rehema kubwa ya Mungu. Mtu mwenyewe alitii, akapeleka habari njema kwa **Dekapoli**, sehemu ya inchi yenye miji kumi.

Agizo hili ni kwa sisi sote tulio-okolewa kwa neema ya Mungu: **"Kwenda kwa nyumba yako kwa watu wako kuwaambia maneno makubwa gani ambayo Bwana alifanya juu yako na namna alivyokurehemu."** *Kwetu* ndipo pahali inapotupasa kuanza kuhubiri Habari Njema!

### J. Kuponyesha wenye magonjwa yasiyoweza kuponyeshwa, na kufufua wafu (5:21-43)

**5:21-23** Wakati waliporudi kwa pwani ya mangaribi, Bwana alizungukwa mbio na **makutano makubwa**. Baba mmoja mwenye taabu kubwa rohoni alikimbia karibu naye. Alikuwa **Yairo, mmoja wa watawala wa sunagogi**. **Binti** yake **mdogo** alikuwa karibu kufa. Alisihi Yesu kwenda na **kumwekea mkono aweze kupona.**

**5:24** Bwana alikubali, akaanza kwenda kwa nyumba yake. Watu wengi **walifuata** wakimsongasonga. Ona ya kwamba mara moja nyuma ya kusoma juu ya makutano wakim*songasonga*, tunasoma juu ya mtu mmoja akim*gusa* na imani kwa kupata kuponyeshwa.

**5:25-29 Mwanamke** mmoja mwenye **kuhangaika sana** alifikia Yesu wakati alipokuwa akikwendea nyumba ya Yairo. Kizuizo hiki hakikuchokoza Bwana. *Sisi* tunatenda namna gani wakati tunapokutana na maneno yanayoonekana kama vizuizo?

> Neno ambalo linanisaidia zaidi ni kufikiri juu ya vizuizo hivi vyote vinavyochelewesha kazi ambayo nilikusudi kufanya, kama mafundisho toka Mungu kunisaidia nisiweke roho zaidi juu ya kazi yangu. Vizuizo hivi havipotezi saa bure (kama sisi tunavyofikiri mara nyingine), lakini ni sehemu kubwa na ya faida zaidi ya kazi ya siku ile – kazi nzuri zaidi ambayo tunaweza kutolea Mungu.
>
> (*Choice Gleanings Calendrier)*

Mwanamke huyu alikuwa ameteswa sana kwa sababu ya kutoka damu kwa **miaka kumi na miwili**. Alifikia **waganga wengi** kupata kusaidiwa, lakini walimaliza mali yake tu na **kuongeza** taabu yake. Wakati tumaini lake kupata kuponyeshwa lilipokuwa karibu kwisha, mtu mmoja alimwambia habari za Yesu. Alikwenda mara moja kumtafuta. Akipita polepole ndani ya makutano, akafika karibu naye na **kugusa vazi lake.** Mara moja damu yake iliacha kutoka na alikuwa na afya njema.

**5:30** Alikusudi kwenda zake bila kuonekana, lakini Bwana hakutaka akose baraka ya kumshuhudia kuwa Mwokozi wake. Bwana alijua ya kwamba **uwezo** ulikuwa umetoka kwake wakati mwanamke alipomgusa; ni kama alilipa bei kumponyesha. Hivi aliuliza, **"Nani aliyegusa mavazi yangu?"** Alijua jibu la ulizo hili, lakini aliliuliza kusudi mwanamke aonekane katikati ya watu.

**5:31 Wanafunzi** wa Bwana walifikiri ulizo lake lilikuwa pumbavu. Watu wengi walikuwa wakimsongasonga saa zote. Kwa nini basi atauliza, **"Nani alinigusa?"** Lakini kuna tofauti. Inawezekana kugusa Bwana kwa sababu ya ukaribu wa mwili tu, au na imani kwa sababu ya hitaji kubwa la roho. Tunaweza kuwa karibu sana naye bila kumwamini, lakini haiwezekani kumgusa na imani bila Bwana kujua neno hili, na bila kupata kuponyeshwa.

**5:32,33** Basi **mwanamke** alikuja, **akiogopa na kutetemeka**; **akaanguka mbele yake** na kukiri Yesu mbele ya watu mara ya kwanza.

**5:34** Halafu Yesu alisema maneno ya kusaidia roho yake. Ni neno kubwa kukiri mbele ya watu ya kwamba tumeamini Bwana. Hatutapata nguvu vizuri katika imani bila kufanya hivi. Wakati tunapomkiri na uhodari mbele ya watu, atajaza roho zetu na ufahamu ya kwamba tumeokolewa kweli kweli. Masemo ya Bwana yalihakikisha kuponyeshwa kwa mwili wake, na bila shaka yalihakikisha baraka kubwa ya wokovu wa roho wake vilevile.

**5:35-38** Saa ile wajumbe walikuwa wamefika na habari ya kwamba **binti** ya Yairo alikuwa amekufa. Hakuna hitaji tena kwa **Mwalimu** kufika. Bwana aliburudisha roho ya Yairo, kisha alifikia nyumba yake akipeleka **Petro, Yakobo na Yoane** pamoja naye. Walikuta watu wakitoa machozi sana kama ilivyokuwa desturi kwa jamaa za inchi ya mashariki kwa wakati wa huzuni. Watu wengine walipewa mshahara waweze kuomboleza.

**5:39-42** Wakati Yesu alipowajulisha ya kwamba **mtoto hakufa lakini alilala tu,** waliacha kuomboleza, wakamcheka sana. Lakini Bwana alipeleka jamaa ya karibu, akakwenda nao karibu na mtoto aliyelala kama mfu, **akashika mkono wake**, **akamwambia** kwa lugha ya Aramaic, **"Msichana, ninakuambia: Simama."** Basi **msichana** yule mwenye miaka 12 alisimama mara moja, **akatembea**. Ndugu zake walishangaa sana sana pamoja na kushindwa kwa furaha.

**5:43** Bwana aliwakataza kutangaza habari za ajabu hili katikati ya watu. Hakuweka roho juu ya sifa ya makutano. Kusudi lake lilikuwa kwenda mbele tu hata msalaba.

Kama msichana angalikufa kweli, kama sura hii ingalionyesha uwezo wa Yesu juu ya pepo wachafu, magonjwa, na mauti. Walimu wengine wa Biblia hawakubali ya kwamba alikufa kweli. Yesu alisema hakufa lakini alilala tu. Labda alikuwa ndani ya usingizi mzito sana, na hali ya kuzimia roho. Bwana angaliweza kumfufua toka wafu lakini alikataa kusema alifanya hivi kama msichana alizimia tu.

Tusikose kusoma maneno ya mwisho ya sura hii: **"Akaamuru wampe chakula."** Neno hili ni neno la sharti vilevile kwa **roho** za waamini wa sasa. Sharti tuwakulishe na Neno la Mungu. Kulisha kondoo za Bwana ni njia moja kwa mwanafunzi wa Yesu kuonyesha mapendo yake kwa Mwokozi wake.

### K. Mtumishi anakataliwa kwa Nazareti (6:1-6)

**6:1-3** Yesu alirudi kwa Nazareti pamoja na **wanafunzi wake**. Hii ilikuwa **inchi yake** mwenyewe, pahali alipotumika kazi kama seremala. **Siku ya sabato** alifundisha **ndani ya sunagogi.** Watu **walishangaa** wakati walipomsikia na hawakuweza kukana hekima ya mafundisho yake wala kukosa kushangaa juu ya maajabu yake. Lakini rohoni mwao hawakuwa tayari kumpokea kama Mwana wa Mungu. Walimjua kama **seremala, mwana wa Maria,** mwenye ndugu waume na **wake** waliokaa katika Nazareti vilevile. Kama angalirudia Nazareti kama Mshindaji wa kujulikana nyuma ya vita, kama wangalikuwa tayari kumpokea. Lakini alikuja na neema na unyenyekevu. Neno hili **liliwachukiza**.

**6:4-6** Kwa saa ile **Yesu** alisema ni kama **nabii** anapokewa vizuri kupita katika inchi nyingine, si katika inchi yake mwenyewe. Watu wa jamaa yake na rafiki zake hawawezi kutambua uzuri wake wala wa utumishi wake. Ni nguvu kutumikia Bwana katika inchi yetu wenyewe kupita katika pahali po pote pengine. Watu wa Nazareti walizarauliwa. Watu wa pahali pengine walisemaga, "Neno zuri linaweza kutoka katika Nazareti?" Hata hivi watu hawa waliozarauliwa wao wenyewe na watu wengine walizarau Bwana Yesu. Walionyesha wazi kiburi na kutokukuamini ndani ya mioyo ya watu! Kutokuamini kwao kulizuiza zaidi ya kazi ya Mwokozi katika Nazareti. Aliponyesha **wagonjwa wachache** tu. Alishangaa juu ya kutokuamini kwa watu. J.G. Miller anatuonya:

> Kutokuamini namna hii kunaweza kuzaa mabaya mengi. Kunafunga njia kwa neema na rehema, na kuacha nusu ndogo tu kusaidia wenye hitaji.

Hivi Yesu alionja tena upekee kwa sababu ya kuzarauliwa na watu. Wengi wa wafuata wake wameshiriki ndani ya huzuni hii. Mara nyingi watumishi wa Bwana wanaonekana kama watu wa chini sana. Haifai tuangalie maneno yanayoonekana kwa macho tu, lakini tutambue vilevile hali nzuri ya roho ya mtu. Watu wa Nazareti walizarau Yesu na kumkataa, lakini Yesu aliona neno hili bure, **akazunguka** katika **vijiji** kando kando akifundisha Neno la Mungu.

### L. Mtumishi anatuma wanafunzi wake kuhubiri (6:7-13)

**6:7** Saa ilikuwa imefika kwa wale **kumi na wawili** kuanza kazi yao katikati ya watu. Walikuwa wamepokea mafundisho mazuri sana toka Mwokozi; sasa watakwenda wao wenyewe kutangaza habari hizi za utukufu. **Aliwatuma, wawili wawili**. Hivi mahubiri yao yatahakikishwa kwa njia ya washuhuda wawili. Na vilevile wakisafiri pamoja

wataweza kusaidiana. Pahali pengine zambi za mwili zinazidi, na ni vizuri kwa wahubiri wawili kusafiri na kuhubiri pamoja. Kisha **aliwapa amri juu ya pepo wachafu.** Ni Mungu tu anayeweza kutolea watu uwezo huu.

**6:8** Kama ufalme wa Bwana wetu ungalikuwa wa dunia hii kama asingalitoa kamwe maagizo ndani ya mashairi 8-11. Yalikuwa namna nyingine na yale ambayo viongozi vya dunia wangaliweza kutoa. Wanafunzi waliagizwa kwenda bila vitu kuwasaidia, **bila mfuko, mkate, feza ndani ya kiuno.** Waliagizwa kumtegemea yeye tu kuwapatia vyote walivyohitaji.

**6:9** Walikuwa na ruhusa kwenda na **viatu** na gongo (labda kazi ya gongo ilikuwa kujilinda wasiumizwe na nyama za mwitu), na kanzu moja tu. Hakuna mtu atakayekuwa na wivu juu ya mali ya wanafunzi, au kukokotwa karibu na dini ya Ukristo kwa sababu ya kugeuka mtajiri! Na sharti uwezo wo wote wa wanafunzi utoke kwa Mungu. Ilikuwa lazima kwao kumtegemea yeye tu kwa maneno yote. Walikwenda na uchache wa vitu kabisa, lakini kama wajumbe wa Mwana wa Mungu, na wenye uwezo toka kwake.

**6:10** Watu wakiwa tayari kuwapokea nyumbani mwao kama wageni wao, sharti wakubali kuingia nyumba ile na **kupanga pale kufika wakati** watakapoondokea inchi ile. Kusudi la agizo hili lilikuwa kuwazuiza wasijitafutie kao zuri kupita. Kazi yao ilikuwa kuhubiri habari za Yule asiyejipendeza mwenyewe, wala kujitafutia mwenyewe faida. Walikatazwa kupunguza uwezo wa mahubiri yao kwa njia ya kujipendeza, na kujaribu kukaa vizuri wao wenyewe.

**6:11** Haikuwa sharti kwa wanafunzi kubaki pahali watu walipowakataa pamoja na mafundisho yao. Kukaa pahali pa namna hii ni kama kutupa lulu mbele ya nguruwe. Wakati wanafunzi walipoondokea pahali pa namna hii ilipasa **kukunguta mavumbi yaliyo chini ya miguu yao**, kama mfano wa Mungu akikataa wale wanaokataa Mwana wake mpendwa.

Mengine ya maagizo haya yalikuwa kwa wakati ule tu, na Bwana Yesu aliyaondosha kwa wakati wa nyuma (Luka 22:35,36), lakini yanafundisha kawaida nyingine iliyo lazima kwa mtumishi wa Kristo kwa kila muda.

**6:12, 13** Wanafunzi **walitoka na kuhubiri** kwamba ilipasa watu kutubu, **walifukuza pepo wachafu wengi, wakapakaa na mafuta watu wengi waliokuwa wagonjwa,** na kuwaponyesha. Kupakaa na **mafuta**, tunafikiri, kulikuwa alama kuonyesha uwezo wa Roho Mtakatifu, akituliza na kupunguza maumivu.

### M. Mtangulizi wa Mtumishi anakatiwa kichwa (6:14-29)

**6:14-16** Wakati mfalme **Herode** aliposikia habari za mtendaji maajabu akisafiri inchini, alifikiri mara moja ya kwamba **Yoane Mbatizaji alikuwa amefufuka toka wafu.** Watu wengine walifikiri alikuwa **Elia**, **au mmoja wa manabii**, lakini Herode aliamini kabisa ya kwamba mtu yule ambaye **alimkatia kichwa** alikuwa amefufuka. Yoane Mbatizaji alikuwa sauti toka Mungu. Herode alikuwa amenyamazisha sauti ile, na sasa zamiri yake ilimtesa sana kwa sababu ya tendo hili. Ilimpasa kujifunza ya kwamba njia ya mkosaji ni ngumu.

**6:17-20** Sasa mwandishi alirudi tena kwa habari za kuuawa kwa Yoane. Mbatizaji alikuwa amehamakia Herode juu ya kuoa **mke wa ndugu yake Filipo**, ndoa isiyopatana na sheria. Herodia, aliyekuwa mke wa Herode sasa, alijaa gazabu, akakusudi na nguvu ya kwamba atajilipiza kisasi. Lakini

Herode aliheshimu Yoane kama **mtu mtakatifu**, akamlinda.

**6:21-25** Nyuma ya wakati Herodia alipata njia kutimiza kusudi lake. Kwa karamu ya **siku ya kuzaliwa** kwa Herode, wakubwa wa serikali wakiwa pahali penyewe vilevile, **Herodia** alitayarisha njia kwa **binti** yake kucheza mbele ya wageni. Neno hili **lilipendeza Herode** sana, naye aliahidi kumpa msichana kitu cho chote alichotaka, **hata nusu ya ufalme** wake. Akisukumwa na mama yake, msichana aliomba kupewa **kichwa cha Yoane Mbatizaji juu ya sahani.**

**6:26-28** **Mfalme** alinaswa ndani ya mtego. Hata kama yeye mwenyewe hakutaka kufanya hivi, na akijua kutenda neno hili ni vibaya, alimpa msichana kitu alichoomba. Mfalme aligeuka mtumwa wa mwanamke mwovu na kushindwa naye na mchezo wa anasa.

**6:29** Wakati **wafuata** waaminifu wa Yoane **waliposikia** habari hizi, walikuja, wakachukua **maiti yake** na kuizika, kisha walikwenda kupasha habari na Yesu.

**N. Kulisha watu elfu tano (6:30-44)**

**6:30** Habari za ajabu hili ziliandikwa ndani ya Habari Njema ine zote. Lilifanyikana kwa mwanzo wa mwaka wa tatu wa utumishi wa Bwana Yesu katikati ya watu. Mitume walikuwa wamerudi sasa tu toka safari yao ya kwanza ya kuhubiri (ona mash. 7-13). Labda walijaa na furaha kwa sababu ya baraka waliyoona, au labda walichoka, na miguu yao iliuma. Bwana akitambua kwamba walihitaji kupata saa kupumzika na kukaa kimya, aliwapeleka ndani ya chombo cha maji kwa pahali pasipo watu kwa pwani ya Bahari ya Galilaya.

**6:31,32** Tunasikia watu kusema mara nyingi, **"Kujeni ninyi peke yenu katika pahali pasipo watu, mupumzike kidogo"** kama ruhusa kwenda kukaa katika hoteli ya bei kubwa. Mwalimu mmoja wa zamani (jina lake Kelly) aliandika,

> "Ingalikuwa vizuri kama tungalihitaji kupumzika zaidi, maana kama tukifanya kazi nyingi zaidi tukijikana wenyewe kwa kusaidia na kuwa baraka kwa watu wengine siku kwa siku, hata Bwana angaliweza kusema nasi kupumzika kidogo." [4]

**6:33,34** Watu wengi walifuata Bwana na mitume wakitembea kufuata pwani ya bahari. **Yesu aliwahurumia**. Walikuwa wakihangaika bila kiongozi kwa maneno ya roho, wenye njaa na bila mchungaji. **Basi akaanza kuwafundisha.**

**6:35,36** Wakati saa zilipokaa kupita **wanafunzi** walianza kusumbuka. Watu walikuwa wengi sana na **walikosa chakula**. Walisukuma Bwana **kuaga watu waende zao**. Makutano yale yaliyowasha huruma rohoni mwa Bwana yalichukiza wanafunzi. Tunasumbushwa na watu na mahitaji yao au tunawapenda?

**6:37,38** Yesu akawajibu, akasema, **"Ninyi muwape chakula."** Hili lilikuwa agizo la namna gani! Wanaume elfu tano pamoja na wanawake na watoto, na hakuna chakula ila mikate mitano tu na samaki wawili – pamoja na Mungu.

**6:39-44** Ndani ya ajabu hili wanafunzi waliona mfano wa namna Mwokozi atakavyojitoa mwenyewe kuwa mkate wa uzima kwa dunia inayokufa kwa njaa rohoni. Mwili wake utavunjwa ili watu waweze kupata uzima wa milele. Ndiyo, maneno mwandishi aliyosema hapa yanatufikirisha sana Karamu ya Bwana iliyo ukumbusho wa mauti yake: **Akatwaa … akazibariki, akavunja … akawapa.**

Wanafunzi walipata mafundisho matamu ya faida kwa utumishi wao wenyewe kwa Bwana:

1. Haikuwa vizuri kwa wanafunzi kuwa na shaka juu ya uwezo wa Bwana kuwapatia vyote walivyohitaji. Akiweza kulisha **watu elfu tano** na mikate **mitano** na samaki **wawili**, ataweza kupatia watumishi wake ambao wanamtegemea mahitaji yao yote. Wanaweza kumtumikia bila kusumbuka juu ya pahali gani chakula chao kitakapopatikana. Wakitafuta kwanza ufalme wa Mungu na haki yake, vitu vyote wanavyohitaji vitaongezwa kwao.
2. Namna gani wapotevu wa dunia hii watasikia Habari Njema? Yesu anasema, **"Ninyi muwape chakula!"** Tukimpa Bwana tulivyo navyo, hata vinaonekana kuwa vidogo sana, anaweza kuvizidisha kuwa baraka kwa watu wengi sana.
3. Aliongoza kazi ya kulisha makutano haya na utaratibu, akiwaketisha kwa mafungo ya watu **mia moja,** na watu **makumi tano.**
4. **Akabariki** na **kuvunja** mikate na samaki. Bila baraka yake vyakula hivi havikuweza kutosha hata kidogo. "Tunakosa kuwa baraka kupita kwa watu kwa sababu hatuna roho za kuvunjika kabisa mikononi mwa Bwana." (*Sehemu chaguliwa*)
5. Yesu hakugawa vyakula hivi yeye mwenyewe. Aliruhusu **wanafunzi wake** kufanya hivi. Ni shauri lake kulisha dunia kwa njia ya watu wake.
6. Kulikuwa na chakula cha kutosha mahitaji ya watu **wote**. Kama waamini wa wakati wa sasa wangalitoa kwa kazi ya Bwana vyote walivyo navyo ila nusu wanavyohitaji kwa mahitaji yao wenyewe kama dunia nzima ingaliweza kusikia Habari Njema kwa muda wa kizazi cha sasa.
7. **Vipande** vilivyovunjika vilijaza **vitunga kumi na viwili** na vilipita vyakula Bwana alivyoanza navyo. Mungu ni mwenye kutoa na ukarimu. Lakini ona ya kwamba hakuna kipande kilichopotezwa bure. Waliokota vyote. Kupoteza vyo vyote bure ni zambi.
8. Moja la maajabu makubwa zaidi lisingalifanyika kama wanafunzi wangalishikana na shauri lao kupumzika. Mara nyingi neno hili ni kweli ndani ya maisha yetu vilevile!

**O. Yesu anatembea juu ya bahari (6:45-52)**

**6:45-50** Anaweza kupatia watumishi wake vyakula vyao na anaweza kuwalinda kwa wakati wa hatari vilevile.

Nyuma ya kutuma wanafunzi kurudi tena kwa pwani ya mangaribi ya bahari ndani ya **chombo**, Yesu alipanda **kilimani kuomba**. Kwa wakati wa giza la usiku aliwaona wakitaabika sana kwa **kuvuta makasia,** kwa sababu **upepo** ulikuwa ukishindana nao. Alikwenda kuwasaidia, **akitembea juu ya maji.** Wakati walipomwona kwanza waliogopa sana wakifikiri ni **pepo**. Halafu alisema nao kutuliza roho zao, akaingia chombo. **Upepo ukakoma** mara moja.

**6:51-52** Kwa mwisho wa habari hizi tunasoma, **"wakashangaa sana moyoni mwao; kwa sababu hawakufahamu habari za mikate, lakini mioyo yao ilikuwa migumu."** Ni kama hata nyuma ya kuona uwezo wa Bwana ndani ya ajabu ya mikate hawakufahamu ya kwamba hakuna neno ambalo linaweza kumshinda. Haikufaa washangae kumwona akitembea juu ya maji. Ajabu hili halikuwa kubwa kupita lile ambalo waliona sasa tu. Kwa sababu walikosa imani, mioyo yao ilikuwa migumu na ufahamu wao wa maneno ya roho ulipunguka.

Kanisa limeona ndani ya ajabu hili mfano wa muda wa sasa na mwisho wake. Yesu mlimani ni mfano wa Kristo kwa utumishi wake sasa mbinguni,

akiombea watu wake. Mitume ni mfano wa watumishi wake wakitaabishwa na majaribu na taabu ya maisha ya sasa. Nyuma kidogo Mwokozi atarudi kwa watu wake, atawaponyesha toka hatari na taabu, na kuwafikisha mbinguni na salama.

### P. Mtumishi anaponyesha watu kwa Genesareti (6:53-56)

Wakati walipokwisha kurudi kwa pwani ya mangaribi ya bahari, Bwana alisongwa na **wagonjwa**. **Pahali po pote** alipokwenda, watu walifikisha kwake wale walioteswa na magonjwa, wakiwabeba juu ya mikeka. Ni kama **pahali pa soko** paligeuka hopitali. Walitaka tu kufika karibu sana naye ili waweze **kugusa hata pindo la vazi lake. Wote ambao walimgusa waliponyeshwa.**

### Q. Desturi za watu zinazoshindana na Neno la Mungu (7:1-23)

**7:1 Wafarisayo na … waandishi** walikuwa viongozi vya Wayuda kwa maneno ya dini, nao walikuwa wamesimamisha utaratibu wa mafundisho yaliyochanganywa na sheria ya Mungu, hata yalikuwa na amri karibu kipimo kimoja na amri ya Maandiko Matakatifu. Mengine ya mafundisho haya yalikana Maandiko, au kupunguza amri ya sheria ya Mungu. Viongozi vya dini walipenda kutolea watu maagizo haya, na watu waliyakubali na kunyenyekea kawaida hii ya dini iliyokosa uwezo wa Mungu.

**7:2-4** Hapa tunaona Wafarisayo na waandishi wakilaumu Yesu kwa sababu **wanafunzi** walikula **na mikono michafu.** Si kusema walikula bila kunawa mikono mbele ya kula chakula, lakini hawakuinawa na utaratibu ule ulioagizwa na mafundisho ya wazee. Kwa kuwa safi kwa maneno ya dini iliwapasa kunawa mpaka kiwiko. Nyuma ya kwenda sokoni iliwapasa kuoga kama ilivyoagizwa na amri ya dini. Kulikuwa na amri juu ya namna kusukula kopo na sufuria. Juu ya Wafarisayo E. Stanley Jones aliandika:

> Walifanya safari ndefu toka Yerusalema kukutana naye [Yesu], na kwa sababu ya roho zao za kushitaki na kulaumu, neno la pekee waliloona lilikuwa mikono isiyooshwa. Hawakutambua mabadili makubwa zaidi ya wokovu yaliyofikia dunia yetu hii tangu zamani – mabadili yaliyosafisha nia na nafsi na miili ya watu … Macho yao yaliona maneno madogo tu, lakini walikuwa kama vipofu kwa maneno makubwa. Hivi wakati wa sasa tunawakumbuka tu kama wenye kulaumu, lakini tunakumbuka Kristo kama mwenye kuleta wokovu na kuchagua wafuata.” [5]

**7:5-8** Yesu hakukawa kuonyesha unafiki wa matendo ya namna hii. Walitenda namna **Isaya** aliyokuwa ametabiri. Walikiri kuwa wenye kupenda Mungu sana na kumwabudu na bidii, lakini rohoni walikuwa wapotovu. Kwa njia ya kawaida zao za dini walitenda kama wenye kuabudu Mungu, lakini badala ya mafundisho ya Biblia walikuwa wamesimamisha mafundisho yao wenyewe. Kwa pahali pa kutambua Neno la Mungu tu kuwa na amri kwa maneno yote ya imani na matendo, waliepuka maagizo na mafundisho wazi ya Maandiko, wakifuata **desturi** za watu.

**7:9,10** Yesu alitaja mfano mmoja wa namna **mafundisho yao** yalivyofuta sheria **ya Mungu**. Moja ya Amri Kumi iliagiza watu **kuheshimu** wazazi wao (hata kwa njia ya kuwasaidia wakati wa mahitaji). Azabu kwa mtu ye yote aliyesema maneno mabaya juu ya **mama au baba** yake ilikuwa **mauti**.

**7:11-13 Lakini** Wayuda walikuwa na mafundisho yaliyotokea zamani yaliyoitwa **Korbane**, maana yake “imetolewa” au “kuwekwa.” Waza juu ya wazazi wa mtu fulani walio na mahitaji makubwa. Mwana wao alikuwa na mali

kuwasaidia, lakini hakutaka kufanya hivi. Alihitaji kusema tu "Korbane," maana yake alikuwa ameweka mali ile **kwa Mungu** au hekalu. Halafu hakuwa na daraka tena kusaidia wazazi wake. Mara nyingine alichunga mali hii kwa faida au kazi yake mwenyewe. Halikuwa neno kubwa kama mwishoni ilitolewa kwa hekalu. Mwalimu mmoja, jina lake Kelly, alisema:

> Viongozi walisimamisha desturi hii kupata mali kwa kazi ya dini, na kutuliza zamiri za watu juu ya Neno la Mungu . . . Ni Mungu aliyeagiza watu kuheshimu wazazi wao, na aliyelaumu ukosefu wa heshima hii. Lakini watu, wakijionyesha kuwa wenye kutii maneno ya dini, waliasi maagizo haya mawili yote ya Mungu! Kwa macho ya Bwana desturi hii ya kusema "Korbane" ilikosea wazazi, na vilevile iliasi agizo la Mungu.[6]

**7:14-16** Kuanza na shairi 14 Bwana alifanya tangazo la kushangaza watu sana, ya kwamba si vitu *vinavyoingia* kinywa cha mtu ambavyo vinamchafua (kama vyakula alivyokula bila kunawa mikono) lakini ni maneno yanayo*toka* ndani ya mtu (kama mafundisho ya watu yanayokataa Neno la Mungu).

**7:17-19** Hata **wanafunzi** walifazaika juu ya tangazo hili. Walikuwa wamepata nguvu na mafundisho ya Agano la Kale na walifikiri nyama ya nguruwe, sungura, vivi hivi vilikuwa si safi. Sasa Yesu alisema wazi ya kwamba mtu hachafuwi na vyakula vinavyoingia kinywani. Ni kama tangazo hili lilionyesha mwisho wa muda wa sheria.

**7:20-23** Ni kitu **kinachotoka** moyoni mwa mtu kinachofanyiza mtu mchafu: **mawazo mabaya, uasherati, wizi, uuaji, uzini, tamaa, maovu, hila, jeuri, macho mabaya, matukano, kiburi, upumbavu.** Tukikumbuka maneno yanayotangulia na kufuata mashairi haya, mafundisho na desturi za watu zinaweza kutajwa pamoja na maneno haya. Mafundisho ya Korbane ni kama uuaji. Wazazi waliweza kufa kwa njaa, kwa sababu kiapo hiki kiovu hakikuweza kuvunjwa.

Moja la maneno makubwa ambayo mashairi haya yanatufundisha ni ya kwamba inatupasa kupima mafundisho yote ya zamani na ya sasa na Neno la Mungu, tukitii yale yanayotoka kwa Mungu, na kukataa yaliyo ya watu. Mtu anaweza kuanza kutoa mafundisho mazuri yanayopatana na Neno la Mungu na kupokewa na wenye kuamini Biblia. Wakati anapokwisha kukubaliwa hivi na wasikiaji, anaanza kuongeza mafundisho yaliyo mawazo ya watu. Wafuata wake wanaowaza mafundisho yake hayawezi kuwa mabaya wanakaa kumfuata kama vipofu, hata kama mafundisho yake yakipunguza ukali wa Neno la Mungu au kulegeza maana yake.

Ni kwa njia hii waandishi na Wafarisayo walipata amri kama walimu wa Neno la Mungu. Lakini sasa walibadilisha kusudi la Neno la Mungu. Neno kubwa ambalo inatupasa kuuliza kila mara ni, "Neno la Mungu linasema nini?"

### R. Mtaifa anabarikiwa kwa sababu ya imani yake (7:24-30)

**7:24,25** Ndani ya tukio la mbele Yesu alikuwa ameonyesha ya kwamba vyakula vyote ni safi. Sasa anaonyesha ya kwamba watu wa Mataifa si wachafu au taka. Yesu alisafiri sasa kwa upande wa kaskazini-mangaribi kwa **mipaka ya Tiro na Sidona,** iliyoitwa vilevile Sirofoinike. Alijaribu kuingia **nyumba** moja bila kutambuliwa na watu, lakini sifa njema yake ilimtangulia na walifahamu mbio ya kwamba alikuwa amefika kwao. Mwanamke wa **Mataifa** alifika kwake na kumwomba kusaidia **binti** yake aliyekuwa na pepo mchafu.

**7:26** Fahamu vizuri ya kwamba

mwanamke huyu alikuwa **Myunani**, si Myuda. Wayuda, watu wachaguliwa wa Mungu, walikuwa na pahali pa mapendeleo karibu naye. Alifanya maagano ya ajabu nao, aliwapa Maandiko, na kukaa pamoja nao ndani ya hema, na nyuma ndani ya hekalu. Lakini Mataifa walikuwa walitengwa mbali na jamaa ya Israeli, na walikuwa wageni kwa maagano ya ahadi. Walikuwa bila Kristo, bila tumaini, wala Mungu duniani (Efe. 2:11,12). Bwana Yesu alifika zaidi kwa taifa la Israeli. Alijionyesha kama Mfalme kwa taifa hili. Habari Njema ilihubiriwa kwanza kwa nyumba ya Israeli. Ni lazima kwa sisi kuona neno hili ili tuweze kufahamu namna alivyotendea mwanamke huyu wa **Sirofoinike**. Ni kama alijibu na ukali wakati mwanamke **alipomwomba kutoa pepo toka binti yake.**

**7:27 Yesu alisema** ya kwamba ilipasa **watoto** (Waisraeli) **kushiba kwanza,** na ya kwamba si vizuri **kukamata chakula cha watoto na kutupia imbwa wadogo** (Mataifa). Hakukataa kufanya neno mwanamke aliloomba, lakini alisema, **"Acha watoto washibe kwanza."** Labda tunafikiri ni jibu kali, lakini kabisa kabisa lilikuwa pimo la imani ya mwanamke kuona kama alitubu na kuamini kweli. Utumishi wa Yesu kwa wakati ule ulikuwa zaidi kwa Wayuda. Mwanamke huyu, akiwa Mtaifa hakustahili kusaidiwa naye. Alikubali neno hili?

**7:28** Alikubali. Ni kama alisema, "**Ndiyo, Bwana,** mimi ni imbwa mdogo Mtaifa tu. Lakini ninaona ya kwamba hata imbwa wadogo wanakula **mavunjiko** ya mkate ambayo watoto wanaacha kuanguka **chini ya meza.** Hili tu ni neno ninaloomba – mavunjiko yanayobaki nyuma ya utumishi wako kwa Wayuda!"

**7:29,30** Haya yalikuwa masemo ya imani kubwa, na Bwana aliyatolea zawabu mara moja kwa njia ya kuponyesha msichana yule toka mbali. Wakati mwanamke aliporudi kwake alikuta **binti** yake alikuwa ameponyeshwa kabisa.

### S. Kiziwi na bubu anaponyeshwa (7:31-37)

**7:31, 32** Toka pwani ya **Bahari ya Kati** Bwana wetu alirudi kwa pwani ya mashariki ya Bahari ya Galilaya – upande wa inchi ulioitwa **Dekapoli**. Neno lililotokea pale liliandikwa ndani ya Habari Njema ya Marko tu. Rafiki **wakaleta kwake kiziwi mwenye utasi.** Labda mtu huyu hakuweza kusema wazi kwa sababu ya kilema mwilini. Au, kwa sababu hakuweza kusikia, hakuweza kuiga vizuri maneno yaliyosemwa. Mtu huyu ni mfano wa mwenye zambi, kiziwi asiyesikia sauti ya Mungu, na kwa sababu hii hawezi kusema na watu wengine juu yake.

| *WATU ELFU TANO* | *WATU ELFU INE* |
|---|---|
| 1. Watu walikuwa Wayuda (Ona Yoane 6:14, 15). | 1. Tunafikiri watu walikuwa Mataifa. (walikaa katika Dekapoli). |
| 2. Makutano walikuwa wameshinda pamoja na Yesu siku moja (6:35). | 2. Kundi hili la watu walikuwa pamoja naye siku tatu (8:2). |
| 3. Yesu alitumika na mikate mitano na samaki wawili (Mt. 14:17). | 3. Alitumika na mikate saba na samaki wadogo wachache (8:5,7). |
| 4. Wanaume elfu tano, pamoja na wanawake na watoto walikulishwa (Mt. 14:21). | 4. Wanaume elfu ine, pamoja na wanawake na watoto walikulishwa (Mt. 15:38). |
| 5. Vipande vilivyobaki vilijaza vitunga kumi na viwili (Mt.14:20). | 5. Vipande vilivyobaki vilijaza vitunga saba (8:8). |

**7:33,34** Yesu **akatenga** mtu huyu na makutano akae peke yake pamoja naye. **Aliingiza vidole ndani ya masikio yake, akatema mate, akagusa ulimi wake**, kama alama kwa mtu huyu ya kwamba atafungua masikio yake na ulimi wake. Kisha Yesu **alitazama juu mbinguni** kuonyesha ya kwamba uwezo wake ulitoka kwa Mungu. Kuugua kwake kulionyesha huzuni yake kwa sababu ya taabu zambi iliyoleta kwa watu. Mwishoni alisema, **"Efata,"** neno kwa Kiaramaic, maana yake **"Funguka."**

**7:35,36** **Mara moja** mtu huyu aliweza kusikia na kusema. Bwana aliagiza watu wasitangaze habari za ajabu hili, lakini hawakutii agizo lake. Haifai kamwe kuasi maagizo ya Bwana, hata kama tukifanya hivi na kusudi jema.

**7:37** Watu walioona maajabu Yesu aliyotenda walishangaa sana sana, wakasema, **"Ametenda mambo yote vizuri; viziwi anawafanya wasikie, na bubu waseme."** Hawakufahamu kweli ya maneno waliyosema. Kama wangaliishi nyuma ya kufa kwa Kristo msalabani kama wangalisema hivi na kushangaa hata kupita.

### T. Watu elfu ine wanakulishwa (8:1-10)

**8:1-9** Ajabu hili linafanana na lile la kulisha watu elfu tano, lakini ni mbali nalo kwa njia nyingine, ona sanduku kwa ukurasa 174.

Yesu alifanya kazi kubwa zaidi na vyakula vidogo kupita, na kulikuwa na mavunjiko mingi kupita. Ndani ya sura 7 tuliona mavunjiko yakianguka toka meza kwa mwanamke Mtaifa. Hapa kundi la Mataifa walikulishwa na kuziba. Mwalimu mmoja, jina lake Erdman aliandika hivi:

> Ni kama ajabu ya kwanza lilionyesha ya kwamba labda mavunjiko yataanguka toka meza kwa Mataifa wenye hitaji; ajabu hili la pili linatuleta kufikiri ya kwamba Yesu, akikataliwa na watu wake wenyewe, atatoa uzima wake kwa dunia, na atakuwa Mkate wa uzima kwa mataifa yote.[7]

Tusifikiri ya kwamba alama hili ya kulisha watu elfu ine halina maana kubwa kwa sisi kwa sababu linafanana sana na ajabu la kulisha watu elfu tano. Sharti tukumbuke na kuamini kabisa ya kwamba kila neno la Maandiko lina kweli ya roho kwa sisi, hata kama inatushinda kuiona kila mara kwa wakati wa sasa.

**8:10** Toka Dekapoli Yesu na **wanafunzi wake** walivuka bahari ya Galilaya kwenda upande wa mangaribi kwa pahali panapoitwa **Dalmanuta** (panaitwa Magadani kwa Mt. 15:39).

### U. Wafarisayo wanaomba alama toka mbingu (8:11-13)

**8:11** Wafarisayo walimngojea, wakitaka kwake **alama toka mbinguni.** Kiburi na upofu wao ulikuwa mkubwa sana. Mbele yao alisimama Alama kubwa zaidi – Bwana Yesu mwenyewe. Alikuwa kweli Alama aliyetoka mbinguni, lakini hawakutambua ukubwa na uzuri wake. Walikuwa wamesikia masemo mazuri zaidi na kuona maajabu yake, walikuwa wamekutana na Mmoja asiyekuwa na zambi hata moja – Mungu kwa mwili wa mtu – lakini kwa sababu ya upofu wao waliomba **alama toka mbinguni!**

**8:12,13** Hatushangai kuona Mwokozi **akiugua katika roho** yake. **Kizazi hiki** cha Wayuda kilibarikiwa kupita vyote vingine. Wafarisayo walikuwa katika kizazi hiki. Lakini katika upofu wao hawakutambua ushuhuda wazi ya kwamba Masiya alikuwa ametokea, wakaomba ajabu mbinguni, si duniani. Yesu alisema kwamba hakutakuwa na alama nyingine.Walikuwa wamekataa kuamini

alama waliyopewa – basi hawatapewa nyingine. **Akiingia chombo tena,** akakwenda kwa upande wa mashariki.

### V. Chachu ya Wafarisayo na Herode (8:14-21)

**8:14,15 Wanafunzi walisahau kuchukua mkate** pamoja nao**,** lakini Yesu alikaa kufikiri juu ya makutano yake na Wafarisayo wakati alipoonya wanafunzi wake juu ya **chachu ya Wafarisayo** na **chachu ya Herod**e. Chachu ndani ya Biblia ni, kwa kawaida, mfano wa uovu unaoenea polepole na ukimya kubadilisha kila kitu ambacho inagusa. Sehemu ya **chachu ya Wafarisayo** ilikuwa unafiki, kawaida ya dini, kujihakikisha mwenyewe, na ushupavu wa dini. Wafarisayo walijionyesha kuwa wenye kuishi maisha matakatifu, lakini roho zao zilijaa uovu na uzalimu. Labda **chachu ya Herode** ilikuwa roho ya shaka, uovu, na mapendo kwa tabia na anasa ya dunia. Waherode walijulikana kwa zambi hizi.

**8:16-21** Wanafunzi hawakufahamu masemo yake hata kidogo. Walikaa kuwaza juu ya vyakula tu. Hivi Bwana aliwauliza maneno tisa mbio mbio. Kwa njia ya maulizo 1-5 aliwahamakia juu ya kukosa kufahamu. Maulizo 6-9 yaliwahamakia juu ya kusumbukia mahitaji yao wakati yeye alipokuwa pamoja nao. Hakulisha watu **elfu tano** sasa tu na mikate **mitano,** na vipande vilivyobaki vilijaza vitunga **kumi na viwili**? Ndiyo! Alifanya hivi. Na hakulisha watu **elfu ine** na mikate **saba** na kuacha vitunga **saba** vikijaa mavunjiko? Ndiyo, alikuwa amefanya hivi. Kwa nini, basi, hawakufahamu ya kwamba aliweza kuwapa wanafunzi wachache vyote walivyohitaji? Hawakutambua ya kwamba Mwumba na Mwenye kutegemeza ulimwengu mzima alikuwa pale chomboni pamoja nao?

### W. Kipofu aliponyeshwa kwa Betesaida (8:22-26)

Habari za ajabu hili ziliandikwa ndani ya Habari Njema ya Marko tu, na linaamsha maulizo ndani ya nia zetu. Kwanza, kwa sababu gani Bwana alipeleka kipofu **inje ya mji** mbele ya kumponyesha? Kwa nini hakumponyesha kwa njia ya kumgusa tu? Kwa nini alitumika na kitu namna nyingine kama mate? Kwa nini mtu huyu aliweza kuona nusu nusu tu kwanza? (Hili ni ajabu la kuponyesha la pekee ndani ya vitabu vya Habari Njema lililofanywa sehemu sehemu, si mara moja kwa saa moja.) Mwishoni, kwa sababu gani Bwana alikataza mtu huyu kupasha habari za ajabu hili **mjini**? Bwana wetu ni mwenye enzi na halazimishwi kutuelezea sababu ya matendo yake. Kulikuwa na sababu nzuri kwa kila kitu alichofanya, hata kama inatushinda kuifahamu. Aliponyesha watu kwa njia mbalimbali, kama vilevile kila mtu anafikia Bwana kwa njia mbalimbali kupata wokovu wa roho. Watu wengine wanafahamu maneno ya roho mara moja nyuma ya kuokolewa. Wengine wanafahamu nusu nusu tu kwanza, lakini nyuma wanajua kabisa ya kwamba wameokolewa kwelikweli.

### X. Kukiri kukubwa kwa Petro (8:27-30)

Mwisho wa sura hii unatufikisha kwa mafundisho matukufu zaidi kwa wale wanafunzi kumi na wawili. Ilikuwa sharti wafahamu kabisa ndani ya roho zao wenyewe kama Yesu alikuwa nani. Kisha Bwana aliweza kuwajulisha maneno ambayo yatampata, na kuwaita kushiriki naye kwa njia ya kujitoa kwa Mungu kabisa, na kuishi maisha ya utumishi kwaye. Mashairi haya, kupita yote mengine, yanafundisha juu ya kuwa mfuata wa kweli wa Yesu. Ni moja la maneno Wakristo wasiyoweka roho juu yake ya kutosha kwa wakati wa sasa.

**8:27,28 Yesu na wanafunzi wake** walitafuta pahali pa kimya kwa upande

wa kaskazini. Walikuwa wakikwendea **Kaisaria Filipi** wakati alipoanza kusema juu ya neno hili, kwa njia ya kuuliza kama watu walisema nini juu yake. Zaidi ya watu walisema Yesu ni mtu mkubwa – kama **Yoane Mbatizaji, Elia,** au **manabii**. Lakini kabisa kabisa mawazo ya heshima ya watu ni aibu tu. Kama Yesu si Mungu, yeye ni mdanganyifu, mwenye wazimu, au hadizi tu.

**8:29,30** Halafu Bwana aliuliza wanafunzi waziwazi kama *wao* walifikiri nini juu yake. **Petro** alisema mara moja ya kwamba yeye ni **Kristo**, ndiye Masiya, maana Mpakaliwa. Petro alijua kweli hii mbele kwa akili yake, lakini alikuwa amegeuka kabisa rohoni mwake. Hakuweza kufurahi tena kamwe na maisha ya kujipendeza mwenyewe. Kristo akiwa Masiya, sharti Petro ajitoe mzima kuishi kwa yeye.

### Y. Mtumishi anatabiri habari za mauti na ufufuko wake (8:31-38)

Kufika sasa tumeona Mtumishi wa Yehova akiishi maisha ya kutumikia watu bila kuacha. Tuliona ya kwamba adui zake walimchukia, na rafiki zake hawakumfahamu vizuri. Aliishi maisha ya uwezo, maisha matakatifu kabisa, maisha ya mapendo na unyenyekevu.

**8:31** Lakini njia ya utumishi kwa Mungu inafikisha wenye kuifuata hata mateso na mauti. Hivi sasa Mwokozi aliwaambia wanafunzi wake wazi ya kwamba **itampasa** (1) **kuteswa**; (2) **kukataliwa**; (3) **kuuawa**; (4) **kufufuliwa tena**. Kwa Yeye njia ya kufikia utukufu itamlazimisha kwanza kupata taabu ya msalaba na mauti. "Roho yake ya utumishi itafunuliwa kwa njia ya kujitoa mwenyewe." (F.W. Grant)

**8:32,33** Ilishinda **Petro** kukubali ya kwamba itapasa Yesu kuteswa na kufa; hakufikiri ya kwamba maneno haya yatapata Masiya. Na hakutaka kufikiri ya kwamba Bwana wake atauawa na adui zake. Alihamakia Mwokozi juu ya kusema maneno ya namna hii. Ni kwa saa hii Yesu alisema na Petro, **"Kwenda nyuma yangu, Shetani; huwazi maneno yaliyo ya Mungu, ila yaliyo ya watu."** Yesu hakusema Petro alikuwa Shetani, au ya kwamba Shetani alikaa ndani yake. Maana ya masemo haya ilikuwa ya kwamba alisema namna Shetani alivyoweza kusema. Shetani anajaribu saa zote kupunguza hamu yetu kutii Mungu ndani ya maneno yote. Anatujaribu kufuata njia isiyo na masumbuko kutufikishia Kiti cha ufalme. Masemo ya Petro yalitoka kwa Shetani na yaliamsha hasira ya Bwana. Kelly aliandika,

> Nini iliamsha kasirani hivi ndani ya Bwana wetu? Ulikuwa mtego unaotaka kutuangusha sisi sote: hamu kujichunga wenyewe, na kuchagua njia isiyo na matata, si njia ya msalaba. Sisi sote tunataka kuepuka taabu, haya na kukataliwa na wenzetu. Tunataka kujitenga na mateso ambayo tutakayopata kwa njia ya kufanya mapenzi ya Mungu ndani ya dunia namna hii; tunataka kukaa na utulivu hapa duniani. Kwa kujumlisha: tunataka kukaa salama hapa duniani, na mbinguni vilevile. Ni nyepesi sana kutegwa na mawazo ya namna hii. Ilishinda Petro kufahamu kwa sababu gani Masiya atapata taabu hii yote. Kama sisi tungaliishi kwa wakati ule, labda tungalisema au kuwaza maneno hata mabaya kupita. Petro hakusema maneno haya kwa sababu alikosa mapendo. Sivyo, alipenda Mwokozi sana. Lakini **ndani ya roho yake** mwenyewe hakuhukumu kwanza mapendo yake kwa dunia.[8]

Ona ya kwamba Yesu **alitazama wanafunzi wake** kwanza, mbele ya **kuhamakia** Petro. Ni kama alisema, "Kama mimi sikwendei msalaba, wanafunzi wangu hawa wataokolewa namna gani?"

**8:34** Halafu Yesu alisema **nao** maneno kama haya, "Mimi nitateswa na kufa kusudi watu waweze kuokolewa. Ninyi mukitaka **kunifuata**, sharti mujinyime maneno yote ya kujipendeza wenyewe, na kuchagua njia ya laumu, mateso na mauti, **na kunifuata**. Itawapasa ninyi kuacha kukaa na raha na anasa, urafiki na watu wa dunia, hamu ya kugeuka watu wa heshima na kujulikana hapa duniani, mali, na hata uzima." Tukisoma maneno namna hii tunafazaika namna gani tunaweza kufikiri ni vizuri kwa sisi kukaa na utulivu na wingi wa mali. Namna gani tunaweza kueleza na kuhakikisha mapendo yetu kwa mali na vitu, roho yetu ya kujifikiri wenyewe na ukosefu wetu wa huruma? Masemo ya Bwana yanatuita kuishi maisha ya kujikana wenyewe, kujitoa mzima kwa yeye, maisha ya maumivu na kujitoa wenyewe.

**8:35** Ni jaribu kwetu kila mara ku**okoa uzima** wetu – kuishi bila shida, kujiwekea hazina kwa mahitaji yetu kwa wakati wa kuja, kuchagua sisi wenyewe maneno tunayotaka, tukijifikiri wenyewe ndani ya maneno haya yote. Hakika hii ni njia ya kupoteza uzima wetu. Kristo anatuita kutoa uzima wetu kwa ajili yake na Habari Njema. Anataka tujitoe mzima – roho, nafsi na mwili – kwa kazi yake takatifu, tayari hata kufa kama ikihitajiwa, ili watu wa dunia waweze kusikia Habari Njema. Hii ndiyo maana ya kupoteza uzima wetu. Ni njia ya hakika kuuokoa.

**8:36,37** Hata mwamini akipata mali yote ya dunia, itakuwa na faida gani kwaye? Angepoteza njia kutumika na uzima yake kwa utukufu wa Mungu na wokovu wa wapotevu. Damani ya uzima wetu inapita mbali mali yote ya dunia. Tuchague basi kama tutatumikia nani, au Kristo, au sisi wenyewe tu.

**8:38** Bwana wetu alifahamu ya kwamba labda wengine wa wanafunzi wake, waliokuwa vijana kwanza, watakwalishwa ndani ya njia ya kumfuata kwa sababu ya kuogopa haya. Hivi aliwakumbusha ya kwamba wale wanaojaribu kuepuka laumu kwa sababu yake watapata haya kubwa zaidi wakati atakaporudi duniani na uwezo. Ni wazo la kutushitusha kabisa! Nyuma kidogo Bwana wetu atarudi tena kwa dunia, si na aibu kama mbele, lakini na utukufu wake mwenyewe na utukufu wa Baba yake na malaika watakatifu. Litakuwa ono bora, la utukufu mkubwa. Siku ile atakuwa na haya juu ya wale walio na haya juu yake kwa wakati wa sasa. Vizuri maneno yake **"anayesikia haya juu yangu … katika kizazi hiki cha uzini na zambi"** yachokoze zamiri zetu. Kuwa na haya juu ya Mwokozi asiye na zambi, ndani ya dunia hii ya kutokuamini na zambi hakupatani hata kidogo!

## 4. SAFARI YA MTUMISHI KWENDA YERUSALEMA (Sura 9, 10)

### A. Mtumishi anageuzwa sura (9:1-13)

Bwana Yesu alikuwa amejulisha wanafunzi wake njia ya laumu, maumivu na mauti ambayo atashika, na aliwaita kumfuata kwa njia ya kuishi maisha ya kujinyima na kujitoa kwa yeye. Sasa anaendelea kuwajulisha habari za furaha kupita: Hata bei ya kumfuata ikiwa kubwa, watapokea zawabu ya utukufu kwa wakati wa kuja.

**9:1-7** Bwana alianza kwa njia ya kusema ya kwamba **wengine** wa wanafunzi **hawataonja mauti hata** watakapoona **ufalme wa Mungu umekuja kwa nguvu.** Alisema juu ya **Petro, Yakobo na Yoane**. Juu ya mlima mrefu aligeuzwa sura mbele yao na waliona **ufalme wa Mungu katika uwezo.** Mashairi haya yanatufundisha ya kwamba kutakuwa na zawabu kubwa kwa wakati

wa kuja kwa watumishi wa Kristo kwa taabu yo yote ambayo walipata kwa njia ya kumfuata saa Bwana atakaporudi pamoja na watumishi wake katika utukufu. Maneno tunayoona juu ya mlima huu ni mfano wa utawala wa Kristo kwa miaka elfu moja kwa wakati wa kuja.

1. Yesu **aligeuzwa sura** – alingaa kabisa. Hata **mavazi yake yalingaa,** meupe kupita mavazi yaliyofuliwa na sabuni ya nguvu kabisa.

   Wakati Kristo alipofika mara ya kwanza, utukufu wake ulifichwa. Alifika na aibu, mtu wa huzuni, na mwenye kujua taabu. Lakini atarudi na utukufu. Watu wote watamtambua siku ile. Itaonekana wazi ya kwamba yeye ni Mfalme wa wafalme na Bwana wa wabwana.
2. **Elia** na **Musa** walikuwa pale. Wao ni mfano wa: (a) watakatifu wa wakati wa Agano la Kale, au (b) sheria (Musa) na manabii (Elia), au (c) watakatifu waliokwisha kufa, na wale waliopelekwa mbinguni bila kufa.
3. **Petro, Yakobo na Yoane** walikuwa pale. Labda wao ni mfano wa watakatifu wa Agano Jipya, au wa wale watakaokuwa hai wakati ufalme utakaposimamishwa.
4. Mwenye kuonekana zaidi alikuwa **Yesu**. Petro alitaka kusimamisha **hema tatu,** lakini alikemewa na **wingu** na **sauti** toka mbingu. Sharti Kristo apate kuwa wa kwanza katika yote (Kol. 1:18). Yeye atakuwa utukufu wa mbingu.
5. Labda **wingu** lilikuwa wingu la utukufu lililobaki ndani ya Pahali Patakatifu pa Patakatifu katika hema na hekalu kwa wakati wa Agano la Kale. Lilionyesha ya kama Mungu alikuwa pale.
6. **Saut**i ilikuwa sauti ya Mungu Baba, akikiri ya kwamba Kristo ni **Mwana wake mpendwa.**

**9:8** Wakati wingu lilipoondoka wanafunzi **hawakuona mtu ila Yesu peke yake.** Ni mfano wa pahali pa sifa kubwa zaidi ambayo atakuwa nayo wakati ufalme utakapokuja katika utukufu. Ingempasa kuwa na pahali pa kwanza, na pa sifa zaidi; ndani ya mioyo ya wafuata wake kwa wakati wa sasa vilevile.

**9:9,10 Waliposhuka toka mlima, akawaagiza** wasimwambie mtu maneno **waliyoona, kufika** nyuma ya **ufufuko wake toka wafu**. Wanafunzi walifazaika juu ya neno hili. Labda hawakufahamu hata kwa saa ile ya kwamba atauawa na kufufuliwa tena. Maana ya **kufufuka toka wafu** ilikuwa nini? Wakiwa Wayuda walijuana na kweli ya kwamba watu wote watafufuliwa, lakini Yesu alisema juu ya ufufuko wa watu fulani tu. Atafufuliwa toka katikati ya wafu – si watu wote watafufuliwa wakati yeye atakapofufuliwa. Tunaona kweli hii ndani ya Agano Jipya tu.

**9:11** Wanafunzi walifazaika juu ya neno lingine vilevile. Walikuwa wameona sasa tu mfano wa ufalme utakaokuja. Lakini je, Malaki hakusema ya kwamba **ilipasa Elia kuja kwanza** kama mtangulizi wa Masiya, kuanza matengenezo ya maneno yote, na kutayarisha kusimamishwa kwa utawala wake juu ya watu wote (Mal. 4:5)? Basi Elia alikuwa wapi? **Atakuja kwanza, kama waandishi** walivyosema?

**9:12,13** Yesu alisema ya kwamba kweli ilipasa **Elia** kufika **kwanza**. Lakini ulizo kubwa kupita kwa wakati ule ule lilikuwa hili: Maandiko ya Agano la Kale hayakutabiri ya kwamba **Mwana wa watu** atapata mateso makubwa na kuzarauliwa? Ndiyo, **Elia alikuja** kweli (kwa njia ya Yoane Mbatizaji na kazi yake), lakini walimtendea namna walivyotaka – namna watu walivyotendea Elia. Mauti ya Yoane Mbatizaji yalikuwa mfano wa namna watakayotendea Mwana wa watu.

Wakikataa mtangulizi; watakataa Mfalme vilevile.

**B. Kijana mwenye pepo anaponyeshwa (9:14-29)**

**9:14-16** Wanafunzi hawakuwa na ruhusa kubaki juu ya mlima wa utukufu. Katika bonde upande wa chini wa mlima kulikuwa na watu waliougua na kutoa machozi kwa sababu ya maumivu na mahitaji. Wakati Yesu na wanafunzi watatu waliokuwa pamoja naye walipokwisha kushuka mlima, walikuta **waandishi,** makutano**,** na **wanafunzi** wasiokuwa mlimani wakibishana sana. Waliacha mara moja wakati Bwana alipotokea katikati yao, na makutano walipiga mbio karibu naye. Aliwauliza, "**Munabishana** nao **kwa sababu ya nini**?"

**9:17,18** Baba mmoja wa kuhangaika sana rohoni alimwambia Bwana habari za **mwana** wake, aliyetawaliwa na **pepo bubu**. Pepo alitupa mtoto chini, alimfanyiza ku**toa povu** na **kusaga meno**. Kifafa hiki kilipunguza nguvu ya mtoto sana. Baba yake alikuwa ameomba **wanafunzi** kusaidia, **lakini hawakuweza.**

**9:19** Yesu alihamakia wanafunzi kwa sababu ya kutokuamini kwao. Alikuwa amewawezesha mbele kutoa pepo wachafu. Itampasa kukaa **pamoja nao** kwa muda gani kufika wakati watakapotumika na amri hii ambayo aliwapa? **Hata wakati gani** itampasa kuvumilia ukosefu wa uwezo ndani ya maisha ya wanafunzi na kushindwa kwao?

**9:20-23** Wakati **walipoleta** mtoto kwa Bwana pepo mbaya alimfanyiza kunyonganyonga na nguvu zaidi. Bwana aliuliza baba tangu wakati gani aliteswa hivi? Baba alijibu na kusema, **Tangu utoto** wake. Mara **nyingi** kifafa ilimtupa **ndani ya moto na ndani ya maji,** na mtoto alikuwa karibu kufa. Halafu baba alisihi Bwana kumsaidia **kama** akiweza. Kilikuwa kilio cha uchungu sana cha roho ya mtu aliyekosa tumaini tangu miaka mingi. **Yesu alimjibu** ya kwamba bila shaka aliweza kuponyesha mtoto, lakini neno kubwa ndilo hili: baba yake aliweza **kuamini** neno hili? Kuna zawabu kila mara kwa wenye imani. Hakuna neno linaloweza kushinda Bwana.

**9:24** Jibu la baba lilionyesha imani na kutokuamini zikichanganyika, neno ambalo watu wa Mungu wanashindana nalo tangu zamani. Aliomba, **"Bwana, ninaamini; usaidie kutokuamini kwangu!"** Tunataka kuamini, lakini tena na tena roho zetu zinajaa na shaka vilevile. Tunachukia kusitasita hivi, na tunapigana na neno hili, lakini ni kama mara nyingi tunashindwa.

**9:25-27** **Wakati Yesu** alipoagiza **roho mchafu** kuondokea mtoto, mtoto alinyongwanyongwa na nguvu zaidi, kisha mwili wake mdogo ulilegea **kama mfu.** Mwokozi akamsimamisha na kumrudisha kwa baba yake.

**9:28,29** Nyuma, wakati Bwana wetu alipokuwa pamoja na **wanafunzi wake peke yao nyumbani,** walimwuliza kwa sababu gani wao hawakuweza kutoa pepo ile. Aliwajibu na kusema ya kwamba maajabu mengine yanahitaji **maombi na kufunga chakula.** Wengi katikati yetu tunajuana na mazuizo na kushindwa ndani ya utumishi wetu kwa Bwana. Tumeshinda na kazi na uaminifu na bila kuchoka, lakini hatuoni uwezo wa Roho ya Mungu pamoja nasi. Sisi vilevile tunasikia na kukumbushwa na masemo ya Bwana, **"Namna hii haiwezi …"** vivi hivi.

**C. Yesu anatabiri tena mauti na ufufuko wake (9:30-32)**

**9:30** Saa ya Bwana wetu kwa Kaisaria Filipi ilikwisha, naye **alipita kwa Galilaya** – safari ambayo itamfikisha kwa Yerusalema na msalaba. Alitaka kusafiri bila watu kumwona. Zaidi

ya kazi yake katikati ya watu ilikuwa imekwisha. Sasa alitaka kushinda pamoja na wanafunzi wake, akiwafundisha na kuwatayarisha kwa maneno yatakayotokea nyuma.

**9:31,32** Aliwaambia waziwazi ya kwamba atafungwa na kuuawa, na ya kwamba **atafufuka** tena **siku ya tatu.** Ni kama hawakufahamu maneno yake vizuri, na **waliogopa kumwuliza** maana yao. Mara nyingi sisi vilevile tunaogopa kuuliza, na tunakosa kubarikiwa.

**D. Ukubwa katika Ufalme (9:33-37)**

**9:33,34 Wakati** walipofikia nyumba katika **Kapernaumu** pahali watakapopanga, Yesu **aliwauliza kama walibishana juu ya nini** njiani. Ilikuwa haya kwao kukubali ya kwamba walikuwa wamebishana juu ya nani katikati yao **atakuwa mkubwa zaidi**. Labda maneno waliyoona juu ya mlima yaliamsha tena tumaini ndani ya roho zao ya kwamba ufalme ulikuwa karibu, na walikuwa wakijitayarisha kwa pahali pa heshima ndani yake. Ni huzuni kubwa kufikiri ya kwamba kwa saa ile ile Bwana alipowajulisha ya kwamba kufa kwake kulikuwa karibu, walijihesabu wenyewe kuwa wakubwa kupita wengine. Kweli moyo wa mtu ni mdanganyifu kuliko vitu vyote, una ugonjwa wa hatari, kama Yeremia alivyosema (Yer. 17:9).

**9:35-37** Yesu alijua kama walikuwa wamebishana juu ya nini, na aliendelea kuwafundisha juu ya unyenyekevu. Alisema ya kwamba njia kupata ukubwa ni kuchagua utumishi wa chini sana na kuishi kwa watu wengine, si kwa faida yetu wenyewe. Akatwaa **mtoto mdogo,** akamweka katikati yao, akamkumbatia. Alisema tena kwa nguvu ya kwamba tendo zuri la huruma **kwa jina lake** kusaidia wale wasioheshimiwa hata kidogo ndilo tendo kubwa kweli. Ni kama linatendwa kwa Bwana mwenyewe, ndiyo hata kwa Mungu Baba. "Ee Bwana Yesu, Mbarikiwa, mafundisho yako yanapima na kufunua tamaa ndani ya moyo wangu. Vunja roho yangu ili wewe uweze kuishi maisha yako ndani yangu."

**E. Mtumishi anakataza kuwa na upendeleo kwa watu kwa sababu ya dini yao (9:38-42)**

Ni kama sura hii inajaa na habari za kuanguka kwa wanafunzi. Juu ya mlima Petro alikuwa amesema maneno yasiyofaa (mash. 5,6). Wanafunzi hawakuweza kutoa pepo bubu (sh.18). Walibishana nani katikati yao aliyekuwa mkubwa zaidi (sh. 34). Ndani ya mash. 38-40 tunawaona wakikataa mtu wa dini nyingine.

**9:38** Alikuwa **Yoane**, mwanafunzi mpendwa, aliyejulisha Yesu ya kwamba walikuta mtu **akitoa pepo wachafu kwa jina lake**. Walimwagiza kuacha kufanya hivi kwa sababu hakuwa mmoja wao. Mtu huyu hakutoa mafundisho ya uwongo na hakuishi maisha ya zambi, lakini hakuungana na wanafunzi.

**9:39 Yesu alisema,** "Musimkataze. Akiwa na imani ya kutosha ndani yangu kwa kutumika na jina langu kutoa pepo wachafu, yeye ni kwa upande wangu na anashindana na Shetani. Huyu si mtu atakayegeuka nyuma kidogo na kusema **maneno mabaya juu yangu** au kuwa adui yangu."

**9:40** Labda unawaza ya kwamba shairi hili halipatani na Matayo 12:30 pahali Yesu aliposema, "Mtu asiye pamoja nami ni juu yangu; naye asiyeokota pamoja nami anasambaza." Vizuri tukumbuke ya kwamba Bwana alisema maneno haya kwa saa mbalimbali, na juu ya matukio mbalimbali. Katika Matayo watu walibishana kama Kristo alikuwa Mwana wa Mungu au alifanya kazi yake kwa uwezo wa pepo mchafu. Basi pale ni wazi ya kwamba mtu ye yote asiyekuwa pamoja na Yesu alikuwa akishindana naye.

Hapa katika Marko hakuna mabi-

shano kama Kristo ni nani, na kama kazi yake ni kazi ya Mungu, lakini kama tukifungana pamoja na nani ndani ya utumishi wetu kwa Bwana. Kwa neno hili tunahitaji roho ya kuvumuliana na mapendo. Mtu ye yote asiyeshindana na Bwana ndani ya kazi yake ni adui ya Shetani, hivi mtu huyu ni kwa upande wa Kristo.

**9:41** Hata tendo dogo sana la huruma tunalofanya kwa **jina** la Kristo litakuwa na zawabu. Bwana ataona hata **kopo ya maji** inayoletwa kwa mwanafunzi **kwa sababu** yeye ni mtu **wa Kristo**. Kutoa pepo mchafu ni tendo la kuonekana mbele ya watu. Kuleta kopo **ya maji** halionekani kuwa neno kubwa lakini maneno haya mawili yote ni ya damani machoni mwa Bwana kama yakitendwa kwa utukufu wake. **"Kwa sababu ninyi ni watu wa Kristo"** ni kamba inayopasa kufunga waamini pamoja. Tukikumbuka maneno haya, yatatusaidia kuepuka roho ya wivu na kushindana ndani ya utumishi wetu kwa Bwana.

**9:42** Ni lazima kwa mtumishi wa Bwana kukumbuka saa zote ya kwamba masemo na matendo yake yanagusa maisha ya watu wengine – yanawasaidia au kuwaangusha. Inawezekana kuangusha mwamini mwenzetu na kuumiza na kupunguza faida ya maisha yake kwa Bwana daima. Mtu akifanya hivi **ingalikuwa afazali** afungiwe **jiwe la kusagia shingoni** na kutupwa katika bahari kupita kukwalisha **mtoto** ndani ya njia ya kufuata Bwana katika utakatifu na kweli.

### F. Kujitiisha bila huruma (9:43-50)

**9:43** Mashairi ya mwisho ya sura hii yanafundisha na nguvu ya kwamba ni lazima kwa mfuata wa Kristo kujitiisha na kujinyima mwenyewe. Inapasa wale wanaotaka kufuata Bwana kweli kweli kushindana na tamaa za mwili saa zote.

Bwana alisema juu ya **mkono, mguu,** na **jicho,** na alieleza ya kwamba ingalikuwa vema kupoteza hata kimoja cha viungo hivi kupita kuangushwa nacho na kwenda katika Gehena.

**Mkono** unaweza kutufikirisha matendo yetu, **mguu** mwenendo wetu, na **jicho** vitu tunavyotamani. Vyote vinaweza kutufikisha kwa uharibifu wa milele kama tusipovihukumu na ukali.

Je, mashairi haya yanafundisha ya kwamba mwamini wa kweli anaweza kupotea kwa mwisho wa maisha yake na kushinda katika Gehena kwa milele? Tungaliweza kufikiri hivi kama tukisoma shairi hili peke yake. Lakini tukilisoma pamoja na mafundisho yote ya Agano Jipya tunafahamu ya kwamba mtu ye yote anayekwenda Gehena hakuwa Mkristo wa kweli hata kidogo. Inawezekana kwa mtu *kusema* yeye alizaliwa tena na kuendelea mbele vizuri kwa wakati. Lakini mtu huyu akidumu kutenda zambi za mwili, neno hili linaonyesha ya kwamba hakuokolewa kamwe.

**9:44-48** Bwana alisema tena na tena juu ya Gehena kama **pahali pasipokoma funza lao, wala moto hauzimiki.** Ni habari ngumu sana. Kama tungaliamini neno hili kweli kweli tusingaliishi kwa vitu vya dunia hii, lakini kwa roho za watu zisizokufa kamwe. Tungeomba, "Bwana, ninaomba uamshe ndani ya moyo wangu bidii kubwa kwa nafsi za watu, waweze kuokolewa."

Ni asante kwa sababu si lazima kamwe kukata mkono au mguu au kungoa jicho la mtu kwa sababu ya mwenendo wake mbaya. Yesu hakufikiri kwamba inapasa kutenda kwa ukali namna hii. Alisema tu ya kwamba ingekuwa *vema* kuacha kutumika na viungo hivi kabisa kupita kuingizwa katika **Gehena** kwa sababu ya kuvitumia vibaya.

**9:49** Ni nguvu sana kufahamu mashairi 49 na 50, hivi tutayaangalia karibu karibu.

**“Kwa sababu kila mtu atatiwa chumvi kwa moto.”** Masemo haya yanaamsha maulizo matatu ndani ya nia zetu: (1) Bwana alikuwa akisema juu ya **moto** wa namna gani? (2) Maana ya **kutiwa chumvi** ni nini? (3) **“kila mtu”** hapa ni waamini, au wasioamini, au watu wote?

Labda **moto** unasema juu ya Gehena (kama ndani ya mash. 44, 46, 48) au juu ya hukumu namna yo yote, hata hukumu ya Mungu juu ya kazi ya mwamini, au mwamini akijihukumu mwenyewe.

**Chumv**i ni mfano wa vitu vinavyolinda vyakula visioze, au kuvisafisha, na kuvitia utamu. Kwa inchi za mashariki watu wanatumika na chumvi kama alama kwamba watatimiza ahadi ya urafiki na uaminifu.

Kama maana ya **kila mtu** hapa ni wasioamini, maneno haya yanatufikilisha ya kwamba moto wa Gehena hautawateketeza, maana mateso ya azabu yao yataendelea kwa milele.

Kama **kila mtu** hapa inasema juu ya waamini, mashairi haya yanafundisha ya kwamba ni sharti (1) kwa kila mwamini kusafishwa kwa njia ya moto wa azabu ya Mungu kwa wakati wa maisha yake hapa duniani; au (2) kwa mwamini kujilinda kuepuka ubovu kwa njia ya kujitawala na kujinyima mwenyewe; au (3) kuhukumiwa kwa kiti cha hukumu cha Kristo.

**“Kila zabihu itatiwa chumvi.”** Maneno haya yanatoka kwa Law. 2:13 (ona vilevile Hes.18:19; 2 Sik.13:5). Chumvi ni mfano wa agano la Mungu na watu wake, na kusudi lake lilikuwa kukumbusha watu ya kwamba agano hili lilikuwa mapatano ya dini ambayo iliwapasa kuchunga kabisa. Wakati tunapotoa miili yetu kama sadaka hai kwa Mungu (Rom. 12:1,2), sharti tuitie chumvi, maana kuchunga ahadi hii bila kuivunja kamwe.

**9:50 “Chumvi ni nzuri.”** Wakristo ni chumvi ya dunia (Mt. 5:13). Mungu anataka Wakristo kuwa wenye kuongoza watu katika haki na usafi. Wakati wao wenyewe wanapotimiza maneno haya katika maisha yao wenyewe, watakuwa baraka kwa watu wote.

**“Lakini kama chumvi ikipoteza utamu wake itakolezwa na nini?“** **Chumvi** inayokosa utamu haina faida. Mkristo asiyetimiza kazi yake kama inavyofaa kwa mfuata wa kweli hazai matunda na hana faida kwa Mungu. Haitoshi ku*anza tu* vizuri kufuata Kristo nyuma ya kumwamini. Kama Mkristo asipojihukumu mwenyewe na ukali kila siku, hataweza ku*timiza* kazi ambayo Mungu alikusudi kwa yeye kufanya wakati alipomwokoa.

**“Muwe na chumvi ndani yenu.”** Wawe na uwezo kwa Mungu hapa duniani. Maisha yao yawe baraka kwa watu kwa utukufu wa Kristo. Usikubali neno lo lote linaloweza kupunguza faida yako kwa yeye.

**“Mukae na salama ninyi kwa ninyi.”** Maneno haya yanaturudisha kwa mashairi 33 na 34, pahali wanafunzi walipobishana nani katikati yao ni mkubwa zaidi. Lazima kiburi kiondoshwe na kukombolewa na utumishi wa unyenyekevu kwa watu wote.

Kwa ufupi, ni kama mashairi 49 na 50 ni mfano wa maisha ya mwamini kama sadaka kwa Mungu. Yanatiwa chumvi na moto, maana yake machanganyiko ya kujihukumu mwenyewe na kujinyima mwenyewe. Yanatiwa chumvi, maana yake sadaka hii inatolewa na ahadi ya kufuata na kutumikia Bwana na bidii yote bila kugeuka. Kama mwamini akirudi nyuma, au kama hahukumu na ukali tamaa yake ya zambi, halafu maisha yake yatakuwa hafifu, yatakosa utamu na faida. Hivi sharti ang’oe kabisa kila neno ambalo linamzuiza asitimize kazi ambayo Mungu alimpa, na vilevile inampasa kukaa na salama na waamini wengine.

**G. Ndoa na Kuachana (10:1-12)**

**10:1** Toka Galilaya Bwana alisafiri kwa upande wa kusini kwa Perea, **upande wa inchi kwa mashariki ya Yorodani**. Utumishi wake katika Perea uliendelea kufika 10:45.

**10:2** **Wafarisayo** walimfikia nyuma ya saa ndogo tu. Walikuwa kama imbwa za mwitu wakimrukia kumwua. Wakitaka kumnasa ndani ya masemo yake walimwuliza kama **kuachana kulikubaliwa na sheria**. Yesu aliwakumbusha vitabu vitano vya Musa, akawauliza, **Musa aliagiza nini?**

**10:3-9** Waliepuka kujibu ulizo lake kwa njia ya kusema ya kwamba **Musa ali***ruhusu* mume kuacha mke wake kama akimwandikia **barua ya kumwondosha na kumwacha**. Lakini neno hili halikuwa mapenzi ya Mungu kweli; lilikubaliwa tu kwa sababu ya **ugumu** wa mioyo ya watu. Tangu kuumbwa kwa watu kusudi la Mungu lilikuwa kwa mwanamume na mwanamke kufungwa pamoja katika ndoa mpaka kufa kunawagawa. Alitaka mwanamume **kuondokea** wazazi wake na kufungwa kabisa pamoja katika ndoa, na kwa yeye na mke wake kuwa **mwili mmoja. Wakiunganishwa** hivi na **Mungu,** hakuna ruhusa kwa mtu kuwatenganisha.

**10:10** Ni kama ilikuwa nguvu hata kwa **wanafunzi** wa Yesu kukubali maneno haya. Kwa wakati ule wanawake hawakuwa na heshima, na hawakulindwa wakae salama bila woga. Mwanamume aliweza kuacha mke wake kama asipopendezwa naye, na mke hakuwa na pahali pa kukimbilia kupata kusaidiwa. Mara nyingi alitendewa kama nusu ya mali ya mume wake tu.

**10:11,12** Wakati wanafunzi walipokaa kuulizana na Bwana, alisema waziwazi ya kwamba kwa mtu kuoa mara ya pili nyuma ya kuvunja ndoa ya kwanza ni **uzini.** Si neno kama alikuwa **mume** aliyeacha mke wake, au **mke** aliacha mume wake. Tukisoma shairi hili peke yake, tungefikiri kwamba kuachana kunakatazwa kabisa kabisa. Lakini ndani ya Mt. 19:9 Bwana Yesu alisema kuna ruhusa kuachana kwa sababu moja. Kama mume au mke alikuwa akitenda uzini, ni kama yule ambaye hakuzini alikuwa na ruhusa kuachana na kuoa tena. Labda 1 Kor. 7:15 linakubali kuachana kama msiyeamini akiondokea mke Mkristo.

Ni ngumu kabisa kuhukumu na haki na utaratibu maneno haya ya kuachana na kuoa tena. Afazali watu wa Mungu waepuke kuachana. Wakati watu wanaokwisha kuachana wanapoomba kupokewa ndani ya ushirika wa kanisa fulani, lazima wazee wa kanisa hili waangalie maneno yao karibu karibu, na wakiongozwa na Bwana. Maneno ya kila mtu aliyeacha mke au mume wake ni namna nyingine na yale ya watu wengine.

Mashairi haya yanaonyesha ya kwamba Bwana anaweka roho sana juu ya utakatifu wa ndoa, lakini pamoja na kufundisha kwamba wanawake wana ruhusa kujisimamia wenyewe vilevile. Dini nyingine haziheshimu wanawake kama Ukristo.

**H. Yesu anabariki watoto wadogo (10:13-16)**

**10:13** Sasa tunaona roho ya mapendo ya Bwana Yesu kwa **watoto wadogo**. Wanafunzi walijaribu kufukuza wazazi **walioleta watoto** wao ili Mwalimu Mchungaji awabariki.

**10:14-16** Bwana **hakupendezwa hata kidogo** na tendo hili la wanafunzi, na alieleza ya kwamba **ufalme wa Mungu** ni wa **watoto wadogo,** na wa watu walio na unyenyekevu na imani namna ya imani ya mtoto. Inapasa watu wazima kugeuka kama watoto wadogo kwa kuweza **kuingia** ufalme wa Mungu.

Mwalimu mmoja, ndiye George MacDonald, alisemaga ya kwamba ali-

kuwa na shaka kama mtu fulani ni Mkristo wa kweli kama asipoona watoto wakicheza karibu na nyumba yake. Inapasa mashairi haya kufundisha mtumishi wa Mungu kufahamu ya kwamba ni neno la lazima kufundisha Neno la Mungu kwa watoto. Roho na nia zao ni kwanza teketeke. W. Graham Scroggie alisema, "Ujitoe kutenda iliyo bora, na kutolea iliyo bora kwa watoto."

### I. Kijana mwenye mali nyingi (10:17-31)

**10:17** Mtu mwenye mali alisimamisha Bwana njiani na ulizo lililoonekana kuwa ulizo la haki. Aliita Yesu **"Mwalimu mwema,"** na alimwuliza kama ilimpasa **kufanya nini kuriti uzima wa milele.**

**10:18** Yesu hakukataa kuitwa **"Mwalimu mwema,"** lakini alitumika na maneno haya kupima imani ya mtu huyu. **Mungu** peke yake ni mwema. Mtajiri huyu alikuwa tayari kukiri ya kwamba Bwana Yesu ni Mungu? Labda sivyo.

**10:19,20** Halafu Mwokozi alitumika na sheria kumfahamisha ya kwamba yeye ni mwenye zambi. Ni kama mtu huyu alifikiri ataweza kuriti ufalme wa Mungu kwa njia ya *matendo* yake. Ikiwa hivi, atii sheria iliyoonyesha nini ilimpasa ku*tenda.* Bwana wetu alitaja amri tano zinazoagiza namna gani inapasa tukae pamoja na watu wengine. Tunaweza kujumlisha amri hizi hivi: "Penda jirani yako kama wewe mwenyewe." Mtu huyu alifikiri alikuwa **amezitii** tangu ujana wake.

**10:21,22** Lakini alipenda jirani yake kweli kwa kipimo alichojipenda mwenyewe? Ikiwa hivi ahakikishe neno hili kwa njia ya kuuza vitu vyake vyote na kuleta mali yenyewe kusaidia watu **masikini**. Lilikuwa agizo gumu, na mtu mwenyewe **alikwenda zake kwa huzuni, kwa sababu alikuwa na mali nyingi.**

Maana ya masemo ya Bwana Yesu haikuwa ya kwamba mtu huyu angaliweza kupata uzima wa milele kwa njia ya kuuza vitu vyake na kutoa mali yenyewe kusaidia watu masikini. Kuna njia moja tu kuokolewa, ndiyo kuamini Bwana. Lakini kwa mtu kuokolewa, lazima akiri ya kwamba yeye ni mwenye zambi asiyetimiza maagizo matakatifu yote ya Mungu. Bwana alikumbusha mtu huyu Amri Kumi kusudi aweze kufahamu yeye ni mwenye zambi. Mtu huyu hakuwa tayari kushiriki mali yake na watu wengine, na neno hili lilionyesha ya kwamba hakupenda jirani yake kwa kipimo alichojipenda mwenyewe. Ingalimpasa kusema, "Bwana, kama hili ndilo neno unalotaka, mimi ni mwenye zambi kweli. Siwezi kujiokoa kwa njia ya matendo yangu mwenyewe. Hivi ninakuomba uniokoe kwa neema yako." Lakini alipenda mali yake zaidi. Hakuwa tayari kuiacha. Hakuwa na roho ya kuvunjika.

Wakati Yesu aliposema na mtu yule kuuza vyote, hakusema ya kwamba *kwa njia hii* atapata wokovu. Alikuwa akimwonyesha ya kwamba alikuwa amevunja sheria ya Mungu, na kwa sababu hii alihitaji wokovu. Kama angalitii mafundisho ya Mwokozi, angalionyeshwa njia ya wokovu.

Lakini kuna neno gumu hapa. Inatupasa sisi tulio waamini kupenda jirani yetu kama sisi wenyewe? Yesu anasema nasi, **"Uza vitu ulivyo navyo, uwape masikini, nawe utakuwa na hazina mbinguni; na kuja, chukua msalaba na unifuate."** Inatupasa sisi sote, kila mtu kujibu ulizo hili, lakini mbele ya kufanya hivi inatupasa kuwaza juu ya maneno haya tusiyoweza kuona bure:

1. Elfu za watu wanakufa kila siku kwa sababu ya njaa.
2. Kupita 50% ya watu hawajasikia Habari Njema hata mara moja.
3. Mali yetu inaweza kusaidia sasa

kupunguza mahitaji ya roho na ya mwili ya watu.

4. Kristo anatufundisha kwa njia ya mfano wa maisha yake kugeuka masikini kusudi watu wengine wawe tajiri (2 Kor. 8:9).
5. Ufupi wa uzima na ukaribu wa kuja kwa Bwana zinatufundisha kutumika na mali yetu kwa yeye *sasa.* Haitawezekana tena nyuma ya kuja kwake.

**10:23-25** Saa mtu huyu alipokwenda zake Yesu alisema ya kwamba ni nguvu sana kwa watajiri kuingia **ufalme wa Mungu**. Wanafunzi walishangaa juu ya masemo haya; walifikiri kuwa na mali ni alama ya baraka ya Mungu. Hivi Yesu alisema tena, **"Watoto, ugumu gani kwao wanaotegemea mali kuingia katika ufalme wa Mungu. Neno jepesi kwa ngamia kupita katika tundu la sindano kuliko tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu."**

**10:26,27** Maneno haya yalifazaisha wanafunzi na waliuliza kama **nani basi anaweza kuokolewa**. Wakiwa Wayuda walioishi kwa wakati wa sheria, ilikuwa taratibu kwao kufikiri juu ya mali kama alama ya baraka ya Mungu. Ndani ya sheria ya Musa Mungu aliahidi usitawi kwa wenye kumtii. Hivi wanafunzi walifikiri kama tajiri asipoweza kuingia ufalme, hakuna mtu mwingine atakayeweza kuingia. Yesu alijibu ya kwamba neno lo lote **lisilowezekana** kwa watu **linawezekana** kwa Mungu.

Mashairi haya yanatufundisha nini?

Kwanza tunaona ya kwamba ni nguvu zaidi kwa watajiri kuokolewa (sh.23), kwani ni nyepesi kwa watu wale kupenda mali yao kupita Mungu. Wangetaka kuishi bila Mungu kupita kuishi bila mali yao. Wanatumainia mali kupita Bwana. Wakikaa kuendelea ndani ya njia hii hawataweza kuokolewa.

Ni kweli ya kwamba katika Agano la Kale mali ilikuwa alama ya upendeleo wa Mungu. Neno hili limegeuka sasa. Kwa pahali pa kuwa alama ya baraka ya Mungu mali inageuka jaribu la bidii na mapendo ya mtu kwa Mungu.

Ni nyepesi kwa ngamia kupita katika tundu la sindano kuliko tajiri kuingia lango la ufalme. Kwa mawazo yetu sisi watu, haiwezekani kwa tajiri kuokolewa. Labda mtu mwingine angependa kusema ya kwamba kwa mawazo ya watu haiwezekani kwa *mtu ye yote* kuokolewa. Ni kweli. Lakini ni nguvu kupita kwa mtu aliye tajiri. Mtu masikini hajuani na vizuizo ambavyo tajiri anashindana navyo. Ni lazima mungu wa mali uondoshwe moyoni mwa tajiri (Luka 16:13), na asimame kama mtu masikini mbele ya Mungu. Neno hili haliwezekani kwa mtu. Mungu tu anaweza kugeuza mtu hivi.

Wakristo wengi wanaojivimbishia mali duniani wanalipa kwa uasi wao mara nyingi kwa njia ya maisha ya watoto wao. Watoto wachache tu wa jamaa namna hii wanaendelea vizuri na kufuata Bwana na bidii.

**10:28-30** **Petro** alitambua neno kubwa la mafundisho ya Mwokozi. Alifahamu kwamba Yesu alikuwa akisema, "Acha vyote na unifuate." Yesu aliyakinisha neno lenyewe kwa njia ya kuahidi kuwapa zawabu watu wote wanaoacha vyote kwa ajili yake na ya Habari Njema.

1. Kwa wakati wa sasa mtu namna hii atapata zawabu ya 10,000%, si mali lakini
   a. **nyumba** – makao ya watu wengine ambao wanampokea nyumbani mwao kwa sababu yeye ni mtumishi wa Bwana.
   b. **ndugu waume na ndugu wanawake, na mama, na watoto** – ndio rafiki Wakristo wanaosaidia roho yake sana.
   c. **mashamba –** inchi alizopata kwa Mfalme kwa njia ya kuhubiri

Habari Njema kwa watu wa inchi hizi.

d. **mateso** – ndiyo sehemu ya zawabu ya wakati wa sasa vilevile. Ni furaha kwa Mkristo kuhesabiwa kustahili kuteswa kwa ajili ya Yesu.

2. Zawabu kwa wakati wa kuja ni **uzima wa milele**. Si kusema tunajipatia uzima wa milele kwa njia ya kuacha vyote kwa Bwana. Uzima wa milele ni zawadi. Lakini wale wanaoacha vyote kwa ajili ya Kristo wataweza kufurahia kupita uzima wa milele mbinguni. Waamini wote watakuwa na uzima ule, lakini si wote watafurahishwa nao kwa kipimo sawasawa.

**10:31** Halafu Bwana aliongeza maonyo: **"Wengi walio wa kwanza watakuwa wa mwisho; nao walio wa mwisho watakuwa wa kwanza."** Haitoshi ku*anza* tu vizuri kufuata Bwana. Neno kubwa ndilo kumfuata vizuri hata mwisho. Mwalimu mmoja, jina lake Ironside, alisema:

> Si kila mtu ambaye anaanza kama mfuata mwaminifu na mwenye bidii atakayeendelea ndani ya maisha ya kujikana mwenyewe kwa ajili ya jina la Kristo, na wengine walioonekana kama wenye mapendo machache tu kwa Bwana watakuwa wale wanaojitoa kabisa na kusimama imara kwa yeye kwa wakati wa mateso.[9]

## J. Mtumishi anatabiri maumivu na mauti yake mara ya tatu (10:32-34)

**10:32** Saa ilikuwa imefika sasa kwa Bwana Yesu **kwendea Yerusalema.** Huzuni na mateso ya Getesemane, haya na maumivu ya msalaba yalikuwa mbele yake.

Alisikia nini rohoni mwake kwa wakati ule? Tunasoma **"Yesu aliwatangulia."** Alikusudi kabisa kufanya mapenzi ya Mungu, hata kama alijua kufanya hivi kutakuwa gumu sana. Bila shaka alisikia upekee – alitembea peke yake mbele ya wanafunzi. Na alisikia furaha – furaha kubwa akijua alikuwa akifanya mapenzi ya Baba yake, furaha wakati alipotazamia utukufu wa wakati wa kuja, furaha ya kukomboa na kujipatia bibi arusi. Kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake alivumilia msalaba na kuzarau haya yake (Ebr.12:2).

Na wakati sisi tunaotembea nyuma yake tunapomtazama, **tunashangaa** vilevile juu ya Mwongozi wetu asiyeona hofu, mwenye kuanzisha na mwenye kutimiliza imani yetu, Bwana wetu mtukufu, Mwana wa Mungu. Erdman aliandika:

> Tusimame kwa muda mfupi na kutazama uso na mwili huu, Mwana wa Mungu, akikwendea msalaba bila kusita. Neno hili haliongezi uhodari wetu wakati tunapomfuata, na kuamsha mapendo mapya wakati tunapoona ya kwamba alikufa kwa ajili yetu kwa kutaka kwake mwenyewe? Na tunashangaa na kustaajabu juu ya maana na siri ya mauti hii.[10]

Wale waliokuwa wakimfuata **waliogopa**. Walijua ya kwamba viongozi vya dini katika Yerusalema walitaka sana kumwua.

**10:33,34** Yesu alijulisha wanafunzi wake mara ya tatu maneno moja moja yote yatakayotokea. Mashairi haya yanaonyesha wazi ya kwamba hakuwa mtu tu:

1. **"Angalieni, tunapanda kwenda Yerusalema"** (11:1 – 13:37).
2. **"Mwana wa watu atatiwa katika mikono ya wakubwa wa makuhani na waandishi"** (14:1,2, 43-53).
3. **"Watamhukumu afe"** (14:55-65).
4. **"Watamtia katika mikono ya Mataifa"** (15:1).
5. **"Watamzihaki na kumtemea mate, na kumpiga fimbo, na kumwua"** (15:2-38).
6. **"Na nyuma ya siku tatu atafufuka"** (16:1-11).

**K. Ukubwa wa kweli ni kutumikia (10:35-45)**

**10:35-37** Nyuma ya unabii huu mchungu ya kwamba kusulibishwa kwa Yesu kulikuwa karibu, **Yakobo na Yoane** walikuja kumwomba neno lililokuwa neno jema, lakini lisilofaa kuomba kwa wakati ule. Walitaka kuwa karibu na Kristo, lakini haikuwa saa kujitafutia wenyewe pahali pa heshima. Neno waliloomba lilionyesha ya kwamba waliamini Yesu atasimamisha ufalme wake, lakini kwa wakati huu ingaliwapasa kuwaza juu ya maumivu ya msalaba ambayo yalimkaribia.

**10:38, 39 Yesu** aliuliza kama wataweza **kunywa kikombe** chake, maana mateso yake, na kushiriki ndani ya **ubatizo** wake, ndio mauti yake. Walisema **wangeweza,** naye alisema walisema kweli. Watateswa kwa sababu walimfuata na uaminifu, na mmoja wao, ndiye Yakobo, atauawa kwa sababu ya imani yake (Mdo. 12:2).

**10:40** Lakini aliendelea kueleza ya kwamba watu hawatapewa pahali pa heshima bila ku*stahil*i kupapokea. Tukumbuke ya kwamba tuna*ingia* katika ufalme kwa neema kwa njia ya imani, lakini wale tu wanaofuata Kristo na uaminifu watapewa *pahali pa heshima.*

**10:41-44** Wale wanafunzi **kumi** wengine **walikasirika** wakati walipoona **Yakobo na Yoane** wakijaribu kujipatia heshima kupita ndugu zao. Lakini hasira yao ilionyesha ya kwamba wao walikuwa na roho ya kujitafutia ukubwa vilevile. Neno hili lilimpa Bwana njia nzuri sana kutoa mafundisho mapya juu ya ukubwa. Katikati ya wasioamini, watu wakubwa ndio wale wanaojaribu kuonyesha ukubwa wao kwa njia ya kutawala watu wengine kwa nguvu na jeuri. Lakini alama ya ukubwa katika ufalme wa Kristo ni utumishi. Inapasa **mtu anayetaka kuwa wa kwanza** kuwa **mtumwa** wa wote.

**10:45** Mfano bora wa mafundisho haya ni Mwana wa watu mwenyewe. **Hakuja kutumikiwa ila kutumika na kutoa uzima wake uwe ukombozi wa wengi.** Waza juu ya maneno haya makubwa: *Alizaliwa* kwa njia ya ajabu. *Alitumikia* wengine kwa miaka yote ya maisha yake. Na *alitoa* uzima wake kwa njia ya mauti kwa ajili ya watu.

Kama tulivyosema mbele, shairi 45 ni shairi kubwa zaidi ya kitabu hiki kizima cha Marko. Ndani yake tunaona kwa ufupi habari za maisha ya Yule aliyekuwa mkubwa kupita wote walioishi duniani tangu zamani.

**L. Kuponyeshwa kwa Baratimayo, ndiye kipofu (10:46-52)**

**10:46** Sasa Bwana pamoja na wanafunzi wake waliondokea Perea na walikwenda kwa Yudea. Walivuka Yorodani na kufikia **Yeriko.** Pale alikutana na **kipofu** mmoja, jina lake **Baratimayo**, mtu aliyekuwa na hitaji kubwa. Alifahamu nini alilotaka, na aliweka roho sana juu ya kujipata kusaidiwa.

**10:47** Baratimayo alitambua kama Bwana wetu ni nani, na alimwita **Mwana wa Daudi**. Ndiyo, taifa la Israeli walikuwa kama wapofu na hawakufahamu ya kwamba Masiya alikuwa katikati yao, lakini Myuda huyu, kipofu kwa mwili, alimtambua kwa roho!

**10:48-52** Baratimayo alikaa kupaza sauti kuomba kupata **rehema,** na alipata jibu. Aliomba Bwana aweze kupata kuona, na Bwana alimpa kitu alichoomba. Alionyesha asante yake kwa Bwana kwa njia ya kufuata **Yesu** kwa safari yake ya mwisho kwenda Yerusalema. Bila shaka ilikuwa furaha kwa Bwana kukuta mwenye imani namna hii katika Yeriko wakati alipokuwa akikwendea msalaba. Ni asante Baratimayo alifikia Bwana siku ile ile, kwani Mwokozi hakupita tena kamwe kwa njia ile.

## 5. KAZI YA MTUMISHI KATIKA YERUSALEMA (Sura 11, 12)

### A. Mtumishi anaingia Yerusalema kama Mfalme (11:1-11)

**11:1-3** Sasa tunaanza kusoma juu ya maneno yaliyotokea katika muda wa juma la mwisho. Yesu alisimama kidogo kwa mtelemuko wa mashariki wa **mlima wa Mizeituni**, karibu na **Betefage** (maana ya jina hili ni 'nyumba ya tini zisizokomea') na **Betania** (nyumba ya wamasikini, wanyenyekevu, wanaoteswa).

Saa ilikuwa imefika kwa yeye kujionyesha wazi kwa Wayuda kama Masiya na Mfalme wao. Atafanya hivi kwa kutimiza unabii wa Zekaria (9:9), akitembea juu ya **mwana-punda**. Hivi alituma **wawili wa wanafunzi wake** toka Betania kwenda Betefage. Akijua yote na akiwa mwenye amri yote, aliwaagiza kuleta **mwana-punda** asiyebeba mtu mbele, na aliyefungwa pale. Kama mtu akiwauliza kwa sababu gani walikamata mwana-punda, wamjibu na kusema **"Bwana anamhitaji.**" Habari hizi zilionyesha wazi ya kwamba Bwana anajua maneno yote.

**11:4-6** Maneno yote yalitokea namna Yesu alivyosema mbele. **Walikuta mwana-punda** aliyefungwa inje, katika njia. Wakati watu walipouliza kama walikwenda na mwana-punda kwa ruhusa ya nani, wanafunzi walijibu namna Yesu alivyowaagiza. Halafu watu **waliwaruhusu** kwenda naye.

**11:7,8** Hata kama mtu hakutembea juu yake mbele, mwana-punda huyu alibeba Mwumba wake bila kuleta matata na alimfikisha hata Yerusalema. Bwana alitembea juu ya **nguo** na **matawi** ya ngazi na kusikia sifa ya watu. Kwa muda huu mdogo basi walikiri kwamba yeye ni Mfalme.

**11:9,10** Watu walipiga sauti:

1. **"Hosana"** – zamani maana ya neno hili ilikuwa "Tunakuomba, utuponyeshe," lakini nyuma liligeuka kilio cha sifa. Labda watu walikuwa wakiomba "Utuponyeshe toka Waroma ambao wanatutesa!"
2. **"Yeye abarikiwe anayekuja kwa jina la BWANA"** – walikuwa wamefahamu ya kwamba Yesu ndiye Masiya ambaye Mungu aliahidi kutuma (Zaburi 118:26).
3. **"Ubarikiwe ufalme wa baba yetu Daudi unaokuja kwa jina la Bwana!"** – walifikiri ya kwamba kusimamishwa kwa **ufalme** kulikuwa karibu, na Kristo akiketi juu ya kiti cha ufalme cha **Daudi**.
4. **"Hosana juu mbinguni!"** – mwito *kusifu* Bwana katika **mbingu juu**, au kwa yeye *kuokoa* toka **juu mbinguni.**

**11:11** Wakati Yesu alipofikia **Yerusalema** aliingia **hekalu** – si ndani ya pahali patakatifu, lakini kiwanja tu. Liliitwa nyumba ya Mungu, lakini makuhani na watu walikataa kumpokea kama ilivyofaa. Hivi, **nyuma ya kuangalia pande zote** kwa saa ndogo alikwenda **Betania pamoja na wanafunzi wake kumi na wawili**. Ilikuwa mangaribi siku ya kwanza ya juma.

### B. Mtini bila matunda (11:12-14)

Habari hizi ni kama maelezo ya Bwana ya namna watu walivyompokea sasa tu na shangwe kubwa katika Yerusalema. Kwa macho yake taifa la Israeli lilikuwa kama **mtini** usio na matunda – ulikuwa na majani, ndio mfano wa kukiri kuwa na imani, lakini hakuna matunda. Walilalamika Hosana, lakini kilio hiki litageuka nyuma ya saa nusu tu kuwa kilio kikali sana: "Mumsulibishe!"

Watu wengine wanafazaika kwa sababu Bwana alihukumu mtini kwa sababu ulikosa matunda, hata kama tuli-

soma ya kwamba **"si wakati wa tini."** Ni kama Bwana alikuwa mwenye kukasirika mbio bila kufikiri vizuri. Neno hili si kweli. Halafu tutaweza kueleza habari hizi namna gani?

Mitini katika inchi za mashariki ilizaa matunda yanayoweza kuliwa hata mbele ya kuonekana kwa majani. Tini hizi zilikuwa kama ahadi ya kwamba kutakuwa na mavuno ya kweli nyuma, ndio kwa **wakati wa tini**. Kama matunda ya mbele yakikosa, hakutakuwa na mavuno ya tini nyuma. Wakati Yesu alipofikia taifa la Israeli, kulikuwa na majani, maana yake watu walikiri kufuata Mungu, lakini hawakuzaa matunda ya kweli kwa Mungu. Yesu alitaka sana kupata matunda ya kweli toka taifa la Israeli. Kwa sababu hawakuzaa matunda mbele, alijua watu hawa wasioamini hawatazaa matunda nyuma vilevile, hivi alilaani mtini. Ulikuwa kama mfano wa hukumu itakayopata Israeli nyuma, kwa mwaka 70 A.D.

Lakini tukio hili *halifundishi* ya kwamba taifa la Israeli lililaaniwa kukaa daima bila kuzaa matunda. Wayuda wamewekwa kando *kwa wakati tu,* lakini saa Kristo atakaporudi kutawala, taifa hili litafufuka na kukubaliwa na Mungu tena.

Ndani ya ajabu hili moja Kristo alilaani kwa pahali pa kubariki, akiharibu uzima kwa pahali pa kulirudisha. Neno hili linafazaisha watu, lakini kufazaika kwao ni bure. Mwumba, akiwa Mungu, ana ruhusa kuharibu kitu kisicho na uzima kwa kutoa mafundisho makubwa yanayookoa watu toka mauti ya milele.

Elezo la mashairi haya ni kwanza kwa taifa la Israeli, lakini lina mafundisho kwa watu wa kila taifa na wa kila wakati, wanaokiri Mungu na masemo tu, bila kutii maagizo yake na unyenyekevu.

### C. Mtumishi anasafisha hekalu (11:15-19)

**11:15,16** Kwa mwanzo wa utumishi wake katikati ya watu Yesu alifukuza **wenye kufanya biashara** toka hekalu (Yoane 2:13-22). Sasa, karibu na mwisho wa utumishi wake, aliingia kiwanja cha **hekalu** tena na kufukuza watu ambao walijipatia wenyewe faida kwa njia ya kazi waliyofanya katika pahali pale patakatifu. Wala hakuruhusu watu wachukue **vyombo kwa uwanja wa hekalu.**

**11:17** Akitaja maneno yaliyoandikwa ndani ya unabii wa Isaya (56:7) na Yeremia (Yer. 7:11), alisema na ukali juu ya kuchafuwa kwa hekalu, na alihukumu wenye kuleta ruhusa kwa watu wa kufanya biashara, na wanyanganyi. Lilikuwa kusudi la Mungu kufanyiza hekalu kuwa **nyumba ya maombi kwa mataifa yote,** si kwa Israeli tu (Isa. 56:7). Lakini watu walikuwa wameligeuza kuwa pango la wanyanganyi, na watu walioogofya wengine, ili kupata mali kwao (Yer. 7:11).

**11:18** Mashitaki yake yaliumiza roho za **waandishi na Wafarisayo** sana. Walitaka **kumwua,** lakini hawakuweza kufanya hivi wazi mbele ya watu, kwa sababu watu walikaa kumheshimu sana.

**11:19** Wakati **usiku ulipokuja alitoka mjini**. Ni kama hii ilikuwa desturi yake, labda kwa sababu ya kuepuka hatari. Hakuwa na woga kwa ajili yake mwenyewe. Tukumbuke ya kwamba sehemu ya kazi yake ilikuwa kulinda kondoo, maana wanafunzi wake wenyewe (Yoane 17:6-19). Na vilevile haikuwezekana kwa yeye kujitoa kwa adui zake mbele ya saa iliyochaguliwa.

### D. Mafundisho ya mtini usiozaa matunda (11:20-26)

**11:20-23** **Asubui**, nyuma ya siku ya kulaani mtini, mitume walipita pahali penyewe wakati walipokwenda Yerusalema. Mtini ulikuwa **umekauka,** ku-

anza na mashina yake. Wakati **Petro** alipoonyesha neno hili na Yesu, Bwana alisema tu, **“Mwamini Mungu.”** Maana ya maneno haya ni nini hapa? Mashairi yanayofuata yanaonyesha ya kwamba Yesu alisukuma wanafunzi kuwa na imani kuondosha mambo magumu. Wanafunzi **wakiamini Mungu,** wataweza kushindana na ukosefu wa matunda na kuondosha vizuizo vinavyoonekana kama milima.

Lakini mashairi haya hayampi mtu amri kuomba kupewa uwezo kufanya maajabu kwa faida au heshima yake mwenyewe. Lazima kila tendo la imani lisimame juu ya ahadi ya Mungu. Tukijua ya kwamba ni mapenzi ya Mungu kuondosha neno gumu fulani, tunaweza kuomba na tumaini ya kwamba neno hili litafanyikana. Ndiyo, tunaweza kuomba na imani juu ya neno lo lote, kama ni neno linalopatana na mapenzi ya Mungu yanayofunuliwa ndani ya Biblia, au na ushuhuda wa Roho Mtakatifu ndani ya roho zetu.

**11:24** Wakati tunapoishi kweli karibu na Bwana na kuomba katika Roho, tunaweza kujua kabisa kwamba Mungu amejibu maombi haya hata mbele ya kuonekana kwa jibu lenyewe.

**11:25,26** Lakini kama tukitaka Mungu kujibu maombi yetu, ni **lazima** kwetu kuwa na roho ya usamehe. Tukiwa na roho ngumu na kali kwa ndugu zetu, tusifikiri Mungu atasikia na kutujibu sisi. Sharti **tusamehe** ndugu zetu kama tukitaka kusamehewa sisi wenyewe. Mashairi haya si juu ya usamehe wa zambi zetu wakati tunapookolewa; saa ile tulisamehewa kwa sababu ya neema ya Mungu kwa njia ya imani. Lakini mafundisho haya ni juu ya Mungu Baba akifundisha watoto wake. Roho ya kutokusamehe ya mwamini inaharibu upatano wake na **Baba mbinguni,** na kuzuiza baraka.

### E. Maulizo juu ya amri ya Mtumishi (11:27-33)

**11:27,28** Wakati Bwana Yesu alipofikia **hekalu**, mara moja viongozi vya dini walifika na kushindana na amri yake kwa njia ya kumwuliza maneno mawili: (1) **“Kwa mamlaka gani unatenda maneno haya?”** na (2) **“Naye ni nani ambaye alikupa wewe mamlaka hii ufanye maneno haya?”** (ndiyo kusafisha hekalu, kulaani mtini, na kuingia Yerusalema kama mshindaji). Walitaka kumnasa, si neno kama alijibu nini. Kama akisema alikuwa na mamlaka kwa sababu alikuwa Mwana wa Mungu, wangalimshitaki na ukufuru. Kama akisema alipewa mamlaka hii na watu, kama wasingalimsadiki. Kama akisema Mungu alimpa mamlaka, wangalishindana na neno hili kwa sababu waliamini wao wenyewe waliwekwa na Mungu kuwa viongozi vya watu kwa maneno ya dini.

**11:29-32** **Lakini Yesu** aliwajibu kwa njia ya ulizo: Yoane Mbatizaji alitumwa na Mungu au sivyo? (**Ubatizo wa Yoane** unasema juu ya utumishi wake mzima.) Hawakuweza kujibu bila kuhangaika na kupata haya. Kama utumishi wa Yoane ulitoka kwa Mungu, kama ingaliwapasa kutii wakati alipowaita kutubu. Kama wangaliona utumishi wa Yoane bure, kama wangalikasirisha watu walioamini **Yoane** alikuwa akisema kwa ajili ya Mungu.

**11:33** Wakati walipokataa kujibu kwa sababu hawakujua jibu lenyewe, Bwana alikataa kusemezana nao juu ya mamlaka yake. Wakikataa amri ya mtangulizi, wasingekubali amri kubwa kupita ya Mfalme mwenyewe!

### F. Mfano wa walimaji waovu wa mizabibu (12:1-12)

**12:1** Maneno ya Bwana Yesu na viongozi vya Wayuda hayakwisha bado hata kama alikataa kujibu ulizo lao. Sasa

aliwatolea mashitaki makali kabisa kwa njia ya **mifano,** kwa sababu walikataa Mwana wa Mungu. **Mtu aliyepanda shamba la mizabibu** alikuwa Mungu mwenyewe. **Shamba la mizabibu** lilikuwa pahali pa mapendeleo pa taifa la Israeli kwa wakati ule. **Ugo**, ndio boma la miti, lilikuwa Sheria ya Musa iliyotenga Israeli na Mataifa, na kuwalinda kama taifa la heshima kwa Mungu. **Walimaji wa mizabibu** walikuwa viongozi vyao kwa maneno ya dini, ndio Wafarisayo, waandishi na wazee.

**12:2-5** Mungu alituma watumishi wake tena na tena, ndio manabii, kwa watu wa Israeli, akitafuta ushirika, utakatifu na mapendo kwao. Lakini watu walitesa manabii na **kuua** wengine.

**12:6-8** Mwishoni Mungu alituma **Mwana** wake mpendwa. Bila shaka **watamheshimu** Yeye. Sivyo. Walifanya shauri la siri, na mwishoni **walimwua**. Kwa njia hii Bwana alitabiri habari za kufa kwake mwenyewe na kuonyesha wauaji wazi.

**12:9** Mungu **atafanya nini** na watu waovu namna hii? **Atawaharibu** na kuwapa watu **wengine** pahali pao pa heshima, labda Mataifa, au kwa baki la Israeli watakaotubu kwa wakati wa mwisho.

**12:10,11** Maneno haya yote yalitimiza maandiko matakatifu ya Agano la Kale. Kwa mfano, ndani ya Zaburi 118:22,23 kuna unabii ya kwamba Masiya **atakataliwa** na viongozi vya Wayuda. Hawakuwa na nafasi kwa **Jiwe** hili ndani ya ramani ya nyumba yao. Lakini nyuma ya mauti yake atafufuliwa toka wafu, na Mungu atampa pahali pa sifa zaidi. Atakuwa **jiwe la kichwa cha pembe** ndani ya jengo la Mungu.

**12:12** Viongozi vya Wayuda walifahamu maana ya masemo yake. Waliamini ya kwamba Zaburi 118 ilisema juu ya Masiya. Sasa wamesikia Bwana Yesu akisema zaburi hii ilikuwa juu yake mwenyewe. **Walitaka kumkamata,** lakini saa yake ilikuwa haijafika bado. **Makutano ya watu** wangalisimamia Yesu. Basi viongozi vya dini **walimwacha** kwanza, wakakwenda zao.

### G. Kumpa Kaisari na kumpa Mungu (12:13-17)

Ndani ya sura 12 Wafarisayo, Waherode, na Wasadukayo walishindana wote na Bwana. Ni sura inayojaa na maulizo. Ona mashairi 9, 10, 14, 15, 16, 23, 24, 26, 28, 35, 37.

**12:13,14 Wafarisayo na Waherode** walikuwa adui wakali, lakini wao wote walichukia Mwokozi na neno hili liliwapatanisha sasa kuwa rafiki. Walijaribu sana kumfanyiza kusema neno ambalo litawapa njia kumshitaki. Hivi walimwuliza kama ni **halali kulipa kodi** kwa serikali ya Waroma.

Wayuda *hawakufurahi* kutawaliwa na Mataifa. Wafarisayo walichukia neno hili hata kupita Waherode. Kama Yesu akisema wazi kwamba inapasa watu kulipa kodi kwa **Kaisari**, wengi wa Wayuda watageuka adui zake. Kama akijibu: Sivyo, kama wangalimfikisha mbele ya serikali ya Waroma mara moja afungwe na kuhukumiwa kama mdanganyi.

**12:15,16** Yesu aliomba mtu **amletee feza ya kodi,** ndiyo dinari. (Ni kama hakuwa nayo yeye mwenyewe.) Feza ile ilikuwa na mfano wa Tiberio Kaisari juu yake, ndio ukumbusho kwa Wayuda ya kwamba taifa lao lilishindwa na kutiishwa na Waroma. Kwa nini walikuwa katika hali hii? Kwa sababu ya kutokuamini na zambi zao. Ingaliwapasa kunyenyekezwa rohoni kwa sababu iliwapasa kutumika na feza iliyokuwa na mfano wa mtawala Mtaifa juu yake.

**12:17** Halafu Yesu alisema, **"Mumpe Kaisari yaliyo ya Kaisari, na yaliyo ya Mungu, mumpe Mungu."**

Walikuwa wamelipa kodi kwa Kaisari kweli, lakini hawakukumbuka ya kwamba ilikuwa sharti kwao kunyenyekea utawala wa Mungu katika maisha yao. Feza ilikuwa na mfano wa Kaisari juu yake, hivi ilikuwa mali ya Kaisari. Mtu ana sura ya Mungu juu yake – Mungu alimwumba kwa sura yake mwenyewe (Mwa. 1:26,27), hivi mtu ni mali ya Mungu.

Waamini wanaagizwa kutii na kusimamia serikali ya inchi pahali walipo. Wanakatazwa kusema maneno mabaya juu ya watawala au kujaribu kuangamiza serikali. Inawapasa kulipa kodi na kuombea watawala wao. Kama mwamini akiagizwa kufanya neno lisilopatana na utawala wa Kristo juu ya maisha yake, inampasa kuasi serikali na kuvumilia azabu. Sharti Mkristo awe na ushuhuda mzuri mbele ya watu wa dunia kwa njia ya kutii maneno haya.

### H. Wasadukayo na fumbo lao juu ya ufufuko (12:18-27)

**12:18** **Wasadukayo walizihaki** mafundisho ya kwamba **miili ya watu watafufuliwa** siku nyingine. Hivi walifikia Bwana na habari zisizosadikika, kwa kujaribu kuzarau mawazo haya.

**12:19** Walikumbusha Yesu ya kwamba kulikuwa na agizo ndani ya sheria ya **Musa** lililokumbuka wajane katika Israeli, kusudi jina la jamaa yao lisipotee. Mtu akikufa na kuacha mke bila kuzaa mtoto, ilipasa **ndugu yake** mume kuoa mjane (Tor. 25:5-10).

**12:20-23** Halafu walipasha habari hizi za kuchekesha za mwanamke aliyeolewa na **ndugu wanaume saba**, mmoja nyuma ya mwingine. **Mwishoni** mwanamke mwenyewe **alikufa.** Hili ndilo ulizo lao: "Katika ufufuko **atakuwa mke wa nani?"**

**12:24** Walifikiri walikuwa wenye akili; Mwokozi aliwaambia ya kwamba walikuwa wajinga kabisa kwa sababu hawakujua **maandiko** yenye mafundisho juu ya ufufuko, wala **uwezo wa Mungu** unaofufua wafu.

**12:25** Ingaliwapasa kujua ya kwamba hakuna ndoa tena mbinguni. Waamini watatambulana na watakuwa wanaume na wanawake lakini hawataoa wala kuolewa. Kwa maneno haya wao ni kama **malaika walio mbinguni.**

**12:26,27** Wasadukayo waliheshimu vitabu vya Musa kupita vitabu vingine vya Agano la Kale, hivi Bwana wetu aliwakumbusha **habari za Musa kwa kijiti kisichoteketea** (Kut.3:6). Pale Mungu alisema juu yake mwenyewe akijiita **Mungu wa Abrahamu, Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo.** Mwokozi alisema juu ya maneno haya kuonyesha ya kwamba **Mungu ni Mungu wa wenye uhai, si wa wafu**.

Basi ile inawezekana namna gani? Abrahamu, Isaka na Yakobo hawakufa mbele ya wakati Mungu alipoonekana na Musa? Ndiyo, walikuwa wafu na maiti zao zilikuwa katika Pango la Makipela kwa Heburoni. Halafu namna gani Mungu ni Mungu wa wenye uhai?

Maneno haya yanaweza kuelezwa hivi:

1. Mungu alitolea Abrahamu, Isaka na Yakobo ahadi juu ya inchi na juu ya Masiya.
2. Ahadi hizi hazikutimizwa mbele ya kufa kwao.
3. Wakati Mungu aliposema na Musa kwa kijiti kilichowaka kwa moto, maiti zao zilikuwa ndani ya kaburi.
4. Hata hivi Mungu alijiita Mungu wa wenye uhai.
5. Ni lazima kwa yeye kutimiza ahadi zake kwa Abrahamu, Isaka na Yakobo.
6. Hivi ufufuko ni neno la lazima kabisa kwa sababu ya maneno yote tunayojua juu ya tabia ya Mungu.

Hivi Bwana aliagana na Wasadukayo na masemo haya: **"Mumepotea sana."**

**I. Amri kubwa (12:28-34)**

**12:28 Mmoja wa waandishi,** akishangaa juu ya namna Bwana wetu alivyojibu wale walioshindana naye, **aliuliza** Yesu **amri gani** ndiyo ya kwanza kuliko zote. Aliuliza na roho nzuri, juu ya neno lililo msingi wa maneno yote. Alitaka kujua nini ndilo kusudi kubwa zaidi la maisha ya watu.

**12:29** Yesu alianza jibu lake kwa njia ya kutaja maneno toka Shema lililokuwa kama taarifa ya imani ya Wayuda toka kitabu cha Torati 6:4. **"Usikie, Israeli, Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja."**

**12:30** Alijumlisha mambo inayopasa mtu kufanya kwa Mungu na maneno haya: **Kumpenda** na **roho**, **nafsi**, **nia** na **nguvu** yake yote. Sharti Mungu awe kwa pahali pa kwanza ndani ya maisha ya mtu. Haifai mapendo kwa mtu au neno lo lote kushindana na mapendo yake kwa Mungu.

**12:31** Amri 6 kufika 10 za Amri Kumi zinatufundisha **kupenda jirani** yetu kama sisi wenyewe. Tunahitaji kupenda Mungu *kupita* sisi wenyewe, na jirani yetu *kama* wenyewe. Hivi maisha yaliyo na faida zaidi kwa Mungu yanaweka Mungu kwanza, na watu kwa pahali pa pili. Yesu hahitaji vitu au mali. Mungu na watu ni wakubwa kupita yote.

**12:32,33 Mwandishi** alikubali, akasema wazi ya kwamba **mapendo** kwa Mungu na kwa **jirani yetu** yana faida nyingi kupita desturi na taratibu za dini. Alifahamu ya kwamba iliwezekana kwa watu kutii desturi zote za dini, na kuonekana kama wenye kupenda Mungu, pamoja na kukosa utakatifu rohoni. Alikubali ya kwamba Mungu anaangalia hali ya roho ya mtu vilevile, pamoja na namna anavyoonekana mbele ya watu kwa njia ya matendo na mwenendo wake.

**12:34 Wakati Yesu** aliposikia masemo haya ya kushangaza, alimwambia mwandishi ya kwamba yeye **si mbali na ufalme wa Mungu**. Watu wa haki wa ufalme hawajaribu kudanganya Mungu, wenzao, au roho zao wenyewe na dini ya kuonekana tu. Wakifahamu ya kwamba Mungu anaangalia roho ya mtu, wanafika kwake kupata kusafishwa toka zambi zao, na uwezo kuishi maisha ya kumpendeza.

Nyuma ya maneno haya, **hakuna mtu aliyesubutu** tena kumwuliza neno.

**J. Mwana wa Daudi ni Bwana wa Daudi (12:35-37)**

**Waandishi** walifundisha ya kwamba Masiya atakuwa mzao wa **Daudi.** Neno hili ni kweli, lakini ni kweli kwa sehemu tu. Hivi Bwana Yesu alikuwa na ulizo juu ya neno hili kwa watu waliokuwa wamemzunguka ndani ya kiwanja cha hekalu. Ndani ya Zaburi 110:1 Daudi aliita Masiya atakayekuja **Bwana** wake. Neno hili liliwezekana namna gani? Namna gani Masiya aliweza kuwa *Mwana* wa Daudi na *Bwana* wake vilevile? Kwa sisi watu wa sasa jibu la ulizo hili ni wazi. Masiya atakuwa Mtu *na* Mungu. Kama **Mwana** wa Daudi atakuwa mtu. Kama **Bwana** wa Daudi atakuwa Mungu.

Makutano yote walimsikiliza kwa furaha. Ni kama walikuwa tayari kukubali jibu lake, hata kama hawakufahamu kweli hii nzima. Hatusomi ya kwamba Wafarisayo na waandishi walisema neno. Ilikuwa kimya ya kuogofya.

**K. Maonyo juu ya waandishi (12:38-40)**

**12:38,39 Waandishi** walionekana kama watu wa kushika dini. Walipenda kutembea na **mavazi marefu**. Neno hili liliwatenga na watu wengine na kuwaonyesha kuwa watu wa dini. Walipenda kusalimiwa na majina ya heshima. Neno hili lilisaidia kiburi yao. Waliketi kwa pahali pa heshima **katika sunagogi**, lakini pahali tunapokaa ha-

pawezi kuongeza utawa wetu. Hawakutaka kujulikana kwa maneno ya dini tu, lakini kuwa na heshima katikati ya watu vilevile. Walitaka kuketi kwa **pahali pazuri zaidi katika karamu.**

**12:40** Ndani ya roho zao walikuwa wenye choyo na hila. Waliiba nyumba na mali ya **wajane** kujitajirisha wenyewe, wakisema mali hii ni kwa Bwana! Waliomba **maombi marefu** – masemo makubwa ya kiburi – maombi ya maneno bure tu.

**L. Sengi mbili za mjane (12:41-44)**

Mapendo ya mjane yalikuwa namna nyingine na roho ya choyo ya waandishi. Waandishi waliiba nyumba za wajane, lakini mjane huyu alitolea Bwana **yote aliyokuwa** nayo. Habari hizi zinaonyesha ya kwamba Bwana anajua maneno yote. Akitazama **watajir**i wakitupa feza nyingi ndani ya **sanduku ya mali** ya hekalu, alijua kwamba kufanya hivi hakuwa *sadaka* kwao, kwa sababu walikuwa na mali nyingi zaidi. Alijua vilevile ya kwamba sengi mbili za mjane zilikuwa **mali yote** aliyokuwa nayo. Hivi Bwana alisema ya kwamba mjane **alitoa kupita watu wale wote pamoja**. Ndiyo, haikuwa mali nyingi, lakini Bwana anapima zawadi zetu akifikiri juu ya kusudi letu, juu ya hesabu ya mali tuliyo nayo, na kama tukibaki na mali ngapi kwa sisi wenyewe. Neno hili linasaidia sana roho za watu wasiokuwa na mali nyingi, lakini walio na hamu kubwa kumtolea zawadi.

Ni mshangao kuona ya kwamba tunasifu tendo la mjane na tunakubali masemo ya Bwana juu yake bila kumwiga! Kama tukiamini kweli kweli maneno tunayosema tunaamini, tungalifanya kama yeye. Zawadi yake ilionyesha ya kwamba aliamini vyote vilikuwa vya Bwana, ya kwamba yeye anastahili kupokea vyote, na sharti apewe vyote. Wakristo wengi kwa wakati wa sasa wangesema mjane hakutenda na akili, na ya kwamba ingalimpasa kujiwekea mali kwa mahitaji yake ya kuja. Lakini haya ndiyo maisha ya imani – kutoa vyote kwa kazi ya Mungu sasa na kumwamini kuwapatia mahitaji yao kwa wakati wa kuja. Ameahidi kufanya hivi kwa wale wanaotafuta kwanza ufalme wa Mungu na haki yake (Mt. 6:33).

Mafundisho haya ya Kristo ni makali? Yanageuza mawazo yetu kabisa? Kama sivyo, hatujafahamu bado kusudi kubwa la utumishi wake.

## 6. HOTUBA YA MTUMISHI KWA MLIMA WA MIZEITUNI (Sura 13)

**A. Yesu anatabiri ya kwamba hekalu litaharibiwa (13:1,2)**

**13:1** Wakati Yesu alipokuwa akiondokea uwanja wa **hekalu** mara ya mwisho mbele ya kufa kwake, **mmoja wa wanafunzi wake** alianza kusema juu ya uzuri wa hekalu na majengo ambayo yalilizunguka. Wanafunzi walikuwa wakiwaza juu ya kazi ngumu ya kusimamisha nyumba na mawe yale makubwa sana.

**13:2** Mwokozi aliwajulisha ya kwamba majengo haya yote yataharibiwa nyuma kidogo. **Hata jiwe moja halitabaki juu ya lingine** bila kubomolewa wakati majeshi ya Waroma watakapoingia Yerusalema kwa mwaka 70 A.D. Kwa nini wataweka roho sana juu ya maneno yaliyo ya wakati tu?

**B. Mwanzo wa uchungu (13:3-8)**

Ndani ya hotuba yake juu ya **Mlima wa Mizeituni** Bwana alikokota mawazo ya wanafunzi juu ya matokeo makubwa kupita. Ni kama mengine ya maneno aliyotabiri yalikuwa juu ya kuharibiwa kwa Yerusalema kwa mwaka 70 A.D., lakini ni wazi ya kwamba mengi yao ni juu ya muda wa Mateso na Kurudi kwa Kristo katika uwezo na utukufu. Maonyo makubwa ya hotuba hii

yaliyo kwa waamini wa kila muda, ndiyo (1) *angalien*i (mash. 5, 9, 23, 33, 35, 37); (2) *musifazaike* (sh.7); (3) *shinda* (sh.13); (4) *ombeni* (mash. 18,33).

**13:3,4** Mwanzo wa hotuba hii ulitanguliwa na ulizo la **Petro, Yakobo, Yoane na Anderea**: Hekalu litaharibiwa **wakati gani,** na **alama gani** itatangulia tukio hili lililotabiriwa? Ndani ya jibu lake, Bwana alisema juu ya uharibifu wa hekalu lile, pamoja na hekalu lingine litakalosimamishwa nyuma. Hekalu lile litaharibiwa kwa wakati wa Mateso Makubwa, mbele ya kuja kwake kwa pili.

**13:5,6** Kwanza, iliwapasa **kukaa na ange** wasidanganywe na watu watakaosema wao ni Masiya. Watu **wengi** watatokea na kujiita Kristo, lakini wao ni wadanganyifu. Hata leo kuna dini nyingi za uwongo zenye wapinga-Kristo.

**13:7,8** Neno la pili, haifai wafikiri habari za **vita na uvumi wa vita** ni alama ya nyakati za mwisho. Kwa muda ule wote mataifa watapigana. Na zaidi ya ule, kutakuwa na **matetemeko ya inchi, njaa, na matata.** Maneno haya yatakuwa kama maumivu wa kwanza ya mwanamke aliye karibu kuzaa mtoto, mwanzo tu wa muda wa taabu kubwa sana, kupita taabu yote tangu zamani.

### C. Mateso ya wanafunzi (13:9-13)

**13:9** Neno la tatu Bwana alilotabiri ni ya kwamba wale ambao watamfuata na kumshuhudia na roho moja bila kugeuka watajaribiwa, na kuteswa. Watapelekwa kwa baraza za hukumu za dini na za serikali.

Mashairi haya ni juu ya ushuhuda wa Wakristo kwa kila wakati, lakini ni kama ni zaidi juu ya waamini Wayuda 144,000 watakaopeleka Habari Njema ya ufalme kwa mataifa yote ya dunia mbele ya kurudi kwa Kristo kutawala.

**13:10** Haifai kutumika na shairi 10 kufundisha ya kwamba *lazima* **Habari Njema ihubiriwe kwa mataifa yote** *mbele ya Bwana Yesu kurudi kwa hewa* kupeleka bibi-arusi yake, ndiye kanisa, pamoja naye mbinguni. *Ingepasa* kuhubiriwa pahali pote duniani, na *labda itahubiriwa* kweli, lakini hatusomi neno hili ndani ya Biblia. Hakuna unabii unaohitaji kutimizwa mbele ya kuja kwa pili kwa Kristo kwa watakatifu wake; angeweza kufika hata saa hii!

**13:11** Bwana aliahidi ya kwamba saa waamini wanaoteswa na kufikishwa mbele ya waamuzi kwa ajili yake watasaidiwa na Mungu kujisimamia. Hawatahitaji kutayarisha mbele maneno watakayosema, labda hawatakuwa na saa kufanya hivi. **Roho Mtakatifu** atawapa maneno yale yale ambayo itawapasa kusema. Haifai kutumika na ahadi hii kama uzuru tusitayarishe mafundisho na hotuba za Habari Njema kwa wakati wa sasa. Ni ahadi ya usaidizi toka Mungu kwa wakati wa hatari kubwa. Ni ahadi kwa wale wanaoteswa kwa ajili ya Kristo, si kwa wahubiri!

**13:12,13** Neno lingine litakaloonekana kwa wakati wa mateso ndilo hili: Wafuata waaminifu wa Bwana wengi watatolewa kwa adui zao. Watu wa jamaa yao wenyewe watapitisha habari zao kwa adui zao. Kushindana na dini ya ukristo kutajaza dunia. Wafuata wa Mwokozi watahitaji kuwa na uhodari mkubwa wasimkane, **lakini yeye anayeshinda hata mwisho ataokolewa**. Maana yake haiko ya kwamba atapokea wokovu wa milele kwa sababu ya kusimama imara; hii ingalikuwa habari njema ya uwongo. Na maana yake si ya kwamba waamini waaminifu wataponyeshwa toka mauti wakati wa Mateso, kwani tunasoma pahali pengine ya kwamba wengi wao watakufa. Tunafikiri maana ya mashairi haya ndiyo ya kwamba wale wanaosimama imara hata mwisho wanahakikisha kwa njia hii ya kwamba wao ni waamini wa kweli na *waliokolewa* kweli kweli.

### D. Mateso Makubwa (13:14-23)

**13:14-18** Shairi 14 linatufikisha kwa mwanzo wa sehemu ya pili ya muda wa Mateso, ndiyo Mateso *Makubwa.* Tunajua neno hili kwa njia ya kusawanisha mashairi haya na **Danieli** 9:27. Kwa wakati ule sanamu kubwa ya kuchukiza sana itasimamishwa katika hekalu kwa Yerusalema. Watu watalazimishwa kuiabudu. Wakikataa watauawa. Waamini wa kweli watakataa kuiabudu.

Kusimamishwa kwa sanamu hii ni mwanzo wa mateso makubwa sana. Wale wanaosoma na kuamini Biblia watafahamu ya kwamba saa ya kukimbia toka **Yudea** imefika. Hawatakuwa na saa kufunga vitu kwa safari. Kukimbia kutakuwa nguvu zaidi kwa wanawake **wenye mimba,** nao wanao**nyonyesha** mtoto. Kama ni kwa **wakati wa baridi,** neno hili litaongeza hatari nyingine.

**13:19** Mateso ya wakati ule yatakuwa makubwa kupita **mateso** yo yote ya zamani au kwa wakati wa kuja. Ni *Mateso Makubwa.* Bwana Yesu hasemi hapa juu ya mateso waamini wanayopata kwa kila wakati. Mateso haya ni namna nyingine, makali kupita yote.

Ona ya kwamba **mateso** haya ni zaidi ya Wayuda. Tunasoma juu ya hekalu (sh.14, Mt. 24:15) na Yudea (sh.14). Ni wakati wa taabu ya Yakobo (Yer. 30:7). Hatusomi juu ya kanisa hapa. Kanisa litapelekwa mbinguni mbele ya mwanzo wa Siku ya Bwana (1 Tes. 4:13-18; linganisha na 1 Tes. 5:1-3).

**13:20** Mabakuli ya hasira ya Mungu yatamwangwa juu ya dunia kwa wakati ule. Utakuwa wakati wa taabu, machafuko na kumwangika kwa damu. Watu wengi zaidi watauawa, hata Mungu atafupisha urefu wa muda wa jua; asipofanya hivi, *hakuna mtu* atakayepona.

**13:21,22** Kwa wakati wa Mateso Makubwa watu wengine wataonekana tena ambao watajiita masiya, lakini ni **masiya za uwongo**. Watu katika taabu yao kubwa watafungana na mtu ye yote anayeahidi kuwasaidia wakae na salama. Lakini waamini watajua ya kwamba Kristo hatatokea kimya, bila matangazo. Hata kama **makristo hawa ya uwongo** wakifanya maajabu (ndiyo, watafanya hivi), **wachaguliwa** hawatadanganywa. Watafahamu ya kwamba maajabu haya yanatoka kwa Shetani.

Maajabu si ya Mungu kila mara. Hata kama watu wasipoweza kuyafanya, mengine yanatoka kwa Shetani, malaika au pepo wachafu. Mwenye uasi atapewa uwezo toka Shetani kufanya maajabu (2 Tes. 2:9).

**13:23** Hivi inapasa waamini **kuangalia.**

### E. Kuja kwa pili (13:24-27)

**13:24,25 Nyuma ya mateso haya** kutakuwa na msukosuko wa kushitusha mbinguni. Giza litafunika dunia mchana na usiku. **Nyota za mbingu zitaanguka,** na nguvu zilizo mbinguni zitatikisika (ndio uwezo unaofanyiza nyota kutembea katika njia zao).

**13:26,27** Halafu watu wa dunia wenye hofu kubwa wataona **Mwana wa watu** akirudi duniani, lakini mara hii si kama Mnazareti mnyenyekevu (Mt. 2:23), lakini kama Mshindaji mwenye utukufu. Atakuja **katika mawingu,** pamoja na malaika na watakatifu waliotukuzwa, wengi sana. Litakuwa ono la utukufu mkubwa, la kustaabisha sana. Atatuma malaika zake kukusanya wachaguliwa wake, ndio wale ambao walimkiri kuwa Bwana na Mwokozi wakati wa Mateso Makubwa. Watakuja toka pahali pote, toka mwisho mmoja wa dunia hata upande wa mwisho mwingine. Watakuja toka la Chine hata Amérique du Sud na kufurahi ndani ya baraka za utawala wa miaka elfu moja wa ajabu wa Kristo duniani. Lakini adui zake wataharibiwa kwa wakati ule ule.

**F. Mfano wa mtini (13:28-31)**

**13:28** **Mtini** ni mfano wa taifa la Israeli. Yesu alifundisha hapa ya kwamba mbele ya kuja kwake mara ya pili mtini **atatoa majani**. Kwa mwaka 1948 taifa la Israeli lilisimamishwa na kuanza kujitawala lenyewe. Kwa wakati wa sasa inchi ile inashawishi inchi nyingine za dunia sana hata kama ni inchi ndogo tu. Ni kama Israeli "anachanua majani." Hakuna matunda kwanza; ndiyo hakutakuwa na matunda kufika wakati Masiya atakaporudi kwa watu walio tayari kumpokea.

**13:29** Kusimamishwa kwa taifa la Israeli na kuongezeka kwa nguvu yake kunatufahamisha ya kwamba Mfalme ni **karibu kutokea – karibu na milango.** Kama kuja kwake na mwanzo wa utawala wake ni karibu hivi, kuja kwake kwa kanisa lake ni karibu sana!

**13:30** Watu wengine wanafikiri kwamba maneno yote yanayotabiriwa ndani ya sura hii yangetimizwa kwa wakati watu walioishi saa Bwana Yesu alipokuwa duniani walipokuwa kwanza na uzima. Mawazo haya si mazuri kwa sababu mengi ya maneno haya, zaidi mashairi 24-27, hayakutimizwa kwa wakati ule.

Wengine wanafikiri ya kwamba **kizazi** walioishi wakati mtini ulipotoa majani, maana wakati Israeli lilipogeuka taifa huru kwa mwaka 1948, watakuwa hai saa Kristo atakapokuja tena.

Sisi tunafikiri ya kwamba labda maana ya **kizazi hiki** ni "taifa hili." Tunafikiri ni "taifa la Wayuda wenye kutokuamini" na wenye kukataa Masiya. Miaka inayopita inaonyesha wazi ya kwamba "kizazi hiki" *hakijapita bado*. Taifa lenyewe lingali hai, na wanaendelea kuchukia Bwana Yesu sana. Yesu alitabiri ya kwamba taifa la Israeli na uadui wake zitaendelea kufika wakati atakapokuja mara ya pili.

**13:31** Bwana wetu alisema tena ya kwamba bila shaka maneno yote aliyotabiri yatatimizwa. **Mbingu na dunia zitapita**, lakini kila neno Bwana alilosema litatimizwa.

**G. Hakuna mtu anayejua siku wala saa (13:32-37)**

**13:32** Yesu alisema, **"Lakini habari za siku ile na saa ile, hakuna mtu anayejua, wala malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba tu."** Adui za Habari Njema wametumika na shairi hili kujaribu kuhakikisha ya kwamba Yesu ni mtu tu, asiyejua maneno yote, kama sisi watu. Na kuna waamini wa kweli wasiojifunza Neno la Mungu vizuri wanaosema Yesu alijifanya mwenyewe hana utukufu, na aliacha kuwa na tabia zilizo za Mungu tu, wakati alipofika duniani kama mtu.

Maelezo haya mawili yote si kweli. Yesu **alikuwa** wote wawili – Mungu na Mtu; na Yeye **ni** wote wawili – Mungu na Mtu. Ana tabia na nia kamilifu ya Mungu, na ya mtu vilevile. Ni kweli ya kwamba Uungu wake ulifunikwa na mwili wa mtu, lakini ulifichwa tu. Hakuna saa wakati asipokuwa Mungu mkamilifu.

Basi namna gani hajui saa ya kuja kwake mara ya pili? Tunafikiri Yoane 15:15 linatusaidia kufahamu neno hili, "… mtumwa hajui anayofanya bwana wake …" Kama Mtumishi mkamilifu, Bwana Yesu hakujulishwa saa atakapokuja. Ndiyo, akiwa Mungu, alijua neno hili. Lakini kama Mtumishi, hakulijua kwa kuweza kulifunua kwa watu.

**13:33-37** Kwa mwisho wa sura hii kuna maonyo tuweze kukaa kuangalia na kuomba kwa sababu **hatujui wakati gan**i Bwana atakapokuja. Sharti tukae na kuangalia wakati wote.

Neno namna hii linatokea kwa wakati wa sasa vilevile. Mtu anaondoka nyumba yake kwenda safari ndefu. Ana-

toa maagizo kwa mtumishi wake, na anasema na zamu vilevile kutazamia kurudi kwake. Yesu alijifananisha na mwenye safari. Anaweza kurudi kwa saa yo yote ya usiku. Haifai watu wake, walio kama zamu, kushindwa na **usingizi**. Hivi aliacha agizo hili kwa watu wake wote: **"Angalieni!"**

## 7. MAUMIVU NA MAUTI YA MTUMISHI (Sura 14, 15)

### A. Shauri la kuua Yesu (14:1,2)

Ilikuwa siku ya kazi tatu ya juma sasa, na nyuma ya **siku mbili** nyingine **Pasaka** itakuliwa, na kuanza siku saba **za karamu ya mikate isiyochachwa**. Viongozi vya dini waliweka roho kabisa kuua Bwana, lakini hawakutaka kufanya hivi kwa siku hizi za karamu ya dini, kwa sababu watu wengi waliheshimu Yesu kama nabii.

Hata kama **wakubwa wa makuhani na waandishi** walikusudi **kutokuua Yesu** kwa **wakati wa karamu**, kusudi la Mungu lilikuwa na uwezo kupita, na Mwana-Kondoo wa Pasaka wa Mungu aliuawa kwa wakati ule ule (ona Mt. 26:2).

### B. Yesu anapakaliwa mafuta kwa Betania (14:3-9)

Roho Mtakatifu na mwandishi wa Habari Njema hii walifanyiza mapendo ya mwanamke huyu kwa Bwana wetu kungaa sana katikati ya giza ya mashauri maovu ya viongozi vya dini na ya Yuda.

**14:3 Simoni, mwenye ukoma** alitayarisha karamu kuheshimu Mwokozi, labda kwa kuonyesha asante yake kwa sababu Bwana alikuwa amemponyesha. Mwanamke mmoja (tunafikiri alikuwa Maria ya Betania, Yn. 12:3) alitumika na marasi nyingi ya **bei kubwa** kupakaa **kichwa** cha Bwana. Alimpenda sana.

**14:4,5 Wengine** wa wageni walifikiri mwanamke alipoteza marasi ile ya bei kubwa bure. Kwa nini **hakuuza** marasi hii na **kutoa mali yenyewe** kusaidia **watu masikini? (Dinari mia tatu** zilikuwa mshahara kwa kazi ya mwaka mmoja mzima.) Hata kwa wakati wa sasa watu wanafikiri kutoa mwaka mmoja wa maisha yao kwa kazi ya Bwana ni kupoteza saa bure. Wangefikiri nini juu ya kutoa maisha yao mazima kwa Bwana!

**14:6-8 Yesu** aliwahamakia juu ya manunguniko yao. Mwanamke alikuwa amefahamu ya kwamba hii ilikuwa saa yake kuheshimu Mwokozi wake. Watu wale walifikiri mahitaji ya wamasikini? Wataweza kuwasaidia daima, kwa sababu kutakuwa na **watu masikini siku zote**, lakini Bwana atakufa nyuma kidogo na kuzikwa. Mwanamke huyu alitaka kumfanyia neno hili wakati ilipowezekana. Labda hataweza kutengeneza **mwil**i wake nyuma ya kufa kwake, hivi alikusudi kumwonyeshea mapendo yake wakati alipokuwa kwanza hai.

**14:9** Utamu wa harufu ya marasi hii umetufikia hata sisi kwa wakati wa sasa. Bwana Yesu alisema mwanamke na habari za tendo lake zitajulishwa duniani pote. Neno hili limefanyikana kweli – kwa njia ya vitabu vya Habari Njema.

### C. Udanganyifu wa Yuda (14:10,11)

Mwanamke huyu aliheshimu Mwokozi sana, lakini **Yuda** hakumheshimu hata kidogo. Alikuwa amekaa pamoja na Bwana Yesu kwa mwaka mmoja au zaidi, na Bwana alimwonyeshea mapendo tu, lakini hata hivi sasa alifikia wakubwa wa makuhani na ahadi kuwatolea Mwana wa Mungu kwa hila. Walifurahi sana na walisema watamlipa mali kwa tendo hili la hila. Yuda alihitaji tu kutayarisha njia kutimiza ahadi yake.

### D. Matayarisho kwa Pasaka (14:12-16)

Hatujui kabisa kabisa namna matukio

yalivyofuatana, lakini tunafikiri tumefikia siku ya kazi ine ya jenga la Pasaka. Wanafunzi hawakufahamu ya kwamba Pasaka hii itakuwa Pasaka ya mwisho, na itatimiza Pasaka zote nyingine zilizokuliwa ndani ya mia ya miaka iliyopita. Waliuliza Bwana kuwajulisha pahali gani watakapokula **Pasaka.** Ali**watuma** kwa Yerusalema na kutafuta **mwanamume anayechukua chungu cha maji** – ono la ajabu kwa sababu vyungu vya maji vilibebwa na wanawake. Mwanamume huyu atawaongoza kwa nyumba yenyewe. Halafu iliwapasa kuomba mwenye nyumba kuwaonyesha chumba pahali **Mwalimu atakapokula Pasaka pamoja na wanafunzi wake.**

Ni vizuri sana kuona Bwana akichagua na kutoa maagizo hivi. Anatenda kama Mtawala Mwenye Enzi wa watu na vitu. Ni vizuri vilevile kuona wenye mioyo tayari kujitoa pamoja na mali yao yote kwa yeye kutumika nayo. Ni baraka kwetu kumfungulia njia kuingia kila sehemu ya maisha yetu!

### E. Yesu anatabiri ya kwamba atatolewa kwa adui (14:17-21)

**Mangaribi** ile **alikuja pamoja na wanafunzi** wake **kumi na wawili** kwa chumba kilichotayarishwa. Wakati walipoketi **na kula, Yesu** alisema ya kwamba mmoja wa wanafunzi atamtoa kwa mikono ya adui. Wao wote walijuana na uovu wa mioyo yao, hivi kila mmoja wao aliuliza kama Bwana alisema juu yake. Halafu Yesu alionyesha ya kwamba Bwana atampa yeye ambaye atamtoa kipande cha mkate aliochovya ndani ya mchuzi. Alisema **Mwana wa watu** alikwendea mauti yake kama ilivyotabiriwa, lakini hukumu ya yule ambaye alimtoa kwa adui zake itakuwa kubwa sana. **Ingalikuwa heri kwake yule mtu kama asingalizaliwa.**

### F. Karamu ya kwanza ya Ukumbusho (14:22-26)

**14:22-25** Nyuma ya kupokea **mkate** Yuda alitoka inje na ulikuwa usiku (Yn. 13:30). Wakati alipokwisha kutoka, Yesu alisimamisha karamu ya ukumbusho. Maana yake inaelezwa vizuri sana na maneno matamu matatu: (1) **Akatwaa** – alitwaa utu; (2) **akavunja** – alikuwa karibu kuvunjwa juu ya msalaba; (3) **akawapa** – alijitoa kwa ajili yetu.

**Mkate** ni mfano wa **mwili** wake ambao ulitolewa; **kikombe** ni mfano wa **damu** yake iliyomwangwa. Kwa njia ya **damu** yake alitia hakika **Agano Jipya**. Hatakula karamu za furaha nyingine kufika wakati atakaporudi duniani kusimamisha **ufalme** wake.

**14:26** Halafu waliimba **wimbo** – tunazani ulikuwa sehemu ya Zaburi 113-118. Kisha **walitoka** Yerusalema, wakavuka mto Kiduroni na kwendea **mlima wa Mizeituni.**

### G. Kujitegemea kwa Petro (14:27-31)

**14:27, 28** Wakati walipokuwa njiani, Mwokozi alionya wanafunzi ya kwamba wao wote watapata haya na kuogopa kujulikana kama wafuata wake nyuma kidogo. Itatokea namna Zekaria alivyotabiri, **Mchungaji** atapigwa na **kondoo** zake **watasambazwa** (Zek. 13:7). Lakini alisema nao na neema ya kwamba hatawakataa; nyuma ya ufufuko wake atawangojea katika **Galilaya.**

**14:29,30** **Petro** alipata uchungu juu ya kufikiri atakana Bwana. Labda wanafunzi wengine watafanya hivi, lakini yeye hatafanya hivi kamwe! Yesu alikomboa neno hili 'kamwe' na 'leo'. **Mbele ya kuwika jogoo** mara **mbili** Petro atakwisha kukana Mwokozi mara **tatu.**

**14:31** Petro alizidi kusema na nguvu ya kwamba hata ikimpasa kufa pamoja na Bwana, **hatamkana** kabisa.

Wao wote walisema vivyo hivyo na kiburi. Tusisahau kamwe ya kwamba sisi ni sawasawa nao. Inatupasa sisi sote kutambua woga na uzaifu wa roho zetu.

### H. Maumivu makubwa katika Getesemane (14:32-42)

**14:32** Giza lilikuwa limefunika inchi na ulikuwa usiku wa siku ya kazi ine, na kukaribia asubui wa siku ya tano. Wakati **walipofikia** pahali palipozungushwa na ua **palipoitwa Getesemane**, Bwana Yesu aliacha wanane wa wanafunzi karibu na pahali pa kuingia.

**14:33,34 Pamoja na Petro, Yakobo na Yoane** aliingia kupita ndani ya shamba. Pale roho yake takatifu ilipatwa na mzigo mzito sana wakati alipotazamia kugeuka zabihu ya zambi kwa sisi. Inatushinda kufahamu uchungu wake mkubwa, yeye aliye bila zambi kufanyizwa zambi kwa ajili yetu. Aliacha wanafunzi wake watatu pale na agizo kuangalia bila kulala. **Alikwenda mbele kidogo** – peke yake. Atakwendea msalaba hivi, peke yake, akibeba hukumu ya kuogofya ya Mungu kwa zambi zetu.

**14:35** Tunashangaa na kustaajabu kuona Bwana Yesu akilala chini kwa udongo akiomba Mungu. Alikuwa akiomba aachiliwe asiende msalabani? Sivyo, hata kidogo. Alifika duniani na kusudi hili. Kwanza, **aliomba saa ile impitie, ikiwezekana.** Kama ikiwezekana kuokoa watu toka zambi kwa njia nyingine bila kufa kwake, kuzikwa, na ufufuko wake, afazali Mungu afunue njia hii. Lakini hakupata jibu toka mbinguni. Hakuna njia nyingine kwa kutuokoa.

**14:36** Aliomba tena, **"Aba, Baba, yote yanawezekana kwako, uniondolee kikombe hiki; lakini si kama ninavyotaka mimi, lakini kama wewe unavyotaka."** Ona ya kwamba aliita Mungu **Baba** yake mpendwa, **anayeweza kufanya maneno yote,** si maneno hapa duniani tu, lakini maneno ya roho vilevile. Maombi yake hapa yalikuwa zaidi juu ya maneno ya roho. Baba Mwenyezi aliweza kupata njia yo yote nyingine iliyo haki, kuokoa wenye zambi? Mbingu zilikuwa kimya, na zilionyesha ya kwamba hakuna njia nyingine. Lazima Mwana Mtakatifu wa Mungu atoe damu yake ili wenye zambi waweze kufunguliwa toka zambi!

**14:37-40** Wakati aliporudi karibu na wanafunzi wake watatu **aliwakuta wakilala** usingizi – neno lililoonyesha wazi uzaifu wa miili yao ya zambi. Yesu alikuwa ameonya Petro **asilale** usingizi kwa **saa** ile. Saa nusu tu zilipita tangu Petro alijisifu ya kwamba hatageuka kamwe. Sasa ilimshinda kukaa na macho. Kama mtu asipoweza kushinda hata kwa **saa moja** na maombi, ataweza kushinda majaribu makubwa ya gafula? Hata roho yake akitaka kufanya hivi kweli kweli, lazima akumbuke uzaifu wa mwili wake.

**14:41,42** Bwana alirudi mara tatu na kukuta wanafunzi wake wakilala usingizi. Halafu alisema nao, **"Laleni sasa na kupumzika. Inafaa. Saa imekuja; tazama, Mwana wa watu ametiwa katika mikono ya wenye zambi."** Basi walisimama na kuanza kwenda. Hawakuhitaji kwenda mbali.

### I. Yesu alitolewa kwa adui na kufungwa (14:43-52)

**14:43 Yuda** alikuwa ameingia shamba mbele pamoja na makutano wakibeba **panga na magongo,** kama wenye kukamata mvunja sheria ya hatari.

**14:44,45 Mhaini** alijulisha makutano mbele ya kwamba itawapasa kukamata yule ambaye **atambusu**. Hivi alifika karibu na Yesu, akamwita **Mwalimu**, **akambusu** tena na tena. Kwa sababu gani Yuda alitoa Yesu kwa adui zake? Alihuzunishwa kwa sababu Yesu

hakuanza kutawala? Tumaini lake lilikwisha ya kwamba atapata pahali pa heshima ndani ya ufalme? Choyo ilimshinda? Labda maneno haya yote yalimsukuma kutenda neno hili ovu sana.

**14:46-50** Halafu askari wakakuja na kukamata Yesu. Petro **akafuta upanga** wake mbio, **akakata sikio la mtumwa wa kuhani mkubwa**. Alifanya hivi akisukumwa na tabia ya mwili, na alitumika na kitu cha dunia kupiga vita ya roho. Bwana alihamakia Petro na alifanya ajabu kurudisha sikio la mtumishi tena kwa pahali pake, kama tunavyosoma katika Luka 22:51 na Yoane 18:11. Halafu Yesu alikumbusha wale ambao walimfunga ya kwamba halikuwa neno la akili kwao kumkamata kwa nguvu! Alikuwa pamoja nao **kila siku hekaluni akifundisha.** Kwa sababu gani hawakumkamata kwa wakati ule? Alijua jibu la ulizo lake: **Sharti Maandiko yatimizwe** yaliyotabiri ya kwamba atatolewa kwa mikono ya adui (Zaburi 41:9), atafungwa (Isaya 53:7), kuteswa na watu (Zaburi 22:12), na kuachwa pekee (Zek. 13:7).

**14:51,52** Marko tu aliandika habari hizi, na watu wengi wanafikiri **kijana** huyu aliyeacha nguo yake mikononi mwa askari wakati alipokimbia kwa haraka alikuwa Marko mwenyewe.

Mwandishi mmoja, jina lake Erdman, anawaza ya kwamba habari hizi ziliingizwa hapa kuonyesha ya kwamba Yesu aliachwa pekee kabisa kwa wakati huu wa hatari na maumivu. Alijuana sana na kuteswa peke yake.

### J. Yesu mbele ya Kuhani Mkubwa (14:53,54)

Habari za hukumu iliyoongozwa na viongozi vya dini ni ndani ya shairi 53 kufika 15:1. Hukumu hii ilikuwa na sehemu tatu: (1) Hukumu mbele ya kuhani mkubwa (mash. 53,54); (2) Kusanyiko la Baraza katikati ya usiku (mash.55-65); (3) kusanyiko la Baraza asubui (15:1).

**14:53** Zaidi ya watu wanafikiri ya kwamba Marko aliandika juu ya hukumu mbele ya Kayafa. Habari za hukumu mbele ya Ana ni katika Yoane 18:13, 19-24.

**14:54 Petro** alifuata Bwana Yesu hata kufika **kiwanja cha kuhani mkubwa,** akikaa mbali kidogo. Mtu mmoja aliandika kwa ufupi habari za kuanguka kwake:

1. Kwanza alipiga vita – na bidii mbaya.
2. Kisha alikimbia – na woga.
3. Mwishoni alifuata toka mbali – si na roho yote, usiku.

**Aliketi**, **akaota moto** pamoja na watumishi, ndio adui za Bwana wake.

### K. Yesu mbele ya Baraza (14:55-65)

**14:55-59** Hata kama hatusomi neno hili waziwazi, tunafikiri shairi 55 ni juu ya mwanzo wa kusanyiko la Baraza katikati ya usiku. Baraza hii ilikuwa fungu la watu 70 walioongozwa na kuhani mkubwa. Usiku ule, Wafarisayo, Wasadukayo, waandishi na wazee (ndio Baraza) hawakuangalia na kuchunga amri za Baraza hata kidogo. Walikatazwa kukutana usiku au kwa siku kubwa za Wayuda. Walikatazwa kulipa rushwa kushawishi watu kushuhudia uwongo. Mtu akihukumiwa kufa, ilikuwa lazima kwa usiku mmoja kupita mbele ya kutimiza hukumu hii. Wasiopokutana ndani ya chumba kikubwa cha mawe (pahali pao pa kukutana karibu na hekalu), hukumu zao hazikuwa za lazima.

Kwa sababu walitaka sana sana kuua Bwana Yesu mbio, viongozi vya dini hawakusita kuasi sheria zao wenyewe. Walikusanya washuhuda wa **uwongo,** lakini ushuhuda wa watu wale haukupatana. Wengine waligeuza na kusudi masemo ya Yesu ya kwamba **ataharibu**

hekalu hili **lililofanyika kwa mikono**, na **ndani ya siku tatu atajenga lingine lisilofanyika kwa mikono.** Maneno Yesu aliyosema kweli ni katika Yoane 2:19. Hakusema juu ya hekalu katika Yerusalema, lakini juu ya hekalu la mwili wake.

**14:60-62** Yesu hakujibu mara moja wakati **kuhani mkubwa** alipomwuliza maneno, lakini wakati alipolapizwa (Matayo 26:63) kama yeye ndiye Kristo, **Mwana wake Mbarikiwa**, Mwokozi, akitii Walawi 5:1, akajibu, Mimi ni yeye. Kisha, kama kutaka kuondosha shaka ndani ya nia za wasikiaji ya kwamba yeye ni kweli Masiya, alimwambia kuhani mkubwa kwamba ataona **Mwana wa watu ameketi mkono wa kuume wa nguvu akikuja** tena duniani **na mawingu ya mbingu.** Maana ya masemo yake ndiyo ya kwamba kuhani mkubwa atamwona amefunuliwa wazi kama Mungu. Wakati alipokuja mara ya kwanza, utukufu wa uungu wake ulifunikwa ndani ya mwili wa mtu. Wakati atakapokuja tena na uwezo na utukufu mkubwa, pazia hili litaondolewa na kila mtu atajua kama yeye ni nani.

**14:63,64 Kuhani mkubwa** alifahamu maana ya masemo ya Yesu. Alipasua **nguo** yake kama alama ya hasira yake kwa sababu alihesabu masemo haya kuwa **ukufuru.** Ingalimpasa yeye kupita Waisraeli wote kuwa tayari kutambua na kupokea Masiya, lakini alimhukumu kupita wote. Lakini Baraza nzima walikubali ya kwamba Yesu alikuwa amekufuru, na **walimhukumu kuwa mwenye kustahili kuuawa.**

**14:65** Maneno yaliyofuata yalikuwa mabaya sana. Wengine wa watu wa Baraza **walianza kutemea** Mwana wa Mungu **mate**, **kumfunika uso** na kusema naye kutaja majina ya wale ambao walimpiga. Ni neno la kushangaza kupita kipimo kuwaza juu ya Mwokozi mwema akitendewa maneno ya haya kubwa namna hii na wenye zambi. **Watumishi** (ndio mapolisi ya hekalu) walifungana na watu wa Baraza na **kumpiga makofi.**

### L. Petro anakana Yesu na kutoa machozi na uchungu (14:66-72)

**14:66-68 Petro** alikuwa akingoja **chini katika kiwanja** cha nyumba. **Mmoja wa vijakazi vya kuhani mkubwa** akipita, akamwangalia karibu karibu, akasema Petro vilevile alikuwa mmoja wa wafuata wa yule Mnazareti, ndiye **Yesu.** Petro, – kwa haya yake – alisema hajui kama kijakazi alikuwa akisema juu ya nini. Alitoka inje hata ukumbi, akasikia **jogoo** akiwika. Ilikuwa taabu kubwa kwa Petro, tunda chungu la zambi.

**14:69,70 Kijakazi huyu alimwona tena** na kuwaambia watu wengine kwamba yeye ni mwanafunzi wa Yesu. Petro alikana maneno haya tena na nguvu. Labda alifazaika kwa sababu gani watu walikaa kumchokoza. Halafu watu waliosimama karibu walisema naye, **"Hakika wewe mmoja wao kwa sababu wewe Mgalilaya."**

**14:71,72** Akilaani na kuapiza, Petro alisema na nguvu ya kwamba **hakujua mtu huyu.** Mara moja nyuma ya kusema hivi, jogoo aliwika. Ni kama hata nyama walikataa uwongo wake. Mara moja Petro alifahamu ya kama maneno ambayo Bwana alisema mbele yametimizwa. Na roho ya kuvunjika **alitoa machozi.** Ona ya kwamba habari hizi za kukana kwa Petro ziliandikwa ndani ya Habari Njema ine zote. Sharti sisi sote tujifunze ya kwamba kiburi ya kujitegemea wenyewe itatupatia haya. Haifai tujitegemee wenyewe; lazima tutegemee uwezo wa Mungu tu.

### M. Hukumu ya asubui mbele ya Baraza (15:1)

Shairi hili linapasha habari za ku-

sanyiko la **Baraza asubui**, labda kuhalalisha maneno waliyofanya usiku wa mbele, na yasiyokuwa halali. Kwa mwisho wake Yesu **alifungwa** na kupelekwa kwa Pilato, liwali Mroma wa Palestina.

**N. Yesu mbele ya Pilato (15:2-5)**

**15:2** Kufika sasa Yesu alihukumiwa na viongozi vya dini juu ya *kutukana Mungu*. Sasa alipelekwa mbele ya Baraza ya hukumu ya serikali na kushitakiwa na *fitina*. Hukumu ile ilikuwa na sehemu tatu: kwanza mbele ya Pilato, nyuma yake mbele ya Herode, na mwishoni mbele ya Pilato tena.

**Pilato aliuliza** kama Bwana Yesu alikuwa **Mfalme wa Wayuda.** Kama neno hili likiwa kweli, ni nyepesi kufikiri ya kwamba atataka kupindua Kaisari, na pale ataweza kushitakiwa juu ya fitina.

**15:3-5 Wakubwa wa makuhani** walishitaki Yesu juu ya maneno mengi, na Pilato alishangaa juu ya roho yake kimya. Alimwuliza kwa sababu gani hakujisimamia mwenyewe, **lakini Yesu** alikataa kujibu washitaki wake.

**O. Yesu au Baraba? (15:6-15)**

**15:6-8** Ilikuwa desturi kwa mtawala Mroma kufungua **mfungwa mmoja** Myuda kwa wakati wa karamu hii – kwa kufurahisha roho za watu. Kulikuwa na mtu mmoja aliyefungwa kwa sababu ya **fitina na uuaji,** jina lake **Baraba**. Wakati Pilato aliposema alikuwa tayari **kufungua** Yesu, watu, wakifundishwa mbele na viongozi vyao vya dini, waliomba Baraba afunguliwe. Watu wale walioshitaki Yesu na fitina kwa Kaisairi, waliomba wafunguliwe mtu aliyehukumiwa juu ya zambi hii yeye mwenyewe. Lilikuwa neno pumbavu, la kushangaza, lakini zambi ni hivi. Kabisa kabisa walikuwa na wivu juu ya Yesu kwa sababu alipendwa sana na watu.

**15:9-14** Pilato aliuliza kama ilimpasa kufanya nini na Yule ambaye walimwita **Mfalme wa Wayuda**. Watu walilalamika na roho kali, **"Umsulibishe**!" Pilato aliuliza kwa sababu gani atasulibishwa, lakini sababu haikuwa. Kasirani ya makutano ilizidi, wakakaa kulalamika tu, "**Umsulibishe!"**

**15:15** Hivi Pilato, aliyekosa roho ya nguvu, alifanya neno walilotaka – **alifungua Baraba**, akaagiza Yesu kupigwa mijeledi na **kumtoa** kwa askari asulibishwe. Ilikuwa hukumu ya uzalimu kabisa. Ndiyo, ulikuwa mfano wa ukombozi wetu – Yule asiye na zambi alitolewa kufa ili wenye zambi waweze kutiwa huru.

**P. Askari wanazihaki Mtumishi wa Mungu (15:16-21)**

**15:16-19 Askari walipeleka** Yesu kwa **kiwanja cha nyumba ya liwali**. Walikusanya **kikosi kizima** cha askari, kisha walitenda sawasawa walifanyiza Yesu Mfalme wa Wayuda. Kama wangalifahamu tu maneno waliyotenda! Alikuwa Mungu Mwana ambaye walivika **vazi jekundu.** Alikuwa Mwumba wao mwenyewe ambaye walitia taji ya **miiba.** Alikuwa mwenye kutegemesha ulimwengu mzima ambaye walizihaki kama **Mfalme wa Wayuda**. Alikuwa Bwana wa uzima na utukufu ambaye **walipiga kichwani**. Walitemea Mkubwa wa salama **mate**. Pamoja na kumzarau walipiga magoti mbele ya Mfalme wa wafalme na Bwana wa wabwana.

**15:20,21** Wakati walipomaliza michezo yao **walimvika mavazi yake mwenyewe, wakamchukua inje wamsulibishe**. Marko aliandika ya kwamba askari waliagiza mtu mmoja aliyekuwa akipita njiani, **Simoni** wa Kurene (ndipo pahali katika Afrika ya kaskazini) kubeba **msalaba wake**. Labda alikuwa mwenye ngozi nyeusi au Myuda aliyesema Kiyunani. Alikuwa na wana wawili, **Alesanduro na Rufu**. Tunafikiri walikuwa waamini (kama **Rufu** ndiye

mtu anayetajwa katika Waroma 16:13). Simoni akibeba msalaba nyuma ya Yesu ni mfano kwetu wa namna inavyotupasa *sisi* kutenda kama wanafunzi wa Mwokozi.

**Q. Kusulibishwa (15:22-32)**

Roho ya Mungu anaonyesha maneno machache tu juu ya kusulibishwa kwa Yesu. Haelezi sana ukali kupita kipimo wa namna hii ya hukumu, wala juu ya maumivu yake makubwa.

Hatujui kabisa kabisa kwa wakati wa sasa kama pahali pa kusulibisha palikuwa wapi. Watu wengine wanafikiri palikuwa inje ya kuta za mji kwa wakati ule, na wengine ya kwamba palikuwa kwa upande wa kaskazini wa mji, karibu na shamba.

**15:22** **Golgota** ni jina kwa Kiaramaic, maana yake **mfupa wa kichwa**. Kalvari ni jina lenyewe kwa Kiroma. Labda pahali penyewe palionekana kama mfupa wa kichwa, au labda palitwa hivi kwa sababu palikuwa pahali pa kusulibisha watu.

**15:23** Askari waliletea Yesu **mvinyo iliyotiwa manemane.** Ilikuwa kama dawa, kupunguza maumivu yake. Lakini Yesu **hakuipokea,** maana alikusudi kubeba zambi na maumivu yote ya watu.

**15:24** Askari walipiga kura kwa mavazi ya watu waliosulibishwa. Wakati walipokamata **mavaz**i ya Mwokozi, walikamata karibu vitu vyake vyote.

**15:25-28** Ilikuwa saa tatu ya asubui wakati **walipomsulibisha.** Walitia andiko juu ya msalaba wake: **MFALME WA WAYUDA**. (Marko aliandika nusu tu ya maandiko mazima yaliyowekwa juu ya msalaba wake; ona Matayo 27:37; Luka 23:38; Yoane 19:19.) **Wanyanganyi wawili** walisulibishwa pamoja naye, mmoja kwa upande wake wa kuume, na mwingine kwa kushoto, kama Isaya alivyotabiri, "akahesabiwa pamoja na wale wenye kukosa" (53:12).

**15:29,30** Bwana Yesu alizarauliwa na wale waliopita njiani (mash. 29,30), **wakubwa wa makuhani** na **waandishi** (sh.31,32a), na wale wanyanganyi wawili (sh.32b).

Labda watu waliopita msalaba walikuwa Wayuda waliokuwa tayari kula Pasaka mjini. Inje ya mji walisimama saa nusu kuzarau Mwana-Kondoo wa Pasaka! Walisema (lakini ulikuwa uwongo) ya kwamba Bwana alisema **ataharibu hekalu** lao ambalo walipenda sana, na kulijenga tena **katika siku tatu**. Kama ilikuwa hivi **ajiokoe** mwenyewe kwa njia ya **kushuka toka msalaba**.

**15:31 Wakubwa wa makuhani na waandishi** walimzarau vilevile juu ya kuokoa **wengine.** Walisema, **"Aliokoa wengine, hawezi kujiokoa yeye mwenyewe."** Masemo yao yalikuwa maneno ya kuumiza sana sana, ya kukata roho, lakini hata hivi yalikuwa kweli. Yalikuwa kweli ndani ya maisha ya Bwana Yesu, na ndani ya maisha yetu vilevile. Hatuwezi kuokoa *wengine* pamoja na kujiokoa *sisi wenyewe* vilevile.

**15:32** Viongozi kwa maneno ya dini walisema naye vilevile ashuke **toka msalaba** kama akiwa Masiya, Mfalme wa Israeli; halafu **watamwamini**. Walisema, **tuone na tutaamini**.[25] Lakini utaratibu wa Mungu ni, "Amini, kisha utaona."

Hata wanyanganyi waliosulibishwa pamoja naye walimtukana.

**R. Saa tatu za giza (15:33-41)**

**15:33** Toka saa sita kufika saa tisa **giza** lilikuwa juu ya **inchi nzima**. Kwa wakati ule Yesu alikuwa akibeba hukumu nzima ya Mungu kwa zambi zetu. Alitengwa na Mungu kwa roho. Hakuna mtu atakayefahamu kamwe ukubwa wa maumivu yake wakati nafsi yake ilipofanywa zabihu kwa zambi.

**15:34** Karibu na mwisho wa maumivu wake, **Yesu alipaza sauti kubwa** (kwa Kiaramaic), **"Mungu wangu,**

**Mungu wangu, kwa nini umeniacha?"** Mungu akikuwa mtakatifu alikuwa **amemwacha** kwani ilimpasa kujitenga na zambi. Bwana Yesu alijifanya mamoja na zambi zetu, na alibeba azabu yao nzima.

**15:35,36 Wengine** wa watu waliosimama karibu walifikiri alikuwa akiita Elia wakati aliposema "Eloi, Eloi." Neno la aibu la mwisho alilotendewa lilikuwa wakati mtu mmoja alipojaza sifongo na **siki**, akaitia juu ya **mti** kumnywesha.

**15:37** Yesu **alitoa sauti** kubwa ya mshindaji – kisha **alitoa roho yake.** Alikufa kwa kutaka kwake mwenyewe, si kwa sababu ya uzaifu wa mwili.

**15:38** Kwa saa ile ile **pazia la hekalu lilipasuliwa vipande viwili toka juu hata chini**. Lilikuwa tendo la Mungu kuonyesha ya kwamba sasa kwa njia ya mauti ya Kristo Wakristo wote wanapewa ruhusa kuingia pahali patakatifu pa Mungu (ona Ebr. 10:19-22). Ulikuwa mwanzo wa muda mpya mzuri sana, muda wakati watu wasipokuwa mbali na Mungu tena, lakini watakapoweza kumkaribia.

**15:39 Akida** alikiri "Hakika mtu huyu alikuwa **Mwana wa Mungu**." Alisema vizuri, lakini ni nguvu kufahamu kama aliamini kweli kweli.

**15:40,41** Marko aliandika ya kwamba **wanawake** wengine walibaki karibu na msalaba. Wanawake walionekana sana ndani ya vitabu vya Habari Njema. Wanaume waliogopa hatari, walijificha. Wanawake walipenda Bwana Yesu kupita hali yao wenyewe. Walikuwa watu wa mwisho kwa msalaba na wa kwanza kwa kaburi.

### S. Maziko ndani ya kaburi la Yosefu (15:42-47)

**15:42** Sabato ilianza wakati wa mangaribi siku ya kazi tano. **Siku iliyotangulia sabato** au siku kubwa nyingine iliitwa **siku ya kutengeneza.**

**15:43** Saa ilikuwa nusu, na neno hili lilimpa **Yosefu wa Arimatea** uhodari kuomba ruhusa karibu na Pilato kuzika **mwili wa Yesu.** Yosefu alikuwa Myuda mwenye kupenda na kuabudu Mungu, labda alikuwa mmoja wa watu wa Baraza (Lk 23:50,51; vilevile Matayo 27:57 na Yoane 19:38).

**15:44,45** Ilikuwa nguvu kwa Pilato kuamini ya kwamba Yesu **alikuwa amekufa**. Wakati **akida** aliposema alikufa kweli, liwali **aliruhusu Yosefu kukamata mwili** wake. (Maneno mbalimbali yalitumiwa hapa kwa mwili wa Yesu. Yosefu aliomba kupewa *mwili* wa Bwana Yesu na Pilato alikubali apewe *maiti* yake.)

**15:46** Na mapendo sana Yosefu (na Nikodemo – Yoane 19:38,39) **walitia mwili dawa usioze, wakaufunika na sanda** na kuulalisha **ndani ya kaburi** jipya la Yosefu. Kaburi lilikuwa chumba kidogo kilichochorwa **toka mwamba.** Mlango wake ulikuwa jiwe mviringo.

**15:47** Wanawake tena, ndio Maria wawili walikuwa pale vilevile. Tunawasifu kwa mapendo yao kwa Bwana, mapendo yasiyopoa wala kuogopa.

## 8. KUSHINDA KWA MTUMISHI (16:1-20)

### A. Wanawake kwa kaburi tupu (16:1-8)

**16:1-4** Siku ya sabato mangaribi wale Maria wawili pamoja na **Salome** walikuja kutia mwili wa Yesu manukato. Walijua itakuwa nguvu. Walijua jiwe kubwa lilikuwa limefingirishwa mbele ya mlango. Walijua mhuri wa Waroma uliowekwa juu yake na walinzi Waroma walikuwa pale. Lakini mapendo yao yaliwasukuma kushinda mazuizo yote na kufika karibu na mwili wa mpendwa wao.

**Asubui mapema** sana siku ya kwanza ya juma walizungumuza **nani**

ambaye **atawafingirishia lile jiwe mbele ya mlango wa kaburi. Walipotazama,** wakaona limekwisha kufingirishwa! Hata ndani ya maisha yetu, tukitaka kuheshimu Bwana, vizuizo vinaondoshwa hata wakati tusipokutana nao bado.

**16:5,6 Wakaingia kaburi**, **wakaona** malaika aliyeonekana kama **kijana** akivaa nguo **nyeupe**. Malaika alifukuza woga wao mbio kwa njia ya kuwaambia ya kwamba **Yesu** alikuwa **amefufuka.** Kaburi lilikuwa tupu.

**16:7** Kisha aliwaagiza kwenda kutangaza habari za ufufuko wake. Ilipasa kuwaambia **wanafunzi** – **na Petro** – ya kwamba atakutana nao katika Galilaya. Ona ya kwamba **Petro** aliyekana Bwana wake, alitajwa na jina lake. Mkombozi mfufuliwa hakumkataa; alikaa kumpenda, na alitaka sana kumwona tena. Alitaka sana kwa kondoo huyu aliyekwenda mbali na Mchungaji kurudishwa karibu naye tena. Lazima mwenye kwenda mbali arudi tena kwa nyumba ya Baba yake.

**16:8** Wanawake **walikimbia toka pahali pa kaburi** na shituko na woga mkubwa. Waliogopa kabisa kumwambia mtu ye yote habari za maneno yaliyotokea. Hatuwezi kushangaa juu ya ile. Neno la kushangalisha ndilo uhodari na mapendo yao kufika sasa.

Marko 16:9-20 yanakosa ndani ya miigo miwili ya kujulikana, na wenye elimu nyingi wa wakati wa sasa wanafikiri kwamba mashairi haya si kweli sehemu ya Habari Njema ya Marko. Lakini kuna sababu nyingi kwa kusema kwamba ni kweli sehemu ya kitabu hiki:

1. Mashairi haya ni ndani ya maandiko karibu yote mengine kwa Kiyunani, na ya viongozi wengi vya kanisa.
2. Isingalikuwa vizuri kumaliza kitabu hiki na shairi 8, kwani neno la mwisho la shairi hili kwa Kiyunani ni *gar*, maana yake *kwani.* Si njia nzuri kumaliza kitabu.
3. Wengine wanafundisha ya kwamba mashairi haya ya mwisho ya Marko yamepotea. Kama neno hili lingalikuwa kweli kama maneno ya Bwana juu ya kulinda Neno lake milele yasingalitimizwa. Ona Matayo 24:35.
4. Maneno yanayoandikwa katika mashairi haya yanapatana na imani ya Ukristo.
5. Namna yalivyoandikwa, na maneno yaliyotumiwa, yanalingana na namna Marko alivyoandika sura yake ya kwanza.

### B. Kuonekana kwa Mwokozi kwa Maria Magdalene (16:9-11)

**16:9** Mwokozi alionekana kwanza kwa **Maria Magdalene**. Mara ya kwanza Yesu aliyoonekana na Maria aliondosha **pepo wachafu saba** waliokaa ndani yake. Tangu siku ile Maria alimtumikia na mapendo na vitu vyake. Aliona kusulibishwa kwake, na pahali mwili wake ulipowekwa.

Ndani ya vitabu vingine vya Habari Njema tunasoma ya kwamba wakati alipokuta kaburi tupu, alikimbia kujulisha Petro na Yoane. Walirudia pahali pa kaburi pamoja naye, wakalikuta tupu, kama alivyosema. Walirudia nyumba zao, lakini Maria alibaki karibu na kaburi. Ni pale Yesu alipoonekana kwake.

**16:10,11 Alirudi tena** mjini kupasha habari hizi njema kwa wanafunzi wenye huzuni. Lakini **hawakuziamini.**

### C. Kuonekana kwa Mwokozi kwa wanafunzi wawili (16:12,13)

**16:12** Tunasoma habari nzima juu ya tukio hili katika Luka 24:13-31. Hapa tunasoma ya kwamba **alitokea** wanafunzi **wawili na sura nyingine,** kwa njia inayokwenda Emau. Kwa Maria ali-

onekana kama mlimaji. Sasa kwa watu hawa wawili alionekana kama msafiri mwenzao. Lakini alikuwa Yesu mwenyewe tu, katika mwili wake wa utukufu.

**16:13** Wakati wanafunzi wale waliporudia Yerusalema walipasha habari za kukutana kwao na Mwokozi aliyekuwa amefufuliwa, lakini watu hawakuamini habari zao, kama vilevile walikuwa wamekataa kuamini Maria.

### D. Kuonekana kwa Mwokozi kwa wanafunzi kumi na mmoja (16:14-18)

**16:14** Alionekana kwa wanafunzi **kumi na mmoja** mangaribi siku ya kwanza ya juma ile ile (Lk. 24:36; Yn. 20:19-24; 1 Kor. 15:5). Hata tukisoma juu ya wanafunzi **kumi na mmoja,** wanafunzi kumi tu walikuwa pale kwa wakati ule. Tomasi hakuwa pamoja nao mara ile. Yesu alikemea wanafunzi juu ya kukataa kuamini habari za Maria na wengine juu ya ufufuko wake.

**16:15** Ndani ya shairi 15 tunasoma agizo Bwana alilotoa mangaribi mbele ya kupanda kwake mbinguni. Hivi muda ulikuwa umepita nyuma ya kuonekana kwake katika shairi 14 na shairi 15. Aliagiza wanafunzi **kuhubiri Habari Njema** kwa kila mtu katika dunia nzima. Mwokozi alitaka kwa dunia nzima kusikia Habari Njema, na alikusudi kufanya hivi kwa njia ya kutumika na wanafunzi kumi na mmoja watakaoacha vyote kwa kumfuata yeye.

**16:16** Kwa sababu ya mahubiri haya wengine wataamini na **kubatizwa** na **kuokolewa,** na wengine watakosa imani na **watahukumiwa.**

Watu wengine wanatumika na shairi 16 kufundisha ya kwamba ni lazima kwa mtu kubatizwa kwa maji kwa kupata wokovu. Tunajua hii si maana yake kwa sababu:

1. Mnyanganyi juu ya msalaba hakubatizwa, lakini Yesu aliahidi ya kwamba atakuwa katika Paradiso pamoja naye (Luka 23:43).
2. Watu wa Mataifa katika Kaisaria walibatizwa *nyuma* ya kuokolewa (Matendo 10:44-48).
3. Kwa sababu gani Yesu hakubatiza watu yeye mwenyewe, kama ubatizo ukiwa neno la lazima kwa wokovu (Yoane 4:1,2)?
4. Paulo alishukuru Mungu kwa sababu alibatiza Wakorinto wachache tu (1 Wakorinto 1:14-16). Asingalitoa mashukuru namna hii kama ubatizo ni sehemu ya lazima ya wokovu.
5. Tunasoma kwa pahali karibu 150 ndani ya Agano Jipya ya kwamba watu wanaweza kupata wokovu kwa njia ya imani tu. Hakuna shairi, au mashairi machache yangaliweza kukana ushuhuda mkubwa sana namna hii.
6. Tunasoma juu ya ubatizo pamoja na mauti na maziko katika Agano Jipya, si pamoja na kuzaliwa tena katika roho.

Basi, kama ni hivi, maana ya shairi 16 ni nini? Tunafikiri ubatizo ni tangazo kwamba mtu ameamini. Si tendo la lazima kwa mtu kupata wokovu.

**16:17,18** Yesu anasema hapa juu ya alama nyingine yatakayofuatana nao wanaoamini Habari Njema. Wakati tunaposoma maneno haya tunajiuliza: “Tunaona alama hizi leo?” Tunafikiri **alama hizi** zilikuwa zaidi kwa muda wa mitume, mbele ya kuandikwa na kuchapwa kwa Biblia nzima. Tunaona zaidi yao ndani ya Kitabu cha Matendo:

1. **Kutokeza pepo** (Matendo 8:7; 16:18; 19:11-16).

2. **Lugha mpya** (Matendo 2:4-11; 10:46; 19:6).
3. **Shika nyoka** (Matendo 28:5).
4. **Kunywa sumu** bila kuumizwa nayo – hatusomi juu ya neno hili ndani ya Matendo, lakini Eusebius aliyeandika historia ya mwanzo wa kanisa aliandika habari hizi juu ya Yoane na Barnaba.
5. **Weka mikono juu ya wagonjwa** wapate kupona (Matendo 3:7; 19:11; 28:8,9).

Kusudi la alama hizi lilikuwa nini? Tunafikiri jibu la ulizo hili ni ndani ya Waebrania 2:3,4. Wakati Agano Jipya lisipoandikwa na kuchapwa bado yote, watu waliuliza mitume na wengine kuhakikisha ya kwamba Habari Njema inatoka kweli kwa Mungu. Kuhakikisha mahubiri yao Mungu alishuhudu pamoja nao kwa alama, na maajabu, na kwa zawadi nyingine za Roho Mtakatifu.

Alama hizi hazihitajiwi tena sasa kwani tuna Biblia nzima. Kama watu wakikataa kuamini Biblia, hawataamini alama vilevile. Marko *hakusema* ya kwamba alama hizi zitaendelea daima. Maneno haya, "hata mwisho wa dunia," *hayaonekani hapa* kwa sababu yaliandikwa kwa Matayo 28:18-20.

Lakini mwalimu mkubwa wa zamani, Martin Luther, alifikiri "ingepasa kutumika na alama hizi kama ikihitajiwa, mbele ya kuacha Habari Njema kusingiziwa na kuangushwa."

**E. Mtumishi anapanda kwa mkono wa kuume wa Mungu (16:19,20)**

**16:19** Siku makumi ine nyuma ya ufufuko wake **Bwana** wetu Yesu Kristo **alichukuliwa juu mbinguni, akaketi kwa mkono wa kuume wa Mungu**, ndipo pahali pa heshima na uwezo.

**16:20** Wanafunzi wake walitii agizo lake, **wakakwenda** na roho zilizowaka na kuhubiri Habari Njema na kupata watu kwa Mwokozi. Uwezo wa **Bwana** ulikuwa **pamoja nao**. **Alama** alizoahidi mbele **zilithibitisha mahubiri** yao.

Tumefikia mwisho wa habari zilizoandikwa na Marko – na Kristo mbinguni, na wanafunzi wachache waaminifu duniani wenye mzigo rohoni kwa dunia nzima kusikia Habari Njema. Walijitoa kabisa kwa kazi hii na kuzaa matunda ya kukaa milele.

Sisi tumewekewa amana kazi ya kuhubiri Habari Njema kwa watu wa kizazi chetu. Kazi yetu ni kujulisha kila mtu Habari Njema. Sehemu moja ya mbili ya watu walioishi duniani tangu mwanzo ni hai wakati wa sasa. Kwa kipimo hesabu yao inaongezeka, kazi ya kuhubiri Habari Njema pahali pote duniani inaongezeka vilevile. Na kwa kazi hii kubwa wafuata wenye kujitoa mzima kwa Kristo wanahitajiwa, wenye mapendo bila kipimo, walio tayari kuishi maisha yao mazima kwa yeye.

Ni mapenzi ya Mungu kwa watu wote wa dunia kusikia Habari Njema. Wewe na mimi tunafanya nini kusaidia kazi hii kubwa?

## NOTES

[1] (1:31) J.R. Miller, *Come Ye Apart,* Reading for March 28.

[2] (3:13-18) James E. Stewart, *The Life and Teaching of Jesus Christ,* pp. 55,56.

[3] (3:20,21) Miller, *Come,* Reading for June 6.

[4] (6:31,32) William Kelly, *An Exposition of the Gospel of Mar*k, p.85.

[5] (7:2-4) E. Stanley Jones, *Growing Spiritually,* p. 109.

[6] (7:11-13) Kelly, Mark, p. 105.

[7] (8:1-9) Charles Erdman, *The Gospel of Mark,* p. 136.

[8] (8:32-33) Kelly, *Mark,* p. 136.

[9] (10:31) Harry A. Ironside, *Expository Notes on the Gospel of Mark*, p. 157.

[10] (10:32 Erdman, *Mark*, p. 147.

## BIBLIOGRAPHIE

Alexander, Joseph Addison. *The Gospel According to Mark,* Edinburgh: The Banner of Truth Trust, 1960

Coates, C.A. *An Outline of Mark's Gospel and other Ministry*, Kingston-on-Thames: Stow Hill Bible and Tract Depot, 1964.

Cole, Alan. *The Gospel According to St. Mark*. Grand Rapids: Wm. B. Eerdmans Publishing Company, 1961.

Erdman, Charles R. *The Gospel of Mark*. Philadelphia: The Westminster Press, 1917.

Ironside, Harry A. *Expository Notes on the Gospel of Mark.* Neptune, N.J.: Loizeaux Brothers, 1948.

Kelly, William. *An Exposition of the Gospel of Mark.* London: C.A. Hammond, 1934.

Lenski, R. C. H. *The Interpretation of St. Mark's Gospel*. Minneapolis: Augsburg Publishing House, 1946.

Swete, Henry Barclay. *The Gospel According to St. Mark*. London: Mac-

# HABARI NJEMA KAMA ALIVYOANDIKA
# LUKA

## Utangulizi

*"Le plus beau livre qu'il y ait"* – Ernest Renan

### I. Nafasi ya pekee katika Kanuni

**"**Kitabu hiki ni kizuri kupita vitabu vyote" ni masemo ya sifa kubwa ya mjuzi wa kupima uzuri, Mfaransa, jina lake Renan, msiyeamini, juu ya Habari Njema ya Luka. Na hakuna *mwamini wa kweli* angalitaka kukana maneno haya. Tunafikiri Luka alikuwa Mtaifa wa pekee aliyechaguliwa na Mungu kuandika sehemu ya Maandiko yake.

Habari Njema ya Luka inaongeza sana ufahamu wetu wa uzuri wa Bwana Yesu na kazi yake. Tunaona mapendo ya Bwana wetu kwa watu wote, si kwa Wayuda tu, na kutaka kwake kwa wote kuokolewa. Tunamwona akiweka roho juu ya watu mmoja mmoja, watu masikini na watu wanaokataliwa na wengine. Luka anatufundisha vilevile juu ya sifa, (na tunaona nyingine za nyimbo za kwanza za Wakristo ndani ya sura 1 na 2), na maombi, na Roho Mtakatifu.

### II. Mwandishi

Luka alikuwa mtu wa Antiokia na mganga. Alikuwa mwenzi wa Paulo kwa muda mrefu. Alisemezana sana na mitume wengine, na ndani ya vitabu viwili alituachia sehemu za dawa ya roho aliyokuwa amepata kwa njia yao.

Zaidi ya walimu wa zamani walifikiri kitabu cha tatu cha Habari Njema kiliandikwa na Luka. Watu wa zamani wenye kujulikana waliofikiri Luka ni mwandishi wa Habari Njema ya tatu walikuwa Justin Martyr, Hegesippus, Clement wa Alesanduria, na Tertullian. Luka ndiyo Habari Njema ya pekee iliyokubaliwa na yule Marcion, mzushi wa kujulikana wa wakati ule.

Luka ndiye mwandishi wa pekee wa Habari Njema aliyeandika kitabu kingine kuongeza juu ya kitabu chake cha Habari Njema. Ni kitabu cha Matendo kinachoonyesha wazi zaidi ya kwamba vitabu hivi viwili viliandikwa na Luka. Kila mara ndani ya Matendo tunayosoma "sisi" tunafahamu ya kwamba Luka alikuwa palepale yeye mwenyewe. Ona Matendo 16:10; 20:5,6; 21:15; 27:1; 28:16 pamoja na 2 Timoteo 4:11. Maneno yaliyoandikwa kwa Teofilo, na namna yalivyoandikwa, yanaonyesha wazi ya kwamba vitabu vya Luka na Matendo viliandikwa na mwandishi mmoja.

Paulo aliita Luka "mganga mpendwa" na alitaja jina lake mbali na Wakristo Wayuda (Kol.4:14), ndilo neno linaloonyesha ya kwamba yeye alikuwa mwandishi wa pekee aliyekuwa mtu wa Mataifa katika Agano Jipya. Vitabu vya Luka na Matendo ni virefu kupita barua zote za Paulo pamoja.

Masemo ambayo Luka alitumika nayo ndani ya maandiko yake (hata maneno ya uganga) pamoja na namna ya maandiko haya, ndiyo ya Myunani mwenye kujifunza, yanathibitisha ya kwamba vitabu hivi viliandikwa na mganga Mkristo, mtu wa Mataifa aliyejuana sana na maneno na desturi za Wayuda. Alipenda kutaja wazi tarehe za matukio mbalimbali (ona 1:1-4; 3:1; vivi hivi) na alikuwa mtu wa kwanza aliyeandika juu ya historia ya kanisa.

### III. Tarehe

Watu wametaja tarehe mbalimbali (75-85 A.D. au hata nyuma kupita). Tunafikiri Habari Njema ya Luka iliandikwa karibu na 60-65 A.D., mbele ya kutimizwa kwa unabii wa Kristo juu ya kuharibiwa kwa Yerusalema 70 A.D.

Karibu walimu wote wanakubali ya kwamba Habari Njema ya Luka kiliandikwa mbele ya Matendo. Matendo kilikwisha karibu na 63 A.D. wakati Paulo alipokuwa katika Roma, hivi Luka kiliandikwa mbele ya tarehe ile. Mwandishi wa Habari Njema hii hakutaja moto mkubwa katika Roma uliotangulia mateso ya Wakristo ambao walihukumiwa na Nero kwa makosa wasiyofanya (64 A.D.). Hakutaja vilevile habari za uuaji wa Petro na Paulo kwa imani yao, hivi tunafikiri Luka kiliandikwa 61-62 A.D.

### IV. Msingi na Jambo Kubwa

Wayunani walitazamia mtu aliye Mungu – mwenye tabia kamilifu ya wanaume na wanawake, lakini bila upungufu wao. Hii ndiyo namna Luka alituonyesha Kristo, Mwana wa watu – mwenye nguvu, lakini mwenye huruma vilevile. Utu wake unaonekana sana ndani ya Luka.

Tunasoma hapa juu ya maombi yake kupita ndani ya vitabu vingine vya Habari Njema. Tunamwona tena na tena kama mwenye huruma na mwenye kushiriki ndani ya taabu ya wengine. Labda kwa sababu hii tunasoma tena na tena juu ya wanawake na watoto. Kitabu hiki kinajulikana vilevile kama Habari Njema ya kueneza Injili. Hapa tunaona Habari Njema ikihubiriwa kwa watu wa Mataifa vilevile na tunaona Bwana Yesu kama Mwokozi wa dunia. Na mwishoni Habari Njema ya Luka ni kitabu kutufundisha kuwa mfuasi wa kweli wa Kristo. Tunaona maneno haya ndani ya maisha ya Bwana wetu mwenyewe na tunasoma juu yake akiyafundisha kwa wanafunzi. Tunakusudi kuwaza zaidi juu ya neno hili ndani ya maelezo yetu ya kitabu hiki. Ndani ya maisha ya Mtu Mkamilifu, ndiye Yesu, tunaona mifano ya mambo yanayohitajiwa ndani ya maisha ya kila mtu. Na masemo yake yatatufundisha juu ya njia ya msalaba ambayo inatupasa kufuata.

Wakati tunapoanza kujifunza Habari Njema ya Luka tunataka sana kusikia Mwokozi wetu akituita kuacha vyote na kumfuata. Kwa njia ya kumtii tutaendelea kujuana naye, na maana ya Maandiko inageuka wazi kupita kwetu.

## HABARI YALIYOMO


1. MWANZO: KUSUDI LA LUKA NA NAMNA YA KUANDIKA KWAKE (1:1-4)
2. KUFIKA KWA MWANA WA WATU NA MTANGULIZI WAKE (1:5–2:52)
3. MATAYARISHO KWA MWANA WA WATU KWA UTUMISHI WAKE (3:1–4:30)
4. MWANA WA WATU ANAHAKIKISHA UWEZO WAKE (4:31–5:26)
5. MWANA WA WATU ANAELEZA UTUMISHI WAKE (5:27–6:49)
6. MWANA WA WATU ANAENEZA UTUMISHI WAKE (7:1–9:50)
7. MAZUIZO KWA UTUMISHI WA MWANA WA WATU YANAONGEZEKA (9:51–11:54)
8. NJIANI KWENDA YERUSALEMA MWANA WA WATU ANAFUNDISHA NA KUPONYESHA WATU (Sura 12-16)
9. MWANA WA WATU ANAFUNDISHA WANAFUNZI WAKE (17:1–19:27)
10. MWANA WA WATU KATIKA YERUSALEMA (19:28–21:38)
11. MAUMIVU MAKALI YA MWANA WA WATU NA MAUTI YAKE (Sura 22, 23)
12. KUSHINDA KWA MWANA WA WATU (Sura 24)

# Maelezo

## 1. MWANZO: KUSUDI LA LUKA NA NAMNA YA KUANDIKA KWAKE (1:1-4)

Luka alianza maandiko yake kwa njia ya kuonyesha pahali wapi alipopata habari kwa kuandika Habari Njema yake na kwa sababu gani na namna gani aliandika. Alipata habari zake toka maandiko ya watu wengine juu ya maisha ya Kristo, na karibu na watu wengine walioona na macho yao wenyewe maneno yaliyotokea ndani ya maisha yake.

**1:1** Luka alisema juu ya maandiko haya, **"Kwa sababu watu wengi wametia mikono yao kutengeneza habari za maneno yale yaliyotimizwa katikati yetu …"** Hatujui kama alisema juu ya watu gani. Labda wawili walikuwa Matayo na Marko, lakini wengine hawakuongozwa na Roho Mtakatifu. (Yoane aliandika Habari Njema yake nyuma.)

**1:2** Luka alitumika vilevile na habari za **wale waliokuwa tangu mwanzo washuhuda na watumishi wa lile neno.** Luka hakusema ya kwamba yeye mwenyewe alikuwa mmoja wa washuhuda wale lakini alisemezana na wengine katikati yao. Aliita watu hawa **"washuhuda na watumishi wa lile neno."** Alitumika hapa na **neno** kama jina moja la Kristo, kama Yoane alivyofanya vilevile ndani ya Habari Njema yake. **Mwanzo** hapa ni muda ulioanza na kuzaliwa kwa Kristo uliotangazwa na Yoane Mbatizaji. Luka alitumika na habari alizosikia na kusoma, lakini hata hivi maneno aliyoandika yaliongozwa na Roho Mtakatifu. Ni Roho Mtakatifu ambaye alimwongoza nini ilimpasa kuandika na kama ilimpasa kufuata taratibu gani.

**1:3** Luka anaonyesha vilevile kwa ufupi kwa nini aliandika maneno haya: "**niliona vema vilevile, kwa sababu nilifuata habari za kweli ya yote tangu mwanzo, kukuandikia kwa taratibu, Teofilo, mwenye heshima."** Sababu ya kuandika kwake ilikuwa nini? "**Niliona vema vilevile."** Akiwa mtu alifahamu ndani ya roho yake ya kwamba ilimpasa kuandika Habari Njema hii. Na tunajua ya kwamba aliongozwa na Mungu ndani ya neno hili vilevile.

Alitafuta kwanza **habari za kweli ya yote**, **tangu mwanzo**, kisha aliandika zote kwa taratibu. Alitafuta maneno haya yote karibu karibu, akiondosha habari zote zisizopatana na historia na zisizokuwa na faida kwa roho. Kisha aliandika habari hizi zote **kwa taratibu**. Hiki ndicho kitabu cha Habari Njema tunachoshika mikononi mwetu leo. Wakati Luka aliposema aliandika yote **kwa taratibu**, si kusema aliandika kwa taratibu ya miaka, lakini kwa taratibu ya roho, maana alikutanisha pamoja mafundisho juu ya neno fulani ya roho. Alituma Habari Njema hii na kitabu cha Matendo kwa **Teofilo,** lakini tunajua maneno machache tu juu ya mtu huyu. Luka alimwita **mwenye heshima,** hivi labda alikuwa mtu wa serikali. Maana ya jina lake ni *rafiki ya Mungu*. Tunafikiri alikuwa Mkristo aliyekuwa na kazi kubwa na ya heshima ndani ya moja ya inchi za ufalme wa Roma.

**1:4** Luka alitaka kumpa Teofilo *mwandiko* wa maneno yaliyotokea kuhakikisha kweli ya maneno yote aliyofundishwa juu ya maisha na utumishi wa Bwana Yesu. Maandiko haya yatachunga habari hizi bila kugeuzwa kwa wakati wa kuja kupita habari zinazopitishwa kwa njia ya masemo tu.

Hivi ndani ya mashairi 1-4 tunapata habari za faida kutusaidia kufahamu hali ya dunia wakati kitabu hiki kilipoandikwa. Tunajua Luka alikuwa akiongozwa na Mungu ndani ya maneno aliyoandika. Hasemi juu ya neno hili

hapa isipokuwa yalikuwa ndani ya mawazo yake wakati aliposema juu ya *tangu mwanzo*. Maneno haya mawili yanaweza kutafsiriwa vilevile *toka juu*[1].

## 2. KUFIKA KWA MWANA WA WATU NA KWA MTANGULIZI WAKE (1:5 – 2:52)

### A. Kuzaliwa kwa Yoane Mbatizaji kunatabiriwa (1:5-25)

**1:5,6** Luka anatupasha kwanza juu ya wazazi wa Yoane Mbatizaji. Waliishi wakati **Herode** Mkubwa aliyekuwa mtu mwovu sana alipokuwa **mfalme** wa **Yudea.** Alikuwa mtu wa Idumea, maana yake mzao wa Esau.

**Zakaria** (maana ya jina lake ni *Bwana anakumbuka*) alikuwa **kuhani** wa zamu ya Abiya, moja ya mafungu 24 ya makuhani ya Wayuda ambayo Daudi alisimamisha (1 Mambo 24:10). Watu wa kila fungu walitumikia hekaluni katika Yerusalema mara mbili kila mwaka, toka sabato moja kufika sabato nyingine. Kulikuwa na makuhani wengi sana kwa wakati ule, na wengine hawakupewa heshima ya kuteketeza uvumba katika Pahali Patakatifu hata mara moja ndani ya maisha yao mazima.

**Elisabeti** (maana ya jina lake ni *kiapo cha Mungu*) alikuwa mzao wa jamaa ya kuhani vilevile, ndiyo jamaa ya **Haruni.** Yeye na mume wake walikuwa Wayuda waaminifu sana. Waliweka roho kabisa juu ya kutii Maandiko ya Agano la Kale karibu karibu ndani ya kuabudu na mwenendo wao. Ndiyo, walikuwa wenye zambi, lakini wakati walipofanya zambi walitoa sadaka au kufanya neno lo lote lingine lililoagizwa.

**1:7** Zakaria na Elisabeti *hawakuwa na watoto*, ndilo hali ya haya kwa Myuda ye yote. Mganga Luka alieleza ya kwamba Elisabeti alikuwa tasa. Zaidi ya ile **wao wawili walikuwa wazee sana**.

**1:8-10** Siku moja Zakaria alikuwa akifanya kazi yake ya kuhani **hekaluni**. Ilikuwa siku kubwa ndani ya maisha yake kwa sababu alikuwa amechaguliwa kwa njia ya kura **kuchoma uvumba** katika pahali patakatifu. **Makutano** yote ya watu walikuwa **wakiomb**a **inje** ya hekalu. Hatujui kama **saa ya kuchoma uvumba** ilikuwa saa gani.

Ona ya kama kwa mwanzo wa kitabu hiki cha Habari Njema tunaona **watu wakiomba** kwa hekalu na kwa mwisho wake tunaona watu wakisifu Mungu kwa hekalu. Ndani ya sura 2 kufika 23 tunasoma juu ya majibu ya maombi yao kwa njia ya Bwana Yesu na kazi yake.

**1:11-14** Wakati makuhani na watu walipokuwa wakiomba ilikuwa saa nzuri kwa ufunuo toka Mungu. **Malaika ya Bwana alitokea kwa upande wa kuume wa mazabahu** – pahali pa upendeleo. **Zakaria** aliogopa sana; makuhani wenzake hawakuona malaika kamwe. Lakini malaika alimwondolea mashaka na habari za ajabu. **Elisabeti** atazaa **mwana**. Jina la mwana huyu litakuwa **Yoane** (maana ya jina hili ni *neema ya Yehova)*. Ataleta **furaha na shangwe** kwa wazazi wake, na zaidi ya ile atakuwa baraka kwa **watu wengi.**

**1:15** Mtoto huyu atakuwa mkubwa mbele ya Bwana (ukubwa wa pekee ulio na faida). Kwanza, atakuwa mkubwa kwa njia ya kujitenga na maneno ya dunia na kuishi kwa Bwana; hatakunywa **mvinyo** (inayofanywa na zabibu) **wala malofu** (inayofanywa na nafaka).

Neno la pili, atakuwa mkubwa kwa sababu **atajazwa Roho Mtakatifu, hata toka tumbo la mama yake**. (Si kusema ya kwamba Yoane aliokolewa tangu kuzaliwa kwake, lakini ya kwamba Roho ya Mungu alikuwa ndani yake tangu mwanzo kumtayarisha kwa kazi yake, ndiyo kuwa mtangulizi wa Kristo.)

**1:16,17** Atakuwa mkubwa kama mtangulizi wa Masiya. **Atageuza** roho za

**Wayuda wengi** kwa Bwana. Utumishi wake utafanana na ule wa nabii Elia, na atajaribu kuleta watu karibu na Mungu kwa njia ya toba. Kama G. Coleman Luck alivyoonyesha:

> Mahubiri yake yataamsha ndani ya roho za wazazi mashaka juu ya hali ya roho ya watoto wao. Vilevile atarudisha roho za watoto waasi kwa "akili ya wenye haki."[2]

Maana yake, atajaribu kukutanisha toka watu wa dunia kundi la waamini watakaokuwa tayari kukutana na Bwana wakati atakapofika. Huu ndio utumishi wa faida kwa sisi sote.

Ona vilevile namna tunavyoona uungu wa Kristo kwa maficho ndani ya mashairi 16 na 17. Ndani ya shairi 16 tunasoma ya kwamba Yoane **atarudisha wana wengi wa Israeli kwa Bwana Mungu wao**. Halafu ndani ya shairi 17 tunaona ya kwamba Yoane **atamtangulia**. Atatangulia nani? Ni wazi ya kwamba alikuwa akisema juu ya *Bwana Mungu wao* (sh.16). Lakini tunajua ya kwamba Yoane alikuwa mtangulizi wa *Yesu*. Maneno haya yanaonyesha wazi ya kwamba Yesu ni Mungu.

**1:18** Mzee **Zakaria** alishangaa sana sana wakati alipowaza juu ya ahadi hii ya neno lisilowezekana hata kidogo kwa watu. Yeye na **mke** wake walikuwa na **miaka mingi kupita** kuweza kuzaa mtoto. Ulizo lake lilionyesha shaka lililojaza roho yake.

**1:19** Malaika alijibu kwa njia ya kumwambia Zakaria kwanza jina lake, ndilo Gabrieli (*mwenye nguvu wa Mungu*). Mara nyingi watu wanamwita malaika mkuu, lakini ndani ya Maandiko anaitwa kila mara **anayesimama mbele ya Mungu** na kuleta habari toka Mungu kwa watu (Dan. 8:16; 9:21).

**1:20** Kwa sababu Zakaria alikuwa na shaka, hataweza kusema maneno tena kufika wakati mtoto atakapozaliwa. Kila mara mwamini ana shaka juu ya neno la Mungu, ushuhuda na furaha zake zinapotea. Kutokuamini kunafunga midomo yake kufika wakati imani yake inaporudi naye anasifu na kushuhudia Mungu tena.

**1:21, 22** Inje ya hekalu **watu** walingoja, na saburi yao ilitaka kwisha. Haikuwa desturi kwa kuhani aliyechoma uvumba kukawa saa ndefu hivi. Wakati mwishoni **Zakaria alipotoka,** ilimpasa kuonyesha mafikiri yake kwa njia ya kupungia mkono. Halafu watu **walifahamu** ya kwamba **alikuwa ameona ono hekaluni.**

**1:23** Wakati kazi yake hekaluni **ilipokwisha** Zakaria alirudi kwake, lakini hakuweza kusema neno, kama malaika alivyotabiri.

**1:24,25** Wakati **Elisabeti** alipopata mimba alijificha kwa **miezi mitano**, akifurahi ndani ya roho yake kwa sababu ilipendeza **Bwana** kuondosha **haya** yake ya kuwa tasa.

### B. Kuzaliwa kwa Mwana wa watu kunatabiriwa (1:26-38)

**1:26, 27** **Katika mwezi wa sita** nyuma ya kutokea kwa Zakaria (au nyuma ya Elisabeti akipata mimba) **Gabrieli** alitokea tena – mara hii kwa **bikira**, jina lake **Maria** aliyekaa katika mji wa Galilaya ulioitwa **Nazareti.** Maria **alipatana kuwa mke wa mtu aliyeitwa Yosefu,** mzao wa **Daudi.** Ilikuwa haki ya Yosefu kuriti kiti cha ufalme cha Daudi, hata kama yeye mwenyewe alikuwa seremala. Kwa wakati ule upatano kuoana ulikuwa agano la nguvu katikati ya mume na mke. Kuvunja upatano ule kulihitaji amri ya sheria, kama amri juu ya kuachana.

**1:28** **Malaika** alisalimu Maria kama mwenye **kubarikiwa** sana na Bwana. Tuone maneno mawili hapa: (1) Malaika *haku*abudu Maria, *wala* kumtolea maombi. Alimsalimu tu. *Hakusema* ya kwamba Maria "amejaa neema," lakini

ya kwamba **amebarikiwa**.

**1:29,30** Hatushangai kuona kwamba Maria alifazaika sana juu ya salamu ile na maana yake. **Malaika** alituliza woga wake, kisha alimwambia ya kwamba **Mungu** alikuwa amemchagua kuwa mama ya Masiya ambaye watu walingoja kufika kwake tangu miaka mingi.

**1:31-33** Ona kweli kubwa zinazofichwa ndani ya tangazo hili:

Utu wa Masiya – **utapata mimba, utazaa mwana.**

Uungu wake na ujumbe wake kuwa Mwokozi – **na utaita jina lake YESU** (maana yake *Yehova ni Mwokozi*).

Ukubwa wake – **atakuwa mkubwa,** yeye mwenyewe na kazi yake.

Yeye ni nani, ndiye Mwana wa Mungu – **ataitwa Mwana wake Mungu aliye juu.**

Haki yake kwa kiti cha ufalme cha Daudi – **Bwana Mungu atampa kiti cha baba yake Daudi**. Neno hili linamsimamisha kama Masiya.

Ufalme wake wa milele juu ya ulimwengu mzima – **atamiliki nyumba ya Yakobo hata milele; na ufalme wake hautakuwa na mwisho**.

Ni wazi ya kwamba mashairi 31 na 32 yanasema juu ya kuja kwa kwanza kwa Kristo, na mashairi 32b na 33 ni juu ya kuja kwake kwa pili kama Mfalme wa wafalme na Bwana wa wabwana.

**1:34,35** Ulizo la Maria, **"Neno hili litakuwa namna gani?"** linaonyesha kushangaa kwake, si shaka yake. **Namna gani** ataweza kuzaa mwana kama hakujua **mume**? Hata kama malaika hakusema hivi wazi, jibu lake kwa ulizo la Maria lilikuwa: atazaa mwana hata *akikuwa bikira*. Itakuwa ajabu la **Roho Mtakatifu** atakayekuja **juu yake**, na **nguvu za** Mungu zitamtulia kivuli. Ndiyo, Maria aliuliza: "**Namna gani**?" – lilionekana kama neno lisilowezekana kwa watu – jibu la Mungu lilikuwa "Roho Mtakatifu":

**"Kwani kile kitu ambacho kitazaliwa nawe kitaitwa kitakatifu, Mwana wa Mungu."** Hapa ni tangazo bora sana kwamba Yesu Kristo atafanyika mtu. Mwana wa Maria atakuwa Mungu akionekana kama mtu. Sisi watu hatutaweza kamwe kufahamu na kueleza siri hii kubwa.

**1:36,37** Halafu malaika alimwambia Maria ya kwamba miezi sita ilikuwa imepita tangu Elisabeti, aliyekuwa tasa mbele, wa jamaa yake, alipata mimba. Ajabu hili liliweza kuondolea Maria mashaka ya kwamba **hakuna neno lisilowezekana kwa Mungu.**

**1:38** Na unyenyekevu mzuri sana **Maria** alijitoa kwa Bwana aweze kutimiza makusudi yake ya ajabu. Kisha **malaika aliondoka kwake.**

### C. Maria anakwenda kuona Elisabeti (1:39-45)

**1:39,40** Biblia haisemi kwa sababu gani Maria alikwenda kuona Elisabeti kwa wakati huu. Labda alitaka kuepuka aibu katika Nazareti wakati watu walipoanza kutambua hali yake. Kama ilikuwa hivi, kukaribishwa na mapendo na Elizabeti kulikuwa tamu sana kwake.

**1:41** Mara moja wakati **Elisabeti aliposikia** sauti ya Maria, **mtoto aliruka tumboni mwa mama yake** – itiko la siri tusiloweza kufahamu la mtangulizi asiyezaliwa bado kwa Masiya asiyezaliwa bado. **Elisabeti alijazwa Roho Mtakatifu**, maana yake Roho Mtakatifu alimtawala, akiongoza masemo na matendo yake.

Tunasoma juu ya watu watatu wakijazwa Roho Mtakatifu ndani ya sura hii: Yoane Mbatizaji (sh.15). Elisabeti (sh. 41), na Zakaria (sh. 67). Neno moja linaloonyesha ya kwamba mtu anajazwa na Roho Mtakatifu ni uwezo wake kusemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za roho (Efe. 5:18,19). Hivi hatushangai kuona nyimbo tatu ndani ya sura hii na nyimbo mbili ndani ya sura

2. Ine za nyimbo hizi zinajulikana na majina ya Kiroma: ( 1) Salamu ya Elisabeti [1:42-45]; (2) *Magnificat* (unatukuza) [1:46-55]; (3) *Benedictus* (mwenye heri) [1:68-79]; (4) *Gloria in Excelsis Deo* (utukufu kwa Mungu aliye juu) [2:14], na (5) *Nunc Dimittis* (sasa unaruhusu ... kwenda) [2:29-32].

**1:42-45** Elisabeti aliongozwa na Mungu wakati aliposalimu Maria kama **"mama ya Bwana wangu."** Hakuwa na wivu hata kidogo moyoni mwake, lakini furaha kubwa tu kwa sababu mtoto huyu asiyezaliwa bado atakuwa **Bwana** wake. Maria **alibarikiwa katikati ya wanawake** kwa sababu alipewa mapendeleo ya kuzaa Masiya. **Uzao** wa **tumbo** lake **umebarikiwa** kwa sababu yeye ni Bwana na Mwokozi. Maria hakuitwa *kamwe* "mama ya Mungu" ndani ya Biblia. Ni kweli ya kwamba alikuwa mama ya Yesu, na ya kwamba Yesu ni Mungu, lakini ni elimu pumbavu kusema juu ya Mungu akiwa na mama, kwa sababu Yesu alikuwa tangu milele. Maria alikuwa kiumbe tu aliyekuwa na mwanzo hapa duniani. Alikuwa mama ya Yesu kwa saa Yesu alipotwaa utu tu.

Elisabeti alipasha juu ya furaha ya mtoto tumboni mwake wakati aliposikia sauti ya Maria mara ya kwanza. Halafu alisema na Maria ya kwamba imani yake itakuwa na zawabu kubwa. Maneno aliyotumaini yatatimizwa. Hakuamini bure. Mtoto wake atazaliwa kweli, kama Mungu alivyoahidi.

### D. Maria anatukuza Bwana (1:46-56)

**1:46-49** Magnificat unafanana na wimbo wa Hana (1 Sam. 2:1-10). Kwanza **Maria** alisifu **Bwana** kwa maneno **yeye** aliyokwisha kufanya kwaye (mash. 46b-49). Ona ya kwamba alisema ndani ya shairi 48 ya kwamba **"vizazi vyote wataniita heri."** Maria hataleta baraka kwa wengine *lakini yeye mwenyewe atabarikiwa*. Alisema juu ya **Mungu** kama **Mwokozi** wake, na kwa njia hii alionyesha wazi ya kwamba yeye mwenyewe alikuwa mwenye zambi.

**1:50-53** Alisifu Bwana vilevile kwa **rehema zake kwa wale ambao wanamwogopa** tangu **vizazi hata vizazi. Anashusha wenye kiburi na wakubwa** na anapandisha **wanyenyekevu** na kushibisha **wenye njaa.**

**1:54,55** Mwishoni alitukuza Bwana kwa uaminifu wake kwa **Israeli** na kutimiza ahadi alizotolea **Abrahamu na wazao wake.**

**1:56** Nyuma ya kushinda pamoja na Elisabeti **kwa karibu miezi mitatu** Maria **alirudi** kwa **nyumba yake** katika Nazareti. Hajakuolewa bado kwa wakati ule. Bila shaka watu walianza kumtazama na mashaka na kumsingizia, lakini aliweza kungojea siku Mungu atakapomthibitisha.

### E. Kuzaliwa kwa mtangulizi (1:57-66)

**1:57-61** Wakati saa ya **Elisabeti** ilipotimia, alizaa **mwana**. **Ndugu** zake na rafiki zake walifurahi sana. **Siku ya nane**, wakati **mtoto** alipotahiriwa, walifikiri ya kwamba bila shaka ataitwa **Zakaria** kama **baba yake**. Walifazaika wakati mama ya mtoto aliposema jina lake litakuwa **Yoane**, kwa sababu hakuna mtu katika **jamaa yake** aliyekuwa na **jina hili.**

**1:62,63** Basi **waliashiria** Zakaria kumwuliza. (Neno hili linaonyesha ya kwamba hakuwa bubu tu lakini kiziwi vilevile.) Wakati walipomletea **kibao cha kuandikia**, aliandika wazi ya kwamba **jina** la mtoto ni **Yoane.** Basi watu **wote walishangaa.**

**1:64-66** Lakini walishangaa hata kupita wakati walipoona ya kwamba Zakaria aliweza kusema tena mara moja nyuma ya kuandika "Yoane." Habari zilienea mbio mbio katika **inchi yote ya vilima vya Yudea,** na watu walifazaika juu ya kazi ambayo mtoto huyu ataka-

yofanya kwa wakati wa kuja. Walitambua ya kwamba **mkono wa Bwana ulikuwa pamoja naye.**

### F. Unabii wa Zakaria juu ya Yoane (1:67-80)

**1:67** Sasa **Zakaria** hakufungwa tena na matunda ya kutokuamini kwake, lakini **alijazwa Roho Mtakatifu.** Alitoa wimbo wa sifa uliotaja mashairi mengi toka Agano la Kale.

**1:68, 69** *Sifa kwa Mungu kwa maneno aliyokwisha kufanya.* Zakaria alifahamu ya kwamba kuzaliwa kwa mwana wake, Yoane, kulionyesha ya kwamba kufika kwa Masiya kulikuwa karibu. Alisema juu ya kufika kwa Masiya kama juu ya neno lililokwisha kutokea hata mbele ya kufika kwake. Imani yake ilimwongoza kusema ya kwamba **Mungu amekuja kwa watu wake, na kuwakomboa** kwa njia ya kutuma Mkombozi. Yehova alikuwa **amenyanyua pembe ya wokovu** katika **nyumba** ya kifalme **ya** … **Daudi**. (Watu waliweka mafuta kupakaa wafalme ndani ya pembe; hivi labda maana yake hapa ni *Mfalme* wa wokovu toka jamaa ya kifalme ya Daudi. Au labda ilikuwa alama ya uwezo, na hivi maana yake ni "Mwokozi mwenye uwezo.")

**1:70, 71** *Sifa kwa Mungu kwa sababu ya kutimizwa kwa unabii*. **Manabii watakatifu** walikuwa wametabiri **tangu mwanzo wa dunia** ya kwamba Masiya atakuja, na atawaokoa **toka adui** na hatari.

**1:72-75** *Sifa kwa Mungu kwa uaminifu wake na kutimiza ahadi zake.* Bwana alikuwa amefanya **agano** la wokovu bila masharti na **Abrahamu**. Ahadi hii ilitimizwa kwa njia ya kuja kwa mzao wa Abrahamu, ndiye Bwana Yesu Kristo. Alileta wokovu toka **adui zao**, na kuwawezesha **kumtumikia bila woga, katika utakatifu na haki.**

**1:76, 77** *Ujumbe wa Yoane, mtangulizi wa Mwokozi*. Yoane atakuwa **nabii** wa Mungu aliye juu, na atatayarisha mioyo ya watu kwa kuja **kwa Bwana**, na kutangaza **wokovu kwa watu wake** kwa njia ya usamehe wa **zambi zao.** Hapa tena tunaona mashairi yaliyo juu ya Yehova katika Agano la Kale yakisema juu ya Yesu ndani ya Agano Jipya. Malaki alitabiri juu ya mjumbe atakayetayarisha njia mbele ya Yehova (3:1). Zakaria alionyesha ya kwamba Yoane ndiye mjumbe huyu. Tunajua ya kwamba Yoane alikuja **kutayarisha** njia mbele ya Yesu. Hivi ni wazi ya kwamba Yesu ni Yehova.

**1:78, 79** *Kuja kwa Kristo kunasawanishwa na mapambazuko* (mwanga) *ya jua.* Kwa mia za miaka dunia ilikuwa katika giza. Sasa, **kwa sababu ya upole wa rehema ya Mungu wetu,** mapambazuko ya asubui yalikuwa karibu. Yatakuja kwa njia ya Kristo kuwaangazia wanaokaa **katika giza, na katika uvuli wa mauti**, na kuongoza miguu ya Israeli **katika njia ya salama** (ona Malaki 4:2).

**1:80** Kwa mwisho wa sura hii tunaona **mtoto akikua na kuongezeka** nguvu katika roho, na **akikaa katika pahali pasipo watu** hata siku ya kutokea kwake **kwa** taifa la **Israeli.**

### G. Kuzaliwa kwa Mwana wa watu (2:1-7)

**2:1-3 Kaisari Augusto alitoa amri kwa watu wote katika dunia kuandikwa. Maandiko haya** yalifanywa kwanza **wakati Kurenio alipokuwa mtawala wa Suria**. Kwa miaka mingi watu walikuwa na shaka juu ya usawa wa Habari Njema ya Luka kwa sababu ya maneno aliyoandika juu ya Kurenio. Kwa wakati wa nyuma yalihakikishwa kwa njia ya maarifa ya mambo ya kale. **Kaisari Augusto** alionyesha enzi yake ya utawala juu ya inchi za Yunani na Roma. Lakini kwa macho ya Mungu mfalme huyu aliyekuwa Mtaifa alikuwa

mtumishi tu mikononi mwake kutimiza shauri lake (ona Mez. 21:1).

**2:4-7** Amri ya Augusto ilifikisha **Yosefu na Maria** kwa **Betelehemu** kwa wakati uliofaa, ili Masiya aweze kuzaliwa pale na kutimiza unabii wa Mika 5:2. Kulikuwa na watu wengi sana katika Betelehemu wakati walipofika **toka Galilaya**. Pahali pa pekee walipoweza kupata kulala usiku palikuwa ndani ya zizi ya nyama ya **nyumba ya wageni.** Neno hili lilikuwa kama mfano wa namna watu watakavyopokea Mwokozi. Saa Maria na Yosefu walipokuwa pale Maria alizaa **Mwana wake wa kwanza**, akamfunika na **mavazi ya kitoto** na **kumlalisha** na mapendo **ndani ya sanduku ya kulisha nyama.**

Hivi Mungu alifikia dunia yetu kama mtoto mchanga katika umasikini wa zizi ya kununuka ya nyama. Ajabu kubwa sana. Darby aliandika hivi juu yake:

> Alianza maisha yake ndani ya sanduku ya kulisha nyama, na aliyamaliza juu ya msalaba, na tangu mwanzo kufika mwisho hakuwa na nafasi kulalisha kichwa chake.[3]

### H. Malaika na wachungaji kondoo (2:8-20)

**2:8** Watu wa kwanza ambao walijulishwa habari za ajabu za kuzaliwa kwa Mwokozi hawakuwa viongozi vya dini katika Yerusalema, lakini wachungaji kondoo vilimani mwa Yudea, watu wanyenyekevu waliofanya kazi yao ya kila siku na uaminifu. James S. Stewart aliandika maneno haya:

> Ndiyo, watu waliofanya kazi yao ya kila siku na uaminifu walikuwa wa kwanza kuona utukufu wa Bwana aliyetokea. Hivi tunaona ya kwamba pahali pa kazi, si neno kama ni kazi isiyo na heshima, ndipo pahali pa kujuana na maneno ya roho. Na vilevile ni watu wanaokaa na roho ya unyenyekevu, ya mtoto wanaofahamu maneno ya ufalme mbio zaidi.[4].

**2:9-11 Malaika ya Bwana** alitokea wachungaji, na nuru ya **kungaa** sana ya utukufu **iliwaangazia,** nao waliogopa sana. Lakini malaika aliwafariji na **habari njema sana ya furaha kubwa** kwa **watu wote**. **Siku** ile ile, katika Betelehemu, ndio mji wa karibu, Mtoto alikuwa **amezaliwa**. Mtoto huyu alikuwa **Mwokozi, ndiye Kristo Bwana**! Maneno haya machache yanatufundisha maneno makubwa mengi: Mtoto huyu alikuwa **Mwokozi,** kama maana ya jina lake, Yesu, inavyoonyesha. Naye ni **Kristo**, Mpakaliwa wa Mungu, Masiya wa Israeli. Mwishoni yeye ni **Bwana**, Mungu akionekana katika mwili.

**2:12** Wachungaji watamtambua namna gani? Malaika aliwapa **alama** yenye sehemu mbili: Kwanza wataona mtoto **amefungwa nguo za kitoto**. Walikuwa wameona watoto waliofungwa na nguo za kitoto mbele. Lakini malaika alikuwa ametangaza sasa tu ya kwamba Mtoto huyu alikuwa Bwana. Hakuna mtu aliyeona Bwana kama **mtoto mchanga aliyefungwa nguo za kitoto.** Sehemu ya pili ya alama ndiyo hii: watamkuta **akilala ndani ya sanduku ya kulisha nyama**. Hatufikiri wachungaji waliona mtoto mchanga ndani ya pahali pa namna hii mbele. Bwana wa uzima na utukufu tu alitendewa na aibu namna hii wakati alipozaliwa ndani ya dunia yetu. Ni neno la kuhangaisha nia zetu kuwaza juu ya Mwumba na Mwenye kutegemeza ulimwengu huu akitokea katikati ya watu, si kama mshindaji wa kujulikana, lakini kama **Mtoto mchanga**. Lakini hii ndiyo namna Mwumba na Bwana alikamata mwili wa mtu.

**2:13,14 Gafula** furaha kubwa sana za mbingu zilionekana. **Makutano makubwa ya jeshi la mbingu** walitokea **wakisifu** Mungu. Kwa wakati wa sasa watu wanaita wimbo wao *Gloria katika*

*Excelsis Deo*. Unaonyesha wazi maana ya kuzaliwa kwa Mtoto. Maisha na utumishi wake zitaleta **utukufu kwa Mungu aliye juu, na salama duniani, katika watu ambao wanampendeza.** Watu ambao wanampendeza ndio wale wanaokiri zambi zao na kutubu, na kupokea Yesu Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wao.

**2:15-19** Wakati **malaika** walipokwenda zao, **wachungaji** walikwendea **Betelehemu** mbio mbio**, wakakuta Maria na Yosefu, na Yesu akilala ndani ya sanduku ya kulisha nyama.** Walipasha habari za kufika kwa malaika na watu waliokwisha kukutana ndani ya nyumba ya ngombe, wakashangaa sana. **Lakini Maria** alifahamu maana ya **maneno haya yote** kupita watu wengine, akayaficha na **kuyafikiri moyoni mwake.**

**2:20 Wachungaji walirudia** makundi yao na furaha tele, wenye roho za kufurika na sifa na kutukuza Mungu, kwa maneno yote ambayo **walisikia na kuona.**

### I. Yesu anatahiriwa na kutolewa kwa Mungu (2:21-24)

Mashairi haya yanapasha juu ya kawaida tatu za dini:

1. **Kutahiriwa kwa** Yesu wakati alipokuwa na **siku nane**. Tohara ilikuwa alama ya agano Mungu alilofanya na Abrahamu. Siku ile **mtoto** alipewa jina, kufuatana na desturi ya Wayuda. Malaika alikuwa amesema na Maria na Yosefu kumwita **YESU**.

2. Kawaida ya pili ni maneno ya **kusafishwa** kwa Maria siku 40 nyuma ya kuzaliwa kwa Yesu (ona Law. 12:1-4). Ilikuwa desturi ya wazazi kuleta mwana-kondoo kwa sadaka ya kuteketezwa na hua au kinda la njiwa kwa sadaka ya zambi.

Lakini watu masikini walikuwa na ruhusa kuleta **"hua wawili au makinda ya njiwa wawili"** (Law. 12:6-8). Maria hakutoa mwana-kondoo; alileta makinda ya njiwa wawili. Neno hili linaonyesha ya kwamba Yesu alizaliwa katika jamaa masikini.

3. Neno la tatu lilikuwa kutoa Yesu katika hekalu kwa **Yerusalema**. Kwa mwanzo Mungu aliagiza wana wazaliwa wa kwanza kuwa mali yake; alikusudi wawe chama cha makuhani (Kut. 13:2). Kwa wakati wa nyuma alichagua kabila la Lawi kufanya kazi ya makuhani (Kut. 28:1,2). Halafu wazazi walikuwa na ruhusa "kununua tena" au "kukomboa" mwana mzaliwa wa kwanza wao kwa njia ya kulipa shekeli tano. Walifanya hivi wakati walipomtoa **kwa Bwana.**

### J. Simioni anaona Masiya mbele ya kufa kwake (2:25-35)

**2:25, 26 Simioni** alikuwa mmoja wa baki la Wayuda wenye kupenda Mungu waliokuwa **wakingojea** kuja kwa Masiya. **Roho Mtakatifu alimfunulia ya kwamba hatakufa mbele ya kuona Kristo wa Bwana,** ndiye Mpakaliwa. "Siri ya BWANA ni pamoja nao ambao wanamwogopa" (Zaburi 25:14). Ni siri namna Mungu anavyojulisha maneno yake kwa wale wanaotembea katika upole na ushirika naye.

**2:27, 28** Simioni aliingia **hekalu** siku ile ile **Yosefu na Maria walipotoa** Yesu kwa Mungu. Likafunuliwa kwake na Roho Mtakatifu ya kwamba Mtoto huyu alikuwa Masiya atakayekuja. Akishika Yesu **katika mikono yake** alitoa wimbo unaoitwa sasa "Nunc Dimittis" (*Sasa uruhusu mtumishi wako aende kwa utulivu kama ulivyosema*).

**2:29-32** Habari za wimbo huu ni hivi: **Bwana, sasa uruhusu mtumishi wako aende kwa utulivu … kwa sababu macho yangu yameona wokovu wako**, ndiye Mtoto huyu, Mkombozi ambaye uliahidi kutuma. Umemwamuru kuleta wokovu kwa watu namna zote. Atakuwa **nuru kuleta ufunuo kwa Mataifa** (wakati wa kuja kwake mara ya kwanza) na

kungaa katika **utukufu** juu ya **watu wako Israeli** (wakati atakapokuja mara ya pili). Simioni alikuwa tayari kufa nyuma ya kukutana na Bwana Yesu. Mauti hayakuwa na uchungu tena. (1 Kor. 15:55)

**2:33** Luka aliweka roho sana kukumbusha watu kwamba Yesu alizaliwa na bikira, hivi alisema tena na tena **Yosefu na mama yake.**

**2:34,35** Nyuma ya kusifu Mungu kwa Masiya, **Simioni alibariki** Yosefu na Maria, na nyuma yake alitoa unabii kwa **Maria**. Unabii huu ulikuwa na sehemu ine:

1. **Mtoto huyu amewekwa kwa kuanguka na kusimama kwa wengi katika Israeli.** Wenye kiburi wasiotubu wataanguka na kuazibiwa.Wale ambao walijinyenyekeza na kupokea Bwana Yesu watasimama na kubarikiwa.

2. **Mtoto atakuwa … kwa alama itakayosingiziwa**. Ni kama kukaa kwa Bwana Yesu duniani kulikemea zambi na uzalimu, na kuliamsha uadui mchungu ndani ya mioyo ya watu.

3. Ndiyo, **upanga utakuchoma roho yako mwenyewe**. Simioni alitabiri hapa huzuni itakayojaza moyo wa Maria wakati atakapoona kusulibishwa kwa Mwana wake (Yoane 19:25).

4. **… ili mawazo ya mioyo mingi yafunuliwe**. Namna mtu anavyotenda wakati anapokutana na Mwokozi inafunua makusudi na mapendo ya roho yake.

### K. Nabii mke Ana (2:36-39)

**2:36,37 Nabii mke Ana**, kama Simioni, alikuwa mmoja wa baki aminifu la Israeli ambaye alikuwa akingoja kufika kwa Masiya. Alikuwa mtu wa **kabila la Aseri** (maana yake mwenye *furaha* na ku*barikiwa*), moja la makabila kumi waliohamishwa kwa kifungo na Waasuria kwa mwaka 721 B.C. Ana alikuwa na miaka kupita mia moja kwani alikuwa na mume kwa **miaka saba** tu, na tangu wakati ule, kwa **miaka 84**, alikuwa mjane. Bila shaka, akiwa nabii mke, alipokea funuo toka **Mungu** na alisema kwa ajili ya Mungu. Alifikia makusanyiko katika **hekalu,** akiabudu pamoja na **kufunga** na maombi **usiku na mchana.** Uzee wake haukumzuiza asitumikie Bwana.

**2:38** Wakati ule ule walipokuwa wakitoa Yesu kwa Bwana, na Simeoni alikuwa akisema na Maria, Ana alifika karibu nao. **Alishukuru Bwana kwa Mkombozi** ambaye aliahidi kutuma, kisha **alisema** juu ya Yesu na waaminifu wote katika **Yerusalema** waliokuwa wakitazamia **ukombozi.**

**2:39** Wakati Yosefu na Maria **walipokuwa wamemaliza maneno yote** kwa usafisho na kutoa, **walirudia Galilaya kwa mji wao, ndio Nazareti**. Luka hakuandika juu ya kufika kwa waakili wala juu ya kukimbia kwao kwenda Misri.

### L. Ujana wa Yesu (2:40-52)

**2:40** Haya ndiyo maneno tunayosoma juu ya kukua kwa **mtoto Yesu**: **alikua na aliongezeka nguvu katika roho**. Kama watoto wote alijifunza kutembea, kusema, kucheza na kutumika. Kwa sababu hii anaweza kushirikiana nasi ndani ya maneno yetu yote. Hakujifunza kusoma na kufanya hesabu tu na maneno mengine watoto wa wakati ule waliyojifunza, lakini **alijazwa hekima**, maana yake namna gani kutumika na maneno haya ndani ya maisha ya kila siku. Kwa maneno ya roho, **neema ya Mungu ilikuwa juu yake**. Alitembea na upatano wa karibu na Mungu, akitegemea Roho Mtakatifu. Alijifunza Neno la Mungu, akishinda saa kwa maombi na alifurahi kufanya mapenzi ya Baba yake.

**2:41-44** Kijana Myuda anageuka mwana wa sheria wakati anapofikia miaka 12. Wakati Bwana wetu alipokuwa na **miaka kumi na miwili**, jamaa yake walifanya safari ya kila mwaka

kwendea **Yerusalema** kwa **Pasaka**. Lakini wakati walipoanza safari ya kurudi kwa Galilaya hawakufahamu ya kwamba Yesu hakuwa katika makutano ya watu ambao walisafiri nao. Bila shaka walifikiri alikuwa pamoja na vijana wengine.

Mbele ya kuhukumu Yosefu na Maria juu ya neno hili, tukumbuke ya kwamba ni nyepesi sana kwa sisi kushinda **siku moja nzima** bila kufahamu ya kwamba **hatuna upatano** wa karibu na Bwana tena kwa sababu ya zambi fulani tusiyokiri bado. Sharti turudi kwa pahali tulipoanguka na kukiri zambi hii na kuiacha kusudi tuweze kuwa na upatano mtamu naye tena.

**2:45-47** Wakati waliporudia **Yerusalema** Maria na Yosefu **walikuta** Yesu **hekaluni, akiketi pamoja na walimu, akisikiliza mafundisho yao na akiwauliza maneno.** Tusifikiri alifanya hivi na kiburi na kushindana na wazee wake. Sivyo. Kama mtoto ye yote alijifunza na unyenyekevu toka walimu wake. Ni kama walimwuliza maneno mengine vilevile kwa sababu **walishangaa kwa akili zake na majibu yake.**

**2:48** Hata wazazi wake **walishangaa** wakati walipokuta Yesu akishiriki na akili ndani ya masemo ya wale waliokuwa na miaka mingi kupita yeye. Hata hivi **mama yake** alionyesha woga na kasirani ndogo wakati alipouliza kama Yesu hakufahamu kwamba walikuwa wakisumbuka kwa sababu yake.

**2:49** Haya ndiyo masemo ya kwanza ya Yesu yaliyoandikwa. Yanaonyesha wazi ya kwamba alifahamu vizuri ya kwamba yeye ni Mwana wa Mungu, na kama kazi yake ilikuwa nini. **"Mulinitafuta sababu gani? Hamukufahamu ya kama imenipasa kufanya kazi ya Baba yangu?"** *Mama yake* alisema, "Baba yako na mimi." *Yeye* alisema, **"kazi ya Baba yangu."**

**2:50** Kwa wakati ule **hawakufahamu** maana ya maneno aliyosema. Yalikuwa namna nyingine na masemo ya mtoto wa miaka kumi na wawili!

**2:51** Basi walikuwa pamoja tena kwa safari yao kurudia **Nazareti**. Tunaona uzuri na usafi wa roho ya Yesu ndani ya maneno haya: **"akakuwa akiwatii."** Hata akiwa Mwumba wa ulimwengu alikubali pahali pa mtoto wa kutii ndani ya jamaa hii ya Wayuda isiyoonekana katikati ya watu. **Lakini mama yake akashika maneno haya yote katika moyo wake.**

**2:52** Ndani ya shairi hili tunaona tena utu wa Bwana wetu, na namna alivyopata nguvu:

1. Aliendelea kupata nguvu katika **akili,**
2. na katika **kimo** (ndio mwili),
3. katika **neema mbele ya Mungu** (ndiyo katika maneno ya roho),
4. na mbele ya **watu**.

Alikuwa mkamilifu kabisa. Luka hasemi neno juu ya miaka kumi na minane Bwana Yesu aliyoshinda katika Nazareti kama mwana wa seremala. Miaka hii inatufundisha faida ya kutayarishwa kwa kazi ambayo tutafanya, saburi, na faida vilevile ya kufanya kazi ya watu wa dunia. Ni maonyo tusijaribu kuanza utumishi kwa Mungu mbele ya watu mara moja bila kupata nguvu kwanza katika imani. Kuona maonyo haya bure kunaweza kuharibu ushuhuda wetu nyuma.

## 3. MATAYARISHO YA MWANA WA WATU KWA UTUMISHI WAKE (3:1– 4:30)

### A. Matayarisho ya mtangulizi wake (3:1-20)

**3:1,2** Luka, fundi la historia, anatufahamisha wazi **mwaka** gani Yoane alipoanza kuhubiri, akitaja viongozi vya serikali na vya dini kwa wakati ule: mfalme mmoja (**Kaisari**), **liwali** mmoja,

watu watatu walioitwa **watawala** na **makuhani wakubwa** wawili. Viongozi vya serikali wanaotajiwa wanatufahamisha ya kwamba taifa la Israeli lilitawaliwa na nguvu na Waroma. Kulikuwa na makuhani wakubwa wawili katika Israeli. Neno hili linaonyesha ya kwamba maneno ya taifa la Israeli hayakuwa taratibu kwa maneno ya dini vilevile. Viongozi hawa walikuwa wenye heshima kwa macho ya watu wa dunia, lakini walikuwa waovu machoni mwa Mungu. Hivi wakati Mungu alipotaka kusema na watu, hakuchagua wakubwa wa serikali, wala wa sunagogi, lakini alituma habari zake kwa njia ya **Yoane mwana wa Zakaria, jangwani.**

**3:3** Yoane alisafiri mara moja kwa **inchi** yote iliyokuwa **kando ya mto Yorodani**, kwa upande wa Yeriko. Aliita taifa la Israeli kutubu **zambi** zao kusudi wapokee usamehe na waweze kuwa tayari kwa kuja kwa Masiya. Aliita watu kubatizwa vilevile kuonyesha ya kwamba walikuwa wametubu kweli. Yoane alikuwa nabii wa kweli, na alililia zambi za watu na kuwaita kufanywa mpya katika roho.

**3:4** Kwa njia hii utumishi wake ulitimiza unabii wa **Isaya** 40:3-5. Alikuwa **sauti ya mtu akilia jangwani**. Kwa maneno ya roho Israeli lilikuwa **jangwa** kwa wakati ule. Lilikuwa taifa la kukauka, bila furaha na bila kuzaa matunda kwa Mungu. Ilipasa watu kugeuka kabisa kwa maneno ya roho kwa kutayarishwa kwa kuja kwa Bwana. Wakati mfalme alipokusudi kufikia pahali fulani kwa wakati ule, kulikuwa na matayarisho mengi, hata kutengeneza njia, aweze kufika salama. Hili ndilo neno ambalo Yoane aliita watu kufanya, si kwa maneno ya ndaki ya inchi, lakini kwa njia ya kutayarisha mioyo yao kupokea Bwana.

**3:5** Maneno yatakayotokea kwa wakati wa kuja kwa Kristo:

**Kila bonde litajazwa** – wanyenyekevu na wenye toba ya kweli wataokolewa na kushibishwa.

**Kila mlima na kilima kitashushwa** – watu wenye kiburi kama waandishi na Wafarisayo watanyenyekezwa.

**Njia zinazokunjama zitanyoshwa** – watoza kodi na watu wengine wenye mwenendo mbaya wataadilishwa.

**3:6** Na **wote wenye mwili** – Wayuda na Mataifa – **wataona wokovu wa Mungu**. Wakati Kristo alipokuja mara ya kwanza watu wote walikuwa na njia kupokea wokovu, lakini si watu wote waliofanya hivi. Wakati atakapokuja tena, shairi hili litatimizwa kabisa. Halafu Israeli wote wataokolewa, na Mataifa vilevile watashiriki baraka za ufalme wake wa utukufu.

**3:7** Yoane alifahamu ya kwamba watu wengi wa **makutano waliokuja** kubatizwa hawakufika na roho ya kweli. Wengine wao hawakuwa na njaa wala kiu kwa haki hata kidogo. Aliwaita uzao wa **nyoka**. Ulizo lake, **"Nani ambaye aliwaonya ninyi kukimbia hasira itakayokuja?"** linaonyesha ya kwamba Yoane hakufanya hivi. Mahubiri yake yalikuwa kwa wale waliokuwa tayari kukiri zambi zao.

**3:8** Wakitaka kweli kutengeneza maneno yao na Mungu, waonyeshe ya kwamba walikuwa wametubu kwelikweli kwa njia ya kugeuza mwenendo wao. Toba ya kweli inazaa **matunda.** Haifai wawaze ilitosha kuwa wazao wa **Abrahamu**. Neno hili halikutosha; undugu na wenye kupenda na kufuata Mungu hautoshi kugeuza mtu kuwa mtu wa Mungu. **Mungu** hakulazimishwa kutumika na wazao wa Abrahamu tu kutimiza makusudi yake; aliweza kukamata hata mawe kando ya mto Yorodani kwa **kunyanyulia Abrahamu watoto.** Tunafikiri *mawe* ni mfano wa watu wa Mataifa ambao Mungu atageuza kwa njia ya ajabu ya neema yake kuwa waamini wenye imani kama ile ya Abrahamu. Neno hili lilitokea kweli. Wazao

wa Abrahamu, kama taifa, walikataa Kristo wa Mungu. Lakini watu wengi wa Mataifa walimpokea kuwa Bwana na Mwokozi wao, na kwa njia hii waligeuka wazao wa Abrahamu kwa roho.

**3:9 Shoka limewekwa katika shina la miti** ni mfano kuonyesha ya kwamba kuja kwa Kristo kutapima kama watu walitubu kweli. Wale wasioonyesha matunda ya toba watahukumiwa.

**3:10** Masemo makali ya Yoane yalikata zamiri za **watu**, **wakamwuliza** namna gani waliweza kuonyesha ya kwamba walikuwa wametubu kweli.

**3:11-14** Ndani ya mashairi haya Yoane aliwajulisha njia nyingine kuhakikisha ya kwamba walikuwa wametubu kweli. Wapende jirani zao kwa kipimo wanachojipenda wenyewe kwa njia ya kushiriki mavazi na **vyakula** na wenye hitaji.

Sharti **watoza kodi** watende kwa haki kabisa kwa maneno ya mali. Walijulikana kama wadanganyifu; kama sasa wangegeuka na kutenda kwa haki, neno hili litahakikisha kwamba walikuwa wametubu kweli.

Mwishoni, **askari** waliagizwa kuepuka zambi namna tatu ambazo walipenda kutenda: jeuri, masingizio, na manunguniko. Lazima tufahamu ya kwamba watu hawaokolewi kwa njia ya kuepuka kufanya maneno haya, lakini kwa njia ya kutoyatenda wanaonyesha ya kwamba wametubu zambi zao kweli, na roho zao ni safi mbele ya Mungu.

**3:15,16a** Hapa tunaona unyenyekevu mkubwa wa Yoane. Angaliweza kujionyesha mwenyewe, kwa wakati, kuwa Masiya, na kujipatia wafuata wengi, lakini hakufanya hivi. Alijisawanisha na Kristo hivi: Hakujiheshimu mwenyewe hata kidogo. Alieleza ya kwamba ubatizo wake ulikuwa ubatizo wa inje, wa mwili, wa kuonekana tu, lakini ule wa Kristo utakuwa wa ndani, wa roho. Alisema ya kwamba yeye mwenyewe **hakustahili** kufungua hata **kamba ya viatu** vya Kristo.

**3:16b,17** Ubatizo wa Kristo utakuwa na **Roho Mtakatifu na moto**. Kwanza atabatiza waamini **na Roho Mtakatifu** – ahadi ya neno litakalotokea siku ya Pentekote wakati waamini watakapobatizwa katika mwili wa Kristo. Lakini nyuma atabatiza **kwa moto**.

Shairi 17 linatufahamisha ya kwamba ubatizo wa **moto** ni ubatizo wa hukumu. Pale tunaona Bwana kama mwenye kupepeta ngano. Wakati anapotupa ngano katika hewa, **makanda** yanaanguka pembeni ya sakafu, kisha yanafagiwa na kuteketezwa.

Wakati Yoane aliposema na waamini na wasioamini pamoja alisema juu ya ubatizo kwa *Roho* na ubatizo kwa *moto* vilevile (Mt. 3:11 na hapa). Lakini wakati aliposema na waamini peke yao (Mk. 1:5) hakutaja ubatizo kwa moto (Mk. 1:8). Hakuna mwamini wa kweli atakayebatizwa kwa moto.

**3:18-20** Sasa Luka alikuwa tayari kuacha kusema juu ya Yoane na kuanza kusema zaidi juu ya Yesu. Hivi, ndani ya mashairi haya alijumlisha utumishi wa Yoane na kutufikisha kwa wakati alipofungwa na **Herode.** Neno hili lilitokea miezi 18 nyuma. Yoane alikuwa **amehamakia** Herode juu ya **ufungu mzinifu** na mke wa ndugu yake. Halafu **Herode** aliongeza neno moja lingine juu ya maneno mabaya yote mengine aliyofanya mbele: alifunga Yoane gerezani.

### B. Matayarisho kwa ubatizo (3:21,22)

Bwana Yesu alikuwa na miaka karibu 30 wakati alipoanza utumishi wake katikati ya watu, kwa njia ya **kubatizwa** katika Mto Yorodani. Tuwaze zaidi juu ya maneno matatu ya ubatizo wake:

1. Wale waliokuwa pale kwa wakati ule: **Yesu** (sh.21); **Roho Mtakatifu** (v.22a), na Mungu **Baba** (sh.22b) walikuwa wote pale saa yenyewe.

2. Luka tu aliandika ya kwamba Yesu **aliomba** kwa wakati wa ubatizo wake (sh.21). Neno hili linapatana na kusudi la Luka kuonyesha Kristo kama Mwana wa watu, aliyetegemea Mungu Baba wakati wote.

Tunaona Bwana Yesu akiomba mara nyingi ndani ya Habari Njema hii. Aliomba hapa, kwa mwanzo wa utumishi wake katikati ya watu. Aliomba wakati alipoanza kujulikana katikati ya watu, na watu wengi walikuwa wakimfuata (5:16). Alishinda usiku mzima akiomba mbele ya kuchagua wanafunzi wake (6:12). Aliomba mbele ya maneno yaliyotokea kwa Kaisari Filipi, pahali pa mafundisho yake makubwa zaidi (9:18). Aliomba juu ya mlima pahali kuonekana kwa sura yake kulipogeuka (9:28). Aliomba mbele ya wanafunzi, na nyuma yake alitoa mafundisho juu ya maombi (11:1). Aliombea Petro mbele ya kurudi nyuma kwa Petro (22:32). Aliomba katika shamba la Getesemane (22:41,44).

3. Mungu alisema mara tatu **toka mbinguni** juu ya utumishi wa **Mwana** wake mpendwa. Kwa miaka 30 alikuwa ametazama maisha yake makamilifu kwa Nazareti, na sasa kwa ubatizo wake alisema, **"Ninapendezwa."** Alisema toka mbinguni mara mbili nyingine: Wakati Petro alipotaka kujenga hema tatu juu ya mlima pahali sura ya Yesu ilipogeuzwa (Luka 9:35), na wakati Wayunani walipofika karibu na Filipo, wakiomba kuona Yesu (Yoane 12:20-28).

### C. Matayarisho kwa njia ya kushiriki ubinadamu (3:23-38)

Mbele ya kuandika juu ya **utumishi** wa Bwana wetu katikati ya watu, Luka alitujulisha kizazi chake. Kama kweli yeye alikuwa mtu, lazima awe mzao wa **Adamu**, kama tunavyoona hapa. Walimu wengi wanafikiri ya kwamba tunaona hapa kizazi cha Maria. Ona ya kwamba shairi 23 halisemi Yesu alikuwa mwana wa Yosefu, lakini **"alizaniwa kuwa mwana wa Yosefu."** Kama neno hili ni sawa, Heli (sh.23) alikuwa baba wa Maria.

Walimu wengi wanafikiri ya kwamba tunaona hapa kizazi cha Bwana kwa njia ya Maria. Wanafikiri hivi kwa sababu:

1. Majina ya kizazi cha Yosefu yanaandikwa ndani ya Habari Njema ya Matayo (1:2-16).
2. Kwa sura za kwanza za Luka tunaona Maria kupita Yosefu, lakini ndani ya sura za kwanza za Matayo tunaona Yosefu kupita Maria.
3. Haikuwa desturi za Wayuda kutaja majina ya wanawake katika kizazi, na kwa sababu hii hatuoni jina la Maria hapa.
4. Ndani ya Matayo 1:16, tunasoma wazi ya kwamba Yakobo alizaa Yosefu. Hapa katika Luka hatusomi ya kwamba Heli alizaa Yosefu. Mara nyingine maana ya *mwana* ni *mkwe*.
5. Luka iliandikwa kwa Kiyunani na tunaona neno hili *tou* (maana yake *wa*) mbele ya kila jina katika kizazi hiki *ila* mbele ya jina la Yosefu. Neno hili linatuleta kufikiri ya kwamba Yosefu alitajwa hapa kwa sababu alikuwa mume wa Maria tu.

Tunataka kusema maneno machache mengine juu ya majina haya:

1. Tunaona ya kwamba Maria alikuwa mzao wa **Daudi** kwa njia ya mwana wake **Natani** (sh. 31). Ndani ya Habari Njema ya Matayo Yesu aliriti, kwa njia ya *sheria,* kiti cha ufalme cha Daudi kwa njia ya mwana wake Solomono.

Kama Mwana wa Yosefu kwa sheria Bwana alitimiza sehemu ile ya agano la Mungu na Daudi iliyoahidi ya kwamba kiti chake cha ufalme kitaendelea milele. Lakini Yesu hakuweza kuwa mwana wa hakika wa Yosefu bila kulaaniwa na Mungu na laana yake kwa Yekonia. Kwa sababu ya laana hii hakuna mzao wa mfalme yule mwovu atakayesitawi (Yer. 22:30).

Kama Mwana wa hakika wa Maria, Yesu alitimiza sehemu ile ile ya agano la Mungu na Daudi, ya kwamba *mzao* wake atakaa juu ya kiti cha kifalme chake milele. Kwa sababu Yesu alikuwa mzao wa Daudi kwa njia ya Natani hakuwa chini ya laana ya Yekonia.

2. **Adamu,** wa **Mungu** (sh.38). Maana yake ndiyo ya kwamba aliumbwa na Mungu.

3. Ni wazi kwamba kizazi hiki cha Masiya kilikwisha na Bwana Yesu. *Hakuna mwingine* anayeweza kamwe kutawala toka kiti cha ufalme wa Daudi.

**D. Matayarisho kwa njia ya majaribu (4:1-13)**

**4:1** Hakuna saa ndani ya maisha ya Bwana wetu wakati asipojazwa kabisa na Roho Mtakatifu, lakini tunaona neno hili zaidi hapa, saa alipojaribiwa na Shetani. Mtu ambaye **anajazwa na Roho Mtakatifu** ni mtu ambaye anajitoa mzima kwaye na kutii kabisa kila neno la Mungu. Mtu anayejazwa Roho Mtakatifu amekiri na kuacha kila zambi na hajifikiri mwenyewe, lakini anajazwa na Neno la Mungu. Wakati Yesu aliporudi **toka Yorodani,** pahali alipobatizwa, **aliongozwa na Roho kwenda jangwani**. Tunafikiri ilikuwa jangwa ya Yudea kwa pwani ya mangaribi ya Bahari ya Chumvi.

**4:2,3** Pale **alijaribiwa na Shetani kwa siku makumi ine – bila kula kitu.** Kwa mwisho wa muda ule alijaribiwa kwa njia tatu. Majaribu haya yalitokea kwa pahali mbalimbali: jangwani, mlimani na kwa hekalu katika Yerusalema. Maneno haya **"alisikia njaa,"** yanatukumbusha utu wa Bwana Yesu. Basi kwa jaribu lake la kwanza Shetani alisema vizuri Bwana atumike na uwezo wake wa Mungu kujipatia vyakula. Lilikuwa jaribu la hila. Ingalikuwa vizuri kufanya hivi, lakini hata hivi ingalikuwa vibaya kwa Bwana kutii Shetani ndani ya neno hili. Ilikuwa lazima kwa yeye kutii Baba yake ndani ya maneno yote.

**4:4 Yesu** alishinda majaribu kwa njia ya kutumika na mashairi toka Biblia (Tor. 8:3). Kutii Neno la Mungu ni neno kubwa kupita kushibisha njaa ya mwili. Yesu hakubishana na Shetani. Mwalimu mmoja (jina lake Darby) alisema, "Shairi moja tu linanyamazisha adui, kama likitumiwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Siri ya kuwa na uwezo kushinda katika vita ya roho ni kutumika na Neno la Mungu kwa halali."

**4:5-7** Ndani ya jaribu la pili **Shetani … alionyeshea** Yesu **falme zote za dunia kwa dakika moja.** Shetani hahitaji saa nyingi kuonyesha maneno yote aliyo nayo. Hakutaka kutoa dunia yenyewe, lakini **falme za dunia** hii. Kwa njia nyingine Shetani ana **amri** kweli juu ya **falme** za dunia hii. Kwa sababu ya zambi ya watu, amegeuka "mkubwa wa dunia hii" (Yoane 12:31; 14:30; 16:11), "mungu wa dunia hii" (2 Kor. 4:4), na "mfalme wa uwezo wa anga" (Efe. 2:2). Ni kusudi la Mungu kwa "ufalme wa dunia hii" kuwa "ufalme wa Bwana wetu na wa Kristo wake" (Ufu. 11:15). Hivi Shetani alitaka kumtolea kwa saa ile ufalme ambao utakuwa wa Kristo kwa wakati wa kuja!

Lakini njia fupi kwa Bwana Yesu kufikia kiti cha ufalme haikuwa. Lilikuwa kusudi la Mungu kwaye kuteswa kwanza na kusulibishwa msalabani mbele ya kutukuzwa. Hakuweza kupata neno njema kwa njia isiyo ya hakika hata kidogo. **Hataabudu** Shetani kamwe, si neno kama bei ya kukataa kufanya hivi ikiwa kubwa zaidi.

**4:8** Hivi Bwana alitaja Torati 6:13 kuonyesha ya kwamba kama Mtu ilimpasa **kuabudu** na **kutumikia** Mungu tu.

**4:9-11** Kwa jaribu la tatu Shetani alipeleka Yesu hata **Yerusalema,** aka-

mweka **juu ya mnara mmoja wa hekalu,** akasema naye kujitupa chini. Ndiyo, Mungu aliahidi ndani ya Zaburi 91:11,12 ya kwamba atalinda Masiya. Labda Shetani alijaribu Yesu kufanya ajabu namna hii mbele ya watu kuwaonyeshea ya kwamba yeye ni Masiya. Malaki alikuwa ametabiri ya kwamba Masiya atatokea gafula kwa hekalu lake (3:1). Kwa njia hii Yesu angeweza kuonekana na kuheshimiwa na watu kama Mwokozi ambaye Mungu aliahidi kutuma, bila kwenda Kalvari.

**4:12** Mara ya tatu Yesu alishinda majaribu kwa njia ya kutaja shairi la Biblia. Torati 6:16 linatukataza kujaribu **Mungu**.

**4:13** Akishindwa na upanga wa Roho, **Shetani** aliacha Yesu **kwa wakati**. Ni kama majaribu yanatufikia wakati na wakati, si saa zote.

Tuwaze juu ya maneno machache mengine hapa:

1. Jaribu la pili na la tatu ndani ya Luka yanageuka kuwa jaribu la tatu na la pili ndani ya Matayo.

2. Kila mara neno lililoahidiwa lilikuwa neno zuri, lakini njia ya kulipata ilikuwa baya. Ni vibaya kila mara kutii Shetani, kumwabudu au kuabudu kiumbe cho chote kingine. Ni vibaya kujaribu Mungu.

3. Jaribu la kwanza liligusa mwili, la pili nafsi, na la tatu roho. Yalipendeza tamaa ya mwili, tamaa ya macho, na kiburi ya uzima.

4. Majaribu haya matatu yanagusa maneno watu wanayotamani zaidi – tamaa ya mwili, kuwa na uwezo na mali, na kuheshimiwa na watu. Mara ngapi wanafunzi wa Yesu wanajaribiwa kuchagua njia ya raha na utulivu, kujulikana duniani, na kuwa na pahali pa heshima ndani ya kanisa.

5. Ndani ya majaribu matatu yote Shetani alitumika na masemo ya dini kufanyiza majaribu yenyewe kuonekana kama kitu kizuri. Alitaja hata mashairi ya Biblia (mash. 10,11). James Stewart alisema hivi:

> Wakati tunapojifunza juu ya majaribu haya tunaona maneno makubwa mawili: 1) Kujaribiwa si zambi. 2) Mwandishi wa Waebrania 2:18 alisema juu ya Yesu, “Kwa kuwa yeye mwenyewe aliteswa wakati alipojaribiwa, anaweza kusaidia wale wanaojaribiwa.”[5]

Watu wengine wanasema majaribu haya yasingalikuwa na maana kama Yesu asingaliweza kufanya zambi. Lakini tunajua kabisa ya kwamba Yesu ni Mungu, na Mungu hawezi kufanya zambi. Bwana Yesu hakuacha kuwa Mungu kamwe. Uungu wake ulifichwa wakati alipoishi duniani, lakini haukuondoshwa. Halafu watu wengine wanasema hakuweza kufanya zambi kama Mungu, lakini kama Mtu aliweza kufanya zambi. Lakini yeye ni Mungu na Mtu pamoja; na haiwezekani kwaye kufanya zambi leo. Kusudi la majaribu haya hayakuwa kuona kama *atafanya* zambi, lakini kuhakikisha ya kwamba *hakuweza* kufanya zambi. Mtu mtakatifu tu, asiyekuwa na zambi, aliweza kuwa Mkombozi wetu.

### E. Matayarisho kwa njia ya mafundisho (4:14-30)

**4:14,15** Kuna muda wa karibu mwaka mmoja nyuma ya shairi 13 na habari za shairi 14. Kwa wakati ule Bwana alitumika katika Yudea. Habari za muda huu ni katika Yoane sura 2 kufika 5 tu.

Wakati **Yesu aliporudi kwa nguvu za Roho hata Galilaya** kuanza mwaka wa pili wa utumishi wake, sifa yake ikaenea **katika inchi hata kando zote.** Wakati **alipofundisha** ndani ya **masunagogi** ya Wayuda, alitukuzwa na watu wote.

**4:16-21** Katika **Nazareti,** ndio mji pahali alipopata nguvu, ilikuwa desturi

yake kufikia sunagogi **siku ya sabato** (ndiyo siku ya saba). Ilikuwa desturi yake kufanya maneno mawili mengine vilevile: Aliomba (Luka 22:39), na alifundisha watu (Marko 10:1). Siku moja **katika sunaogi** alisimama **kusoma** sehemu ya Maandiko Matakatifu. Mtumishi alimpa hati ndefu ya unabii wa Isaya. Bwana alifungua hati kufika sehemu tunayoita Isaya 61, akasoma shairi moja na sehemu ya kwanza ya shairi 2. Tangu zamani watu walisema mashairi haya yanasema juu ya utumishi wa Masiya. Wakati Yesu aliposema, **"Leo andiko hili limetimia kwa masikio yenu,"** alisema waziwazi kabisa ya kwamba yeye ni Masiya wa Israeli.

Tuwaze juu ya maana kubwa wa utumishi wa Masiya. Alikuja kutengeneza maneno magumu mno yanayotesa watu tangu zamani:

Umasikini: **Kuhubiri Habari Njema kwa masikini.**

Huzuni: **Kuponyesha wenye roho ya kuvunjika.**

Utumwa: **Kuhubiri wokovu kwa wafungwa.**

Upofu: … **na vipofu kupata kuona tena.**

Uzalimu: **Kufungua walioonewa**.

**Kwa ufupi, alikuja kuhubiri mwaka wa Bwana uliokubaliwa** – mwanzo wa muda mpya kwa elfu elfu za watu wenye taabu na maumivu wa dunia hii. Alijionyesha kwa watu kama jibu kwa mambo mabaya yote ambayo yanawatesa. Ni kweli kabisa; Kristo ni jibu kwa mabaya haya yote, ya mwili na ya roho.

Ona ya kwamba aliacha kusoma nyuma ya maneno haya "… **kuhubiri mwaka wa Bwana uliokubaliwa."** Hakuongeza mwisho wa shairi hili toka Isaya 61:1,2 … na siku ya kisasi cha Mungu wetu." Kusudi la kuja kwake mara ya kwanza lilikuwa kuhubiri **mwaka wa Bwana uliokubaliwa.** Muda huu wa sasa wa neema ndio wakati wa kukubaliwa na siku ya wokovu. Wakati atakaporudi duniani mara ya pili atatangaza siku ya kisasi cha Mungu wetu. Ona ya kwamba muda **unaokubaliwa** ndio **mwaka**, lakini muda wa kisasi ni *siku*.

**4:22** Wasikiaji walishangaa sana juu ya **maneno** yake ya **neema.** Walifazaika namna gani **mwana wa Yosefu**, mseremala, alikomea vizuri hivi.

**4:23** Bwana alijua ya kwamba sifa hii ya watu haitadumu. Hawakufahamu kweli kama yeye ni nani, wala wema wake. Kwa macho yao alikuwa mtoto wa mji wao aliyeendelea vizuri katika Kapernaumu. Alijua ya kwamba **watasema** naye, **"Mganga, ujiponyeshe mwenyewe!"** Maana ya masemo yao hapa *haikuwa* "Ponyesha ugonjwa wako mwenyewe namna unavyosema unaweza kuponyesha wengine." Maneno yanayofuata yanaonyesha mafikiri yao **"Mambo yote tuliyosikia yamefanyika katika Kapernaumu, uyafanye hapa vilevile katika inchi yako,"** ndiyo kwa Nazareti. Lilikuwa mwito wa kuzarau – afanye maajabu kwa Nazareti namna alivyofanya pahali pengine, na kwa njia hii aepuke zihaka ya watu.

**4:24-27** Ndani ya jibu lake Bwana alionyesha neno tunaloona tena na tena, ndilo ya kwamba watu wa kujulikana hawana heshima katika inchi **yao wenyewe.** Aliendelea kusema juu ya maneno mawili yaliyotokea katika Agano la Kale wakati manabii wa Mungu wasioheshimiwa na watu wa Israeli walitumwa kwa Mataifa. Wakati wa **njaa kubwa** katika Israeli, **Elia** hakutumwa kwa mmoja wa wajane wa Israeli (nao walikuwa wengi), lakini alitumwa kwa mjane mtaifa katika **Sidona**. Na kulikuwa na **wakoma wengi katika Israeli** kwa wakati wa **Elisa**, lakini nabii huyu alitumwa karibu na **Namani**, mtu wa Mataifa, je-

madari la jeshi la Wasuria. Unafikiri Wayuda waliwaza nini wakati waliposikia masemo haya? Kwa macho yao wanawake, watu wa Mataifa na wakoma walikuwa chini kupita watu wote wengine, na hawakuwa na heshima. Lakini Bwana, ndani ya masemo yake, aliwaweka wote watatu *juu kupita* Wayuda waliokosa imani! Alikuwa akisema ya kwamba maneno haya yaliyotokea katika Agano la Kale yalikuwa karibu kutokea tena. Alikuwa ametenda maajabu, lakini atakataliwa hata hivi, si na watu wa Nazareti tu, lakini na taifa la Israeli. Halafu atakwenda kwa Mataifa, kama Elia na Elisa walivyofanya.

**4:28** Watu wa Nazareti walifahamu maana ya masemo yake. Kufikiri Mataifa watapendelewa kuliwakasirisha sana. Askofu Ryle alisema,

> Watu wanachukia sana elimu ya mamlaka na enzi ya Mungu, ndiyo kweli Kristo aliyotangaza sasa tu. Hakuna lazima kwa Mungu kutenda maajabu katikati yao.[6]

**4:29,30** Watu **wakamtoa inje ya mji … hata ukingo wa kilima**, wakikusudi **kumtupa chini**. Bila shaka walisukumwa na Shetani ndani ya mambo haya kujaribu tena kuharibu Mriti wa kiti cha ufalme cha Mungu. Lakini kwa njia ya ajabu alipita katikati ya makutano, akaondoka mjini. Adui zake hawakuwa na uwezo kumzuiza. Tunafikiri hakurudia Nazareti tena kamwe.

## 4. MWANA WA WATU ANAHAKIKISHA UWEZO WAKE (4:31 – 5:26)

### A. Uwezo kutokeza pepo mchafu (4:31-37)

**4:31-34** Watu wa Kapernaumu walifahamu ya kwamba mafundisho ya Bwana Yesu yalikuwa na uwezo, na yalichokoza zamiri zao. Mashairi 31-41 yanaonyesha desturi ya maneno Bwana Yesu aliyofanya siku ya sabato. Tunaona uwezo wake juu ya pepo wachafu na gonjwa. Kwanza alifikia **sunagogi,** akakuta pale **mtu mwenye pepo mchafu**. Tunasoma mara nyingi ya kwamba pepo ni **wachafu**, maana wao wenyewe ni wachafu na wanachafua maisha ya watu ambao wanakaa ndani yao. Tunaona neno hili wazi ndani ya mashairi haya. Kwanza kulikuwa na kilio cha hofu kubwa: **"Ee tuna nini nawe!"** Halafu pepo alionyesha wazi ya kwamba alijua Yesu kama **Mtakatifu wa Mungu** atakayeharibu majeshi ya Shetani kwa wakati wa kuja.

**4:35** **Yesu** alitoa maagizo mawili kwa pepo, **"Nyamaza, umtokee!"** Pepo alifanya hivi, nyuma ya kuangusha mtu mwenyewe bila kumwumiza.

**4:36,37** Watu *walishangaa sana!* Kwa njia gani masemo ya Yesu yalikuwa namna nyingine, hata **pepo wachafu** walimtii? **Amri na uwezo** wa masemo yake yalitoka wapi? Hatushangai kusoma ya kwamba **habari zake zikaenea pahali po pote pa inchi iliyo pande zote!**

Maajabu yote yanayoonekana kwa macho ambayo Bwana Yesu alifanya ni mifano ya maajabu ya roho anayofanya. Tunaona neno hili ndani ya maajabu katika Luka:

Kutokeza pepo wachafu (4:31-37) – kuponyeshwa toka uchafu wa zambi.

Kuponyeshwa toka homa kwa mama ya mke wa Petro (4:38,39) – kufunguliwa toka uzaifu unaoletwa na zambi.

Kuponyeshwa kwa mkoma (5:12-16) – kuponyeshwa toka machukio makubwa, na kukosa matumaini ya zambi (ona vilevile 17:11-19).

Mtu mwenye kupooza (5:17-26) – kufunguliwa toka kupooza kwa zambi na kupewa uwezo kutumikia Mungu.

Mwana wa mjane anafufuliwa (7:11-

17) – wenye zambi ni wafu katika zambi na makosa, na wanahitaji uzima (ona vilevile 8:49-56).

Kutulizwa kwa zoruba (8:22-25) – Kristo anaweza kutuliza zoruba ndani ya maisha ya wanafunzi wake.

Jeshi (Legioni), pepo mchafu (8:26-39) – zambi inazaa jeuri na wazimu na kuondosha watu katika jamii ya watu wengine. Bwana analetea mtu huyu adabu na heshima tena na ushirika naye mwenyewe.

Mwanamke aliyegusa upindo wa vazi lake (8:43-48) – umasikini, huzuni na mafazaiko kwa sababu ya zambi.

Kulisha watu elfu tano (9:10-17) – dunia inakufa kwa njaa ya mkate wa Mungu. Kristo anashibisha mahitaji kwa njia ya wanafunzi wake.

Mwana mwenye pepo mchafu (9:37-43a) – jeuri na ukali wa zambi, na uwezo wa Kristo kuponyesha.

Mwanamke mwenye pepo mchafu wa uzaifu (13:10-17) – zambi inafanyiza mtu kuwa kiwete na mwenye kilema, lakini Yesu anaponyesha kabisa.

Mgonjwa wa tumbo la maji (14:1-6) – zambi inaleta maumivu na taabu, na hatari.

Mwombaji kipofu (18:35-43) – zambi inafanyiza watu kuwa wapofu kwa maneno ya milele. Macho yao yanafunguliwa wakati wanapozaliwa tena.

**B. Uwezo juu ya homa (4:38,39)**

Halafu Yesu alifikia **nyumba ya Simoni** kuona **mama ya mke wa Simoni aliyekuwa na homa sana**. Wakati Bwana **alipokemea homa,** homa **ilimwacha mara moja** naye aliponyeshwa kabisa, kwani aliweza kusimama na kutumikia watu wa nyumba yake. Lilikuwa ajabu kwa sababu karibu wenye homa ya nguvu wote wanapata nguvu tena polepole tu. (Watu wa dini nyingine wanafundisha ya kwamba inapasa makuhani yao kukaa bila kuoa. Ni nguvu kukubali mafundisho haya kwa sababu tunaona hapa ya kwamba Petro alikuwa na mke!)

**C. Uwezo juu ya magonjwa na pepo wachafu (4:40,41)**

**4:40** Wakati siku ya sabato ilipokwisha, watu walikuwa huru kufanya kazi tena; na **walileta** wagonjwa na wenye pepo wachafu wengi **kwake.** Hakuna mtu aliyefika bila kupata faida. **Aliponyesha** kila mtu mwenye ugonjwa na kutoa kila pepo mchafu. Kwa wakati wa sasa kuna watu wengine wanaosema wanaweza kufanya maajabu kuponyesha wenye imani, lakini wanafanya maajabu haya kwa watu ambao walichaguliwa mbele. Yesu aliponyesha *kila mtu.*

**4:41 Pepo wachafu** waliotokezwa ndani ya watu walijua ya kwamba Yesu alikuwa **Kristo, Mwana wa Mungu.** Lakini Yesu alikataa ushuhuda wa pepo wachafu. Sharti wanyamazishwe. **Walijua yeye ni Masiya**, lakini Mungu alikuwa na watumishi wengine, wazuri zaidi, kutangaza neno hili.

**D. Uwezo kwa njia ya kuhubiri vijijini kando kando (4:42-44)**

**Kesho** yake Yesu aliondoka pale, akakwenda kwa **pahali pasipo watu** karibu na Kapernaumu. Makutano **walimtafutatafuta**, wakakuja kwake. Walimsihi asiondoke, lakini Yesu **aliwakumbusha** kwamba kulikuwa na kazi kwaye kufanya ndani ya **miji mingine** ya **Galilaya** vilevile. Hivi Yesu alipita toka sunagogi moja kwenda lingine, na lingine, **akihubiri** habari njema juu ya **ufalme wa Mungu**. Yesu alikuwa Mfalme mwenyewe. Alitaka kutawala juu yao, lakini iliwapasa kutubu kwanza. Hatatawala juu ya watu wanaofungana na zambi zao. Hiki ndicho kikwazo. Walitaka kuponyeshwa toka masumbuko yao na serikali, lakini si toka zambi zao.

### E. Uwezo kwa njia ya kufundisha wengine: Kuitwa kwa wanafunzi (5:1-11)

Mwito wa Petro una mafundisho kwa sisi:

1. Bwana **alitumika na chombo** cha Petro kama mimbari kwa kufundisha makutano. Kama tukitia vitu vyetu mikononi mwa Mwokozi, ni ajabu namna anatumika navyo na kutuletea sisi zawabu vilevile.

2. Alimwambia Petro wazi pahali gani atapata samaki wengi – wakati Petro na wale waliokuwa pamoja naye walipokuwa wamesumbuka **usiku mzima** bila kupata kitu. Bwana anayejua maneno yote anajua pahali samaki wanapokuwa. Kazi tunayofanya kwa nguvu na akili yetu wenyewe ni bure. Sharti tuongozwe na Bwana ndani ya utumishi wetu kwa yeye.

3. Petro alikuwa fundi la kuvua samaki, lakini hata hivi alikubali shauri la Mseremala, basi mikila ilijazwa samaki. **"… kwa neno lako nitashusha mikila."** Tunaona hapa faida ya kuwa na unyenyekevu, tayari kupokea mafundisho na kuwa na roho ya kutii.

4. Mikila ilijazwa **kilindini**. Kilindi ni mfano wa taabu na huzuni na hasara tunayoweza kupata kwa njia ya kuishi maisha ya imani, nazo zinazaa matunda.

5. **Mikila yao** ilianza kukatika, na vyombo vyao **vilianza kuzama** (mash. 6,7). Mara nyingine utumishi wetu unaoongozwa na Kristo unazaa matatata, lakini ni matata ya kufurahisha roho zetu!

6. Ono hili la utukufu wa Bwana lilizaa ndani ya **Petro** ufahamu ya kwamba yeye mwenyewe hakustahili hata kidogo. Ilikuwa hivi na Isaya vilevile (6:5), na ni vivyo hivyo na wote wanaoona Mfalme katika uzuri wake.

7. Petro alikuwa akifanya kazi yake ya kila siku wakati Kristo alipomwita kuwa mvuvi wa **watu**. Wakati unapongojea Mungu kukuongoza, kaa kufanya kazi yo yote unayoweza, na roho yote, kwa Bwana. Mungu anaongoza watu saa wanaopofanya kazi kwa yeye, si wakati wanapokaa bure!

8. Kristo aliita Petro kuacha kazi ya kuvua samaki na kuikomboa na kazi ya kukamata **watu**. Bei ya samaki zote baharini haiwezi kusawanishwa na furaha kubwa ya kuona hata mtu mmoja akiokolewa kwa milele!

9. Petro, **Yakobo na Yoane** walileta vyombo vyao kwa pwani siku ile wakati walipopata samaki kupita siku zote nyingine, **wakaacha vyote, wakafuata Yesu.**

### F. Uwezo juu ya ukoma (5:12-16)

**5:12** Mganga Luka alisema **mtu** huyu **alijaa ukoma.** Ukoma ulikuwa umeenea mwilini mwake, na hakuwa na tumaini ya kwamba ataweza kupona. Lakini imani ya mkoma huyu inatushangaza. Alisema, **"Unaweza kunisafisha."** Asingaliweza kusema hivi na mtu ye yote mwingine duniani. Lakini alitumainia uwezo wa **Bwana** kabisa. Wakati aliposema, **"Ukitaka,"** hakuonyesha shaka ya kwamba labda Bwana hatataka, lakini alimwomba kumsaidia hivi hata kama yeye mwenyewe hakustahili kuponyeshwa. Alitegemea rehema na neema ya Bwana.

**5:13** Ilikuwa hatari kwa mtu kugusa mkoma kwa maneno ya afya, ilimchafua kwa maneno ya dini, na kumwondoshea heshima machoni mwa watu. Lakini Mwokozi hakuchafuwa; sivyo, lakini uwezo ulitoka kwake na kuingia mwili wa yule mkoma na kumponyesha pia. Hakupona polepole, lakini **mara moja ukoma uliondoka kwake**. Waza kwanza juu ya furaha kubwa ya mkoma huyu aliyekosa tumaini na asiyeweza kujisaidia mwenyewe – na sasa, kwa dakika moja aliponyeshwa kabisa!

**5:14** Yesu **alimwagiza asimwambie mtu** ye yote juu ya kuponyeshwa kwake. Hakutaka kukokota makutano ya watu karibu naye watakaotaka kumfanyiza mfalme. Aliagiza mtu aliyeponyeshwa **kwenda karibu na kuhani** na kutoa **zawadi** kwa kusafishwa kwake, kama **Musa** alivyoamuru (Law.14:4). Kila sehemu ya sadaka hii ilisema juu ya Kristo. Ilikuwa kazi ya **kuhani** kuangalia mwili wa mkoma kuona kama alipona kweli. Kuhani hakuweza *kuponyesha* mtu; aliweza *kusema tu* ya kwamba mtu ameponyeshwa. Kuhani huyu hakuona kamwe mbele mkoma aliyeponyeshwa. Ingalipasa kumfahamisha ya kwamba nyuma ya muda wa miaka mingi Masiya amekuja. Ungalikuwa **ushuhuda** kwa makuhani wote. Lakini walikuwa wapofu kwa maneno ya roho na walikosa imani.

**5:15,16** Hata kama Bwana hakutaka habari za ajabu hili kutangazwa, habari zenyewe zilienea mbio **na makutano makubwa wakakusanyika** kwake wapate kupona. Yesu **aliondoka katikati ya watu mara nyingi na kwenda pahali pasipo watu** kwa kuomba. Mwokozi wetu alikuwa mtu wa maombi. Habari Njema hii ilimwonyesha kama Mwana wa watu, na inatupasha kupita Matayo, Marko na Yoane juu ya maisha yake ya maombi.

**G. Uwezo juu ya kupooza (5:17-26)**

**5:17** Habari za utumishi wa Yesu zilikaa kuenea katikati ya watu, na uadui wa **Wafarisayo na walimu wa torati** ulikaa kuongezeka. Hapa tunawaona wakikutana katika **Galilaya** na kusudi la kujaribu kupata njia kumshitaki. **Uwezo wa Bwana ulikuwa pamoja naye kuponyesha** wagonjwa. Yesu alikuwa na uwezo kuponyesha kwa kila wakati, lakini mara nyingine mambo mengine yalimzuiza asifanye hivi, kama katika Nazareti, pahali asipofanya kazi nyingi za nguvu kwa sababu ya kutokuamini kwa watu (Matayo 13:58).

**5:18,19 Watu wane walileta** mtu mwenye kupooza **juu ya kitanda** kwa nyumba pahali Yesu alipokuwa akifundisha. **Iliwashinda** kumleta ndani ya nyumba karibu na Yesu **kwa sababu ya makutano**, hivi walipanda juu ya dari wakampitisha juu ya kitanda chake pahali walipoondosha nusu ya matofali, na kumshusha hata mbele ya Yesu.

**5:20,21** Yesu aliona **imani** yao ambayo iliwasukuma kufanya neno kubwa namna hii kwa kuleta mgonjwa karibu naye. **Wakati alipoona imani yao**, maana **imani** ya wanaume wale wane, pamoja na imani ya mgonjwa, **alisema** na mwenye kupooza, "**Ee, mtu, zambi zako zimesamehewa.**" Basi **waandishi na Wafarisayo** hawakusikia maneno namna hii mbele. Walijua ya kwamba **Mungu** tu anaweza **kusamehe** zambi. Hawakuwa tayari kukubali ya kwamba Yesu ni Mungu, wakalalamika alikufuru.

**5:22,23** Halafu Bwana aliendelea kuhakikisha ya kwamba kweli alikuwa amesamehe zambi za mtu huyu. Kwanza aliwauliza **nini ni jepesi kusema, "Zambi zako zimesamehewa," au kusema, "Simama, utembee?"** Si nguvu ku*sema* maneno haya, lakini ni nguvu kuya*fanya* - hayawezekani kwa watu. Labda ni nyepesi kupita kusema **"Zambi zako zimesamehewa,"** kwani hakuna njia kufahamu kwamba zilisamehewa kweli. Ukisema, **"Simama, utembee,"** halafu inaonekana wazi ya kwamba mgonjwa amepona.

Wafarisayo hawakuweza *kuona* kama zambi za mtu huyu zilisamehewa, hivi walikataa kuamini. Kwa sababu hii Yesu alifanya ajabu lingine ambalo waliweza *kuona,* kuhakikisha ya kwamba zambi zake zilikuwa zimesamehewa kweli. Aliwezesha mwenye kupooza kutembea.

**5:24 "Lakini mupate kujua ya**

**kuwa Mwana wa watu ana amri kwa dunia kusamehe zambi"** – Jina hili, **Mwana wa watu,** linaonyesha tena utu mkamilifu wa Bwana. Yeye ni namna nyingine na watu wa dunia, mkamilifu kabisa, atakayeteswa, kutoa damu yake na kufa, ndiye aliyepewa ukuu wa ulimwengu mzima.

**5:25** Mwenye kupooza alitii agizo la Bwana, akasimama, akanyanyua kile kitu ambacho alilalia, akakwenda zake kwa nyumba yake, **akisifu Mungu.**

**5:26** Watu **wote wakashangaa sana, nao vilevile wakasifu Mungu.** Walikubali ya kwamba walikuwa **wameona maajabu**, maana tangazo la usamehe na ajabu kulihakikisha.

## 5. MWANA WA WATU ANAELEZA UTUMISHI WAKE (5:27 – 6:49)

### A. Mwito wa Lawi (5:27, 28)

**Law**i alikuwa Myuda na **mtoza kodi** aliyelipiza watu kodi kwa serikali ya Waroma. Watu namna ya Lawi walichukiwa na Wayuda wenzao, si kwa sababu walitumikia Waroma tu, lakini vilevile kwa sababu hawakutenda kwa haki. Siku moja wakati Lawi alipokuwa akifanya kazi yake, Yesu alipita njiani na kumwita kumfuata. Mara moja Lawi **akaacha vyote, akaondoka, akamfuata.** Waza juu ya mavuno makubwa ambayo tendo hili moja la Lawi lilizaa! Lawi, ndiye Matayo, aligeuka mwandishi wa kitabu cha kwanza cha Habari Njema. Vizuri tufuate Bwana wakati anapotuita.

### B. Mwana wa watu anaita wenye zambi kwa sababu gani? (5:29-32)

**5:29,30** Labda Lawi alitayarisha karamu hii kubwa kwa sababu tatu: 1) Alitaka kuheshimu Bwana; 2) alitaka kutoa ushuhuda mbele ya watu ya kwamba alikuwa mfuata wa Yesu sasa; 3) alitaka rafiki zake kujua Yesu vilevile. Zaidi ya Wayuda wasingalikubali kula pamoja na **watoza kodi**. Yesu alikula pamoja na **watoza kodi na wenye zamb**i. Ndiyo, hakushiriki ndani ya zambi zao au kufanya neno lo lote lililoweza kuharibu ushuhuda wake, lakini kwa njia ya kula pamoja nao alipata njia kuwafundisha, kuwaonya na kuwa baraka kwa watu wengine.

**Waandishi na Wafarisayo** walichambua Yesu kwa sababu alikaa pamoja na watu hawa waliozarauliwa, watu wa chini kabisa.

**5:31** **Yesu alijibu** ya kwamba tendo lake lilipatana kabisa na kusudi lake wakati alipokuja duniani. Watu wenye afya njema hawahitaji mganga **"ila wenye ugonjwa."**

**5:32** Wafarisayo walifikiri wao ni **wenye haki**. Hawakufahamu kwamba walikuwa na zambi. Hivi utumishi wa Mganga Mkubwa haukuwa na faida kwao. Lakini watoza kodi hawa na wenye zambi walifahamu kwamba walikuwa wenye **zambi** na walihitaji kuokolewa toka zambi zao. Mwokozi alifika duniani kwa watu wa namna hii. Ndiyo, Wafarisayo *hawakuwa* wenye haki. Walihitaji wokovu vilevile, kama watoza kodi hawa. Lakini hawakuwa tayari kukiri zambi zao. Hivi walihukumu Mganga kwa sababu alifika karibu na watu hawa ambao walikuwa wagonjwa sana.

### C. Maelezo kwa sababu gani wanafunzi wa Yesu hawakufunga chakula (5:33-35)

**5:33** Halafu Wafarisayo waliuliza Yesu juu ya desturi ya kufunga chakula. **Wanafunzi wa Yoane Mbatizaji** waliiga mwenendo wa bwana wao mwenye kujinyima anasa za mwili. Na wafuata wa **Wafarisayo** walifunga chakula kama sehemu ya dini yao. Lakini wafuata wa Yesu hawakufanya hivi. Kwa nini?

**5:34,35** Bwana Yesu alijibu kusema

hakuna hitaji kwa wanafunzi wake kufunga wakati yeye **alipokuwa kwanza pamoja nao**. Hapa anaunganisha kufunga chakula pamoja na huzuni na maombolezo. **Wakati atakapoondoshwa kwao** kwa njia ya kufa, halafu wakati ule **watafunga chakula** kama alama ya huzuni yao.

### D. Mifano mitatu juu ya daraka mpya, 5:36-39

**5:36** Ndani ya mifano mitatu hii tutaona ya kwamba daraka mpya ilikuwa imeanza na haikuwezekana kuchanganya maneno ya zamani na maneno ya sasa.

Ndani ya **mfano** wa *kwanza*, vazi la **zamani** linasema juu ya utaratibu wa sheria ya zamani, lakini **vazi jipya** linasema juu ya muda wa neema. Maneno haya hayapatani. Mwisho wa kuyachanganya ni kuyaharibu mbili yote. Kuondosha kipande toka vazi jipya kunaharibu lile vazi jipya na **hakilingani na vazi la zamani** kwa kuonekana wala nguvu yake. J.N. Darby alisema ya kwamba Yesu hataongeza Kikristo juu ya dini ya Wayuda. Mwili na sheria zinapatana, lakini haiwezekani kamwe kwa neema na sheria, au haki ya Mungu na haki ya watu kuchanganyika.

**5:37,38** Mfano wa *pili* unafundisha ya kwamba si akili njema kuweka **mvinyo mpya** ndani ya **viriba vya zamani**. **Mvinyo mpya** inachemuka na **kupasua** viriba vya zamani visivyoweza kunyoloshwa tena, na halafu mvinyo **inamwangika.** Utaratibu na desturi ngumu za dini ya Wayuda hazikutosha tena kwa furaha, bidii, na nguvu ya daraka mpya. Ndani ya sura hii namna watu wale wane walivyoleta mwenye kupooza karibu na Bwana ni mfano wa **mvinyo mpya**. Ni vivyo na furaha na bidii ya Lawi (Matayo). **Viriba vya zamani** vya kukauka ni mfano wa baridi na ugumu wa Wafarisayo na namna walivyoshikana na dini ya zamani.

**5:39** Mfano wa tatu unasema ya kwamba **hakuna mtu akikunywa mvinyo ya zamani** atataka **mvinyo mpya; kwani anasema: "ile ya zamani ni nzuri zaidi."** Shairi hili linaonyesha ya kwamba ni nguvu kwa watu kukomboa mambo ya zamani na mambo mapya, dini ya Wayuda na Ukristo, sheria na neema. Kama Darby alivyosema, "mtu anayejuana na utaratibu na desturi za dini za baba yake hafurahi kuziacha na kuzikomboa na mafundisho mapya na uwezo wa ufalme."

### E. Mwana wa Watu ni Bwana wa Sabato (6:1-11)

**6:1,2** Mashairi yanayofuata yanapasha habari za maneno yaliyotokea kwa siku za sabato mbili. **Siku hii ya sabato** Bwana na wanafunzi wake walikuwa wakipita katika **mashamba ya ngano**. Wanafunzi **walichuma masuke, wakimenya** katika mikono yao na kula. **Wafarisayo** hawakuweza kuwahamakia juu ya kuchuma masuke kwani tendo hili lilikubaliwa na sheria (Tor. 23:25), lakini waliwahukumu juu ya kufanya hivi **siku ya sabato**. Mara nyingine walisawanisha tendo la kuchuma masuke na tendo la kuvuna, na tendo la kumenya mbegu na kazi ya kupura.

**6:3-5** Ndani la jibu lake Bwana aliwakumbusha juu ya neno lililotokea ndani ya maisha ya Daudi. Halikuwa kamwe kusudi la sheria ya sabato kukataza kazi za lazima. **Daudi** na watu wake walikuwa wamekataliwa na walikimbia na **walikuwa na njaa**. Waliingia **nyumba ya Mungu na kula mikate ya onyesho** iliyokuwa halali kuliwa na **makuhani** tu. Mungu alikubali tendo hili la Daudi lisilokuwa sawa. Kulikuwa na zambi katika Israeli. Mfalme mchaguliwa alikataliwa. Halikuwa kusudi la Mungu kwa watu kutii na nguvu sheria hii ya kutokula mkate wa onyesho, na kuacha mfalme mchaguliwa wa Mungu kufa kwa njaa.

Habari hizi ndani ya Luka zinafanana na zile za Daudi. Kristo na wanafunzi wake walikuwa na njaa. Wafarisayo wangalifurahi kuwaona wakikufa kwa njaa kwa pahali pa kuchuma ngano siku ya sabato. Lakini **Mwana wa watu ni Bwana wa sabato vilevile**. Ni yeye aliyetoa sheria hii zamani, na hakuna mwingine anayeweza kueleza maana yake ya kweli vizuri kupita yeye.

**6:6-8 Siku ya sabato nyingine waandishi na Wafarisayo waliangalia Yesu karibu karibu kuona kama ataponyesha mtu mwenye mkono wa kupooza siku ile**. Wakijuana na desturi zake walifikiri atafanya hivi, na kweli ilitokea hivi. Kwanza alisema na **mtu yule kusimama** katikati ya makutano ndani ya sunagogi. Neno hili lilikokota macho ya watu wote juu ya neno lililokuwa karibu kutokea.

**6:9 Halafu Yesu** aliuliza washitaki wake kama ni **vizuri kutenda mema au kutenda mabaya siku ya sabato**. Kama walijibu vizuri, wangesema ni vizuri kutenda mema siku ya sabato, na vibaya kutenda mabaya. Kama ni vizuri kutenda mema, ni vizuri kwa Yesu kuponyesha mgonjwa huyu. Kama ni vibaya kutenda **mabaya,** wao hawakuchunga sabato kwa sababu walikuwa wakifanya shauri kumwua yeye.

**6:10** Ilishinda adui za Yesu kumjibu. Basi Yesu aliagiza mgonjwa **kunyosha mkono** wake wa kupooza. (Luka tu alitujulisha ya kwamba ulikuwa mkono wake wa kuume.) Pamoja na agizo la kunyolosha mkono wake Bwana alimpa uwezo vilevile kufanya hivi. Wakati mtu huyu alipotii agizo la Bwana, **mkono wake uliponyeshwa** na kuwa mzima tena.

**6:11** Wafarisayo na waandishi wali**jazwa gazabu**. Walitaka kuhukumu Yesu kwa sababu ya kuvunja sabato. Lakini Yesu alisema maneno machache tu, na mtu mgonjwa aliponyeshwa, bila Yesu kufanya kazi yo yote. Basi waliendelea kusemezana namna gani wataweza kumhukumu.

Mungu alikusudi kwa siku ya sabato kusaidia watu. Wakati tunapofahamu neno hili tunajua ya kwamba kazi za lazima au za rehema zinakubaliwa siku ile.

### F. Wanafunzi kumi na wawili wanachaguliwa (6:12-19)

**6:12** Yesu **aliomba usiku mzima** mbele ya kuchagua wanafunzi wale kumi na wawili. Neno hili ni onyo kwa sisi. Mara nyingi tunajaribu kufanya kazi kwa Mungu bila kuweka kwanza saa ya kutosha kwa maombi tuweze kufahamu mapenzi yake. Luka tu alitupasha juu ya **usiku huu wa maombi**.

**6:13-16** Hawa ndio watu **kumi na wawili** ambao Bwana **alichagua** toka wale ambao walimfuata:

1. **Simoni (kwake alimpa jina lingine**, **Petro**), mwana wa Yona, mmoja wa wanafunzi wa kujulikana zaidi.
2. **Anderea ndugu yake**. Alikuwa Anderea ndiye aliyeleta Petro kwa Bwana.
3. **Yakobo**, mwana wa Zebedayo. Alipewa heshima ya kwenda pamoja na Petro na Yoane kuona Yesu mlimani. Aliuawa na Herode Agrippa I.
4. **Yoane,** mwana wa Zebedayo. Yesu aliita Yakobo na Yoane "wana wa ngurumo" (Mk. 3:17). Yoane huyu aliandika Habari Njema na barua zilizoitwa na jina lake, na kitabu cha Ufunuo.
5. **Filipo**, mtu wa Betesaida, aliyefikisha Natanaeli karibu na Yesu. Si Filipo ambaye tunasoma habari zake katika Matendo.
6. **Bartolomayo** (watu wanafikiri hili lilikuwa jina lingine kwa Natanaeli). Anatajwa pamoja na wanafunzi kumi na wawili tu.
7. **Matayo**, mtoza kodi, aliyeitwa

Lawi vilevile. Aliandika Habari Njema ya kwanza.

8. **Tomasi**, aliyeitwa Mpacha. Huyu alisema hataamini ya kwamba Bwana amefufuliwa kufika saa atakapoona kitu kuhakikisha neno hili.
9. **Yakobo, mwana wa Alufayo**. Labda ni yeye aliyekuwa mwongozi ndani ya kanisa kwa Yerusalema, nyuma ya kuuawa kwa Yakobo, mwana wa Zebedayo, na Herode.
10. **Simoni** aliyeitwa **Zelote**. Tunaona maneno machache tu juu yake ndani ya Maandiko Matakatifu.
11. **Yuda**, **mwana wa Yakobo**. Labda alikuwa yeye aliyeandika Barua ya Yuda (Tadeo ndilo jina lake la jamaa, Mt. 10:3; Marko 3:18).
12. **Yuda Iskariota,** mtu wa Keriota katika Yuda, mwanafunzi wa pekee asiyekuwa mtu wa Galilaya. Alitoa Bwana wetu kwa adui zake, na Yesu alimwita "mwana wa upotevu."

Wanafunzi hawa hawakuwa wote wenye akili au uwezo zaidi. Walikuwa watu namna namna. Neno ambalo liliwafunganisha pamoja na kuwafanyiza wakubwa lilikuwa ukaribu na uaminifu wao kwa Bwana Yesu. Tunafikiri walikuwa vijana wenye miaka 20-30 wakati Mwokozi alipowachagua. Vijana wanajifunza mbio zaidi, wana bidii zaidi, nao ni tayari kupita kuvumilia magumu. Alichagua wanafunzi kumi na wawili tu, watu waliofaa kabisa kwa kazi ambayo alitaka wafanye. Aliweza kuwatuma kufanya kazi hii, na watu watawaamini na kuokolewa kwa sababu ya ushuhuda wao, na watakaa kufanya vivyo hivyo, na kuleta tena watu wengine kwa Bwana hata mwishoni dunia nzima itasikia Habari Njema.

Nyuma ya kuchagua wanafunzi ilikuwa lazima kuwafundisha kawaida na utaratibu wa ufalme wa Mungu. Baki la sura hii linajumlisha tabia na mwenendo inayopasa kuonekana ndani ya maisha ya wanafunzi wa Bwana Yesu.

**6:17-19** Hotuba inayofuata ni mbali na hotuba juu ya mlima katika Matayo 5-7. Ile katika Matayo ilitolewa juu ya mlima; ile hapa katika Luka ilitolewa pahali pa uwanda. Ile mlimani ilikuwa na heri, ndiyo baraka tu; ile ya Luka ilikuwa na heri na ole vilevile. Kuna tofauti nyingine katika hotuba hizi, kwa masemo, urefu, vivi hivi.

Ona ya kwamba Bwana alitoa hotuba hii kali juu ya kuwa mwanafunzi wake kwa **makutano** vilevile, si kwa wale wanafunzi kumi na wawili tu. Ni kama wakati makutano makubwa walipofuata Yesu, alipima roho zao kwa njia ya kusema nao waziwazi, bila kuficha magumu. Mtu mmoja alisema Kristo alibembeleza watu kwanza na masemo polepole, na nyuma aliwapepeta kuondosha wale ambao hawakumfuata na roho ya kweli.

**Watu** walikuwa wamefika **toka Yudea yote, na Yerusalema** kwa upande wa kusini, toka **Tiro na Sidona** kwa upande wa kaskazini-mangaribi, Wayuda na watu wa Mataifa vilevile. Wagonjwa na wenye pepo wachafu walisonga Yesu waweze kumgusa; wakijua ya kwamba **uwezo** wa kuponyesha **ulitoka kwake.**

Lazima tufahamu ya kwamba mafundisho ya Mwokozi ni namna nyingine kabisa na mafundisho yote watu waliyopewa mbele. Tukumbuke ya kwamba alikuwa akikwenda msalaba. Atakufa, atazikwa, na siku ya tatu atafufuka tena na kurudia mbingu. Sharti habari njema za wokovu bila bei zienee pahali pote duniani. Sharti watu wazisikie ili waweze kukombolewa. Namna gani watu wa dunia pote wataweza kusikia Habari Njema? Viongozi vya wakati wa sasa wangekutanisha jeshi kubwa la watu, na mali, na vyakula kwa mahitaji yao, vivi hivi.

### G. Heri na Ole (6:20-26)

**6:20** Yesu alichagua **wanafunzi** kumi na wawili, akawatuma wakiwa masikini, wenye njaa na kuteswa. Dunia nzima itasikia Habari Njema kwa njia ile? Ndiyo, kwa njia ile ile tu, hakuna njia nyingine! Mwokozi alianza hotuba yake na heri ine na ole ine. **"Heri ninyi masikini."** Hakusema heri watu masikini, lakini heri *ninyi* masikini. Umasikini si baraka; unafanana na laana mara nyingine. Hapa Yesu anasema juu ya kuchagua umasikini sisi wenyewe kwa ajili yake. Hasemi juu ya watu walio masikini kwa sababu ya uvivu au hasara yo yote. Anasema juu ya wale wanaochagua kuwa masikini ili waweze kushiriki habari za Mwokozi na watu wengine. Umasikini namna hii ni akili kabisa. Kama wanafunzi wangalikuwa tajiri, kama watu wengi wangalifika karibu nao na kusema wanataka kufuata Kristo, wakitumaini kwamba watageuka watajiri vilevile. Na vilevile kama wanafunzi wangalikuwa tajiri wasingalijuana na baraka ya kulazimishwa kutegemea Bwana kwa mahitaji yao ya kila siku. Wenye ufalme wa Mungu ni wale wanaofurahi kuwa na mali ya kutosha mahitaji yao ya kila siku tu, na kutumika na mali yo yote kupita ile kwa kazi ya Bwana.

**6:21 "Heri ninyi wenye njaa sasa.**" Bwana hasemi hapa juu ya watu elfu elfu wanaokosa vyakula vya kutosha. Anasema juu ya wanafunzi wake wanaochagua kula vyakula vya bei chini ili watu wengine waweze kusikia Habari Njema. Wanafunzi hawa watapokea zawabu siku nyingine kwa sababu walijinyima sasa.

**"Heri ninyi munaolia sasa."** Machozi ya wasioamini hayana faida. Bwana Yesu anasema hapa juu ya kutoa machozi kwa ajili ya wapotevu, kwa sababu ya matengo kanisani. Anasema juu ya taabu na huzuni yote tunayopata ndani ya kazi yetu kwa Bwana wetu. Wale wanaopanda na machozi watavuna na furaha.

**6:22 "Heri ninyi wakati watu watakapowachukia, na kuwatenga ninyi … kuwatukana ninyi, na kutupa inje jina lenu kama kitu kibaya."** Baraka hii si kwa watu wanaoteswa kwa sababu ya zambi zao au ujinga wao wenyewe. Ni kwa wale wanaochukiwa, na kutengwa, na kutukanwa, na kusingiziwa kwa sababu ya *uaminifu wao kwa Kristo.*

Maneno sita ambayo yanatusaidia kufahamu heri hizi ndiyo haya: **"kwa ajili ya Mwana wa watu."** Maneno haya yote yaliyo mabaya au magumu yanageuka heri au baraka kama tukiyavumilia kwa ajili ya mapendo yetu kwa Bwana.

**6:23** Mateso kwa Kristo yanatuletea shangwe na **zawabu kubwa mbinguni**. Wale wanaoteswa sasa wana ushirika na watumishi waaminifu wa Mungu wa zamani.

Heri hizi ine zinaonyesha namna ya mtu anayefaa kabisa kwa ufalme wa Mungu: mtu anayejikana mwenyewe na anayeendelea na uaminifu.

**6:24 Lakini** ole ine zinazofuata zinasema juu ya wale walio na faida ndogo zaidi ndani ya ufalme mpya wa Mungu. Ni huzuni, kwa sababu hawa ndio watu wanaoheshimiwa zaidi duniani sasa. **"Ole wenu wenye mali."** Ni vibaya sana kujivimbishia mali sasa wakati elfu za watu wanapokufa kwa njaa kila siku, na wakati watu wengi sana wanapokosa njia kusikia habari njema ya wokovu kwa njia ya kuamini Kristo. Wakristo wawaze sana juu ya maneno haya ya Kristo kama wakijaribiwa kujivmbishia mali duniani, wakifikiri kwamba labda kwa wakati wa kuja watahitaji mali hii wao wenyewe. Ni vibaya kuishi kwa dunia hii ya sasa. Ona vilevile ya kwamba **ole** hii kwa watajiri inahakikisha ya kwamba wakati Bwana Yesu aliposema mbele ndani ya

shairi 20, "Heri ninyi masikini" hakufikiri juu ya umasikini wa roho. Ingalikuwa hivi kama shairi 24 lingesema "ole kwenu ninyi mulio tajiri katika roho," ndiyo maana isiyotosha hata kidogo. Wenye mali ambao hawaitumii kwa baraka ya milele ya wengine **wamepokea** zawabu yo yote watakayopokea – ndiyo furaha ya vitu walivyotaka kujipatia hapa duniani.

**6:25 "Ole wenu munaoshiba."** Hawa ndio waamini wanaokula ndani ya hoteli na kulipa bei kubwa kwa vyakula vyao, na wanaonunua vyakula vya bei gali dukani. Bwana anasema wata**ona njaa** kwa wakati wa kuja, maana siku atakapogawa zawabu kwa waamini ambao walijikana wenyewe kwa kumtumikia na uaminifu.

**"Ole wenu munaocheka sasa."** Ole hii ni kwa wale wanaoshinda saa nyingi wakijifurahisha na michezo na furaha za dunia. Ni kama kusudi la maisha yao ni kujifurahisha wenyewe tu na wanasahau kabisa taabu na upotevu wa watu wasiojua Mwokozi bado. Watu **wanaocheka sasa wataomboleza** na **kulia** wakati watakapofahamu umasikini wa roho zao na kukumbuka namna walivyopoteza maisha yao kwa njia ya kuishi kwa kujifurahisha wenyewe.

**6:26 "Ole wenu wakati watu wote watakaposema mema juu yenu."** Kwa nini? Kwa sababu neno hili linaonyesha wazi ya kwamba unapunguka katika mwenendo na ushuhuda wako kwa Kristo. Habari Njema inachukiza waovu. Wale wanaopokea sifa toka watu wa dunia ndio wale wanaofungana na **manabii wa uwongo** wa Agano la Kale waliobembeleza watu kwa njia ya kuwaambia maneno waliyotaka kusikia. Waliweka roho juu ya kupendeza watu kupita kusifiwa na Mungu.

### H. Silaha ya siri ya Mwana wa watu: Mapendo (6:27-38)

**6:27-29a** Sasa Bwana Yesu alifunulia wanafunzi silaha moja ya siri – silaha ya **mapendo**. Silaha hii itawasaidia sana sana katika kazi yao kueneza Habari Njema duniani. Lakini wakati Bwana anaposema juu ya **mapendo**, si namna ya mapendo ya binadamu. Ni mapendo *yasiyo ya ulimwengu*. Ni mapendo ya roho yanayoonekana ndani ya watu waliozaliwa tena tu. Si ndani ya mtu asiyekaliwa na Roho Mtakatifu. Inawezekana kwa mwuaji kupenda watoto wake mwenyewe, lakini haya si namna ya mapendo Yesu anayosema juu yake hapa. Kwa mapendo ya roho inatupasa *kuchagua kupenda* hata watu wabaya na adui. Mtu ye yote anaweza kupenda rafiki zake, lakini anahitaji mapendo ya roho kupenda adui zake. *Haya* ndiyo namna ya mapendo ambayo tunasoma juu yake katika Agano Jipya (kwa Kiyunani ni *agapê*). Ni **kutendea mema wale ambao wanawachukia ninyi, kuwabariki wale ambao wanawalaani ninyi, kuwaombea wenye kufanya jeuri kwenu;** ni kugeuza shavu la pili kama mtu akikupiga shavu moja.

F.B. Meyer alieleza:

> Ni mapendo kwa wale ambao ni nguvu kupenda … mapendo yanayofurahi pamoja na kweli, yanatumaini maneno yote, yanavumilia maneno yote, hayapunguki hata kidogo – mapendo ya namna hii yanawezekana kwa uwezo wa Roho Mtakatifu tu.[7]

Hakuna neno linaloweza kushinda mapendo namna hii. Watu wa dunia wanapigana na wale ambao wanawatendea mabaya. Hawajui namna gani kutendea wale ambao wanawarudishia mema kwa mabaya.

**6:29b-31** Mwenye mapendo namna hii akiibiwa hiya yake, ni tayari kumpa mwizi kanzu yake vilevile. Akiibiwa kitu cho chote haombi kitu hiki kirudishwe kwake. Anatendea watu mema anayotaka kutendewa mwenyewe.

**6:32-34** Wasioamini wanaweza **ku-**

**penda watu wale ambao wanawapenda.** Ni desturi ya watu kufanya hivi, na wanaweza kufanya hivi bila kuwa na uzima wa Mungu rohoni.

**6:35** Hivi Yesu alisema tena ya kwamba inatupasa **kupenda adui zetu, kutenda mema, na kukopesha, bila kutumaini kupata kitu tena.** Ni wazi ya kwamba wale wanaotenda hivi ni Wakristo na **wana wa Mungu aliye juu.** Ndiyo watu *hawageuki* wana wa Mungu kwa njia ya matendo namna hii; neno hili linawezekana tu kwa njia ya kuamini Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi (Yoane 1:12). Lakini kwa njia ya kutenda hivi waamini wa kweli *wanaonekana* kwa watu wa dunia kama wana wa Mungu. Mungu alitutendea sisi namna tunavyosoma ndani ya mashairi 27-35. **Yeye ni mwema sana kwa watu wasio na shukuru, na waovu.** Sisi tukitenda hivi tunaonyesha ya kwamba tumezaliwa na Mungu, na tuko watu wa jamaa ya Mungu.

**6:36** Kuwa na **huruma** ni kusamehe wakati tungeweza kulipiza kisasi. Mungu **Baba** alikuwa na **huruma** kwa sisi kwa njia ya kutokutuazibu namna tulivyostahili, na anataka sisi kuwa na huruma kwa watu wengine vilevile.

**6:37** Kuna maneno mawili ambayo wenye mapendo hawafanyi – **Hawahukumu** na **hawapatilizi.** Yesu alisema, **"Musihukumu na hamutahukumiwa."** Haifai tuhukumu makusudi ya matendo ya watu kwani hatujui roho zao na kwa sababu gani wanafanya maneno wanayofanya. Na vilevile haifai tuhukumu waamini wengine juu ya matendo yao au kipimo cha mali wanayotolea Bwana (1 Kor. 4:1-5). Ni Mungu aliye Mwamuzi wa maneno yote namna hii. Haifai tuwe na roho ya kulaumu na kukaripia isiyopatana na sheria ya mapendo.

Hata hivi ni *lazima* kwa Wakristo kuhukumu maneno fulani. Sharti tupime kama watu wengine ni waamini wa kweli ili tuweze kutambua nira na wasioamini (2 Kor. 6:14). Sharti wahukumu zambi ndani ya jamaa na ndani ya kanisa. Ni lazima tufahamu yaliyo mema au mabaya, bila kuhukumu makusudi au kuharibu sifa njema ya mtu.

**"Achilieni na mutaachiliwa."** Inatupasa kuwa tayari kusamehe wengine kama tukitaka kusamehewa sisi wenyewe. Lakini mashairi mengine yanafundisha ya kwamba tukipokea Kristo kwa imani, zambi zetu zinasamehewa, bila sisi kusamehe wengine. Basi maneno haya yanapatana namna gani? Kuna usamehe namna mbili – usamehe wa *mwamuz*i na usamehe wa *mzazi. Usamehe wa mwamuzi* ndio usamehe wa Mungu kwa kila mtu anayeamini Bwana Yesu Kristo. Ni kusema Kristo amebeba azabu ya zambi hii, na hakuna hukumu tena kwa mwenye zambi anayeamini.

*Usamehe wa mzazi* ni usamehe wa Mungu Baba kwa mtoto wake ambaye alikosa na aliyekiri na kuacha zambi yake. Halafu mwamini anarudishwa tena kwa upatano na ushirika katika jamaa ya Mungu, bila azabu kwa zambi. Kama Baba, Mungu hawezi kutusamehe wakati tusipokuwa tayari kusamehe ndugu zetu. Yeye mwenyewe hafanyi hivi na hawezi kuwa na upatano na wale wanaokataa kusamehe wenzao. Ndani ya shairi hili Yesu alifikiri juu ya usamehe wa mzazi wakati aliposema **"na mutaachiliwa"** (maana mutasamehewa).

**6:38** Alama ya mapendo ni kutoa (ona Yoane 3:16; Efe. 5:25). Utumishi wa Wakristo ni utumishi wa kutoa. Wale wanao**toa** na ukarimu wanapokea zawabu ya ukarimu. Tunaona hapa mfano wa mtu aliye na mfuko kwa nguo yake upande wa mbele. Anabeba mbegu ndani ya mfuko huu. Ukubwa wa ma-

vuno yake utakuwa kwa kipimo anachosambaza mbegu hii. Zawabu yake itakuwa **kipimo kizuri kilichoshindiliwa, na kusukwasukwa na kumwangika.** Anaipokea katika kifua chake ni kusema katika mfuko wa nguo yake. Tunaona neno hili tena na tena ndani ya maisha yetu. Tunavuna kwa kipimo tunachopanda. **Namna tunavyotendea** wengine **tutatendewa** wenyewe. Tukipanda vitu na mali ya dunia, tutavuna hazina kubwa sana ya roho. Ni kweli vilevile ya kwamba vyote tunavyochunga kwa sisi wenyewe tunavipoteza, lakini vyo vyote tunavyotoa tunabaki navyo.

### I. Mfano wa mdanganyifu kipofu (6:39-45)

**6:39** Tumeona ya kwamba Bwana Yesu alifundisha wanafunzi wake kuwa wenye kutoa. Sasa aliwaonya ya kwamba wanaweza kuwa baraka kwa watu wengine kwa kipimo cha hali yao yenyewe ya roho tu. **Kipofu** hawezi **kuongoza kipofu** bila kuanguka wao wawili katika shimo. Hatuwezi kutoa tusiyokuwa nayo sisi wenyewe. Kama tukiwa vipofu kwa kweli nyingine za Neno la Mungu, hatuwezi kusaidia watu wengine na kweli hizi. Ukosefu wo wote ndani ya mwenendo wetu wa roho utapitishwa kwa wanafunzi wetu.

**6:40 "Mwanafunzi hapiti mwalimu wake, lakini kila mtu aliye mtimilifu atakuwa kama mwalimu wake."** Mtu hawezi kufundisha maneno asiyojua. Hawezi kuongoza wanafunzi wake kuwa na mwenendo wa karibu na Bwana kupita ukaribu wake mwenyewe. Kwa kipimo anachowafundisha wanageuka kufanana naye, lakini hawataweza kumpita. Mwanafunzi aliye mtimilifu anafika kwa kipimo cha bwana wake. Ukosefu wo wote katika mwenendo na mafundisho ya roho ya mwalimu utapitishwa kwa wanafunzi wake vilevile.

**6:41-42** Kweli hii inaonyeshwa hata wazi kupita ndani ya mfano wa **kitakataka** na **boriti**. Siku moja mtu fulani anapita sakafu ya nafaka pahali wanapopura ngano, na upepo unafikisha kipande kidogo sana cha kapi jichoni mwake. Anajaribu sana kuondosha kitakataka hiki, lakini uchungu wake unaongezeka tu. Saa ile ile mtu mwingine anapita njiani, anaona uchungu wa mtu wa kwanza na anataka kumsaidia, lakini kuna **boriti** ndani ya **jicho la mtu** huyu wa pili! Hivi hawezi kumsaidia kwa sababu yeye mwenyewe hawezi kuona vizuri. Mafundisho ya habari hizi ni wazi: Mwalimu hawezi kusema na wanafunzi wake juu ya vipaku ndani ya maisha yao kama ana vipaku namna hii na labda vipaku vikubwa kupita ndani ya maisha yake mwenyewe. Tukitaka kusaidia watu wengine, lazima maisha yetu yawe bila kipaku.

**6:43-45** Kwa mfano wa ine Bwana alitumika na **mti** na **matunda** yake. Mti unazaa matunda **mema** au **mabaya**. Tunapima mti kwa njia ya matunda na kipimo cha matunda unayozaa. Ni vivyo hivyo na maneno ya kufuata Yesu. Mtu aliye na roho safi na anayetembea karibu na Bwana anaweza kutoa baraka kwa watu wengine **katika hazina njema ya moyo wake.** Lakini mtu mbaya katika hazina mbaya ya moyo wake **anatoa lililo baya.**

Hivi ndani ya mashairi 39-45 Bwana alifundisha wanafunzi ya kwamba mwenendo wao na hali yao ya roho ni neno kubwa kupita maneno yo yote wanayosema au kufanya.

### J. Bwana anataka utii (6:46-49)

**6:46 "Kwa nini munaniita Bwana, Bwana, nanyi hamutendi maneno ambayo ninasema?"** Maana ya *Bwana* ni ya kwamba ana amri juu ya maisha yetu mazima, ya kwamba tuko mali yake na ni lazima kwetu kufanya neno lo lote analoagiza. Kumwita **Bwana** na

kukataa kumtii hakupatani hata kidogo. Haitoshi kumwita tu Bwana na kinywa tu. Tukimwamini na kumpenda kweli tutamtii vilevile. Hatumpendi wala kumwamini kweli kama tusipofanya maneno anayosema.

Unaniita "Njia" na hunifuati,
Unaniita "Uzima" na huishi ndani
yangu,
Unaniita "Bwana" na hunitii,
Kama nikikuhukumu, usinishitaki.

Unaniita "Mkate" na hunikuli,
Unaniita "Kweli" na huniamini,
Unaniita "Bwana" na hunitii wala
kunitumikia,
Kama nikikuhukumu,
usinishikaki

*– Geoffrey O'Hara*

**6:47-49** Kusimamisha kweli hii hata nguvu kupita, Bwana anatupasha habari za wajengaji wawili. Ni desturi yetu kutumika na habari hizi kwa kuhubiri Habari Njema; tunasema mwenye akili ni kama mwamini na anaokolewa; mpumbavu ni mfano wa mtu anayekataa kuamini Kristo na anapotea. Ndiyo, tunaweza kueleza habari hizi hivi, lakini kuna maana nyingine vilevile.

Mwenye akili ndiye **anayefikia** Kristo (kupata wokovu), **anayesikia masemo** yake (mafundisho), na **kuyafanya** (kutii). Anajenga maisha yake sawasawa na mafundisho ya Kristo, namna tunavyoona ndani ya sura hii. Hii ndiyo njia nzuri kujenga maisha yako. Wakati wa matata (tufani na garika) nyumba hii inasimama **imara** kwa sababu **imejengwa juu ya mwamba,** ndiye Kristo na mafundisho yake.

Mpumbavu ni yule anayesikia mafundisho, lakini hayapokei (uasi). Anajenga maisha yake juu ya maneno ambayo yeye mwenyewe anafikiri ni mema, ndiyo maneno mabaya ya dunia hii. Wakati wa taabu na matata **nyumba** yake **inayokosa msingi** inapelekwa na garika. Labda roho yake imeokolewa lakini maisha yake yamepotea bila faida kwa Mungu.

Mwenye akili ndiye mwenye njaa, anayeomboleza na anayeteswa – kwa ajili ya Mwana wa watu. Watu wa dunia wangeita mtu namna hii mpumbavu; Yesu anamwita mwenye akili.

Mpumbavu ndiye anayekula vyakula vya bei nyingi, ambaye anajifurahisha na maneno mengi ya dunia, na anayependwa na watu wengi. Watu wa dunia wanamwita mwenye akili. Yesu anamwita mpumbavu.

## 6. MWANA WA WATU ANAENEZA UTUMISHI WAKE (7:1 – 9:50)

### A. Mtumwa wa akida anaponyeshwa (7:1-10)

**7:1-3** Nyuma ya kumaliza hotuba yake Yesu aliondoka katika makutano, **akaingia Kapernaumu**. Pale **wazee wa Wayuda** walikutana naye kumwomba kusaidia mtumishi wa akida Mtaifa. Ni kama akida huyu alitendea Wayuda mema, na aliwajengea sunagogi. Maakida wengine tunaosoma habari zao katika Agano Jipya walikuwa watu wema vilevile. Ona Luka 23:47; Matendo 10:1-48.

Haikuwa desturi za maakida kupenda watumwa wao hivi. Wakati **mtumwa** huyu aliposhikwa na ugonjwa akida aliomba **wazee wa Wayuda** kusihi Yesu kumponyesha. Hatusomi juu ya akida Mroma mwingine aliyeomba Yesu kusaidia **mtumwa.**

**7:4-7** Wazee hawa hawakuamini Yesu wao wenyewe, lakini urafiki wao kwa akida huyu uliwasukuma kufikia Yesu kwa wakati huu wa hitaji. Walisema juu ya akida ya kwamba akida **anastahili**. Lakini wakati akida mwenyewe alipofika karibu na Yesu alisema "**sistahili**," maana yake "sina heshima na ukubwa wa kutosha."

Matayo aliandika ya kwamba akida yeye mwenyewe alifikia Yesu. Hapa katika Luka alituma wazee. Wote wawili walisema kweli. Kwanza alituma wazee; nyuma yake alikwenda kukutana na Yesu yeye mwenyewe.

Unyenyekevu na imani ya akida huyu zinatushangaza. **Hakufikiri** kwamba **alistahili** kwa Yesu **kuingia** nyumba yake. Na vilevile hakufikiri **alistahili kufika karibu** na Yesu yeye mwenyewe. Lakini aliamini ya kwamba Yesu aliweza kuponyesha toka mbali, maana bila kufika yeye mwenyewe, lakini kwa njia ya kusema **neno** tu.

**7:8** Akida aliendelea kueleza ya kwamba alifahamu maneno ya **amri** na usimamizi. Yeye mwenyewe alikuwa chini ya amri ya serikali ya Waroma na ilimpasa kutimiza maagizo yao. Na zaidi ya ile alikuwa na **amri juu ya askari** waliotii maagizo yake mara moja. Alitambua ya kwamba amri ya Yesu juu ya gonjwa ilikuwa kama ile ya Waroma juu yake mwenyewe, na kama amri yake juu ya askari waliokuwa chini yake.

**7:9,10** Tunafahamu kwa nini **Yesu alishangaa** juu ya imani ya akida mtaifa huyu. Hakuna mtu katika **Israeli** aliyekiri na uhodari namna hii ya kwamba Yesu ni mwenye amri zote. **Imani kubwa namna hii** haikuweza kukosa zawabu. Wakati wazee waliporudia **nyumba** walikuta **mtumwa** alikuwa **amepona kabisa**.

Tunasoma mara mbili tu ndani ya vitabu vya Habari Njema ya kwamba Yesu **alishangaa** – hapa juu ya imani ya akida Mtaifa, na kwa sababu ya kutokuamini kwa Israeli (Marko 6:6).

### B. Kufufuliwa kwa mwana wa mjane (7:11-17)

**7:11-15 Naina** ulikuwa mji mdogo kwa upande wa kusini-mangaribi wa Kapernaumu. Wakati Yesu alipokuwa akikaribia mji ule aliona watu wakikwenda kuzika **mwana wa pekee** wa **mjane**. Bwana **alihurumia** mama huyu aliyefiwa mwana wake. Aligusa jeneza kusimamisha watu, akaagiza **kijana kusimama**. Mara moja uzima ulirudia maiti, na kijana **alikaa**. Halafu Yule aliye Bwana wa mauti vilevile, si juu ya ugonjwa tu, alimrudisha **kwa mama yake.**

**7:16,17** Watu **waliogopa sana.** Walikuwa wameona ajabu la uwezo kabisa, ndilo kufufuliwa kwa mfu. Waliamini kwamba Bwana Yesu alikuwa **nabii mkubwa** ambaye alitokea kwao toka Mungu. Lakini tunafikiri hawakufahamu ya kwamba Yesu *mwenyewe* alikuwa Mungu wakati waliposema, **"Mungu ameangalia watu wake."** Walifikiri ajabu hili lilihakikisha ya kwamba Mungu alikuwa akitumika katikati yao. Habari zenyewe zilienea katika **inchi yote kando kando.**

Mganga Luka alitupasha habari za watoto watatu waliokuwa "wa pekee" waliosaidiwa na Yesu: mwana wa mjane; binti ya Yairo (8:42); na mtoto aliyekaaliwa na pepo wachafu (9:38).

### C. Mwana wa watu anasaidia imani ya mtangulizi wake (7:18-23)

**7:18-20** Habari za maajabu haya zilifikia **Yoane** Mbatizaji aliyekuwa gerezani mwa boma la Machaerus, kwa pwani wa upande wa mashariki wa Bahari ya Chumvi. Kama Yesu alikuwa Masiya kweli, basi kwa sababu gani hakutumika na uwezo wake kufungua Yoane toka gereza? Hivi Yoane alituma **wawili wa wanafunzi wake** kuuliza Yesu kama yeye ni kweli Masiya, au kwamba Kristo hajafika bado. Labda tunashangaa juu ya ulizo hili la Yoane, lakini vizuri tukumbuke ya kwamba wakati wa taabu au maumivu makubwa imani yetu inaweza kupunguka vilevile kwa muda mdogo.

**7:21-23** Yesu alijibu Yoane na kumkumbusha ya kwamba alikuwa akifanya maajabu namna manabii wa-

liyotabiri Masiya atafanya (Isa 35:5,6; 61:1). Halafu aliongeza neno dogo lingine kwa Yoane, **"Heri yeye asiyechukizwa nami."** Labda lilikuwa kemeo kwa Yoane, maana Yoane **alichukizwa** kweli kwa sababu Yesu hakuanza kutawala na kutenda namna watu walivyofikiri Masiya atatenda. Au labda lilikuwa onyo kwa Yoane asiache kumwamini.

C. G. Moore alisema,

> Hakuna neno linalopima imani yetu kupita kuona Yesu akifunua uwezo wake bila kutumika nao … Kweli neema nyingi inahitajiwa wakati wajumbe wanaporudi wakisema: "Ndiyo, ana uwezo wote, naye ni kweli Masiya, lakini hakusema hata neno moja juu ya kukuondosha gerezani …" Hakuna elezo kwa sababu gani ni hivi, na kwa nini milango ya gereza haikufunguliwa, na halafu neno hili: "Heri yeye asiyechukizwa nami." [8]

### D. Mwana wa watu anasifu mtangulizi wake (7:24-29)

**7:24** Hatujui kama Yesu alisema nini na Yoane wakati walipokuwa peke yao, lakini mbele ya watu alikuwa na sifa tu kwa mtangulizi wake. Wakati makutano ya watu walipokwendea jangwa karibu na Yorodani, walifikiri watakuta nini? Mtu zaifu mwenye kugeukageuka? Sivyo. Hakuna mtu aliyeweza kusema juu ya Yoane Mbatizaji ya kwamba alikuwa kama **unyasi ukitikisikwa kwa upepo**.

**7:25** Walifikiri watakuta mchezaji mwenye mali nyingi akiishi katika anasa? Mtu namna ya wale wanaokaa **nyumbani mwa mfalme** kwa faida yao wenyewe?

**7:26** Sivyo. Walikwenda kuona **nabii** – aliyetangaza neno la Mungu aliye hai si neno kama itakuwa hasara kwake. Ndiyo, alikuwa **mkubwa kupita nabii**.

**7:27** Yeye mwenyewe alitajwa ndani ya unabii wa Agano la Kale na alipewa heshima kubwa ya kukutanisha watu na Mfalme. Yesu alitaja shairi toka unabii wa Malaki, ndilo 3:1 kuonyesha ahadi ndani ya Agano la Kale ya kwamba Yoane atakuja. Lakini aligeuza neno moja saa alipofanya hivi: Ndani ya Malaki 3:1 tunasoma, "Tazameni, ninatuma mjumbe wangu, naye atatayarisha njia mbele yangu." Lakini wakati Yesu alipotaja shairi hili alisema, "Tazama, ninatuma mjumbe wangu mbele ya uso wako, atakayetengeneza njia yako mbele yako." Kwa pahali pa kusoma "mbele *yangu*" tunasoma "mbele **yako.**"

Godet alieleza neno hili hivi:

> Kwa mafikiri ya nabii, yule aliyekuwa akituma, alikuwa vilevile yule mbele yake njia ilitayarishwa, ndiye Yehova. Hivi tunasoma *mbele yangu* ndani ya Malaki. Lakini Yesu alikuwa akisema juu yake mwenyewe, si juu ya Baba, hivi hatuoni Yehova akisema juu yake mwenyewe, lakini akisema kwa Yesu: *mbele yako*. Maneno haya yanaonyesha ya kwamba kwa mafikiri ya nabii, na ya Yesu, kutokea kwa Masiya ni tokea kwa Yehova. [9]

**7:28** Yesu aliendelea kusifu Yoane akisema ya kwamba **"katika waliozaliwa na wanawake, hakuna nabii mkubwa kuliko Yoane Mbatizaji."** Maana yake haiko ya kwamba alikuwa mtu mzuri kuliko, lakini kwamba alipewa kazi ya heshima kubwa, ndiyo kuwa mtangulizi wa Masiya. Kulikuwa na watu wengine wenye bidii na heshima na mapendo makubwa kwa Bwana kama Yoane. Lakini hakuna mtu mwingine aliyepewa heshima ya kutangaza kuja kwa Mfalme. Bwana aliongeza ya kwamba **aliye mdogo katika ufalme wa Mungu ni mkubwa kuliko** Yoane. Kufurahishwa na baraka za **ufalme** ni neno **kubwa kupita** kuwa mtangulizi wa Mfalme.

**7:29** Ndani ya shairi hili Yesu alikumbusha wasikiaji wake namna watu walivyopokea mahubiri ya Yoane siku

ile jangwani. **Watu** wote, hata wale waliojulikana kuwa wenye zambi, kama **watoza kodi** walitubu zambi zao na **walibatizwa** katika Yorodani. Waliamini mahubiri ya Yoane, na kwa njia hii **walihesabia Mungu kuwa na haki,** maana yake Mungu alitenda kwa haki wakati alipotaka watu wa Israeli kutubu kwanza kusudi Kristo aweze kuwatawala. Maana ya neno hili *kuhesabia haki* hapa si kufanyiza Mungu haki; hakuna mtu anayeweza *kufanyiza* Mungu kuwa mwenye haki. Maana yake ni ya kwamba maagizo na masharti ya Mungu yalikuwa haki.

### E. Mwana wa watu anashitaki kizazi chake mwenyewe (7:30-35)

**7:30-34 Wafarisayo** na walimu wa sheria walikataa kupokea ubatizo wa Yoane, na hivi **walikataa** shauri la Mungu kwa baraka yao. Ndiyo, haikuwezekana kupendeza **kizazi** ambacho waliongoza. Yesu aliwasawanisha na **watoto** waliocheza **katika soko** bila kuweza kupatana kama watacheza ndoa au maziko. Walikuwa wakaidi na wenye kuhangaika. Hawakukubali neno lo lote Mungu alilotaka kufanya katikati yao. **Yoane Mbatizaji** alikuwa mgumu na mwenye kujikana mwenyewe. Hawakufurahi juu ya maisha yake, wakisema alikuwa mwenye pepo. **Mwana wa watu** alikula pamoja na **watoza kodi na wenye zambi,** maana yake alikaa pamoja na wale ambao alifikia kubariki. Lakini Wafarisayo hawakufurahi juu ya neno hili vilevile, wakamwita **mlafi** na mnywaji mvinyo. Hakuna neno lililoweza kuwapendeza!

Mwalimu Ryle, anatuonya:

> Sharti tuache kujaribu kupendeza watu wote kwani haiwezekani, na kujaribu kufanya hivi ni kupoteza saa bure. Vizuri tufuate Kristo tu, si neno kama watu wa dunia wanasema nini. Hatutaweza kamwe kuwapendeza wala kunyamazisha mashitaki yao. Walinungunikia Yoane Mbatizaji na nyuma yake walinungunikia Bwana wake. Watakaa kufanya hivi kufika wakati hata mmoja wa wafuata wake asipobaki hai duniani. [10]

**7:35 "Lakini hekima imepata haki yake kwa watoto wake wote." Hekima** hapa ndiye Mwokozi mwenyewe.Wanafunzi wachache ambao wanamheshimu ni **watoto** wa hekima. Hata zaidi ya watu wakimkataa, wanafunzi hawa waaminifu watashuhudia na maisha yao ya mapendo, utakatifu na uaminifu ya kwamba yeye ni kweli Masiya.

### F. Mwenye zambi anapakaa Mwokozi na mafuta (7:36-39)

**7:36** Ndani ya habari zinazofuata tunaona mfano wa neno hili. Kama Dr. H.C. Woodring alivyosema, "Kama ikishinda Mungu kufanyiza viongozi vya dini kuheshimu Kristo, atafanyiza makahaba kufanya hivi." Simoni, **Mfarisayo, aliita** Yesu kufikia nyumba yake na **kula pamoja naye**, labda kwa sababu alitaka kujua kupita juu ya Yesu, au labda kwa sababu ya uadui rohoni mwake mwenyewe.

**7:37,38** Mwanamke mwenye zambi aliingia chumbani wakati ule. Hatujui kabisa kama alikuwa nani. Watu wengine wanasema alikuwa Maria Magdalene, lakini hatuoni neno hili wazi ndani ya Maandiko Matakatifu. Mwanamke huyu **alileta chupa** la alabastro yenye malasi. Wakati Yesu alipokuwa akilala juu ya **malazi** na kula chakula, kichwa chake kikiwa karibu na meza, mwanamke **alisimama kwa miguu yake. Alinawa miguu yake na machozi yake, akaipangusa na nywele zake na kuibusu. Kisha aliipakaa na marasi** ya bei kubwa. Zawadi hii na kuabudu kwake kulionyesha ya kwamba kwa macho yake Bwana Yesu alistahili yote.

**7:39** Mawazo ya Simoni yalikuwa namna nyingine na yale ya mwanamke. Alifikiri ya kwamba ingalipasa manabii,

kama Wafarisayo, kukaa mbali na wenye zambi. **Kama** Yesu **angalikuwa nabii** kweli, asingaliruhusu **mwenye zambi** kumwonyeshea mapendo makubwa namna hii.

### G. Mezali ya wenye deni wawili (7:40-50)

**7:40-43** Yesu alijua mawazo ndani ya nia ya **Simoni,** akamwomba ruhusa na adabu kusema neno naye. Halafu na akili nyingi aliendelea kupasha habari za **mkopeshaji** na **wadeni wawili**. Mmoja alikuwa na **deni** ya dinari mia tano, na deni ya mtu wa pili ilikuwa makumi tano. **Wakati** watu wale wawili wasipoweza **kurudisha mali** yenyewe, mkopeshaji alizima deni zao. Halafu Yesu aliuliza Simoni kama **mtu gani angalipenda** mkopeshaji **kupita**, yule mwenye deni ya dinari mia tano au yule mwenye deni ya makumi tano. Mfarisayo alijibu vizuri, **"Ninazania yule aliyesamehewa zaidi."** Ndani ya mashairi yanayofuata Yesu aliendelea kuonyesha ya kwamba Simoni akisema hivi alijihukumu mwenyewe.

**7:44-47** Tangu Bwana **alipoingia nyumba** ya Simoni, mwanamke alimtendea na mapendo, lakini Mfarisayo hakupokea Yesu vizuri. Hakumpa maji kunawa miguu yake, hakumbusu wala kupakaa kichwa chake na mafuta. Kwa nini? Mwanamke alifahamu ya kwamba alikuwa amesamehewa zambi nyingi, lakini Simoni hakufikiri alikuwa na zambi nyingi. **"Naye aliyesamehewa kidogo alipenda kidogo."**

Yesu hakusema ya kwamba Mfarisayo hakuwa mwenye zambi kubwa sana, lakini ya kwamba Simoni hakukubali neno hili na hakupata usamehe. Kama angalifahamu ukubwa wa zambi zake kama angalipenda Bwana na mapendo makubwa sana kama kahaba. Sisi sote ni wenye zambi sana. Sisi sote tunaweza kupata usamehe, na kupenda Bwana sana.

**7:48** Halafu Yesu alitangaza wazi mbele ya watu wote ya kwamba **zambi** za mwanamke zilikuwa **zimesamehewa.** Hakupata usamehe wa zambi *kwa sababu ya* mapendo yake kwa Kristo, lakini mapendo yake kwa Bwana yalikuwa *tunda* la usamehe ambao alikuwa amepokea.

**7:49,50** Wageni wengine nyumbani mwa Simoni waliulizana rohoni mwao kama Yesu alikuwa na amri kusamehe zambi. Roho ya mtu wa asili inachukia neema, lakini Yesu alisema tena na **mwanamke** ya kwamba **imani** yake imemwokoa, hivi aende zake na salama. Hili ni neno ambalo wanganga wa sasa hawawezi kufanya. Hata wakijaribu kutoa uzuru kwa damiri za watu zenye mizigo mizito ya hatia, hawawezi kamwe kuletea watu furaha na salama kama Yesu anavyoweza.

Watu wengine wanasema Bwana Yesu akikula nyumbani mwa Mfarisayo ni mfano mzuri kwa Wakristo kuiga, na wanaanza kushiriki na wasioamini ndani ya furaha zao za dunia. Waza juu ya onyo la mwalimu Ryle juu ya neno hili:

> Bwana wetu alikuwa akifanya "kazi ya Baba wake" wakati alipokula nyumbani mwa Mfarisayo. Alieleza kwa Mfarisayo namna zambi zinavyoweza kusamehewa bila kulipa kitu. Alieleza siri ya mapendo ya kweli kwa Bwana na namna imani inavyookoa. Ni vizuri kwa Wakristo kufikia nyumba za wasioamini na kuiga Bwana Yesu na kusemezana na watu wa nyumba juu ya maneno ya Mungu na mahitaji ya roho zao, lakini waepuke kushiriki nao ndani ya maneno na anasa za dunia. [11]

### H. Wanawake wengine waliotumikia Yesu (8:1-3)

Ni vizuri kukumbuka ya kwamba ndani ya vitabu vya Habari Njema tunasoma juu ya habari chache tu za maisha na utumishi wa Bwana wetu. Roho Mtakatifu alichagua habari fulani na ali-

acha nyingi nyingine. Hapa tunasoma ya kwamba Yesu alihubiri habari njema ya **ufalme wa Mungu** pamoja na wanafunzi wake katika **miji na vijiji** vya Galilaya . Wakati walipofanya hivi, **wanawake** wengine waliosaidiwa na Bwana Yesu wao wenyewe, waliwatumikia, tunafikiri kwa njia ya kuwapatia vyakula na pahali pa kulala. Mmoja wao alikuwa **Maria Magdalene**. Watu wengine wanafikiri alikuwa mwanamke wa Magdala. Alikuwa amefunguliwa kwa njia ya ajabu toka utawala wa **pepo wabaya saba.** Jina la mwanamke mwingine lilikuwa **Yoana**, mke wa **mlinzi mali wa Herode.** Jina la mwingine lilikuwa **Susana**, na kulikuwa na wanawake **wengi wengine**. Bwana hakuona matendo yao ya mapendo bure! Hawakufikiri wakati waliposhiriki vitu na mali yao na Yesu, ya kwamba kwa nyakati za kuja Wakristo watasoma juu ya ukarimu wao.

Bwana Yesu alihubiri habari njema juu ya ufalme wa Mungu. **Ufalme wa Mungu** ndio pahali utawala wa Mungu unapokubaliwa hata kama hatuwezi kuuona na macho mara nyingine. Matayo anauita "ufalme wa mbinguni," lakini ni neno moja tu. Maana yake ni "Aliye juu anatawala katika ufalme wa watu" (Dan. 4:17) au "mbingu zinatawala" (Dan. 4:26).

Waza juu ya maendeleo ya ufalme ndani ya Agano Jipya:

1. Yoane Mbatizaji alitangaza ya kwamba ufalme wa mbinguni umekaribia (Mt. 3:1,2).

2. Halafu ufalme ulikuwa pale pale, maana Mfalme mwenyewe alikuwa katikati yao. Ona Luka 17:21. Hizi ndizo habari njema ambazo Yesu alitangaza. Alisema yeye ndiye Mfalme wa Israeli (Lk. 23:3).

3. Halafu tunaona taifa la Israeli wakikataa ufalme wa Mungu (Lk. 19:14; Yn. 19:15).

4. Leo ufalme ni siri (Mt. 13:11). Kristo, Mfalme, si hapa kwa wakati wa sasa, lakini utawala wake unakubaliwa ndani ya mioyo ya watu wengine duniani. Kwa njia moja ufalme kwa wakati wa sasa ni watu wote wanaokiri kukubali utawala wa Mungu, hata kama hawakuokolewa kweli. Tunaona neno hili ndani ya mfano wa mpandaji na mbegu (Lk. 8:4-15), mfano wa magugu na ngano (Mt. 13:24-30), na samaki ndani ya mkila (Mt. 13:47-50). Lakini kabisa kabisa wale tu waliogeuka na kuzaliwa tena (Mt. 18:3; Yn. 3:3) ni ndani ya ufalme. (Ona picha kwa Matayo 3:1,2.)

5. Ufalme utasimamishwa duniani siku nyingine na Bwana Yesu atatawala kwa miaka 1000 kama Mfalme wa wafalme na Bwana wa wabwana (Ufu. 11:15; 19:16; 20:4).

6. Muda wa mwisho wa ufalme unaitwa ufalme wa milele wa Bwana na Mwokozi Yesu Kristo (2 Pet. 1:11). Huu ndio ufalme wa milele.

### I. Mfano wa mpandaji (8:4-15)

**8:4-8 Mfano** wa **mpandaji** unaonyesha ufalme kwa wakati wa sasa. Unafundisha ya kuwa wakati wa sasa kuna waamini wa kweli ndani yake na wengine vilevile wanaosema tu kwamba wao ni watu wa Mungu. Ni onyo la nguvu juu ya **namna gani tunasikia** Neno la Mungu likihubiriwa na kufundishwa kwani wakati tunapolisikia, deni yetu kulitii inaongezeka na halafu Mungu atatufunulia kweli nyingine tena. Lakini kufunga masikio yetu kwa Neno la Mungu ni hasara kwetu. Bwana Yesu alisema **mfano huu** kwa **makutano ya watu wengi**, na aliueleza kwa wanafunzi wake nyuma.

Mfano ni juu ya **mpandaji mbegu, mbegu yake**, namna ine za udongo zilizopokea **mbegu**, na matunda ine.

| *Namna ya udongo* | *Tokeo* |
|---|---|
| 1. **Karibu na njia** | **Ilikanyagwa** na watu na **kuliwa** na ndege |
| 2. **Mwamba** | **Ilikauka** kwa sababu ya ukosefu wa **maji** |
| 3. **Miiba** | Ilizuizwa isikomee |
| 4. **Udongo mzuri** | **Ilizaa matunda** hata mia moja |

Bwana alimaliza mfano huu na maneno haya: **"Mwenye masikio ya kusikia asikie!"** Au kusema, wakati unaposikia neno la Mungu, waza sana juu ya namna gani unalipokea. Sharti mbegu ianguke ndani ya **udongo mzuri** kwa kuzaa matunda.

**8:9,10** Wakati **wanafunzi** walipouliza maana ya mfano huu, Bwana Yesu aliwaambia ya kwamba si watu wote watakaofahamu **siri za ufalme wa Mungu.** Wanafunzi **watawezeshwa** kufahamu mafundisho ya Kristo kwa sababu walikuwa tayari kuamini na kutii. Lakini na kusudi Yesu alifundisha kweli nyingi kwa njia ya **mifano** ili wale ambao hawakumpenda kweli **hawataweza kufahamu,** ili **wakiona hawataona, na wakisikia, wasitambue.** Ndiyo, waliona na kusikia na macho na masikio ya mwili. Walijua kwamba Yesu alikuwa amesema juu ya mpandaji mbegu na mbegu yake. Lakini **hawakufahamu** maana ya ndani ya mfano huu. Hawakufahamu kwamba mioyo yao ilikuwa migumu, bila toba, kama udongo wenye miiba, na ya kwamba maneno waliyosikia hayakuwa faida kwao.

**8:11-15** Bwana alieleza **mfano** huu kwa wanafunzi tu. Walikuwa wamekubali mafundisho waliyopokea mbele, hivi watapewa mafundisho mengine. Yesu alieleza ya kwamba **mbegu ndiyo Neno la Mungu,** maana kweli ya Mungu – mafundisho yake mwenyewe.

Wasikiaji **karibu na njia** walisikia neno, lakini nusu nusu tu. Halikugeuka sehemu ya maisha yao, hivi haikuwa nguvu kwa Shetani (ndege za hewa) kulikula.

Wasikiaji waliokuwa kama **mwamba** walisikia neno vilevile, lakini hawakuruhusu neno kuvunja roho zao ngumu, wakabaki bila kutubu. Mbegu haikunyeshwa maji, hivi ilikauka na kufa. Labda wakati waliposikia Neno kwanza walikiri na furaha kulipokea, lakini hawakuamini kwelikweli. Hawakuwa na **shina**. Wakati walipopata matata waliacha imani yao.

Ni kama mbegu iliyoanguka juu ya udongo katika miiba iliota vizuri kwa wakati, lakini ilionekana nyuma ya kwamba wasikiaji hawakuwa waamini wa kweli na hawakuendelea vizuri. **Masumbuko, mali na anasa ya maisha ya sasa** zilitawala maisha yao na kusonga Neno.

**Udongo mzuri** ndiyo waamini wenye **roho nzuri**. Wanapokea neno na wanaliruhusu kufanya kazi ndani ya maisha yao na kuyageuza. Wananyenyekea na kutii mafundisho, wakigeuka kufanana na Kristo na kuzaa **matunda** kwa Mungu.

### J. Kazi ya wale wanaosikia (8:16-18)

**8:16** Haionekani wazi mara moja nini inafunga mashairi haya na yale ambayo yaliwatangulia. Yesu alikaa kuonyesha kwamba ni neno kubwa nini wanafunzi watafanya na mafundisho yake. Anajisawanisha na mtu anayewasha taa. Haikufaa kuficha taa hii chini ya **chombo** au **kitanda**, lakini kuiweka juu ya **kinara** ili watu wote waweze **kuona nuru** yenyewe. Alikuwa akifundisha maneno makubwa juu ya ufalme, na kwa njia ya kufanya hivi alikuwa akiwasha taa. Basi wafanye nini nayo?

Kwanza, haifai waifunike na **kitunga** (chombo) (Matayo 5:15, Marko 4:21, na Luka 11:33). Watu wanatumika na kitunga ndani ya kazi ya biashara. Hivi kuficha taa chini ya kitunga ni kama kuruhusu haraka na masumbuko ya

biashara kupunguza ushuhuda wa Mkristo kwa Bwana. Ingekuwa vizuri kupita kuweka taa **juu ya** kitunga, maana kuwa na ushuhuda wazi kwa Bwana hata kwa soko, na kutangaza Habari Njema ndani ya kazi yetu.

Neno la pili ndilo hili: Haifai mwanafunzi kuficha taa **chini ya kitanda.** Kitanda kinasema juu ya pumziko, raha, uvivu na kujifurahisha mwenyewe. Maneno haya yote yanaweza kuzuiza nuru isingae! Inapasa mwanafunzi kuweka taa juu ya kinara, maana yake inampasa kutangaza kweli ya Mungu kwa njia ya kuishi maisha mema mbele ya watu.

**8:17** Ni kama shairi hili linaonyesha ya kwamba tukifunga njia kwa neno la Mungu kutangazwa kwa sababu ya kazi nyingine, au uvivu, neno hili **litaonyeshwa wazi.** Kuficha kweli ya Mungu **kama siri kutafunuliwa.**

**8:18** Hivi tukae na ange na kuangalia kabisa **namna tunavyosikia.** Tukiwa waaminifu na kushiriki kweli ya Mungu na watu wengine, Mungu atatuongezea kweli nyingine. Lakini kama tukikosa kuwa na bidii ya kutangaza Habari Njema, Mungu atatuondolea kweli ambayo tunafikiri tunayo. Tunapoteza neno ambalo hatutumiki nalo. G.H. Lang anasema:

> Wanafunzi walisikiliza na nia tayari kufahamu na kuamini na kutii; wale wengine walikuwa walegevu au wenye kutaka kujua kitu kigeni tu, au walisikiliza na roho ya uadui. Watu wa kwanza watafunuliwa kweli nyingine; wale wengine wataondolewa hata kweli walizosikia. [12]

## K. Mama ya Yesu, na ndugu zake (8:19-21)

Halafu Yesu aliambiwa ya kwamba **mama na ndugu** zake walikuwa wakingoja kumwona, lakini hawakuweza kufika karibu naye **kwa sababu ya makutano.** Bwana Yesu alijibu kusema msingi wa undugu wa kweli naye ni kutii **neno la Mungu**. Wale wanaopokewa ndani ya jamaa yake ndio wote wanaotetemeka kwa Neno lake, ambao wanalipokea na unyenyekevu na kulitii kabisa. Makutano ya watu wa dunia hawawezi kamwe kuzuiza jamaa yake *ya roho* kusemezana naye.

## L. Mwana wa watu anatuliza tufani (8:22-25)

**8:22** Ndani ya baki la sura hii tunaona ya kwamba Yesu ni **Bwana** juu ya tufani, bahari, pepo wachafu, gonjwa, na hata mauti. Zote zinamtii; watu tu wanakataa!

Zoruba zinaweza kuanza gafula kwa Bahari ya Galilaya, na ni hatari kwa wasafiri. Lakini labda zoruba hii ilianzwa na Shetani kujaribu kuharibu Mwokozi wa dunia!

**8:23** Yesu alikuwa **akilala** usingizi wakati zoruba ilipoanza; kulala kwake kunahakikisha utu wake. Lakini *zoruba* ililala (ilikoma) wakati Yesu alipoikemea, ndilo neno lililoonyesha uungu wake.

**8:24** Wanafunzi **waliamsha** Mwokozi, wakiogopa watazama baharini. Bwana na roho ya kutulia kabisa ali**kemea upepo** na mawimbi, yakakoma, ilikuwa **kimya**. Neno alilofanya kwa bahari ya Galilaya anaweza kufanya kwa watumishi wake wa sasa vilevile kwa wakati wa masumbuko na hatari.

**8:25** Akauliza wanafunzi, **"Imani yenu ni wapi?"** Haikufaa wasumbuke. Hawakuhitaji kumwamusha. Hakuna hatari hata kidogo wakati tulipo chomboni pamoja na Kristo.

Ilishinda wanafunzi kufahamu uwezo mkubwa wa Bwana wao. **Walishangaa** kuona ya kwamba zoruba na mawimbi yalimtii. Sisi tunafanana nao. Mara nyingi tunakata tamaa ndani ya masumbuko ya maisha yetu. Halafu wakati Bwana anapokuja kutusaidia tuna-

shangaa kuona uwezo wake. Na tunafazaika kwa sababu gani hatukumwamini kupita.

**M. Mwenye wazimu wa Gerase anaponyeshwa (8:26-39)**

**8:26,27** Wakati Yesu na wanafunzi wake walipofikia pwani walikuwa katika inchi ya **Wagerase**. **Mtu mmoja** mwenye **pepo wachafu** alikutana nao pale. Matayo aliandika juu ya watu wawili wenye pepo wachafu. Labda neno namna hii lilitokea mara mbili, au labda aliongeza habari nyingine wakati alipoandika. Ndani ya habari tunazosoma hapa pepo wachafu walifanyiza mtu huyu kuondosha **nguo** zake, kujitenga na watu, na kukaa katika **makaburi.**

**8:28, 29 Wakati alipoona Yesu** alimsihi asimtese. Alikuwa pepo mchafu aliyesema kwa njia ya mtu mwenye kutaabishwa.

Kukaliwa na pepo wachafu ni neno linaloweza kutokea kweli. Pepo hawa walikuwa viumbe vya roho waliokaa ndani ya mtu huyu wakitawala mafikiri yake, masemo yake na matendo yake. Pepo wachafu hawa walimfanyiza kuwa mkali sana hata **alivunja minyororo** ambayo watu walitumika nayo kumfunga na **alikimbia jangwani.** Hatushangai juu ya neno hili wakati tunapokumbuka kwamba ndani ya mtu huyu mmoja kulikuwa na pepo za kutosha kuua nguruwe elfu mbili (ona Marko 5:13).

**8:30,31** Jina la mtu huyu lilikuwa **Jeshi** kwa sababu jeshi zima la **pepo** walikaa ndani yake. Pepo hawa walitambua kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu aliye juu. Walijua kwamba hawataweza kuepuka uharibifu, lakini walimsihi **asiwaagize kuondoka na** kwenda **katika kilindi** mara moja.

**8:32, 33** Waliomba ruhusa, nyuma ya kuondokea mtu huyu, kuingia **kundi la nguruwe** waliokuwa karibu juu ya **mlima**. Walipewa ruhusa, na halafu nguruwe **walitelemuka chini ya genge hata katika bahari, wakazama ndani ya maji.** Wakati wa sasa watu wengine wanasema haikuwa vizuri kwa Bwana kuharibu mali ya mtu mwingine. Lakini kama wenye kulinda nguruwe walikuwa Wayuda walikuwa wakifanya kazi chafu iliyokatazwa na sheria. Na vilevile, si neno kama walikuwa Wayuda au watu wa Mataifa, ingaliwapasa kufahamu ya kwamba damani ya mtu mmoja inapita mbali ile ya nguruwe elfu mbili.

**8:34-39** Habari za matokeo haya zilienea mbio katika inchi kando kando. Wakati makutano walipoona mtu yule mwenye pepo mbele akiketi akivaa mavazi na mwenye akili njema, walishitushwa sana sana hata **Wagerase waliomba** Yesu kuwaondokea. Walihesabu nguruwe zao kuwa na faida kupita Mwokozi wao! Darby alisema:

> Watu wa dunia wanasihi Yesu kuondoka. Ukaribu na uwezo wa Mungu ulichokoza utulivu wao kupita jeshi la pepo wachafu. Basi anakwenda zake. Mtu yule aliyeponyeshwa alitaka kuwa pamoja naye lakini Bwana alisema naye kurudi kwa watu wake aweze kushuhudia neema na uwezo wa Mungu ndani ya maisha yake. [13]

Saa Yesu alipofikia Dekapoli tena wakati wa nyuma watu walimpokea vizuri (Marko 7:31-37). Labda lilikuwa tunda la ushuhuda mwaminifu wa mtu huyu aliyeponyeshwa toka pepo wachafu?

**N. Kuponyesha wasioweza kuponyeshwa na kufufua wafu (8:40-56)**

**8:40-42** Yesu alivuka Bahari ya Galilaya tena na kufikia pwani yake ya mangaribi. Pale makutano mengine **walimngojea. Yairo, mkubwa wa sunagogi**, alitaka sana kumwona kwa sababu alikuwa na binti mwenye miaka **kumi na miwili** aliyekuwa karibu kufa. Alisihi

Yesu kufikia nyumba yake mbio. Lakini makutano walimsonga na ilimshinda kwenda mbio.

**8:43** Katikati ya makutano haya kulikuwa na mwanamke mwenye woga na kukata tamaa aliyeteswa na ugonjwa wa **kutoa damu tangu miaka kumi na miwili**. Luka, mganga, aliongeza kusema ya kwamba alikuwa amelipa mali yake yote kwa waganga bila kupata kusaidiwa. (Na Marko alisema kwamba ugonjwa wake uliongezeka!)

**8:44,45** Mwanamke huyu alifahamu ya kwamba Yesu alikuwa na uwezo kumponyesha, hivi alipita polepole katika makutano kufika karibu naye, akainama na ku**gusa upindo wa nguo yake** (ona Hes. 15:38,39; Tor. 22:12). **Mara moja aliacha kutoa damu** na aliponyeshwa kabisa. Alijaribu kwenda zake tena polepole, lakini alizuizwa na ulizo la Yesu: **"Nani ambaye alinigusa?" Petro** na wanafunzi wengine walifikiri hili ni ulizo la namna gani wakati watu wengi walipokuwa wakimsonga!

**8:46 Lakini Yesu** alitambua kwamba mwenye imani alikuwa amemgusa, kwa sababu alifahamu **uwezo** ulikuwa ume**toka kwake**. Si kusema ya kwamba uwezo wake ulipunguka lakini uwezo toka kwake ulihitajiwa kuponyesha mwanamke.

**8:47,48 Mwanamke … akakuja akitetemeka, akaanguka mbele yake,** akaeleza kwa sababu gani **alimgusa** na namna alivyoponyeshwa mara moja. Alikuwa amekiri wazi mbele ya watu maneno yaliyotokea na Bwana alisifu **imani** yake wazi vilevile na kumruhusu kwenda zake na **salama.** Yesu anajua kila mara mtu anapomgusa na imani na mtu mwenyewe anabarikiwa. Hakuna mtu anayekiri mbele ya watu kwamba Yesu ni Mwokozi wake bila kupatishwa nguvu katika imani yake.

**8:49** Hatufikiri kwamba kuponyeshwa kwa mwanamke kulihitaji saa nyingi, lakini hata hivi mjumbe alifika na habari ya kwamba **binti** ya Yairo alikuwa **amekufa** na ya kuwa Mwalimu hakuhitaji kufika kule. Walikuwa na imani ya kutosha ya kwamba Yesu aliweza kuponyesha wagonjwa, lakini si kufufua wafu.

**8:50** Lakini **Yesu** hakuwaacha mbio hivi. Alijibu na masemo ya faraja, na aliahidi baba **"Usiogope, amini tu, naye atapona."**

**8:51-53** Wakati alipofikia nyumba ya Yairo alikwendea chumba mara moja, akipeleka pamoja naye **Petro, Yakobo na Yoane** tu pamoja na wazazi wa mtoto. Watu wote walikuwa wakiombolea bila tumaini, lakini Yesu aliwaagiza kuacha kufanya hivi kwa sababu msichana **hakufa, lakini amelala usingizi**. Watu walimzarau wakati aliposema hivi kwa sababu walikuwa wameamini kabisa ya kwamba **alikuwa amekufa.**

Basi alikufa kweli, au alilala na usingizi mzito tu, hali ya kuzimia roho? Zaidi ya walimu wanasema amekufa. Wanatukumbusha ya kwamba Yesu alisema Lazaro alikuwa amelala, maana yake kwamba alikuwa mfu. Sir Robert Anderson anasema kwamba msichana hakufa.[14] Alieleza mawazo yake hivi:

1. Yesu alisema msichana atapona. Neno ambalo alitumika nalo ndilo neno ndani ya shairi 48 la sura hii lililo juu ya kuponyesha, si juu ya kufufua toka wafu.
2. Yesu alitumika na neno lingine kwa kulala saa ya kusema juu ya Lazaro.
3. Watu walifikiri msichana alikuwa mfu, lakini Yesu hakutaka watu kufikiri kwamba alimfufua toka wafu wakati alipojua alikuwa amelala tu.

Anderson anasema kwamba inatupasa kuchagua tu kama tutaamini nani. Yesu

alisema alilala usingizi. Watu walifikiri alikuwa amekufa.

**8:54-56** Si neno. Yesu alisema naye, **"Kijana, amka. Akasimama mara moja."** Nyuma ya kumrudisha kwa wazazi wake Yesu aliwakataza wasitangaze habari za ajabu hii katikati ya watu. Hakutafuta sifa na heshima toka watu.

Tumefika sasa kwa mwisho wa mwaka wa pili wa utumishi wa Yesu katikati ya watu. Sura 9 inaanza mwaka wa tatu na habari za kutuma wanafunzi kumi na wawili.

### O. Mwana wa watu anatuma wanafunzi wake kuhubiri (9:1-11)

**9:1,2** Habari hizi zinafanana na zile tunazosoma ndani ya Matayo 10:1-15, lakini kuna tofauti vilevile. Kwa mfano, katika Matayo wanafunzi waliagizwa kufikia Wayuda tu, na waliagizwa kufufua wafu pamoja na **kuponyesha wagonjwa.** Hatujui sababu kwa tofauti hii. Bwana Yesu alikuwa na uwezo na amri kufanya maajabu na alileta **uwezo na amr**i kwa wengine vilevile. **Uwezo** ndio nguvu kufanya neno fulani. **Amri** ndiyo ruhusa kutumika na uwezo ule. Kwa wakati ule Biblia nzima ilikuwa haijaandikwa bado na mahubiri ya wanafunzi yalithibitishwa na alama na maajabu (Ebr. 2:3,4). Mungu ana uwezo kuponyesha watu kwa njia ya ajabu lakini hatujui kwamba kwa wakati wa sasa inapasa maajabu ya kuponyesha kufanyikana pamoja na mahubiri.

**9:3-5** Sasa wanafunzi walikuwa na njia kutenda katika maisha yao maneno ambayo Bwana alikuwa amewafundisha. Iliwapasa kumtegemea yeye tu kuwapa vitu walivyohitaji – hawakuwa na **mfuko, vyakula,** au **mali** au **kanzu mbili**. Waliagizwa **kukaa** katika nyumba ya kwanza pahali watu walipowakaribisha – bila kuhamahama kutafuta kao zuri kupita. Walikatazwa kukaa pahali fulani kwa muda mrefu kupita kipimo wala kushurutisha wale waliokataa mahubiri yao, lakini **kukunguta mavumbi toka miguu yao kuwa ushuhuda juu yao.**

**9:6** Tunafikiri wanafunzi walihubiri **Habari Njema** na kuponyesha wagonjwa katika **miji** ya Galilaya. Mahubiri yao yalikuwa juu ya ufalme – ya kwamba Mfalme alikuwa katikati yao na alikuwa tayari kutawala watu wenye roho ya toba.

**9:7 Herode** Antipa alikuwa **mtawala** katika Galilaya na Perea kwa wakati ule. Alitawala juu ya sehemu moja ya ine ya inchi ya ufalme wa baba yake, ndiye Herode Mkubwa. Herode alisikia habari za Mmoja akifanya maajabu ya uwezo katika inchi yake. Mara moja damiri ilianza kumchokza wakati alipokumbuka **Yoane** Mbatizaji. Herode alikuwa amenyamazisha ushuhuda wa uhodari wa Yoane kwa njia ya kumkatia kichwa lakini alikaa kukumbuka uwezo wa maisha yake. Alikuwa nani basi aliyekaa kukumbusha Herode habari za Yoane? Kulikuwa na wengine waliosema **Yoane alikuwa amefufuliwa toka wafu.**

**9:8,9** Wengine walifikiri alikuwa **Elia** au **mmoja wa manabii** wengine wa Agano la Kale. **Herode** alijaribu kunyamazisha mashaka ya roho yake kwa njia ya kukumbusha watu wengine kwamba alikuwa **amekatia** Yoane Mbatizaji **kichwa**, lakini alikaa na woga tu. **Huyu** alikuwa nani basi? Herode **alijaribu kumwona**, lakini hakuweza kufika saa ndogo tu mbele ya kusulibishwa kwa Mwokozi.

Uwezo wa maisha yanayojazwa Roho Mtakatifu! Bwana Yesu, mseremala asiyejulikana wa Nazareti alitetemesha Herode bila kukutana naye kamwe! Mtu anayejazwa na Roho Mtakatifu ana uwezo mkubwa kushawishi maisha ya watu wengine!

**9:10 Wakati mitume waliporudi**

toka safari yao ya kuhubiri walipasha Bwana maneno yote yaliyotokea. Labda hii ingekuwa desturi nzuri kwa watumishi wote wa Mungu. Mara nyingi habari tunazotolea watu juu ya baraka Bwana alizoleta kwa njia ya utumishi wetu hazitukuzi Bwana lakini sisi wenyewe na zinaamsha wivu na matengo katikati ya Wakristo. Bwana wetu alipeleka mitume **kwa jangwa** karibu na Betesaida (maana ya jina hili ni *nyumba ya kuvua samaki*). Ni kama kulikuwa na Betesaida miwili kwa wakati ule, mmoja kwa upande wa mangaribi wa Bahari ya Galilaya, na wa pili kwa upande wa mashariki. Pahali pake kabisa hapajulikani.

**9:11** Waliweza kukaa peke yao na kustarehe kwa muda mfupi tu. Watu wengi walifika karibu nao mbio. Bwana Yesu alikaa tayari kupokea na kubariki watu wakati wo wote – na hapa tunasoma ya kwamba **akawakaribisha,** akisema nao **habari za ufalme wa Mungu,** na **kuponyesha wote waliohitaji kupona.**

### P. Watu elfu tano wanakulishwa (9:12-17)

**9:12** Wakati jua lilipoanza kushuka wanafunzi wake kumi na wawili walianza kusumbuka wakati walipoona kundi lile kubwa wakihitaji vyakula! Hivi waliomba Bwana ku**agana na makutano** na kuwaruhusu kwenda zao. Nasi tunafanana nao! Juu ya mahitaji yetu wenyewe tunasema, kama Petro, "uniagize kufika kwako …" Lakini juu ya mahitaji ya watu wengine ni nyepesi kusema, **"Uwaage."**

**9:13** Yesu hakukubali kutuma makutano kwa vijiji kandokando kujipatia vyakula. Kwa nini wanafunzi wafanye safari kusaidia watu pahali pengine, bila kusaidia wale waliokuwa karibu? Wao wenyewe walishe makutano! Walijibu kusema walikuwa na **mikate mitano na samaki wawili** tu, wakisahau ya kwamba utajiri wote wa Bwana Yesu ulikuwa tayari kwa hitaji hili kubwa.

**9:14-17** Bwana alisema nao kuketisha makutano yale ya **wanaume elfu tano,** pamoja na wanawake na watoto. Nyuma ya kuleta asante, **alivunja** mkate na kukaa kuwapa **wanafunzi,** nao waliuleta kwa watu. Kulikuwa na vyakula vya kutosha watu wote waliokuwa pale. Ndiyo, vingine vilibaki, kupita vile ambavyo walikuwa navyo kwa mwanzo, vya kutosha kujaza **vitunga kumi na viwili,** kimoja kwa kila mwanafunzi!

Habari hizi zina maana kubwa kwa wanafunzi waliopewa kazi ya kuhubiri Habari Njema kwa dunia nzima. Wale watu **elfu tano** ni mfano wa elfu elfu za watu waliokuwa wapotevu kwa sababu ya njaa kwa Neno la Mungu. Wanafunzi ni mfano wa Wakristo wasioweza kusaidia, walio na mali nusu, na wasio tayari kushiriki mali hii na watu wengine. Pamoja na agizo la Bwana, "Ninyi muwape chakula," soma Matayo 28:20. Mafundisho makubwa kwa sisi ndiyo haya: kama tukitolea Bwana mali na vitu tulivyo navyo, anaweza kuvizidisha kulisha makutano makubwa yenye njaa ya roho. Vitu vingine vya mapambo nyumbani mwetu visivyo vitu vya sharti, au mavazi ya mapambo zaidi au vitu vya damani kama vito au zahabu – tunaweza kuviuza na kununua traités kugawa kwa watu zinazoweza kuwasaidia kuamini Bwana Yesu na kuabudu Mwana-Kondoo wa Mungu kwa milele.

Ingewezekana kwa Habari Njema kuhubiriwa kwa watu wote duniani kama Wakristo wa wakati wa sasa wangejitoa wenyewe, pamoja na vyote walivyo navyo, kwa Kristo. Haya ndiyo mafundisho makubwa ya ajabu hili la kulishwa kwa watu elfu tano.

### Q. Petro anakiri kwamba Yesu ni Kristo (9:18-22)

**9:18** Mara moja nyuma ya ajabu la kulishwa kwa makutano makubwa, Petro alikiri kwamba Yesu ni Kristo katika Kaisaria Filipi. Labda ajabu hili

la kuzidisha mikate na samaki lilifunua macho ya wanafunzi kuona utukufu wa Bwana Yesu kama Mpakaliwa wa Mungu? Kufika saa ile alikuwa amewafundisha polepole juu yake mwenyewe na kazi aliyoweza kufanya ndani yao na kwa njia yao. Kuanza sasa alikwenda mbele na roho moja kwa msalaba. Yesu aliomba **peke yake.** Hatusomi hata mara moja ya kwamba aliomba pamoja na wanafunzi. Aliwaombea. Aliomba mbele yao, aliwafundisha kuomba, lakini maombi yake mwenyewe yalikuwa mbali na maombi yao. Nyuma ya kuomba hivi peke yake aliuliza wanafunzi wake kama **watu** walisema **yeye** ni nani.

**9:19,20** Walikuwa na majibu mbalimbali. Wengine walisema **Yoane Mbatizaji,** wengine **Elia**; wengine walisema alikuwa mmoja wa **manabii** wa Agano la Kale aliyefufuliwa. Lakini wakati Yesu alipouliza wanafunzi wake kama wao walifikiri nini, **Petro** alikiri bila shaka ya kwamba yeye ni **Kristo** (ndiye Masiya) **wa Mungu**.

James Stewart alisema juu ya tukio hili kwa Kaisaria Filipi:

> Ulizo la Yesu halikuwa nguvu kujibu. Watu pahali pote walikuwa wakisema maneno mbalimbali juu yake. Na watu hawakusema tu juu ya Yesu; walisema maneno *makubwa* juu yake. Wengine walisema alikuwa Yoane Mbatizaji aliyefufuliwa toka wafu. Wengine walisema Yesu aliwakumbusha Elia. Wengine walitaja Yeremia au nabii mwingine. Hata kama watu walijibu maneno mbalimbali, walipatana ndani ya neno moja: Yesu alikuwa mkubwa, mwenye kujulikana sana kwa wakati ule …
>
> Hata leo vilevile watu wanasema maneno mbalimbali juu ya Yesu, lakini wanapatana ya kwamba yeye ni mmoja wa wakubwa zaidi duniani.
>
> Lakini hili si neno Kristo alilosema juu yake mwenyewe. Alisema yeye ni namna nyingine kabisa na watu wa dunia, namna ya peke yake, asiye na kifani (kwa mfano ona Mt. 10:37; 11:27; 24:35; Yn. 10:30; 14:6) [15]

**9:21,22** Wakati Petro alipokiri neno hili kubwa sana, Bwana **aliwakataza kuwaambia** watu wengine; hakutaka neno lo lote kumzuiza katika njia kwenda msalaba. Halafu Mwokozi aliwafunulia habari za maneno yaliyokuwa karibu kumpata. **Itampasa kuteswa, kukataliwa** na viongozi vya dini vya Israeli, **kuuawa** na **kufufuliwa tena siku ya tatu**. Hili lilikuwa tangazo la kushangaza sana. Tusisahau ya kwamba maneno haya yalisemwa na Mtu wa pekee asiyekuwa na zambi aliyeishi hapa duniani. Yalisemwa na Masiya wa kweli wa Israeli. Yalikuwa masemo ya Mungu akionekana katika mwili. Yanatujulisha ya kwamba wenye maisha ya utimilizo, maisha kamilifu, maisha ya kutii mapenzi ya Mungu, watajuana na mateso, kukataliwa, mauti kwa njia moja au nyingine, na ufufuko kwa uzima usio na mwisho. Wanaishi maisha kusaidia watu wengine.

Tangazo hili la Mwokozi halikupatana hata kidogo na mawazo ya watu juu ya Masiya na kazi yake. Watu walitazamia kiongozi mwenye heshima atakayeharibu adui zao. Bila shaka hata wanafunzi walishangaa. Lakini kama Yesu ni kweli Kristo wa Mungu, kama walivyokiri hawakuwa na sababu ya kulegea au kuogopa. Akiwa Mpakaliwa wa Mungu, kusudi lake litatimizwa. Si neno kama nini ikiwapata au kumpata yeye, walikuwa kwa upande wa washindaji.

### R. Mwito kuchukua msalaba (9:23-27)

**9:23** Nyuma ya kujulisha wanafunzi nini itampata yeye, Bwana aliita wanafunzi **kumfuata**. Itawapasa kujikana wenyewe na kuchukua **msalaba** wao. Maana ya **kujikana** mwenyewe ni kuwa tayari kuacha kuwa na ruhusa ya kufanya

shauri au kuchagua maneno sisi tunayotaka, na ni kukubali ya kwamba yeye ni Bwana wa kila sehemu ya maisha yetu. **Kuchukua msalaba** ni kuchagua kuishi namna yeye alivyoishi, na kushiriki ndani ya maneno ambayo yalimpata yeye:

Kukataliwa na wapenzi wetu.

Kuzarauliwa na watu wa dunia. Kuachana na jamaa na nyumba na inchi na hali njema ya maisha ya sasa.

Ni kutegemea Mungu ndani ya maneno yote.

Ni kutii maongozi ya Roho Mtakatifu.

Ni kutangaza habari watu wasizopenda kusikia.

Ni maisha ya upekee.

Ni kushindana na vita ya viongozi vya dini nyingine.

Ni kupata mateso kwa ajili ya haki.

Masingizio na haya.

Ni kujitoa kuishi kwa ajili ya wengine.

Kujihesabu mfu kwa mimi mwenyewe na kwa dunia.

Lakini ni kushikana *vilevile* na maisha yaliyo maisha ya faida ya kweli! Ni kufahamu kusudi la maisha yetu. Na ni kupokea zawabu ya milele. Hatufurahi kuwaza juu ya maisha ya kubeba msalaba. Ni nguvu kwa sisi kuamini ya kwamba neno hili ni kweli mapenzi ya Mungu kwa sisi. Lakini maneno ya Kristo: **"Kama mtu akipenda kuja nyuma yangu,"** ni kwa kila mtu mmoja mmoja.

**9:24** Sisi watu tungependa **kuokoa** maisha yetu kwa njia ya kuishi kwa sisi wenyewe tukifanya maneno yanayopendeza miili yetu, tukikumbuka wakati wa sasa tu, na kutumika na zawadi ambazo Mungu alitupa sisi kwa kazi fulani kujivimbishia mali ya dunia kusudi tuweze kuishi bila masumbuko kwa miaka ya kuja. Lakini hii ndiyo njia kwa sisi **kupoteza** uzima wetu, maana kupoteza kusudi la Mungu kwa **maisha** yetu na furaha kubwa ya roho ambayo tungaliweza kupata kwa njia hii. Lakini tunaweza kupoteza **maisha** yetu kwa ajili ya Mwokozi. Watu wanafikiri tuko wazimu kama tukifanya hivi, kama tusipotumika na zawadi ambazo Mungu alitupa sisi kwa faida yetu wenyewe, kama tukitafuta kwanza ufalme na haki ya Mungu, kama tukijitoa mzima kwa yeye. Lakini maisha namna hii, ya kujitoa kabisa ni maisha ya furaha zaidi, maisha bila masumbuko, kwani tunayaweka yote juu ya Mungu.

**9:25** Mwokozi alifahamu ya kwamba mapendo kwa mali na vitu vya dunia yana uwezo kabisa kutuzuiza tusijitoe mzima kwake. Hivi alisema nao maneno kama haya: "Kama ungaliweza kujivimbishia mali yote ya **dunia nzima,** na feza na zahabu na nyumba na vitu, lakini kama kwa njia ya kufanya hivi ungepoteza kusudi la kweli kwa maisha yako, vitu vile vyote vitakuwa na faida gani kwako? Utakuwa navyo kwa muda fupi tu, kisha utalazimishwa kuviacha kwa milele. Ungekuwa upumbavu kabisa kuuza maisha yako mafupi kwa vitu vya dunia vilivyo mavumbi tu."

**9:26** Neno lingine linalozuiza watu wasijitoe mzima kwa Bwana ni woga wa kupata haya. Ni upumbavu kabisa kwa kiumbe kuwa na haya juu ya Mwumba wake, kwa mwenye zambi kuwa na **haya** juu ya Mwokozi wake. Bwana alijua ya kwamba sisi sote tunajaribiwa kwa njia hii na alitoa maonyo ya nguvu juu yake. Kama tukiepuka haya kwa njia ya kuishi maisha ya kikristo kwa jina tu, tukifungana na desturi za watu wa dunia, **Mwana wa watu atakuwa na haya** juu yetu **wakati atakapokuja katika utukufu wake, na wa Baba yake**, na wa **malaika watakatifu.** Alitaja utukufu namna tatu wakati atakapokuja mara ya pili kama kuonyesha ya kwamba haya au laumu yote tunayopata kwa

ajili yake sasa itaonekana kuwa ndogo sana wakati atakapokuja katika utukufu. Ni ndogo tu wakati zinaposawanishwa na laumu na haya ya wale ambao wanamkana sasa.

**9:27** Nyuma ya kusema juu ya utukufu wake, aliwaambia ya kwamba **wengine** wa wanafunzi waliokuwa **wakisimama** pale **wataona ufalme wa Mungu** mbele ya kufa kwao**.** Maneno yake yalitimizwa ndani ya mashairi 28-36 wakati Petro, Yakobo na Yoane walipokuwa mlimani. Wakati ule waliona mfano wa maneno yatakayotokea wakati Bwana Yesu atakaposimamisha ufalme wake duniani. Petro alisema juu yake ndani ya barua yake ya pili:

> Hatukufuata hadizi zilizotengenezwa kwa hila, wakati tulipowajulisha ninyi uwezo na kuja kwa Bwana wetu Yesu Kristo, lakini sisi wenyewe tuliona ukubwa wake. Maana alipata kwa Mungu Baba heshima na utukufu, wakati sauti ilipokuja toka utukufu mkubwa: "Huyu ni Mwana wangu mpendwa, ambaye ninapendezwa naye." Basi tulisikia sauti hii ikitoka mbinguni, wakati tulipokuwa pamoja naye katika mlima mtakatifu (1:16-18).

Ona maendeleo ndani ya mafundisho ya Bwana hapa. Alikuwa amewapasha sasa tu ya kwamba atakataliwa yeye mwenyewe, atateswa na kuawa nyuma kidogo. Alikuwa ameita wanafunzi wake kumfuata kwa njia ya kuishi maisha ya kujikana mwenyewe, na kupata mateso, na kujitoa kama zabihu kwa Mungu. Lakini ni kama sasa anasema, "Lakini mukumbuke! Kama mukiteswa pamoja nami, mutatawala pamoja nami vilevile. Utukufu unafuata msalaba. Zawabu itakuwa kubwa zaidi kupita bei ya kunifuata."

### S. Mwana wa watu anageuzwa sura (9:28-36)

**9:28,29** Nyuma ya **karibu siku nane** Yesu alichukua **Petro, Yoane, na Yakobo, akapanda juu ya kilima kuomba.** Hatujui pahali pa **kilima** hiki, labda ulikuwa mlima wa Hermoni uliofunikwa na theluji. Wakati Bwana alipokuwa akiomba alianza **kuonekana** namna nyingine. Hata leo maombi yanageuza kuonekana kwa mtu. **Uso** wa Bwana ulingaa na **mavazi yake** yalikuwa meupe kabisa. Kama tulivyosema mbele, hili lilikuwa mfano wa utukufu wake kwa wakati wa ufalme wake kwa wakati wa kuja. Wakati alipokuwa hapa duniani utukufu huu ulifichwa ndani ya mwili wa mtu. Alikuwa hapa katika aibu, kama mtumwa. Lakini wakati wa utawala wake kwa miaka elfu moja utukufu wake utafunuliwa wazi. Watu wote watamwona katika ubora na enzi.

**9:30,31 Musa na Elia** walisemezana naye juu ya habari za **kufa kwake atakakotimiza katika Yerusalema.** Ona ya kwamba walisema juu yake kama tendo linalokwisha kumalizwa, si kama mwisho wa uzima, lakini kama kuondokea pahali pamoja kwenda pahali pengine.

**9:32,33** Wanafunzi walikuwa na macho mazito na usingizi wakati maneno haya yalipokuwa yakitokea. Askofu Ryle alisema:

> Ona ya kwamba wanafunzi hawa waliolala usingizi hapa kwa wakati Bwana alipoonekana katika utukufu ndio wale waliolala wakati wa taabu yake kubwa katika shamba la Getesemane. Kweli ni sharti kwa miili yetu (nyama na damu) kugeuzwa mbele ya kuweza kuingia mbinguni. Inashinda miili yetu zaifu kuangalia pamoja na Kristo kwa wakati wake wa taabu, na kukaa na macho pamoja naye katika utukufu wake. Ni lazima kwa miili yetu kugeuzwa kabisa mbele ya kuweza kufurahi mbinguni. [16]

**Wakati walipokwisha kuamka, waliona** kungaa kwa utukufu wa Kristo.

Kama ukumbusho wa tokeo hili kubwa Petro alitaka kusimamisha **hema tatu, moja** kuheshimu Yesu, **moja** kwa Musa, na moja kwa **Elia**. Lakini mawazo haya yalitoka kwa bidii yake bila ufahamu.

**9:34-36 Sauti** ya Mungu ilitoka katika **wingu** ambalo liliwafunika kuwajulisha kwamba Yesu alikuwa **Mwana** wake **mpendwa**, na kusema nao **kumsikia** na **kumtii yeye**. Mara moja wakati **sauti** isiposikiwa tena, Musa na Elia hawakuonekana tena, na Yesu alisimama pale **peke yake**. Itakuwa hivi katika ufalme. Yeye atakuwa mkubwa na mwenye sifa zaidi ndani ya maneno yote. Hatashiriki utukufu wake na mwingine.

Wanafunzi waliondoka pale na hofu kubwa hata hawakusemezana na watu wengine juu ya maneno waliyoona na kusikia.

### T. Mtoto mwenye pepo mchafu anaponyeshwa (9:37-43a)

**9:37-39 Kesho yake** Yesu na wanafunzi wake walishuka tena toka kilima cha utukufu kukutana na makutano ya watu wenye hitaji. Pamoja na nyakati za baraka sana za roho Mungu anatupa sisi kazi ya kila siku kufanya kusaidia watu wengine. Mtu mmoja **wa makutano** ambaye alikutana naye alikuwa baba mwenye huzuni kubwa aliyesihi Yesu kusaidia mwana wake aliyekuwa na pepo mchafu. Alikuwa **mtoto wake wa pekee** na baba yake alimpenda sana. Ilikuwa huzuni kubwa kwake kuona mwana wake akiteswa hivi, na kupasuliwa na kupondwa vibaya na kutokwa na pofu. Maneno haya yalitokea tena na tena.

**9:40** Baba alikuwa amefikia **wanafunzi** mbele kupata kusaidia, lakini wanafunzi hawakuweza. Kwa nini walishindwa? Labda walikuwa wamefikiri juu ya utumishi wao kama kazi tu? Hawakukumbuka ya kwamba walihitaji kutegemea Bwana wao kuwawezesha?

**9:41** Bwana **Yesu** alihuzunishwa sana wakati alipoona maneno haya. Bila kutaja mtu ye yote na jina, alisema, "Ee kizazi pasipo imani …" Labda alikuwa akisema maneno haya na wanafunzi, au makutano, au baba ya mtoto, au wao wote pamoja. Wao wote walikuwa zaifu na hawakuweza kusaidia mahitaji ya watu wengine, hata kama ndani ya Bwana mwenyewe waliweza kupata uwezo wote waliohitaji kwa kufanya hivi. Itampasa **kukaa katikati yao kwa muda gani** na kuvumilia uzaifu wao? Kisha alisema na baba, **"Ulete mwana wako hapa."**

**9:42,43a** Wakati mtoto **alipokuwa njiani** kufika karibu na Yesu, **pepo mchafu** alimtupa chini na kumpasua. Lakini Bwana hakuogopeshwa na uwezo huu wa pepo mchafu; ni kutokuamini kwa watu ambako kulimzuiza kupita uwezo wa pepo wachafu. Alihamakia **pepo mchafu, akaponyesha mtoto, akamrudisha kwa baba yake**. Watu **walishangaa**, wakatambua kwamba Mungu alikuwa amefanya ajabu na walikuwa wameona **enzi ya Mungu.**

### U. Mwana wa watu anatabiri mauti na ufufuko wake (9:43b-45)

**9:43b,44** Labda wanafunzi watafikiri Bwana wao atakaa kufanya maajabu kufika wakati taifa zima watakapomtangaza kuwa Mfalme. Kuondosha mafikiri namna hii ndani ya nia zao Bwana aliwakumbusha tena ya kwamba itakuwa **lazima kwa Mwana wa watu kutolewa kwa mikono ya watu**, maana yake kuuawa.

**9:45** Kwa sababu gani **hawakufahamu** unabii huu? Kwa sababu walirudi tena kwa mafikiri yao ya mbele ya kwamba Masiya atakuwa mtu mkubwa mhodari atakayependwa na watu wote. Walifikiri kufa kwake kungeharibu makusudi yao. Matumaini yao yalikuwa

nguvu sana hata iliwashinda kufikiri neno lingine. Hakuwa Mungu ambaye aliwafichia kweli hili, lakini wao wenyewe walikataa kuliamini. **Waliogopa** hata **kuuliza** Bwana kueleza maana ya masemo yake, kwa sababu hawakutaka ahakikishe neno ambalo waliogopa!

**V. Ukubwa wa kweli katika Ufalme (9:46-48)**

**9:46** Pamoja na kutazamia mwanzo wa ufalme wa utukufu, wanafunzi walitaraji kuwa na cheo ya heshima ndani ya ufalme. Hata kwa wakati ule walikuwa wakibishana nani katikati yao **atakayekuwa mkubwa zaidi.**

**9:47,48 Yesu** akijua neno hili lilikuwa likihangaisha mafikiri yao aliketisha **mtoto mdogo** karibu naye na alieleza ya kwamba mtu ye yote anayepokea **mtoto mdogo kwa jina lake** anampokea yeye. Labda hatufahamu mara moja namna gani tendo hili linatufundisha juu ya kujitafutia ukubwa, lakini ni kama linaonyesha kwamba ukubwa wa kweli ni kulinda watoto wadogo, watu wasioweza kujisaidia wenyewe, wale wanaoonekana bure hata watu wa dunia hawaweki roho juu yao. Hivi wakati Yesu aliposema **"yule aliye mdogo zaidi katikati yenu atakuwa mkubwa,"** alisema juu ya mtu yule ambaye anajinyenyekeza kukaa pamoja na waamini wanaoonekana bure na wanazarauliwa.

Katika Matayo 18:4 Bwana Yesu alisema ya kwamba yule aliye mkubwa zaidi katika ufalme wa mbinguni ndiye ambaye anajinyenyekeza kama mtoto mdogo. Hapa katika Luka, anafundisha zaidi juu ya kujinyenyekeza kushirikiana na watoto wa Mungu wenye heshima nusu zaidi. Neno kubwa ambalo Mwokozi alifundisha ndani ya vitabu hivi viwili ni juu ya kujinyenyekeza, kama alivyofanya yeye mwenyewe.

**W. Mafundisho ya Bwana kukataza kutoshiriki kwa waamini wa kweli na wale wa kanisa lingine (9:49,50)**

**9:49** Matukio katika mashairi haya ni mfano wa namna ya matendo ambayo Bwana alitaka wanafunzi kuepuka. Walikutana na mtu **aliyetoa pepo wachafu** kwa **jina** la Yesu. **Walimkataza** kufanya hivi kwa sababu **hakuwa** mmoja wa wafuata wenzao! Walikuwa wamekataa kupokea mwamini kwa jina la Bwana. Ingaliwapasa kufurahi kwa sababu pepo mchafu alikuwa ametoka mtu huyu. Haifai kamwe kuwa na wivu kama mtu au jamii ya watu wakitoa pepo wachafu kupita hesabu wao waliyotoa. Inapasa kila mfuata wa Yesu kukaa na ange asiwe na wivu kama wengine wakiwa na uwezo na heshima kupita ndani ya kazi yao kwa Bwana.

**9:50 Yesu akamwambia, "Musimkataze, kwa maana yeye asiye adui yenu ni upande wenu."** Mtu asipokuwa kwa *upande wa* Kristo, na kazi yake, yeye ni *adui* yake. Haiwezekani kusimama katikati. A.L. Williams alisema juu ya *utumishi* wetu kwa Kristo:

> Ni lazima kukumbuka ya kwamba wakati watu wa jamii nyingine wanapofanya kazi kwa jina la Kristo, sharti kazi hii iendeleshe kazi ya Bwana mbele … Jibu la Bwana Yesu linatufundisha neno kubwa: Hakuna kundi au jamii ya dunia, hata wakiwa watakatifu sana, wanaoweza kusema wao tu wana ruhusa toka Mungu kutumika na jina lake na uaminifu." [29]

## 7. MAZUIZO KWA UTUMISHI WA MWANA WA WATU YANAONGEZEKA (9:51 – 11:54)

**A. Wasamaria wanakataa Mwana wa watu (9:51-56)**

**9:51 Siku** za kupokewa kwa Yesu juu mbinguni zilikuwa zikikaribia. Yesu

alijua neno hili vizuri. Alijua vilevile ya kwamba msalaba utatangulia siku ile, hivi alikaza uso wake kwenda **Yerusalema** na maneno yote ambayo yalimngojea kule.

**9:52,53** Walipita kwa **kijiji** cha Wasamaria, lakini watu wale hawakufurahi kupokea Mwana wa Mungu kwani walijua alikuwa akikwenda **Yerusalema.** Wasamaria na Wayuda walichukiana sana. Kiburi chao cha taifa lao kiliwazuiza **wasipokee** Bwana wa Utukufu.

**9:54-56** **Yakobo na Yoane** walikasirika sana kwa sababu ya ukosefu huu wa adabu, hata walitaka kuita **moto toka mbinguni** kuharibu watu wale. Yesu **aliwakemea** mara moja. Hakufika **kuharibu uzima wa watu lakini kuwaokoa**. Huu ulikuwa mwaka wa kukubaliwa wa Bwana, si siku ya kisasi cha Mungu wetu. Ingalipasa kwao kuonyesha neema, si roho ya kisasi.

**B. Vizuizo vya wenye kutaka kufuata Bwana (9:57-62)**

**9:57** Ndani ya mashairi haya tunakutana na watu watatu waliotaka kufuata Bwana. Katika maisha yao tunaona zaidi maneno matatu yanayotaka kuzuiza watu wasifuate Bwana na roho yote. Mtu wa kwanza alifikiri alitaka **kufuata** Bwana kwelikweli pahali pote. Hakungoja kwa Bwana kumwita, lakini alimjulisha tu ya kwamba alikuwa tayari kumfuata. Alijitegemea mwenyewe, na hakufahamu bei ya kufuata Bwana. Hakujua maana ya maneno ambayo alisema.

**9:58** Labda mtu huyu hakufahamu jibu la **Yesu** mara moja. Ni kama alisema na mtu huyu, "Unafahamu maana ya kunifuata? Ni kuachana na mengi ya maneno mazuri unayofurahia sasa. Mimi sina nyumba. **Mbweha** na **ndege** wana pahali pao, lakini si mimi. Wewe ni tayari kunifuata hata kama ikikupasa kuachana na vitu vile ambavyo watu wa dunia wanafikiri wanastahili kuwa navyo?" Wakati tunaposoma ya kwamba **Mwana wa watu alikosa pahali pa kulalisha kichwa chake** tunataka kumhurumia. Lakini mwalimu mmoja aliandika, "Bwana hakuhitaji huruma yako. Ujihurumie mwenyewe kama ukiwa na nyumba ambayo inakuzuiza wakati Kristo anapotaka umtumikie pahali pengine." Hatusomi habari nyingine juu ya mtu huyu, hivi tunafikiri hakuwa tayari kuachana na maneno mazuri ya dunia hii na kufuata Mwana wa Mungu kweli.

**9:59** Mtu wa pili alisikia Kristo akimwita **kumfuata**. Alitaka kufanya hivi, lakini kulikuwa na neno moja alilotaka kufanya **kwanz**a. Alitaka kwenda na **kuzika baba yake**. Ona maneno aliyosema: **"Bwana … niende kwanza…"** Ni kusema, "**Bwana** … **mimi kwanza.**" Aliita Yesu **Bwana,** lakini aliweka maneno yeye mwenyewe aliyotaka kwanza. Maneno haya "Bwana" na "mimi kwanza" hayapatani hata kidogo. Ni lazima kwetu kuchagua "Bwana" au "mimi." Hatujui kama **baba** wa mtu huyu alikuwa amekufa au kama mwana wake alikusudi kungoja kwanza kufika saa ya mauti yake. Si neno. Neno kubwa ndilo hili: aliweka neno lingine mbele ya mwito wa Kristo. Ni taratibu kwa mwana kuonyesha heshima kwa baba yake kwa mwisho wa maisha yake, lakini ni zambi kabisa kuacha mtu ye yote au kitu cho chote kushindana na Kristo kwa pahali pa kwanza ndani ya maisha yako. Mtu huyu alikuwa na kazi nyingine, labda kazi ya biashara ambayo ilimkokota kuacha njia ya kufuata Bwana na roho moja.

**9:60** Bwana alimhamakia juu ya kuwa na nia mbili, akasema, **"Uache wafu wazike wafu wao, lakini wewe kwenda kupasha habari za ufalme wa Mungu."** Wale walio wafu *katika roho* wanaweza kuzika wafu *wa mwili*, lakini

hawawezi kuhubiri Habari Njema. Haifai wafuata kuweka roho kufanya kazi ambayo wasioamini wanaweza kufanya. Kazi kubwa ya mwamini ni kuendelesha shauri la Kristo mbele hapa duniani.

**9:61** Mtu huyu wa tatu aliyesema alitaka kufuata Yesu alifanana na mtu wa kwanza kwa njia ya kujitoa kwa moyo **kufuata** Kristo. Alifanana na mtu wa pili kwa njia ya kusema maneno yale mawili yasiyopatana, **"Bwana … mimi kwanza."** Alitaka kuagana **kwanza** na watu wa jamaa yake. Neno hili lilikuwa jema tu, lakini hata desturi hizi nzuri za maisha yetu ya kila siku hazifai kama tukiziweka mbele ya kutii Bwana mara moja na ndani ya maneno yote.

**9:62** Yesu alimwambia ya kwamba **akiweka mkono wake juu ya jembe la kukokotwa** (mfano wa kufuata Yesu), na kisha anatazama **nyuma**, **hafai kwa ufalme wa Mungu.** Wafuata wa Kristo hawavutwi mbio na mapendo kwa jamaa au rafiki. Ndiyo, mapendo haya si mabaya, lakini haifai wayaruhusu kuwazuiza wasijitoe mzima kwa Bwana na kazi yake. Maneno haya **"hafai kwa ufalme wa Mungu"** si juu ya wokovu lakini ni juu ya utumishi. Si neno la ku*ingia* ufalme lakini ni neno la *utumish*i katika ufalme, nyuma ya kuingia. Tunaweza kuingia ufalme kwa njia ya imani kwa sababu ya Bwana Yesu Kristo na kazi yake.

Hivi kwa njia ya watu hawa watatu tunaona mambo matatu ambayo yanaweza kutuzuiza tusifuate Bwana na roho ya kweli:

1. Mapendo kwa vitu na anasa ya dunia.
2. Kazi, labda kazi ya biashara.
3. Jamaa na rafiki.

Sharti Kristo atawale ndani ya mioyo yetu bila mshindani.

### C. Wanafunzi makumi saba wanatumwa (10:1-16)

**10:1-12** Tunasoma hapa tu ndani ya vitabu vya Habari Njema juu ya kutumwa kwa wanafunzi **makumi saba**. Habari hizi zinafanana na habari za kutumwa kwa wanafunzi kumi na wawili katika Matayo 10. Lakini wanafunzi wale walitumwa kwa upande wa kaskazini wa inchi. Wanafunzi 70 walitumwa kwa upande wa kusini, kwa njia Bwana atakayofuata kwenda Yerusalema. Ni kama iliwapasa kutayarisha njia kwa safari ya Bwana toka Kaisari Filipi kwa kaskazini, kupita kwa Galilaya na Samaria, kuvuka Yorodani, kupita kwa kusini kwa Perea, kisha kuvuka Yorodani tena hata Yerusalema.

Utumishi wa wale makumi saba ulikuwa kwa wakati tu, lakini mafundisho ya Bwana kwa watu hawa ni kwa Wakristo wa kila wakati. Tunaweza kuyajumlisha hivi:

1. Bwana aliwatuma **wawili wawili** (sh.1). Neno hili litahakikisha kweli ya ushuhuda wao, "Katika vinywa vya washuhuda wawili au watatu kila neno lisimamishwa" (2 Kor. 13:1).

2. Ingepasa mtumishi wa Bwana kukaa **kuomba** Bwana **kutuma watenda kazi katika mavuno** yake (sh.2). Kila mara hitaji kwa watenda kazi linapita hesabu yao. Wakati tunapoomba Bwana kutuma watenda kazi inatupasa kuwa tayari kwenda sisi wenyewe. Ona: **ombeni** (sh.2), **kwendeni** (sh.3).

3. Wanafunzi wa Yesu wanatumwa katikati ya watu wa dunia wasiopenda maneno ya Mungu (sh.3), nao ni kama **wana-kondoo kati ya imbwa za poli.** Wasizanie wataheshimiwa na watu wa dunia; watapata mateso na hata mauti.

4. Haifai wafikiri juu ya kukaa vizuri wao wenyewe (sh.4a). **"Musichukue mfuko wa kutia feza; wala ndaha, wala viatu." Mfuko wa kutia feza** unatufikirisha juu ya kujiwekea mali kwa mahitaji yetu kwa wakati wa kuja.

**Ndaha** ni kwa vyakula. Labda **viatu** ni jozi ya viatu vya akiba. Vyote vinasema juu ya umasikini, "kama masikini, lakini tunatajirisha wengi" (2 Kor. 6:10).

5. **"Musisalimu mtu katika njia"** (sh. 4b). Haifai watumishi wa Mungu kupoteza saa na kutoa salamu ndefu za heshima kama ilivyokuwa desturi kwa inchi zile za mashariki kwa wakati ule. Hata kama iliwapasa kuwa na adabu, sharti watumike na saa yao kutangaza Habari Njema, si kwa masemo marefu yasiyo na faida. Hakuna saa kwa kuchelewa bure.

6. Wafurahi na ukarimu wa watu wo wote ambao wanawakaribisha nyumbani (mash. 5,6). Watu wa nyumba fulani wakifurahia salamu yao, halafu mwenye nyumba ni **mwana wa salama,** atakayepokea habari za salama. Kama akikataa kupokea wanafunzi, wasilegee rohoni; salama yao **itarudi kwao** tena, maana yake hakuna kitu kilichopotea bure na watu wengine wataipokea.

7. Sharti wanafunzi **wakae katika nyumba ile** ya wale ambao waliwapokea kwanza (sh.7). Haifai wahame **toka nyumba** moja **kwenda nyingine** kama watu wanaotafuta pahali pazuri zaidi, lakini wakae na asante.

8. Wasisite kula na kunywa vyakula na vinyweo vyo vyote vinavyowekwa mbele yao (sh.7). Wakiwa watumishi wa Bwana wanastahili kuvipokea.

9. Miji na vijiji vinasimamia au kushindana na Bwana vilevile, namna watu mmoja mmoja wanavyofanya (mash. 8,9). Sharti mitume wahubiri pahali gani watu wanapokubali kusikiliza na kuwakaribisha nyumbani mwao, na kuletea watu hawa baraka za Habari Njema, na inawapasa **kula vyakula vinavyowekwa mbele yao**. Wagonjwa wataponyeshwa katika miji na vijiji vinavyopokea wajumbe wa Bwana, na Mfalme mwenyewe ni **karibu** sana nao (sh.9).

10. Inawezekana kwa kijiji kukataa Habari Njema na halafu watu wa kijiji hiki hawatakuwa na njia kuisikia tena kamwe (mash. 10-12). Haifai watu kuchezacheza na Habari Njema kwani siku nyingine wataisikia mara ya mwisho. Wakikataa nuru ya Habari Njema hawataweza kuipokea tena kamwe. Miji na vijiji wanaobarikiwa kwa njia ya kusikia Habari Njema na wanaikataa watapata hukumu kali kupita mji wa **Sodomo.** Kupewa heshima kusikia Habari Njema kunaleta daraka kubwa.

**10:13,14** Wakati Yesu aliposema maneno haya alikumbuka miji mitatu katika Galilaya iliyobarikiwa kupita mingine kwa sababu ya Habari Njema. Watu wa miji ile walimwona akifanya maajabu katika njia za miji yao. Walikuwa wamesikia mafundisho yake ya neema. Lakini walimkataa kabisa. Kama angalifanya katika **Tiro na Sidona** maajabu aliyofanya katika **Korazini na Betesaida** kama wangalitubu kabisa na kuiketi katika gunia na majivu. Kwa sababu kazi za uwezo za Yesu hazikugusa roho za watu wa miji ya Galilaya, hukumu yao itakuwa kubwa kupita ile ya **Tiro na Sidona**. Na kweli kwa wakati wa nyuma Korazini na Betesaida iliangamizwa kabisa, na kwa wakati wa sasa watu hawajui kabisa pahali gani miji hii iliposimama.

**10:15** Wakati Yesu alipoondokea Nazareti alihama kukaa katika Kapernaumu. Mji ule **ulipandishwa hata mbingu,** maana yake ulibarikiwa sana sana kwa sababu Mwokozi wa dunia alikaa pale, lakini watu walimzarau. Kwa sababu hii **utashushwa hata Hadeze.**

**10:16** Kwa mwisho wa mafundisho yake kwa wanafunzi makumi saba Yesu aliwaambia ya kwamba wao walikuwa wajumbe wake. Watu wakiwakataa wanamkataa yule ambaye aliwatuma, na wakimkataa yeye, wanakataa Mungu, Baba.

Mwalimu Ryle alisema,

> Hakuna masemo katika Agano Jipya yanayoonyesha na uwezo kupita ukubwa na heshima ya kuwa mtumishi mwaminifu wa Mungu, na hatia ya wale wanaokataa kusikia mahubiri na mafundisho yake. Kumbuka ya kwamba Bwana Yesu hakusema maneno haya kwa mitume kumi na miwili, lakini aliyasema kwa wanafunzi wale makumi saba. Hatujui majina yao wala kusoma maneno mengine juu yao. Mwalimu mwingine alisema: "Kukataa mjumbe au kumzarau ni kama matukano kwa mkubwa ambaye alimtuma, na ambaye anamsimamia. Mitume na wanafunzi makumi saba walikuwa wajumbe wa Kristo na walimsimamia; wale ambao walikataa na ushuhuda wao walikataa Bwana wao." [17]

**D. Wanafunzi makumi saba wanarudi (10:17-24)**

**10:17,18** Wakati **waliporudi** toka safari yao walifurahi sana kwa sababu hata **pepo wachafu waliwatii**. Tunaweza kufahamu jibu la Yesu kwa njia mbili. Usitawi wao ulimfikirisha **kuanguka kwa Shetani** kwa wakati wa kuja. Neno hili litatokea kweli wakati wa kuja. Mikaeli na malaika zake watamtupa **toka mbinguni** (Ufu.12:7-9), kwa wakati wa Mateso Makubwa, mbele ya Utawala wa Utukufu wa Kristo duniani.

Tunaweza kufikiri juu ya maneno haya kama maonyo kuepuka kiburi. Ni kama Yesu alikuwa akisema, "Ndiyo, munajisifu kwa sababu pepo wachafu wanawatii ninyi. Mukumbuke basi – kiburi kinazaa zambi. Lusifero alianguka na kufukuzwa toka mbinguni kwa sababu ya kiburi. Mukae na ange na kuepuka hatari hii."

**10:19** Bwana alikuwa amewapa wanafunzi wake **amri** juu ya roho wabaya. Hakuna kitu kilichoweza kuwaumiza kwa safari yao. Ni vivyo hivyo na watumishi wote wa Mungu; wanalindwa.

**10:20** Hata hivi **haifai wafurahi** kwa sababu walikuwa na uwezo juu ya **pepo, lakini wafurahi** kwa sababu wao wenyewe walikuwa wamepokea wokovu. Hii ni mara ya pekee tunayosoma juu ya Bwana akikataza wanafunzi kufurahi. Ni hatari kwa sisi kujivuma wakati tunapoona baraka ndani ya utumishi wetu kwa Bwana, lakini wakati tunapofurahi kwa sababu **majina yetu yanaandikwa mbinguni** tunakumbushwa deni yetu kubwa kupita kipimo kwa Mungu na Mwana wake. Hakuna hatari kwa kiburi wakati tunapofurahia wokovu tuliopokea kwa njia ya neema.

**10:21** **Yesu** alikuwa amekataliwa na makutano, lakini akiangalia wanafunzi wake **alifurahi katika Roho Mtakatifu** na kushukuru **Baba** kwa hekima yake. Wale wanafunzi makumi saba hawakuwa **wenye hekima na akili** wa dunia hii. Hawakuwa wenye kujifunza sana lakini walikuwa kama **watoto wachanga**. Lakini walikuwa watoto wenye imani na mapendo, wenye roho ya kutii bila shaka katika mambo yote. Elimu ya wenye kujifunza sana haikuwasaidia. Kiburi yao kiliwafanyiza vipofu katika roho, hata hawakuweza kuona faida kubwa ya kweli ya Mwana mpendwa wa Mungu. Mungu anaweza kutumika vizuri zaidi kwa njia ya watoto wachanga. Bwana wetu alifurahia wote ambao Baba alimpa na alifurahishwa na baraka hawa makumi saba waliyoona ndani ya safari yao, iliyokuwa kama malimbuko ya kuharibiwa kwa Shetani kwa wakati wa kuja.

**10:22** Mwana **alipewa vitu vyote na Baba** yake, vitu vilivyo mbinguni, duniani, au chini ya dunia. Mungu aliweka ulimwengu mzima chini ya amri ya Mwana wake. **Hakuna mtu anayejua Mwana ila Baba.** Baba tu anatambua na kujua siri ya kweli hii ya namna gani Mungu aliweza kugeuka Mtu na kukaa ndani ya mwili wa namna ya mtu. Sisi viumbe vya dunia hii hatuwezi kufahamu neno hili kamwe. Wala hatuwezi

kujua **Baba ila kwa njia ya Mwana na mtu ye yote Mwana anayependa kumfunulia.** Mungu vilevile ni mjuu kupita akili na ufahamu wa mtu. Mwana anamjua kabisa, na Mwana amemfunua kwa wazaifu, watu wa chini nao wanaozarauliwa lakini ambao wanamwamini yeye (1 Kor. 1:26-29). Wale walioona Mwana wameona Baba. Mwana pekee aliye katika kifua cha Baba, huyu ndiye alimfunua wazi (Yoane 1:18).

Mwalimu Kelly alisema, "Kweli Mwana anafunua Baba, lakini watu wanashindwa kila mara wanapojaribu kufahamu kabisa fumbo lisiloweza kufahamikana ya utukufu wa Kristo mwenyewe."

**10:23,24** Wakati walipokuwa **peke yao,** Bwana aliwaambia **wanafunzi** ya kwamba waliheshimiwa sana kuweza kuishi kwa wakati ule. **Manabii na wafalme** wa wakati wa Agano la Kale **walitaka kuona** siku za Masiya lakini hawakuziona. Hivi hapa Bwana alionyesha ya kwamba yeye ni yule ambaye manabii walitazamia – Masiya. Ilikuwa heshima kwa wanafunzi ku**ona** maajabu na ku**sikia** mafundisho ya Tumaini la Israeli.

### E. Mwana-sheria na Msamaria Mwema (10:25-37)

**10:25** Labda **mwana-sheria,** fundi la kujua mafundisho ya sheria ya Musa, hakuuliza na roho ya kweli, lakini na udanganyifu akitaka kuona kama Mwokozi atakataa sheria. Kwa mafikiri yake, **Yesu** alikuwa **Mwalimu** tu, na alifikiri aliweza kupata **uzima wa milele** kwa njia ya kazi zake njema.

**10:26-28** Bwana alikumbuka maneno haya yote wakati alipojibu ulizo lake. Kama mwana-sheria angalikuwa na roho ya unyenyekevu na toba, kama Bwana angalimjibu wazi kupita. Basi alikokota mafikiri yake juu ya **sheria. Sheria** iliagiza nini? Iliagiza mtu **kupenda Bwana** na roho yote, na **jirani** yake **kama** yeye mwenyewe. Yesu alisema naye kwamba akifanya hivi, **ataishi**.

Wakati unaposoma maneno haya, labda unafikiri Bwana alifundisha kwamba lazima tutimize sheria kwa kupata uzima wa milele. Sivyo, hata kidogo. Halikuwa kusudi la Mungu kamwe kwa mtu kuokolewa kwa njia ya kushika sheria. Amri Kumi zilitolewa kwa watu waliokuwa wenye zambi hata mbele. Kusudi la sheria si kuokoa watu toka zambi, lakini kuwafahamisha kama zambi ni nini. Ni kuonyeshea mtu zambi na hatia yake kubwa.

Haiwezekani kwa mwenye zambi kupenda Mungu na **roho** yake **yote,** na **jirani** yake kwa kipimo anachojipenda mwenyewe. Kama angaliweza kufanya hivi tangu siku ya kuzaliwa kwake kufika siku ya kufa kwake asingalihitaji wokovu. Asingalipotea. Lakini zawabu yake itakuwa maisha marefu hapa duniani tu, si uzima wa milele mbinguni. Atakaa hai kwa miaka yote angaliyoishi bila kufanya zambi. Uzima wa milele ni kwa wenye zambi wale tu wanaokubali kwamba wamepotea na wanaookolewa kwa neema ya Mungu.

Hivi neno Yesu alilojibu, **"Fanya hivi nawe utaishi"** halikuwezekana. Kama mwana-sheria angaliuliza na roho ya kweli maneno Yesu aliyosema juu ya sheria yangalimsukuma kusema, "Kama hili ndilo Mungu anataka, mimi ni mpotevu; siwezi kujisaidia mwenyewe na sina tumaini. Tafazali uniokoe kwa sababu ya mapendo na rehema na neema yako!"

**10:29** Lakini mwana-sheria hakufanya hivi, lakini alijaribu **kujihakikisha mwenyewe.** Kwa nini alifanya hivi? Hakuna mtu ambaye alikuwa amemshitaki. Rohoni mwake alifahamu kwamba alikuwa na hatia, na neno hili liliamsha kiburi na hamu kushindana ndani yake. Basi aliuliza, **"Jirani yangu ni nani?"** Lilikuwa ulizo la hila.

**10:30-35** Kwa kujibu ulizo hili Bwana **Yesu** alipasha habari za Msamaria mwema. Watu wanajuana na habari hizi. Tunafikiri yule aliyeanguka katika mikono wa wanyanganyi alikuwa Myuda. Walimwacha **karibu kufa** kwa njia inayokwenda **Yeriko**. **Kuhani** na **Mlawi** waliokuwa Wayuda walikataa kumsaidia; labda waliogopa hali yake ilikuwa mtego tu na ya kwamba wao vilevile wataibiwa kama wakichelewa karibu na mtu huyu. Basi **Msamaria**, mtu aliyechukiwa na Wayuda, alimsaidia na dawa na kumpeleka kwa **nyumba ya wageni** na aliacha mali kwa **mahitaji** yake. Kwa mafikiri ya Msamaria huyu Myuda alikuwa jirani yake.

**10:36,37** Halafu Mwokozi alikuwa na ulizo tusiloweza kuepuka: **Nan**i ya watu hawa **watatu** alikuwa **jirani** ya mtu huyu asiyeweza kujisaidia mwenyewe? Ndiyo, yule ambaye **alimhurumia**. Basi mwana-sheria **aende na kufanya vivyo hivyo**. "Kama Msamaria aliweza kutenda kama jirani ya kweli kwa Myuda kwa njia ya kumhurumia, halafu watu wote ni jirani." [18]

Ni nyepesi kwa sisi kuwaza juu ya kuhani na Mlawi kama mifano kuonyesha kwamba sheria haina uwezo hata kidogo kusaidia mwenye zambi. Sheria iliagiza "Penda jirani yako kama wewe mwenyewe" bila kumpa mtu uwezo kutii agizo hili. Na si nguvu kuona Msamaria kama mfano wa Bwana Yesu ambaye alifika pahali tulipokuwa, alituokoa toka zambi zetu na kutupatia vyote tunavyohitaji kwa safari yetu duniani kufikia hata mbingu na kwa milele. Labda makuhani na Walawi hawatasaidia kama inavyofaa, lakini Msamaria Mwema ni mwaminifu wakati wote.

Habari hizi za Msamaria mwema zilianza na ulizo hili: "Jirani yangu ni nani?" na zilikwisha na ulizo: "Unatendea nani kama jirani?"

### F. Maria na Marata (10:38-42)

**10:38-41** Sasa Bwana alianza kusema juu ya Neno la Mungu na maombi kama njia mbili kupata baraka ya Mungu (10:38–11:54).

**Maria aliketi mbele ya miguu ya Yesu, akasikia maneno yake**, lakini **Marata alihangaika** na kazi nyingi ya kutayarisha vyakula kwa Mgeni wake, Mfalme. Alitaka Bwana kuhamakia ndugu yake kwa sababu hakumsaidia, lakini Yesu alimhamakia yeye na roho ya mapendo kwa sababu ya kusumbuka sana.

**10:42** Bwana anapendezwa na mapendo yetu kupita utumishi wetu. Ni nyepesi kujivuma juu ya utumishi wetu lakini kuwaza juu ya Bwana wetu na kumwabudu **ni kitu kimoja kinachohitajiwa … sehemu iliyo njema, nayo haitaondoshwa kwetu**. "Bwana anataka kutugeuza kuwa kama Maria na wenye kupenda jirani zetu." [19]

Charles R. Erdman aliandika:

> Bwana wetu anafurahi juu ya kazi yo yote ambayo tunafanya kwa yeye, lakini anajua tunahitaji kwanza kukaa kwa miguu yake na kujifunza mapenzi yake; halafu ndani ya kazi yetu tutakuwa na utulivu na upole na amani, na mwishoni utumishi wetu utafikia utimilifu wa ule wa Maria wakati siku nyingine alipomwangia miguu ya Yesu marasi ya harufu tamu inayojaza dunia hata sasa. [20]

### G. Ombi la wanafunzi (11:1-4)

Habari za maneno zilizotokea nyuma ya mwisho wa sura 10 na mwanzo wa sura 11 ziliandikwa katika Yoane 9:1 – 10:21.

**11:1** Hapa Luka aliandika tena juu ya maombi ndani ya maisha ya Bwana wetu. Neno hili lilipatana na kusudi la Luka kuonyesha Kristo kama Mwana wa watu, mwenye kutegemea Mungu Baba yake wakati wote. Wanafunzi walifahamu kwamba maombi yalikuwa neno kubwa, neno la uwezo katika

maisha ya Yesu. Wakimsikia akiomba walipata hamu kuomba vilevile. Hivi **mmoja wa wanafunzi wake** alimwomba **kuwafundisha kuomba.** Hakusema, "Utufundishe *namna gani* kuomba," lakini **"Utufundishe kuomba."** Bila shaka alitaka maneno mawili haya yote.

**11:2** Kipeo cha ombi ambacho Bwana aliwapa kwa wakati huu si sawasawa na ombi linaloitwa "ombi la Bwana" katika Habari Njema ya Matayo kwa maneno yote. Kuna maana kwa tofauti hii.

Kwanza, Bwana alifundisha wanafunzi wake kuita Mungu **Baba yetu.** Waamini katika Agano la Kale hawakujuana na ukaribu na ushirika namna hii. Maana yake ni ya kwamba sasa waamini wanaweza kusema na Mungu kama **Baba** ya mapendo mbinguni. Nyuma yake tunafundishwa ya kwamba inatupasa kuomba **jina** la Mungu liwekwe **takatifu**. Neno hili linaonyesha hamu rohoni mwa mwamini kwa Mungu kupata heshima, kutukuzwa na kuabudiwa. Ndani ya masemo **"Ufalme wako uje"** tunaona hamu yetu kwa kufika kwa siku wakati Mungu atakaposhinda kabisa uovu wa dunia, na ndani ya Kristo, atatawala juu ya **dunia,** pahali **mapenzi** yake **yatakapofanyika kama mbinguni.**

**11:3** Hivi nyuma ya kuomba kwanza kwa Mungu na haki yake, mwombaji anafundishwa kujulisha mahitaji yake ya kila siku, na maneno ambayo angependa kupokea yeye mwenyewe, mahitaji ya mwili na ya roho. Inatupasa kutegemea Bwana kwa mahitaji yetu ya **kila siku,** tukikiri ya kwamba vitu vema vyote vinatoka kwake.

**11:4** Halafu kuna ombi kwa usamehe wa **zambi**, kama sisi wenyewe tulikuwa na roho ya usamehe kwa watu wengine. Si ombi kwa usamehe toka azabu ya zambi. Usamehe ule unategemea kazi Kristo aliyotimiza kwa Kalvari, na tunaupokea kwa njia ya imani tu. Lakini tunasoma hapa juu ya usamehe wa baba kwa mtoto. Wakati tunapokwisha kuokolewa Mungu anatutendea kama watoto. Akiona tuna roho ngumu ndani yetu inayokataa kusamehe watu wengine, atatuazibu kufika wakati roho zetu zinapovunjika na tunarudi karibu naye na kupatanishwa naye tena. Usamehe huu ni juu ya upatano wetu na Mungu.

Watu wengine wanafazaika juu ya ombi **"Usitulete katika majaribu."** Tunajua Mungu hajaribu watu kufanya zambi. Lakini anakubali kwa sisi kupata mambo magumu na majaribu; maneno haya ni faida kwetu. Inatupasa kukumbuka saa zote ya kwamba ni nyepesi sana kuacha njia ya Mungu na kufanya zambi. Sharti tuombe Mungu kutulinda na kutuzuiza tusitende zambi, hata wakati labda sisi wenyewe tungetaka kuifanya. Ingetupasa kuomba ili saa ambayo tungetaka kufanya zambi iwe mbali na saa tunapoweza kupata njia kuifanya. Ombi hili "Usitulete katika majaribu" linaonyesha kwamba tunafahamu hatuwezi kushinda majaribu kwa nguvu yetu. Linakwisha na "utuokoe **kwa uovu.**"

### H. Mifano miwili juu ya maombi (11:5-13)

**11:5-8** Akiendelea na mafundisho juu ya maombi, Bwana alitoa mifano kuonyesha kwamba Mungu ni tayari kabisa kusikia na kujibu maombi ya watoto wake. Habari hizi ni juu ya mgeni mmoja aliyefikia nyumba ya rafiki yake **saa sita ya usiku.** Mwenye nyumba hakuwa na vyakula vya kutosha kwa mgeni wake, hivi alifikia jirani yake, akapiga hodi kwa mlango wake, na kumwomba kumpa **mikate mitatu**. Kwanza jirani yake hakufurahi hata kidogo juu ya kuamshwa toka usingizi wake na hakwenda kufungua mlango. Lakini mtu aliyekuwa inje alikaa kupiga mlango na kulalamika, hivi mwishoni

jirani aliamka, **akampa** vyakula alivyohitaji.

Habari hizi **hazitufundishi** ya kwamba Mungu anachukizwa wakati tunapoomba neno fulani tena na tena. Na **hazifundishi** ya kwamba njia ya pekee kwa sisi kupata jibu kwa maombi yetu ni kudumu katika maombi haya.

Lakini mafundisho ya habari hizi ndiyo haya: mtu huyu akiwa tayari kusaidia rafiki yake kwa sababu rafiki huyu alikaa kuombaomba, *kuzidi sana* Mungu ni tayari kusikia vilio vya watoto wake.

**11:9** Zinatufundisha vilevile kwamba haifai kwa sisi kuchoka na kulegea katika maombi yetu. "Inatupasa kukaa kuomba … kusikia … kupiga hodi … Mara nyingine Mungu anajibu ombi letu mara ya kwanza tunapoliomba, lakini mara nyingine anajibu tu wakati tunapokwisha kuomba kwa neno fulani siku nyingi.

> Mungu anajibu maombi: Mara nyingine wakati roho za waamini ni zaifu, anatoa mara moja zawadi wanazoomba kwake.
>
> Lakini mara nyingine anataka kupatisha imani yetu nguvu na kutufundisha kuwa na raha rohoni na kumwamini hata wakati anaponyamaza.
>
> Maana Mungu wetu ni mwenye mapendo naye atafanya yaliyo mema zaidi; yeye ni kweli na atatimiza ahadi zake zote; Yeye ni nguvu yetu.
>
> – *M.G.P.*

Ni kama mfano huu unatufundisha kudumu kupita na kupita katika maombi – kuomba, kutafuta na kupiga hodi.

**11:10** Mfano huu unafundisha ya kwamba **kila mtu anayeomba atapewa;** naye **anayetafuta atapata**; naye **anayepiga hodi atafunguliwa.** Ni ahadi ya kwamba wakati tunapoomba Mungu anatupatia sisi kitu tunachoomba au kitu kizuri kupita. Anasema "hapana" wakati anapojua neno ambalo tuliomba si kwa baraka kubwa zaidi kwasi. Hivi kukataa kufanya neno ambalo tuliomba ni vizuri kuliko kufanya neno tuliloomba.

**11:11,12** Mfano unafundisha ya kwamba Mungu hatatudanganya kamwe kwa njia ya kutupa sisi **jiwe** wakati tunapoomba kupewa **mkate**. Kwa wakati ule mkate ulikuwa mviringo na ulifanana na jiwe. Mungu hatatuzarau kamwe kwa njia ya kutuletea kitu tusichoweza kula wakati tunapoomba vyakula. Tukiomba kupewa **samaki** hatauletea **nyoka**, ndicho kitu ambacho kinaweza kutuharibu. Na tukiomba kupewa **yai,** hatatuletea **nge**, maana kitu ambacho kitaleta maumivu makubwa.

**11:13** Baba ya dunia hatoi zawadi mbaya; hata kama akiwa na tabia ya zambi anajua **kuwapa watoto wake zawadi njema. Basi Baba yetu aliye katika mbingu atawapa wote ambao wanamwomba Roho Mtakatifu.**

J.G. Bellet anasema, "Ona ya kwamba zawadi ambayo Baba anachagua kuwa ile tunayohitaji zaidi, na ile anayotaka zaidi kutupa sisi ni Roho Mtakatifu." Wakati Yesu aliposema maneno haya, Roho Mtakatifu alikuwa hayatolewa bado (Yn. 7:39). Haifai kwetu kuomba *kupewa* Roho Mtakatifu kukaa ndani yetu kwa wakati wa sasa kwa sababu anakuja kukaa ndani yetu siku tunapookolewa (Rom. 8:9b; Efe. 1:13,14).

Lakini ni taratibu kwa sisi kuomba kwa Roho Mtakatifu kwa njia nyingine. Inatupasa kuomba tuwe tayari kupokea mafundisho toka kwake, tuweze kuongozwa naye, na uwezo wake utujaze kwa utumishi wetu wote kwa Kristo.

Wakati Yesu alipofundisha wanafunzi juu ya kupewa **Roho Mtakatifu** tunawaza alifikiri juu ya *uwezo* wa Roho kuwawezesha kuishi maisha ya wanafunzi wa kweli namna alivyowafundisha ndani ya sura za mbele. Tunafikiri kwa saa hii walikuwa wamefahamu kwamba hawataweza hata kidogo kufanya ma-

neno haya kwa nguvu yao wenyewe. Neno hili ni kweli kabisa. **Roho Mtakatifu** ndiye uwezo ambaye anaweza kutuwezesha kuishi kwa yeye. Hivi Yesu alionyesha kwamba Mungu anataka sana kuleta uwezo huu kwa wale ambao wanamwomba.

**I. Yesu anajibu wagombezi wake (11:14-26)**

**11:14-16** Makutano walishangaa sana wakati walipoona Yesu **akifukuza pepo mwenye bubu.** Hata kama **makutano walishangaa,** uadui wa wengine uliongezeka. **Wengine** walisema **alifukuza pepo** kwa **Belzebuli, mkubwa wa pepo wachafu**. Wengine walisema naye kufanya **alama toka mbingu.** Labda walifikiri neno hili litahakikisha ya kwamba mashitaki ya watu hayakuwa kweli.

**11:17,18** Ndani ya mash.17-26 Bwana alijibu mashitaki yao ya kwamba alitoa pepo wachafu kwa sababu yeye mwenyewe alikaliwa na Belzebuli. Jibu lake juu ya alama toka mbinguni ni ndani ya shairi 29. Kwanza Bwana aliwakumbusha kwamba **kila ufalme unaotengwa kwake wenyewe** utapata kuharibiwa, na kila **nyumba inayotengwa kwake** yenyewe itaanguka. Kama Shetani alitumika naye (Yesu) kutoa pepo wachafu, Shetani angalifanya vita na watumishi wake mwenyewe. Ni neno la kuchekesha kuwaza juu ya Shetani kushindana na yeye mwenyewe na kuzuiza makusudi yake mwenyewe.

**11:19** Vilevile Bwana alikumbusha wagombezi wake ya kwamba wengine wa wenyeji wao walikuwa saa ile ile wakitoa pepo wachafu. Kama yeye mwenyewe alifanya hivi kwa uwezo wa Shetani, ni wazi ya kwamba wao walifanya hivi kwa uwezo wa Shetani vilevile. Ndiyo, Wayuda hawatakubali neno hili kamwe. Hata hivi namna gani wataweza kukana ya kwamba uwezo wa kutoa pepo wachafu unatoka au kwa Mungu au kwa Shetani? Kama Yesu akitenda kwa uwezo wa Shetani, halafu Wayuda walitegemea uwezo ule vilevile. Kwa njia ya kumhukumu yeye walijihukumu wenyewe vilevile.

**11:20** Elezo la haki ndilo hili: **Yesu alifukuza pepo wachafu kwa kidole cha Mungu.** Basi maana ya **kidole cha Mungu** ni nini? Ndani ya Matayo 12:28 tunasoma, "Kama mimi kwa Roho ya Mungu nikitoa peo wachafu, ufalme wa Mungu umekwisha kuwafikia ninyi." Hivi tunafahamu ya kwamba ndani ya Luka 11:20 Roho ya Mungu anaitwa **kidole cha Mungu**. Tendo la Yesu akitoa pepo wachafu kwa Roho ya Mungu lilihakikisha ya kwamba ufalme wa Mungu umekuja kwa watu wa kizazi hiki. Ufalme ulikuwa umefika. Mfalme mwenyewe alisimama kati yao. Bwana Yesu alikuwa pale, akifanya maajabu namna hii. Mambo haya yalihakikisha kabisa ya kwamba Mtawala mpakaliwa wa Mungu alikuwa amefikia watu duniani.

**11:21,22** Kufika wakati ule, Shetani alikuwa **mtu wa nguvu**, **mwenye silaha** aliyelinda nyumba yake. Wale waliokaliwa na pepo wachafu walifungwa kabisa naye, na mwenye kushindana naye hakuwa. **Mali zake** zilikuwa **salama,** maana hakuna aliyeshindana naye. Lakini Bwana Yesu alikuwa na **nguvu kupita** Shetani, naye **alikuja kwake**, akamshinda, alimnyanganya **silaha zake** na kugawanya **nyara yake.**

Hata wagombezi wake hawakuweza kubisha ya kwamba Yesu alikuwa akitoa pepo wachafu. Neno hili lilikuwa na maana moja tu: Shetani alikuwa ameshindwa, na wale walioteswa naye walifunguliwa toka taabu yao. Haya ndiyo mafundisho ya mashairi haya.

**11:23** Halafu Bwana Yesu alisema ya kwamba kila mtu **asiye pamoja** naye **ni adui** yake, naye **asiyekusanya pamoja** naye **anasambaza.** Tulionyesha

mbele kwamba inaonekana ya kuwa mafundisho ya shairi hili hayapatani na yale ya 9:50. Kama yakisema juu ya Kristo na kazi yake, mtu asiye pamoja na Kristo ni adui yake. Lakini kama yakisema juu ya utumishi wa Wakristo, wale wasio adui zao ni upande wao. Shairi la kwanza (11:23) ni juu ya wokovu; shairi la pili (9:50) ni juu ya utumishi.

**11:24-26** Ni kama sasa Bwana Yesu alianza kushitaki wagombezi wake yeye mwenyewe. Walikuwa wamesema kwamba alitawaliwa na pepo wachafu. Sasa Bwana Yesu alisawanisha taifa lao na mtu aliyeponyeshwa toka utawala wa pepo mchafu kwa wakati. Ilikuwa hivi na taifa la Israeli. Mbele ya uhamisho (toka inchi yao) walitawaliwa na pepo ya kuabudu sanamu. Lakini muda wa uhamisho uliwasafisha toka **pepo** mbaya ile, na tangu wakati ule Wayuda hawakushikwa tena na hamu ya kuabudu sanamu. Nyumba yao **imefagiwa na imepambwa**, lakini wamekataa kuruhusu Bwana Yesu kuingia na kukaa pale. Hivi alitabiri ya kwamba kwa wakati wa kuja **pepo yule mchafu** atakusanya **pepo saba wengine walio waovu kupita yeye mwenyewe**, nao **wataingia** na **kukaa nyumbani.** Hali ya mwisho ya mtu yule ni baya kuliko ya kwanza. Kwa wakati wa Mateso Makubwa Wayuda wataabudu sanamu sana sana na kukikiri kwamba mpinga Kristo ndiye Mungu (Yn. 5:43), na kwa zambi ile watavuna azabu kali sana kupita azabu zote ambazo walipata mbele.

Hata kama mashairi haya yanasema zaidi juu ya Israeli kama *taifa*, lina mafundisho kwa *mtu mmoja mmoja* vilevile. Haitoshi kwa mtu kutengeneza mwenendo wake tu. Lazima akaribishe Bwana Yesu Kristo ndani ya roho na maisha yake. Kama sivyo roho yake itakuwa wazi na tayari kufanya zambi mbaya kupita mbele.

**J. Heri kupita Maria (11:27, 28)**

Mwanamke mmoja alitoka **katikati ya makutano** kusalimu Yesu na masemo haya, **"Heri tumbo ambalo lilikuzaa, na maziwa uliyonyonya!"** Jibu la Bwana wetu lina maana kubwa. Hakubisha ya kwamba Maria, mama yake, alibarikiwa, lakini neno kubwa zaidi ni **kusikia Neno la Mungu na kulishika.** Hata bikira Maria alikuwa heri kwa sababu alikuwa mama yake, alikuwa heri kupita kwa sababu aliamini Kristo na kumfuata. Undugu kwa roho ni neno kubwa kupita undugu kwa mwili. Ingepasa maneno haya kunyamazisha wale wanaotaka kuabudu Maria.

**K. Alama ya Yona (11:29-32)**

**11:29** Ndani ya shairi 16 watu wengine walikuwa wamejaribu Bwana Yesu kwa njia ya kumwomba kuwapa **alama** toka mbingu. Alijibu ombi hili sasa kwa njia ya kusema **kizazi kibaya** wanatafuta alama. Alisema zaidi juu ya **kizazi** cha Wayuda walioishi kwa wakati ule. Watu wale walioishi saa ile walikuwa wamebarikiwa kupita mataifa mengine kwa sababu Mwana wa Mungu alikaa katikati yao. Walikuwa wamesikia masemo yake na kuona maajabu yake. Lakini maneno haya hayakutosha kwao. Walisema kama wangeweza kuona tu kazi kubwa moja ya uwezo zaidi toka mbinguni kama wangemwamini. Bwana aliwajibu kusema ya kwamba **hawatapewa alama, ila alama ya nabii Yona.**

**11:30** Alikuwa akiwaza juu ya ufufuko wake mwenyewe toka mauti. **Kama Yona** alivyoponyeshwa toka bahari nyuma ya kukaa ndani ya tumbo la samaki kwa siku tatu na usiku tatu, vivyo hivyo Bwana atafufuliwa toka wafu nyuma ya kukaa kaburini kwa siku tatu na usiku tatu. Ni kusema, ajabu la mwisho na la kuthibitisha zaidi la utumishi wa Bwana Yesu duniani, litakuwa ufufuko wake. Wakati Yona alipokwenda kuhubiri katika mji ule wa Mataifa,

alikwenda, kwa mfano, kama mmoja aliyefufuliwa toka wafu.

**11:31, 32 Malkia wa kusini**, malkia mtaifa, alifanya safari ndefu sana kusikia akili ya Solomono. Hakuona ajabu hata moja. Kama angaliishi kwa wakati Bwana Yesu alipokuwa duniani angalimpokea na furaha nyingi! Hivi malkia huyu **atasimama siku ya hukumu** juu ya watu wale waovu waliobarikiwa kwa njia ya kuona maajabu ya Bwana Yesu, na kumkataa hata hivi. Huyu aliyekuwa amefika duniani alikuwa **mkubwa kupita Yona**, na **mkubwa kupita Solomono. Watu wa Ninawe walitubu wakati waliposikia mahubiri ya Yona,** lakini watu wa Israeli walikataa kutubu wakati waliposikia mahubiri ya yule aliyekuwa **mkubwa kupita Yona.**

Wasioamini kwa wakati wa sasa wanacheka habari za Yona wakisema ni hadizi ya Waebrania tu. Yesu alisema juu ya Yona kama mtu aliyeishi kwelikweli, namna alivyosema juu ya Solomono. Watu wengine wanasema wataamini kama wakiona ajabu. Sivyo. Imani haisimami juu ya maneno tunayoweza kuona au kusikia au kugusa, lakini juu ya neno la Mungu lenye uzima. Mtu akikataa kuamini neno la Mungu, hataamini vilevile hata kama mtu akifufuliwa toka wafu. Mungu hapendezwi wakati watu wanapoomba alama. Neno hili si imani. Msiyeamini anasema, "Afazali niweze ona, halafu nitaamini. Mungu anasema, "Amini, halafu utaona."

### L. Mfano wa taa inayowashwa (11:33-36)

**11:33** Ni nguvu kufahamu mara moja namna gani mashairi haya yanaungamana na yale ambayo yanayatangulia. Lakini wakati tunapoyaangalia karibu karibu tunaona neno hili wazi. Yesu alikumbusha wasikiaji wake ya kwamba **hakuna mtu** anayeweka **taa** inayowaka pahali pa kufichwa au **chini ya kitunga.** Anaiweka juu ya **kinara**, iweze kuonekana wazi na kuleta nuru kwa kila mtu anayeingia nyumbani.

Ona mafundisho ya mashairi haya: Mungu ndiye **aliyewasha taa**. Kwa njia ya Bwana Yesu na kazi yake ameleta nuru kubwa kwa dunia. Si kosa la Mungu kama mtu asipoona Nuru. Ndani ya sura 8 Bwana Yesu alisema juu ya kazi ya wale ambao walikuwa wanafunzi hata kwa saa ile. Kazi yao ilikuwa kutangaza Habari Njema, si kuificha chini ya kitunga. Hapa ndani ya 11:33 alionyesha kutokuamini kwa wagombezi wake wenye tamaa walioogopa kupata haya.

**11:34** Makusudi yao yasiyokuwa safi yalizaa kutokuamini kwao. Kwa njia ya mwili, ni **jicho** linaloleta **nuru** kwa **mwili mzima**. Kama jicho likiwa na afya njema, mtu anaweza kuona nuru. Lakini jicho likiwa na ugonjwa, halafu nuru inazuizwa isiingie.

Ni vivyo hivyo kwa maneno ya roho. Kama mtu akitaka kujua kwelikweli kama Yesu ni Kristo wa Mungu, Mungu atamfunulia kweli hii wazi. Lakini kama makusudi yake si safi, kama akitaka kukaa kufungana na choyo yake, na akikaa kuogopa kama watu watasema nini juu yake, halafu yeye ni kipofu na hafahamu kwanza uzuri na wema wa Mwokozi.

**11:35** Yesu alikuwa akisema na watu waliowaza wao ni wenye hekima sana. Walifikiri walikuwa na nuru nyingi sana. Lakini Bwana Yesu aliwaonya ya kwamba **nuru** iliyokuwa ndani yao ilikuwa **giza** tu. Mawazo yao kwamba walikuwa wenye akili sana, na kiburi yao, ziliwazuiza wasifike karibu naye.

**11:36** Mtu mwenye makusudi safi, ambaye anafungua roho yake nzima kwa Yesu, Nuru ya dunia, anajazwa na nuru ya roho. Maisha yake ya roho yanatiwa nuru na Kristo, kama vile mwili

wake unatiwa nuru wakati anapokaa karibu na taa.

### M. Usafi wa inje na wa ndani (11:37-41)

**11:37-40** Wakati Yesu alipofikia nyumba ya **Mfarisayo mmoja** ambaye alimwita kula kwake, mwenye nyumba alishangaa kwa sababu **hakunawa mbele ya chakula**. Yesu alijua mawazo yake na alimhamakia juu ya unafiki na kuweka roho juu ya mambo ya kuonekana. Alimkumbusha ya kuwa neno kubwa zaidi si **usafi wa inje wa kikombe** lakini **usafi wa ndani**. Kwa upande wa inje Wafarisayo walionekana kama watu wazuri, lakini walikuwa waovu na wanyanganyi rohoni. Mungu ambaye **alifanya inje** ya mtu alimfanya kwa **ndani** vilevile, naye anataka maisha yetu ya ndani kuwa safi. "Mtu anaangalia kuonekana kwa inje, lakini BWANA anatazama moyo" (1 Sam. 16:7).

**11:41** Bwana alijua tamaa na choyo ya Wafarisayo hawa na namna walivyojifikiri wenyewe tu, hivi alisema na yule ambaye alimwita kula kwake **kutoa kwanza sadaka ya vitu alivyokuwa navyo** kwa kusaidia wenye hitaji. Akionyesha mapendo yake kwa watu wengine kwa njia hii, **halafu vitu vyote** vitakuwa **safi** kwake. H. A. Ironside aliandika:

> Wakati mapendo ya Mungu yanapojaza moyo wa mtu, naye anaweka roho juu ya mahitaji ya wengine, halafu maneno haya mengine ya kuonekana inje yatakuwa na faida. Lakini mtu yule ambaye anajivimbishia mali na vitu bila kukumbuka wenye mahitaji na wagonjwa ambao wanamzunguka, anaonyesha wazi ya kwamba mapendo ya Mungu hayakai ndani yake." [21]

Mwandishi mwingine alijumlisha maneno haya hivi:

> Bwana Yesu alisema maneno haya makali wakati alipokuwa mgeni nyumbani mwa Mfarisayo (sh.37). Tungewaza kwamba si adabu kufanya hivi. Sisi tunajaribiwa kunyamaza wakati inapotupasa kusimamia kweli. Lakini kuumiza roho ya mwenye nyumba ni vizuri kupita kuficha imani yetu.

### N. Wafarisayo wanakemewa (11:42-44)

**11:42 Wafarisayo** walikuwa wenye kuweka roho sana juu ya maneno ya kuonekana na sheria za dini, kama kutoa zaka za **mboga** namna mbalimbali, lakini hawakukumbuka ushirika wao na Mungu na watu. Walitesa watu masikini na hawakupenda Mungu. Bwana hakuwahamakia juu ya kulipa zaka za **mnanaa** na **mchicha** na kila mboga, lakini alionyesha ya kwamba haifai waweke roho zaidi zaidi juu ya maneno haya, na kukosa kufanya kazi ya lazima ya kila siku, kama **hukumu na mapendo ya Mungu.** Waliweka roho juu ya maneno watu wengine waliyoweza kuona, lakini si juu ya yale yaliyoonekana kwa Mungu tu.

**11:43** Walipenda kuwa na pahali pa kuonekana katika **masunagogi** na kukokota macho ya watu juu yao katika **soko**. Hivi walikuwa wenye kiburi vilevile.

**11:44** Mwishoni Bwana aliwasawanisha na **makaburi** yasiyoonekana. Kwa wakati wa sheria ya Musa, mtu ye yote aliyegusa kaburi alikuwa mchafu kwa siku saba (Hesabu 19:16), hata kama kwa wakati ule hakufahamu kwamba lilikuwa kaburi. **Wafarisayo** walionekana kama viongozi wazuri wa dini, lakini walikuwa **kama makaburi** yasiyoonekana yaliyojaa ubovu na uchafu, na kuchafua wengine na kiburi yao.

### O. Wana-sheria wanashitakiwa (11:45-52)

**11:45 Wana-sheria** walikuwa waandishi – mafundi ya kazi ya kueleza na

kuonyesha maana ya Sheria ya Musa. Ndiyo, waliwaambia watu wengine nini iliwapasa kufanya – bila kufanya maneno haya wao wenyewe. Mmoja wao aliumizwa na masemo makali ya Yesu, akakumbusha Bwana ya kwamba kwa njia ya kushitaki Wafarisayo alikuwa akitukana wana-sheria **vilevile.**

**11:46** Neno hili lilimpa Bwana njia kusema na ukali juu ya zambi nyingine za wana-sheria. Kwanza walitesa watu na **mizigo** namna namna ya sheria, bila kuwasaidia kubeba mizigo hii. Kama Kelly alivyosema, "Walijulikana kwa njia ya kuzarau watu wale ambao waliwaheshimu."[22] Mengi ya maagizo yao yalikuwa maagizo ya watu na yalikuwa juu ya mambo madogo.

**11:47,48** Wana-sheria walikuwa wauaji wanafiki. Walitenda kama wenye kuheshimu manabii wa Mungu, hata na kusimamisha **nguzo za ukumbusho** juu ya makaburi ya **manabii** wa Agano la Kale. Maneno haya yalionyesha ya kwamba waliwaheshimu sana, lakini Bwana Yesu alijua kwamba hawakufanya hivi na roho ya kweli. Ndiyo, matendo yao yalionyesha kwamba hawakufungana na wazazi wao Wayuda **walioua** manabii, lakini ndani ya roho zao waliwaiga. Saa ile ile walipojenga **makaburi** ya manabii, walifanya shauri kwa hila kuua Nabii mkubwa zaidi wa Mungu, Bwana Yesu mwenyewe. Na watakaa kuua manabii na mitume waaminifu wa Mungu.

**11:49** Kwa njia ya kusawanisha shairi 49 na Matayo 23:34 tunaona ya kwamba Yesu mwenyewe ni **akili ya Mungu**. Hapa kwa Luka 11 alitoa maneno ya **akili ya Mungu** kusema, **"Nitatuma manabii na mitume."** Ndani ya Matayo haonyeshi kwamba maneno haya yalitoka katika Agano la Kale au pahali po pote pengine, lakini anayanena kama masemo yake mwenyewe. (Ona vilevile 1 Kor. 1:30 pahali tunaposoma juu ya Kristo kama akili.) Bwana Yesu aliahidi kwamba **atatuma … manabii na mitume** kwa watu wa kizazi chake, na ya kwamba watu **watawatesa na kuwaua.**

**11:50,51** Atataka **toka** kizazi **kile damu** ya wanenaji wote waliosema kwa ajili ya Mungu, kuanza na mnenaji wa kwanza ambaye tunapata habari zake ndani ya Agano la Kale, ndiye **Abeli**, na hata kufika damu ya yule wa mwisho, ndiye **Zakaria**, **aliyeuawa kati ya mazabahu na nyumba ya Mungu** (2 Mam. 24:21). Ndani ya Maandiko ya Agano la Kale la Wayuda, 2 Mambo ya Siku ni kitabu cha mwisho. Hivi wakati Bwana Yesu alipotaja **Abeli** na **Zakaria,** aliwaza juu ya watumishi wote wa Mungu waliouawa, kuanza na Abeli. Na wakati aliposema maneno haya alijua vilevile ya kwamba watu wa kizazi kile watamwua yeye mwenyewe juu ya msalaba. Kitakuwa kitendo cha kuogofya kabisa, uuaji wa mwisho wa watu wote wa Mungu ambao waliua mbele. Kwa sababu watamwua yeye, **damu ya wote** waliouawa katika vizazi vya mbele itakuwa juu yao.

**11:52** Mwishoni Bwana Yesu alikemea **wana-sheria** juu ya **kuondosha ufunguo wa elimu**, maana yake kunyimia watu Neno la Mungu. Walisema waliheshimu Maandiko Matakatifu, lakini walikaa kumkataa Yule ambaye Maandiko yalitangaza habari zake. Na **walizuiza** watu wengine wasifike karibu na Kristo. Hawakumtaka wao wenyewe, na hawakutaka watu wengine kumpokea.

### P. Jibu la waandishi na Wafarisayo (11:53, 54)

Waandishi na Wafarisayo walikasirika sana juu ya mashitaki ya Bwana. **Wakaanza kumsonga kwa nguvu** na kujaribu sana kumtega ndani ya masemo yake waweze kupata njia kumhukumu hata kufa. Maneno haya yalionyesha wazi ya kwamba Bwana alijua kabisa hali ya roho zao.

## 8. NJIANI KWENDA YERUSALEMA MWANA WA WATU ALIFUNDISHA NA KUPONYESHA WATU (Sura 12-16)

### A. Maonyo na mambo ya kutia moyo (12:1-12)

**12:1 Makutano ya watu elfu nyingi** walikuwa **wamekusanyika** wakati Yesu alipokuwa akihukumu Wafarisayo na wana-sheria. Mashindano ya masemo yanakutanishaga watu wengi, lakini bila shaka watu hawa walikokotwa na mashitaki makali ya Yesu ya viongozi hawa wa dini wanafiki. Hata kama watu hawafurahii wenye kuhukumu zambi na ukali, wanakubali rohoni mwao kama masemo yale ni haki. Akigeuka kwa **wanafunzi wake,** Yesu aliwaonya, **"Angalieni chachu ya Wafarisayo."** Alieleza ya kwamba chachu ni mfano wa unafiki. Mnafiki ndiye mtu anayeonekana kwa watu namna nyingine na hali ya kweli ya roho yake. Wafarisayo walijuana sana na kufanya hivi.

**12:2,3** Siku nyingine maneno haya yote ambayo **walificha yatafunuliwa** wazi, na maneno yote waliyofanya **katika giza** yataonekana katika **nuru**.

Ndiyo, ni lazima kwa unafiki kuonekana wazi, lakini ni lazima vilevile kwa kweli kushinda. Kufika wakati ule wanafunzi walihubiri kama kwa siri, kama katika giza, na kwa makutano madogo. Lakini nyuma ya kukataliwa kwa Masiya na Israeli, na kuja kwa Roho Mtakatifu, watakwenda kuhubiri bila woga kwa jina la Bwana Yesu, na kutangaza Habari Njema pahali pote. **Itahubiriwa "juu ya dari za nyumba."** Godet alisema**, "**Wale waliosikiwa na watu wachache tu kwa wakati ule watageuka walimu wa dunia."[23]

**12:4,5** Na roho ya mapendo Bwana aliita wanafunzi wake "**rafiki zangu,**" na aliwaonya wasiwe na haya juu ya urafiki huyu mtamu, hata wakati wa mateso makali. Wafuata waaminifu wa Bwana watapata mateso na hata kufa kwa sababu ya kutangaza Habari Njema pahali po pote. Lakini kuna mpaka kwa mambo mabaya ambayo hata Wafarisayo waliweza kuwatendea. Mpaka huu ndio mauti ya mwili. Haifai waogope ile. Mungu ataazibu watesaji wao na azabu kubwa zaidi, ndiyo mauti ya milele katika **Gehena**. Hivi ilipasa wanafunzi **kuogopa** Mungu kupita watu.

**12:6,7** Kusaidia roho za wanafunzi na kuwakumbusha ya kwamba Mungu anawalinda, Bwana alisema juu ya namna Baba anavyotunza hata **ndege**. Ndani ya Matayo 10:29 tunasoma ya kwamba ndege wawili wanauzwa kwa sengi mbili. Hapa kwa Luka 12 tunasoma ya kwamba **ndege watano wanauzwa kwa sengi mbili.** Bei zao ni chini kabisa, lakini **Mungu** hasahau hata mmoja wao. Kama Mungu akilinda hata ndege hawa, kuzidi sana atawalinda wale wanaokwenda kutangaza Habari Njema ya Mwana wake! Anajua hata hesabu ya **nyole za vichwa vyao.**

**12:8** Mwokozi aliwaambia wanafunzi ya kwamba **mtu** ye yote ambaye **anamkiri** sasa, yeye mwenyewe atakiri mtu huyu mbele ya malaika za Mungu. Anasema hapa juu ya waamini wa kweli wote. Kumkiri ni kumpokea kama Bwana na Mwokozi wa pekee.

**12:9** Wale ambao wanamkana **mbele ya watu watakanwa mbele ya malaika za Mungu.** Ni kama Bwana alifikiri zaidi Wafarisayo wakati aliposema maneno haya, lakini ni kweli kwa watu wote ambao wanakataa Kristo, na walio na haya kumkiri. Siku ile atasema, "Sikukujua kamwe."

**12:10** Halafu Mwokozi alieleza kwa wanafunzi ya kwamba watu wakimlaumu yeye, neno hili ni mbali na matukano ya **Roho Mtakatifu**. Wale wanaosema maneno **mabaya juu ya**

**Mwana wa watu** wanaweza **kusamehewa** kama wakitubu na kuamini, lakini hakuna usamehe kwa **matukano ya Roho Mtakatifu**. Hii ilikuwa zambi ya Wafarisayo (ona Matayo 12:22-32). Zambi hii ni nini? Ni zambi ya kusema maajabu yote ambayo Bwana Yesu alifanya yalitendwa na Shetani. Ni matukano **juu ya Roho Mtakatifu** kwa sababu Bwana Yesu alifanya maajabu yake yote kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Ni kama walisema Roho Mtakatifu ni Shetani. Hakuna usamehe kwa zambi hii kwa wakati wa sasa au kwa wakati wa kuja.

Mwamini wa kweli hawezi kutenda zambi hii, hata kama wengine wanateswa na woga ya kwamba wameitenda kwa sababu wamerudi nyuma. Kurudi nyuma si zambi isiyoweza kusamehewa. Mwamini aliyerudi nyuma anaweza kurudishwa kwa upatano mzuri na Bwana. Woga rohoni mwake unaonyesha wazi ya kwamba *hakutenda* zambi isiyoweza kusamehewa.

Na vilevile kwa msiyeamini kukataa Kristo si zambi isiyoweza kupata usamehe. Mtu anaweza kukataa tena na tena kupokea Mwokozi, lakini labda atageuka nyuma ya wakati na kumwamini. Ndiyo, kama akikufa mbele ya kufanya hivi, hakuna usamehe tena kwa zambi yake. Lakini zambi ambayo Bwana wetu alisema hapa haiwezi kusamehewa ni zambi ya Wafarisayo wakati waliposema alifanya maajabu yake kwa uwezo wa Belzebuli, mkubwa wa pepo wachafu.

**12:11,12** Wanafunzi hawakuweza kuepuka kufikishwa mbele ya **serikali** kwa kuhukumiwa. Bwana Yesu aliwaambia ya kwamba hawakuhitaji kutayarisha mbele **maneno watakayosema. Roho Mtakatifu** atawafundisha saa ile maneno ambayo wanapaswa kusema. *Si kusema* ya kwamba watumishi wa Mungu hawahitaji kuweka saa kwa maombi na kutayarisha mafundisho mbele ya kuhubiri Habari Njema na kufundisha Neno la Mungu. Si uzuru kwa uvivu! Lakini ni ahadi toka Bwana ya kwamba wale wanaohukumiwa kwa sababu ya ushuhuda wao kwa Kristo watasaidiwa na **Roho Mtakatifu.** Na ni ahadi kwa watu wote wa Mungu ya kwamba wakitembea katika Roho watapewa maneno yanayofaa kusema kwa wakati wa hatari.

**B. Maonyo juu ya choyo (12:13-21)**

**12:13** Saa ile mtu mmoja katika makutano aliomba Bwana kukata mabishano yake na **ndugu yake** juu ya **uriti**. Hatujui kama mtu huyu alifikiri hakupewa sehemu ya uriti ambayo ilimpasa kupokea, au kwamba alitaka kupita sehemu yake.

**12:14** Bwana alimkumbusha mbio ya kwamba hakufika duniani kwa kuangalia maneno madogo namna hii. Alifika kutayarisha njia kwa watu wenye zambi wa dunia kupata wokovu. Hakukubali kuacha neno la kugawa uriti wa watu kumzuiza ndani ya kazi hii kubwa. (Na vilevile alikosa amri toka sheria kuhukumu maneno namna hii.)

**12:15** Lakini Bwana alitumika na matokeo haya kuonya wasikiaji wake juu ya uovu mmoja wa kuzuru kwa siri unaofichama ndani ya roho za watu, ndio choyo. **Choyo** kwa kupata mali nyingi ni moja ya maneno yanayosukuma watu na uwezo sana, lakini ni mbali kabisa na kusudi la Mungu kwa maisha ya mtu. **"Uzima wa mtu hauko katika wingi wa mali zake."** Mwalimu J.R. Miller alisema:

> Kristo alisema tena na tena juu ya hatari ya mali lakini watu wachache tu wanaogopa utajiri. Hawafikiri kwamba choyo ni zambi kwa wakati wa sasa. Mtu akivunja sheria la sita au la nane anahukumiwa na kuhayarishwa sana, lakini akivunja sheria ya kumi, watu wanasema yeye ni

mtu wa kuendelea vizuri katika biashara. Biblia inasema ya kwamba kupenda mali ni shina moja la mabaya yote (1 Tim. 6:10), lakini kila mtu anayetaja shairi hili anasema zaidi juu ya "mapendo," na anaeleza ya kwamba hili ndilo neno baya, si mali yenyewe.

Tukitazama watu ambao wanatuzunguka, tungeweza kufikiri kweli ya kwamba uzima wa mtu ni kweli katika wingi wa mali zake. Watu wanafikiri wanageuka wakubwa kwa kipimo wanachojipatia mali. Hili ni kosa kubwa. Mtu anapimwa kwa hali ya roho yake, si kwa hesabu ya mali yake. [24]

**12:16-18 Mfano** wa **tajiri mpumbavu** unaonyesha ya kwamba vitu na mali *si* neno la faida kubwa zaidi ya maisha yetu. Kwa sababu vyakula mashambani mwake viliota vizuri zaidi mlimaji tajiri huyu alisumbuka sana kama atafanya nini na mavuno haya yote. Gala zake zote zilijaa tele na nafaka. Basi alifanya shauri **kubomoa gala** zake na **kujenga** nyingine kubwa zaidi. Angaliweza kuponyesha mali na masumbuko haya yote kama angaliangalia kando kando yake tu na kuona elfu elfu za watu wenye hitaji, na kutumika na mavuno yake ya kuzidi kusaidia njaa yao ya mwili na ya roho. "Roho za wamasikini, nyumba za wajane, na vinywa vya watoto ni gala zisizoweza kuharibika kamwe." (Ambrose)

**12:19** Nyuma ya kujengwa kwa gala zake mpya, mlimaji tajiri alikusudi kuacha kazi. Ona roho yake ya kujitegemea mwenyewe: gala zangu, roho yangu, mavuno yangu, mali yangu. Alikuwa ametayarisha maneno yote kwa wakati wa kuja. **Atapumzika, atakula, kunywa, na kufurahi.**

**12:20,21** Lakini alianguka kabisa wakati alipowaza juu ya miaka iliyokuwa mbele yake kama saa yake, na **Mungu** alimwambia ya kwamba atakufa **usiku ule ule**. Halafu nani atapata mali yake yote? Yatageuka mali ya mtu mwingine. Mtu mmoja alisema ya kwamba mashauri ya mpumbavu yanakwisha siku ya kufa kwake. Kweli mtu huyu alikuwa mpumbavu.

**"Vitu vile … vitakuwa vya nani?" Mungu** aliuliza. Ni vizuri kwa sisi kujiuliza vilevile, "Kristo akikuja leo, vitu vyangu vyote vitageuka mali ya nani?" Kutumika navyo kwa Mungu sasa ni vizuri kupita kuviacha kwa watumishi wa Shetani kuvipata. Tunaweza kutumika navyo sana kuvimbisha hazina mbinguni na kuwa na **utajiri kwa Mungu.** Au tunaweza kuvipoteza kwa mwili wetu, na kuvuna uharibifu (Gal. 6:8).

### C. Masumbuko au imani (12:22-34)

**12:22,23** Hatari moja kubwa kwa Wakristo ni kuacha hitaji lao kwa vyakula na mavazi kuwa neno kubwa zaidi, neno la kwanza katika maisha yao. Tunaweka roho sana sana juu ya kutumika kazi kupata mali, hata kazi ya Bwana inasukumwa kwa pahali pa nyuma. Lakini Agano Jipya linafundisha ya kwamba lazima Kristo na kazi yake awe kwa pahali pa kwanza ndani ya maisha yetu, na **vyakula** na **mavazi** yanapaswa kuwa kwa pahali pa nyuma. Inatupasa kutumika kazi na nguvu kujipatia vitu tunavyohitaji kwa maisha yetu ya sasa, kisha kujitoa kabisa kwa kazi ya Mungu, na kumwamini yeye kwa mahitaji yetu kwa wakati wa kuja. Haya ndiyo maisha ya imani.

Wakati Bwana aliposema **haifai kwetu kusumbukia** vyakula na mavazi, hakufikiri ya kwamba tukae tu bure na kungoja kupewa vitu hivi. Maisha ya Wakristo *si* maisha ya uvivu. Neno ambalo anatutaka sisi kufahamu ni ya kwamba haifai kuweka saa na roho zaidi juu ya kazi ya kujipatia mali kwa mahitaji yetu. Kuna mambo ndani ya maisha ya Mkristo yaliyo makubwa kupita **vyakula** na mavazi. Sisi ni hapa kama wajumbe wa Mfalme, na kazi yetu ya

heshima sana ni kutangaza habari zake. Sharti maneno yetu wenyewe, namna tunavyokaa na namna tunavyoonekana (mavazi yetu) yawe kwa pahali pa pili.

**12:24** Yesu alisema juu ya **kunguru** kama mfano wa namna **Mungu** anavyolinda viumbe vyake. Hawasumbuki sana sana kutafuta vyakula kwa mahitaji yao wakati wa kuja. Wanaishi wakitegemea Mungu kila saa. Ndiyo, hawapandi wala **kuvuna**, lakini maana ya neno hili si kusema kwamba haifai watu kufanya kazi ya mishahara kila siku. Maana yake ndiyo hii: Mungu anajua mahitaji ya viumbe alivyoumba na atawapatia vitu vile kama wakimtegemea yeye. **Kama Mungu akikulisha kunguru**, kuzidi sana atakulisha wale ambao aliwaumba, na kuwaokoa kwa neema yake, na kuita kuwa watumishi wake. Kunguru hawana vyumba vya kuweka akiba, wala gala, lakini siku kwa siku Mungu anawapatia vitu wanavyohitaji. Basi kwa sababu gani sisi tutapoteza maisha yetu na kazi ya kujenga gala kubwa zaidi?

**12:25,26** Yesu aliuliza, **"Nani katikati yenu, kwa kusumbuka anaweza kuongeza kimo chake urefu wa mkono mmoja?"** Ulizo hili linaonyesha upumbavu wa kusumbuka juu ya maneno ambayo hatuwezi kugeuza (kama maneno yatakayotokea kwa wakati wa kuja.) (Neno hili "kimo" linaweza kutafsiriwa vilevile "urefu wa maisha yake".) Kama ni hivi, kwa nini tunasumbukia wakati wa kuja? Ni vizuri zaidi kwa sisi kutumika na saa yetu na nguvu yetu yote kwa Kristo na kumtegemea yeye kwa wakati wa kuja.

**12:27,28** Halafu Bwana alisema juu ya mahitaji ya **maua** kuonyesha upumbavu wa kutumika na zawadi nzuri zaidi tulizopewa kwa kujipatia mavazi. **Maua haya** hayafanyi kazi wala hayasokoti, lakini yana mapambo yanayopita hata **mavazi mazuri sana ya Solomono**. Kama **Mungu** akitoa mapambo namna hii kwa majani ya shamba yanayopambwa leo, na kesho yatatupwa katika tanuru ya moto, hataweka roho zaidi juu ya mahitaji ya watoto wake? Tunaonyesha **udogo wa imani yetu** wakati tunapokaa kusumbuka na kuruka hapa na kule tukijaribu kujipatia vitu vingi. Tunapoteza maisha yetu tukifanya maneno ambayo Mungu angalifanya kwa sisi kama tungalitumika na saa na zawadi zetu kwa yeye.

**12:29-31** Mahitaji yetu ya kila siku ni madogo tu. Basi kwa sababu gani tunaweka saa na nguvu nyingi kwa kazi ya kujipatia vyakula na mavazi? Na kwa nini tuna **roho ya shaka** na kusumbuka juu ya wakati wa kuja? **Mataifa ya dunia** wasiojuana na Mungu kama Baba wao wanaweka roho juu ya vyakula, mavazi, na namna gani kupendeza miili yao. Maneno haya ni makubwa sana katika maisha yao. Lakini haikuwa kamwe kusudi la Mungu kwa watoto wake kuweka saa na kusumbuka sana kujipatia vitu kupendeza miili yao. Kuna kazi anayotaka ifanywe hapa duniani, naye ameahidi kuwasaidia wale wanaojitoa kwake na roho moja. **Tukitafuta ufalme** wake, hatatuacha kamwe kuwa na njaa au watupu. Ingekuwa huzuni kubwa kufika kwa mwisho wa maisha yetu na kufahamu kwamba tumepoteza sehemu kubwa zaidi ya saa yetu tukisumbuka kupata vitu ambavyo Mungu alivyokusudi kutupatia kwa safari yetu kwenda mbinguni bila hitaji kwa sisi kusumbuka sana kuvipata!

**12:32** Wanafunzi walikuwa kama **kundi dogo** la kondoo bila askari kuwalinda, waliotumwa katika dunia hii ya uadui. Ndiyo, walikosa wenye kuwasimamia. Lakini lilikuwa kusudi la Mungu kwa vijana hawa, wasio na kitu, kuriti **ufalme** pamoja na Kristo. Kwa wakati wa nyuma watatawala pamoja naye juu ya dunia nzima. Kwa sababu hii Bwana alisema nao haifai **wasumbuke** juu ya mahitaji yao ya sasa, kwa sababu **Baba** alikuwa amewatayarishia

heshima ya utukufu mkubwa kwa wakati wa kuja.

**12:33,34** Kwa pahali pa kuvimbisha mali na kufanya mashauri kwa wakati wa sasa wanaweza kutumika na vitu hivi kwa Bwana sasa. Kwa njia hii wataweza kujitayarishia uriti mbinguni kwa milele. Hata kuchakaa kwa miili yao hakuwezi kupunguza hazina yao mbinguni, wala wizi, wala wanyanganyi. Hatari moja ya kuwa na mali ni ya kwamba inatushinda kuwa nayo bila kuitegemea! Kwa sababu hii Bwana Yesu alisema, "**Pahali munapoweka hazina yenu, pale itakapokuwa mioyo yenu.**" Tukituma mali yetu mbele, mapendo yetu kwa vitu vya dunia hii vinavyoharibika yatapunguka.

### D. Mfano wa mtumishi mwangalifu (12:35-40)

**12:35** Zaidi ya kutegemea Bwana kwa mahitaji yao ya kila siku, iliwapasa kukaa saa zote kutazamia kuja kwake. Ilipasa **viuno** vyao **kufungwa**, na **taa** zao **zikiwaka**. Kwa inchi za mashariki watu walikuwa na mkaba **kiunoni** kufunga mavazi yao marefu saa ya kutembea mbio au kukimbia. Kufungwa kwa kiuno kunatufikirisha juu ya kazi ambayo inapasa mtu huyu kufanya, na kuwaka kwa taa yake ya kwamba sharti awe na ushuhuda mwema kwa Bwana wake.

**12:36** Ilipasa wanafunzi kutazamia kurudi kwa Bwana kila dakika, kama bwana anayerudi **toka arusi.** Kelly aliandika:

> Haifai wazuizwe na vitu vya dunia, ili dakika ile ile Bwana anapopiga hodi, kama katika mfano huu, wawe tayari kumfungulia mara moja, bila kujitayarisha kwanza. Wanamngojea na hamu rohoni, wanampenda, hivi wakati anapopiga hodi wanamfungulia mlango mara moja.[25]

Habari hizi za mtu **akirudi toka ndoa** si mfano wa Karamu ya Ndoa ya Mwana-Kondoo au wa kuja kwa Bwana kupeleka waamini mbinguni. Kwa njia ya mfano huu Bwana alitaka kufundisha kweli moja tu, ndiyo ya kwamba inatupasa kutazamia kuja kwake. Kusudi lake halikuwa kuonyesha namna maneno yatakayofuatana wakati atakapokuja tena.

**12:37** Wakati mtu huyu anaporudi toka ndoa anakuta **watumishi** wake **wakimngojea** na hamu, tayari kutii maagizo yake na kumtumikia. Anapendezwa sana na roho zao nzuri hata anageuza maneno: **Yeye mwenyewe** anajifungia kitambaa cha mtumishi, ana**wa**ketisha kwa meza na ku**wa**patia vyakula vyao. Mfano huu unagusa roho yetu kabisa na kutufikirisha ya kwamba Bwana wetu aliyefikia dunia hii kama mtumwa atajinyenyekeza na kwa neema atatumikia watu wake tena siku nyingine mbinguni.

**12:38** **Zamu ya pili ya usiku** ni saa tatu kufika saa sita ya usiku. **Zamu ya tatu** ni toka saa sita kufika saa tisa ya usiku. Hata ilikuwa zamu gani wakati Bwana aliporudi, **watumishi** wake walikuwa wakingoja kufika kwake.

**12:39,40** Bwana aliendelea kusema sasa juu ya mtu aliyekuwa na **mwizi** nyumbani mwake wakati asipofikiri mwizi atafika, na asipoangalia kwa muda mfupi. Kama **mwenye nyumba angalijua** saa mwizi atakapokuja angaliangalia **asiache mwizi kuingia nyumbani mwake**. Habari hizi zinatufundisha ya kwamba hatujui saa ya kuja kwa Kristo; hakuna mtu anayejua siku na saa ya kutokea kwake. Siku ile waamini waliovimbisha hazina hapa duniani watazipoteza zote kwani, kama mtu mmoja alivyosema, "Au Mkristo ataacha mali yake au atakwenda kwa pahali mali yake ilipo." Kama tukitazamia kurudi kwa Kristo kwelikweli, tutauza vyote tulivyo navyo na kujiwekea hazina mbinguni pahali mwizi asipoweza kuziiba.

### E. Watumishi waaminifu na wasioaminifu (12:41-48)

**12:41,42** **Petro** aliuliza kama **mfano** huu wa Kristo juu ya uangalifu ulikuwa

kwa wanafunzi tu, au kwa watu wote. Bwana alijibu ya kwamba ulikuwa kwa watu wote wanaokiri kuwa wasimamishi wa Mungu. Msimamishi **mwaminifu na mwenye akili** ndiye anayewekwa juu ya nyumba ya bwana wake na kuwapa watu **posho** yao. Kazi kubwa ya msimamishi huyu ni kuangalia mahitaji ya watu, si kupenda mali na kuwa na choyo.

**12:43,44** Wakati Bwana atakapokuja na kuona msimamishi wake akiweka roho kabisa juu ya mahitaji ya roho ya wanaume na wanawake, atampa zawabu. Labda zawabu hii ni mfano wa kutawala pamoja na Kristo kwa wakati wa utawala wake wa miaka elfu moja (1 Petro 5:1-4).

**12:45** **Mtumwa huyu** anasema anatumikia Kristo, lakini kabisa kabisa yeye ni msiyeamini. Kwa pahali pa kulisha watu wa Mungu anawatendea mabaya, na anaanza kula na kunywa na kulewa (labda Bwana alifikiri juu ya Wafarisayo wakati aliposema maneno haya.)

**12:46** Kuja kwa Bwana kutafunua ya kwamba hakuwa mwamini wa kweli, na ataazibiwa **pamoja na wasioamini** wote wengine. Maneno haya **"atamkata vipande viwili"** yanaweza kufasiriwa vilevile "atampiga na nguvu sana."

**12:47, 48** Mashairi haya yana mafundisho makubwa juu ya utumishi wo wote. Mtu anayependelewa zaidi anapewa kazi kubwa zaidi. Waamini watapewa zawabu za vipimo mbalimbali mbinguni. Na wasioamini watapokea azabu ya kipimo mbalimbali katika Gehena. Ni lazima kwa watu wanaojua **mapenzi** ya Mungu yanayofunuliwa ndani ya Maandiko kuyatii vilevile. Wale waliopewa mengi, kwao mengi yatatafutiwa. Wale wasiobarikiwa hivi wataazibiwa kwa matendo yao yasiyofaa, lakini azabu yao itakuwa ndogo kupita.

### F. Matokeo ya kuja kwa kwanza kwa Kristo duniani (12:49-53)

**12:49** Bwana Yesu alijua ya kwamba kuja kwake **duniani** hakutaleta salama mara moja. Kwanza kutakuwa na matengo, magomvi, mateso, kumwangika kwa damu. Hakufika na kusudi la kutupa **moto** wa namna hii **duniani**, lakini haya yalikuwa matokeo ya kuja kwake. Ndiyo, hata kama kwa wakati wa utumishi wake duniani kulikuwa na mateso na matengo, uovu wa mioyo ya watu ulifunuliwa wazi kabisa kwa wakati wa **kusulibishwa kwa Bwana**. Alijua ya kwamba ilikuwa sharti kwa maneno haya yote kutokea, na yeye mwenyewe alikuwa tayari kwa **moto** ule wa mateso kuwaka juu yake mwenyewe kwa wakati wa kutimia.

**12:50** Alikuwa na **ubatizo kubatizwa** nao. Ulikuwa **ubatizo** wake hata kufa kwa Kalvari. Alisukumwa sana rohoni kufikia msalaba kutimiza ukombozi kwa wanadamu. Haya na maumivu na mauti yalikuwa mapenzi ya Baba kwaye, naye alitaka sana kuyatii.

**12:51-53** Alijua vizuri ya kwamba kuja kwake hakutaleta **utulivu duniani** kwa wakati ule. Hivi alionya wanafunzi ya kwamba watu wakifika kwake, watu wa jamaa zao watawatesa na kuwafukuza. Mtu mmoja wa jamaa akiamini Kristo, neno hili litatenga jamaa. Neno moja linaloonyesha uovu wa roho za watu ni ya kwamba ndugu wasioamini wangetaka mwana wao kuwa mlevi na mwasherati kupita kwa yeye kushuhudia Kristo kama mfuata wake! Kuna watu wengine wanaofundisha ya kwamba Yesu alikuja kufunganisha pamoja watu wote (wasioamini na waamini) kuwa "udugu mmoja wa watu." Masemo haya ya Yesu yanahakikisha ya kwamba mafundisho yale ni uwongo. Aliwatenga, kupita matengo yao yote ya mbele!

### G. Alama za wakati (12:54-59)

**12:54,55** Ndani ya mashairi ya mbele Bwana Yesu alisema na wanafunzi wake. Sasa Mwokozi alisema na **makutano.** Aliwakumbusha ya kwamba walijua kama mvua itanyesha au jua litawaka. Walifahamu ya kwamba wakati walipoona **wingu** kwa **upande wa mangaribi,** vizuri wajitayarishe kwa mvua. Na wakati **upepo** ulipovuma toka **kusini,** jua litakuwa kali, na mapando yatakauka mashambani. Watu walikuwa na akili, na waliweza kutambua maneno haya. Lakini zaidi ya kuwa na akili, walihitaji kuwa na kutaka kuyafahamu.

**12:56** Haikuwa hivi kwa maneno ya roho. Hata wakiwa na akili kama watu wote wengine, hawakutambua ukubwa wa **wakati** ule. Mwana wa Mungu mwenyewe alikuwa amefikia dunia hii, na alisimama katikati yao. Lakini hata kama walikuwa na akili kufahamu maneno haya, hawakutaka kuyajua, hivi walijidanganya wenyewe.

**12:57-59** Kama wangalitambua ukubwa wa saa ile, kama wangalifanya haraka kupatana na **mshitaki** wao. Ndani ya shairi 58, labda mshitaki, mtawala, mhukumu, na askari, ni wote mifano ya Mungu. Saa ile yote Mungu alikuwa akitembea katikati yao na kuwasihi na kuwapa njia kuokolewa. Iliwapasa kutubu na kumwamini. Kama wakikataa kufanya hivi itawapasa kusimama mbele ya Mungu, Mwamuzi wao. Bila shaka watahukumiwa kuwa na hatia kwa sababu ya kutokuamini kwao. Watatupwa **katika kifungo**, kuazibiwa kwa milele. Hawatatoka kule kufika wakati watakapokwisha **kulipa sengi ya mwisho,** maana hawatatoka **kamwe** kwa sababu hawataweza kulipa kamwe deni kubwa namna hii.

Hivi Yesu alikuwa akisema iliwapasa kutambua wakati ule walioishi ndani yake, na kutengeneza maneno yao na Mungu kwa njia ya kutubu zambi zao na kujitoa kwake mzima.

### H. Ukubwa wa toba (13:1-5)

**13:1-3** Kwa mwisho wa sura 12 taifa la Wayuda hawakutambua vizuri wakati ule walipoishi. Ndani ya sura 13 Bwana Yesu aliendelea na maonyo watubu mbio wasipotee kwa milele. Alisema zaidi kwa taifa la Israeli, lakini mafundisho haya ni kwa mtu mmoja mmoja vilevile. Ndani ya mashairi yanayofuata aliandika juu ya misiba mikubwa miwili iliyokuwa imetokea. Msiba wa kwanza ulikuwa uuaji wa **Wagalilaya** waliokuwa wamefikia Yerusalema kuabudu. **Pilato**, liwali la Yudea, aliagiza wauawe wakati walipokuwa wakitoa zabihu. Hakuna habari nyingine juu ya tukio hili baya mno. Labda Wayuda katika Yerusalema walizani **Wagalilaya hawa** walikuwa wametenda zambi mbaya sana, na ya kwamba mauti yao ilikuwa alama kwamba Mungu hakupendezwa nao hata kidogo. Lakini Yesu alionyesha kwamba mawazo yao hayakuwa sawa na alionya Wayuda kama **wasipotubu,** wao wote **wataangamia sawasawa nao.**

**13:4,5** Msiba wa pili ulitokea **wakati mnara wa Siloamu** ulipoanguka na kuua watu kumi na wanane. Hakuna habari nyingine juu ya tukio baya hili. Bwana alionyesha ya kwamba msiba huu haukuwa hukumu kwa zambi kubwa fulani lakini ulikuwa onyo kwa taifa zima la Israeli ya kwamba wasipotubu, hukumu kubwa namna hii itawapata wote. Neno hili lilitokea kweli katika 70 A.D. wakati Tito alipoingia Yerusalema.

### I. Mfano wa mtini usiozaa (13:6-9)

Bwana Yesu aliendelea kuwaambia **mfano** wa mtini. **Mtini** huu ni mfano wa Israeli **waliopandwa** ndani ya **shamba la mizabibu** la Mungu, ndilo dunia. Mungu alitafuta **matunda** juu ya mti huu lakini **hakupata** kitu. Hivi alisema na mlimaji wa shamba (mfano wa Bwana Yesu) ya kwamba **kwa miaka mitatu** alitafuta **matunda** juu ya mti huu bila kupata kitu. Labda miaka mitatu hii ni mfano wa

miaka mitatu ya utumishi wa Bwana wetu katikati ya watu. Mtini ulipewa saa ya kutosha kwa kuzaa matunda. Kama matunda yasipoonekana nyuma ya miaka mitatu, hautakuwa na matunda kamwe. Kwa sababu ya ukosefu wa matunda Mungu aliagiza **ukatwe** ili **udongo** uweze kutumiwa kwa mapando mengine. Mlimaji aliombea mtini uachwe kwa mwaka mmoja mwingine mbele ya kukatwa. Kama matunda yakikosa nyuma ya mwaka ule mwingine, aliweza **kuukata**. Hili ndilo neno lililotokea. Kwa mwaka wa ine Israeli walikataa na kusulibisha Bwana Yesu. Kwa sababu hii mji wao mkubwa uliharibiwa na watu walisambazwa.

G.H. Lang alieleza maneno haya hivi:

> Mwana wa Mungu alijua mawazo ya Baba yake, ndiye mwenye shamba la mzabibu na ya kwamba alikuwa ametoa agizo hili la kuogopesha: "ukatwe." Uvumilivu wake kwa Israeli ulikwisha. Hakuna taifa wala mtu hata mmoja anayestahili kulindwa na Mungu kama wasipozaa matunda ya haki kwa utukufu na sifa ya Mungu. Mtu anaishi kusudi aheshimu na kupendeza Mwumba wake; wakati asipofanya hivi, kwa nini basi hataondoshwa kwa pahali pake pa mapendeleo kwa njia ya mauti?" [26]

### J. Kuponyeshwa kwa mwanamke aliyeinama (13:10-17)

**13:10-13** Masemo ya mkubwa wa sunagogi yalionyesha namna Waisraeli walivyofikiri juu ya Bwana Yesu. Kwa **miaka 18 mwanamke** huyu aliteswa kwa sababu ya kupindamana sana kwa mfupa wa mgongo wake, na **hakuweza kujinyanyua** hata kidogo. Hakuomba Bwana kumponyesha, lakini **Bwana Yesu** akimwona alisema maneno ya kumponyesha, akaweka mikono yake juu yake na kunyolosha mgongo wake.

**13:14** **Mkubwa wa sunagogi** alisema na watu na hasira kwamba iliwapasa kufika kuponyeshwa **siku sita** za kwanza za juma, lakini si siku ya saba. Ndiyo, alikuwa kiongozi cha watu kwa maneno ya dini, lakini hakuweka roho juu ya mahitaji ya watu. Hata wakifika siku sita za kwanza za juma mkubwa huyu asingaliweza kuwasaidia. Aliweka roho juu ya kutimiza maagizo madogo yote ya dini, lakini hakuwa na mapendo na huruma. Kama mgongo wake ungalipindamana namna ya ule wa mwanamke huyu kwa miaka 18, asingaliweka roho kama angaliponyeshwa siku gani ya juma!

**13:15,16** **Bwana Yesu** alihamakia unafiki wake na ule wa viongozi wengine. Aliwakumbusha ya kwamba hawakusita **kufungua ngombe au punda toka pahali pake siku ya sabato** na kumpeleka kunyweshwa. Kama wakiwa na huruma namna hii kwa **nyama** tu siku ya sabato, ilikuwa vibaya kwa Yesu kufanya kazi ya kuponyesha **mwanamke huyu** aliyekuwa **binti ya Abrahamu**? Maneno haya "binti ya Abrahamu" yanaonyesha kwamba hakuwa Myuda tu, lakini alikuwa mwenye imani ya kweli vilevile. Kupindamana kwa mgongo wake ilikuwa kazi ya **Shetani**. Tunajua kwa njia ya mashairi mengine ndani ya Biblia ya kwamba magonjwa mengine yanaletwa na Shetani. Vivimba vya Yobu vililetwa na Shetani. Mwiba wa Paulo mwilini mwake ulikuwa mjumbe wa Shetani kumtesa. Lakini Shetani hawezi kufanya hivi kwa mwamini bila ruhusa ya Mungu. Na Mungu anageuza ugonjwa au mateso namna hii kuwa kwa utukufu wake mwenyewe.

**13:17** Watetaji wa Bwana Yesu **walihayarishwa** kabisa na masemo yake, lakini makutano yote **walifurahi** sana kwa sababu walifahamu Bwana alikuwa amefanya **ajabu kubwa.**

### K. Mifano ya Ufalme (13:18-21)

**13:18,19** Nyuma ya kuona ajabu huu kubwa sana, watu wangaliweza ku-

fikiri ufalme utasimamishwa mara moja. Kwa njia ya mifano miwili Bwana Yesu aliwaonyesha kwamba mawazo yao hayakuwa sawa. Mifano hii miwili ya **ufalme wa Mungu** inaonyesha namna ufalme utakavyokuwa katika muda nyuma ya kukataliwa kwa Kristo, na mbele ya kurudi kwake duniani kutawala. Inaonyesha kukua kwa Ukristo, ndio watu wanaokiri Kristo kwa kinywa tu, na wengine walio waamini wa kweli (ona mafundisho juu ya 8:1-3).

Kwanza alisawanisha **ufalme wa Mungu** na punza ya haradali, moja ya mbegu ndogo zaidi. Wakati inapotupwa ndani ya udongo inaota kuwa kijiti, si mti. Hivi wakati Yesu aliposema inageuka mti mkubwa alionyesha ya kwamba kukua kwake hakukuwa cha kawaida. Ukubwa wa mti huu ulitosha kwa **ndege** kukaa ndani ya matawi yake. Maneno haya yanatufikirisha ya kwamba Ukristo ulikuwa mdogo tu kwa mwanzo wake, mdogo kama punza ya haradali. Lakini ulipata nguvu na kuenea katikati ya watu wengi kuwa namna tunaujua wakati wa sasa. Ndani yake kuna watu wote wanaokiri kufuata Bwana, hata wale wasiozaliwa tena kweli. **Ndege za hewa** ndio tai. Ni mifano ya uovu, na inaonyesha ya kwamba hata uovu namna namna umepata pahali pa kukaa katika Ukristo.

**13:20,21** Mfano wa pili unasawanisha **ufalme wa Mungu na chachu** ambayo **mwanamke** aliweka **ndani ya vipimo vitatu vya unga.** Tunafikiri ya kwamba chachu ni mfano wa uovu kila mara ndani ya Maandiko. Maneno haya yanatuleta kufikiri ya kwamba mafundisho ya uwongo yamechanganywa na chakula safi cha watu wa Mungu na kuenea katikati yao kwa siri.

### L. Mlango mwembamba kuingia Ufalme (13:22-30)

**13:22,23** Wakati Yesu **aliposafiri kwenda Yerusalema** mtu mmoja alimwuliza kama watu **wachache** tu **wataokolewa**. Labda mtu huyu alikuwa akifazaika kweli juu ya neno hili.

**13:24** Bwana Yesu alimjibu na agizo wazi. Alisema na mwenye kuuliza lazima aangalie kabisa yeye mwenyewe **aingie kwa mlango mwembamba**. Wakati Yesu aliposema **"Fanyeni nguvu kuingia katika mlango mwembamba,"** hakutaka kusema ya kwamba kwa kupata wokovu inatupasa kusumbuka sana. **Mlango mwembamba** hapa unasema juu ya kuzaliwa tena – watu wanaokolewa kwa neema tu kwa njia ya imani. Yesu alikuwa akionya mtu huyu aangalie sana kuingia kwa mlango huu. **"Watu wengi watatafuta kuingia, nao hawataweza"** wakati mlango utakapofungwa. Maana yake si ya kwamba watajaribu kuingia kwa njia ya kuzaliwa tena, lakini ya kwamba kwa wakati wa uwezo na utukufu wa Kristo, watataka kuingia ufalme wake, lakini saa ya kufanya hivi itakuwa imepita. Wakati wa neema, ndio wakati wa sasa, utakuwa umepita.

**13:25-27 Mwenye nyumba** atasimama na **kufunga mlango.** Tunaona hapa mfano wa taifa la Wayuda wakipiga **mlango** na kuomba Bwana **kuwafungulia.** Atakataa kufanya hivi akisema kwamba hawajui. Watabisha jibu hili wakisema walikuwa wamekaa karibu naye. Lakini masemo yao hayatamsukuma kugeuka. Walikuwa **wenye kutenda uzalimu**, na hawatapewa ruhusa kuingia.

**13:28-30** Kukataa kwa mwenye nyumba kufungua mlango **kutaleta watu kulia na kusaga meno**. **Kulia** kunaonyesha majuto na toba, na **kusaga meno** kunaonyesha ya kwamba watu wale wanachukia Mungu sana sana. Maneno haya yanaonyesha ya kwamba mateso ambayo watu watapata katika Gehena hayatageuza roho zao. Waisraeli wasioamini **wataona Abrahamu na Isaka na Yakobo na manabii wote katika ufalme wa Mungu.** Watu hawa walifikiri watakuwa pale vilevile kwa sababu wa-

likuwa wa jamaa ya Abrahamu, Isaka na Yakobo, lakini **watatupwa inje.** Mataifa watasafiri kwa ufalme wa Kristo toka pande zote za dunia na kufurahi na kubarikiwa. Mungu alikusudi kubariki Wayuda kwanza, lakini wengi wao watakataliwa, na Mataifa ambao waliwahesabu kama imbwa watafurahi na kubarikiwa kwa wakati wa utawala wa Kristo kwa miaka elfu moja.

### M. Manabii wanauawa katika Yerusalema (13:31-35)

**13:31** Ni kama kwa wakati ule Bwana Yesu alikuwa katika sehemu ya inchi iliyotawaliwa na Herode. **Wafarisayo wengine** walifika karibu naye na kumsukuma **kuondoka** pale kwa sababu **Herode** alijaribu **kumwua**. Haikuwa desturi ya Wafarisayo kusumbukia usitawi na salama ya Yesu. Labda walikuwa wakishiriki ndani ya shauri la Herode kuogopesha Yesu aende Yerusalema, pahali bila shaka atakapofungwa.

**13:32** Masemo yao hayakuweza kuogopesha Bwana wetu. Alitambua kwamba lilikuwa shauri la Herode, akasema na Wafarisayo **warudi** na habari karibu na **yule mbweha.** Watu wengine wanafikiri haikufaa kwa Bwana Yesu kuita Herode mbweha. Wanafikiri akifanya hivi aliasi agizo la Maandiko pahali tunapokatazwa kusema maneno mabaya juu ya mtawala wa watu (Kutoka 22:28). Lakini maneno Bwana Yesu aliyosema hayakuwa mabaya; yalikuwa kweli kabisa. Ndani ya habari zake kwa Herode alisema kwamba alikuwa na kazi kufanya kwa muda mfupi. **Atafukuza pepo wachafu na kufanya kazi ya kuponyesha watu** kwa siku chache ambazo zilibaki. Halafu **siku ya tatu**, maana yake, siku ya mwisho, atakuwa amemaliza kazi yake hapa duniani. Hakuna neno ambalo litamzuiza asifanye kazi yake. Hakuna uwezo wa dunia ambao uliweza kumzuru mbele ya wakati wa kutimia.

**13:33** Na vilevile haikuwezekana kwaye kuuawa katika Galilaya. Zaidi ya watumishi wa Mungu Mjuu sana, wale ambao waliosema kwa ajili yake, waliuawa katika **Yerusalema**. Hii ndiyo maana ya semo la Bwana Yesu **"kwani haliwezekani nabii kuangamia inje ya Yerusalema."**

**13:34,35** Nyuma ya kusema maneno haya ya kweli juu ya mji huu mwovu, aligeuka na huruma kubwa na kuutolea machozi na uchungu. Alipenda mji huu sana, mji huu **ulioua manabii** na **kupiga kwa mawe** wale waliotumwa kwake. **Tena na tena alitaka kukusanya** watu wa mji huu namna **kuku anavyokusanya watoto wake chini ya mabawa yake … , lakini hawakutaka.** Walikuwa wakaidi sana. Kwa sababu hii mji wao, hekalu lao, na inchi yao **zitaachwa ukiwa.** Watakaa katika inchi nyingine kwa miaka mingi. Ndiyo, **hawataona** Bwana kufika wakati wanapogeuza mawazo yao juu yake. Shairi 35b ni juu ya kuja kwa pili kwa Kristo. Baki la taifa la Israeli watatubu kwa **wakati** ule na watasema, **"Amebarikiwa yeye anayekuja kwa jina la Bwana." (Zab. 118:26).** Halafu watu wake watakuwa tayari kwa wakati wa uwezo wake.

### N. Kuponyeshwa kwa mwenye ugonjwa wa tumbo la maji (14:1-6)

**14:1-3** Siku ya **sabato** mkubwa wa **Wafarisayo** aliita Bwana kufikia nyumba yake kula chakula. Hakufanya hivi kwa sababu ya ukarimu wa kweli, lakini kwa kujaribu kwa ajili ya viongozi vya dini kupata njia kuhukumu Mwana wa Mungu. Yesu aliona **mtu mmoja** pale aliyeteswa na **tumbo la maji**, maana maji yalibaki mengi sana mwilini mwake. Yesu alijua mawazo ya washitaki wake, akawuliza na ukali kama ni **halali kuponyesha watu siku ya sabato.**

**14:4-6** Wangalipenda sana kusema kwamba si halali kufanya hivi, lakini walikosa njia kuhakikisha mawazo yao, **hivi**

**walinyamaza.** Hivi Bwana **aliponyesha** mtu huyu, **akamruhusu kwenda zake**. Kwa macho ya Yesu kuponyesha mtu huyu ilikuwa kazi ya rehema, na Mungu wa mapendo haachi kamwe kufanya kazi za rehema, hata siku ya sabato! (Yn. 5:17). Halafu aligeuka na kusema na Wayuda. Aliwakumbusha ya kwamba nyama ya mmoja wao akianguka **ndani ya shimo**, bila shaka **watamwondosha** kule **hata siku ya sabato.** Ingekuwa faida kwao kufanya hivi. Lakini walikosa huruma kwa mtu huyu aliyeteswa, na wangependa kuhukumu Bwana Yesu kwa sababu alimsaidia. Lakini **hawakubisha mawazo ya Bwana** na bila shaka walimkasirikia hata kupita.

### O. Mfano wa mgeni mwenye kutamani ukubwa (14:7-11)

Wakati Bwana Yesu alipoingia nyumba ya Mfarisayo, labda alikuwa ameona wageni wakijitafutia **viti vya mbele** karibu na meza, ndipo pahali pa heshima zaidi. Yeye alikuwa mgeni vilevile, lakini neno hili halikumzuiza asiseme mawazo yake wazi. Aliwaonya wasijitafutie ukubwa. **Wakati walipoitwa** kula chakula nyumbani mwa mtu iliwapasa kukamata **pahali** pa chini zaidi, si pahali pa juu zaidi. Labda wakati tunapojitafutia pahali pa heshima, tutapata haya nyuma, saa mwenye nyumba anapotuomba kukamata pahali pa chini kidogo. Tukiwa na unyenyekevu wa kweli mbele ya Mungu haitawezekana kwa sisi kushushwa kupita, lakini **kupandishwa** juu tu. Bwana Yesu alifundisha ya kwamba ni vizuri kupandishwa kwa pahali pa juu, na ya kwamba haifai tujikamatie pahali pa juu sisi wenyewe. Yeye mwenyewe alikuwa mfano mzuri sana wa mwenye kujishusha (Flp. 2:5-8). Alijinyenyekeza na Mungu alimtukuza. **Mtu ye yote ambaye anajitukuza atanyenyekezwa** na Mungu.

### P. Namna ya wageni wanaoheshimiwa na Mungu (14:12-14)

Bila shaka mkubwa wa Wafarisayo alita wenye heshima waliokaa karibu na nyumba yake. Yesu aliona neno hili mara moja. Aliona ya kwamba watu wa chini hawakuitwa. Halafu alifundisha kweli kubwa moja ya ukristo – ya kwamba inatupasa kuwapenda wale wasio wa kupendeza, na wasioweza kuturudishia mema. Ni desturi ya watu kuita kwa chakula **ndugu** na **rafiki** zao na **jirani** zao **wenye mali**, wakitaraji kwamba wao watawaita tena. Hata wasioamini wanafanya hivi. Lakini tunahitaji uzima wa Mungu rohoni kutenda mema kwa **wamasikini, vilema na viwete na vipofu**. Mungu ana zawabu kubwa kwa wale wanaotendea watu wa namna hii mema. Hata wageni hawa **hawawezi kuturudishia mem**a, Mungu mwenyewe anaahidi kutulipa wakati wa **ufufuko wa wenye haki.** Ufufuko huu unaitwa ufufuko wa kwanza ndani ya Maandiko Matakatifu. Ni ufufuko wa waamini wote wa kweli wakati Kristo atakapokuja kuwapeleka mbinguni, na tunafikiri kwa mwisho wa muda wa Mateso Makubwa vilevile. Maana ufufuko wa kwanza si neno linalotokea siku moja tu, lakini unatokea sehemu sehemu kwa wakati mbalimbali.

### Q. Mfano wa wenye kutoa uzuru (14:15-24)

**14:15-18 Mmoja wa** wageni waliokuwa pale kwa chakula pamoja na Yesu alisema ingalikuwa vizuri sana kuweza kushiriki ndani ya baraka za **ufalme wa Mungu.** Labda maneno ambayo Bwana Yesu alifundisha sasa tu yaligusa roho yake. Au labda hakuwaza zaidi juu ya maneno aliyosema. Bwana Yesu alimjibu ya kwamba hata ingekuwa vizuri sana **kula mkate katika ufalme wa Mungu**, ni huzuni kwa sababu wengi wa watu wanaoitwa wanakataa kuja, wakitoa uzuru namna namna. Alisawa-

nisha Mungu na **mtu mmoja aliyetayarisha karamu kubwa na kuita watu wengi.** Wakati chakula kilipokuwa tayari alituma **mtumishi wake** kujulisha wale walioitwa kwamba **vyote ni tayari.** Neno hili linatukumbusha habari hizi kubwa ya kwamba Bwana Yesu amemaliza kwa Kalvari kazi iliyohitajiwa kwa wokovu wa watu, na sasa Habari Njema inatangazwa kujulisha watu kwamba kazi hii kubwa ilitimizwa. Mtu mmoja aliyeitwa kwa karamu alitoa uzuru kusema alikuwa **amenunua** shamba na alitaka **kwenda kuliona.** Lakini ni desturi kwenda kutazama shamba mbele ya kulinunua. Basi aliweka mapendo kwa vitu vya dunia mbele ya mwito wa neema.

**14:19,20** Mtu mwingine alikuwa amenunua **ngombe jozi tano** na alikuwa **akikwenda kuwajaribu**. Yeye ni mfano wa watu wanaoweka kazi ya biashara mbele ya mwito wa Mungu. Mtu wa tatu alisema **alioa mke**, hivi hakuweza **kuja.** Mara nyingi jamaa na rafiki wanazuiza watu wasipokee Habari Njema.

**14:21-23** Wakati **mtumwa yule** alipojulisha **bwana wake** ya kwamba zaidi ya watu walikataa kufikia karamu, **bwana** wake alimtuma mjini upesi na kuita **masikini, na vilema, na viwete, na vipofu**. Labda wale walioitwa kwanza walikuwa mfano wa viongozi vya Wayuda. Wakati walipokataa Habari Njema, Mungu aliituma kwa watu wengine **wa mji** wa Yerusalema. Wengi wao walikuja, lakini hata hivi **nafasi ilikuwa** nyumbani mwa bwana. Halafu Bwana aliagiza mtumwa **kwenda katika barabara** na kando kando **kushurutisha** watu **kuingia.** Bila shaka huu ni mfano wa Habari Njema ikihubiriwa kwa watu wa Mataifa. Haikufaa kuwasukuma na nguvu, lakini kuwakokota na mapendo kusudi **nyumba** ya bwana ipate **kujaa.**

**14:24** Lakini wale **walioitwa** kwa karamu **kwanza** walikataa kuja.

### R. Bei ya kuwa mfuata wa kweli (14:25-35)

**14:25 Watu wengi sana** walikuwa wakifuata Bwana Yesu kwa wakati huu. Viongozi wengi wangalifurahi sana kama wangalikuwa na wafuata wengi namna hii. Lakini Bwana hakutafuta watu ambao watamfuata kwa uchunguzi tu, lakini wale waliokuwa tayari kuishi na kumfuata na roho yote, na kuwa tayari hata kufa kwa ajili yake kama ikihitajiwa. Hivi alianza kupepeta makutano kwa njia ya kuwajulisha mambo ya nguvu na ya kushurutisha utii yaliyo lazima kwa mwanafunzi wa kweli, mambo wasiyoweza kuepuka.

**14:26** Kwanza aliwaambia wale waliotaka kumfuata, kama wakitaka kuwa wanafunzi wa kweli lazima wampende yeye kupita watu na vitu vyote. Hakusema kamwe ya kwamba inapasa watu kuchukia **baba, mama, mke, watoto, ndugu na ndugu wake**. Sivyo. Lakini alisema na nguvu lazima mapendo yao kwa Kristo yawe makubwa sana sana, hata mapendo yao kwa maneno yote mengine yatakuwa kama kuchukia wakati yanapo*sawanishwa* nayo (ona Mt. 10:37). Haifai kamwe mapendo kwa watu wa jamaa yao kuwazuiza wasitii Bwana kabisa katika maneno yote pia.

Neno lililo nguvu zaidi kwa yule anayetaka kuwa mfuata wa kweli wa Bwana katika maneno yote ndilo hili: **"hata uzima wake pia."** Haitoshi tu kwa mapendo kwa ndugu zetu kupunguka; sharti **tuchukie uzima wetu mwenyewe vilevile**! Kwa pahali pa kuishi kwa sisi wenyewe inatupasa kuishi kwa Kristo. Inatupasa kujiuliza juu ya kila tendo kama ni kwa faida yetu au kama litatukuza Kristo. Kwa pahali pa kuweka roho juu ya kukaa vizuri na bila hatari sisi wenyewe, sharti tuweke

roho kwanza juu ya kazi kubwa ya kutukuza Kristo na kueneza habari zake. Masemo ya Mwokozi ni yenye amri zote. Alisema wazi sana kama tusipompenda yeye kupita yote, kupita jamaa na kupita uzima wetu wenyewe, **hatuwezi** kuwa wanafunzi wake.

**14:27** Neno la pili alilofundisha ndilo hili: Inapasa mwanafunzi wa kweli **kuchukua msalaba wake mwenyewe na** kumfuata. Msalaba huu *si* maumivu ya mwili au ya roho, lakini ni maisha ya pekee, laumu, mateso, na hata mauti ambayo mtu anachagua yeye mwenyewe kwa ajili ya Kristo. Si waamini wote **wanaochukua msalaba.** Inawezekana kuuepuka na kuishi kama Mkristo. Lakini kama tukikusudi kujitoa mzima kwa Kristo tutakutana na uadui ambao Mwana wa Mungu alijuana nao wakati alipokuwa duniani. *Huu ndio msalaba*. Sharti mwanafunzi **afuate** Kristo. Maana yake aishi namna ya maisha Kristo aliyoishi wakati alipokuwa duniani – maisha ya kujikana mwenyewe, ya aibu, mateso, laumu, majaribu na mabishano na wenye zambi juu yake.

**14:28-30** Halafu Bwana Yesu alitumia mifano miwili kuonyesha kwamba inapasa mwamini kufahamu **bei** ya kumfuata, na kuchagua kama yeye ni tayari kulipa bei yenyewe. Alisawanisha maisha ya Mkristo na kujenga nyumba, na kupiga vita. Mtu **akikusudi kujenga mnara** anaangalia kwanza kama akiwa na **mali ya kutosha kumaliza** kazi yenyewe. Hataanza kujenga kama akikosa mali ya kutosha. Kama akiwa na mali ya kutosha kwa **msingi tu** wenye kutazama **wataanza kumzihaki wakisema, "Mtu huyu alianza kujenga na hakuweza kumaliza."** Ni vivyo hivyo na wanafunzi. Inawapasa kufahamu bei ya kutoa maisha yao mazima kuishi kwa Kristo tu. Kama wasipofanya hivi labda wataanza kufuata vizuri sana, lakini nyuma kidogo roho zao zitapoa na wenye kutazama watawacheka kwa sababu walianza vizuri lakini waliacha kufuata na kutukuza Bwana na roho moja. Watu wa dunia wanazarau kabisa Wakristo wanaokosa bidii ya kweli.

**14:31,32** Ni lazima kwa **mfalme anayekwenda kupiga vita** na adui aliye na jeshi kubwa kupita jeshi lake, kufikiri kwanza na kufahamu kama kweli jeshi lake dogo litaweza kushinda adui. Anafahamu vizuri ya kwamba sharti wapige vita na roho na nguvu yote au watashindwa kabisa. Ni vivyo hivyo na maisha ya Mkristo wa kweli. Hakuna njia kufuata nusu nusu tu.

**14:33** Labda hili ni shairi katika Biblia nzima **lisilopendwa** na watu wengi zaidi. Linasema waziwazi: **"Kila mmoja wenu, asipoacha vitu vyake vyote, hawezi kuwa mwanafunzi wangu."** Hakuna njia kuepuka maana ya maneno haya. Hayasemi kwamba inapasa kuwa na *roho tayari* kuacha vyote. Yanasema *lazima* aache vyote. Bwana Yesu alijua vizuri maana ya maneno aliyosema. Alijua ya kwamba hakuna njia nyingine kutimiza kazi ile kubwa ya kutangaza Habari Njema duniani pote. Anataka wanaume na wanawake ambao wanamheshimu kupita yote duniani. Ryle aliandika:

> Mtu anayepata faida kubwa zaidi ndiye anayeacha vyote kwa ajili ya Kristo. Anabeba msalaba kwa miaka michache hapa duniani, na kwa wakati wa kuja ana uzima wa milele. Hazina aliyo nayo sasa ni nzuri zaidi, na anaibeba pamoja naye ngambo ya kaburi. Yeye ni tajiri katika neema sasa, naye ni tajiri kwa utukufu kwa wakati wa kuja. Na neno lililo zuri zaidi ndilo hili: Hatapoteza kamwe yote anayopata kwa njia ya imani katika Kristo. Hayataondoshwa kamwe (Luka 10:42).[27]

**14:34,35** **Chumvi** ni mfano wa mwanafunzi. Ni vizuri kuona mtu akiishi na roho yote kwa Bwana. Lakini

sasa tunasoma juu ya **chumvi inayo-haribika.** Kwa wakati wa sasa chumvi ambayo tunatumika nayo saa ya kupika chakula haiwezi kupoteza utamu wake kwa sababu ni chumvi safi isiyo-changanywa na vitu vingine, lakini kwa wakati Biblia ilipoandikwa, mara nyingi chumvi ilichanganywa na uchafu na takataka. Hivi iliwezekana kwa chumvi kupotea na kuacha baki ndani ya sahani lisilo na faida tena. Halikuwa na faida hata kwa kutia udongo mbolea, na lili-tupwa tu.

Ni mfano wa mwanafunzi aliyeanza vizuri kufuata Bwana lakini anayerudi nyuma na kuvunja ahadi yake kumfuata na roho yote. Mwanafunzi ni hapa duni-ani kwa kusudi moja tu; ni huzuni ku-mwona akikosa kutimiza kusudi hili. Tunasoma juu ya chumvi ya kwamba **"watu wanaitupa."** *Hatusomi* ya kwa-mba *Mungu* anaitupa; neno hili hali-wezekani kamwe. Lakini **watu wana-itupa**, maana yake wanakanyaga ushu-huda wa mtu aliyeanza kujenga na asiyeweza kumaliza kazi yenyewe. Kelly aliandika:

> Hapa tunaona hatari ya neno lili-loanza vizuri na kwisha vibaya. Kitu gani katika dunia pia kinachokosa faida kama chumvi iliyopoteza utamu wake, ndilo faida yake ya pekee? Haina faida kwa kazi yo yote nyingine. Ni vivyo hivyo na mwana-funzi anayeacha kuwa mwanafunzi wa Kristo. Amepokea nusu ya nuru ya Neno la Mungu na nuru hii ina-mzuiza asifungane na ubatili na zambi za dunia tena, lakini hafurahii neema na kweli ya Mungu kumlinda kufuata njia ya Kristo.. Chumvi ina-yokosa utamu inageuka kitu cha zarau na hukumu.[28]

Bwana Yesu alimaliza mafundisho yake juu ya kuwa mwanafunzi wa kweli na maneno haya: **"Yeye mwenye ma-sikio ya kusikia asikie!"** Maneno haya yanaonyesha ya kwamba si kila mtu atakayesikia mafundisho haya magumu juu ya kuwa mwanafunzi wa kweli. Lakini kama mtu ni tayari kufuata Bwana Yesu, hata bei ya kufanya ni kubwa sana, ingempasa kusikia na ku-fuata.

John Calvin, ndiye Mkristo wa kuju-likana wa zamani, alisema, "Niliacha yote kwa Kristo, na nilipata nini? Nili-pata yote ndani ya Kristo."

### S. Mfano wa kondoo aliyepotea (15:1-7)

**15:1, 2** Ni kama mafundisho ya Bwana wetu ndani ya sura 14 yalikokota kwake watoza kodi waliozarauliwa na watu, na watu wengine wenye zambi za kujulikana. Hata kama Yesu alihamakia zambi zao, wengi wao walikubali kwamba alisema kweli. Walisimama upande wa Kristo, si upande wao we-nyewe. Na roho ya toba ya kweli wa-likiri kwamba yeye ndiye Bwana. Pahali po pote watu walipokuwa tayari kukiri zambi zao, Bwana aliwafikia na ku-saidia roho zao na kuwabariki.

**Wafarisayo na waandishi** hawaku-furahi hata kidogo juu ya Yesu akifanya urafiki na watu waliojikiri kuwa **wenye zambi**. Hawakuwa na neema kwa watu namna hii ambao walihesabu kama wakoma kwa maneno ya roho, na hawakufurahi kwa Bwana Yesu kuwa nayo. Hivi walimshitaki, **"Mtu huyu anakaribisha wenye zambi na kula pamoja nao."** Lilikuwa shitaki la kweli, wakizani alikuwa akifanya neno lisilofaa, lakini kabisa kabisa hili lilikuwa kusudi kwa sababu yake Yesu kufika duniani!

Kwa kujibu shitaki lao Bwana Yesu alipasha mifano ya kondoo aliyepotea, pata (sarafu) iliyopotea, na mwana mpotevu. Alifikiri zaidi juu ya wa-andishi na Wafarisayo wakati alipopasha mifano hii, kwani hawakukubali kamwe ya kwamba wao ni wapotevu mbele ya Mungu. Ndiyo, walikuwa wapotevu ki-

pimo kimoja na watoza kodi na wenye zambi, lakini hawakukubali neno hili. Mifano hii mitatu inaonyesha wazi ya kwamba Mungu anafurahi sana wakati anapoona wenye zambi wanaokiri zambi zao na kutubu, lakini hapati furaha hata nusu kwa njia ya wanafiki wanaofikiri wao ni wenye haki kabisa, na walio wenye kiburi hata inawashinda kukubali hali yao mbaya.

**15:3,4** Hapa mchungaji ni mfano wa Bwana Yesu. Kondoo **makumi tisa na tisa** ni mfano wa waandishi na Wafarisayo. Kondoo **mpotevu** ni mfano wa mtoza kodi au mwenye zambi anayekiri zambi zake. Wakati mchungaji anapofahamu kwamba **mmoja** wa kondoo zake **amepotea,** anaacha wale **makumi tisa na tisa jangwani** (si ndani ya luba) na anakwenda **kutafuta** yule mmoja aliyepotea **kufika wakati anapompata**. Kwa Bwana Yesu hii ilikuwa safari yake kufika duniani, miaka aliyoshinda akihubiri na kufundisha, kukataliwa kwake, maumivu yake, na mauti. Sisi watu hatutajua kamwe mambo magumu yote Bwana Yesu aliyovumilia mbele ya kupata kondoo yule mpotevu.

**15:5** Wakati **alipopata kondoo alimweka juu ya mabega yake** na kumfikisha kwa nyumba yake. Ni kama sasa kondoo huyu alikuwa amefikishwa pahali pa baraka na upatano wa karibu na Bwana asipojua mbele wakati alipokuwa pamoja na kondoo wengine.

**15:6** Halafu mchungaji aliita **rafiki** na **jirani** zake **kufurahi pamoja naye** juu ya wokovu wa **kondoo** mpotevu. Ni mfano wa furaha ya Mwokozi wakati mwenye zambi anapotubu.

**15:7** Mafundisho haya ni wazi kabisa: **Kuna furaha mbinguni juu ya mwenye zambi mmoja anayetubu**, lakini hakuna furaha juu ya wenye zambi makumi tisa na tisa wasiokubali kamwe kwamba wao ni wapotevu. Shairi 7 halifundishi ya kwamba kuna watu wengine wasiohitaji kutubu. Watu wote ni wenye zambi, na inawapasa wote kutubu kwa kupata wokovu. Shairi hili linasema juu ya wale **wanaofikiri hawahitaji kutubu.**

### T. Mfano wa pata (sarafu) iliyopotea (15:8-10)

Labda **mwanamke** ndani ya habari hizi ni mfano wa Roho Mtakatifu anayetafuta wapotevu na **taa** ya Neno la Mungu. **Zile sarafu za feza** tisa zinasema juu ya wale wasiotubu, lakini ile sarafu moja iliyopotea inatuleta kufikiri juu ya mtu aliye tayari kukiri ya kwamba yeye ni mbali na Mungu. Ndani ya mfano wa mbele kondoo alikwenda mbali na kundi na kutaka kwake mwenyewe. Sarafu haina uzima ndani yake na inatufikirisha ya kuwa mwenye zambi anakosa uzima. Yeye ni **mfu** ndani ya zambi zake.

Mwanamke anakaa **kutafuta** sarafu **na bidii** kufika **saa anapoipata.** Halafu anaita **rafiki na jirani** zake kufurahi pamoja naye. Ile sarafu moja ilimfurahisha kupita zile sarafu tisa zisizopotea. Ni vivyo hivyo na Mungu. **Mwenye zambi** ambaye anajinyenyekeza na kukiri kwamba amepotea anafurahisha roho ya Mungu. Hapati furaha namna hii toka watu wale wasiofahamu kamwe kwamba wanahitaji kutubu.

### U. Mfano wa mwana aliyepotea (15:11-32)

**15:11-16** Mungu Baba anaonyeshwa hapa kama **mtu** aliyekuwa na **wana wawili. Mwana aliyezaliwa nyuma** ni mfano wa mwenye zambi anayetubu, lakini mzaliwa wa kwanza ni mfano wa waandishi na Wafarisayo. Wao ni wana wa Mungu kwa njia ya kuumbwa, si kwa ukombozi. Mwana wa pili alijulikana vilevile kama **mwana mpotevu** kwa maneno ya kupoteza mali. Mwana huyu alichoka na nyumba ya baba yake, na alikusudi kuondoka. Hakutaka ku-

ngojea kufa kwa baba yake, hivi aliomba kupewa **sehemu** yake ya uriti mbele. Basi baba aligawia kila mwana sehemu yake ya uriti. Nyuma kidogo mwana wa pili alikwenda safari **kwa inchi ya mbali**, akapoteza mali kwa maisha ya uasherati. Lakini wakati mali yake ilipokwisha, njaa kubwa iliingia inchi ile naye aliachwa masikini kabisa. Aliweza kupata namna moja tu ya kazi, ndiyo kazi ya kulisha **nguruwe** – kazi isiyoweza kupendeza Myuda hata kidogo. Wakati alipokaa kuangalia nguruwe wakikula **makanda** yao alipatwa na wivu. Nguruwe hawa walipewa vyakula, lakini **hakuna mtu** ambaye alimsaidia **yeye.** Rafiki zake za mbele wakati alipokuwa na mali nyingi, walikuwa wamepotea.

**15:17-19** Lakini muda huu wa njaa uligeuka baraka kwake. Ulimkumbusha ya kwamba **watumishi wa mshahara** nyumbani mwa baba yake walikaa vizuri kupita yeye. Walikuwa na vyakula vya kutosha mahitaji yao, lakini yeye mwenyewe alikuwa akikonda kwa sababu ya **njaa**. Wakati alipofikiri juu ya neno hili alifanya shauri **kwenda** karibu na **baba** yake na roho ya toba, kukiri zambi yake, na kuomba usamehe. Alifahamu kwamba **hakustahili kuitwa mwana wa baba yake tena**, akaomba kupewa **kazi ya mshahara**.

**15:20** Wakati alipokuwa kwanza mbali na nyumba ya baba yake, **baba akamwona, akamhurumia, akapiga mbio, akamwangukia shingo lake, akambusu sana.**

**15:21-24 Mwana** alikiri zambi yake lakini hakuweza kuomba kupewa kazi ya mshahara, **kwani baba** alianza kusema na kuagiza watumwa kumvalisha na **vazi bora** zaidi, kuweka **pete kwa kidole chake na viatu kwa miguu yake**. Aliagiza vilevile watayarishe karamu kubwa kwa sababu mwana wake **aliyepotea alipatikana** tena. Ni kama kwa mawazo ya baba mwana huyu alikuwa **mfu** lakini sasa **alikuwa hai tena.** Mtu mmoja alisema, "Mwana huyu alitaka kukaa na furaha, lakini hakupata furaha katika inchi ya mbali. Aliipata tu wakati alipofahamu ilimpasa kurudia nyumba ya baba yake." Tunasoma vilevile ***wakaanza*** **kufurahi,** lakini hatusomi ya kwamba furaha yao *ilikwisha*. Ni vivyo hivyo na wokovu wa mwenye zambi.

**15:25-27** Wakati **mwana mzaliwa wa kwanza** aliporudia nyumba toka **shamb**a na kusikia makelele haya yote ya furaha **aliuliza** mtumishi mmoja **sababu** ya maneno haya. Mtumishi alimjulisha ya kwamba **mdogo** wake alikuwa amerudi kwake, na ya kwamba **baba** yake alifurahi sana sana.

**15:28-30** Basi mwana wa kwanza alijazwa hasira kali na wivu. Alikataa kushiriki ndani ya furaha ya baba yake. Wakati **baba** alipomwita kula karamu pamoja nao, alikataa akisema baba yake hakumpa yeye **kamwe** zawabu kwa kazi na kutii kwake. **Hakupewa kamwe hata mwana-mbuzi**, au kinda la ngombe mwenye kunona. Alinungunika kwa sababu saa mwana mpotevu aliporudi nyuma ya kupoteza mali ya baba yake na **makahaba,** baba yake alimtayarishia karamu kubwa. Ona ya kwamba alisema **"huyu mwana wako,"** si "ndugu yangu."

**15:31,32** Jibu la baba linaonyesha kwamba kuna furaha wakati mwana **mpotevu** anaporudi, lakini furaha inakosa wakati mwana mkaidi asiye na asante anapokataa kupatanishwa.

Mwana wa kwanza ni mfano wa waandishi na Wafarisayo. Hawakufurahi hata kidogo juu ya Mungu akirehemu watu walio wenye zambi kabisa. Walifikiri (lakini mafikiri haya hayakupatana na yale ya Mungu) ya kwamba walikuwa wamemtumikia na uaminifu, bila kuasi maagizo yake, lakini hawaku-

pokea zawabu. Walikuwa wadanganyi kwa maneno ya dini, na wenye zambi. Kiburi yao iliwageuza kuwa kama vipofu hata hawakufahamu kwamba walikuwa mbali sana na Mungu ambaye aliwabariki sana sana. Kama wangalitubu tu na kukubali zambi zao, moyo wa Baba ungalifurahishwa, nao wangalishiriki ndani ya karamu ile kubwa.

### 5. Mfano wa mlinzi mali asiyekuwa na haki (16:1-13)

**16:1,2** Sasa Bwana Yesu aliacha kusema na Wafarisayo na waandishi na aligeuka kusema kwa **wanafunzi wake** na kuwafundisha juu ya kulinda mali. Ni nguvu kueleza maana ya mashairi haya wazi. Kwa nini? Kwa sababu ni kama yanasifu udanganyifu.Tutaona nyuma ya kwamba neno hili si kweli. Yule **tajiri** ndani ya mashairi haya ni mfano wa Mungu mwenyewe. **Mlinzi mali** ndiye mtu aliyepewa kazi ya kulinda mali ya mtu mwingine. Ndani ya mashairi haya, kila mwanafunzi wa Bwana ni mlinzi mali vilevile. Basi **mlinzi** ambaye tunasoma habari zake hapa alishitakiwa na kuiba mali ya bwana wake. Bwana wake alimwita kutoa hesabu ya uwakili wake, na kumwondosha kwa kazi yake.

**16:3-6** **Mlinzi mali** afanye nini basi? Alijua sharti atafute njia kujiwekea mali tayari kwa mahitaji yake kwa wakati wa kuja. Hakuweza kutumika kazi ngumu kama kulima shamba tena, na kiburi yake ilimkataza **kuomba watu** kumsaidia na mali (lakini kiburi haikumzuiza asiibe). Basi afanye nini? Alikumbuka njia moja ambayo iliweza kumpatia rafiki kumsaidia wakati atakapokuwa na mahitaji. Alifikia mmoja wa wanunuzi wa bwana wake, akamwuliza **hesabu ya deni yake**. Wakati mnunuzi alipojibu **vipimo mia vya mafuta,** alisema naye kulipa kwa vipimo **makumi tano** tu kumaliza deni yake.

**16:7** Mnunuzi **mwingine** alikuwa na deni ya **vipimo mia vya ngano**. Mlinzi mali alisema naye kulipa **vipimo makumi nane** tu kumaliza deni yake.

**16:8** Neno ambalo linatushitusha zaidi ndani ya habari hizi ni kusikia tajiri **akisifu mlinzi mali asiye na haki.** Kwa nini atamsifu juu ya kutenda wizi namna hii? Mashairi yanayofuata yanaonyesha ya kwamba mlinzi mali hakupata sifa kwa sababu ya udanganyifu wake, lakini kwa sababu alitazamia wakati wa kuja. Alikuwa ametenda na akili kusudi awe na mali kwa mahitaji yake kwa wakati wa kuja. Lakini tukiwaza juu ya maisha yetu wenyewe, inatupasa kukumbuka kwamba watoto wa Mungu hawatazamii maisha hapa duniani, lakini yale ya mbinguni. Maneno ambayo mlinzi mali alifanya yalimtayarishia rafiki kwa wakati atakapolazimishwa kuacha kazi. Vivyo hivyo Mkristo akitumika na vitu vya Bwana yake vizuri sasa, atakuwa na wenye kumkaribisha wakati atakapofikia mbingu.

Bwana alisema, **"Watu wa dunia hii ni wenye akili kutazama mbele kuliko wana wa nuru katika kizazi chao wenyewe."** Maana ya masemo haya ndiyo ya kwamba wasioamini na wazalimu wana akili kujitayarisha mali kwa mahitaji yao kwa wakati wa kuja, kupita akili ya waamini wa kweli kujiwekea hazina mbinguni.

**16:9** Inatupasa **kujipatia rafiki** *kwa njia ya* **mali ya uzalimu**. Maana yake inatupasa kutumika na mali na vitu kwa kazi ya kuleta wasioamini karibu na Kristo na kwa njia hii kuanza urafiki nao utakaodumu milele. Mwalimu mmoja, jina lake Pierson, alieleza neno hili wazi:

> Tunaweza kutumika na mali kununua Biblia, vitabu, traités, vivi hivi, na kwa njia hii kupata watu kwa Kristo. Kwa njia hii vitu vya dunia vinageuka kuwa na faida kwa roho na kwa milele. Fikiri juu ya mtu aliye na dollars 100. Anaweza kutumika

> na mali hii yote kwa karamu pamoja na ndugu na rafiki. Kama akifanya hivi, kesho yake hakuna faida inayobaki. Au anaweza kutumika na mali ile kununua Biblia nyingi, ndilo Neno la Mungu. Halafu anapanda mbegu hii ya ufalme wa Mungu pamoja na akili na maombi. Halafu mbegu hii inaota kuwa mavuno, si mavuno ya Biblia, lakini ya roho za watu. Kwa njia ya mali ya uzalimu amejipatia rafiki ambao watamsaidia saa ya mahitaji yake na kumpokea katika makao ya milele, ndiyo mbingu.[29]

Haya ndiyo mafundisho ya Bwana wetu. Kwa njia ya kutumika vizuri na mali ya dunia tunaweza kushiriki ndani ya baraka ya roho, ya milele, ya wanaume na wanawake. Siku nyingine wakati sisi wenyewe tutakapofikia mbingu, watu wengine waliookolewa kwa sababu ya mali tuliyotolea Bwana, na kwa sababu ya maombi yetu, watakuwa pale kutukaribisha. Wataturudishia asante na kusema nasi: "Ni wewe ambaye uliniita kufika hapa."

Mwalimu mwingine, ndiye Darby, alisema:

> Mtu ni mlinzi mali wa Mungu, na taifa la Israeli lilikuwa mlinzi wa mali ya Mungu. Waliwekwa ndani ya shamba la Mungu na Mungu aliwawekea amana sheria yake, ahadi, maagano na ibada. Lakini taifa la Israeli lilipoteza baraka hizi zote. Mtu hakuwa mlinzi mali mwaminifu hata kidogo. Basi Mungu, kwa enzi na neema yake, anatumika na yale ambayo mtu asiyotumia vizuri hapa duniani kwa kuzaa nayo matunda kwa mbingu. Haifai mtu kutumika na vitu vya dunia kujifurahisha mwenyewe sasa katika dunia iliyo mbali kabisa na Mungu, lakini avitumie akitazamia wakati wa kuja. Haifai kwetu kusumbuka kujipatia vitu hivi ili tuweze kupata faida yao sasa, lakini kwa kutumika navyo vizuri kuwa akiba kwa wakati wa kuja. Ni vizuri kugeuza vyote kuwa rafiki kwa wakati wa nyuma kupita kuwa na mali sasa. [30]

**16:10** Tukiwa wakili **waaminifu** katika **kitu kidogo kabisa** (mali), halafu tutakuwa **waaminifu** katika kile **kilicho kikubwa** (hazina ya roho). Lakini mtu aliye mzalimu kwa namna anavyotumika na mali ambayo Mungu alimwekea, huyu atakuwa mzalimu kwa mambo makubwa kupita vilevile. Mungu anaita mali kitu **kidogo kabisa.**

**16:11** Haifai mtu asiyetenda kwa haki saa anapotumika na **mali ya uzalimu** kwa Mungu kufikiri Mungu atamwekea **mali za kweli**. Mali inaitwa **mali ya uzalimu**. Mali yenyewe si mbaya, lakini inageuka mali ya **uzalimu** kwa sababu watu wanatumika nayo zaidi kwa maneno yasiyo kwa utukufu wa Mungu. Ni namna nyingine na **mali za kweli**. Faida ya mali ya dunia ni kwa wakati tu na inageukageuka, lakini faida ya maneno ya roho haitageuka kamwe kwani ni ya milele.

**16:12** Ndani ya shairi hili tunaona ya kwamba **mali ya mtu mwingine** ni namna nyingine na **mali yenu wenyewe**. Yote tuliyo nayo, mali yetu, saa yetu, zawadi zetu – ni mali ya Bwana na inatupasa kutumika nayo kwa yeye. "**Mali yenu wenyewe**" ndiyo zawabu ambazo tutapokea ndani ya maisha yetu ya sasa na kwa wakati wa kuja kwa sababu ya kutumikia Kristo na uaminifu. Kama tusipotumika kwa haki na ile iliyo yake, namna gani ataweza kutupa sisi **mali yetu wenyewe**?

**16:13** Haiwezekani kuishi kwa vitu na kwa **Mungu** pamoja. Kama mapendo ya mali yakitutawala hatuwezi kutumikia Bwana vilevile. Kwa kujipatia mali inatupasa kuweka saa na nguvu yetu yote kwa kazi ile. Wakati tunapofanya hivi, tunaibia Mungu yaliyo yake, ndipo pahali pa kwanza ndani ya maisha

yetu. Roho yetu ni pahali hazina yetu ilipo. Wakati tunapojaribu kujipatia mali, tunatumikia **mali**, lakini haiwezekani hata kidogo **kutumikia Mungu** na mali pamoja. Mali inataka kula nguvu yetu yote, na vyote tulivyo navyo, na saa zote ambazo ingalitupasa kutumikia Bwana.

### W. Wafarisayo wenye choyo (16:14-18)

**16:14** Wafarisayo walikuwa wenye kiburi na wadanganyifu, na zaidi ya ile walikuwa wenye choyo. Walifikiri ya kwamba utawa ni njia kujipatia faida. Walichagua dini kama kazi kwa kujipatia mali. Kusudi la utumishi wao halikuwa kutukuza Mungu na kusaidia majirani yao, lakini kujipatia wenyewe mali. **Walizarau** mafundisho ya Bwana Yesu ya kwamba ingewapasa kuacha kuweka roho juu ya mali duniani na kujiwekea hazina mbinguni. Walitegemea mali kupita ahadi za Mungu. Hawakukubali kuruhusu kitu cho chote kuwazuiza wasijiwekee mali.

**16:15** Mbele ya watu Wafarisayo walionekana kuwa watawa na wenye kupenda Mungu. Walijihesabu kuwa wenye haki kwa macho ya **watu**, lakini Mungu aliona choyo ya **roho** zao. Hakudanganywa. Namna ya maisha yao yaliyokubaliwa na watu wengine (Zaburi 49:18), **ilikuwa machukizo kwa macho ya Mungu**. Walifikiri walisitawi kwa sababu walishika kazi ya dini pamoja na kuwa na utajiri. Lakini kwa macho ya Mungu walikuwa wazini wa roho. Walikiri kwamba walipenda Yehova, lakini kabisa kabisa mali ilikuwa mungu wao.

**16:16** Ni nguvu kuona namna mashairi 16-18 yanavyofuatana. Wakati tunapoyasoma kwanza hatufahamu namna yanavyofuatana, na kwa nini maneno yale yalitangulia yale yanayofuata. Njia nzuri kuyafahamu ni kukumbuka ya kwamba neno kubwa tulilosoma juu yake ndani ya sura 16 lilikuwa choyo na uzalimu wa Wafarisayo. Watu wale waliojivuna juu ya kushika sheria vizuri sana wanaonekana kuwa wadanganyifu na wenye choyo. Tunaona kwamba roho ya sheria ni mbali na roho ya Wafarisayo.

**Torati na manabii zilikuwa hata Yoane.** Masemo haya ya Yesu yalionyesha kwamba muda wa sheria ulioanza na Musa ulikwisha na Yoane Mbatizaji. Sasa madaraka mengine yalianza. Kuanza na Yoane habari njema ya **ufalme wa Mungu ilihubiriwa**. Yoane Mbatizaji alikwenda kutangaza kufika kwa Mfalme wa kweli wa Israeli. Aliagiza watu kama wakitubu, Bwana Yesu atawatawala. Watu wengi walipokea mahubiri yake, na yale ya Bwana mwenyewe, na ya wanafunzi nyuma yake.

**"Kila mtu anajiingiza kwa nguvu kule"** ni kusema ya kwamba wale waliopokea habari hizi waliingia ufalme na roho moja na kushinda vizuizo vyote.

**16:17,18** Ndiyo, muda mpya ulikuwa umeanza, lakini kweli zote za zamani juu ya mwenendo wa utawa hazikugeuka. Ingalikuwa **nyepesi kupita kwa mbingu na dunia kutoweka kuliko nukta moja ya torati kuanguka.** Nukta inaweza kusawanishwa na kipande kidogo sana cha herufi.

Wafarisayo walifikiri walikuwa ndani ya ufalme wa Mungu, lakini Bwana alikuwa alisema kwamba sheria za zamani juu ya mwenendo wa utawa hazikwisha. Ni kama alisema nao: "Hamuwezi kuona bure sheria hizi za Mungu juu ya utawa pamoja na kufikiri kwamba ninyi ni ndani ya ufalme." Labda waliuliza, "Ni sheria gani za utawa tunazoona bure?" Halafu Bwana alionyesha kwamba sheria ya ndoa haitapita kamwe. Kila mtu **anayeacha mke wake na kuoa mwingine, anazini; naye anayeoa mke aliyeachwa na**

**mme wake, anazini** vilevile. Hili ndilo neno Wafarisayo walilotenda kwa maneno ya roho. Mungu alikuwa amefanya agano na Wayuda, lakini sasa Wafarisayo hawa walikuwa wakigeuka mbali na Mungu na kuweka roho zaidi juu ya kujipatia mali. Labda wengine walikuwa wakitenda uzini kwa mwili vilevile.

### X. Mtu mwenye mali na Lazaro (16:19-31)

**16:19-21** Bwana alimaliza hotuba yake juu ya kazi ya mlinzi mali kwa njia ya kufundisha juu ya watu wawili na habari zao nyuma ya kufa kwao. Ona ya kwamba habari hizi *hazikuitwa* mfano.

Tajiri huyu hakuhukumiwa kwa Hadeze kwa sababu ya mali yake. Msingi wa wokovu ni imani ndani ya Bwana Yesu, na watu wanahukumiwa kwa sababu wanakataa kumwamini yeye. Tajiri huyu alionyesha kwamba hakuokolewa kweli kwa sababu ya namna alivyoona bure mahitaji ya **masikini aliyelala inje ya mlango wake.** Kama angalikuwa na mapendo ya Mungu rohoni mwake, kama asingaliweza kuishi kila siku na anasa, na akijaza tumbo lake na vyakula vitamu vyote wakati masikini huyu alipokuwa inje ya mlango wake akiomba kupewa **makombo** ya mkate. Angalijiingiza kwa ufalme wa Mungu kwa nguvu na kuacha mapendo yake kwa mali.

Tufahamu vilevile ya kwamba Lazaro hakuokolewa kwa sababu alikuwa masikini. Alikuwa ameamini Bwana na kupokea wokovu.

Waza kwanza juu ya tajiri. Anaitwa Dives mara nyingine (kilatin kwa *tajiri*). Alivaa mavazi ya bei kubwa yaliyoshonwa kwa yeye tu, na meza yake ilijaa vyakula vizuri zaidi. Aliishi kwa kujifurahisha mwenyewe na mwili wake tu. Hakuwa na mapendo ya kweli kwa Mungu, wala kutaka kusaidia watu wenzake.

Hali ya **Lazaro** ilikuwa namna nyingine kabisa. Alikuwa na taabu na **umasikini**, na alifikishwa kila siku kwa lango la nyumba ya tajiri. Alikonda sana na mwili wake ulifunikwa na **vidonda**. Aliteswa na **imbwa** wachafu waliokuja **kulamba vidonda vyake.**

**16:22** Wakati **masikini alipokufa alichukuliwa na malaika katika kifua chake Abrahamu.** Watu wengi wanafazaika kama kweli **malaika** wakishiriki ndani ya kazi ya kupeleka roho za waamini mbinguni. Mwandishi wa kitabu hiki hana shaka juu ya neno hili. Malaika wanatumikia waamini katika maisha yao ya sasa; kwa nini hawatafanya hivi saa ya kufa kwao vilevile? **Kifua cha Abrahamu** ni mfano wa pahali pa heri. Wayuda wangalifikiri kuwa na ushirika na Abrahamu kuwa furaha tele. Tunafikiri **kifua cha Abrahamu** ndicho mbingu. Wakati **tajiri alipokufa** mwili wake **ulizikwa** – ule mwili ambao alibembeleza sana, na kupoteza mali nyingi juu yake.

**16:23,24** Ndiyo, mwili wake ulizikwa ndani ya kaburi, lakini nafsi yake, ndiyo ufahamu wa moyo wake, ilifika **Hadeze. Hadeze** ni Kiyunani kwa *Sheol*, ndipo pahali pa roho za wafu. Kwa wakati wa Agano la Kale ilikuwa kao kwa roho za waokolewa na wa wapotevu pamoja. Lakini hapa tunasoma juu yake kama kao la wapotevu, kwa sababu tunasoma ya kwamba tajiri alikuwa **katika azabu.**

Bila shaka wanafunzi walishituka kabisa wakati Yesu aliposema Myuda huyu tajiri alikwenda **Hadeze**. Katika Agano la Kale walifundishwa ya kwamba utajiri ni alama ya baraka ya Mungu. Liliahidi ya kwamba Mwisraeli akitii Bwana atasitawi. Basi namna gani Myuda tajiri atakwenda Hadeze? Bwana Yesu alikuwa ametangaza sasa tu ya

kwamba mahubiri ya Yoane Mbatizaji yalikuwa mwanzo wa muda na utaratibu mpya. Kuanza saa ile utajiri si alama ya baraka ya Mungu tena, lakini **unapima** uaminifu wa mtu kama mlinzi mali wa Mungu. Sharti yule aliyepewa mali nyingi atoe nyingi vilevile.

Watu wengine wanafikiri kwamba nyuma ya kufa kwa mtu na kufika ufufuko mtu huyu hajui kitu, lakini shairi 23 linaonyesha kwamba mawazo haya si kweli. Tunashangaa juu ya maneno yote ambayo tajiri alijua. **Aliona Abrahamu mbali, na Lazaro katika kifua chake.** Aliweza kusema na Abrahamu. Akimwita **Baba Abrahamu**, alimsihi **kumrehemu**, akiomba kwa **Lazaro** ampe **maji nusu apoleshe ulimi wake.** Ndiyo, tunaweza kuuliza namna gani nafsi isiyo na mwili inaweza kusikia kiu kwa sababu ya **moto.** Tunafikiri masemo haya yalikuwa mfano wa maumivu ya kweli.

**16:25 Abrahamu** aliita tajiri **mwana,** kama kuonyesha kwamba alikuwa mzao wa Abrahamu kwa njia ya mwili, lakini ni wazi ya kwamba hakuwa mzao wake kwa maneno ya roho. Abrahamu alimkumbusha ya kwamba wakati alipokuwa hai alikuwa na vitu vingi na kukaa na anasa. Alimkumbusha vilevile umasikini na mateso ya **Lazaro**. Sasa, nyuma ya kufa kwao, maneno haya yaligeuka.

**16:26** Tunajifunza ya kwamba maneno tunayochagua katika maisha ya sasa si kwa wakati wa sasa tu lakini **kwa milele**. Hakuna njia kwa sisi kuyageuza nyuma ya mauti. Hakuna njia kupita toka pahali watu waliohukumiwa wanapokaa kwenda pahali pa wale waliookolewa.

**16:27-31** Nyuma ya kufa kwake gafula tajiri alipata hamu kutangaza Habari Njema. Alitaka mtu kwenda kuonya **ndugu zake watano** wakae na ange wasifikie **pahali pale pa azabu.** Abrahamu alijibu ya kwamba ndugu hawa watano, wakiwa Wayuda walikuwa na Maandiko ya Agano la Kale, nayo yalitosha kuwaonya juu ya hatari hii. Tajiri alikana masemo ya **Abrahamu** na alijibu kama mtu **akikwenda kwao toka wafu** bila shaka watatubu. Sivyo, Abrahamu alijibu. Lazima watu wasikie na kutii Neno la Mungu. Hakuna njia nyingine. Kama watu wakikataa kusikia Biblia, watakataa kuamini vilevile hata mmoja akikwenda kwao **toka wafu**. Neno hili lilihakikishwa ndani ya maisha ya Bwana Yesu mwenyewe. Alifufuliwa toka wafu, lakini watu hawamwamini mpaka leo.

Kwa njia ya Agano Jipya tunajua ya kwamba wakati mwamini anapokufa, mwili wake unazikwa kaburini, lakini nafsi yake inakwenda kukaa pamoja na Bwana mbinguni (2 Kor. 5:8; Flp. 1:23). Wakati msiyeamini anapokufa, mwili wake unazikwa vilevile, lakini nafsi yake inakwenda kwa Hadeze, pahali pa mateso na majuto.

Wakati Kristo atakaporudi toka mbinguni, miili ya waamini itafufuliwa toka kaburi na kukutanishwa na roho na nafsi zao (1 Tes. 4:13-18). Halafu watakaa pamoja na Kristo kwa milele. Kwa hukumu ya kiti kikubwa cheupe, miili, roho na nafsi za wasioamini watakutanishwa (Ufu. 20:12,13). Kisha watatupwa ndani ya ziwa la moto, pahali pa azabu ya milele.

Hivi kwa mwisho wa sura 16 kuna onyo la kuogopesha sana kwa Wafarisayo, na kwa watu wote wanaoishi zaidi kujipatia mali. Kufanya hivi ni hatari kubwa kwa nafsi zao. Kuomba kupewa mkate hapa duniani ni vizuri kupita kuomba maji katika Hadeze.

## 9. MWANA WA WATU ANAFUNDISHA WANAFUNZI WAKE (17:1 – 19:27)

### A. Hatari ya makwao (17:1,2)

Si wazi namna mawazo ndani ya sura

hii yanafuatana. Ni kama Luka anaunganisha habari juu ya maneno mbalimbali. Lakini maneno Kristo aliyosema kwa mwanzo wa sura hii yanatufikirisha habari za tajiri kwa mwisho wa sura 16. Kukaa katika raha na utajiri na anasa kunaweza kuwa kikwazo kwa wale wasioendelea kwanza sana ndani ya imani. Mtu akijulikana kuwa Mkristo mzuri, watu wengine wataiga mwenendo wake. Ni vibaya sana kuongoza waamini wa sasa wenye hamu kufuata Bwana Yesu Kristo, kuishi kwa vitu vya dunia na kuabudu mali.

Na mafundisho haya ni juu ya kukwalisha kwa njia nyingine vile. **"Hawa wadogo"** wanaweza kupewa hamu kwa maneno ya dunia. Wanaweza kukwalishwa na zambi za mwili. Wanaweza kukwalishwa kwa njia mbalimbali zinazoweza kuwaondosha katika njia ya kufuata Bwana na imani na mapendo na utawa.

Bwana Yesu alijua vizuri hali ya dunia hii na roho za watu, hivi alisema sharti **makwao yatokee.** Lakini neno hili halipunguzi ukubwa wa hukumu ya wale kwa njia yao makwao yale yanakuja. **Ingefaa** watu hawa **wafungiwe jiwe la kusagia** na watupwe katika **bahari**. Ukali wa masemo haya unatufikirisha ya kwamba Bwana hakufikiri juu ya mauti ya mwili tu, lakini hukumu ya milele vilevile.

Hatufikiri ya kwamba Bwana Yesu alifikiri juu ya watoto wadogo tu wakati aliposema juu ya **hawa wadogo**, lakini juu ya waamini wa sasa walio wadogo ndani ya imani yao vilevile.

### B. Juu ya hitaji la kuwa na roho ya usamehe (17:3,4)

Inawezekana kwa Wakristo kuumiza watu wengine, na kuna hatari vilevile kubaki na chuki ya siri rohoni mwetu, na kukataa kusamehe yule ambaye alituumiza wakati anapoomba kusamehewa. Agano Jipya linafundisha utaratibu huu kwa maneno ya kusamehe:

1. Mkristo akitendewa mabaya na Mkristo mwingine, inampasa kwanza kumsamehe rohoni mwake (Efe. 4:32). Kufanya hivi kutamzuiza asiwe na uchungu rohoni mwake mwenyewe.
2. Nyuma yake inampasa kufikia yule ambaye alimtendea mabaya peke yake na **kumkemea** (sh.3, ona vilevile Matayo 18:15). **Akitubu,** inapasa kumwambia kwamba amesamehewa. Hata akianguka tena na tena, na nyuma yake anasema anatubu, sharti asamehewe (sh.4).
3. Kama mtenda mabaya asipotubu wakati anapokemewa peke yake, halafu inapasa mtu aliyekosewa kumfikia tena pamoja na washuhuda mmoja au wawili (Mt. 18:16). Kama akikataa kuwasikiliza inapasa kuleta neno lenyewe mbele ya kanisa. Mtenda mabaya akikataa kusikia kanisa, sharti aondoshwe kanisani (Mt. 18:17).

Kusudi la makemeo na azabu hii si kulipiza mtenda mabaya kwa mabaya aliyotenda, wala kumnyenyekeza, lakini kumrudisha kuwa na upatano mzuri tena na Bwana na waamini wenzake. Sharti makemeo yawe pamoja na mapendo. Hatuwezi kujua kama mtenda mabaya alitubu na roho ya kweli. Sharti tuamini masemo yake kwamba ametubu. Kwa sababu hii Yesu alisema, **"Na akikukosea mara saba katika siku moja, na mara saba katika siku moja anarudi kwako akisema: Ninatubu, umsamehe."** Baba yetu anatutendea sisi na neema namna hii. Hata tukimkosea mara ngapi, tunaweza kujua kwamba "tukikiri zambi zetu yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee zambi zetu, na kutusafisha na uzalimu wote" (1 Yn. 1:9).

### C. Juu ya imani (17:5,6)

**17:5** Kwa mafikiri ya **wanafunzi** ilikuwa nguvu kusamehe mtu mmoja

mara saba kwa siku moja. Wataweza kweli? Hawakufikiri ya kwamba walikuwa na neema ya kutosha kutenda hivi. Hivi waliomba **Bwana** kuwaongezea **imani** yao.

**17:6** Jibu **la Bwana** lilionyesha kwamba neno kubwa si kipimo cha imani lakini namna ya imani. Hawakuhitaji kuongezewa imani lakini kutumika na imani ambayo walikuwa nayo. Kiburi na kujifikiri kuwa mkubwa kunatuzuiza tusisamehe ndugu zetu. Lazima inapasa kiburi hiki kungolewa. Kama **imani** ya kipimo cha mbegu ya haradali ikitosha kungoa **mtini** na kuupanda **baharini**, haitakuwa nguvu kwa imani yetu kutuwezesha kushinda ugumu wa mioyo yetu ambao unatuzuiza tusisamehe ndugu yetu tena na tena na tena .

### D. Juu ya watumwa wa faida (17:7-10)

**17:7-9** Hakuna njia kwa mtumwa wa kweli wa Kristo kujivuna. Sharti angoe mawazo yote ya ukubwa wake mwenyewe na kuyakomboa na ufahamu kwamba hastahili hata kidogo. Haya ndiyo mafundisho ya habari hizi za mtumwa. **Mtumishi** huyu alishinda mchana mzima **akilima shamba au kulinda kondoo. Wakati aliporudi toka shamba** kwa mwisho wa kushinda jua zima akitenda kazi ngumu, bwana wake hakumwagiza kuja na **kuketi kula chakula**. Sivyo, alimwagiza kujifungia nguo na **kuletea bwana wake vyakula**. Nyuma ya kumaliza kazi ile tu mtumwa alikuwa na ruhusa **kula** chakula chake mwenyewe. Bwana wake wa kazi **hakumtolea asante** kwa sababu alifanya maneno haya. Ni kazi ya lazima kwa mtumwa. Yeye ni mali ya bwana wake na kazi yake kubwa ni kutii maagizo yake.

**17:10** Vivyo hivyo wanafunzi ni watumwa wa Bwana Yesu Kristo. Wao ni mali yake – roho zao, nafsi zao na miili yao. Hakuna kazi wanayoweza kufanya inayotosha kumlipa kwa kazi kubwa ambayo aliwafanyia kwa Kalvari. Hivi hata wakati mwanafunzi anapokwisha **kufanya** yote **aliyoagizwa** ndani ya Agano Jipya, inampasa kukubali kwamba yeye ni mtumwa **asiye na faida** aliyefanya tu **maneno ambayo ilimpasa kufanya.**

Mwalimu Roy Hession, alisema kwamba alama tano za mtumwa ndizo hizi:

1. Sharti akubali kuvimbishiwa kazi nyingi kupita kipimo, bila kuwaza juu ya nguvu yake mwenyewe.
2. Akubali kufanya kazi yenyewe bila kupokea asante.
3. Wakati anapokwisha kufanya kazi ile yote, haifai kushitaki bwana wake juu ya kujifikiri mwenyewe tu.
4. Sharti akiri kwamba yeye ni mtumishi asiye na faida.
5. Sharti akubali kwamba kipimo cha kazi na magumu yote ambayo alivumilia na upole na unyenyekevu hakipiti hata kidogo maneno ambayo ilimpasa kufanya. [31]

### E. Yesu anasafisha wakoma kumi (17:11-19)

**17:11** Zambi nyingine ndani ya maisha ya mwanafunzi wa Yesu ni ukosefu wa roho ya asante. Tunaona neno hili ndani ya habari za wakoma kumi. Tunasoma kwamba Bwana Yesu alikuwa akisafiri kwa mipaka ya **Samaria na Galilaya** kwenda **Yerusalema.**

**17:12-14 Wakati alipoingia kijiji kimoja … watu kumi wenye ukoma** walimwona. Kwa sababu ya ugonjwa wao, hawakumkaribia, lakini walipaza sauti toka mbali wakimsihi kuwaponyesha. Kama zawabu kwa imani yao Yesu alisema nao **kwenda** na **kujionyesha kwa makuhani.** Maana yake saa walipofikia kuhani watakuwa wameponyeshwa toka ukoma. Kuhani hakuwa na uwezo kuwaponyesha, lakini alipewa *amri kusema* kwamba walikuwa wameponyeshwa. Wakoma walitii agizo la

Bwana, wakashika njia kwendea nyumba ya makuhani, na wakati walipokwenda waliponyeshwa toka ugonjwa ule.

**17:15-18** Wao wote walikuwa na imani na waliponyeshwa, lakini mmoja tu wa wale watu kumi alirudi kushukuru Bwana. Na **huyu** mmoja **alikuwa Msamaria,** mmoja wa majirani ya Wayuda waliozarauliwa nao, na wasiokuwa na ushirika nao. Mtu huyu **alianguka kifudifudi mbele ya miguu ya Yesu na kumwabudu. Yesu** alimwuliza kama hawakuwa watu **kumi walioponyeshwa**, lakini mmoja tu, **"mgeni huyu"** alikuwa amerudi kutoa mashukuru. Basi wale **tisa** wengine walikuwa **wapi**? Hata mmoja wao hakurudi **kumpa Mungu utukufu**.

**17:19** Akigeuka, akasema na Msamaria, **"Simama, kwenda zako, imani yako imekuokoa."** Sehemu moja ya kumi tu wanariti utajiri wa kweli wa Kristo. Yesu anatubariki na baraka nyingine tena wakati tunaporudi (sh.15) na kumshukuru (sh.16). **"Imani yako imekuokoa"** – labda wale tisa waliponyeshwa toka ukoma wa mwili, lakini mtu wa kumi aliokolewa toka zambi vilevile (mash.17,18)!

### F. Juu ya kuja kwa Ufalme (17:20-37)

**17:20, 21** Ni nguvu kujua kama **Wafarisayo** waliuliza na roho ya kweli juu ya kuja kwa **ufalme** au kama walikuwa wakizihaki tu. Lakini tunajua, wakiwa Wayuda, walitumaini ya kwamba ufalme utasimamishwa na uwezo na utukufu mkubwa. Walitazamia alama kubwa ambazo waliweza kuona na macho, na mabadiliko makubwa kwa serikali za inchi. Mwokozi aliwaambia kwamba **"Ufalme wa Mungu haufiki kwa kutazamia."** Maana kwa utaratibu wa wakati ule ufalme wa Mungu **haukuja** na mambo ya kuonekana. Haukuwa ufalme wa dunia ambao utadumu kwa wakati tu, ambao watu waliweza kuona **hapa** au **kule.** Sivyo, Mwokozi alisema, **ufalme wa Mungu** ulikuwa **ndani** yao, maana *katikati* yao. Haukuweza kuwa ndani ya mioyo ya Wafarisayo kwa sababu wadanganyifu hawa wenye roho ya nguvu kwa maneno ya dini hawakuwa na nafasi ndani ya mioyo yao kwa Kristo Mfalme. Hivi Mwokozi alisema **ufalme wa Mungu** ulikuwa *katikati* yao. Ni yeye aliyekuwa Mfalme wa kweli wa Israeli na alikuwa amefanya maajabu yake kuhakikisha mbele ya watu wote kwamba yeye ndiye. Lakini Wafarisayo hawakutaka kumpokea. Hivi ufalme wa Mungu ulikuwa umejionyesha kwao lakini hawakuuona hata kidogo.

**17:22** Wakati aliposema na Wafarisayo, Bwana alisema juu ya ufalme kama neno linalokwisha kufika. Wakati aliposema **na wanafunzi,** alisema juu ya ufalme kama neno la wakati wa kuja utakaosimamishwa wakati atakapokuja tena. Lakini kwanza alisema juu ya muda nyuma ya kuja kwake kwa kwanza na mbele ya kuja kwake kwa pili. **Siku zitakuja** wakati wanafunzi **watataka kuona siku moja ya siku za Mwana wa watu**, lakini **hawataiona**, maana yake, watafikiri na hamu juu ya **moja ya siku zile** wakati alipokuwa duniani na walikuwa na ushirika mtamu pamoja naye. Siku zile zilikuwa kama alama ya maneno yatakayotokea wakati atakaporudi na uwezo na utukufu mkubwa.

**17:23,24** Kutakuwa na watu wengi ambao watajiita kristo, na watawala watatangaza kwamba Masiya amekuja. Lakini haifai wafuata wa Bwana wadanganywe na watu wale. Kuja kwa pili kwa Kristo kutaonekana wazi, namna watu wanavyoweza kuona **lalo mbinguni.**

**17:25** Bwana Yesu aliwaambia wanafunzi tena ya kwamba mbele ya ku-

fanyikana kwa maneno haya, **yeye** mwenyewe **atateswa maneno mengi na kukataliwa** na **kizazi** kile**.**

**17:26,27** Halafu Bwana aligeuka kusema tena juu ya kuja kwake kwa kutawala. Alifundisha ya kwamba **siku** zilizotangulia tokeo lile la utukufu mkubwa zitakuwa kama **siku za Noa.** Watu **walikula, walikunywa, walioa na kuolewa.** Maneno haya si mabaya; yanafaa kwa maisha ya kila siku ya watu. Lakini ubaya wao ndio huu: watu waliishi kwa maneno haya tu na hawakuwa na saa kufikiri Mungu. Wakati **Noa** na jamaa yake walipokwisha **kuingia safina, garika ilikuja na kuharibu** watu wote wengine. Hivi kuja kwa pili kwa Kristo kutakuwa hukumu kwa wale wanaokataa rehema yake.

**17:28-30** Halafu Bwana alisema tena ya kwamba siku zitakazotangulia kuja kwake kwa pili zitafanana na zile **za Loti**. Namna watu walivyoishi kwa wakati ule ilikuwa imeendelea kidogo; watu **hawakula** na **kunywa** tu, lakini **walinunua, waliuza, walipanda, walijenga**. Ulikuwa muda wa baraka na salama na usitawi bila Mungu. **Siku ile ile Loti,** mke na binti zake **walipotoka Sodomo, moto na kiberiti zikatoka kwa mbingu na kuangamiza mji** ule mwovu. **Itakuwa vivyo hivyo wakati Mwana wa watu atakapofunuliwa.** Wale wanaoweka roho juu ya anasa, kujipendeza wenyewe, na biashara wataharibiwa.

**17:31** Kwa **siku** ile itakuwa hatari kwa watu kupenda sana vitu vya dunia. Mtu akiwa **juu ya dari ya nyumba, asijaribu** kuponyesha vitu vilivyo **nyumbani** mwake. Akiwa **shambani**, **asirudi** tena kwa nyumba yake, lakini akimbie toka pahali pale patakapokuwa karibu kuhukumiwa.

**17:32** Hata kama **mke wa Loti** alilazimishwa kutoka Sodomo, roho yake ilibaki mjini. Alionyesha neno hili wakati alipogeuka na kutazama nyuma. Alikuwa ameondokea mji wa Sodomo, lakini Sodomo ulikuwa kwanza ndani ya roho yake. Kwa sababu hii Mungu alimhukumu kwa njia ya kumgeuza kuwa nguzo ya chumvi.

**17:33 Mtu anayejaribu kuokoa uzima** wake kwa njia ya kuchunga mwili wake tu, bila kulinda roho yake, **ataipoteza**. Lakini mtu ye yote **anayetoa roho yake** kwa muda huu wa mateso kwa sababu ya uaminifu wake kwa Bwana **ataiponyesha** kwa milele.

**17:34-36** Kuja kwa Bwana kutakuwa wakati wa mtengano. **Watu wawili** watakuwa wakilala **ndani ya kitanda kimoja, mmoja atatwaliwa** kwa hukumu. **Mwingine**, ndiye mwamini, ataachwa kuingia ufalme wa Kristo. **Wanawake wawili watakuwa wakisaga pamoja;** mmoja, msiyeamini **atatwaliwa** kwa gazabu ya Mungu, **mwingine**, mtoto wa Mungu, ataachwa kufurahishwa na baraka za utawala wa Kristo kwa miaka elfu moja.

Ona ya kwamba mashairi 34 na 35 yanapatana na mafundisho ya mviringo wa dunia. Utakuwa usiku kwa sehemu moja ya dunia na mchana kwa sehemu nyingine kwa saa ile ile. Watu walifahamu neno hili nyuma ya miaka mingi tu.

**17:37** Masemo ya Bwana yalifahamisha wanafunzi ya kwamba kuja kwake kutakuwa wakati wa hukumu kubwa na wa machafuko sana juu ya dunia hii iliyokuwa imeacha Mungu. Hivi waliuliza kama hukumu hii itatokea pahali gani. Aliwajibu kusema **pahali maiti iko, pale pale tai watakusanyika. Tai** ni mfano wa hukumu zilizokuwa karibu. Maana ya jibu lake ndiyo ya kwamba hukumu itapata watu wote wenye kutokuamini na uasi, si neno kama wao ni pahali gani.

Ndani ya sura 17 Bwana Yesu ali-

kuwa ameonya wanafunzi ya kwamba mbele ya kutokea kwake katika utukufu itakuwa sharti kwao kupata taabu na mateso makubwa. Kuwatayarisha kwa maneno haya Bwana alileta mafundisho mengine juu ya maombi. Ndani ya mashairi yanayofuata tutasoma juu ya mjane aliyeomba, juu ya Mfarisayo aliyeomba, juu ya mtoza kodi na mtu masikini walioomba vile.

### G. Mfano wa mjane aliyedumu (18:1-8)

**18:1 Mfano** wa mjane aliyeomba unafundisha ya kwamba inapasa **watu kuomba siku zote, pasipo kuchoka**. Agizo hili ni kwa watu wote na juu ya maombi namna zote, lakini hapa ni zaidi kwa wokovu wa Mungu toka taabu namna namna. Ni maombi **bila kuchoka** katika muda huu mrefu na wa kuchokesha, nyuma ya kuja kwake kwa kwanza na mbele ya kuja kwake kwa pili.

**18:2,3** Ndani ya mfano huu tunaona **mwamuzi** mzalimu asiyeogopa **Mungu** wala kuheshimu **wenzake**. Na tunaona **mjane** aliyekuwa akiteswa na **adui. Mjane** huyu **alifikia** mwamuzi tena na tena akimsihi kukata mashitaki yake kwa **haki**, ili aweze kuponyeshwa toka **matendo mabaya** ya adui yake.

**18:4,5** Mhukumu aliona mashitaki yake bure. Mjane alikuwa akitendewa mabaya bila haki, lakini neno hili halikusukuma mwamuzi kumsaidia. Lakini mwanamke alidumu kumfikia na kumwomba kumsaidia; na kuombaomba kwake kulisukuma mhukumu kukata neno lake kwa kumsaidia.

**18:6,7 Halafu Bwana** alieleza kwa wanafunzi kama **mhukumu mzalimu** alisaidia mjane masikini kwa sababu ya kuombaomba kwake, kuzidi sana **Mungu** atasaidia **wachagulifu wake**. Labda **wachaguliwa** hawa ndio zaidi baki la Wayuda kwa wakati wa Mateso Makubwa, lakini ni kweli vilevile juu ya waamini wote wanaoteswa kwa kila wakati. Mungu amekawa kufika sasa kwa sababu yeye ni mvumilivu na hataki mtu ye yote kupotea.

**18:8** Lakini siku inakaribia wakati atakapoacha kushindana na watu, na halafu ataazibu wale wanaotesa wafuata wake. Bwana Yesu alimaliza mfano huu na ulizo hili: **"Wakati Mwana wa watu anapokuja ataona imani katika dunia?"** Tunafikiri aliwaza juu ya *namna* ya imani ya mjane yule masikini. Lakini labda alikumbuka vilevile ya kwamba wakati Bwana atakaporudi kutakuwa na baki aminifu tu walio wafuata wake kweli. Kwa wakati wa sasa sisi sote tuwe na namna ya imani ambayo inamlilia mchana na usiku.

### H. Mfano wa Mfarisayo na mtoza kodi (18:9-14)

**18:9-12** Mfano huu ya pili ni kwa wale **wanaojisifu** kwamba wao ni **wenye haki,** na wanaozarau **watu wote** wengine kama watu wa chini. Bwana aliita mtu wa kwanza **Mfarisayo,** na kwa njia hii alionyesha wazi kama alikuwa akisema na watu wa tabia gani. Ndiyo, Mfarisayo alionekana kama mwenye kuomba, lakini hakusema na **Mungu** kweli. Alijivuna juu ya haki yake mwenyewe na juu ya namna alivyoshika dini. Kwa pahali pa kujisawanisha na ukamilifu wa Mungu, na kufahamu zambi zake mwenyewe, alijisawanisha na watu wengine na kujivuna kusema yeye anawapita kwa uzuri. Alisema tena na tena: "**nina**", ndilo neno linalofunua hali ya kweli ya roho yake.

**18:13** Habari za **mtoza kodi** zilikuwa namna nyingine. **Akisimama** mbele ya Mungu, alifahamu ya kwamba hakustahili hata kidogo kumkaribia. Alinyenyekezwa kabisa. **Hakutaka kunyanyua macho yake kwa mbingu, lakini alipiga kifua chake, akisema: "Mungu, unirehemu mimi mwenye za-**

**mbi!"** Alijiona mwenyewe kuwa mwenye zambi, asiyestahili kupokea kitu cho chote toka Mungu.

**18:14** Bwana Yesu alikumbusha wasikiaji wake ya kwamba Mungu anakubali na kupendezwa kama watu wake wakiwa na roho ya unyenyekevu na toba mbele yake. Yule **aliyeshuka nyumbani amehesabiwa kuwa na haki** alikuwa mtoza kodi, si Mfarisayo. Mungu anatukuza wanyenyekevu, lakini ananyenyekeza wale ambao wanajitukuza wenyewe.

### I. Yesu na watoto wadogo (18:15-17)

Habari hizi zinaonyesha tena ukubwa wa maneno tuliyosikia sasa tu, ndiyo ya kwamba tunahitaji unyenyekevu wa mtoto mdogo kwa kuweza kuingia **ufalme wa Mungu**. Mama wenye kubeba **watoto** wao **wadogo** walikuwa wakizunguka Bwana Yesu aweze kubariki watoto wao. **Wanafunzi wa Yesu** hawakufurahi juu ya neno hili, lakini Bwana aliwahamakia, **akaita watoto kwake akisema** na roho ya mapendo, **"Ufalme wa Mungu ni kwao wa namna hii."** Shairi 16 ndilo jibu kwa ulizo la watu kama "Nini inapata watoto wadogo wakati wanapokufa?" Watakwenda mbinguni mara moja. Bwana Yesu alisema waziwazi, **"Ufalme wa Mungu ni kwao wa namna hii."**

Watoto wanaweza kuokolewa hata wakati wao wana miaka michache tu. Inapasa kuruhusu mtoto ye yote, hata akiwa na miaka michache sana tu, kuja kwa Yesu, na kumsaidia kupata nguvu katika imani yake.

Watoto wadogo hawahitaji kugeuka watu wa kukomea kusudi waokolewe, lakini watu wa kukomea wanahitaji imani na unyenyekevu namna ya **mtoto mdogo kuingia ufalme** wa Mungu.

### J. Mtawala mwenye mali nyingi (18:18-30)

**18:18,19** Mashairi haya yanasema juu ya mtu mmoja **asiyepokea** ufalme wa Mungu kama mtoto mdogo. Siku moja **mtawala mmoja** alifika karibu na Bwana Yesu, akamwita **Mwalimu mwema,** na kuuliza kama ilimpasa **kufanya nini** ili aweze **kuriti uzima wa milele.** Mwokozi alimwuliza kwanza kwa sababu gani alimwita *Mwalimu mwema*, akimkumbusha ya kwamba mmoja tu ni **mwema,** ndiye **Mungu.** Bwana Yesu hakukataa ya kwamba yeye ni Mungu, lakini alijaribu kuongoza mtu huyu kukiri neno hili. Kama yeye ni mwema, hivi yeye ni Mungu kwani Mungu tu ni mwema.

**18:20** Halafu Yesu alijibu ulizo lake kama ilimpasa kufanya nini kuriti uzima wa milele. Tunajua ya kwamba uzima wa milele si uriti na ya kwamba haupatikani kwa njia ya matendo mema. Uzima wa milele ni zawadi ya Mungu kwa njia ya Yesu Kristo. Wakati Yesu alipotaja **amri** kumi hakusema hata kidogo kwamba mtawala aliweza kuokolewa kwa njia ya kushika sheria. Sivyo, lakini alitaja sheria kumfahamisha zambi zake. Bwana alitaja amri sita kufika kumi za sheria zinazofundisha namna inavyotupasa kutendea wenzetu.

**18:21-23** Ni kama mafundisho haya hayakugusa roho ya mtawala, kwa sababu alisema na kiburi kwamba alikuwa **ameshika** amri hizi **tangu ujana wake**. Yesu alimjulisha kwamba alikosa **neno moja,** ndilo mapendo kwa jirani yake. Kama angalishika amri hizi zote kweli, angaliuza vitu vyake **vyote** na kugawa mali yenyewe kwa watu **masikini**. Lakini hakupenda jirani kwa kipimo alichojipenda mwenyewe. Aliishi maisha ya kujipendeza mwenyewe, bila kupenda watu wengine kweli kweli. Neno hili lilionekana wazi wakati **aliposikia maneno** ya Yesu. **Alikuwa na huzuni sana** kwa sababu **alikuwa na mali nyingi.**

**18:24** Bwana **Yesu** akimtazama alisema ni ngumu sana kwa **wenye mali**

kuingia **ufalme wa Mungu**, maana ni nguvu sana kuwa na mali bila kuipenda na kuitegemea.

Mashairi haya yanaamsha maulizo magumu ndani ya nia za Wakristo na wasioamini vilevile. Namna gani tunaweza kusema tunapenda majirani yetu na mapendo ya kweli wakati tunapoishi vizuri katika utajiri sisi wenyewe na watu wengine wanapokufa kwa milele kwa sababu ya ukosefu wa mali kuwahubiri Habari Njema?

**18:25** Yesu alisema ni **nyepesi kwa ngamia kupita katika tundu la sindano kuliko tajiri kuingia ufalme wa Mungu.** Watu wameeleza shairi hili kwa njia mbalimbali. Wengine wanafikiri tundu la sindano ni lango dogo kwa upande wa ndani wa ukuta wa mji, na ya kwamba ngamia aliweza kuingia kwa njia ya kupiga magoti yake tu. Lakini mganga Luka anatumika hapa na neno linaloonyesha sindano la mganga tu, hivi maana ya maneno haya ya Yesu ni wazi tu. Kama haiwezekani kwa ngamia kupita katika tundu la sindano, vivyo hivyo *haiwezekani* **kwa tajiri kuingia ufalme wa Mungu.** Maana yake haiko ya kwamba tajiri hawezi, hata akipima sana, kuingia ufalme. Neno hili ni kweli kwa mtu masikini vilevile. Maana yake ndiyo hii: *Haiwezekani* kwa mtu **kuingia ufalme wa mbinguni** *kama tajiri*. Angali anaabudu mali yake na kuiacha kuzuiza roho yake isipate wokovu, hawezi kuokolewa. Watajiri wachache tu wanaokolewa, ndio wale wanaofika kwake Mungu na roho ya kuvunjika.

**18:26,27** Wakati wanafunzi waliposikia maneno haya walianza kufazaika **nani basi anaweza kuokolewa**. Kwa mafikiri yao utajiri ulikuwa alama ya baraka ya Mungu (Tor. 28:1-8). Kama Wayuda wenye mali wasingaliweza kuokolewa, nani basi ataweza kupata wokovu? Bwana alijibu na kusema **Mungu** anaweza kufanya maneno yasiyowezekana kwa watu. Ndiyo, Mungu anaweza kuondosha mapendo ya mali na choyo ya mtu anayeishi bila huruma kwa yeye mwenyewe tu, na kuyakomboa na mapendo ya kweli kwa Bwana. Ni ajabu ya neema ya Mungu.

Ndiyo, mashairi haya yanaamsha maulizo na mafazaiko ndani ya watu wa Mungu. Mtumishi si juu kupita Bwana wake; Bwana Yesu aliacha utajiri wa mbingu kuokoa roho zetu za zambi na hatia. Haifai kwa sisi kuwa watajiri hapa duniani, pahali yeye alipokuwa masikini. Bei ya nafsi za watu, ukaribu wa kurudi kwa Kristo, mapendo ya kushurutisha ya Kristo – ingepasa maneno haya yote kutuongoza kutoa mali yote inayowezekana kwa kazi ya Bwana.

**18:28-30** Wakati **Petro** alipokumbusha Bwana kwamba wanafunzi walikuwa **wameacha** nyumba na jamaa zao kusudi wamfuate, Bwana alijibu kusema wale wanaojitoa hivi kwa yeye watapewa zawabu kubwa hapa duniani, na kwa wakati wa kuja. Maana ya mwisho wa shairi 30, **"katika ulimwengu unaokuja uzima wa milele"** haiko ya kwamba tunapata uzima wa milele kwa njia ya kuacha vyote, lakini ya kwamba tutaweza kufurahishwa kupita na utukufu wa mbingu. Ni kutimilizwa kwa uzima mpya ambao tulipokea siku tulipookolewa.

### K. Yesu anatabiri tena habari za kufa na ufufuko wake (18:31-34)

**18:31-33** Hii ni mara ya tatu Bwana **aliyochukua wale kumi na wawili** na kuwajulisha maneno yote moja moja ambayo yatampata (ona 9:22,44). Alisema ya kwamba mateso yake yatatimiza maneno **manabii** wa Agano la Kale **waliyoandika.** Na roho ya kutulia, na akijua yote ambayo yalikuwa mbele yake, alitabiri kwamba **atatiwa** katika mikono ya Mataifa. Tungefikiri labda atauawa kwa siri, au kutupiwa mawe katikati ya machafuko.[32] Lakini manabii

walikuwa wametabiri kwamba atatiwa kwa hila kwa mikono ya adui, ya kwamba **atazihakiwa na kutendewa jeuri na kutemewa mate,** na ilikuwa sharti kwa unabii huu kutimizwa. Atapigwa fimbo na kuuawa, lakini **siku ya tatu atafufuka.**

Sura za mwisho za Luka zinafunua matokeo aliyojua mbele na kuwaambia:

**Tunapanda kwenda Yerusalema** (18:35–19:45).

Mwana wa watu **atatiwa katika mikono ya Mataifa** (19:47–23:1).

**Atazihakiwa na kutendewa jeuri** (23:1-32).

**Watamwua** (23:33-56).

**Siku ya tatu atafufuka** (24:1-12).

**18:34** Tunashangaa kwa sababu wanafunzi **hawakufahamu maneno haya hata kidogo**, na maana ya masemo yake **imefichwa kwao.** Ni nguvu kwa sisi kutambua kwa nini walichelewa kufahamu neno hili. Labda walikuwa wakiwaza zaidi juu ya mwokozi ambaye atawafungua toka utawala wa Roma na kusimamisha ufalme mara moja, na walikataa mawazo juu ya mambo yo yote mengine ambayo yaliweza kutokea. Mara nyingi sisi watu tunaamini maneno tunayo*taka* kuamini, na tunashindana na kweli isiyopatana na *mawazo* yetu.

**L. Kipofu anaponyeshwa (18:35-43)**

**18:35-37** Bwana Yesu alikuwa ameondokea Perea sasa na kuvuka Yorodani. Luka alisema neno tunalosoma sasa lilitokea wakati **alipokuwa akikaribia Yeriko**. Matayo na Marko walisema ilitokea wakati alipo*toka* Yeriko (Mt. 20:29; Mk.10:46). Matayo alisema vilevile ya kwamba kulikuwa na vipofu wawili; Marko na Luka wanasema kulikuwa na mmoja. Labda Luka alikuwa akisema juu ya sehemu mpya ya mji, lakini Matayo na Marko walisema juu ya sehemu yake ya zamani. Au labda kulikuwa na ajabu kupita moja la kipofu akiponyeshwa na kuweza kuona tena. Tunafikiri kwamba tungalijua kupita, maneno haya yanayo*onekana* kwamba hayapatani yangalifahamika wazi.

**18:38** Kipofu masikini alitambua **Yesu** kuwa Masiya, kwani alimwita **Mwana wa Daudi**. Aliomba Bwana **kumrehemu**, maana yake kumwezesha kuona tena.

**18:39** Watu wengine walijaribu kunyamazisha kipofu, lakini alizidi **kupaza sauti** kuita Bwana. Hata kama watu hawakuweka roho juu ya kipofu masikini Bwana Yesu alimwekea roho sana.

**18:40,41** **Hivi Yesu alisimama**. Waza juu ya masemo haya ya Darby: "Siku moja Yosua aliagiza jua kusimama mbinguni, lakini hapa *Bwana* wa jua, na mwezi, na mbingu, anasimama kwa neno la kipofu masikini." Yesu aliagiza masikini **aletwe kwake**, **akamwomba** kama alitaka nini. Bila kusita masikini alisema wazi kwamba alitaka kupata **kuona**. Ombi lake lilikuwa fupi, alijua neno ambalo alitaka, na aliomba na imani.

**18:42,43** **Yesu** alimpa masikini kitu alichoomba na **mara moja** mtu huyu **alipata kuona**. Halafu **alifuata** Bwana, **akitukuza Mungu**. Habari hizi zinatufundisha kwamba tunaweza kuwa na uhodari kuamini Mungu kufanya maneno makubwa yasiyowezekana kwa watu. Imani kubwa inamheshimu sana.

John Newton aliandika,

*Unafika kwa Mfalme,*
*Umletee ombi kubwa;*
*Mwenye neema na uwezo*
*Atapenda kulijibu.*

**M. Zakayo anaokolewa (19:1-10)**

Wokovu wa Zakayo unaonyesha wazi kweli ya Luka 18:27, "Maneno yasiyowezekana na watu yanawezekana na Mungu." Zakayo alikuwa tajiri, na mara nyingi haiwezekani kwa tajiri kuingia ufalme wa Mungu. Lakini Zakayo ali-

jinyenyekeza mbele ya Mwokozi, na hakuruhusu mali yake kutenga roho yake na Mungu.

**19:1-5** Wakati Yesu **alipopita katika Yeriko** kwa safari yake ya tatu na ya mwisho kwenda Yerusalema, **Zakayo akatafuta kumwona**; bila shaka alitaka kuona tu kama yeye ni mtu wa namna gani. Hata akiwa **mkubwa wa watoza kodi**, hakuwa na haya kufanya neno lililo mbali na yale ambayo watu wanafanyaga, ili aweze kuona Mwokozi. Akiwa mtu **mfupi** alijua hataweza kumwona vizuri njiani, hivi **akatangulia mbio, akapanda juu ya mkuyu** kando ya njia pahali Yesu atakapopita. Bwana Yesu aliona tendo lake la imani. Wakati alipokaribia pahali pale **akatazama juu, akaona** Zakayo. Alimwagiza **kushuka mbio,** akisema alitaka kufikia **nyumba** ya mtoza kodi huyu. Hii ni mara ya pekee tunayosoma juu ya Mwokozi akiomba kupokewa kama mgeni ndani ya nyumba ya watu.

**19:6** Zakayo alitii agizo la Bwana, **akampokea na furaha.**

**19:7** Watu wote ambao waliona neno hili **walimnungunikia** kwa sababu aliingia **nyumba ya mwenye zambi**. Hawakufahamu au kukumbuka ya kwamba akiingia dunia namna ya dunia yetu hakuna nyumba nyingine – zote zilikuwa nyumba za wenye zambi!

**19:8** Wokovu ulikuwa umegeuza mtoza kodi huyu kabisa. Alijulisha Mwokozi ya kwamba **alikusudi kuwapa masikini nusu ya mali yake**. (Kufika wakati ule alikuwa amewanyanganyia mali yao!) Alikusudi vilevile kurudisha **mara ine** mali ambayo alijipatia kwa njia isiyokuwa haki. Hii ilipita hesabu iliyoagizwa na sheria (Kut. 22:4,7; Law. 6:5; Hes. 5:7). Kusudi la Zakayo lilionyesha ya kwamba sasa alitawaliwa na mapendo; mbele ya kuokolewa kwake alitawaliwa na choyo.

Bila shaka mbele ya wokovu wake Zakayo alikuwa amejikamatia vitu kwa njia isiyokuwa haki. Labda watu wangefikiri alikuwa akijivuna sasa juu ya ukarimu wake, na kutegemea neno hili kwa wokovu wake. Sivyo hata kidogo. Alikuwa akisema ya kwamba uzima mpya ambao alipata ndani ya Kristo ulimpa hamu kutoa malipo kwa zambi za mbele, na akiwa na asante rohoni kwa Mungu kwa wokovu wake, alitaka kutumika na mali yake kwa utukufu wa Mungu na kwa baraka ya majirani yake.

Shairi 8, kupita mashairi yote mengine ndani ya Biblia, linafundisha juu ya kutengeneza mabaya tuliyotenda mbele ya kuokolewa. Kama tuliiba mali ya mtu mbele ya kuzaliwa tena, neema ya Mungu ndani ya mwamini wa sasa itamsukuma kurudisha mali hii kwa mtu huyu.

**19:9 Yesu** alisema wazi ya kwamba **wokovu umefikia nyumba ya Zakayo,** kwa sababu alikuwa **mwana wa Abrahamu**. Wokovu haukufika kwa sababu Zakayo alizaliwa Myuda. Hapa semo hili "mwana wa Abrahamu" lina maana kubwa kupita kuzaliwa kwa mwili; linaonyesha ya kwamba Zakayo alikuwa na imani ndani ya Bwana kama Abrahamu. Vilevile wokovu haukufikia Zakayo kwa sababu ya mali aliyotoa kusaidia masikini na kwa kurudisha mali aliyoiba mbele (sh.8). Maneno haya ni *matunda* ya wokovu, si *sababu* yake.

**19:10** Bwana Yesu alijibu wale ambao walimshitaki juu ya kukaa kwake ndani ya nyumba ya mwenye zambi na kusema, **"Mwana wa watu alikuja kutafuta na kuokoa yule aliyepotea."** Ni kusema kwamba wokovu wa Zakayo ulitimiza kusudi la kuja kwa Kristo duniani.

### N. Mfano wa feza kumi (19:11-27)

**19:11** Wakati Mwokozi alipokaribia **Yerusalema** toka Yeriko, wengi wa wafuata wake walifikiri **ufalme wa Mungu utaonekana mara moja**. Ndani ya **mfano** wa feza kumi Bwana aliharibu

tumaini hili. Aliwaonyesha kwamba kutakuwa na muda nyuma ya kuja kwake mara ya kwanza na kuja kwake kwa pili, na kwamba ndani ya muda huu ilipasa wanafunzi wake kumtumikia na bidii.

**19:12,13** Habari namna ya mfano wa **mtu mwenye heshima** ndani ya mashairi haya yalitokea kweli ndani ya maisha ya Arkelao. Alichaguliwa na Herode kumkomboa, lakini watu walimkataa. Alikwenda Roma kuwekwa hakika katika kazi hii. Saa aliporudi aliwapa watumishi wake zawabu, na kuharibu adui zake.

Ndani ya mfano Bwana Yesu mwenyewe ni **mwenye heshima aliyekwenda** mbinguni kungojea wakati **atakaporudi** na kusimamisha **ufalme** wake duniani. **Watumishi kumi** ni mfano wa wanafunzi wake. Alimpa kila mtu feza moja na kumwagiza **kufanya biashara** na feza hii kufika siku atakaporudi. Watu wamepewa zawadi na uwezo kipimo mbalimbali kwa kazi ya Bwana (ona Mt. 25:14-30), lakini wao wote wanashiriki ndani ya maneno mengine, ndiyo heshima ya kutangaza Habari Njema, na kuwa wajumbe wa Kristo duniani, na ruhusa ya maombi. Bila shaka feza inasema juu ya maneno haya.

**19:14 Watu wake** ndio mfano wa taifa la Wayuda. Walimchukia, na zaidi ya ile, nyuma ya kwenda kwake walituma **wajumbe kumfuata wakisema: "Hatutaki mtu huyu kutawala juu yetu."** Labda wajumbe hawa ni mfano wa namna walivyotendea watumishi wa Kristo kama Stefano na wengine waliokufa kwa sababu ya imani yao.

**19:15** Hapa tunaona Bwana, kwa mfano, akirudi kusimamisha **ufalme** wake. Nyuma yake atafanya hesabu na **wale** ambao aliwapa **feza.**

Waamini wa wakati wa sasa watatoa hesabu ya utumishi wao kwa kiti cha hukumu cha Kristo. Neno hili litatokea mbinguni, nyuma ya kuja kwa Bwana kupeleka watu wake kwake.

Baki aminifu la Wayuda watakaoshuhudia Kristo kwa wakati wa Mateso Makubwa watahukumiwa wakati Kristo atakapokuja mara ya pili. Ni kama mashairi haya yanapasha zaidi juu ya hukumu ile.

**19:16** Mtumishi **wa kwanza** alipata **feza kumi** na feza **moja** ambayo alipewa. Alifahamu kwamba mali hii haikuwa mali yake (alisema **"feza yako"**) na alijaribu sana kutumika nayo kupatia bwana wake faida.

**19:17** Bwana alimsifu na kusema alikuwa **mwaminifu kwa neno dogo sana** – ndio ukumbusho kwamba hata wakati tunapokwisha kufanya yote tunayoweza tuko watumishi wasio na faida. Kwa zawadi yake alipewa **mamlaka juu ya miji kumi**. Ni kama zawabu kwa utumishi mwaminifu itakuwa kwa kipimo cha utumishi wa mtu huyu katika ufalme wa Kristo, na kwa kadiri ya mapendo yake, na kwa kipimo alichojitoa kwa Bwana.

**19:18,19 Mtumishi wa pili** alipata **feza tano** na feza yake moja. Atapewa **mamlaka juu ya miji mitano.**

**19:20,21** Mtu wa tatu **alikuja** na uzuru tu. Alikuwa amefunga **feza** yake **ndani ya kitambaa** na kuirudisha kwa bwana. Hakupata faida hata kidogo na feza yenyewe. Kwa nini? Ni kama alishitaki yule mtu mwenye heshima kusema yeye ni **mtu mkali** aliyetaka kupata faida bila kujisumbusha mwenyewe. Lakini masemo yake yalimhukumu mwenyewe. Kama alifikiri mtu mwenye heshima alikuwa na roho namna hii, ingalimpasa kuweka feza yake kwa wale wanaolinda feza ili aipate pamoja na faida wakati aliporudi.

**19:22** Kwa njia ya kusema tena maneno ambayo mtumishi alisema, Yesu hakukubali kwamba masemo yale yalikuwa kweli. Yalikuwa masemo ya roho

ya zambi ya mtumishi yaliyoshitaki bwana kwa uvivu wake mwenyewe. Kama mtumishi angaliamini maneno haya yeye mwenyewe, kama angalitenda namna nyingine.

**19:23** Shairi 23 linatuongoza kufikiri kwamba inatupasa kutumika sisi wenyewe na vyote tulivyo navyo kwa Bwana, au kuvitoa kwa mkono wa mtu mwingine ambaye atatumika navyo kwa Yeye.

**19:24-26** Yule mwenye heshima aliagiza **waondoshe feza ya mtumishi wa tatu, na kuileta kwa mtumishi wa kwanza aliyepata feza kumi.** Kama tusipotumika kwa Bwana wakati tunapoweza, hatutapewa njia kufanya hivi tena nyuma. Lakini tukiwa waaminifu na kufanya yale tunayoweza, hata kama ni kazi ndogo tu, Mungu hatakosa kamwe kutupatia vitu tunavyohitaji kumtumikia hata kupita. Labda unafikiri si haki kuleta **feza** ile kwa mtu aliyekuwa na feza **kumi**, lakini ni kawaida ya asili isiyoweza kugeuka ya kwamba kwa maneno ya Roho, wale wanaopenda Bwana sana sana na kumtumikia na bidii kabisa watakaa kupewa njia kumtumikia hata kupita. Lakini tukikosa kufanya kazi ambayo tunagawiwa, yote itaondolewa kwetu.

Yule mtumishi wa tatu alipoteza zawabu yake, lakini hakuazibiwa kwa njia nyingine. Ni kama hakupoteza wokovu wake.

**19:27** Wenyeji wa inchi waliokataa kwa mtu mwenye heshima yule kuwatawala wanaitwa adui, na kuhukumiwa kufa. Ni unabii wa huzuni wa mwisho wa taabu wa taifa waliokataa Masiya.

### 10. MWANA WA WATU KATIKA YERUSALEMA (19:28–21:38)

#### A. Kuingia Yerusalema na shangwe (19:28-40)

**19:28-34** Ilikuwa sasa siku ya kwanza ya juma lililotangulia kusulibishwa kwa Yesu. Alikuwa amekaribia mtelemuko wa mashariki wa kilima cha Zeituni kwa njia kwenda **Yerusalema. Wakati alipokaribia Betefage na Betania . . . alituma wawili wa wanafunzi wake** kwa **kijiji** mbele yake kukamata **mwanapunda** aweze kutembea juu yake kuingia Yerusalema. Alijulisha wanafunzi pahali watakapopata nyama yule, na kama **wenye nyama** watasema nini. Wakati wanafunzi walipokwisha kueleza neno walilotaka, wenye nyama yule walikuwa tayari kuwapa mwanapunda yao kusudi Yesu aweze kutumika naye. Labda walikuwa wamebarikiwa mbele kwa njia ya utumishi wa Bwana, na kusema watafurahi kumsaidia wakati wo wote.

**19:35-38** Wanafunzi waliweka **mavazi yao wenyewe juu ya mwanapunda ili Bwana aweze kukaa juu yake. Watu wengi walitandika nguo zao njiani** mbele yake wakati alipopanda kilima cha Zeituni toka upande wake wa chini wa mangaribi kwenda Yerusalema. Halafu wafuata wake wote wakaanza kufurahi na kusifu Mungu kwa **sauti kubwa juu ya maajabu yote ambayo waliona mbele**. Walimwita **Mfalme** wa Mungu, wakaimba kwamba mwisho wa kuja kwake ulikuwa **salama katika mbingu na utukufu pahali pa juu.** Ona ya kwamba waliimba **"Salama katika mbingu,"** si "Salama katika dunia." Salama haikuweza kuwa duniani kwa sababu Mkubwa wa Salama alikuwa amekataliwa na atauawa nyuma kidogo. Lakini kutakuwa na **salama mbinguni** kwa sababu ya ukaribu wa mauti ya Kristo juu ya msalaba wa Kalvari na kupanda kwake mbinguni.

**19:39,40 Wafarisayo** hawakufurahi hata kidogo kwa Yesu kupata heshima hivi mbele ya watu wengi. Walisema naye vizuri **ahamakie wanafunzi wake**. Lakini Yesu **alijibu** ya kuwa hakuna njia

kuepuka sifa ya namna hii. **Kama** wanafunzi wasipomsifu, atapata sifa **toka mawe**! Hivi alihamakia Wafarisayo kwani walikuwa wenye mioyo migumu kupita mawe yasiyokuwa na uzima.

**B. Mwana wa watu anatoa machozi juu ya Yerusalema (19:41-44)**

**19:41,42** Wakati Yesu **alipokaribia** Yerusalema, aliombolezea **mji huu** ambao hawakumpokea kama Masiya wao. Wangalipata **salama** kama wangalimpokea kama Masiya. Lakini hawakuweza kufanya hivi tena sasa. Walikuwa wamechagua nini watafanya na Mwana wa Mungu. Walikuwa **vipofu** kwa sababu walikuwa wamemkataa. Hawaku*taka* kumwona, hivi hawaku*weza* kumwona tena.

Waza kwanza juu ya ajabu ya machozi ya Mwokozi. Kama W. H. Griffith Thomas alivyosema, "Tuketi kwa miguu ya Yesu kufika saa tunapojifunza siri ya machozi yake, halafu tukitazama zambi na huzuni za mji, na inchi kando kando, tutatoa machozi vilevile."[33]

**19:43,44** Yesu alionyesha kwa ufupi namna jemadari ya Waroma, jina lake Tito **atakavyozunguka** Yerusalema kwa wakati wa kuja, kufunga wenyeji wake ndani bila njia ya kukimbia, kuwaua wote, vijana na wazee, na **kuangush**a kuta na nyumba zote. **Hata jiwe moja** halitabaki **juu ya lingine kwa sababu** Yerusalema **haukujua wakati Mungu alipokuja kwake**. Bwana Yesu alikuwa amefikia mji na kuwapa njia kupata wokovu, lakini watu hawakumtaka.

**C. Hekalu linasafishwa mara ya pili (19:45,46)**

Yesu alikuwa amesafisha **hekalu** mbele wakati alipoanza utumishi wake katikati ya watu (Yoane 2:14-17). Sasa wakati alipokuwa akifikia mwisho wa utumishi huu aliingia hekalu tena na **kufukuza** watu wale waliokuwa wakigeuza **nyumba ya maombi** kuwa **pango la wanyanganyi.** Hata kwa wakati wa sasa ni hatari kuchanganya biashara na maneno ya Mungu. Wakristo wanatumia njia mbalimbali zilizo kama chachu kupata mali kwa kanisa: kuhubiri kwa kupokea faida, vivi hivi – wanafanya maneno haya yote kwa Jina la Kristo!

Kristo alitaja mashairi toka Agano la Kale (Isaya 56:7 na Yeremia 7:11) kuonyesha haki ya maneno aliyokuwa akifanya. Ni sharti kwa maneno yote ambayo tunataka kufanya kutengeneza maneno ya kanisa yajengwe juu ya Neno la Mungu.

**D. Mafundisho kila siku hekaluni (19:47,48)**

**Yesu alikuwa akifundisha kila siku** kwa kiwanja cha hekalu, pahali watu wote walipoweza kufika. Viongozi vya dini walitaka sana kupata njia kumshitaki kusudi waweze **kumharibu**, lakini **watu** waliweka roho sana kusikia yule Mnazareti mwenye kufanya maajabu. Saa yake ilikuwa haijafika bado. **Lakin**i ilikuwa karibu, na halafu **wakubwa wa makuhani, waandishi** na Wafarisayo wataweza kufanya neno walilotaka.

Siku ya pili ya juma ilikuwa imefika sasa. Kesho yake, siku ya tatu, ilikuwa siku ya mwisho ya mafundisho ya Yesu kwa watu. Tunasoma juu yake katika 20:1–22:6.

**E. Mabishano juu ya mamlaka (20:1-8)**

**20:1,2** Mashairi haya yanatuonyesha Bwana akitangaza Habari Njema bila kuchoka kwa **hekalu,** na viongozi katika Israeli wakifanya shauri na jeuri kushindana kama nani alimpa ruhusa kufundisha. Kwa macho yao Yesu alikuwa mseremala bure wa Nazareti tu asiyejifunza ndani ya darasa za kujulikana na kupokea cheo ya elimu. Basi **nani alimpa mamlaka** kufundisha na kuhubiri kwa watu wengine na kusafisha hekalu? Walitaka kujua!

**20:3-8** Yesu **alijibu** kwa njia ya kuwauliza neno moja; kama wangalijibu vizuri kama wangalipokea jibu kwa ulizo lao. Ni Mungu aliyekubali **ubatizo wa Yoane,** au alibatiza na mamlaka ya watu tu? Kama wangalikubali kwamba Yoane alihubiri na ruhusa toka Mungu, basi kwa sababu gani hawakutii mahubiri yake na kupokea Masiya ambaye alitabiri juu yake? Lakini kama walisema Yoane alikuwa mhubiri tu namna ya wahubiri wengine wa dunia, makutano watakasirika sana, kwani walikaa kuheshimu **Yoane** kama **nabii** toka Mungu. Hivi **walijibu,** "Hatujui **pahali anapotoka.**" Yesu alisema, *"Kama ni hivi, mimi vilevile sitawaambia ninyi kama nikifundisha na mamlaka ya nani."* Kama hawakuweza kusema maneno haya machache tu juu ya Yoane, kwa nini basi walikuwa na shaka juu ya mamlaka ya Yule aliyekuwa mkubwa kupita Yoane? Mashairi haya yanaonyesha ya kwamba neno kubwa moja mwenye kufundisha Neno la Mungu analohitaji ni kujazwa Roho Mtakatifu. Mtu huyu anaweza kushinda wale waliojifunza ndani ya darasa na universités za dunia tu na kupokea cheo cha elimu.

Hata leo watu wanakaa kuuliza, "Ulijifunza wapi na kupokea cheo cha elimu? Nani alikutia mkono na kukuweka kwa kazi ya Mungu?" Labda watu wanauliza hivi wakisukumwa na wivu juu ya mhubiri anayetangaza Habari Njema kwa uwezo wa Mungu, bila kupata kwanza mafundisho na elimu katika université.

### F. Mfano wa walimaji waovu (20:9-18)

**20:9-12** Mapendo makubwa moyoni mwa Mungu unaonekana wazi tena ndani ya mfano huu. Mungu ndiye **aliyekopesha shamba la mizabibu** (Israeli) kwa **walimaji** (viongozi vya taifa lile – ona Isa. 5:1-7). Alituma watumishi wake karibu na **walimaji** wa shamba la mizabibu kupata **nusu ya matunda** kwa yeye mwenyewe. Watumishi hawa walikuwa manabii wa Mungu, kama Isaya na Yoane Mbatizaji, waliojaribu kuita Israeli kutubu na kuamini. Lakini watawala wa Israeli walitesa manabii kila mara.

**20:13** Mwishoni Mungu alituma **Mwana wake mpendwa** akifikiri ya kwamba bila shaka **watamheshimu yeye** (lakini Mungu alijua ya kwamba Kristo atakataliwa). Ona ya kwamba alionyesha tofauti katikati yake na wengine wote. Wao walikuwa watumishi; yeye alikuwa Mwana.

**20:14** Kama ilivyokuwa desturi yao, **walimaji** shamba la mizabibu walikusudi kuondosha **mriti** katikati yao. Wao wenyewe tu walitaka kuwa viongozi na walimu wa watu – **"ili uriti upate kuwa wetu."** Walikataa kunyenyekea Yesu na kuachana na heshima yao kama viongozi vya dini. Walifikiri kama wakimwua watakuwa na amri juu ya Israeli peke yao.

**20:15-17** Hivi **walimtupa inje ya shamba la mizabibu, wakamwua**. Halafu Yesu aliuliza wasikiaji wake Wayuda kama **mwenye shamba la mizabibu** atatendea **walimaji** waovu namna gani. Ndani ya Matayo, wakubwa wa makuhani na wazee walijihukumu wenyewe wakati walipojibu atawaua (Mt. 21:41). Hapa katika Luka Bwana mwenyewe alitoa jibu, **"Atakuja na kuangamiza hawa walimaji, na lile shamba la mizabibu atawapa wengine."** Maana yake ilikuwa ya kwamba Wayuda wale waliokataa Kristo wataharibiwa, na Mungu atawapa **wengine** pahali pao pa heshima. Labda wale "wengine" ni watu wa Mataifa au Wayuda waliozaliwa tena kwa wakati wa mwisho. Wayuda walishituka sana juu ya mawazo namna hii. Walisema, **"Hapana, hata kidogo."** Bwana alitaja Zaburi 118:22 kuthibitisha unabii huu.

**Wajengaji** Wayuda walikuwa **wamekataa** Kristo, **Jiwe.** Hawakuwa na nafasi kwaye ndani ya mashauri yao. Lakini lilikuwa kusudi la Mungu kwa Kristo kuwa na pahali pa kwanza, pa juu na heshima zaidi, hivi alimweka kuwa **jiwe kubwa la pembeni**, jiwe linalohitajiwa sana na lililo katika pahali pa heshima zaidi.

**20:18** Ndani ya shairi 18 tunasoma juu ya kuja kwa Kristo mara mbili: Kwa kuja kwake kwa kwanza tunamwona kama **jiwe** juu ya udongo; watu walikwalishwa na aibu na unyenyekevu kwake na **walivunjikavunjika** kwa sababu **walimkataa**. Ndani ya sehemu ya pili ya shairi hili, tunaona jiwe likianguka chini toka mbingu na kusagasaga wasioamini kuwa **uvumbi.** [34]

### G. Kutoa mali kwa Kaisari na kwa Mungu (20:19-26)

**20:19,20 Wakubwa wa makuhani na waandishi** walifahamu kwamba Yesu alisema mfano ule **juu yao**, wakataka sanasana **kumkamata. Walituma wapelelezi** kumnasa ndani ya masemo yake kusudi wapate njia kumfunga na kumshitaki kwa **liwali** Mroma. Wapelelezi hawa walianza na kumsifu na kusema yeye ni mwaminifu, mwenye kusema maneno ya Mungu bila kuogopa watu. Walitaraji kwamba atasema neno baya juu ya Kaisari.

**20:21,22** Halafu walimwuliza kama ni vizuri kwa Myuda **kulipa kodi kwa Kaisari.** Kama Yesu akisema sivyo, jibu hili litawapa njia kumshitaki na maasi na kumfikisha kwa Waroma ahukumiwe. Kama akijibu ndiyo, atakasirisha Waherodia (na zaidi ya Wayuda).

**20:23,24** Yesu alifahamu kwamba walimwekea mtego. Aliomba apewe **dinari**; labda hakuwa na dinari hata moja yeye mwenyewe. Kwa njia ya kuwa na dinari na kutumika nazo Wayuda walionyesha ya kwamba walitawaliwa na Mataifa. Halafu aliwauliza, **"Ina sura ya nani, na maandiko ya nani?"** Walikubali kujibu "**Ya Kaisari**."

**20:25,26** Halafu Yesu aliwanyamazisha na agizo hili, **"Mumpe Kaisari vitu vya Kaisari, na Mungu vitu vya Mungu."** Ilionekana wazi ya kwamba waliweka roho juu ya kupatia Kaisari faida kupita kuleta faida kwa Mungu. "Mali ilikuwa ya Kaisari, na ninyi ni mali ya Mungu. Watu wa dunia wapewe dinari zao basi, lakini Mungu apate viumbe vyake." Ni nyepesi sana kubishana juu ya maneno madogo na kusahau maneno makubwa na ya kwanza ndani ya maisha yetu. Na ni nyepesi vilevile kulipa deni zetu kwa wenzetu pamoja na kuibia Mungu yaliyo yake.

### H. Wasadukayo na fumbo yao juu ya ufufuko (20:27-44)

**20:27** Basi mtego wa mbele wa wakubwa ulikufa bure, hivi sasa **Wasadukayo walifika kwake** na ulizo juu ya dini. Hawakuamini ya kwamba wafu watafufuliwa tena kamwe, hivi walijaribu kwa njia ya mfano wa neno lisilowezekana, kufanyiza mafundisho **ya ufufuko** kuonekana kama kitu cha kuchekesha.

**20:28-33** Walikumbusha Yesu ya kwamba katika Sheria ya **Mus**a ilipasa mwanamume asiyekuwa na mke kuoa mjane wa ndugu yake kwa kulinda jina na vitu vya jamaa (Tor. 25:5). Walipasha habari za mwanamke mmoja aliyeolewa kwa **ndugu saba**, mmoja nyuma ya mwingine. Hata wakati wa kufa kwa ndugu ya saba mwanamke **hakuwa na mtoto**. Mwishoni yeye **alikufa vilevile**. Walitaka kujua kwamba **katika ufufuko atakuwa mke wa nani?** Walifikiri walikuwa watu wa akili kabisa kutunga ulizo namna hii usioweza kupata jibu!

**20:34 Yesu alijibu** ya kwamba maneno ya ndoa yalikuwa kwa maisha ya **sasa tu**; hayataendelea mbinguni. Hakusema ya

kwamba waume na wake hawatatambuana mbinguni, lakini kukaa kwao pamoja kutakuwa namna nyingine kabisa.

**20:35** Maana ya semo, "**wale wanaohesabiwa kuwa wamestahili kufikia wakati ule utakaokuja"** si kwamba watu hawa walikuwa wamejistahilisha wenyewe kwa kuweza kufika mbinguni; wenye zambi wanaweza kupata ustahili kwa njia ya Mmoja tu, ndiye Kristo. "Wale tu wanahesabiwa kuwa wanastahili ndio wale ambao wanajihukumu wenyewe, wanaothibitisha haki ya Kristo, na wanaokiri kwamba Yeye tu anastahili."[35`] Semo hili **kufufuka toka wafu** ni juu ya ufufuko wa waamini tu. Kabisa kabisa maana yenyewe ni **ufufuko toka kati ya wafu**. Hatusomi ndani ya Biblia ya kwamba wafu wote, waliookolewa na wapotevu, watafufuliwa pamoja.

**20:36** Ndani ya shairi hili tunaona uzuri wa kupita wa maneno ya mbinguni. Hakuna mauti tena; kwa njia hii watu watakuwa **sawasawa na malaika.** Wataonekana vilevile kama **wana wa Mungu.** Waamini ni wana wa Mungu hata sasa, lakini hawaonekani kuwa hivi. Mbinguni watafunuliwa kuonekana wazi kama wana wa Mungu. Tunajua neno hili kwa sababu walishiriki ndani ya ufufuko wa kwanza. "Wakati atakapoonekana tutafanana naye kwa maana tutamwona kama alivyo" (1 Yoane 3:2) "Wakati Kristo, aliye uzima wetu atakapofunuliwa, ninyi vilevile mtafunuliwa pamoja naye katika utukufu" (Kol. 3:4).

**20:37,38** Kwa kuhakikisha kweli ya ufufuko, Yesu alitaja habari za Kutoka 3:6 pahali **Musa** aliposema juu ya **Mungu** akijiita **Mungu wa Abrahamu … Isaka, na … Yakobo**. Basi, Wasadukayo wangalifikiri tu, wangalifahamu ya kwamba (1) Mungu **si Mungu wa wafu lakini wa walio hai**. (2) **Abrahamu, Isaka, na Yakobo** walikuwa wamekufa. Hivi ni wazi ya kwamba Mungu atawafufua. Bwana hakusema, "Ni*li*kuwa Mungu wa Abrahamu, lakini "Mimi *ni* …". Mungu akiwa Mungu wa walio hai, yeye ni Mungu wa ufufuko vilevile.

**20:39-44 Wengine wa waandishi** walikubali masemo haya ya Yesu. Lakini Yesu hakumaliza masemo yake kwanza. Alisoma Zaburi 110:1, pahali **Daudi** aliita Masiya **Bwana** wake. Wayuda waliamini kwamba Masiya atakuwa **Mwana** wa **Daudi**. Basi namna gani aliweza kuwa **Bwana** wa Daudi na **Mwana** wake vilevile? Jibu la ulizo hili ni Bwana Yesu mwenyewe. Alikuwa Mzao wa Daudi kama Mwana wa watu; alikuwa Mwumba wa Daudi vilevile. Lakini walikuwa vipofu hata iliwashinda kufahamu maneno haya.

### I. Maonyo juu ya waandishi (20:45-47)

**Halafu** Yesu alionya makutano waziwazi wawe na ange kwa maneno ya **waandishi.** Walivaa **mavazi marefu** waonekane kama watu wa Mungu. Walipenda kuitwa majina ya heshima katika **masoko.** Walijipatia **pahali pa heshima** katika **masunagogi** na pahali pa karamu. Lakini walinyanganya mali ya wajane wasioweza kujisimamia, wakifunika uovu wao na **maombi marefu**. Watahukumiwa zaidi kwa udanganyifu wao.

### J. Sengi mbili za mjane (21:1-4)

Wakati Yesu alipoangalia **wenye mali wakiweka zawadi zao ndani ya sanduku ya hazina ya hekalu,** alishangaa juu ya tofauti katika **wenye mali** na yule **mjane huyu masikini**. Wao walitoa nusu ya mali yao, lakini mjane alitoa **yote**. Kwa mafikiri ya Mungu alitoa **kupita mali yote** ambayo watu wale wengine waliyotoa. Wao walitoa **toka mali iliyozidi kwao**; mjane **katika uhitaji wake** alitoa **yote**

**aliyokuwa nayo**. Zawadi watu wanazotoa kwa sababu hawahitaji mali yenyewe haziheshimu Bwana, lakini zawadi za wale ambao wanajinyima wenyewe kwa kuweza kuzitoa ni za damani sana kwa macho ya Bwana.

### K. Maneno yatakayotokea kwa wakati wa kuja (21:5-11)

Mashairi 5-33 ni hotuba kubwa ya unabii. Inafanana na ile kwa Matayo 24 na 25, lakini si ndani ya maneno yote. Tunahitaji kujikumbusha tena na tena ya kwamba kuna sababu kwa tofauti katikati ya vitabu vya Habari Njema.

Ndani ya hotuba hii Bwana alisema juu ya uharibifu wa Yerusalema katika 70 A.D., na vilevile juu ya maneno yatakayotangulia kuja kwake kwa pili. *Sehemu* ya unabii huu *ilitimizwa* wakati Tito alipozunguka Yerusalema kwa vita, lakini *utatimizwa kabisa* kwa vita kwa mwisho wa muda wa Mateso Makubwa.

Ni kama habari za hotuba hii zinafuatana hivi:

1. Yesu alitabiri ya kwamba Yerusalema utaharibiwa (mash.5,6).
2. Wanafunzi waliuliza kama maneno haya yatatokea wakati gani (sh.7).
3. Yesu alitoa habari za maneno yatakayotangulia kuja kwake mara ya pili (mash. 8-11).
4. Halafu alipasha juu ya kuangamizwa kwa Yerusalema na muda utakaofuata (mash.12-24).
5. Mwishoni alipasha juu ya alama zitakazotangulia kuja kwake kwa pili, na alionya wafuata wake waishi wakitazamia kuja kwake (mash. 25-26).

**21:5,6** Watu **wengine** walisema juu ya uzuri na mapambo ya **hekalu** la Herode, lakini Yesu aliwaonya wasiweke roho juu ya **vitu** hivi vya dunia vitakavyopita nyuma kidogo. Katika **siku zitakazokuja** hekalu litabomolewa kabisa.

**21:7** Wafuata walitaka kujua mara moja **wakati gani** maneno haya yatakapotokea, na **alama gani** itaonyesha ya kwamba yalikuwa karibu. Bila shaka waliwaza juu ya uharibifu wa Yerusalema.

**21:8-11** Ni kama kwanza jibu la Mwokozi lilipeleka mawazo yao hata mwisho wa muda ule wakati hekalu litakapoharibiwa tena mbele ya kusimamishwa kwa ufalme. Kutakuwa na masiya za uwongo na habari za **vita** na fitina. Zaidi ya vita katikati ya mataifa kutakuwa na maneno mabaya kama **matetemeko makubwa ya dunia, na njaa, na tauni pahali mbalimbali, maogopesho, na alama kubwa toka mbingu.**

### L. Muda mbele ya mwisho (21:12-19)

**21:12-15** Ndani ya mashairi yaliyotangulia, Yesu alipasha juu ya maneno yatakayotokea mbele ya mwisho wa muda ule. Shairi 12 linaanza na maneno haya **"Lakini mbele ya maneno haya yote…"** Hivi tunafikiri ya kwamba mashairi 12-24 yanapasha juu ya muda toka wakati wa hotuba ile, kufika muda wa Mateso ya kuja. Wanafunzi wake watafungwa, watateswa, watasimama mbele ya wakubwa wa serikali na wa dini kuhukumiwa, na kufungwa gerezani. Labda watafikiri kwamba itakuwa taabu na kuharibika kwa ushuhuda wao, lakini Bwana atakuwa juu ya maneno haya yote na kuyafanyiza kuwa **ushuhuda** kwa utukufu wake. Haifai wafikiri mbele kama watajibu nini kujisimamia kwa siku ile ya hatari. Mungu atawapa **akili** saa yenyewe kusema maneno yale yatakayofunga vinywa vya **adui** zao.

**21:16-18** Kutakuwa na udanganyifu ndani ya jamaa, **ndugu** wasioamini watatoa Wakristo kwa adui, na **wengine** watauawa kwa sababu ya kusimama imara kwa Kristo. Labda unafikiri shairi 16, **"wengine wenu watawaua,"** na shairi 18 pahali tunaposoma, **"Lakini unyole wa vichwa vyenu hautapotea hata mmoja"** hayapatani, lakini maana

ya mashairi haya ni moja tu: Hata wengine watauawa kwa sababu ya imani yao, watalindwa kabisa kabisa kwa maneno ya roho.

**21:19** Shairi 19 linaonyesha kwamba wale wanaovumilia taabu na saburi kwa ajili ya Kristo wanahakikisha kwamba waliokolewa kweli. Waamini wa kweli watasimama imara kwa Bwana, si neno kama ikiwapasa kuvumilia taabu ya kipimo gani.

### M. Uharibifu wa Yerusalema (21:20-24)

Sasa Bwana alionyesha maneno mengine juu ya uharibifu wa **Yerusalema** kwa mwaka 70 A.D. Kwa wakati ule mji **utazungukwa** na jeshi la Waroma.

> Wakristo wa wakati ule – mwaka 70 A.D., walipewa alama kuwaonyesha uharibifu wa Yerusalema na maangamizo ya hekalu yalikuwa karibu. "Wakati munapoona Yerusalema umezungukwa na jeshi, jueni uharibifu wake ni karibu." Waliagizwa kukimbia wakati walipoona alama hii. Labda wenye kutokuamini waliweza kusema wataweza kukimbia namna gani wakati jeshi la adui walipozunguka mji, lakini neno la Mungu ni kweli kila mara. Jemadari la Waroma aliondoa jeshi lake kwa muda mfupi, na Wayuda wenye imani walipata njia kukimbia, wakakwenda kwa pahali palipoitwa Pella na walipona. [36]

Watu wangalijaribu kuingia mji tena wangalikufa. Mji utakuwa karibu kuhukumiwa kwa sababu wenyeji wake walikuwa wamekataa Mwana wa Mungu. Itakuwa taabu zaidi kwa wanawake **wenye mimba** na mama wenye watoto wadogo **wa kunyonya** kukimbia na kuepuka hukumu ya Mungu juu ya **inchi** ya Israeli na juu ya **Wayuda**. Wengi wao watauawa na wale watakaopona watapelekwa kwa inchi nyingine kama wafungwa.

Sehemu ya mwisho ya shairi 24 ni unabii wa kushangaza juu ya **Yerusalema** wa zamani ya kwamba mji ule utatawaliwa na Mataifa kufika **kutimizwa kwa nyakati za Mataifa.** Si kusema ya kwamba kwa muda nyingine Wayuda hawatatawala Yerusalema, lakini ya kwamba kwa muda ule Mataifa watakaa kuingia Yerusalema na kuleta vizuizi.

Ndani ya Agano Jipya tunasoma juu ya mali ya Mataifa, juu ya kutimizwa kwa Mataifa, na juu ya nyakati za Mataifa.

*Mali* ya Mataifa (Rom.11:12) inasema juu ya hali ya baraka ya Mataifa sasa wakati Mungu alipoweka Wayuda kando kwa wakati.

*Utimilifu* wa Mataifa (Rom. 11:25) ni wakati bibi arusi ya Kristo ya Mataifa itakapotimizwa na kupelekwa toka duniani, na wakati Mungu atakapoanza kutumika na Israeli tena.

Kabisa kabisa *nyakati* za Mataifa (Luka 21:24) zilianza wakati Wayuda walipopelekwa kwa Babeli kama wafungwa kwa 521 B.C. na zitaendelea kufika wakati Mataifa hawatakuwa na amri juu ya Yerusalema tena.

Tangu wakati Mwokozi aliposema maneno haya, Yerusalema umekuwa zaidi chini ya amri ya Mataifa. Mfalme Julian aliyekana dini (331-363 A.D.) alijaribu kuonyesha kwamba Ukristo ni uwongo kwa njia ya kuhakikisha kwamba unabii huu wa Bwana si kweli. Neno hili lilisukuma Wayuda kujenga hekalu tena. Walianza kazi hii na furaha, wakitumika hata na majembe ya feza kwa kuchimba, na wakibeba udongo ndani ya shela za rangi ya zambarau. Lakini walilazimishwa kuacha kazi hii kwa sababu ya tetemeko la inchi na vitu vya kuviringana vya moto vilivyotoka katika udongo.[37]

### N. Kuja kwa pili (21:25-28)

Mashairi haya yanaonyesha mapinduko makubwa ya mambo duniani

yatakayotokea mbele ya kuja kwa Kristo mara ya pili. Kutakuwa na maneno ya kuogopesha mbinguni vilevile, na kuhamishwa kwa **jua … mwezi na nyota** ambayo watu wataweza kuona toka dunia. Wataogopa sana sana, lakini kuna tumaini kwa wale wanaopenda Mungu:

> **Wataona Mwana wa watu akikuja katika wingu pamoja na uwezo na utukufu mkubwa. Wakati maneno haya yanapoanza kuja, tazameni juu, munyanyue vichwa vyenu kwa sababu ukombozi wenu umekaribia.**

### O. Mtini na miti yote (21:29-33)

**21:29-31** Alama nyingine inayoonyesha ukaribu wa kurudi kwa Bwana ni **kuchipuka** kwa **mtini na miti yote. Mtini** ni mfano mzuri wa taifa la Israeli; litaonyesha alama za uzima mpya kwa siku za mwisho. Kwa mia za miaka Waisraeli walisambazwa na kufichwa katikati ya mataifa, lakini kwa mwaka 1948, taifa la Israeli lilisimamishwa tena na kukubaliwa katikati ya jamaa ya mataifa.

Labda kuchipuka kwa miti mingine ni mfano wa kuongezeka kwa serikali mpya ndani ya inchi mpya nyingi zinazoonekana duniani. Maana ya alama hizi ni ya kwamba ufalme wa utukufu wa Kristo utasimamishwa nyuma kidogo.

**21:32** Yesu alisema ya kwamba **kizazi hiki hakitapita hata maneno haya yote yatakapotimia.** Lakini maana ya “kizazi hiki” ni nini?

1. Watu wengine wanafikiri alisema juu ya kizazi kilichoishi kwa wakati Bwana aliposema maneno haya, na ya kwamba maneno yote yalitimizwa wakati wa uharibifu wa Yerusalema. Lakini neno hili si kweli kwa sababu Kristo hakurudi kwa wakati ule katika wingu pamoja na uwezo na utukufu mkubwa.

2. Wengine wanaamini ya kwamba “kizazi hiki” kinasema juu ya wale watakaoishi kwa wakati alama hizi zitakazoanza kutokea wakati Kristo atakaporudi. Maneno yote yaliyotabiriwa yatatokea kwa muda wa kizazi kimoja.

3. Watu wengine wanafikiri kwamba “kizazi hiki” kinasema juu ya Wayuda wenye uadui kwa Kristo. Bwana alikuwa akisema kwamba taifa la Wayuda watapona, wamesambazwa bila kuharibiwa, na ya kwamba roho yao ya uadui kwa Kristo haitageuka kwa mia za miaka. Labda maelezo 2 na 3 yote ni mazuri.

**21:33** Mbingu na dunia za sasa zita**pita,** lakini maneno Bwana Yesu aliyotabiri yatatimizwa pia.

### P. Maonyo kutazama na kuomba (21:34-38)

**21:34,35** Lakini sharti wanafunzi wakae na ange, wasiweke roho na saa zaidi juu ya maneno kama kula na kunywa na mahitaji mengine ya kila siku, ili siku ya kuja kwa Bwana isije kwa **gafula** saa wasioitazamia. Itafikia hivi **wote wanaofikiri dunia** ni kao lao la daima.

**21:36** Wanafunzi wa kweli wanapaswa **kutazamia** kila wakati **pamoja na maombi** na kujitenga na wazalimu wa dunia hii ambao watamwangiwa gazabu ya Mungu. Wao watakubaliwa na **kusimama mbele ya Mwana wa watu.**

**21:37,38** Bwana alifundisha kila siku hekaluni, **lakini usiku alilala** kwa kilima kinachoitwa Zeituni, bila nyumba ndani ya dunia hii ambayo aliumba. Halafu **asubui mapema watu wote** walimzunguka tena **kumsikiliza.**

## 11. MAUMIVU MAKALI YA MWANA WA WATU NA MAUTI YAKE (Sura 22,23)

### A. Shauri kuua Yesu (22:1,2)

**22:1** Hapa **Karamu ya Mkate usiotiwa chachu** inasema juu ya muda unaoanza na **Pasaka** na kuendelea kwa siku saba nyingine wakati watu walipokula mkate pasipo chachu. Pasaka

ilikuwa kwa siku ya kumi na ine ya mwezi Nisan, ndio mwezi wa kwanza wa mwaka kwa Wayuda. Siku saba toka siku ya kumi na tano kufika siku ya makumi mbili na moja zilijulikana kama **Karamu ya Mkate Usiotiwa Chachu,** lakini ndani ya shairi la kwanza la sura hii, jina hili linasema juu ya karamu zima. Kama Luka angaliandika zaidi kwa Wayuda, kama asingalihitaji kueleza mwunganisho wa **Karamu ya Mkate Usiotiwa Chachu** na **Pasaka.**

**22:2 Wakubwa wa makuhani na waandishi** walikaa kufanya shauri **namna gani waliweza kuua** Bwana Yesu, lakini walifahamu kwamba iliwapasa kufanya hivi bila kuleta machafuko katikati ya watu, kwa **sababu waliogopa watu,** kwani wengi wao walikaa kuheshimu Bwana Yesu sana.

**B. Udanganyifu wa Yuda (22:3-6)**

**22:3 Shetani aliingia Yuda aliyeitwa Iskariota,** mmoja wa wanafunzi **kumi na wawili**. Ndani ya Yoane 13:27 tunasoma ya kwamba neno hili lilifanyikana wakati Yesu alipokwisha kumpa kipande cha mkate saa ya karamu ya Pasaka. Labda Luka alitaka kusema tu ya kwamba neno hili lilitokea, bila kuonyesha kama ilikuwa saa gani.

**22:4-6** Basi Yuda alipigania bei na **wakubwa wa makuhani na wakubwa wa askari** (ndio wakubwa wa walinzi wa hekalu). Alikuwa ametayarisha njia **kutoa** Yesu katika mikono yao bila kuanza machafuko katikati ya watu. Walikubali shauri lake na walisema **watamlipa feza** – vipande makumi tatu vya feza, kama tunavyosoma pahali pengine. Hivi Yuda alikwenda zake kutimiza shauri lake.

**C. Matayarisho kwa Pasaka (22:7-13)**

**22:7** Ni nguvu kupatanisha saa zote zinazotajwa ndani ya mashairi haya. Tungefikiri **Siku Kubwa ya Mkate Usiotiwa Chachu** itakuwa siku ya kumi na tatu ya Nisan, saa ilipopasa Wayuda kuondosha nyumbani mwao mikate yote yenye chachu. Lakini hapa katika Luka tunasoma ilikuwa **siku ilipowapasa kutoa sadaka ya Pasaka,** ndiyo siku ya kumi na ine ya Nisan. Leon Morris, pamoja na wenye elimu wengine, wanafikiri watu walitumika na calendriers namna mbili, moja ambayo watu wote walitumika nayo, na nyingine ambayo Yesu na watu wengine walitumika nayo.[38] Tunafikiri ya kwamba matukio ya siku ya kazi ine ya mwisho yalianza hapa na kuendelea kufika shairi 53.

**22:8-10** Bwana alituma **Petro na Yoane** kuingia Yerusalema kutengeneza karamu ya **Pasak**a. Maagizo yake yalionyesha kwamba alijua maneno yote ambayo watakuta. Nyuma ya kuingia **mjini watakutana na mwanamume akibeba mtungi wa maji.** Lilikuwa ono la kushangaza kwa sababu ilikuwa desturi ya wanawake kubeba mitungi ya maji ndani ya miji ile ya inchi za mashariki. Mwanamume ni mfano mzuri wa Roho Mtakatifu, anayeongoza wenye hamu ya roho kwa pahali pa ushirika na Bwana.

**22:11-13** Ndiyo, Bwana alijua pahali mtu huyu atakapotembea, na alijua vilevile kwamba mwenye nyumba fulani atampa yeye na wanafunzi wake ruhusa kutumika na **chumba chake kikubwa cha juu kilichopambwa.** Labda mtu huyu alijuana na Bwana na alikuwa amejitoa mzima pamoja na vitu vyake vyote kwa Yeye. Chumba hiki cha mwenye nyumba kilikuwa kizuri kupita chumba ambacho wanafunzi walifikiri watakuta. Wakati Yesu alipozaliwa katika Betelehemu, nafasi haikuwa kwa yeye ndani ya nyumba ya wageni. Sasa Bwana aliagiza wanafunzi wake kuomba ruhusa kutumika na **chumba cha wageni**, lakini walipewa chumba kizuri kupita – **chumba**

**kikubwa cha juu kilichopambwa.**

Wanafunzi walikuta kila neno namna Bwana alivyosema, **wakatayarisha Pasaka.**

### D. Pasaka ya Mwisho (22:14-18)

**22:14** Kwa mia za miaka Wayuda walikula Pasaka kukumbuka ajabu ya wokovu wao toka Misri na mauti, kwa njia ya damu ya mwana-kondoo mkamilifu. Bila shaka ukumbusho wa maneno haya ulijaza mawazo ya Mwokozi wakati **alipoketi** pamoja na **mitume** wake kushika karamu hii mara ya mwisho. Yeye alikuwa Mwana-Kondoo wa Pasaka wa kweli, na damu yake itamwangika nyuma kidogo kwa wokovu wa wote ambao watamwamini.

**22:15,16** **Pasaka** ya siku **ile** ilikuwa na maana kubwa sana kwaye na alikuwa na **hamu kubwa** kuikula pamoja nao mbele ya ku**teswa** kwake. Hatashika Pasaka tena kufika saa atakaporudi duniani na kusimamisha **ufalme** wake wa utukufu. Masemo yake **"Kwa hamu kubwa nimetaka"** yanaonyesha kuwaka sana kwa kutaka kwake, na yanaita waamini wote wa muda gani na pahali gani duniani kukumbuka ya kwamba Yesu ana hamu kubwa sana kushiriki nao kwa meza yake.

**22:17,18** Wakati **alipokamata kikombe** chenye mvinyo, ndiyo sehemu ya karamu ya Pasaka, **alishukuru** na kuileta kwa mitume, akiwakumbusha tena ya kwamba **hatakunywa matunda ya mzabibu kufika wakati wa** utawala wake wa miaka elfu moja. Shairi 18 linamaliza habari za Pasaka.

### E. Karamu ya kwanza ya Ukumbusho wa Bwana (22:19-23)

**22:19,20** Karamu ya Ukumbusho ilifuata Pasaka mara moja. Bwana Yesu alisimamisha ukumbusho mtakatifu huu ili wafuata wake kwa mia za miaka ya kuja watamkumbuka katika mauti yake. Aliwapa kwanza **mkate**, mfano wa **mwil**i wake **utakaotolewa kwa ajili yao** nyuma kidogo. Nyuma yake **kikombe** kilikuwa mfano wazi kabisa wa **damu** yake ya damani itakayomwangwa kwa msalaba wa Kalvari. Alisema juu yake kama **kikombe cha agano jipya ndani ya damu yake, iliyomwangwa kwa watu wake**. Ni kusema ya kwamba **agano jipya** alilofanya zaidi na taifa la Israeli lilithibitishwa kwa **damu** yake. Agano jipya hili litatimizwa kabisa kwa wakati wa ufalme wa Bwana wetu Yesu Kristo duniani,lakini sisi waamini tunabarikiwa nayo hata kwa wakati wa sasa.

Hatuhitaji kueleza tena ya kwamba mkate na mvinyo ni *mifano* ya mwili na damu yake. Kwa saa ile mwili wake haukutolewa kwanza na damu yake haiyamwangika kwanza. Hivi ni pumbavu kusema mifano hii iligeuzwa kwa njia ya ajabu kuwa mwili na damu yake. Vilevile Wayuda walikatazwa kula damu, na hivi wanafunzi walijua ya kwamba Yesu hakusema juu ya damu kabisa, lakini juu ya *mfano* wa damu yake.

**22:21** Ni kama Yuda alikuwa pale kwa karamu ya mwisho. Lakini Yoane 13 inaonyesha ya kwamba alikwenda zake wakati Yesu alipokwisha kumpa kipande cha mkate kilichochovywa ndani ya mchuzi. Neno hili lilitokea mbele ya kusimamishwa kwa Karamu ya Ukumbusho, hivi watu wengi wanafikiri ya kwamba Yuda hakuwa pale wakati mkate na mvinyo ilipopitishwa.

**22:22** Mateso na mauti ya Bwana Yesu **yaliamuriwa** tangu zamani, lakini Yuda alimtia kwa mikono ya adui na kutaka kwake mwenyewe. Ni kwa sababu hii Yesu alisema, **"ole wake yeye mtu yule, anayetolewa naye."** Hata kama Yuda alikuwa mmoja wa wanafunzi kumi na wawili, hakuwa mwamini wa kweli.

**22:23** Shairi hili linaonyesha ku-

shangaa kwa wanafunzi, na shaka ndani ya roho zao wenyewe. Hawakujua nani **katikati yao** atakayetenda **neno hili.**

### F. Ukubwa wa kweli ni kutumikia watu wengine (22:24-30)

**22:24,25** Ni huzuni kubwa kuona hali ovu sana ya mioyo ya watu. Ilifunuliwa wakati mara moja nyuma ya Karamu ya Bwana, wanafunzi walibishana **katikati** yao **nani atakayekuwa mkubwa zaidi!** Bwana Yesu **aliwakumbusha** ya kwamba ndani ya kawaida yake, ukubwa ni mbalimbali kabisa na ukubwa wa mawazo ya watu. Watu walifikiri ya kwamba **wafalme** ambao walitawala **Mataifa** walikuwa watu wakubwa, na **waliitwa "wafanya uzuri,"** lakini lilikuwa jina tu; kabisa kabisa walikuwa watawala wakali. Waliitwa watu wazuri, lakini uzuri ule haukuonekana ndani ya matendo yao.

**22:26** Lakini ukubwa namna hii **haukuwa** kusudi la Mwokozi kwa wafuata wake. Inapasa yule anayetaka kuwa mkubwa kuwa kama **mdogo.** Na wale wanaotaka kuwa wa kwanza wajinyenyekeze kutumikia wengine. Magizo haya yalikuwa namna nyingine kabisa na desturi zilizokubaliwa na watu, ya kwamba kijana ni chini kupita mzee, na yule wa kwanza ni mkubwa kwa njia ya kutawala wengine.

**22:27** Watu walifikiri kuwa mgeni kwa karamu ni heshima kupita kuwa mwenye kutumikia. Lakini Bwana Yesu alikuja kama mtumishi wa watu, na sharti wale ambao wanataka kumfuata wamwige ndani ya neno hili.

**22:28-30** Bwana akiwa mwenye neema, alisifu wanafunzi wake kwa sababu **walikaa pamoja naye katika majaribu yake**. Walikuwa wamegombana sasa tu. Nyuma kidogo wao wote watamwacha na kukimbia. Lakini alijua kwamba ndani ya roho zao walimpenda, na walikuwa wamelaumiwa kwa ajili ya jina lake. Zawabu yao itakuwa **kuketi juu ya viti vya ufalme wakihukumu makabila kumi na mawili ya Israeli** wakati Kristo atakaporudi na kuketi juu ya kiti cha ufalme cha Daudi na kutawala dunia. Mungu Baba aliahidi kumpa Kristo ufalme huu, naye aliahidi vivyo hivyo ya kwamba wao watatawala pamoja naye juu ya Israeli jipya.

### G. Yesu anatabiri kwamba Petro atamkana (22:31-34)

Sasa tutasoma mara ya tatu na ya mwisho juu ya ukosefu wa uaminifu wa watu. Mara ya kwanza ilikuwa udanganyifu wa Yuda. Ya pili ilikuwa tamaa ya ukubwa ya wanafunzi. Sasa tutaona woga wa Petro.

**22:31,32** Namna Kristo alivyotaja jina lake mara mbili, **Simoni, Simoni**, inaonyesha mapendo na huruma ya Bwana kwa mwanafunzi huyu mwenye kusitasita. **Shetani** alikuwa **ametaka** wanafunzi wote ili aweze **kuwapepeta** kama **ngano**. Yesu alikuwa akisema na wanafunzi wote wakati aliposema na Petro. **Lakini** Bwana alikuwa **ameombea** Simoni ili **imani** yake isipunguke. (**"Nimekuombea"** – ndilo neno la maana kubwa; ona vilevile Ebr. 7:25.) Halafu nyuma, wakati Petro atakapogeuka kwa Bwana tena, Petro **apatishe ndugu** zake **nguvu**. Kugeuka hapa si kwa kupata wokovu, lakini ni juu ya kurudishwa kwa Bwana nyuma ya kurudi nyuma.

**22:33,34** Petro alijitumainia na kiburi kisichofaa wakati aliposema yeye ni tayari kwenda pamoja na Yesu **katika kifungo hata kufa**. Lakini Bwana alimwambia ya kwamba hata **mbele ya** asubui **atakana mara tatu** kwamba **alijua** Bwana!

Katika Marko 14:30 Bwana alisema ya kwamba mbele ya kuwika kwa jogoo, mara mbili, Petro atamkana mara tatu. Ndani ya Matayo 26:34, Luka 22:34 na

Yoane 13:38 Bwana alisema mbele ya kuwika kwa jogoo Petro atamkana mara tatu. Ni nguvu kupatanisha habari hizi zilizo mbalimbali kidogo. Labda jogoo aliwika kupita mara moja, katikati ya usiku na kwa mapambazuko ya asubui. Na vilevile tuone ya kwamba ndani ya vitabu vya Habari Njema tunasoma juu ya Petro akikana Kristo mara sita. Alimkana mbele ya:

Kijakazi mmoja (Mt. 26:69,70; Mk. 14:66-68).

Kijakazi mwingine (Mt. 26:71,72).

Makutano ya watu waliosimama karibu (Mt. 26:73,74; Mk. 14:70,71).

Mwanamume mmoja (Lk. 22:58).

Mwanamume mwingine (Lk.22:59, 60).

Mtumishi wa kuhani mkubwa (Yn. 18:26,27). Tunafikiri mtu huyu hakuwa mmoja wa wale waliotajwa mbele kwa sababu ya maneno aliyosema – “Sikukuona katika shamba pamoja naye?” (sh. 26).

**H. Maagizo mengine kwa utumishi wao (22:35-38)**

**22:35** Mbele, wakati Bwana **alipotuma** wanafunzi wake kuhubiri, aliwaagiza kwenda **bila mfuko na ndaha na viatu**. Walikwenda na vitu vichache tu kwa mahitaji yao, na walikiri ya kwamba **hawakukosa kitu**.

**22:36** Lakini sasa alikuwa karibu kuwaondokea, na utumishi wao kwaye utageuka kuwa namna nyingine. Watapata umasikini, njaa, na hatari, na itawapasa kwenda na vitu watakavyohitaji. Sasa iliwapasa kwenda na **mfuko,** na **ndaha,** na kama wakikosa **upanga**, iliwapasa **kuuza vazi** lao **kupata mali kwa kuununua.** Kwa nini Bwana alisema na wanafunzi **kununua upanga**? Tunajua ya kwamba hatataka wanafunzi kutumika na upanga huu kupiga vita na watu wengine. Neno hili lingalikana mafundisho yake ndani ya mashairi mengine kama:

“Ufalme wangu si wa dunia hii; kama ufalme wangu ungekuwa wa dunia hii, watumishi wangu wangenipigania” (Yn. 18:36).

“Wote wanaoshika upanga wataharibiwa kwa upanga” (Mt. 26:52).

“Pendeni adui zenu …” (Mt. 5:44).

“Mtu akikupiga shavu la kuume, umgeuzie la pili vilevile” (Mt. 5:39; ona vilevile 2 Kor. 10:4).

Basi Bwana aliwaza nini wakati aliposema juu ya upanga?

1. Wengine wanasema alifikiri juu ya upanga wa Roho, ndilo Neno la Mungu (Efe. 6:17). Kama ni hivi, halafu mfuko na ndaha, na vazi ni mfano wa nini?
2. Mwalimu Williams anasema ni kulindwa na serikali taratibu, kama kwa Waroma 13:4.
3. Mwingine, kama Lange, anasema kazi ya upanga ni kusaidia mwenye upanga kujipigania mwenyewe, si kwa kupiga vita na adui. Lakini Matayo 5:39 halipatani na elezo hili.
4. Wengine wanafikiri upanga ni kusaidia mtu asiumizwe na nyama za mwitu tu.

**22:37** Shairi 37 linaeleza kwa sababu gani ilipasa wanafunzi kwenda na mfuko, ndaha na upanga kuanza sasa. Bwana alikuwa pamoja nao kufika saa ile na aliwapatia vitu walivyohitaji. Nyuma kidogo atawaondokea kama ilivyotabiriwa katika Isaya 53:12. Maneno yaliyoandikwa juu yake yalikuwa na **mwisho**, maana yake maisha na utumishi wake duniani zitakwisha wakati **atakapohesabiwa pamoja na wakosaji.**

**22:38** Wanafunzi hawakufahamu hata kidogo masemo haya ya Bwana. **Walileta panga mbili** wakifikiri zitatosha kwa matata yo yote ambayo itawapata. Halafu Bwana alimaliza mazungumuzo yao akisema, **“Inafaa.”** Ni kama wana-

funzi waliwaza kama wakitumia panga hizi wataweza kuzuiza adui wasimwue. Bwana wao hakufikiri hivi hata kidogo!

### I. Maumivu shambani mwa Getesemane (22:39-46)

**22:39** Shamba la Getesemane lilikuwa kwa mtelemuko wa mangaribi wa **kilima cha Zeituni**. Yesu alikwenda pale mara nyingi kwa kuomba, na **wanafunzi**, pamoja na yule ambaye atamtoa kwa adui, walijua neno hili.

**22:40** Kwa mwisho wa Karamu ya Ukumbusho, Yesu na wanafunzi wake waliondokea chumba cha juu, wakakwendea shamba lile. Wakati walipofika aliwaonya **kuomba wasiingie majaribu.** Labda aliwaza zaidi juu ya **kujaribiwa** kwao kuacha Mungu na Kristo wake wakati adui watakapofika kumfunga.

**22:41,42** Kisha aliondokea wanafunzi, akaingia shamba mbali kupita, **akaomba** peke yake. Aliomba **kama** ikipendeza **Baba**, amwondolee **kikombe hiki; hata hivi** alitaka **mapenzi** ya Mungu kufanywa, **si** mapenzi yake mwenyewe. Tunafikiri maana ya ombi hili ilikuwa: Kama kuna njia nyingine kuokoa watu bila kwa Mimi kufa msalabani, ufunue njia hii sasa. Lakini mbingu zilikuwa kimya kwa sababu **hakuna** njia nyingine.

Hatufikiri ya kwamba maumivu ya Kristo shambani yalikuwa sehemu ya kazi yake ya upatanisho. Kazi ya ukombozi ilitimizwa ndani ya saa zile tatu za giza juu ya msalaba. Lakini maumivu yake katika Getesemane yalitazamia Kalvari. Kuwaza juu ya kukutana na zambi zetu kulikuwa mateso makali zaidi kwa Bwana Yesu.

**22:43,44** **Maumivu** yake yalionyesha utu mkamilifu wake wazi**. Malaika toka mbingu alitokea, akampatisha nguvu.** Mganga Luka tu aliandika habari hizi, na vilevile ya kwamba **jasho yake ilikuwa kama matone ya damu.**

**22:45,46** **Wakati** Yesu aliporudi **karibu na wanafunzi wake** aliwakuta **wakilala** usingizi, si kwa sababu waliona bure maneno yaliyotokea, lakini kwa sababu ya kushindwa na huzuni. Aliwaonya tena **kusimama** na **kuomba** kwa sababu saa ya hatari kubwa ilikuwa karibu, nao watajaribiwa kumkana mbele ya wakubwa.

### J. Yesu anatolewa kwa adui na kufungwa (22:47-53)

**22:47,48** Sasa **Yuda** alikuwa amefika pamoja na wakubwa wa makuhani, wazee, na wakubwa wa hekalu kufunga Yesu. Yuda alikuwa amewapa alama mbele wajue mtu ambaye iliwapasa kufunga, ndiyo busu. Stewart alisema:

> Ilikuwa aibu kubwa kupita yote wakati pale shambani Yuda alipotoa bwana wake kwa adui zake, si pamoja na kelele, wala na kumpiga, au kumtoboa, lakini na busu.[39]

Na huzuni kubwa sana **Yesu** aliuliza, **"Yuda, unatoa Mwana wa watu kwa kumbusu?"**

**22:49-51** Wanafunzi walifahamu **maneno yatakayotokea,** na walikuwa tayari kupiga vita. **Mmoja wao,** ndiye Petro alishika **upanga**, akakata **sikio la kuume la mtumishi wa kuhani mkubwa.** Yesu alimhamakia kwa sababu alitumika na kitu cha dunia kupiga vita ya roho. Saa yake ilikuwa imefika na lazima makusudi Mungu aliyofanya mbele yatimizwe. Kwa neema Yesu **aligusa sikio** la yule aliyeumizwa, **akamponyesha.**

**22:52,53** Halafu **Yesu** aligeuka kwa viongozi vya Wayuda, akawauliza kwa sababu gani walikuwa **wametoka** na panga na magongo kumkamata kama juu ya **mnyanganyi.** Hakuwafundisha **kila siku kwa** pahali pa **hekalu**, nao hawakujaribu kumfunga saa ile? Lakini yeye mwenyewe alijua jibu kwa ulizo

hili, "… **lakini saa hii ni yenu, na mamlaka ya giza**." Ilikuwa karibu saa sita ya usiku siku ya kazi ine sasa.

Ni kama hukumu ya Bwana wetu ilikuwa na sehemu tatu. Kwanza, alifikishwa mbele ya Ana. Nyuma yake alifikishwa kwa Kayafa. Mwishoni alihukumiwa na Baraza. Tunafikiri ya kwamba maneno tunayosoma toka hapa kufika shairi 65 yalitokea toka saa 7 kufika saa 11 ya usiku, siku ya kazi tano.

### K. Petro anakana Yesu na kutoa machozi na uchungu sana (22:54-62)

**22:54-57** Wakati Bwana alipoingizwa **katika nyumba ya kuhani mkubwa, Petro akafuata kwa mbali,** akaketi pamoja na wale ambao waliota **moto** katika kiwanja**. Mjakazi mmoja aliangalia** Petro, akasema yeye alikuwa mmoja wa wafuata wa Yesu. Na roho ya kutia huruma Petro **alikana** kwamba alijua Yesu.

**22:58-62** Nyuma kidogo mtu mwingine alimwona na kusema Petro alikuwa mmoja wa wafuata wa Yesu wa Nazareti. **Petro** alikana neno hili tena. **Nyuma ya saa moja** nyingine, mtu mwingine alitambua kwamba yeye ni **Mgalilaya** na mmoja wa wafuata wa Bwana. **Petro** alikana kwamba alijua maneno ambayo mtu huyu alisema, na saa yenyewe **jogoo aliwika.** Saa ile ile **Bwana aligeuka na kuangalia Petro, na Petro alikumbuka** maneno yake kwamba **mbele ya kuwika kwa jogoo,** Petro atamkana **mara tatu.** Basi **Petro,** akiona tazamo hili la Mwana wa Mungu, alikimbia inje, na kulia kwa **uchungu sana.**

### L. Askari wanazihaki Mwana wa watu (22:63-65)

Askari hawa ndio wale waliopewa kazi ya kulinda hekalu takatifu. Sasa wale walinzi wa nyumba takatifu ya Mungu walianza kuzihaki Yesu na **kumpiga.** Nyuma ya kufunika macho yake na kitambaa **wakampiga kwa uso wake, wakauliza** kutaja **yule** ambaye alimpiga. Walifanya maneno mengi mengine, lakini Bwana alivumilia na saburi "mabishano makubwa namna hii ya wenye zambi juu yake" (Ebr. 12:3).

### M. Hukumu ya asubui mbele ya Baraza (22:66-71)

**22:66-69** Kwa mapambazuko ya asubui **wazee walileta** Yesu kwa **Baraza** yao. Watu wa Baraza hii walimwuliza waziwazi kama yeye ni Masiya. Yesu aliwajibu akisema si faida kusemezana nao juu ya neno hili, kwa sababu hawakuwa tayari kupokea kweli. Lakini aliwajulisha kwamba Yule ambaye alisimama mbele yao katika aibu **ataketi siku nyingine kwa mkono wa kuume wa uwezo wa Mungu** (Ona Zab. 110:1).

**22:70,71 Halafu walimwuliza** wazi kama alikuwa **Mwana wa Mungu.** Walijua vizuri maana ya ulizo lao. Walifahamu kwamba **Mwana wa Mungu** alikuwa sawa na Mungu. Bwana Yesu alijibu **"Mimi ni yeye"** (ona Marko 14:62). Walifikiri ametoa ukufuru wakati aliposema yeye ni sawa na Mungu. Hawakuhitaji **ushuhuda mwingine.** Kwa sheria yao azabu kwa ukufuru ilikuwa mauti. Lakini Wayuda walitawaliwa na Waroma, na hawakuwa na amri kuua wafungwa. Hivi iliwapasa kupeleka Yesu kwa Pilato. Walijua Pilato ataona mashitaki ya *dini* kama ukufuru kama kitu bure, hivi iliwapasa kushitaki Yesu juu ya maneno ya *serikali*.

### N. Yesu mbele ya Pilato (23:1-7)

**23:1,2** Nyuma ya kutokea mbele ya Baraza **nzima**, Yesu alipelekwa kuhukumiwa na **Pilato**, ndiye liwali la Waroma. Viongozi vya dini vya Wayuda walimshitaki kwa Pilato juu ya maneno matatu. Kwanza, walisema **aligeuza mafikiri ya taifa** wasiheshimu Waroma tena. Neno la pili, walisema alikataza watu

**wasimpe Kaisari kodi.** Na neno la tatu, walimshitaki juu ya kujifanyiza **Mfalme.**

**23:3-7** Wakati **Pilato alipouliza** Yesu kama alikuwa **Mfalme wa Wayuda, alijibu** ni kweli. **Pilato** hakufikiri neno hili ni hatari kwa Kaisari ya Waroma. Nyuma ya kusemezana na Yesu peke yake (Yoane 18:33-38a), aligeuka kusema na **wakubwa wa makuhani na** kwa makutano ya kwamba **hakuona kosa** hata moja ndani yake. Makutano walikaa kusema kwamba alikoroga watu **kuanza** katika inchi **ya Galilaya** kufika hata Yerusalema. **Wakati Pilato aliposikia** watu wakitaja **Galilaya** alifikiri alikuwa amepata njia kujiondosha ndani ya maneno haya. Galilaya **ilitawaliwa na Herode,** hivi alituma Yesu kwa **Herode** aliyekuwa **katika Yerusalema kwa saa ile ile.**

**Herode** Antipa alikuwa mwana wa Herode Mkubwa aliyeagiza watoto wadogo wote wa Betelehemu kuuawa. Alikuwa Antipa aliyeua Yoane Mbatizaji kwa sababu alimshitaki juu ya zambi yake na mke wa ndugu yake. Yesu alimwita "mbweha" katika Luka 13:32.

### O. Maulizo ya kuzarau ya Herode (23:8-12)

**23:8 Herode alifurahi** kuona **Yesu** akitokea mbele yake. **Alikuwa amesikia habari nyingi juu yake** na kwa **siku nyingi** alitaka **kuona Yesu akifanya ajabu** mbele yake.

**23:9-11** Lakini hata kama **Herode alimwuliza** maneno mengi namna namna, Mwokozi hakumjibu. Wakubwa wa makuhani na waandishi walizidi kumshitaki, lakini Yesu hakufungua kinywa chake. Basi **Herode** aliweza kuruhusu askari zake kumzihaki tu, ku**mchekea** kwa njia ya **kumvika mavazi mazuri na kumrudisha kwa Pilato**.

**23:12 Mbele ya wakati huu Herode na Pilato walikuwa adui,** lakini sasa waligeuka rafiki. Walifungana pamoja kuwa *adui* za Bwana Yesu. Mwalimu mmoja alisema na huzuni: "Ni haya kubwa kuona ya kwamba Shetani anaweza kusukuma watu waovu kuacha uadui wao kwa kutenda mabaya, lakini inashinda Wakristo kuwa rafiki kwa kutenda mema."

### P. Hukumu ya Pilato: Bila kosa lakini hukumu ya mauti (23:13-25)

**23:13-17 Pilato** hakutenda kwa haki mbele wakati asipofungua mfungwa wake, hivi sasa alikuwa katika mtego. Aliita wakubwa wa Wayuda kukutana mbio na kuwaelezea ya kwamba **wala Herode** wala yeye mwenyewe hawakuona kosa katika Yesu, **"… hakufanya neno hata moja la kustahili kufa."** Hivi alikusudi Bwana apigwe na fimbo na kufunguliwa. Stewart alionyesha ya kwamba:

> Shauri hili halikuwa haki hata kidogo. Pilato, akisukumwa na woga, alijaribu kusimamia Yesu na kupendeza makutano vilevile, lakini alishindwa ndani ya maneno haya mawili yote. Hatushangai kuona kwamba makuhani walikasirika na walikataa hukumu ile kabisa.[40]

**23:18-23** Wakubwa wa makuhani walikasirika sana. Walitaka Yesu kuuawa na **Baraba** kufunguliwa. Baraba alijulikana kwa sababu ya uovu wake, na alitiwa **katika kifungo** kwa sababu ya **fitina na uuaji.** Pilato katika uzaifu wake alijaribu tena kusimamia Bwana, lakini hakusikiwa kwa sababu ya malalamiko makali ya watu. Si neno kama alisema nini, **walikaa kutaka** Mwana wa Mungu kuuawa.

**23:24,25** Basi **Pilato** alisema mbele ya kwamba Yesu hakuwa na kosa, lakini sasa alimhukumu kufa kupendeza watu. **Alifungua** Baraba vilevile kwa saa ile.

### Q. Mwana wa watu anapelekwa kwa Kalvari (23:26-32)

**23:26** Ilikuwa sasa karibu saa tatu

asubui ya siku ya kazi tano. Wakati walipopeleka Yesu kwa pahali pa kusulibishwa, askari waliagiza mtu mmoja, jina lake **Simoni, Mkurene,** kubeba **msalaba**. Hatujui maneno mengi juu ya mtu huyu, lakini ni kama wana wake wawili waligeuka Wakristo wa kujulikana kwa wakati wa nyuma (Marko 15:21).

**23:27-30** Makutano ya wafuata waliohurumia Yesu walikuwa wakitoa machozi. Yesu alisema na **wanawake** katika makutano, akiwaita **binti za Yerusalema**, kwamba haifai wamhurumie yeye lakini wajililie wenyewe. Alikuwa akiwaza juu ya uharibifu wa Yerusalema ulioletwa na Tito kwa mwaka 70 A.D. Mateso na taabu ya **wakati ule** zitakuwa kubwa sana hata wanawake **tasa** walioIaumiwa mbele, walibarikiwa sasa. Utakuwa wakati wa hofu kubwa sana hata wanaume watataka **milima kuwaangukia, na vilima kuwafunika**.

**23:31** Halafu Bwana Yesu aliongeza maneno mengine, **"Kama wanafanya maneno haya wakati mti ni mbichi, watafanya neno gani wakati mti unapokauka?"** Yeye mwenyewe alikuwa mti **mbichi**, na Waisraeli wasioamini walikuwa mti **unaokauka**. Kama Waroma wakivimbishia Mwana wa Mungu asiyekuwa na zambi, haya na mateso mengi namna hii, azabu kubwa gani, ya kuogofya zaidi, itaangukia wauaji wa Mwana mpendwa wa Mungu?

**23:32 Wawili wengine, watenda wabaya, walipelekwa** pamoja na Yesu kwa kusulibishwa.

**R. Kusulibishwa (23:33-38)**

**23:33** Pahali watu waliposulibishwa paliitwa **Mfupa wa Kichwa** (au Kalvari – maana yake mfupa wa kichwa kwa Kiroma). Labda palifanana na mfupa wa kichwa, au paliitwa hivi kwa sababu palikuwa pahali pa mauti, kwani mara nyingi mfupa wa kichwa unatumiwa kama mfano wa mauti. Maandiko Matakatifu yanapasha habari za kusulibishwa kwa Bwana na maneno machache tu, ndiyo maneno mawili: **"kule walimsulibisha."**

> Utufundishe maana ya msalaba huu
> Ulionyanyuliwa na kubeba
> Mtu wa huzuni, mhukumiwa
> Kutoa damu yake, hata kufa.[41]

Kulikuwa na misalaba mitatu kwa Kalvari siku ile. Msalaba wa Yesu ulikuwa katikati, na misalaba kwa upande wake wa kuume na kushoto ilibeba watenda mabaya. Neno hili lilitimiza Isaya 53:12 – "Akahesabiwa pamoja na wale wenye kukosa."

**23:34** Na mapendo na huruma kubwa sana **Yesu** alitoa sauti toka msalaba, **"Baba, uwasamehe, kwa sababu hawajui neno wanalofanya."** Labda ombi hili lilizuiza gazabu kubwa sana ya Mungu kwa wakati ule! Morgan aliandika maneno haya juu ya mapendo ya Mwokozi:

> Yesu hakuwa na uchungu rohoni, wala kasirani, wala hamu kwa watu wale ambao walimtendea mabaya kuazibiwa [41]

Halafu askari waligawanya **nguo zake, na kupiga kura** kwa vazi lake lililofumwa kipande kimoja.

**23:35-38 Wakubwa** walisimama mbele ya msalaba wakimzihaki na kusema naye **kujiponyesha** kama alikuwa kweli Kristo, **mchaguliwa wa Mungu. Askari vilevile walimzihaki . . . wakimpa siki** na kusema naye **kujiokoa** kama akiweza. Waliweka maandiko kwa kichwa cha msalaba na maneno haya juu yake:

**HUYU NI MFALME WA WAYUDA**

Tunataja tena maandiko ya Stewart:

> Ona ya kwamba maneno haya yaliandikwa kwa lugha tatu, Kiyunani, Kiroma, na Kiebrania, ili watu wote ndani ya makutano yale waweze kuyasoma na kuyafahamu. Lakini

> kwa mafikiri ya Kanisa la Kristo ni mfano wa enzi ya Bwana wake. Kwani hizi zilikuwa lugha kubwa tatu za dunia. Kiyunani ni kwa maneno ya elimu na lugha hii ilisema, Yesu ni mfalme! Kiroma ilikuwa lugha ya serikali; pale vilevile Yesu ni Mfalme. Na Kiebrania ndiyo lugha ya dini; Yesu ndiye Mfalme pale! Hivi hata saa alipotundikwa na akikufa, ilikuwa kweli ya kwamba "juu ya kichwa chake kulikuwa na taji nyingi" (Ufu. 19:12). [42]

### S. Wanyanganyi wawili (23:39-43)

**23:39-41** Vitabu vya Habari Njema nyingine vinaonyesha ya kama wanyanganyi wawili wote walizihaki Bwana kwanza. Kama yeye ni **Kristo**, kwa nini basi **hakuwaponyesha** wote? Lakini nyuma kidogo mnyanganyi mmoja aligeuka, **akahamakia** mwenzake kwa masemo yake mabaya. Wao wawili walikuwa wakiteswa kwa sababu walivunja sheria. Walistahili kuazibiwa. Lakini **mtu huyu** juu ya msalaba wa tatu **hakufanya neno lisilofaa.**

**23:42** Akigeuka kusema **na Yesu, mnyanganyi** aliomba **Bwana kumkumbuka wakati** atakapokuja tena na kusimamisha **ufalme** wake duniani. Imani yake inatushangaza. Yule mnyanganyi aliyekuwa akikufa aliamini ya kwamba Yesu atafufuka toka wafu na mwishoni atatawala dunia.

**23:43** Kama zawabu kwa imani yake **Yesu** aliahidi ya kwamba siku ile ile **watakuwa katika Paradiso** pamoja. Paradiso ndiyo mbingu ya tatu (2 Kor. 12:2,4), ndilo kao la Mungu. **Leo – pamoja nami – katika Paradiso!** Ajabu kabisa. Charles R. Erdman aliandika:

> Habari hizi zinatufundisha kwamba toba na imani zinahitajiwa kwa wokovu. Lakini kuna mafundisho makubwa mengine hapa vilevile. Zinaonyesha kwamba sakramenti hazihitajiwi kwa wokou. Mnyanganyi hakubatizwa, wala kula mkate kwa Karamu ya Ukumbusho. … Alikiri imani yake wazi mbele ya makutano ya adui, na zihaka na kucheka kwa watawala na askari, na aliokolewa bila sakramenti. Zinaonyesha vilevile kwamba matendo mema hayahitajiwa kwa wokovu. ... Zinaonyesha kwamba nafsi hailali. Ndiyo, mwili utakufa lakini kuna ufahamu wa nafsini. Zinaonyesha wazi vilevile ya kwamba hakuna "purgatoire." Nyuma ya kuishi katika zambi na haya, yule mnyanganyi aliingia mara moja hali ya baraka. Lakini inatupasa kusema tena ya kwamba wokovu si kwa watu wote. Kulikuwa na wanyanganyi wawili, lakini mmoja tu aliokolewa. Mwishoni tuseme kwamba msingi wa furaha nyuma ya mauti ni upatano na ushirika wa karibu na Kristo. Ahadi mnyanganyi huyu aliyopewa ndiyo hii: "Utakuwa pamoja nami." Hili ndilo tumaini letu la baraka, "kwenda na kukaa pamoja na Kristo" maana ni "vizuri zaidi sana."[43]

Toka upande mmoja wa msalaba wa Kristo inawezekana kwa mtu mmoja kwenda mbinguni, na toka upande wa pili kwenda Gehena. Wewe unasimama kwa upande gani wa msalaba?

### T. Saa tatu za giza (23:44-49)

**23:44 Giza** lilikuwa juu ya inchi (maana ya *inchi* kwa Kiyunani inaweza kuwa **dunia** vilevile) **toka saa sita azuhuri kufika saa tisa.** Neno hili lilikuwa alama kwa Israeli. Walikuwa wamekataa nuru, hivi sasa Mungu atawahukumu na giza nafsini.

**23:45 Pazia la hekalu lilipasuka** toka juu kwenda chini. Tukio hili lilikuwa mfano kuonyesha ya kwamba kwa njia ya mauti ya Bwana Yesu Kristo njia ilifunguliwa kwa wote wenye imani kufikia Mungu (Ebr. 10:20-22).

**23:46,47** Kwa saa hizi tatu za giza Yesu alibeba azabu ya zambi zetu katika mwili wake juu ya msalaba. Kwa mwisho wa muda huu aliweka **roho**

yake katika **mikono** ya Mungu, **Baba** yake. **Mkubwa wa askari,** Mroma, alishangaa sana wakati alipoona maneno haya, **akatukuza Mungu na kusema, "Kweli mtu huyu alikuwa mwenye haki!"**

**23:48,49 Makutano yote** waliokusanyika kuangalia walishindwa kabisa na huzuni na woga. Wengine wa wafuata waaminifu wa Yesu, pamoja na **wanawake waliofuatana naye toka Galilaya, wakasimama … wakiangalia** tukio lenye maana kubwa zaidi ya historia ya dunia**.**

### U. Maziko ndani ya kaburi la Yosefu (23:50-56)

**23:50-54** Kufika wakati ule **Yosefu** alifuata Bwana kwa siri**.** Alikuwa **mmoja** wa watu wa Baraza**,** lakini hakukubali hukumu yao kwa maneno ya Yesu. Sasa Yosefu alifikia **Pilato** na uhodari na **kuomba** apewe ruhusa kuondosha **mwili wa Yesu** toka msalaba na kuuzika. (Ilikuwa kati ya saa tisa na saa kumi na mbili ya mangaribi.) Alipewa ruhusa, na Yosefu **aliufunga ndani ya nguo ya sanda, akauweka katika kaburi lililochongwa katika mwamba,** pahali mtu asipowekwa mbele. Neno hili lilitokea siku ya kazi tano, **siku** ya **Matengenezo.** Tukumbuke ya kwamba **sabato** ya Wayuda ilianza siku ya kazi tano kwa wakati wa mangaribi. Kwa sababu hii tunasoma hapa "sabato ilianza kuingia."

**23:55,56 Wanawake** waaminifu **… toka Galilaya walifuata** Yosefu wakati alipoweka **mwili** ndani ya **kaburi**. Kisha **walirudi kwao kutayarisha manukato na malasi ya mafuta** ili waweze kutia dawa hii kwa mwili wa Mpendwa wao. Ni kama wakati Yosefu alipozika mwili wa Yesu alijizika mwenyewe vilevile. Tendo hili lilimtenga kwa milele na taifa hili waliosulibisha Bwana wa uzima na utukufu. Hatashiriki ndani ya dini ya Wayuda tena kamwe, lakini ataishi maisha safi akijitenga nao na kutoa ushuhuda juu yao.

Siku ya kazi sita wanawake walipumzika, wakitii agizo la sheria juu ya sabato.

## 12. KUSHINDA KWA MWANA WA WATU (Sura 24)

### A. Wanawake kwa kaburi tupu (24:1-12)

**24:1** Halafu siku ya kwanza ya juma asubui **mapema** wanawake walirudia **kaburi,** wakibeba **manukato waliyoweka tayari** kwa mwili wa Yesu. Lakini wataweza kufikia mwili wake namna gani? Walijua jiwe kubwa lilikuwa limefingirishwa mbele ya kaburi. Hatujui jibu la ulizo hili, lakini tunajua ya kwamba walimpenda sana, na mara nyingi wenye mapendo wanasahau masumbuko tunayopata kufikia mpendwa wetu.

Mapendo yao yaliwasukuma kuamka asubui mapema (sh.1), na walipokea zawabu tamu sana (sh.6). Hata leo Bwana anakutana na wale wanaoamka asubui mapema kukutana naye (Mez. 8:17).

**24:2-10** Saa walipofika **walikuta jiwe limefingirishwa** mbali na **kaburi.** Wakati **walipoingia** waliona mara moja kwamba **mwili wa Bwana Yesu** haukuwa pale. Walishangaa na kufazaika sana wakati malaika **wawili** (ona Yoane 20:12) walipotokea wakivaa **nguo za kungaa sana**, wakawaambia ya kwamba Yesu alikuwa **hai**; haikuwa faida kwao kumtafuta kaburini. Alikuwa **amefufuka** kama alivyoahidi wakati alipokuwa **kwanza pamoja nao katika Galilaya**. Hakuwaambia mbele kwamba **Mwana wa watu** atatiwa katika mikono ya **wenye zambi na kusulibishwa**, na ya kwamba **siku ya tatu atafufuka?** (Lk 9:22; 18:33). Halafu walikumbuka maneno haya yote. **Walirudia mji** mbio na **kuwaambia wanafunzi kumi na mmoja habari.** Wengine wa watu hawa wa kwanza waliotangaza ufufuko wa Yesu

Kristo walikuwa **Maria Magdalene, Yoana**, na **Maria mama ya Yakobo.**

**24:11,12** Wanafunzi **hawakuamini habari zao** hata kidogo. Yalionekana bure kwao – kufika wakati Petro **alipofikia kaburi** yeye mwenyewe na **kuona vile vitambaa vimewekwa peke yao.** Mwili wa Yesu ulizungushwa na nguvu na vitambaa mbele. Hatusomi kama vilifunguliwa sasa, au vilikuwa kwa umbo la mwili. Lakini vitambaa vikiwa kwanza pale vinaonyesha kwamba mwili haukuibwa; wizi wasingalikuwa na saa kufungua vitambaa hivi. Basi Petro alirudi kwake akijaribu kufahamu maana ya siri hii kubwa!

### B. Wanafunzi wakikwendea Emau (24:13-35)

**24:13** Mmoja wa wanafunzi **wawili** waliokuwa wakikwenda Emau alikuwa Kleopa; hatujui kama wa pili alikuwa nani. Labda alikuwa mke wake. Au, kama watu wengine walivyosema, labda alikuwa Luka mwenyewe. Tunajua neno moja tu kwa hakika, ya kwamba hakuwa mmoja wa wanafunzi kumi na mmoja wa kwanza (ona sh.33). Watu wenyewe walikuwa wakizungumuza na huzuni nyingi juu ya mauti na kuzikwa kwa Bwana wakati walipokuwa **wakirudi kwa Emau toka Yerusalema,** safari ya karibu **11 km**.

**24:14-18** Wakati walipotembea mgeni alifika na kutembea pamoja nao. Alikuwa Bwana aliyekuwa amefufuka, lakini **hawakumtambua.** Aliwauliza kama walikuwa wakisemezana juu ya nini. Kwanza walisimama na huzuni kubwa. Halafu **Kleopa** alionyesha kushangaa kwa sababu hata mgeni **katika Yerusalema** angesikia habari za maneno **yaliyotokea.**

**24:19-24** Yesu aliwauliza neno lingine, "**Maneno gani**?" Walijibu na kusifu **Yesu** kwanza, kisha waliendelea na habari za hukumu na kusulibishwa kwake. Walisema juu ya namna tumaini lao liliharibiwa, kisha juu ya habari ya kwamba **mwili wake** haukuwa kaburini tena. Ndiyo, hata **malaika** walisema **alikuwa hai.**

**24:25-27** Halafu Yesu aliwahamakia na upole kwa sababu hawakufahamu kwamba haya ndiyo maneno **manabii** waliyotabiri juu ya Masiya. Itampasa kuteswa kwanza, kisha atatukuzwa. **Kuanza** na kitabu cha Mwanzo Bwana aliwakumbusha ndani ya **Maandiko yote** maneno ambayo **Manabii** walitabiri juu **yake mwenyewe**, ndiye Masiya. Yalikuwa mafundisho matamu kabisa, na sisi sote tungalipenda kuwa pamoja naye saa ile! Lakini sisi tuna Agano la Kale, na tuna Roho Mtakatifu kutufundisha, hivi sisi vilevile tunaweza kuona ndani ya **Maandiko maneno yote yaliyoandikwa juu yake.**

**24:28,29** Wanafunzi walikuwa wakikaribia nyumba yao sasa. Waliomba mwenye kusafiri pamoja nao kulala usiku nyumbani mwao. Kwanza alitenda sawasawa alitaka kuendelea na safari yake. Akiwa mwenye adabu hakutaka kuingia nyumba yao na nguvu. Lakini walimsukuma kulala pamoja nao, na kweli walipokea zawabu tamu sana!

**24:30,31** Wakati walipokaa kwa chakula cha mangaribi, Mgeni wao aligeuka Mwenye kukaribisha wageni!

> Chakula chao kidogo kiligeuka ushirika mtakatifu, na nyumba yenyewe iligeuka nyumba ya Mungu. Hili ndilo neno linalotokea kila pahali Kristo anapokwenda. Watu ambao wanampokea kama mgeni wao wanabarikiwa wao wenyewe. Watu hawa wawili walikuwa wamempokea nyumbani mwao, na sasa yeye alifungua macho yao. (Ligue pour la Lecture de la Bible)

Wakati **alipovunja mkate** na **kuwapa, walimtambua**. Waliona alama za misumari mikononi mwake? Hatujui. Tunajua tu ya kwamba kwa njia ya ajabu

**macho** yao **yalifunguliwa** nao walimtambua. Kisha **alitoweka** na hawakumwona tena.

**24:32** Basi walishika njia kufanya safari ya siku ile mara ya pili, na kurudia Yerusalema. Hatushangai kusoma ya kwamba mioyo yao iliwaka **ndani** yao **wakati alipokuwa akisemezana nao** na **kuwafunulia maana ya maandiko.** Mwalimu aliyetembea pamoja nao alikuwa Bwana Yesu Kristo aliyefufuliwa!

**24:33** Hawakulala usiku ule katika Emau lakini walirudia **Yerusalema** saa ile ile, wakakuta **wanafunzi kumi na mmoja** na watu wengine waliokuwa wamekusanyika **pamoja.** "Mitume kumi na mmoja" ni kama jina lililotumiwa kwa wale wanafunzi waliochaguliwa na Yesu kwa mwanzo wa utumishi wake, bila Yuda. Katika Yoane 20:24 tunaona ya kwamba hawakuwa wote pale saa yenyewe.

**24:34** Mbele ya wanafunzi wa Emau kuweza kupasha habari zao za furaha, wanafunzi wa Yerusalema walitangaza na furaha nyingi ya kwamba **Bwana amefufuka** hakika na **kuonekana kwa Simoni** Petro.

**24:35** Halafu wale wawili wa Emau walipata njia kusema, "Ndiyo, tunajua, kwa sababu alitembea pamoja nasi, aliingia nyumbani mwetu, na kujifunua kwetu **kwa njia ya kuvunja mkate**."

### C. Alionekana kwa wale kumi na mmoja (24:36-43)

**24:36-41** Mwili wa ufufuko wa Bwana Yesu ulikuwa **mwili na mifupa** kama mbele, ambao watu waliweza kugusa. Ni mwili uliozikwa, lakini ulikuwa umegeuzwa vilevile kwani sasa haukuweza kufa tena. Na mwili huu wa utukufu, Yesu aliweza kuingia chumba hata wakati milango ilipofungwa (Yn. 20:19).

Alifanya hivi siku ya kwanza ile ya juma kwa saa ya mangaribi. Wanafunzi walinyanyua macho, wakamwona, kisha walimsikia akisema, **"Salamu kwenu."** Waliogopa sana wakifikiri ni roho. Halafu aliwaonyesha alama za mateso yake ndani ya mikono na miguu yake, nao walianza kufahamu, lakini hata hivi ilikuwa nguvu kwa wengine kuamini ya kwamba ni kweli.

**24:42,43** Basi kuwaonyesha kwamba ni kweli yeye Yesu, **alikula** kipande cha **samaki** na **asali** mbele yao.

### D. Ufahamu unafunguliwa (24:44-49)

**24:44-47** Ni kama mashairi haya yanajumlisha mafundisho ya Mwokozi nyuma ya ufufuko wake na mbele ya kurudi kwake mbinguni. Alieleza ya kwamba ufufuko wake ulitimiza **maneno** ambayo yeye mwenyewe aliwaambia. **Torati ya Musa na Manabii na Zaburi** zilikuwa sehemu kubwa tatu za Agano la Kale, nazo pamoja ni Agano la Kale zima. Mambo makubwa yaliyotabiriwa juu ya Kristo katika Agano la Kale yalikuwa nini?

1. Ya kwamba itakuwa lazima kwake **kuteswa** (Zaburi 22:1-21; Isa. 53:1-9).
2. Ya kwamba ilikuwa sharti kwake **kufufuliwa toka wafu** siku ya tatu (Zab. 16:10; Yona 1:17; Hos. 6:2).
3. **Na maneno ya toba na kusamehe zambi yahubiriwe kwa jina lake katika mataifa yote, kuanza kwa Yerusalema.**

Yesu **alifungua akili yao wapate kufahamu maana ya maandiko haya.** Ndiyo, sura hii inapasha juu ya maneno mengi yaliyofunguliwa: *kaburi* lililofunguliwa (sh.12), *nyumba* iliyofunguliwa (sh. 29), *macho* yaliyofunguliwa (sh.31), *Maandiko* yaliyofunguliwa (sh.32), *midomo* iliyofunguliwa (sh.35), *akili* iliyofunguliwa (sh.45), *mbingu* zilizofunguliwa (sh.51).

**24:48,49** Wanafunzi walikuwa **washuhuda** wa ufufuko. Ilikuwa lazima

kwao kwenda kutangaza habari hizi za utukufu. Lakini kwanza iliwapasa kungojea kufika kwa **Ahadi ya Baba**, maana kufika kwa Roho Mtakatifu siku ya Pentekote. Saa yenyewe watapewa **nguvu** zinazotoka juu kushuhudia Kristo. Mungu Baba alitoa ahadi ya Roho Mtakatifu ndani ya mashairi ya Agano la Kale kama Isaya 44:3; Ezekieli 36:27; Yoeli 2:28.

**E. Mwana wa watu anapanda mbinguni (24:50-53)**

**24:50,51** Kristo alipanda mbinguni siku makumi ine nyuma ya ufufuko wake. Alipeleka wanafunzi wake **hata Betania**, kwa matelemuko ya mashariki ya kilima cha mizeituni; **akanyanyua mikono yake, akawabariki.** Saa alipokuwa akifanya hivi **akachukuliwa juu katika mbingu.**

**24:52,53 Walimwabudu**, kisha **walirudia Yerusalema na furaha kubwa**. Kwa siku kumi zilizofuata walishinda **hekaluni wakisifu na wakibariki Mungu.**

Kwa **mwanzo** wa Habari Njema ya Luka tuliona hekaluni waamini wenye kupenda Mungu wakimwomba kwa kuja kwa Masiya ambaye walimngojea tangu miaka mingi. Habari Njema ilikwisha kwa pahali pale pale na waamini wenye kupenda Mungu **wakisifu na kubariki Mungu** kwa jibu la maombi haya, na kwa ukombozi uliotimizwa. Ni mwisho tamu kabisa kwa kitabu hiki "kizuri zaidi duniani" (Renan). **Amina.**

### NOTES

[1] (1:4) The same word (another) occurs in John 3:7: "You must be born again" (or "from above").

[2] (1:16,17) G. Coleman Luck, *Luke* p.17.

[3] (2:7) J. N. Darby, *Synopsis of the Books of the Bible,* III:293

[4] (2:8) Stewart, *Life and Teaching*, p. 24.

[5] (4:13) Stewart, *Life and Teaching,* p. 45.

[6] (4:28) John Charles Ryle, *Expository Thoughts on the Gospels,* St. Luke, 1:121.

[7] (6:27-29a) F. B. Meyer, *The Heavenlies*, p. 26.

[8] (7:21-23) C. G. Moore, quoted by W. H. Griffith Thomas, *Outline Studies in the Gospel of Luke,* p. 129.

[9] (7:27) F. L. Godet, *Commentary on the Gospel of Luke*, I:350.

[10] (7:30-34) Ryle, *St. Luke*, I:230.

[11] (7:49) *Ibid.,* p. 239.

[12] (8:18) G. H. Lang, *The Parabolic Teaching of the Scripture,* p. 60.

[13] (8:34-39) Darby, *Synopsis*, III:340.

[14] (8:51-53) Sir Robert Anderson, *Misunderstood Texts of the New Testament*, p. 51.

[15] (9:19-20) Stewart, *Life and Teaching*, pp. 109, 110.

[16] (9:32, 33) Ryle, *Gospels, St. Luke,* I:320.

[17] (10:16) Ryle, *St. Luke,* I:357, 358.

[18] (10:36, 37) F. Davidson, ed., *The New Bible Commentary,* p. 851.

[19] (10:42) C. A. Coates, *An Outline of Luke's Gospel*, p. 129.

[20] (10:42) Charles R. Erdman, *The Gospel of Luke,* p. 112.

[21] (11:41) Harry A. Ironside, *Addresses on the Gospel of Luke,* p. 390.

[22] (11:46) William Kelly, *An Exposition of the Gospel of Luke*, p. 199.

[23] (12:2,3) Godet, *Luke,* II:89.

[24] (12:15) J. R. Miller, *Come Ye Apart*, reading for June 10.

[25] (12:36) Kelly, *Luke,* p.214.

[26] (13:6-9) Lang, *Parabolic Teaching,* p. 230.

[27] (14:33) Ryle, *Gospels, St. Luke,* II:86.

[28] (14:34,35) Kelly, *Luke,* p. 249.

[29] (16:9) Arthur T. Pierson, further documentation unavailable.

[30] (16:9) J. N. Darby, *The Man of Sorrows*, p. 178.

[31] (17:10) Roy Hession, *The Calvary Road,* p. 49.

[32] (18:31-33) Ryle, *Gospels, St. Luke,* II:282.

[33] (19:41,42) Griffith Thomas, *Luke,* p. 303.

[34] (20:18) Others take the stone to refer to the repentant sinner falling in contrition on Jesus in true brokenness and being saved vs. the Christ-rejector being smashed to powder at the future judgment.

[35] (20:35) Coates, *Luke's Gospel,* p. 252.

[36] (21:20-24) *Christian Truth Magazine, November 1962*, p. 303.

[37] (21:20-24) Edward Gibbon, *The Decline and Fall of the Roman Empire*, II:95-101.

[38] (22:7) Leon Morris, *The Gospel According to Luke,* pp. 302-304.

[39] (22:47, 48) Stewart, *Life and Teaching,* p. 154.

[40] (23:13-17) *Ibid.* p. 161.

[41] (23:33) Stewart, *Life and Teaching*, p. 166.

[42] (23:34) Morgan, *Luke,* p. 269.

[43] (23:35-38) Stewart, *Life and Teaching*, p. 168.

## Bibliographie

Coates, C.A. *An Outline of Luke's Gospel, Kingston on Thames: Stow Hill Bible Tract Depot, n.d.*

Darby, J.N. *The Gospel of Luke,* London: James Carter, n.d.

____ . *The Man of Sorrows:* Glasgow: Pickering and Inglis, n.d.

____ . *Notes of Addresses on the Gospel of Luke,* London: C.A. Hammond, n.d.

Eerdman, Charles R. *The Gospel of Luke,* Philadelphia: The Westminster Press, 1921.

Goldenhuys, Norval, *Commentary on the Gospel of Luke,* 2 vols. Grand Rapids: Zondervan Publishing House, 1977.

Ironside, H. A. *Addresses on the Gospel of Luke*. New York: Loizeaux Brothers, 1947.

Kelly, William. *An exposition of the Gospel of Luke*, London: Pickering and Inglis, n.d.

Luck, G. Coleman. *Luke,* Chicago: Moody Press, 1960.

Morgan, G. Campbell. *The Gospel According to Luke,* New York: Fleming H. Revell Co., 1931.

Morris, Leon, *The Gospel According to St. Luke, TBC.* Grand Rapids: Wm. B. Eerdman Publishing Company, 1974.

Thomas, W. H. Griffith. *Outline Studies in the Gospel of Luke.* Grand Rapids: Kregel Publications, 1984.

# HABARI NJEMA KAMA ALIVYOANDIKA
# YOANE

## UTANGULIZI

*"Kitabu chenye maana zaidi duniani nzima"*

— A.T. Robertson

### I. Nafasi ya peke yake katika Kanuni

Yoane anatupasha wazi ya kwamba kusudi la kitabu chake ni kutangaza Habari Njema – "mupate kuamini" (Yn. 20:31). Ndani ya mia za miaka inayopita miigo midogo milioni ya kitabu hiki imechapwa na kutolewa kwa watu.

Lakini Wakristo wenye kupenda na kukomea zaidi wanapenda kitabu hiki sana, labda kupita vitabu vyote vingine vya Biblia. Yoane hakutuambia tu maneno yaliyotokea ndani ya maisha ya Bwana wetu. Alileta vilevile hotuba ndefu za mawazo yake, ndiye mtume mwenye kukomea aliyetembea pamoja na Kristo toka ujana wake katika Galilaya kufika hata uzee sana katika wilaya ya Asia. Shairi la kujulikana kupita yote mengine ndani ya Agano Jipya ni Yoane 3:16.

Hata kama Habari Njema ya Yoane ingalikuwa kitabu *cha pekee* katika Agano Jipya, tungalipata ndani yake mambo ya kujifunza (nyama, na maziwa) kutosha kwa maisha yetu yote.

### II. Mwandishi

Watu wameshindana na kubishana sana ndani ya miaka 150 inayopita kama nani aliandika Habari Njema hii ya ine. Bila shaka ni kwa sababu inashuhudia uungu wa Bwana wetu Yesu Kristo wazi kabisa. Watu walijaribu kuhakikisha kwamba Habari Njema hii haikuandikwa na mtu aliyeona maneno haya na macho yake mwenyewe, lakini na mtu wa akili sana aliyeishi miaka 50 kufika 150 nyuma ya wakati ule. Wanasema maandiko yake yanaonyesha mawazo ya kanisa juu ya Kristo, si maneno ambayo Yesu alisema na kutenda yeye mwenyewe.

Hatusomi ndani ya Habari Njema hii kama nani ndiye mwandishi wake, lakini kuna sababu nyingi kutufikirisha kwamba alikuwa Mtume Yoane, ndiye mmoja wa mitume kumi na wawili.

Clement ya Alexandria aliandika ya kuwa wakati Yoane alipokwisha kuishi miaka mingi, rafiki zake za karibu walimfikia kwa Efeso, na kumwomba kuandika Habari Njema itakayoongeza juu ya mambo yaliyoandikwa ndani ya Matayo, Marko na Luka. Hivi akiongozwa na Roho Mtakatifu Yoane aliandika Habari Njema hii inayoonyesha maana ya ndani ya *masemo* ya Yesu na ya *alama* zake kupita vitabu vingine vya Habari Njema.

*Ushahidi wa kuonekana kwa macho*

Theofilos wa Antiokia (karibu miaka 170 A.D.) ni mwandishi wa kwanza aliyetaja Yoane kuwa mwandishi wa kitabu hiki. Sehemu za Habari Njema hii ya ine zinaonekana ndani ya maandiko ya Ignatius, Justin Martyr (tunazani), Tatian, … na wazushi Basilides na Valentinus.

Kufika karibu 1850 A.D. watu wa dini ya uwongo walioitwa Alogi ndio watu wa pekee waliokataa kwamba Yoane aliandika Habari Njema ya ine.

Tunawaza mwisho wa Yoane 21 uliandikwa na viongozi vya kanisa kwa Efeso karibu na 100 A.D. Shairi 24 linatufikirisha mwanafunzi "aliyependwa na Yesu" kwa shairi 20, na katika sura 13. Watu wanafikiri alikuwa mtume Yoane.

Kwa miaka mingi watu walifikiri Habari Njema hii iliandikwa *karibu na mwisho* wa 200 A.D., lakini tarehe zinazotajwa ndani ya vipande vya miigo ya Yoane vilivyopatikana nyuma, zinatufikirisha kwamba iliandikwa kwa wakati Yoane alipokuwa kwanza hai.

*Ushahidi ndani ya maandiko yenyewe*

Ndani ya miaka 1880 kufika 1890 A.D., mwenye elimu mmoja, jina lake Askofu Westcott, alitaja maneno namna namna yaliyoonyesha kwamba Yoane alikuwa mwandishi wa kitabu hiki. Alionyesha kwamba (1) mwandishi alikuwa *Myuda* – namna alivyoandika na maneno ambayo alitumika nayo, na kujuana na desturi za Wayuda na habari za Agano la Kale inasimamia mawazo haya. (2) *Alikuwa Myuda aliyeishi katika Palestina* (1:28; 2:1,11; 4:46; 11:18, 54; 21:1, 2). Alijuana sana na Yerusalema na hekalu (5:2; 9:7; 18:1; 19:13,17,20, 41; ona vilevile 2:14-16; 8:20; 10:22). (3) *Aliona na macho yake mwenyewe* maneno aliyotaja ndani ya maandiko yake: habari za pahali, watu, saa na muda, na desturi (4:46; 5:14; 6:59, 12:21; 13:1; 14:5, 8; 18:6; 19:31). (4) *Alikuwa mtume* na alijua maneno mengi ya ndani ndani ya mitume na ya Bwana mwenyewe (6:19, 60, 61; 12:16; 13:22, 28; 16:19). (5) Mwandishi alitaja majina ya wanafunzi wengine, lakini hakutaja jina lake mwenyewe. Neno hili linatufikirisha kwamba yule mtu asiyetajwa ndani ya 13:23; 19:26; 20:2; 21:7, 20 ni *mtume Yoane.* Soma vilevile 1:14; 19:35 na 21:24, ndiyo mashairi mengine yanayoonyesha kwamba mwandishi aliona maneno haya na macho yake mwenyewe.

## III. Tarehe

Irenaeus alisema wazi ya kwamba Yoane aliandika Habari Njema yake wakati alipokuwa kwa Efeso. Kama ilikuwa kweli, haikuandikwa mbele ya miaka 69 au 70 A.D. wakati alipofika kule. Yoane hakutaja uharibifu wa Yerusalema, hivi labda aliandika Habari Njema yake mbele ya tukio lile la kuogofya.

Walimu wengine wanafikiri aliandika katika muda wa miaka 45-66 A.D., lakini zaidi yao wanafikiri pamoja na Irenaeus, Clement ya Alesanduria, na Jerome kwamba kitabu cha Yoane kiliandikwa nyuma ya kuandikwa kwa Matayo, Marko na Luka. Au labda hatusomi juu ya uharibifu wa Yerusalema ndani ya Habari Njema hii kwa sababu iliandikwa karibu miaka kumi na tano na hata makumi mbili *nyuma* ya tukio hiki, na watu walikuwa wameanza kulisahau. Irenaeus aliandika kwamba Yoane aliishi kufika utawala wa mfalme Trajan (aliyeanza kutawala kwa mwaka 98 A.D.). Tunasoma tena na tena juu ya "Wayuda" ndani ya Habari Njema hii, na neno hili linaonyesha kwamba Wayuda walikuwa wameanza kushindana na imani ya Wakristo na kuanza kuwatesa.

Hata kama haiwezekani kutaja wazi kabisa kama Yoane aliandika Habari Njema yake kwa mwaka gani, wenye elimu wanafikiri iliandikwa ndani ya muda wa miaka 85-95 A.D.

## IV. Msingi na Jambo Kubwa

Yoane aliandika juu ya maajabu au maalama saba kuonyesha kwamba Yesu ni Mungu: (1) Kugeuza maji kuwa mvinyo kwa ndoa katika Kana ya

Galilaya (2:9). (2) Kuponyesha mwana wa mkubwa wa ufalme (4:46–54). (3) Kuponyesha kiwete kwa birika la Betesaida (5:2–9). (4) Kulisha watu 5000 (6:1–14). (5) Yesu akitembea juu ya bahari ya Galilaya kuponyesha wanafunzi wake toka tufani (6:16–21). (6) Kuponyesha mtu aliyekuwa kipofu tangu kuzaliwa kwake (9:1–7). (7) Kufufua Lazaro toka wafu (11:1–44). Alifanya alama ya nane kwa wanafunzi wake tu, nyuma ya ufufuko wake – ajabu la kuvua samaki wengi sana (21:1-14).

Mwalimu mmoja, jina lake Charles R. Erdman, alisema Habari Njema ya ine "imesaidia watu wengi zaidi kuamini Kristo, imesukuma waamini wengi zaidi kumfuata na uaminifu na roho nzima, na kufazaisha walimu juu ya maneno mengi zaidi, kupita kitabu cho chote kingine."

Tukisoma Habari Njema ya Matayo, Marko na Luka tungefikiri utumishi wa Bwana Yesu duniani uliendelea kwa mwaka mmoja tu. Ndani ya Habari Njema ya Yoane tunasoma juu ya siku kubwa zilizoshikwa kila mwaka, nazo zinaonyesha kwamba utumishi wake uliendelea kwa miaka mitatu. Fikiri juu ya mashairi haya: Karamu ya kwanza ya Pasaka (2:12, 13); "karamu ya Wayuda," labda Pasaka au Purimu (5:1); Pasaka ya pili (au ya tatu) (6:4); Siku kubwa ya vibanda (7:2); karamu ya Kutabaruku (10:22); na Pasaka ya mwisho (12:1).

Yoane, kupita Matayo, Marko, na Luka, anataja na utaratibu kabisa wakati gani maneno fulani yaliyotokea. Kwa mfano anataja saa saba (4:52); siku ya tatu (2:1); siku mbili (11:6); na siku sita (12:1).

Maandiko ya Habari Njema hii, barua za Yoane, na kitabu cha Ufunuo Yoane aliyoandika, ilikuwa namna nyingine na maandiko ya watu wengine. Hata kama aliandika kwa Kiyunani, mawazo yake yalikuwa kwa Kiebrania. Alisema kwa mafungu ya maneno machache yenye maana na kweli kubwa. Alitumika na maneno machache kupita waandishi wengine, lakini yalikuwa yenye maana kubwa. Alitumika na maneno makubwa fulani tena na tena. Ona Baba (mara 118), amini (100), dunia (78), mapendo (45), ushuhuda, kushuhudu, vivi hivi (mara 47), uzima (37), nuru (24).

Hesabu 7, na 7 mara hesabu nyingine, zinaonekana tena na tena ndani ya Habari Njema hii. Hesabu hii inatufikirisha juu ya ukamilifu ndani ya Maandiko Matakatifu (ona Mwanzo 2:1-3). Ndani ya Habari Njema hii Roho ya Mungu anakamilisha na kutimiza ufunuo wa Mungu ndani ya Yesu Kristo, hivi tunaona hesabu hii *saba* tena na tena.

Mara saba ndani ya Yoane Bwana Yesu alisema "Mimi ni … ": "Mkate wa Uzima" (6:35, 41, 48, 51); "Nuru ya Dunia" (8:12; 9:5); "Mlango" (10:7, 9); "Mchungaji Mwema" (10:11, 14); "Ufufuko na Uzima" (11:25); "Njia, na Kweli na Uzima" (14:6); na "Mzabibu" (15:1,5). Kuna mara saba nyingine alipojiita "Mimi" bila kuongeza neno fulani nyingine, kama kwa 4:26; 6:20; 8:24, 28, 58; 13:19; 18:5, 8 (mara mbili).

Ndani ya sura 6, inayofundisha juu ya Mkate wa Uzima, neno kwa Kiyunani linalotafsiriwa "mkate" na "mikate" linaonekana mara 21, ndiyo 7 x 3. Na ndani ya hotuba juu ya Mkate wa Uzima tunasoma mara saba juu ya "mkate toka "mbinguni," na mara saba juu ya mkate "ulioshuka toka mbinguni.

Yoane aliandika na kusudi la kuaminisha wasomaji wake ya kwamba "Yesu ni Kristo, Mwana wa Mungu, na kwa kuwafundisha kwamba yeye *ni* **Mungu.**

## HABARI YALIYOMO

1. MANENO YA MBELE: KUJA KWA KWANZA KWA MWANA WA MUNGU (1:1–18)
2. MWAKA WA KWANZA WA UTUMISHI WA MWANA WA MUNGU (1:19 – 4:54)
3. MWAKA WA PILI WA UTUMISHI WA MWANA WA MUNGU (Sura 5)
4. MWAKA WA TATU WA UTUMISHI WA MWANA WA MUNGU: GALILAYA (Sura 6)
5. MWAKA WA TATU WA UTUMISHI WA MWANA WA MUNGU: YERUSALEMA (7:1 – 10:39)
6. MWAKA WA TATU WA UTUMISHI WA MWANA WA MUNGU: PEREA (10:40 – 11:57)
7. UTUMISHI WA MWANA WA MUNGU KWA WATU WAKE MWENYEWE (Sura 12 – 17)
8. MAUMIVU NA MAUTI YA MWANA WA MUNGU (Sura 18, 19)
9. KUSHINDA KWA MWANA WA MUNGU (Sura 20)
10. MANENO YA MWISHO: MWANA MFUFULIWA PAMOJA NA WATU WAKE (Sura 21)

# Maelezo

### 1. MANENO YA MBELE: KUJA KWA KWANZA KWA MWANA WA MUNGU (1:1-18)

Yoane alianza Habari Njema yake kwa njia ya kusema juu ya *Neno* – lakini hakueleza mara moja kama Neno hili ni nini au nani. Tunatumika na maneno kuonyesha mawazo yetu kwa watu wengine. Lakini Yoane hakuandika juu ya *masemo* lakini juu ya *Mtu*, ndiye Bwana Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Mungu alijionyesha wazi kwa watu wa dunia kwa njia ya Bwana Yesu. Kwa njia ya kufika duniani, Kristo alitufunulia Mungu wazi. Kwa njia ya kutukufia msalabani, ametuonyeshea ukubwa wa mapendo wa Mungu. Hivi Kristo ni Neno la Mungu lenye uzima kwa watu, mwenye kuonyesha mawazo ya Mungu.

#### A. Neno katika milele na katika wakati wa sasa (1:1-5)

**1:1 Katika mwanzo alikuwa Neno**. Yeye mwenyewe hakuwa na mwanzo, lakini alikuwa tangu milele. Hakuumbwa. Hakuwa na mwanzo. **Neno alikuwa pamoja na Mungu,** Mwenye kukaa pamoja na Mungu. **Neno lilikuwa Mungu.** Hakukaa tu **pamoja na Mungu**, lakini yeye mwenyewe **alikuwa Mungu.**

Biblia inafundisha kwamba kuna Mungu mmoja, na watatu ndani ya yule mmoja – Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Watatu hawa wote ni Mungu. Tutasoma tena na tena ndani ya Habari Njema ya kwamba *Yesu Kristo ni Mungu*. Hapa ni mara ya kwanza. Haitoshi kusema kwamba yeye ni “mungu” (kama miungu mingine), au ya kwamba yeye ni kama Mungu. Biblia inafundisha ya kwamba yeye *ni* **Mungu**.

**1:2** Ni kama shairi 2 linasema maneno ya shairi 1 mara ya pili, lakini si

hivi. Shairi hili linaonyesha kwamba Kristo ni Mungu tangu milele, bila **mwanzo**. Mwanzo wake haukuwa kama mtoto mchanga kwa Betelehemu. Wala hakugeuka mungu nyuma ya ufufuko wake, kama watu wengine wanavyo-fundisha sasa. Yeye ni Mungu tangu milele.

**1:3 Vitu vyote vilifanyika kwa huyu**. Yeye mwenyewe hakuumbwa, lakini alikuwa Mwumba wa **vitu vyote.** Ali-umba watu, nyama, nyota za mbingu, malaika – **vitu vyote** vinavyoonekana na visivyoonekana kwa macho. **Pasipo yeye hakikufanyika hata kitu kimoja kilichofanyika.** Ni yeye aliyefanya kila kitu. Akiwa Mwumba, yeye ni mkubwa kupita kitu cho chote alichoumba. Watatu wote wa Umungu walishiriki ndani ya kazi ya kuumba: “Mungu ali-umba mbingu na dunia” (Mwa.1:1) “Roho ya Mungu akatulia juu ya uso wa maji” (Mwa. 1:2). “Katika yeye (Kristo) vitu vyote viliumbwa … kwa njia yake na kwa ajili yake” (Kol. 1:16b)

**1:4 Ndani yake ulikuwa uzima.** Maana ya neno hili si kusema tu kwamba alikuwa na uzima, lakini ya kwamba **uzima** wote *unatoka* kwake, wa mwili na wa roho. Wakati tulipoza-liwa duniani, tulipokea uzima wa mwili. Wakati tunapozaliwa tena, tunapokea uzima wa roho. Wote unatoka kwake.

**Uzima ulikuwa nuru ya watu.** Yule ambaye alitupa sisi uzima ni **nuru ya watu** vilevile. Anatuongoza. Ndiyo, tuna uzima lakini zaidi ya ile inatupasa kujua namna gani inatupasa kuishi, kujua kusudi la maisha yetu na njia kutu-fikisha mbinguni. Kristo ambaye alitupa sisi **uzim**a anatupa sisi **nuru** kwa njia yetu hapa duniani.

Kuna majina saba mazuri sana kwa Bwana wetu Yesu Kristo ndani ya sura hii ya kwanza ya Habari Njema. Anaitwa (1) Neno (mash. 1, 14); (2) Nuru (mash. 5, 7); (3) Mwana-kondoo wa Mungu (mash. 29, 36); (4) Mwana wa Mungu (mash. 34, 49); (5) Kristo (Masiya) (sh.41); (6) Mfalme wa Israeli (sh.49); na (7) Mwana wa watu (sh.51). Majina mane ya kwanza yanatajwa mara mbili au zaidi, na ni kwa watu wote wa dunia. Majina matatu ya mwisho yanatajwa mara moja moja tu, na ni zaidi kwa Israeli, watu wa zamani wa Mungu.

**1:5 Nuru ilingaa katika giza.** Kufika kwa zambi duniani kulileta **giza** kwa nia za watu. Kulileta **giza** kwa dunia nzima, maana watu hawakujua Mungu wala hawakutaka kumjua. Bwana Yesu ali-ingia katika **giza** hili – **nuru** iliyongaa katika giza.

Au labda maana yake ni ya kwamba **giza halikui***shinda.* Hata kama watu waliikataa, uadui wao haukuzuiza **nuru** ya kweli isingae.

### B. Utumishi wa Yoane Mbatizaji (1:6-8)

**1:6** Shairi 6 ni juu ya Yoane Mbatizaji, si juu ya mwandishi wa kitabu hiki. Yoane Mbatizaji alitumwa **kutoka kwa Mungu** kuwa mtangulizi wa Bwana Yesu Kristo. Kazi yake ilikuwa kutangazia watu kuja kwa Kristo na kuwaambia ku-jitayarisha kumpokea.

**1:7 Mtu huyu alikuja** kuwa ushuhuda ya kwamba Yesu alikuwa kweli **Nuru** ya dunia, ili watu **wote** waweze ku-mwamini.

**1:8** Kama Yoane angalitaka kukokota macho ya watu juu yake mwenyewe kama asingalifanya kazi aliyopewa. Kazi yake ilikuwa kukokota macho ya watu juu ya Yesu, si juu yake mwenyewe.

### C. Kuja kwa kwanza kwa Mwana wa Mungu (1:9-18)

**1:9 Ilikuwa nuru ya kweli.** Tangu eoni zinazopita watu wamesema wao ndio viongozi na waokozi, lakini Yule ambaye Yoane alishuhudia alikuwa **nuru ya kweli** inayotia nuru kila mtu anayekuja katika ulimwengu. Ni kwa sababu **nuru**

**ya kweli ilikuja duniani** kila mtu anapewa nuru. Si kusema ya kwamba kwa njia ya kuja kwa nuru kila mtu alipata kujua habari nyingine juu ya Kristo ndani ya roho yake. Na vilevile maana yake haiko kwamba watu wote wamesikia habari za Bwana Yesu kwa wakati nyingine. Maana yake ni ya kwamba **nuru** inangaa juu ya watu wote, wa mataifa yo yote, na wenye rangi yo yote. Ni kusema ya kwamba kwa njia ya kungaa juu ya watu wote, Bwana Yesu amefunua tabia ya kweli ya watu. Yeye alikuwa mkamilifu, na kuja kwake kulionyesha kwamba watu wa dunia si wakamilifu hata kidogo. Wakati chumba ni giza, huwezi kuona uvumbi juu ya vitu ndani yake. Lakini wakati nuru inapowashwa, hali ya kweli ya chumba inaonekana. Vivyo hivyo kungaa kwa **nuru ya kweli** kunafunua hali ya kweli ya roho za watu.

**1:10** Tangu wakati wa kuzaliwa katika Betelehemu kufika siku aliporudi mbinguni, Bwana Yesu **alikuwa** ndani ya **ulimwengu** ule ule sisi tunaokaa ndani yake kwa wakati wa sasa. Ni yeye aliyeumba ulimwengu huu, na ulimwengu ni mali yake. Lakini watu wa dunia hawakutambua neno hili, wakazani alikuwa mtu tu kama wao. Walimtendea kama mgeni na mhuni.

**1:11 Alikuja kwake.** Hakuingia shamba la mtu mwingine bila ruhusa, lakini aliishi kwa inchi yeye mwenyewe aliyofanya. **Watu wake hawakumpokea.** Ndiyo, watu wote wa dunia walimkataa, lakini taifa la Wayuda walikuwa watu wachaguliwa wake mwenyewe duniani. Wakati alipokuja duniani alifika kwao kama Masiya yao, lakini **hawakumpokea.**

**1:12** Hivi sasa anajitoa tena kwa watu wote wa dunia na anawapa wote ambao **wanampokea uwezo wa kuwa watoto wa Mungu.**

Shairi hili linaonyesha wazi namna gani tunaweza **kugeuka watoto wa Mungu**. Si kwa njia ya matendo mema, wala kwa njia ya watu wa kanisa fulani – lakini kwa njia ya kumwamini **yeye**, maana kuamini **jina lake.**

**1:13** Kwa kugeuka mtoto hapa duniani, inampasa **kuzaliwa**. Vivyo hivyo kwa kugeuka mtoto wa Mungu inapasa mtu kuzaliwa mara ya pili. Shairi hili linatujulisha *njia tatu* zisizowezesha mtu kuzaliwa tena, na *njia ya pekee* kwaye kuzaliwa tena. **Si kwa damu**. Maana yake mtu hageuki Mkristo kwa sababu ana wazazi walio Wakristo. Wokovu haupitishwi kwa njia ya **damu**. Wala si kwa **mapenzi ya mwili.** Ni kusema mtu hawezi kujipatia uzima mpya kwa **nguvu** yake mwenyewe. Hata akitaka kuokolewa, **mapenzi** yake mwenyewe hayatoshi kumwokoa. Wala si **kwa mapenzi ya mtu**. Hakuna mtu anayeweza kuokoa mtu mwingine. Kwa mfano, mwalimu anaweza kutaka sana kwa mtu fulani kuokolewa, lakini hana uwezo kumzalisha tena. Basi, neno hili linafanyikana namna gani? Jibu lenyewe ndilo hili: **"lakini kwa Mungu."** Mungu tu ana uwezo kuzalisha mtu tena.

**1:14 Neno alifanyika mwili** wakati Yesu alipozaliwa kama mtoto mchanga ndani ya sanduku ya kulisha nyama kwa Betelehemu. Alikuwa tangu zamani kama Mwana wa Mungu pamoja na Baba mbinguni, lakini sasa alichagua kuja duniani ndani ya mwili wa mtu. **Akakaa kwetu.** Hakuonekana kwa muda fupi tu, lakini kwelikweli Mungu alikuja kwa dunia hii na kuishi hapa kama Mtu katikati ya watu. Maana ya Neno hili "**alikaa**" ni "kusimamisha hema." Mwili wake ulikuwa hema ndani yake aliishi katikati ya watu kwa miaka makumi tatu na tatu.

**"Tukatazama utukufu wake."** Ndani ya Biblia maana ya "utukufu" ni mara nyingi nuru ya kungaa sana iliyoonekana wakati Mungu alipoonekana. Maana

yake ni vilevile ukamilifu na ubora wa Mungu. Wakati Bwana Yesu alipokuwa duniani alifunika utukufu wake ndani ya mwili wa mtu. Lakini hata hivi utukufu wake ulifunuliwa kwa njia mbili. Kwanza ulikuwa **utukufu** wa *maisha yake safi na mema.* Maisha yake yalikuwa matakatifu, bila kipaku. Na tena **utukufu** wake ulionekana wazi juu ya mlima (Mt 17:1,2). Kwa wakati ule Petro, Yakobo na Yoane waliona uso wake ukingaa kama jua, na mavazi yake yalingaa kama nuru. Wanafunzi wale watatu walionyeshwa mbele utukufu bora wa Bwana, utukufu ambao atakuwa nao wakati atakaporudi duniani na kutawala kwa miaka elfu moja.

Wakati Yoane aliposema **"tukatazama utukufu wake,"** bila shaka alifikiri zaidi **utukufu** wa *maisha na mwenendo wake mwema.* Yeye na wanafunzi wengine waliona ajabu la maisha makamilifu aliyoishi hapa duniani. Bila shaka aliwaza vilevile juu ya maneno yaliyotokea mlimani. **Utukufu** ambao wanafunzi waliona uliwaonyeshea ya kwamba alikuwa kweli Mwana wa Mungu. Yesu ni **Mwana pekee akitoka kwa Baba,** maana yake hakuwa na Mwana mwingine kama yeye. Ndiyo, waamini wa kweli wote ni wana wa Mungu, lakini Yesu ni Mwana wa Mungu namna nyingine. Kama Mwana wa Mungu, yeye ni sawa na Mungu.

Mwokozi **amejaa neema na kweli**. Alikuwa na wema kwa watu wasiostahili kuupokea, na vilevile alitenda kwa haki na kweli kabisa, na hakukubali zambi kamwe, wala kutoa uzuru kwa watu kuitenda. Mungu peke yake anaweza kuwa mwenye neema timilifu pamoja na haki kabisa.

**1:15** Yoane **alishuhudia** Yesu kwamba alikuwa Mwana wa Mungu. Wakati Bwana asipoanza utumishi wake katikati ya watu bado, Yoane alikuwa amepasha watu habari zake. Halafu wakati Yesu alipokuja, Yoane alisema, "Huyu ndiye niliwapasha habari zake." Yesu alizaliwa miezi sita **nyuma** ya Yoane, na alitokea katikati ya watu muda fulani nyuma ya wakati Yoane alipokuwa akihubiri na kubatiza watu. Lakini Yesu alikuwa **mbele ya** Yoane. Alikuwa mkubwa kupita Yoane; alistahili kupokea heshima kupita Yoane, kwa sababu **alikuwa mbele** ya Yoane. Yeye ni tangu milele – Mwana wa Mungu.

**1:16** Wote wanaoamini Bwana Yesu wanapokea nguvu ya roho toka **utimilifu wake. Utimilifu wake** ni mkubwa sana hata unatosha kwa waamini wote ndani ya inchi zote na kwa kila muda. Tunafikiri maana ya **neema juu ya neema** ni "neema nyingi." Ni **neema** ya Mungu anayomwangia watoto wake wapendwa.

**1:17** Yoane anaonyesha tofauti katikati ya muda wa Agano la Kale na Agano Jipya. **Torati iliyotolewa kwa mkono wa Musa** haikuonyesha neema. Iliagiza watu kutii na iliwahukumu hata mauti kama wasipofanya hivi. Ilionyeshea watu nini iliwapasa kufanya lakini haikuwapa uwezo kufanya hivi. Ilitolewa kuonyeshea watu kwamba wao ni wenye zambi, lakini haikuweza kuwaokoa toka zambi zao. **Lakini neema na kweli zilikuja kwa mkono wa Yesu Kristo**. Hakuja kuhukumu dunia lakini kuwaokoa wale wasiostahili, ambao hawakuweza kujiokoa wenyewe, na waliokuwa adui zake. Hii ndiyo **neema** ya kweli.

Si **neema** tu, lakini **kweli** vilevile ilikuja **kwa njia ya Yesu Kristo.** Alisema juu yake mwenyewe, "Mimi ni … kweli." Matendo na masemo yake yote yalikuwa haki na maaminifu kabisa. Hakuficha **kweli** kusudi aweze kutenda kwa neema. Alipenda wenye zambi, lakini hakupenda zambi zao. Alijua kwamba mishahara ya zambi ni mauti. Hivi alikufa yeye mwenyewe kulipa azabu ya mauti ambayo sisi tulistahili kupokea, ili aweze kututendea kwa wema

tusiostahili kwa njia ya kuokoa nafsi zetu, na kututayarishia pahali pa kukaa mbingini.

**1:18 Hakuna mtu aliyeona Mungu wakati wo wote.** Mungu ni roho na hatuwezi kumwona na macho. Hana mwili, hata kama ndani ya Agano la Kale alionekana kwa watu mara nyingine kwa mfano wa Malaika au Mtu kwa kusema na watu wake. Bwana Yesu ni **Mwana pekee** wa Mungu. Hakuna mwingine kama yeye. Yeye ni karibu sana na Baba, na hata wakati alipokuwa hapa duniani alikuwa **katika kifua cha Baba** vilevile. Alikuwa mmoja na Mungu na sawa na Mungu, na alifunulia watu kama Mungu ni namna gani. Wakati watu walipoona Yesu, waliona Mungu. Walisikia Mungu akisema nao. Walijuana na mapendo na huruma yake. Mawazo na mashauri ya Mungu kwa watu **yamefunuliwa** wazi na Kristo.

## 2. MWAKA WA KWANZA WA UTUMISHI WA MWANA WA MUNGU (1:19–4:54)

### A. Ushuhuda wa Yoane Mbatizaji (1:19-34)

**1:19** Wakati habari zilipofikia **Yerusalema** ya kwamba mtu aliyeitwa **Yoane** alipokuwa akiagiza taifa la Israeli kutubu kwa sababu Masiya alikuwa akikaribia, **Wayuda walituma** wengine wa **makuhani na Walawi** kufahamu kama mtu huyu alikuwa nani. **Makuhani** ndio wale waliofanya kazi kubwa hekaluni, na **Walawi** walifanya utumishi mwingine pale. Waliuliza Yoane, **"Wewe nani?"** "Wewe ndiye Masiya ambaye tunangoja kufika kwake kwa miaka mingi sana?"

**1:20** Watu wengine wangejitafutia heshima kwa njia ya kusema wao ni Kristo. Lakini Yoane alikuwa mshuhuda mwaminifu. Alisema wazi kwamba yeye **siye Kristo (Masiya).**

**1:21,22** Wayuda walingojea Elia kufika duniani mbele ya kuja kwa Kristo (Mal. 4:5). Hivi waliwaza kama Yoane si Masiya, labda alikuwa **Elia**. Lakini Yoane alisema yeye si Elia vilevile. Katika Torati 18:15 Musa alikuwa amesema, "Bwana Mungu wako atakusimamishia nabii toka katikati yako, mmoja wa ndugu zako, sawasawa nami; mumsikilize yeye." Wayuda walikumbuka unabii huu, wakafikiri labda Yoane ni **nabii** huyu. Lakini Yoane alijibu siye. Watu hawa waliotumwa kulizana naye wangalipata haya kama wangalirudi kwao bila **jibu**, hivi waliomba Yoane kuwaambia wazi kama yeye ni nani.

**1:23 Akasema: "Mimi ni sauti ya mtu anayepaza sauti jangwani."** Ndani ya jibu lake Yoane alitaja sehemu ya Isa. 40:3, pahali tunaposoma kwamba mtangulizi atatokea kutangaza kwamba Kristo atakuja. Hivi Yoane alisema yeye ndiye mtangulizi huyu. Yeye alikuwa **sauti,** na Israeli walikuwa **jangwa**. Kwa sababu ya zambi zao walikuwa wamekwenda mbali na Mungu, na walikuwa wamekauka rohoni, kama jangwa. Yoane alijiita **sauti** tu. Hakujionyesha kuwa mtu mkubwa aliyestahili kupokea sifa na heshima, lakini **sauti** – si kwa watu kuona lakini kusikia. Yoane alikuwa **sauti,** lakini Kristo alikuwa Neno. Neno linahitaji sauti kwa kulitangaza, na sauti haina faida bila neno. Neno ni kubwa sana kupita sauti, lakini sisi vilevile tunaweza kuwa sauti kwa Bwana.

Habari za Yoane ndizo hizi: **"Nyosheni njia ya Bwana."** Maana yake, "Masiya anakuja. Ondosheni toka maisha yenu maneno yote yanayoweza kuwazuiza musimpokee. Tubuni zambi zenu, ili aweze kuja na kutawala juu yenu kama Mfalme wa Israeli."

**1:24,25 Wafarisayo** walijivuma sana juu ya kujua sheria na kujaribu kutii hata maagizo yote madogo sana sana ya Agano la Kale. Wengi wao walikuwa wadanganyifu waliojaribu kuonekana kama watu wa dini, lakini walioishi

maisha ya zambi. Walitaka kujua nani alimpa Yoane amri kubatiza watu kama yeye si mmoja wa watu wakubwa ambao walitaja.

**1:26,27 Yoane** alijibu, **“Mimi ninabatiza na maji.”** Hakutaka watu kufikiri kwamba *yeye* ni mtu mkubwa. Kazi yake ilikuwa tu kutayarisha watu kwa Kristo. Wakati wasikiaji wake walipotubu zambi zao, aliwabatiza na maji kama alama kuonyesha kwamba walikuwa wamegeuka rohoni. Yoane alikaa kusema juu ya Yesu wakati alipoongeza, **“Mmoja anasimama katikati yenu ambaye hamjui.”** Wafarisayo hawakumtambua kuwa Masiya ambaye walitazamia kwa muda mrefu. Ni kama Yoane alisema na Wafarisayo, “Musifikiri mimi ni mtu mkubwa. **Yule** aliye mkubwa ndiye Bwana Yesu; lakini **hamujui** kama yeye ni nani.” Ni yeye anayestahili. Alikuja nyuma ya Yoane Mbatizaji, lakini ni yeye **anayestahili** kupokea sifa na ukubwa. Ilikuwa kazi ya mtumwa kufungua kiatu cha bwana wake, lakini Yoane alifikiri **hakustahili** kufanya hata kazi ile ya chini kwa Kristo.

**1:28** Hatujui kabisa kama **Betania** ulikuwa wapi, lakini haukuwa Betania kile kingine karibu na Yerusalema.

**1:29 Kesho yake**, nyuma ya kufika kwa Wafarisayo toka Yerusalema, **Yoane** alinyanyua macho yake, **akaona Yesu anakuja kwake, akalalamika, “Tazama Mwana-kondoo wa Mungu** anayechukua **zambi ya ulimwengu!”** Mwana-kondoo alikuwa nyama ya sadaka kwa Wayuda. Mungu alikuwa amefundisha watu wachaguliwa wake kuchinja mwana-kondoo na kunyunyiza damu yake kama sadaka. Mwana-kondoo alichinjwa kwa pahali pao, na damu yake ilimwangwa ili zambi zao ziweze kusamehewa.

Lakini damu ya wana-kondoo waliochinjwa kwa wakati wa Agano la Kale haikuweza kuondoa zambi. Walikuwa mifano tu iliyotazama mbele kwa siku ile wakati Mungu atakapoleta **Mwana-kondoo** atakaye*ondoa* zambi kweli. Kwa mia za miaka Wayuda waliopenda Mungu walingojea kufika kwa **Kondoo** huyu. Sasa amekuja, na Yoane, na sauti ya mshindaji, alitangaza kufika kwa **Mwana-kondoo** wa kweli **wa Mungu.**

Wakati aliposema Yesu anachukua **zambi ya ulimwengu,** maana yake haiko ya kwamba zambi za kila mtu zinasamehewa. Mauti ya Kristo ilitosha kulipa kwa zambi za ulimwengu mzima, lakini wenye zambi wale tu wanaopokea Bwana Yesu kuwa Mwokozi wao wanasamehewa.

J.C. Jones alionyesha kwamba shairi hili linaonyesha bora ya upatanisho wa Kristo:

1. Zabihu za dini ya Wayuda zilikuwa wana-kondoo wasio na akili; zabihu ya Ukristo ni Mwana-kondoo wa Mungu.
2. Zabihu za dini ya Wayuda zili*kumbusha* zambi kila mwaka; zabihu ya Ukristo ili*ondosha* zambi. “Aliondosha zambi kwa njia ya kujitoa mwenyewe kuwa zabihu ya zambi.”
3. Faida ya zabihu za Wayuda ilikuwa kwa taifa moja tu; faida ya zabihu ya Ukristo ni kwa mataifa yote; “anachukua zambi za ulimwengu.”[1]

**1:30,31** Yoane alikaa kuwakumbusha bila kuchoka kwamba alikuwa akitayarisha njia tu kwa Mmoja aliye mkubwa kupita yeye mwenyewe na aliyekuwa karibu kutokea. Yesu alikuwa mkubwa kupita Yoane kwa kipimo Mungu ni mkubwa kupita mtu. Yoane alizaliwa miezi michache mbele ya Yesu, lakini Yesu alikuwa tangu milele. Wakati Yoane aliposema, **“Sikumjua,”** maana yake si kusema ya kwamba hakumwona mbele.

Wazazi wa Yoane na Yesu walikuwa ndugu na tunawaza kwamba walijuana. Lakini Yoane hakutambua Yesu kuwa Masiya kufika wakati wa ubatizo wake.

Kazi ya Yoane ilikuwa kutayarisha njia ya Bwana, kisha kumwonyesha kwa watu wa **Israeli** wakati alipotokea. Kwa sababu hii Yoane alibatiza watu kwa **maji** – kuwatayarisha kwa kuja kwa Kristo. Hakufanya hivi kukokota watu karibu na yeye mwenyewe kuwa wanafunzi wake.

**1:32** Shairi hili ni juu ya wakati Yoane alipobatiza Yesu katika Yorodani. Wakati Bwana alipotoka maji, **Roho** wa Mungu alimshukia **kama hua**, **akakaa juu yake** (ona Mt. 3:16). Mwandishi aliendelea kueleza neno hili.

**1:33** Mungu alikuwa amefunulia Yoane kwamba Masiya alikuwa karibu kutokea, na wakati atakapokuja **Roho** atashuka na kukaa **juu yake**. Halafu wakati neno hili lilipokuwa likifanyikana na Yesu, Yoane alifahamu kwamba huyu ndiye atakayebatiza **kwa Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu** ni mmoja wa wale watatu katika Uungu. Yeye ni sawasawa na Mungu Baba na Mungu Mwana.

Yoane alibatiza **na maji**, lakini Yesu atabatiza na **Roho Mtakatifu**. Neno hili lilitokea siku ya Pentekote (Mdo. 1:5; 2:4, 38). Kwa wakati ule **Roho Mtakatifu** alishuka toka mbinguni kukaa ndani ya mwili wa kila mwamini na kufanyiza kila mwamini kuwa kiungo cha kanisa, Mwili wa Kristo (1 Kor. 12:13).

**1:34** Kwa sababu ya maneno Yoane aliyoona wakati wa ubatizo wa Yesu, **alishuhudu** waziwazi ya kwamba Yesu wa Nazareti ni **Mwana wa Mungu** atakayefika duniani. Wakati Yoane aliposema Kristo ni **Mwana wa Mungu,** maana yake ilikuwa kwamba alikuwa Mungu Mwana.

### B. Mwito wa Anderea, Yoane, na Petro (1:35-42)

**1:35,36** **Kesho yake** ndiyo siku ya tatu tuliyosoma juu yake. **Yoane** alikuwa **pamoja na wawili wa wanafunzi** wake mwenyewe. Watu hawa walikuwa wamesikia mahubiri ya Yoane na kuyaamini. Lakini walikuwa hawajakutana na Yesu bado wao wenyewe. Sasa Yoane alishuhudia Bwana waziwazi mbele ya watu. Siku iliyopita alikuwa amesema juu yake kama Mwana-kondoo wa Mungu na kazi yake kuondoa zambi ya ulimwengu. Sasa alisema juu yake kama Mwana-kondoo wa Mungu tu. Habari zake zilikuwa fupi; hazikuwa juu yake mwenyewe, lakini zote juu ya Mwokozi.

**1:37** Yoane alipoteza **wawili wa wanafunzi** wake kwa sababu ya mahubiri yake maaminifu, lakini alifurahi kwa sababu walikwenda kufuata **Yesu**. Vivyo hivyo inatupasa sisi kuweka roho juu ya rafiki zetu kufuata Bwana, kwa pahali pa kutuheshimu sisi.

**1:38** Mwokozi anaweka roho juu ya wote ambao wanamfuata. Hapa aliuliza wanafunzi wale wawili, **"Munatafuta nini?"** Alijua jibu kwa ulizo hili; anajua maneno yote, lakini alitaka kusikia jibu lao, ndilo **"Rabi … unakaa wapi?"** Jibu hili lilionyesha hamu yao kuwa pamoja na Bwana na kujuana naye kupita. Hawakutaka kukutana tu naye. Walikuwa na hamu sana kushiriki naye. Rabi ni Kiebrania kwa Mwalimu (au kusema "mkubwa wangu").

**1:39** **Aliwaambia, "Kujeni na mutaona."** Hamu ya kila mtu anayetaka na roho ya kweli kujua kupita juu ya Mwokozi itashibishwa. Yesu aliita wanafunzi hawa wawili kumfuata kwa pahali alipopanga kwa wakati ule – bila shaka ilikuwa nyumba ya wamasikini tu.

**Walikuja na waliona pahali alipokaa; wakakaa kwake siku ile; ilikuwa karibu na saa kumi.** Ilikuwa heshima kubwa sana kwa watu hawa kushinda usiku ule nyumbani mwa Mwumba wa ulimwengu. Walikuwa katikati ya Wayuda wa kwanza waliotambua kwamba yeye ni Masiya.

**Saa kumi** ni saa ine ya asubui, au saa kumi ya mangaribi. Zaidi ya watu wa-

nafikiri ni saa ine ya asubui (saa ya Waroma).

**1:40 Mmoja** wa wanafunzi hawa wawili alikuwa **Anderea.** Anderea hajulikani sana kwa wakati wa sasa kama **ndugu yake Simoni Petro,** lakini tunaona kwamba yeye alikuwa wa kwanza wa wanafunzi hawa wawili aliyekutana na Bwana. Jina la mwanafunzi wa pili halitajwi, lakini karibu walimu wote wa Biblia wanafikiri alikuwa Yoane – mwandishi wa Habari Njema hii. Wanafikiri kwamba unyenyekevu wake ulimzuiza asitaje jina lake.

**1:41** Mara nyingi wakati mtu anapokutana na Yesu, anataka watu wa jamaa yake kukutana naye vilevile. Hataki kuchunga habari hizi njema kwa roho yake tu. Hivi Anderea alifika mbio karibu na **ndugu yake mwenyewe, ndiye Simoni,** na habari zake za ajabu: **"Tumeona Masiya, maana yake Kristo!"** Lilikuwa tangazo la kushangaza kabisa! Kwa miaka elfu ine au zaidi watu walikuwa wamengojea kufika kwa yule aliyeahidiwa, ndiye Kristo, Mpakaliwa wa Mungu. Sasa **Simoni** alisikia toka kinywa cha ndugu yake mwenyewe habari za kushitusha ya kwamba **Masiya** alikuwa karibu! Habari za Anderea zilikuwa fupi tu, maneno matano tu, "**Tumeona Masiya, maana yake Kristo,"** – lakini Mungu alitumika nazo kukokota Petro kwake. Neno hili linatuonyesha kwamba hatuhitaji kuwa wahubiri wakubwa wanaojua kuunganisha masemo ya elimu ndani ya hotuba zao. Sharti tupashe habari za Yesu kwa watu na masemo ya kila siku wanayoweza kufahamu vizuri. Ni kazi ya Mungu kuwaaminisha.

**1:42** Anderea alileta ndugu yake kwa pahali pazuri na mtu mzuri. Hakumfikisha kwa kanisa, kwa dini fulani au mhubiri wa kujulikana. **Alimpeleka kwa Yesu.** Lilikuwa tendo la faida kabisa! Kwa sababu ya bidii ya Anderea, Simoni aligeuka mvuvi mkubwa wa watu kwa wakati wa nyuma, na mmoja wa viongozi katikati ya mitume. Simoni aliheshimiwa na watu kupita Anderea, lakini bila shaka Anderea atashiriki ndani ya zawabu ya Simoni kwa sababu alikuwa Anderea ambaye alimpeleka kwa Yesu. Anderea hakuhitaji kujulisha Bwana jina la Simoni kwa sababu alilijua. Na alijua vilevile ya kwamba Simoni alikuwa mwenye roho ya kugeukageuka. Na mwishoni, alijua kwamba roho ya Simoni itageuzwa, naye atakuwa imara kama mwamba. Yesu alijua maneno haya yote namna gani? Kwa sababu yeye ni Mungu.

Jina la Simoni liligeuzwa kweli kuwa **Kefa** ( maana yake **jiwe** kwa Kiaramaic), naye aligeuka kuwa mtu mwenye roho ya nguvu, zaidi nyuma ya kurudi kwa Bwana mbinguni na kushuka kwa Roho Mtakatifu.

### C. Mwito wa Filipo na Natanaeli (1:43-51)

**1:43** Hii ni siku ya ine tunayosoma juu yake ndani ya sura hii. Mwalimu mmoja, jina lake Bosch, alionyesha kwamba siku ya kwanza tunaona *Yoane peke yake* (mash. 15-28); siku ya pili tunaona *Yoane na Yesu* (mash. 29-34); siku ya tatu tunaona *Yesu na Yoane* (mash. 35-42); na siku ya ine tunaona *Yesu peke yake* (mash. 43-51). Bwana alikuwa akikwenda kwa kaskazini kwa sehemu ya inchi inayoitwa **Galilaya. Aliona Filipo** pale, alimwita kumfuata. Neno hili **"Unifuate!"** ni neno kubwa kwa sababu ya yule ambaye alilisema na kwa sababu ni heshima kubwa kulitii. Hata sasa Mwokozi anakaa kuita watu vivyo hivyo pahali po pote.

**1:44 Betesaida** ulikuwa **mji** kwa pwani ya Bahari ya Galilaya. Miji michache tu imeheshimiwa sana kama mji huu. Bwana alifanya mengine ya maajabu yake makubwa zaidi pale (Luka 10:13). Ulikuwa mji wa **Filipo, Anderea, na Petro**. Hata hivi ulikataa Mwokozi, na

kwa sababu hii uliangamizwa pia. Hata sasa watu hawajui kabisa kabisa pahali uliposimama.

**1:45 Filipo** alitaka kushiriki furaha yake mpya, furaha ya wokovu, na mtu mwingine, hivi alikwenda **kuona Natanaeli.** Waamini wapya wana bidii zaidi kuleta watu wengine kwa Kristo. Habari za Filipo zilikuwa wazi na fupi. Alimwambia Natanaeli kwamba alikuwa ameona Masiya aliyetabiriwa na **Musa** katika torati, na **manabii – Yesu wa Nazareti.** Habari zake hazikuwa sawa kabisa. Alisema Yesu alikuwa **mwana wa Yosefu**, lakini Yesu alizaliwa na bikira Maria na hakuna mtu wa dunia aliyekuwa baba yake. **Yosefu** alimlea kama mtoto wake na kumfanya mwana kwa sheria, hata kama hakumzaa.

**1:46** Lakini **Natanaeli alifazaika**. **Nazaret**i haukuwa mji wa heshima katika Galilaya. Ilikuwa nguvu kwaye kufikiri kwamba Masiya ataishi katika mji masikini namna hii. Alimwambia Filipo mafikiri yake na **Filipo** hakubishana naye. Alifikiri njia nzuri zaidi kujibu Natanaeli ni kumpeleka kwa Yesu. Haya ndiyo mafundisho makubwa kwa wote wanaotaka kuleta watu kwa Kristo. Usibishane nao wala kuwaaminisha na hotuba ndefu. Uwaite tu **kuja kuona.**

**1:47** Shairi hili linaonyesha kwamba Yesu anajua maneno yote. Bila kukutana na **Natanaeli** mbele, alisema juu yake kwamba yeye ni **Mwisraeli kweli, hana hila ndani yake**. Watu walijua kwamba Yakobo wa zamani hakutenda biashara kwa haki kila mara, lakini nyuma Yakobo aligeuka, na jina lake liligeuzwa kuwa Israeli. Lakini Natanaeli alikuwa mtu wa haki kabisa, Mwisraeli wa kweli bila "Yakobo", ndiyo hila, ndani yake.

**1:48 Natanaeli** alishangaa kabisa wakati Mgeni huyu aliposema naye kama mtu ambaye alimjua mbele. Ni kama alifichwa kabisa na matawi na majani marefu wakati alipoketi **chini ya mtini**. Lakini Yesu **alimwona** hata hivi.

**1:49** Labda ulikuwa uwezo wa Bwana Yesu kumwona wakati alipofichwa kwa macho ya watu wa dunia ulioaminisha **Natanaeli**, au alikuwa Roho Mtakatifu ambaye alimfunulia kwamba Yesu alikuwa **Mwana wa Mungu** na **Mfalme wa Israeli.**

**1:50** Bwana alikuwa amehakikisha kwa njia mbili kwa Natanaeli kwamba yeye ni Masiya. Alionyesha tabia yake, na alikuwa ameona Natanaeli wakati macho yo yote mengine yasingaliweza kumwona. Njia hizi mbili zilitosha kwa Natanaeli, naye aliamini. Lakini sasa Bwana Yesu aliahidi kwamba **ataona** maneno hata **makubwa kuliko haya.**

**1:51** Kila mara Bwana Yesu aliposema maneno haya **Kweli, kweli** (maana yao "Amina, amina"[2]) tunajua atasema maneno makubwa sana. Hapa alionyeshea Natanaeli mfano wa maneno ambayo yatatokea kwa wakati wa kuja. Atarudi tena na kutawala juu ya dunia nzima. Halafu ulimwengu utajua kwamba mwana wa mseremala aliyeishi kwa Nazareti, mji mzarauliwa, alikuwa Mwana wa Mungu na Mfalme wa Israeli. Siku ile **mbingu zitafunguka** na upendeleo wa Mungu utakuwa juu ya Mfalme wakati atakapotawala, na Yerusalema utakuwa mji wake mkuu.

Labda Natanaeli alikuwa amewaza juu ya habari za kipandio cha Yakobo (Mwa. 28:12). Kipandio, chenye malaika wakipanda na kushuka juu yake, ni mfano wa Bwana Yesu Kristo mwenyewe, njia ya pekee inayofikisha mbinguni. **Malaika za Mungu** watapanda na kushuka juu ya **Mwana wa watu. Malaika** ni watumishi **wa Mungu,** wakisafiri kama ndimi za moto kufanya kazi yake. Wakati Yesu atakapotawala kama Mfalme, **malaika** hawa watapita katika mbingu na dunia wakifanya mapenzi yake.

Yesu alisema na Natanaeli kwamba alikuwa ameona mambo madogo tu kuonyesha kwamba yeye ni Masiya. Wakati Kristo atakapotawala kwa wakati wa kuja, Natanaeli ataona Bwana Yesu wazi kama Mwana mpakaliwa wa Mungu. Saa ile watu wote watajua kwamba kweli Mtu mwema alitoka Nazareti.

**D. Alama ya kwanza: Maji yanageuzwa kuwa mvinyo (2:1-11)**

**2:1** Bila shaka **siku ya tatu** ilikuwa **siku ya tatu** ya Bwana katika Galilaya. Kwa Yoane 1:43 tunasoma Bwana alifikia inchi ile. Hatujui waziwazi kama **Kana** kilikuwa wapi, lakini shairi 12 la sura hii inatufikirisha kwamba kilikuwa karibu na Kapernaumu lakini pahali pa juu kupita.

**Kulikuwa na ndoa kwa Kana** siku ile, na **mama yake Yesu alikuwa pale.** Ona ya kwamba Maria aliitwa hapa **mama ya Yesu**. Mwokozi hakujulikana katikati ya watu kwa sababu alikuwa Mwana wa Bikira Maria, lakini Maria alijulikana kwa sababu alikuwa mama wa Bwana Yesu. Ndani ya Maandiko ni Kristo aliyepewa heshima zaidi kila mara, si Maria.

**2:2 Yesu na wanafunzi wake waliitwa kwa arusi.** Ilikuwa vizuri kwa wale waliotayarisha ndoa hii kuita Kristo. Ni vizuri kwa watu kufanya vivyo hivyo kwa wakati wa sasa vilevile, lakini sharti bibi arusi na bwana arusi wawe waamini wa kweli. Na vilevile watoe maisha yao kwa Mwokozi na kusudi kwa nyumba yao kuwa pahali ambapo atapenda kufika.

**2:3 Mvinyo** ilipunguka mbele ya mwisho wa karamu. Wakati **mama wa Yesu** alipofahamu neno hili, alimwambia Mwana wake habari hizi. Alijua ataweza kufanya ajabu kwa kuwapatia mvinyo nyingine, na labda alitaka wageni wote kwa karamu kujua kwamba Mwana wake alikuwa Mwana wa Mungu. Mvinyo ni mfano wa furaha mara nyingi ndani ya Maandiko. Wakati Maria aliposema **"Hawana mvinyo,"** alionyesha hali ya watu wasiookolewa bado. Hakuna furaha ya kweli, ya kudumu, kwa msiyeamini.

**2:4** Ni kama jibu la Bwana kwa mama yake lilikuwa kali kidogo, bila mapendo, lakini halikuwa hivi kweli. Alimheshimu wakati alipomwita **mwanamke**. Wakati alipouliza, **"Mwanamke, nina nini nawe?"** alionyesha kwamba ndani ya kazi yake kwa Mungu haikuwa lazima kwaye kutii maagizo ya mama yake, lakini alifanya mapenzi ya Baba yake mbinguni tu ndani ya maneno yote. Maria alitaka Yesu kutukuzwa, lakini ilipasa Yesu kumkumbusha kwamba saa kwa neno hili ilikuwa **haijafika bado**. Mbele ya kuweza kuonekana mbele ya ulimwengu kama Kristo Mshindaji ilimpasa kufa kuwa zabihu kwa zambi kwa Kalvari.

> Williams anaonyesha pahali pengine tunapoona maneno haya "Nina nini nawe?" ndani ya Biblia. Maana yao ni, "Tuna ushirika kwa njia gani?" Jibu la ulizo hili ni, "Hakuna." Daudi alisema maneno haya mara mbili na wana wa Zeruya. Haikuwezekana kwaye kuwa na ushirika nao kwa maneno ya roho. Elisa alisema hivi ndani ya 2 Wafalme 3 kwa Yoramu, mwana wa Ahaba, kuonyesha kwamba alikuwa mbali sana naye kwa maneno ya roho. Pepo wachafu walisema maneno haya mara tatu kuonyesha kwamba Shetani na Kristo hawana ushirika hata kidogo. Na mwishoni Bwana aliye Mungu, na asiyekuwa na zambi, aliyasema kwa bikira Maria mwenye tabia ya zambi, kuonyesha kwamba kulikuwa na Sauti Moja tu iliyokuwa na amri kusema naye, ndiyo sauti ya Mungu Baba.[2]

**2:5** Maria alifahamu maana ya maneno yake, hivi aliagiza watumishi kufanya **lo lote analosema** nao. Haya ndiyo

maneno makubwa kwa sisi sote. Ona ya kwamba Maria hakuwaagiza kumtii *yeye*, au mtu ye yote mwingine. Alisema nao kutii Bwana Yesu tu. Tunapata mafundisho ya Bwana Yesu ndani ya Agano Jipya tu. Wakati tunaposoma kitabu hiki cha damani, tukumbuke ya kwamba haya yalikuwa masemo ya mwisho ya Maria ndani yake, **"Lo lote analosema kwenu fanyeni."**

**2:6** Kwa pahali pa arusi kulikuwa na mitungi mikubwa **sita** ya **mawe,** kila mmoja kwa vipimo vya litres 80 au 120 za **maji** kwa Wayuda kujisafisha kama wakichafuwa. Kwa mfano, Myuda akigusa maiti alichafuwa kufika wakati alipotimiza maneno fulani kwa kusafishwa.

**2:7** **Yesu** aliagiza **wajaze mitungi na maji**. Watumishi walifanya hivi mara moja. Bwana alitumika na vitu vilivyokuwa pale kufanya ajabu. Aliruhusu watu kuleta **mitungi** na **kuijaza na maji,** kisha alifanya neno ambalo yeye tu aliweza kufanya – aligeuza maji kuwa mvinyo! Watumishi walijaza mitungi na maji, si wanafunzi. Neno hili lilizuiza watu kusema kwamba kulikuwa na hila. Na vilevile mitungi **ilijazwa tele,** hivi njia haikuwa kusema mvinyo iliongezwa nyuma.

**2:8** Basi ajabu lilikuwa limefanyika. Bwana aliagiza watumishi **kuteka** nusu ya mvinyo toka mitungi na **kupelekea mkubwa wa karamu.** Neno hili linaonyesha kwamba alama hii ilifanywa palepale. Maji hayakugeuka kuwa mvinyo polepole, ndani ya muda fulani lakini ndani ya nusu ya dakika.

**2:9** **Mkubwa wa karamu** alikuwa na kazi ya kuangalia kazi ya kutayarisha meza na vyakula. **Wakati alipoonja** kinyweo ambacho watumishi walileta, alifahamu kwamba ajabu lilikuwa limefanyikana. Hakujua **pahali mvinyo ilipotoka**, lakini alifahamu kwamba ilikuwa mvinyo nzuri sana, hivi **aliita bwana arusi** mara moja.

Inapasa Mkristo kufikiri nini juu ya kunywa mvinyo? Mara nyingine mganga anasema na mgonjwa kunywa mvinyo kama dawa, na neno hili linapatana na mafundisho ya Agano Jipya (1 Tim. 5:23). Lakini kwa sababu watu wengi wanakunywa kupita kipimo, zaidi ya Wakristo wanakataa kabisa kunywa mvinyo. Ni nyepesi kwa mtu kufungwa na mapendo kwa mvinyo na vinyweo vingine vya nguvu kama malofu, hivi njia nzuri zaidi kuepuka hatari hii ni kujitenga nayo kabisa. Na vilevile inatupasa kukumbuka ya kwamba matendo yetu yanaweza kuwa maangukisho kwa watu wengine. Kwa Mkristo kunywa malofu mbele ya wasioamini ni ushuhuda mbaya, na kwa sababu hii ni tendo lisilofaa kwa Mkristo.

**2:10** Mkubwa wa karamu alionyesha ya kwamba Bwana Yesu alitenda namna nyingine na watu wa dunia wanavyotenda. Kwa wakati wa karamu ilikuwa desturi kuleta kwanza **mvinyo** iliyo nzuri zaidi kwani saa ile wageni wanaweza kuonja utamu wake vizuri sana. Nyuma, wakati wanapokwisha kula na kunywa, hawaweki roho tena juu ya uzuri wa kinyweo. Lakini kwa arusi hii mvinyo nzuri zaidi ililetwa kwa mwisho. Kuna mafundisho kwa roho zetu ndani ya neno hili. Dunia inapatia watu maneno yanayoonekana mazuri zaidi kwanza, na kukokota roho za vijana. Halafu wakati wanapokwisha kupoteza maisha yao na furaha burebure za dunia, wanabaki na takataka tu kwa wakati wa uzee wao. Lakini maisha ya Mkristo si hivi hata kidogo. Uzuri na utamu wake zinakaa kuongezeka. Kristo anachunga mvinyo nzuri zaidi kwa wakati wa mwisho.

Maandiko haya ni zaidi kwa taifa la Wayuda. Furaha ya kweli ilikosa ndani ya dini yao kwa wakati ule. Watu walifungana na desturi zao za kuabudu, lakini

utamu haukuwa ndani yake. Hawakujuana na furaha ya kweli, ya roho. Bwana Yesu alijaribu kuwafundisha kutia imani yao ndani yake ili aweze kuwapa furaha tele. Maji ya desturi za kuabudu ya Wayuda yangeweza kugeuzwa kuwa mvinyo ya furaha ya kweli katika Kristo.

**2:11** Watu walieneza habari za alama nyingine, ambazo wanasema Yesu alifanya kwa ujana wake. Kwa kuhakikisha kwamba habari hizi si kweli Roho Mtakatifu aliongoza mwandishi kuandika hapa ya kwamba Yesu **alifanya mwanzo huu wa alama** katika Kana.

Kugeuza maji kuwa mvinyo kulikuwa alama, ndiyo ajabu yenye maana. Mungu tu anaweza kugeuza maji kuwa mvinyo. Kusudi lake lilikuwa kuonyesha kwamba Yesu alikuwa Kristo wa Mungu. Kwa njia ya alama hii **akaonyesha utukufu wake.** Alifunua kwa watu ya kwamba alikuwa kweli Mungu – katika mwili wa mtu. **Wanafunzi wake walimwamini.** Ndiyo, walimwamini mbele vilevile, lakini sasa imani yao ilipatishwa nguvu.

### E. Mwana wa Mungu anasafisha nyumba ya Baba yake (2:12-17)

**2:12** Mwokozi aliondokea Kana sasa, **akashuka** kwenda **Kapernaumu pamoja na mama yake na ndugu na wanafunzi wake**. Walibaki pale siku chache tu. Nyuma yake Bwana alipanda kwenda Yerusalema.

**2:13** Hapa ndio mwanzo wa ushuhuda wa Bwana kwa mji wa **Yerusalema,** kufika shairi 21 la sura 3. Alianza, na alimaliza utumishi wake katikati ya watu kwa njia ya kusafisha hekalu kwa wakati wa **Pasaka** (ona Mt. 21:12, 13; Marko 11:15-18; Luka 19:45, 46). Pasaka ilikuwa siku kubwa iliyoshikwa kila mwaka kukumbuka wakati Waisraeli walipoponyeshwa toka utumwa katika Misri na kuongozwa kuvuka Bahari Nyekundu, na kupita katika jangwa hata kufikia inchi ya ahadi. Tunasoma juu ya Pasaka ya kwanza ndani ya Kutoka 12. Bwana Yesu akiwa Myuda mwenye kufuata Mungu na bidii **alipanda Yerusalema** kwa siku kubwa ile.

**2:14** Wakati alipofikia **hekalu,** aliona kwamba lilikuwa limegeuka pahali pa soko. Alikuta **wabadilisha feza** wakiketi pale na watu **wakiuza ngombe, na kondoo, na hua** kwa sadaka ambazo waabudaji walitolea Mungu. **Wabadilishaji feza** walibadilisha mali ya watu waliotoka mbali na kuwapa mali ya Yerusalema, ili waweze kulipa kodi ya hekalu. Mara nyingi walililipiza wasafiri toka mbali kupita hesabu ya haki.

**2:15** Hatusomi ya kwamba Bwana alipiga watu na **fimbo** ile, lakini ilikuwa alama ya amri aliyoshika mkononi. Akiitikisa **alifukuza** wenye kufanya biashara toka hekalu na **kupindua meza** za wenye kubadilisha feza.

**2:16** Sheria ilikubali watu masikini kutoa hua mbili kwa zabihu zao kwani walikosa mali ya kutosha kununua **nyama mkubwa. Bwana aliagiza wale waliouza hua** kuondosha vitu hivi vya biashara. Haikufaa kufanyiza **nyumba ya Baba** yake kuwa **nyumba ya biashara**. Tangu zamani Mungu ameonya watu wasijaribu kujipatia mali kwa njia ya kazi ya Mungu. Matendo haya ya Bwana hayakuwa makali wala kukosa haki; lakini yalionyesha utakatifu wake na haki yake.

**2:17** Wakati **wanafunzi wake** walipoona maneno haya, walikumbuka unabii katika Zaburi 69:9 ya kwamba wakati Masiya atakapokuja, **wivu** wa nyumba ya Mungu utamkula kabisa. Sasa waliona bidii kubwa sana ya Yesu kwa watu kuabudu Bwana kwa usafi na utakatifu, na walifahamu kwamba mwandishi alikuwa amesema juu ya Yesu.

Inatupasa kukumbuka kwamba mwili wa Mkristo ni hekalu la Roho Mtakatifu. Bwana Yesu alitaka sana kwa hekalu katika Yerusalema kuwa safi, na vivyo

hivyo ni lazima kwa sisi kuchunga miili yetu safi kwa yeye.

### F. Yesu anatabiri kwamba atakufa na kufufuliwa tena (2:18-22)

**2:18** Ni kama Wayuda walitaka kuona alama au ajabu saa zote. Ni kama walisema, "Ukifanya ajabu kubwa la uwezo kwa sisi kuona, halafu tutakuamini." Basi Bwana alikuwa amefanya maajabu mengi, lakini hawakumwamini. Ndani ya shairi 18 waliuliza nani ambaye alimpa amri kufukuza wenye kufanya biashara toka hekalu. Walisema sharti awaonyeshe **alama** kwamba yeye ni kweli Masiya.

**2:19** Bwana Yesu aliwajibu na habari za ajabu ya mauti na ufufuko wake. Aliwaambia kwamba **watavunja** hekalu lake, lakini atalisimamisha tena **kwa siku tatu.** Shairi hili linaonyesha uungu wa Kristo tena. Mungu tu aliweza kusema kwamba **"nitalisimamisha kwa siku tatu."**

**2:20** **Wayuda** hawakufahamu maneno aliyosema. Walifikiri zaidi juu ya vitu vya dunia, si kweli za roho. Walikumbuka hekalu moja tu, ndilo hekalu la Herode lililosimama katika Yerusalema kwa wakati ule. Watu walihitaji **miaka makumi ine na sita kujenga hekalu lile**, na iliwashinda kufahamu namna gani mtu ye yote ataweza kulijenga tena **kwa siku tatu.**

**2:21** Lakini Bwana Yesu alikuwa **akisema** juu ya **mwili wake** mwenyewe, uliokuwa kao kwa utimilifu wote wa Mungu. Wayuda hawa walikuwa wamechafua hekalu katika Yerusalema; vivyo hivyo watamwua yeye nyuma ya miaka michache.

**2:22** Kwa wakati wa nyuma, wakati Bwana Yesu alipokwisha kusulibishwa na **kufufuliwa toka wafu, wanafunzi wake walikumbuka ahadi** yake kwamba atafufuka tena nyuma ya siku tatu. Wakati walipoona na macho yao wenyewe kutimia kwa unabii huu, **waliamini lile andiko na lile neno alilosema Yesu.**

Tena na tena ndani ya Maandiko tunasoma kweli zilizo **nguvu** kufahamu. Lakini hapa tunaona ya kwamba inatupasa kuchunga hazina ya Neno la Mungu ndani ya roho zetu. Siku nyingine Bwana atatufahamisha maneno haya wazi, hata kama hatuyafahamu kwa wakati wa sasa. Wakati tunaposoma **wakaamini lile andiko,** maana yake ndiyo kwamba waliamini unabii katika Agano la Kale juu ya ufufuko wa Masiya.

### G. Watu wengi walikiri kwamba waliamini Kristo (2:23-25)

**2:23** Kwa sababu ya **alama** Yesu alizofanya katika **Yerusalema wakati wa Pasaka**, **watu wengi waliamini jina lake.** Si kusema ya kwamba na imani ya kweli walitoa maisha yao mazima kwake, lakini ya kwamba walimpokea. Walionyesha kwamba walifuata Yesu bila imani ya kweli. Walikuwa kama watu wengi kwa wakati wa sasa wanaojiita Wakristo bila kuzaliwa tena na bila kuwa na imani ya kweli.

**2:24** Hata kama watu wengi walimwamini, **Yesu hakujiaminisha kwao,** maana **hakuwaamini** (ni neno moja kwa Kiyunani). Alifahamu kwamba hawakufika kwake na roho ya kweli. Walikuwa wakitafuta mashangazo tu. **Alijua watu wote** – mawazo na makusudi yao. Alijua sababu ya matendo yao. Alijua kama walikuwa na imani ya kweli au kama ilikuwa mwigo tu.

**2:25** Hakuna mtu anayejua roho za watu vizuri kupita Bwana mwenyewe. **Hakuhitaji mtu hata mmoja kushuhudia habari za mtu;** kwa sababu yeye mwenyewe alijua **yaliyo ndani ya watu** na sababu ya matendo yao.

### H. Yesu anafundisha Nikodemo juu ya kuzaliwa tena (3:1-21)

**3:1** Habari za **Nikodemo** ni namna nyingine na habari tulizosoma sasa tu.

Wengi wa Wayuda katika Yerusalema walikiri kwamba waliamini Bwana, lakini alijua ya kwamba hawakuwa na imani ya kweli. Nikodemo alikuwa namna nyingine. Bwana Yesu alitambua kwamba alikuwa na hamu kabisa kujua kweli. Ingalipasa shairi 1 kuanza na *"Lakini* **palikuwa mtu mmoja wa Wafarisayo, jina lake Nikodemo, mkubwa mmoja wa Wayuda."**

Nikodemo alijulikana kama mwalimu wa Wayuda. Labda alifikia Yesu aweze kujifunza maneno mengine ili aweze kupitisha mafundisho haya kwa Wayuda.

**3:2** Biblia haitujulishi kwa sababu gani Nikodemo **alikuja kwa Yesu usiku.** Tunazani ingalikuwa haya kwake kwa watu kumwona kufikia Yesu kwani zaidi ya Wayuda walikuwa hawajakubali Yesu kuwa Masiya. Hata hivi alifikia Yesu. Alikiri kwamba Bwana alikuwa **mwalimu** aliyetumwa na **Mungu,** kwani hakuna mtu aliyeweza kufanya maajabu namna hii bila kusaidiwa na **Mungu**. Nikodemo alikuwa amejifunza maneno mengi, lakini hata hivi hakutambua Bwana kuwa Mungu katika mwili wa mtu. Alikuwa sawasawa na watu wengi kwa wakati wa sasa wanaosema Yesu alikuwa mtu mkubwa, mwalimu mzuri sana, na mfano mzuri kwa sisi kuiga. Maneno haya yote ni kweli kwa sehemu tu. Yesu *alikuwa*, naye *ni* Mungu.

**3:3** Kwanza tunafazaika juu ya jibu la Yesu kwa Nikodemo. Bwana wetu alisema naye, "Nikodemo, umefika kwangu kupata mafundisho, lakini neno unalohitaji zaidi ni **kuzaliwa tena**. Ni neno hili ambalo unahitaji kwanza. Kwa njia ya kuzaliwa mara ya pili tu utaweza **kuona ufalme wa Mungu.**"

Bwana alianza kusema na Nikodemo na masemo haya **"Kweli, kweli"**. Masemo haya yanatufahamisha kwamba kweli kubwa zitafuata.

Nikodemo alikuwa Myuda, na pamoja na Wayuda wengine wote alitazamia kuja kwa Masiya kufungua Israeli toka utumwa wa Roma. Ufalme wa Roma ulitawala dunia wakati ule na ilipasa Wayuda kunyenyekea sheria zao na serikali yao. Nikodemo alitazamia na hamu kubwa wakati Masiya atakaposimamisha ufalme wake duniani, wakati Wayuda watakapokuwa taifa lenye heshima zaidi duniani, na wakati adui zao zote watakapoharibiwa. Lakini sasa Yesu alijulisha Nikodemo ya kwamba mtu akitaka kuingia ufalme **inampasa kuzaliwa tena**. Kwa kupata uzima wa dunia ilitupasa kuzaliwa na mwili wa dunia, na kwa kupata uzima wa milele inatupasa kuzaliwa tena. Ni kusema ya kwamba watu wenye maisha yaliyogeuzwa tu wanaweza kuingia ufalme wa Kristo. Utawala wake utakuwa utawala wa haki, hivi lazima watu wake wawe wenye haki vilevile. Hataweza kutawala watu waliokuwa wakiendelea ndani ya zambi zao.

**3:4** Hapa tunaona tena ya kwamba ilikuwa nguvu sana kwa watu kufahamu masemo ya Bwana Yesu. **Nikodemo** alifikiri maneno ya dunia tu. Alifazaika namna gani mtu mzima ataweza kuingia **tumboni mwa mama yake** kwa **kuzaliwa tena.**

Habari hizi zinaonyesha kwamba "mwenye kufuata tabia ya asili hapokei maneno ya Roho ya Mungu kwa sababu maneno haya ni upumbavu kwake, wala hawezi kuyafahamu, kwa sababu yanatambulikana na Roho" (1 Kor. 2:14).

**3:5** Akiendelea na maelezo yake Yesu alimwambia Nikodemo kwamba inampasa **kuzaliwa kwa maji na kwa Roho.** Isipokuwa hivi hataweza kamwe **kuingia ufalme wa Mungu**.

Maana ya masemo haya ya Yesu yalikuwa nini? Watu wengi wanafikiri alisema juu ya *maji ya dunia*, kama maji ya kunywa na kuvua nguo, vivyo hivyo, na ya kwamba Bwana Yesu alikuwa akisema ni lazima kubatizwa kwa kupata wokovu. Lakini mafundisho haya haya-

patani na mafundisho ya Biblia. Ndani ya Neno la Mungu tunasoma tena na tena kwamba mtu anaokolewa kwa njia ya imani ndani ya Bwana Yesu Kristo peke yake. Ubatizo ni kwa watu wale wanaokwisha kuokolewa, lakini si kupatia watu wokovu.

Wengine wanafikiri **maji** ndani ya shairi hili yanasema juu ya Neno la Mungu. Ndani ya Efe. 5:25,26 maji na Neno la Mungu yanatajwa pamoja. Na ndani ya 1 Pet. 1:23 na Yak. 1:18 watu wanazaliwa tena kwa njia ya Neno la Mungu. Hivi inawezekana kwa maji kuwa mfano wa Biblia. Tunajua kwamba hakuna wokovu bila Maandiko Matakatifu. Sharti mwenye zambi aamini habari za Neno la Mungu, mbele ya kuweza kuzaliwa tena.

Lakini **maji** yanasema juu ya Roho Mtakatifu vilevile. Ndani ya Yoane 7:38-39 Bwana Yesu alisema juu ya mito ya maji ya uzima, na tunasoma waziwazi ya kwamba alitumika na neno hili *maji* wakati alipokuwa akisema juu ya Roho Mtakatifu. Kama maji ndani ya sura 7 yakisema juu ya Roho Mtakatifu, labda yanasema juu ya Roho Mtakatifu ndani ya sura 3 vilevile?

Lakini ndani ya sura 3 Yesu alisema, **"Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuingia ufalme wa Mungu."** Kama maana ya **maji** ikisema juu ya **Roho**, Roho anatajwa mara mbili ndani ya shairi hili. Lakini ni taratibu kutafsiri neno hili "*na"* na neno lingine, ndilo "*hata*." Hivi shairi hili linaweza kusema, **"Mtu asipozaliwa kwa maji,** *hata* **kwa Roho, hawezi kuingia ufalme wa Mungu."** Tunafikiri hii ndiyo maana ya kweli ya shairi hili. Kuzaliwa katika mwili wa dunia tu hakutoshi.[8] Sharti mtu azaliwe kwa roho vilevile kwa **kuingia ufalme wa mbinguni.** Mtu anazaliwa tena kwa roho wakati anapoamini Bwana Yesu Kristo na kuzalishwa tena na Roho Mtakatifu wa Mungu. Tunasoma tena juu ya "kuzaliwa kwa Roho" ndani ya mash. 6 na 8 vilevile.

**3:6** Hata kama ingaliwezekana kwa Nikodemo kuingia tumbo la mama yake tena na kuzaliwa mara ya pili, neno hili lisingaliweza kuondosha tabia ya zambi ndani yake. Maana ya **"kilichozaliwa kwa mwili ni mwili"** ni ya kwamba watoto wenye wazazi wa dunia wanazaliwa katika zambi, bila tumaini kwamba wataweza kujiokoa wenyewe. Lakini kilichozaliwa kwa Roho ni roho. Mtu anazaliwa tena kwa roho wakati anapoamini Bwana Yesu. Wakati anapozaliwa tena kwa njia ya Roho Mtakatifu, anapokea tabia mpya, na kustahilishwa kwa ufalme wa Mungu.

**3:7 Haikufaa Nikodemo kushangaa** juu ya mafundisho ya Bwana Yesu. Ilimpasa kufahamu ya kwamba **inapasa mtu kuzaliwa tena,** na ya kwamba hawezi hata kidogo kutengeneza yeye mwenyewe tabia yake ya zambi. Lazima afahamu ya kwamba mtu akitaka kuwa ndani ya ufalme wa Mungu, sharti awe mtakatifu na safi na mwenye tabia mpya.

**3:8** Bwana Yesu akiendelea na mafundisho yake alisema juu ya upepo. Alikumbusha Nikodemo kwamba **upepo unavuma pahali unapotaka**, na mtu anaweza **kusikia sauti yake,** lakini hawezi kuona **pahali unapotoka wala unapokwenda.** Kuzaliwa tena kunafanana na **upepo**. Kwanza, kunafanyikana kupatana na mapenzi ya Mungu. Mtu hana amri juu yake yeye mwenyewe. Neno la pili, hakuonekani kwa macho. Huwezi kuona saa mtu anapozaliwa tena, lakini utaona matunda ya kuzaliwa tena ndani ya maisha yake. Mtu anageuka nyuma ya kuokolewa. Anachukia sasa maneno maovu ambayo alipenda mbele. Sasa anapenda maneno ya Mungu aliyozarau mbele. Kama hakuna mtu anayefahamu upepo kabisa, vivyo hivyo uzazi mpya ni kazi ya ajabu

ya Roho ya Mungu ambayo mtu hawezi kufahamu kabisa. Na vilevile kama tusipojua pahali na wakati gani **upepo** utakapovuma, vivyo hivyo hatujui mbele saa gani na pahali gani mtu atakapozaliwa tena.

**3:9 Nikodemo** alionyesha tena kwamba haiwezekani kwa mtu wa dunia kufahamu maneno ya Mungu. Bila shaka alikaa kufikiri juu ya uzazi mpya kama tukio la dunia, si la roho, hivi aliuliza Bwana Yesu, **"Maneno yale yanawezekana namna gani?"**

**3:10** Yesu **alijibu** kusema ingalipasa Nikodemo, aliye **mwalimu katika Israeli,** kufahamu **maneno haya**. Maandiko ya Agano la Kale yalifundisha wazi kwamba wakati Masiya atakaporudi duniani kusimamisha ufalme wake, atahukumu kwanza adui zake na kuharibu vitu vyote vya kuchukiza. Wale tu waliokuwa wamekiri zambi zao na kuziacha wataweza kuingia ufalme.

**3:11** Halafu Bwana Yesu alisema na nguvu tena kwamba mafundisho yake ni haki kabisa, lakini hata hivi watu hawayaamini. Alijua kweli ya maneno haya tangu zamani, na alishuhudu tu maneno aliyojua na **kuona**. Lakini Nikodemo na zaidi ya Wayuda walikataa kuamini ushuhuda wake.

**3:12 Maneno ya dunia** ambayo Bwana alitaja ndani ya shairi hili yalikuwa nini? Yalikuwa ufalme wake wa **dunia**. Nikodemo alijifunza Agano la Kale na alijua kwamba siku nyingine Masiya atakuja na kusimamisha ufalme hapa duniani na ya kwamba Yerusalema utakuwa mji wake mkubwa. Lakini Nikodemo hakufahamu kwamba kwa kuingia ufalme ule ilipasa mtu kuzaliwa tena. Basi **maneno ya mbingu** Bwana aliyotaja yalikuwa nini? Ni kweli za ajabu zinazoelezwa ndani ya mashairi yanayofuata – ajabu kubwa ya namna gani mtu anapokea uzazi huu mpya.

**3:13** Mtu mmoja tu aliweza na kustahili kusema juu ya maneno ya mbingu. Ni yeye tu **aliyekuwa mbinguni**. Bwana Yesu hakuwa mwalimu wa dunia tu aliyetumwa na Mungu, lakini ni yeye aliyekaa pamoja na Mungu Baba tangu milele, na **alishuka** kwa dunia. Wakati aliposema **hapana mtu aliyepanda mbinguni,** hakusema ya kwamba watakatifu wa Agano la Kale kama Enoka na Elia hawakwenda mbinguni. Watu hawa hawakupanda mbinguni, lakini *walipelekwa* kule, lakini yeye **alipanda mbinguni** kwa uwezo wake mwenyewe. Elezo lingine ndilo ya kwamba hakuna mtu aliyekuwa na ruhusa kukaa pamoja na Mungu kama yeye. Aliweza kupanda kwa pahali Mungu alipokuwa kwa sababu alikuwa ameshuka toka mbingu kufika duniani. Hata saa Bwana Yesu aliposimama pale pamoja na Nikodemo alisema alikuwa **mbinguni**. Neno hili liliwezekana namna gani? Tunaona hapa kwamba, kama Mungu, Bwana alikuwa pahali pote kwa saa moja. Tafsiri nyingine za Biblia kwa wakati wa sasa hazichapi maneno mawili wa mwisho ya shairi hili, ndiyo **"aliye mbinguni"**, yanaonekana ndani ya maandiko mengi na ni sehemu ya Agano Jipya.

**3:14** Sasa Bwana Yesu alikuwa karibu kufunulia Nikodemo kweli za mbinguni. Uzazi mpya unafanyikana namna gani? Ni lazima kwa zambi za watu kuazibiwa. Haiwezekani kwa watu kwenda mbinguni na zambi zao. Kama **Musa alivyonyanyua nyoka** ya shaba juu ya mti **jangwani** wakati Waisraeli wote walipoumwa na nyoka, **vivyo hivyo sharti Mwana wa watu atanyanyuliwa**. (Soma Hesabu 21:4-9.) Wakati waliposafiri jangwani kwendea inchi ya ahadi Waisraeli walishushwa mioyoni, na saburi yao ilipunguka na walinungunikia Bwana. Bwana alituma nyoka wakali katikati yao kuwaazibu, na watu wengi walikufa. Wakati wale waliopona walipolilia Bwana na roho ya toba, Bwana alia-

giza Musa kufanya **nyoka** ya shaba na kuifunga juu ya mti. Mwisraeli aliyeumwa na nyoka na aliyeangalia nyoka aliponyeshwa kwa njia ya ajabu.

Yesu alitaja habari hizi toka Agano la Kale kama mfano wa namna gani uzazi mpya unatokea. Wanaume, wanawake na watoto wameumwa na nyoka ya zambi na wamehukumiwa kufa kwa milele. Nyoka ya shaba ilikuwa mfano wa Bwana Yesu. Ndani ya Biblia, shaba ni mfano wa hukumu. Bwana Yesu hakuwa na zambi na hakustahili kamwe kuhukumiwa, lakini alitukomboa sisi na kupokea azabu ambayo sisi tulistahili kupata. Mti ni mfano wa msalaba wa Kalvari, pahali Bwana Yesu aliponyanyuliwa. Tunaokolewa kwa njia ya kutazama kwake na imani.

**3:15** Mwokozi asiyejua zambi alifanywa zambi kwa sisi, ili sisi tuweze kufanywa haki ya Mungu ndani yake. **Kila mtu anayemini** Bwana Yesu Kristo anapokea **uzima wa milele** kama zawadi.

**3:16** Hili ni moja la mashairi ambayo watu wengi zaidi wanajua kwa sababu linapasha Habari Njema wazi sana. Linajumlisha maneno Bwana Yesu aliyokuwa akifundisha juu ya namna gani watu wanazaliwa tena. Tunasoma **Mungu alivyopenda ulimwengu. Ulimwengu** ni watu wote wa dunia. Mungu hapendi zambi za watu wala uovu wa kawaida ya dunia, lakini anapenda watu, na hataki hata mmoja kupotea.

Alionyesha ukubwa wa mapendo yake kwa njia ya **kutoa Mwana wake wa pekee**. Mungu hana Mwana mwingine kama Bwana Yesu, na kwa sababu ya mapendo yake makubwa sana alikuwa tayari kutoa **Mwana wake wa pekee** kwa waasi na wenye zambi. *Si kusema* kwamba watu wote wanaokolewa**.** Ni lazima kwa mtu kukubali na kupokea kazi Kristo aliyofanya kwaye mbele ya kupokea uzima wa milele toka Mungu. Kwa sababu hii tunasoma, **"ili kila mtu akimwamini asipotee."** Hakuna mtu anayelazimishwa kupotea. Njia ni tayari kwa watu wote kuokolewa, lakini ni lazima kwa mtu kupokea Bwana Yesu Kristo kama Mwokozi wake mwenyewe. Wakati anapofanya hivi, anapata **uzima** wa milele hata kwa wakati wa sasa.

**3:17** Mungu si mtawala mkali anayetaka kumwangia wanadamu hasira yake. Anapenda watu sana na amelipa bei kubwa zaidi kuwaokoa. Angaliweza **kutuma Mwana wake ulimwenguni kuhukumu ulimwengu,** lakini **hakufanya hivi.** Alimtuma hapa kuteswa, kutoa damu yake na kufa **kusudi ulimwengu uokolewe naye.** Kazi ya Bwana Yesu msalabani ilikuwa na faida kubwa sana sana hata wenye zambi pahali pote wangeweza kuokolewa kama wakimpokea kuwa Mwokozi wao.

**3:18** Watu wote wa dunia wanatengwa kwa mafungu mawili: waamini, na wasioamini. Kila mtu anayeamini Mwokozi **hahukumiwi, lakini** wale wasioamini **wamekwisha kuhukumiwa.** Bwana Yesu amemaliza kazi iliyohitajiwa kwa wokovu wa watu, na sasa inapasa kila mtu kuchagua kama atampokea, au kama atamkataa. Ni neno la kuogopesha kabisa kukataa kupokea zawadi kubwa namna hii ya mapendo. Mtu akikataa kuamini Bwana Yesu, itakuwa lazima kwa Mungu kumhukumu.

Kuamini **jina** lake ni sawaswa na kumwamini *yeye.* Ndani ya Biblia, kama ukitaja jina la mtu, ni kama ukisema juu ya mtu mwenyewe. Ukiamini **jina** lake, ni sawasawa unamwamini yeye.

**3:19** Yesu ni **nuru** iliyofika **duniani**. Alikuwa Mwana-Kondoo wa Mungu asiyekuwa na zambi wala kipaku. Alikufa kwa zambi za dunia nzima. Watu wanampenda kwa sababu alifanya hivi? Sivyo, wanachukizwa naye. Wanapenda zambi zao kupita kuwa na Yesu kama Mwokozi wao, hivi wanamkataa. Kama vidudu wanaondoka mbio mbio toka nuru, vivyo

hivyo watu waovu wanakimbia Kristo.

**3:20** Watu wanaopenda zambi wanachukia **nuru,** kwa sababu nuru inaonyesha uovu wao. Wakati Yesu alipokuwa hapa duniani, wenye zambi hawakukaa na raha karibu naye kwa sababu utakatifu wake ulifunua uovu wao. Njia nzuri zaidi kuonyesha kukunjama kwa mti ni kuusimamisha kando ya mti wa kunyoka wima. Bwana Yesu alifika duniani kama Mtu mkamilifu, na kwa njia hii alifunua upotofu wa watu wote wengine.

**3:21** Mtu akiwa na roho ya haki mbele ya Mungu, atakuja **kwa nuru**, ndiye Bwana Yesu, na kufahamu kutokufaa na zambi zake mwenyewe. Halafu ataamini Mwokozi, na kuzaliwa tena kwa njia ya imani katika Kristo.

### I. Utumishi wa Yoane Mbatizaji katika Yudea (3:22-36)

**3:22** Sehemu ya kwanza ya sura hii ilikuwa juu ya ushuhuda wa Bwana Yesu ndani ya mji wa Yerusalema. Kuanza na shairi 22 kufika mwisho wa sura, Yoane anapasha habari za utumishi wa Kristo katika **Yudea**. Bila shaka alikaa kutangaza habari njema pale. Wakati watu walipofikia nuru **walibatizwa**. Inaonekana sawasawa Yesu aliwabatiza yeye mwenyewe, lakini ndani ya Yoane 4:2 tunaona kwamba wanafunzi wake waliwabatiza.

**3:23 Yoane** huyu ndani ya shairi hili ni Yoane Mbatizaji. Alikaa kuhubiri habari zake za toba kwa inchi ya Yudea na kubatiza Wayuda waliokuwa tayari kutubu kusudi wawe tayari kwa kuja kwa Masiya. **Yoane vilevile alikuwa akibatiza katika Ainoni … kwa sababu maji mengi yalikuwa pale.** Neno hili halihakikishi kabisa kwamba kwa ubatizo huyu mwili mzima wa mtu uliingizwa ndani ya maji lakini tunafikiri ilikuwa hivi. **Maji mengi** hayakuhitajiwa kama ubatizo ulikuwa kunyunyiza maji nusu tu juu ya kichwa cha mtu.

**3:24** Shairi hili linaeleza habari ya kwamba Yoane alikaa kuhubiri, na Wayuda waliopenda Mungu walipokea mahubiri yake vizuri. Nyuma kidogo **alifungwa gerezani** na kukatiwa kichwa kwa sababu ya ushuhuda wake mwaminifu. Kufika wakati ule aliendelea na kazi yake ya kuhubiri.

**3:25** Shairi hili linaonyesha wazi kwamba **wengine wa wanafunzi wa Yoane** walikuwa na mabishano na Wayuda juu ya **maneno ya kusafisha**. Maana yake nini? Maana ya **kusafisha** hapa ni ubatizo na walikuwa wakibishana kama ubatizo wa nani ulikuwa na faida na uwezo mkubwa kupita, ule wa Yoane au wa Yesu. Labda **wengine wa wanafunzi wa Yoane** walifikiri ubatizo wa bwana wao ulikuwa mzuri kupita. Au labda Wafarisayo waliamsha wivu ndani ya roho zao juu ya Yesu kwa sababu alikuwa na wafuata wengi.

**3:26** Hivi **wanafunzi** wa Yoane Mbatizaji **walimfikia** kuulizana naye juu ya neno hili. Ni kama walisema maneno kama haya: “Kama ubatizo wako ni mzuri kupita, kwa nini watu wengi wanakuacha na kwenda kufuata Yesu? (**“Yeye aliyekuwa pamoja nawe ngambo ya Yorodani”** ndiye Kristo.) Yoane alikuwa ameshuhudia Bwana Yesu, na kwa sababu ya ushuhuda wake, wengi wa wanafunzi wake mwenyewe walimwacha, wakakwenda kufuata Yesu.

**3:27** Kama ndani ya jibu lake Yoane alifikiri juu ya Bwana Yesu, maana yake ilikuwa kwamba baraka ambayo Yesu alikuwa nayo ilionyesha kwamba Mungu alimkubali. Kama Yoane alisema juu yake mwenyewe, maana ya jibu lake ndiyo ya kwamba hakujaribu kamwe kuonekana kama mtu mkubwa. Hakusema ubatizo wake ulikuwa mzuri kupita ule wa Yesu. Alisema tu kwamba hakuwa na kitu asichopewa **toka mbingu.** Neno hili ni kweli kwa sisi sote, na haifai tujivune au kujaribu kuonekana

kama wenye heshima kwa macho ya watu.

**3:28** Yoane alikumbusha wanafunzi ya kwamba alikuwa ameonyesha tena na tena kwamba yeye **si Kristo**, lakini **alitumwa** tu kutayarisha njia kwa Masiya. Kwa sababu gani watabishana juu yake na kufanya chama kwa ajili yake? Hakuwa na heshima yeye mwenyewe, lakini alijaribu tu kuongoza watu kutazama Bwana Yesu.

**3:29** Bwana Yesu alikuwa **bwana arusi.** Yoane Mbatizaji alikuwa **rafiki** tu **ya bwana arusi**. **Bwana arusi** alikuwa mwenye **bibi arusi**. Hivi ilikuwa taratibu kwa watu kufuata Yesu, si Yoane. **Bibi arusi** hapa anasema juu ya wote watakaogeuka wanafunzi wa Bwana Yesu. Ndani ya Agano la Kale Israeli linaitwa mke wa Yehova. Nyuma, ndani ya Agano Jipya, tunasoma juu ya wote walio ndani ya kanisa la Kristo kama bibi arusi. Lakini hapa ndani ya Habari Njema ya Yoane, neno hili lilitumiwa kusema juu ya wote walioacha kufuata Yoane Mbatizaji wakati Masiya alipotokea. Si Israeli wala kanisa. Yoane hakuhuzunishwa kwa sababu wafuata wake walimwacha na kufuata Yesu. Alifurahi sana kusikia **sauti ya bwana arusi**. Alifurahi kuona watu wakifikiri zaidi juu ya Yesu. **Furaha** yake **ilitimizwa** wakati watu waliposifu na kuheshimu Kristo.

**3:30** Kusudi zima la utumishi wa Yoane Mbatizaji linajumlishwa ndani ya shairi hili. Alitumika sana kuleta wanaume na wanawake kwa Bwana, na kuwasaidia kufahamu ukubwa wake wa kweli. Yoane alifahamu kwamba kwa kufanya hivi ilimpasa kujificha mwenyewe. Mtumishi wa Kristo anayekokota macho ya watu juu yake mwenyewe si mwaminifu kwa Bwana wake.

Ndani ya sura hii tunasoma juu ya maneno matatu yaliyo "sharti": kwa *mwenye zambi* (Yn. 3:7); kwa *Mwokozi* (Yo. 3:14); na kwa *mwamini* (Yn. 3:30).

**3:31 Yesu ndiye anayetoka juu na ni juu ya yote.** Masemo haya yanaonyesha kwamba Yesu ni wa mbinguni na juu ya yote. Yoane Mbatizaji alionyesha kwamba **yeye** mwenyewe ni mtu **wa dunia**, na **anasema maneno ya dunia.** Ni kusema alikuwa na wazazi waliokuwa watu wa dunia. Hakuweza kusema na amri sawa na Mwana wa Mungu. Alikuwa chini ya Bwana Yesu, kwa sababu **Yeye anayetoka mbinguni ni juu ya yote**. Kristo ni Mtawala mkubwa kupita wote, hivi ni vizuri kwa watu kumfuata yeye kupita mjumbe wake.

**3:32** Lakini wakati Bwana Yesu aliposema maneno alisema na amri. Aliwaambia watu maneno **aliyokwisha kuona na kusikia,** bila kuanguka wala udanganyifu. Hata hivi **hakuna mtu anayekubali ushuhuda wake**. Ni kusema zaidi ya watu hawakupokea ushuhuda wake. Kuna watu mmoja mmoja wanaopokea masemo ya Bwana Yesu. Lakini Yoane alifikiri juu ya jamii ya wanadamu, na alisema zaidi yao walikataa mafundisho ya Mwokozi. Yesu alikuwa yule aliyeshuka toka mbinguni, lakini watu wachache tu walikubali kumsikia.

**3:33** Shairi hili ni juu ya watu wachache walioamini masemo ya Yesu kwamba ni kweli maneno ya Mungu. Kwa njia ya kuyapokea **walitia mhuri ya kuwa Mungu ni kweli.** Ni vivyo hivyo leo. Ni njia kuonyesha kwamba mtu anayekubali **ushuhuda** wa Kristo anakubali kwamba **Mungu ni kweli**. Ni njia nyingine kusema kwamba ushuhuda wa Kristo ni ushuhuda wa *Mungu*, na kupokea ushuhuda wa Kristo ni kupokea ushuhuda wa Mungu.

**3:34** Yesu ndiye **aliyetumwa na Mungu.** Alisema **maneno ya Mungu**. Kusimamisha neno hili Yoane alisema kwamba **Mungu hatoi Roho kwa kipimo**. Namna Kristo alivyopakaliwa

na Roho Mtakatifu ya Mungu ilikuwa mbali na namna watu wo wote walivyopakaliwa. Kuna watu waliofahamu kwamba walisaidiwa na Roho Mtakatifu ndani ya utumishi wao, lakina hakuna mmoja mwenye utumishi uliojazwa Roho Mtakatifu kama Mwana wa Mungu. Manabii walipokea nusu ya ufunuo toka Mungu, lakini Roho alifunua ndani ya Kristo, na kwa njia yake, hekima na mawazo ya moyo wa Mungu, pamoja na mapendo yake yanayopita kipimo.

**3:35** Hapa ni mara moja ya mara saba tunazosoma ndani ya Habari Njema ya Yoane ya kwamba **Baba anapenda Mwana.** Alionyesha mapendo haya kwa njia ya kumpa amri juu ya **vitu vyote**, hata juu ya maisha na miisho ya watu, ndilo neno linaloelezwa ndani ya shairi 36.

**3:36** Mungu amempa Kristo amri kuwapa wote ambao wanamwamini **uzima wa milele**. Hili ni moja la mashairi yanayoeleza wazi zaidi ndani ya Biblia namna mtu anaweza kuokolewa. Ni kwa njia ya **kuamini Mwana tu**. Vizuri tufahamu ya kwamba maneno ya shairi hili ni sauti ya Mungu ikisema nasi. Anatoa ahadi isiyoweza kuvunjwa kamwe. Anasema wazi kabisa ya kwamba mtu ye yote **anayeamini Mwana** wake **ana uzima wa milele.** Kupokea ahadi hii ni kuamini tu neno lililo kweli. Wale **wasiotii Mwana** wa Mungu **hawataona uzima, lakini gazabu ya Mungu inakaa** juu yao hata sasa. Shairi hili linaonyesha kwamba namna tutakavyokaa kwa milele ni tunda la neno gani tunalofanya na **Mwana** wa Mungu. Tukimpokea, Mungu atatupa sisi **uzima** wa milele kama zawadi, lakini kama tukimkataa, hatutafurahishwa na **uzima** wa milele kamwe, lakini zaidi ya ile, **gazabu** ya Mungu ni tayari kutuangukia.

Ona ya kwamba hatusomi neno ndani ya shairi hili juu ya kushika sheria, kwenda kanisani, kutenda mema au kufanya kazi ili kujistahilisha mbingu.

### J. Kuzaliwa tena kwa mwanamke wa Samaria (4:1-30)

**4:1,2 Wafarisayo walisikia kwamba Yesu** anafanya na kubatiza **wanafunzi wengi kupita Yoane** na ya kwamba heshima ya Yoane ilikuwa ikipunguka. Labda walijaribu kutumika na habari hizi kuamsha wivu na magomvi katikati ya wanafunzi wa Yoane na wale wa Yesu. **Yesu hakubatiza** watu yeye mwenyewe. **Wanafunzi wake** walifanya kazi hii, lakini watu walibatizwa kama wafuata au wanafunzi wa Bwana.

**4:3** Kwa njia ya kuondokea **Yudea** na kusafiri kwa **Galilaya**, Yesu alizuiza Wafarisayo wasilete matengo katikati ya wanafunzi. Lakini kulikuwa na sababu nyingine vilevile kwa safari hii. **Yudea** ilikuwa kao la wakubwa wa dini ya Wayuda, lakini watu wengi wa Mataifa walikaa katika Galilaya. Bwana Yesu alifahamu kwamba viongozi vya Wayuda walikuwa wameanza kumkataa yeye na ushuhuda wake, hivi aligeuka kwa Mataifa na habari za wokovu.

**4:4** Njia fupi toka Yudea kwenda Galilaya ilipita kwa **Samaria,** lakini Wayuda wachache tu walisafiri kwa njia hii. Walizarau Wasamaria sana hata walifanya safari ndefu wakipita kwa Perea kuzunguka Samaria. Hivi wakati tunaposoma **imepasa Yesu apite katikati ya Samaria,** hakuchukua njia hii kwa sababu ilikuwa fupi, lakini kwa sababu ya hitaji la roho la mtu mmoja ambaye aliweza kusaidia kwa **Samaria.**

**4:5** Kwa safari yake kwenda **Samaria** Bwana Yesu alifikia mji, **jina lake Sukari**. Karibu na mji huu lilikuwa shamba ambalo Yakobo alimpa **mwana wake Yosefu** (Mwa. 48:22). Wakati Yesu aliposafiri kwa inchi hii, bila shaka aliwaza sana juu ya maneno yaliyotokea pale zamani.

**4:6** Kulikuwa na chemchemi ya maji pale iliyoitwa **kisima cha Yakobo**. Hata sasa wasafiri wanaweza kwenda kukiona.

Ilikuwa **karibu na saa sita azuhuri** wakati **Yesu** alipofikia kisima. **Alichoka** nyuma ya kufanya safari ndefu na miguu, **akakaa kwa kisima**. Hata Yesu alikuwa Mungu Mwana, alikuwa Mtu vilevile. Kama Mungu, hawezi kuchoka kamwe, lakini kama mtu alichoka kama sisi. Ni nguvu kwa sisi kufahamu maneno haya, lakini watu wenye nia ya umtu hawataweza kamwe kufahamu Bwana Yesu Kristo kabisa. Kwa Mungu kushuka na kufikia dunia na kuishi kama Mtu katikati ya watu ni siri inayoshinda ufahamu wetu.

**4:7** Wakati Yesu alipoketi kando ya kisima, **mwanamke** mmoja **alikuja** toka mji kuteka maji. Kama ilikuwa kweli saa sita azuhuri, hii si saa nzuri kwa wanawake kwenda kuteka maji, kwa sababu ya ukali wa jua. Lakini mwanamke huyu alikuwa mwanamke mwenye tabia mbaya, na labda alichagua saa hii kuteka maji kwa sababu ya haya, na hakutaka kukutana na wanawake wengine. Lakini Bwana Yesu alijua kwamba atafika pale kwa kisima kwa wakati ule. Alijua hitaji la roho yake, na alikusudi kukutana naye na kumponyesha toka maisha yake ya zambi.

Ndani ya mashairi haya tunaona Bwana Yesu, fundi mkubwa wa kazi ya kutafuta wapotevu, na namna gani alifahamisha mwanamke hitaji la roho yake na kumwonyesha namna gani aliweza kupata kusaidiwa. Alisema na mwanamke huyu mara saba tu. Mwanamke alisema mara saba vilevile – mara sita kwa Bwana na mara moja kwa wanaume wa mji. Labda kama tungalisema na Bwana mara nyingi kama yeye, ushuhuda wetu kwa Bwana ungalizaa matunda kupita vilevile. Bwana Yesu alianza kusema naye, **akamwomba, "Unipe maji ya kunywa."**

**4:8** Shairi hili linaeleza kwa sababu gani Bwana alimwomba kumpa maji ya kunywa. **Wanafunzi walikuwa wamekwendea Sukari kununua vyakula.** Ni kama walikwenda na ndoo zao, hivi Bwana alikosa njia kujipatia maji toka kisima.

**4:9** Mwanamke alitambua kwamba Yesu alikuwa **Myuda,** na alishangaa kwa sababu alisema naye mwanamke wa **Samaria**. Wasamaria waliamini wao ni wazao wa Yakobo, na ya kwamba wao ni Waisraeli wa kweli. Lakini neno hili halikuwa kweli kabisa. Wengine wa wazao wao walikuwa watu wa Mataifa. Walichagua Mlima Gerizimu kuwa pahali pao kwa kuabudu. Bwana Yesu na mwanamke waliweza kuona mlima huu toka pahali waliposemezana. Wayuda hawakupenda Wasamaria hata kidogo na hawakuwahesabu kuwa Wayuda safi. Kwa sababu hii mwanamke alisema na Bwana Yesu, **"Namna gani wewe Myuda unaomba maji kwangu, nami ni mwanamke wa Samaria?"** Hakufahamu hata kidogo kwamba alikuwa akisemezana na Mwumba wake mwenyewe, mwenye mapendo makubwa kupita tofauti bure katikati ya watu.

**4:10,11** Kwa njia ya kuomba kitu kwake, Bwana aliamusha hamu ndani ya mwanamke huyu kujua kupita juu yake. Aliendelea kumfazaisha kwa njia ya kusema juu yake mwenyewe kama Mungu na Mtu. Alikuwa kwanza **zawadi ya Mungu** – Yule ambaye **Mungu** alitoa kuwa Mwokozi wa dunia, Mwana wake wa pekee. Lakini alikuwa Mtu vilevile – aliyekuwa amechoka na safari yake na aliyeomba **maji ya kunywa.** Kama mwanamke angalifahamu kwamba yule ambaye alisema naye alikuwa Mungu kwa mwili wa mtu, **angalimwomba yeye** kumbariki, naye **angalimpa maji yaliyo hai.** Lakini mawazo ya mwanamke yalikuwa juu ya maji ya dunia tu na ya kwamba hakuwa na njia kuyapata bila ndoo. Hakufahamu maana ya masemo ya Bwana hata kidogo.

**4:12** Mafazaiko yake yalikaa kuonge-

zeka wakati alipowaza juu ya baba **Yakobo,** ambaye aliwapa **kisima** hiki. Alikunywa maji ya kisima hiki yeye mwenyewe, kwa **mahitaji yake mwenyewe, na yale ya wana wake na makundi yake.** Tena sasa, nyuma ya mia za miaka msafiri huyu mwenye kuchoka, ambaye alimwomba kumpa maji ya kunywa toka kisima cha Yakobo, alisema aliweza kumpa maji mazuri kupita yale ambayo Yakobo aliwapa. Kama akiwa na maji mazuri kupita, kwa sababu gani aliomba kupewa maji toka kisima cha Yakobo?

**4:13** Halafu Bwana alianza kueleza tofauti kati ya maji ya kisima cha Yakobo na maji yeye aliyotaka kumpa. **Kila mtu atakayekunywa maji haya ataona kiu tena.** Mwanamke Msamaria alifahamu neno hili vizuri. Alifika kila siku kuteka maji toka kisima hiki, lakini hitaji lake kwa maji halikushibishwa kamwe. Ni vivyo hivyo na visima vyote vya dunia. Watu wanatafuta furaha na salama ndani ya maneno ya dunia, lakini maneno haya hayawezi kushibisha kiu ya roho zao.

**4:14 Maji** Bwana Yesu anayotoa yanashibisha kiu kabisa. **Mtu ye yote anayekunywa** ya baraka za Kristo **hatakuwa na kiu tena kamwe,** na zaidi ya ile baraka hizi **zitafurika** toka roho yake kama **toka kisima** kusaidia watu wengine vilevile. Maana ya **yanayochemuka hata uzima wa milele** ni ya kama faida ya maji haya Kristo anayotoa si kwa dunia hii tu, lakini itaendelea kwa milele. Vyote tunavyoweza kupata duniani haviwezi kushibisha mahitaji ya roho, lakini baraka Kristo anazotoa ni nyingi sana na zinapita kipimo cha mioyo yetu.

Furaha za dunia ni kwa miaka michache tu, lakini furaha Kristo anazotoa **zinaendela hata milele.**

**4:15** Wakati **mwanamke** aliposikia habari za maji haya ya ajabu, alitaka kuyapata mara moja. Lakini alikaa kufikiri juu ya maji ya *dunia*. Hakutaka kufika kwa kisima kile kila siku **kuteka** maji na kubeba ndoo nzito kichwani kuyafikisha kwake. Hakufahamu kwamba maji ambayo Bwana Yesu alisema juu yake yalikuwa maji ya roho anayowapa watu ambao wanamwamini.

**4:16** Halafu mazungumuzo yao yaligeuka. Mwanamke alikuwa ameomba kupewa maji, lakini Bwana Yesu alisema naye **kwenda kuita mume wake.** Kwa sababu gani? Mbele ya mwanamke huyu kupata wokovu, ilimpasa kufahamu na kukiri kwamba yeye ni mwenye zambi. Sharti afike karibu na Bwana na toba ya kweli na kukiri zambi na haya yake. Bwana Yesu alijua habari za maisha yake ya zambi, na alikuwa akimwongoza kufahamu neno hili yeye mwenyewe.

Wale tu wanaojua kwamba wao ni wapotevu wanaweza kupata wokovu. Watu wote wamepotea lakini si watu wote wanaokubali neno hili. Wakati tunapojaribu kuleta watu kwa Kristo, tusikose kuwafundisha waziwazi juu ya zambi zao. Sharti wafahamu kwamba wao ni wafu katika zambi na makosa, ya kwamba wanahitaji Mwokozi, ya kwamba hawawezi kujiokoa wenyewe, ya kwamba Yesu ndiye Mwokozi ambaye wanahitaji, na ya kwamba atawaokoa kama wakitubu zambi zao na kumwamini yeye.

**4:17** Kwanza **mwanamke** alijaribu kuficha kweli bila kusema uwongo. Alisema, **"Sina mume."** Labda kwa njia ya sheria neno hili lilikuwa kweli, lakini alikuwa akificha uovu wake kwa wakati ule, ndio kwamba alikaa pamoja na mtu asiyekuwa mume wake.

Bwana Yesu, akiwa Mungu, alijua maneno haya yote. Halafu alisema naye **"Umesema vema, 'Sina mume.'"** Hata kama mwanamke aliweza kudanganya watu, hakuweza kudanganya Mtu huyu. Alijua maneno haya yote.

**4:18** Hata kama Bwana alijua maneno yote, hakutumia ufahamu wake kuha-

yarisha mtu bila sababu. Lakini mara nyingine ilimpasa kufanya hivi, kama ikihitajiwa kufungua mtu toka utumwa wa zambi. Bila shaka mwanamke alishituka sana wakati aliposikia Bwana akisema habari zake zote. Ndiyo, alikuwa na **waume watano** mbele**,** na mtu ambaye alikaa naye kwa wakati ule **hakuwa mume** wake.

Watu wana mawazo mbalimbali juu ya shairi hili. Wengine wanafundisha ya kwamba, au waume wale watano wa mbele walimwacha, au walikufa, na ya kwamba hakuzini nao. Hatujui kama mawazo haya ni kweli, lakini mwisho wa shairi hili unaonyesha kwamba alikuwa mzinzi mwanamke. **"Yeye uliye naye sasa si mume wako.**" Neno hili lilikuwa neno kubwa, na kufika wakati mwanamke alipokiri zambi yake, Bwana hakuweza kumbariki kwa njia ya kumpa maji ya uzima.

**4:19** Wakati maisha ya **mwanamke** yalipofunuliwa wazi hivi mbele yake alifahamu kwamba yule ambaye alisema naye alikuwa mtu namna nyingine. Lakini hakufahamu kwanza kwamba alikuwa Mungu lakini alifikiri alisema kwa ajili ya Mungu, ya kwamba alikuwa **nabii** wa Mungu.

**4:20** Ni kama sasa mwanamke alikuwa amefahamu ukubwa wa zambi zake na alijaribu kusema juu ya maneno mengine. Aliuliza kama ilipasa watu kuabudu wapi. Pamoja na kuonyesha mlima wa Gerizimu alisema, **"Baba zetu waliabudu katika kilima hiki,"** akakumbusha Bwana kwamba **Wayuda** walisema inapasa watu kuabudu katika **Yerusalema.**

**4:21** **Yesu** hakuona masemo ya mwanamke bure, lakini alitumika nayo kufundisha kweli nyingine. Alimwambia ya kwamba kwa **wakati wa kuja** watu **hawataabudu** kwa mlima **Gerizimu** wala kwa **Yerusalema.** Katika Agano la Kale Mungu alichagua Yerusalema kuwa pahali ilipopasa watu kumwabudu. Hekalu kwa Yerusalema lilikuwa kao la Mungu, na Wayuda ambao walimpenda walifikia Yerusalema na sadaka na matoleo yao. Sasa, kwa muda huu wa Habari Njema maneno haya yamegeuka. Mungu hana pahali fulani tena inapopasa watu kufikia kumwabudu. Bwana aliendelea kueleza maneno haya ndani ya mashairi yanayofuata.

**4:22** Wakati Bwana aliposema, **"Munaabudu ambacho hamukijui,"** alihukumu namna ya kuabudu kwa Wasamaria. Hakuwa sawasawa na walimu wengine wanaofundisha dini zote zina faida na kwamba mwishoni zitatufikisha mbinguni. Bwana Yesu alimwambia mwanamke kwamba utaratibu wa kuabudu wa Wasamaria haukusimamishwa na Mungu na haukukubaliwa naye. Ulisimamishwa na watu na kuongozwa nao bila ukubali wa Neno la Mungu. Mungu alikuwa ameweka Wayuda mbali kwa yeye kama watu wake wachaguliwa duniani na aliwafundisha namna gani iliwapasa kumwabudu.

Wakati Bwana aliposema **"wokovu unatoka kwa Wayuda,"** alifundisha kwamba alikuwa ameweka Wayuda kuwa wajumbe wake na kwamba ni wao waliotolewa Maandiko Matakatifu. Na vilevile Masiya alizaliwa kwa njia ya taifa la Wayuda. Alizaliwa na mama Myuda.

**4:23** Halafu alipasha mwanamke kwamba tangu kufika kwa Masiya duniani, Mungu hakuwa tena na pahali fulani duniani pahali inapopasa watu kuabudu. Sasa wale wanaoamini Bwana Yesu wanaweza kuabudu Mungu saa yo yote na pahali po pote. Maana ya kuabudu kwa kweli ni kwamba mwamini anafika mbele ya Mungu na imani na kumsifu na kumwabudu *pale*. Labda mwili wake ni ndani ya pango au gerezani au shambani, lakini roho yake inaweza kukaribia Mungu katika pahali patakatifu mbinguni

kwa imani. Yesu alijulisha mwanamke kwamba kuanza na wakati ule waabudaji wa kweli wataabudu Baba **katika roho na kweli**. Wayuda walikuwa wamepunguza kuabudu kwao kwa maneno waliyofanya kwa kuonekana kwa watu tu. Walifikiri kwamba kwa njia ya kushika na kutii kila neno dogo la sheria na kufuata kawaida nyingine ya dini walikuwa wakiabudu Baba. Lakini hawakumwabudu katika roho. Hata kama wakiinama chini mbele ya Mungu, lilikuwa neno la kuonekana tu lakini roho zao hazikuwa safi mbele yake. Labda walikuwa wakilemea wamasikini au kutenda biashara yao kwa udanganyifu.

Wasamaria walikuwa na utaratibu wa kuabudu lakini haukuwa kwa amri ya maandiko matakatifu ya Mungu. Walikuwa wameanza dini yao wenyewe. Hivi wakati Bwana Yesu aliposema **sharti tuabudu katika roho na kweli** alihamakia Wayuda pamoja na Wasamaria. Lakini aliwajulisha vilevile ya kwamba tangu kufika kwake duniani iliwezekana kwa watu kukaribia Mungu kwa njia ya kuabudu katika roho na kweli. Waza juu ya maneno haya: Baba anatafuta wenye kumwabudu hivi. Anaweka roho juu ya kuabudu kwa watu wake. Wewe na mimi tunamwabudu hivi?

**4:24 Mungu ni Roho** – maneno haya yanatuonyesha kama Mungu ni namna gani. Yeye si mtu tu mwenye kuanguka na mwenye **vizuizo** vya binadamu. Halazimishwi kuwa kwa pahali pamoja tu kwa saa moja. Hatuwezi kumwona na macho, lakini yeye ni pahali po pote kwa saa yo yote. Yeye ni mkamilifu ndani ya njia zake zote. Hivi **wale ambao wanamwabudu sharti wamwabudu katika roho na kweli,** bila hila wala udanganyifu. Haifai wajionyeshe kuwa watu wa dini wakati rohoni wao ni waovu. Haifai wafikiri wanaweza kupendeza Mungu kwa njia ya kawaida ya dini. Hata kama Mungu mwenyewe alisimamisha kawaida hii, ni lazima kwa mtu kumkaribia na roho ya kuvunjika na toba. Kuna "lazima" nyingine ndani ya sura hii: kwa mwenye kutafuta roho za watu kwa Mungu (4:4), na kwa waabudaji (4:24).

**4:25** Wakati mwanamke alipokuwa akisikiliza Bwana, alianza kufikiri juu ya Masiya. Roho Mtakatifu aliamsha ndani ya roho yake hamu kwa kuja kwake. Alisema ya kwamba wakati atakapokuja, atawafundisha maneno yote. Masemo yake yalionyesha kwamba alikuwa amefahamu vizuri sababu ya kuja kwa Kristo.

**"Masiya … anayeitwa Kristo"** inaonyesha kwamba maana ya maneno haya mawili ni moja. **Masiya** ndiyo Kiebrania na **Kristo** ni Kiyunani.

**4:26** Yesu alisema naye, **"Mimi ninayesema nawe ndiye.**" Kabisa kabisa alisema "Mimi ninayesema nawe ni" lakini wenye kutafsiri walifikiri kuandika *ndiye* ni nyepesi kupita kufahamu. Lakini wakati Bwana aliposema "mimi ni" alitumika na **moja la majina** ambayo Mungu alijiita mwenyewe ndani ya Agano la Kale. Alisema, "MIMI NI ninasema nawe," Au kusema "Yehova anasema nawe." Anamjulisha kweli kubwa ya kwamba yeye alikuwa Masiya ambaye mwanamke alitazamia na alikuwa Mungu mwenyewe. Yehova katika Agano la Kale ni Yesu katika Agano Jipya.

**4:27** Wakati **wanafunzi** waliporudi toka Sukari walikuta Yesu akisema na mwanamke huyu. Bila shaka walishangaa kidogo juu ya neno hili, kwa sababu mwanamke alikuwa Msamaria. Labda hawakufahamu kwamba alikuwa mwanamke wa zambi. Lakini hata mmoja wao hakuuliza kama alitafuta nini kwake au kwa sababu gani **alisema naye**.

**4:28 Halafu mwanamke aliacha chungu chake!** Chungu hiki kilikuwa kama mfano wa vitu vyote alivyotumika

navyo ndani ya maisha yake kushibisha hamu kubwa ya roho yake. Vilikuwa vyote bure. Sasa alikuwa amekutana na Yesu na hakuhitaji vitu hivi tena!

Hakuacha **chungu cha maji** tu, lakini **alikwenda zake mjini.** Wakati mtu anapookolewa, anaanza mara moja kufikiri juu ya watu wengine wanaohitaji maji ya uzima. J. Hudson Taylor alisema, "Wengine wangetaka sana kufuata mitume ndani ya kazi yao; mimi ningefurahi kupita kushika kazi ya mwanamke wa Samaria, maana wao walikwenda zao kutafuta vyakula, lakini yeye alisahau chungu chake cha maji kwa sababu ya bidii yake kwa roho za watu."

**4:29,30** Hakutumia masemo makubwa, lakini ushuhuda wake ulikuwa na uwezo. Aliita watu wa mji kuja na kutazama **mtu ambaye aliniambia maneno yote ambaye niliyatenda.** Vilevile aliamsha ndani ya roho zao mawazo ya kwamba labda Mtu huyu alikuwa Masiya. Yeye mwenyewe hakuwa na shaka juu yake kwa sababu Bwana alikuwa amemwambia kwamba yeye ni **Kristo**. Lakini aliamsha ulizo hili ndani ya mafikiri yao ili wao wenyewe waweze kufika karibu na Yesu na kuona kama ni kweli. Bila shaka mwanamke huyu alijulikana mjini kwa sababu ya maisha yake ya zambi na haya, na watu walishangaa kumwona akisimama sasa bila haya katikati yao na kushuhudia Bwana Yesu Kristo! Ushuhuda wake ulikuwa na uwezo. Watu wa mji walitoka nyumba zao, wakakwenda kutafuta Yesu.

### K. Furaha ya Mwana kufanya mapenzi ya Baba (4:31-38)

**4:31** Sasa **wanafunzi** walikuwa wamerudi na chakula, wakasukuma Bwana **kula**. Hawakufahamu kwamba mambo makubwa yalikuwa yakitokea. Kwa saa hii wakati watu wa mji katika Samaria waliposikia juu ya Bwana wa utukufu, wanafunzi walifikiri maneno ya chakula kwa miili yao tu.

**4:32** Bwana Yesu alikuwa amepata **vyakula** na msaada ndani ya kazi hii ya kufikisha waabudaji karibu na Baba yake. Kwa sababu ya furaha hii kubwa hakuweka roho juu ya maneno ya chakula kwa mwili wake. Ndani ya maisha yetu tunapata maneno tunayotafuta. Wanafunzi walitafuta vyakula na walirudi navyo. Bwana Yesu alitafuta roho za watu. Aliweka roho juu ya kuokoa watu toka zambi zao, na kuwapa maji ya uzima wa milele. Yeye vilevile alipata aliotafuta. Sisi tunatafuta nini?

**4:33** Kwa sababu wanafunzi walifikiri maneno ya dunia tu, hawakufahamu maana ya masemo ya Bwana. Hawakufahamu ya kwamba furaha ya baraka ya roho inaweza kufanyiza watu kusahau kwa wakati hitaji la mwili kwa chakula na kinyweo. Hivi walifikiri labda mtu mwingine **aliletea** Bwana Yesu chakula.

**4:34** Bwana Yesu alijaribu tena kugeuza mawazo yao toka vitu vya dunia na kuwafikirisha vitu vya roho. Chakula chake kilikuwa kufanya mapenzi ya Mungu na kumaliza kazi ambayo Bwana alimpa. Si kusema ya kwamba Bwana Yesu hakula chakula lakini ya kwamba kusudi kubwa la maisha yake halikuwa kubembeleza mwili wake lakini kufanya mapenzi ya Mungu.

**4:35** Labda wanafunzi walikuwa wamesemezana juu ya mavuno yaliyokuwa karibu. Au ilikuwa mezali katikati ya Wayuda, **"Imebaki miezi mine hata mvuno."** Bwana Yesu alitumika tena na mfano wa **mavuno** ya dunia kufundisha kweli za roho. Haifai wanafunzi wafikiri mavuno yalikuwa kwanza mbali. Haifai wapoteze maisha yao wakitafuta vyakula na mavazi na kufikiri kwamba wataweza kufanya kazi ya Mungu nyuma. Wafahamu kwamba mashamba **yamekwisha kuwa meupe, tayari kwa mavuno**. **Mashamba** ndiyo mfano wa ulimwengu. Kwa saa Bwana aliposema maneno haya alikuwa ndani ya shamba la mavuno la

roho za wanaume na wanawake Wasamaria. Aliwaambia wanafunzi ya kwamba kazi kubwa ya kukusanya mavuno ilikuwa ikiwangojea, na sharti wajitoe kufanya kazi hii mara moja na kwa bidii.

Hivi kwa wakati wa sasa Bwana anasema na sisi tulio waamini, **"Munyanyue macho yenu, mutazame mashamba"**. Wakati tunapowaza juu ya mahitaji kwa Habari Njema kwa dunia hii kubwa, Bwana atatupa mzigo rohoni kwa wapotevu ambao wanatuzunguka pande zote. Halafu itakuwa kazi yetu kwenda kuhubiri kwa pahali pake na kukusanya mavuno.

**4:36** Halafu Bwana alifundisha wanafunzi juu ya kazi ambayo aliwaita kufanya. Alikuwa amewachagua kuwa wavunaji. Hawatapokea **mshahara** hapa duniani tu lakini watakusanya **matunda** kwa milele vilevile. Kuna zawabu nyingi kwa wenye kutumikia Kristo kwa wakati wa sasa. Lakini zaidi ya ile kwa wakati wa kuja watapata furaha kubwa wakati watakapoona watu wengine mbinguni kwa sababu ya uaminifu wao katika kazi ya kuhubiri Habari Njema.

**Shairi 36** *halifundishi* kwamba mtu anapokea uzima wa milele kwa njia ya kuvuna na uaminifu lakini ya kuwa **matunda** ya kazi yake yataendelea kwa milele.

Mbinguni mpandaji mbegu na mvunaji watafurahi pamoja. Hapa duniani ni lazima kutayarisha shamba kwanza kupokea mbegu. Nyuma ngano inavunwa. Vivyo hivyo inapasa Habari Njema kuhubiriwa kwanza, nyuma yake inapasa kuitoa maji ya maombi. Lakini kwa wakati wa mavuno wote walioshiriki ndani ya kazi hii **watafurahi pamoja.**

**4:37** Ndani ya neno hili Bwana aliona kutimia kwa semo moja la wakati ule, ndilo **"Mmoja anapanda, mwingine anavuna."** Wakristo wengine wanaitwa kuhubiri Habari Njema kwa miaka mingi bila kuona matunda ya kazi yao. Halafu kwa mwisho wa miaka ile, watu wengine wanakuja, na watu wengi wanaamini Bwana.

**4:38** Yesu alikuwa akituma wanafunzi wake kwa pahali palipotayarishwa na watu wengine. Kwa muda wa Agano la Kale manabii walikuwa wametabiri kuja kwa muda wa Habari Njema na ya kwamba Masiya atakuja. Na vilevile Yoane Mbatizaji alikuja kama mtangulizi wa Bwana na alijaribu kutayarisha roho za watu kupokea Masiya. Bwana yeye mwenyewe alikuwa amepanda mbegu kwa Samaria, na kutayarisha mavuno kwa wavunaji. Sasa ilikuwa saa kwa wanafunzi kuingia shamba na kuvuna, na Bwana alitaka wafahamu ya kwamba hata kama wakiona watu wengi kuamini Bwana walikuwa wakishiriki **ndani ya kazi** ya watu wengine**.**

Watu wachache tu wanaokolewa kwa sababu ya ushuhuda wa mtu mmoja tu. Zaidi ya waamini walikuwa wamesikia Habari Njema mara nyingi mbele ya kupokea Mwokozi. Hivi haifai yule anayefikisha mtu huyu karibu na Bwana kwa mwisho, ajisifu ya kama yeye ndiye mtumishi wa pekee ambaye alitumiwa na Mungu kwa kazi hii ya ajabu.

### I. Wasamaria wengi wanaamini Yesu (4:39-42)

**4:39** Kwa sababu ya ushuhuda wazi wa mwanamke wa Samaria watu **wengi** wa kijiji **waliamini** Bwana Yesu. Mwanamke aliwaambia tu, **"Aliniambia mambo yote ambayo nilitenda,"** na maneno haya yalitosha kuwafikisha karibu na Mwokozi. Vizuri ushuhuda wake uwe mfano mzuri kwetu ndani ya ushuhuda wetu kwa Kristo.

**4:40** Wasamaria walipokea Bwana Yesu vizuri kupita Wayuda. Ni kama **Wasamaria** walitambua ukubwa wa Bwana Yesu na **walimsihi akae kwao.** Basi **alikaa nao siku mbili.** Ilikuwa baraka na heshima kubwa kwa Wa-

samaria kuwa na Bwana wa uzima na utukufu kama mgeni wao kwa muda huu!

**4:41,42** Watu wanaokolewa kwa njia mbalimbali. Wengine waliamini kwa sababu ya ushuhuda wa mwanamke. **Wengi wengine waliamini kwa sababu** ya maneno Bwana Yesu aliyosema yeye mwenywe. Mungu anatumika kwa njia mbalimbali kuleta wenye zambi kwake. Neno kubwa, la lazima, ni kwa watu kuwa na imani ndani ya Bwana Yesu. Ni vizuri sana kusikia Wasamaria wakitoa ushuhuda wazi namna hii kwa Mwokozi. Hawakuwa na shaka hata kidogo juu ya wokovu wao, si kwa sababu ya masemo ya mwanamke lakini kwa sababa ya maneno ya Bwana Yesu mwenyewe. Nyuma ya **kumsikia** na kuamini maneno yake, Wasamaria walifahamu kabisa ya kwamba **huyu ndiye kweli Kristo, Mwokozi wa ulimwengu.** Roho Mtakatifu tu aliweza kuwafahamisha neno hili. Ni kama Wayuda walifikiri kwamba Bwana Yesu atakuwa Masiya wa taifa lao wenyewe tu. Lakini Wasamaria walifahamu kwamba **ulimwengu** mzima utabarikiwa kwa njia ya kuja na kazi ya Kristo.

### M. Alama ya pili: Kuponyeshwa kwa mwana wa mkubwa wa mfalme (4:43-54)

**4:43,44** **Nyuma ya kushinda** pamoja na Wasamaria kwa **siku mbili** Bwana alikwenda tena kwa Galilaya. Shairi 44 linaweza kutufazaisha. Bwana yeye mwenywe alisema kwamba **nabii hana heshima katika inchi yake mwenyewe.** Lakini Galilaya ilikuwa inchi ya Yesu. Nazareti ulikuwa mji wa Galilaya. Labda alikwenda kwa upande mwingine wa Galilaya, si kwa Nazareti. Na ni kweli ya kwamba mara nyingi mtu anaheshimiwa na watu wa pahali pangine kupita na wenyeji wa mji wake mwenyewe. Kwa macho ya jamaa na rafiki zake yeye ni kijana tu na mmoja wao. Bila shaka Bwana Yesu mwenyewe hakuheshimiwa na watu wake kwa kipimo kilichofaa.

**4:45** Wakati aliporudi kwa **Galilaya** alipokewa vizuri kwa sababu watu wa pale walikuwa wameona **maneno yote** aliyofanya katika **Yerusalema** kwa karamu. Wagalilaya hawa walikuwa Wayuda. Walikuwa wamekwenda Yerusalema kwa kuabudu na waliona Bwana kule na kazi za uwezo alizofanya. Sasa walikubali kwaye kukaa katikati yao katika Galilaya, si kwa sababu walifikiri yeye ni Mwana wa Mungu lakini kwa sababu walijua kupita juu yake kwani watu wote walisema juu yake pahali po pote alipokwenda.

**4:46** Hivi kijiji **Kana** kiliheshimiwa kwa sababu Bwana mwenyewe aliwafikia tena. Wakati alipofika mara ya kwanza watu wengine walimwona akigeuza maji kuwa mvinyo. Sasa watamwona akifanya ajabu kubwa nyingine. **Mkubwa mmoja wa ufalme** alikuwa pale aliyekuwa na **mwana mgonjwa kwa Kapernaumu.** Bila shaka mtu huyu alikuwa Myuda na mtumishi wa mfalme Herode.

**4:47** Mtu huyu **alisikia** kwamba Yesu alikuwa kwa **Yudea** na alikuwa amerudia Galilaya. Ni kama aliamini kwamba Yesu aliweza kuponyesha mgonjwa kwani alikwenda kwake na **kumsihi kushuka kuponyesha mwana wake** aliyekuwa karibu kufa. Ni kama alikuwa na imani kubwa kupita zaidi ya watu wa inchi yake.

**4:48** Akisema na **Wayuda,** si kwa mkubwa wa mfalme tu, Bwana aliwakumbusha moja ya desturi za taifa lao, ya kwamba walitaka kuona maajabu mbele ya **kuamini**. Lakini Bwana Yesu hakupendezwa zaidi na imani iliyotegemea maajabu. Alitaka watu kuamini Neno lake, peke yake. Tunaheshimu Bwana kupita wakati tunapoamini neno fulani kwa sababu yeye alilisema, si kwa sababu alisimamisha neno hili na alama. Ni desturi ya watu kutaka kuona mbele ya kuamini. Lakini Bwana Yesu anatu-

fundisha kwamba inatupasa kuamini kwanza, na nyuma yake tutaona.

**4:49** **Mkubwa wa ufalme**, akiwa na imani ya kweli ya kwamba Bwana Yesu ataweza kusaidia mwana wake, alitaka sana kwa Bwana kufika kwake. Kwa njia moja imani yake ilikuwa na upungufu. Alifikiri ilikuwa lazima kwa Yesu kufikia kitanda cha mtoto mbele ya kuweza kumponyesha. Mwokozi hakumhamakia juu ya neno hili, lakini alimsaidia kwa *kipimo* cha imani yake.

**4:50** Ndani ya shairi hili tunaona imani ya mtu huyu ikipata nguvu. Yesu alisema naye kurudi kwake na ahadi ya kwamba **"Mwana wako ni hai."** Mwana wake alikuwa ameponyeshwa! Bila kuona ajabu au neno lo lote mkubwa wa ufalme **aliamini neno** aliloambiwa na Bwana **Yesu**, akashika njia kurudi kwake. Hii ndiyo imani ya kweli!

**4:51,52** **Wakati alipokaribia nyumba** yake, **watumishi wake** walitoka na habari za furaha ya kwamba **mwana** wake alikwisha kupona. Mtu huyu hakushangazwa na habari hizi. Alikuwa ameamini ahadi ya Bwana Yesu, na nyuma ya kuamini aliona kwamba neno hili lilikuwa limetokea kweli. Baba **aliuliza** watumishi **saa gani** mwana wake alipo**anza kuwa hajambo.** Jibu lao lilionyesha kwamba hakupona polepole, lakini mara moja.

**4:53** Bila shaka ajabu hili lilitokea kweli. Kwa saa saba ya siku iliyopita **Yesu** alikuwa **amesema** na mkubwa wa ufalme kwa Kana, **"Mwana wako anaishi." Saa ile ile** kwa Kapernaumu mwana wake alipona, na homa ilimwacha. Matukio haya yalifundisha mkubwa wa ufalme ya kwamba haikuwa sharti kwa Bwana kuwa palepale kufanya ajabu au kujibu maombi. Yangepasa kusaidia roho za Wakristo wote wakati wanapoomba. Tuna Mungu wa uwezo mkubwa naye anasikia maombi yetu na anaweza kutimiza makusudi yake pahali po pote duniani kwa saa yo yote.

Mkubwa wa ufalme **aliamini na nyumba yake yote.** Shairi hili na mashairi mengine namna hii katika Agano Jipya yanaonyesha kwamba Mungu anapenda kuona jamaa nzima wakiamini na kuwa moja ndani ya Kristo. Si mapenzi yake kwa nusu ya jamaa tu kuwa mbinguni (maana wengine katika jamaa hii wakiwa wasioamini). Hivi tunasoma hapa kwamba **nyumba yake yote** waliamini Mwana wake.

**4:54** Ajabu hili la kuponyesha mwana wa mkubwa wa ufalme halikuwa ajabu la pili Yesu alilofanya tangu mwanzo wa utumishi wake. Ilikuwa **alama ya pili** alilofanya katika **Galilaya** nyuma ya **kutoka Yudea.**

## 3. MWAKA WA PILI WA UTUMISHI WA MWANA WA MUNGU (Sura 5)

### A. Alama ya tatu: Kuponyeshwa kwa mwenye kupooza (5:1-9)

**5:1** Kwa mwanzo wa sura hii tunasoma juu ya moja ya siku kubwa ya Wayuda. Hatujui kama ilikuwa siku kubwa gani – labda ilikuwa **Pasaka**. Yesu alizaliwa hapa duniani kama Myuda na alitii sheria za Mungu kwa Wayuda, hivi **akapanda kwenda Yerusalema kwa karamu**. Kama Yehova wa Agano la Kale Bwana Yesu mwenyewe alianzisha Pasaka. Sasa, kama Mtu, mwenye kutii Baba yake, alitii sheria zile yeye mwenyewe alizofanya.

**5:2** Katika **Yerusalema** kulikuwa na birika lililoitwa **Betesaida**,[12] maana yake "nyumba ya rehema" au "nyumba ya huruma." Birika hili lilikuwa karibu na **Mlango wa Kondoo**. Birika lilizungushwa na **Baraza tano** pahali watu walipoweza kukaa. Walimu wengine wanafikiri Baraza hizi ni mfano wa sheria ya Musa isiyoweza kusaidia mtu kutoka katika taabu yake kubwa.

**5:3** Ni kama birika la Betesaida lilijulikana kama pahali maajabu ya kuponyesha yalitukia. Hatujui kama maajabu yalitukia kwa saa fulani, kama kwa siku kubwa, au kwa mwaka mzima. **Wagonjwa wengi** walizunguka birika wakitumaini kuponyeshwa. Kulikuwa na **vipofu, viwete, na wenye kupooza.** Wote walikuwa mfano wa mwenye zambi katika uzaifu na upofu na kupooza kwake, wasio na faida.

Watu hawa waliokuwa wakiteswa na matunda ya zambi miilini mwao walikuwa wakingojea **kuchemuka kwa maji.** Walitaka sana sana kuponyeshwa toka magonjwa yao.

**5:4** Kuna habari chache tu za maneno yaliyotukia. Tunasoma tu kwamba wakati fulani **malaika alishuka, akaingia lile birika, akichemusha maji.** Mtu wa **kwanza** aliyeweza kuingia birika kwa wakati ule aliponyeshwa. Lilikuwa ono la kuamsha huruma rohoni kutazama wagonjwa wale wote wakijaribu kuingia maji, na halafu mtu mmoja tu akipata kusaidiwa.

Sehemu ya mwisho ya shairi 3 (kuanza na "wakingojea kuchemuka kwa maji") na shairi 4 zima linakosa ndani ya tafsiri nyingi za Biblia, lakini maneno haya ni ndani ya tafsiri nyingi zaidi za zamani na yanatusaidia kufahamu habari hizi.

**5:5,6** Mmoja wa wanaume waliongoja kwa birika alikuwa mgonjwa kwa **miaka makumi tatu na minane**. Alikuwa mgonjwa hata mbele ya kuzaliwa kwa Mwokozi. Bwana Yesu alijua habari zake zote. Hakukutana naye mbele lakini alijua kwamba alikuwa mgonjwa **tangu miaka mingi.**

Na mapendo na huruma **alimwuliza, "Unataka kuwa mzima?"** Yesu alijua kwamba hili ndilo neno mgonjwa huyu alilotaka kupita yote. Lakini alitaka mtu huyu kukiri wazi kwamba hakuweza kujiponyesha mwenyewe na kwamba alihitaji sana sana kuponyeshwa. Ni vivyo hivyo na wokovu. Bwana anajua hitaji letu kubwa kwa wokovu, lakini anataka kutusikia sisi tukikiri na midomo yetu wenyewe ya kwamba tumepotea, ya kwamba tunamhitaji yeye, na tunampokea kuwa Mwokozi wetu mwenyewe. Hatupati wokovu kwa mapenzi yetu wenyewe, lakini ni lazima kwa sisi kuchagua kukiri hitaji letu kubwa; kisha Mungu ataweza kutuokoa.

**5:7** Jibu la **mgonjwa** lilikuwa la kutia huruma. Kwa miaka ile yote alikuwa amelala karibu na birika akingoja kuingia ndani ya maji, lakini kila mara maji **yaliyochemuka** hakuwa na mtu kumsaidia, na mtu mwingine aliingia mbele yake. Habari zake zinatukumbusha kwamba si faida kwetu kutegemea mtu mwingine kutuokoa toka zambi zetu.

**5:8 Kitanda** cha mtu huyu kilikuwa mkeka mdogo. Yesu alisema naye **kusimama,** kubeba kitanda chake na **kutembea.** Ni mafundisho kwa sisi ya kwamba wakati tunapookolewa, hatuagizwi kusimama tu, lakini kutembea vilevile. Bwana Yesu anatuponyesha toka tauni la zambi, kisha anataka mwenendo wetu kumtukuza yeye.

**5:9** Mwokozi haagizi mtu kamwe kufanya kitu fulani bila kumpa uwezo anaohitaji kukifanya. Wakati alipokuwa akisema na mtu huyu, uzima na uwezo mpya ziliingia mwili wake, akaponyeshwa mara moja. Viungo vya mwili wake vilivyokuwa zaifu na kukosa kuwa na faida vilipata nguvu tena. Halafu mgonjwa alitii agizo la Bwana mara moja. **Alichukua kitanda chake, akatembea.** Bila shaka kuweza kufanya hivi nyuma ya miaka makumi tatu na minane kulijaza roho yake na furaha!

Ajabu hili lilifanyikana siku ya **sabato,** siku ya saba ya juma. Wayuda hawakuwa na ruhusa kufanya kazi yo yote siku ya sabato. Mtu huyu alikuwa Myuda, lakini hakuogopa kubeba kitanda chake wakati alipoagizwa na Bwana Yesu kufanya hivi.

**B. Ushindani wa Wayuda (5:10-18)**

**5:10** Wakati **Wayuda** walipoona mtu huyu akibeba kitanda chake siku ya **sabato** walimwuliza kwa sababu gani alifanya hivi. Watu hawa waliweka roho kabisa kutii maagizo ya dini yao, hata pamoja na ukali, lakini mara nyingi wao wenyewe walikosa rehema na huruma kwa watu wengine.

**5:11** Jibu la mgonjwa aliyeponyeshwa halikuwa ngumu kufahamu. Alisema tu ya kwamba yule ambaye alimponyesha alimwagiza **kuchukua kitanda chake na kutembea.** Ingepasa kutii mtu ye yote anayeweza kuponyesha mwingine aliyekuwa na ugonjwa kwa miaka makumi tatu na minane, hata kama akiagiza mtu yule kubeba kitanda siku ya sabato! Mgonjwa aliyepona hakujua kwa wakati huu kwamba Bwana Yesu alikuwa nani, lakini alisema juu yake na roho ya asante kabisa.

**5:12** Wayuda walitaka sana kujua kama nani alikuwa na ukaramisu kusema na mtu huyu kuasi mafundisho yao juu ya sabato, hivi waliomba mgonjwa aliyepona awaonyeshe mtu mwenyewe. Sheria ya Musa iliagiza kwa mtu ye yote asiyeshika sabato kuuawa kwa njia ya kutupiwa mawe. Wayuda hawakuweka roho juu ya kuponyeshwa kwa mwenye kupooza.

**5:13** Mgonjwa **aliyeponyeshwa** hakujua kama nani alimponyesha. Hakuweza kumwonyesha kwa sababu **Yesu** alikuwa amejitenga na kundi la watu waliokuwa wamekutana.

Tangu wakati ule utumishi wa Bwana Yesu Kristo uligeuka. Kwa sababu alikuwa amefanya ajabu hili siku ya sabato aliamsha kasirani na machukio ya viongozi vya Wayuda. Walianza kumwinda na kujaribu kumwua.

**5:14** Nyuma ya maneno haya **Yesu alikuta** mtu aliyeponyeshwa **hekaluni**. Bila shaka alikuwa pale akishukuru Mungu kwa ajabu kubwa lililofanyikana ndani ya maisha yake. Bwana Yesu alimkumbusha kwamba kwa sababu alibarikiwa hivi alikuwa na lazima kubwa sasa. **"Angalia umekuwa mzima; usifanye zambi tena, neno baya zaidi lisikushike."** Ni kama mtu huyu alipatwa na ugonjwa wake kwa sababu ya zambi fulani aliyotenda. Si kila ugonjwa ulio tunda la zambi. Kuna watu wengi wenye ugonjwa usio tunda la zambi waliyofanya. Kwa mfano, mtoto mchanga anaweza kuwa mgonjwa mbele ya kuweza kuchagua kutenda zambi.

Yesu alisema, **"Usifanye zambi tena,"** akionyesha kipimo kikamilifu cha utakatifu wa Mungu. Kama angalisema, "kuanza sasa fanya zambi nusu tu," kama asingalikuwa Mungu. Mungu hawezi kukubali zambi yo yote. Halafu Yesu aliongeza onyo nyingine: **"neno baya zaidi lisikushike."** Bwana hakuonyesha kama neno lile baya litakuwa nini. Bila shaka alitaka mtu mwenyewe kufahamu kwamba tunda la zambi ni baya kupita ugonjwa wa mwili. Watu wanaokufa katika zambi zao watahukumiwa kwa gazabu na maumivu ya milele.

Kukosea neema ya Mungu ni zambi kubwa kupita kukosea sheria. Ingalikuwa vibaya sana kwa mtu huyu kuendelea ndani ya maisha yake ya zambi yaliyozaa ugonjwa wake mbele.

**5:15** Kama mwanamke wa Samaria, **mtu** huyu alitaka kupasha watu wengine juu ya Mwokozi wake. Aliwaambia Wayuda kwamba **alikuwa Yesu ambaye alimfanya kuwa mzima.** Alitaka kusifu Yesu, hata kama Wayuda hawakutaka kusikia sifa ile. Neno walilotaka zaidi lilikuwa kufunga Yesu na kumwazibu.

**5:16** Habari hizi zinaonyesha uovu mkubwa sana wa moyo wa mtu. Mwokozi alikuwa amefika na kufanya tendo kubwa kuponyesha mtu, na Wayuda hawa walikasirika sana sana kwa sababu alilitenda siku ya **sabato**. Wali-

weka roho juu ya kufuata dini yao na moyo baridi kuliko kutafuta baraka na heri ya wenzao. Hawakufahamu kwamba yule aliyesimamisha sabato zamani ndiye aliyefanya tendo la rehema siku ile. Bwana Yesu hakuasi sheria ya sabato. Sheria ilikataza watu kufanya kazi ya utumishi siku ile, lakini haikukataza watu kufanya matendo ya lazima na ya rehema.

**5:17** Wakati Mungu alipomaliza kazi ya kuumba dunia ndani ya siku sita, alistarehe siku ya saba. Hii ndiyo siku ya sabato. Lakini wakati zambi ilipoingia dunia raha ya Mungu iliharibiwa. Kuanza saa ile alitumika bila kuacha kurudisha wanaume na wanawake kwa ushirika naye. Atatengeneza njia kwa ukombozi wao. Atatangaza Habari Njema kwa kila kizazi. Hivi tangu Adamu alipofanya zambi kufika sasa, Mungu **anatumika kazi** bila kuacha**.** Ni vivyo hivyo na Bwana Yesu. Amefanya kazi ya Baba yake, na hakutumika kazi za mapendo na neema siku sita za juma tu.

**5:18** Hili ni shairi kubwa sana. Linatujulisha kwamba **Wayuda** walitaka hata kupita mbele **kuua** Bwana Yesu, **kwa sababu** pamoja na kuponyesha mtu siku ya **sabato** alisema vilevile kwamba yeye ni **hali moja na Mungu!** Walifikiri kwamba Bwana alikuwa ameasi sheria ya sabato, lakini neno hili halikuwa kweli. Hawakufahamu kwamba Mungu hakukusudi kamwe kwa sabato kuwa mzigo kwa watu. Kama ingewezekana kwa mtu kuponyeshwa toka ugonjwa wake siku ya sabato, Mungu hakuagiza alazimishwe kuteswa siku moja nyingine.

Wakati Yesu aliposema juu ya **Mungu** kama **Baba yake**, walifahamu kwamba alisema yeye ni **mmoja na Mungu.** Walifikiri ni ukufuru mbaya sana. Sivyo; ilikuwa kweli kabisa.

Bwana Yesu alitaka kwa haki kusema yeye ni mmoja na Mungu? Kama sivyo kama angalieleza neno hili kwa Wayuda. Lakini mashairi yanayofuata yanaonyesha hata wazi kupita kwamba yeye ni mmoja na Mungu. J. Sidlow Baxter alijumlisha neno hili hivi:

> Alionyesha kwamba yeye ni sawa na Mungu kwa njia saba:
>
> 1) Kwa njia ya kazi: "Yote anayofanya Baba, yule Mwana anafanya vilevile" (sh.19).
>
> 2) Kwa njia ya kujua: "Maana Baba anapenda Mwana, na anamwonyesha yote anayofanya yeye mwenyewe" (sh.20).
>
> 3) Kwa maneno ya kufufua: "Kama Baba anavyofufua wafu … hivi Mwana anaweka hai wale ambao anawataka" (sh. 21 pamoja na mash. 28 na 29).
>
> 4) Kwa maneno ya kuhukumu: "Maana Baba hamhukumu, hata mtu mmoja, lakini amempa Mwana hukumu yote" (sh. 22 pamoja na sh. 27).
>
> 5) Kwa njia ya heshima: "ili watu wote waheshimu Mwana kama wanavyoheshimu Baba" (sh. 23).
>
> 6) Kwa njia ya kuleta uzazi wa pili: "Yeye anayesikia neno langu na kumwamini yeye ambaye alinituma ana uzima wa milele … amepita kutoka mauti kuingia uzima" (mash. 24, 25).
>
> 7) Kwa njia ya kuwa mwenye uzima: "Maana kama Baba ana uzima ndani yake mwenyewe, vivyo hivyo alimpa Mwana kuwa na uzima ndani yake mwenyewe" (sh.26).[18]

### C. Yesu anasimamia kweli ya kuwa yeye ni sawa na Mungu (5:19-29)

**5:19** Mwokozi alikuwa mmoja kabisa na Mungu Baba hata hakuweza kutenda maneno peke yake. Si kusema kwamba hakuwa na uwezo kufanya neno yeye mwenyewe, lakini alifungana na Mungu karibu sana hata aliweza kufanya maneno yale tu ambayo aliona **Baba** akifanya. Hata kama Bwana alisema yeye ni sawa na Mungu, hakusema alitenda peke yake na kwa ruhusa yake mwenyewe.

Ni wazi ya kwamba Bwana Yesu ali-

taka Wayuda kufikiri yeye ni mmoja na Mungu. Ingalikuwa upumbavu kwa mtu wa dunia kusema anaweza kufanya maneno haya Mungu tu **anayofanya**. Yesu alisema kwamba aliona maneno ambayo Baba **anafanya**. Kwa kuweza kusema hivi alihitaji kuwa pamoja na Baba wakati wote na kujua maneno yaliyotokea mbinguni. Na zaidi ya ile Yesu anasema alifanya maneno a**nayoona Baba anafanya**. Maneno haya yote yanaonyesha kwamba alikuwa na umoja na Mungu na kwamba yeye ni mwenye uwezo wote.

**5:20** Kama alama ya mapendo ya Baba kwa Mwana wake **anamwonyesha yote anayofanya mwenyewe.** Yesu **hakuona** tu **maneno** haya; alikuwa na uwezo kuyafanya vilevile. Halafu Mwokozi aliendelea kusema ya kwamba Mungu **atamwonyesha maneno makubwa kupita haya**, ili watu **wa shangae**. Walikuwa wameona Bwana Yesu akifanya maajabu. Sasa tu walikuwa wamemwona akiponyesha mtu mwenye kupooza kwa miaka makumi tatu na minane. Lakini wataona maneno **makubwa kupita** yale. Ajabu la kwanza la namna hii litakuwa kufufua wafu (sh. 21). La pili litakuwa kazi ya kuhukumu watu (sh. 22).

**5:21** Hapa ni semo lingine lililo wazi ya kwamba Mwana na Baba ni sawasawa. Wayuda walishitaki Yesu juu ya kujifanya sawa na Mungu. Hakubisha mashitaki yale, lakini maneno yaliyoonyesha wazi ni ya kwamba yeye na Baba ni mmoja. **Kama Baba anavyofufua wafu na kuwaweka hai, hivi Mwana anawaweka hai wale ambao anawataka.** Isingaliwezekana kusema neno namna hii juu yake kama angalikuwa mtu tu.

**5:22** Agano Jipya linafundisha kwamba Mungu **Baba … amempa Mwana kazi yote ya hukumu.** Kwa Bwana Yesu kuweza kufanya kazi hii ni lazima kwa yeye kuwa mwenye haki kabisa na kujua maneno yote. Sharti atambue mafikiri na makusudi ndani ya mioyo ya watu. Ni neno la kushangaza kuwaza juu ya Mwamuzi wa dunia nzima akisimama mbele ya Wayuda hawa, akisimamia amri yake, lakini hata hivi hawakumtambua!

**5:23** Hapa tunaona kwa sababu gani Mungu alimpa Mwana wake amri kufufua wafu na kuhukumu ulimwengu. Alifanya hivi **ili watu wote waheshimu Mwana kama wanavyoheshimu Baba.** Hili ni neno kubwa sana, na moja la mashairi haya ndani ya Biblia yanayohakikisha wazi zaidi uungu wa Bwana Yesu Kristo. Ndani ya Biblia nzima tunajifunza kwamba inatupasa kuabudu Mungu tu. Amri Kumi zilikataza watu kuwa na mungu yo yote ila Mungu mmoja wa kweli. Tena sasa tunajifunza kwamba **inapasa wote kuheshimu Mwana kama wanavyoheshimu Baba.** Neno hili linaonyesha wazi sana ya kwamba Yesu Kristo ni Mungu.

Watu wengi wanasema wanaabudu Mungu, lakini wanakana kwamba Yesu Kristo ni Mungu. Wanasema alikuwa mtu mwema na alikuwa sawasawa na Mungu kupita mtu ye yote mwingine aliyeishi tangu zamani. Lakini shairi hili linaonyesha wazi kwamba yeye ni mmoja kabisa na Mungu, na linaagiza watu *kumheshimu na heshima wanayoonyeshea Mungu Baba.* Mtu **asiyeheshimu Mwana**, mtu huyu **haheshimu Baba vilevile**. Ni bure kwa mtu kusema anapenda Mungu bila kupenda Bwana Yesu Kristo vilevile. Kama usipofahamu bado kama Yesu Kristo ni nani, waza sana juu ya shairi hili. Kumbuka kwamba ni Neno la Mungu, na amini kweli hii ya ajabu ya kwamba Yesu Kristo ni Mungu aliyeonekana katika mwili.

**5:24** Ndani ya mashairi yaliyotangulia tulisoma ya kwamba Bwana Yesu alikuwa na uwezo kutoa uzima, na vilevile ya kwamba alipewa kazi ya

kuhukumu. Sasa tunajifunza namna gani mtu anaweza kupokea uzima huu wa roho toka kwake na kuepuka **hukumu**.

Hili ni moja la mashairi ya Habari Njema watu wanayopenda zaidi. Watu wengi sana wamepokea uzima wa milele nyuma ya, na kwa sababu ya kulisoma. Linaonyesha njia ya wokovu wazi sana. Bwana Yesu alilianza na masemo haya **"Kweli, kweli"** kufahamisha watu kwamba atasema neno kubwa sana. Halafu aliongeza, **"Ninawaambia ninyi."** Mwana wa Mungu anasema na sisi sote mmoja mmoja.

**"Yeye anayesikia neno langu."** Kusikia neno la Yesu si kusikiliza na masikio tu, lakini kulipokea, kuliamini, na kulitii. Watu wengi wanasikia Habari Njema ikihubiriwa, lakini hawafanyi kitu juu ya maneno waliyosikia. Bwana anasema hapa kwamba sharti mtu apokee mafundisho yake kama mafundisho kutoka kwa Mungu, na kuamini ya kwamba yeye ni kweli Mwokozi wa ulimwengu.

**"Na kumwamini yeye ambaye alinituma."** Ndiyo, ni kuamini Mungu. Maana yake ni ya kwamba mtu anaokolewa kwa njia ya kuamini Mungu tu? Watu wengi wanasema wanaamini Mungu, lakini hawakuokolewa. Sivyo. Tunajifunza hapa kwamba inapasa mtu kuamini Mungu aliyetuma Bwana Yesu Kristo duniani. Inampasa kuamini kwamba Mungu **alituma** Bwana Yesu kuwa Mwokozi wetu. Sharti aamini maneno Mungu anayosema juu ya Bwana Yesu, ndiyo ya kwamba yeye ni Mwokozi wa pekee, na ya kwamba zambi zinaweza kuondolewa tu kwa njia ya kazi yake kwa Kalvari.

**"Ana uzima wa milele."** Ona ya kwamba hatusomi kwamba atakuwa na uzima wa milele, lakini **ana** uzima ule sasa. **Uzima wa milele** ni uzima wa Bwana Yesu Kristo. Si uzima unaoendelea kwa milele tu, lakini namna nyingine ya uzima. Ni uzima wa Mwokozi tunaopokea wakati tunapomwamini. Ni uzima wa roho ambao mtu anapokea wakati anapozaliwa tena, mbali na uzima wa mwili aliopokea wakati wa kuzaliwa duniani.

**"Hafiki kwa hukumu."** Ni kusema hahukumiwi sasa na hatahukumiwa kamwe kwa wakati wa kuja. Mtu anayeamini Bwana Yesu **hahukumiwi,** kwa sababu Kristo alilipa azabu kwa zambi zake kwa Kalvari. Mungu hataki malipo mara mbili kwa azabu hii. Kristo ameilipa kama Mkombozi wetu na malipo haya yanatosha. Amemaliza kazi yenyewe, na haiwezekani kuongeza kitu kwa kazi iliyokwisha. Mkristo hataazibiwa kamwe kwa zambi zake.[4]

**"Lakini amepita kutoka mauti kuingia uzima."** Mtu aliyeamini Kristo **amepita toka mauti** ya roho **kuingia uzima** wa roho. Mbele ya kuokolewa alikuwa mfu katika zambi na makosa. Hakuwa na mapendo kwa Mungu wala upatano na Bwana Yesu. Wakati alipoamini Yesu Kristo, Roho ya Mungu alikuja kukaa ndani yake, naye alipewa uzima wa Mungu.

**5:25** Hapa ni mara ya tatu Bwana alisema **kweli kweli** ndani ya sura hii, na mara ya saba ndani ya Habari Njema hii kufika hapa. Wakati Bwana aliposema **saa inakuja, na iko sasa,** hakusema juu ya muda wa dakika makumi sita, lakini juu ya wakati alipokuja duniani.

**Wafu** tunaosoma habari zao ndani ya shairi hili ni nani? Wafu gani **watasikia sauti ya Mwana wa Mungu na kuwa hai?** Ni wale waliofufuliwa na Bwana wakati wa utumishi wake hapa duniani. Lakini zaidi ya hawa ni wale walio **wafu** katika zambi na makosa. **Wanasikia sauti ya Mwana wa Mungu** wakati Habari Njema inapohubiriwa. Wakati wanapokubali habari hizi na kupokea Mwokozi, wanapita toka mauti kuingia uzima.

Tukiamini kwamba shairi 25 linasema

juu ya maneno ya roho, si maneno ya mwili, tunaonyesha sasa kwa njia gani ni sawa, au mbalimbali na mashairi 28 na 29:

| *Sh.25* | *Mash. 28,29* |
|---|---|
| Uzima toka mauti | Uzima nyuma ya mauti |
| "Saa inakuja, na iko sasa" | "saa itakuja" |
| "wafu" | "wote walio katika makaburi" |
| "watakaposikia sauti" | "watasikia sauti yake" |
| "wale wanaosikia watakuwa hai" | "nao watatoka" |

**5:26** Shairi hili linaeleza namna gani mtu anaweza kupokea uzima toka Bwana Yesu**.** Kama **Baba** ana **uzima** na kuutoa, vivyo hivyo **alimpa Mwana kuwa na uzima ndani yake mwenyewe** ili aweze kutoa uzima kwa wengine. Shairi hili linaonyesha wazi tena uungu wa Kristo na umoja wake na Baba. Hakuna mtu aliye na uzima ndani yake mwenyewe. Sisi sote mmoja mmoja tulipewa uzima, lakini wala Baba wala Bwana Yesu walipewa uzima. Walikuwa na uzima ndani yao tangu milele. Uzima ule haukuwa na mwanzo kamwe. Haukutoka pahali po pote kamwe ila kwa Baba na Mwana.

**5:27** Mungu aliamuru kwa Mwana kuwa na uzima ndani yake mwenyewe. Zaidi ya ile Mungu **alimpa amri** vilevile kuwa Mwamuzi wa ulimwengu. Yesu alipewa amri hii kuhukumu **kwa sababu yeye ni Mwana wa watu.** Bwana ameitwa Mwana wa Mungu na **Mwana wa watu** vilevile. Jina hili *Mwana wa Mungu* linatukumbusha ya kwamba yeye ni mmoja na Mungu Baba na Mungu Roho Mtakatifu. Kama Mwana wa Mungu, yeye ni mmoja na Baba na Roho Mtakatifu, na kama Mwana wa Mungu anatoa uzima. Lakini yeye ni **Mwana wa watu** vilevile. Alifika duniani kama Mtu, aliishi katikati ya watu, na alikufa juu ya msalaba kama Mkombozi kwa wanaume na wanawake. Alikataliwa na kusulibishwa wakati alipofika duniani kama Mtu. Wakati atakapokuja tena atahukumu adui zake na ataheshimiwa ndani ya dunia ile ile pahali alipotendewa jeuri na kuteswa sana mbele. Kwa sababu yeye ni Mungu na Mtu, anawezeshwa kuwa Mwamuzi.

**5:28** Bila shaka Wayuda walishangaa sana wakati waliposikia Kristo akisema maneno haya kusimamia kweli ya kwamba yeye na Mungu Baba ni mmoja. Yesu alijua mawazo yao, hivi aliwaambia hapa kwamba **haifai washangae** juu ya maneno haya. Halafu aliendelea kuwafunulia kweli nyingine za kuwashangaza hata kupita. Kwa wakati wa kuja wote **wenye miili kaburini watasikia sauti yake**. Ingekuwa pumbavu kabisa kwa mtu ye yote asiye Mungu kutabiri kwamba miili kaburini itasikia sauti yake siku nyingine! Mungu tu aliweza kusema neno namna hii.

**5:29** Wafu wote watafufuliwa siku nyingine. Wengine watafufuliwa kwa ufufuo wa **uzima**, na wengine kwa **hukumu**. Kila mtu aliyeishi tangu mwanzo ni ndani ya moja la makundi haya mawili![4]

Shairi 29 *halifundishi* kwamba watu waliotenda mema wataokolewa kwa sababu ya matendo yao mema, na ya kwamba wenye kutenda mabaya watahukumiwa kwa sababu ya mwenendo wao mwovu. Mtu haokolewi kwa sababu ya kutenda mema, lakini anatenda mema kwa sababu ameokolewa. Matendo mema si msingi wa wokovu, lakini **matunda** yake. **Wale waliofanya mabaya** ndio wale wasioamini Bwana Yesu kamwe, na kwa sababu hii maisha yao ni maovu kwa macho ya Mungu. Watafufuliwa kusimama mbele ya Mungu kwa hukumu ya azabu kwa milele.

### D. Washuhuda wane kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu (5:30-47)

**5:30** Wakati tunaposoma, **"Mimi siwezi kufanya neno peke yangu mwenyewe"** labda tunafikiri kwanza kwamba Bwana Yesu hana uwezo kufanya neno lo lote peke yake. Neno hili si kweli. Maana ya maneno haya ni ya kwamba yeye na

Mungu Baba ni mmoja kabisa hata Mwana hakuweza kutenda peke yake. Hakuweza kufanya neno kwa amri yake mwenyewe tu. Hakuwa na roho ya ukaidi hata kidogo, lakini alifanya maneno yote na ushirika na upatano mkamilifu na Baba yake.

Walimu wa uwongo wametumika na shairi hili mara nyingi kuonyesha kwamba Yesu Kristo hakuwa Mungu. Wanasema kwa sababu hakuweza kufanya neno lo lote peke yake mwenyewe alikuwa mtu tu. Lakini shairi hili halihakikishi neno hili hata kidogo. Watu wanafanya mapenzi yao wenyewe bila kufikiri kwamba ni mapenzi ya Mungu au sivyo. Lakini Yesu hakutenda hivi kwa sababu yeye ni Mwana wa Mungu. Angaliweza kutenda hivi kwa njia ya *mwili*, lakini si kwa njia ya *roho* hata kidogo. Kwa nguvu ya *mwili wake* aliweza kufanya maneno yote, lakini *kwa roho* hakuweza kufanya neno baya; na ingalikuwa vibaya kwaye kufanya neno lo lote lisilokuwa mapenzi ya Mungu Baba kwa yeye. Semo hili linaweka Bwana Yesu mbali na mtu ye yote aliyeishi tangu zamani.

Kama Bwana Yesu alivyosikiliza Baba yake na kufundishwa naye kila siku, vivyo hivyo alifikiri, alifundisha na kutenda. Neno hili **hukumu** hapa halina maana ya kuhukumu maneno kwa njia ya sheria, lakini ni kwa yeye kufahamu nini ni taratibu kwaye kufanya na kusema.

Hivi kwa sababu Mwokozi hakufikiri faida yake mwenyewe aliweza kuhukumu maneno kwa haki na bila upendeleo. Aliweka roho juu ya neno moja tu, ndilo kupendeza Baba yake na kufanya kutaka kwake. Mara nyingi maneno ambayo sisi tunataka kufanya na kuamini yanaongoza mawazo yetu na mafundisho yetu. Haikuwa hivi na Mwana wa Mungu. Hakufikiri faida yake mwenyewe, na hukumu zake zilikuwa bila upendeleo.

**5:31** Ndani ya baki la sura hii Bwana Yesu alipasha juu ya ushuhuda wa wengine wa uungu wake: ushuhuda wa Yoane Mbatizaji (mash. 32-35); ushuhuda wa kazi zake (sh.36); ushuhuda wa Baba (mash.37, 38); ushuhuda wa Maandiko ya Agano la Kale (mash. 39-47).

Alianza na kusema juu ya kutoa ushuhuda. Alisema, **"Kama nikijishuhudia mimi mwenyewe, ushuhuda wangu si kweli."** Maana ya masemo yake haiko kwamba aliweza kusema wakati wo wote neno lisilo kweli. Alionyesha tu ya kwamba ushuhuda wa mtu mmoja peke yake hautoshi mbele ya mwamuzi. Mungu alikuwa ameamuru kwamba sharti washuhuda wawe wawili au watatu. Hivi Bwana Yesu atataja sasa washuhuda, si wawili au watatu tu, lakini wane kushuhudia uungu wake.

**5:32** Watu wengine wanafikiri shairi hili linasema juu ya Yoane Mbatizaji, wengine wanafikiri linasema juu ya Mungu Baba, au Roho Mtakatifu. Sisi tunaamini linasema juu ya **ushuhuda** wa Mungu Baba.

**5:33** Nyuma ya kusema juu ya Mshuhuda mkubwa zaidi, ndiye Baba yake, Bwana alisema tena juu ya ushuhuda wa **Yoane**. Alikumbusha Wayuda wasioamini kwamba walikuwa **wametuma watu** karibu na **Yoane** kusikia masemo yake, na ya kwamba ushuhuda wake ulikuwa juu ya Bwana Yesu Kristo tu. Yoane hakusema juu yake mwenyewe lakini aliwaongoza kufikiri Mwokozi. **Alishuhudia** Yule aliye **kweli.**

**5:34** Bwana Yesu alikumbusha wasikiaji wake kwamba hakusema yeye ni sawasawa na Mungu kwa sababu ya **ushuhuda** wa watu tu, ndio ushuhuda zaifu. Alisema hapa juu ya ushuhuda wa Yoane Mbatizaji kwa sababu alikuwa mtu aliyetumwa na Mungu, na kwa sababu ya ushuhuda wake kwamba Bwana Yesu alikuwa kweli Masiya na

Mwana-kondoo wa Mungu anayechukua zambi ya ulimwengu.

Halafu aliongeza kusema, **“Lakini ninasema maneno haya ili ninyi mupate kuokolewa.”** Kwa sababu gani Bwana Yesu alisema maneno mengi hivi na Wayuda? Alitaka kuhakikisha tu kwamba alisema haki lakini wao walianguka? Sivyo; aliwajulisha kweli hizi za ajabu ili waweze kutambua kama yeye ni nani na kumpokea kama Mwokozi ambaye Mungu aliahidi kutuma. Shairi hili linatuonyeshea roho ya mapendo na huruma ya Bwana Yesu. Alisema na wale ambao walimchukia na watajaribu kumwua nyuma kidogo. Hakuwachukia hata kidogo. Aliweza kuwapenda tu.

**5:35** Hapa Bwana alisifu Yoane Mbatizaji akimwita **taa inayowaka na kuangaza,** maana yake alikuwa mwenye bidii sana, mwenye kazi inayoleta **nuru** kwa watu wengine, na mwenye kujitoa kabisa kwa kazi ya kuonyeshea watu njia kufika kwa Yesu. Wakati Yoane alipoanza kuhubiri, Wayuda wengi walifika kusikiliza mtu huyu aliyeonekana namna nyingine. Walimpokea kama mwalimu mzuri wa dini **kwa wakati**.

Kwa sababu gani, nyuma ya kupokea Yoane vizuri, hawakupokea yule Yoane alihubiri habari zake? Walifurahi kwa muda mdogo, lakini hawakuwa na toba ya kweli. Walipokea mtangulizi, lakini walikataa kupokea Mfalme mwenyewe! Yesu alisifu Yoane sana. Kwa mtumishi ye yote ya Kristo kuitwa **taa inayowaka na kuangaza** ni sifa ya kweli toka Mwana wa Mungu. Vizuri sisi sote tunaopenda Bwana Yesu tuwe na hamu vilevile kuwa taa za kuwaka kwa Yeye, tukijitoa kabisa kuleta nuru kwa dunia.

**5:36** Lakini kulikuwa na ushuhuda mkubwa kupita ule **wa Yoane**. Maajabu ambayo Mungu Baba alimpa kufanya **yalishuhudu** kwamba **alitumwa** kweli na **Baba.** Maajabu hayahakikishi uungu wa mwenye kuyatenda kila mara. Ndani ya Biblia tunasoma juu ya watu waliopewa uwezo kufanya maajabu, na tunasoma vilevile juu ya viumbe viovu vyenye uwezo kutenda maneno yasiyowezekana kwa watu. Lakini maajabu ya Bwana Yesu yalikuwa namna nyingine na maajabu haya. Tuone kwanza ya kwamba alikuwa na uwezo *ndani yake mwenyewe* kutenda kazi hizi kubwa za uwezo, lakini wengine *walipewa* uwezo huu. Watu wengine waliweza kufanya maajabu lakini hawakuweza kupitisha uwezo huu kwa watu wengine. Bwana Yesu alifanya maajabu yeye mwenyewe, na zaidi ya ile aliwapa mitume yake amri kufanya vivyo. Na vilevile Mwokozi alifanya **maajabu** yale yale yaliyotabiriwa katika Agano la Kale kwamba Masiya atayafanya. Mwishoni, maajabu aliyofanya yalikuwa namna nyingine, makubwa kupita, na mengi kupita.

**5:37, 38** Bwana alisema tena ya kwamba **Baba** alimshuhudia. Labda neno hili lilikuwa kwa wakati wa ubatizo wake. Saa ile sauti ya Mungu Baba ilisikiwa toka mbinguni ikisema kwamba Yesu alikuwa Mwana wake mpendwa aliyependezwa naye. Na tukumbuke ya kwamba ndani ya maisha na utumishi mzima wa Bwana Yesu Baba alitoa ushuhuda tena na tena kwamba alikuwa Mwana wa Mungu mwenyewe.

Wayuda wasioamini **hawakusikia sauti** ya Mungu **wakati wo wote, wala kuona sura yake** kwa sababu **hawakulinda neno lake** ndani yao. Mungu anasema na watu kwa njia ya Neno lake, ndiyo Biblia. Wayuda hawa walikuwa na Maandiko ya Agano la Kale, lakini hawakumpa Mungu njia kusema nao kwa njia ya Maandiko. Mioyo yao ilikuwa migumu na masikio yao ilikuwa mazito na hawakusikia vizuri.

Hawakuona Mungu kamwe kwa sababu **hawakuamini** yeye **aliyetumwa naye**. Mungu Baba hana mwili ambao sisi watu tunaweza kuona. Yeye ni Roho

na hatuwezi kumwona. Lakini Mungu alijifunua kwa watu ndani ya Bwana Yesu Kristo. Wale walioamini Kristo waliona sura ya Mungu. Kwa macho ya wasioamini alikuwa sawasawa na watu wengine tu.

**5:39** Tunaweza kufahamu sehemu ya kwanza ya shairi hili kwa njia mbili. Labda Bwana Yesu alikuwa akisema na Wayuda **kutafuta Maandiko**. Au labda alisema ya kwamba Wayuda **walitafuta maandiko** kwa sababu walifikiri kwamba kwa njia ya kuwa na maandiko walikuwa na **uzima wa milele.** Ni kama Bwana Yesu alisema tu kwamba Wayuda walitafuta **Maandiko** na kufikiri ya kuwa kwa njia ya kufanya hivi walipokea **uzima wa milele.** Hawakufahamu kwamba Maandiko ya Agano la Kale yaliyopasha habari za Masiya atakayekuja yalisema juu ya Yesu. Ni neno la kuogofya kukumbuka ya kwamba watu wanaoshika Maandiko mikononi mwao waliweza kuwa wapofu kabisa. Na neno baya zaidi ni kufikiri Bwana Yesu alikuwa akisema nao kwa njia hii, lakini hata hivi walikataa kumpokea. Ona mwisho wa shairi hili: **"yananishuhudia."** Maneno haya yanaonyesha wazi kwamba habari kubwa za Agano la Kale zilikuwa kuja kwa Kristo.

**5:40** Wayuda **hawakutaka kuja** kwa Kristo **kupata uzima**. Kwa nini? Si kwa sababu iliwashinda kufahamu Habari Njema au iliwashinda kuamini Yesu. Hakuna neno ndani ya Bwana Yesu kuwazuiza kumwamini. Ni kutaka kwa mtu mwenyewe ambako kunamzuiza. Anapenda zambi zake kupita Mwokozi. Hataki kuachana na zambi zake.

**5:41** Wakati Bwana alipohamakia Wayuda kwa sababu walikataa kumpokea, hakutaka wafikiri kwamba alihuzunishwa rohoni kwa sababu **hawakumheshimu**. Hakufika duniani kupokea sifa toka **watu** wa dunia hii. Hakutegemea sifa yao lakini sifa ya Baba yake. Kukataliwa na watu hakupunguza utukufu wake.

**5:42** Kwa sababu gani watu hawakupokea Mwana wa Mungu? Kwa sababu **hawakuwa na mapendo ya Mungu ndani yao**, maana walijipenda wenyewe kupita Mungu. Kama wangalipenda Mungu, wangalipokea Yule aliyetumwa na Mungu. Kwa njia ya kukataa Bwana Yesu walionyesha wazi kwamba **hawakupenda** Baba yake hata kidogo.

**5:43** Bwana Yesu alikuja **kwa jina la Baba yake**, maana alikuja kufanya mapenzi yake, kutukuza Baba yake, na kutii Baba yake kwa maneno yote. Kama watu wangalipenda Mungu kweli, wangalimpenda yeye aliyejaribu kupendeza Mungu ndani ya maneno yote aliyosema na kufanya.

Halafu Yesu alitabiri kwamba **mwingine atakuja kwa jina lake mwenyewe** na Wayuda **watampokea.** Labda alifikiri juu ya walimu wengi wa uwongo waliotokea nyuma yake na waliotaka kuheshimiwa na taifa la Wayuda. Au labda aliwaza juu ya viongozi vya dini za uwongo watakaotokea nyuma na kusema wao ndio Kristo. Tunafikiri zaidi alisema juu ya mpinga Kristo. Wakati wa kuja mtawala atajisimamisha katikati ya Wayuda na kuwaagiza kumwabudu kama Mungu (2 Tes. 2:8-10). Zaidi ya Wayuda watapokea mpinga Kristo huyu kama mtawala wao, na watahukumiwa na Mungu (1 Yn. 2:18).

**5:44** Halafu Bwana alionyesha neno lingine kwa sababu yake Wayuda hawakumpokea. Waliweka roho juu ya kukubaliwa na wenzao kupita juu ya ukubali wa Mungu. Waliogopa maneno ambayo rafiki zao watasema kama wakiacha dini ya Wayuda. Hawakukubali kupokea laumu na mateso watakayopata kama wakigeuka wafuata wa Bwana Yesu. Mtu akikaa kuogopa maneno watu wengine watakayosema au kufanya,

hawezi kuokolewa. Mtu akitaka kuamini Bwana Yesu Kristo, inampasa kutaka ukubali wa Mungu kupita ukubali wa mtu ye yote. Lazima inampasa kutafuta **utukufu ule unaotoka kwa Mungu aliye wa pekee.**

**5:45** Bwana Yesu **hatahitaji kushitaki** Wayuda **kwa Baba.** Ndiyo, aliweza kuwashitaki juu ya maneno mengi lakini hakuhitaji kufanya hivi kwa sababu maandiko ya **Musa** yalitosha kwa mashitaki haya. Wayuda walijisifu sana juu ya Agano la Kale na zaidi juu ya vitabu vitano vilivyoandikwa na **Musa,** vilivyoitwa Tora. Walijisifu kwa sababu vitabu hivi vililetwa kwa Israeli. Lakini shairi 46 linaonyesha kwamba hawakutii maandiko ya Musa.

**5:46** Kwa mafikiri ya Bwana Yesu maandiko ya Musa yalikuwa na amri ya kipimo kimoja na masemo yake mwenyewe. Tukumbuke kwamba "Kila andiko limepewa kwa maongozi ya Mungu" (2 Tim. 3:16). Si neno kama tukisoma Agano Jipya au Agano la Kale, tunasoma Neno la Mungu. Kama Wayuda **wangaliamini** maneno ya **Musa,** wangaliamini Bwana Yesu Kristo vilevile kwa sababu Musa **aliandika juu ya** kuja kwa Kristo. Kwa mfano soma Tor. 18:15,18:

> BWANA Mungu wako atakusimamishia nabii toka katikati yako, mmoja wa ndugu zako, sawasawa nami; mumsikilize yeye; … Nitawasimamishia nabii toka katikati ya ndugu zao sawasawa nawe; na nitatia maneno yangu kinywani mwake, naye atawaambia yote ambayo nitamwagiza.

Ndani ya mashairi haya Musa alitabiri kuja kwa Kristo, na alisema na Wayuda kumsikiliza na kumtii wakati atakapofika. Sasa Bwana Yesu alikuja, lakini Wayuda hawakumpokea. Hivi alisema Musa atawashitaki kwa Baba kwa sababu walisema waliamini Musa lakini hawakufanya maneno Musa aliyoagiza. Maneno haya ya Yesu, **yeye aliandika habari zangu,** yanaonyesha wazi kwamba kuna unabii juu ya Bwana Yesu ndani ya Agano la Kale.

**5:47 Kama** Wayuda wasipoamini **maandiko** ya Musa, hawataamini **masemo** ya Yesu vilevile. Agano la Kale na Agano Jipya yanafungana pamoja. Mtu akiwa na shaka kwamba Agano la Kale limeandikwa kwa maongozi ya Mungu, hatapokea masemo ya Yesu kama Neno la Mungu vilevile. Watu wakiwa na shaka juu ya sehemu fulani ya Biblia, nyuma kidogo watakuwa na shaka juu ya Biblia nzima.

## 6. MWAKA WA TATU WA UTUMISHI WA MWANA WA MUNGU: GALILAYA (Sura 6)

### A. Alama ya ine: Kulisha watu elfu tano (6:1-15)

**6:1 Nyuma ya maneno haya –** maneno haya yanaonyesha kwamba muda fulani ulikuwa umepita tangu habari tulizosoma ndani ya sura 5. Hatujui urefu wa muda huu, lakini tunajua ya kwamba ndani yake **Yesu** alisafiri toka inchi karibu na Yerusalema kufikia bahari ya Galilaya. Tunafikiri kwamba maana ya kwenda ngambo ya bahari ni kwamba alikwenda toka pwani ya upande wa kaskazini-mangaribi wa bahari hata pwani wa kaskazini-mashariki. **Bahari ya Galilaya** iliitwa **Bahari ya Tiberia** vilevile kwa sababu mji wa Tiberia ulikuwa kwa pwani wake wa mangaribi. Mji huu ulikuwa mji mkubwa wa wilaya ya Galilaya na ulipata jina lake toka Tiberio, mfalme wa Waroma.

**6:2, 3** Makutano **makubwa yalimfuata,** si kwa sababu waliamini kwamba yeye ni Mwana wa Mungu, lakini **kwa sababu waliona** alama alizofanyia **wagonjwa**. Mungu hapendezwi sana kama imani ya watu inategemea alama. Anataka zaidi imani ya watu kutegemea Neno

lake tu. Alama hazihitajiwi kuhakikisha Neno la Mungu. Neno lo lote Mungu analosema ni kweli. Hakuna uwongo ndani yake.

**6:4** Hatujui kwa sababu gani Yoane alisema hapa kwamba **Pasaka ilikuwa karibu.** Labda alifikiri juu ya Pasaka saa Bwana Yesu alipotoa hotuba yake nzuri sana tunayosoma ndani ya sura hii juu ya Mkate wa kweli wa Uzima. Hakufikia Yerusalema kwa Pasaka. Yoane aliita **Pasaka karamu ya Wayuda.** Mungu alikuwa amesimamisha Pasaka katika Agano la Kale kwa Wayuda, na kwa sababu hii ilikuwa **karamu ya Wayuda**. Lakini labda maana ya **karamu ya Wayuda** ni kwamba Mungu hakuihesabu kuwa moja za karamu zake, kwa sababu Wayuda waliishika kama desturi tu bila kukumbuka maana yake ya kweli. Hivi haikuwa tena moja ya karamu za Yehova.

**6:5** **Yesu** hakukasirika wakati alipoona **makutano makubwa** wakikaribia, na kufikiri wataharibu ustarehe wake au saa yake kushinda pamoja na wanafunzi wake. Wazo lake la kwanza lilikuwa kuwapatia **chakula**. Hivi aligeuka kwa **Filipo** na kuuliza pahali gani watakapoweza kununua **mikate** kulisha watu hawa wote. Wakati Yesu alipouliza neno, hakufanya hivi kwa sababu yeye mwenyewe hakujua jibu lenyewe. Kusudi la ulizo lake lilikuwa kufundisha watu. Alijua jibu la ulizo hili, lakini Filipo hakujua.

**6:6** Bwana alitaka kufundisha Filipo neno kubwa na **kujaribu** imani yake. **Yeye mwenyewe alijua** atafanya ajabu kulisha makutano haya makubwa. Lakini Filipo alifahamu kwamba ataweza kufanya hivi? Alikuwa na imani kubwa au ndogo?

**6:7** Ni kama imani ya Filipo haikuwa kubwa sana. Alifanya hesabu mbio, akafahamu kwamba hata **dinari mia mbili** hazitatosha kununua **mkate** wa kutosha kumpa kila mtu hata **chakula nusu** tu. Hatujui kama mikate mingapi iliweza kununuliwa kwa **dinari mia mbili** kwa wakati ule, lakini bila shaka ilikuwa mikate mingi sana. Mshahara wa mtu wa kazi kwa siku moja ulikuwa dinari moja.

**6:8,9** **Anderea** alikuwa **ndugu ya Simoni Petro.** Walikaa karibu na Betesaida, kwa pwani ya Bahari ya Galilaya. Anderea vilevile alifikiri itakuwa nguvu kulisha makutano makubwa namna hii. Aliona mtoto mdogo mmoja mwenye **mikate mitano ya shayiri na samaki wadogo wawili**, lakini alifikiri si faida kujaribu kulisha **watu wengi kama hawa** na vyakula hivi vidogo. **Kijana** huyu alikuwa na chakula nusu tu, lakini alikuwa tayari kumpa Bwana atumike nacho. Kwa sababu ya roho yake tayari kutenda mema, habari zake ziliandikwa ndani ya vitabu vine vya Habari Njema. Alifanya neno dogo tu, lakini Mungu aliweza kufanya kazi kubwa nalo, na habari za kazi hii zimejulikana pahali pote duniani.

**6:10** Bwana alichagua pahali pazuri, pahali pa **majani mengi,** na kuagiza watu wakalishwe. Pahali pa majani mengi palikuwa pachache tu kwa upande ule wa inchi, lakini Bwana alitaka makutano kuweza kula kwa pahali pazuri na safi.

Iliandikwa kwamba kulikuwa na elfu za **wanaume** pale, hivi tunafahamu kulikuwa na wanawake na watoto vilevile. Hesabu ile **elfu tano** ilionyesha kwamba kufanyika kwa ajabu kubwa kulikuwa karibu.

**6:11** **Yesu akatwaa mikate, akashukuru.** Kama yeye alifanya hivi mbele ya kula au kupitisha vyakula kwa watu, kuzidi sana inatupasa sisi kushukuru Mungu mbele ya kula chakula. Kisha ali**gawia wanafunzi** chakula hiki. Kuna mafundisho makubwa hapa kwa sisi. Bwana Yesu hakufanya kazi hii yote peke yake. Aliomba watu kumsaidia ndani yake.

Wakati Bwana **alipogawia wanafunzi** mkate, ulikuwa umeongezeka sana kwa njia ya ajabu, na mikate ile mitano na samaki mbili ndogo ilitosha kulisha

makutano yale makubwa. Wanafunzi walipitapita katikati ya wale walioketi. Vyakula vilitosha kabisa kwa sababu tunasoma ya kwamba aliwapa samaki **kwa kadiri walivyotaka**.

Griffith Thomas ametukumbusha kwamba habari hizi ni mfano mzuri sana wa:

> a) dunia hii inayopotea; b) wanafunzi waliokosa uwezo; c) Mwokozi mkamilifu. Ajabu hili lilikuwa ajabu la kuumba. Hakuna mtu wa dunia anayeweza kukamata mikate mitano na samaki ndogo mbili na kuzizidisha kulisha watu wengi hivi.

**6:12** Waza juu ya shairi hili tamu. Kama Yesu angalikuwa mtu tu, kama asingaliweka roho juu ya **vipande** vilivyobaki. Mtu akiweza kukulisha watu elfu tano haweki roho juu ya mavunjiko nusu! Lakini Yesu ni Mungu, naye hataki vitu vya damani ambavyo anatupa sisi kupotea bure. Hivi alitoa agizo wakusanye vipande vya vyakula vilivyobaki kusudi **kitu cho chote kisipotee.**

Watu wengi wanajaribu kueleza ajabu hili. Wanasema wakati makutano walipoona kijana mdogo akitolea Yesu mikate yake mitano na samaki ndogo mbili, zamiri zao ziliwashitaki juu ya kujifikiri wenyewe tu, hivi walifungua vyakula ambavyo walikuwa navyo na kuvishiriki na watu wengine. Kwa njia hii kulikuwa na vyakula vya kutosha mahitaji ya watu wote. Lakini maelezo namna hii hayapatani na maneno yaliyotokea, kama tutaona ndani ya shairi 13.

**6:13 Vitunga kumi na viwili** vilijazwa na vipande vya mikate mitano wakati watu walipomaliza kula. Isingaliwezekana kukusanya vyakula vingi hivi kama kila mtu alikula tu chakula ambacho yeye alileta. Maelezo ya watu ni neno la kuchekesha tu. Kuna elezo moja tu la kweli, ndilo hili: Ajabu kubwa la uwezo lilikuwa limefanyika.

**6:14** Watu wenyewe walitambua ya kwamba lilikuwa ajabu. Hawakuweza kufanya hivi kama wangalikula vyakula vyao wenyewe tu. Walifahamu kwamba lilikuwa ajabu na walikuwa tayari kukiri kwamba Yesu ni **nabii yule ambaye atakuja katika dunia.** Kwa njia ya Agano la Kale walijua kwamba nabii atakuja, na walimtazamia kuwafungua toka utawala wa Waroma. Walikuwa wakingojea mtawala wa dunia, lakini hawakuwa na imani ya kweli. Hawakukubali kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu wala kukiri zambi zao na kumpokea kuwa Mwokozi wao.

**6:15** Kwa sababu ya ajabu hili, watu walitaka kuchukua Yesu **wamfanye mfalme.** Kama Yesu angalikuwa mtu tu, kama bila shaka angalikubali. Watu wanapenda sana kutukuzwa na kupewa pahali pa heshima. Lakini Yesu hakuwa na kiburi. Alijua alifika duniani kuwa Mkombozi kwa wenye zambi msalabani. Hatafanya neno lo lote lililoweza kumzuiza asitimize shauri hili. Mbele ya kutawala kama mfalme ilimpasa kuteswa, kutoa damu yake, na kufa kama sadaka kwa zambi zetu. Kisha ataweza kutukuzwa.

### B. Alama ya tano: Yesu anatembea juu ya maji na anaponyesha wanafunzi wake (6:16-21)

**6:16, 17** Ilikuwa **mangaribi**. Yesu alikuwa amekwenda kwa kilima peke yake. Bila shaka makutano walikuwa wamerudia nyumba zao, wakiacha wanafunzi peke yao. Halafu wanafunzi wali**telemuka hata bahari** na kujitayarisha kwa safari yao ya kuvuka bahari ya Galilaya.

**Usiku ulikuwa umeingia wakati walipokuwa wakivuka bahari kwenda Kapernaumu** na **Bwana Yesu hakuwa pamoja nao.** Alikuwa wapi? Alikuwa juu ya kilima akiomba. Ni mfano wa wafuata wa Kristo kwa wakati wa sasa. Maisha ya sasa ni kama tufani na **giza**. Hawawezi kuona Bwana Yesu na macho. Hata hivi anajua maneno yanayotokea. Yeye ni mbinguni akiombea wale ambao anapenda.

**6:18** Wakati na wakati upepo unashuka bonde la Yorodani mbio, na saa unapofikia bahari ya Galilaya unaleta mawimbi makubwa sana. Ni hatari kwa vyombo vidogo kuwa **baharini** kwa wakati ule.

**6:19** Ni kama wanafunzi walikuwa wamevuta makasia kwa karibu kilomètres tano. Walikuwa katika hatari kubwa wakati waliponyanyua macho, na **waliona Yesu akitembea juu ya bahari na kukaribia chombo**. Hili lilikuwa ajabu kubwa lingine la kushangaza. Mwana wa Mungu alikuwa akitembea juu ya maji ya bahari ya Galilaya. **Wanafunzi waliogopa** kwa sababu hawakufahamu kabisa kama Bwana alikuwa nani.

Ona ya kwamba Yoane hakutumika na masemo makubwa ya elimu kutujulisha habari za ajabu hili kubwa.

**6:20** Halafu Bwana aliwafariji na masemo haya matamu sana, **"Ni mimi, musiogope."** Kama angalikuwa mtu tu wangaliweza kuwa na woga. Lakini yeye ni Mwumba anayetegemeza ulimwengu, hivi hawakuhitaji kuogopa. Yeye aliyefanya bahari ya Galilaya aliweza kutuliza maji yake vilevile, na kufikisha wanafunzi wake wenye woga kwa pwani na salama. "Ni mimi." Hii ni mara ya pili ndani ya Habari Njema ya Yoane Bwana Yesu aliyosema maneno haya. Maana yao kabisa ni "MIMI NIKO". Ni jina la Yehova; na Bwana Yesu alijiita na jina hili hapa.

**6:21** Wakati walipofahamu kwamba alikuwa Bwana Yesu, **walimpokea katika chombo**, na **mara moja** chombo kilifika pahali walipokwenda. Lilikuwa ajabu lingine. Hawakuhitaji kukaa kuvuta makasia tena. Bwana Yesu aliwafikisha kwa **inchi kavu** mara moja. Ni Bwana wa ajabu kabisa!

### C. Watu wanaomba kuona alama (6:22-34)

**6:22** Siku moja ilipita tangu siku watu elfu tano walipokulishwa. Makutano ya **watu** walikuwa kwanza kwa upande wa kaskazini-mashariki wa bahari ya Galilaya. Walikuwa wameona wanafunzi wakiingia **chombo** kidogo mangaribi iliyopita, na walijua kwamba **Yesu hakwenda** pamoja nao. Kulikuwa na chombo kimoja tu pale, ndicho chombo ambacho **wanafunzi** waliingia.

**6:23** Kesho yake vyombo vilikuwa vimefika **toka Tiberia, karibu na pahali** Bwana Yesu alipokulisha makutano. Lakini haikuwezekana kwa Bwana kuondoka ndani ya kimoja cha vyombo hivi kwa sababu vilikuwa vimefika sasa tu. Labda makutano walivuka kwenda Kapernaumu ndani ya vyombo hivi, kama tunavyosoma ndani ya mashairi yanayofuata.

**6:24 Watu** walikuwa wameangalia karibu karibu maneno ambayo Yesu alifanya. Walijua amekwenda kilimani kuomba. Walijua kwamba hakuvuka bahari pamoja na wanafunzi ndani ya chombo chao. Tena kesho yake hakuonekana pahali po pote. Hivi walivuka bahari kwenda **Kapernaumu**, pahali walipofikiri wanafunzi wake watakuwa. Hawakufahamu namna gani ingewezekana kwa **Yesu** kuwa pale, lakini walifanya shauri kwenda hata hivi na kumtafuta.

**6:25,26** Basi walikwenda Kapernaumu, **wakamkuta** pale. Wakishangaa sana walimwuliza **saa gani** alifika.

**Yesu hakujibu** ulizo lao **waziwazi**. Alifahamu kwamba hawakumtafuta kwa sababu yake mwenyewe, lakini kwa sababu ya vyakula ambavyo aliwapa. Walikuwa wamemwona akifanya ajabu kubwa sana siku iliyopita. Neno hili lingalipasa kuwaaminisha kwamba yeye ndiye Mwumba na Masiya. Lakini walifikiri juu ya vyakula tu. Walikuwa wamekula **mikate** na kushiba.

**6:27** Hivi Yesu aliwaonya kwanza **wasifanye kazi kwa chakula chenye**

**kuharibika.** Hakusema maneno haya juu ya chakula walichohitaji kwa mahitaji yao ya kila siku, lakini aliwaonya wasiweke maneno haya kwanza. Kushibisha njaa ya mwili si kitu kikubwa kupita vyote. Mtu si mwili tu, lakini roho na nafsi vilevile. Inampasa kufanya kazi **kwa chakula kinachodumu hata uzima wa milele.** Haifai kutumika na nguvu na zawadi zake zote kushibisha mwili utakaokuliwa na funza nyuma ya miaka michache. Lazima aweke roho kulisha roho yake kila siku na Neno la Mungu. "Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno linalotoka katika kinywa cha Mungu." (Mt. 4:4) Sharti tutumike na bidii kujifunza Neno la Mungu kupita.

Wakati Bwana Yesu aliposema kwamba **Mungu Baba alimtia mhuri**, alitaka kusema **Mungu** alimtuma na kumkubali. Wakati sisi tunapotia neno lo lote mhuri, ni kusema tunaahidi kwamba neno lenyewe ni kweli. Mungu alitia Mwana wa watu mhuri, maana kuonyesha kwamba alikuwa mwenye kusema kweli.

**6:28** Halafu watu waliuliza Bwana kama iliwapasa kufanya nini ili waweze **kufanya kazi za Mungu**. Ni desturi ya watu kujaribu kutumika kazi kwa kuweza kufika mbinguni. Mtu anataka kufanya kitu kumstahilisha kupokea wokovu. Kama akiwa na njia kufanya kitu kwa wokovu wake, neno hili lingalimpa njia kujisifu; ndilo neno analopenda sana kufanya.

**6:29** Yesu alitambua hila yao. Walitenda kama wenye kutaka kutumikia Mungu, lakini hawakutaka kuwa na upatano na Mwana wa Mungu. **Yesu** aliwaambia kwamba neno la kwanza ambalo inawapasa kufanya ni kupokea Yule ambaye Mungu **alituma.** Ni vivyo hivyo leo. Watu wengi wanajaribu kufika mbinguni kwa njia ya kutenda kazi njema. Lakini mbele ya kuweza kufanya kazi njema sharti **waamini** Bwana Yesu Kristo. Kazi njema hazitangulii wokovu; ni tunda la wokovu. **Kazi** njema ya pekee mwenye zambi anayoweza kufanya ni kukiri zambi zake na kupokea Kristo kama Bwana na Mwokozi wake.

**6:30** Shairi hili linaonyesha tena uovu wa mioyo ya watu. Siku moja tu ilipita tangu walipoona Bwana Yesu akikulisha watu elfu tano na mikate mitano na samaki wawili. Sasa, siku moja tu tangu alipofanya ajabu hili kubwa, walifika kwake na kumwomba kuwaonyeshea **alama** kuhakikisha kwamba yeye ni kweli Mwana wa Mungu. Kama zaidi ya wasioamini, walitaka kuona kwanza na walisema wataamini nyuma. **"Tuone, na tukuamini."** Lakini hii si kawaida ya Mungu. Mungu anasema kwa mwenye zambi, "Ukiamini, halafu utaona."

**6:31** Wakirudi kwa Agano la Kale, Wayuda walikumbusha Yesu ajabu ya mana[5] jangwani. Ni kama walisema kwamba Yesu hakufanya kamwe neno la kushangaza sana kama hili. Walitaja sehemu toka Zaburi 78:24, 25, **"Akanyesha mana juu yao wapate kula, akawapa ya nafaka za mbingu."** Ni kama walisema Musa aliita mkate toka mbinguni; alikuwa mkubwa kupita Yesu kwa sababu Yesu alizidisha tu chakula ambacho *walikuwa nacho*!

**6:32** Jibu la Bwana lilionyesha maneno mawili: Kwanza, *si* **Musa** ambaye aliwapa mana, lakini Mungu. Na, neno la pili, mana haikuwa mkate wa kweli wa roho, **mkate toka mbinguni.** Mana ilikuwa chakula kusaidia hitaji la mwili, lakini haikuwa na faida tena nyuma ya mauti. Bwana Yesu alikuwa akisema hapa juu ya **mkate** wa **kweli** ambao Mungu anatoa toka mbinguni. Ni mkate kwa roho, si kwa mwili. Kwa njia ya kusema **Baba yangu,** Kristo alionyesha kwamba yeye ni Mungu.

**6:33** Bwana Yesu alijifunua kama **mkate wa Mungu unaoshuka toka**

**mbinguni na** kuleta **uzima.** Alionyesha kwamba **mkate wa Mungu** ni bora kupita mana jangwani. Mana haukuleta uzima lakini ilisaidia tu uzima wa mwili. Ilikuwa kwa Israeli tu, si kwa dunia nzima. **Mkate wa kweli unashuka toka mbinguni na kuwapa watu uzima** – si kwa inchi moja tu lakini kwa **dunia** nzima.

**6:34** Hata saa ile Wayuda hawakufahamu kwamba Bwana Yesu alikuwa akisema juu yake mwenyewe kama mkate wa kweli, hivi walimwomba kuwapa **mkate** ule. Walikaa kufikiri juu ya mkate walioweza kushika mikononi mwao, maana hawakuwa na imani ya kweli mioyoni mwao.

**D. Yesu, Mkate wa Uzima (6:35-65)**

**6:35** Sasa **Yesu** alisema na watu wazi kabisa ya kwamba yeye ni **mkate wa uzima.** Njaa ya roho ya watu wanaofika kwake inashibishwa kwa milele. Wale ambao wanamwamini wataona kwamba hawatakuwa na kiu tena kamwe. Ona maneno haya **Mimi ni** ndani ya shairi hili na fahamu kwamba Bwana alikuwa akionyesha ya kuwa yeye na Yehova ni sawasawa. Ingekuwa upumbavu kwa mtu mwenye zambi kusema maneno ya shairi 35. Mtu wa dunia hawezi kushibisha njaa na kiu yake mwenyewe ya roho; ataweza kufanya hivi kwa dunia nzima namna gani?

**6:36** Ndani ya shairi 30 Wayuda wasioamini walikuwa wameomba kupewa alama kuwasaidia kuamini. Hapa Yesu alisema kwamba alikuwa amewaambia ya kwamba walikuwa **wamemwona yeye** – alama kubwa kupita zote, **lakini hata hivi hawakuamini.** Kama ikiwashinda kutambua Mwana wa Mungu akisimama mbele yao kama mtu mkamilifu, hawataaminishwa na alama yo yote aliyoweza kutenda.

**6:37** Bwana hakushushwa moyo kwa sababu ya kutokuamini kwa Wayuda. Alijua mashauri na makusudi yote ya Baba yake yatatimizwa. Hata kama Wayuda waliokuwa wakimsikia walikataa kumpokea, alijua kwamba wale waliochaguliwa na Mungu watafika kwake.

Hili ni shairi kubwa sana kwa sababu inapasha na maneno machache kweli kubwa zaidi za Biblia. Kweli ya kwanza ni ya kama Mungu amempa Kristo watu fulani, na ya kuwa **wote** ambao alimpa wataokolewa. Kweli ya pili ni neno lililo lazima kwa mtu kufanya. Kwa mtu kupata wokovu, inampasa kufikia Bwana Yesu na kumpokea na imani. Mungu anachagua watu fulani kuokolewa, lakini Biblia haifundishi kamwe ya kwamba anachagua watu wengine kuhukumiwa. Ni kwa sababu ya neema ya Mungu tu mtu ye yote anaokolewa. Lakini mtu ye yote akipotea, ni kosa lake mwenyewe.

Lakini pamoja na kufundisha ya kwamba Mungu amechagua watu wengine kuokolewa, Biblia inafundisha vilevile kwamba ni lazima kwa mtu kuchagua kupokea Habari Njema. Mungu anataka watu wote kuokolewa, maana kila mtu anayeamini Bwana Yesu Kristo ataokolewa. Mungu haokoi watu wasiotaka kupokea wokovu. Ni lazima kwa mtu kufika karibu naye na roho ya toba na imani. Halafu Mungu atamwokoa. Hakuna mtu anayefikia Mungu kwa njia ya Kristo **atakayetupwa inje kabisa.**

Inatushinda kupatanisha mafundisho haya na nia zetu za mtu. Lakini sharti tuyaamini hata ikitushinda kuyafahamu. Ni mafundisho ya Biblia na tunayasoma wazi hapa.

**6:38** Ndani ya shairi 37 Bwana Yesu alisema kwamba mwishoni mashauri yote ya Mungu yatatimizwa kwa maneno ya wokovu wa wale aliopewa. Kwa sababu neno hili lilikuwa mapenzi ya Baba, Bwana yeye mwenyewe atatumika kulitimiza, kwa sababu kazi yake ilikuwa

kufanya mapenzi ya Mungu. Kristo alisema, **"Sikushuka toka mbinguni nifanye mapenzi yangu"** na kwa njia ya masemo haya alionyesha wazi ya kwamba maisha yake hayakuanza ndani ya sanduku ya kulisha nyama kwa Betelehemu. Alikuwa tangu milele pamoja na Mungu Baba mbinguni. Wakati alipofika duniani alikuwa Mwana mwenye kutii wa Mungu. Yeye mwenyewe alikamata pahali pa mtumishi kwa kutimiza **mapenzi** ya Baba yake. Si kusema kwamba hakuwa na kutaka yeye mwenyewe, lakini ya kwamba **kutaka kwake** kulipatana kabisa na kutaka kwa Baba yake.

**6:39 Yalikuwa mapenzi ya Baba** kwa kila mtu aliyeletwa kwa Kristo kuokolewa na kulindwa kufika ufufuko wa wenye haki, wakati watakapofufuliwa na kupelekwa mbinguni. Hakufikiri hapa juu ya waamini mmoja mmoja, lakini waamini wote watakaookolewa kwa miaka yote. Ilikuwa kazi ya Bwana Yesu kuangalia ili hata mmoja wa waamini wale asipotee lakini wao wote pamoja, mwili mzima wa Kristo, **wafufuliwe pamoja siku ya mwisho.**

Kwa *Wakristo,* **siku ya mwisho** ni **siku** Bwana Yesu atakapofika kwa mawingu, wakati Wakristo wote waliokufa watakapofufuliwa kwanza, wakati waamini walio kwanza hai watakapogeuzwa, na wakati wote watakapogeuzwa kukutana na Bwana katika hewa, kukaa pamoja na Bwana kwa milele. Kwa *Wayuda* siku ya mwisho ni kuja kwa Masiya katika utukufu.

**6:40** Halafu Bwana aliendelea kueleza namna gani mtu anaweza kuingia jamaa ya wakombolewa. Ni **mapenzi** ya Mungu kwa kila mtu **anayetazama Mwana na kumwamini kupata uzima wa milele.** Maana ya *kutazama* **Mwana** hapa si kumwona na macho ya mwili lakini na macho ya imani. Lazima mtu aone au kutambua kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu na Mwokozi wa dunia. Kisha ni kumwamini. Na kutaka kwake inampasa kuchagua kumwamini na kumpokea kuwa Mwokozi wake mwenyewe. Wote wanaofanya hivi **wanapokea uzima wa milele** kwa wakati wa sasa, na wanaweza kujua kabisa kwamba watafufuliwa **siku ya mwisho.**

**6:41** Watu hawakuwa tayari kupokea Bwana Yesu siku ile na walionyesha neno hili kwa njia ya **kumnungunikia**. Alikuwa amesema kwamba yeye ni **mkate ulioshuka toka mbinguni**, na walifahamu kwamba hili ndilo neno kubwa. Haiwezekani kwa mtu, au hata nabii kufanya hivi. Basi **walinungunika juu yake** kwa sababu hawakuwa tayari kuamini masemo yake.

**6:42** Walifikiri **Yesu** alikuwa **mwana wa Yosefu**, lakini neno hili halikuwa kweli. Yesu alizaliwa na bikira Maria. Yosefu hakuwa baba yake, lakini mimba yake ilikuwa ya Roho Mtakatifu. Lakini walikataa kuamini kwamba alizaliwa na bikira, na hivi walikaa katika giza na kutokuamini. Ni vivyo hivyo leo. Watu wanaokataa kupokea Bwana Yesu kama Mwana wa Mungu aliyeingia duniani kwa njia ya tumbo la bikira wanakataa kweli kubwa zote juu ya Kristo na kazi yake kubwa.

**6:43** Hawakusema maneno haya kwa **Yesu** wazi uso kwa uso, lakini alijua masemo yao, akawakataza **wasimnungunikie**. Mashairi yanayofuata yanaeleza kwa sababu gani manunguniko yao yalikuwa bure na pasipo faida. Kwa kipimo Wayuda walichokataa ushuhuda wa Bwana Yesu, kwa kipimo hiki mafundisho yake yalikuwa nguvu kupita kufahamu. Kwa kipimo watu walichokataa Habari Njema, iligeuka nguvu kupita kwao kuipokea. Bwana aliwapasha maneno yasiyokuwa nguvu kufahamu nao walikataa kuyaamini, halafu aliwapasha maneno yaliyokuwa nguvu kupita, lakini

wasikiaji walishindwa kabisa kuyafahamu; walibaki wajinga kabisa.

**6:44** Watu hawana tumaini hata kidogo na hawawezi kujisaidia wenyewe. Mtu hana nguvu yeye mwenyewe kufika karibu na Bwana Yesu. Isipokuwa Mungu Baba anaanza kwanza kufanya kazi ndani ya roho na maisha yake, hatafahamu kamwe hatia yake kubwa wala hitaji lake la Mwokozi. Ni nguvu kwa watu wengi kufahamu shairi hili. Wanafikiri linafundisha kwamba labda mtu hawezi kuokolewa hata kama akitaka sana. Sivyo! Shairi hili linaonyesha wazi sana kwamba ni Mungu anayeanza kutumika ndani ya maisha yetu na kujaribu kutukokota kwake. Sisi ni huru kupokea Bwana Yesu au kumkataa. Lakini tusingalikuwa na hamu kamwe kukaribia Mungu, kama Mungu asingalisema na mioyo yetu kwanza. Halafu Bwana aliongeza tena ahadi yake **kufufua** kila mwamini wa kweli **siku ya mwisho.** Kama tulivyoona mbele, siku ile ndiyo siku Kristo atakapokuja kwa watakatifu wake, wakati wafu watakapofufuliwa, nao walio kwanza hai watakapogeuzwa. Ni ufufuko wa waamini tu.

**6:45** Nyuma ya kusema na nguvu ya kwamba hakuna mtu aliyeweza kufika kwake kamwe kama Baba asipomvuta kwanza, Bwana anaendelea na kueleza namna gani Baba anavuta watu. Kwanza alitaja shairi toka Isaya 54:13, **"Nao wote watakuwa wamefundishwa na Mungu."** Mungu hachagui tu watu lakini anasema na mioyo yao kwa njia ya mafundisho toka Neno lake la damani.

Kisha inapasa mtu kuchagua na kutaka kwake. Wale wanaopokea mafundisho toka Neno la Mungu na kujifunza toka Baba ndio wale wanaokuja kwa Kristo. Hivi tunaona hapa tena kweli hizi kubwa mbili pamoja ndani ya Maandiko: Mungu ni mwenye enzi, na mtu anaweza kuchagua.

Yesu alisema, **"Imeandikwa katika manabii,"** ndivyo vitabu vya manabii. Alitaja shairi toka Isaya, lakini alifikiri juu ya maandiko yote ya manabii. Watu wanavutwa kwa Mungu kwa njia ya mafundisho ya Neno la Mungu na Roho ya Mungu.

**6:46** Maana ya "wamefundishwa na Mungu" **haiko** ya kwamba **waliona** Mungu. Kuna mmoja tu **aliyeona Baba,** ndiye aliyetoka kwa Mungu, Bwana Yesu mwenyewe.

Wote wanaofundishwa na Mungu wanafundishwa juu ya Bwana Yesu Kristo.

**6:47** Shairi hili ni moja la mashairi wazi zaidi na mafupi zaidi ndani ya Biblia nzima juu ya njia ya wokovu. Haiwezekani kwa mtu ye yote kukosa kufahamu maana ya masemo haya ya Bwana Yesu – ya kwamba mtu ye yote **ambaye anamwamini ana uzima wa milele**. Ona ya kuwa alianza habari hizi kubwa sana na maneno haya **"Kweli, kweli"**. Hili ni moja la mashairi mengi ndani ya Agano Jipya yanayofundisha kwamba watu hawaokolewi kwa njia ya matendo mema wala kushika sheria, si kwa sababu ya kufungana na kanisa fulani, lakini kwa njia ya kuamini Bwana Yesu Kristo tu.

**6:48, 49** Sasa Bwana Yesu alisema ya kwamba *yeye* ndiye **mkate wa uzima** ambao alikuwa amesema juu yake. **Mkate wa uzima** ndio **mkate** unaoleta uzima kwa wale ambao wanaukula. Wayuda walisema naye mbele juu ya **mana jangwani,** kama kusema na Bwana Yesu alete vyakula vizuri sana kama mana ile. Basi sasa Bwana aliwakumbusha kwamba **baba** zao walikula **mana jangwani** nao wote **walikufa**. Neno hili lilionyesha kwamba **mana** ile ilikuwa kwa uzima wa sasa tu. Haikuweza kuleta uzima wa milele kwa watu ambao waliikula. Kwa njia ya kusema, **"Baba zenu"** Bwana alijitenga na watu waovu wa dunia hii na kuonyesha tena uungu wake.

**6:50** Bwana Yesu alijiita mwenyewe **mkate unaoshuka mbinguni**. Mtu akikula mkate huu **hatakufa.** Si kusema kwamba mwili wake hautakufa, lakini ya kwamba atakuwa na uzima wa milele mbinguni. Na hata mwili wake ukikufa, atafufuliwa siku ya mwisho, na atakuwa pamoja na Bwana kwa milele.

Ndani ya shairi hili na mashairi yanayofuata Bwana Yesu alisema tena na tena juu ya watu *wakikula mkate huu, ndio yeye mwenyewe.* Maana ya masemo haya ilikuwa nini? Ilikuwa kwamba inapasa watu kula nusu ya mwili wake wa umtu? Sivyo. Neno hili haliwezekani na lingekuwa neno la kuchukiza. Watu wengine wanafikiri alifundisha kwamba inatupasa kufanya hivi kwa njia ya kula kwa karamu ya ukumbusho; ya kwamba kwa njia ya ajabu mkate na mvinyo zinageuzwa kuwa mwili na damu ya Kristo, na ya kwamba ni lazima kwa sisi kutwaa sehemu ya vitu hivi ili tuweze kuokolewa. Lakini Yesu hakutaka kusema hivi. Maneno yanayotangulia na kufuata yanaonyesha wazi kwamba maana ya **kula** hapa ni kumwamini. Wakati tunapoamini Bwana Yesu Kristo kuwa Mwokozi wetu, tunatwaa Bwana kwa sisi wenyewe kwa njia ya imani. Tunashiriki ndani ya faida yake na kazi yake. Augustine, mtu wa Mungu aliyeishi zamani alisema, "Amini na umekula."

**6:51** Yesu ni **mkate wa uzima**. Hana uzima yeye mwenyewe tu, lakini anatoa uzima. Watu wanaokula mkate huu … **watakaa milele**. Itawezekana namna gani? Namna gani Bwana anaweza kuletea wenye zambi uzima wa milele? Jibu la ulizo hili ni ndani ya sehemu ya mwisho ya shairi hili: **"Mkate ambao nitautoa ni mwili wangu, ambao nitautoa kwa ajili ya uzima wa dunia."** Bwana Yesu alitazamia hapa mauti yake msalabani. Atatoa **uzima** wake kuwa ukombozi kwa wenye zambi. Mwili wake utavunjwa, na damu yake itamwangwa kama zabihu kwa zambi. Atakufa kama Mkombozi. Atalipa azabu iliyohitajiwa kwa zambi zetu. Atafanya hivi kwa sababu gani? Alifanya hivi **kwa ajili ya uzima wa dunia.** Hatakufa kwa taifa la Wayuda tu, au hata kwa wachaguliwa tu, lakini damani ya mauti yake itatosha kwa dunia nzima. Si kusema kwamba watu wote wa dunia wataokolewa, lakini ya kwamba kazi ya Bwana Yesu Kristo kwa Kalvari ilitosha kuokoa dunia nzima kama watu wote wangalimwamini.

**6:52** **Wayuda** walikaa kufikiri juu ya **mkate** na **nyama** ya dunia. Iliwashinda kufahamu kwamba Bwana Yesu alikuwa akisema juu ya vitu hivi vya dunia kufundisha kweli za roho. Hivi walishindana katikati yao, namna gani **Mtu huu** (walifikiri alikuwa mtu kama wao tu) ataweza kuwapa **mwili wake** kula. Sharti imani itangulie kuona na macho, na inatayarisha roho yako kufahamu, moyo wako kuamini, na kutaka kwako kutii. Utapata majibu kwa maulizo yako yote wakati unapojiweka chini ya amri ya Kristo, kama Paulo alivyofanya wakati alipolia, "Bwana, unataka nifanye nini?"

**6:53** Mara hii vilevile **Yesu**, anayejua maneno yote alijua mawazo na masemo yao. Hivi aliwaonya sana kama wasipokula **mwili** wake na **kunywa damu yake**, **hawatakuwa na uzima ndani yao.** Hakusema juu ya mkate na mvinyo zinazotumiwa kwa karamu ya ukumbusho wa Bwana. Wakati Bwana aliposimamisha karamu hii, usiku alipotolewa kwa mikono ya adui, mwili wake ulikuwa haujavunjwa bado, na damu yake ilikuwa haijamwangwa bado. Wanafunzi walikula wa mkate huu na kunywa nusu ya mvinyo, lakini hawakula wa mwili wake na kunywa ya damu yake ya mtu. Bwana Yesu alikuwa akisema tu ya kwamba tusipojikamatia na imani faida ya mauti yake kwa Kalvari, hatutaweza kuokolewa kamwe. Lazima

tumwamini, kumpokea, kumtegemea, na kumkamata kuwa wetu wenyewe.

**6:54** Tukiangalia shairi hili pamoja na shairi 47 tunaona wazi kwamba maana ya kula mwili wake na kunywa damu yake ni kumwamini. Ndani ya shairi 47 tunasoma "Yeye mwenye kuniamini mimi ana uzima wa milele." Ndani ya shairi 54, tunajifunza kwamba yeye **anayekula mwili wake** na **kunywa damu yake ana uzima wa milele**. Hivi kwa njia ya kusawanisha mashairi haya mawili tunafahamu kwamba **kula mwil**i wake na **kunywa damu** yake ni kumwamini. Wote ambao wanamwamini watafufuliwa **siku ya mwisho**. Maneno haya ni juu ya miili ya waamini waliokufa.

**6:55 Mwili** wa Bwana Yesu ni **chakula cha kweli**, na **damu yake ni kikunywa cha kweli.**[22] Ni namna nyingine na chakula na kinyweo cha dunia hii iliyo na faida kwa muda mfupi tu. Damani ya mauti ya Kristo inaendelea kwa milele. Wale wanaoshiriki ndani yake kwa njia ya imani wanapokea uzima unaoendelea kwa milele.

**6:56** Kuna umoja wa kweli kati ya Bwana na wale ambao wanamwamini. Yeye **mwenye kula mwili wake na kunywa damu yake anakaa ndani** yake, **na** Bwana anakaa ndani ya mtu yule. Hakuna ushirika wa karibu kupita ule. Wakati tunapokula chakula tunaingiza chakula hiki ndani yetu nacho kinageuka sehemu ya mwili wetu. Wakati tunapopokea Bwana Yesu kuwa Mkombozi wetu, anaingia na kukaa ndani ya maisha yetu, nasi vilevile tunakaa ndani yake.

**6:57** Halafu Bwana alileta mfano mwingine wa ushirika wa karibu sana katikati yake na watu wake. Mfano huu ulikuwa mwunganisho wake mwenyewe na Mungu Baba. **Baba aliye hai** (ndiye mwenye kuleta uzima) alikuwa **ametuma** Bwana Yesu duniani. Hapa duniani aliishi kama mtu **kwa Baba**, maana yake kwa umoja na upatano. Aliweka roho juu ya maneno yote ya Mungu Baba yake. Alikuwa hapa duniani kama mtu, na watu wa dunia hawakufahamu kwamba alikuwa Mungu ndani ya mwili wa mtu. Hata kama watu wa dunia hawakumfahamu, yeye na Baba yake walikuwa mmoja. Walikuwa na ushirika na upatano wa karibu sana. Ni vivyo hivyo na waamini ndani ya Bwana Yesu. Wao ni hapa duniani, na watu wa dunia hawawafahamu lakini wanawachukia, na mara nyingi wanawatesa. Lakini kwa sababu wameamini Bwana Yesu **wanaishi kwa sababu** yake na **kwaye.** Uzima wao na uzima wake zinafungana pamoja, na uzima ule utaendelea milele.

**6:58** Ni kama shairi hili linajumlisha maneno yote ambayo Bwana alisema ndani ya mashairi yaliyotangulia. Yeye ni **mkate ulioshuka toka mbinguni.** Yeye ni bora kupita **mana baba waliyokula** jangwani. Mkate ule ulikuwa na faida kwa wakati tu. Lakini Kristo ni Mkate wa Mungu anayeleta uzima wa milele kwa wote ambao wanamkula.

**6:59** Makutano walikuwa wamefuata Yesu na wanafunzi wake hata Kapernaumu toka upande wa kaskazini-mashariki wa bahari ya Galilaya. Ni kama walimkuta ndani ya sunagogi[6] naye aliwatolea hotuba juu ya Mkate wa Uzima pale.

**6:60** Kwa wakati huu Bwana Yesu alikuwa na **wanafunzi wengi kupita** wanafunzi wake 12 wa kwanza. Mtu ye yote ambaye alimfuata na kupokea mafundisho yake alijulikana kama mwanafunzi. Lakini si wote waliojulikana kama wanafunzi wake walikuwa waamini wa kweli. Sasa **wengi** wa wale waliokiri kuwa **wanafunzi wake** walisema, **"Neno hili ni gumu."** Walifikiri mafundisho yake yalikuwa mabaya. Si kusema kwamba iliwashinda kuyafahamu, lakini yaliwachukiza. Wakati waliposema, **"Nani anayeweza kulisikia,"** maana ya ma-

semo yao ilikuwa “Nani atakubali kusikiliza mafundisho mabaya namna hii?”

**6:61** Hapa tunaona tena kwamba Bwana alijua maneno yote. **Yesu alijua** maneno ambayo wanafunzi walikuwa wakisema. Alijua walinungunika kwa sababu alisema alitoka mbinguni, na ya kwamba hawakufurahi wakati aliposema inapasa watu kula mwili wake na kunywa damu yake kupata uzima wa milele. Hivi aliwauliza, **“Neno hili linawachukiza ninyi?”**

**6:62** Walichukizwa kwa sababu alisema alishuka mbinguni. Sasa aliwauliza kwamba watafikiri **nini** kama wakimwona **akipanda mbinguni** tena, ndilo neno atakalofanya nyuma ya kufufuliwa toka wafu. Na walichukizwa kwa sababu alisema inapasa watu kula mwili wake. Basi watafikiri nini kama wakiona mwili huu **ukipanda** mbinguni **pahali alipokuwa mbele?** Namna gani watu wataweza kula mwili wake na kunywa damu yake ya dunia wakati atakapokwisha kurudia Baba yake mbinguni?

**6:63** Watu hawa walikuwa wakifikiri juu ya mwili wa dunia wa Kristo, lakini hapa aliwaambia kwamba watu hawapati uzima wa milele kwa njia ya kula mwili lakini kwa njia ya kazi ya Roho Mtakatifu wa Mungu. Mwili hauwezi kuleta uzima; **Roho Mtakatifu** tu anaweza kufanya hivi. Hawakufahamu kwamba iliwapasa kupokea masemo yake kwa njia ya roho. Hivi Bwana Yesu alieleza kwamba **maneno ambayo alisema** kwao yalikuwa **roho nayo yalikuwa uzima;** ya kwamba iliwapasa kufahamu masemo yake juu ya kula mwili wake na kunywa damu yake na maana yao ya roho, ndiyo kwamba ni *kumwamini,* halafu wale ambao walipokea masemo yake watapata uzima wa milele.

**6:64** Hata saa Bwana Yesu alipokuwa akisema maneno haya, alitambua kwamba wengine wa wasikiaji wake hawakumfahamu kwa sababu **walikataa kuamini.** Hawakufahamu kwa sababu hawakutaka, si kwa sababu hawakuweza. **Yesu alijua tangu mwanzo** ya kwamba wengine waliokiri kuwa wafuata wake **hawatamwamini** na ya kwamba mmoja wa wanafunzi wake **atamtoa kwa adui**. Ndiyo, **Yesu alijua** maneno haya yote tangu milele, lakini tunafikiri hapa alisema juu ya mwanzo wa utumishi wake duniani.

**6:65** Sasa alieleza ya kwamba sababu ya kutokuamini kwao, alisema nao ya kwamba **hakuna mtu** anayeweza kuja kwake ila **apewe ruhusa na Baba yake.** Masemo namna hii yanaumiza kiburi ya mtu anayefikiri anaweza kujipatia mwenyewe wokovu. Bwana Yesu aliwaambia watu ya kwamba wanaweza kupata kutoka kwa Mungu **Baba** tu uwezo **kufika** kwake.

### E. Mawazo namna namna juu ya masemo ya Mwokozi (6:66 -71)

**6:66 Wengi** wa watu waliofuata Bwana kufika sasa hawakufurahi hata kidogo juu ya masemo yake, hivi hawakuwa tayari kumfuata tena. Wanafunzi hawa hawakuwa waamini wa kweli. Walifuata Bwana kwa sababu mbalimbali, lakini si kwa sababu walimpenda kweli kweli au kufahamu kama yeye ni nani.

**6:67** Halafu **Bwana** aligeuka kwa wanafunzi wake wa kwanza **kumi na wawili,** akawauliza kama wao vilevile watamwacha.

**6:68** Jibu la Petro lilikuwa zuri sana. Ni kama alisema, “**Bwana**, tutakuacha namna gani? **Wewe** unafundisha maneno ambayo yanafikisha watu hata **uzima wa milele**. Kama tukikuacha wewe, hakuna mwingine ambaye tutaweza kwendea. Kukuacha wewe kutatufikishia upotevu.”

**6:69** Petro aliendelea kusema kwa ajili ya wale kumi na wawili, akasema ya kwamba **wameamini na kujua** ya kuwa Bwana Yesu ndiye *Kristo,* **Mwana wa**

**Mungu wa uzima.”** Ona ya kuwa alisema **“tumeamini na kujua.”** Imani ilitangulia kujua. Kwanza iliwapasa kuamini Bwana Yesu Kristo; kisha **walijua** ya kwamba yeye ni kweli Mwana wa Mungu kama alivyosema.

**6:70** Ndani ya mashairi 68 na 69 Petro alisema “sisi” akifikiri wanafunzi kumi na wawili. Hapa ndani ya shairi 70 Bwana Yesu alionyesha kwamba si wanafunzi wale kumi na wawili wote walikuwa waamini wa kweli. Ndiyo, Bwana alikuwa **amewachagua** wote **kumi na wawili,** lakini **mmoja** wao alikuwa **shetani**. Hakuwa mwamini wa kweli.

**6:71** Bwana Yesu alijua kwamba **Yuda Iskariota atamtoa kwa adui**. Alijua kwamba Yuda hakumpokea kuwa Bwana na Mwokozi wake. Na vilevile shairi hili linaonyesha kwamba Petro hakuwa mkamilifu na hakujua maneno yote wakati aliposema juu ya wanafunzi!

Bwana Yesu alianza hotuba yake juu ya mkate wa uzima na mafundisho yasiyokuwa nguvu kufahamu, lakini ilionekana nyuma kidogo ya kwamba Wayuda walikataa masemo yake. Kwa kipimo walichofunga mioyo na nia zao kwa kweli, kwa kipimo kile mafundisho yaligeuka kuwa nguvu kupita. Mwishoni, Bwana alisema juu ya kula mwili wake na kunywa damu yake. Iliwashinda kabisa kupokea masemo haya! Walisema, “Neno hili ni gumu, nani anayeweza kulisikia?” na waliacha kumfuata. Tunda la kukataa kweli lilikuwa hukumu ya upofu wa roho. Walikuwa wame*kataa* kuona, hivi nyuma kidogo hawaku*weza* tena kuona.

## 5. MWAKA WA TATU WA UTUMISHI WA MWANA WA MUNGU: YERUSALEMA (7:1–10:39)

### A. Yesu anakemea ndugu zake (7:1-9)

**7:1** Miezi michache ilipita nyuma ya sura 6 na mwanzo wa sura 7. **Yesu** alibaki **katika Galilaya**. **Hakutaka** kukaa **katika Yudea**, makaa ya wakubwa wa **Wayuda**[7] kwa sababu walikuwa wakitafuta **kumwua.** Ni wakubwa na viongozi hawa ambao walimchukia zaidi, na waliotafuta njia **kumwua**.

**7:2** **Siku kubwa ya vibanda** ilikuwa moja ya matukio makubwa ya Wayuda kila mwaka. Ilikuwa kwa wakati wa mavuno, na ilikuwa ukumbusho wa wakati Waisraeli walipokaa katika vibanda vilivyosimamishwa saa yenyewe nyuma ya kutoka kwao katika inchi ya Misri. Ilikuwa siku kubwa ya furaha, na ilitazamia siku Masiya atakapotawala, na taifa la Wayuda wakombolewa watakapokaa inchini na salama na kusitawi.

**7:3** Tunafikiri **ndugu** za Bwana walikuwa wana ambao Maria alizaa nyuma ya kuzaa Yesu, lakini undugu huu haukuwapa uzima wa milele. Hawakuamini Bwana Yesu kweli kweli. Walisema naye aende kwa Yerusalema kwa siku kubwa ya vibanda na kufanya mengine ya maajabu yake pale **ili wanafunzi** wake wapate **kuona** maneno aliyofanya. **Wanafunz**i hawa hawakuwa wanafunzi wake kumi na wawili, lakini watu waliokiri kufuata Bwana katika Yudea.

Hata kama ndugu zake hawakumwamini, walitaka Bwana kujionyesha wazi mbele ya watu. Labda walikuwa wakijitafutia heshima kwa njia ya kuwa ndugu ya mtu mkubwa wa kujulikana. Au labda walikuwa na wivu kwa sababu ya heshima aliyopokea, na walimsukuma kwenda Yudea wakitaraji atauawa pale.

**7:4** Labda walisema maneno haya na uchungu. Ni kama ndugu zake walifikiri alikuwa akitafuta kujulikana katikati ya watu. Kwa sababu gani alikuwa akifanya maajabu haya yote katika Galilaya kama asipotaka kujulikana? Ni kama walisema naye, “Una njia sasa kugeuka mtu wa kujulikana namna unavyotaka. Vizuri uendee Yerusalema kwa siku kubwa. Ku-

takuwa na mia za watu pale na utakuwa na njia kufanya maajabu mbele yao. Galilaya ni pahali pa kimya, na ni kama unafanya maajabu yako hapa kwa siri. Kwa nini unafanya hivi kama ukitaka kugeuka mtu wa kujulikana katikati ya watu?" Waliongeza, **"Kama ukifanya maneno haya, ujionyeshe mwenyewe kwa dunia."** Maana ya masemo yao ni hii, "Ukiwa kweli Masiya, na ukifanya maajabu haya kuhakikisha neno hili, kwa sababu gani huyafanyi kwa Yudea mbele ya watu wengi?"

**7:5** **Ndugu zake** hawakutaka atukuzwe. **Hawakuamini** kwamba alikuwa Masiya, lakini walisema maneno haya na uchungu, na roho zao hazikuwa safi mbele ya Bwana. Bila shaka ilikuwa huzuni kabisa kwa Bwana Yesu kujua kwamba ndugu zake mwenyewe walikuwa na shaka juu ya masemo na matendo yake. Mara nyingi wafuata waaminifu wa Bwana wanaona kwamba ndugu na rafiki ambao wanapenda zaidi ni wenye kushindana nao na ukali kupita watu wengine.

**7:6** Utaratibu wa matukio ya maisha ya Bwana ulitengenezwa tangu mwanzo hata mwisho. Aliishi kila siku kupatana na shauri la maneno yaliyotayarishwa mbele kwa siku ile. **Wakati** wa kujionyesha wazi kwa dunia ilikuwa haujafika bado. Alijua maneno yaliyokuwa mbele yake na ya kwamba hayakuwa mapenzi ya Mungu kwa yeye kwenda Yerusalema kujionyesha kwa watu kwa wakati huu. Lakini alikumbusha ndugu zake kwamba **wakati** wao ulikuwa **tayari siku zote**. Waliishi kila siku wakifanya mapenzi yao wenyewe, si mapenzi ya Mungu. Waliweza kusafiri pahali po pote na kufanya neno lo lote walilotaka kwani waliweka roho juu ya kutimiza mapenzi yao wenyewe tu.

**7:7** **Dunia** haikuweza **kuchukia** ndugu za Bwana kwa sababu walikuwa watu wa dunia. Walifungana na dunia na kushindana na Yesu. Maneno yote ya maisha yao yalipatana na dunia, ndiyo utaratibu ambao watu wamesimamisha kwa maneno ya elimu, ufundi mbalimbali kama kupiga muziki, kuchora sanamu, na zaidi maneno ya dini bila kukumbuka Mungu. Katika Yudea waliwaza zaidi juu ya maneno ya dini kwa sababu wenye kuchukia Kristo zaidi walikuwa watawala wa Wayuda.

Dunia ilichukia Kristo **kwa sababu** alishuhudia kwamba **kazi zao** ni **mbovu.** Ni huzuni kabisa kuwaza juu ya uovu wa roho za watu waliotaka kuua Mtu safi asiyekuwa na zambi. Ukamilifu wa maisha ya Yesu ulionyesha uovu wa maisha ya watu wote wengine. Watu hawakufurahi juu ya uovu wao kufunuliwa hivi, lakini kwa pahali pa kutubu na kusihi Mungu kuwahurumia, walijaribu kuua Yule ambaye alifunua zambi zao.

**7:8** Ni huzuni kusoma juu ya Bwana akisema na ndugu zake **kupanda kwa karamu.** Walitenda kama watu wa Mungu. Walikwenda kushika siku kubwa ya vibanda. Lakini Kristo alisimama pale katikati yao, nao hawakumpenda. Watu wanapenda kawaida za dini kwa sababu wanaweza kuzifanya bila mapendo ya kweli rohoni. Lakini wanafazaika na kusumbuka wakati wanaposimama mbele ya Yesu Kristo mwenyewe. Alisema nao ya kwamba **hatapanda kwa karamu hii kwanza**[27] kwa sababu wakati wake **hakutimia bado.** Alikataa kwenda pamoja na ndugu zake na kujifunua mbele ya makutano. Saa kwa neno hili ilikuwa haijafika kwanza. Ndani ya shairi 10 tutaona kwamba alikwenda kwa karamu nyuma, kama kwa maficho.

**7:9** Hivi Bwana Yesu **alikaa katika Galilaya** wakati ndugu zake walipokuwa wamekwendea karamu. Siku kubwa ya vibanda ilikuwa wakati wa furaha, lakini waliacha katika Galilaya Yule ambaye aliweza kuwapa furaha hii.

**B. Yesu anafundisha hekaluni (7:10-31)**

**7:10** Nyuma ya **kwenda kwa ndugu zake** kwa Yerusalema, Bwana Yesu alisafiri kule vilevile. Akiwa Myuda mwenye kushika dini alitaka kufikia **karamu**. Lakini akiwa Mwana mwenye kutii wa Mungu, **hakuweza kufanya hivi kwa wazi, lakini kama kwa siri.**

**7:11** Bila shaka **Wayuda** ambao **walimtafuta kwa karamu** walikuwa watawala waliotaka kumwua. Hawakuuliza, **"Yeye ni wapi?"** kwa sababu walitaka kumwabudu, lakini wapate njia kumwua.

**7:12** Kufazaika **kwa watu** juu ya Bwana katikati yao yalikaa kuongezeka. Maajabu aliyofanya yaliwasukuma kufikiri kama alikuwa nani. Watu waliulizana katikati yao juu yake kama yeye ni nabii wa kweli au wa uwongo. **Wengine walisema**: "**Yeye ni mtu mwema," wengine wakasema: "Hapana, lakini anadanganya makutano."**

**7:13** Uadui wa watawala Wayuda ulikuwa umeongezeka sana sana hata watu waliogopa kumtaja **kwa wazi**. Bila shaka wengi wa watu walikuwa wamefahamu kwamba alikuwa kweli Masiya wa Israeli, lakini waliogopa kusema hivi wazi, wakiogopa wakubwa watawatesa.

**7:14** **Karamu** ya vibanda iliendelea kwa siku chache. Katikati ya karamu **Yesu akapanda, akaingia hekalu** kwa pahali watu walipokuwa na ruhusa kukusanyika, **akafundisha**.

**7:15** Watu wale ambao walimsikia **walishangaa** juu ya elimu yake na uwezo wake wa kufundisha. Walijua kwamba Yesu hakufikia darasa yenye heshima kwa kujifunza maneno haya. Hata kwa wakati wa sasa watu wa dunia wanashangaa juu ya waamini wanaoweza kuhubiri na kufundisha Neno la Mungu bila kujifunza ndani ya darasa za elimu nyingi.

**7:16** Ni vizuri sana kuona tena namna Bwana alikataa kujitukuza mwenyewe, lakini alijaribu kutukuza Baba yake tu. **Alijibu** tu kwamba mafundisho yake **si yake**, lakini yalitoka kwa **Yule ambaye alimtuma.** Alifundisha tu maneno ambayo Mungu Baba alimfundisha yeye. Hakutenda peke yake.

**7:17** Haingekuwa nguvu kwa Wayuda kujua kama masemo yake yalikuwa kweli. **Kama mtu akitaka kweli kweli kufanya** mapenzi ya Mungu, Mungu atamfunulia kama mafundisho ya Kristo yalitoka kwa Mungu au yalikuwa maneno ambayo yeye mwenyewe alitaka kufundisha. Kuna ahadi tamu sana hapa kwa mtu ye yote anayetaka kujua kweli. Kama mtu akitaka na roho ya haki kujua kweli, Mungu ataifunua kwake.

**7:18** Mtu ye yote **anayesema kwa amri yake mwenyewe anatafuta utukufu wake mwenyewe.** Lakini haikuwa hivi na Bwana Yesu. Alitafuta **utukufu wa** Baba **ambaye alimtuma**. Kusudi lake lilikuwa haki kabisa, hivi hotuba yake ilikuwa **kweli** kabisa. **Uzalimu hakuwa ndani yake.**

Iliwezekana kusema maneno namna hii juu ya Yesu tu. Ndani ya utumishi wa kila mwalimu mwingine kuna maneno nusu ya kujitukuza mwenyewe. Ingepasa kila mtumishi wa Bwana kujaribu sana kutukuza Mungu tu.

**7:19** Halafu Bwana alishitaki Wayuda. Aliwakumbusha kwamba **Musa** ndiye ambaye aliwapa **sheria.** Walijisifu juu ya neno hili. Walisahau kwamba kuwa na sheria bila kutii maagizo yake si faida. Hata kama walijisifu juu ya kuwa na sheria, ni kama hawakuitii, kwani hata kwa saa ile walikuwa wakifanya shauri kuua Bwana Yesu. Sheria ilikataza uuaji waziwazi. Walikuwa wakiasi sheria kwa njia ya kutaka kumwua.

**7:20** Ukali wa mashitaki ya Yesu ulikata roho za makutano, lakini kwa pahali pa kukubali kwamba alisema kweli,

walianza kumtukana. Walisema ana **pepo**. Walishindana na masemo yake kwamba mtu **alitafuta kumwua.**

**7:21** Halafu **Yesu** alisema tena juu ya mgonjwa aliyeponyeshwa kwa birika la Betesaida. Lilikuwa ajabu hili lililoamsha machukio ya viongozi vya Wayuda juu yake, na ni kwa saa ile walipoanza kufanya shauri ovu kumwua. Bwana aliwakumbusha kwamba **alifanya kazi moja,** nao **wote** walichukizwa. Hawakushangaa kwa sababu ya uzuri wa ajabu hili, lakini walichukizwa kwa sababu alilifanya siku ya sabato.

**7:22** Sheria ya **Musa** iliagiza kwa mtoto mume kutahiriwa siku nane nyuma ya kuzaliwa. Tohara **haikuanza** na **Musa**, lakini na **'baba'** zao, maana na Abrahamu, Isaka na Yakobo. Hata kama siku ya nane nyuma ya kuzaliwa kwa mtoto ilikuwa **siku ya sabato**, Wayuda hawakufikiri ni vibaya kutahiri mtoto siku ile. Walifikiri ni kazi ya lazima iliyokubaliwa na Bwana.

**7:23** Basi wakitahiri **mtoto siku ya sabato**, kwa kutii **sheria ya Musa** juu ya tohara, kwa sababu gani watahukumu Bwana Yesu juu ya kufanyiza **mtu kuwa mzima kabisa siku ya sabato?** Sheria ikikubali kazi ya lazima, haitakubali vilevile kazi ya rehema?

Kwa tohara mwili ulikatwa kidogo tu, na faida yake kwa mwili ni nusu pamoja na kuumia kidogo. Bwana Yesu alikuwa ameponyesha mwili mzima wa mtu siku ya sabato, lakini Wayuda walimhamakia juu ya kufanya hivi.

**7:24** Wayuda walihukumu maneno kwa namna **yalivyoonekana kwa macho,** lakini haikuwa hukumu ya haki. Kazi ambazo walifanya wao wenyewe na walizofikiri ni njema, zilikuwa mbaya kwa mafikiri yao wakati Bwana alipozifanya. Ni desturi ya watu kuhukumu maneno kwa namna yanavyoonekana, si kwa namna ya kweli. Bwana Yesu hakuasi sheria ya Musa; Wayuda ndio wale walioasi sheria kwa njia ya kumchukia yeye bila sababu.

**7:25** Kwa wakati huu ilikuwa imeonekana wazi katika Yerusalema kwamba viongozi vya Wayuda walikuwa wameshauri kuua Mwokozi. Wengine wa watu waliuliza kama mhubiri huyu hakuwa yule ambaye wakubwa walitafuta.

**7:26** Iliwashinda kufahamu kwa nini Bwana Yesu alipewa ruhusa kuhubiri wazi, na **uhodari** namna hii. Kama watawala wakimchukia sana, kwa nini walimruhusu kuendelea na mahubiri yake? Walikuwa wamefahamu kwamba yeye ni **kweli** Masiya?

**7:27** Watu wasioamini kwamba Yesu ni Masiya walifikiri walijua pahali alipotoka. Walifikiri alitoka kwa Nazareti. Walijua mama yake, na walifikiri kwamba Yosefu alikuwa baba yake. Wayuda wa wakati ule waliamini ya kwamba wakati Masiya atakapokuja, atatokea gafula na kwa siri. Hawakujua kwamba atazaliwa kama mtoto mchanga na kukomea kuwa mwanamume. Ingaliwapasa kujua kwa njia ya Agano la Kale kwamba atazaliwa katika Betelehemu, lakini ni kama hawakujua habari hizi juu ya kuja kwa Masiya. Kwa sababu hii walisema, **"Wakati Kristo atakapokuja, hapana mtu mwenye kujua pahali anapotoka."**

**7:28** Basi **Yesu akapaza sauti** yake kwa makutano waliokuwa wakisikiliza mazungumzo ya watu. Ndiyo, **walimjua** kweli kama mtu wa dunia, na walijua **pahali alipotoka.** Walimjua kama Yesu wa Nazareti. Lakini hawakujua kwamba alikuwa Mungu vilevile. Aliendelea kueleza neno hili ndani ya baki la shairi hili.

Kama mtu, alikaa kwa Nazareti. Lakini iliwapasa kufahamu vilevile kwamba **hakuja** kwa kutaka kwake mwenyewe, lakini alitumwa na Mungu Baba "ambaye **hamumjui**." Kwa njia ya masemo haya Bwana Yesu alisema wazi kwamba yeye

ni sawa na Mungu. **Hakuja** kwa roho yake mwenyewe, maana na amri yake mwenyewe na kufanya mapenzi yake mwenyewe. Alitumwa duniani na Mungu wa **kweli**, na ni Mungu huyu ambaye **hawakujua.**

**7:29** Lakini Yesu alimjua. Alikaa pamoja na Mungu tangu milele na alikuwa sawasawa na Mungu Baba kwa njia zote. Hakutumwa tu **toka** Mungu, lakini alikuwa sawa naye kwa maneno yote. Wakati aliposema **"ndiye alinituma"** alisema wazi kabisa kwamba yeye ni Kristo wa Mungu, Mpakaliwa wa Mungu ambaye Mungu alituma duniani kutimiliza kazi ya ukombozi.

**7:30** Wayuda walifahamu maana ya masemo ya Yesu na ya kwamba alikuwa akisema yeye ndiye Masiya. Walifikiri ni ukufuru kabisa na walitaka kumkamata, lakini hakuna mtu ambaye alimtia **mikono kwake, kwa sababu saa yake haijafika bado.** Alilindwa kwa uwezo wa Mungu toka mashauri maovu ya watu kufika saa chaguliwa ilipofika wakati atakapotolewa kuwa zabihu kwa zambi.

**7:31** Hata hivi **watu wengi waliamini Bwana Yesu.** Walifikiri hivi: Yesu angeweza kufanya nini zaidi kuhakikisha kwamba yeye ni Masiya? Wakati **Kristo** atakapokuja, kama Yesu si Masiya, ataweza kufanya **alama nyingi zaidi** au za kushangaza kupita zile ambazo Yesu alikuwa amefanya? Ulizo lao linaonyesha kwamba waliamini maajabu ya Yesu yalihakikisha kwamba yeye ni Masiya.

### C. Uadui wa Wafarisayo (7:32-36)

**7:32 Wafarisayo** waliotembea katikati ya watu **walisikia** mazungumzo yao. **Watu walikuwa wakinungunika** juu ya Mwokozi. Walimsifu kwa siri, si kusema maneno mabaya juu yake. Wafarisayo waliogopa kwamba sifa yao itaongezeka sana hata watataka kupokea Yesu kama kiongozi, hivi **walituma watumishi wamkamate.**

**7:33** Bila shaka Yesu alisema maneno ya shairi hili kwa watumishi waliotumwa kumfunga, na kwa Wafarisayo na watu wengine vilevile.

Bwana Yesu aliwakumbusha kwamba atakuwa pamoja nao kwa **muda kidogo tu**, kisha atarudi kwa Mungu Baba **yake** ambaye **alimtuma.** Bila shaka masemo haya yalikasirisha Wafarisayo hata kupita.

**7:34** Kwa wakati wa kuja Wafarisayo **watamtafuta** na **hawatamwona**. Neno hili litatokea wakati watakapohitaji Mwokozi, lakini saa yao itakuwa imepita. Atakuwa amerudi mbinguni, na kwa sababu ya kutokuamini na uovu wao, hawataweza kukutana naye pale. Inatupasa kuwaza sana juu ya masemo haya. Yanatukumbusha kwamba mtu akikataa kuamini Bwana leo, labda hatakuwa na njia tena kuokolewa siku nyingine.

**7:35 Wayuda** hawakufahamu maana ya masemo ya Bwana. Hawakufahamu kwamba atarudi mbinguni. Walifikiri kwamba labda atakwenda safari ya kuhubiri kwa Wayuda waliosambazwa **katikati ya Wayunani**, au labda kufundisha hata Wayunani vilevile.

**7:36** Watu walikaa kushangaa juu ya masemo ya Yesu na maana yao, ya kwamba **watamtafuta na hawatamwona**. Atakwenda wapi pahali wasipoweza kumfuata? Walikuwa wapofu kabisa rohoni kwa sababu ya kutokuamini kwao. *Hawakutaka* kupokea Bwana Yesu, na kwa sababu hii *hawakuweza kumpokea*.

### D. Ahadi ya Roho Mtakatifu (7:37-39)

**7:37** Wayuda walikuwa na desturi moja isiyoandikwa ndani ya Agano la Kale, ndiyo kubeba maji toka birika la Siloamu na kuyamwanga ndani ya bakuli la feza pahali pa mazabahu ya zabihu za kuteketezwa. Walifanya hivi kila siku kwa siku saba za karamu ya vibanda. Hawakufanya hivi siku ya nane, hivi

watu walishangaa sana kusikia mwito wa Bwana Yesu siku ile kwa watu kuja kwake na kunywa maji ya uzima. Wayuda walikuwa wametimiza desturi hii ya dini, lakini hitaji la roho yao halikushibishwa kwa sababu hawakufahamu maana ya kweli ya siku ile. Mbele ya kwenda kwao kurudia nyumba zao, **siku ya mwisho, siku ile kubwa ya karamu, Yesu akasimama, akapaza sauti yake**, akiwaita **kuja** kwake kupokea kushibishwa kwa hamu ya roho zao. Ona ya kwamba aliita nani: **mtu**, si Wayuda au wenye mali au wagonjwa tu, lakini **mtu ye yote.** Habari Njema yake ni kwa watu wote. Kila mtu anayefikia Kristo ataokolewa.

Lakini ona neno hili moja linalohitajiwa. Maandiko yanasema, **"Mtu akiona kiu.**" Kiu hapa ni kiu ya roho. Mtu asiyefahamu kwamba yeye ni mwenye zambi hatataka kamwe kuokolewa. Mtu asiyefahamu kwamba amepotea kabisa hatafikia Bwana kamwe. Mtu asiyefahamu ukosefu wa roho yake hatataka kamwe kwenda karibu na Bwana kumwomba kusaidiwa. Mwokozi aliita mwenye kiu kuja kwake – si kwa kanisa, au mwalimu, au ubatizo, au meza ya Bwana. Yesu alisema **"aje kwangu."** Kwake tu. **"Aje kwangu, anywe."** Maana ya **kunywa** hapa ni kujitwalia Kristo kuwa Mwokozi **wetu**. Ni kumwamini na kumpokea kuwa Bwana na Mwokozi wetu. Ni kumpokea ndani ya maisha yetu namna tunavyokunywa na kupokea maji mwilini mwetu.

**7:38** Shairi hili linaonyesha kwamba kuja kwa Kristo na kunywa ni sawasawa na *kumwamini*. Mahitaji ya wote wanaoamini yatatimizwa na watapokea **mito** ya baraka za roho **itakayotoka** kwao kuwa baraka kwa watu wengine. Tena na tena ndani ya Agano la Kale tunaona kwamba wale wanaopokea Masiya watasaidiwa wao wenyewe, na watakuwa baraka kwa watu wengine (ona Isa. 55:1). Maana ya semo hili, **"mito ya maji ya uzima itatoka tumbo lake"** ni ya kwamba toka roho zao zitatoka mito ya baraka kusaidia watu wengine. Mwandishi mmoja, jina lake Temple, anatoa onyo hili: "Mtu ye yote aliye na Roho Mtakatifu akipanga ndani yake hawezi kuchunga Roho huyu kwa baraka yake mwenyewe tu. Roho akikaa ndani ya mtu, atatoka kwake kuwa baraka kwa watu wengine. Isipokuwa hivi Roho hakai ndani ya mtu huyu."

**7:39** Kwa shairi hili tunaona wazi kwamba "maji ya uzima" (sh. 38) ni **Roho** Mtakatifu. Hivi shairi hili linafundisha kwamba wote wanaopokea Bwana Yesu Kristo wanapokea Roho ya Mungu vilevile. Watu wengine wanafundisha kwamba Roho Mtakatifu anakuja kukaa ndani ya watu saa fulani nyuma ya kuokolewa kwao, lakini mafundisho haya si kweli. Shairi hili linaonyesha wazi kwamba wote wanaoamini Kristo wanapokea Roho Mtakatifu. Wakati Bwana Yesu aliposema neno hili, **Roho Mtakatifu alikuwa hajakuja bado**. Alikuja siku ya Pentekote tu, nyuma ya kurudi kwa Bwana Yesu mbinguni na kutukuzwa. Tangu saa ile kila mwamini wa kweli anakaaliwa na Roho Mtakatifu.

### E. Mawazo mbalimbali juu ya Yesu (7:40-53)

**7:40,41 Wengi** wa watu waliokuwa wakisikiliza waliamini sasa ya kwamba Bwana Yesu alikuwa **nabii** ambaye Musa alisema juu yake katika Tor. 18:15,18. **Wengine** walikubali kwamba Yesu alikuwa **Kristo**, Masiya. Lakini wengine waliamini neno hili si kweli hata kidogo. Walifikiri kwamba Yesu alitoka kwa Nazareti katika Galilaya, na ya kuwa hakuna unabii ndani ya Agano la Kale juu ya **Kristo akitoka Galilaya.**

**7:42 Kristo** atatoka kweli kwa **Betelehemu**, kama Wayuda walivyoamini, na alikuwa mzao wa **Daudi**. Kama wangalijaribu kujua kupita juu ya maneno haya, wangaliona kwamba *kweli alizaliwa* ka-

tika Betelehemu, na *alikuwa kweli mzao* wa Daudi kwa njia ya Maria.

**7:43** Kwa sababu ya mawazo haya mbalimbali **kulikuwa na magawanyiko katikati ya makutano kwa sababu ya** Kristo. Ni vivyo hivyo sasa. Watu wengine wanasema alikuwa mtu kama sisi. Wengine wanakubali kwamba alikuwa mkubwa kupita watu wote walioishi tangu zamani. Lakini wale wanaoamini Neno la Mungu wanajua kwamba "Kristo ... ni juu ya maneno yote, Mungu mbarikiwa kwa milele" (Rom. 9:5).

**7:44** Watu walikaa kujaribu kufunga Bwana Yesu, lakini hawakuweza. Hakuna uwezo duniani unaoweza kuzuiza mtu yule anayefanya mapenzi ya Mungu. "Hatutakufa kufika wakati kazi yetu itakapokwisha." Saa ya kufa kwa Bwana ilikuwa haijafika bado, hivi watu hawakuweza kumwumiza kwa njia yo yote.

**7:45** Sasa **Wafarisayo** na **wakubwa wa makuhani** walikuwa wametuma **watumish**i kukamata Yesu. **Watumishi** walirudi, lakini Bwana hakuwa pamoja nao. **Wakubwa wa makuhani na Wafarisayo** walikasirika na kuuliza kwa **sababu gani hawakumleta.**

**7:46** Kwa wakati huu wenye zambi walilazimishwa kusema maneno mema juu ya Mwokozi, hata kama wao wenyewe hawakumpokea. Walijibu, **"Mtu hajasema bado kama mtu huyu anavyosema!"** Bila shaka watumishi hawa walikuwa wamesikia masemo ya watu wengi, lakini hata mmoja wao aliyesema na amri, neema, na hekima kama Mwokozi.

**7:47,48** Wakitaka kuogopesha watumishi, **Wafarisayo** walisema walikuwa **wamedanganywa** na Yesu. Waliwakumbusha ya kwamba **watawala** wote wa taifa la Wayuda hawaku**mwamini.** Masemo mabaya kabisa. Ilikuwa haya kubwa kwa viongozi vya taifa la Wayuda kukosa kutambua Masiya wakati alipokuja.

Wafarisayo hawa hawakuamini Bwana Yesu wao wenyewe, na zaidi ya ile ni wazi kwamba hawakutaka watu wengine kumwamini vilevile. Ni vivyo hivyo sasa. Watu wengi wasiotaka kuokolewa wao wenyewe wanajaribu kwa kila njia kuzuiza ndugu zao na rafiki zao wasiokolewe vilevile.

**7:49** Wafarisayo walisema hapa juu ya makutano ya Wayuda kwamba walikuwa wajinga na **kulaaniwa.** Walifikiri kama makutano walijua hata nusu ya mafundisho ya sheria na Maandiko, kama wangalijua kwamba Yesu si Masiya. Hawakukumbuka kwamba labda wao wenyewe walianguka!

**7:50** Halafu **Nikodemo** alisema nao, ndiye **aliyefikia Yesu usiku** na kujifunza kwamba ni lazima kwaye kuzaliwa tena. Ni kama Nikodemo alikuwa ameamini Bwana Yesu Kristo na kupata wokovu. (Ona Yoane 3.) Sasa alisimama katikati ya viongozi vya Wayuda na kusimamia Bwana wake.

**7:51** Alisema nao ya kwamba hawakutendea Yesu kwa haki. **Torati** ya Wayuda **haikuhukumu mtu mbele** ya kumsikia kwanza. Lakini viongozi vya Wayuda walikuwa wakifanya hivi na Yesu. Ni wazi kwamba waliogopa kujua kweli juu yake.

**7:52** Halafu watawala waligeukia mmoja wao, ndiye Nikodemo. Walimwuliza na cheko la kuzarau kama yeye **vilevile** alikuwa mmoja wa wafuata wa Yesu **toka Galilaya?** Hakujua kwamba **hakuna** habari ndani ya Agano la Kale juu ya **nabii ye yote akitoka Galilaya?** Ulizo hili lilifunua ujinga wa watawala wenyewe. Hawakusoma habari za nabii Yona? Yona alitoka Galilaya.

**7:53** Basi karamu ya vibanda ilikwisha na watu walirudia nyumba zao. Wengine walikuwa wamekutana na Mwokozi uso kwa uso na walimwamini. Zaidi yao walimkataa, na viongozi vya Wayuda waliweka roho hata kupita mbele

juu ya kumwua. Walifikiri alikuwa hatari kwa dini yao na desturi za maisha yao.

**F. Mwanamke wa uzini (8:1-11)**

**8:1** Shairi hili linafungana na shairi la mwisho la sura 7: "Wakakwenda kila mtu kwa nyumba yake, **lakini Yesu alikwenda kwa mlima wa Mizeituni."** Maneno Bwana aliyosema mbele yalikuwa kweli, ya kwamba "Mbweha wana pango, na ndege za anga wana vioto, lakini Mwana wa watu hana pahali pa kulalisha kichwa chake" (Mt. 8:20).

**8:2** Mlima wa Mizeituni ulikuwa karibu na hekalu. **Asubui mapema** Bwana Yesu alishuka mlima, akatambuka bonde la Kiduroni na kupanda ngambo yake kuingia mji, pahali pa **hekalu**. **Watu wote walifika karibu naye, naye aliketi kuwafundisha.**

**8:3** **Waandishi** (kazi yao ilikuwa kufanya miigo ya Maandiko Matakatifu na kuyafundisha ) **na Wafarisayo** walitaka sana kutega Bwana Yesu aseme neno lisilo taratibu. Walikuwa **wamefikisha** kwake **mwanamke aliyekamatwa** saa alipotenda **uzini,** wakamsimamisha katikati ya makutano yale, mbele ya Yesu.

**8:4** Walishitaki **mwanamke** juu ya uzini. **Alikamatwa** saa alipotenda zambi hii mbaya sana. Bila shaka mashitaki yao yalikuwa kweli. Basi mwanamume mwenyewe alikuwa wapi? Mara nyingi wanawake wanaazibiwa lakini wanaume walio na hatia vilevile hawapati azabu.

**8:5** Hila yao ilionekana wazi sasa. Walitaka Bwana kubisha **torati ya Musa.** Kama wakiweza kufanya hivi, wataweza kuongoza makutano kufikiri mabaya juu ya Yesu. Walikumbusha Bwana kwamba **katika torati Musa aliamuru** mtu namna hii **kuuawa kwa njia ya kutupiwa mawe.** Wafarisayo wenye makusudi maovu walitaraji kwamba Bwana Yesu hatakubali amri hii ya Musa, wakamwuliza kama alifikiri nini juu ya neno hili. Walifikiri ilikuwa lazima kusimamia haki na torati ya Musa kwa njia ya kuazibu mwanamke mbele ya watu. Kama Darby alivyosema,

> Moyo mwovu wa mtu unafarijiwa na kutulizwa wakati mtu anapokutana na mtu mwingine aliye hata mwovu kupita. Anafikiri zambi ya mtu huyu ni hata kubwa kupita yake mwenyewe, na wakati anapohukumu mtu mwingine na roho yote, anasahau uovu wake mwenyewe. Kwa njia hii anafurahi katika uzalimu (1 Kor. 13:6).[28]

**8:6** Hawakuwa na mashitaki kwa Bwana, lakini walijua kama akiacha mwanamke kwenda zake bila kumhukumu atashindana na torati ya Musa, nao wataweza **kumshitaki** kusema hatendi kwa haki. Lakini kama akihukumu mwanamke kufa, labda wataweza kutumika na neno hili kuonyesha kwamba yeye ni adui ya serikali ya Waroma, na ya kwamba alikosa rehema. **Lakini Yesu aliinama, akaandika kwa udongo kwa kidole chake.** Hakuna njia kwa sisi kujua kama aliandika nini kwani Biblia haitujulishi neno hili.

**8:7** Wayuda walikaa kumsukuma kuwajibu. Hivi Yesu alisema kwamba ingepasa mwanamke kuazibiwa namna torati ilivyoagiza, lakini ya kwamba ingepasa aazibiwe na wale wasiofanya zambi wao wenyewe. Hivi Bwana alisimamisha torati ya Musa. Hakusema kwamba haifai mwanamke kutopokea azabu iliyoamuriwa na Torati. Lakini alishitaki kila mmoja wa wanaume wale juu ya zambi zao wenyewe. Lazima wale wanaotaka kuhukumu wengine wawe safi wao wenyewe. Mara nyingi watu wanatumika na shairi hili kutoa uzuru juu ya zambi. Wanafikiri hawana hatia kwa sababu watu wote wengine wamefanya maneno mabaya. Lakini shairi hili si uzuru kwa kutenda zambi, lakini linahukumu wale waliofanya zambi hata kama hawakupatikana.

**8:8** Halafu Bwana **aliinama tena na**

**kuandika juu ya udongo**. Ni mara ya pekee tunayosoma juu ya Bwana akiandika maneno, na maneno aliyoandika yamefutwa zamani.

**8:9 Wale walioshitaki** mwanamke **walishitakiwa na zamiri zao wenyewe.** Hawakuwa na maneno mengine kusema. Walianza kwenda zao, wakitoka **mmoja mmoja**. Wao wote walikuwa na hatia, wakianza **toka wazee** hata vijana. **Yesu akabaki peke yake, na yule mwanamke akisimama** karibu.

**8:10** Na sauti ya neema Bwana alisema na mwanamke kwamba wote **ambao walimshitaki** walikuwa wameondoka! Hakuna mmoja wa makutano yale aliyejasiri kumshitaki.

**8:11** Wakati mwanamke alipojibu, **"Hapana mtu, Bwana,"** Bwana alimjibu na masemo haya matamu sana, **"Wala mimi sikuhukumu; kwenda, usifanye zambi tena."** Bwana hakuwa na amri ya serikali kuhukumu maneno namna hii. Ilikuwa amri ya serikali ya Waroma tu. Hakuhukumu wala kusamehe mwanamke. Hii haikuwa kazi yake kwa wakati ule. Lakini alimwonya asifanye zambi tena.

Ndani ya sura 1 ya Yoane tulisoma kwamba "neema na kweli zilikuja kwa njia ya Yesu Kristo." Tunaona mfano wa neno hili hapa. Masemo haya **"wala mimi sikuhukumu,"** ndiyo mfano wa neema; maneno ya **"kwenda, usifanye zambi tena"** ni masemo ya kweli. Bwana hakusema, "Jaribu kufanya zambi nusu tu." Yesu Kristo ni Mungu, na anasimamia ukamilifu kwa maneno yote. Hivi anaweka mbele yake njia bora ya Mungu mwenyewe.[8]

## G. Yesu nuru ya dunia (8:12-20)

**8:12** Maneno tutakayosoma sasa yalitokea katika chumba cha hazina hekaluni (ona sh.20). Watu wengi walikaa kufuata Bwana. Aligeuka kwao na moja la masemo yake makubwa mengi yanayoonyesha kwamba yeye ni Masiya. Alisema, **"Mini ni nuru ya dunia."** Dunia hii ni katika giza la zambi, ujinga, na ukosefu wa kusudi. **Nuru ya dunia** ni Yesu. Bila yeye hakuna njia kwa watu kufunguliwa toka giza la zambi. Bila yeye, hakuna neno kutuongoza, kutufahamisha maana ya uzima, na ya milele. Yesu aliahidi kwamba mtu ye yote ambaye anamfuata **hatakwenda kwa giza kabisa, lakini atakuwa na nuru ya uzima.**

Maana ya kufuata Yesu ni kumwamini. Watu wengi wanafikiri wanaweza kuishi kama Yesu alivyoishi bila kuzaliwa tena, lakini neno hili si kweli. Kufuata Yesu ni kufika kwake na roho ya toba, kumwamini kama Bwana na Mwokozi, kisha kutoa maisha yetu mazima kwake. Watu wanaofanya hivi wataongozwa naye kwa wakati wa maisha yao ya sasa na watakuwa na tumaini zuri sana kwa wakati unaofuata kaburi.

**8:13 Wafarisayo** walishindana na Yesu juu ya neno moja la sheria. Walimkumbusha kwamba alijishuhudia mwenyewe. Kwa macho ya watu ushuhuda wa mtu juu yake mwenyewe hautoshi kwa sababu mawazo ya mtu juu yake mwenyewe si sawa kila mara. Wafarisayo hawakuogopa kuonyesha shaka juu ya **kweli** ya masemo ya Yesu.

**8:14** Bwana alikubali kwamba ilikuwa lazima kwa washuhuda kuwa wawili au watatu. Lakini ndani ya maisha yake mwenyewe, **ushuhuda** wake ulikuwa **kweli** kwa sababu yeye ni Mungu. Alijua kwamba alikuja toka mbinguni na atarudi tena kule. Lakini wao **hawakujua pahali alipotoka na pahali atakapokwenda**. Walifikiri yeye ni mtu tu kama wao na walikataa kuamini kwamba alikuwa Mwana wa milele wa Mungu na sawa na Mungu Baba.

**8:15** Wafarisayo walihukumu watu kwa namna walivyoonekana kwa inje, maneno waliyoweza kuona na macho tu.

Walifikiri Yesu ni mseremala wa Nazareti na hawakufahamu kwamba alikuwa namna nyingine na mtu ye yote aliyeishi tangu zamani. Bwana Yesu alisema kwamba **hahukumu mtu**. Labda maana ya neno hili ni ya kwamba hakuhukumu kwa namna ya dunia, kama Wafarisayo walivyofanya. Au maana yake ni kwamba hakufika duniani *kuhukumu* watu lakini *kuwaokoa*.

**8:16 Kama** Bwana **angalihukumu**, **hukumu** yake ingalikuwa haki na **kweli.** Yeye ni Mungu na neno lo lote analofanya analifanya **pamoja na Baba ambaye alimtuma**. Bwana Yesu alionyesha tena na tena kwa Wafarisayo umoja wake na **Mungu Baba**. Ni neno hili lililoamsha uadui mchungu juu yake ndani ya roho zao.

**8:17,18** Bwana alikubali kwamba **torati** ya Musa iliagiza kwa **washuhuda kuwa wawili**. Hakuna neno ambalo alisema lilibisha neno hili.

Kama wakitaka sana kuwa na washuhuda wawili, haikuwa nguvu kupata washuhuda hawa. Kwanza, ali**jishuhudia** mwenyewe kwa njia ya maisha yake bila zambi na masemo yake safi yaliyotoka kinywa chake. Vilevile **Baba alishuhudia** Bwana Yesu kwa njia ya maneno aliyosema juu yake toka mbingu na maajabu ambayo alimpa kufanya. Kristo alitimiza unabii katika Agano la Kale juu ya Masiya, lakini hata hivi viongozi wa Wayuda walikataa kuamini.

**8:19** Bila shaka Wafarisayo waliuliza na sauti ya kuzarau, **"Baba yako yuko wapi?" Yesu aliwajibu** ya kwamba hawakutambua kama yeye ni nani na hawakujua **Baba** yake. Bila shaka wangebisha na nguvu kwamba hawajui Mungu lakini ilikuwa kweli hata hivi. Kama wangepokea Yesu Kristo, **wangejua Baba yake vilevile.** Lakini hakuna mtu anayeweza kujua Mungu Baba ila kwa njia ya Yesu Kristo. Hivi kwa sababu walikataa Mwokozi, hawakuweza kusema na roho ya kweli kwamba walijua na kupenda Mungu.

**8:20** Hapa tunaona kwamba mambo tuliyosoma juu yao ndani ya mashairi yaliyotangulia yalitukia katika **chumba cha hazina hekaluni.** Mara hii vilevile Bwana alilindwa na Mungu, na **hakuna mtu** aliyeweza **kumkamata** au kumwua. **Saa yake ilikuwa haijakuja bado. Saa ile** ndiyo wakati atakaposulibishwa kwa Kalvari kufa kwa zambi za dunia.

### H. Mabishano ya Wayuda na Yesu (8:21-59)

**8:21 Yesu** alionyesha tena kwamba alijua maneno yote yatakayotokea. Aliwaambia wajuzi wake ya kwamba **atakwenda zake** – hakufikiri mauti na kuzikwa kwake tu, lakini ufufuko wake vilevile na kupanda kurudia mbingu. Wayuda **watatafuta** Masiya, bila kufahamu kwamba alikuwa amewafikia, nao walikataa kumpokea. Kwa sababu hii **watakufa katika zambi zao**. Maana ya maneno haya ndiyo ya kwamba kwa milele watazuizwa wasiingie mbinguni pahali Bwana alipokuwa akikwenda. Ni kweli ya kuogopesha! Wale wanaokataa kupokea Bwana Yesu wanakosa tumaini la kufikia mbingu. Ni neno la kuogofya kufa bila usamehe wa zambi, bila Mungu, bila Kristo, bila tumaini kwa milele!

**8:22 Wayuda** hawakufahamu kwamba Bwana alikuwa akisema juu ya kurudia mbingu. Maana ya "nitakwenda zangu" ilikuwa nini? Ataepuka shauri lao kumwua kwa njia ya kujiua mwenyewe? Kwa nini watafikiri hivi? Kama **akijiua mwenyewe**, hakuna neno kuwazuiza kufanya vivyo vilevile na kumfuata ndani ya mauti yake. Habari hizi zinaonyesha tena giza la kutoamini. Ujinga wao wa maana ya maneno Bwana aliyosema ni neno la kutushangaza kabisa!

**8:23** Bila shaka Bwana alifikiri juu ya ulizo lao la upumbavu kwamba atajiua

mwenyewe wakati aliposema nao, **“Munatoka chini.”** Mawazo yao yote yalikuwa juu ya maneno ya chini, ya dunia hii tu, ya wakati wa sasa tu. Hawakuwa na ufahamu wa maneno ya roho hata kidogo. Lakini Kristo **alitoka juu**. Mawazo, masemo na matendo yake yote yalikuwa ya mbingu. Maneno yote wao waliyotenda yalikuwa ya **dunia hii**, lakini maisha yake mazima yalifikirisha watu maneno ya mbingu.

**8:24** Mara nyingi Bwana alisema neno mara mbili kuonyesha kwamba ni neno kubwa. Hapa alionya watu tena kwamba watakufa katika zambi zao kama wakikaa kukataa kumwamini. Hakuna njia nyingine kupata usamehe wa zambi, na wale **wanaokufa** na **zambi** zisizosamehewa hawawezi kuingia mbinguni nyuma ya kufa.

**8:25** Wayuda walifazaishwa kabisa na mafundisho ya Bwana Yesu. Basi walimwuliza kama **yeye ni nani.** Ni kama waliuliza hivi na kuzarau, “Unafikiri wewe ni nani hata unasema nasi hivi?” Au labda walitaka kusikia kweli kama atasema nini juu yake mwenyewe. Tufikiri sana juu ya jibu lake: **“Sawasawa nilivyowaambia ninyi tangu mwanzo.”** Alikuwa Masiya ambaye walisikia habari zake tena na tena toka Bwana Yesu, lakini walikuwa wakaidi na walikataa kunyenyekea kweli hii. Lakini jibu lake linaweza kuwa na maana nyingine vilevile – mwenendo wa Bwana Yesu ulipatana kabisa na mahubiri yake. Hakusema neno fulani na kutenda neno lingine. Alionyesha ndani ya maisha yake maneno yote aliyofundisha. Maisha yake yalipatana na mafundisho yake.

**8:26** Maana ya shairi hili haionekani wazi. Ni kama Bwana Yesu alisema ya kama kulikuwa na **maneno mengi mengine** aliyoweza **kusema** na **kuhukumu** juu ya Wayuda hawa wasioamini. Angeweza kufunua wazi mawazo maovu mioyoni mwao. Lakini alisema maneno yale tu ambayo Baba alimpa kusema. Na Baba akiwa **kweli,** anastahili kwa sisi kumwamini na kumsikiliza.

**8:27** Wayuda **hawakufahamu** ya kwamba **Yesu** alikuwa akisema **nao juu ya** Mungu **Baba**. Ni kama ufahamu wao ulikaa kupunguka. Mbele wakati aliponyesha kwamba alikuwa Mwana wa Mungu, walifahamu kwamba alisema yeye ni sawa na Mungu Baba. Hawakufikiri juu ya neno hili sasa.

**8:28** Halafu **Yesu** alitabiri tena maneno yatakayotokea. Kwanza Wayuda watanyanyua **Mwana wa watu**, maana watamsulibisha. Wakati watakapokwisha kufanya hivi **watajua** kwamba alikuwa Masiya. Watajua kwa sababu ya tetemeko la inchi na giza, lakini zaidi kwa sababu ya ufufuko wake toka wafu. Ona masemo yake, **“Mutafahamu ya kuwa mimi** ***ndiye.*****”** Neno hili *ndiye* si ndani ya Kiyunani. Hivi maana ya ndani kupita ni **“Mutafahamu kwamba mimi ni** Mungu.” Halafu watafahamu kwamba hakufanya neno lo lote kwa amri yake mwenyewe, lakini alikuja duniani kama mwenye kutegemea Baba na alisema maneno yale tu ambayo **Baba alimfundisha** kusema.

**8:29, 30** Ushirika wa Bwana na Mungu Baba ulikuwa kamili sana. Masemo haya yote yalionyesha umoja wake na Mungu. Kwa muda mzima wa utumishi wake duniani Baba alikuwa **pamoja naye.** Hakumwacha **pekee** saa yo yote. Kwa kila wakati Yesu alifanya maneno yaliyopendeza Mungu. Maneno haya yaliweza kusemwa na Mmoja asiyekuwa na zambi tu. Hakuna mtu aliyezaliwa na wanadamu aliyeweza kusema na roho ya kweli, **“Ninafanya saa zote maneno ambayo yanampendeza.”** Mara nyingi zaidi tunafanya maneno ambayo yanatupendeza sisi wenyewe. Wakati na wakati tunafanya maneno kupendeza watu wengine. Bwana Yesu tu alijazwa na hamu kufanya maneno yaliyopendeza Mungu.

**Wakati aliposema maneno haya** mazuri sana, Yesu alikuta kwamba watu **wengi** walisema walimwamini. Bila shaka wengine walikuwa waamini wa kweli.

**8:31** Halafu **Yesu** alionyesha tofauti ya wale waliokuwa wanafunzi na wale waliokuwa **wanafunzi** wake **wa kweli.** Mwanafunzi ndiye mtu ye yote anayekiri kuwa mwenye kujifunza, lakini **mwanafunzi wa kweli** ndiye aliyejitoa kabisa kufuata Bwana Yesu Kristo. Waamini wa kweli ndio wale **wanaokaa katika Neno** lake. Wanaendelea ndani ya mafundisho ya Kristo. Hawaachi kumfuata. Wenye imani ya kweli ndio watu wanaodumu katika imani. Hawaokolewi kwa njia ya kukaa ndani ya Neno lake, lakini wanakaa ndani ya Neno lake kwa sababu wameokolewa.

**8:32** Ahadi ndani ya shairi hili ni kwa kila mwanafunzi wa kweli: **Atajua kweli, na kweli itamweka huru.** Wayuda hawakujua kweli, nao walikuwa katika utumwa kabisa. Walikuwa watumwa wa ujinga, makosa, zambi, sheria, na uchawi. Watu wanaojua Bwana Yesu kweli wanafunguliwa toka utumwa wa zambi, wanatembea katika nuru, na wanaongozwa na Roho Mtakatifu.

**8:33** Wengine wa Wayuda waliosimama karibu walisikia maneno Bwana aliyosema juu ya kuwekwa huru, na walichukizwa nayo. Walijivuna juu ya kuwa wazao wa Abrahamu na walisema kwamba **hawakuwa katika utumwa kamwe.** Lakini hawakusema kweli. Taifa lao walikuwa watumwa wa Wamisri, Waasuria, Wababeli, Wapersi, Wayunani na sasa wa Waroma. Lakini zaidi ya ile, hata saa walipokuwa wakisema na Bwana Yesu walikuwa watumwa wa zambi na Shetani.

**8:34** Ni wazi ya kwamba Bwana alikuwa akisema juu ya **utumwa wa zambi.** Alikumbusha wasikiaji Wayuda ya kwamba **mtu ye yote anayetenda zambi ni mtumwa wa zambi.** Wayuda hawa walijionyesha kuwa watu wa dini kabisa, lakini hawakutenda kwa haki, hawakuwa na heshima kwa Mungu, lakini watageuka wauaji nyuma kidogo – kwa sababu hata kwa saa ile walikuwa wakifanya shauri kuua Mwana wa Mungu.

**8:35** Halafu Yesu alisawanisha **mtumwa** wa mtu na **mwana** wa mtu huyu. **Mtumwa** hajui kama atakaa nyumbani mwa mtu huyu kwa muda gani, lakini **mwana** anajua hii ni nyumba yake daima. Hatujui kama Yesu alikuwa akisema juu ya Mwana wa Mungu au juu ya wale watakaogeuka watoto wa Mungu kwa njia ya kuamini Kristo, lakini tunajua alikuwa akiwaambia Wayuda hawa kwamba hawakuwa wana, lakini watumwa, na waliweza kuondoshwa nyumbani kwa saa yo yote.

**8:36** Ni wazi kwamba "**Mwana**" ndani ya shairi hili ni Kristo mwenyewe. Wale **wanaofunguliwa** naye ni **huru kweli.** Ni kusema kwamba wakati mtu anapofika karibu na Mwokozi na kupewa uzima wa milele naye, anafunguliwa toka utumwa wa zambi namna zote.

**8:37** Bwana alikubali ya kwamba kwa njia ya uzao wa mwili, Wayuda hawa walikuwa **wazao wa Abrahamu**, lakini ilionekana kwamba hawakuwa uzao wake kwa maneno ya *roho*. Hawakuwa wenye kupenda Mungu kama Abrahamu. Walitafuta njia **kuua** Bwana Yesu kwa sababu mafundisho yake hayakupata **nafas**i ndani ya roho zao. Ni kusema kwamba hawakuacha maneno ya Kristo kuzaa matunda ndani ya maisha yao. Walishindana na mafundisho yake na walikataa kumnyenyekea.

**8:38** Maneno ambayo Yesu aliwafundisha ndiyo yale aliyoagizwa na **Baba** yake kusema. Yeye na Baba yake walikuwa moja kabisa hata maneno aliyosema yalikuwa maneno ya Mungu Baba. Bwana Yesu alikuwa onyesho kamilifu la Baba yake wakati alipokuwa

hapa duniani. Lakini Wayuda walifanya maneno ambayo walijifunza na **baba** yao. Bwana Yesu hakusema juu ya baba yao ya dunia, lakini juu ya *Shetani.*

**8:39** Wayuda walikaa kusema kwamba **Abrahamu** alikuwa **mzazi** wao. Walijivuna kwa sababu **Abrahamu** alikuwa **baba** yao. Lakini Bwana Yesu alionyesha kwamba hata wakiwa *uzao* wa Abrahamu (sh.37), hawakuwa **watoto** wake. Mara nyingi watoto wanatembea, kusema na kufanana na wazazi wao. Lakini haikuwa hivi na Wayuda hawa. Maisha yao yalikuwa namna nyingine na maisha ya Abrahamu. Hata kwa njia ya mwili walikuwa wazao wa Abrahamu, kwa njia ya roho walikuwa watoto wa Shetani.

**8:40** Halafu Yesu alionyesha wazi kabisa kwa njia gani walikuwa namna nyingine na Abrahamu. Yesu alifika duniani kusema nao maneno ya **kweli** tu. Wao walichukizwa na kukwalishwa na mafundisho yake na walijaribu **kumwua. Abrahamu hakufanya hivi,** lakini alifungana na kweli na haki.

**8:41** Ilionekana wazi kabisa kama baba yao alikuwa nani kwa sababu walitenda namna yeye alivyotenda. Walifanya **kazi za baba yao,** ndiye Shetani. Labda Wayuda walishitaki Yesu juu ya **kuzaliwa katika uzini**, lakini walimu wengi wanafikiri neno hili lilisema juu ya kuabudu sanamu. Wayuda walikuwa wamesema kwamba hawakutenda uzini wa roho kamwe. Tangu zamani waliabudu **Mungu** mmoja wa kweli tu na kumwita Yeye tu **Baba** yao.

**8:42** Bwana Yesu alionyesha masemo yao hayakuwa kweli, na kama wangalipenda Mungu **wangalimpenda** Yule **aliyetumwa** na Mungu. Ni upumbavu kwa mtu kusema anapenda Mungu pamoja na kuchukia Bwana Yesu Kristo. Yesu alisema **alitoka kwa Mungu,** maana yake alikuwa Mwana wa Mungu tangu milele. Aliwakumbusha vilevile kwamba **alikuja toka Mungu.** Ni wazi ya kwamba alisimama pale katikati yao. Alikaa mbinguni pamoja na Baba muda mrefu mbele ya kutokea hapa duniani. Lakini Baba **alimtuma** duniani kuwa Mwokozi wa dunia, naye akiwa mwenye kutii, alifika.

**8:43** Ndani ya shairi hili tunasoma juu ya **usemi** na **neno**. **Neno** la Kristo ndilo maneno aliyofundisha. **Usemi** wake ndio maneno ambayo alitumika nayo kueleza kweli alizofundisha. **Iliwashinda kufahamu hata usemi wake.** Wakati aliposema juu ya mkate, walifikiri juu ya mkate tunaokula hapa duniani. Wakati aliposema juu ya maji, hawakufahamu kwamba alisema juu ya maji ya roho. Kwa nini iliwashinda kufahamu usemi wake? Kwa sababu hawakuwa tayari kupokea mafundisho yake.

**8:44** Sasa Bwana Yesu alisema waziwazi kabisa kwamba **Shetani** alikuwa **baba** yao. Si kusema kwamba walizaliwa na Shetani namna waamini wanavyozaliwa na Mungu. Wao ni watoto wa Shetani kwa njia ya *kumwiga* na kuishi namna yeye alivyoishi. **“Tamaa za baba yenu munataka kuzifanya”** – hii ilikuwa hamu ya mioyo yao.

Shetani alikuwa **mwuaji tangu mwanzo.** Alileta mauti kwa Adamu na watu wote wa dunia. Hakuwa **mwuaji** tu, lakini alikuwa **mwongo vilevile**. **Hakukaa katika kweli kwa sababu hakuna kweli ndani yake.** Wakati aliposema **uwongo, alisema yaliyo yake mwenyewe,** kwa sababu **yeye ni mwongo, na baba ya wongo**. Wayuda waliiga Shetani kwa njia hizi. Walikuwa wauaji kwa sababu walikusudi mioyoni mwao kuua Mwana wa Mungu. Walikuwa wawongo kwa sababu walisema Mungu ni Baba yao. Walitenda kama watu wa Mungu, lakini maisha yao yalikuwa maovu.

**8:45** Ni kama watu ambao wanajitoa kusema uwongo hawawezi kutambua

kweli tena. Bwana Yesu alikuwa akisimama mbele yao naye alisema **kweli** kila mara. Lakini **walikataa kumwamini.** Neno hili lilionyesha uovu wa roho zao.

**8:46** Kristo tu, Mwana wa Mungu aliye bila zambi, aliweza kusema maneno namna hii. Hakuna mtu duniani aliyeweza kuhakikisha kwamba alikuwa na **zambi** hata moja. Tabia yake haikuwa na upungufu. Matendo yake yote yalikuwa makamilifu. Alisema maneno ya kweli tu, lakini hata hivi **hawakumwamini**.

**8:47** Mtu akipenda Mungu na mapendo ya kweli, atasikia na kutii **maneno ya Mungu**. Wayuda walionyesha kwa njia ya kukataa mafundisho ya Mwokozi ya kwamba hawakuwa watu wa **Mungu**. Shairi 47 linaonyesha wazi kwamba maneno Bwana Yesu aliyosema yalikuwa maneno ya Mungu mwenyewe.

**8:48 Wayuda** walitukana Bwana Yesu tena kwa sababu walishindwa kumjibu kwa njia yo yote nyingine. Wakati walipomwita **Msamaria** ni kama walisema hakuwa Myuda wa kweli, lakini adui ya Israeli. Na walisema vilevile kwamba alikuwa na **pepo**, wakifikiri alikuwa mwenye wazimu. Walifikiri mwenye wazimu tu aliweza kusema maneno kama yale Yesu aliyosema juu yake mwenyewe.

**8:49** Ona **namna Yesu alivyojibu** adui zake bila kukasirika. Mafundisho yake hayakuwa masemo ya mwenye **pepo**, lakini ya mmoja mwenye bidii **kuheshimu** Mungu **Bab**a. Hawakumlaumu kwa sababu walifikiri alikuwa mwenye wazimu, lakini kwa sababu aliweka roho kabisa juu ya maneno ya Baba yake mbinguni.

**8:50** Ingaliwapasa kujua kwamba **hakujitafutia mwenyewe utukufu** wakati wo wote. Kusudi la maneno yote aliyofanya lilikuwa kutukuza Baba yake. Hata kama alisema hawakumheshimu yeye, maana ya masemo haya haikuwa kwamba **alijitafutia mwenyewe utukufu.** Halafu aliongeza kusema, **"Yuko mmoja anayetafuta na kuhukumu."** Alisema juu ya Mungu. Mungu Baba atatafuta utukufu kwa Mwana wake mpendwa, na atahukumu wote watakaokataa kumtukuza.

**8:51** Hapa tunaona lingine la masemo ya ajabu na enzi ya Bwana Yesu ambalo linaweza kusemwa tu na Mmoja aliye Mungu. Linaanza na maneno tuliyoona mbele kutufahamisha ukubwa wao: **"Kweli, kweli ninawaambia ninyi."** Yesu aliahidi kwamba **mtu akishika neno** lake, mtu huyu **hataona kufa hata milele**. Maana ya kufa hapa si *mauti ya mwili,* kwani waamini wengi wanakufa kila siku. Bwana Yesu alisema juu ya **kufa** *kwa roho.* Alisema kwamba wale ambao wanamwamini wataponyeshwa toka **mauti** ya milele na maumivu katika Gehena.

**8:52** Sasa **Wayuda** walifikiri hata kupita mbele ya kwamba Yesu alikuwa mwenye pepo. Walimkumbusha kwamba **Abrahamu** na **manabii walikufa** wote. Tena Yesu alisema mtu **ye yote akishika neno lake hataona kufa hata milele.** Maneno haya yanapatana namna gani?

**8:53** Walifahamu kwamba Bwana alikuwa akisema yeye ni **mkubwa kupita baba yao Abrahamu** na **manabii**. Abrahamu hakuponyesha mtu ye yote kamwe toka mauti, na hakuweza kujiponyesha mwenyewe. Vivyo hivyo na manabii. Lakini Yesu alisema aliweza kuponyesha watu toka mauti. Bila shaka alifikiri yeye ni mkubwa kupita baba zao.

**8:54** Wayuda walifikiri Yesu alitaka kukokota mafikiri ya watu juu yake mwenyewe. **Yesu** aliwakumbusha kwamba haikuwa hivi. Alikuwa **Baba** ambaye alimtukuza, **Mungu** yule ambaye walisema walipenda na kutumikia.

**8:55** Wayuda walisema Mungu ni Baba yao, lakini hawakumjua. Lakini walikuwa wakisema na mmoja ambaye **alijua** Mungu Baba *kweli,* na aliyekuwa

sawa naye. Walitaka Yesu kukataa kwamba yeye ni sawa na Baba, lakini Yesu alisema kama akifanya hivi atakuwa **mwongo**. Alijua Mungu Baba na kushika **neno lake**.

**8:56** Kwa sababu Wayuda walikaa kutaja Abrahamu ndani ya mabishano yao, Bwana aliwakumbusha kwamba Abrahamu alitazamia **siku** ya Masiya, na ya kwamba **aliiona** kwa imani na **alifurahi**. Bwana Yesu alikuwa akisema kwamba Abrahamu alikuwa akitazamia Yeye. Abrahamu aliamini kwamba atakuja.

Abrahamu aliona siku ya Kristo wakati gani? Labda ilikuwa wakati alipopeleka Isaka kwa Mlima Moria kumtoa kama zabihu ya kuteketezwa kwa Mungu. Maneno yote yaliyotokea siku ile yalikuwa mfano wa mauti ya Masiya na ufufuko wake, na labda Abrahamu aliyaona kwa imani. Hivi Bwana Yesu alisema unabii wote ndani ya Agano la Kale juu ya Masiya ulitimizwa ndani yake mwenyewe.

**8:57 Wayuda** walionyesha tena ya kwamba iliwashinda kufahamu kweli ya Mungu. Yesu alikuwa amesema "Abrahamu alifurahi kuona siku yangu," lakini jibu la Wayuda lilionyesha kwamba walifikiri alisema ameona Abrahamu. Lakini Bwana Yesu alikuwa akisema kwamba yeye ni mkubwa kupita Abrahamu. Abrahamu alimtazamia na kumtumainia yeye. Abrahamu alitazamia siku ya Kristo na imani.

Wayuda hawakuweza kufahamu neno hili. Walisema Yesu **hakufika bado miaka makumi tano.** (Alikuwa na miaka karibu makumi tatu na tatu tu kwa wakati ule.) Aliweza **kuona Abrahamu namna gani?**

**8:58** Bwana Yesu alionyesha tena wazi kwamba yeye ni Mungu. Hakusema **"Mbele Abrahamu hajazaliwa, mimi** *nilikuwa.*" Kama angalisema hivi watu wangaliweza kufikiri alianza kuwa mbele ya Abrahamu. Hivi alitumika na jina la Mungu: **Mimi NIKO**. Bwana Yesu alikaa pamoja na Mungu Baba tangu milele. Hakuna siku alipoanza kuwa. Hivi alisema, **"Mbele Abrahamu hajazaliwa, mimi NIKO."**

**8:59** Wayuda walijaribu kuua Yesu mara moja, lakini **"Yesu akajificha, akatoka hekalu."** Wayuda walifahamu maana ya maneno Yesu aliyosema. "Mbele Abrahamu hajazaliwa, mimi NIKO." Alikuwa akisema kwamba yeye ni BWANA! Kwa mafikiri yao, haya yalikuwa masemo ya ukufuru, na kwa sababu hii walitaka kumtupia mawe. Hawakuwa tayari kuamini kwamba Masiya alikuwa akisimama pale katikati yao. Walikataa kutawaliwa naye!

**I. Alama ya sita: Kuponyeshwa kwa mtu aliyezaliwa kipofu (9:1-12)**

**9:1** Labda neno hili lilitukia **wakati Yesu** alipokuwa akiondokea hekalu au muda fulani nyuma ya habari tulizosoma ndani ya sura 8. Mtu huyu alikuwa **kipofu tangu kuzaliwa kwake**. Hakuwa na tumaini hata nusu kwamba ataweza kuona siku nyingine, ndilo neno linaloonyesha wazi ukubwa wa ajabu ambalo lilimwezesha kuona.

**9:2 Wanafunzi waliuliza** kama upofu wake ulikuwa tunda la zambi yake mwenyewe au tunda la zambi ya wazazi wake. Basi upofu wake uliweza kuwa tunda la zambi yake mwenyewe kama alikuwa **kipofu** *tangu kuzaliwa* kwake? Walifikiri kwamba alizaliwa kipofu kwa sababu ya zambi ambazo Mungu alijua atafanya nyuma ya kuzaliwa? Ni wazi ya kwamba walifikiri upofu wake ulikuwa tunda ya zambi katika jamaa yake. Tunajua neno hili si kweli kila mara. Ndiyo, ugonjwa, mateso na mauti ziliingia duniani kama tunda la zambi, lakini *si* kweli ya kwamba mateso ya mtu fulani ni matunda ya zambi zake kila mara.

**9:3** Yesu hakusema kwamba mtu huyu hakutenda zambi, wala wazazi wake,

lakini ya kwamba upofu huu haukuwa tunda la zambi ndani ya maisha yao. Mungu aliruhusu mtu huyu kuzaliwa kipofu kusudi **kazi za uwezo za Mungu** ziweze kuonekana kwa njia yake. Hata mbele ya kuzaliwa kwa mtu huyu Bwana Yesu alijua kwamba atamwezesha kuona.

**9:4** Mwokozi alifahamu kwamba alikuwa na miaka karibu mitatu kwa utumishi wake katikati ya watu mbele ya kusulibishwa. Sharti atumike na kila dakika kwa kazi ya Mungu. Kulikuwa na mtu hapa aliyezaliwa kipofu. Ilikuwa lazima kwa Bwana kufanya ajabu kuponyesha mtu huyu, si neno kama ilikuwa siku ya sabato. Muda wa kazi yake katikati ya watu utakwisha nyuma kidogo, naye hatakuwa duniani tena. Neno hili ni onyo la nguvu kwa kila Mkristo kwamba siku za maisha yetu zinapita mbio mbio, na **usiku unakuja** wakati kazi yetu hapa duniani itakapokwisha. Ni lazima kutumika na saa tulizo nazo kutumikia Bwana vizuri.

**9:5** Wakati Yesu alipokuwa **duniani** kama mtu, alikuwa **nuru ya dunia** waziwazi. Wakati alipopita katikati ya watu akifanya maajabu na akifundisha watu, waliona **nuru ya dunia** na macho yao. Bwana Yesu ni nuru ya dunia leo vilevile na anaahidi wote wanaofika kwake kwamba hawatatembea katika giza. Lakini ndani ya shairi hili alisema zaidi juu ya utumishi wake hapa duniani.

**9:6** Hatusomi kwa sababu gani Bwana alichanganya **mate** na **udongo** kuweka juu ya **macho ya kipofu.** Watu wengine wanafikiri ya kwamba wakati Bwana alipofungua macho ya wapofu alitumika na vitu zaifu visivyokuwa na faida kutimiza makusudi yake. Hata sasa anatumika na wanaume na wanawake waliofanywa toka mavumbi tu, kufungua macho ya wapofu rohoni.

**9:7** Halafu Bwana alisema na kipofu kuonyesha imani yake kwa njia ya **kwenda** na **kunawa katika birika ya Siloamu.** Hata kama alikuwa kipofu tunafikiri alijua pahali pa birika na aliweza kwenda kutii agizo la Bwana. Maana ya **Siloamu** ilikuwa **Kutumwa,** na inatufikirisha Masiya "aliyetumwa". Yule aliyefanya ajabu hili alitumwa hapa duniani na Mungu Baba. Kipofu **alikwenda na kunawa**, akarudi akiona. Haifai kusema alipata *kuona tena* kwani hii ilikuwa mara ya *kwanza* aliyoweza kuona. Ajabu hili lilifanyikana palepale na mtu mwenyewe aliweza kuona mara moja. Bila shaka alishangaa kabisa wakati alipoona mara ya kwanza dunia hii pahali alipokaa!

**9:8, 9** **Jirani** za mtu huyu walishituka kabisa. Ilikuwa nguvu kwao kuamini kwamba huyu ndiye mtu **aliyekaa na kuomba** zawadi miaka ile yote. (Ingepasa kuwa hivi kila mara wakati mtu anapopata wokovu. Ingepasa jirani zetu kuweza kuona kwamba tumegeuka.) **Wengine** walisema ndiye aliyekuwa kipofu mbele. **Wengine** walikuwa na shaka kidogo, wakasema anafanana naye. Lakini mtu mwenyewe aliondosha mashaka yote, akasema wazi kwamba alizaliwa kipofu.

**9:10** Maajabu yote ya Yesu yalizaa maulizo namna namna ndani ya roho za watu. Mara nyingine maulizo haya yalileta njia kwa mwamini kushuhudia Bwana. Hapa watu waliuliza kama neno hili lilifanyikana **namna gani.**

**9:11** Ushuhuda wa mtu huyu haukuwa nguvu kuamini. Alipasha tu ya kwamba aliponyeshwa akileta utukufu kwa yule aliyefanya ajabu hili. Kwa saa ile mtu huyu hakufahamu kama Yesu alikuwa nani. Alimwita tu, **"Mtu anayeitwa Yesu."** Lakini nyuma ufahamu wake uliongezeka na alifahamu kama Yesu ni nani.

**9:12** Mara nyingi wakati tunaposhuhudia Bwana Yesu Kristo tunaamsha hamu ndani ya watu wengine kumjua vilevile.

**J. Ushindani wa Wayuda unakaa kuongezeka (9:13-41)**

**9:13** Ni kama watu walitenda na roho nzuri wakati **walipopeleka** huyu aliyekuwa **kipofu** mbele karibu na **Wafarisayo**. Labda hawakufahamu kwamba viongozi vya dini watachukizwa na kuponyeshwa kwa mtu huyu.

**9:14** Yesu alikuwa amefanya ajabu hili siku ya **sabato**, lakini Wafarisayo hawakufahamu kwamba halikuwa kusudi la Mungu kamwe kukataza matendo ya rehema na wema kutendwa siku ile.

**9:15** Basi mtu huyu alipata njia tena kushuhudia Yesu. Wakati **Wafarisayo** vilevile walipomwuliza **namna gani alivyopata kuona,** akawaambia habari zenyewe vilevile. Hakutaja jina la Yesu mara hii. Hatufikiri kwamba alizuizwa na woga, lakini kwa sababu alifahamu karibu watu wote walijua ni nani aliyefanya tendo hili la ajabu. Kwa wakati huu Bwana Yesu alijulikana katikati ya watu wa Yerusalema.

**9:16** Sasa kulikuwa na **mtengo** tena juu ya Yesu. Alikuwa nani? **Wengine wa Wafarisayo** walitangaza na ujasiri kwamba Yesu si mtu wa Mungu, kwa sababu alifanya neno hili siku ya **sabato. Wengine** walifikiri mwenye zambi hawezi kufanya ajabu kubwa namna hii. Hivi watu walilazimishwa kuchagua kama watasimama kwa upande wa Wafarisayo au wa Yesu.

**9:17** Wafarisayo waliuliza **mtu aliyekuwa kipofu mbele** kama alifikiri nini juu ya Yesu. Kwa saa ile mtu huyu hakufahamu kwamba Yesu ni Mungu. Lakini imani yake ilikuwa imepata nguvu kidogo, na alisema Yesu ni **nabii**. Aliamini ya kwamba yule aliyefungua macho yake alitumwa na Mungu, na alikuwa na habari toka Mungu.

**9:18, 19** Wengi wa **Wayuda** hawakuwa tayari **kuamini** kwamba ajabu lilifanyikana. Basi **waliita wazazi** wa mtu huyu kuona kama watasema nini.

Nani atajua vizuri kupita wazazi kama mtoto wao alizaliwa kipofu? Bila shaka maneno watakayosema yataondosha mashaka ndani ya roho za watu. Hivi Wafarisayo **waliwauliza** kama huyu alikuwa **mwana** wao na **namna gani** aliwezeshwa kuona.

**9:20, 21** Ushuhuda wa **wazazi wake** ulikuwa wazi. **Huyu** alikuwa **mwana** wao kweli na kwa miaka ile yote ya huzuni alikuwa **kipofu**.

Walikataa kuongeza habari nyingine. **Hawakujua** namna gani aliweza kuona sasa au yeye **nani** aliyefungua macho yake. Walisema Wafarisayo waulize mwana wao wao wenyewe. Ataweza kujibu **yeye mwenyewe.**

**9:22,23** Shairi 22 linaeleza woga wa **wazazi**. Walikuwa wamesikia ya kwamba mtu ye yote akikiri kwamba Yesu ni Masiya **atafukuzwa toka sunagogi.** Kutokezwa hivi ilikuwa hatari kubwa kwa Myuda. Atapoteza njia kujipatia mali kwa mahitaji yake, na faida yote ya dini ya Wayuda. **Kwa sababu hii wazazi** walisema na Wafarisayo waulize mwana wao.

**9:24 "Umpe Mungu utukufu!"** Inawezekana kutafsiri maneno haya kwa njia mbili. Kwanza yalikuwa kama kiapo. Labda Wafarisayo walikuwa wakisema, "Sema kweli. **Tunajua mtu huyu ni mwenye zambi.**" Au labda Wafarisayo walitaka Mungu tu atukuzwe kwa ajabu hili, si Yesu, kwa sababu walifikiri Yesu ni mwenye zambi.

**9:25** Wafarisayo walishindwa tena na tena. Kila mara walipojaribu kuaibisha Bwana Yesu, aliheshimiwa kupita mbele. Ushuhuda wa mtu huyu ulikuwa mtamu sana. **Hakujua maneno mengi** juu ya Bwana Yesu. lakini **alijua neno hili** kabisa: "Mimi **nilikuwa kipofu, na sasa** ninaona." Hawakuweza kubisha ushuhuda huu.

Ni vivyo hivyo na watu wanaozaliwa tena. Hata watu wa dunia wakiwa na

shaka, hata wakicheka na kuzarau, hawawezi kubisha ushuhuda wetu kwamba mbele tulikuwa wapotevu, lakini sasa tumeokolewa kwa neema ya Mungu.

**9:26,27** Wafarisayo walianza kuuliza **tena,** awajulishe kama neno hili lilifanyikana namna gani. Sasa yule aliyekuwa kipofu mbele alianza kukasirika. Aliwakumbusha kwamba **aliwaambia maneno haya mbele** nao **hawakusikiliza**. **Kwa sababu gani walitaka kusikia tena?** Walitaka kugeuka **wanafunzi** wa Yesu? Bila shaka aliuliza neno hili na roho ya kutia uchungu. Alijua kwamba walichukia Yesu, na hawakutaka kumfuata hata kidogo.

**9:28** Wafarisayo walishindwa kabisa kugeuza ushuhuda wa mtu huyu, hivi walianza kumtukana. Walimshitaki kuwa **mwanafunzi** wa Yesu, wakionyesha neno hili kuwa baya sana! Na walikiri kwamba wao walikuwa **wanafunzi wa Musa,** wakionyesha kwamba neno hili ni zuri zaidi.

**9:29** Walisema **Mungu alisema na Musa,** lakini walisema na kuzarau juu ya Yesu. Kama wangaliamini maandiko ya Musa, wangalipokea Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wao. Na kama wangalifikiri kidogo, wangalikumbuka kwamba Musa hakuwezesha kuona hata mtu mmoja aliyezaliwa kipofu. Huyu aliyesimama katikati yao alikuwa mkubwa kupita Musa, lakini hawakufahamu neno hili.

**9:30** Sasa majibu ya mtu huyu yaligeuka makali, akasema na Wafarisayo maneno kama haya: "Ninyi ni watawala katika Israeli na walimu wa Wayuda. Halafu Mtu mmoja anasimama katikati yenu anayewezesha kipofu kuona, nanyi **hamujui pahali anapotoka**. Haya yenu!"

**9:31** Mtu huyu alikaa kuongezeka katika uhodari na imani. Alikumbusha Wafarisayo kwamba si desturi ya Mungu **kusikia wenye zambi** au kufanya maajabu kwa njia yao. Mungu hakubali watu waovu, wala kuwawezesha kufanya kazi za uwezo. Lakini waabudaji wa **Mungu** wanakubaliwa naye.

**9:32,33** Mtu huyu alifahamu ya kwamba tangu zamani ya kale yeye ni mtu wa kwanza **aliyezaliwa kipofu**, na kuwezeshwa kuona. Ilimshinda kufahamu namna gani Wafarisayo waliweza kuona ajabu hili pamoja na kushitaki mwenye kulitenda.

**Kama** Bwana Yesu **asingalitoka kwa Mungu,** kama **asingaliweza kufanya** ajabu namna hii kamwe.

**9:34** Halafu Wafarisayo walimtukana tena. Ni kama walifikiri labda upofu wa mtu huyu ulikuwa tunda la **zambi zake.** Alipata ruhusa wapi **kuwafundisha**? Hawakufahamu kwamba alikuwa na ruhusa kabisa kuwafundisha! Kama mwalimu Ryle alivyosema, "Mara nyingi Roho Mtakatifu anatumika na watu wasio na elimu nyingi, kupita na watu wakubwa na wenye kujifunza sana." Halafu Wafarisayo **walimtokeza inje.** Tunafikiri maana ya maneno haya hapa ni ya kwamba hawakumwondosha hekaluni tu, lakini katika dini ya Wayuda. (Ona mafundisho juu ya 9:22,23.) Lakini sababu gani walimwondosha? Kwa sababu alizaliwa kipofu na aliwezeshwa kuona siku ya sabato. Aliondoshwa kwa sababu alikataa kusema mabaya juu ya Yule ambaye alifanya ajabu hili kubwa.

**9:35** Lakini **Yesu** alimtafuta. Ni kama alisema, "Kama wao wakikufukuza, mimi ninakupokea." Wale wanaofukuzwa kwa ajili ya Yesu hawapungukiwi kitu, lakini wanabarikiwa sana kwa njia ya upatano mtamu na wa karibu na Yesu. Ona namna Bwana alivyoongoza mtu huyu kumwamini kuwa Mwana wa Mungu! Alimwuliza tu, **"Unaamini Mwana wa Mungu?"**

**9:36** Mtu huyu alikuwa amepokea kuona kwa macho ya mwili, lakini alihitaji kwa macho yake ya roho kufu-

nguliwa vilevile. Aliuliza Bwana kama Mwana wa Mungu ni **nani** ili aweze **kumwamini.**

**9:37** Halafu **Yesu** alimjulisha kwamba yeye mwenyewe alikuwa Mwana wa Mungu. Si mtu wa dunia tu aliyetenda ajabu hili kubwa ndani ya maisha yake. Alikuwa Mwana wa Mungu **ambaye alisema naye** sasa.

**9:38** Akisikia habari hizi mtu huyu aliamini Yesu mara moja, akaanguka mbele yake na **kumwabudu**. Alikuwa amepokea wokovu wa roho pamoja na kupona kwa mwili. Ilikuwa siku kubwa kabisa ndani ya maisha yake!

Ona ya kwamba mtu huyu hakuabudu Bwana kufika saa alipojua kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu. Akiwa Myuda, hakuabudu mtu. Lakini mara moja wakati alipojifunza kwamba aliponyeshwa na Mwana wa Mungu, **alimwabudu** – si kwa sababu ya kazi aliyokwisha kufanya lakini kwa sababu alikuwa Mungu Mwana.

**9:39** Wakati tunaposoma shairi hili kwanza labda tunafazaika namna gani linapatana na Yoane 3:17, "Maana Mungu hakutuma Mwana wake ulimwenguni kuhukumu ulimwengu …" Lakini hatuhitaji kufazaika. Kusudi la kuja kwa Kristo duniani halikuwa kuhukumu, lakini kuokoa. Lakini wale wanaokataa kumpokea watahukumiwa.

Mahubiri ya Habari Njema yanazaa matunda namna mbili. **Watu wanaokubali** kwamba wao ni vipofu kwa roho wanapewa kuona. Lakini **wale wanaosema wanaona** vizuri, bila Bwana Yesu, wanaendelea ndani ya upofu wao.

**9:40** **Wengine wa Wafarisayo** walifahamu kwamba Bwana Yesu alikuwa akisema juu yao na upofu wao. Hivi walifika kwake na kuuliza na ukaramisu kama alifikiri wao ni **vipofu vilevile**. Walifikiri Bwana atajibu, Sivyo.

**9:41** Tunaweza kufafanua jibu la Bwana hivi: "**Kama** mukikubali kwamba ninyi ni **vipofu** na wenye zambi, na munahitaji Mwokozi, zambi zenu zinaweza kusamehewa, na kuokolewa. Lakini munasema kwamba hamuna mahitaji ya roho. Munasema ninyi ni wenye haki na hamuna zambi. **Kwa sababu hii,** hakuna usamehe wa zambi kwa ninyi." Wakati Bwana Yesu aliposema, **"musingekuwa na zambi,"** hakusema walikuwa bila zambi kabisa. Alisema ya kama wangalikubali tu upofu wao ambao uliwazuiza kutambua kwamba yeye ni Masiya, zambi yao ingalikuwa kama si kitu wakati inapofananishwa na zambi kubwa sana ya kukiri kwamba wanaona, bila kumtambua kama Mwana wa Mungu.

### K. Yesu mlango wa zizi la kondoo (10:1-10)

**10:1** Mashairi haya yanaungana na sehemu ya mwisho ya sura 9. Pale Bwana Yesu alikuwa amesema na Wafarisayo waliosema wao ndio wachungaji wa haki wa Israeli. Hapa ndani ya mwanzo wa sura 10 Bwana Yesu alikumbuka zaidi Wafarisayo hawa. Mwanzo wa masemo yake, **"Kweli, kweli ninawaambia ninyi"** yalionyesha kwamba atasema maneno yenye maana kubwa.

**Zizi la kondoo** lilikuwa pahali kondoo walipochungwa usiku. Lilizungushwa na boma na kulikuwa na pahali pamoja tu kuingia kama mlango. Hapa **zizi** ni mfano wa taifa la Wayuda.

Watu wengi walifikia Wayuda wakisema wao ndio viongozi vyao kwa maneno ya roho. Walijiweka wenyewe kuwa masiya yao. Lakini hawakufika kwa njia iliyotabiriwa ndani ya Agano la Kale kwa Masiya kufika. Walipanda **kuingia pahali pengine**. Walijionyesha kwa Israeli kwa njia ambayo wao wenyewe walichagua. Watu hawa hawakuwa wachungaji wa haki. Walikuwa wizi na wanyanganyi. Wizi ndio watu wanaokamata vitu vi-

sivyo vyao; wanyanganyi wanafanya hivi na nguvu na jeuri. Wafarisayo walikuwa wizi na wanyanganyi. Waliweka roho juu ya kutawala Wayuda, na hata hivi walijaribu kwa njia zote kuwazuiza wasipokee Masiya wa kweli. Walitesa wale waliofuata Yesu, na mwishoni wataua Yesu.

**10:2** Ndani ya shairi hili Yesu alisema juu yake mwenyewe. Alifikia kondoo wapotevu wa nyumba ya Israeli. Alikuwa **mchungaji** wa kweli **wa kondoo**. Aliingia kwa **mlango**, maana alifika namna ilivyotabiriwa ndani ya Agano la Kale. Hakujiweka mwenyewe kuwa Mwokozi, lakini alifika akitii mapenzi ya Baba yake ndani ya kila neno.

**10:3** Walimu wa Maandiko hawapatani kama **zamu** ndani ya shairi hili ni nani. Wengine wanafikiri ni manabii wa Agano la Kale waliotabiri ya kwamba Kristo atakuja. Wengine wanafikiri ni Yoane Mbatizaji kwani yeye ndiye mtangulizi wa Mchungaji wa kweli. Na wengine wanafikiri **zamu** ndani ya shairi hili ni Roho Mtakatifu anayefungua mlango kwa Bwana Yesu kuingia ndani ya mioyo na maisha ya watu.

**Kondoo** walisikia **sauti** ya mchungaji. Walitambua sauti yake kama sauti ya mchungaji wa kweli. Kama kondoo wanavyojua sauti ya mchungaji wao mwenyewe, vivyo hivyo wengine wa Wayuda walitambua Masiya wakati alipotokea. Ndani ya kitabu hiki cha Habari Njema tumesikia Mchungaji akiita kondoo zake **kwa majina yao.** Aliita wanafunzi wengine ndani ya sura 1, nao wote walisikia sauti yake na kuitika. Aliita kipofu ndani ya sura 9. Hata leo Bwana Yesu anaita wale walio tayari kumpokea. Anawaita mmoja mmoja.

Labda maana ya **"anatoa kondoo zake inje"** ni ya kwamba Bwana aliongoza wale waliosikia sauti yake kutoka zizi la Israeli. Ni kama walikuwa wafungwa pale. Hawakuwa na uhuru wakati walipotawaliwa na torati. Bwana **anaongoza** kondoo zake na kuwaingiza kwa uhuru wa neema yake. Ndani ya sura 9 Wayuda walifukuza mtu huyu toka sunagogi. Hawakufahamu kwamba kwa njia ya kufanya hivi walisaidia kazi ya Bwana.

**10:4 Wakati** mchungaji wa kweli **anapotoa kondoo zake inje,** hawasukumi kwenda mbele yake, lakini **anawaongoza**. Hawaombi kwenda pahali po pote asipokwenda yeye mwenyewe kwanza. Saa zote yeye ni mbele ya kondoo zake kama Mwokozi wao, Kiongozi wao na Mfano wao. Wale walio **kondoo** za kweli za Kristo **wanamfuata**. *Hawageuki* kondoo zake kwa njia ya kumwiga, lakini kwa njia ya kuzaliwa tena. Halafu wakati wanapokwisha kuokolewa wanataka kwenda pahali gani anapowaongoza.

**10:5** Roho inayosaidia kondoo kutambua sauti ya mchungaji wa kweli inamsukuma vilevile **kukimbia mgeni**. Wageni walikuwa Wafarisayo na viongozi wengine wa Wayuda walioweka roho juu ya kondoo kwa faida yao wenyewe tu. Tunaona neno hili ndani ya maisha ya mtu aliyewezeshwa kuona. Alitambua sauti ya Bwana Yesu lakini alijua Wafarisayo walikuwa wageni. Hivi alikataa kuwatii, hata kama kwa sababu ya kuasi kwake alitokezwa katika sunagogi.

**10:6 Yesu alisema mfano huu** juu ya Wafarisayo, **lakini hawakufahamu** neno hili kwa sababu hawakuwa kondoo wa kweli. Kama wangalikuwa kondoo wa kweli, kama wangalisikia sauti yake na kumfuata.

**10:7 Sasa Yesu** alitumika na mfano mwingine. Hakusema tena juu ya mlango wa zizi, kama ndani ya shairi 2. Sasa alisema juu yake mwenyewe kama **lango la kondoo.** Mfano huu haukuwa juu ya kuingia zizi la Israeli, lakini juu ya kondoo wachaguliwa kutoka dini ya Wayuda na kuingia kwa Kristo, **mlango.**

**10:8** Wengine walikuwa wamefika

**mbele ya** Kristo wakijionyesha kuwa watu wakubwa wenye amri, lakini kondoo wachaguliwa wa Israeli hawakuwasikia, wakifahamu walijaribu kujikamatia heshima isiyo yao.

**10:9** Shairi hili ni shairi wazi na tamu sana na ni jepesi kufahamu hata kwa watoto. Lina maana kubwa vilevile inayoshinda hata wenye elimu kubwa. Kristo ni **mlango**. Ukristo si dini, wala kanisa. Ni Mwenye uzima, ndiye Bwana Yesu Kristo. **"Kama mtu ataingia kwa mimi."** Watu wanaweza kupokea wokovu kwa njia ya Kristo tu. Ubatizo hautoshi, wala karamu ya ukumbusho. Lazima tuingie kwa Kristo, na kwa uwezo yeye anaotoa. Anaita kila mtu; Kristo ni Mwokozi wa Wayuda na watu wa Mataifa vilevile. Lakini kwa mtu kupokea wokovu, sharti aingie. Sharti apokee Kristo kwa imani. Hakuna wokovu kwaye kama asipochagua kufanya hivi yeye mwenyewe. Wale wanaoingia **wanaokolewa** toka azabu, uwezo, na mwishoni hata toka pahali pa zambi.

Nyuma ya kupokea wokovu **wanaingia na kutoka**. Labda ni kusema kwamba wanaingia kwa imani kuabudu Mungu, kisha wanatoka tena kushuhudia Bwana duniani. Wale wanaoingia **wanapata chakula**. Kristo si Mwokozi tu, na mwenye kuleta uhuru, lakini yeye ni mwenye kutegemeza na kushibisha mahitaji ya roho. Kondoo zake **wanakulishwa** na Neno la Mungu.

**10:10** Kusudi la **mwizi** ni **kuiba na kuchinja, na kuharibu.** Anakuja kwa kujipatia mwenyewe faida tu, hata **kuua** kondoo. Lakini Bwana Yesu hafikii mioyo ya watu kwa kujipatia mwenyewe faida. Anakuja kutoa baraka, si kwa kujipendeza mwenyewe. Anakuja kusudi **watu wapate uzima, na waupate tele**. Tunapokea uzima mara moja wakati tunapompokea kuwa Mwokozi wetu. Lakini nyuma yake tunaona kwamba watu wanafurahishwa naye kwa kipimo mbalimbali. Kwa kipimo tunapojitoa kuongozwa na Roho Mtakatifu, kwa kipimo hiki tunafurahishwa na uzima ambao tumepewa. Hatuna **uzima** tu, lakini tuna **uzima tele**.

### L. Yesu, Mchungaji Mwema (10:11-18)

**10:11** Bwana Yesu alisema mara nyingi, **"Mimi ni"**, ndilo moja la majina ya Mungu. Kila mara aliyotumika na jina hili alionyesha kwamba yeye ni mmoja na Mungu Baba. Hapa alijionyesha kama **mchungaji mwema anayetoa uzima wake kwa ajili ya kondoo**. Ni desturi kwa kondoo kuagizwa kutoa uzima wao kwa mchungaji. Lakini Bwana Yesu alikufa kwa ajili ya kondoo.

**10:12 Mtu wa mshahara** ni mtu anayetumika kazi kwa kupata mali. Kwa mfano, mchungaji kondoo anaweza kulipa mtu mwingine mshahara kulinda kondoo zake. Wafarisayo walikuwa watu wa mshahara. Waliweka roho juu ya watu kwa kipimo walichoweza kujipatia mali kwa njia yao. **Kondoo hazikuwa mali ya mtu wa mshahara,** hivi kwa wakati wa hatari alikimbia na kuacha kondoo kuliwa na **imbwa ya poli.**

**10:13** Maneno tunayofanya ni matunda ya namna tulivyo. Mtu wa mshahara alitumika kwa kupata mshahara. **Hakuweka roho juu ya kondoo.** Aliweka roho juu ya hali yake mwenyewe kupita juu ya kondoo. Kuna watu wengi wa mshahara kanisani kwa wakati wa sasa – watu wanaochagua utumishi kanisani kama kazi nzuri bila masumbuko, lakini hawapendi kondoo za Mungu na mapendo ya kweli.

**10:14, 15** Bwana alijiita tena **mchungaji mwema**. Neno kwa **mwema** hapa kwa Kiyunani ni *kalos,* maana yake "kamili, pasipo upungufu, bora kupita yote." Yeye ni maneno haya yote. Halafu aliendelea kusema juu ya umoja wa

moyo wake na **kondoo** zake. Anawajua **walio wake**, **nao** wanamjua yeye. Hii ni kweli tamu kabisa.

Na kweli tamu nyingine ndiyo hii: Alisema, "Sawasawa **Baba anavyonijua, mimi vilevile ninajua Baba.**" Vivyo hivyo anajua kondoo zake, nao wanamjua yeye. Hii ni kweli ya kufurahisha roho tele! Bwana alisawanisha umoja wa moyo na kondoo zake na umoja wa Baba wake na yeye mwenyewe. Ukaribu na ushirika, upatano na kujua – maneno haya yote yanayofunga Baba na Mwana pamoja yanafunganisha Mchungaji na kondoo vilevile. Alisema, **"Nami ninatoa uzima wangu kwa ajili ya kondoo,"** akitazamia tena, kama alivyofanya mara nyingi mbele, siku atakapokufa msalabani kama Mkombozi kwa wenye zambi.

**10:16** Shairi 16 ni kama ufunguo wa sura hii nzima. Wale **kondoo wengine** Bwana aliosema juu yao walikuwa Mataifa. Alifika duniani zaidi kwa sababu ya kondoo za Israeli, lakini alifikiri juu ya wokovu wa Mataifa vilevile. Kondoo za Mataifa **hawakuwa** wa **zizi** la Wayuda. Lakini Bwana Yesu mwenye roho ya huruma tele alifikiri kondoo hawa vilevile, na akiwa Mungu, alisukumwa rohoni **kuwaleta** karibu naye vilevile. Alijua kwamba watakuwa tayari kupita Wayuda **kusikia sauti yake**.

Kwa mwisho wa shairi hili Bwana aliacha kusema juu ya **zizi** la Wayuda na alianza kusema juu ya **kundi** la Wakristo. Shairi hili linaonyesha mbele kwamba ndani ya Kristo Wayuda na Mataifa watakuwa moja, na ya kwamba maneno yaliyotenga watu hawa mbele hayatakuwa tena.

**10:17** Ndani ya mashairi 17 na 18 Bwana alieleza kama atafanya nini kuleta wachaguliwa Wayuda na Mataifa kwake. Alitazamia wakati wa mauti, kuzikwa, na ufufuko wake. Asingalisema maneno namna hii kama angalikuwa mtu tu. Alisema juu ya **kutoa uzima wake** na **kuutwaa tena** kwa uwezo wake mwenyewe. Aliweza kufanya hivi kwa sababu yeye ni Mungu. **Baba** alipenda Bwana Yesu **kwa sababu** alikuwa tayari kufa na kufufuka tena, ili kondoo wapotevu waweze kuokolewa.

**10:18 Hakuna mtu** aliyeweza **kuondolea** Bwana uzima wake. Yeye ni Mungu, hivi yeye ni mkubwa kupita mashauri yote ya viumbe vyake kumwua. Alikuwa na **uwezo kutoa uzima wake na kuutwaa tena.** Lakini unauliza, watu hawakuua Bwana Yesu? Ndiyo, walifanya hivi. Tunasoma ile wazi ndani ya Matendo 2:23 na 1 Tes. 2:15. Bwana Yesu aliwaruhusu kufanya hivi. Neno hili linaonyesha **uwezo wake kutoa uzima wake**. Zaidi ya ile "alitoa roho yake" (Yn. 19:30), ndilo tendo la nguvu na kutaka kwake mwenyewe.

Alisema, **"Agizo hili nilipokea kwa Baba yangu."** Baba alisema na Bwana kutoa uzima wake na kufufuka toka wafu. Hivi alikufa na kufufuka kutimiza mapenzi ya Baba. Bwana Yesu alikuwa mwenye kutii hata mauti, na kufufuka tena siku ya tatu, kama ilivyoandikwa ndani ya Maandiko.

### M. Matengano katikati ya Wayuda (10:19-21)

**10:19** Masemo ya Bwana Yesu yalileta **matengano tena katika Wayuda.** Kuja kwa Kristo duniani, na kuingia nyumbani na mioyoni mwa watu kunazaa upanga, si salama. Watu wanaweza kuwa na salama na Mungu wakati wanapopokea Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wao.

**10:20, 21** Bwana Yesu alikuwa mtu mkamilifu wa pekee aliyeishi tangu zamani. Hakusema neno baya au kufanya tendo ovu kamwe. Lakini upotovu wa mioyo ya watu ulikuwa mkubwa sana.

Hata wakati alipofika na masemo ya mapendo na hekima, watu walisema **ana pepo** na ni mwenye **wazimu,** na si faida kumsikiliza. Lakini kulikuwa na **wengine** waliotambua **masemo** na kazi zake kuwa zile za mtu mwema, si za **pepo.**

**N. Kazi za Yesu zinahakikisha kwamba yeye ni Kristo (10:22-39)**

**10:22** Kuanza na shairi hili Bwana hakusema na Wafarisayo tena, lakini kwa Wayuda wote. Hatujui urefu wa muda nyuma ya shairi 21 na mwanzo wa shairi 22. Hii ni mara ya pekee tunayosoma juu ya karamu ya Kutabaruku. Kwa Kiebrania inaitwa *Hanukkah.* Wenye elimu wanafikiri karamu hii ilisimamishwa na Yudas Maccabeus saa ya kuweka hekalu kwa Mungu tena nyuma ya kuchafuwa na Antiochus Epiphanes, mwaka165 B.C. Wayuda walishika karamu hii kila mwaka, lakini haikuwa moja ya karamu za BWANA. **Ilikuwa** wakati wa **baridi** wa mwaka, na rohoni mwa watu vilevile.

**10:23, 24** Utumishi wa Bwana katikati ya watu ulikuwa karibu kwisha na kufa kwake msalabani kulikaribia. **Baraza ya Solomono** ilikuwa na dari na ilipakana na hekalu la Herode. Wakati Bwana alipotembea pale, kulikuwa na nafasi nyingi kwa Wayuda kumzunguka.

**Wayuda wakamzunguka, wakamwambia: "Hata wakati gani utatuhangaisha sisi? Kama wewe ni Kristo, utuambie waziwazi."**

**10:25, 26 Yesu** aliwakumbusha masemo yake na **kazi** zake. Alikuwa amewaambia mara nyingi kwamba yeye ni Masiya, na maajabu aliyofanya yalihakikisha kwamba masemo yake yalikuwa kweli. Aliwaambia Wayuda tena kwamba alifanya maajabu yake kwa amri ya Baba yake na kwa utukufu wake. Kwa njia hii alionyesha kwamba yeye ndiye yule ambaye Baba alituma duniani.

Hawakukubali kupokea Masiya, na walionyesha kwa njia hii ya kwamba **hawakuwa kondoo zake**. Kama wangaliwekwa mbali kuwa watu wake, kama wangalikuwa tayari kumwamini.

**10:27** Mashairi yanayofuata yanaonyesha wazi kabisa ya kwamba hakuna kondoo ya kweli ya Kristo atakayepotea kamwe. Hii ni kweli nzuri sana. Wale walio **kondoo** za kweli za Kristo **wanasikia sauti** yake. **Wanaisikia** wakati wanaposikia Habari Njema ikihubiriwa na wanaitika kwa njia ya kumwamini. Kisha **wanasikia** sauti yake kila siku na kutii Neno lake. Bwana Yesu anajua kondoo zake. Anajua kila kondoo na jina lake. Hatakosa kujua maneno ya kila mmoja. Hakuna kondoo atakayepotea kwa sababu Bwana hakuangalia maneno yake. Kondoo za Kristo **wanamfuata,** kwanza kwa njia ya kumwamini na kupata wokovu, kisha kwa njia ya kutembea pamoja naye na kumtii.

**10:28** Kristo **anatoa uzima wa milele** kwa kondoo zake, ndio uzima usiokwisha kamwe. Uzima huu *hauwezi kubadilika* kwa njia ya mwenendo wao. Ni **uzima wa milele**, maana hauna mwisho. Lakini **uzima wa milele** ni *namna* ya uzima vilevile. Ni uzima wa Bwana Yesu mwenyewe. Ni uzima ambao unatuwezesha kufurahia maneno ya Mungu hapa duniani, na uzima unaofaa kwa pahali petu mbinguni vilevile. Waza sana juu ya maneno haya yanayofuata: **"Hawatapotea hata milele."** Kama kondoo ye yote ya Kristo angalipotea, Bwana Yesu asingalitimiza ahadi yake, na neno hili haliwezekani. Yesu Kristo ni Mungu, naye hawezi kukosa kufanya neno aliloahidi. Ameahidi ndani ya shairi hili ya kwamba hakuna mmoja wa kondoo zake atakayeshinda milele katika gehena.

Kama ni hivi, inawezekana kwa mtu kuokolewa na nyuma yake kufanya maneno yo yote anayotaka? Anaweza kuendelea ndani ya anasa na zambi za

dunia? Sivyo, hataki kufanya maneno haya tena. Anataka kufuata Mchungaji. Hatuishi kama Wakristo kusudi tuweze kugeuka Wakristo, au tusipoteze wokovu wetu. Tunaishi kama Wakristo kwa sababu *tuko* Wakristo. Tunataka kuishi maisha matakatifu, si kwa sababu tunaogopa tutapoteza wokovu wetu, lakini kwa sababu roho zetu zinajaa na mashukuru kwa Bwana ambaye alitukufilia. Kweli hii ya kwamba hatuwezi kupotea kamwe haituruhusu kuishi maisha maovu. Sivyo; inatusukuma kuishi maisha matakatifu.

Hakuna mtu anayeweza **kunyanganya** mwamini toka **mkono** wa Kristo. Mkono wake ni mkono wa uwezo wote. Uliumba ulimwengu, na hata sasa unautegemeza. Hakuna uwezo wo wote unaoweza kunyanganya kondoo toka mkono ule.

**10:29** Mwamini ni mkononi mwa Kristo, na zaidi ya ile yeye ni **mkononi mwa Baba** vilevile. Mungu Baba ni **mkubwa kupita wote, na hakuna mtu anayeweza kunyanganya mwamini toka mkono wa Baba.**

**10:30** Halafu Bwana Yesu alisema tena kwamba yeye na Mungu ni sawasawa. Alisema: **"Mimi na Baba yangu ni mmoja."** Kristo na **Baba ni mmoja** kwa *uwezo*. Yesu alikuwa amesema juu ya uwezo unaolinda kondoo za Kristo. Hivi aliongeza kusema kwamba uwezo wake ni sawasawa na uwezo wa Mungu Baba. Neno hili ni kweli kwa maneno yote ya uungu wao. Bwana Yesu Kristo ni Mungu kabisa na sawasawa na Baba kwa kila njia.

**10:31** **Wayuda** walifahamu maana ya masemo ya Mwokozi. Walifahamu kwamba alionyesha tena waziwazi kabisa ya kwamba yeye ni Mungu, hivi **wakatwaa mawe tena, wampige.**

**10:32** Mbele ya kupata njia kumtupia mawe, **Yesu** aliwakumbusha **kazi njema nyingi** alizokuwa amefanya akiagizwa **na Baba** yake. Halafu aliwauliza kazi gani iliwakasirisha sana hata walitaka **kumtupia mawe.**

**10:33** Wayuda walisema kwamba hawakutaka kumwua kwa sababu ya ajabu yo yote aliyofanya. Walitaka kumtupia mawe kwa sababu walifikiri **alitukana** wakati aliposema yeye ni sawasawa na Mungu Baba. Walikataa kabisa kwamba yeye ni mkubwa kupita mtu. Lakini waliweza kuona wazi kwamba alijionyesha kuwa **Mungu**. Walikataa neno hili kabisa.

**10:34** Sasa Bwana Yesu alitaja sehemu ya Zaburi 82:6. Alisema hii ni sehemu ya **torati** yao, ndiyo sehemu ya Agano la Kale waliyoamini ni Neno la Mungu, lililoandikwa kwa maongozi yake. Shairi zima linasema, "Nikasema: Ninyi ni miungu, na ninyi wote wana wake Aliye Juu." Zaburi hii iliandikwa kwa waamuzi wa Israeli. Waliitwa **"miungu,"** si kwa sababu walikuwa watakatifu, lakini kwa sababu walisimamia Mungu saa walipohukumu watu. Maana ya neno kwa "miungu" kwa Kiebrania *(elohim)* ni "wenye uwezo" na lilitumiwa mara nyingine kwa watu wenye heshima kama waamuzi. (Baki la zaburi ile linaonyesha wazi kwamba walikuwa watu tu na si miungu kwa sababu hawakuhukumu kwa haki, lakini walikuwa na upendeleo kwa watu fulani, vivi hivi.)

**10:35** Bwana alitumika na shairi hili toka Zaburi kuonyesha kwamba Mungu alitumia neno hili **miungu** kusema juu ya watu ambao **Neno la Mungu lilifikia.** Ni kusema, watu hawa walisema kwa ajili ya Mungu. Mungu alisema kwa taifa la Israeli kwa njia yao. Bwana alisema, **"Na maandiko hayawezi kuvunjika,"** akionyesha kwamba Agano la Kale liliandikwa kwa maongozi ya Mungu. Alisema ni maandiko yasiyoanguka kwa neno lo lote, na lazima hayatatimizwa, na haiwezekani kuyakana. Kila neno moja

moja la Maandiko liliongozwa na Mungu, si mawazo ya watu tu.

**10:36** Basi kama waamuzi wa Agano la Kale, wasiohukumu kwa haki waliitwa "miungu," yeye mwenyewe, kupita wao, aliweza kusema yeye ni Mwana wa Mungu. Neno la Mungu *liliwafikia;* Yeye *alikuwa,* naye *ni* Neno la Mungu. Wao *waliitwa* miungu. Yeye *alikuwa* na *ni* Mungu. Haikuwezekana kamwe kusema juu yao kwamba **Baba aliwatakasa na kuwatuma katika dunia.** Walizaliwa duniani kama wana wote wa Adamu, mwenye zambi. Lakini Yesu alitakaswa na Mungu **Baba** tangu milele kuwa Mwokozi wa dunia, na **alitumwa katika dunia** toka mbingu pahali alipokaa tangu milele pamoja na Baba yake. Hivi alikuwa na ruhusa kweli kusema kwamba yeye ni sawasawa na Mungu. Hakutukana wakati aliposema yeye ni **Mwana wa Mungu**, sawasawa na Baba. Wayuda wenyewe waliita "miungu" watu waovu waliosema tu au kuhukumu tu kwa ajili ya Mungu. Lakini yeye alistahili kweli kuitwa Mwana wa Mungu kwani yeye *ni* Mungu.

**10:37, 38** Mwokozi alitaja tena maajabu aliyokuwa amefanya kuhakikisha kwamba ametumwa na Mungu. Ona ya kwamba hapa anayaita **"kazi za Baba yangu."** Si maajabu yote yanayofanywa kwa uwezo toka Mungu. Kazi zake zilihakikisha kwa njia mbili kwamba yeye ni Masiya. Kwanza zilikuwa kazi zilizotabiriwa ndani ya Agano la Kale kwamba zitatendwa na Masiya. Na vilevile zilikuwa kazi za rehema na huruma zilizosaidia watu na zisizotendwa na mtu mwovu. Zilionyesha kwamba "Baba ni ndani yangu, nami ni ndani ya Baba."

**10:39** Wayuda walifahamu kwamba Bwana Yesu alisema na nguvu kupita mbele ya kuwa yeye ni Mungu, hivi walijaribu tena kumkamata, lakini hawakuweza. Saa ilikuwa ikikaribia wakati atakapowaruhusu kumkamata, lakini ilikuwa haijafika bado.

## 6 MWAKA WA TATU WA UTUMISHI WA MWANA WA MUNGU: PEREA (10:40–11:57)

### A. Yesu anavuka Yorodani (10:40-42)

**10:40** Bwana **alikwenda tena ngambo ya Yorodani hata pahali** alipoanza utumishi wake. Alifikia mwisho wa miaka mitatu ya masemo na kazi za ajabu. Aliimaliza kwa pahali alipoianza, inje ya kawaida ya kuabudu ya Wayuda, kwa pahali pa kukataliwa na upekee.

**10:41** Tunafikiri wale ambao **walimfikia pale** walikuwa waamini wa kweli. Walikuwa tayari kukataliwa pamoja naye, inje ya kambi ya Israeli. Wafuata hawa walisifu **Yoane Mbatizaji** sana. Walikumbuka kwamba Yoane hakufanya maneno makubwa ya kujulikana *katikati ya watu*, lakini kila neno alilosema juu ya Bwana Yesu lilikuwa **kweli** na lilitimizwa ndani ya utumishi wa Mwokozi. Ingepasa kuwa hivi ndani ya maisha ya kila Mkristo. Labda sisi hatuwezi kufanya maajabu ya uwezo katikati ya watu, lakini tunaweza kutoa ushuhuda wa kweli juu ya Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo, ndilo neno la damani sana machoni mwa Mungu.

**10:42** Ni tamu sana kuona ya kwamba hata Bwana Yesu alikataliwa na taifa la Israeli, kulikuwa na waamini wengine wenye roho ya unyenyekevu ambao walimpokea. Tunasoma kwamba **wengi walimwamini kule**. Ni vivyo hivyo kwa kila muda. Kila mara kuna baki la watu walio tayari kufungana pamoja na Bwana Yesu, wakichukiwa na kuzarauliwa na kukataliwa na watu wa dunia, lakini wakiwa na ushirika mtamu na Mwana wa Mungu.

### B. Ugonjwa wa Lazaro (11:1-4)

**11:1** Sasa tumefikia ajabu kubwa la mwisho Bwana Yesu alilofanya katikati ya watu. Kwa njia nyingine lilikuwa ajabu lake kubwa zaidi – ndilo kufufua

mfu. **Lazaro** alikaa ndani ya kijiji kidogo kilichoitwa **Betania,** karibu kilomètres 3 toka Yerusalema kwa upande wa mashariki. **Betania** kilijulikana vilevile kama **kijiji cha Maria na ndugu yake Marata**. Mwalimu mmoja aliandika,

> Tuone kwamba neno linaloleta heshima kwa inchi au miji au vijiji vyo vyote ni watoto wachaguliwa wa Mungu wanaokaa pale. Jina la kijiji cha Marata na Maria linatajwa ndani ya Maandiko, lakini kuna majina ya miji mikubwa ya wakati ule yasiyotajwa ndani ya Agano Jipya. [34]

**11:2** Yoane anaeleza kwamba ndiye **Maria yule aliyepakaa Bwana na marasi, na alipangusa miguu yake na nyole zake**. Roho Mtakatifu alitaja tendo hili la kushangaza lililoonyesha mapendo yake makubwa. Bwana anafurahia sana matendo yanayoonyesha mapendo ya kweli ya watu wake.

**11:3** Ni kama Yesu alikuwa kwa upande wa mashariki wa mto Yorodani wakati Lazaro aliposhikwa na ugonjwa. **Ndugu zake wake** wawili walituma habari mara moja kujulisha **Yesu** kwamba **yeye ambaye** alimpenda alikuwa **mgonjwa**. Walifikiri ya kwamba kwa sababu ya mapendo yake kwa Lazaro atakuja mara moja kuwasaidia.

**11:4 Wakati Yesu … aliposema, "Ugonjwa huu si wa kufa"** hakutaka kusema ya kwamba Lazaro hatakufa, lakini ya kwamba **mauti** haitakuwa mwisho wa **ugonjwa huu**. Kusudi la ugonjwa huu ulikuwa **utukufu wa Mungu, ili Mwana wa Mungu atukuzwe kwa neno hili.** Mungu aliruhusu neno hili kutokea ili Yesu aweze kuja na kufufua Lazaro toka wafu, na kwa njia hii aweze kuonekana tena kama Masiya wa kweli. Watu watatukuza **Mungu** kwa sababu ya ajabu hili.

Hakuna neno kutuleta kufikiri kwamba ugonjwa wa Lazaro ulikuwa tunda la zambi. Tunamwona kama mwanafunzi mwaminifu wa Bwana aliyependwa sana naye.

### C. Safari ya Yesu kwenda Betania (11:5-16)

**11:5** Wakati watu wa jamaa yetu wanaposhikwa na ugonjwa, tusifikiri ni kwa sababu Mungu hapendezwi nasi. Hapa ugonjwa unaonyesha mapendo yake, si gazabu yake.

**11:6,7** Sisi tungefikiri kama Bwana angependa watu hawa watatu kweli, angeshika njia mara moja kufikia nyumba yao. Sivyo. **Wakati aliposikia habari hizi alikaa kule siku mbili pahali pale.** Mungu hakatai kujibu maombi yetu, lakini mara nyingine anakawa. Labda anatufundisha kungoja kwanza, na kama tukingoja na saburi tutaona kwamba atajibu maombi yetu akifanya neno lililo hata zuri kupita. Hata mapendo yake kwa Marata, Maria na Lazaro hayakuweza kusukuma Kristo kutenda mbele ya saa iliyochaguliwa. Alitii Mungu Baba yake ndani ya kila neno na kulifanya kwa saa ambayo iliyowekwa mbele.

**Nyuma** ya siku mbili (sisi tungeweza kufikiri saa zilizopotea bure) Bwana alisema na **wanafunzi vizuri waendee Yudea tena.**

**11:8 Wanafunzi** walikumbuka sana namna **Wayuda walivyojaribu kutupia Kristo mawe** saa alipowezesha kipofu kuona. Walishangaa kwa sababu alitaka kurudia Yudea tena, ndipo pahali pa hatari kwa yeye.

**11:9** Ona **jibu la Yesu:** Kwa **siku moja** kuna **saa kumi na mbili** za jua wakati watu wanapoweza kufanya kazi yao. Wakati mtu anapotumika kwa muda huu, hakuna hatari ya kwamba atakwaa au kuanguka, **kwa sababu anaona** pahali anapokwenda na maneno anayofanya. **Nuru ya dunia hii,** ndiyo nuru ya mchana, inamzuiza asife kwa sababu ya kukwaa.

Maana ya roho ya masemo ya Bwana

ndiyo hii: Bwana Yesu alikuwa akitembea akitii mapenzi ya Mungu. Hakuna hatari kwamba atauawa mbele ya saa iliyowekwa mbele. Atalindwa kufika saa kazi yake itakapokwisha.

Neno hili ni kweli ndani ya maisha ya kila mwamini. Tukitembea pamoja na Bwana na kufanya mapenzi yake, hakuna neno duniani linaloweza kutuua mbele ya saa ambayo Mungu alichagua mbele.

**11:10** Mtu **anayetembea usiku** ndiye asiye mwaminifu kwa Mungu lakini anaishi akifanya mapenzi yake mwenyewe. Ni nyepesi kwa mtu huyu **kukwaa kwa sababu** anakosa nuru ya Mungu kumwongoza.

**11:11** Bwana alisema kwamba Lazaro *alilala usingizi*. Vizuri tufahamu ya kwamba hatusomi *kamwe* ndani ya Agano Jipya juu ya usingizi wa roho, lakini juu ya usingizi wa mwili tu. Maandiko hayafundishi ya kwamba wakati wa kufa nafsi ya mtu ni katika hali ya usingizi. Wakati mwamini anapokufa, nafsi yake inakwenda karibu na Kristo, maana ni vizuri zaidi. Bwana Yesu alifunua hapa kwamba anajua maneno yote. Alijua kwamba Lazaro alikuwa amekufa, hata kama alikuwa amesikia habari za ugonjwa wake tu. Alijua kwa sababu yeye ni Mungu. Inawezekana kwa mtu wa dunia kuamsha mtu toka usingizi wa mwili, lakini Bwana tu aliweza kuamsha Lazaro toka mauti. Yesu aliwajulisha kwamba alikusudi kufanya hivi.

**11:12** **Wanafunzi** wake hawakufahamu maneno Yesu aliyosema juu ya usingizi, na ya kama alikuwa akisema juu ya mauti. Labda walifikiri kwamba usingizi unaonyesha mgonjwa alikuwa akipona, na kama Lazaro alikuwa akilala usingizi **atapona**. Au, kama Lazaro alihitaji usingizi tu, Bwana na wanafunzi hawakuhitaji kwenda Betania kumsaidia. Au labda wanafunzi waliogopa hatari kama wakikwendea nyumba ya Maria na Marata saa hii.

**11:13,14** Hapa tunasoma wazi ya kwamba wakati **Yesu aliposema** juu ya usingizi, maana yake ilikuwa **mauti**, lakini wanafunzi hawakufahamu neno hili. Hivi sasa **Yesu** aliwaambia **waziwazi, "Lazaro amekufa.**" Wanafunzi hawakushituka juu ya habari hizi! Hawakuuliza Bwana, "Unajua namna gani?" Alisema na amri, hivi hawakuwa na shaka juu ya maneno aliyosema.

**11:15** Bwana Yesu hakufurahi kwa sababu Lazaro alikufa, lakini **alifurahi** kwa sababu **hakuwa** kwa Betania saa ya kufa kwake. Kama angalikuwa pale kama Lazaro asingalikufa. Hatusomi hata mara moja ndani ya Agano Jipya juu ya mtu akikufa pahali Bwana Yesu alipokuwa. Sasa wanafunzi hawataona mtu akiponyeshwa toka ugonjwa tu, lakini wataona ajabu kubwa zaidi, ndilo kufufuliwa kwa mtu toka mauti. Kwa njia hii imani yao itapatishwa nguvu. Hivi Bwana Yesu alisema **alifurahi** kwa ajili yao kwa sababu hakuwa kwa Betania saa Lazaro alipokufa.

Bwana aliongeza, **"mupate kuamini"**, lakini hakusema hivi kwa sababu wanafunzi hawakumwamini mbele, lakini kwa sababu ajabu watakaloona kwa Betania litapatisha imani yao nguvu sana. Hivi aliwasukuma **kwenda** pamoja naye.

**11:16** **Tomasi** alifikiri kama Bwana Yesu akikwenda kule, bila shaka atauawa na Wayuda. Na wanafunzi wakikwenda pamoja naye, aliamini kwamba watauawa vilevile. Hivi na roho nzito na ukosefu wa uhodari na imani, alisema vizuri wao wote waende pamoja naye.

### D. Yesu: Ufufuko na Uzima (11:17-27)

**11:17, 18** Tunajulishwa kwamba Lazaro alikuwa kaburini kwa **siku ine,** na neno hili linahakikisha kwamba alikufa kweli. Roho Mtakatifu aliweka roho

kabisa kuonyesha wazi kabisa kwamba ufufuko wa Lazaro ulikuwa ajabu kweli. Ni kama Lazaro alikufa saa ndogo tu nyuma ya kwenda kwa wajumbe kuita Yesu. Ilikuwa safari ya siku moja toka Betania kwenda Betabara, pahali Yesu alipokuwa. Nyuma ya kusikia habari za ugonjwa wa Lazaro Yesu alibaki pale kwa siku mbili. Halafu siku moja nyingine ilihitajiwa kwa Yesu kwenda Betania. Habari hizi zinaeleza kwa sababu gani Lazaro alikuwa kaburini siku ine.

Tulisoma mbele kwamba **Betania** kilikuwa **karibu kilomètres tatu** toka **Yerusalema** kwa upande wa mashariki.

**11:19** Kwa sababu Betania kilikuwa karibu na Yerusalema, **Wayuda wengi** toka pale waliweza **kufikia wanawake waliokuwa pamoja na Marata na Maria kuwafariji.** Hawakujua ya kwamba nyuma kidogo faraja yao haitahitajiwa tena, na nyumba hii ya maombolezo itageuka nyumba ya furaha tele.

**11:20 Wakati Marata aliposikia kwamba Yesu alikuwa akikaribia alitoka** kukutana **naye**. Walikutana inje kidogo ya kijiji. Hatujui kwa nini Maria alibaki **nyumbani**. Labda hakusikia habari za kukaribia kwa Yesu, au alishindwa na huzuni, au alikuwa akingoja tu na imani na maombi. Labda kwa sababu ya ukaribu wake na Bwana alifahamu kwamba neno kubwa sana lilikuwa karibu kutokea. Hatujui.

**11:21 Marata** alikuwa na imani ya kweli ambayo ilimwezesha kuamini kwamba Yesu angaliweza kuzuiza Lazaro asife. Hata hivi imani yake haikuwa kamilifu kabisa. Alifikiri Bwana ataweza kufanya hivi tu kama alikuwa pale yeye mwenyewe. Hakufahamu kwamba Bwana aliweza kuponyesha mtu toka mbali vilevile, na hata kumfufua toka wafu. Mara nyingi kwa wakati wa huzuni masemo yetu yanafanana na yale ya Marata. Tunafikiri kama mpenzi wetu angalipewa dawa fulani au neno fulani lingine lingalitokea kama asingalikufa. Vizuri tukumbuke ya kwamba maneno haya yote ni mikononi mwa Bwana, na hakuna neno linalopata watoto wake bila ruhusa yake.

**11:22** Imani ya ndugu msichana mtawa huyu ya Lazaro ilikaa kungaa. Hakujua kama Bwana Yesu atasaidia *namna gani*, lakini aliamini kwamba bila shaka atasaidia. Aliamini kwamba **Mungu** atafanya neno aliloomba na ya kwamba mwisho wa taabu hii itakuwa baraka. Lakini hata sasa Marata hakuamini kwamba ndugu yake atafufuliwa toka wafu. Neno ambalo Marata alitumika nalo kwa “omba” lilitumiwa kwa kiumbe akisihi Mwumba. Ni kama Marata alikuwa hajafahamu bado kwamba Bwana Yesu alikuwa Mungu. Alifahamu yeye ni mtu mkubwa, lakini labda si mkubwa kupita manabii wa zamani.

**11:23** Kwa kupatisha imani ya Marata nguvu Bwana Yesu alifanya tangazo la kushangaza, ya kwamba Lazaro **atafufuka.** Ni tamu kuona namna na upole sana Bwana aliongoza mwanamke huyu mwenye huzuni kufahamu na kuamini ya kwamba yeye ni Mwana wa Mungu.

**11:24 Marata** alifahamu kwamba Lazaro **atafufuliwa** siku nyingine lakini hakuwaza kwamba itawezekana siku ile ile! Aliamini kwamba **wafu watafufuliwa**, lakini alifikiri neno hili litatokea **“siku ya mwisho.”**

**11:25** Ni kama Bwana alisema naye, “Hunifahamu, Marata. Sisemi kwamba Lazaro atafufuka siku ya mwisho. Mimi ni Mungu, nami ninashika uwezo wa **ufufuko** na **uzima** mkononi mwangu. Ninaweza kufufua Lazaro toka wafu sasa hivi, na nitafanya hivi.”

Halafu Bwana alitazamia mbele kwa wakati wa kuja, saa waamini wote wa kweli watakapofufuliwa. Neno hili litatokea wakati Bwana Yesu atakapokuja tena kupeleka watu wake mbinguni.

Kwa wakati ule kutakuwa na waamini wa aina mbili. Kutakuwa na wale waliokuwa waamini mbele ya kufa kwao, na kutakuwa na waamini watakaokuwa hai saa atakapokuja. Atafikia aina ya kwanza kama *Ufufuko*, na wale walio kwanza hai kama *Uzima*. Tunasoma juu ya watu wa kwanza ndani ya sehemu ya pili ya shairi 25 – **"yeye ambaye ananiamini, hata anapokufa, ataishi."** Ni kusema ya kama waamini wale waliokufa mbele ya kuja kwa Kristo watafufuliwa toka wafu.

Burkett alisema:

> Mapendo yaliyo nguvu kuliko mauti! Kaburi haliweza kutenga Kristo na rafiki zake. Rafiki wengine wanakwenda pamoja nasi hata karibu na kaburi, lakini wanaachana nasi pale. Lakini wala uzima wala mauti haziwezi kututenga na mapendo ya Kristo.

**11:26** Tunasoma ndani ya shairi hili ya kwamba waamini walio kwanza hai wakati Mwokozi atakapokuja **hawatakufa hata milele.** Watabadilishwa kwa dakika moja, kwa kufunga na kufungua jicho (1 Kor. 15:52), na kupelekwa mbinguni pamoja na wale waliofufuliwa toka wafu. Hizi ndizo kweli za damani sana tulizojulishwa kwa njia ya kufa kwa Lazaro! Mungu analeta utamu toka uchungu na kilemba cha kupambwa pahali pa majivu (Isa. 61:3). Halafu Bwana aliuliza Marata, akijaribu imani yake, **"Unaamini maneno haya?"**

**11:27** Imani ya Marata iliwaka kabisa sasa. Alikiri kwamba **Yesu ni Kristo, Mwana wa Mungu**, ambaye manabii walisema **anakuja duniani**. Ona kwamba alisema maneno haya *mbele* ya kufufuliwa kwa ndugu yake, si nyuma!

### E. Yesu anatoa machozi kwa kaburi la Lazaro (11:28-37)

**11:28, 29** Mara moja nyuma ya kusema maneno haya, Marata alirudia kijiji, na kusalimu ndugu yake Maria na habari hizi kubwa, **"Mwalimu amekuja na anakuita."** Mwumba wa ulimwengu na Mwokozi wa dunia alikuwa amefikia Betania na **kumwita**. Ni vivyo hivyo leo. Bwana huyu wa ajabu anasimama na kuita watu na Habari Njema. Kila mtu anaitwa kufungua mlango wa moyo wake na kumpa Bwana ruhusa kuingia. Basi Maria hakukawa. **Aliondoka upesi**, akakwenda kwa Yesu.

**11:30, 31** **Yesu** alikuwa kwanza inje ya kijiji cha Betania wakati alipokutana na Marata na Maria.

**Wayuda** hawakujua kwamba alikuwa karibu, kwa sababu Marata alimwambia Maria tu peke yake. Hivi walifikiri **Maria** alikuwa amekwenda **kwa kaburi alie kule.**

**11:32** **Maria … alianguka kwa miguu** ya Mwokozi. Labda alifanya hivi kwa kumwabudu, au kwa sababu ya huzuni yake kubwa. Kama Marata, alisema na huzuni kama Yesu angalikuwa kwa Betania **ndugu yao asingalikufa.**

**11:33** Yesu aliugua na k**ufazaika** rohoni wakati alipoona huzuni ya Maria na rafiki zake. Bila shaka alifikiri juu ya huzuni na taabu zote na mauti zilizofikia dunia kwa sababu ya zambi za watu.

**11:34** Bwana alijua **pahali** Lazaro alipozikwa, lakini aliuliza watu waliokuwa pale ili kuamusha tumaini na imani ndani yao na kuwapa njia kusaidia. Bila shaka wenye kuomboleza walifikisha Bwana kwa kaburi na huzuni kubwa.

**11:35** **Yesu akalia machozi.** (Tunasoma mara mbili nyingine ndani ya Agano Jipya juu ya Yesu **akitoa machozi**: juu ya mji wa Yerusalema, na katika shamba la Getesemane.) **Machozi yake** yalionyesha utu wake, na huzuni yake kubwa wakati alipoona matunda ya kuogopesha ya zambi. **Yesu akitoa machozi** anaonyesha kwamba si vibaya kwa Wakristo kutoa machozi wakati wapenzi wao wanapokufa. La-

kini huzuni ya Wakristo si namna ya ile ya wasioamini wasio na tumaini.

**11:36** Machozi ya Mwana wa watu yalionyeshea **Wayuda** mapendo yake kwa Lazaro, lakini wengi wao hawakufahamu kwamba *wao vilevile* walipendwa naye na mapendo makubwa sana yasiyoweza kwisha.

**11:37** Mara hii tena watu wengine walifazaika wakati walipoona Bwana Yesu katikati yao. Walimtambua kuwa yule aliyefungua macho ya **kipofu**. Waliuliza kwa nini **hakuzuiza Lazaro asife**. Ndiyo, Bwana Yesu angaliweza kufanya hivi, lakini alikusudi kufanya ajabu kubwa kupita, ambalo litawapa wenye imani tumaini kubwa zaidi.

**F. Alama ya saba: kufufuliwa kwa Lazaro (11:38-44)**

**11:38** Ni kama **kaburi** la Lazaro lilikuwa **pango** chini ya udongo, na mtu angaliweza kuingia kwa njia ya kushuka na ngazi. **Jiwe** liliwekwa juu ya mwingilio wa pango. Halikuwa sawasawa na kaburi la Bwana Yesu lililochongwa toka mwamba, na bila shaka mtu aliweza kuliingia na miguu kama ndani ya kilima bila kupanda au kushuka.

**11:39** Yesu aliagiza watu waliosimama pale na kutazama **waondoshe jiwe** toka mwingilio. Angaliweza kufanya hivi yeye mwenyewe kwa njia ya kusema neno tu, lakini si desturi ya Mungu kufanyia watu maneno wanayoweza kufanya wao wenyewe.

**Marata** alichukizwa sana na wazo la kufungua kaburi. Alijua maiti ya ndugu yake ilikuwa imelala pale kwa **siku ine** na aliogopa kwamba ilikuwa imeanza kuoza. Ni kama maiti ile haikuwekwa dawa isioze, na ilizikwa siku mtu aliyokufa, kama ilivyokuwa desturi kwa wakati ule. Tunasoma tena kwamba maiti ya Lazaro ilikuwa ndani ya kaburi **siku ine,** ndilo neno lililohakikisha kwamba hakuzimia tu. Wayuda wote walijua ya kwamba alikuwa **amekufa**. Ufufuko wake ulikuwa ajabu kweli.

**11:40** Haionekani wakati gani **Yesu** aliposema maneno ya shairi 40. Ndani ya shairi 23 alikuwa amesema na Marata kwamba ndugu yake atafufuka. Ona namna maneno yanavyofuatana ndani ya shairi 40, **"Amini ... ona."** Ni kama Bwana Yesu alikuwa amesema, "Kama utaamini tu, utaniona nikifanya ajabu kubwa ambayo Mungu tu anaweza kufanya. Utaona **utukufu wa Mungu** ukifunuliwa ndani yangu. Lakini sharti **uamini** kwanza, kisha **utaona.**"

**11:41** Basi waliondosha **jiwe** toka kaburi. Mbele ya kufanya ajabu hili, **Yesu** alishukuru **Baba** yake kwa sababu alisikia ombi lake. Hatusomi ndani ya sura hii kwamba Yesu aliomba mbele, lakini bila shaka alisemezana na Baba yake kwa wakati huu mzima na kuomba jina la Mungu liweze kutukuzwa kwa njia ya ufufuko wa Lazaro. Hapa alishukuru Baba akitangulia ajabu hili litakalofanyikana.

**11:42** Yesu aliomba na sauti ili **watu waweze** kusikia na **kuamini** kwamba Baba **alimtuma**, kwamba Baba alimwagiza nini ilimpasa kufanya na kusema, na ya kwamba saa zote alifungamana na Mungu Baba ndani ya maneno yote. Tunaona neno hili wazi tena hapa.

**11:43** Tunasoma mara chache tu ndani ya Agano Jipya juu ya Bwana Yesu **akipaza sauti kubwa.** Alifanya hivi hapa. Watu wengine wamesema kwamba asipotaja jina la **Lazaro** wazi, wafu ndani ya makaburi yote wangalitoka inje!

**11:44** Basi Lazaro **alitoka** kaburi namna gani? Wengine wanafikiri alitoka akikwenda chopi au akikokota mwili wake na mikono na magoti; wengine wanakumbuka kwamba mwili wake mzima ulizungukwa na kufungwa na sanda hata hakuweza kutoka kwa nguvu yake mwenyewe. Wanafikiri labda mwili wake ulibebwa kwa hewa toka kaburi na

kusimamishwa mbele ya Bwana Yesu. **Uso wake ulifungwa kwa kitambaa** vilevile, ndilo neno lingine lililohakikisha kwamba alikuwa amekufa. Isingaliwezekana kwa mtu **aliyefungiwa usoni** na **kitambaa** namna hii kuishi kwa siku ine. Mara hii tena Bwana alisema na watu waliosimama karibu kusaidia, na **kufungua** sanda zilizofunga Lazaro, **aende zake**. Kristo tu anaweza kufufua wafu, lakini anatugawia sisi kazi ya kuondosha vikwazo, na kusaidia kufungua watu toka desturi zao za zambi ambazo zinawafunga.

### G. Wayuda waamini na wasioamini (11:45-57)

**11:45, 46** Ajabu hili lilifahamisha **wengi** wa wale waliokuwa wakitazama ya kwamba Bwana Yesu Kristo ni kweli Mungu, na **walimwamini.** Hakuna mwingine ila yeye aliyeweza kuita mwili kutoka kaburi siku ine nyuma ya kufa!

Lakini wale wenye moyo mwovu na wa kutokuamini na uasi hawakukubali kuamini hata wakati walipoona mtu akifufuliwa toka wafu. Hivi **wengine wa Wayuda** walioona ajabu hili hawakuwa tayari kupokea Kristo kama Masiya hata kama neno hili lilihakikishwa tena na tena. Walikwenda zao kuwaambia **Wafarisayo** maneno yaliyokuwa yametokea kwa Betania. Walifanya hivi ili Wafarisayo waweze kuja na kuamini Yesu? Sivyo; labda waliwaambia kuongeza uadui wao na bidii yao kutafuta njia kumwua.

**11:47 Wakubwa wa makuhani na Wafarisayo wakakusanya Baraza** kusemezana pamoja kama iliwapasa kufanya nini juu ya neno hili. Ni kama walisema, "Kwa sababu gani hatukufanya kitu mbele? **Mtu huyu** anafanya maajabu mengi, nasi tunakaa bure." Wayuda walijihukumu wenyewe na masemo haya. Walikubali kwamba Bwana Yesu alifanya **alama nyingi**. Basi kwa nini hawakumwamini? *Hawakutaka* kuamini kwa sababu walipenda zambi zao kupita Mwokozi.

Ryle alisema,

> Tunashangaa juu ya masemo yao. Adui wakali zaidi za Bwana walilazimishwa kukubali kwamba Bwana alifanya maajabu mengi. Wangalipenda sana kukana kweli hii kama wangaliweza. Ni kama hawakujaribu kufanya hivi. Kulikuwa na maajabu mengi zaidi, na watu wengi zaidi ambao waliyaona hata Wafarisayo walikosa uhodari kujaribu kuyakana. Wakafiri na wenye mashaka wa wakati wa sasa waeleze namna gani wanaweza kuita maajabu haya hila na maono ya uwongo! Wafarisayo kwa wakati Bwana Yesu alipoishi duniani na waliojaribu kwa njia zote kushindana na Bwana hawakuwa na uhodari kukana kwamba alitenda maajabu, hivi ni upumbavu kukana maajabu haya sasa nyuma ya miaka 1800. [37]

**11:48** Viongozi walifahamu kwamba haifai wakae bure tena. Waliogopa zaidi ya watu wataaminishwa na maajabu ya Yesu. Watu wakikiri Yesu kuwa mfalme wao, neno hili litaamsha matata na Waroma. Watafikiri Yesu amekuja kuangamiza ufalme wao, na watakuja na kuazibu Wayuda. Maana ya **"wataondoa pahali petu na taifa letu"** ni ya kwamba Waroma wataharibu hekalu lao na kusambaza Wayuda. Maneno haya yalitokea kwa mwaka 70 A.D. – lakini si kwa sababu Wayuda *walipokea* Yesu, lakini kwa sababu *walimkataa.*

**11:49, 50 Kayafa** alikuwa **kuhan**i **mkubwa** toka 26-36 A.D. Ni yeye aliyehukumu Bwana Yesu na alikuwa pale wakati Petro na Yoane walipoletwa mbele ya Baraza katika Matendo 4:6. Maneno aliyosema hayahakikishi kwamba alikuwa ameamini Bwana Yesu.

Kayafa alisema mawazo ya Wafarisayo na makuhani wakubwa kwamba Wayuda watakufa kwa sababu ya Yesu hayakuwa sawa. Alitabiri kwamba alikuwa Yesu ambaye atakufa kwa ajili ya

taifa la Wayuda. Alisema ni vizuri kwa Yesu **kufa kwa ajili ya watu** ili **taifa zima** lisiangamizwe na Waroma. Tungeweza kufikiri Kayafa alifahamu kusudi la kufika kwa Yesu duniani, na ya kwamba alikuwa amempokea kama Mkombozi wa wenye zambi, ndilo mafundisho makubwa ya Wakristo. Ni huzuni ya kwamba haikuwa hivi. Maneno aliyosema yalikuwa kweli, lakini yeye mwenyewe hakuamini Yesu na kupokea wokovu.

**11:51, 52** Mashairi haya yanaeleza kwa nini Kayafa alisema maneno haya. **Hakusema kwa amri yake mwenyewe** na kutaka kwake mwenyewe. Alisema maneno ambayo Mungu alimpa kusema. Yalikuwa unabii ya kwamba **Yesu atakufa kwa taifa la Israeli**. Kayafa alipewa unabii huu kwa sababu **yeye alikuwa kuhani mkubwa mwaka ule.** Mungu alisema kwa njia yake kwa sababu ya utume wake, si kwa sababu ya haki yake mwenyewe, kwani alikuwa mwenye zambi.

Unabii wa Kayafa **haukuwa** juu ya Bwana ya kwamba atakufa kwa **taifa** la Israeli **tu, lakini vilevile** ya kwamba **atakusanya pamoja** wachaguliwa wake katikati ya Mataifa. Watu wengine wanafikiri Kayafa alifikiri juu ya Wayuda waliosambazwa duniani, lakini tunafikiri aliwaza juu ya Mataifa watakaoamini Kristo kwa njia ya mahubiri ya Habari Njema.

**11:53,54** Ajabu kwa Betania halikuaminisha Wafarisayo, lakini uadui wao kwa Mwana wa Mungu ulikaa kuongezeka. **Kuanza siku ile walifanya shauri la kumwua.**

Bwana Yesu alifahamu kwamba uadui wa Wayuda ulikaa kuongezeka, akakwenda kwa mji ulioitwa **Efuraimu**. Hatujui leo kama Efuraimu ulikuwa wapi ila ya kwamba ulikuwa pahali pa kimya **karibu na jangwa.**

**11:55** Habari ya kwamba **Pasaka ilikuwa karibu** zinatukumbusha kwamba Bwana alikaribia mwisho wa utumishi wake katikati ya watu. Atasulibishwa kwa *Pasaka hii*. **Ilipasa watu wafikie Yerusalema mbele ya Pasaka ili waweze kusafishwa.** Kwa mfano, kama Myuda alikuwa amegusa maiti, ilimpasa kufuata utaratibu fulani kuoga na kutoa zabihu. Ni huzuni kwa sababu Wayuda walikuwa wakijisafisha wenyewe, pamoja na kufanya shauri la kuua Mwana-Kondoo ya Pasaka. Kweli uovu wa watu ni mkubwa sana!

**11:56,57** Wakati watu walipokusanyika **hekaluni,** walianza kufikiri juu ya mwenye kutenda maajabu, jina lake **Yesu,** aliyekuwa inchini mwao. Walisemezana na kuulizana kama **atafikia karamu.** Shairi 57 linaonyesha kwa sababu gani wengine walifikiri hatakuja.

**Wakubwa wa makuhani na Wafarisayo** walikuwa wameleta amri kwa Yesu kufungwa. Sharti mtu ye yote aliyejua pahali alipokuwa ajulishe serikali **wapate kumkamata** na kumwua.

## 7. UTUMISHI WA MWANA WA MUNGU KWA WATU WAKE MWENYEWE (Sura 12–17)

### A. Yesu anapakaliwa mafuta kwa Betania (12:1-8)

**12:1 Yesu** alipenda sana kukaa nyumbani mwa **Lazaro**, Marata na Maria. Alikuwa na upatano mtamu pamoja nao. Ilikuwa hatari kwaye kufikia **Betania** kwa wakati huu kwani kijiji hiki kilikuwa karibu na Yerusalema, ndipo pahali pakubwa pa adui zake.

**12:2** Hata kama watu wengi walikuwa adui zake, kulikuwa na wengine waliokuwa rafiki zake waaminifu. **Lazaro alikuwa mmoja wa wale waliokula chakula pamoja na Bwana, na**

**Marata alitumikia.** Maandiko hayatujulishi kama Lazaro aliona nini nyuma ya kufa kwake na kufika saa alipofufuliwa. Labda Mungu alimkataza kusema juu ya maneno haya.

**12:3** Tunasoma juu ya mwanamke akipakaa Bwana Yesu na mafuta kupita mara moja ndani ya vitabu vya Habari Njema. Kila mara ni mbalimbali kidogo lakini walimu wanafikiri kwamba habari tunazosoma hapa zinapatana na zile tunazosoma kwa Marko 14:3-9. Mapendo makubwa ya Maria yalimsukuma kutwaa **ratli ya marasi ya nardo safi** na kupakaa **miguu** ya Yesu. Kwa njia ya tendo hili alionyesha mawazo yake ya kwamba Kristo anastahili kupokea vyote tunavyoweza kumtolea, sisi wenyewe pamoja na vyote tulivyo navyo.

Kila mara tunaposoma juu ya Maria tunamkuta kwa miguu ya Yesu. Hapa tunamwona akipanguza **miguu yake kwa nyole zake.** Nyole za mwanamke ni utukufu wake, hivi alikuwa akiweka utukufu wake kwa miguu ya Bwana. Bila shaka harufu ya marasi hii tamu ilifungana na mavazi ya Maria kwa wakati. Vivyo hivyo wakati Wakristo wanapoabudu Bwana, utamu wa saa hii unafungana nao vilevile.

**12:4, 5** Tabia ya zambi ya Yuda ilionekana wazi hapa na kupunguza utamu wa saa ile. **Yule** aliyekuwa karibu **kutoa** Bwana wake **kwa mikono ya adui** hakufurahi hata kidogo kwa **marasi** hii ya bei kubwa kutumiwa kupakaa miguu yake.

**Yuda** hakufikiri Yesu alistahili **dinari mia tatu**. Alifikiri ingalipasa **kuuza** marasi hii na **kuwapa masikini**. Alisema hivi na roho ya udanganyifu tu. Hakupenda wamasikini kama vile hakupenda Bwana. Alikuwa karibu kumtoa kwa adui zake, si kwa **dinari mia tatu,** lakini dinari makumi tatu tu. Ryle aliandika:

> Tunashangaa kuona mtu akifuata Kristo kama mwanafunzi wake kwa miaka mitatu na kuona maajabu yake yote, kusikia mafundisho yake yote, kutendewa naye na mapendo tena na tena, na hata hivi kuwa mwovu hivi rohoni. Ni neno linaloshinda ufahamu wetu, lakini habari za Yuda zinaonyesha kwamba neno hili linawezekana. Watu wachache tu wanafahamu kipimo cha kuanguka kwa watu kwa zambi. [39]

**12:6** Yoane aliongeza kusema kwamba Yuda hakusema hivi kwa sababu alihurumia **wamasikini, lakini kwa sababu** alikuwa **mwizi** na mwenye choyo. Alikuwa mwenye kuchunga sanduku ya mali; na **alichukua vilivyowekwa ndani yake** kwa faida yake mwenyewe.

**12:7** Bwana Yesu alijibu na masemo kama haya, "Usimzuize kufanya hivi. **Ameweka marasi hii kwa siku ya maziko yangu.**[40] Anataka kuniabudu sasa na kunionyeshea mapendo yake makubwa kwa njia ya kunipakaa nayo. Ana ruhusa kufanya hivi."

**12:8** Hakutakuwa na wakati kamwe bila watu **masikini** ambao wengine wataweza kusaidia. Lakini utumishi wa Bwana ulikuwa ukikaribia mwisho. Maria hatakuwa na njia kumpakaa na mafuta **siku zote**. Neno hili lingepasa kutukumbusha ya kwamba siku kwa sisi kufanya kazi ya Mungu zinapita mbio. Haifai kwa sisi kukawia kamwe kufanya kitu cho chote tunachoweza kwa Mwokozi wetu.

### B. Shauri la kuua Lazaro (12:9-11)

**12:9** Habari zilienea mbio kwamba Yesu alikuwa karibu na Yerusalema. Haikuwezekana kumficha tena. **Wengi wa Wayuda** walifikia Betania kumwona, na wengine walifika kuona **Lazaro aliyefufuliwa na Yesu toka wafu.**

**12:10, 11** Hapa tunaona tena wazimu wa kuchukia moyoni mwa mtu. **Wakubwa wa makuhani wakafanya shauri waue Lazaro vilevile.** Lazaro hakuchagua kutenda neno baya wakati

alipofufuliwa toka wafu! Hata hivi walifikiri alistahili kufa!

**Kwa sababu** ya Lazaro, **wengi wa Wayuda … waliamini Yesu.** Hivi ni kama Lazaro alikuwa amegeuka adui ya watawala, na walifikiri ilipasa kumwondosha duniani. Wale wanaoleta watu wengine kwa Bwana wanateswa mara nyingi na adui za Kristo na hata kuuawa.

Walimu wengine wanafikiri ya kwamba wakubwa wa makuhani walitaka kuondosha neno lo lote lililoshuhudia ufufuko, kwa sababu wengine wao walikuwa Wasadukayo waliokana kwamba kuna ufufuko, na kwa sababu hii walitaka Lazaro kuuawa.

### C. Kuingia Yerusalema kama mshindaji (12:12-19)

**12:12,13** Tumefika sasa kwa siku **Yesu** alipoingia **Yerusalema** kama mshindaji. Ilikuwa siku ya Bwana iliyotangulia kusulibishwa kwake.

Ni nguvu kujua kama **makutano** walifikiri nini juu ya Yesu. Walifahamu kwamba alikuwa Mwana wa Mungu na Masiya wa Israeli? Au walifikiri alikuwa Mfalme tu ambaye atawafungua toka utawala wa Waroma? Bila shaka wengine walikuwa waamini wa kweli, lakini ni kama zaidi yao hawakuweka roho juu ya Bwana.

Matawi ya **ngazi** ni alama ya raha na salama nyuma ya huzuni (Ufu. 7:9). Maana ya **"Hosana"** ni "Uponyeshe sasa, tunakuomba." Tukiweka mawazo haya mawili pamoja, ni kama watu walifikiri kwamba Yesu ndiye aliyetumwa na Mungu kuwaokoa toka ukali wa Waroma na kuwapa raha na salama nyuma ya muda mrefu wa huzuni wa kutawaliwa na Mataifa.

**12:14,15** Yesu alitembea juu ya **mwana-punda**, kama ilivyokuwa desturi kwa wakati ule. Lakini zaidi Bwana alitimiza unabii ndani ya Zekaria 9:9. Pale nabii alitabiri kwamba wakati **Mfalme** atakapofikia Israeli atakuja akitembea **juu ya mwana-punda**. **Binti ya Sayuni** ndio mfano wa Wayuda, na **Sayuni** ni kilima katika mji wa Yerusalema.

**12:16 Wanafunzi hawakufahamu** ya kwamba maneno yaliyokuwa yakitokea yalitimiza unabii wa Zekaria na ya kwamba Yesu alikuwa akiingia Yerusalema kama Mfalme wa kweli wa Israeli. **Lakini** nyuma, wakati Bwana alipokuwa amerudia mbingu **kutukuzwa** kwa mkono wa kuume wa Baba wanafunzi walitambua kwamba maneno haya yalitimiza unabii wa Maandiko.

**12:17, 18** Wengine katika makutano waliokuwa wakiona Yesu akiingia Yerusalema walimwona vilevile akifufua **Lazaro … toka wafu.** Watu hawa walipasha wengine waliosimama karibu nao kwamba huyu aliyetembea juu ya mwana-punda ndiye aliyefufua Lazaro toka wafu. Wakati habari za **alama** hii kubwa zilipoenea katikati ya watu, **makutano** makubwa sana walikuja kukutana na Yesu. Lakini walifika kwa sababu walitaka kuona mambo ya kustaajabisha, si kwa sababu walikuwa wenye imani ya kweli.

**12:19** Wakati hesabu ya watu waliotaka kuona Mwokozi ilipokaa kuongezeka, **Wafarisayo** walisumbuka sana sana. Kila neno walilojaribu kufanya kupunguza heshima ya Yesu lilikufa bure, wakalalamika kwamba **dunia yote imekwenda kumfuata**. Hawakufahamu kwamba sifa ya makutano haitadumu, na hesabu ya wale waliokuwa tayari kuabudu Yesu kama Mwana wa Mungu ilikuwa ndogo tu.

### D. Wengine wa Wayunani wanataka kuona Yesu (12:20-26)

**12:20 Wayunani** waliokuja kuona Yesu walikuwa watu wa Mataifa walioshika dini ya Wayuda. **Kufika kwao kwa karamu** kwa Yerusalema kulionye-

sha kwamba hawakufuata dini ya wazazi wao. Kufika kwao kwa Bwana Yesu wakati huu kulikuwa mfano ya kwamba wakati Wayuda walipokataa Bwana Yesu, Mataifa watasikia Habari Njema na wengi wao wataamini.

**12:21** Hatusomi kwa sababu gani **walifikia Filipo**. Labda walifika kwake kwa sababu jina lake lilikuwa jina la Wayunani na kwa sababu alikuwa **mtu wa Betesaida katika Galilaya.** Walikuwa na ombi zuri: **"Bwana, tunataka kuona Yesu."** Hamu ya kila mtu anayetaka neno hili na roho ya kweli itatimizwa.

**12:22** Labda Filipo alikuwa na shaka kidogo kama Yesu atataka kuona Wayunani hawa. Bwana alikuwa amekataza wanafunzi mbele wasifikie Mataifa na Habari Njema, hivi **Filipo** alikwenda na kumwambia **Anderea**, nao pamoja **walimwambia Yesu.**

**12:23** Wayunani walitaka kuona Yesu kwa sababu gani? Labda walifahamu kwamba viongozi Wayuda walitaka kumwua, na walitaka kumpeleka kwa inchi yao kuponyesha uzima wake. Mawazo yao hayakupatana na mawazo ya Yesu. Aliwaambia kwamba **atatukuzwa** kwa njia ya kufa kwake kama zabihu kwa zambi, si kwa njia ya kuponyesha uzima wake.

**12:24** Mbegu haizai matunda bila **kuanguka kwanza katika udongo na kufa**. Bwana Yesu alijisawanisha hapa na **mbegu ya ngano.** Kama asipokufa atabaki **peke yake**. Atafurahi na baraka za mbingu **peke yake,** bila wenye zambi waliookolewa kushiriki katika utukufu wake. Lakini kama akikufa, atatayarisha njia ya wokovu kwa watu wengi.

Neno hili ni kweli kwa sisi vilevile. T.G. Ragland anasema ya kwamba:

> Kama tukikataa kuwa mbegu za ngano – tukianguka udongoni na kufa, kama tusipokuwa tayari kuhatarisha mali au heshima au afya au nyumba au ukaribu wa jamaa, kwa ajili ya Kristo, *tutabaki peke yetu*. Lakini kama tukitaka kuzaa matunda, inatupasa kufuata Bwana wetu mwenyewe, kwa njia ya kugeuka mbegu ya ngano na kufa, *halafu tutazaa matunda mengi.* [43]

**12:25** Watu wengi wanafikiri ya kwamba maneno ya faida zaidi kwa maisha yetu ni vyakula, mavazi na furaha na anasa. Wanaishi kwa maneno haya. Lakini wakiishi hivi kwa faida yao wenyewe, hawafahamu ya kwamba hali ya roho yao ni neno kubwa kupita hali ya mwili. Kwa sababu ya kukosa kuweka roho juu ya hali njema ya roho zao, wanapoteza faida ya maisha yao. Lakini kuna wengine wanaohesabu maneno haya kuwa bure kwa ajili ya Kristo. Wanaachana na maneno yote ambayo watu wa dunia wanapenda sana kwa sababu wanapenda Kristo zaidi. Maisha yao yatazaa matunda ya milele.

**12:26** Tukitaka kutumikia Kristo inatupasa **kumfuata**. Bwana anataka watumishi wake kutii mafundisho yake na kufanana naye kwa mwenendo wao. Lazima mauti yake yawe mfano kwao. Bwana aliahidi kuwa pamoja nao na kuwalinda wakati wote, si kwa maisha wa sasa tu lakini kwa milele. Kwa wakati wa kuja Mungu ataonyesha ukubali wake kwa kazi yo yote ambayo tulifanya. Mateso au haya au laumu yo yote tunayopata sasa zitaonekana ndogo sana siku ile wakati zinaposawanishwa na utukufu wa kupokea sifa toka Mungu **Baba** mbinguni.

### E. Yesu anakaribia mauti yake sasa (12:27-36)

**12:27** Bwana alifikiri kupita na kupita juu ya matukio ambayo yatampata sasa tu. Aliwaza juu ya msalaba, na wakati atakapogeuka mwenye kubeba zambi zetu, na kuvumilia gazabu ya Mungu. **Roho yake ilifazaika** sana. Ilimpasa kuomba namna gani kwa

wakati ule? Aombe **Baba** yake **kumwokoa toka saa ile?** Hakuweza kuomba hivi kwa sababu **kusudi** la kufika kwake duniani kwa saa ile lilikuwa kwenda msalabani. Alizaliwa aweze kufa.

**12:28** Hivi Bwana Yesu hakuomba kuokolewa toka msalaba, lakini **jina** la Baba yake litukuzwe. Aliweka roho juu ya heshima ya Mungu kupita kukaa na salama yeye mwenyewe. Halafu Mungu alisema naye toka mbinguni kwamba *alikuwa* **ametukuza** jina lake na **atalitukuza** tena. Jina la Mungu lilitukuzwa ndani ya maisha ya Yesu hapa duniani. Miaka yake makumi tatu ya kwanza kwa Nazareti, miaka mitatu ya utumishi katikati ya watu, masemo na kazi za ajabu za Mwokozi – mambo haya yote yalitukuza jina la Baba. Lakini mauti, kuzikwa, ufufuko na kupanda mbinguni kwa Kristo zitatukuza Mungu zaidi.

**12:29** Wengine waliosimama karibu walisikia sauti ya Mungu lakini walifikiri ni ngurumo. Ni desturi ya watu wanaokataa kuamini maajabu kujaribu kueleza maneno yote kwa njia ya matukio ya dunia. Wengine walifahamu kwamba hawakusikia ngurumo, lakini hawakutambua kwamba ilikuwa sauti ya Mungu. Walizania ni sauti ya **malaika.** Sauti ya Mungu inaweza kusikiwa tu na watu wanaosaidiwa na Roho Mtakatifu. Watu wanaweza kusikia Habari Njema tena na tena bila kufahamu maana yake isipokuwa Roho Mtakatifu anasema nao kwa njia yake.

**12:30** Bwana alielezea wasikiaji ya kwamba *yeye* aliweza **kusikia sauti hii** bila masikio ya mtu, lakini ilitolewa kusudi watu waliokuwa wakisimama karibu waweze kuisikia vilevile.

**12:31** Alisema **"Sasa ni hukumu ya dunia hii."** Dunia ilikuwa karibu kusulibisha Bwana wa uzima na utukufu. Kwa njia ya kufanya hivi itajihukumu yenyewe na itahukumiwa kwa sababu ya tendo la kuogofya la kukataa Kristo. Hii ndiyo maana ya masemo ya Mwokozi hapa. Wanadamu wenye hatia kubwa watahukumiwa. **Mkubwa wa dunia hii** ni Shetani. Ndiyo, Shetani alishindwa kabisa kwa Kalvari. Alifikiri alikuwa ameondosha maneno ya Bwana Yesu duniani. Haikuwa hivi hata kidogo. Mwokozi alitayarisha njia ya wokovu kwa watu, na alishinda Shetani na majeshi yake yote vilevile. Shetani hahukumwi kwanza sasa, lakini tunajua kabisa kwamba ataangamizwa. Kwa wakati wa sasa anaendeleza kazi yake mbaya duniani, lakini nyuma kidogo **atatupwa** ndani ya ziwa la moto.

**12:32** Sehemu ya kwanza ya shairi ni juu ya mauti ya Kristo juu ya msalaba. Alifungwa na misumari juu ya msalaba wa mti na **kunyanyuliwa juu ya dunia.** Bwana alisema ya kwamba akisulibishwa, hivi **atakokota watu wote** kwake. Watu wameeleza maneno haya kwa njia mbalimbali. Wengine wanafikiri Kristo anakokota watu wote, au kwa wokovu, au kwa hukumu. Wengine wanafikiri kama Kristo akinyanyuliwa kwa njia ya kuhubiriwa kwa Habari Njema, kutakuwa na uwezo mkubwa ndani ya mahubiri haya, na roho za watu zitakokotwa kwake. Lakini sisi tunafikiri kwamba kwa sababu ya kusulibishwa kwa Bwana Yesu, watu *namna* **zote** wanakokotwa kwake, toka kila kabila na taifa na lugha.

**12:33** Wakati Bwana Yesu aliposema juu ya kunyanyuliwa, alionyesha namna ya **kufa kwake**, ndiyo kwa njia ya kusulibishwa. Hapa tunaona tena kwamba Bwana alijua maneno yote mbele. Alijua kwamba hatakufa kitandani au kwa njia ya tukio mbaya lo lote, lakini ya kwamba atafungwa kwa msalaba na misumari.

**12:34** Semo hili la Bwana juu ya **kunyanyuliwa** lilifazaisha **watu**. Walijua

kwamba Yesu alisema yeye ni Masiya, lakini walijua vilevile kwa njia ya Agano la Kale kwamba Masiya atakaa milele (ona Isa. 9:7; Zab. 110:4; Dan. 7:14; Mika 4:7). Ona ya kwamba watu walifikiri Yesu alisema, **"Mwana wa watu anapaswa kunyanyuliwa."** Lakini neno alilosema ndilo "nikinyanyuliwa juu ya dunia" (sh. 32). Bwana Yesu alijiita Mwana wa watu mara nyingi, na labda alisema vilevile mbele juu ya Mwana wa watu akinyanyuliwa.

**12:35** Wakati watu walipouliza Yesu kama Mwana wa watu alikuwa nani, alisema yeye ni **nuru** ya dunia. Aliwakumbusha kwamba **nuru** hii itakuwa pamoja nao kwa wakati mfupi tu. Iliwapasa kufikia Nuru na kutembea katika Nuru; kama wasipofanya hivi **giza litawashinda** nyuma kidogo, na watahangaika katika ujinga.

Ni kama Bwana alijisawanisha na jua na nuru ya mchana. Jua linapanda asubui kufika saa sita, kisha linashuka tena mangaribi, likituacha na saa chache tu ya nuru. Sharti tutumike na saa hizi kwani wakati wa usiku hatuna nuru kutusaidia. Kwa maneno ya roho, mtu anayeamini Bwana Yesu anatembea katika nuru. Mtu ambaye anamkataa **anatembea katika giza** na **hajui pahali anapokwenda.** Haongozwi na Mungu, na anahangaika.

**12:36** Bwana Yesu alionya wasikiaji wake tena **kumwamini wangalikuwa** na saa. Wakifanya hivi **watageuka wana wa nuru**. Wataongozwa na Mungu katika maisha yao mazima na hata milele. Nyuma ya kusema maneno haya Bwana **aliondokea** watu, akajificha kwa wakati.

### F. Zaidi ya Wayuda hawakuamini (12:37-43)

**12:37** Yoane alishangaa kwa sababu **watu hawakuamini** Bwana Yesu, hata kama alikuwa **amefanya alama nyingi** mbele yao. Kama tulivyosema mbele, sababu kwa kutokuamini kwao haikuwa ukosefu wa ushuhuda wa Bwana. Alikuwa ameshuhudia uungu wake tena na tena, lakini watu hawakutaka kuamini. Walitaka kutawaliwa na mfalme lakini hawakutaka kutubu.

**12:38** Kutokuamini kwa Wayuda kulitimiza unabii na ulizo katika Isaya 53:1, **"Ni nani aliyeamini habari zetu?"** Jibu la ulizo hili ni "Watu wachache tu!" Ndani ya Maandiko mkono ni mfano wa uwezo na nguvu, hivi **mkono wa Bwana** unasema juu ya uwezo mkubwa wa Mungu. Uwezo wa Mungu **unafunuliwa** kwa watu wale tu wanaoamini habari juu ya Bwana Yesu Kristo. Hivi kwa sababu watu wachache tu walipokea tangazo juu ya Masiya, uwezo wa Mungu haukufunuliwa kwa watu wengi.

**12:39** Wakati Bwana Yesu alipotukia kwa taifa la Israeli, walimkataa. Aliwarudia tena na tena na kuwaita kupokea wokovu wake, lakini walikaa kukataa. Kwa kipimo watu wanachokataa Habari Njema, kwa kipimo kile inageuka nguvu kupita kwao kuiamini nyuma. Wakati watu wanapofunga macho yao kwa Nuru, kwa kipimo kile Mungu anafunga macho yao na inageuka nguvu kupita kuona Nuru. Anawapiga na upofu wa roho, ndiyo hukumu yake kwa sababu wanakataa Mwana wake.

**12:40** Habari hizi zinatoka kwa Isa. 6:9,10. Mungu **alipofusha macho** ya watu wa Israeli na **alifanya migumu mioyo yao**. Alifanya hivi nyuma tu, wakati walipokwisha kufunga macho yao na kufanya migumu mioyo yao wao wenyewe. Kwa sababu ya ukaidi wao walikaa kuchagua kukataa Masiya, walijikatia mbali na uwezo wa kuona, ufahamu, wokovu, na kuponyeshwa.

**12:41** Ndani ya Isaya 6 tunasoma juu ya Isaya akiona **utukufu** wa Mungu. Yoane anaeleza sasa ya kwamba utukufu Isaya **alioona** na **kusema juu yake** ulikuwa **utukufu** wa *Kristo*. Hivi hili ndilo shairi lingine ya mashairi mengi

yanayohakikisha kwamba Yesu Kristo ni Mungu.

**12:42** **Wengi** wa **wakubwa** wa Wayuda waliamini kwamba Yesu ni Masiya, lakini waliogopa kujulisha watu wengine mawazo yao kwa sababu waliogopa watafukuzwa toka sunagogi. Tungependa kufikiri kwamba watu hawa walikuwa waamini wa kweli wa Bwana Yesu, lakini tuna shaka rohoni. Mtu akiwa na imani ya kweli, atakiri neno hili wazi mara moja au kwa wakati wa nyuma, si neno kama bei yake ikiwa nini.

**12:43** Ni wazi ya kwamba watu hawa waliweka roho juu ya **sifa** na ukubali wa **wenzao** kupita juu ya **sifa ya Mungu.** Inawezekana kwa mtu namna hii kuwa mwamini wa kweli wa Kristo? Soma 5:44 kuona jibu kwa ulizo hili.

**G. Hatari ya kutokuamini (12:44-50)**

**12:44** Ndani ya shairi hili Bwana alionyesha ya kwamba mtu **akimwamini yeye,** hamwamini yeye tu, **lakini** vilevile Baba yake ambaye **alimtuma**. Hapa tena Bwana alifundisha umoja wake na Mungu Baba. Haiwezekani kumwamini yeye bila kuamini Baba. Na haiwezekani kuamini Baba bila kuheshimu Mwana kuwa mwenye heshima kama yeye.

**12:45** Hatuwezi kuona Mungu Baba na macho yetu, kwani yeye ni Roho. Lakini Bwana Yesu alikuwa amefikia dunia kutujulisha kama Mungu ni namna gani, si kwa mwili lakini kwa tabia. Hivi mtu aliyeona Kristo ameona Mungu Baba.

**12:46** Ni kama Bwana alipenda sana kutumika na **nuru** kama mfano. Alijisawanisha tena na **nuru inayofika duniani** kusudi wale ambao wanamwamini **wasikae katika giza.** Bila Kristo, watu wanakaa katika giza kubwa. Hawafahamu maneno ya uzima, mauti, na milele. Lakini wale wanaoamini Kristo hawahangaiki tena kujaribu kujua kweli, kwa sababu wamempata yeye aliye kweli.

**12:47** Wakati Kristo alipokuja duniani mara ya kwanza, kusudi lake **halikuwa kuhukumu dunia lakini kuiokoa**. Hakuhukumu wale waliokataa kusikia maneno yake au kumwamini. Si kusema ya kwamba hatahukumu wasioamini hawa kwa wakati wa kuja, lakini hukumu haikuwa kusudi la kuja kwake mara ya kwanza.

**12:48** Bwana alitazamia sasa wakati wa kuja, saa watu wote ambao walikataa maneno yake watasimama mbele ya Mungu kwa hukumu. Kwa wakati ule **masemo** au mafundisho ya Bwana Yesu yatatosha kwa kuwahukumu.

**12:49** Mafundisho ya Bwana hayakuwa maneno aliyotunga yeye menyewe wala kujifunza ndani ya chuo. Kama Mtumishi na Mwana mwenye kutii, alisema maneno yale tu ambayo Baba alimwagiza **kusema**. Hili ndilo neno litakalohukumu watu siku ya mwisho. Neno Yesu alilosema lilikuwa Neno la Mungu, na watu walikataa kulisikia. Baba alimwagiza **nini** ilimpasa **kunena**, na nini ilimpasa **kusema**. Kuna tofauti. "**Maneno nitakayonena"** ndiyo neno kubwa la habari zenyewe.. **"na kuyasema"** ni juu ya maneno gani atatumika nayo kufundisha watu kweli ya Mungu.

**12:50** Yesu alijua kwamba Baba alimpa amri ya kuleta uzima wa milele kwa wale ambao watamwamini. **Hivi** alisema maneno ambayo **Baba** alimpa kusema.

Kufika sasa Bwana Yesu alijijulisha kwa taifa la Israeli. Tulisoma juu ya alama saba, na kila alama lilionyesha tukio moja wakati mwenye zambi anapoamini Kristo. Alama hizi zilikuwa:

1. Kugeuza maji kuwa mvinyo kwa karamu ya ndoa kwa Kana katika Galilaya (2:1-12). Huu ni mfano wa mwenye zambi asiyejuana na furaha ya Mungu mbele, akigeuzwa kwa uwezo wa Kristo.
2. Kuponyeshwa kwa mwana wa

mkubwa wa ufalme (4:46-54). Huu ni mfano wa mwenye zambi aliye mgonjwa na anayehitaji kuponyeshwa rohoni.

3. Kuponyeshwa kwa kiwete kwa birika la Betesaida (sura 5). Mwenye zambi ni bila nguvu, na hawezi kujisaidia mwenyewe. Yesu alimponyesha toka uzaifu wake.
4. Kukulishwa kwa watu elfu tano (sura 6). Mwenye zambi ni bila chakula, mwenye njaa, na mwenye hitaji la kupewa nguvu. Bwana analeta chakula kwa roho yake, asiye na njaa tena kamwe.
5. Kutuliza Bahari ya Galilaya (6:16-21). Mwenye zambi ni kwa pahali pa hatari. Bwana anamponyesha toka tufani.
6. Kuponyeshwa kwa mtu aliyezaliwa kipofu (sura 9). Mtu huyu ni mfano wa upofu wa moyo wa mtu kufika wakati uwezo wa Kristo unapomgusa. Hawezi kuona uovu wake mwenyewe, wala uzuri wa Mwokozi, kufika wakati anapopewa nuru na Roho Mtakatifu.
7. Kufufuliwa kwa Lazaro toka wafu (sura 11). Alama hii inatukumbusha kwamba mwenye zambi ni mfu katika makosa na zambi, na anahitaji uzima toka juu.

Kusudi la alama hizi zote ni kuhakikisha kwamba Yesu ni Kristo, Mwana wa Mungu.

### H. Yesu ananawa miguu ya wanafunzi (13:1-11)

Sura 13 ni mwanzo wa hotuba ya Yesu katika chumba cha juu. Hakutembea tena katikati ya Wayuda wenye roho ya uadui. Alikuwa amekwenda pamoja na wanafunzi wake kwa chumba cha juu ndani ya nyumba moja katika Yerusalema kukaa pamoja nao mara ya mwisho na upatano mtamu, mbele ya kuhukumiwa na kusulibishwa. Sura 13-17 za Yoane ni sura zinazopendwa sana katika Agano Jipya nzima.

**13:1** Siku moja mbele ya kusulibishwa kwake, Bwana **Yesu alifahamu kwamba saa imefika** kwa yeye kufa, kufufuliwa, na kurudi mbinguni. **Alipenda watu wake**, ndio wale waliokuwa waamini wa kweli. **Aliwapenda hata mwisho** wa utumishi wake duniani, na atawapenda kwa milele. Na vilevile **aliwapenda na mapendo matimilifu**, kama alivyoonyesha nyuma kidogo.

**13:2** Yoane hasemi wazi kama ilikuwa **chakula** gani, au Pasaka, au Karamu ya Ukumbusho, au chakula cha mangaribi tu. **Shetani** alifahamisha **Yuda** kwamba saa ilitimia **kutoa Yesu** kwa mikono ya adui zake. Yuda alikuwa ametayarisha njia kutoa Yesu kwa adui zake **kwa siku nyingi** mbele, na sasa alipewa ruhusa kutimiza shauri lake ovu.

**13:3** Shairi 3 linaonyesha wazi kama alikuwa *nani* ambaye alifanya kazi hii ya mtumwa – hakuwa rabi au mwalimu tu, lakini **Yesu** mwenyewe, akikumbuka uungu wake. Alijua kazi ambayo alipewa, ya kwamba **ametoka kwa Mungu** na alikuwa ameanza safari yake kurudi **kwa Mungu.**

**13:4** Kujua kwamba yeye ni nani, na ya kama kazi yake ilikuwa nini, kulimwezesha kujishusha na kunawa miguu ya wanafunzi. **Akisimama toka pahali pa chakula akaondosha mavazi yake** marefu ya inje. Halafu alitwaa kitambaa na kujifungia kiuno kama mtumwa. Tungefikiri tutasoma habari hizi ndani ya Habari Njema ya Marko, Habari Njema ya Mtumishi Mkamilifu. Ni ajabu kubwa zaidi kuzisoma ndani ya Habari Njema ya Mwana wa Mungu.

Tendo hili lenye maana linatukumbusha kwamba Bwana aliondokea utukufu wa mbingu, akashukia dunia hii kama Mtumishi na kutumikia watu wale ambao aliumba.

**13:5** Namna ya viatu watu walivyo-

vaa katika inchi za mashariki kwa wakati ule ililazimisha wenye kuvivaa **kunawa miguu** yao mara nyingi. Ilikuwa adabu kwa mwenye nyumba kuwa na mtumwa mwenye kazi ya kunawa miguu ya wageni. Hapa mwenye kukalisha wageni alikuwa Mwana wa Mungu aliyegeuka mtumwa na kufanya kazi hii ya chini, na tunaona Yesu akinawa miguu ya mwenye kumtoa kwa adui zake! Habari hizi zina mafundisho makubwa kwa sisi!

**13:6** **Petro** alishituka kabisa juu ya Bwana **akinawa miguu** *yake,* akamjulisha kwamba hakufurahi kwa mwenye heshima kubwa kama Bwana kujishusha kunawa miguu yake asiyestahili hata kidogo.

**13:7** Halafu **Yesu** alielezea Petro ya kwamba maneno haya aliyofanya yalikuwa mfano wa *kusafishwa kwa roho.* Petro **hakufahamu** *maana* ya tendo hili kwanza saa ile lakini **ataijua** nyuma kidogo, kwa sababu Bwana aliieleza. Na **ataijua** nyuma ndani ya maisha yake mwenyewe wakati alipokwisha kukana Bwana mara tatu, na alirudishwa karibu naye tena.

**13:8** Petro alionyesha kwamba sisi watu ni wenye kugeukageuka kabisa. Alisema na Bwana na nguvu: **"Hutanawa miguu yangu kamwe."** Maana ya *kamwe* hapa ni *hapana kwa milele.* Bwana alijibu Petro ya kwamba hatakuwa na ushirika naye kama hamnawi. Halafu tunapokea maelezo ya maana ya tendo la kunawa miguu. Wakati Wakristo wanapotembea hapa duniani wanasikia na kuona maneno machafu na wanatumika pamoja na wasioamini, na roho na nia zao zinachafuwa. Hivi mwamini anahitaji saa zote kusafishwa rohoni.

Tunasafishwa kwa njia ya maji ya Neno la Mungu. Wakati tunaposoma Biblia, au kusikia mahubiri na kusemezana na wenzetu, roho zetu zinasafishwa toka zambi na uchafu ambazo zinatuzunguka. Lakini wakati tunapokosa kusoma Biblia, uovu wa dunia hautusumbushi tena. Wakati Yesu aliposema na Petro, **"huna shirika pamoja nami,"** maana yake haiko kusema Petro hawezi kuokolewa bila kuoshwa na Bwana, lakini kwamba sharti roho yake isafishwe saa zote kwa njia ya kusoma Maandiko Matakatifu, kusudi aweze kuwa na upatano na ushirika mzuri pamoja na Bwana.

**13:9, 10** Sasa **Petro** aligeuka kabisa tena. Dakika moja mbele alisema "kamwe." Sasa alisema na Bwana kumnawa mwili mzima.

Wakati mtu aliporudi toka pahali alipooga, miguu yake ilichafuwa tena. Mtu huyu hakuhitaji kuoga tena mwili mzima, lakini kunawa miguu yake tu. **"Yeye aliyeoga hahitaji ila kunawa miguu yake tu, lakini yeye ni safi kabisa."** Chombo cha *kuogea* ni namna nyingine na *kibakuli*. Kinasema kwamba mtu anasafishwa kabisa siku anapopokea wokovu. Ni kusafishwa toka *azabu* ya zambi. Neno hili linatokea mara moja tu kwa njia ya damu ya Kristo. Kibakuli kinasema juu ya kusafishwa toka uchafu wa zambi tunakohitaji kila saa kwa njia ya Neno la Mungu. Tunaogwa mara moja tu, lakini tunahitaji kunawa miguu tena na tena. **"Ninyi ni safi, lakini si wote"** ni kusema wanafunzi wote wa- lioshwa, maana walizaliwa tena – ila mmoja wao, ndiye Yuda. Yuda hakupokea wokovu kamwe.

**13:11** Bwana mwenye kujua maneno yote **alijua** kwamba Yuda **atamtoa kwa adui** zake, hivi alisema juu yake kwamba hakuoshwa na kukombolewa kamwe.

### I. Yesu anafundisha wanafunzi wake kumwiga (13:12-20)

**13:12** Ni kama Bwana Yesu **alinawa miguu** ya wanafunzi *wote*, kisha alivaa **mavazi yake na kukaa tena** kuwaelezea maana ya maneno aliyokwisha kufanya. Alianza maelezo yake na ulizo. Mwokozi alitumika na maulizo mara nyingi ndani ya mafundisho yake. Kuna mafundisho

ya faida nyingi kwa sisi ndani ya maulizo ya Bwana.

**13:13, 14** Wanafunzi walikubali mbele kwamba Yesu ni **Mwalimu na Bwana** wao, na ilikuwa vema kwao kufanya hivi, lakini aliwaonyesha kwa njia ya mfano wake ya kama nafasi ya juu zaidi ndani ya cheo cha ufalme ni nafasi ya mtumishi.[9]

**Kama Bwana na Mwalimu** wao **alinawa miguu** ya wanafunzi, nini iliwazuiza wasinawe **miguu ya wenzao?** Bwana alikuwa akisema kwamba iliwapasa kunawana miguu *na maji?*[10] Alikuwa akisimamisha amri mpya kwa kanisa? Sivyo, maneno haya yalikuwa na maana ya roho. Alikuwa akiwaambia kwamba iliwapasa kusaidiana na kusafishana kwa njia ya kushirikiana mara kwa mara kwa njia ya kusoma Neno la Mungu pamoja. Mkristo fulani akiona ndugu yake akipoa rohoni na kurudi kwa maneno ya dunia, inampasa kumwonya na mapendo na Neno la Mungu.

**13:15,16** Bwana alikuwa **amewapa mfano** wa namna gani iliwapasa **kusaidiana** kwa maneno ya roho.

Kama majivuno au machuki yakituzuiza tusijinyenyekeze kutumikia ndugu zetu, tukumbuke kwamba **hatuko wakubwa kupita Bwana wetu**. Yeye alijinyenyekeza kunawa miguu ya wale wasiostahili na wasiokuwa na asante, na alijua mmoja wao atamtoa kwa mikono wa adui zake. Wewe ungekuwa tayari kutumikia na unyenyekevu mtu fulani ukijua alikuwa karibu kukuuza kwa adui zako kwa mali? Haifai wale **waliotumwa** (ndio wanafunzi) kufikiri wao ni wakubwa kupita Bwana wao na kukataa kufanya neno lo lote ambalo **mwenye kuwatuma** (Bwana Yesu) alikuwa amefanya.

**13:17** Ni vizuri **kujua** kweli hizi juu ya unyenyekevu na kutumikia wengine bila kujifikiri mwenyewe. Ni baraka kubwa zaidi ***kuzitenda***.

**13:18** Maneno Bwana aliyofundisha sasa tu juu ya utumishi **hayakuwa** kwa Yuda. Hakuwa mmoja wa wale ambao Bwana atatuma duniani pote na Habari Njema. Yesu alijua kwamba ilikuwa **sharti** kwa Maandiko, kama Zaburi 41:9, **yatimizwe**. Yuda alikuwa amekula pamoja na Bwana kwa miaka mitatu, lakini hata hivi **alinyanyua kisigino chake** juu yake, maana yake alitoa Bwana kwa adui. Ndani ya Zaburi 41 mhaini aliitwa "rafiki yangu ya karibu."

**13:19** Bwana alijulisha wanafunzi wake mbele ya kutokea kwao, habari za kutolewa kwake kwa adui ili **wakati zitakapotimizwa** wanafunzi watajua kwamba Yesu ni Mungu kweli. Wakati Yesu aliposema **"mimi ndiye"** (kwa mwisho wa shairi 19) alionyesha kwamba yeye ni Yehova wa Agano la Kale. Hivi, unabii unaotimizwa unahakikisha uungu wa Kristo, pamoja na kusimamia ya kwamba kuandika kwa Maandiko yaliongozwa na Mungu kweli.

**13:20** Bwana wetu alijua kwamba labda kutolewa kwake na Yuda kwa adui zake kutakuwa kikwazo kwa wanafunzi wengine na kuamsha shaka ndani ya roho zao. Hivi aliongeza maneno haya kutia roho zao nguvu. Wakumbuke kwamba walikuwa wakitumwa kwa kazi kwa Mungu. Wafungamishwe karibu karibu na Bwana, hata watu wakiwapokea nyumbani, ni kama walipokea Bwana. Vilevile, wote waliopokea Kristo walipokea Mungu Baba. Wafarijiwe basi wakati walipokumbuka walifungamishwa na Mungu Mwana na Mungu Baba.

### J. Yesu anatabiri kwamba atatolewa kwa adui (13:21-30)

**13:21, 22** Kujua kwamba mmoja wa wanafunzi wake atamtoa kwa mikono ya adui kulikuwa **mzigo mzito** kwa roho ya Bwana. Ni kama alimpa Yuda njia mara ya mwisho kuachana na shauri lake ovu. Bila kutaja jina lake wazi alionyesha

kwamba alijua **mmoja** wa wanafunzi kumi na wawili **atamtoa**. Lakini hata neno hili halikugeuza nia ya mhaini.

Wanafunzi wengine hawakuwa na mashaka juu ya Yuda. Walishangaa kusikia kwamba mmoja wao atatenda neno ovu namna hii, wakafazaika kama alikuwa nani.

**13:23** Kwa wakati ule watu hawakuzunguka meza wakiketi juu ya viti saa ya kula chakula, lakini walikaa juu ya vitanda vya chini. Mwanafunzi **aliyependwa na Yesu** alikuwa Yoane, mwandishi wa kitabu hiki. Hakutaja jina lake lakini hakuogopa kusema kwamba Bwana alimpenda sana. Bwana alipenda wanafunzi wake wote, lakini ni kama Yoane alikuwa na ushirika wa karibu zaidi naye.

**13:24, 25** Kwa sababu hii **Petro, bila kusema neno, alimpungia mkono** kumwomba kuuliza Yesu jina la mwenye kumtoa.

**Akiegamia kifua cha Yesu,** Yoane alimwuliza na sauti ndogo na Yesu alimjibu vivyo hivyo.

**13:26** Yesu alisema ataleta **kipande cha mkate** nyuma ya **kukitowelea** ndani ya mvinyo au mchuzi wa nyama kwa yule ambaye atamtoa kwa mikono ya adui. Wengine wanasema ilikuwa desturi kwa inchi za mashariki kwa mwenye nyumba kumpa mgeni mheshimiwa kipande hiki cha mkate. Kwa njia ya kufanyiza **Yuda** mgeni mheshimiwa, Bwana alijaribu tena na mapendo na neema kuamsha roho ya toba ndani yake. Watu wengine wanasema ilikuwa desturi kupitisha mkate huu kwa karamu ya Pasaka. Kama neno hili ni kweli, Yuda aliondokea pahali pa chakula saa ya Pasaka na mbele ya kusimamishwa kwa karamu ya Ukumbusho wa Bwana.

**13:27** Shetani alikuwa ameweka mawazo ndani ya nia ya Yuda kutoa Yesu kwa adui. Sasa **Shetani alimwingia**. Kwanza Yuda aliwaza tu juu ya kutoa Yesu, na alipendezwa na mawazo yenyewe na kuyakubali. Sasa Shetani alimtawala kabisa. Yesu akijua kwamba mwenye kumtoa hatageuka, alisema naye **kufanya** neno lenyewe **upesi.** Hakumsukuma kutenda mabaya lakini alionyesha huzuni tu.

**13:28, 29** Shairi 28 linaonyesha wazi kwamba wanafunzi wengine hawakusikia maneno Yoane na Yesu waliyosema mbele. Hawakujua kwamba Yuda alikuwa karibu kutoa Bwana wao kwa adui.

**Wengine walifikiri** Yesu alisema na Yuda kwenda **kununua** vitu vingine kwa **karamu** au kutoa zawadi kwa **wamasikini** kwa sababu Yuda alikuwa mwenye kuchunga mali.

**13:30** Yuda alipokea **mkate** uliokuwa alama ya upendeleo, kisha akaondokea Bwana na wanafunzi, na **ulikuwa usiku.** Haukuwa **usiku duniani** tu, lakini **ndani ya roho** ya Yuda vilevile – usiku wa giza na majuto bila mwisho. Ni giza kila mara watu wanapokataa Mwokozi.

### K. Amri mpya (13:31-35)

**13:31** Nyuma ya kuondoka kwa Yuda, **Yesu** alianza kusema kwa mioyo ya wanafunzi bila kizuizo. Alisema, **"Sasa Mwana wa watu ametukuzwa."** Bwana alitazamia kazi ya ukombozi ambayo alikuwa karibu kutimiza. Labda mauti yake ilionekana kama alikuwa ameshindwa, lakini kwa njia yake wenye zambi wataweza kuokolewa. Atafufuka tena na kupanda kurudi mbinguni, na alitukuzwa sana ndani ya maneno haya yote. Na **Mungu ametukuzwa** ndani ya kazi ya Mwokozi. Ilitangaza kwamba yeye ni Mungu *mtakatifu* asiyeweza kuacha zambi kupita bila azabu, lakini Mungu wa *mapendo* vilevile asiyetaka mauti ya mwenye zambi hata mmoja. Na ilitangaza kwamba yeye ni Mungu wa *haki,* anayeweza kuhesabia haki wenye zambi hata hivi. Uungu wake ulitukuzwa sana kwa kila njia kwa Kalvari.

**13:32 “Kama Mungu ametukuzwa ndani yake,”** ndilo neno la kweli, **“Mungu atamtukuza ndani yake mwenyewe.”** Mungu ataweka roho kwa Mwana wake mpendwa kupewa heshima ya kufaa. **“Na atamtukuza mara moja”** – bila kukawa. Mungu Baba alitimiza unabii huu juu ya Bwana Yesu kwa njia ya kumfufua toka wafu na kumkalisha kwa mkono wake wa kuume mbinguni. Hakungoja kufika kwa kusimamishwa kwa ufalme lakini **alitukuza** Mwana wake mara moja.

**13:33** Hii ni mara ya kwanza Bwana Yesu aliita wanafunzi wake **watoto wadogo** – jina la mapendo. Aliwaita na jina hili nyuma ya kuondoka kwa Yuda tu. Atakuwa **pamoja nao** kwa **wakati kidogo tu,** mbele ya kufa kwake msalabani. **Watamtafuta** lakini hawataweza kumfuata kwa sababu atarudi mbinguni. Bwana alikuwa amewaambia **Wayuda** maneno haya vilevile, lakini na maana nyingine. Ataondokea wanafunzi wake kwa wakati tu (sura 14), lakini ataondokea Wayuda kabisa. Alikuwa akirudi mbinguni, nao hawakuweza kumfuata kwa sababu ya kutokuamini kwao.

**13:34** Wakati Bwana alipokuwa mbali na wanafunzi wake alitaka watawaliwe na **agizo la mapendo**. Agizo hili halikuwa mpya kwa wakati ule kwa sababu Amri Kumi zilifundisha watu kupenda Mungu na jirani zao. Lakini **lilikuwa jipya** kwa njia nyingine. Lilikuwa **jipya** kwa sababu Roho Mtakatifu atawezesha waamini kulitii. Lilikuwa **jipya** kwa sababu lilikuwa *zuri kupita* agizo la zamani. Agizo la zamani lilisema, “Penda *jirani* yako,” lakini agizo jipya lilisema, “Penda *adui* zako.” Na ndani ya shairi hili tunaona kwamba lilikuwa jipya kwa sababu liliagiza mapendo ya *kipimo kikubwa kupita:* **“Kama mimi nilivyowapenda ninyi, ninyi mupendane vilevile.”**

**13:35** Neno linaloonyesha kwamba mtu ni Mkristo si msalaba mdogo wa chuma anachovaa kwa mwili wake au kufunga kwa vazi lake, wala mavazi yaliyo namna nyingine na yale ya wasioamini. Si nguvu kukiri kuwa Mkristo kama maneno haya tu yangalihitajiwa. Alama ya kweli ya Mkristo ni **mapendo** yake kwa Wakristo wenzake. Mapendo namna hii yanahitaji uwezo toka Mungu unaoletwa tu kwa watu wanaokaaliwa na Roho Mtakatifu.

### L. Yesu anatabiri kwamba Petro atamkana (13:36-38)

**13:36 Simoni Petro** hakufahamu kwamba Yesu alisema juu ya kufa kwake. Alifikiri atakwenda safari kwa pahali pengine, na hakufahamu kwamba hataweza kwenda pamoja naye. Bwana alieleza kwamba Petro **atamfuata** *kweli* kwa wakati wa kuja, maana wakati atakapokufa, lakini si kwa wakati ule.

**13:37** Kama ilivyokuwa desturi yake, **Petro** hakukawa kusema kwamba alikuwa tayari kufa kwa ajili ya Bwana. Alifikiri ataweza kuvumilia maumivu haya kwa nguvu yake mwenyewe. Kwa wakati wa nyuma alikufa kweli kwa ajili ya Bwana, lakini alikuwa amepewa nguvu na uhodari toka Mungu kwa kuweza kufanya hivi.

**13:38 Yesu** alimjulisha kwamba bidii yake ilikosa ufahamu. Alimpasha neno ambalo Petro hakujua mwenyewe, ya kwamba mbele ya mapambazuko ya asubui Petro atakana Bwana **mara tatu**. Basi Petro alikumbushwa uzaifu na ukosefu wa uhodari wake na ya kwamba hakuweza kufuata Bwana hata kwa saa chache kwa nguvu yake mwenyewe.

### M. Yesu: Njia, Kweli, na Uzima (14:1-14)

**14:1** Watu wengine wanasema shairi hili linafungana na mwisho wa sura 13, na Yesu alilisema na Petro, kumfariji, hata kama atakana Bwana wake. Lakini namna lilivyoandikwa kwa Kiyunani

inaonyesha kwamba alilisema kwa wanafunzi wake *wote.* Ni kama alisema, "Nitawaondokea ninyi, na hamutaweza kuniona, lakini **musifazaike moyoni; munaamini Mungu,** hata kama hamwoni na macho. Sasa **muniamini mimi** vivyo hivyo." Hapa tena Bwana alionyesha wazi kwamba yeye na Mungu ni sawasawa.

**14:2 Nyumba ya Baba** ndiyo mbingu, pahali kuna makao mengi. Kuna nafasi ya kutosha kwa wakombolewa wote. **Kama sivyo,** Bwana **angaliwaambia.** Asingaliamsha tumaini la uwongo ndani ya roho zao. **"Ninakwenda kuwatengenezea ninyi pahali."** Semo hili linaweza kuelezwa kwa njia mbili. Bwana alikwendea Kalvari kutayarishia watu wake pahali. Kufa kwake kwa zambi zao kulipatia waamini pahali pale. Lakini Bwana alirudia mbingu vilevile kutayarisha pahali. Hatujui maneno mengi juu ya pahali pale, lakini tunajua pahali panatayarishwa kwa kila mtoto wa Mungu.

**14:3** Shairi hili ni juu ya wakati Bwana **atakaporudi tena** kwa hewa, wakati waamini waliokufa watakapofufuliwa, wakati waamini hai watakapogeuzwa, na wakati makutano makubwa wa wote waliokombolewa kwa damu ya Yesu watakapopelekwa mbinguni (1 Tes. 4:13-18; 1 Kor. 15:51-58). Saa ile Kristo atakuja yeye mwenyewe. Hakika, namna Kristo alivyokwenda zake, vivyo hivyo **atarudi tena**. Anataka sana kwa watu wake kuwa pamoja naye kwa milele.

**14:4,5** Alikuwa akikwenda zake mbinguni, nao walijua **njia kufikia mbingu**, kwani alikuwa amewaambia tena na tena.

Ni kama **Tomasi** hakufahamu maana ya maneno Bwana aliyosema. Labda alifikiri, kama Petro, juu ya kufanya safari tu hapa duniani.

**14:6** Shairi hili tamu linaeleza wazi kabisa kwamba Bwana Yesu Kristo mwenyewe ndiye **njia** kufika mbinguni. Haonyeshi tu njia, lakini yeye mwenyewe *ni* **njia**. Wokovu unapatikana ndani ya Yesu. Ukipokea Yesu kuwa Mwokozi wako, unapokea wokovu. Bwana Yesu ni njia *ya pekee* kufika kwa Mungu. **Mtu hakuji kwa Baba ila kwa yeye**. Njia kufikia Baba si Amri Kumi, ubatizo au karamu ya ukumbusho, si kuwa mtu wa kanisa fulani. Ni kwa njia ya Kristo tu, yeye peke yake. Kwa wakati wa sasa watu wengi wanasema si neno kama tukiamini nini kama tukiamini neno lenyewe na roho moja. Wanasema kuna maneno mazuri ndani ya kila dini, na kwamba mwishoni dini zote zinafikisha watu mbinguni. Lakini Yesu alisema, **"Mtu hakuji kwa Baba, ila kwa mimi."**

Na Bwana ni **kweli**. Yeye si mwenye kufundisha tu kweli; yeye *ni* **kweli**. Yeye ni Kweli ndani ya mwili. Wale walio na Kristo wana Kweli. Haipatikani pahali po pote pengine.

Kristo Yesu ni **uzima**. Uzima unatoka kwake, uzima wa roho, na wa milele. Wale ambao wanampokea yeye wana uzima wa milele kwa sababu yeye *ni* Uzima.

**14:7** Halafu mara moja tena Bwana alifundisha umoja wa siri ambao unatushinda kufahamu wa Baba na yeye mwenyewe. Kama wanafunzi wangalitambua kweli kama Yesu alikuwa nani, **wangalijua Baba vilevile**, kwa sababu Kristo alifunua Baba kwa watu. **Kuanza saa ile**, na zaidi nyuma ya ufufuko wake wanafunzi watafahamu kwamba Yesu alikuwa Mungu Mwana. Halafu watafahamu kwamba kujua Kristo ni **kujua** Baba, na wakiona Bwana Yesu ni kuona Mungu.

Shairi hili halifundishi ya kwamba Mungu Baba na Bwana Yesu ni Nafsi moja, Lakini kuna *Nafsi* tatu ndani ya *Mungu mmoja* – Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.

**14:8** **Filipo** alitaka **Bwana** kumpa ufunuo mwingine wa **Baba**, na halafu hataomba tena neno lingine. Hakufahamu kwamba Bwana mwenyewe, na yote aliyofanya na kusema ulikuwa ufunuo wa Baba.

**14:9** Yesu alimjibu na saburi. Filipo alikuwa amekaa pamoja na Bwana kwa muda **mrefu**. Alikuwa mmoja wa wanafunzi wa kwanza (Yn.1:43). Hata hivi alikuwa hajafahamu uungu wa Kristo, na umoja wake na Baba. Hakufahamu kwamba wakati alipoangalia Yesu, aliona Mmoja aliyeonyesha **Baba** na ukamilifu.

**14:10, 11** Maneno **"Mimi ni ndani ya Baba, na Baba** ni **ndani yangu"** yanaonyesha ukaribu wa **Baba** na Mwana. Hata kama wao ni Nafsi mbalimbali, wao ni moja kwa maneno ya tabia na kutaka kwao. Haifai tushangae kama hatuwezi kufahamu maneno haya. Hakuna mtu wa dunia ambaye atayafahamu kamwe. Mungu anajua maneno tusiyoweza kujua kamwe. Kama tungalimfahamu kabisa tungalikuwa sawasawa naye kwa ukubwa! Yesu alikuwa na uwezo kusema maneno na kufanya alama, lakini alifika duniani kama Mtumishi wa Yehova, na alitii Baba kabisa ndani ya masemo na matendo yake.

Ingepasa wanafunzi **kuamini** kwamba alikuwa mmoja na **Baba** kwa sababu yeye mwenyewe alisema hivi. Lakini kama wasipoamini neno hili, iliwapasa kuamini kwa sababu ya **kazi** alizofanya.

**14:12** Bwana alitabiri kwamba wale ambao walimwamini watafanya maajabu kama yeye, na hata **kazi kubwa kupita.** Ndani ya Matendo tunasoma juu ya mitume wakifanya maajabu kuponyesha miili ya watu, yaliyofanana na yale ambayo Bwana alifanya. Lakini tunasoma juu ya maajabu hata makubwa kupita – kama wokovu wa watu elfu tatu siku ya Pentekote. Bila shaka wakati Bwana aliposema juu ya **kazi kubwa kupita** alifikiri juu ya kutangazwa kwa Habari Njema katika dunia nzima, wokovu wa watu wengi sana, na kusimamishwa kwa kanisa. Kuokoa roho za watu ni kazi **kubwa kupita** kuponyesha miili yao. Bwana Yesu alitukuzwa wakati aliporudia mbingu na Roho Mtakatifu alipotumwa duniani. Kwa uwezo wa Roho Mtakatifu mitume walifanya maajabu yale yaliyokuwa makubwa kupita.

**14:13** Bila shaka wanafunzi walifarijiwa sana kujua kwamba, hata Bwana alikuwa karibu kuwaondokea, wataweza kuomba Baba kwa jina lake na kupata maneno waliyoomba. Maana ya shairi hili haiko kwamba mwamini anaweza kupata kitu cho chote anachotaka toka Mungu. Maneno haya **kwa jina langu** yanatusaidia kufahamu ahadi hii – **mukiomba lo lote kwa jina langu**. Kuomba kwa jina la Yesu si kuongeza tu jina la Yesu kwa mwisho wa ombi lako. Ni kuomba maneno yanayopatana na nia na kutaka kwake. Ni kuomba maneno yale ambayo yatatukuza Mungu, yatakuwa baraka kwa watu, na kusaidia roho zetu wenyewe.

Tukitaka kuomba kwa jina la Kristo, inatupasa kumfuata karibu karibu. Bila kufanya hivi hatutaweza kujua mapenzi yake. Kwa kipimo tunapomfuata karibu karibu, maneno ambayo sisi tunataka yatakuwa sawasawa na yale yeye anayotaka. **Baba anatukuzwa ndani ya Mwana** kwa sababu Mwana anataka tu maneno yanayopendeza Mungu. Tukiomba hivi na kupata majibu kwa maombi yetu, Mungu anatukuzwa sana.

**14:14** Ndani ya shairi hili Bwana alitoa ahadi tena mara ya pili kutia mioyo ya watu wa Mungu nguvu. Ishi ukifanya mapenzi ya Mungu, tembea karibu sana na Bwana, **omba neno lo lote** ambalo Bwana angetaka, na utapata majibu kwa maombi yako.

**N. Ahadi ya kuja kwa Msaidizi mwingine (14:15-26)**

**14:15** Bwana Yesu alikuwa karibu kuondokea wanafunzi wake, nao watahuzunishwa sana. Wataweza kumwonyeshea **mapendo** yao namna gani? Kwa njia ya kutii amri zake. Si kwa njia ya machozi, lakini kwa njia ya utii. **Amri** za Bwana ndizo mafundisho ambayo alitutolea ndani ya Habari Njema ine, na ndani ya vitabu vingine vyote vya Agano Jipya.

**14:16** Neno linalotumiwa hapa kwa **omba** si neno linalotumiwa na mtu wa chini akiomba kitu toka mkubwa wake. Ni neno linalotumiwa na mtu kuomba kitu toka mtu aliye mamoja naye. Bwana ataomba Baba kutuma **Msaidizi mwingine**. Maana ya neno kwa **Msaidizi** (*Paraclete*) ni mmoja anayeitwa kusaidia mwingine. Linatafsiriwa Mwombezi vilevile (1 Yn. 2:1). Bwana Yesu ni Mwombezi au Msaidizi, na Roho Mtakatifu ni **Msaidizi mwingine** – si wa namna nyingine kabisa, lakini na tabia sawasawa naye. Roho Mtakatifu **atakaa** pamoja na waamini **milele**. Ndani ya Agano la Kale, Roho Mtakatifu alikuja juu ya watu kwa saa mbalimbali na mara nyingi aliwaacha tena. Wakati wa sasa atakuja na kukaa **milele.**

**14:17** Roho Mtakatifu anaitwa **Roho ya kweli** kwa sababu mafundisho yake ni kweli na anatukuza Kristo aliye kweli. **Dunia haiwezi kupokea Roho Mtakatifu** kwa sababu haiwezi kumwona. Wasioamini wanataka kuona mbele ya kuamini – hata kama wakiamini kuna upepo na umeme wasizoweza kuona vilevile. Wasioamini hawajui wala kufahamu Roho Mtakatifu. Anachokoza roho zao juu ya zambi zao lakini hawafahamu kwamba ni yeye. Wanafunzi walijuana na Roho Mtakatifu akitumika ndani ya maisha yao na walikuwa wakimwona akitumika kwa njia ya Bwana Yesu.

**"Anakaa pamoja nanyi, naye atakuwa ndani yenu."** Mbele ya Pentekote Roho Mtakatifu alikuja juu ya watu na kukaa **pamoja** nao. Lakini tangu Pentekote, wakati mtu anapoamini Bwana Yesu, Roho Mtakatifu anakuja kukaa ndani ya maisha ya mtu huyu kwa milele. Daudi aliomba, "Usiniondoe Roho Mtakatifu wako," lakini ombi hili halitoshi kwa wakati wa sasa. Roho Mtakatifu haondoshwi kamwe toka maisha ya mwamini, hata kama inawezekana kwa mwamini kumhuzunisha, kuzuiza kazi yake ndani yake, au kumzima.

**14:18** Bwana **hataacha** wanafunzi wake kama **mayatima**. **Atawafikia** tena. Ndiyo, aliwafikia nyuma ya ufufuko wake, lakini hatufikiri alisema juu ya neno hili hapa. Alikuja kwao kwa njia ya Roho Mtakatifu siku ya Pentekote. Kuja kwake kwa roho ndiyo maana ya kweli hapa. "Pentekote ilikuja kama kuja kwa Yesu." Na atakuja kwao yeye mwenyewe kwa mwisho wa muda huu, wakati atakapopeleka wachaguliwa wake kwake mbinguni.

**14:19** Hakuna msiyeamini aliyeona Bwana Yesu nyuma ya kuzikwa kwake. Nyuma ya kufufuliwa kwake wale ambao walimpenda tu walimwona. Lakini hata nyuma ya kupanda kwake kwenda mbinguni wanafunzi wake walikaa kumwona kwa imani. Bila shaka hii ndiyo maana ya maneno haya, **"lakini mutaniona**." Wakati watu wa dunia wasipoweza kumwona tena, wanafunzi wake watakaa kumwona. **"Kwa sababu mimi ni hai, nanyi mutakuwa hai vilevile."** Alikuwa akitazama mbele kwa uzima wake nyuma ya ufufuko. Utakuwa kama arabuni ya uzima kwa wote ambao walimwamini. Hata wakikufa, watafufuliwa na hawatakufa tena kamwe.

**14:20** Tunafikiri **"Katika siku ile"** ni tena juu ya kushuka kwa Roho Mtakatifu. Atafundisha waamini katika kweli

ya kwamba namna Baba na Mwana wanafungana pamoja, vivyo hivyo kutakuwa na kiungo cha ajabu cha uzima na ushirika katikati ya Kristo na watakatifu wake. Ni nguvu kueleza namna gani Kristo ni **ndani** ya mwamini na mwamini ni **ndani** ya Kristo vilevile. Mfano mmoja ni chuma ndani ya moto. Chuma si ndani ya moto tu, lakini moto ni ndani ya chuma vilevile.[10] Lakini huu si mfano mzuri sana. Maana ya Kristo ndani ya mwamini ni ya kama uzima wake umepitishwa kwaye. Anakaa ndani ya mwamini kwa njia ya Roho Mtakatifu. Maana ya mwamini akiwa ndani ya Kristo ni ya kwamba anasimama mbele ya Mungu ndani ya ustahili wote wa Kristo na kazi yake.

**14:21** Tunahakikisha kwamba tunapenda Bwana Yesu kwelikweli kwa njia ya kutii **maagizo** yake. Ni bure kusema tunampenda kama tusipotaka kumtii. Ndiyo, Baba anapenda watu wote wa dunia, lakini ana mapendo bora zaidi kwa wale wanaopenda Mwana wake. Kristo anawapenda vilevile na anajifunua kwao kwa njia bora zaidi. Kwa kipimo tunachopenda Mwokozi wetu tutajuana naye vizuri kupita.

**14:22 Yuda** huyu si Yuda **Iskariota** aliyetoa Bwana kwa adui zao. Ilishinda Yuda huyu kufahamu namna gani Bwana ataonekana kwa wanafunzi bila kuonekana kwa **dunia** vilevile. Bila shaka alifikiri juu ya Mwokozi akikuja kama mfalme mshindaji. Hakufahamu kwamba Bwana **atajionyesha** kwa watu kwa njia ya roho. Watamwona kwa imani kwa njia ya Neno la Mungu.

Tukiwa na Roho ya Mungu tunaweza kujua Kristo vizuri kupita wanafunzi wakati alipokuwa duniani. Wakati alipokuwa hapa, wale waliosimama mbele ndani ya makutano walikuwa karibu naye kupita wale waliosimama kwa upande wa nyuma. Lakini sasa, kwa imani, sisi sote tunaweza kuwa na ushirika na upatano karibu zaidi naye. Jibu la Kristo kwa Yuda linaonyesha kwamba atajionyesha kwetu kwa kipimo tunachotii Neno la Mungu. Tukitii Neno la Mungu, Baba na Mwana watakuja na kukaa kwetu.

**14:23** Mtu **akipenda** Bwana na mapendo ya kweli, **atataka kutii** maagizo yake yote, si nusu yao tu. **Baba** anapenda wale wanaotii Mwana wake bila mashaka na kusita. Baba na Mwana ni karibu zaidi na wenye roho ya mapendo na kutii.

**14:24** Lakini wale ambao **hawampendi hawatii** masemo yake. Nao hawakataa masemo ya Kristo tu lakini yale ya Baba vilevile.

**14:25** Wakati Bwana alipokuwa **pamoja** na wanafunzi, aliwafundisha kwa kipimo fulani. Hakuweza kuwafunulia kweli nyingine kwa sababu wasingaliweza kuzifahamu.

**14:26** Lakini **Roho Mtakatifu** atawafunua maneno mengine. Alitumwa na **Baba** kwa **jina** la Kristo siku ya Pentekote. Roho alikuja kwa **jina** la Kristo, maana yake alikuja kusimamisha maneno ya Kristo duniani. Hakufika kujitukuza mwenyewe, lakini kukokota watu karibu na Mwokozi. Bwana alisema juu yake, **"Atawafundisha ninyi yote."** Alifanya hivi kwanza kwa njia ya mafundisho ya mitume; nyuma yake kwa njia ya maandiko ya Neno la Mungu tuliyo nayo sasa. Roho Mtakatifu **anatukumbusha** maneno **yote** ambayo Mwokozi alifundisha mbele. Ni kama mafundisho ya Bwana Yesu yalikuwa kama mbegu yaliyoelezwa kupita na Roho Mtakatifu ndani ya baki la Agano Jipya.

### O. Yesu anaachia wanafunzi wake salama yake (14:27-31)

**14:27** Ni desturi ya watu walio karibu na mauti kuandika hati ya kuriti,

ndani yake wanaachia wapenzi wao vitu vyao. Bwana Yesu alifanya vivyo hivyo hapa. Lakini hakuwaachia vitu vya dunia, lakini kitu kimoja wasichoweza kununua na mali – ndiyo **salama**, **salama** rohoni ya zamiri, kwa sababu zambi zao zimesamehewa nao walipatanishwa na Mungu. Kristo anaweza kuileta kwa sababu aliinunua na damu yake mwenyewe kwa Kalvari. Haitoi namna **dunia inavyotoa** – nusu nusu, na choyo, na kwa saa ndogo. Zawadi yake ya **salama** ni kwa milele. Basi kwa nini Mkriso **atafazaika** moyoni na **kuwa na woga**?

**14:28** Yesu alikuwa amewaambia mbele namna atakavyowaondokea, na namna atakavyorudi tena kuwapeleka mbinguni pamoja naye. **Kama wangalimpenda wangalifurahi** juu ya habari hizi. Ndiyo, walimpenda, lakini hawakufahamu kabisa kabisa kama alikuwa nani, na kwa sababu hii kipimo cha mapendo yao hakikuwa kikubwa kama ilivyofaa.

**"Mungalifurahi kwa sababu ninakwenda kwa Baba; kwa maana Baba yangu ni mkubwa kuliko mimi."** Tungeweza kufikiri kwanza kwamba maneno haya yanabisha maneno Bwana aliyosema mbele kidogo ya kuwa yeye ni sawasawa na Mungu Baba. Sivyo; kama mashairi haya yanavyoeleza. Wakati Yesu alipokuwa hapa duniani, watu walimchukia na kumwinda na kumtesa na kumfukuza. Watu walimtukana, walimzarau na kumtemea mate usoni. Alivumilia jeuri hii yote toka viumbe vyake.

Mungu Baba hakutendewa mabaya namna hii toka watu. Alikaa mbinguni, mbali na uovu wa wenye zambi. Wakati Bwana Yesu atakaporudi mbinguni, atakuwa pahali matendo ya jeuri namna hii yasipokuwa tena kamwe. Hivi ingalipasa wanafunzi kufurahi wakati aliposema **atakwenda kwa Baba**, kwani *kwa njia hii* **Baba** alikuwa kweli **mkubwa kupit**a yeye. Baba hakuwa mkubwa kupita *kama Mungu*, lakini mkubwa kupita kwa sababu hakufikia kamwe dunia hii mbovu kama mtu na kuteswa na kutendewa jeuri. Kwa tabia na sifa ya uungu, Mwana na Baba ni sawasawa. Lakini wakati tunapokumbuka nafasi ya chini na unyenyekevu wa Yesu kama Mtu hapa duniani tunafahamu kwamba *kwa njia ile* Mungu **Baba** alikuwa mkubwa kupita yeye kwa *pahali* alipokaa lakini si kwa *nafsi* yake.

**14:29** Akifahamu woga wa wanafunzi wake, Bwana aliwafunua maneno haya kusudi wasitiwe uchungu, na kulegea rohoni, na kuogopa, lakini waweze **kuamini.**

**14:30** Bwana Yesu alijua kwamba saa ilipokuwa ikikaribia wakati atakapotolewa kwa mikono ya adui na ya kwamba hatakuwa na saa nyingi tena **kusemezana** na watu wake. Hata kwa saa ile Shetani alikuwa akikaribia, lakini Mwokozi alijua kwamba adui huyu hatakuta neno kwake litakaloangushwa na majaribu ya Shetani. Yesu tu aliweza kusema kwamba Shetani **hakuweza kuta kitu** cho chote ndani yake.

**14:31** Tunaweza kufananua shairi hili hivi: "Saa ya kutolewa kwangu ni karibu. Ninakwendea msalaba bila kulazimishwa kwenda. Ni mapenzi ya Baba kwa mimi kufanya hivi. Tendo hili litajulisha dunia kwamba **ninapenda Baba** yangu sana. Kwa sababu hii ninakwenda hivi sasa bila ushindani." Nyuma ya kusema maneno haya Bwana alisema na wanafunzi wake **kusimama** na **kwenda** pamoja naye. Si wazi kama waliondokea chumba cha juu kwa saa ile. Labda alimaliza hotuba yake wakati walipotembea njiani.

### P. Yesu, mzabibu wa kweli (15:1-11)

**15:1** Katika Agano la Kale tunasoma juu ya taifa la Israeli kama mzabibu

uliopandwa na Bwana. Lakini taifa la Israeli hawakuwa waaminifu na hawakuzaa matunda, hivi Bwana Yesu alisema *juu yake mwenyewe* kwamba yeye ni **mzabibu wa kweli,** ndiye mwenye kutimiza mifano yote mengine. Mungu **Baba ni mlimaji.**

**15:2** Walimu wa Neno la Mungu wanaeleza maana ya **tawi lisilozaa matunda** kwa njia mbalimbali. Wengine wanasema ni mtu anayekiri kuwa Mkristo lakini anakosa imani ya kweli. Hakuzaliwa tena na hakufungwa pamoja na Bwana Yesu kwa njia ya imani. Wengine wanasema ni Mkristo wa kweli anayepoteza wokovu wake kwa sababu ya kukosa kuzaa matunda. Neno hili haliwezekani hata kidogo kwa sababu kuna mashairi mengine mengi yanayofundisha ya kwamba wokovu wa mwamini ni wa milele. Wengine wanafikiri ni mwamini anayerudi nyuma. Anakwenda mbali na Bwana na anaingia tena ndani ya maneno ya dunia. Tunda la Roho halionekani ndani ya maisha yake – mapendo, furaha, salama, uvumilivu, neema, wema, uaminifu, upole, ujizuiza (Gal. 5:22, 23).

Bwana anafanya nini kwa tawi lisilozaa matunda? Neno hili **"analiondoa"** (*airo* kwa Kiyunani) linaweza kutafsiriwa kwa njia mbalimbali. Kwa Yoane 1:29 maana yake ni kuondoa vilevile. Kwa 1 Kor. 11:30 maana yake ni azabu ya mauti ya mwili.

**Tawi linalozaa matunda** ni Mkristo anayekaa kupata nguvu na kugeuka kupita na kupita kufanana na Bwana Yesu. Hata matawi namna hii yanahitaji kusafishwa. Kama mzabibu unahitaji kusafishwa toka vidudu, kawa, na ukungu, vivyo hivyo Mkristo anahitaji kusafishwa toka vitu vya dunia ambavyo vinafungana naye.

**15:3** Wanafunzi walikuwa wamesafishwa na **neno la Bwana.** Walikuwa wamesafishwa na **neno** wakati walipookolewa. Wakati Mwokozi alipokuwa akisema nao, neno lake lilisaidia kusafisha maisha yao. Hivi ni kama shairi hili ni juu ya kuhesabiwa haki *na* kutakaswa.

**15:4** Maana ya **kukaa** ni kubaki pahali ulipo. Mkristo amewekwa ndani ya Kristo. Ndani ya mwendo wake inampasa kukaa na ushirika wa karibu na Bwana. **Tawi** linabaki ndani ya mzabibu kwa njia ya kupata uzima na chakula toka mzabibu. Hivi sisi tunakaa ndani ya Kristo kwa njia ya kushinda na maombi, kusoma na kutii Neno lake, kushiriki na watu wake, na kukumbuka saa zote kwamba tumeungwa naye. Wakati tunapokumbuka neno hili siku zote, tunafahamu kwamba anakaa ndani yetu na kutupatisha nguvu rohoni. **Tawi linaweza kuzaa matunda wakati linapokaa ndani ya mzabibu tu**. Kuna njia moja tu kwa waamini kuzaa tunda la tabia inayofanana na ile ya Kristo. Ni kukaa karibu na Bwana saa zote.

**15:5** Kristo mwenyewe ni **mzabibu,** na waamini ni **matawi** ya mzabibu. Tawi linaacha uzima wa mzabibu kupita ndani yake kama maji. Mara nyingine tunaomba, "Bwana, unisaidie kuishi kwa wewe." Ni vizuri kupita kuomba, "Bwana Yesu, ishi maisha yako kwa njia yangu." **Hatuwezi kufanya neno pasipo yeye**. Kazi ya tawi la mzabibu ni moja tu, ndiyo kuzaa matunda. Halina faida kwa kujenga nyumba au kufanya vitu vya nyumba. Halina faida hata kwa kuwasha moto. Lakini lina faida kwa kuzaa matunda – kama likikaa ndani ya mzabibu.

**15:6** Watu wameeleza shairi hili kwa njia mbalimbali. Wengine wanafikiri linasema juu ya mwamini anayeanguka na kufanya zambi na anapotea kwa milele. Elezo hili halipatani hata kidogo na mashairi mengi ndani ya Biblia yanayofundisha kwamba mtoto wa kweli wa Mungu hatapotea kamwe. Watu we-

ngine wanafikiri mtu huyu anatenda kama Mkristo lakini hakuzaliwa tena. Wanataja Yuda kama mfano wa mtu wa namna hii.

Tunafikiri mtu huyu ni mwamini wa kweli, kwani mashairi haya yanafundisha juu ya waamini wa kweli. Ni juu ya kukaa ndani ya Kristo na *kuzaa matunda*, si juu ya wokovu. Lakini mwamini huyu haweki roho juu ya kukaa ndani ya Bwana na juu ya kushinda na maombi, na halafu anakaa mbali na Bwana. Kwa sababu ya maneno haya anaingia ndani ya zambi na kuharibu ushuhuda wake kwa Kristo. Kwa sababu hakai ndani ya Kristo **anatupwa inje kama tawi –** si na Kristo, lakini na watu. Matawi yanakusanywa na **kutupwa kwa moto na kuteketezwa.** Si Mungu anayefanya hivi, lakini watu. Maana yake nini? Watu wanazarau Mkristo namna hii aliyerudi nyuma. Wanatupa ushuhuda wake kama Mkristo ndani ya moto. Tunaona neno hili ndani ya maisha ya Daudi. Daudi alikuwa mwamini wa kweli, lakini aliacha kutembea karibu na Bwana, na alitenda uzini na uuaji. Alifanyiza adui za Mungu kutukana. Hata kwa wakati wa sasa watu wanazarau jina la Daudi (na la Mungu wa Daudi). Ni kama wanamtupa ndani ya moto.

**15:7** Kwa kuendelea ndani ya maisha ya maombi inatupasa kukaa ndani ya Bwana. Kwa kipimo tunachotembea karibu naye tutaanza kufikiri namna yeye anavyofikiri. Kwa kipimo tunachojuana naye kwa njia ya kusoma Neno lake, tutafahamu mapenzi yake. Kwa kipimo mapenzi yetu yanapatana na mapenzi yake tunaweza kujua kwamba tutapata majibu kwa maombi yetu.

**15:8** Kwa kipimo watoto wa Mungu wanachofanana na Kristo duniani, **Baba anatukuzwa**. Watu wanalazimishwa kukubali kwamba huyu ni Mungu mkubwa anayeweza kugeuza wenye zambi kuwa watu watakatifu namna hii. Ona ya kwamba ndani ya sura hii tunasoma kwanza juu ya matunda (sh.2), matunda zaidi (sh.2), na mwishoni juu ya **matunda mengi** (sh.8).

**“Na mutakuwa wanafunzi wangu.”** Ni kusema *tunahakikisha* kwamba tuko **wanafunzi** wake wakati tunapokaa ndani yake. Watu wengine wanaweza kuona kwamba tuko wanafunzi wa kweli, na tunafanana na Bwana wetu.

**15:9** Mapendo ya Mwokozi wetu kwa sisi ni sawasawa na **mapendo ya Baba** kwa Mwana wake. Kweli tunainama na kuabudu wakati tunaposoma maneno namna hii. Ni mapendo yaliyo sawasawa na mapendo ya Baba. Ni mapendo tusiyoweza kupima, na yaliyo makubwa kupita kujua na ufahamu wa mtu. Bwana anasema nasi, “**Mkae katika mapendo yangu,”** maana yake tukaa kufikiri na kufurahishwa nayo ndani ya maisha yetu.

**15:10** Mwanzo wa shairi hili unatuambia namna gani tunaweza kukaa katika mapendo yake; ni kwa njia ya kutii **maagizo** yake. Njia ya pekee kukaa na furaha ndani ya Yesu ni kuamini na kutii. Sehemu ya pili ya shairi hili inatuonyesha Mfano Mkamilifu. Bwana Yesu **alitii amri za Baba yake**. Alitii mapenzi ya Mungu ndani ya maneno yote aliyofanya. Alikaa na kufurahi ndani ya **mapendo** ya Baba yake. Hakuna neno lililoharibu utamu wa ushirika huu wa mapendo.

**15:11** Yesu **alifurahi** sana ndani ya ushirika wake na Mungu Baba yake. Alitaka wanafunzi wake kuwa na furaha iliyo tunda la kumtegemea yeye. Alitaka wawe na **furaha** *yake* wao wenyewe. Watu wanafikiri furaha ndiyo kuishi maisha yao bila Mungu kwa kila njia. Bwana alifundisha kwamba tunapata furaha ya kweli kwa njia ya kukumbuka na kuingiza Mungu katika maisha yetu kwa kila njia tunayoweza. “**Na furaha**

**yenu itimizwe.**" Furaha yao itatimia kwa njia ya kukaa ndani ya Kristo na kutii maagizo yake. Watu wengi wametaja mashairi ya Yoane 15 kuamsha shaka ndani ya roho za waamini juu ya wokovu ulio wao kwa milele, na kwamba wataweza kupotea tena. Wanataja mashairi mengine kuonyesha kwamba mwishoni inawezekana kwa kondoo ya Mungu kupotea. Lakini kusudi la Bwana si "na mashaka yenu yatimie" lakini **"furaha yenu itimizwe."**

**Q. Agizo la kupendana (15:12-17)**

**15:12** Bwana ataondokea wanafunzi wake nyuma kidogo, nao watabaki katika dunia ya uadui. Watakuwa katika hatari ya kushindana na kupigana. Hivi Bwana aliwaachia agizo hili, **"Mupendane, kama mimi nilivyowapenda ninyi."**

**15:13** Wawe na mapendo yaliyo tayari kufa kwa wenzao. Watu walio tayari kufa kwa wenzao hawatakaa na magomvi nao. Mfano mkubwa zaidi ya mapendo ni kwa mtu kutoa uzima wake **kwa sababu ya rafiki zake**. Inapasa wanafunzi wa Kristo kuwa na roho namna hii. Wengine wanatoa uzima wao wa mwili kwa wengine; na wengine wanashinda maisha yao mazima wakitumikia watu wa Mungu bila kuchoka. Bwana Yesu ndiye mfano wetu. Alitoa uzima wake kwa ajili ya rafiki zake. Ndiyo, walikuwa adui zake saa alipowakufia, lakini wakati wanapookolewa, wanageuka rafiki zake. Hivi tunaweza kusema alikufia rafiki zake na adui zake.

**15:14** Tunaonyesha kwamba sisi ni **rafiki** zake kwa njia ya kufanya **maneno yo yote ambayo** anatuagiza. Hatugeuki rafiki zake kwa njia hii, lakini ni njia kwa sisi kuonyeshea watu wa dunia kwamba tuko rafiki zake.

**15:15** Bwana anaonyesha wazi tofauti katikati ya **watumishi** na **rafiki**. Inapasa **watumishi** kufanya tu kazi waliyoagizwa, lakini **rafiki** wanaambiwa maneno ya siri. Tunamwambia **rafiki** mashauri yetu kwa wakati wa kuja. Tunamwambia habari za ndani ndani. Ndiyo, wataendelea kuwa watumishi wa Bwana daima, lakini zaidi ya ile, watakuwa rafiki zake. Hata saa ile Bwana alikuwa akiwafunulia **maneno aliyosikia** kwa **Baba** yake. Alikuwa akiwaambia habari za kuondoka kwake mwenyewe, na za kuja kwa Roho Mtakatifu, ya kwamba yeye mwenyewe atakuja tena, na namna gani iliwapasa kumtumikia wakati asipokuwa pamoja nao.

Mtu mmoja alionyesha kwamba kama matawi *tunapokea* (sh.5); kama wanafunzi *tunafuata* (sh.8); na kama rafiki *tunashiriki* habari (sh.15).

**15:16** Kama labda watajaribiwa kulegea na kuacha kumfuata, Yesu aliwakumbusha kwamba alikuwa **Yeye** ambaye **aliwachagua**. Labda **aliwachagua** kuokolewa, kuwa wanafunzi wake, au kuzaa matunda. Aliwaweka kufanya kazi ambayo aliwapa. **Inatupasa kwenda na kuzaa matunda**. Labda matunda haya ni mapendo, furaha, salama, vivi hivi. Au labda ni watu ambao tunafikisha karibu na Bwana kupata wokovu. Namna hizi mbili zinalingana. Lazima tuonyeshe matunda namna ya kwanza mbele ya kuweza kuzaa matunda ya namna ya pili.

Masemo ya Bwana, **"matunda yenu yapate kukaa"** yanatufikirisha kwamba matunda hapa ni nafsi za watu wanaookolewa. Bwana Yesu alichagua wanafunzi kwenda kuzaa **matunda** *ya kukaa.* Hakuweka roho juu ya wale waliosema tu kwamba walimwamini, lakini wale waliookolewa kwelikweli. **"Kusudi neno gani mutakaloomba … "** Maombi ndiyo msingi wa utumishi unaozaa matunda. Wanafunzi walitumwa kwa kazi yao na ahadi ya kwamba **Baba** atawapa neno **lo lote** watakaloomba kwa **jina** la Kristo.

**15:17** Mbele ya kujulisha wanafunzi

kwamba watu wa dunia watawachukia aliwaagiza **kupendana**, na kufungana pamoja kushindana na adui zao.

**R. Yesu anatabiri kuchukia kwa dunia (15:18 – 16:4)**

**15:18, 19** Haikufaa wanafunzi kushituka au kulegea **kama dunia ikiwachukia.** (Maana ya *kama* hapa haiko ya kwamba labda neno hili halitatokea; litatokea kweli.) Dunia ilichukia Bwana, na itachukia watu wale ambao wanafanana naye.

Watu wa dunia wanapenda wale wanaoishi namna wao wanavyoishi – wenye kutukana na kuzini, au watajiri wasiofanya maneno namna hii lakini wanaoishi kwa faida yao wenyewe tu. Mwenendo mtakatifu wa Wakristo unawahukumu, na **kwa sababu hii dunia inawachukia.**

**15:20 Mtumwa** asifikiri watu wa dunia watamtendea vizuri kupita Bwana wake. Atateswa namna Kristo alivyoteswa. Watakataa masemo yake namna walivyokataa masemo ya Mwokozi.

**15:21** Atachukiwa na kuteswa **"kwa ajili ya jina langu."** Ni kwa sababu Mkristo amefungwa pamoja na Kristo; Kristo amemtenga na dunia; anaitwa na jina la Kristo na kufanana naye. Dunia haijui Mungu. **Hawajui** kwamba Baba **alituma** Bwana duniani kuwa Mwokozi. Lakini ujinga wao si uzuru.

**15:22** Bwana hafundishi hapa kwamba watu wasingalikuwa wenye zambi kama asingalikuja. Watu ni wenye zambi tangu wakati wa Adamu. Lakini zambi yao ilikuwa ndogo kupita zambi ya watu kwa wakati ule. Watu hawa waliona Mwana wa Mungu na kusikia masemo yake ya ajabu. Hawakuona kosa hata moja ndani yake. Lakini walimkataa hata hivi. Ni kwa sababu hii zambi yao ilikuwa kubwa zaidi. Tukisawanisha zambi hii ya kuogofya, ndiyo zambi ya kukataa Bwana wa utukufu, na zambi zao nyingine, zambi zile nyingine zilikuwa kama si kitu. Sasa **hawakuwa na uzuru kwa zambi zao**. Walikuwa wamekataa Nuru ya dunia!

**15:23** Wakichukia Kristo walichukia **Baba yake vilevile**. Wao ni moja. Hawakuweza kusema walipenda Mungu; kwani kama wangalipenda Mungu, wangalipenda yule ambaye Mungu alituma vilevile.

**15:24** Hawakusikia mafundisho ya Kristo tu lakini waliona maajabu yake vilevile. Neno hili liliongeza hukumu yao. **Waliona kazi alizofanya ambazo mtu ye yote hakufanya kamwe.** Wakiwa na ushahidi ule hawakuwa na uzuru kukataa Kristo. Bwana alisawanisha zambi zao zote na zambi hii moja, na kusema zile walizofanya mbele zilikuwa kama si kitu wakati zinaposawanishwa na zambi hii kubwa ya kumkataa. Kwa sababu **walichukia** Mwana, walichukia **Baba** yake, ndiyo hukumu yao ya kuogofya sana.

**15:25** Bwana Yesu alifahamu kwamba namna watu walivyomtendea ilitimiza unabii katika Agano la Kale. Kwa Zaburi 69:4 tunasoma kwamba Kristo **atachukiwa … bila sababu.** Neno hili **lilitokea kweli sasa**. Na Bwana alisema kwamba Agano la Kale ambalo waliheshimu sana *lilitabiri* kwamba watu watamchukia bila sababu. Lakini hata kama neno hili lilitabiriwa, si kusema kwamba ilikuwa *lazima* kwa watu wale kuchukia Kristo. *Wao wenyewe walichagua* kumchukia, lakini Mungu alijua mbele kwamba watafanya hivi, na aliongoza Daudi kuandika maneno haya ndani ya Zaburi 69.

**15:26** Lakini hata kama watu walikataa Kristo, **Msaidizi**, ndiye Roho Mtakatifu, atakaa kushuhudia Kristo. Tunasoma hapa kwamba Bwana alisema *yeye* **atatuma** Roho toka **Baba**. Katika Yoane 14:16 alikuwa *Baba* aliyetuma

Roho Mtakatifu. Hivi tunaona tena hapa kwamba Baba na Mwana ni sawasawa. Mungu tu aliweza kutuma mwingine aliye Mungu. **Roho ya kweli … anatoka kwa Baba**. Maana yake ni ya kwamba anatumwa saa zote toka Mungu, na kuja kwake siku ya Pentekote kulikuwa hivi. Roho anashuhudia Kristo. Hii ndiyo kazi yake kubwa. Hakokoti mafikiri ya watu juu yake mwenyewe, hata kama yeye ni mmoja na Mungu Baba na Mungu Mwana. Anakaa kuongoza watu, wenye zambi na waamini, kufikiri juu ya Bwana wa utukufu.

**15:27** Roho atashuhudia Kristo kwa njia ya wanafunzi. Wao **walikuwa pamoja** na Bwana **tangu mwanzo** wa kazi yake katikati ya watu, na waliweza kupasha habari zake vizuri zaidi. Kama angalikuwa na kosa na upungufu, wao wangaliweza kuliona kupita watu wengine. Lakini hawakumwona akifanya zambi namna yo yote kamwe. Waliweza kutoa ushuhuda kwamba yeye ni Mwana wa Mungu asiye na zambi, na Mwokozi wa dunia.

**16:1** Tunafikiri wanafunzi, kama Wayuda wengine – walitumaini kwamba Masiya atasimamisha ufalme wake na kuharibu utawala wa Roma. Lakini Bwana aliwaambia kwamba atakufa, atafufuka, na kurudia mbingu. Roho Mtakatifu atakuja na wanafunzi watakuwa washuhuda wa Kristo. Watu watawachukia na kuwatesa. Bwana aliwaambia maneno haya mbele ili **wasiangushwe** au kuogopeshwa.

**16:2,3** Wayuda walifikiri **kuondoshwa katika sunagogi** ndilo moja la maneno mabaya zaidi lililoweza kuwapata. Litapata Wayuda hawa waliokuwa wanafunzi wa Yesu. Dini ya Ukristo itachukiwa sana sana hata wale waliojaribu kuiondosha duniani **watafikiri** wanapendeza **Mungu.** Neno hili linaonyesha kwamba inawezekana kwa mtu kufanya na bidii sana neno analofikiri ni njema, lakini lililo *baya* sana.

Wayuda hawakutambua kwamba Kristo ni Mungu, na kwa sababu hii walikataa kumpokea, na kwa sababu walimkataa yeye walikataa kupokea **Baba**.

**16:4** Bwana alijulisha wanafunzi maneno haya tena mbele ya kutokea kwao kusudi wasitikiswe na mateso haya saa yatakayotokea. **Watakumbuka** kwamba Bwana alitabiri mbele kwamba watateswa. Bwana hakuwaambia maneno mengi mbele juu ya mambo haya kwa sababu alikuwa kwanza pamoja nao na alitaka wasikie vizuri maneno mengine aliyohitaji kuwafundisha. Lakini sasa alikuwa karibu na kuwaondokea, hivi ilikuwa lazima awajulishe maneno ambayo yatawapata.

### S. Kuja kwa Roho ya Kweli (16:5-15)

**16:5** Ni kama Bwana alihuzunishwa kidogo kwa sababu wanafunzi hawakuweka roho juu ya maneno ambayo yatampata. Ndiyo, walikuwa wameuliza kama **alikwenda wapi,** lakini hawakufikiri juu yake zaidi.

**16:6** Walifikiri juu ya maneno wao wenyewe watakayopata, kupita juu ya maneno yaliyokuwa mbele yake, ndio msalaba na kaburi. Watapata mateso ndani ya utumishi wao kwa Kristo. **Walihuzunishwa** juu ya taabu wao watakayopata kupita juu ya taabu ya Bwana.

**16:7** **Lakini** hawataachwa bila mwenye kuwasaidia na kuwafariji. Kristo atatuma Roho Mtakatifu kuwa **Msaidizi** wao. Kuja kwa **Msaidizi** huyu kutakuwa **faida** kwa wanafunzi. Atawapa uwezo na uhodari, atawafundisha na kuwasaidia kujuana na Kristo karibu zaidi. **Msaidizi** hatakuja mbele ya wakati Kristo atakapokwisha kurudi mbinguni na kutukuzwa. Roho Mtakatifu alikuwa duniani mbele ya saa ile, lakini sasa

alikuja kuhakikisha dunia maneno ya zambi na kusaidia wakombolewa.

**16:8** Roho Mtakatifu atakuja **kuhakikisha dunia maneno ya zambi, na maneno ya haki, na maneno ya hukumu**. Watu wanafikiri maana ya maneno haya ni ya kwamba atafahamisha wenye zambi juu ya maneno haya ndani ya maisha yao. Neno hili ni kweli, lakini si mafundisho ya shairi hili. Roho Mtakatifu akiwa **duniani** anaihukumu. Asingalipasa kuwa hapa kwa sababu ingalipasa Bwana Yesu kuwa hapa na kutawala dunia. Lakini dunia ilimkataa, naye alirudi mbinguni. Roho Mtakatifu ni hapa kwa pahali pa Kristo aliyekataliwa, na neno hili linaonyesha hatia kubwa ya dunia.

**16:9** Roho Mtakatifu anathibitisha dunia hatia ya kosa kwa maneno ya **zambi ya kutokuamini Kristo.** Kristo anastahili kuaminiwa. Hakuna neno lililoweza kuzuiza watu wasimwamini. Lakini walikataa. Na kuwa duniani kwa Roho Mtakatifu ni ushuhuda wa zambi yao kubwa.

**16:10** Mwokozi alisema yeye ni mwenye haki, lakini watu walisema alikuwa na pepo mchafu. Mungu alikata neno hili kwa njia ya kusema maneno kama haya: "Mwana wangu ni mwenye haki, na nitahakikisha neno hili kwa njia ya kumfufua toka wafu na kumpeleka mbinguni tena." Roho Mtakatifu anashuhudu kwamba Kristo ni mwenye haki na dunia inaanguka.

**16:11** Roho Mtakatifu akiwa hapa anahukumu dunia juu ya **hukumu** kwa wakati wa kuja. Akiwa hapa inaonyesha kwamba Shetani anakwisha kuhukumiwa kwa msalaba, na wote wanaokataa Mwokozi watashiriki ndani ya hukumu yake ya kuogofya kwa wakati wa kuja.

**16:12** Bwana alikuwa na **maneno mengi mengine** kuwaambia wanafunzi, lakini hawakuweza kuyafahamu. Tunaona hapa kwamba watu hawawezi kufahamu mafundisho ya ndani ndani mara moja. Aliwafundisha mambo rahisi kwanza, "amri juu ya amri, mstari juu ya mstari."

**16:13** **Roho ya kweli** ataendelea na kazi Bwana aliyoanza. **Atawaongoza katika kweli yote.** Ni kama mitume walipewa **kweli yote** wakati walipokuwa hai. Halafu waliandika kweli hizi, na tuna maandiko yao ndani ya Agano Jipya wakati wa sasa. Agano Jipya, pamoja na Agano la Kale ni maandiko ya ufunuo mzima wa Mungu kwa watu. Lakini Roho anaongoza watu wa Mungu katika yote yaliyo kweli kwa eoni zote. Anafanya hivi kwa njia ya Maandiko. **Atasema maneno yale** tu anayoongozwa kusema na Baba na Mwana. Na **"atawatangazia habari za maneno yatakayokuja."** Tunasoma habari hizi ndani ya Agano Jipya, zaidi katika kitabu cha Ufunuo pahali maneno ya kuja yanapofunuliwa.

**16:14** Kazi yake kubwa zaidi itakuwa **kutukuza** Kristo. Kwa njia hii tunaweza kujaribu mafundisho na mahubiri yote. Kama yakitukuza Mwokozi, yanatoka kwa Roho Mtakatifu. **"Atatwaa katika yaliyo yangu"** ni kusema Roho atapokea kweli kubwa juu ya Kristo. Ni kweli hizi anazofunulia waamini.

**16:15** **Yote yaliyo ya Baba,** tabia yake kamilifu, ni ya Mwana vilevile. Kristo alisema juu ya maneno haya ndani ya shairi 14. Roho alifunulia mitume kazi na utumishi na neema na ukamilifu wote wa Bwana Yesu.

### T. Huzuni itageuzwa kuwa furaha (16:16-22)

**16:16** Haijulikani kama Bwana alisema juu ya muda wa urefu gani ndani ya shairi 16. Labda alisema kwamba hatakuwa pamoja nao kwa siku tatu, na halafu ataonekana tena kwao nyuma ya ufufuko wake. Labda maana yake ni

kwamba atarudia Baba yake mbinguni, na halafu nyuma ya **wakati kidogo** (muda wa sasa) atarudi kwao tena (Kuja kwake mara ya pili). Au labda maana yake ni kwamba **hawatamwona** na macho yao ya mwili, lakini nyuma ya kufika kwa Roho Mtakatifu siku ya Pentekote, watamwona kwa imani namna wasivyomwona mbele.

**16:17 Wanafunzi wake** walifazaika juu ya masemo yake. Ndani ya shairi 10 alikuwa amesema, "Ninakwenda kwa Baba yangu, na hamunioni tena." Halafu sasa alisema, **"Wakati kidogo, na hamunioni; na tena wakati kidogo, na mutaniona**." Masemo haya hayakupatana kwa mafikiri yao.

**16:18** Waliulizana kama maana ya **"wakati kidogo"** ni nini. Hata sasa tunafazaika juu yake. Hatujui kama ni siku tatu mbele ya kufufuliwa kwake, siku makumi ine kufika siku ya Pentekote, au miaka kupita 1900 mbele ya kuja kwake mara ya pili!

**16:19, 20** Bwana Yesu ni Mungu na maulizo yake yalionyesha kwamba alijua mawazo ya wanafunzi wake. Hakuwajibu waziwazi, lakini aliongeza habari nyingine juu ya "wakati kidogo." **Watu wa dunia watafurahi** kwa sababu waliweza kusulibisha Bwana Yesu, lakini wanafunzi **watalia na kuomboleza.** Lakini nyuma ya muda mfupi tu **huzuni** yao **itageuka kuwa furaha,** kama ilitokea kweli – kwanza kwa njia ya ufufuko wake, na nyuma wakati Roho Mtakatifu alipokuja. Mwishoni, kwa wanafunzi wote wa kila muda, huzuni itageuka furaha wakati Bwana atakapokuja tena.

**16:21** Mwanamke anapata maumivu makali wakati saa yake ya kuzaa mtoto inapokaribia, lakini ni mshangao kuona ya kwamba nyuma ya kuzaliwa kwa **mtoto** anasahau mbio **uchungu** aliopata. Itakuwa vivyo hivyo na wanafunzi. Wakati watakapoona Bwana tena watasahau mbio taabu waliyopata saa alipokuwa mbali nao.

**16:22** Sharti tuseme tena kwamba hatujui kama Bwana alisema juu ya saa gani wakati aliposema, **"nitawaona ninyi tena."** Alisema hivi juu ya ufufuko wake, au juu ya kutuma Roho Mtakatifu siku ya Pentekote, au wakati atakapokuja mara ya pili? Hata kama ni saa gani, tunda lake ni **furaha** isiyoweza kuondoshwa kwao.

### U. Maombi kwa Baba kwa jina la Yesu (16:23-28)

**16:23** Kufika wakati ule, wanafunzi walikwenda karibu na Bwana Yesu na maulizo yao na maneno yote waliyotaka. Lakini **siku ile** (muda ambao utaanza wakati Roho Mtakatifu atakaposhuka siku ya Pentekote) hatakuwa pamoja nao tena katika mwili, hivi hawatamfikia tena na maulizo yao. Hivi hawatakuwa na mwingine ambaye wataweza kwendea? Sivyo. **Siku ile wataweza kuomba Baba**. Atawapa maneno wanayoomba kwa ajili ya Yesu. Atatupa sisi maneno tunayoomba, si kwa sababu sisi tunastahili, lakini kwa sababu Bwana Yesu anastahili.

**16:24** Mbele ya wakati ule, wanafunzi hawakuomba kamwe kwa Mungu Baba kwa **jina** la Bwana. Sasa Bwana alisema nao **kuomba. Furaha yao itatimizwa** wakati watakapopata jibu kwa maombi yao.

**16:25** Maana ya mengi ya mafundisho ya Bwana hayakuonekana wazi kila mara. Alisema kwa njia ya **mifano**. Hata ndani ya sura hii maana yake si wazi kabisa mara nyingine. Wakati wa kuja kwa Roho Mtakatifu, **mafundisho juu ya Baba** yaligeuka wazi kupita. Ndani ya vitabu vya Matendo na Barua kweli haikufunuliwa kwa njia ya mifano tena, lakini na masemo waziwazi.

**16:26 "Siku ile"** inasema tena juu ya muda wa Roho Mtakatifu, ndio muda

wa sasa. Tunabarikiwa sasa kwa sababu tunaweza kuomba Baba kwa **jina** la Bwana Yesu. **"Sisemi nanyi ya kwamba nitawaombea kwa Baba,"** maana yake Bwana hatahitaji kusukuma Baba kujibu maombi yetu. Lakini hata hivi inatupasa kukumbuka kwamba Bwana Yesu ni Mpatanishi katikati ya Mungu na watu, na anaombea watu wake mbele ya kiti cha kifalme cha Mungu.

**16:27** **Baba** alipenda wanafunzi kwa sababu walikuwa wamepokea Kristo na **walimpenda na kuamini** kwamba yeye ni Mungu. Kwa sababu hii Bwana hakuhitaji kusihi Baba kwa ajili yao. Wakati Roho Mtakatifu atakapokuja watafurahi ndani ya ukaribu wa kupita na Baba. Wataweza kumkaribia bila woga, kwa sababu **walipenda** Mwana wake.

**16:28** Hapa Bwana alionyesha tena kwamba yeye ni sawasawa na Mungu Baba. Hakusema "Nilitoka kwa *Mungu*" kama nabii tu aliyetumwa na Mungu lakini **"Nilitoka kwa Baba."** Ni kusema kwamba yeye ni Mwana wa milele wa Baba ya milele, sawa na Mungu Baba. Alikuja **katika dunia** kama mmoja aliyeishi pahali pengine mbele ya kufika hapa. Wakati alipopanda, aliondokea dunia na **alirudia Baba.**

**V. Mateso na salama (16:29-33)**

**16:29,30** **Wanafunzi wake** walifikiri ya kwamba sasa, mara ya kwanza, waliweza kumfahamu. **Walisema** sasa hakusema mfano tena.

Walifikiri kwamba sasa **walimtambua** mara ya kwanza. Sasa **waliamini kabisa** kwamba alijua maneno yote na ya kwamba **alitoka kwa** *Mungu*. Lakini Bwana alikuwa amesema kwamba alitoka kwa *Baba*. Walifahamu maana ya neno hili? Walifahamu kwamba Yesu alikuwa mmoja na Mungu Baba na Roho?

**16:31** Ulizo la **Yesu** linaonyesha kwamba alifikiri imani yao haijatimia kwanza. Alijua walimpenda na kumwamini, lakini walijua kabisa kwamba alikuwa Mungu katika mwili? (1 Tim. 3:16)

**16:32** Nyuma kidogo atafungwa, kuhukumiwa, na kusulibishwa. Wanafunzi wake wote watamwacha na kukimbia kwa nyumba zao. Lakini Bwana hakuwa pekee kwa sababu **Baba** atakuwa **pamoja** naye. Lakini hawajafahamu bado umoja wake na Mungu Baba. Ni neno hili ambalo litamtegemeza wakati wao wote watakapokwisha kukimbia kujiponyesha wenyewe.

**16:33** Bwana aliwaambia maneno haya yote kusudi **wapate kuwa na salama**. Wakati watakapochukiwa, kufukuzwa, kuteswa, kuhukumiwa bila haki, na kuumizwa sana, waliweza kuwa na **salama** *ndani yake*. Yeye alishinda **dunia** kwa msalaba wa Kalvari. Hata kwa wakati wa mateso waliweza kujua kabisa kwamba walikuwa pamoja na Mshindaji.

Na wakati Roho Mtakatifu atakapokuja, watapewa uwezo mpya wa kustahimili, na uhodari mpya kushindana na adui.

**W. Yesu anaomba kwa utumishi wake (17:1-5)**

Sasa tunafikia sehemu ya Maandiko inayoitwa ombi la kuhani mkubwa, ndiye Bwana Yesu. Ndani ya ombi hili aliombea watu wake. Ni mfano wa utumishi wake kwa wakati wa sasa mbinguni pahali anapoombea watu wake. Marcus Rainsford aliandika:

> Ombi hili zima ni mfano mzuri wa maombi ya Bwana wetu mbarikiwa kwa mkono wa kuume wa Mungu. Hakuna neno la kushitaki watu wake; hakuna neno juu ya kuanguka kwao, au upungufu kwao ... Sivyo. Alisema juu yao namna walivyokuwa ndani ya kusudi la Baba, kama wenye kushiriki naye mwenyewe,

> na kama wenye kupokea kujazwa ambako alishuka toka mbingu kuwapatia. ... Maombi yake yote kwa watu wake yalikuwa kwa mahitaji ya roho zao, na baraka za mbinguni. Bwana haombi wapewe utajiri au heshima, au pahali pa kujulikana duniani, au kuzidishwa cheo, lakini aliomba sana walindwe toka uovu, wenye kutengwa na dunia. Kusitawi rohoni ni usitawi mzuri zaidi, usitawi wa kweli.

**17:1 Saa ilikuwa imefika.** Adui zake walikuwa wameshindwa mara nyingi wakati walipojaribu kumkamata, kwa sababu saa yake ilikuwa *haijafika bado*. Lakini sasa wakati ulifika kwa Bwana kuuawa. Aliomba, **"Tukuza Mwana wako."** Alitazamia kufa kwake msalabani. Kama angalibaki kaburini, watu wa dunia watajua alikuwa mtu tu. Lakini kama Mungu akimtukuza kwa njia ya kumfufua toka wafu, neno hili litahakikisha kwamba alikuwa Mwana wa Mungu na Mwokozi wa dunia. Mungu alijibu ombi hili kwa njia ya kufufua Bwana Yesu siku ya tatu, na nyuma ya wakati kumrudisha mbinguni na kumtia taji ya utukufu na heshima.

Bwana aliendelea kuomba, **"Kusudi Mwana wako akutukuze wewe."** Maana ya ombi hili inaelezwa ndani ya mash. 2-3. Yesu anatukuza Baba kwa njia ya kuwapa wenye kumwamini uzima wa milele. Mungu anatukuzwa sana wakati wanaume na wanawake wazalimu wanapookolewa na kuonyesha uzima wa Bwana Yesu ndani ya maisha yao hapa duniani.

**17:2** Kwa sababu ya kazi yake ya ukombozi msalabani, Mungu alimpa Mwana wake **amri juu ya wote** wenye mwili. **Amri** hii ilimwezesha kuwapa wote ambao Baba alimpa **uzima wa milele.** Hapa tunakumbushwa tena kwamba mbele ya kuumbwa kwa ulimwengu, Mungu alichagua watu wengine kuwa mali ya Kristo. Lakini kumbuka ya kuwa Mungu ni tayari kumpa wokovu mtu ye yote anayepokea Yesu Kristo. **Kila** mtu anayeamini Mwokozi anaweza kupokea uzima wa milele.

**17:3** Hapa tunaona namna gani watu wanapokea **uzima wa milele**. Ni kwa njia ya kujua **Mungu na Yesu Kristo.** Maneno haya **"Mungu pekee wa kweli"** yanaonyesha kwamba yeye ni namna nyingine kabisa na sanamu, zisizo miungu. Shairi hili halionyeshi kwamba Yesu Kristo si Mungu wa kweli. Jina lake linatajwa pamoja na jina la Mungu Baba kuwa moja naye ndani ya kuleta uzima wa milele. Neno hili linaonyesha kwamba wao ni sawasawa. Hapa Bwana alijiita mwenyewe **Yesu Kristo.** Maana ya **Kristo** ndiyo Masiya. Watu wengine wanasema Yesu hakujitaja kamwe kuwa Masiya, lakini shairi hili linaonyesha kwamba mawazo haya si kweli.

**17:4** Bwana Yesu alisema maneno haya sawasawa alikwisha kufa, kuzikwa na kufufuliwa tena. Alikuwa **ametukuza** Baba na maisha yake bila zambi, maajabu yake, mateso yake na kufa kwake, na ufufuko wake. Alikuwa **amemaliza kazi** ya wokovu **ambayo Baba alimpa kufanya**. Ryle alisema,

> Kusulibiwa kwa Mwokozi kulileta utukufu kwa Baba. Kulitukuza hekima, uaminifu, utakatifu na mapendo yake. Kulionyesha hekima yake kutayarisha njia aweze kukaa mwenye haki yeye mwenyewe pamoja na kuhakikisha wasiogopa Mungu. – Kulionyesha uaminifu wake wakati alipotimiza ahadi yake kwamba uzao wa mwanamke utaponda kichwa cha nyoka. – Kulionyesha utakatifu wa Mungu uliolazimisha maagizo ya sheria yake kutimizwa na Mkombozi wetu mkubwa. – Kulionyesha mapendo yake yaliyoletea wenye zambi Mpatanishi namna hii, Mkombozi na Rafiki, kama Mwana wake aliye tangu milele na hata milele, kama yeye mwenyewe.

> Kusulibiwa kwa Mwokozi kulileta utukufu kwa Mwana. Kulitukuza huruma yake, saburi yake, na uwezo wake. Kulimwonyesha kuwa mwenye huruma zaidi wakati alipotukufia, akiteswa kwa pahali petu, akikubali kuhesabiwa zambi na laana kwa ajili yetu, na akinunua ukombozi wetu na damu yake mwenyewe. – Kulimwonyesha kuwa mwenye saburi zaidi, kwa njia ya kutokufa namna zaidi ya watu wanavyokufa, lakini kuwa tayari kuvumilia uchungu na maumivu makubwa yanayopita sisi watu kufahamu, wakati angalipoweza kusema neno tu kuita malaika za Baba yake, na kufunguliwa. – Kulimwonyesha kuwa mwenye uwezo mkubwa zaidi, kwa njia ya kubeba mzigo wa makosa yote ya dunia, na kushinda Shetani na kunyanganya nyara yake.

**17:5** Mbele ya kufika duniani Kristo alikaa mbinguni pamoja na Baba. Wakati malaika walipoangalia Bwana, waliona utukufu wa Uungu wake. Walifahamu yeye ni Mungu. Lakini wakati alipofika kukaa katikati ya watu, utukufu wa Uungu wake ulifichwa. Hata akiwa Mungu, zaidi ya watu ambao walimwangalia hawakuona utukufu ule. Walimwona kama Mwana wa mseremala tu. Hapa ndani ya shairi 5 Mwokozi anaomba utukufu wake ufunuliwe tena. **"Unitukuze, Baba, pamoja nawe mwenyewe,"** maana yake "unitukuze tena mbele yako mbinguni na utukufu ambao nilikuwa nao pamoja nawe mbele ya kuja kwa dunia." Ombi hili linaonyesha wazi kwamba Kristo alikuwa mbele ya kufika duniani.

### X. Yesu anaombea wanafunzi wake (17:6-19)

**17:6** Yesu alikuwa amejulisha **jina la Baba** kwa wanafunzi. Ndani ya Maandiko maana ya "jina" ni mtu mwenyewe, namna yake, tabia yake. Kristo alikuwa ameonyesha tabia ya Baba wazi kabisa. Mwana **alipewa wanafunzi toka dunia.** Walitengwa na makutano makubwa ya wasioamini na kuletwa kwa Kristo. "Wali*chaguliwa* na Baba mbele ya kuumbwa kwa dunia, na kugeuka mali ya Kristo kama zawadi toka Baba, na kwa sababu walinunuliwa kwa damu." (J.G. Bellett)

Bwana alisema, **"Wameshika neno lako."** Hata kama walikuwa wenye kuanguka, alisema waliamini na kutii mafundisho yake. "Hakusema neno juu ya maneno waliyokwisha kufanya au waliyokuwa karibu kufanya – ndiyo kumwacha." (Rainsford)

**17:7, 8** Bwana alikuwa ameelezea wanafunzi wake kwamba hakusema wala kutenda kwa amri yake mwenyewe, lakini alisema maneno yale tu aliyoagizwa na Baba. Hivi **waliamini** kwamba Baba alikuwa **ametuma** Mwana.

Na vilevile si Kristo *aliyechagua* kuja duniani, lakini alikuja kwa sababu ya kutii mapenzi ya Baba. Alikuwa Mtumishi mkamilifu wa BWANA.

**17:9** Kama Kuhani Mkubwa aliombea wanafunzi; **hakuombea dunia.** Si kusema kwamba hakuomba kwa dunia kamwe. Wakati alipokuwa msalabani aliomba, "Baba, uwasamehe, kwa sababu hawajui neno wanalofanya."

Lakini hapa alikuwa akiomba kama mjumbe wa waamini mbele ya kiti cha ufalme cha Mungu. Pale aliweza kuomba kwa watu wake tu.

**17:10** Hapa tunaona tena mwungano mkamilifu wa Baba na Mwana. Hakuna mtu aliyeweza kusema maneno namna hii. Tungeweza kusema kwa Mungu, **"Wote walio wangu ni wako,"** lakini hatuwezi kusema, **"Walio wako ni wangu."** Mwana aliweza kusema hivi kwa sababu alikuwa sawasawa na Baba. Ndani ya mashairi haya (6-19) Yesu aliombea kundi lake masikini na kusema juu yao, **"Ninatukuzwa ndani yao."**

**17:11** Hapa tena Bwana Yesu ali-

omba sawasawa alikuwa amerudi mbinguni. Ona jina hili, **"Baba Mtakatifu."** Linaonyesha *ukubwa* wa Baba, na *ukaribu* wake kama **Baba** vilevile!

Ombi la Yesu, **"wawe mmoja"** ni juu ya umoja wa tabia ya roho wa Wakristo, kama Baba na Mwana walivyo moja kwa tabia ya roho, maana Wakristo wawe kama Bwana Yesu.

**17:12 Wakati alipokuwa pamoja na wanafunzi**, Mwokozi aliwalinda kwa **jina** la Baba, maana kwa uwezo na amri yake. Alisema **hapana mmoja wao aliyepotea, ila yule mwana wa upotevu**, ndiye Yuda. Lakini maneno haya hayaonyeshi ya kwamba Yuda alikuwa mmoja wa wale ambao Baba alimpa Mwana, au ya kwamba Yuda alikuwa mwamini wa kweli kwa wakati wo wote. Hii ndiyo maana ya masemo yake: "Nilichunga wale ambao ulinipa, wala hapana mmoja wao aliyepotea, lakini mwana wa upotevu alipotea, maandiko yatimizwe." Maana ya jina la **"mwana wa upotevu"** ni ya kama Yuda alihukumiwa kwa maangamizi au laana ya milele. Yuda hakulazimishwa kutoa Kristo kwa adui zake ili kutimiza unabii, lakini alichagua kufanya hivi, na kwa njia ya kufanya hivi **Maandiko yalitimizwa.**

**17:13** Bwana alieleza kwa sababu gani aliomba mbele ya wanafunzi wake. Ni kama alisema nao, "Sitaacha kamwe kuomba hivi mbinguni mbele ya Mungu, lakini sasa ninaomba hivi **duniani** kwa masikio yenu, ili muweze kufahamu vizuri kupita namna gani nitakaa kuwasaidia ninyi kule, kusudi muweze kushiriki katika **furaha yangu**."

**17:14** Bwana aliwapa wanafunzi **Neno** la Mungu, nao walilipokea. Kwa sababu hii watu wa **dunia waliwachukia**. Walifanana na Bwana Yesu, basi watu wa **dunia waliwazarau.**

**7:15** Bwana **hakuomba** Baba **apeleke** waamini mbinguni mara moja. Iliwapasa kubaki duniani kwanza kupata nguvu katika neema na kushuhudia Kristo. **Lakini** Kristo aliomba wachungwe **kwa yule mwovu.**

**17:16** Wakristo **si wa dunia,** kama Kristo **hakuwa wa dunia**. Inatupasa kukumbuka neno hili wakati tunapojaribiwa kushiriki ndani ya michezo ya dunia au kuingia ushirika na wale wasiotaka jina la Yesu.

**17:17** Maana ya **kutakasa** ni kuweka mbali. Neno la Mungu linatakasa waamini. Wakati wanapolisoma na kulitii **wanawekwa mbali** na dunia waweze kutumikia Bwana. Hili ndilo neno Bwana aliloomba hapa. Alitaka watu waliotengwa na dunia, na waliowekwa mbali kwa Mungu ili aweze kutumika nao kwa kazi yake. Yesu alisema, **"Neno lako ni kweli."** Hakusema, kama watu wengi wanavyofanya kwa wakati wa sasa, "Kuna kweli *ndani ya* neno lako," lakini **"Neno lako NI kweli."**

**17:18** Baba **alituma** Bwana Yesu **katika dunia** kufunulia watu tabia ya Mungu. Saa Bwana alipoomba alifahamu kwamba atarudia mbingu nyuma kidogo. Lakini lazima vizazi kwa wakati wa kuja vipewe ushuhuda kuwajulisha kama Mungu ni namna gani. Sharti kazi hii ifanywe na waamini, kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Wakristo hawataweza kamwe kuonyesha tabia ya Mungu vizuri kama Kristo alivyofanya, kwa sababu hawawezi kamwe kuwa sawasawa na Mungu. Lakini hata hivi waamini ni hapa duniani kuwa wajumbe wake. Ni kwa sababu hii Yesu **aliwatuma katika dunia.**

**17:19** Maana ya *kutakasa* si kila mara *kufanyiza* takatifu. Kristo *n*i takatifu kwa tabia yake. Maana ya masemo yake hapa ni ya kwamba *alijiweka mbali* kwa kazi ambayo Baba yake alimtuma kufanya – ndiyo kufa kama zabihu. Labda maana yake ni ya kwamba alijiweka mbali inje ya dunia na kuingia utukufu. Mwandishi mmoja, jina lake

Vine alisema, "Utakaso wake ni mfano wa, na uwezo kwa, utakaso wetu." Ingetupasa kujitenga na dunia na kupata mahitaji yetu yote kwake.

### Y. Yesu anaombea waamini wote (17:20-26)

**17:20** Lakini Kuhani Mkubwa hakuombea mitume tu, lakini aliendelea kuombea vilevile waamini wa vizazi vya kuja wasiozaliwa bado. Kila mwamini anayesoma shairi hili anaweza kusema, "Miaka zaidi ya 1900 imepita tangu Kristo aliniombea mimi."

**17:21** Aliomba waamini wawe na roho ya umoja, lakini mara hii maombi yake yalikuwa vilevile kwa wokovu wa wenye zambi. Ombi hili la Yesu halikuwa juu ya umoja wa kanisa, lakini juu ya umoja wa tabia takatifu. Aliomba waamini waweze kuwa **moja** wakionyesha tabia ya Mungu na ya Kristo. Neno hili **litaaminisha watu wa dunia** kwamba **alitumwa** na Mungu. Wakiona umoja huu, watu wa dunia watasema, "Ninaona Kristo ndani ya Wakristo hawa namna Baba alivyoonekana ndani ya Kristo."

**17:22** Ndani ya shairi 11 Bwana aliomba juu ya umoja katika ushirika. Ndani ya shairi 21 alisema juu ya umoja katika kutoa ushuhuda. Sasa alisema juu ya umoja katika **utukufu**. Alitazamia wakati watakatifu watakapopokea miili yao ya utukufu. **"Utukufu ambao ulinipa"** ndio utukufu wa ufufuko na kupanda kwake mbinguni.

Hatuna utukufu huu kwanza. Mungu amekusudi **kutuletea** utukufu huu, lakini hatutaupokea kufika wakati Mwokozi wetu atakaporudi kutupeleka mbinguni. Utaonekana wazi wakati Kristo atakaporudi kusimamisha ufalme wake duniani. Kwa wakati ule watu wa dunia watatambua umoja wa Baba na Mwana, na wa Mwana na watu wake, na wataamini kwamba Yesu ndiye aliyetumwa na Mungu (lakini saa kwa wasioamini kupata wokovu itakuwa imepita).

**17:23 Dunia** itatambua kwamba Yesu alikuwa Mungu Mwana, na itajua vilevile ya kwamba waamini walipendwa na Mungu kama Kristo vilevile alivyopendwa na Mungu. Habari hizi zinataka kushinda ufahamu wetu, lakini ni habari za kweli!

**17:24** Mwana anataka watu wake kuwa pamoja naye katika utukufu. Ni kama ombi hili linapata jibu kila mara mwamini anapokufa. Kutambua neno hili kunatufariji wakati wa kufa kwa wapenzi wetu. Kufa ni kwenda kufika karibu na Kristo na **kuona utukufu** wake. **Utukufu** huu si utukufu wa uungu wake tu ambao alikuwa nao pamoja na Mungu mbele ya kuumbwa kwa dunia. Ni utukufu wake vilevile aliopata kama Mwokozi na Mkombozi. **Utukufu** huu unahakikisha kwamba Mungu **alipenda** Kristo **mbele ya kuwekwa kwa misingi ya dunia.**

**17:25 Dunia** haikuona Mungu akifunuliwa ndani ya Yesu. Lakini wanafunzi wachache waliona, nao waliamini **kwamba** Mungu alikuwa **ametuma** Yesu. Mangaribi iliyotangulia kusulibishwa kwake, kulikuwa na wenye imani wachache tu katika dunia nzima – nao walikuwa karibu kumwacha!

**17:26** Bwana Yesu alikuwa **amejulisha jina** la Baba kwa wanafunzi wake wakati alipokuwa pamoja nao. Ni kusema aliwafunulia Baba. Masemo na matendo yake yalikuwa masemo na matendo ya Baba. Waliona ndani ya Kristo mfano mkamilifu wa Baba. Yesu anakaa **kujulisha** jina la Baba kwa njia ya utumishi wa Roho Mtakatifu. Tangu siku ya Pentekote Roho Mtakatifu anafundisha waamini juu ya Mungu Baba. Zaidi kwa njia ya Neno la Mungu tunaweza kujua kama Mungu ni namna gani. Wakati watu wanapopokea Baba namna anavyofunuliwa na Bwana Yesu, Baba **anawapenda** sana. Kwa sababu Bwana

Yesu anakaa ndani ya waamini wote, Baba anaweza kuwaona na kuwatendea namna anavyoona na kutendea Mwana wake wa pekee. Kwa sababu Bwana Yesu ni ndani ya mwamini, Mungu anaweza kumpenda namna anavyopenda Kristo. Hatuwezi kuwa karibu kupita naye. Ni ajabu kubwa!

## 8. MAUMIVU NA MAUTI YA MWANA WA MUNGU (Sura 18, 19)

### A. Yuda anatoa Bwana kwa adui (18:1-11)

**18:1** Bwana Yesu na wanafunzi wake walikuwa katika Yerusalema wakati alipotoa mafundisho katika sura 13–17. Sasa **Yesu** aliondokea mji, akakwenda kwa mashariki na kukaribia Mlima Mzeituni. Njiani alivuka **Mto Kiduroni**, akafikia shamba la Getesemane, kwa mtelemuko wa mangaribi wa Mlima Mzeituni.

**18:2, 3** **Yuda** alijua kwamba Bwana alishinda saa nyingi akiomba shambani. **Alijua** kwamba ataweza kukuta Bwana kwa pahali pa maombi.

Tunafikiri **kikosi cha askari** walikuwa askari Waroma, lakini **viongozi** vyao walikuwa Wayuda, wajumbe wa **wakubwa wa makuhani na Wafarisayo.** Walikuja na **taa, mienge, na silaha**. "Walikuja kutafuta NURU ya dunia na taa."

**18:4** Bwana **alikwenda** kukutana nao, bila kuwangojea kufika karibu naye. Neno hili linaonyesha ukubali wake kwenda msalabani. Askari wangaliweza kuacha silaha zao nyumbani mwao; Mwokozi hatashindana nao. Kwa njia ya kuwauliza, **"Munatafuta nani?"** alitaka waseme na midomo yao wenyewe kwa sababu gani walikuwa wamefika.

**18:5** Walitafuta **Yesu Mnazareti**, bila kufahamu hata kidogo kwamba alikuwa Mwumba wao na mwenye kuwategemeza – Rafiki yao mzuri zaidi. Yesu alijibu, **"Ni mimi."** Hakuwa Yesu wa Nazareti tu, lakini Yehova vilevile. Kama tulivyosema mbele, MIMI NIKO ni moja la majina ya Yehova katika Agano la Kale (Kut. 3:14). Labda **Yuda** alifazaika tena juu ya neno hili wakati **aliposimama pamoja na** watu wengine wa makutano pale?

**18:6** Kwa dakika fupi Bwana alijifunua kwa watu wale kuwa MIMI NIKO, Mungu Mwenyezi. Neno hili liliwashitusha kabisa hata **walirudi nyuma na kuanguka chini.**

**18:7** Bwana **aliwauliza tena** kama walitafuta **nani**, wakamjibu kama mbele – hata nyuma ya kusikia maneno mawili ambayo Yesu alisema nao sasa tu.

**18:8, 9** Yesu **aliwajibu tena** kwamba yeye ndiye, na ya kama yeye ni Yehova. **"Nimewaambia ninyi ya kwamba, NI MIMI."** Alisema nao vilevile, kama walimtafuta yeye, vizuri waache wanafunzi **kwenda zao**. Ni tamu sana kuona namna Bwana alivyofikiri wengine, hata wakati yeye mwenyewe alipokuwa katika hatari ya kufa. Hivi maneno ya Yoane 17:12 yalitimizwa.

**18:10** **Simoni Petro** alifikiri ilikuwa saa kupiga vita kujaribu kuponyesha Bwana wake toka makutano. Bila kuagizwa na Bwana wake, **alifuta upanga** wake na **kupiga mtumwa wa kuhani mkubwa.** Bila shaka alikusudi kumwua, lakini Mkono Usioonekana kwa watu uliruhusu upanga **kukata sikio lake la kuume tu.**

**18:11** **Yesu** alihamakia **Petro** kwa bidii yake isiyopatana na mapenzi ya Mungu. Baba yake alikuwa amempa **kikombe** cha mateso na mauti, naye alikusudi **kukikunywa.** Luka, mganga, aliandika kwamba Bwana aligusa na kuponyesha sikio la Malko (Lk. 22:51).

### B. Yesu alikamatwa na kufungwa (18:12-14)

**18:12, 13** Hii ni mara ya kwanza watu waovu waliyoweza kukamata **Yesu** na kufunga mikono yake.

**Ana** alikuwa kuhani mkubwa mbele. Haijulikani kwa sababu gani Yesu alipelekwa mbele yake **kwanza** na si mbele **ya Kayafa** aliyekuwa mkwe wake na **kuhani mkubwa** kwa wakati ule. Neno kubwa ndilo ya kwamba Yesu alihukumiwa kwanza mbele ya Wayuda kujaribu kuhakikisha kwamba alikuwa mwenye kukufuru na kufundisha maneno ya uwongo. Tungeweza kuita hukumu hii hukumu ya *dini*. Nyuma yake alipelekwa kuhukumiwa na serikali ya Waroma, na pale alijaribu kuhakikisha kwamba alikuwa adui ya Kaisari. Wayuda walitawaliwa na Waroma, hivi iliwapasa kunyenyekea Baraza ya hukumu ya Waroma. Kwa mfano, hawakuwa na ruhusa kuhukumu mtu kufa na kutimiza hukumu hii wao wenyewe. Ilikuwa lazima kwa Pilato kufanya hivi.

**18:14** Yoane alieleza kwamba kuhani mkubwa huyu ndiye **Kayafa** aliyetabiri kwamba **inafaa mtu mmoja afe kwa ajili ya** taifa (ona Yn 11:50). Alikuwa karibu na kushiriki ndani ya kutimiza unabii huu. James Stewart aliandika:

> Mtu huyu aliheshimiwa kuwa mlinzi wa hali ya roho ya taifa la Wayuda. Alichaguliwa kuwa mwenye kueleza sheria na kuwa mjumbe wa Mungu Mjuu sana. Alipewa mapendeleo matukufu kuingia mara moja kila mwaka katika pahali patakatifu sana hekaluni. Ni mtu huyu aliyehukumu Mwana wa Mungu. Ni mfano wa kuogopesha kabisa ya kuwa hata mtu akizungukwa sana na maneno ya dini, neno hili haliwezi kuongeza uzuri wa roho yake wala kumwokoa.[49]

### C. Petro anakana Bwana wake (18:15-18)

**18:15** Zaidi ya walimu wa Biblia wanafikiri **mwanafunzi mwingine** aliyetajwa hapa alikuwa Yoane, lakini ya kwamba hakutaja jina lake mwenyewe kwa sababu ya unyenyekevu, na kwa sababu ya tendo la haya la Petro. Hatujui kwa njia gani Yoane **alijulikana na kuhani mkubwa**, lakini kwa sababu ya neno hili alipata njia **kuingia kiwanja.**

**18:16, 17 Petro** hakuweza kuingia kufika wakati Yoane alipotoka na kusema na kijakazi aliyengoja mlango. Tukijua maneno yaliyotokea nyuma, tuna shaka kama tendo hili la Yoane lilisaidia Petro. Tuone vilevile ya kwamba mara ya kwanza Petro aliyokana Bwana haikuwa mbele ya askari mwenye uwezo, lakini mbele ya **kijakazi aliyengoja mlango**. Alikana kwamba alikuwa mwanafunzi wa Bwana.

**18:18** Petro alikaa katikati ya adui za Bwana wake na alijaribu kuficha kama alikuwa nani. Kama wanafunzi wengi wengine wa Bwana tangu wakati ule, **aliota moto** pamoja na watu wa dunia.

### D. Yesu mbele ya Kuhani Mkubwa (18:19-24)

**18:19** Si wazi kama **kuhani mkubwa** hapa ni Ana au Kayafa. Tunafikiri alikuwa Ana, na ya kwamba aliitwa kuhani mkubwa kwa adabu kwa sababu alikuwa kuhani mkubwa mbele. **Basi kuhani mkubwa akauliza Yesu juu ya wanafunzi wake na juu ya mafundisho yake.** Ni kama alifikiri maneno haya yaliweza kuwa hatari kwa sheria ya Musa na kwa serikali ya Waroma. Watu hawa hawakuwa na mashitaki juu ya Yesu, na walitafuta neno kumshitaki juu yake.

**18:20 Yesu alimjibu** kwamba alifanya kazi yake yote **waziwazi** mbele ya watu. Hakufanya neno kwa maficho. Alikuwa **amefundisha** mbele ya **Wayuda,** ndani ya **masunagogi na hekaluni.**

**18:21** Jibu lake lilifungua njia kwa Wayuda kuulizana na watu ambao walisikiliza mafundisho yake. Washuhuda waonyeshe kama alikuwa amesema maneno mabaya.

**18:22** Jibu la Yesu lilikasirisha Wayuda. Walikosa neno la kusema, hivi **mmoja wa watumishi alipiga Yesu kofi** kwa sababu ya **namna alivyojibu kuhani mkubwa.**

**18:23** Na upole na akili Mwokozi aliwaonyesha kwamba walitenda bila haki. Iliwashinda kumshitaki juu ya kusema mabaya; lakini walimpiga kwa sababu ya kusema kweli.

**18:24** Mashairi tuliyosoma sasa tu yalipasha habari za hukumu mbele ya Ana. Yoane hakuandika juu ya hukumu ya Yesu mbele ya Kayafa. Ilitokea katikati ya Yoane 18:24 na 28.

### E. Petro alikana Bwana mara ya pili na ya tatu (18:25-27)

**18:25** Sasa tunasoma juu ya **Petro** tena. Ilikuwa baridi kwa wakati wa asubui, naye **aliota moto**. Bila shaka mavazi yake na masemo yake yalionyesha kwamba alikuwa mvua samaki toka Galilaya. Mtu mwingine aliyesimama karibu naye alimwuliza kama alikuwa mwanafunzi wa Yesu. Lakini Petro **alikana** Bwana tena.

**18:26** Sasa alikuwa mtu **wa jamaa** ya Malko aliyesema na Petro. Alikuwa ameona Petro akikata sikio la ndugu yake. "**Sikukuona katika shamba pamoja** na Yesu?"

**18:27** **Petro alikana** Bwana mara ya tatu, na **mara moja** alisikia j**ogoo** akiwika. Alikumbuka maneno ya Bwana, "Jogoo hatawika hata utakapokwisha kunikana mara tatu" (Yn. 13:38). Vitabu vingine vya Habari Njema vinatuambia kwamba kwa saa ile Petro alitoka na kutoa machozi na uchungu.

### F. Yesu mbele ya Pilato (18:28-40)

**18:28** Hukumu ya Yesu mbele ya watu wa dini ilikwisha na hukumu yake mbele ya watu wa serikali ilikuwa karibu kuanza katika nyumba ya hukumu. Wayuda hawakutaka kuingia nyumba ya Mtaifa. Walifikiri neno hili **litawachafua** na kuwazuiza wasile **Pasaka**. Hawakukumbuka kwamba walikuwa wakifanya shauri kuua Mwana wa Mungu. Kuingia nyumba ya Mtaifa kungalikuwa msiba, lakini uuaji ulikuwa neno dogo kwa mafikiri yao. Augustine alisema,

> Upofu mkubwa wa uovu! Wangalichafuwa na nyumba ya mtu mwingine, lakini si na zambi yao wenyewe. Waliogopa kuchafuwa na nyumba ya hukumu ya mwamuzi wa taifa lingine, na hawakuogopa kuchafuwa kwa damu ya ndugu asiyekuwa na kosa.

**"Wapate kula Pasaka"** – tunafikiri ilikuwa karamu *iliyofuata* Pasaka. Walikuwa wamekula Pasaka usiku uliopita.

**18:29** Basi **Pilato**, liwali la Waroma, alitoka **inje** kusemana na Wayuda, akaanza na kuwauliza kama **walishitaki** mfungwa huyu juu ya nini.

**18:30** Wayuda walimjibu na uhodari na bila adabu. Walisema walikuwa wamehukumu mfungwa huyu na ya kwamba alikuwa na hatia. Basi walitaka tu Pilato kuagiza auawe.

**18:31** Lakini **Pilato** akijaribu kuepuka daraka hii, alisema nao, kama wangalihukumu Yesu na kumkuta kuwa na hatia, kwa sababu gani **hawakumhukumu kwa torati yao?** Jibu lao lilikuwa na maana kubwa. Walisema kwamba taifa lao halikuwa huru. Walitawaliwa na Waroma, na hawakuwa na amri **kuua mtu**. Jibu lao lilionyesha utumwa wao kwa Mataifa, na walitaka kusukuma machukizo ya mauti ya Kristo juu ya Pilato.

**18:32** Shairi 32 linaweza kuwa na maana mbili: (1) Katika Matayo 20:19 Yesu alitabiri kwamba atatolewa kwa Mataifa kuuawa. Hapa katika shairi 32 walikuwa wakifanya hivi. (2) Bwana alikuwa amesema tena na tena kwamba "atanyanyuliwa" (Yn. 3:14; 8:28; 12:32, 34), maana yake kusulibishwa. Wayuda waliua watu kwa njia ya kuwatupia

mawe, lakini Waroma walisulibisha wenye hatia. Hivi kwa njia ya kukataa kuua Yesu, Wayuda walitimiza, bila kujua, unabii huu juu ya namna ya kufa kwa Masiya (ona Zab. 22:16 vilevile).

**18:33 Pilato** alileta Yesu ndani ya **nyumba ya hukumu** kuulizana naye peke yake, akamwuliza: **"Wewe ni mfalme wa Wayuda?"**

**18:34 Yesu akajibu** na maneno kama haya: "Wewe ni liwali. Umesikia siku yo yote kwamba nilijaribu kupindua taifa la Roma? Umesikia kamwe ya kuwa nilitangaza kwamba mimi ni mfalme atakayeangamiza ufalme wa Kaisari? Unajua maneno haya wewe mwenyewe, au ulisikiliza tu masemo ya Wayuda hawa?"

**18:35** Na sauti ya kuonyesha zarau Pilato aliuliza, **"Mimi Myuda?"** Ni kama alionyesha na jibu hili kwamba yeye ni mtu mkubwa asiye na saa kwa maneno haya madogo ya Wayuda. Lakini jibu lake linaonyesha vilevile kwamba hakujua kama Yesu alishitakiwa juu ya nini. Alijua tu maneno watawala wa Wayuda waliyosema.

**18:36** Halafu Bwana alikiri kwamba **alikuwa** Mfalme kweli, lakini si namna ya mfalme Wayuda waliyofikiri. Hakuwa mfalme atakayekuwa hatari kwa Roma. **Ufalme** wa Kristo hausimamishwi na silaha za dunia. Kwa sababu hii wanafunzi wake **hawakupiga vita** ili asikamatwe na Wayuda. **Ufalme** wa Kristo **si wa dunia hii,** maana si ya ulimwengu huu. Uwezo na amri yake si ya ulimwengu; makusudi yake si ya dunia.

**18:37** Wakati **Pilato** alipouliza kama alikuwa **mfalme, … Yesu alijibu, "Wewe unasema ya kwamba mimi ni mfalme."** Lakini ufalme wake ni juu ya **kweli**, na hausimamishwi na panga na ngabo. **Alifika duniani kushuhudia kweli,** ndiyo **kweli** juu ya Mungu, Kristo mwenyewe, Roho Mtakatifu, mtu, zambi, wokovu, na mafundisho makubwa yote mengine ya Ukristo. **Kila mtu anayependa kweli anasikia sauti yake.** Ni kwa njia hii ufalme wake unapata nguvu.

**18:38 Pilato** alifikiri nini wakati **aliposema naye**, **"Kweli ni kitu gani?"** Alifazaika? Au aliuliza na sauti ya kuzarau? Au aliuliza na roho ya kweli? Hatujui, lakini tunajua Kweli ndani ya mwili wa mtu alisimama mbele yake, naye hakumtambua. Pilato alikubali sasa mbele ya Wayuda kwamba **hakuona hata kosa moja kwake.**

**18:39** Ilikuwa **desturi** ya Wayuda kwa wakati wa **Pasaka** kuomba Waroma kuwafungulia mmoja wa wafungwa wao. Pilato alikumbuka desturi hii sasa na alijaribu kupendeza Wayuda na **kufungua** Yesu.

**18:40** Shauri lake lilikufa bure. Wayuda hawakutaka Yesu; walitaka **Baraba. Baraba alikuwa mnyanganyi.** Watu wale waovu walitaka mnyanganyi kupita Mwumba wao.

### G. Hukumu ya Pilato: Bila hatia lakini alihukumiwa kufa (19:1-16)

**19:1 Pilato** alitenda bila haki hata kidogo wakati alipoagiza Huyu asiyekuwa na hatia kupigwa mijeledi. Labda alitaraji ya kwamba Wayuda wakiona Yesu akiazibiwa hivi wataacha kuomba *auawe*. Ilikuwa desturi ya Waroma kuazibu wafungwa hawa kwa njia ya kuwapiga mijeledi. Mfungwa alipigwa na fimbo au mti. Fimbo ilikuwa na vipande vidogo vya chuma au mfupa, na vitu vikali hivi vilipasua mwili wa mtu, na kuacha vidonda vikubwa.

**19:2,3 Askari** walizarau Yesu kwa sababu alisema alikuwa Mfalme. Taji kwa Mfalme! Lakini ilikuwa **taji ya miiba.** Bila shaka aliumia sana wakati waliposukuma taji hii juu ya kichwa chake. Miiba ni mfano wa laana iliyo-

pata binadamu kwa sababu ya zambi. Tunaona hapa mfano wa Bwana Yesu akibeba laana ya zambi zetu ili sisi tuweze kuvaa taji ya utukufu. **Vazi jekundu** lilikuwa alama nyingine ya kuzarau. Nyekundu ilikuwa rangi ya kifalme. Lakini linatukumbusha vilevile namna zambi zetu ziliwekwa juu ya Yesu ili sisi tuweze kuvikwa na vazi la haki ya Mungu.

Ni huzuni kubwa kufikiri juu ya Mwana wa Mungu akipigwa na **mikono** ya viumbe vyake! Na kusikia wakitumia midomo ambayo aliumba kumzarau!

**19:4 Halafu Pilato alitoka tena inje**, akawaambia kwamba ataleta Yesu **inje**, lakini ya kwamba Yesu hakuwa na kosa. Kwa njia hii Pilato alijihukumu na masemo yake mwenyewe. Hakuona kosa ndani ya Kristo, lakini alikataa kumfungua.

**19:5** Wakati Yesu **alipotoka** na **taji ya miiba na vazi jekundu,** Pilato alimwita **"Mtu huyu!"** Hatujui kama alisema hivi na sauti ya kuzarau, au huruma, au bila kuonyesha mawazo ya roho yake.

**19:6 Wakubwa wa makuhani** walitambua kwamba Pilato alisita, hivi walilalamika na ukali kwamba inapasa Yesu kusulibishwa. Ni watu wa *dini* walioongoza watu wengine ndani ya uuaji wa Mwokozi. Ndani ya mia za miaka inayopita tangu wakati ule ni viongozi vya kanisa waliotesa waamini wa kweli na ukali zaidi. Ni kama **Pilato** alichoka na Wayuda na kuchukia kwao bila sababu kwa Yesu. Alisema maneno kama haya nao: "Kama haya ndiyo mawazo yenu, **mumtwale ninyi wenyewe na kumsulibisha**. Kwa mafikiri yangu yeye hana hatia." Lakini Pilato alijua kwamba Wayuda hawakuweza kumwua kwa sababu Waroma tu walikuwa na amri kufanya hivi.

**19:7** Wakati Wayuda walipoona kwamba hawakuweza kuhakikisha kwamba Yesu alikuwa mtu wa hatari kwa utawala wa Kaisari, walitaja mashitaki yao ya dini. Kristo alikuwa amesema yeye ni sawasawa na Mungu kwa sababu yeye ni **Mwana wa Mungu.** Wayuda walifikiri kusema hivi ni matukano yaliyostahili kuazibiwa na mauti.

**19:8, 9** Kufikiri kwamba labda Yesu alikuwa Mwana wa Mungu kulisumbusha roho ya Pilato. Hakuwa na salama mbele juu ya maneno haya ya Yesu, na sasa **alizidi kuogopa.**

Halafu Pilato aliingiza Yesu **nyumbani mwa hukumu**, akamwuliza kama **alitoka wapi**. Uzaifu wa roho wa Pilato ulionekana wazi. Alikuwa amesema mbele kwamba Yesu hakutenda neno baya, lakini alikosa uhodari kumfungua kwa sababu aliogopa Wayuda. Kwa sababu gani **Yesu hakujibu ulizo** lake? Tunafikiri alinyamaza kwa sababu alijua Pilato hakuwa tayari kufanya maneno aliyojua ilimpasa kufanya. Hatajulishwa maneno mengine kwa sababu hakutii maneno aliyokwisha kujua.

**19:10 Pilato** alijaribu kulazimisha Bwana kumjibu kwa njia ya kumwogopesha. Alikumbusha Yesu kwamba, akiwa liwali la Waroma, alikuwa na **mamlaka** au amri **kumfungua** au **kumsulibisha.**

**19:11** Ni shangazo kuona namna Yesu alivyojitawala mwenyewe. Alikuwa na roho ya utulivu kupita Pilato. Na sauti kimya alijibu kusema **mamlaka** yo yote ambayo Pilato alikuwa nayo **alipewa** na Mungu. Serikali zote zinasimamishwa na Mungu, na mamlaka yote, au kwa maneno ya dunia, au maneno ya roho, inapewa na Mungu.

**"Yeye ambaye alinitoa mikononi mwako** ana zambi kubwa zaidi" – labda Bwana alisema juu ya (1) *Kayafa*, kuhani mkubwa; (2) *Yuda* ambaye alimtoa kwa adui; au (3) *Wayuda* wenyewe. Wayuda walikuwa na Maandiko

Matakatifu yaliyotabiri kuja kwa Masiya. Ingaliwapasa kumtambua wakati alipokuja. Lakini walimkataa na hata saa ile walikuwa wakilalamika auawe. Shairi hili linaonyesha kwamba kuna vipimo mbalimbali vya hatia. Pilato alikuwa na hatia, lakini hatia ya Kayafa, na Yuda, na Wayuda waovu wote ilikuwa *kubwa zaidi.*

**19:12** Wakati Pilato alipokuwa karibu kukusudi kufungua Yesu, Wayuda walitoa mashitaki yao ya mwisho na makubwa zaidi. Walisema, "Kama ukifungua mtu huyu, wewe si rafiki ya Kaisari." (Mfalme wa Waroma aliitwa Kaisari.) Wayuda wale hawakupenda Kaisari hata kidogo. Walimchukia. Wangalitaka kumharibu na kujifungua toka utawala wake. Tena walitenda sawasawa walitaka kuchunga ufalme wake usiharibiwe na Yesu huyu aliyejiita mfalme! Waliazibiwa kwa udanganyifu wao mbaya wakati askari Waroma walipoingia Yerusalema kwa A.D. 70 na kuangamiza mji kabisa na kuua wenyeji wake.

**19:13** Pilato hakutaka Wayuda kumshitaki kwa Kaisari. Basi akiwa zaifu, alikubali kufanya neno makutano walilotaka. **Alileta Yesu inje,** akakaa juu ya kiti cha hukumu kwa **pahali panapoitwa Pahali pa Mawe.**

**19:14** Karamu ya Pasaka ilikuliwa mangaribi ya mbele. **Maandalio ya Pasaka** ndiyo matayarisho kwa karamu ambayo ilifuata. Tunafikiri **"karibu na saa sita"** ilikuwa saa 12 ya asubui, lakini hatujui kabisa. Pilato akasema na Wayuda, **"Tazama, Mfalme wenu!"** Tunafikiri alisema hivi kukasirisha Wayuda, akiwashitaki rohoni mwake juu ya kumtega hivi kuhukumu Yesu.

**19:15** Wayuda walisema tena na nguvu kwamba lazima Yesu asulibishwe. Pilato aliwauliza na kuzihaka, "Munataka kusulibisha **mfalme wenye** mwenyewe?" Halafu Wayuda na unyonge mkubwa walisema, **"Hatuna mfalme ila Kaisari."** Taifa lililokosa imani! Walichagua mfalme mpagano mwovu na kukataa Mungu wao!

**19:16** Pilato alikubali kupendeza Wayuda, akatia Yesu katika mikono ya askari **asulibishwe**. Alipenda sifa ya watu kupita sifa ya Mungu.

### H. Kusulibishwa (19:17-24)

**19:17** Labda neno linalotafsiriwa msalaba hapa ni nguzo moja au vipande viwili vya mbao vilivyofungwa pamoja. Ulikuwa kipimo mtu alichoweza kubeba. Yesu alianza kubeba msalaba wake, lakini tunasoma ndani ya vitabu vingine vya Habari Njema kwamba nyuma kidogo ulilетwa kwa mtu mmoja, jina lake Simoni wa Kurene. Labda **Pahali pa Mfupa wa Kichwa** palipewa jina hili kwa sababu 1) inchi kwa upande ule ilifanana na kichwa cha mfu kwa sababu ya mapango kilimani; au 2) kwa sababu wavunja sheria waliuawa pale; labda mifupa ya vichwa vyao ililala pale, hata kama sheria ya Musa iliagiza mifupa izikwe.

**19:18** Mikono na miguu ya Bwana Yesu ilifungwa kwa msalaba na misumari, kisha msalaba ulinyanyuliwa na kuachwa kuanguka ndani ya tundu lililotayarishwa mbele udongoni. Mtu mkamilifu wa pekee aliyeishi tangu zamani alipokewa hivi na watu wake mwenyewe! Kama hujamwamini na kumpokea kuwa Bwana na Mwokozi wako, vizuri ufanye hivi sasa wakati unaposoma habari hizi za namna alivyokukufilia. Wizi wawili walikufa pamoja naye, hapa mmoja na kule mmoja. Neno hili lilitimiza unabii wa Isa. 53:12, "Akahesabiwa pamoja na wale wenye kukosa."

**19:19** Ilikuwa desturi kuweka anwani kwa upande wa juu wa msalaba wa yule aliyesulibishwa na kuonyesha kwamba zambi yake ilikuwa nini. Pilato

aliagiza waandike, **YESU MNAZARETI, MFALME WA WAYUDA** na kuiweka juu ya msalaba wa katikati.

**19:20 Pahali pale … palikuwa karibu na mji.** Bwana Yesu alisulibishwa inje ya mpaka wa mji. Hatujui kabisa wakati wa sasa kama palikuwa wapi.

**19:21** Wakubwa wa makuhani hawakufurahi juu ya maneno yaliyoandikwa. Walitaka kuongeza kwamba Yesu *alisema* ya kwamba alikuwa mfalme wa Wayuda (ndilo neno la kweli).

**19:22 Pilato** alikataa kugeuza maandiko yenyewe. Alikuwa amekwisha kuchoka na maneno ya Wayuda hawa na alikataa kufanya tena maneno waliyotaka. Ingalikuwa vizuri kama angalikuwa na roho ya nguvu namna hii mbele!

**19:23** Wakati watu waliposulibishwa **askari** walikuwa na ruhusa kugawa katikati yao vitu vya wale waliouawa. Hapa tunawaona wakigawa mavazi ya Kristo. Ni kama kulikuwa na vipande vitano. Waligawa vipande vine, lakini cha tano, kanzu, haikushonwa na haitakuwa na faida tena kama ikikatwa.

**19:24** Hivi walipiga kura kuona kama itakuwa ya nani. Hawakujua ya kwamba wakati walipofanya hivi, walitimiza unabii wa kushangaza ulioandikwa miaka elfu moja mbele (Zab. 22:18)! Kuona kutimizwa kwa unabii tena na tena kunatukumbusha tena kwamba Kitabu hiki ni kweli Neno lililoongozwa na Mungu, na ya kwamba Yesu Kristo ni kweli Masiya ambaye Mungu aliahidi atakuja.

### I. Yesu anaweka mama yake kwa mikono ya Yoane (19:25-27)

**19:25** Walimu wengi wanafikiri wanawake wane wanatajwa ndani ya shairi hili: (1) Maria, ndiye **mama** ya Yesu; (2) **ndugu mke** ya Maria aliyeitwa Salome na aliyekuwa mama ya Yoane; (3) **Maria, mke wa Kleopa;** (4) **Maria Magdalene.**

**19:26, 27** Hata wakati Bwana alipokuwa na maumivu makali yeye mwenyewe, alikuwa na huruma kwa watu wengine. Akiona **mama yake,** na Yoane, **mwanafunzi** wake, alisema na mama yake ya kwamba Yoane atakuwa kama mwana kwake kuanza wakati ule. Bwana hakukosa adabu wakati alipoita mama yake, **"Mwanamke".** Lakini vizuri tuone kwamba hakumwita "Mama". Neno hili linatufundisha ya kuwa haifai kwetu kutukuza Maria na kumwabudu. Yesu alisema na Yoane hapa kulinda Maria namna alivyoweza kulinda mama yake mwenyewe. Yoane alitii na alipeleka Maria **kwa nyumba yake mwenyewe.**

### J. Kazi ya Kristo ilikwisha (19:28-30)

**19:28** Bila shaka saa tatu za giza zilikuwa katikati ya mashairi 27 na 28 – toka saa sita kufika saa tisa. Ni kwa muda huu wakati Yesu alipoachwa na Mungu, aliteswa na azabu kwa zambi zetu. Kilio chake, **"Nina kiu!"** kinaonyesha kiu mwilini mwake, kiu inayoongezeka saa ya kusulibishwa. Lakini kinatukumbusha vilevile kwamba kiu yake ya roho kwa wokovu wa nafsi za watu ilikuwa kubwa zaidi.

**19:29** Askari walimkunywesha siki. Tunafikiri walifunga sifongo iliyojazwa siki juu ya fimbo na hisopo na kuitia kwa kinywa chake. (**Hisopo** ni pando lililotumiwa kwa wakati wa Pasaka vilevile – Kut. 12:22.) Siki hii ni mbali na mvinyo iliyochanganyika na nyongo ambayo watu walitaka kumpa mbele (Mt. 27:34). Yesu alikataa kunywa mvinyo ile kwa sababu ingalipunguza maumivu yake. Ilikuwa lazima kwake kubeba zambi zetu na ufahamu wote.

**19:30 "Imekwisha!"** Ndiyo kazi ambayo Baba yake alimpa! Kumwanga nafsi yake kama toleo kwa zambi! Kazi ya ukombozi na ya upatanisho! Ndiyo, alikuwa kwanza hai, lakini mauti, kuzikwa na kupanda kwake mbinguni – ni

kama maneno haya yote yalikuwa yamefanyikana. Hivi Bwana Yesu aliweza kutangaza kwamba njia ilikuwa imetayarishwa kwa wenye zambi kuokolewa. Shukuru Mungu leo kwa kazi Bwana Yesu Kristo aliyokwisha kumaliza kwa msalaba wa Kalvari!

Walimu wengine wanasema maana ya **"akainama kichwa chake"** ni ya kama aliinamisha kichwa chake nyuma. Vine anasema "Kichwa chake hakikuanguka tu mbele na uzaifu nyuma ya mauti – ni kama yeye mwenyewe aliinamisha kichwa chake *nyuma* kama kwa kupumzika."

Kisha **alitoa roho yake**. Ndiyo, alikufa kwa kutaka kwake mwenyewe. Yeye mwenyewe alichagua saa ya kufa kwake. Akiwa na nguvu na akili yote ali*ruhusu* **roho yake** kuondoka – hakuna mtu tu aliyeweza kufanya hivi.

### K. Kuchomwa kwa mbavu ya Mwokozi (19:31-37)

**19:31** Tunaona tena ya kwamba Wayuda hawa waliweka roho sana juu ya kuchunga maagizo madogo madogo pamoja na uuaji. Walifikiri haifai **kuacha maiti kubaki msalabani** siku ya sabato. Kutakuwa na karamu ya dini siku ile. Hivi waliomba Pilato aagize **miguu** ya watu wale watatu **kuvunjwa** kusudi wafe mbio kupita.

**19:32** Hatusomi kama miguu yao ilivunjwa namna gani. Tunafikiri ilivunjwa kupita mara moja kwa sababu kuivunja pahali pamoja tu kusingalitosha kufanyiza mtu mwenyewe kufa.

**19:33** Askari hawa walijuana sana na maneno namna hii. Walitambua kwamba Yesu ... amekwisha kufa. Walijua kwamba hakuzimia tu. Basi hawakuvunja miguu yake.

**19:34** Hatusomi kwa sababu gani mmoja wa askari alichoma mbavu yake. Labda alikuwa akionyesha wazi tu uovu na machukio ya roho yake kwa Mungu na Kristo. Watu hawapatani juu ya maana ya **damu na maji**. Wengine wanafikiri yanaonyesha kwamba Yesu alikufa kwa sababu ya kuvunjwa kwa moyo wake – lakini tulisoma mbele kwamba Yesu alichagua kufa. **Damu** ni mfano wa kusafishwa toka hatia ya zambi; maji yanasema juu ya kusafishwa na **Neno la Mungu** toka uchafu wa zambi.

**19:35** Labda shairi hili linasema juu ya miguu ya Yesu isiyovunjwa, juu ya kuchomwa kwa mbavu yake, au labda juu ya maneno yote ya kusulibishwa. Bila shaka **naye aliyeona** alikuwa Yoane aliyeandika Habari Njema hii.

**19:36** Shairi hili linaturudisha kwa shairi 33 na kutimiza kwa maneno yaliyoandikwa katika Kut.12:46: "Hamutavunja mfupa wake hata mmoja." Shairi lile linasema juu ya mwanakondoo ya Pasaka. Mungu aliamuru mifupa isivunjwe. Kristo ni Mwanakondoo ya kweli ya Pasaka, na alitimiza maneno yote ya mfano huu.

**19:37** Shairi hili linatazama nyuma kwa shairi 34. Askari hakujua kwamba tendo lake lilitimiza unabii mwingine wa ajabu wa andiko (Zek.12:10). Matendo maovu ya watu hayawezi kuzuiza makusudi ya Mungu. Unabii wa Zekaria utatimizwa kwa wakati wa kuja saa waamini Wayuda watakapoona Bwana akirudia dunia. "Watamtazama yeye ambaye walimchoma. Ndiyo, watamwombolezea kama mtu anavyoombolezea mwana wake mzaliwa pekee."

### L. Maziko katika kaburi la Yosefu (19:38-42)

**19:38** Shairi hili linaanza habari za maziko ya Yesu. Kufika wakati ule **Yosefu wa Arimatea** hakuonyesha imani yake wazi kwa sababu ya **woga wa Wayuda**. Sasa alikwenda na uhodari na kuomba kupewa mwili wa Yesu

aweze kuuzika. Wakati alipofanya hivi alijiingiza katika hatari ya kuondoshwa toka sunagogi, na hatari ya mateso na jeuri. Lakini ni huzuni kwa sababu hakusimamia Bwana wake mkataliwa wakati alipokuwa hai na kutumikia makutano ya watu kwanza.

**19:39,40** Wasomaji wa Habari Njema ya Yoane walikuwa wamesoma juu ya **Nikodemo** mbele, wakati **alipofikia Yesu usiku** (sura 3), na wakati aliposema na watu wa Baraza kwamba iliwapasa kusikia ushuhuda wake (Yn. 7:50-51). Sasa alifika karibu na Yosefu, akileta **machanganyiko ya manemane na uude, karibu na ratli mia.** Tunafikiri manukato haya yalikuwa unga uliowekwa juu ya mwili. Nyuma yake **walifunga mwili na sanda ya kitani.**

**19:41** Karibu habari zote ndani ya mashairi haya zinatimiza unabii. Isaya alikuwa ametabiri kwamba watu watakusudi kuzika Masiya pamoja na waovu lakini ya kwamba atakuwa pamoja na watajiri katika kufa kwake (Isa. 53:9). Bila shaka **kaburi jipya shambani** lilikuwa mali ya tajiri. Katika Matayo tunasoma kwamba lilikuwa mali ya Yosefu wa Arimatea.

**19:42** Mwili wa **Yesu** uliwekwa ndani ya kaburi hili. Wayuda waliweka roho juu ya kuondosha mwili katikati yao kwa sababu karamu yao itaanza wakati wa mangaribi. Lakini maneno haya yote ni sehemu ya shauri la Mungu kwa mwili kuwa udongoni kwa siku tatu mchana na usiku. Tukumbuke kwamba Wayuda walihesabu sehemu tu ya siku kama siku nzima. Hivi Bwana akiwa kaburini kwa sehemu ya siku tatu alitimiza unabii wake katika Mt. 12:40.

## 9. KUSHINDA KWA MWANA WA MUNGU (Sura 20)

### A. Kaburi wazi (20:1-10)

**20:1 Siku ya kwanza ya juma Maria Magdalene alikuja kwa kaburi** mapema. Tunafikiri kaburi lilikuwa chumba kidogo kilichochorwa toka kilima na **jiwe** kwa lango lake lilikuwa mviringo na panapana. Litaweza kufingirishwa ndani ya kisima kirefu kidogo mbele ya kaburi kukifunga. Wakati Maria alipofika, **jiwe lilikuwa limeondoshwa**. Ndani ya Matayo 28 tunasoma kwamba neno hili lilitokea *nyuma* ya ufufuko.

**20:2** Maria alikimbia mara moja karibu na Petro na Yoane na habari hizi za kushangaza kwamba mwili wa Bwana ulikuwa umehamishwa toka kaburi. Hakusema nani alifanya neno hili, lakini **wameondoa**. Wanawake waliokuwa kwa kaburi na kwa wakati wa ufufuko wake walikuwa waaminifu na wenye mapendo makubwa kwa Bwana wao. Wanafunzi walikuwa wameacha Bwana na kukimbia. Wanawake walibaki palepale bila kujifikiri wenyewe.

**20:3, 4** Labda Petro na Yoane walifikiri nini wakati **walipotoka mji** mbio kwenda kwa shamba karibu na Kalvari? Hatujui. Tunafikiri Yoane alikuwa kijana kupita Petro na alifikia **kaburi kwanza.**

**20:5** Ni kama mlango kuingia kaburi ulikuwa mdogo na ilipasa mtu kuinama kuingia au kuangalia ndani. Yoane aliona sanda ya kitani imewekwa. Ilikuwa imeondoshwa mwilini, au ilikuwa kwa umbo iliofunga mwili? Basi **Yoane hakuingia kaburi.**

**20:6,7** **Petro** alikuwa amefika vilevile sasa, akaingia kaburi bila kusita. **Aliona sanda ya kitani imewekwa,** lakini mwili wa Mwokozi haukuwa pale.

Namna **kitambaa cha kichwa** kimewekwa na kukunjwa peke yake inaonyesha kwamba Bwana aliondoka kaburini na utaratibu, si haraka haraka. Kama mtu angaliiba mwili asingaliweka roho juu ya **kukunja** kitambaa!

**20:8** Yoane aliingia kaburi na kuona namna sanda na kitambaa vilivyowekwa

kwa utaratibu. Akaona, lakini si kwa macho ya mwili tu lakini **akaona, akaamini.** Sasa alifahamu kabisa. Aliona vitu vilivyoshuhudia ufufuko wa Kristo **na … aliamini**.

**20:9** Kufika wakati ule wanafunzi hawakufahamu kabisa **andiko** katika Agano la Kale ya kwamba **sharti** Masiya **afufuke toka wafu**. Bwana Yesu mwenyewe aliwaambia tena na tena, lakini hawakufahamu.Yoane alikuwa wa kwanza aliyefahamu na kuamini.

**20:10** Halafu wanafunzi walirudi pahali walipopanga; tunazani walikaa katika Yerusalema. Bila shaka walifikiri kwamba si faida kukaa kungoja kwa kaburi. Ingekuwa vizuri kupita kwenda kuwaambia wanafunzi wengine habari za maneno waliyoona.

**B. Ono la Maria Magdalene (20:11-18)**

**20:11** Waza juu ya maneno mawili ya kwanza ya shairi hili – **Lakini Maria.** Wanafunzi wale wawili wengine walikuwa wamerudi kwao, *lakini Maria* ... Hapa tunaona tena mapendo makubwa ya mwanamke. Alikuwa amesamehewa zambi nyingi, hivi alipenda sana. Alibaki peke yake inje ya kaburi, akitoa machozi kwa sababu alifikiri watu, labda adui za Bwana, walikuwa wameiba mwili wake.

**20:12** Mara hii, wakati alipoangalia ndani ya kaburi, aliona malaika wawili wakiketi **pahali ulipowekwa mwili wa Yesu.**

**20:13** Ni kama Maria hakusituka wakati alipowaona. Alijibu ulizo lao bila woga. Jibu lake lilionyesha wazi kwamba hata kwa saa ile hakufahamu kwamba Yesu alikuwa amefufuka na alikuwa hai tena.

**20:14** Saa hii neno lilifanyiza Maria kugeuka na kuangalia nyuma yake. **Yesu** mwenyewe alisimama pale, lakini hakumtambua. Ilikuwa kwanza asubui mapema, labda mbele ya mpambazuko. Alikuwa ametoa machozi kwa saa ndefu na hakuweza kuona vizuri. Labda vilevile Mungu alimzuiza asitambue Bwana kufika saa iliyokubaliwa naye.

**20:15** Bwana alijua majibu ya maulizo haya; lakini alitaka kusikia Maria akiyajibu na sauti yake mwenyewe. **Maria** alifikiri **alikuwa mlinzi shamba**. Mwokozi wa dunia anaweza kuwa karibu sana na watu bila kutambuliwa nao. Zaidi anafikia watu kama mtu wa chini, si kama mtu wa kujulikana duniani. Ndani ya majibu yake, Maria hakutaja jina la Bwana. Alikumbuka Mmoja tu na hakufikiri kusema kama alikuwa nani.

**20:16** Sasa Maria alisikia sauti ambayo alijuana nayo sana ikiita jina lake. Alikuwa sauti ya **Yesu** kweli! Alimwita **Raboni**, maana yake "**Mwalimu** wangu mkubwa." Alikaa kufikiri juu yake kama Mwalimu Mkubwa ambaye alimjua. Hakufahamu kwanza ya kwamba sasa alikuwa mkubwa kupita Mwalimu wake – alikuwa Bwana na Mwokozi wake. Hivi Bwana alitayarisha njia kumweleza namna gani atamjua sasa.

**20:17** Maria alikuwa amejua Yesu mbele kama Mtu. Alikuwa ameona maajabu yake wakati alipokuwa katikati yao. Hivi alifikiri kama hakumwona tena na macho, hatabarikiwa naye tena. Ilipasa Bwana kutengeneza mawazo haya. Alisema naye, **"Usikwamane nami** kama mtu wa dunia tu. **Sijapanda kwa Baba yangu.** Wakati nitakaporudi mbinguni, Roho Mtakatifu atatumwa duniani. Wakati atakapokuja atanifunua kwa roho yako namna usivyonijua mbele. Utanipenda na kujua kwamba mimi ni karibu zaidi nawe kupita mbele, namna isipowezekana wakati nilipokuwa hapa duniani."

Kisha alisema naye **kwenda** karibu na **ndugu** zake na kuwaambia habari hizi mpya. Ni mara ya kwanza aliyoita

wanafunzi wake **"ndugu zangu."** Alitaka wajue kwamba Baba yake alikuwa Baba yao, na Mungu wake alikuwa Mungu wao. Mbele ya wakati huu waamini hawakuwa "wana" na "wariti wa Mungu."

Bwana Yesu hakusema, "Baba yetu," lakini Mungu ni Baba yetu namna nyingine na namna alivyo Baba wa Bwana Yesu. Yeye ni **Baba** wa Bwana Yesu tangu milele. Kristo ni Mwana tangu zamani. Mwana ni sawasawa na Baba. Sisi tume*fanywa* wana wakati tulipookolewa na tutakuwa wana milele. Kama wana wa Mungu, sisi si sawa na Mungu, na hatutakuwa sawa naye kamwe.

**20:18 Maria Magdalene** alitii agizo la Bwana. Bila shaka alipewa heshima hii kubwa kuletea mitume habari hizi za ajabu kama zawabu, kwa sababu ya mapendo yake makubwa kwa Kristo.

**C. Yesu anaonekana kwa wanafunzi wake (20:19-23)**

**20:19** Ilikuwa siku ya kwanza sasa, **mangaribi. Wanafunzi walikuwa wamekusanyika**, labda ndani ya chumba cha juu pahali walipokutana usiku, siku tatu mbele. Walikuwa wamefunga milango **kwa sababu ya kuogopa Wayuda**. Gafula waliona **Yesu** akisimama **katikati yao**, na kumsikia akisema, **"Salama kwenu."** Ni wazi kwamba Bwana aliingia chumba bila kufungua mlango. Lilikuwa ajabu. Tukumbuke kwamba mwili wake wa ufufuko ulikuwa mwili wa nyama na mifupa. Lakini hata hivi alikuwa na uwezo kupita milango iliyofungwa na kutenda maneno mengine yasiyowezekana kwa watu. Maneno haya **"Salama kwenu"** yalikuwa na maana mpya sasa kwa sababu Kristo alikuwa amefanya salama kwa njia ya damu ya msalaba wake. Wale wanaohesabiwa haki kwa njia ya imani wana salama na Mungu.

**20:20** Nyuma ya kuwatangazia salama, **aliwaonyeshea** alama za maumivu yake msalabani, kwa njia yao salama ilipatikana kwao. Waliona alama za misumari na kidonda cha mkuki. Furaha ilijaza roho zao wakati walipofahamu ni kweli **Bwana** wao aliyesimama katikati yao. Alikuwa amefanya maneno aliyosema mbele kwamba atafanya. Alikuwa amefufuka toka wafu. Bwana aliyefufuliwa ndiye msingi wa furaha ya Mkristo.

**20:21** Shairi hili ni tamu sana. Haifai kwa waamini kujifurahisha wenyewe tu na salama yake. Sharti waishiriki na watu wengine. Hivi aliwatumia duniani **kama Baba alivyomtuma yeye:**

Kristo alifika duniani kama mtu masikini.
Alikuja kama mtumishi.
Alijifanya mwenyewe hana utukufu.
Alifurahi kufanya mapenzi ya Baba yake.
Alijifanya mmoja na watu.
Alikwenda pahali pote akitenda mema.
Alifanya kila neno kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.
Kusudi lake lilikuwa kufa msalabani.

Sasa alisema na wanafunzi wake, **"Ninawatuma ninyi vilevile."**

**20:22** Hili ni moja la mashairi yaliyo nguvu zaidi kufahamu ndani ya kitabu hiki kizima. Tunasoma kwamba Yesu **akapulizia** wanafunzi na kusema, **"Mupokee Roho Mtakatifu."** Lakini Roho Mtakatifu aliletwa nyuma tu, ndiyo siku ya Pentekote. Namna gani Bwana aliweza kusema maneno haya bila neno lenyewe kufanyikana mara moja?

Shairi hili linaelezwa kwa njia mbalimbali: (1) Wengine wanasema Bwana aliahidi tu ya kwamba wanafunzi watapokea Roho Mtakatifu siku ya Pentekote. (2) Wengine wanasema wanafunzi hawakupokea uwezo wote wa Roho Mtakatifu kwa wakati ule, lakini aliwasaidia tu kujua kweli kupita, au

kupokea uwezo na kuongozwa kwa kazi yao. Wanasema wanafunzi walipokea arabuni ya Roho Mtakatifu. (3) Wengine wanasema wanafunzi walipokea ujazi wa Roho Mtakatifu. Ni nguvu kuamini neno hili wakati tunaposoma mashairi kama Luka 24:49 na Matendo 1:4,5,8, yaliyoandikwa kupasha juu ya kufika kwa Roho Mtakatifu kwa wakati wa kuja. Yoane 7:39 linaonyesha wazi kwamba Yesu atatukuzwa na kurudia mbingu mbele ya kufika kwa Roho Mtakatifu.

**20:23** Hili ni shairi gumu vilevile linaloelezwa kwa njia mbalimbali. (1) Wengine wanasema Bwana Yesu aliwapa mitume yake (pamoja na wale waliowaza kwamba wao waliriti madaraka yao) *uwezo* kusamehe zambi au kuzifunga. Elezo hili linabisha kabisa mafundisho ya Biblia ya kwamba Mungu tu anaweza kusamehe zambi (Luka 5:21). (2) Mwalimu mmoja, Gaebelein, anataja neno la mwalimu mwingine: “Shairi hili ni juu ya kuhubiri Habari Njema, na linaonyesha nini inahitajiwa kwa zambi za mtu kusamehewa, na ya kama mtu akikataa maneno haya, zambi zake zitafungwa.” (3) Elezo la tatu (linalofanana na lile la pili), ndilo elezo sisi tunalokubali, ni ya kuwa wanafunzi walipewa amri ku*tangaza* kwamba zambi za mtu fulani zimesamehewa.

Tulete mfano wa elezo hili la tatu: Wanafunzi wanakwenda kuhubiri Habari Njema. Watu wengine wanatubu zambi zao na kupokea Bwana Yesu. Wanafunzi wana amri kuwaambia kwamba zambi zao **zinasamehewa**. Wengine wanakataa kutubu na hawaamini Kristo. Wanafunzi wanawaambia kwamba wao wangali na zambi zao, na kama wakikufa watapotea kwa milele.

Tuone vilevile kwamba wanafunzi walipewa amri na Bwana namna gani kutenda kwa maneno ya zambi fulani. Katika Matendo 5:1-11 Petro alitumika na amri hii, na mwisho wake ulikuwa mauti ya Anania na Safira. Paulo alifunga zambi ya mtenda mabaya katika 1 Kor. 5:3-5, 12-13, na alisamehe zambi katika 2 Kor. 2:4-8. Mashairi haya ni juu ya usamehe wa azabu ya zambi hizi kwa maisha hapa duniani.

**D. Shaka inageuka imani (20:24-29)**

**20:24** Tusihukumu Tomasi mbio mbio kwa sababu hakuwa pale. Hatujui nini ilimzuiza.

**20:25** Alihitaji kuona neno kuhakikisha kwamba Bwana alifufuka kweli **mbele ya kuamini** neno hili. Anafanana na watu wengi wa wakati wa sasa, lakini mawazo haya yanakosa akili. Hata leo wenye elimu wanaamini maneno mengi wasiyoweza kuona na macho au kugusa.

**20:26** Nyuma ya juma moja Bwana alionekana kwa **wanafunzi wake** tena. Mara hii **Tomasi alikuwa pamoja nao.** Mara hii vilevile Bwana Yesu aliingia chumbani kwa njia ya mshangao, akawasalimu tena akisema, **“Salama kwenu.”**

**20:27** Bwana Yesu alitendea na huruma mfuata wake aliyekosa imani. Alisema naye kuona kwamba Bwana alifufuka kweli kwa njia ya kuingiza **mkono** wake ndani ya kidonda cha mkuki kwa **mbavu** zake.

**20:28** Halafu Tomasi aliamini. Hatujui kama aliingiza mkono wake ndani ya mbavu za Bwana. Lakini alijua sasa kwamba Yesu alifufuka kweli na ya kwamba yeye ni **Bwana** na **Mungu.**

**20:29** Tuone ya kwamba **Yesu** alikubali kwa Tomasi kumwabudu kama Mungu. Kama Yesu angalikuwa mtu tu, ingalimpasa kukataa. Lakini kuna namna ya imani inayopendeza Bwana kupita ile ya Tomasi. Tomasi aliamini tu nyuma ya kuona na macho. Bwana alisema, **“Heri wale wasioona, lakini wameamini.”**

Neno la Mungu linahakikisha kitu

kupita vitu vyote vingine. Mungu akisema neno, tunamheshimu kwa njia ya kuliamini; lakini hatumheshimu kama tukitaka kuona au kusikia maneno mengine kuhakikisha neno lake. Inatupasa kuamini kwa sababu yeye amesema hivi, na tunajua hawezi kusema uwongo au kuanguka.

### E. Kusudi la Habari Njema ya Yoane (20:30, 31)

Mengine ya maajabu ya Yesu hayakuandikwa ndani ya Habari Njema ya Yoane. Roho Mtakatifu alichagua alama zile zitakazotimiza shauri lake zaidi.

Hapa tunaona kama Yoane aliandika Habari Njema hii na kusudi gani. Aliliandika ili wasomaji wake **waweze kuamini ya kwamba Yesu ni Masiya,** na **Mwana wa Mungu.** Kama **wakiamini watapokea uzima wa milele kwa jina lake**.

Umeamini?

## X. MANENO YA MWISHO: MWANA MFUFULIWA PAMOJA NA WATU WAKE (Sura 21)

### A. Kristo anaonekana kwa wanafunzi wake kwa Galilaya (21:1-14)

**21:1** Habari hizi zinatokea kwa **bahari ya Tiberia** (Galilaya). Wanafunzi walikuwa wamesafiri kwa upande wa kaskazini kurudia nyumba zao. Bwana Yesu alikutana nao pale. Maana ya **"alijionyesha hivi"** ndiyo ya kwamba Yoane ataanza kupasha namna Bwana alivyotokea kwao.

**21:2** Saba wa wanafunzi walikuwa pamoja kwa wakati ule – **Petro, Tomasi. Natanaeli,** Yakobo na Yoane (**wana wa Zebedayo**) na **wawili wengine** ambao hatujui majina yao.

**21:3** **Simoni Petro** alisema atakwenda **kuvua samaki** kwa bahari na wanafunzi wengine walisema watakwenda pamoja naye. Hatuwezi kushangaa juu ya neno hili, lakini walimu wengine wa Biblia wanafikiri safari hii haikuwa mapenzi ya Mungu, na ya kwamba walikwenda bila kuomba kwanza. **Usiku ule hawakupata kitu.** Hawakuwa wavuvi wa kwanza walioshinda usiku wakivua bila kupata samaki. Ni mfano ya kwamba masumbuko yetu ya umtu ni bure kama hatusaidiwi na Mungu, zaidi kwa kazi ya kuleta watu karibu na Bwana Yesu.

**21:4** **Yesu** alikuwa akiwangoja wakati **walipokaribia pwani** asubui, lakini **hawakumtambua**. Labda ilikuwa kwanza giza, au labda Mungu aliwazuiza wasimtambue.

**21:5** Wakati Bwana alipowauliza kama walikuwa na chakula **walimjibu** na huzuni: **"Hapana."**

**21:6** Wanafunzi walifikiri huyu alikuwa mgeni tu akitembea kwa pwani ya bahari. Hata hivi walifanya neno ambalo aliwaambia kufanya, **wakatupa wavu kwa upande wa kuume wa chombo,** wakashangaa kabisa kupata **samaki** wengi sana. Wengi kabisa hata iliwashinda kukokota wavu! Neno hili linaonyesha kwamba Bwana Yesu alijua pahali samaki walipokuwa baharini. Linatufundisha vilevile ya kwamba wakati Bwana anapoongoza kazi yetu, hatutakuwa na wavu bure bila samaki. Anajua pahali watu walipo walio tayari kuokolewa, naye ni tayari kutuongoza kuwafikia kama tukimruhusu kufanya hivi.

**21:7** Wa kwanza aliyetambua **Bwana** alikuwa Yoane, naye alijulisha **Petro** mara moja. Petro **alijivika na vazi lake,** akakwenda kwa pwani. Hatujui kama aliogelea au kutembea na miguu kwa sababu maji yalikuwa nusu, au kama alitembea juu ya maji (ndiyo mafikiri ya watu wengine).

**21:8** Wanafunzi wengine waliingia chombo kidogo na kukokota **wavu** kwa karibu mètres 100 kufika pwani.

**21:9** Mwokozi alikuwa na vyakula

vya asubui tayari – **samaki** na **mkate.** Hatujui kama Bwana alikamata **samaki** hawa baharini au kama alifanya ajabu kuwapata, lakini tunajifunza kwamba hahitaji kusaidiwa na kazi yetu ndogo. Wakati tutakapofika mbinguni, bila shaka tutaona kwamba watu wengi waliokolewa kwa sababu ya mahubiri na ushuhuda wa mtu mmoja mmoja, na wengi wengine waliokolewa na Bwana mwenyewe bila kusaidiwa na mtu.

**21:10, 11** Halafu Bwana aliwaagiza kuleta wavu pamoja na **samaki** – si kuwapika, lakini kuwahesabu. Neno hili litawakumbusha ya kwamba kwa kupata baraka ndani ya kazi ya Bwana sharti watii neno lake kabisa.

Biblia inatupasha kama kulikuwa na samaki wengapi; **mia moja makumi tano na watatu.** Watu wameeleza hesabu hii kwa njia mbalimbali: (1) Ilikuwa hesabu ya lugha mbalimbali duniani kwa wakati ule. (2) Ni hesabu ya mataifa na makabila duniani watakaookokotwa na wavu wa Habari Njema. (3) Ni hesabu ya namna mbalimbali za samaki ndani ya bahari ya Galilaya, au duniani. Bila shaka inasema juu ya aina mbalimbali za watu watakaookolewa kwa njia ya mahubiri ya Habari Njema – toka kila kabila na taifa. Wavuvi walijua lilikuwa ajabu kwa **wavu** kufikia pwani bila **kupasuka**. Neno hili linafundisha kwamba tukifanya kazi ya Mungu namna anavyoagiza tutakuwa na vyote tunavyohitaji kila mara. Hataacha wavu wetu kupasuka.

**21:12** Bwana aliwaita kuja na kula **chakula cha asubui,** na wanafunzi walizunguka moto wa makala kula vitu vizuri ambavyo Bwana alikuwa ametayarisha. Bila shaka Petro alikumbuka moto mwingine pahali aliposimama na kukana Bwana wake! Ni kama wanafunzi walikuwa na hofu wakati walipoona Bwana akisimama pale kwa mwili wake wa ufufuko. Walijua **alikuwa Bwana,** na wangalipenda kumwuliza maneno mengi, lakini waliogopa.

**21:13** Halafu **Yesu** aliwapa mkate na samaki wapate kula. Bila shaka walikumbuka siku nyingine wakati alipokulisha watu elfu tano na mkate na samaki wachache.

**21:14** Hii ilikuwa **mara ya tatu** Yoane aliyoandika juu ya Yesu akionekana **kwa wanafunzi wake**. Ndani ya vitabu vingine vya Habari Njema tunasoma juu ya mara nyingine vilevile. Katika Habari Njema ya Yoane alionekana kwa wanafunzi mangaribi ya siku ya ufufuko, tena nyuma ya juma moja, na halafu sasa kwa pwani ya bahari ya Tiberia.

### B. Kurudishwa kwa Petro karibu na Bwana (21:15-17)

**21:15** Bwana alisaidia kwanza mahitaji ya mwili ya wanafunzi wake. Halafu wakati miili yao ilipokuwa moto na walipokwisha kula, aligeuka kusema na **Petro** juu ya maneno ya roho. Petro alikuwa amekana Bwana mara tatu. Tangu wakati ule alikuwa ametubu na kurudishwa karibu na Bwana. Ndani ya mashairi haya Bwana alionyesha mbele ya watu kwamba Petro alipokwisha kurudi karibu naye.

Maneno mbalimbali mawili ya Kiyunani yanatafsiriwa **mapendo** ndani ya mashairi haya. Neno Bwana Yesu alilotumia ni kwa mapendo ya nguvu kupita neno lililotumiwa na Petro. Petro hakujivuna tena juu ya kipimo cha mapendo yake kwa Bwana, na ya kwamba hatamwacha tena kamwe, si neno kama wanafunzi wote wengine wakifanya hivi. Alikuwa amefahamu uzaifu wake.

Bwana Yesu alisema, **"Kulisha wana-kondoo zangu."** Njia nzuri sana kwa sisi kuonyesha mapendo kwa

Kristo ni kulisha wana-kondoo ndani ya kundi lake. Ona ya kwamba Bwana hasemi tena juu ya kuvua samaki, lakini juu ya kuchunga kondoo. Kuvua samaki kunatufikirisha juu ya kuhubiri Habari Njema; kuchunga kondoo kunatufikirisha juu ya kufundisha na kulinda kondoo.

**21:16** Bwana aliuliza Petro **mara ya pili** kama alimpenda. Petro alimjibu namna alivyojibu mbele; hakujisadiki mwenyewe tena. Mara hii Bwana alisema naye, **"Chunga kondoo zangu."** Kuna wana-kondoo na kondoo ndani ya kundi la Kristo, nao wote wanahitaji kuchungwa na mapendo, na mwenye kupenda Mchungaji.

**21:17** Petro alikana Bwana mara tatu mbele, na sasa alipata njia kukiri mara tatu kwamba alimpenda.

Mara hii Petro alisema kwamba Yesu ni Mungu, na **anajua maneno yote.** Alisema **mara ya tatu kwamba alimpenda**. Halafu Bwana alisema naye mara ya mwisho kuonyesha mapendo yake kwa njia ya kulisha **kondoo** za Kristo. Neno kubwa moja ambalo mashairi haya yanatufundisha ni ya kwamba mapendo yetu kwa Kristo tu yanatosha kama sababu ya kumtumikia.

### C. Yesu anatabiri mauti ya Petro (21:18-23)

**21:18** Wakati Petro **alipokuwa kijana** alikuwa huru kwenda **pahali po pote alipotaka**. Lakini Bwana alimwambia kwamba kwa mwisho wa maisha yake atafungwa na kupelekwa kuuawa.

**21:19** Shairi hili linaeleza shairi 18. Petro **atatukuza Mungu** kwa njia ya kufa kwa Kristo. Huyu aliyekana Bwana mbele atapewa uhodari kutoa uzma wake kwaye. Shairi hili linatukumbusha kwamba tunaweza kutukuza Mungu kwa njia ya kuishi kwaye, na kwa njia ya kufa kwaye vilevile. Halafu Bwana alimwambia: **"Unifuate."** Ni kama saa aliposema hivi alianza kwenda zake.

**21:20** Ni kama **Petro** alianza kufuata Bwana, halafu **akigeuka aliona** Yoane **akifuata** vilevile. Mara hii Yoane alieleza ya kwamba ndiye **aliyeegamia kifua cha Yesu** wakati wa chakula cha **Pasaka,** na kuuliza nani ndiye atamtoa.

**21:21** Wakati **Petro** alipoona Yoane, bila shaka alijiuliza kama **nini itapata** Yoane. Atakufa vilevile kwa sababu ya imani yake? Au atakuwa kwanza hai wakati Bwana atakapokuja tena? Hivi aliuliza Bwana kama nini itapata Yoane.

**21:22** Bwana alijibu kusema haifai Petro kusumbuka juu ya nini itapata Yoane wakati wa kuja. Hata kama akiishi kufika wakati Kristo atakapokuja mara ya pili, neno hili lisingaligeuza maneno ya Petro. Mara nyingi wafuata wa Yesu wanaanguka ndani ya kazi yao kwa Bwana kwa sababu ya kufikiri maneno ya wenzao kupita maneno ya Bwana.

**21:23** Lakini watu waligeuza maneno Bwana aliyosema. **Hakusema** Yoane atakuwa hai wakati atakaporudi tena. Alisema tu kama angalikuwa hai wakati ule, kwa nini ile itageuza maneno yatakayopata Petro? Watu wengi wanaona maana hapa – namna Bwana alivyotaja Yoane pamoja na kuja kwake mara ya pili – kwani Yoane alipewa heshima ya kuandika Ufunuo wa Yesu Kristo, ndani yake alieleza moja moja mambo ya wakati wa mwisho.

### D. Ushuhuda wa mwisho wa Yoane (21:24, 25)

**21:24** Yoane alitoa ushuhuda ya kwamba maneno aliyoandika yalikuwa kweli. Watu wengine wanafikiri maneno

haya ni ushuhuda wa wazee wa kanisa kwa Efeso.

**21:25** Yesu ni Mungu, na maana ya masemo yake na hesabu ya kazi zake ni bila kipimo. Hata wakati alipokuwa kwanza duniani alitegemeza na kutembeza vitu vyote – jua, mwezi, na nyota, ndiyo kazi ya ajabu kabisa. Na tunajua nusu tu juu ya maajabu aliyofanya hapa duniani. Wakati alipoponyesha watu, waza juu ya kazi aliyofanya ndani ya miili yao, akigusa mashipa na mifupa, na mnofu, damu, na viungo vingine vya mgonjwa mwenyewe. Waza juu ya namna alivyotawala samaki na nyama, na kuongoza maneno ya watu, na kila kipande kidogo zaidi (atome) cha dunia hii. Ndiyo, **dunia yote** haiwezi kutosha kwa **vitabu** vyote vingalihitajiwa kuandika juu ya maneno haya yote.

Hivi tunafikia mwisho wa mafundisho haya juu ya Habari Njema ya Yoane. Hatushangai kwa sababu ni kimoja cha vitabu ambavyo watu wanapenda zaidi katika Biblia. Haiwezekani kukisoma bila kupendana kupita na Bwana na Mwokozi wetu ambaye kinatupasha habari zake.

## NOTES

[1] (1:29) J. Cynddylan Jones, *Studies in the Gospel According to St. John,* ukurasa 103.

[2] (2:4) George Williams, *The Student's Commentary on the Holy Scriptures,* ukurasa 194.

[3] (5:24) Kuna mashairi mengine yanayofundisha ya kwamba siku nyingine mwamini atasimama mbele ya Kiti cha Hukumu cha Kristo (Rom. 14:10; 2 Kor. 5:10). Lakini hataazibiwa kwa zambi zake kwa wakati ule kwa sababu Kristo alipokea hukumu kwa zambi hizi kwa Kalvari. Kwa kiti cha hukumu cha Kristo, Bwana ataangalia maisha na utumishi wa mwamini, naye atapokea zawabu, au hasara. Hatahukumiwa kwa neno la wokovu wake, lakini kwa kipimo cha matunda ya maisha yake.

[4] (5:29) Kama hili lingalikuwa shairi la pekee juu ya ufufuko, tungalifikiri wafu wote wangalifufuliwa kwa saa moja. Lakini kuna mashairi mengine, zaidi Ufunuo 20, yanayofundisha kwamba kuna muda wa miaka elfu moja au zaidi nyuma ya ufufuko wa kwanza na mbele ya ufufuko wa pili. Ufufuko wa kwanza ni wa watu wale waliookolewa kwa sababu ya kuamini Kristo. Ufufuko wa pili ndio wa watu wasioamini bila imani.

[5] (6:31) Mana ilikuwa chakula kidogo kiviringo Mungu alicholetea watu wake kwa njia ya ajabu jangwani. Iliwapasa kuokota mana kila asubui toka udongo kwa siku sita ya kwanza ya kila juma.

[6] (6:59) Sunagogi ndipo pahali pa kusanyiko pa Wayuda. Si sawasawa na hekalu kwa Yerusalema lililokuwa pahali pa pekee walipoweza kutoa sadaka za nyama.

[7] (7:1) Vizuri tufahamu ya kwamba maana ya neno hili "Myuda" kwa Kiyunani inaweza kuwa *Myuda* (asiye Mgalilaya); (2) Myuda ye yote, hata yule anayeamini Kristo; (3) au adui wa ukristo, zaidi kiongozi kwa maneno ya dini. Yoane alitumika na neno hili zaidi na maana hii ya adui, hata kama yeye mwenyewe alikuwa Myuda wa namna ya pili.

[8] (8:11) 7:53 – 8:11 hayaonyekani ndani ya miigo mizee zaidi ya Yoane, lakini yanaonekana ndani ya miigo kupita 900 (ndiyo mingi zaidi). Watu wengine wanafikiri mashairi haya si sehemu ya Maandiko Matakatifu. Sisi tunaamini kwamba ni taratibu kuyahesabu kama sehemu ya Maandiko Matakatifu. Yanapatana kwa maneno yote na yale yanayofundishwa ndani ya Biblia nzima. Augustine aliandika kwamba watu wengine walifikili haifai kuhesabu mashairi haya kuwa Neno la Mungu kusudi

yasiwape watu ruhusa kutenda zambi.

[9] (13:13,14) Kwa inchi za mangaribi watu walinawa miguu ya watu mara nyingine, lakini huu ulikuwa mfano mmoja tu wa utumishi mnyenyekevu.

[10] (14:20) Mifano mingine ni ndege katika hewa, na hewa ikiwa ndani ya ndege, na samaki ikiwa ndani ya maji, na maji ndani ya samaki.

[11] (17:26) Rainsford, *Our Lord Prays,* p. 173.

## BIBLIOGRAPHIE

Godet, F.L. *Commentary on the Gospel of John,* Grand Rapids: Zondervan Publishing House, (1969 (Reprint of 1893 ed., 2 vols. in one).

Hole, F. B. *The Gospel of John Briefly Expounded.* London: The Central Bible Truth Depot, n.d.

Ironside, H.A. *Addresses on the Gospel of John.* New York: Loizeaux Brothers, 1956.

Jones, J. Cynddylan. *Studies in the Gospel according to St. John.* Toronto: William Briggs, 1885.

Kelly, William. *An Exposition of the Gospel of John.* London: C.A. Hammond Trust Bible Depot, 1966.

Lenski, R. C. H. *The Interpretation of St. John's Gospel.* Minneapolis: Augsburg, 1942.

Macauley, J. C. *Obedience Unto Death: Devotional Studies in St. John's Gospel.* Grand Rapids: Wm. M. Eerdmans Publishing Co., 1942.

Pink, Arthur W. *Exposition of the Gospel of John. Vol. III,* Swengel, Pennsylvania: Bible Truth Depot, 1945.

Rainsford, Marcus. *Our Lord Prays for His Own.* Chicago: Moody Press, 1955.

Ryle, J. C. *Expository Thoughts on the Gospels: St. John.* London: James, Clarke and Co., Ltd., 1957.

Tasker, R. V. G. *The Gospel According to St. John.* Grand Rapids: Wm. B. Eerdmans Publishing Company, 1968.

Tenney, Merrill C. *JOHN: The Gospel of Belief.* Grand Rapids: Wm. B. Eerdmans Publishing Company, 1948.

Thomas, W. H. Griffith. *The Apostle John: Studies in His Life and Writings.* Grand Rapids: Wm. B. Eerdmans Publishing Company, 1968.

Van Ryn, A. *Meditations in John.* Chicago: Moody Press, 1949.

Vine, W. E. *John, His Record of Christ.* London: Oliphants, 1957.

Westcott, B. F. *The Gospel According to St. John.* Grand Rapids: Wm. B. Eerdmans Publishing Co., 1954.

# MATENDO YA MITUME

## UTANGULIZI

*"Kristo anaonekana zaidi, kwa njia ya kanisa,*
*na kwa uwezo wa Roho Mtakatifu."*

— W. Graham Scroggie

### I. Nafasi ya peke yake katika Kanuni

Kitabu cha Matendo ni kitabu cha pekee cha historia ya kanisa kilichoandikwa kwa *maongozi ya Mungu.* Ni kitabu cha *kwanza* cha historia ya kanisa vilevile kinachopasha habari za mwanzo wake. Ni msingi wa vitabu vingine vyote vilivyoandikwa nyuma na vilivyoongeza maneno machache. Tunahitaji kitabu hiki kabisa kutuongoza toka habari za maisha ya Bwana wetu zinazoandikwa ndani ya vitabu vya Habari Njema, na kutufikisha kwa Barua za Agano Jipya. Tungeuliza kama barua hizi ziliandikwa kwa makusanyiko gani na kama yalianza namna gani. Kitabu cha Matendo kinajibu maulizo haya na maulizo mengi mengine. Ni kiungo toka maisha ya Kristo na namna inavyotupasa kuishi kama yeye, namna tunayojifunza ndani ya Barua, na vilevile ni kiungo toka dini ya Wayuda na Ukristo, toka Sheria na Neema.

### II. Mwandishi

Karibu watu wote wanakubali kwamba mwandishi wa Habari Njema ya Luka ni mwandishi wa kitabu cha Matendo vilevile (ona mwanzo wa mafundisho juu ya Luka).

Maandiko ya waandishi wengi wa kwanza yanahakikisha kwamba Luka aliandika Matendo. Ni vivyo hivyo na waandishi wa historia ambao waliwafuata.

Maandiko yenyewe yanahakikisha kwamba yaliandikwa na Luka. Alianza kitabu chake akitaja kitabu kingine alichoandika mbele kwa mtu mmoja, jina lake Teofilo. Ndani ya Luka 1:1-4 mwandishi alitaja Teofilo vilevile. Namna ya kuandika kwake, na huruma, na maneno madogo mengi mengine yanaonyesha kwamba mwandishi mmoja aliandika vitabu hivi viwili.

Maandiko ya kitabu hiki yanaonyesha kwamba mwandishi wake alisafiri pamoja na Paulo. Ona 16:10-17; 20:5–21:18; 27:1–28:16, pahali mwandishi alipoandika kama mtu aliye palepale yeye mwenyewe.

Mwandishi wa mashairi haya alitaja majina ya watu wengine waliosafiri pamoja na Paulo vilevile kwa wakati ule, na majina ya watu wengine *wasiokuwa* pamoja naye. Tukiondosha majina haya yote toka mashairi haya, mtu mmoja tu alibaki pamoja na Paulo, ndiye Luka.

### III. Tarehe

Ni lazima kujaribu kufahamu tarehe ya kuandikwa kwa kitabu hiki cha kwanza cha historia ya kanisa. Watu wana mawazo mbalimbali juu ya neno hili.

1. Wengine wanafikiri kiliandikwa kwa muda wa kupita miaka mia moja A.D., lakini neno hili haliwezekani kwani Luka asingaliishi kupita miaka 80 au 85 A.D.

2. Watu wengi wanafikiri Luka na Matendo viliandikwa kwa muda wa miaka 70-80 A.D. Tarehe hii ingempa Luka njia kusaidiwa na maandiko ya Marko (karibu miaka 65 A.D.

3. Elezo zuri lingine ni ya kama Luka alimaliza kuandika Matendo muda mfupi nyuma ya habari za mwisho zinazoandikwa ndani ya kitabu hiki, ndizo mara ya kwanza Paulo aliyofungwa kwa Roma.

Labda Luka alikusudi kuandika kitabu cha tatu (lakini ni kama neno hili halikuwa mapenzi ya Mungu), hivi hakutaja maneno mabaya sana yaliyopata Wakristo kwa miaka wa 63 kufika 70 A.D. Ndani ya muda ule mfalme Nero alitesa Wakristo na ukali sana kwa Italia nyuma ya kuteketezwa kwa Roma (mwaka 64), vita ya Wayuda na Waroma (66-70), na neno lililokuwa baya zaidi kwa Wayuda na Wakristo, ndilo maangamizo ya Yerusalema. Habari hizi zote hazikutajwa ndani ya Matendo, hivi ni kama Luka aliandika Matendo kwa wakati Paulo alipokuwa gerezani katika Roma, karibu 62 au 63 A.D.

## IV. Msingi na Jambo Kubwa

Kitabu cha Matendo ya Mitume kinajaa na habari zilizotokea. Tunaona Roho Mtakatifu akianza kanisa, akiwezesha kanisa, na akilieneza. Tunasoma juu ya Roho Mtakatifu mwenye enzi akitumika na watu zaifu kushinda mazuizo makubwa sana na kufanya kazi za ajabu kabisa.

Matendo kinaendelea na habari tulizosoma kwa mwisho wa vitabu vya Habari Njema, na kupasha habari za miaka ya masukosuko ya kwanza ya kanisa. Ulikuwa muda wakati kanisa lilipoachana na dini ya Wayuda, na lilipoanza kuonekana kama ushirika mpya kabisa wa Wayuda na watu wa Mataifa walio moja ndani ya Kristo.

Wakati tunaposoma kitabu hiki, tunashiriki ndani ya furaha na uchangamfu rohoni wakati tunapoona Mungu akitumika. Pamoja na ile tunaona vilevile mazuizo ya zambi na Shetani.

Sura 12 za kwanza ni zaidi juu ya Petro akihubiri na uhodari kwa taifa la Israeli. Kuanza na sura 13 Mtume Paulo alianza kuonekana kupita na kupita kama mtume aliyeongozwa na Roho Mtakatifu, mwenye bidii, akitumika bila kuchoka kwa ajili ya Mataifa.

Matendo yanapasha habari za karibu miaka 33. J.B. Phillips alionyesha kwamba ndani ya muda huu mfupi watu wachache wasiojulikana waligusa dunia kwa njia ya ushuhuda wao, ili kusukuma hata adui zao kusema juu yao na hasira kali ya kwamba watu hawa "walipindua dunia!" (17:6)

## HABARI YALIYOMO

1. KANISA KATIKA YERUSALEMA (SURA 1–7)
   A. AHADI YA BWANA MFUFULIWA KUTUMA ROHO MTAKATIFU (1:1-5)
   B. AMRI YA BWANA KWA MITUME MBELE YA KUPANDA MBINGUNI (1:6-11)
   C. WANAFUNZI WAKIOMBA WANANGOJA KATIKA YERUSALEMA (1:12-26)
   D. SIKU YA PENTEKOTE NA KUZALIWA WA KANISA (2:1-47)
   E. KUPONYESHWA KWA KIWETE, NA AGIZO LA PETRO KWA ISRAELI (3:1-26)
   F. MATESO NA KUONGEZEKA KWA KANISA (4:1 – 7:60)

2. KANISA KATIKA YUDEA NA SAMARIA (8:1 – 9:31)
   - A. UTUMISHI WA FILIPO KWA SAMARIA (8:1-25)
   - B. FILIPO NA TOWASHI YA ETIOPIA (8:26-40)
   - C. WOKOVU WA SAULO WA TARSO (9:1-31)

3. KANISA KUFIKIA MWISHO WA DUNIA (9:32 – 28:31)
   - A. PETRO ANAHUBIRI HABARI NJEMA KWA MATAIFA (9:32 – 11:18)
   - B. MWANZO WA KANISA KWA ANTIOKIA (11:19-30)
   - C. HERODE ALITESA KANISA, AKAKUFA (12:1-23)
   - D. SAFARI YA KWANZA YA PAULO KUHUBIRI: GALATIA (12:24 – 14:28)
   - E. BARAZA KWA YERUSALEMA (15:1-35)
   - F. SAFARI YA PILI YA PAULO KUHUBIRI: ASIA NDOGO NA YUNANI (15:36 –18:22)
   - G. SAFARI YA TATU YA PAULO KUHUBIRI: ASIA NDOGO NA YUNANI (18:23 – 21:26)
   - H. PAULO ANAFUNGWA NA KUHUKUMIWA (21:27 – 26:32)
   - I. SAFARI YA PAULO KWENDA ROMA NA KUVUNJIKA KWA MERIKEBU (27:1 – 28:16)
   - J. PAULO ALIPEWA RUHUSA KUKAA KWAKE MWENYEWE NA ANASHUHUDIA WAYUDA KATIKA ROMA (28:17-31)

# Maelezo

## 1. KANISA KATIKA YERUSALEMA (Sura 1-7)

### A. Ahadi ya Bwana Mfufuliwa kutuma Roho Mtakatifu (1:1-5)

Luka, mganga mpendwa, alianza kitabu hiki na kukumbusha **Teofilo** habari ambazo alimwandikia mbele – ndizo kitabu kinachoitwa sasa Habari Njema ya Luka (ona Lk.1:1-4). Ndani ya mashairi ya mwisho ya Habari Njema hii, alikuwa amemwambia Teofilo kwamba mara moja mbele ya kupanda mbinguni, Bwana Yesu alikuwa ameahidi wanafunzi wake kwamba watabatizwa na Roho Mtakatifu (Lk. 24:48-53).

Sasa Luka aliendelea na habari hizi, akianza na kusema tena juu ya ahadi hii ya furaha kubwa. Ilikuwa vizuri kwa yeye kufanya hivi, kwa sababu ndani ya ahadi hii zilifichwa mbegu za habari zote za kushinda kwa roho tunazoona ndani ya kitabu cha Matendo. Luka alisema kwamba ndani ya Habari Njema yake aliandika mambo yote **Yesu** aliyo*anza* **kufanya na kufundisha.** Ndani ya kitabu cha Matendo anaendelea na habari hizi na kupasha maneno Yesu aliyo*endelea* kufanya na kufundisha kwa njia ya Roho Mtakatifu nyuma ya kupanda kwake mbinguni.

Ona ya kwamba utumishi wa Bwana ulikuwa na sehemu mbili: *kufanya* na *kufundisha.* Bwana Yesu mwenyewe alikuwa mfano mkamilifu wa neno hili. Alifanya yeye mwenyewe maneno aliyohubiri.

**1:2** Tunafikiri kwamba Teofilo alikumbuka kwamba kitabu cha mbele cha Luka kilikwisha na habari za kupanda mbinguni kwa Mwokozi. Hapa katika Matendo Luka aliandika juu yake **akichukuliwa juu.** Teofilo angekumbuka vilevile mafundisho ya mwisho ya Bwana kwa **mitume** kumi na mmoja mbele ya kuwaondokea.

**1:3** Kwa muda wa **siku makumi ine** nyuma ya ufufuko wake na mbele ya kupanda juu, Bwana alikuwa ameonekana kwa wanafunzi wake, akionyesha **wazi kabisa** kwamba alikuwa

amefufuka kweli (ona Yoane 20:19, 26; 21:1,14).

Kwa muda huu alikuwa amesemezana nao juu ya habari za **ufalme wa Mungu.** Hakusema zaidi juu ya falme za dunia hii, lakini ufalme pahali Mungu anapoheshimiwa kama Mfalme.

**Ufalme** si kanisa. Bwana Yesu alijionyesha kwa taifa la Israeli kama Mfalme, lakini walimkataa (Mt. 23:37). Hivi ufalme wake hapa duniani hautasimamishwa kufika wakati taifa la Israeli linapotubu na kumpokea kama Masiya (Mdo. 3:19-21).

Kwa wakati wa sasa, Mfalme si hapa duniani. Lakini ana ufalme duniani usioonekana kwa macho (Kol. 1:13). Ndani ya ufalme huu ni watu wote ambao wanamheshimu kama Mfalme wao (Mt. 25:1-12). Wengine wa watu wale wana*onekana* tu kama wenye kumheshimu (Mt. 13:1-52). Wengine ni wale waliozaliwa tena kweli rohoni (Yn. 3:3,5). Mifano ndani ya Matayo 13 inaonyesha hali ya **ufalme** kwa wakati wa sasa.

Kanisa ni neno jipya kabisa. Hakuna unabii juu yake ndani ya Agano la Kale (Efe. 3:5). Ni waamini wote tangu siku ya Pentekote kufika kupelekwa kwao mbinguni. Kama Bibi-Arusi ya Kristo, kanisa litatawala pamoja naye kwa wakati wa utawala wake wa miaka elfu moja na kushiriki utukufu wake kwa milele. Kristo atarudi kama Mfalme kwa mwisho wa Mateso Makubwa, ataharibu adui zake na kusimamisha utawala wake wa haki juu ya dunia nzima (Zab. 72:8).

Hata kama atatawala toka Yerusalema kwa miaka elfu moja tu (Ufu. 20:4), **ufalme** wake ni ufalme wa milele kwa sababu mwishoni adui zote za Mungu watakwisha kuharibiwa, naye atatawala kwa milele mbinguni bila ushindani wala mazuizo (2 Pet. 1:11).

**1:4** Halafu Luka alipasha juu ya Bwana akikutana na wanafunzi wake wakati **walipokusanyika** ndani ya chumba katika **Yerusalema**. Mkombozi mfufuliwa **aliwaagiza** kubaki katika **Yerusalema**. Labda walifazaika kwa sababu gani iliwapasa kubaki katika Yerusalema? Kwa mawazo yao ulikuwa mji wa machukio, jeuri na mateso!

Ndiyo, **ahadi ya Baba** itatimizwa katika **Yerusalema.** Roho Mtakatifu atafika kwa mji ule ule pahali Mwokozi aliposulibishwa. Kwa Roho Mtakatifu kuwa pale pale kutakuwa ushuhuda kwamba watu walikataa Mwana wa Mungu. "Roho atahakikisha dunia maneno ya zambi, na maneno ya haki, na maneno ya hukumu" (Yn. 16:8) – na neno hili litatokea kwanza kwa **Yerusalema.** Wanafunzi watapokea Roho Mtakatifu katika mji ule ule pahali wao wenyewe walipoacha Bwana na kukimbia kujiponyesha wenyewe. Watapatishwa nguvu na uhodari kwa pahali pa uzaifu na woga ambazo walikuwa nazo mbele.

Hii haikuwa mara ya kwanza Mwokozi aliyosema nao juu ya **Ahadi ya Baba**. Alisema juu yake tena na tena, na zaidi wakati alipotoa hotuba yake katika chumba cha juu saa alipokula pamoja nao mara ya mwisho. Alisema nao juu ya kuja kwa Msaidizi (ona Lk. 24:49; Yn. 14:16, 26; 15:26; 16:7,13).

**1:5** Sasa wakati alipokutana nao mara ya mwisho alitoa ahadi hii tena. Wengine katikati yao, labda wao wote, walikuwa **wamebatizwa na maji na Yoane** (Mbatizaji**).** Lakini ubatizo wa Yoane ulionekana inje, kwa mwili. Lakini nyuma ya siku si nyingi[1] **watabatizwa katika Roho Mtakatifu,** na ubatizo huu utakuwa ubatizo wa roho na hautaonekana kwa macho. Ubatizo wa kwanza ulionyesha kwamba walikuwa sehemu ya taifa la Israeli waliotubu. Ubatizo wa pili utawaingiza ndani ya kanisa, Mwili wa Kristo, na utawapatisha uwezo kutumikia Mungu.

Yesu aliahidi kwamba **watabatizwa**

**katika Roho Mtakatifu nyuma ya siku si nyingi,** lakini hakusema neno juu ya ubatizo katika moto mara hii (ona Mt. 3:11-12; Lk. 3:16-17). Ubatizo ule ni ubatizo wa hukumu kwa wasioamini tu na utatokea kwa wakati wa nyuma.

**B. Amri ya Bwana kwa mitume mbele ya kupanda kwake mbinguni (1:6-11)**

**1:6** Labda maneno haya yalitokea kwa mlima wa Zeituni kwa upande wa Betania. Bwana Yesu alirudi mbinguni toka pahali pale (Lk. 24:50-51).

Wanafunzi walikuwa wamefikiri juu ya kuja kwa Roho Mtakatifu. Walikumbuka kwamba nabii Yoeli alisema juu ya kumwangwa kwa Roho Mtakatifu saa ya utawala wa utukufu wa Masiya (Yoeli 2:28). Hivi walifikiri kwamba Bwana atasimamisha **ufalme** wake nyuma kidogo, kwani alikuwa amesema kwamba watapewa Roho Mtakatifu "nyuma ya siku si nyingi." Ulizo lao lilionyesha kwamba walikaa kufikiri Kristo atasimamisha **ufalme** wake duniani mara moja.

**1:7** Bwana *hakuwahamakia* juu ya mawazo haya. Aliwaambia tu kwamba hawawezi **kujua** wakati gani ufalme wake utakapokuja. Baba alikuwa amechagua siku yenyewe katika **mamlaka** yake mwenyewe, lakini hakuchagua kuifunua.

Maneno haya **nyakati au majira** yanatumiwa ndani ya Biblia kusema juu ya matukio mengine yaliyotabiriwa na Mungu juu ya taifa la Israeli lakini yasiyofanyikana kwanza. Wanafunzi wakiwa Wayuda, walifahamu kwamba maneno haya yalisema hapa juu ya muda wa siku zilizoitangulia, pamoja na kusimamishwa kwa utawala wa miaka elfu moja wa Kristo duniani.

**1:8** Halafu Bwana aliwaongoza kufikiri juu ya maneno yaliyokuwa karibu kutokea – namna ya utumishi wao na pahali watakapomtumikia. Watakuwa **washuhuda, katika Yerusalema, na katika Yudea yote, na Samaria, hata mpaka wa dunia.**

Lakini kwanza inapasa **wapokee nguvu – nguvu ya Roho Mtakatifu. Nguvu** hii inahitajiwa kabisa kwa ushuhuda wao. Inawezekana kwa mtu kuwa mwenye akili kabisa, na kujifunza sana, lakini bila **nguvu** hii ya roho ushuhuda wake ni bure. Lakini inawezekana kwa mtu kuwa mjinga, mwenye sura isiyopendeza, au asiyejifunza, lakini akijazwa na **uwezo wa Roho Mtakatifu**, kuwa na ushuhuda wa kuwaka unaokokota watu karibu na Mungu. Wanafunzi wenye woga walihitaji **nguvu** kwa ushuhuda wao, na uhodari rohoni kuhubiri Habari Njema. Watapokea **nguvu** wakati **Roho Mtakatifu** atakapokuja **juu** yao.

Mungu kwa neema yake aliwaongoza kuanza ushuhuda wao katika **Yerusalema.** Mji ule ule pahali Bwana wetu aliposulibishwa ulikuwa mji wa kwanza ulioitwa kutubu na kumwamini.

Nyuma yake **Yudea,** kwa upande wa kusini wa Palestina, sehemu ya inchi iliyokuwa na Wayuda wengi, na mji wake mkubwa, ndio Yerusalema.

Halafu **Samaria,** pahali pa katikati ya Palestina. Zaidi ya watu wa upande ule hawakuwa Wayuda safi lakini walikuwa wameoa watu wa Mataifa, na kwa sababu ya neno hili Wayuda waliwachukia na hawakuwa na ushirika nao.

Kisha **mpaka wa dunia** ambayo watu walijua kwa wakati ule – inchi za Mataifa wasiobarikiwa na maneno ya dini kufika wakati ule. Maneno haya yanatuonyeshea njia kugawa kitabu cha Matendo:

1. *Ushuhuda* katika **Yerusalema** (sura 1 – 7).
2. *Ushuhuda* katika **Yudea** na **Samaria** (8:1 – 9:31)

3. *Ushuhuda* hata **mpaka wa dunia** (9:32 – 28:31)

**1:9** Mara moja nyuma ya kuagiza wanafunzi wake, Mwokozi **alinyanyuliwa** kwenda mbinguni, **wingu likampokea toka macho yao.** Likuwa tukio la ajabu sana, lakini maneno machache tu yaliandikwa juu yake. Neno hili linahakikisha tena kwamba kuandika kwa maandiko ya Biblia yaliongozwa na Mungu. Watu wangalisema maneno mengi zaidi juu yake.

**1:10** Halafu bila kuonyesha kushangaa, Luka alipasha habari za **watu wawili … wakivaa nguo nyeupe** wakitokea. Bila shaka walikuwa malaika walioonekana duniani kwa mfano wa watu. Labda walikuwa malaika waliotokea kwa kaburi nyuma ya ufufuko (Lk. 24:4).

**1:11** Malaika waliita wanafunzi **watu wa Galilaya** kwanza**.** Ni kama wanafunzi wote ila Yuda Iskariota walikuwa watu toka upande wa mangaribi wa bahari ya Galilaya.

Waliwauliza kwa sababu gani **walikaa kutazama mbinguni**? Kwa sababu ya huzuni, au na kuabudu, au kwa sababu ya kushangaa? Labda yalikuwa machanganyiko ya maneno yale matatu, lakini zaidi kwa sababu ya huzuni. Hivi malaika waliwafariji na kusema kwamba Kristo aliyepanda kwenda mbinguni atakuja tena.

Hii ndiyo ahadi wazi sana kwamba Bwana atakuja tena mara ya pili kusimamisha ufalme wake duniani. Ahadi hii si juu ya kupeleka kanisa lake mbinguni, lakini juu ya utawala wake duniani.

1. Alipanda toka mlima wa Zeituni (sh.12).
   Atarudi tena kwa mlima wa Zeituni (Zek. 14:4)
2. Alipanda katika mwili.
   Atarudi vivyo hivyo (Mal. 3:1).
3. Alipanda mbele ya macho ya watu.
   Atarudi vivyo hivyo (Mt. 24:30).
4. Alipokewa katika wingu (sh. 9).
   Atakuja katika mawingu ya mbingu (Mt. 24:30).
5. Alipanda na utukufu.
   Atarudi na uwezo na utukufu mkubwa (Mt. 24:30).

### C. Wanafunzi walingoja katika Yerusalema pamoja na maombi (1:12-26)

**1:12** Ndani ya Luka 24:52 wanafunzi walirudia Yerusalema na *furaha kubwa*. Mapendo makubwa ya Mungu yaliwaka mioyoni mwao na kufanyiza nyuso zao kungaa.

Ilikuwa safari ndogo, kama kilomètre moja tu **toka mlima wa Zeituni** kushuka kwa bonde la Kiduroni, na kupanda tena kufikia mji. Huu ulikuwa urefu wa safari uliokubaliwa kwa Myuda kufanya siku ya **sabato** kwa wakati wa **Agano Jipya.**

**1:13** Nyuma ya kuingia mji **walipanda chumbani mwa juu pahali walipokaa.**

Hii ilikuwa mara ya ine na ya mwisho Roho ya Mungu alitaja majina ya mitume (Mt. 10:2-4; Mk. 3:16-19; Lk. 6:14-16). Lakini jina la mtu mmoja lilikosa. Yuda Iskariota aliyetoa Bwana kwa adui zake alikuwa ameangamizwa.

**1:14** Wanafunzi hawa walikutana **kwa moyo mmoja**. Tunakuta maneno haya matatu mara kumi na moja ndani ya kitabu cha Matendo, nayo ni kama ufunguo mmoja wa siri ya baraka. Wakati ndugu wanapokaa na roho ya umoja, Mungu anaamuru baraka – hata uzima kwa milele (Zaburi 133).

Ufunguo wa pili ndio hii: **walishinda katika kuomba.** Hata sasa vilevile Mungu anatumika wakati watu wanapoomba. Lakini sisi watu tungependa kufanya neno lo lote kupita kuomba. Wakati **tunapoomba** na bidii na imani, bila haraka, kwa moyo mmoja,

tutaona uwezo wa Roho ya Mungu.

Ni wazi kabisa kwamba roho ya *umoja na maombi ndiyo maneno yaliyotangulia Pentekote.*

**Wanawake** wengine walikutana pamoja na wanafunzi. Hatuoni majina yao lakini tunafikiri ndio wale waliofuata Yesu. **Maria mama ya Yesu, na … ndugu zake** walikuwa pale vilevile. Tuone maneno mengine hapa:

1. Hii ni mara ya mwisho tunayoona jina la **Maria** ndani ya Agano Jipya. Wanafunzi hawakuomba *kwa* Maria, lakini **pamoja** naye. Alikuwa akingoja pamoja nao kupokea zawadi ya Roho Mtakatifu.
2. **Maria** anaitwa **mama ya Yesu,** lakini si "mama ya Mungu." Yesu ni jina la Bwana wetu kama mtu. Kama mtu alizaliwa na **Maria,** na hivi ni taratibu kwa **Maria** kuitwa mama ya Yesu. Hakuitwa "mama ya Mungu" hata mara moja ndani ya Biblia. Yesu Kristo alikuwa kweli Mungu, lakini kusema juu ya Mungu akiwa na mama ni mafundisho mapumbavu bila maana. Kama Mungu, Kristo alikuwa tangu milele.
3. **Ndugu za Yesu** walitajwa hapa *nyuma* ya jina la Maria, na neno hili linatuleta kufikiri kwamba walikuwa wana wa Maria na ndugu wenye mama mmoja na Yesu. Watu wengine wanafundisha kwamba **Maria** alikuwa bikira daima na hakuzaa watoto wengine nyuma ya kuzaa Yesu, lakini mashairi mengine ndani ya Biblia yanakana mafundisho haya. (Kwa mfano, soma Mt. 12:46; Mk. 6:3; Yn. 7:3, 5; 1 Kor. 9:5; Gal. 1:19. Ona Zab. 69:8 vilevile.)

**1:15** Siku moja wakati **karibu wanafunzi mia moja na makumi mbili** walipokusanyika, **Petro** aliongozwa kuwakumbusha mashairi ya Agano la Kale juu ya yule atakayekataa Masiya.

**1:16,17** Kwanza Petro alisema kwamba ilipasa unabii mmoja ulioandikwa na **Daudi juu ya Yuda … kutimizwa.** Lakini mbele ya kutaja **shairi hili** aliwakumbusha kwamba Yuda alikuwa mmoja wa wanafunzi kumi na wawili na alishiriki nao ndani ya utumishi wao kama mitume, lakini hata hivi **alikuwa kiongozi chao waliokamata Yesu**. Ona ya kwamba Petro aliandika na kiasi juu ya tendo hili baya sana. Yuda alichagua yeye mwenyewe kuwa haini, na hivi alitimiza unabii kwamba mmoja atauza Bwana kwa adui zake.

**1:18, 19** Mashairi haya yaliandikwa na Luka lakini si kama sehemu ya hotuba ya Petro. Yanapasha habari za Yuda kufika kufa kwake, na kutayarisha njia kwa kuwekwa kwa mkombozi wake.

Hakuna mabishano kati ya habari za namna ya kufa kwa Yuda kwa Mt. 27:3-10 na zile hapa kwa Matendo. Matayo alisema kwamba nyuma ya kuwapa wakubwa wa makuhani na wazee vile vipande vya feza, Yuda alitoka na kujitundika. Halafu wakubwa wa makuhani walikamata mali ile na kununua pahali pa kuzika wafu.

Hapa katika Matendo, Luka anasema kwamba Yuda **alinunua shamba** na mali yenyewe, **akaanguka kifudifudi … na matumbo yake yote yalitoka.**

Wakati tunaposoma habari za Matayo na zile za Luka pamoja, ni kama wakubwa wa makuhani walitayarisha maneno ya kupata shamba. Lakini ni kama Yuda alilinunua kwa sababu ilikuwa mali yake, nao walifanya kazi ya kulinunua tu. Alijitundika kwa mti katika shamba la kuzika watu, lakini ni kama kamba ilivunjwa na kutupa mwili wake na kuufanyiza **kupasuka**.

Matukio haya yalijulikana **katika Yerusalema** na shamba la mfinyanzi liliitwa **Akeldama, maana yake: Shamba la damu** kwa lugha ya Kiaramaik.

**1:20** Nyuma ya maelezo haya ya Luka, Petro aliendelea na hotuba yake. Kwanza alieleza ya kwamba ndani ya Zab. 69:25 Daudi alisema juu ya mwenye kutoa Yesu: **"Kikao chake kikae tupu, wala mtu asikae ndani yake."**

Halafu alitaja unabii ule uliopaswa kutimizwa sasa: **"Mtu mwingine atwae usimamizi wake"** (Zab.109:8). Kwa mafikiri ya Petro ilipasa kuchagua mtu mwingine kukomboa Yuda. Ni vizuri kuona hamu ya Petro kutii Neno la Mungu.

**1:21, 22** Maneno mawili yaliyokuwa lazima kwa mtu atakayekomboa Yuda:

1. Sharti awe mtu aliyekuwa **pamoja na wanafunzi** kwa miaka mitatu ya utumishi wa Kristo – tangu wakati **alipobatizwa na Yoane** kufika kupanda kwake mbinguni.
2. Sharti awe **mshuhuda** wa **ufufuko** wa Bwana.

**1:23-26** Walitaja watu wawili waliofaa kwa kazi ile, Yosefu ... aliyepewa jina la Yusto, na **Matia.** Basi, watachagua nani? Mitume waliomba Mungu kuwafunulia mapenzi yake. Halafu **walipiga kura** na **Matia** alichaguliwa kukomboa Yuda aliyekuwa amekwenda **pahali pake**, ndio upotevu wa milele.

Tuna maulizo mawili juu ya habari hizi:

1. Ilikuwa vizuri kwa mitume kutaja **Matia**? Ingaliwapasa kungoja kwa Mungu kutayarisha mtume Paulo kwa kazi ile?

2. Ilikuwa taratibu **kupiga kura** kutambua mapenzi ya Mungu?

Jibu kwa ulizo la kwanza ndilo ya kwamba hakuna neno lililoandikwa kuonyesha kwamba mitume walianguka ndani ya neno hili. Walikuwa wameshinda katika maombi; walijaribu kutii Maandiko, na ni kama walikuwa na nia moja wakati walipochagua mtu kukomboa Yuda. Na vilevile utumishi wa Paulo ulikuwa namna nyingine na ule wa mitume, na hakuna neno lililoonyesha kwamba Mungu alikusudi kwa Paulo kukomboa Yuda. Wakati Yesu alipokuwa duniani aliamuru mitume kuhubiri kwa Israeli, lakini Paulo alipewa utumishi wake na Kristo toka utukufu na alitumwa kwa Mataifa.

Juu ya kupiga kura – neno hili lilikubaliwa katika Agano la Kale kusaidia watu kutambua mapenzi ya Mungu juu ya neno fulani: "Kura inatupwa katika mikunjo ya nguo, lakini hukumu zake zote zinatoka kwa BWANA" (Mez. 16:33).

Ni kama Bwana alikubali kwa mitume kuchagua Matia kwa njia ya kupiga kura, kwa sababu tangu wakati ule mitume waliitwa *"wale kumi na wawili"* (ona Mdo. 6:2).

## MAFUNDISHO JUU YA MAOMBI NDANI YA KITABU CHA MATENDO

Kitabu cha Matendo kinatufundisha juu ya kushinda kwa njia ya maombi. Hata ndani ya sura 1 tunaona wanafunzi wakiomba mara mbili. Nyuma ya kupanda kwa Bwana mbinguni, jibu la maombi ya wanafunzi toka chumba cha juu lilikuwa Pentekote. Wakati walipoomba Mungu kuwaongoza kama ilipasa nani kukomboa Yuda, Mungu alijibu na kuchagua Matia kwa njia ya kupiga kura. Maneno namna hii yalitokea tena na tena ndani ya kitabu hiki.

Wale waliookolewa siku ya Pentekote walidumu katika maombi (Mdo. 2:42). Mashairi yanayofuata (43-47) yanaonyesha ya kwamba walifanya hivi na roho nzuri ya ushirika.

Nyuma ya kufunguliwa kwa Petro na Yoane, waamini waliomba kupewa uhodari (Mdo. 4:29). Nyuma ya maombi yao, pahali walipokuwa palitikiswa, wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakasema Neno la Mungu pasipo woga (Mdo. 4:31).

Mitume kumi na wawili walifikiri

ingekuwa vizuri kwa wanaume saba kuchaguliwa kuangalia maneno ya mali ili wao wenyewe wawe na saa kupita kwa maombi na kufundisha Neno la Mungu (Mdo. 6:3, 4). Halafu waliomba, wakachagua watu saba na kuwawekea mikono (Mdo. 6:6). Habari zinazofuata zinapasha habari za kufurahisha sana za kushinda kwa Habari Njema (Mdo. 6:7, 8).

Stefano aliomba wakati watu walipokuwa karibu kumwua (Mdo. 7:60). Ndani ya sura 9 tunasoma habari za jibu moja kwa ombi hili – wokovu wa mtu mmoja aliyekuwa akitazama, ndiye Saulo wa Tarso.

Petro na Yoane waliombea Wasamaria walioamini, basi wao walipokea Roho Mtakatifu (Mdo. 8:15-17).

Nyuma ya kuokolewa kwake, Saulo wa Tarso aliomba nyumbani mwa Yuda; Mungu alijibu ombi hili kwa njia ya kutuma Anania karibu naye (Mdo. 9:11-17).

Petro aliomba kwa Yopa, na Dorika alifufuliwa (Mdo. 9:40), na halafu watu wengi waliamini Bwana (Mdo. 9:42).

Kornelio, akida mtaifa la askari mia, aliomba (Mdo. 10:2); maombi yake yalifika juu kama ukumbusho mbele ya Mungu (Mdo. 10:4). Malaika ya Mungu alionekana kwake ndani ya ono na kumwagiza kutuma kuita mtu mmoja jina lake Petro (Matendo 10:5). Kesho yake Petro alikuwa akiomba (Mdo. 10:9). Kwa jibu lake alikuwa na ono toka mbingu ambalo lilimtayarisha kufungua milango ya ufalme kwa Kornelio na watu wengine wa Mataifa (Mdo. 10:10-48).

Wakati Petro alipokuwa gerezani Wakristo walimwombea pasipo kuchoka (Mdo. 12:5). Mungu alijibu maombi yao na kumwondosha gerezani kwa njia ya ajabu – hata waombaji walishangaa sana (Mdo. 12:6-17).

Manabii na walimu kwa Antiokia walifunga chakula na waliomba (Mdo. 13:3). Huu ulikuwa mwanzo wa safari ya kwanza ya kuhubiri kwa Paulo na Barnaba. Maombi haya yalifanya kazi kubwa sana, yakagusa hata miisho ya dunia, na hata sisi, kwa njia ya Paulo na Barnaba, watumishi wa Mungu.

Wakati Paulo na Barnaba walipofikia Listra na Ikonio na Antiokia tena, waliombea wale walioamini kwa safari yao ya mbele (14:23). Timoteo alikuwa mmoja wao. Labda kwenda kwa Timoteo pamoja nao kwa safari yao ya pili kulikuwa jibu la maombi ya Paulo na Sila?

Katika gereza kwa Filipi kwa saa sita ya usiku Mungu alijibu maombi ya Paulo na Sila kwa njia ya tetemeko la inchi na kwa njia ya kuokoa mlinzi wa gereza na jamaa yake (Mdo. 16:25-34).

Paulo aliomba pamoja na wazee kwa Mileto (Mdo. 20:36); maombi haya yalifanyiza mapendo yao makubwa kwa Paulo kuonekana wazi, kwa sababu hawatamwona tena hapa duniani.

Wakristo kwa Tiro waliomba pamoja na Paulo kwa pwani (Mdo. 21:5), na bila shaka walikaa kumwombea kwa safari yake nzima kufika Roma na mauti yake.

Mbele ya kuvunjwa kwa merikebu, Paulo aliomba na sauti mbele ya watu wote waliokuwa pamoja nao, na alishukuru Mungu kwa vyakula. Neno hili lilifurahisha wasafiri wenzake sana (Mdo. 27:35,36). Kwa kisanga cha Melita Paulo aliombea baba mgonjwa wa liwali. Mgonjwa huyu aliponyeshwa kwa njia ya ajabu (Mdo. 28:8).

Hivi tunaona ya kwamba waamini kwa wakati wa mwanzo wa kanisa walikuwa watu wa maombi. Na wakati Wakristo walipoomba Mungu alifanya kazi kubwa! ❖

### D. Siku ya Pentekote na kuzaliwa kwa Kanisa (2:1-47)

**2:1** Siku kubwa ya **Pentekote** ilikuwa mfano wa kumwangwa kwa Roho Mtakatifu, na ilikuwa siku makumi tano

nyuma ya siku kubwa ya Malimbuko, iliyokuwa mfano wa ufufuko wa Kristo. Siku hii ya **Pentekote** wanafunzi **walikuwa wote na moyo mmoja kwa pahali pamoja**. Labda walisemezana juu ya mashairi katika Agano la Kale juu ya Karamu ya Pentekote (kwa mfano ona Walawi 23:15,16). Au labda walikuwa wakiimba Zaburi 133, "Tazama, ni wema na ya kupendeza sana kwa ndugu kukaa pamoja kwa umoja!"

**2:2** Saa Roho Mtakatifu alipokuja, watu walisikia neno, waliona ono, na kupatwa na ajabu. **Uvumi** waliosikia **ulitoka mbingu** na **kujaza nyumba nzima**, kama **upepo unaovuma na nguvu sana. Upepo** ni mfano mmoja wa Roho Mtakatifu (mifano mingine ni mafuta, moto, na maji), unaosema juu ya matendo yake yenye enzi tusiyoweza kujua mbele.

**2:3** Waliona **ndimi kama za moto, zilizogawanyika na kukaa juu ya kila mwanafunzi.** Hazikuwa ndimi za moto, lakini **ndimi kama za moto**.

Neno hili ni mbali na ubatizo wa moto. Hata kama tukisoma juu ya ubatizo wa Roho na ubatizo wa moto pamoja (Mt. 3:11,12; Lk. 3:16,17), maneno haya yalitokea kwa wakati mbalimbali. Ubatizo wa kwanza ni ubatizo wa baraka, kwa waamini; ubatizo wa pili ni wa hukumu, wa wasioamini. Kwa njia ya ubatizo wa Roho waamini walikaaliwa na Roho na kupewa uwezo, na kanisa lilianzwa. Kwa njia ya ubatizo wa moto, wasioamini wataharibiwa.

Wakati Yoane Mbatizaji alipohubiri kwa fungu la waamini na wasioamini pamoja (ona Mt. 3:6,7), alisema Kristo atawabatiza na Roho Mtakatifu na moto (Mt. 3:11). Wakati aliposema kwa wenye kutubu kweli kweli (Mk.1:5) alisema Kristo atawabatiza na Roho Mtakatifu (Mk. 1:8).

Basi maana ya **ndimi kama za moto zilizogawanyika** kwa Matendo 2:3 ni nini? Bila shaka **ndimi** ni juu ya masemo, na tunafikiri juu ya zawadi ya ajabu ambayo wanafunzi walipokea kwa wakati ule, ndio uwezo wa kusema kwa lugha nyingine. Labda **moto** unasema juu ya Roho Mtakatifu akitoa zawadi hii, na juu ya mahubiri na ushuhuda wa uhodari, bidii, na shangwe ya wenye kujaa Roho Mtakatifu. Ni tunda ndani ya maisha, na ushuhuda wa wenye kujaa Roho Mtakatifu.

**2:4** Ajabu ambalo wanafunzi walipatwa nalo saa ya Pentekote lilikuwa kujazwa **Roho Mtakatifu**, na kuweza kusema **kwa lugha nyingine.**

Kufika saa ile Roho Mtakatifu alikuwa *pamoja* na wanafunzi, lakini kuanza sasa alikaa *ndani* yao (Yn. 14:17). Hivi kuanza na shairi hili namna Roho Mtakatifu alitendea watu iligeuka kabisa. Kwa wakati wa Agano la Kale Roho Mtakatifu alikuja juu ya watu lakini hakuwakalia (Zab. 51:11). Kuanza na siku ya Pentekote Roho Mtakatifu alikaa ndani ya watu daima: alikuja kukaa hata milele (Yn. 14:16).

Siku ya Pentekote Roho Mtakatifu hakukaa tu ndani ya waamini, lakini aliwajaza vilevile. Roho ya Mungu anakaa ndani yetu mara moja wakati tunapookolewa, lakini kwa kujazwa na Roho inatupasa kuweka saa kujifunza Neno la Mungu, kuweka saa kuwaza juu yake na maombi, na kuishi maisha ya kutii Bwana. Kwa sababu hii tunaagizwa, "mujazwe Roho" (Efe. 5:18).

Kuja kwa Roho Mtakatifu siku ya Pentekote kulifunganisha waamini pamoja vilevile kuwa kanisa, Mwili wa Kristo.

Kwa sababu katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa katika mwili mmoja – kama Wayuda au Wayunani – kama tukiwa watumwa au wenye huru – nasi sote tumekunyweshwa katika Roho mmoja (1 Kor. 12:13). Kuanza saa ile waamini Wayuda na waamini Mataifa waligeuka mtu mpya mmoja ndani ya

Kristo Yesu na viungo vya Mwili mmoja (Efe. 2:11-22)

Wanafunzi **waliojazwa na Roho Mtakatifu walianza kusema na lugha nyingine, kama Roho Mtakatifu alivyowapa kusema.** Mashairi yanayofuata yanaonyesha kwamba waliwezeshwa kwa ajabu kusema kwa *lugha nyingine* wasiyojifunza kamwe. Hawakusema maneno ovyo lakini masemo watu wa inchi nyingine waliyoweza kufahamu. Zawadi hii ya lugha ilikuwa moja ya alama na maajabu ambayo Mungu alitumika nayo kushuhudia kweli ya maneno mitume waliyohubiri (Ebr. 2:3, 4). Kwa wakati ule Agano Jipya halijaandikwa bado. Tangu mwisho wa kuandika kwa neno zima la Mungu, hakuna hitaji tena kwa alama hizi za roho (lakini Roho ya Mungu mwenye enzi angeweza kutumika nazo kama akitaka).

Haifai kusema kwamba kusema kwa **lugha** nyingine siku ya Pentekote kunahakikisha kwamba neno hili linatokea kila mara pamoja na zawadi ya Roho. Hivi hatusomi juu ya lugha pamoja na habari za:

1. Kuzaliwa tena kwa watu 3000 (Mdo. 2:41);
2. Kuzaliwa tena kwa watu 5000 (Mdo. 4:4);
3. Wasamaria wakipokea Roho Mtakatifu (Mdo. 8:17).

Tunasoma juu ya zawadi ya **lugha** mara mbili nyingine tu ndani ya Matendo:

1. Wakati watu wa Mataifa walipookolewa nyumbani mwa Kornelio (Mdo. 10:46);

2. na wakati wafuata wa Yoane walipobatizwa mara ya pili kwa Efeso (Mdo. 19:6).

Mbele ya kuacha shairi 4, inatupasa kuonyesha kwamba walimu wa Biblia hawapatani wote juu ya mafundisho ya ubatizo wa Roho Mtakatifu, kama ulitokea mara ngapi, na kama mwisho wake ulikuwa nini.

Ulitokea mara ngapi:

1. Wengine wanafikiri ulitokea mara moja tu, ndiyo siku ya Pentekote. Huu ulikuwa umbo wa Mwili wa Kristo, na waamini wote tangu wakati ule wanashiriki ndani ya umbo ule.
2. Ulitokea kwa sehemu tatu au ine – kwa Pentekote (sura 2); kwa Samaria (sura 8); kwa nyumba ya Kornelio (sura 10); kwa Efeso (sura 19).
3. Unatokea kila mara mtu anapookolewa.

Juu ya kazi yake ndani ya maisha ya watu, wengine wanafikiri ni "kazi ya pili ya neema," inayofanyikana nyuma ya kuokolewa kwa mtu, ambayo inamtakasa kupita, kwa kipimo mbalimbali. Mawazo haya hayapatani na mafundisho ya Maandiko Matakatifu. Kama tulivyoona mbele, ubatizo wa Roho Mtakatifu :

1. Ulifunganisha waamini pamoja kuwa kanisa (1 Kor. 12:13);
2. Uliwapa waamini nguvu (Mdo. 1:8).

**2:5-13 Wayuda wenye haki** toka mataifa yote chini ya mbingu walikuwa wamefikia **Yerusalema** kwa karamu ya Pentekote. Wakati waliposikia habari za maneno yaliyotokea, walikusanyika kwa nyumba pahali mitume walipokaa. Kwa wakati ule, kama sasa vilevile, watu wanavutwa kuona kazi ya Roho Mtakatifu.

Wakati **makutano** walipofikia nyumba, mitume walikuwa wameanza kusema kwa lugha. Wageni hawa walishangaa sana wakati waliposikia wanafunzi hawa toka Galilaya wakisema kwa lugha mbalimbali. Lilikuwa ajabu lililofanywa kwa njia ya wasemaji, si kwa njia ya wasikiaji. Si neno kama wasikiaji walikuwa Wayuda au walishika dini ya Wayuda, kama walitoka kwa upande wa mashariki au mangaribi, toka kaskazini au kusini, kila mtu alisikia kwa **lugha**

**yake mwenyewe habari za matendo makubwa ya Mungu.**

Watu wengi wanafikiri kusudi la zawadi ya lugha kwa Pentekote lilikuwa kutangaza Habari Njema kwa watu wenye lugha mbalimbali pamoja kwa saa moja. Kwa mfano, mwandishi mmoja aliandika kwamba "Mungu alitoa sheria yake kwa lugha moja kwa taifa moja, lakini alitoa habari njema yake kwa lugha zote kwa mataifa yote."

Lakini maandiko hayasemi hivi wazi. Wale waliosema kwa lugha walitangaza **matendo makubwa ya Mungu** (2:11). Lilikuwa alama kwa watu wa Israeli (1 Kor. 14:21,22), na kusudi la kuwashangaza. Lakini Petro alihubiri Habari Njema kwa lugha ambayo zaidi ya wasikiaji, labda wote, waliweza kufahamu.

Wasikiaji wageni walifikiri maneno mbalimbali. Wengine waliweka roho sana juu ya maneno waliyosikia, lakini wengine walishitaki mitume kusema **wamelewa na mvinyo mpya**. Wanafunzi walikuwa wakiongozwa kweli na uwezo usio wao, lakini ulikuwa uwezo wa Roho Mtakatifu, si wa **mvinyo!**

Wasiamini ni mbio kila mara kujaribu kueleza kazi za Mungu kwa njia ya matukio ya dunia. Siku moja wakati sauti ya Mungu iliposikiwa toka mbinguni, wengine walisema ni ngurumo (Yn.12:28,29). Sasa wasiamini walisawanisha furaha zilizoletwa na kufika kwa Roho Mtakatifu na **mvinyo mpya**.

**2:14** Mwanafunzi aliyekuwa amekana Bwana wake na matukano mbele alisimama sasa kusema na makutano. Hakuwa mfuata zaifu na kugeukageuka kama mbele, lakini alikuwa mwenye nguvu kama simba. Alikuwa amegeuzwa na Pentekote. **Petro** alikuwa amejazwa sasa na Roho Mtakatifu.

Kwa Kaisaria Filipi Bwana alikuwa ameahidi kumpa Petro funguo za ufalme wa mbinguni (Mt. 16:19). Hapa ndani ya Matendo 2 tunamwona akitumika na funguo hizi kufungulia Wayuda mlango (sh.14); nyuma, katika sura 10, atafanya vivyo hivyo kwa Mataifa.

**2:15** Kwanza mtume alieleza kwamba maajabu yaliyotokea siku ile hayakuwa matunda ya mvinyo mpya. Ilikuwa saa tatu ya asubui **tu**, si saa kwa watu wengi hivi kulewa. Vilevile Wayuda walioshiriki ndani ya kazi ya sunagogi siku kubwa hawakula wala kunywa mbele ya saa ine asubui, au labda hata mbele ya saa sita, kupatana na saa zabihu ya kila siku ilipotolewa.

**2:16-19** Elezo la kweli lilikuwa kwamba Roho ya Mungu alikuwa amemwangwa, kama **lililosemwa na nabii Yoeli** (Yoeli 2:28).

Lakini maneno yaliyotokea siku ya Pentekote hayakutimiza unabii mzima wa Yoeli. Zaidi ya habari tunazosoma ndani ya mashairi 17-20 hazikufanyikana kwa wakati ule. Lakini maneno yaliyotokea kwa Pentekote yalikuwa kama malimbuko ya maneno yatakayotokea **siku za mwisho, mbele ya siku ya Bwana iliyo kubwa yenye ajabu.** Kama unabii mzima wa Yoeli ungalitimizwa siku ya Pentekote, kwa nini kulikuwa na ahadi katika Matendo 3:19 kwamba taifa la Israeli wakitubu na kumpokea Yule ambaye walimsulibisha, atarudi na kuleta nyakati za ufufuko toka uso wa Bwana?

Mashairi haya toka Yoeli yanaonyesha kwamba mara nyingine shairi la unabii linatimizwa kwa sehemu kwanza, na wakati wa nyuma linatimizwa pia.

Roho Mtakatifu alimwangwa kweli siku ya Pentekote, lakini hakumwangwa juu ya watu *wote.* Unabii huu utatimizwa pia kwa mwisho wa muda wa Mateso. Mbele ya kurudi kwa Kristo na utukufu, kutakuwa na **maajabu** mbinguni na **alama** duniani (Mt. 24:29,30). Halafu Bwana Yesu Kristo atatokea duniani kushinda adui zake na kusimamisha ufalme wake. Kwa mwanzo wa utawala wake wa miaka elfu moja,

Roho ya Mungu atamwangwa juu ya **watu wote**, Wayuda na Mataifa vilevile, na neno hili litaendelea kwa zaidi ya utawala wa miaka elfu moja. Kazi za Roho Mtakatifu zitaonekana kwa njia mbalimbali kwa watu, si neno kama wao ni wanaume au wanawake, wazee au vijana, wenye kujulikana katikati ya watu au sivyo. Kutakuwa na **maono** na **ndoto,** ambazo zinatufikirisha maneno watu watakayojulishwa, na unabiii, ambao unatufikirisha kupitisha kujua kwa maneno haya kwa watu wengine. Hivi zawadi za ufunuo kupitisha habari hizi kwa watu wengine zitaonekana. Maneno haya yote yatatokea kwa wakati unaoitwa na Yoeli **siku za mwisho** (sh.17), ndizo siku za mwisho za Israeli, si za kanisa.

**2:20** Alama mbinguni zitaonekana **mbele ya kutimia kwake** ... **ya siku ya Bwana.** Hapa **siku ya Bwana** ndiyo siku Bwana atakaporudi yeye mwenyewe duniani kuharibu adui zake na kutawala na uwezo na utukufu mkubwa.

**2:21** Petro alimaliza mashairi toka Yoeli na ahadi ya kwamba **kila mtu anayeita jina la Bwana ataokolewa**. Habari hizi njema ni kwa watu wa kila wakati wanaoamini Bwana. Semo hili **Jina la Bwana** linasema juu ya maneno yote Bwana aliyo. Hivi **kuita jina** lake ni **kutaja** Bwana mwenyewe ambaye tunamwamini kama njia ya pekee kupata wokovu.

**2:22-24** Lakini Bwana ni nani? Petro atatangaza sasa habari za kushitusha kwamba Yesu huyu ambaye walisulibisha ni Bwana na Kristo. Alifanya hivi kwa njia ya kusema kwanza juu ya maisha ya Yesu, kisha juu ya kufa na ufufuko wake, kupanda kwake mbinguni, na mwishoni kutukuzwa kwake kwa **mkono wa kuume wa Mungu** Baba. Haifai wakae kufikiri kwamba **Yesu** ni kwanza ndani ya kaburi inchini mwa Yuda. Ilikuwa lazima kuwaambia ya kwamba Yule ambaye walikuwa wameua ni mbinguni, nao watalazimishwa kusimama mbele yake siku nyingine.

Tunaweza kujumlisha mafundisho ya Petro hivi: **Yesu wa Nazareti** alionyeshwa kuwa **Mtu** toka **Mungu** kwa njia ya **maajabu** mengi aliyofanya kwa uwezo wa **Mungu** (sh. 22). **Mungu akijua na kukusudi yote tangu zamani, alimtoa** kwa mikono ya Wayuda. Halafu Wayuda walimtoa kwa Mataifa (watu bila sheria) **asulibishwe na kuuawa** (sh. 23). Lakini **Mungu alimfufua** toka wafu, **akilegeza uchungu wa mauti. Haikuwezekana** afungwe na mauti **kwa sababu:**

1. Ilikuwa lazima kwa Mungu mtakatifu kumfufua. Yule asiyekuwa na zambi alikuwa amekufia wenye zambi. Ilikuwa sharti kwa Mungu kumfufua kuhakikisha kwamba alikubali kabisa kazi Kristo aliyofanya kukomboa watu.
2. Sharti unabii ndani ya Agano la Kale juu ya kufufuliwa kwake utimizwe. Hili ndilo neno Petro alilofundisha zaidi ndani ya mashairi yanayofuata.

**2:25-27** Ndani ya Zaburi 16 Daudi aliandika kama nabii juu ya maisha, mauti, ufufuko na kutukuzwa kwa Bwana.

Kwa maneno ya maisha yake **Daud**i alipasha juu ya matumaini ya kutimia ya yule aliyeishi kila siku, kila saa na ushirika mkamilifu wa Baba yake. **Moyo, ulimi, na mwil**i – alijazwa kabisa na furaha na **matumaini**.

Kwa maneno ya mauti yake, Daudi **aliona mbele** ya kwamba Mungu **hataacha roho yake katika Hadeze,** wala kuacha **Mtakatifu wake aone uharibifu**. Maana yake, **nafsi** ya Bwana yake haitabaki tupu, wala mwili wake hautaoza. (Haifai kutumika na shairi hili kuhakikisha kwamba Bwana alikwenda kwa pahali pa roho za wafu chini sana duniani kwa wakati wa mauti yake. Nafsi yake ilikwenda mbinguni – Lk. 23:43 – na mwili wake uliwekwa kaburini.)

**2:28** Juu ya ufufuko wa Bwana, Daudi alionyesha kwamba Mungu atamwonyesha njia ya uzima. Ndani ya Zaburi 16:11 Daudi aliandika, "Utanijulisha njia ya uzima." Katika Matendo 2:28 Petro alisema, **"Umenijulisha njia ya uzima,"** ndilo neno linalokwisha kufanyikana. Bila shaka Roho Mtakatifu alimwongoza kufanya hivi kwa sababu kwa wakati ule Bwana alikuwa amefufuliwa.

Daudi alitabiri kutukuzwa kwa Mwokozi kwa wakati wa sasa wakati aliposema, "Utanijaza furaha kwa uso wako," au kama tunavyosoma katika Zaburi 16:11, "Mbele ya uso wako ni furaha tele, kwa mkono wako wa kuume ni mambo ya kupendeza kwa milele."

**2:29** Petro alisema kwamba **Daud**i hakuweza kusema maneno haya juu yake mwenyewe kwa sababu *mwili wake ulioza kweli*. Alikufa, na Wayuda wa wakati ule walijua pahali pa **kaburi lake**. Walijua hakufufuliwa.

**2:30, 31** Wakati **Daudi** alipoandika zaburi ile alisema kama **nabii**. Alikumbuka ahadi ya Mungu **kusimamisha** mmoja wa wazao wake **kuketi juu ya kiti chake cha ufalme** milele**.** Daudi alifahamu kwamba Huyu atakuwa Masiya, na ya kwamba hata kama atakufa, **nafsi** yake **haitaachwa** bila mwili katika Hadeze, na mwili wake hautaoza.

**2:32, 33** Halafu Petro alisema maneno aliyosema mbele – bila shaka lilikuwa tangazo lililoshitusha Wayuda ambao walimsikiliza. Masiya huyu ambaye **Daudi** alitabiri habari zake alikuwa **Yesu** wa Nazareti. **Mungu alikuwa amemfufua** toka wafu – mitume yote walikuwa washuhuda wa ufufuko wake. Nyuma ya ufufuko wake Bwana Yesu **alitukuzwa kwa mkono wa kuume wa Mungu,** na sasa **Roho Mtakatifu** alikuwa ametumwa kama **Baba** alivyoahidi. Haya ndiyo maelezo ya maneno yaliyokuwa yametokea katika Yerusalema siku ile.

**2:34, 35 Daudi** alikuwa ametabiri vilevile ya kwamba Masiya atatukuzwa. Hakusema juu yake mwenyewe ndani ya Zab. 110:1. Alitaja tena maneno Yehova aliyosema na Masiya, **"Keti kwa mkono wangu wa kuume hata niweke adui zako chini ya miguu yako."** (Ona ya kwamba ndani ya mashairi 33-35 kuna muda nyuma ya kutukuzwa kwa Kristo na saa atakaporudi kuazibu adui zake na kusimamisha ufalme wake.)

**2:36** Halafu mara moja tena Wayuda walisikia tangazo lile kubwa: "kila nyumba ya Israeli ijue kwa kweli, MUNGU AMEFANYA **huyu Yesu ambaye mulisulibisha** KUWA BWANA NA KRISTO. Walikuwa **wamesulibisha** Mpakaliwa wa Mungu, na kuja kwa Roho Mtakatifu kulikuwa ushuhuda kwamba Yesu alikuwa ametukuzwa mbinguni (ona Yn. 7:39).

**2:37** Roho Mtakatifu alifanya kazi kubwa sana ndani ya roho za wasikiaji. Wakati waliposikia maneno haya ya Petro, walichomwa katika moyo na kulalamika mara moja, **"Tutafanya nini?"** Walikuwa wametambua ukubwa wa hatia yao. Walifahamu sasa kwamba Yesu ambaye walimwua alikuwa Mwana mpendwa wa Mungu! Yesu huyu alikuwa amefufuliwa toka wafu na alitukuzwa sasa mbinguni. Itawezekana kweli kwa wauaji hawa kuepuka hukumu?

**2:38** Petro alisema nao sharti **watubu na kubatizwa kwa jina la Yesu Kristo wapate ondoleo la zambi zao.** Kwanza iliwapasa **kutubu** na kukubali kwamba walikuwa wenye hatia.

Nyuma yake iliwapasa **kubatizwa** wapate **ondoleo la zambi** zao. Watu wengi, wakati wanaposoma shairi hili wanafikiri watu wanaokolewa kwa njia ya kubatizwa, lakini hii *si* maana ya shairi hili hata kidogo:

1. Mashairi mengi katika Agano Jipya

yanafundisha kwamba watu wanapata wokovu kwa njia ya kuamini Bwana Yesu Kristo tu. Kwa mfano soma Yn. 1:12; 3:16, 36; 6:47; Mdo. 16:31; Rom. 10:9. Haiwezekani kwa shairi moja au mashairi mawili kubisha ushuhuda wa mashairi yale yote mengine.

2. Mwizi msalabani alijua kabisa kwamba ameokolewa bila kubatizwa (Lk. 23:43).
3. Hatusomi kwamba Mwokozi alibatiza mtu ye yote. Kwa sababu gani hakufanya hivi kama ubatizo ni neno la lazima kwa wokovu?
4. Mtume Paulo alikuwa na asante kwa sababu alibatiza Wakorinto wachache tu. Kwa nini alikuwa na asante juu ya neno hili kama ubatizo uliweza kusaidia kuokoa watu? (1 Kor. 1:14-16).

Sharti tuone ya kwamba Wayuda tu waliagizwa kubatizwa kwa usamehe wa zambi zao (ona Mdo. 22:16). Hii ndiyo siri ambayo inatusaidia kufahamu maana ya mashairi haya. Taifa la Israeli walikuwa wamesulibisha Bwana wa utukufu. Wayuda walikuwa wamelalamika, "Damu yake iwe juu yetu na juu ya watoto wetu" (Mt. 27:25). Hivi watu wa Israeli walikubali kuwa wenye hatia ya mauti ya Masiya.

Sasa wengine wa Wayuda walikuwa wamefahamu kwamba walikuwa wameanguka. Kwa njia ya kutubu walikubali zambi zao mbele ya Mungu. Kwa njia ya kuamini Bwana Yesu kama Mwokozi wao walizaliwa tena na kupokea usamehe wa milele kwa zambi zao. Kwa njia ya kubatizwa mbele ya watu walijitenga na *taifa* waliosulibisha Bwana na walifanywa mamoja *naye.* Hivi ubatizo ulikuwa alama kwa watu ya kwamba walikuwa wameoshwa toka zambi yao ya kukataa Kristo (na zambi zao nyingine zote). Hawakufungana na dini ya Wayuda tena lakini pamoja na Wakristo. Lakini ubatizo haukuwaokoa. Waliweza kuokolewa kwa njia ya kuamini Kristo tu. Kufundisha maneno mengine ni kufundisha Habari Njema nyingine, na kulaaniwa (Gal. 1:8, 9).

Mwalimu Ryrie alieleza ubatizo kwa **ondoleo la zambi** kwa njia nyingine:

> Si kusema kwamba kusudi la ubatizo ni kuondoa zambi, kwani tunasoma pahali pote ndani ya Agano Jipya kwamba zambi zinasamehewa za mtu anayeamini Kristo, si kama tunda la ubatizo. Maana yake ni ubatizo wa mtu aliyekwisha kuondolewa zambi zake kwa njia ya imani. Watu wa makutano haya kwa Pentekote walitubu na kuondolewa zambi zao, na kwa sababu hii waliombwa kubatizwa.

Petro alisema na watu kwamba wakitubu na **kubatizwa watapokea zawadi ya Roho Mtakatifu**. Maneno yalifuatana hivi kwa wakati wa mwanzo wa kanisa tu. Mwalimu mwingine, H.P. Barker anaonyesha wazi ndani ya kitabu chake *(The Vicar of Christ)* ya kwamba kulikuwa na jamii mbalimbali ine za waamini ndani ya Kitabu cha Matendo waliopokea Roho Mtakatifu, lakini kila mara maneno yalifuatana namna nyingine kidogo.

Hapa katika Matendo 2:38 tunasoma juu ya *Wayuda* walioamini na kugeuka Wakristo. Kawaida kwa Wayuda ilikuwa hivi:

1. Walitubu.
2. Walibatizwa katika maji.
3. Walipokea Roho Mtakatifu.

Tunasoma juu ya wokovu wa *Wasamaria* katika Mdo. 8:14-17. Pale tunasoma ya kwamba:

1. Waliamini.
2. Walibatizwa katika maji.
3. Mitume waliwaombea.
4. Mitume waliwawekea mikono.
5. Walipokea Roho Mtakatifu.

Katika Mdo. 10:44-48 tunasoma juu

ya wokovu wa *Mataifa.* Kawaida hapa ilikuwa:

1. Waliamini.
2. Walipokea Roho Mtakatifu.
3. Walibatizwa katika maji.

Mwishoni tunasoma juu ya *wanafunzi wa Yoane Mbatizaji,* katika Matendo 19:1-7:

1. Waliamini.
2. Walibatizwa tena.
3. Mtume Paulo aliwawekea mikono.
4. Walipokea Roho Mtakatifu.

Hivi kulikuwa na njia ine ndani ya kitabu cha Matendo kupata wokovu? Sivyo, hata kidogo! Wokovu ulipatikana kwa wakati ule, na sasa, na kwa wakati wa kuja, kwa njia ya kuamini Bwana tu. Lakini kwa muda huu wa mabadaliko tunaosoma habari zake katika Matendo, Mungu alichagua kugeuza kawaida ya namna watu walivyopokea Roho Mtakatifu, bila kutufunulia kwa sababu gani alifanya hivi.

Basi kawaida gani ya kawaida hizi ine ni kwa wakati wa sasa? Kwa sababu taifa la Israeli walikataa Masiya, hawastahili tena kupokea baraka ambazo wangaliweza kupokea. Kwa wakati wa sasa Mungu anaita toka Mataifa watu kwa jina lake (Mdo.15:14). Hivi kawaida tunayoona ndani ya Matendo 10 ni kawaida kwa *wakati wa sasa*, ndiyo:

Imani.
Kupokea Roho Mtakatifu.
Ubatizo kwa maji.

Tunaamini hii ndiyo kawaida kwa wakati wa sasa kwa waamini wote, wa Wayuda na wa Mataifa. Watu wanaweza kuuliza, "Wakati gani kawaida ya Matendo 2:38, iliyokuwa kwa Wayuda, ilikombolewa na ile kwa Matendo 10:44-48?" Haiwezekani kutaja mwaka fulani. Lakini ndani ya kitabu cha Matendo tunaona namna polepole mahubiri ya Habari Njema kwa Wayuda yalipunguka na kukataliwa nao, na mahubiri kwa Mataifa yaliongezeka. Kwa mwisho wa kitabu cha Matendo tunaona kwamba taifa la Israeli lilikuwa limewekwa kando kwa sababu ya kutokuamini, na hawakustahili tena kupokea baraka ya watu wachaguliwa wa Mungu. Kwa muda wa Kanisa taifa la Israeli litahesabiwa pamoja na Mataifa, na kawaida ya Matendo 10:44-48 ni kwa Wayuda waamini wa sasa vilevile.

**2:39** Halafu Petro aliwakumbusha kwamba **ahadi** ya Roho Mtakatifu ni **kwa ajili yao na watoto wao** (ndio Wayuda) **na kwa watu wote walio mbali** (Mataifa), na **wote watakaoitwa na … Mungu.**

Hapa ni ahadi ya kwamba watu wale wale waliosema mbele, "Damu yake iwe juu yetu na juu ya watoto wetu" watapewa neema ya Mungu pamoja na watoto wao vilevile kama wakiamini Bwana!

Mara nyingi watu wanaanguka wakati wanapotumika na shairi hili na kufundisha ya kwamba watoto wanaokolewa kwa sababu wazazi wao ni Wakristo. Ona elezo la Mwalimu Spurgeon la maneno haya:

> Ingepasa Kanisa la Mungu kujua ya kwamba "kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho?" (Yn. 3:6). "Nani anayeweza kutoa kitu safi katika kitu kichafu?" (Yobu 14:4) Kuzaliwa hapa duniani ni pamoja na uchafu wa dunia lakini hakuleti salama. Kwa agano jipya tunaandikwa wazi kwamba wana wa Mungu wanazaliwa, si kwa damu, wala si kwa mapenzi ya mwili; wala si kwa mapenzi ya mtu, lakini Mungu" (Yn. 1:13).[1]

Sharti tuone kwamba **ahadi** si kwa **ajili yenu, na watoto wenu** tu, lakini **kwa watu wote walio mbali, na wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu**. Ni kwa kila mtu anayeamini Habari Njema.

**2:40** Sehemu tu ya hotuba ya Petro inaandikwa ndani ya sura hii, lakini neno kubwa ndani ya baki lake ni maonyo kwa wasikiaji Wayuda wajiponyeshe wenyewe toka **kizazi hiki kipotevu** waliokataa na kuua Bwana Yesu. Waliweza kufanya hivi kwa njia ya kupokea Yesu kama Masiya na Mwokozi na kutoa ushuhuda wazi kwa njia ya ubatizo mbele ya watu kwamba wamejitenga na taifa la Israeli wenye hatia.

**2:41** Kulikuwa na watu wengi waliotaka kubatizwa siku ile, kama ushuhuda kwamba **walipokea neno la Petro kwa furaha** kama neno kutoka kwa Bwana.

Siku ile kundi la waamini **walizidishwa** na **watu kama elfu tatu**. Wokovu wa watu wale wengi ulihakikisha kwamba utumishi wa Petro ulikuwa utumishi wa Roho Mtakatifu. Bila shaka mvuvi huyu wa Galilaya alikumbushwa maneno ya Bwana Yesu, "Nitawafanyiza ninyi wavuvi wa watu" (Mt. 4:19). Na labda alikumbushwa vile vile masemo ya Mwokozi, "Kweli, kweli ninawaambia ninyi, yeye ambaye ananiamini mimi, kazi ninazofanya, yeye atazifanya vilevile; na atafanya kazi kubwa kuliko hizi; kwa sababu ninakwenda kwa Baba yangu." (Yn. 14:12)

Ni vizuri kuona namna hesabu ya wale waamini wa sasa iliandikwa – *kama* **elfu tatu**. Ni vizuri kwa watumishi wa Bwana kuhesabu waamini wa sasa na ange kidogo, kwani labda wengine wanakiri Kristo na kinywa tu.

**2:42** Kuendelea katika imani kunahakikisha ya kuwa mtu aliamini kweli. Waamini hawa walihakikisha kwamba waliamini kweli kwa njia ya kudumu katika:

1. **Mafundisho ya mitume.** Mitume walitoa mafundisho haya kwa njia ya kuhubiri wakiongozwa na Roho Mtakatifu. Mafundisho haya yanachungwa ndani ya Agano Jipya kwasi sasa.

2. **Ushirika.** Alama nyingine iliyohakikisha kwamba waliokolewa kweli ilikuwa hamu ya waamini wa sasa kuwa pamoja na watu wa Mungu na kushiriki maneno pamoja nao. Walikuwa wametengwa na dunia na kuwekwa kwa Mungu na ushirika na Wakristo wengine.

3. **Kuvunja mkate.** Ndani ya Agano Jipya maneno haya yalisema juu ya Karamu ya Ukumbusho wa Bwana, na vilevile kwa watu wakikula vyakula pamoja. Habari zinazotangulia na kufuata zinafahamisha msomaji kama yana maana gani. Ni wazi ya kwamba hapa yanasema juu ya Karamu ya Ukumbusho, si juu ya kula vyakula tu. Ndani ya Matendo 20:7 tunaona kwamba ilikuwa desturi ya Wakristo wa kwanza kuvunja mkate siku ya kwanza ya juma. Kwa wakati wa mwanzo wa kanisa Wakristo walikula chakula kingine pamoja vilevile kwa "karamu ya mapendo," kuonyesheana mapendo, lakini nyuma ya wakati maneno yasiyokuwa taratibu yaliingia ndani ya karamu hii ya "agape," maana yake mapendo, na watu hawakukutana kwa karamu ile tena. Walikaa kukutana pamoja kuvunja mkate kukumbuka Bwana tu.

4. **Maombi**. Hii ilikuwa desturi kubwa ya ine ya kanisa kwa wakati wa mwanzo, na kwa njia hii walionyesha kwamba walitegemea Bwana kabisa kuongoza kuabudu kwao, na ndani ya maneno yote mengine, kuwalinda na kuwawezesha kumtumikia.

**2:43** Watu walishikwa na roho ya heshima na woga, na Roho Mtakatifu alitumika na uwezo ndani ya mioyo yao. Walishangazwa sana wakati walipoona **mitume** wakifanya **maajabu na alama** nyingi. **Maajabu** yanashangaza watu.

Kazi ya **alama** ilikuwa kuleta mafundisho. *Ajabu* liliweza kuwa *alama* vilevile.

**2:44, 45** Waamini walikaa kukutana pamoja, na walikuwa na **vitu vyote ushirika**. Mapendo ya Mungu yalijaza mioyo yao kabisa hata hawakuhesabu **vitu vyao** vilikuwa mali zao wenyewe (Mdo. 4:32). Wakati kulipokuwa na **hitaji kubwa** katikati ya waamini, waliuza vya vitu vyao na kugawa mali waliyopata kusaidia wenye hitaji. Hivi hali yao yote ilikuwa sawasawa.

> Waamini wale walikuwa na roho moja na walijaa na mapendo ya Mungu yaliyozima roho ya kujifikiri wenyewe. Na kwa sababu ya umoja wao walishiriki maneno yote pamoja, si kwa sababu ya lazima au sheria, lakini kwa sababu walibarikiwa wote na Kristo. Walitajirishwa naye na baraka isiyoweza kupunguzwa, lakini kwa kipimo walichotumika nayo kwa kipimo kile iliongezeka kwao, hata "waliuza mali na vitu vyao, wakagawia watu wote kama kila mtu alivyokuwa na uhitaji."[2]

Watu wengi kwa wakati wa sasa wanafikiri hatuhitaji kuiga waamini wa wakati ule ndani ya desturi hii. Ni kama wanasema hatuhitaji kupenda jirani zetu kama sisi wenyewe! Desturi hii ya kushiriki mali na vitu vyao na wenye mahitaji ilikuwa tunda la kujazwa na Roho Mtakatifu. Imesemwa ya kwamba Mkristo wa kweli hawezi kufurahi kukaa na mali kupita hesabu anayohitaji yeye mwenyewe kama wengine wakikosa mali ya kutosha kwa mahitaji yao.

**2:46** Shairi hili linaonyesha namna Pentekote ilivyogeuza maisha ya watu kwa maneno ya dini na nyumbani mwao.

Kwa *maneno ya dini* tukumbuke kwamba waamini hawa wa sasa walikuwa Wayuda. Hata kama kanisa lilikuwa limeanzwa, hawakuacha maneno yote ya dini na hekalu la Wayuda mara moja. Walikaa kuachana na desturi hizi polepole ndani ya muda mzima wa kitabu cha Matendo. Hivi waamini walikaa **kufikia hekalu**[3] kwa wakati kwa kuabudu na kusikia mafundisho ya Agano la Kale. Zaidi ya ile walikutana nyumbani kufanya maneno tuliyosoma ndani ya shairi 42.

Kwa maneno ya maisha yao ya kila siku *nyumbani mwao,* tunasoma walivunja **mkate,** na **kupokea chakula chao kwa furaha.** Hapa **kuvunja mkate** kunasema juu ya kula vyakula tu. Furaha ya wokovu wao ilienea ndani ya maneno yote ya maisha yao.

**2:47** Maisha ya wale waliokwisha kuokolewa toka giza na kuingizwa ndani ya ufalme wa Mwana wa Mungu yalijaa na sifa na mashukuru.

Kwa mwanzo waamini **walipendeza watu wote,** lakini neno hili liligeuka nyuma ya wakati. Ni kama imani ya Wakristo inaamsha uadui na kuchukia ndani ya roho za wasioamini. Mwokozi alionya wanafunzi kukaa na ange kwa sifa ya watu (Lk. 6:26), na alisema nao kwamba watachukiwa na kuteswa na watu (Mt. 10:22, 23).

**Na Bwana aliongezea kanisa kila siku wale waliokuwa wakiokolewa.** Ilipasa watu waliosikia Habari Njema kuchagua na kutaka kwao wenyewe kupokea Yesu Kristo kuwa Mwokozi wao. Hata kama Bwana alichagua watu na kuongezea kanisa, ilipasa kila mtu kuchagua yeye mwenyewe neno atakalofanya.

Ndani ya sura hii tumesoma juu ya kumwangwa kwa Roho Mtakatifu, hotuba kubwa ya Petro, na habari nusu juu ya namna ya maisha ya waamini wa kwanza. Kuna andiko zuri juu ya maisha ya waamini kwa wakati wa mwanzo wa kanisa ndani ya "Historia la Kanisa" katika *Encyclopaedia Brittanica, 13th edition :*

> Neno linaloonekana zaidi ndani ya maisha ya Wakristo wa kwanza ni ya kwamba walifahamu walikuwa watu wa Mungu walioitwa na kuwekwa mbali na dunia. Walifahamu kwamba Kanisa lilisimamishwa na Mungu, si na watu. Lilitawaliwa na Mungu, na hata dunia iliumbwa kwa ajili yake. … Mawazo haya yalitawala maneno yote ya maisha ya Wakristo wa kwanza. Walifahamu kwamba wao waliunganishwa pamoja, mbali na watu wa dunia. Walikuwa wenyeji wa mbingu, si wa dunia, na walijaribu kutii magizo ya mbingu. Dunia hii ya sasa ni kwa wakati tu, na maisha yao ya kweli yalikuwa kwa wakati wa kuja. Kristo atarudi nyuma kidogo, na kazi za mshahara na masumbuko na furaha za muda wa sasa si neno kubwa …Maisha yao ya kila siku yalitawaliwa na Roho Mtakatifu na kuonyesha matunda ya Roho. Kwa sababu hii maisha yao yalikuwa namna nyingine na maisha ya kila siku ya watu wengine.

Kusoma andiko hili linatusaidia kufahamu kwamba kanisa kwa wakati wa sasa limekwenda mbali sana na nguvu na umoja ambao lilikuwa nao kwa wakati wa mwanzo wake.

## MAFUNDISHO JUU YA KANISA NYUMBANI

Neno hili *kanisa* (kwa Kiyunani *ekklesia*) linaonekana mara ya kwanza katika Matendo ndani ya 2:47, na tunataka kufikiri sasa juu ya ukubwa wake ndani ya mawazo ya Wakristo wa kwanza.

Mara nyingi kwa wakati wa sasa tungeita kanisa ndani ya Matendo na baki la Agano Jipya kanisa la nyumba. Wakristo wa kwanza walikutana ndani ya nyumba, si ndani ya majengo yaliyosimamishwa kwa kanisa. Mwalimu Unger anasema Wakristo walikaa kukutana nyumbani kama kanisa kwa miaka 200.

Labda tungefikiri walikutana ndani ya nyumba zao kwa sababu walikosa mali kujenga nyumba kwa kanisa kukutana ndani yao. Watu wa sasa wanafikiri ni mapenzi ya Mungu kwa kanisa kukutana ndani ya nyumba kubwa zinazosimamishwa kwa kanisa kukutana ndani yao.

Sivyo. Mawazo haya hayapatani na imani ya kikristo. Si mapendo kutumika na mali nyingi kusimamisha nyumba nzuri sana kwa kanisa wakati elfu za watu duniani wanapokaa na mahitaji makubwa.

Ni ukosefu wa huruma, na vile ni kupoteza mali bure kujenga nyumba kubwa za bei nyingi zinazotumiwa kwa kuabudu kwa saa nusu tu kila juma. Watu wengine wanafikiri nyumba namna hii zinahitajiwa kukokota wasioamini kufika kusikia Habari Njema. Inatupasa kukumbuka kwamba zaidi ya makusanyiko ya kanisa kwa wakati wa mwanzo yalikuwa kwa waamini. Wakristo walikutana kusikia mafundisho ya mitume, kwa ushirika, kuvunja mkate na kwa maombi (Mdo. 2:42). Hawakujaribu kuleta wasioamini kwa Kristo kwa njia ya kuwaita kufikia makusanyiko ya kanisa siku ya Bwana, lakini kwa njia ya kuwapasha habari za Yesu wakati walipokutana nao siku nyingine, pahali pa kazi, sokoni, darasani, vivyo hivyo. Halafu wakati watu walipoamini waliwaleta kushiriki na waamini wengine ndani ya kanisa nyumbani waweze kulishwa na kujengwa na Neno la Mungu.

Kukutana ndani ya nyumba ni njia nzuri sana kwa waamini wa inchi yo yote kukusanyika. Tunafikiri ya kwamba kwa wakati wa sasa zaidi ya makanisa wanakutana ndani ya nyumba, si ndani ya majengo makubwa.

Kwa mitume na Wakristo kwa wakati wa mwanzo, Mungu alichagua kusimamisha kanisa kuwa *njia ya pekee* kwa Habari Njema kuenezwa duniani, na mi-

tume walikubali kutumika kwa njia ya *makanisa namna hii tu*. ❖

**E. Kuponyeshwa kwa kiwete, na hotuba ya Petro kwa Israeli (3:1-26)**

**3:1** Ilikuwa saa tisa wakati **Petro na Yoane walipopanda pamoja kwenda hekaluni** katika Yerusalema. Kama tulivyoona mbele, Wakristo Wayuda walikaa kuabudu hekaluni kwa wakati nyuma ya mwanzo wa kanisa. Waliachana na dini ya Wayuda polepole. Haifai waamini wa wakati wa sasa kuwaiga ndani ya neno hili, kwani sasa tuna ufunuo mzima wa Agano Jipya na tunaagizwa "kwenda kwake inje ya kambi tukichukua laumu lake" (Ebr. 13:13. Ona vilevile 2 Kor. 6:17, 18).

**3:2** Wakati walipokaribia hekalu waliona watu wakibeba kiwete na kumfikisha kwa pahali alipokaa kila siku kwa **mlango** wa hekalu **ulioitwa Mzuri**. Mtu huyu alizaliwa **kiwete** na hakuweza kufanya kitu kujisaidia. Wakati tunaposawanisha hali yake na jengo na mapambo ya hekalu, tunakumbushwa ya kwamba leo vilevile watu masikini wengi na wenye uzaifu mwilini na rohoni wanakaa karibu na makanisa makubwa ya mapambo na utajiri bila kusaidiwa.

**3:3** Ni kama kiwete hakuwa na tumaini tena kwamba ataweza kuponyeshwa, hivi alikaa pale siku zote akiomba kusaidiwa na watu waliopita njiani.

**3:4** **Petro** hakuona mtu huyu kama kiwete masikini tu asiyeweza kujisaidia, lakini kama mtu ndani yake uwezo mkubwa wa Mungu utaweza kuonekana. Wakati Petro alipomwagiza kumtazama, hakukusudi kukokota macho yake juu yake na Yoane, lakini kwa kiwete kuweza kusikiliza na kuweka roho juu ya masemo yake.

**3:5, 6** Basi **aliwaangalia** sana **akizani** watampa zawadi. Bila shaka maneno aliyosikia yaliondosha tumaini rohoni mwake kwanza, na kumsitusha sana vilevile. Petro hakuwa na mali aliyoweza kumpa. Lakini aliweza kumpa kitu kizuri kupita. Kwa amri ya **Yesu Kristo wa Nazareti** aliagiza kiwete **kusimama na kutembea!**

Tuna habari za Mkristo mmoja wa kujulikana zamani, jina lake Thomas Aquinas, aliyefika karibu na papa ya Roma saa ya kuhesabu mali. Papa alijivuma, "Hatuhitaji kusema tena kama Petro, 'Sina feza wala zahabu!'" Aquinas alimjibu, "Na huwezi kusema pamoja na Petro, 'Simama na tembea!'"

**3:7** Wakati Petro aliposaidia kiwete kusimama, **nguvu** iliingia ndani ya **miguu na mifundo ya miguu yake** iliyokuwa zaifu mbele. Tunaona tena hapa kuchangamana kwa maneno ya Mungu na ya mwanadamu. Petro alisaidia mtu huyu kusimama; halafu Mungu alimponyesha. Sharti sisi tufanye kazi tunayoweza; kisha Mungu atafanya kazi ambazo zinatushinda.

**3:8** Ajabu hili lilifanyikana mara moja, si polepole. Ona namna Roho Mtakatifu alivyoongoza maneno kuonyesha furaha ya mtu huyu: **aliondoka upesi, akasimama … akaanza kutembea … akaingia … akirukaruka.**

Wakati tunapokumbuka kwamba mtoto mdogo anajifunza kutembea polepole, pamoja na kuangukaanguka, tunafahamu kwamba kweli ingekuwa furaha kubwa kwa mtu huyu kuweza kutembea na kuruka mara moja, mara ya kwanza katika maisha yake.

Ajabu hili lililofanywa kwa jina la Yesu lilikuwa ushuhuda tena kwa watu wa Israeli ya kwamba Yule ambaye walimsulibisha alikuwa hai na tayari kuwaponyesha na kuwaokoa.

**3:9, 10** Watu walijuana na kuona kiwete huyu akilala kila siku kwa mlango wa hekalu, na habari za ajabu la kuponyeshwa kwake zilienea mbio. **Watu**

hawakuweza kukana kwamba ajabu kubwa lilikuwa limefanyikana, na bila shaka walifazaika sana kama maana ya neno hili lilikuwa nini.

**3:11** Mtu **aliyeponyeshwa alishika Petro na Yoane,** kama waganga wake, **na watu wote walikimbia kukusanyika** kwa **baraza ya Solomono** karibu na hekalu wakishangaa sana. Neno hili lilimpa Petro njia nzuri kwa mahubiri.

**3:12** Petro alianza na kuondosha mawazo wa watu toka mtu aliyeponyeshwa na toka mitume, kwani wao hawakuweza kueleza maana ya ajabu hili.

**3:13-16** Halafu aliwafikirisha mbio Yule aliyetenda ajabu hili. Alikuwa Yesu, ambaye walimkataa na **kuua. Mungu alikuwa amemfufua toka wafu** na **kumtukuza** mbinguni. Sasa **kwa njia ya kumwamini** huyu Yesu, **kiwete** alikuwa ameponyeshwa toka uzaifu wake.

Uhodari wa Petro toka Mungu wakati aliposhitaki watu wa Yuda unatushangaza. Aliwashitaki juu ya mambo mane:

1. **Walitoa** Yesu (kwa mataifa ahukumiwe).
2. **Walimkana mbele ya Pilato, wakati alipokusudi kumfungua.**
3. **Walikana yule Mtakatifu; yule mwenye haki, wakataka wapewe mwuaji** (ndiye Baraba).
4. **Waliua yule Mkubwa wa uzima.**

Sawanisha maneno haya na namna Mungu alivyotendea Yesu:

1. **Alimfufua toka wafu** (sh.15).
2. **Alimtukuza** (sh.13).

Ona vilevile ya kwamba **imani** ndani ya Kristo ndilo elezo la ajabu hili la kuponyesha (sh. 16). Ndani ya shairi hili, kama ndani ya mashairi mengine vilevile, **jina** lilitumiwa kusema juu ya mtu mwenyewe. Hivi maana ya **imani katika jina lake** ndiyo **imani ndani ya** Kristo.

**3:17** Nyuma ya kushitaki wanaume wa Israeli na ukali juu ya mauti ya Bwana Yesu, aligeuka na kusema nao na neema akiwaita **ndugu** Wayuda, **waliotenda neno hili kwa ujinga,** na akiwasukuma kutubu na kuamini.

Ni kama neno Petro alilosema ya kwamba Wayuda walisulibisha Bwana Yesu kwa ujinga halikupatana na maneno yaliyotokea kweli. Hakufika na maneno yaliyohakikisha kwamba yeye ni Masiya? Hakufanya maajabu makubwa katikati yao? Hakuwakasirisha kwa njia ya kusema yeye ni sawasawa na Mungu? Ndiyo, maneno haya yote yalikuwa kweli. Lakini hata hivi hawakujua kwamba Yesu Kristo ni Mungu katika mwili. Hawakufikiri Masiya atafika na unyenyekevu lakini kama askari mshindaji mwenye uwezo. Walifikiri Yesu ni mdanganyi.

Hawakujua kwamba yeye ni kweli Mwana wa Mungu. Labda walifikiri walitumikia Mungu kwa njia ya kumwua. Hivi Mwokozi mwenyewe alisema saa ya kusulibishwa kwake, “Hawajui neno wanalofanya” (Lk. 23:34), na kwa wakati wa nyuma Paulo aliandika, “Kama [watawala wa dunia hii] wangalijua, wasingalisulibisha Bwana wa utukufu” (1 Kor. 2:8).

Kusudi la masemo haya yote lilikuwa kufahamisha watu wa Israeli kwamba, hata zambi yao ilikuwa kubwa sana, iliweza kusamehewa kwa sababu ya neema ya Mungu.

**3:18** Bila kutoa uzuru kwa zambi zao, Petro alionyesha kwamba **Mungu** alitimiza makusudi yake hata hivi. **Manabii** katika Agano la Kale walitabiri kwamba Masiya **atateswa** kwa mikono ya Wayuda. Lakini sasa yeye mwenyewe alijitoa kuwa Bwana na Mwokozi wao. Kwa njia yake waliweza kupokea usamehe kwa zambi zao.

**3:19** Ingepasa Waisraeli **kutubu** na kugeuza mawazo yao kabisa. Kama wakifanya hivi, **zambi zao zitao-**

**ndoshwa, ili zipate kuja nyakati za ufufuko toka uso wa Bwana.**

Inatupasa kukumbuka kwamba Petro alikuwa akihubiri kwa watu wa Israeli (sh.12). Hotuba yake ilionyesha kwamba lazima taifa la Israeli watubu mbele ya kurudishwa kwa Mungu na kubarikiwa. **Nyakati za ufufuko toka uso wa Bwana** ndizo baraka za ufalme wa Kristo duniani kwa wakati wa kuja, kama tunavyosoma ndani ya shairi 20.

**3:20** Nyuma ya toba ya Israeli, Mungu **atatuma** Masiya, ndiye **Yesu,** kwa wakati wa kuja kwa pili kwa Kristo, kusimamisha utawala wake duniani kwa miaka elfu moja, kama tulivyoona mbele.

**3:21** Halafu watu wanauliza, "Kama taifa la Israeli wangalitubu wakati Petro alipokuwa akihubiri, Bwana Yesu angalirudi duniani saa yenyewe?" Watu wa kujulikana, wenye kupenda Mungu wanajibu ulizo hili kwa njia mbalimbali. Wengine wanasema angalirudi; wanasema kama asingalirudi ahadi hii si ahadi ya kweli. Wengine wanasema mashairi haya ni unabii na yanaonyesha namna matukio haya yatafuatana. Lakini ulizo hili halina maana, kwa sababu taifa la Israeli hawakutubu, na Bwana hakurudi.

Shairi 21 linaonyesha wazi kwamba **Mungu** alijua mbele ya kuwa taifa la Israeli watakataa Kristo, na muda huu wa neema utatangulia Kuja kwake kwa pili. **Ilikuwa lazima kwa Kristo kupokewa mbinguni kufika wakati wa kutengenezwa kwa maneno yote. Wakati wa kutengenezwa kwa maneno yote** unatazamia utawala wa Kristo kwa miaka elfu moja. Watu wengine wamesema ni wakati wa wokovu wa watu wote, lakini mafundisho haya hayapatani na mafundisho ya Biblia. Wakati ule unatazamia saa viumbe vyote vitakapofunguliwa toka utumwa wa ubovu na Kristo atatawala na haki kama Mfalme wa dunia nzima.

**Manabii** ya Agano la Kale walikuwa wametabiri juu ya **wakati wa kutengeneza** maneno yote.

Watu wamejaribu kutumika na shairi 21 kufundisha kwamba Kanisa halitakwenda mbinguni mbele ya muda wa Mateso. Wanasema kama ni lazima kwa mbingu kupokea Yesu kufika mwanzo wa utawala wake wa miaka elfu moja, hataweza kurudi mbele ya saa ile kupeleka kanisa mbinguni. Jibu kwa mawazo haya ndilo ya kwamba Petro alikuwa akisema na watu wa Israeli (sh.12). Alikuwa akisema juu ya namna Mungu atakavyotendea Israeli kama taifa. *Kwa maneno ya taifa la Israeli* Bwana Yesu atabaki mbinguni kufika wakati atakaporudi kutawala kwa mwisho wa muda wa Mateso. Lakini Wayuda mmoja mmoja wanaomwamini kwa muda wa Kanisa watashiriki pamoja na waamini Mataifa wakati Kanisa litakapopelekwa. Neno hili lingeweza kutokea wakati wo wote. Na vilevile wakati Kanisa litakapopelekwa, Bwana hataondokea mbingu; sisi tutakwenda kwake katika mawingu.

**3:22** Kama mfano wa unabii ndani ya Agano la Kale uliotazamia utawala wa utukufu wa Kristo, Petro alitaja Torati 18:15,18,19. Mashairi haya yanaonyesha Bwana Yesu kama **Nabii** wa Mungu kwa muda wa usitawi wa Israeli, akitangaza mapenzi na sheria ya Mungu.

Wakati Musa aliposema, **"Bwana Mungu atawanyanyulia ninyi Nabii kama mimi,"** hakufikiri Nabii huyu atakuwa kama yeye mwenyewe kwa akili na mwenendo, lakini kwamba atanyanyuliwa na Mungu namna yeye Musa alivyonyanyuliwa naye. "Atamnyanyua Yeye namna alivyoninyanyua mimi." Wao wawili *walinyanyuliwa na Mungu.*

**3:23** Wakati Kristo atakapotawala

duniani, watu wote watakaokataa **kusikia** na kumtii **watapotea na kuharibiwa.** Na kwa wakati wa sasa vilevile watu ambao wanamkataa watahukumiwa vivyo hivyo kwa milele, lakini mafundisho makubwa ya shairi 23 ni ya kwamba siku ile Kristo atatawala na fimbo la chuma na ya kwamba wale ambao wanamwasi na kumkataa watauawa mara moja.

**3:24** Kwa kutia nguvu kwa masemo yake juu ya wakati wa kutengenezwa kwa maneno yote, Petro aliongeza kwamba **manabii wote tangu Samweli** walihubiri habari za **siku hizi.**

**3:25** Halafu Petro alikumbusha wasikiaji Wayuda kwamba walitolewa ahadi hii ya nyakati za baraka kwa sababu walikuwa **wana wa manabii** na wazao wa Abrahamu. **Mungu alikuwa amefanya agano na Abrahamu** kubariki **makabila yote ya dunia** katika **uzao** wake. Ahadi zote za baraka za muda ule wa miaka elfu moja zina msingi wao ndani ya **Uzao** huyu, ndiye Kristo. Hivi iliwapasa kupokea Bwana Yesu kama Masiya sasa.

**3:26** Lakini **Mungu** alikuwa **amefufua Mtumishi wake** (3:13), na **kumtuma** kwanza kwa taifa la Israeli. Shairi lile linasema juu ya kuzaliwa kwa Yesu duniani, si juu ya ufufuko wake. Kama wangempokea **angegeuza kila mmoja wao toka maovu yake.**

Tunaona kwamba ndani ya hotuba yake kwa Waisraeli Petro alisema zaidi juu ya *ufalme,* si juu ya *kanisa*. Roho ya Mungu alikawia na uvumilivu na rehema, akisihi watu wa Mungu wa zamani kupokea Bwana Yesu mtukufu kama Masiya, na hivi kuharakisha kufika kwa ufalme wa Kristo duniani.

Lakini Waisraeli walikataa kusikia.

### F. Mateso na kuongezeka kwa kanisa (4:1 – 7:60)

**4:1-4** Kanisa jipya lilikuwa karibu kupata mateso mara ya kwanza. Kama mbele, mateso haya yalitoka kwa viongozi vya Israeli kwa maneno ya dini. **Makuhani na mkubwa wa hekalu, na Wasadukayo** walitokea kushindana na mitume.

Mwalimu mmoja, jina lake Scroggie anatuleta kufikiri kwamba **makuhani** wanatufikirisha juu ya kutokuvumilia kwa maneno ya dini, **mkubwa wa hekalu** juu ya uadui wa serikali, na **Wasadukayo** juu ya kutokuamini. **Wasadukayo** walikataa mafundisho ya ufufuko, na walishindana na mitume kwani **ufufuko** ulikuwa kama msingi wa mahubiri yao!

Viongozi hawa walichukizwa kwa sababu mitume walikuwa wakifundisha watu; walifikiri neno hili lilikuwa ruhusa yao tu. Walikasirika vilevile kwa sababu walikuwa wakihubiri **ufufuko *toka* wafu unaopatikana kwa Yesu.** Kama **Yesu alifufuliwa toka wafu**, mafundisho ya Wasadukayo yalionyeshwa kuwa uwongo.

Watu wengi wanafikiri kwamba kwa mwisho wa dunia watu wote watafufuliwa, lakini mawazo haya si kweli. Ona ya kwamba ndani ya shairi 2 mitume walihubiri **ufufuko *toka* wafu**. Shairi hili na mashairi mengine vilevile yanasema juu ya *ufufuko toka wafu*, hivi tunaona ya kwamba watu wengine watafufuliwa, lakini wengine (wasioamini) watabaki kaburini kwanza kwa wakati.

Kwa sababu ilikuwa karibu saa tisa ya mangaribi wakati kiwete aliponyeshwa, viongozi waliagiza mitume kufungwa kwanza kufika asubui.

Lakini hata kama wakubwa hawakufurahi hata kidogo, watu wengi sana waligeuka kwa Bwana. Karibu wanaume (*andres*, ndio wanaume kwa Kiyunani) **elfu tano** waliamini. Walimu hawajui kama wengine wa watu wale ndio watu 3000 waliookolewa wakati wa Pentekote. Wanawake na watoto hawakuwa ndani ya hesabu hii.

**4:5,6 Kesho yake** wakubwa wa

dini, waliojulikana kama Baraza, walikusanyika na kusudi la kulazimisha mitume kuacha kufanya matendo haya ya kuchukiza katikati ya watu. Hawakuweza lakini walifungua njia kwa mitume kushudia Kristo tena!

Pamoja na **watawala, wazee na waandishi** wao walikuwa

1. **Ana, kuhani mkubwa** – Bwana Yesu aliletwa mbele yake. Alikuwa kuhani mkubwa mbele, lakini kwa heshima walikaa kumwita kuhani mkubwa.
2. **Kayafa**, mume wa binti ya Ana, aliyeongoza kuhukumiwa kwa Bwana.
3. **Yoane na Alesandura** – hatujui kama walikuwa nani.
4. Wote **waliokuwa wazao wa jamaa ya kuhani mkubwa.**

**4:7** Wakisimamisha mitume mbele yao, walianza na kuwauliza kama **kwa nguvu gani, au kwa jina la nani** walikuwa wamefanya ajabu hili. Hii ni mara ya tatu **Petro** aliyopata njia kushuhudia Kristo na kuhubiri Habari Njema mbele ya viongozi vya dini naye alifanya hivi bila woga.

**4:8-12** Kwanza aliwakumbusha ya kwamba hawakufurahi kwa sababu mitume walikuwa **wametendea mema** mwenye kilema huyu **asiyeweza kujisaidia mwenyewe.** Petro hakusema hivi, lakini yule aliyeponyeshwa aliomba kupewa mali kwa lango la hekalu, na wakubwa hawakuweza kumponyesha. Halafu mtume aliwashitusha kabisa wakati alipotangaza **kwa jina la Yesu … ambaye walimsulibisha,** mtu huyu aliponyeshwa. **Mungu** alikuwa **amefufua** Yesu **toka wafu**, na ni kwa uwezo wake ajabu hili lilifanywa. **Yesu** hakuwa na nafasi ndani ya makusudi ya Wayuda, hivi **walimkataa na kumsulibisha**. Lakini **Mungu alimfufua toka wafu** na kumtukuza mbinguni. Hivi **Jiwe hili lililokataliwa** liliwekwa kuwa **jiwe kubwa la pembeni**, jiwe lililohitajiwa kabisa kumaliza jengo. Na kweli yeye ni ya lazima na anahitajiwa kabisa. Hakuna **wokovu** bila yeye. Hakuna Mwokozi mwingine. Wala **hakuna jina lingine chini ya mbingu walilopewa watu tupate kuokolewa nalo.**

Wakati tunaposoma mashairi 8-12, tukumbuke kwamba maneno haya yalisemwa na mtu yule aliyekana na kulaani Bwana mara tatu mbele.

**4:13** Ni nguvu kwa watu wa elimu na dini wanaokosa imani ya kweli kufahamu kazi ambayo mahubiri ya Habari Njema inafanya ndani ya roho za watu. Walifazaika namna gani wahubiri hawa **wasio na elimu, wenye ujinga** waliweza kuamsha roho za watu, ndilo neno wao wenyewe hawakuweza kufanya.

> *Katika Agano Jipya hakuna tofauti katikati ya wenye daraja kanisani* kama maaskofu, mapadre, vivi hivi, na watu wasio mapadre wala wasio na maarifa fulani kwa kazi fulani kanisani. Tofauti hii ilianzwa na Wakatoliki zamani. John Huss, Mkristo wa inchi ya Czechoslovakia, alishindana sana na maneno haya, na alifundisha na hata kutoa uzima wake kwa kweli ya kwamba waamini wote wa kweli ni makuhani. Ni kweli hii ya kwamba waamini wote ni ukuhani wa kifalme na kwamba kila mwamini alishuhudia kweli hii iliyokuwa uwezo ulioendesha Kanisa kwenda mbele. Bila vitu vyote tulivyo navyo sasa kwa kazi ya kutangaza Habari Njema, Habari Njema ya neema ya Mungu ilitetemesha ufalme mzima, na kulikuwa na watakatifu (ndio waamini) hata nyumbani wa Kaisari. [4]

Watu wa Baraza walishangaa juu ya **uhodari wa Petro na Yoane**. Wangalitaka kuwaona bure kama wavuvi wajinga wa Galilaya. Lakini ndani ya maisha ya mitume hawa waliona wenye kujitawala wenyewe, maisha yaliyopewa uwezo, na uhodari ambao uliwafikirisha Yesu wakati aliposimama

mbele yao kuhukumiwa. Walitambua ya kwamba **walikuwa pamoja na Yesu** mbele, lakini elezo la kweli ndilo ya kwamba walijazwa na Roho Mtakatifu *sasa*.

**4:14-18** Na midomo yao ilifungwa wakati walipoona mtu huyu aliyeponyeshwa akisimama pamoja na mitume. Hawakuwa na njia kubisha kwamba ajabu hili limefanyikana.

J. H. Jowett aliandika:

> Labda watu wa dunia wanaweza kukushinda na mabishano yao na elimu yao. Lakini hawawezi kushinda ushuhuda wa maisha ya mtu anayekwisha kukombolewa. "Wakiona yule mtu aliyeponyeshwa akisimama pamoja nao, hawakuweza kujibu neno." [5]

Wakitaka kufanya shauri kama watafanya nini juu ya maneno haya, waliagiza Petro na Yoane kutoka kwanza kwa saa ndogo. Hawakuweza kuazibu mitume kwa sababu ya kutenda mema, lakini kama wasipowazuiza kukaa kufanya hivi, dini yao wenyewe itapata hasara kwa sababu hesabu ya wafuataji wao itapunguka sana. Basi walikataza Petro na Yoane wasiseme na watu mmoja mmoja juu ya **Yesu**, wala kuhubiri habari zake katikati ya watu.

**4:19, 20 Petro na Yoane** hawakukubali kuzuizwa hivi wasitangaze habari za Mwokozi. Kazi yao ya kwanza ilikuwa kutii **Mungu**, si mtu. Ingalipasa watawala kukubali neno hili. Mitume walikuwa wameona ufufuko na kupanda kwa Kristo. Walikuwa wamesikia mafundisho yake kila siku. Ilikuwa kazi yao kushuhudia Bwana na Mwokozi wao Yesu Kristo.

**4:21, 22** Uzaifu wa watawala ulionekana wazi kwa sababu hawakuweza kuazibu mitume; **watu wote** walijua habari za ajabu hili la neema lililokwisha kufanyikana. Walijua mtu huyu aliyekuwa na miaka **kupita makumi ine** kwa sababu taabu yake ilikuwa imeonekana wazi mbele ya watu kwa miaka mingi. Hivi watu wa Baraza waliweza kuonya na kuogopesha mitume tu na kuwafungua.

**4:23** Nyuma ya **kufunguliwa** na watawala, mitume walifikia waamini **wenzao** mara moja. Tangu zamani neno moja linaloonyesha hali ya roho ya Mkristo ni kama ushirika na upatano wake ni pamoja na watu gani.

**4:24-26** Wakati waamini walipokwisha **kusikia** habari za maneno yaliyokwisha kutokea, walisifu Mungu Mwumba wa vitu **vyote** (na aliye mkubwa kupita viumbe hivi waliokuwa wakishindana na kweli yake sasa). Walitumika na masemo ya **Daudi** ndani ya Zaburi 2 juu ya kushindana kwa serikali na **Kristo wake**. Zaburi hii inatazama mbele kwa wakati Kristo atakapokuja na kusimamisha ufalme wake, na wakati wafalme na watawala watakapojaribu kuzuiza kusudi lake. Lakini Wakristo hawa wa kwanza walifahamu ya kwamba maneno ambayo yaliwapata yalifanana na habari zile. Walionyesha uzuri wa hali yao ya roho kwa namna waliweza kuingiza mashairi ya Maandiko Matakatifu ndani ya maombi yao.

**4:27, 28** Pale katika Yerusalema Waroma na Wayuda walikuwa **wamefungana pamoja** juu ya **Mwana Mtakatifu** wa *Mungu,* ndiye **Yesu**, Herode kama mjumbe wa Wayuda, na Pilato kwa Mataifa. Lakini shairi 28 linatushangaza. Tungefikiri tutasoma ya kwamba watawala hawa walikusanyika pamoja kufanya neno lo lote mioyo yao miovu ilikusudi kufanya. Sivyo. Tunasoma walikusanyika **watimize yote kama mkono wa** *Mungu* **na mapenzi yake yalivyokusudi tangu zamani yatokee.** Matheson anaeleza:

> Kwa njia ya shauri lao ku*shindana* na mapenzi ya Mungu waliya*saidia* ... Walikutana pamoja kupiga vita na Kristo, lakini hawakufahamu ya kwa-

mba kwa njia ya kufanya hivi walimtukuza sana … Mungu wetu hashindi vita vya watu, lakini anatumika nazo kwa utukufu wake.

**4:29, 30** Nyuma ya kuonyesha wazi imani yao ya kwamba Mungu atashinda, Wakristo hawa waliomba maneno matatu:

1. **Tazama maogopesho yao.** Hawakusema na Mungu kama ilimpasa kuazibu watu hawa waovu.
2. **Uwape watumishi wako nguvu.** Hawakuwaza juu ya kukaa bila hatari wao wenyewe, lakini juu ya kuhubiri Neno la Mungu bila woga.
3. **Ukinyosha mkono wako kuponyesha**. Wakati Habari Njema ilipohubiriwa kwanza ilithibitishwa na Mungu kwa njia ya **alama na maajabu** yaliyofanywa **kwa jina la ... Yesu.** Wanafunzi waliomba Mungu kukaa kuthibitisha utumishi wa mitume kwa njia hii.

**4:31** Wakati walipomaliza maombi, pahali walipokusanyika palitikiswa. **Wao wote walijaa Roho Mtakatifu**, ndilo neno lililoonyesha kwamba walikuwa wakitii Bwana na kujitoa kwake. Waliendelea **kusema Neno la Mungu pasipo woga,** kama walivyoomba katika shairi 29.

Tunasoma mara saba ndani ya kitabu cha Matendo juu ya watu wakijaa au kujazwa Roho Mtakatifu, kwa makusudi mbalimbali:

1. Kwa kusema (Mdo. 2:4; 4:8; na hapa).
2. Kwa kutumikia (Mdo. 6:3).
3. Kwa kulinda waamini (Mdo. 11:24).
4. Kwa kukemea (Mdo. 13:9).
5. Kwa saa ya kufa (Mdo. 7:55).

**4:32-35** Wakati mioyo ya watu inapojaa na mapendo kwa Kristo, wanapendana na wenzao vilevile. Walionyesha kwamba walikuwa moja ndani ya Kristo kwa njia ya kushiriki mali na vitu vyao na wenye mahitaji katikati yao, na walikuwa na vitu vyote kwa ushirika. Wakati kulipokuwa na **hitaji** waliuza **mashamba au nyumba** na kuleta **mal**i **yenyewe** kwa mitume kwa kugawa. Ona ya kwamba **waliigawa** tu kwa wakati wa **hitaji fulani**; hawakuigawa kwa watu wote sawasawa kwa saa moja.

F. E. Marsh alisawanisha Kanisa kwa wakati wa mwanzo wake na Ukristo wa wakati wa sasa hivi:

> “Ni huzuni kufikiri, kama mhubiri Luka angaliandika habari za Ukristo wa sasa ingalimpasa kugeuza masemo katika Mdo. 4:32-35 hivi: ... “Na wengi wa watu walioamini walikuwa na mioyo migumu na roho kama mawe, na kila mtu alisema kwamba vitu vyake ndivyo vyake mwenyewe tu, na walikuwa na vitu vyote vya sasa nyumbani mwao. Na uwezo mkubwa walishuhudia uzuri wa dunia hii, nao wote walijifikiri wenyewe tu. Wengi wao walikosa mapendo, maana wengi waliokuwa na mashamba walinunua mashamba mengine; mara nyingine walitoa mali nusu kusudi majina yao yachapwe ndani ya journaux waweze kusifiwa kwa mali ambayo walikwisha kutoa.”

Kuna uwezo wa siri ndani ya maisha ya watu ambao wanajitoa mzima kwa Bwana. Hivi hatushangai kusoma ndani ya shairi 33 kwamba **“Na mitume walishuhudia ufufuko wake Bwana Yesu kwa nguvu nyingi. Neema kubwa ikakuwa juu yao wote.”** Ni kama wakati Mungu anapoona watu walio tayari kutia mali yao mikononi mwake, anawawezesha kumshuhudia na utamu na uwezo zaidi.

Watu wengi wanafikiri kwamba watu wa sasa hawahitaji kuiga waamini wa kwanza kwa namna walivyoshiriki mali yao na wenye mahitaji. Mawazo haya yanaonyesha umasikini wa roho yao. Kama tungalijazwa na uwezo wa Pentekote, matunda ya Pentekote yangalionekana ndani ya maisha yetu vilevile.

Ona maalama mawili ya kanisa bora ndani ya shairi 33 – **nguvu nyingi** na **neema kubwa.** Vance Havner alitaja maalama mane mengine: woga mkubwa (Mdo. 5:5, 11); mateso makubwa (8:1); furaha kubwa (Mdo. 8:8; 15:3); hesabu kubwa ya watu walioamini (Mdo. 11:21).

**4:36,37** Mashairi haya yanatufikisha kwa mwanzo wa sura 5. Ukarimu wa **Barnaba** ulikuwa namna nyingine na unafiki wa Anania (Mdo. 5:1). **Yosefu** alikuwa **Mlawi aliyeitwa Barnaba na mitume**. Haikuwa desturi kwa Walawi kuwa na mashamba kwani Bwana aliwalinda kwa njia nyingine. Hatujui kama alipata shamba namna gani au kwa sababu gani, lakini tunajua mapendo makubwa sana yalisukuma **mwana huyu wa faraja kuuza shamba** hili na **kuweka feza yenyewe kwa miguu ya mitume.**

**5:1-4** Wakati Mungu anapotumika na uwezo, **Shetani** ni palepale kushindana, kuzuiza na kuharibu kazi yake. Lakini wakati watumishi wake wanapojazwa na Roho Mtakatifu, unafiki na udanganyifu zitafunuliwa mbio.

Ni kama **Anania** na **Safira** waliona ukarimu wa Barnaba na watu wengine. Labda walitaka kupokea sifa toka watu kama wakifanya vivyo, hivi **waliuza sehemu ya vitu vyao** na walileta nusu ya mali waliyopata kwa mitume. Walifanya zambi wakati walipotenda sawasawa walitoa mali yote waliyopata kwa kitu walichouza, lakini walitoa nusu yake tu. Hakuna mtu aliyesema nao kuuza kitu chao. Na **nyuma ya kukiuza**, hawakulazimishwa kutoa mali yote ambayo walipata, lakini walitenda sawasawa walileta yote, pamoja na kuchunga nusu yake kwa mahitaji yao wenyewe.

**Petro** alishitaki **Anania** juu ya kusema uwongo **kwa Roho Mtakatifu**, si **kwa watu**. Wakati aliposema uwongo **kwa Roho Mtakatifu** alisema uwongo kwa Mungu, kwa sababu **Roho Mtakatifu** *ni* **Mungu.**

**5:5,6 Anania** akisikia mashitaki haya **alianguka, akakufa, vijana** wakabeba maiti yake kwa kuizika. Ilikuwa hukumu ya kuogopesha toka Mungu kwa kanisa hili jipya. Hukumu hii haikuondosha wokovu wa Anania na kumwondolea uzima wake wa milele, lakini ilionyesha huzuni na kasirani ya Mungu juu ya zambi hii ya kwanza iliyotokea katika kanisa lake takatifu.

**5:7-11 Nyuma ya karibu saa tatu** Safira alitokea, na **Petro** alimshitaki juu ya kupatana na mume wake kujaribu **Roho ya Bwana**. Alimjulisha nini iliyopata mume wake, na ya kwamba yeye atakufa vivyo hivyo. Safira alianguka **mara moja**, akakufa, na walimbeba inje kumzika.

Namna Petro alivyoweza kuhukumu Anania na Safira ni mfano wa uwezo wa kutenda maajabu ambao mitume waliopewa. Labda ulitimiza ahadi ya Bwana Yesu, "Wo wote mukiwafungia zambi, zinafungwa kwao" (Yn. 20:23). Vivyo hivyo tunaona uwezo wa Paulo kutoa kwa Shetani Mkristo aliyetembea katika zambi ili mwili wake uharibiwe (1 Kor. 5:5). Watu hawakupewa uwezo huu nyuma ya muda wa mitume.

Hatushangai kusoma kwamba woga mkubwa ulipata kanisa zima, na wote waliosikia habari za mauti ya watu hawa wawili.

**5:12-16** Nyuma ya kufa kwa Anania na Safira **mitume** walikaa kufanya maajabu katikati ya watu waliokuwa wamekusanyika kwa **baraza ya Solomono**. Uwezo wa Mungu ulionekana wazi sana katikati yao hata watu wengine hawakuungana nao mbio na kukiri kupokea Mwokozi. Hata hivi **waliheshimu mitume sana,** na watu wengi **waliamini** Bwana Yesu. **Watu** walibeba **wagonjwa wao inje kwa njia juu ya vitanda** na mikeka ili **kivuli cha Petro kiweze kufikia wengine** katikati

yao wakati alipopita njiani. Uwezo wa Mungu ulionekana wazi ndani ya maisha ya mitume, na ya kwamba alitumika nao kubariki watu wengine. Makutano walikuja toka miji kandokando ya Yerusalema, wagonjwa na wenye pepo wachafu, na **waliponyeshwa wote.**

Waebrania 2:4 linaonyesha wazi ya kwamba Mungu alitumika na maajabu haya kushuhudia kazi ya mitume. Wakati kuandika kwa Agano Jipya kulipokwisha, **maajabu** haya hayakuhitajiwa tena. Vizuri tuone ya kwamba watu **wote** walioletwa kwa mitume **waliponyeshwa.** Kwa wakati wa sasa watu wengine wanaongoza "makusanyiko makubwa kuponyesha watu kwa imani," lakini hawaponyeshi wote wanaofikishwa kwao!

**5:17-20** Utumishi kwa uwezo wa Roho unazaa matunda namna mbili kila mara: Watu wengine wanapata uzima wa milele, na wengine wanageuka watesaji wakali wa Wakristo na adui za Habari Njema. Ilitokea hivi hapa katika Matendo. **Kuhani mkubwa** (tunafikiri alikuwa Kayafa) na rafiki zake Wasadukayo walikasirika sana kwa sababu wanafunzi hawa wa Yesu walikuwa na uwezo mkubwa katikati ya watu. Waliogopa kwamba uwezo wao wenyewe kama viongozi vya pekee vya watu kwa maneno ya dini utapunguka, na walizarau mafundisho yao juu ya ufufuko wa mwili, ndiyo mafundisho waliyokana kabisa.

Hawakuweza kushinda **mitume** ila kwa njia ya nguvu, hivi waliagiza wafungwe na kuwekwa gerezani. **Usiku ule malaika wa Bwana** aliwaleta inje ya **gereza**, akawaagiza kurudia **hekalu** na **kuwaambia watu maneno yote ya uzima huu**. Luka alipasha habari hizi za ajabu ya **malaika** bila kushangaa na hatusomi kwamba mitume walishangaa vilevile.

**Malaika** aliita imani ya Wakristo **uzima huu**. Si kanuni za imani na maagizo fulani, lakini *Uzima* – **uzima** wa ufufuko wa Bwana Yesu unaoletwa kwa watu wote ambao wanamwamini.

**5:21** Kwa mapambazuko mitume walikuwa wakifundisha **hekaluni.** Saa yenyewe **kuhani mkubwa** alikutana na watu wa **Baraza (wazee wote)** na walingoja kwa wafungwa **waletwe** toka gereza.

**5:22-25** Lakini **watumishi** hawakuleta wafungwa! Walifika na habari ya kwamba maneno yote kwa **kifungo** yalikuwa taratibu – lakini wafungwa hawakuwa ndani! **Milango** ilifungwa vizuri na **walinz**i walisimama kwa pahali pao, lakini kifungo kilikuwa tupu. Zilikuwa habari za kuwasumbusha kabisa! **Mlinzi wa hekalu na wakubwa wa makuhan**i walifazaika kama mambo haya yatakoma namna gani. Halafu mjumbe alifika na habari kwamba wafungwa walikuwa **hekaluni** tena kama mbele na walikuwa **wakifundisha watu!** Tunawaheshimu kwa uhodari wao, na ingetupasa sisi kuiga mitume wale kwa mwanzo wa kanisa na kusimama na nguvu kwa maneno tunayoamini, hata kama tukipata mateso.

**5:26 Watumishi** hawakuleta mitume kwa **nguvu. Waliogopa watu** watawatupia mawe kama wakitendea wafuata hawa wa Yesu kwa ukali, kwa sababu **watu** waliwaheshimu sana.

**5:27, 28 Kuhani mkubwa** alisema kwa ajili ya watu wa Baraza: **"Hatukuwaamuru ninyi kwa nguvu musifundishe kwa jina hili?"** Hakutaja jina la Bwana Yesu Kristo na kusudi. **"Mumejaza Yerusalema na mafundisho yenu."** Hata kama hakukusudi kufanya hivi, semo lake lilikuwa sifa kwa utumishi wa mitume. **"Munataka kuleta damu ya mtu huyu juu yetu."** Lakini viongozi vya Wayuda walikuwa wamefanya hivi mbele wakati walipolalamika, "Damu yake iwe juu yetu na juu ya watoto wetu" (Mt. 27:25).

**5:29-32** Mitume waliomba mbele

wapewe uhodari kusema maneno ya Mungu bila woga. Sasa, na uhodari toka juu, walisema kwamba imewapasa **kutii Mungu kuliko watu.** Walisema wazi ya kwamba **Mungu alifufua Yesu ambaye** Waisraeli walikuwa **wamemwua** kwa njia ya **kumtundika juu ya mti**, lakini ya kwamba **Mungu alikuwa amemtukuza kwa mkono wake wa kuume … Mkubwa na Mwokozi,** naye alikuwa **tayari kuwapa Waisraeli toba na usamehe wa zambi.** Nao, mitume **walikuwa washuhuda wa maneno haya, pamoja na Roho Mtakatifu, ndiye Mungu amewapa wote ambao wanamtii** kwa njia ya kuamini Mwana wake.

Wakati **Mungu** aliposema juu ya ku**fufua Yesu** (sh. 30), labda alisema juu ya kuzaliwa kwa **Yesu** kama mtu, au juu ya ufufuko wake toka wafu. Tunafikiri maana yake hapa ni kwamba alisema juu ya kuzaliwa kwake kuwa **Mwokozi.**

**5:33-37** Mitume walisema maneno haya na nguvu na uwezo kabisa, hata **watawala walifanya shauri kuwaua**. Lakini Gamalieli alikuwa na neno la kusema. Alikuwa mmoja wa walimu (rabi) wenye heshima zaidi wa Waisraeli na **mwalimu** wa Saulo wa Tarso. Masemo yake hayaonyeshi kwamba alikuwa Mkristo au kama alisimamia Wakristo. Yalikuwa masemo ya akili ya dunia tu.

Nyuma ya kuagiza **mitume** kutoka chumbani kwanza, alikumbusha watawala wa Wayuda kwamba mambo haya yasipotoka kwa Mungu, yatakufa bure nyuma kidogo. Alitaja habari za watu wawili: 1) **Teuda** alisema yeye ni mtu mkubwa na alikuwa na wafuata **karibu mia ine,** lakini aliuawa na wafuata wake walisambazwa. 2) Nyuma yake **Yuda Mgalilaya** alijaribu kukutanisha Wayuda kuasi serikali; yeye **vilevile aliuawa,** na wafuata wake **walisambazwa.**

**5:38, 39** **Kama** dini hii ya Wakristo isipotoka **kwa Mungu,** vizuri waiache tu, nayo itakufa nyuma kidogo. (Lakini neno hili si kweli kila mara. Chama nyingi za watu wasiofuata Mungu hata kidogo zimesitawi kwa mia za miaka na kupata wafuata wengi kupita wale wanaoshika kweli. Hata hivi kwa wakati unaopendeza Mungu zitakufa vile.)

Gamalieli alikaa kusema **kama** mambo haya yakitoka **kwa Mungu,** hawataweza **kuyashinda,** na wataonekana kuwa wenye **kupigana na Mungu.**

**5:40** Watawala walikubali masemo yake, hivi **waliita mitume,** wakaagiza **wapigwe,** wakawaamuru **wasiseme kwa jina la Yesu; wakawaacha kwenda zao.** Mapigo haya hayakuwa haki hata kidogo; yalionyesha kasirani tu ya watu waliokwisha kufunga mioyo yao kwa kweli ya Mungu. Na agizo la watawala kwa mitume waache kuhubiri kwa **jina la Yesu** lilikuwa bure kabisa.

Hivi Shetani alishindwa tena.

**5:41, 42** Kupigwa kwa mitume kulizaa matunda mawili: 1) Walifurahi sana sana kwa sababu **wamehesabiwa kama wamestahili kupata mateso kwa ajili ya jina la Yesu**. 2) Kuliongeza bidii yao kuhubiri Habari Njema, na **kila siku**, **ndani ya hekalu**, na katika nyumba zao, hawakuacha **kufundisha na kuhubiri Habari Njema ya Yesu Kristo.**

## MAFUNDISHO JUU YA MKRISTO NA SERIKALI

Wakati Wakristo wa kwanza walipoendelea kutangaza Habari Njema walikutana na mazuizo na uadui kupita na kupita toka serikali, zaidi toka viongozi vya dini walioshiriki sana na serikali kwa wakati ule. Waamini walikuwa tayari kwa neno hili.

Ilikuwa desturi yao kuheshimu na kutii watawala wao kwa sababu walichaguliwa na Mungu, nao ni watumishi wa Mungu kuendesha mambo yote vizuri. Hivi wakati Paulo kwa ujinga alipohamakia kuhani mkubwa, na ali-

hamakiwa juu ya neno hili, aliomba usamehe mara moja, akitaja Kutoka 22:28, “Usilaani mkubwa wa watu wako” (Mdo. 23:5).

Lakini wakati sheria za watu isipopatana na maagizo ya Mungu, Wakristo waliasi sheria za serikali na walikuwa tayari kupata azabu kama ikihitajiwa. Kwa mfano, wakati Petro na Yoane walipokatazwa kuhubiri Habari Njema, walijibu, “Kama ni haki mbele ya Mungu kuwasikiliza ninyi kuliko Mungu, hukumuni ninyi wenyewe; maana sisi hatuwezi kuacha kusema maneno tuliyoona na kusikia” (Mdo. 4:19, 20). Na wakati Petro na mitume waliposhitakiwa kwa sababu waliendelea kufundisha kwa jina la Kristo, Petro alijibu, “Imetupasa kutii Mungu kuliko watu” (Mdo. 5:29).

Hatusomi hata mara moja ya kama walikusudi kupindua serikali au kufungana na watu wengine waliotaka kufanya hivi. Hata kama walipata mateso walitaka watawala wao kubarikiwa tu (Mdo. 26:29).

Wala hawakutenda uzalimu kamwe kujipatia faida toka serikali kwa njia ya kulipa rushwa. Kwa mfano liwali Feliki alingoja bure kupokea rushwa toka Paulo (Mdo. 24:26).

Wakiwa wenyeji wa inchi, maneno mengine yalikuwa haki yao, na mambo haya hayakuharibu ushuhuda wao kwa Kristo. Ona Mdo. 16:37; 21:39; 22:25-28; 23:17-21; 25:10,11).

Lakini hawakushiriki ndani ya kazi ya serikali ya dunia hii. Kwa nini? Hatusomi jibu, lakini tunajua kwamba bidii yao ya pekee ilikuwa kuhubiri Habari Njema ya Kristo. Walijitoa kwa kazi hii bila kukubali mazuizo. Bila shaka waliamini kabisa kwamba Habari Njema ndilo jibu kwa mashaka na maneno magumu yote ya watu, na ya kwamba utawala wa serikali haukuweza kusaidia. ❖

**6:1** Kama Shetani asipoweza kuharibu ushuhuda wa Wakristo toka inje, atajaribu kuleta magawanyiko ndani ya kanisa. Tunaona neno hili ndani ya mashairi yanayofuata.

Kwa wakati wa mwanzo wa kanisa ilikuwa desturi ya kila siku kusaidia na mali wajane masikini wasiosaidiwa na njia nyingine. Wengine wa waamini Wayuda waliosema kwa Kiyunani walinungunika **kwa sababu wajane wao** hawakutendewa sawasawa na wajane wa **Waebrania** (wale toka Yerusalema na Yudea).

**6:2,3** Ukubwa wa kanisa ulikaa kuongezeka, na mitume **kumi na wawili** walifahamu lazima wasimamishe utaratibu kwa kuangalia na kuchunga maneno namna hii. Wao wenyewe hawakutaka kupunguza kazi yao ya **kufundisha Neno la Mungu** kwa kuchunga maneno ya mali, hivi walisema vizuri kanisa wachague **watu saba** wenye ushuhuda mzuri waliojaa Roho Mtakatifu na akili na kuwaweka juu ya kazi hii kanisani.

Watu hawa hawakuitwa watumishi ndani ya Biblia, lakini tunaweza kufikiri juu ya kazi yao kama ile ya watumishi. Kuna mafundisho mengine juu yao ndani ya 1 Timoteo 3:8-13.

**6:4** Halafu mitume wataweza **kudumu** katika **kuomba na kuhubiri Neno**. Ona ya kwamba **maombi** ni kwanza, mbele ya **kuhubiri Neno**. Sharti tuseme na Mungu juu ya watu mbele ya kusema na watu juu ya Mungu.

**6:5, 6** Majina ya wanaume saba waliochaguliwa yanatufahamisha kwamba zaidi yao walikuwa Wayuda wenye lugha ya Kiyunani mbele ya kuokolewa, kama vilevile watu wale waliokuwa na manunguniko. Hawatakuwa na njia kunungunika tena. Neno hili linaonyesha neema na mapendo ya Mungu ndani ya roho za mitume yaliyoshinda roho za kujifikiri wenyewe tu mioyoni mwa watu.

Tunajua habari za wawili tu wa watumishi hawa – **Stefano,** mtu wa kwanza

kanisani aliyeuawa kwa sababu ya imani yake; na **Filipo,** mhubiri aliyefikisha Habari Njema kwa Samaria, aliyeongoza towashi ya Etiopia kuamini Kristo, na aliyepokea Paulo nyumbani mwake kwa Kaisaria.

Nyuma ya kuomba, mitume walionyesha ushirika wao na watu wale saba waliochaguliwa na kanisa kwa njia ya **kuwawekea** mikono.

**6:7** Tukisoma shairi 7 pamoja na mashairi ambayo yanalitangulia ni kama kusimamishwa kwa watumishi kuchunga maneno ya mali ya kanisa kulisaidia kazi ya Habari Njema kuendelea mbele vizuri sana. Wakati **Neno la Mungu lilipoendelea,** hesabu ya **wanafunzi** ikaongezeka sana **katika Yerusalema**, na hata **makuhani Wayuda wengi** waligeuka wafuata wa Bwana Yesu.

**6:8** Sasa tunaanza kusoma zaidi juu ya mmoja wa watumishi hawa, ndiye **Stefano.** Mungu alitumika naye sana kufanya maajabu na kuhubiri Neno la Mungu. Yeye ni mtu wa kwanza tunayesoma habari zake katika Matendo asiyekuwa mtume aliyefanya maajabu na alama. Hatujui kwa sababu gani alipewa uwezo huu.

**6:9** Wayuda katika sunagogi hawakufurahi hata kidogo juu ya utumishi wa uwezo wa Stefano. Masunagogi yalikuwa pahali Wayuda walipokutana siku ya sabato kupokea mafundisho toka sheria. Yaliitwa na majina kupatana na majina ya watu waliokutana pale. Labda **Walibertino** walikuwa Wayuda waliofunguliwa na Waroma toka utumwa. Kurene ulikuwa mji katika Afrika, na ni kama Wayuda wengine toka pale walikuwa wamekaa kwa Yerusalema. Wayuda wa Alesanduria walitoka kwa bandari ya Misri iliyoitwa na jina hili. **Kilikia** ilikuwa wilaya kwa kusini kabisa ya Asia Ndogo. Ni kama jamii za Wayuda toka pahali pale pote walikuwa na masunagogi katika au karibu na Yerusalema.

**6:10-14** Wayuda hawa wenye bidii hawakuweza kushinda Stefano na maneno kwani alisema nao na hekima na uwezo wa Roho Mtakatifu. Wakitaka sana kumnyamazisha, **walishawishi** washuhuda wa uwongo kwa siri kushitaki Stefano kusema alitukana **Musa na Mungu.** Bado kidogo Stefano alisimama mbele ya Baraza akihukumiwa na kusema maneno ya kukufuru j**uu ya** hekalu na **juu ya torati**. Walimshuhudia na uwongo kusema kwamba Yesu alisema **ataharibu** hekalu na **kugeuza** desturi zote za sheria ambazo **Musa aliwapa** Waisraeli.

**6:15** Watu wa Baraza walisikia mashitaki haya, lakini wakati walipotazama Stefano **hawakuona** uso wa pepo mchafu lakini uso kama **uso wa malaika.** Waliona uzuri ambao unatushinda kufahamu wa maisha ya mtu ambaye alijitoa mzima kwa Bwana, mwenye bidii kabisa kutangaza Kweli, na aliyeweka roho juu ya kupendeza Mungu kupita juu ya masemo ya watu. Walitazama nusu ya utukufu wa Kristo ukionekana ndani ya uso wa mfuata wake mwaminifu.

Ndani ya sura 7 tunasoma ushuhuda wa Stefano. Alianza polepole na kukumbusha wasikiaji wake habari za historia ya Wayuda, akiendelea kusema zaidi juu ya watu wawili, Yosefu na Musa, waliosimamishwa na Mungu, waliokataliwa na Israeli, na nyuma waliotukuzwa kama waokozi. Stefano hakusawanisha wazi maneno ambayo yaliwapata na maneno yaliyopata Kristo, lakini ni wazi ya kwamba yalifanana. Mwishoni Stefano alishitaki viongozi vya Wayuda na ukali sana, akiwahukumu kwa sababu ya kushindana na Roho Mtakatifu, kuua Mwenye Haki, na kutokushika sheria ya Mungu.

Bila shaka Stefano alijua kwamba alikuwa akijihatarisha mwenyewe. Angaliweza kujiponyesha kwa njia ya kupunguza ukali wa masemo yake. Lakini alitaka kufa kupita kupunguza heshima na utukufu wa Bwana wake. Tunamheshimu kwa uhodari wake!

**7:1-8** Mashairi haya yanaturudisha kwa mwanzo wa taifa la Waebrania. Hatujui kwa sababu gani Stefano alisema maneno mengi juu ya historia ya Abrahamu. Labda alitaka:

1. kuonyesha kwamba alijuana na habari hizi na alipenda taifa la Israeli sana;
2. kuendelea na habari za Yosefu na Musa. Wao wawili walikuwa mfano wa kukataliwa kwa Kristo;
3. kuonyesha kwamba Abrahamu aliabudu Mungu vizuri, hata kama hakuabudu kwa pahali fulani tu. (Stefano alikuwa ameshitakiwa juu ya kusema maneno mabaya juu ya hekalu – "pahali hapa patakatifu.")

Habari kubwa ndani ya historia ya Abrahamu ndizo hizi:

1. Mungu alimwita wakati alipokuwa kwanza kwa inchi ya **Mesopotamia** (mash. 2, 3).
2. Safari yake kwenda **Harani**, na nyuma yake kwa Kanana (sh.4).
3. Ahadi ya Mungu kumpa Abrahamu inchi ile – hata kama Abrahamu mwenyewe hakupokea hata sehemu yake – hivi ilimpasa kununua pango la Makipela kuwa pahali pa maziko kwa jamaa yake (sh.5). Ahadi hii itatimizwa kwa wakati wa kuja (Ebr. 11:13-40).
4. Unabii kwamba Waisraeli watakuwa watumwa katika Misri, lakini watafunguliwa nyuma ya wakati (mash. 6, 7). Sehemu mbili zote za unabii huu zilitimizwa na watu waliokataliwa na taifa la Israeli: Yosefu (mash. 9-19); Musa (mash. 20-36). **Miaka mia ine** tunayoona ndani ya shairi 6 na katika Mwa. 15:13 inasema juu ya wakati Waisraeli walipoteswa katika Misri. Ndani ya Kutoka 12:40 na Gal. 3:17 tunasoma juu ya miaka 430 tangu Yakobo na jamaa yake walipofika katika Misri kufika kutoka kwao na kupokea sheria. Kwa miaka makumi tatu ya kwanza waliyokuwa katika Misri Waisraeli hawakuteswa; walitendewa na heshima.
5. **Agano la tohara** (sh. 8a).
6. Kuzaliwa kwa **Isaka, Yakobo,** kisha **baba wakubwa kumi na wawili** (sh. 8b). Mmoja wao alikuwa Yosefu aliyekuwa mmoja wa wana kumi na wawili wa Yakobo.

**7:9-19** Kuna mifano mingi ya Kristo ndani ya Agano la Kale, na **Yosefu** ni mmoja wa mifano wazi na ya damani zaidi. Bila shaka zamiri za Wayuda walioishi kwa wakati wa Kristo ziliwachoma sana wakati waliposikiliza Stefano akipasha habari za maisha ya Yosefu, na kukumbushwa namna walivyotendea Yesu wa Nazareti!

1. **Yosefu aliuzwa** na ndugu zake **kwenda Misri** (sh. 9).

2. Yule aliyekataliwa alinyanyuliwa kwa pahali pa uwezo na utukufu katika **Misri** (sh.10).

3. **Njaa** inchini mwa Kanana ilisukuma ndugu za Yosefu kwenda **Misri**, lakini hawakutambua ndugu yao (mash. 11, 12).

4. **Mara ya pili** ndugu zake walipofika Misri **Yosefu alijitambulisha kwao.** Halafu yule aliyekataliwa mbele aligeuka mwokozi wa jamaa yake (mash.13,14). Ona ya kama katika shairi 14 watu makumi saba na watano walitajwa, lakini watu makumi saba tu walitajwa katika Mwanzo 46:27. Stefano alitaja tafsiri ya Kiyunani ya Mwanzo 46:27, na Kutoka 1:5 iliyotaja makumi saba na watano. Tafsiri ya Kiebrania inataja makumi saba kwa sababu ya tofauti kwa namna ya kuhesabu watu wa jamaa ya Yakobo.

5. Kufa kwa jamaa ya Yosefu na kuzikwa kwao inchini mwa Kanana (mash. 15, 16). Kuna neno gumu lingine kueleza ndani ya shairi hili linalosema **Abrahamu alinunua** kaburi toka wana

wa **Hemora** katika Sekemu. Kwa Mwanzo 23:16, 17 tunasoma kwamba *Abrahamu* alinunua *pango la* Makipela katika Heburoni toka wana wa Heti. *Yakobo* alinunua sehemu ya inchi katika Sekemu toka wana wa Hamori (Mwa. 33:19). Kuna njia tatu kueleza maneno haya: (1) Labda Abrahamu alinunua sehemu ya inchi katika Sekemu vilevile. Labda nyuma Yakobo alinunua sehemu ya inchi ile katika Sekemu vilevile. (2) Labda Stefano alitumika na jina la Abrahamu kwa pahali pa mzao wa Abrahamu, ndiye Yakobo. (3) Labda Stefano alijumlisha habari za kununua inchi za Abrahamu na Yakobo pamoja kwa ufupi.

6. Kuongezeka kwa jamaa ya Yakobo **katika Misri** na utumwa wao nyuma ya mauti ya Yosefu (mash. 17-19). Halafu Stefano aliendelea kukumbusha wasikiaji wake namna gani watu wake walitendea Musa.

**7:20-43** Stefano alikuwa akionyesha wazi pamoja na uhodari, ya kwamba mara mbili mbele Wayuda walikataa waokozi ambao Mungu alisimamisha kuwaokoa. Wa pili alikuwa **Musa**.

Stefano alikuwa ameshitakiwa kusema alitukana Musa (Mdo. 6:11). Anahakikisha sasa ya kwamba taifa la Israeli walikuwa na hatia – kwa sababu walikataa mtu huyu aliyechaguliwa na Mungu.

Kwanza Stefano aliwakumbusha habari za maisha ya Musa:

1. Kuzaliwa kwake, ujana na masomo yake katika Misri (mash. 20-22). Labda "**hodari kwa maneno"** yanasema juu ya maandiko yake, kwani yeye mwenyewe alisema hakuweza kusema vizuri (Kut. 4:10).

2. Mara ya kwanza aliyokataliwa na **ndugu zake** wakati aliposaidia mmoja wao aliyeumizwa na Mmisri (mash. 23-28). Ona shairi 25! Linatukumbusha namna Kristo alivyokataliwa na watu wake!

3. Alifukuzwa na kukaa **inchini mwa Midiani** (sh. 29).

4. Mungu alionekana kwake katika **kijiti** kilichowaka kwa moto, akamtuma kurudia **Misri kuponyesha** watu wake (mash. 30-35).

5. Aligeuka mkombozi wa taifa lake (sh. 36).

6. Unabii wake juu ya kuja kwa Mwokozi (sh. 37). (**Kama mimi** – maana yake "namna alivyoninyanyua.")

7. Kazi yake kama mwenye kutoa sheria **kwa kanisa jangwani** (sh. 38).

8. Watu walikataa Musa mara ya pili, wakati walipoabudu **mwana-ngombe** ya zahabu (mash. 39-41). Kuna habari nyingine juu ya Waisraeli wakiabudu sanamu ndani ya mashairi 42 na 43. Wakikiri **kutolea Mungu … sadaka**, **walichukua hema ya Moloki**, namna moja ya kuabudu sanamu ya kuchukiza mno, na waliinama mbele ya **Refani,** sanamu ya nyota. Kwa zambi hii Mungu aliwaonya kwamba atawahamisha kwenda Babeli (au Damasiki, Amosi 5:25-27) kama wafungwa.

Habari zilizotokea zamani zinatokea tena na tena kwa kila kizazi. *Watu hawageuki.* Hawafahamu habari mpya toka Mungu (sh.25). Wanakataa kusikiliza maonyo kukaa pamoja na salama (sh. 27). Mungu akituma mwokozi kwao, wanamkataa (sh.39). Wakati wanapoponyeshwa toka kikao kiovu, wanachagua kuabudu sanamu kwa pahali pa Mungu wa rehema (sh. 41). Hii ndiyo tabia ya watu wa dunia – waasi, bila asante, wapumbavu. Lakini *Mungu habadiliki.* Mungu aliyesema na Musa ndiye aliyesema na wazazi wake (sh.32). Mungu huyu anasikia wakati watu wake walipo na matata (sh. 34). Anakuja kuokoa (sh. 34). Anaongoza watu wake toka mauti hata uzima (sh.36). Anaacha wale ambao wanamkataa wafanye mapenzi yao wenyewe (sh.42). Huyu ndiye Mungu wetu mkubwa – mwenye rehema, uwezo, utakatifu. Habadiliki kamwe, si neno kama maneno gani yakitokea

(Mal. 3:6). Maneno haya yalikuwa maonyo kwa wasikiaji wa Stefano wasichezecheze na Mungu. Ni tumaini la hakika vilevile ya kwamba kwa milele kila ahadi ya Mungu itatimizwa.[6]

**7:44-46** Stefano alishitakiwa na kusema maneno mabaya juu ya hekalu. Alijibu na kukumbusha wasikiaji wakati Waisraeli walipokuwa na **hema ya ushuhuda jangwani**. Kwa wakati ule watu walikuwa wakiabudu majeshi ya mbinguni vilevile. Wakati **Yosua** alipoongoza Israeli kuingia **inchi** ya Kanana, na wenyeji wake wapagano walipokwisha kufukuzwa, **hema** ile ililetwa **inchini** mwa Kanana na kusimama **mpaka siku za Daudi**. **Baba** zao **walikuwa wameomba kupewa kao kwa Mungu wa Yakobo** na **walipata neema mbele ya Mungu.**

**7:47-50** Mungu hakumpa Daudi ruhusa kujenga hekalu, lakini **Solomono alimjengea nyumba.**

Halafu hekalu lilikuwa kao la Mungu katikati ya watu wake, lakini Mungu hakukaa ndani ya nyumba ile tu. Solomono alisema neno hili wazi wakati hekalu lilipowekwa kwa Mungu (1 Waf. 8:27). Na Isaya alikuwa ameonya watu kwamba Mungu haweki roho zaidi juu ya nyumba, lakini juu ya hali ya roho za watu (Isa. 66:1, 2). Anataka kuona mtu mwenye roho ya kuvunjika, anayetetemeka kwa ajili ya neno lake.

**7:51-53** Viongozi vya Wayuda walikuwa wameshitaki Stefano juu ya kusema mabaya juu ya sheria. Alijibu sasa na mashitaki mafupi.

Ni *wao* **waliokuwa wenye shingo gumu, wasiotahiriwa katika mioyo, wala masikio.** "Aliwahamakia, si kama Israeli wa Mungu, lakini kama Mataifa wakaidi wasiotahiriwa katika mioyo wala masikio." Walikuwa wana wa **baba** zao waliokaa kushindana na **Roho Mtakatifu** siku zote. **Baba** zao walikuwa wametesa **manabii waliotabiri kwamba Kristo atakuja.** Sasa wao walikuwa wameua yule **Mwenye Haki**. Ni wao wasioshika torati ambayo walipokea **kwa amri ya malaika.**

Basi! Hakuhitaji kuongeza maneno mengine! Wao walitaka kushitaki na kuhukumu Stefano, lakini alikuwa Stefano aliyegeuka mwamuzi, nao walishitakiwa. Hotuba yake ilikuwa moja ya maonyo ya mwisho ya Mungu kwa taifa la Wayuda mbele ya Habari Njema kuhubiriwa kwa Mataifa.

**7:54-60** Mara moja wakati Stefano aliposema, "Ninaona **mbingu zimefunguka"** makutano walikataa kumsikiliza tena. Wakapiga kelele, wakamrukia, wakamsukuma inje ya mji, **wakamtupia mawe.**

Roho Mtakatifu alitaja jina la kijana mmoja aliyechunga mavazi ya wauaji wale. Jina lake lilikuwa **Saulo.** Ni kama Roho anataka kusema nasi, "Kumbukeni jina hili. Mutalisikia tena."

Kufa kwa Stefano kulifanana na kufa kwa Bwana wetu:

1. Aliomba, **"Bwana Yesu, pokea roho yangu"** (sh. 59). Yesu alikuwa ameomba, "Baba, katika mikono yako ninaweka roho yangu" (Lk. 23:46).
2. Stefano aliomba, **"Bwana, usiwahesabie zambi hii"** (sh. 60). Yesu alikuwa ameomba, "Baba, uwasamehe, kwa sababu hawajui neno wanalofanya" (Lk. 23:34).

Maneno haya yanatufikirisha kwamba kwa njia ya kuwaza juu ya Bwana na kumtazamia, Stefano "alikuwa amebadilishwa kufanana na Bwana toka utukufu hata utukufu, kama vile utukufu unaotoka kwa Bwana, aliye Roho" (2 Kor. 3:18).

Halafu wakati alipomaliza ombi hili **akalala**. Wakati mauti inapoitwa "kulala" au usingizi katika Agano Jipya, ni juu ya kufa kwa mwili, si roho. Roho ya mwamini anakwenda karibu na Kristo kwa wakati wa mauti (2 Kor. 5:8); usingizi ndio mfano wa kufa kwa *mwili*.

Wayuda hawakuwa na ruhusa kuazibu watu na kufa; neno hili lilikuwa ruhusa

ya Waroma ambao waliwatawala (Yn. 18:31b). Stefano alikuwa ameshitakiwa juu ya kusema maneno mabaya juu ya hekalu, mashitaki yasiyokuwa kweli, lakini mara hii alihukumiwa na kuuawa na Wayuda. Bwana Yesu alikuwa ameshitakiwa juu ya kukusudi kuharibu hekalu (Mk. 14:58), lakini ushuhuda wa washahidi haukupatana.

## 2. KANISA KATIKA YUDEA NA SAMARIA (8:1 – 9:31)

### A. Utumishi wa Filipo kwa Samaria (8:1-25)

**8:1** Roho ya Mungu alisema tena juu ya **Saulo**. Bila shaka alikuwa na vita rohoni mwake, lakini hatatesa Wakristo kwa muda mrefu tena. **Saulo alikuwa akikubali kufa kwa** Stefano**,** lakini kwa njia ya kufanya hivi alikuwa akitayarisha njia kwa mwisho wa kazi yake kama mtesi mkubwa.

**"Kwa siku ile"** – Maneno haya yalianza muda mpya. Mauti ya Stefano ulikuwa mwanzo wa mateso makubwa kwa **kanisa**. Waamini **walisambazwa katika … Yudea na Samaria.**

Bwana alikuwa ameagiza wafuata wake kuanza kumshuhudia katika Yerusalema, na nyuma yake kuenea hata Yudea, Samaria, na mwisho wa dunia. Kufika wakati ule walishuhudia Kristo katika Yerusalema tu. Labda waliogopa kumshuhudia pahali pengine. Sasa mateso yaliwalazimisha.

**Mitume** walibaki mjini. Ulikuwa wakati wa taabu kwa waamini. Mmoja wao alikuwa ametoa uzima wake. Wao wenyewe walikuwa wakifukuzwa kama nyama. Lakini kwa maneno ya roho haukuwa muda wa giza hata kidogo. Mbegu ya ngano ilikuwa imepandwa udongoni, na bila shaka itazaa matunda mengi. Pepo za mateso zilisambaza mbegu za Habari Njema kwa pahali palipo mbali, na hakuna mtu anayeweza kujua kipimo cha mavuno!

**8:2** Hatujui majina ya **watu watawa** waliozika Stefano. Labda walikuwa Wakristo waliokuwa kwanza katika Yerusalema. Au labda walikuwa Wayuda wenye kuogopa Mungu waliokuwa wameona ndani ya Stefano neno ambalo lilimstahili kuzikwa na utaratibu.

**8:3** Lakini **Saulo** – tunaona jina lake tena. Na nguvu nyingi alitesa kanisa, akiondosha waamini nyumbani mwao na **kuwatupa katika kifungo.** Bila shaka ilimshinda kusahau Stefano – utulivu wake – imani yake – uso wa malaika! Labda kwa njia ya kutesa Wakristo alijaribu kuondosha ukumbusho wa Stefano katika nia yake.

**8:4-8** Kusambazwa kwa Wakristo hakunyamazisha ushuhuda wao. Walipeleka Habari Njema ya wokovu **kila pahali walipokwenda. Filipo** (tuliona jina lake ndani ya sura 6) alikwendea **mji wa Samaria** kwa upande wa kaskazini. Pamoja na kutangaza habari za Kristo alifanya **maajabu** mengi na kutoa **pepo wachafu** ndani ya watu. Watu wengi **waliopooza, na viwete** waliponyeshwa. Watu walitii Habari Njema na kulikuwa na **furaha nyingi**.

Kwa mwanzo wa kanisa waamini walitii maagizo ya Yesu Kristo:

> Walikwenda kuhubiri kama Kristo alivyofanya (Yn. 20:21; Mdo. 8:1-4).
>
> Waliuza vitu vyao kwa kuweza kusaidia watu masikini (Lk. 12:33; 18:22; ona Mdo. 2:45; 4:34).
>
> Waliacha baba, mama, nyumba na mashamba, na walikwenda kila pahali wakihubiri Neno (Mt. 10:37; ona Mdo. 8:1-4).
>
> Walifanya wanafunzi na kuwafundisha kufanya kazi na kutii (Mdo. 28:18-19; ona 1 Tes. 1:6).
>
> Walibeba msalaba na kufuata Kristo (Mdo. 4; 1 Tes. 2).
>
> Walifurahi katika taabu na mateso (Mt. 5:11,12; ona Mdo. 16; 1 Tes. 1:6-8).
>
> Waliacha wasioamini kuzika wafu wao na walikwenda kuhubiri Habari Njema (Lk. 9:59,60).

Walikungutia mavumbi ya miguu yao na kwenda pahali pengine kama watu wakikataa kusikia Habari Njema (Lk. 9:5; ona Mdo. 13:51).

Waliponyesha wagonjwa, wakatoa pepo wachafu, kufufua wafu, na kuzaa matunda yaliyobaki (Mk. 16:18; Mdo. 3–16).

**8:9-11** Mmoja wa watu waliosikia Filipo, aliyejulikana zaidi aliitwa **Simoni**. Watu wa **Samaria** walifikiri yeye ni mtu mkubwa kwa sababu ya matendo ya **uchawi** wake. Yeye mwenyewe alisema yeye ni mtu mkubwa, na wengine wa watu walifikiri yeye ni **"uwezo wa Mungu ulioitwa Mkubwa."**

**8:12, 13** Wakati watu wengi **walipoamini** mahubiri ya **Filipo** na **kubatizwa**, **Simoni alisema vilevile** yeye ni mwamini, **alibatizwa,** na alifuata **Filipo**, akishangaa juu ya **maajabu** ambayo Filipo alitenda.

Lakini ilionekana kwamba Simoni hakuzaliwa tena. Alikuwa amebatizwa, lakini hakuwa na uzima wa milele.

Ona ya kwamba **Filipo alihubiri** Habari Njema **ya ufalme wa Mungu, na jina lake Yesu Kristo. Ufalme wa Mungu** ndio mahali watu wanaponyenyekea utawala wa Mungu. Kwa wakati wa sasa, Mfalme si hapa. Kwa pahali pa ufalme hapa duniani, tuna ufalme wa roho usioonekana wazi, lakini unaoonekana ndani ya maisha ya wote ambao wanamfuata na uaminifu. Kwa wakati wa kuja Mfalme atarudi duniani na kusimamisha ufalme. Yerusalema utakuwa mji wake mkubwa. Kwa kuingia ufalme wa Mungu, au ufalme wa roho wa sasa, au ufalme utakaosimamishwa nyuma, inapasa mtu kuzaliwa tena, ndiyo kuamini **jina la Yesu Kristo**. Hili ndilo neno kubwa la mahubiri ya Filipo.

**8:14-17** Wakati **mitume … katika Yerusalema waliposikia** kwamba **Wasamaria walipopokea Neno la Mungu, walituma Petro na Yoane kwao**. Wakati walipofika, waamini **walikuwa wamebatizwa kwa jina la Bwana Yesu,** lakini walikuwa hawajapokea **Roho Mtakatifu**. Wakiongozwa na Mungu mitume **waliomba** waamini hawa **waweze kupokea Roho Mtakatifu**, **wakaweka mikono juu yao, nao walipokea Roho Mtakatifu mara moja.**

Kwa nini matokeo hapa yalifuatana namna nyingine na yale kwa siku ya Pentekote? Kwa Pentekote Wayuda:

1. Walitubu.
2. Walibatizwa.
3. Walipokea Roho Mtakatifu.

Hapa Wasamaria:

1. Waliamini.
2. Walibatizwa.
3. Mitume waliwaombea na kuweka mikono juu yao.
4. Walipokea Roho Mtakatifu.

Kuna neno moja ambalo tunajua hakika: wao wote waliokolewa kwa njia moja tu, ndiyo imani ndani ya Yesu Kristo. Yeye ni njia ya pekee kwa watu kupokea wokovu. Lakini kwa wakati huu wa mabadiliko toka dini ya Wayuda kwa Ukristo, Mungu alichagua kutenda kwa njia mbalimbali kwa waamini wa pahali mbalimbali. Ilipasa waamini Wayuda wajitenge na taifa la Israeli kwa njia ya ubatizo mbele ya kupokea Roho Mtakatifu. Tena Wasamaria waliombewa na mitume, na kuwekewa mikono yao. Kwa nini?

Labda walifanya hivi kuonyesha umoja wa kanisa, si neno kama waamini ndani yake walikuwa Wayuda au Wasamaria. Ingewezekana kwa waamini Wayuda katika kanisa kwa Yerusalema kufikiri wao ni wazuri kupita, na juu kupita ndugu zao waamini Wasamaria na kukaa mbali nao. Kuepuka matengo namna hii, au kuwa na makanisa mawili (moja la Wayuda na moja la Wasamaria), Mungu alituma mitume kuwekea waamini wa Samaria mikono ku-

onyesha ushirika nao kama waamini ndani ya Bwana Yesu. Wao wote walikuwa viungo ndani ya mwili mmoja, wote moja ndani ya Kristo.

Ndani ya shairi 16 tunasoma kwamba **walibatizwa katika jina lake Bwana Yesu tu** (ona vilevile Mdo. 10:48 na 19:5). Maana ya maneno haya si kwamba ubatizo ulikuwa namna nyingine na ubatizo "kwa jina la Baba, na la Mwana na la Roho Mtakatifu" (Mt. 28:19). W. E. Vine aliandika kwamba "Luka hakuandika kawaida kwa ubatizo, lakini alipasha tu habari zilizotokea." Misemo yote miwili inaonyesha utii na umoja, na waamini wote wa kweli wanakiri na furaha uaminifu wao kuungana na Utatu Mtakatifu, na kwa Bwana Yesu.

**8:18-21 Simoni** mchawi alishangaa sana wakati alipoona kwamba **Wasamaria walipewa Roho Mtakatifu** wakati mitume **walipowawekea mikono.** Hakufahamu hata kidogo maana ya ndani ya maneno haya, lakini alifikiri uwezo huu usio wa ulimwengu ungeweza kumsaidia vizuri ndani ya kazi yake. Hivi alitaka kulipa mitume mali kununua uwezo huu.

Jibu la Petro lilionyesha kwamba **Simoni** hakuwa mwamini wa kweli:

1. **"Feza yako ipotee mbali nawe."** Hakuna mwamini *atakayepotea* kamwe (Yn. 3:16).
2. **"Huna shirika wala sehemu katika neno hili,"** maana yake hakuwa mmoja wa waamini.
3. **"Roho yako si kweli mbele ya Mungu,"** maana yake alikuwa mtu asiyeokolewa.
4. **"Wewe ni katika uchungu wa nyongo, na katika kifungo cha uovu"** (sh.23). Maneno haya si kweli kwa mtu aliyezaliwa tena.

**8:22-24** Petro alisukuma **Simoni kutubu** na **kuomba** Mungu kumsamehe shauri hili ovu. Simoni aliomba Petro kuwa mpatanishi wake na Mungu. Alikuwa mtangulizi wa watu wale wasiotaka kufikia Bwana wao wenyewe, lakini wanaotaka kufikia Mungu kwa njia ya mpatanishi. Masemo ya Simoni yanaonyesha kwamba hakutubu kweli, **"Muniombee kwa Bwana, yasinipate mambo haya muliyosema."** Hakuwa na huzuni kwa sababu ya zambi yake, lakini kwa sababu ya matunda ya zambi katika maisha yake.

**8:25 Nyuma ya kushuhudu na kuhubiri Neno la Bwana,** Petro na Yoane walirudia Yerusalema, lakini walikaa **kuhubiri katika miji mingi ya Wasamaria**.

### B. Filipo na towashi ya Etiopia (8:26-40)

**8:26** Kwa wakati huu wa baraka ya Roho Mtakatifu katika Samaria **malaika ya Bwana** aliongoza **Filipo** kwenda pahali pengine kumtumikia. Ilimpasa kuondokea pahali watu wengi walipokuwa wakibarikiwa, na kuhubiri kwa mtu mmoja. Malaika aliweza kuongoza **Filipo** lakini hakuweza kufanya kazi ya Filipo, ndiyo kuhubiri Habari Njema. Watu, si malaika, walipewa heshima ya kufanya kazi hii.

Bila kuuliza kwa nini ilimpasa kuondokea pahali pale watu wengi walipokuwa wakibarikiwa, **Filipo** alisafiri kwa kusini toka Samaria kwenda **Yerusalema,** kisha alifuata moja ya njia zilizokwenda **Gaza**. Haijulikani wazi kama Gaza ulikuwa **jangwa**, au njia inayofikisha pale ndiyo jangwa. Si neno; **Filipo** aliondokea makao ya watu na baraka ya Roho; akashika njia kwenda pahali pa jangwa.

**8:27-29** Njiani alifikia magari ya watu waliosafiri pamoja. Ndani ya gari kubwa zaidi alisafiri **towashi mwenye mamlaka**[7] **chini ya Kandake**,[8] **malkia ya Etiopia,** aliyewekwa juu ya hazina yake yote. (Etiopia ilikuwa inchi kwa kusini ya Misri.) Ni kama mtu huyu

alikuwa ameanza kufuata dini ya Wayuda, na kwa sababu hii alikwendea **Yerusalema kwa kuabudu,** na sasa alikuwa akirudi kwake. Basi pale ndani ya gari lake alikuwa **akisoma kitabu cha nabii Isaya.** Dakika ile ile **Roho** aliongoza **Filipo kujongea karibu na gari hili.**

**8:30, 31 Filipo** alianza kusemezana naye na kumwuliza naye na upole, "**Unafahamu maneno haya unayosoma?"** Towashi alikubali kwamba alihitaji mtu kumwongoza, akaomba Filipo **kuketi pamoja naye** ndani ya **gari**. Ni tamu kuona ya kuwa hakukumbuka kwamba Filipo alikuwa mtu wa taifa lingine.

**8:32, 33** Ni ajabu kuona namna Mungu alivyoongoza Filipo kufikia gari kwa saa towashi alipokuwa akisoma Isaya 53, inayopasha habari za Masiya na mateso yake!

Mashairi haya ndani ya Isaya yanapasha habari za Huyu aliyekuwa mpole na **kimya** mbele ya adui zake; yule **asiyehukumiwa na haki**; Yule asiyekuwa na tumaini kwamba atakuwa na wazao kwa sababu aliuawa kwa ujana wake bila kuoa.

**8:34, 35 Towashi** aliuliza kama Isaya alikuwa akisema **juu yake mwenyewe au juu ya mtu mwingine**. Ulizo hili lilifungulia **Filipo** njia kumwambia namna Maandiko haya yalitimizwa ndani ya maisha na mauti ya Yesu wa Nazareti. Bila shaka towashi alisikia watu wakisema juu ya mtu huyu **Yesu** wakati alipokuwa kwa Yerusalema, habari zisizokuwa njema kila mara. Sasa **towashi** alijifunza kwamba **Yesu** wa Nazareti ndiye Mtumishi mwenye maumivu wa Yehova ambaye Isaya aliandika juu yake.

**8:36** Tunafikiri Filipo alielezea Mwetiopia habari za ubatizo wa Wakristo, kufungamanishwa kwa mwamini na Kristo na kufa, kuzikwa na utukufu wake. Sasa wakati walipokuwa wakikaribia pahali pa **maji**, **towashi** alipasha Filipo kwamba alitaka **kubatizwa.**

**8:37, 38** Shairi 37 linaonyesha kwamba kwa kubatizwa inapasa mtu kuamini na roho ya kweli kwamba **Yesu Kristo** ni Mwana wa Mungu.

**Gari** lilisimamishwa, na **Filipo** na towashi **waliingia ndani ya maji**, Filipo alibatiza **towashi** nao **walitoka maji** tena. Hivi pale kwa njia iliyopita jagwani Mkristo alibatiza mwamini huyu mpya. Kanisa halikuwa pale, wala mitume. Bila shaka watumishi waliosafiri pamoja na towashi waliona ubatizo wa bwana wao; wakafahamu kwamba sasa alikuwa mfuata wa Yesu wa Nazareti.

**8:39** Mara moja nyuma ya ubatizo **Roho ya Bwana alinyakua Filipo.** Hakumwongoza tu kwenda pahali pengine, lakini alimwondosha gafula kwa njia ya ajabu. Hivi **towashi** hatakaa kufikiri juu ya mtu huyu ambaye alimbatiza, lakini juu ya Bwana mwenyewe.

Inapasa mhubiri wa Habari Njema kuomba macho ya wasikiaji wake yaweze kukokotwa juu ya Bwana Yesu tu.

Towashi **akakwenda zake akifurahi.** Kutii Bwana kunajaza mioyo yetu na furaha kubwa sana.

**8:40** Halafu **Filipo** aliendelea na kazi yake ya kuhubiri Habari Njema kwa **Azoto** (pahali palipoitwa Asidodi katika Agano la Kale) kwa upande wa kaskazini wa Gaza na kwa upande wa mangaribi wa Yerusalema, akaendelea kwenda kwa kaskazini akifuata pwani kufikia **Kaisaria.**

Halafu nini ilipata towashi? Filipo hakuweza kumfundisha Neno la Mungu namna inavyopasa wahubiri kufanya kwa waamini wa sasa kuwasimamisha imara ndani ya imani. Aliweza tu kumweka mikononi mwa Mungu na Maandiko Matakatifu ya Agano la Kale. Lakini kwa uwezo wa Roho Mtakatifu bila shaka mwanafunzi huyu mpya alirudia Etiopia[9] na kuwaambia watu wote

juu ya neema ya Bwana Yesu Kristo ambayo ilimwokoa.

### MAFUNDISHO JUU YA UBATIZO WA MWAMINI

Ubatizo wa towashi unaonyesha, pamoja na maneno mengi mengine, ya kwamba kwa wakati wa mwanzo wa kanisa walifundisha juu ya ubatizo wa Wakristo na walibatiza waamini (Mdo. 2:38; Mdo. 22:16). Ubatizo huu ni mbali na ubatizo wa Yoane, ulioonyesha toba ya mwenye kubatizwa (Mdo. 13:24; 19:4). Ubatizo wa Wakristo ulionyesha kwamba mwenye kubatizwa alikiri mbele ya watu wengine kwamba alifanywa mamoja na Kristo.

Kila mara wakati watu walipookolewa walibatizwa vilevile (Mdo. 2:41; 8:12; 18:8), wanawake na wanaume (Mdo. 8:12), Mataifa na Wayuda vilevile (Mdo. 10:48). Nyumba nzima walibatizwa (Mdo. 10:47, 48; 16:15, 33). Tunasoma juu ya mbili za nyumba hizi kwamba watu wote ndani yao *waliamini*. *Hatusomi kamwe* kwamba watoto wachanga walibatizwa.

Waamini walibatizwa muda mfupi tu nyuma ya kuokolewa (Mdo. 8:36; 9:18; 16:33). Hawakuhitaji kungoja kwanza kwa muda fulani kuonyesha kwamba walikuwa wameamini kweli. Kwa wakati ule ilikuwa hatari kwa waamini wa sasa kupata mateso, ndilo neno lililozuiza watu kukiri mbio kwamba waliamini Kristo.

Habari za Simoni (Mdo. 8:13) zinaonyesha kwamba ubatizo huu haukuweza kuokoa roho ya mtu. Hata nyuma ya kukiri kwamba aliamini na kubatizwa alikuwa "katika uchungu wa nyongo, na katika kifungo cha uovu" (Mdo. 8:23). Roho yake "haikuwa kweli mbele ya Mungu" (Mdo. 8:21).

Kama tulivyosema mbele, watu walibatizwa kwa njia ya kuingiza mwili mzima ndani ya maji (Mdo. 8:38, 39) – "wakatelemuka wote wawili ndani ya maji, Filipo na yule towashi, akambatiza … walipotoka katika maji." Hata kwa wakati wa sasa, wengi wanaobatiza kwa njia ya kunyunyiza tu maji juu ya kichwa cha mwenye kubatizwa wanakubali kwamba waamini kwa wakati wa mwanzo wa kanisa walibatiza kwa njia ya kuingiza mwili mzima ndani ya maji.

Ni kama mara mbili ubatizo unatajwa pamoja na usamehe wa zambi. Siku ya Pentekote Petro alisema, "Tubuni mukabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo mupate ondoleo la zambi zenu ..." (Mdo. 2:38) . Na nyuma Anania alisema na Saulo, "Simama ubatizwe, usafishe zambi zako, ukiitia jina la Bwana ..." (Mdo. 22:16). Kila mara wale walioagizwa kubatizwa walikuwa Wayuda; hakuna mtu wa Mataifa aliyeagizwa kamwe kubatizwa kwa ondoleo la zambi. Wakati mwamini Myuda alipobatizwa, alionyesha mbele ya watu kwamba alijitenga na taifa waliokataa na kusulibisha Masiya. Alikuwa amepata usamehe kwa sababu ya imani yake ndani ya Bwana Yesu. Bei ya usamehe yake ilikuwa damu ya damani ya Bwana. Usamehe wake ulikuwa umeonyeshwa wazi kwa njia ya maji ya ubatizo ambao ulimwondosha mbele ya watu toka msingi wa Wayuda na kumweka juu ya msingi wa Wakristo.

Hatusomi katika Matendo maneno Bwana Yesu aliyosema katika Matayo 28:19, "...mukiwabatiza kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu." Wasamaria walibatizwa kwa jina la Bwana Yesu (Mdo. 8:16), na wanafunzi wa Yoane vivyo hivyo (Mdo. 19:5). Lakini si kusema kwamba mara nyingine watu hawakubatizwa kwa majina matatu yote. Labda maana ya "kwa jina la Bwana Yesu," ni "kwa amri ya Bwana Yesu."

Wafuata wa Yoane walibatizwa mara mbili – kwanza na ubatizo wa Yoane kwa toba, na tena wakati walipookolewa, na ubatizo wa mwamini (Mdo.

19:3,5). Neno hili linatufahamisha kwamba, hata mtu alibatizwa wakati alipokuwa mtoto mchanga, ni vizuri kumbatiza tena nyuma ya kuamini na kuokolewa. ❖

### C. Wokovu wa Saulo wa Tarso (9:1-31)

**(9:1,2)** Kuanza na sura 9 habari zinageuka. Kufika sasa Petro alijulikana zaidi wakati alipohubiri kwa taifa la Israeli. Kuanza sasa Mtume Paulo ataonekana kupita na kupita, na Habari Njema itaendelea kupita kwa Mataifa.

Ni kama **Saulo** alikuwa na miaka karibu 30 kwa wakati huu. Warabi walifikiri ataendelea vizuri sana ndani ya maneno ya dini ya Wayuda. Alikuwa na bidii kupita wenzake wote.

Wakati alipoona hesabu ya Wakristo ikikaa kuongezeka (walijulikana vile kama watu wa **Njia**) alifikiri maneno haya yatakuwa hatari kwa dini yake mwenyewe. Hivi na nguvu nyingi alianza kuharibu wafuata wa dini hii. Alipata ruhusa toka **kuhani mkubwa** kwenda **Damasiki** katika Suria na kutafuta wafuata wa Yesu, **kuwafunga na kuwaleta kwa Yerusalema** kuhukumiwa na kuazibiwa.

**9:3-6** Saulo na wale waliosafiri pamoja naye walikuwa **wakikaribia Damasiki** wakati **gafula nuru** kubwa **toka mbingu ilipomwangaza. Akaanguka chini, akasikia sauti ikimwambia, "Saulo, Saulo, kwa sababu gani unanitesa?** Wakati Saulo alipouliza, **"Wewe nani, Bwana?"** aliambiwa, **"Mimi ndimi Yesu ambaye unamtesa."**

Tukitaka kufahamu kushituka kwa Saulo kwa wakati ule, ni lazima kwa sisi kukumbuka kwamba aliamini kabisa kwamba **Yesu** wa Nazareti alikufa na kuzikwa kaburini. Basi mwongozi wa dini ile akiwa mfu, sasa ilipasa tu kuua wafuata wake; halafu dunia haitachafuwa tena na pigo hili.

Lakini sasa alisikia habari hizi za kumponda kabisa, ya kwamba Yesu hakuwa mfu hata kidogo, lakini alifufuliwa toka wafu na kutukuzwa kwa mkono wa kuume wa Mungu mbinguni! Ono hili la Mwokozi aliyetukuzwa liligeuza makusudi yote ya maisha yake.

Saulo alijifunza vilevile siku ile kwamba wakati alipokuwa akitesa wanafunzi wa **Yesu, alitesa** Bwana mwenyewe. Mmoja wa viungo vya Mwili duniani akiumizwa, Kichwa mbinguni anaumia vilevile.

Hivi Saulo alijifunza kwanza kama Yesu ni nani, kisha alitumwa kwa Damasiki, pahali atakapojifunza nini itampasa kufanya.

**9:7-9 Watu waliosafiri pamoja na Saulo** walishangaa sana. Walikuwa wamesikia sauti toka mbingu, bila kusikia maneno ambayo Saulo alisikia (Mdo. 22:9). Hawakuona Bwana; **Saulo** tu alimwona, na aliitwa kuwa mtume wakati ule.

Yule Mfarisayo mwenye kiburi **akashikwa na mkono** sasa na **kupelekwa hata Damasiki**. Alibaki pale kwa **siku tatu pasipo kuona kitu, wala kula, wala kunywa.**

**9:10-14** Tunafikiri habari hizi zilishitusha Wakristo kwa **Damasiki** sana, labda ziliwaogopesha vilevile. Walijua Saulo alikuwa akisafiri kwa Damasiki kuwafunga. Walikuwa wameomba Mungu kuzuiza kusudi lake. Labda wengine walikuwa wameomba aweze kuokolewa. Sasa walisikia kwamba adui mkubwa ya imani yao alikuwa amegeuka Mkristo. Ilikuwa nguvu kwao kuamini habari hizi.

Wakati Mungu alipoagiza **Anania,** mmoja wa waamini wa **Damasiki**, kwenda **kuona Saulo**, **Anania** alimwambia kwamba aliogopa mtu huyu sana, lakini wakati aliposikia kwamba **Saulo** alikuwa **akiomba** sasa kwa pahali pa kujaribu kufunga Wakristo, alikwendea **nyumba ya Yuda** katika njia inayoitwa **Nyoloka**.

**9:15,16 Bwana** alikuwa na mashauri ya ajabu kwa Saulo: **"… mtu huyu ni chombo kichagulifu kwangu, achukue Jina langu mbele ya Mataifa, na wafalme, na wana wa Israeli. Maana nitamwonyesha mambo makubwa mangapi atakayoteswa kwa ajili ya jina langu."** Saulo atakuwa mtume kwa **Mataifa**, na kwa njia hii atasimama mbele ya **wafalme**. Lakini atahubiri kwa watu wa taifa lake vilevile, nao watamtesa zaidi.

**9:17, 18** Na roho ya neema na mapendo **Anania** alionyesha ushirika wake kwa mwamini huyu wa sasa kwa njia ya **kuwekea Saulo mkono**. Alimwita "**Ndugu Saulo,**" na alimwelezea kwamba alikuwa amefika kusudi **Saulo apate kuona** na **ajazwe Roho Mtakatifu.**

Ona ya kwamba **Saulo** alipewa **Roho Mtakatifu** kwa njia ya kuwekewa mikono wa mwanafunzi tu wa Yesu. **Anania** hakuwa mtume wala mhubiri. Neno hili ni kemeo kwa watu wale wanaofikiri kwamba mapadre na maaskofu tu wana ruhusa kufanya kazi namna hii.

Kuna maneno fulani yanayotokea ndani ya maisha ya mtu anayeokolewa kweli. Kulikuwa na maneno fulani ndani ya maisha ya Saulo yaliyohakikisha kwamba alizaliwa tena kweli. Maneno gani? Francis W. Dixon anataja mengine:

1. Alikutana na Bwana na kusikia sauti yake (Mdo. 9:4-6). Alipokea ufunuo toka Mungu. Neno lile liliweza kumwaminisha na kumgeuza kuwa mtumishi mnyenyekevu aliyefuata Bwana na roho yote.
2. Alijazwa na hamu kutii Bwana na kufanya mapenzi yake (Mdo. 9:6).
3. Alianza kuomba (Mdo. 9:11).
4. Alibatizwa (Mdo. 9:18).
5. Alishiriki na watu wa Mungu (Mdo. 9:19).
6. Alianza kushuhudia Kristo na uwezo (Mdo. 9:20).
7. Alipata nguvu katika neema (Mdo. 9:22).

### MAFUNDISHO JUU YA UTUMISHI WA KILA MWAMINI KANISANI

Moja la maneno makubwa sana tunayojifunza ndani ya Matendo ni ya kwamba Ukristo hauendeleshwi mbele kwa njia ya ushuhuda wa watu wachaguliwa waliojifunza kazi ya askofu au padre, lakini na waamini wote mmoja mmoja.

> "Kanisa liliendelea zaidi kwa mwanzo wa Ufalme wa Roma kwa njia ya mahubiri ya waamini mmoja mmoja waliojaribu kuleta wasioamini kwa Kristo, si kwa njia ya walimu, wahubiri au mitume." (Harnack)

> "Kazi ya kuhubiri Habari Njema kwa watu wote duniani na kuendesha Ukristo mbele si zaidi ndani ya mikono ya watu wachaguliwa waliojifunza, lakini ni mzigo wa waamini wote mmoja mmoja." (Bryan Green)

> "Kila mwamini ndani ya kanisa la pahali fulani alikwenda kushuhudia Kristo kwa watu mmoja mmoja, na alileta waamini wa sasa kwa kanisa pahali walipojifunza zaidi na kupatishwa nguvu katika imani yao mpya ndani ya Mkombozi. Kisha waamini hawa wa sasa walikwenda kufanya vivyo hivyo." (A.J. Stewart)

Kanisa kwa wakati wa mitume halikuongozwa na askofu au président. Ndani ya kanisa la pahali fulani kulikuwa na watakatifu na waangalizi na watumishi (Flp.1:1). *Watakatifu wote walikuwa watumishi kwa wakati ule.* Waangalizi walikuwa wazee na viongozi vya waamini kwa maneno ya roho. Watumishi waliangalia maneno ya mali ya kanisa lile, vivi hivi.

Kanisa la pahali fulani halikuongozwa na askofu au mwangalizi mmoja tu, lakini wazee walitumika

pamoja kama wachungaji wa kanisa.

Labda unataka kuuliza, "Habari gani ya mitume, manabii, wahubiri wa Habari Njema, wachungaji na walimu? Watu hawa hawakuwa waangalizi wa makanisa kwa wakati wa mwanzo wao?" Tunapata jibu kwa ulizo hili katika Efe. 4:12. Zawadi hizi zilitolewa kwa kujenga na kupatisha watakatifu nguvu kusudi watakatifu hawa waweze kuendelesha kazi ya kanisa wao wenyewe na kujenga mwili wa Kristo. Kusudi lao halikuwa kubaki pale kama kiongozi au mwangalizi wa pekee wa kanisa lile, lakini kukaa kutumika kupatisha waamini nguvu kufika siku ile watakapoweza kuangalia na kuendesha kazi ya kanisa lao wao wenyewe. Halafu viongozi na waangalizi wataweza kuhama pahali pengine na kupatisha makanisa *mengine* nguvu.

Wenye elimu ya historia ya kanisa wanasema utaratibu wa kuwa na mapadre na maaskofu kuongoza makanisa ulianza karibu na miaka 100 A.D. au zaidi. Haukuwa kwa muda wa Matendo. Utaratibu huu umezuiza kazi ya kuhubiri Habari Njema duniani pote na kuenea kwa kanisa, kwa sababu unaweka mzigo wa *kupita kipimo* juu ya *watu wachache.*

Waamini katika Agano Jipya si walimu tu; wao ni makuhani vilevile. Kama makuhani watakatifu, wana ruhusa, kwa njia ya imani kutokea mbele ya Mungu wakati wo wote kumwabudu (1 Pet. 2:5). Kama ukuhani wa kifalme wamepewa heshima ya kutangaza uzuri wa Yule ambaye aliwaita kutoka giza na kuingia katika nuru yake ya ajabu (1 Pet. 2:9). Waamini wote ni makuhani, lakini si wote walipewa zawadi ya kuhubiri au kufundisha; lakini wote wanaweza kuabudu na kutoa ushuhuda. Kanisani sasa hakuna makuhani walio na amri kuongoza kuabudu na utumishi wa waamini. ❖

**9:19-25** Wanafunzi katika **Damasiki** walikaribisha **Saulo** mioyoni na nyumbani mwao. Nyuma kidogo alifikia masunagogi na kutangaza na uhodari kwamba Yesu **ni Mwana wa Mungu**. Wasikiaji wake Wayuda walijazwa na hofu. Walifahamu kwamba alichukia jina la Yesu mbele. Tena sasa alifundisha kwamba Yesu ni Mungu! Iliwezekana namna gani?

Hatujui kama alikaa **katika Damasiki** kwa muda gani mara hii ya kwanza. Gal.1:17 linaonyesha kwamba aliondokea Damasiki na alikwenda kwa Arabia kwa wakati. Labda alikuwa pale nyuma ya shairi 21 na mbele ya shairi 22.

Katika Arabia **Saulo** alikuwa na njia na saa kuwaza juu ya mambo makubwa yaliyokuwa yametokea katika maisha yake, na zaidi juu ya Habari Njema ya neema ya Mungu ambayo aliwekewa. Wakati aliporudia **Damasiki** (sh. 22), aliweza kufazaisha **Wayuda** katika masunagogi na kuwaonyesha wazi kwamba **Yesu huyu ni** Masiya wa Israeli. Neno hili liliwakasirisha sana hata **walifanya shauri** kuua mtu huyu aliyefungana nao mbele lakini ambaye aliwageukia sasa na kukataa maneno ambayo alisimamia mbele. **Saulo** alipona kwa sababu wanafunzi wakamtwaa **usiku**, wakamshusha **kwa ukuta wa mji ndani ya kitunga.** Ilikuwa haya kabisa kutoka mji kwa njia hii, lakini **Saulo** hakuwa mwenye kiburi tena kama mbele. Alikuwa mwenye roho ya kuvunjika sasa aliyekuwa tayari kubeba laumu kwa ajili ya Kristo, ambayo watu wengine wangekataa.

**9:26-30** Tungefikiri kwamba ilikuwa hatari kubwa zaidi kwa **Saulo** kufikia **Yerusalema**, lakini hakuogopa kwani aliamini kwamba yalikuwa mapenzi ya Mungu kwa yeye kufika kule.

Hatujui kabisa kwamba hii ilikuwa mara ya kwanza Saulo aliyofika kwa **Yerusalema** kama Mkristo, ndiyo miaka mitatu nyuma ya kuokolewa kwake (Gal. 1:18). Mara ya kwanza aliyofikia

**Yerusalema** alikutana na Petro na Yakobo tu, si na wanafunzi wengine. Hapa, ndani ya shairi 27 tunasoma kwamba **Barnaba … akampeleka kwa mitume.** Labda shairi hili linasema juu ya Petro na Yakobo tu, au juu ya mitume yote. Kama Barnaba alimpeleka kwa mitume yote, hii ni mara nyingine Saulo aliyofikia **Yerusalema**, tusiyosoma habari zake pahali pengine.

**Wanafunzi** katika **Yerusalema waliogopa** kwanza kupokea **Saulo** wakifikiri kwamba yeye si mwamini wa kweli. Maana ya jina la **Barnaba** ni *'mwana wa faraja'* naye aligeuka rafiki ya **Saulo** na alipasha watu juu ya wokovu wake, na namna alivyoshuhudia Kristo bila woga kwa **Damasiki.** Halafu waamini walifahamu kwamba **Saulo** alikuwa mwamini wa kweli wakati walipomwona akihubiri **kwa jina la Bwana Yesu na uhodari katika Yerusalema.** Wayuda toka **Yunani** walishindana naye zaidi. Wakati **ndugu** waliposikia kwamba Wayuda wale walitaka kumwua, walisafiri pamoja na **Saulo** hata bandari ya **Kaisaria,** na toka pale alisafiri kufika **Tarso**, mji wake karibu na pwani ya kusini-mashariki ya Asia Ndogo.

**9:31** Kisha **makanisa** katika Palestina walikuwa na salama kwa wakati na hesabu ya waamini iliongezeka, wakakuwa na njia kupata nguvu katika roho.

## 3. KANISA KUFIKIA MWISHO WA DUNIA (9:32 – 28:31)

### A. Petro anahubiri Habari Njema kwa Mataifa (9:32 – 11:18)

**9:32-34** Kuanza sasa tunasoma tena juu ya **Petro** aliyekuwa akiangalia waamini wengine kwa pahali mbalimbali katika Yudea. Alifikia **Luda** kwa upande wa kaskazini-mangaribi wa Yerusalema, kwa njia inayokwenda Yopa. Alikuta pale mtu mmoja mwenye kupooza **aliyelala kitandani kwa miaka minane. Petro** alimwita na jina lake na kumwambia kwamba Yesu Kristo anamponyesha. Ainea alisimama **mara moja.** Tunafikiri kwamba pamoja na kuponyeshwa mwilini alipata wokovu wa roho vilevile.

**9:35** Kuponyeshwa kwa mwenye kupooza kulikuwa ushuhuda mkubwa kwa Bwana katika mji wa **Luda na** kando kando kwa pwani ya **Saroni** na watu wengi **waligeuka kwa Bwana.**

**9:36-38** **Yopa** ulikuwa bandari kubwa zaidi kwa Bahari ya Kati karibu na kilomètres 50 kwa upande wa kaskazini-mangaribi wa Yerusalema. Mmoja wa Wakristo wa pale alikuwa mwanamke mwenye roho ya mapendo, jina lake Tabita au **Dorika**. Alijulikana kwa sababu ya kazi yake ya kushona mavazi kwa wamasikini. Wakati **alipokufa** gafula wanafunzi walituma habari kwa **Luda** kuomba **Petro** kuja **mara moja.**

**9:39-41** Wakati Petro alipofika, alikuta **wajane wote wakitoa machozi,** pamoja na kumwonyeshea **mavazi ambayo Dorika aliwashonea**. Aliwaomba kutoka inje, halafu **alipiga magoti na aliomba**, akasema: **Tabita, amka**. Mwanamke alifufuliwa mara moja na kufika karibu na rafiki zake Wakristo.

**9:42** Habari za ajabu hili la ufufuko **zilienea sana** na **watu wengi waliamini Bwana.** Lakini wakati tunaposoma mashairi 42 na 35 pamoja, ni kama hesabu ya watu waliookolewa kwa sababu ya kuponyeshwa kwa Ainea ilipita hesabu ya wale walioamini kwa sababu ya kufufuliwa kwa Dorika.

**9:43** Petro **alikaa katika Yopa kwa siku nyingi,** na alipanga nyumbani mwa mtu mmoja, jina lake **Simoni, mtengenezaji wa ngozi.** Waza juu ya namna ya kazi ya Simoni. Wayuda hawakufikiri kazi hii ni nzuri kwa sababu ililazimisha mwenye kuifanya kugusa maiti za nyama, ndilo neno ambalo lilimchafua kwa maneno ya dini yake. Hata hivi kwa njia ya kupanga nyumbani mwa **Simoni,** Petro alionye-

sha kwamba hakufungwa na desturi hii ya Wayuda tena.

Walimu wengine wameonyesha kwamba ndani ya sura tatu zinazofuata tunasoma juu ya mzao wa mmoja wa wana wa Noa. Bila shaka towashi wa Etiopia (sura 8) alikuwa mzao wa Hamu. Saulo wa Tarso (sura 9) alikuwa mzao wa Semu. Tena sasa ndani ya sura 10 tunasoma juu ya Kornelio aliyekuwa mmoja wa wazao wa Yafeti. Ni kama ushuhuda kwamba Habari Njema ni kwa mataifa yote, na kwamba ndani ya Kristo maneno haya yote yanayotenga watu yanaondoshwa. Petro alitumika na funguo za ufalme kufungua mlango wa imani kwa Wayuda ndani ya sura 2, na katika sura 10 alifanya vivyo hivyo kwa Mataifa.

**10:1, 2** Habari za sura 10 zinaanza kwa Kaisaria, karibu kilomètres 50 kwa upande wa kaskazini wa Yopa. **Kornelio** alikuwa akida la askari mia za **kundi la Italia.** Pamoja na ile aliabudu na kuogopa Mungu, **alitoa sadaka na ukarimu** kusaidia Wayuda wamasikini ambao walimzunguka, na **kuomba** Mungu siku zote. Mwalimu mmoja, ndiye Ryrie anafikiri kwamba Kornelio aliogopa Mungu wa dini ya Wayuda na utawala wake, lakini alikuwa hajageuka bado mfuata wa dini ya Wayuda kabisa.

Hatujui kama Kornelio aliokolewa kweli au sivyo. Watu wanaofikiri alikuwa ameokolewa wanataja mashairi 2 na 35. Bila shaka Petro alifikiri **Kornelio** wakati aliposema kwamba "katika kila kabila yeye ambaye anamwogopa yeye (Mungu) na kutenda haki anakubaliwa naye." Wale wanaofikiri **Kornelio** alikuwa hajaokolewa bado wanataja Matendo 11:14, pahali tunaposoma juu ya malaika akimwahidi kwamba Petro atamwambia namna gani ataweza kuokolewa.

Sisi tunafikiri **Kornelio** alitii katika maisha yake maneno ambayo Mungu alikwisha kumjulisha. Maneno haya hayakutosha kumwokoa, lakini Mungu alitayarisha njia kwaye kupata nuru ya Habari Njema. Mbele ya kufika kwa Petro, hakujua kwamba hakika alikuwa ameokolewa, lakini alipatana rohoni na wale walioabudu Mungu wa kweli.

**10:3-8** Siku moja **karibu na** saa tisa **Kornelio** alikuwa na **ono**. **Malaika ya Mungu** alionekana kwake na kusema naye akimwita kwa jina lake. Kornelio alikuwa Mtaifa na hakujuana na kazi ya malaika kama Wayuda, hivi aliogopa akifikiri malaika alikuwa Bwana. Malaika alimjulisha kwamba Mungu alipendezwa na **maombi** na **sadaka** zake, akamwagiza **kutuma** watu kwa **Yopa** kwa kusini na kuita mtu mmoja, jina lake **Simoni Petro,** aliyepanga **nyumbani mwa Simoni, mtengenezaji ngozi … kando ya pwani.** Kornelio hakuwa na shaka juu ya agizo hili, lakini alitii mara moja na **kutuma wawili wa watumishi wa nyumba yake** pamoja na askari mmoja aliyekuwa mtu wa kuogopa Mungu vilevile.

**10:9-14** **Kesho yake**, karibu na saa sita **Petro alipanda** kwa dari ya nyumba ya Simoni **aombe**. **Alikuwa na njaa** kwa wakati ule na angalipenda kula, lakini vyakula havikuwa tayari kwanza. Njaa yake ilikuwa tayarisho jema kwa maneno yaliyokuwa tayari kutokea. Roho yake **ilizimia**, **akaona chombo kikimshukia** kama **nguo kubwa toka mbingu kwa pembe zake ine** hata udongo. Ndani yake walikuwa **namna zote za nyama wenye miguu ine** ... **ndege**, na nyoka, nyama safi na **wasio safi. Sauti** toka mbingu iliagiza mtume **mwenye njaa kusimama, kuchinja na kula!** Kumbuka kwamba sheria ya Musa ilikataza Myuda kula nyama **asiye safi**, na Petro alijibu: **"Hata kidogo, Bwana!"** Haifai kamwe kusema hivi na Bwana. Hakuna mtu anayesema 'Bwana' na roho ya kweli ataongeza: 'Hata kidogo.'

**10:15, 16** Wakati Petro alipoeleza

kwamba hajakula vyakula visivyo safi, **sauti** toka mbinguni ilisema, **"Vitu Mungu alivyotakasa usiviite vichafu."** Neno hili lilifanyikana **mara tatu,** kisha chombo kilipokewa tena **mbinguni.**

Ni wazi kwamba maana ya ono hili haikuwa juu ya vyakula safi na visivyo safi tu. Maagizo haya si kwa Wakristo. Maana kubwa ya ono hili lilikuwa kwamba Mungu alikuwa karibu kufungulia Mataifa mlango wa imani. Akiwa Myuda, Petro alifikiri Mataifa si safi; ni wageni, mbali na Wayuda, watu wasiokuwa na Mungu. Lakini sasa Mungu atafanya neno jipya. Nyama na ndege wachafu walikuwa mfano wa Mataifa, nao watapokea Roho Mtakatifu vilevile kama Wayuda (nyama na ndege safi). Maneno yaliyotenga watu, kama taifa na dini, yataondoshwa, na waamini wote wa kweli wa Bwana Yesu watakuwa sawasawa ndani ya ushirika wa Wakristo.

**10:17-23a Wakati Petro** alipokuwa akiwaza juu ya maneno haya, watumishi wa **Kornelio** walisimama mbele ya **mlango**. Akiongozwa na **Roho Mtakatifu,** Petro alishuka toka dari ya nyumba kuwasalimu. Wakati aliposikia habari za kuja kwao, **aliwaingiza nyumbani** na kuwakaribisha kulala usiku. Watumishi walisifu bwana wao sana wakisema yeye ni **"mwenye haki, na kuogopa Mungu, aliye na sifa njema kwa kabila lote la Wayuda."**

**10:23b-29 Kesho yake Petro alishika njia** kwenda **Kaisaria pamoja na** watumishi watatu wa Kornelio na **ndugu wengine wa Yopa.** Ni kama walisafiri jua zima, wakafikia **Kaisaria kesho yake**.

**Kornelio,** akingojea kufika kwao, **alikusanya jamaa zake na rafiki zake.** Wakati **Petro** alipofika, Kornelio **alianguka mbele yake** kwa kumwabudu. Petro alikataa kuabudu kwake, akasema yeye mwenyewe alikuwa **mtu tu**. Ingalikuwa vema kama watu wale ambao walikomboa Petro wakati wa kufa kwake wangalikuwa wanyenyekevu kama yeye na kukataa kuruhusu watu kupiga magoti mbele *yao*!

Akiona kwamba watu wengi walikuwa wamekutana nyumbani, **Petro** alieleza kwamba haikuwa desturi kwa Myuda kama yeye kuingia nyumba ya Mtaifa, lakini **Mungu** alikuwa amemfunulia kwamba haifai kufikiri tena juu ya Mataifa kama wachafu. Kisha aliuliza **kwa sababu gani walimwita kuja.**

**10:30-33 Kornelio** alipasha habari za ono lake **siku ine** mbele wakati malaika alipomjulisha kwamba **maombi yake yalisikiwa,** na alisema naye **kuita Petro**. Kornelio alikuwa na hamu kubwa kusikia neno la Mungu, akasema, **"Basi sasa sisi sote tuko hapa mbele ya Mungu, tupate kusikiliza maneno yote uliyoamriwa na Bwana."**

**10:34, 35** Kwa mwanzo wa hotuba yake **Petro** alikiri kwamba kufika saa ile aliamini baraka ya Mungu ilikuwa kwa taifa la Israeli tu. Sasa alifahamu kwamba **Mungu** hana upendeleo kwa mtu kwa sababu yeye ni wa taifa fulani, lakini anafikiri zaidi kama akiwa na roho ya haki na toba, si neno kama yeye ni Myuda au Mtaifa. **"Katika kila kabila yeye ambaye anamwogopa yeye na kutenda haki anakubaliwa naye."**

Watu wanaeleza shairi 35 kwa njia mbalimbali:

1. Wengine wanafikiri kwamba mtu akitubu zambi zake kweli na kutafuta Mungu, anaokolewa hata pasipo kusikia habari za Bwana Yesu. Wanafikiri kwamba hata hajui habari za kufa kwa Kristo kwa ajili yake, Mungu anajua neno hili na anampokea kwa sababu ya sadaka ya Kristo. Anamhesabia faida ya kazi ya Kristo kwa sababu ana imani ya kweli.
2. Watu wengine wanaamini kwa-

mba hata mtu akiogopa Mungu na kutenda yaliyo haki, maneno haya hayamwokoi. Watu wanaokolewa kwa njia ya kuamini Bwana Yesu Kristo tu. Lakini Mungu akiona kwamba mtu akitembea kwa kipimo cha kweli anayojua, atamfungulia njia kusikia Habari Njema aweze kuokolewa.

Tunafikiri elezo la pili ndilo elezo la haki.

**10:36-38** Halafu Petro alikumbusha wasikiaji wake ya kwamba Habari Njema ilitumwa kwanza kwa Wayuda, lakini **Yesu Kristo ... ni Bwana wa wote** – wa Mataifa na Wayuda. Bila shaka watu nyumbani mwa Kornelio walikuwa wamesikia habari ya **Yesu wa Nazareti;** ilianza katika **Galilaya**, kwa wakati **Yoane** alipobatiza watu, na ilienea **katika Yudea nzima. Yesu** huyu **alitiwa mafuta kwa** Roho Mtakatifu na alitumikia watu wengine, **akiwatendea mema na kuponyesha wale waliokuwa wakiteswa na Shetani.**

**10:39-41** Mitume walikuwa **washuhuda** wa **maneno yote Yesu aliyofanya**. Walisafiri pamoja naye kwa Yudea na **Yerusalema**. Maisha yake yalikuwa makamilifu, lakini hata hivi watu walimwua kwa njia ya **kumtundika mtini**. **Mungu alimfufua** toka wafu **siku ya tatu**, akaonekana wazi kwa **washuhuda waliochaguliwa mbele na Mungu.** Ni kama hakuna msiyeamini aliyeona Bwana Yesu nyuma ya ufufuko wake. Lakini mitume walimwona, na **walikula na kunywa pamoja naye** vilevile. Neno hili linaonyesha kwamba watu waliweza kugusa mwili wa ufufuko wa Mwokozi.

**10:42** Nyuma ya ufufuko wake Bwana aliagiza mitume kutangaza kwamba yeye ni **Mwamuzi wa wahai na wafu**. Tangazo hili linapatana na mashairi mengi mengine ndani ya Biblia yanayofundisha kwamba Mungu Baba ametia hukumu yote mikononi mwa Mwana wake (Yn. 5:22). Hivi tunajua ya kama Mwana wa watu atahukumu Wayuda na Mataifa vilevile.

**10:43** Lakini Petro hakukaa kusema juu ya hukumu. Aliendelea na kutangaza kweli kubwa sana, ndiyo namna gani watu wanaweza kuepuka hukumu. Kama **manabii wote** katika Agano la Kale walivyofundisha, **mtu ye yote anayeamini** jina la Masiya **atapewa usamehe wa zambi,** si Wayuda tu lakini watu wa mataifa yote ya dunia. Unataka kupokea usamehe kwa zambi zako? Basi amini Bwana Yesu!

**10:44-48 Wakati Petro alipokuwa akisema … Roho Mtakatifu aliangukia watu hawa wa Mataifa**. Wao wote walisema **kwa lugha,** na kutukuza **Mungu**. Lilikuwa alama kwa watu wote waliokuwa pale kwamba Kornelio na watu wa nyumba yake walikuwa **wamepokea Roho Mtakatifu** kweli. Wageni Wayuda toka Yopa **walishangaa** wakati walipoona watu wa **Mataifa** waliweza kupokea **Roho Mtakatifu** bila kushika dini ya Wayuda kwanza. Lakini **Petro** alifahamu mara moja kwamba tofauti haikuwa tena, na kwamba kwa macho ya Mungu waamini wote wa Wayuda na Mataifa walikuwa sawasawa. Hivi aliamuru watu wa nyumba ya Kornelio **wabatizwe.**

Ona maneno Petro aliyosema: **watu waliopokea Roho Mtakatifu kama sisi.** Watu hawa wa Mataifa waliokolewa namna Wayuda walivyookolewa – kwa njia ya imani tu. Hawakuhitaji kushika sheria, kutahiriwa, au neno lo lote lingine.

Ona vilevile namna matukio haya yalivyofuatana. Mataifa:

1. **Walisikia neno**, maana waliamini (sh. 44).
2. **Walipokea Roho Mtakatifu** (mash. 44, 47).
3. **Walibatizwa** (sh. 48).

Kwa muda huu wa sasa matukio yanafuatana vivyo hivyo wakati Wayuda au Mataifa wanapookolewa, na Mungu

anapoita na kuokoa watu toka mataifa kuwa watu wake.

Nyuma ya kuona kazi ya neema ya Roho ya Mungu katika Kaisaria, hatushangai kuona waamini wakisihi Petro **kukaa** pamoja nao **kwa siku nyingine**.

**11:1-3** Habari zilienea mbio kwa **Yudea** ya kwamba Petro alikuwa amehubiri kwa watu wa **Mataifa** nao walipokea wokovu. Hivi, wakati **Petro** aliporudia **Yerusalema**, wale **wenye tohara** walibishana naye juu ya kula pamoja na Mataifa. **Wale wa tohara** walikuwa Wayuda waliozaliwa tena lakini waliofungana kwanza na desturi nyingine za Wayuda. Kwa mfano, waliamini kwamba ilipasa Mtaifa kutahiriwa aweze kupokea baraka ya kutimia ya Bwana. Walifikiri haikufaa kwa Petro kula chakula pamoja na Mataifa.

**11:4-14** **Petro** alijisimamia kwa njia ya kuwapasha maneno yote moja moja yaliyotokea: **ono** lake la **kutelemushwa kwa chombo kama nguo toka mbinguni**, ono la **malaik**a kwa Kornelio, kufika kwa wajumbe toka Kornelio, agizo la Roho aende pamoja nao, na namna **Roho Mtakatifu** alivyoshukia Mataifa. **Mungu** alikuwa ametumika waziwazi kwa njia hizi zote, na kujaribu kuzizuiza kungalikuwa kushindana na Bwana.

Ndani ya jibu lake **Petro** aliongeza habari nyingine tusizosoma ndani ya sura 10:

1. Alisema **chombo … toka mbinguni … kilifika** kwake (sh. 5).
2. Alisema alikitazama **sana** (sh. 6).
3. Alisema **ndugu sita** walisafiri pamoja naye toka Yopa hata Kaisaria (sh. 12).
4. Ndani ya shairi 14 tunasoma ya kuwa malaika aliahidi Kornelio kwamba Petro **atamwambia** namna gani **yeye** na **wote wa nyumba yake wataokolewa.** Shairi hili linaonyesha wazi kwamba Kornelio hakuokolewa mbele ya kufika kwa Petro.

**11:15** Petro alisema hapa kwamba **Roho Mtakatifu alishukia** Mataifa **wakati alipoanza kusema.** Kwa Matendo 10:44 tunasoma alikuwa akisema mbele. Labda neno fulani lilimwachisha kusema kwa wakati, na halafu alianza kusema tena nyuma.

**11:16** Wakati **Roho Mtakatifu** aliposhukia Mataifa, Petro alikumbuka Pentekote mara moja. Halafu alikumbuka kwamba Bwana aliahidi wanafunzi wake **"watabatizwa kwa Roho Mtakatifu."** Alifahamu kwamba ahadi hii ilikuwa imetimizwa kwa sehemu siku ya Pentekote na ilikuwa ikitimizwa tena sasa.

**11:17** Halafu Petro aliuliza wenye tohara: **Kama Mungu** alichagua kuwapa Mataifa Roho Mtakatifu, **kama** alivyofanya mbele kwa Wayuda walio**amini** … , Petro **alikuwa nani** aweze **kuzuiza Mungu?**

**11:18** Ni vizuri kuona ya kwamba wakati Wakristo Waebrania walipokuwa wamesikia maelezo ya Petro walitambua kwamba **Mungu** alikuwa amefanya kazi hii. Hawakubishana na Petro tena, lakini walisifu **Mungu** kwa sababu aliwapa **Mataifa** vilevile **toba kwa kupata uzima.**

### B. Mwanzo wa Kanisa kwa Antiokia (11:19-30)

**11:19** Mwandishi anarudi sasa kwa muda wa **mateso** yaliyofuata kuuawa kwa **Stefano**. Hivi habari tutakazosoma sasa zilitokea *mbele* ya kuokolewa kwa Kornelio.

**Wale waliosambazwa nyuma ya mateso** walipeleka Habari Njema kwa:

1. **Foiniki**, kwa inchi kwa kaskazini-mashariki ya Bahari ya Kati, pahali pa bandari za Tiro na Sidona. Kwa wakati wa sasa inaitwa Liban.
2. **Kipuro,** kisanga kikubwa kwa

upande wa kaskazini-mashariki ya Bahari ya Kati.

3. **Kurene**, mji wa bandari kwa pwani ya kaskazini kwa Afrique, ndiyo Libye kwa wakati wa sasa.

Lakini watu hawa walihubiri Habari Njema **kwa Wayuda tu.**

**11:20, 21** Lakini wengine wa waamini wa **Kipuro na Kurene** walikwenda **Antiokia** na walihubiri Habari Njema kwa **Wayunani.** Mungu alibariki mahubiri yao na **watu wengi waliamini, wakageuka kwa Bwana.**

Kufika kwa Wakristo kwa Antiokia kulisaidia sana kuendelesha kanisa. Antiokia ulikuwa kwa mto Orontes inchini mwa Suria, kwa upande wa kaskazini wa Palestina. Ulikuwa mji wa tatu kwa ukubwa na kujulikana wa ufalme wa Roma. Kwa wakati wa nyuma Paulo na wenzi wake walianza safari zao za kuhubiri pale na kupeleka Habari Njema kwa Mataifa.

**11:22-24 Habari** za baraka kwa Antiokia zilifikia **kanisa kwa Yerusalema,** nao walituma **Barnaba**, mtu mwema na mwenye roho nzuri, kwa Antiokia. Mtu huyu alitambua mara moja kwamba Bwana alikuwa akifanya kazi kubwa katikati ya Mataifa hawa, hivi aliwasihi **kuambatana na Bwana** na roho moja. Ilikuwa baraka kabisa kwa kanisa hili la sasa kuweza kupokea katikati yao **mtu huyu mwema, aliyejaa Roho Mtakatifu na imani! Watu wengi waliamini Bwana** wakati alipokuwa pamoja nao. Na kulikuwa na roho ya umoja na ushirika na kanisa kwa Yerusalema.

**11:25, 26** Halafu **Barnaba** alikumbuka **Saulo wa Tarso**! Alikuwa **Barnaba** aliyefikisha Saulo kwa Yerusalema kukutana na mitume. Kisha **Saulo** aliondoshwa mbio toka Yerusalema kumponyesha toka mashauri mabaya ya Wayuda. Tangu wakati ule Saulo alikaa kwa **Tarso**, mji wake. Barnaba alitaka kupatisha roho ya Saulo nguvu kwa kazi yake, na vile alitaka kanisa la **Antiokia** kupata faida ya mafundisho yake. Basi Barnaba **alikwenda Tarso na kuleta Saulo kwa Antiokia, na kwa mwaka mmoja** walitumika pamoja na kanisa lile na **kufundisha watu wengi.**

**Antiokia** ndipo pahali pa **kwanza wanafunzi walipoitwa Wakristo.** Bila shaka lilikuwa jina la laumu kwanza, lakini nyuma ya wakati, wote waliopenda Mwokozi walifurahi kuitwa na jina hili.

**11:27-30 Antiokia** uligeuka pahali Habari Njema ilipohubiriwa zaidi kwa *Mataifa*, lakini hata hivi Wakristo wa pale waliendelea na ushirika na upatano mzuri na kanisa katika **Yerusalema,** waliohubiri Habari Njema zaidi kwa *Wayuda*.

Neno hili lilionekana wazi wakati **manabii wengine walipotoka Yerusalema kwenda Antiokia** kwa wakati ule. **Manabii** hawa walikuwa waamini waliowezeshwa na Roho Mtakatifu kusema kwa ajili ya Mungu. Bwana aliwafunulia habari fulani, nao walipitisha habari hizi kwa watu. **Mmoja wao, jina lake Agabo,** alitabiri kwamba **kutakuwa na njaa kubwa** duniani. Neno hili lilitokea kweli kwa wakati wa **Kaisari Klaudio**. **Wanafunzi** kwa **Antiokia** walifanya shauri mara moja **kutuma zawadi** kwa **ndugu zao Wakristo katika Yudea**. Ilikuwa alama tamu lililoonyesha kwamba magawanyiko katikati ya Wayuda na Mataifa yalikuwa yakipunguka (ona Waefeso 2:14) na uadui katikati ya Wayuda na Mataifa ulikuwa ukiondoshwa na msalaba wa Kristo. Neema ya Mungu ilionekana wazi ndani ya **wanafunzi** hawa waliotoa mara moja, na roho moja, **kwa kadiri ya uwezo wa kila mtu.** Walituma mali yenyewe **kwa wazee kwa mikono ya Barnaba na Saulo**. Hii ni mara ya kwanza tunayosoma juu ya **wazee** kanisani. Wayuda walikuwa na **wazee** ndani ya

masunagogi yao. Hatusomi namna gani wanaume hawa katika Yerusalema waligeuka **wazee**. Ndani ya makanisa ya Mataifa, mitume au wale ambao waliwakomboa, walichagua na kuweka **wazee** (Mdo. 14:23; Tito 1:5). Katika 1 Tim. 3:1-7 na Tit. 1:6-9 tunaona kama ilipasa wazee kuwa watu wa namna gani.

### C. Herode alitesa kanisa, akakufa (12:1-23)

**12:1, 2** Shetani alikaa kupiga vita na kanisa bila kuacha. Mara hii alitumika na **mfalme Herode**. Herode huyu alikuwa Herode Agrippa I, mwana wa mwana wa Herode Mkubwa. Klaudio, mfalme wa Waroma, alikuwa amemweka kuwa mfalme wa Yudea. Alikuwa mtu wa kushika sheria ya Musa, na alijaribu sana kupendeza Wayuda. Na kusudi hili **alitendea mabaya watu wengine wa kanisa** na **aliua Yakobo, ndugu ya Yoane kwa upanga**.

**Yakobo** huyu ndiye aliyekuwa pamoja na Petro na Yoane mlimani wakati Bwana alipogeuzwa sura mbele yao. Mama yake ndiye aliyeomba ruhusa kwa wana wake wawili kuketi kando ya Kristo katika ufalme wake.

Sura hii inaonyesha namna Mungu anavyotendea na kutumika na watu wake. **Yakobo** aliuawa na adui, lakini Petro aliponyeshwa kwa njia ya ajabu. Sisi watu hatufahamu kwa nini mmoja aliuawa na mwingine aliponyeshwa, lakini kwa imani tunategemea mapendo na hekima ya Mungu. Mara nyingine anatumika na mambo yanayoonekana mabaya kwetu kutubariki zaidi.

**12:3, 4 Wayuda** walipendezwa sana juu ya kuuawa kwa Yakobo, hivi Herode alifikiri vizuri atendee **Petro** vivyo hivyo. Lakini zilikuwa **siku za mikate pasipo chachu,** na haikuwa vizuri kuua watu kwa siku kubwa za dini, na vilevile watu wangefikiri zaidi maneno ya kuabudu kwao, si juu ya tendo la Herode kuwapendeza, hivi aliagiza **Petro** afungwe gerezani kwanza. Basi Petro alilindwa na makundi mane ya askari waliokombolana wane wane.

**12:5 Kanisa** katika Yerusalema waliombea Petro sana, wakikumbuka Yakobo aliyeuawa sasa tu. G.C. Morgan alisema, "Maombi yale ya bidii yalikuwa na uwezo kupita Herode, na uwezo kupita gehena."

**12:6-11 Usiku ule … wakati Herode** alipokusudi **kumtoa, Petro alikuwa akilala usingizi** akifungwa na pingu za mikono **katikati ya askari wawili**. Mtu mmoja aliita usingizi wake "kushinda kwa imani." Labda Petro alikumbuka ahadi ya Bwana kwamba ataishi miaka mingi (Yn. 21:18), na hivi alijua Herode hatamwua mbele ya saa iliyochaguliwa na Mungu. Gafula **malaika ya Bwana** alitokea, na **nuru** ilijaa chumbani. Akiamsha **Petro** kwa njia ya kumpiga kwa **mbavu, malaika** alimwagiza kusimama **mbio**.

Minyororo **ilianguka** mara moja toka mikono yake. Halafu **malaika** aliagiza **Petro** kuvaa nguo na **viatu vyake na kumfuata**. **Petro** alifanya hivi, **akafuata** malaika pamoja na kushangaa na kufazaika, **walipita mlinzi wa kwanza, na wa pili**. Wakati **walipofikia mlango wa chuma, mlango ulifungika** nao walitoka gereza. Wakati walipopita katika **njia moja** ya mji **malaik**a alitoweka. Halafu **Petro alianza kufahamu** kwamba hakuota ndoto, lakini alikuwa huru kweli, na ya **kwamba Bwana** alikuwa amemwokoa kwa njia ya ajabu **toka mikono ya Herode** na Wayuda.

**12:12** Wakati alipoanza kuwaza juu ya maneno haya, Petro alikumbuka kwamba bila shaka wanafunzi **walikuwa wakiomba nyumbani mwa Maria, mama ya Yoane** aliyeitwa **Marko** vilevile. Ni kama waliomba usiku mzima, kwani Petro aliondokea gereza asubui mapema.

**12:13-15 Petro aligonga mlango**,

akangoja. **Msichana mmoja, jina lake Roda, akakuja kusikiliza kama ni nani.** Wakati alipotambua sauti ya **Petro** alifurahi sana sana hata **alisahau kufungua mlango** lakini **alikimbia** karibu na watu nyumbani kuwajulisha habari hizi njema. Walifikiri na kumwambia kwamba ana wazimu, lakini Roda **alikaa kusema** kwamba kweli Petro alisimama **kwa mlango**. Wakasema ni **malaika yake**, lakini Roda alizidi kusema ni Petro mwenyewe.

Mara nyingi waamini hawa wanahamakiwa juu ya kuomba bila imani; walishangaa wakati Mungu alipojibu maombi yao! Haifai tuwahamakie kwani mara nyingi tunafanana nao, lakini tufarijiwe kwa sababu Mungu anajibu maombi hata namna hii yanayotolewa bila imani. Sisi vilevile tuko waamini wanaokosa imani mara nyingi.

**12:16,17 Lakini Petro** alikaa kusimama na **kugonga mlango**. Wakati mwishoni **walipofungua mlango**, mashaka yao yalikombolewa na sifa. Petro aliwanyamazisha, akawapasha habari za ajabu Mungu alilotenda kumwondosha gerezani, akawaomba kupasha habari hizi kwa **Yakobo** (tunafikiri alikuwa mwana wa Alfayo) **na kwa ndugu wengine**, kisha **aliondoka.** Hatujui pahali gani alipokwenda kwa wakati ule.

**12:18, 19** Asubui **askari** walifazaika kabisa wakati hawakukuta **Petro** gerezani, wakaogopa sana. Bila shaka **Herode** vilevile alikasirika wakati asipoweza kukamata Petro, na maelezo yote ya **askari** hayakuweza kumfahamisha neno lililotokea, akaagiza wauawe. Yeye mwenyewe alikwenda **Kaisaria** kupolesha roho yake.

**12:20** Hatujui kwa sababu gani **Herode alikasirikia sana watu wa Tiro na Sidona,** ndiyo bandari mbili kwa pwani wa Bahari ya Kati. Wakati **watu** wa miji hii waliposikia kwamba alifikia Kaisaria, walifikiri hii ni saa nzuri kujaribu kupatana naye tena kwa sababu walihitaji ngano waliyoweza kununua toka Yudea. Walifanya urafiki na **Blasto, msaidizi wa mfalme** na kujaribu kupatana tena na mfalme.

**12:21-23** Siku moja **Herode** alitokea kusema na watu akivikwa na mavazi ya mapambo ya **kifalme.** Watu walipiga kelele wakilalamika, **"Ni sauti ya Mungu, si sauti ya mtu!"** Herode hakujaribu kukataa sifa hii iliyofaa kwa Mungu tu, wala **kutukuza Mungu**. Hivi **malaika ya Bwana alimpiga** na ugonjwa mbaya, akakufa, kwa 44 A.D.

Hivi mtu huyu aliyeua Yakobo kupendeza Wayuda aliuawa yeye mwenyewe na Mungu anayeweza kuharibu mwili na nafsi vilevile katika gehena. "Yo yote mtu (**Herode**) anayopanda, ndiyo atakayovuna" (Gal. 6:7).

### D. Safari ya kwanza ya kuhubiri ya Paulo: Galatia (12:24 – 14:28)

**12:24** Lakini Habari Njema ilikaa kuenea. Mungu anatumika na kasirani ya watu kwa sifa yake, na atafunga baki la kasirani (Zab. 76:10). Anaharibu shauri la mataifa, lakini shauri la Bwana linasimama milele (Zab. 33:10, 11).

**12:25** Nyuma ya **kumaliza kazi yao** kwa **Yerusalema,** ndiyo kufikisha zawadi ya waamini wa Antiokia, **Barnaba na Saulo** walirudi kwa Antiokia. **Walipeleka Marko pamoja nao.** Marko alikuwa mtoto wa ndugu ya **Barnaba**, na aliandika Habari Njema ya pili kwa wakati wa nyuma.

Hatujui kama **Barnaba na Saulo** walikuwa katika **Yerusalema** saa Yakobo alipouawa, wakati Petro alipofungwa, na wakati wa mauti wa Herode.

Walimu wengi wa Biblia wanafikiri sura 13 inaanza sehemu nyingine ya kitabu cha Matendo. Kuanza sasa Mtume Paulo alijulikana zaidi, na Habari Njema ilienea kwa Mataifa toka Antiokia katika Suria.

**13:1** Tuliona ndani ya sura 11 ya kwamba kulikuwa na **kanisa katika**

**Antiokia** sasa. Hawakuwa na kiongozi mmoja tu, lakini kulikuwa na **manabii na walimu** watano au zaidi. Tuliona mbele kwamba nabii alikuwa mtu aliyepewa na Roho Mtakatifu zawadi ya kupokea ufunuo toka Mungu na kuhubiri maneno haya kwa watu wengine. Hivi **manabii** walisema kwa ajili ya Bwana na kutabiri maneno yatakayotokea. **Walimu** walikuwa watu waliopewa na Roho Mtakatifu uwezo kuelezea watu wengine maana ya Neno la Mungu na kuwasaidia kulifahamu.

Haya ndiyo majina ya **manabii na walimu hawa:**

1. **Barnaba.** Tulisoma mbele juu ya mtumishi huyu mwema na mwaminifu wa Kristo aliyetumika pamoja na Paulo. Hapa jina lake linatajwa kwanza, labda kwa sababu aliokolewa mbele ya Paulo, au hesabu ya miaka aliyotumikia Kristo ilipita ile ya Paulo.
2. **Simeoni aliyeitwa Nigeri.** Jina lake linatufikirisha kwamba alizaliwa Myuda, wa jamii ya Wayuda wa Afrique. Labda alikuwa mweusi. Hatujui maneno mengine juu yake.
3. **Lukio wa Kurene.** Tunafikiri alikuwa mmoja wa watu toka Kurene waliofikia **Antiokia** kwa mwanzo kuhubiri Habari Njema ya Bwana Yesu (Mdo. 11:20).
4. **Manaeni** (jina lake katika Agano la Kale liliandikwa Menahemu). **Alipata nguvu pamoja na Mfalme Herode.** Ni neno la kushangaza ya kwamba hata kama alikaa karibu sana na mfalme yule mwovu **Herode** Antipa, alikuwa mmoja wa watu wa kwanza aliyeamini Bwana Yesu.
5. **Saulo**. Jina lake linatajwa kwa mwisho hapa, lakini yeye, kupita wengine alikuwa mwenye kuonyesha kweli ya Mungu kwa njia ya maisha yake na mafundisho yake.

Watu hawa watano wanaonyesha kwamba ndugu za kanisa la mwanzo walifungana pamoja na hawakufikiri rangi ya ngozi ya mtu. Neno kubwa halikuwa kama mtu alikuwa *nani,* lakini kama alikuwa mtu *wa nani.*

**13:2** Manabii na walimu hawa walikuwa wamekutana kwa maombi pamoja na kufunga chakula, labda pamoja na watu wote wa kanisa. **Walitumikia Bwana** (kwa kuomba pamoja) na kufunga (maana kujinyimia mahitaji ya miili yao) kusudi waweze kufika mbele ya Mungu bila vizuizo.

Lakini kwa sababu gani walikuwa wamekutana pamoja kwa maombi? Labda walikuwa na mzigo mkubwa rohoni kwa watu wa dunia hii nzima kusikia Habari Njema? Hatujui, na hatujui vilevile kama waliomba usiku mzima, lakini ni kama muda wa maombi yao ulipita muda sisi watu wa sasa tunaposhinda kwa makusanyiko yetu kwa maombi.

Wakati walipoomba, **Roho Mtakatifu** alisema nao **kuweka Barnaba na Saulo kwa kazi** ambayo alikusudi wafanye. Tukio hili linahakikisha kwamba **Roho Mtakatifu** ni mwenye nafsi anayeweza kusema na kufikiri na kuonyesha mapenzi yake, si roho ya kuvuta tu. Namna gani alijulisha habari hizi kwa manabii na walimu? Hatupewi jibu kwa ulizo hili, lakini ni kama alisema kwa njia ya mmoja wa manabii – au Simeoni au Lukio au Manaeni.

**Barnaba** alitajwa kwanza hapa, mbele ya **Saulo**, lakini wakati waliporudi kwa Antiokia Saulo alitajwa kwanza.

Shairi hili ni shairi kubwa sana kwa sababu linaonyesha namna **Roho Mtakatifu** alivyoongoza kanisa kwa wakati wa mwanzo, na namna wanafunzi walivyotambua maongozi yake.

**13:3** Wakati Roho Mtakatifu alipokwisha kufunua mapenzi yake, waliendelea na maombi na kufunga. Halafu watu wale watatu (Simeoni na Lukio na

Manaeni) **waliweka mikono juu ya** Barnaba na Saulo. Hili halikuwa tendo la kutiwa mikono la askofu kama ilivyo desturi ya Wakristo kwa wakati wa sasa. Lilikuwa tendo la kuonyesha ushirika wao na watu hawa wawili ndani ya kazi ambayo Roho Mtakatifu aliwaita kufanya. Hatusomi ndani ya Agano Jipya juu ya kuweka mkono kumpa mtu fulani amri kupitisha mkate na mvinyo kwa karamu ya ukumbusho, na kazi fulani nyingine ndani ya kanisa. Barnhouse aliandika,

> Kwa wakati wa sasa tunaanguka sana kama tukififikiri mtu mmoja anaweza kuwa na zawadi zote zinazohitajiwa kwa mtu kuwa kiongozi mzuri. Pahali pengine duniani kuna makanisa makubwa na mia za watu walio na kiongozi mmoja tu anayepaswa kuhubiri, kufariji, vivi hivi. Ona Waroma 12:6-8. … Si lazima kwa mwamini kujifunza ndani ya séminaire au université kwa kumwezesha kufundisha Neno la Mungu kwa watu. Akijua Maandiko na akipewa zawadi ya kuhubiri inampasa kutumika na zawadi hii kila mara anapopata njia.

Tukumbuke kwamba kwa wakati huu Barnaba na Saulo walikuwa wametumikia Bwana kwa kadiri ya miaka minane. Kwa saa hii watumishi wenzao kwa Antiokia walionyesha tu kwamba walishiriki nao ndani ya kazi hii ya kuhubiri Habari Njema kwa Mataifa.

Maana ya **wakawatuma waende zao** ilikuwa "waliwaruhusu kwenda" au "waliwafungua" wafanye kazi hii.

**13:4** Shairi hili linaanza habari za safari ya kwanza ya Paulo kwa kuhubiri, zinazoendelea kufika 14:26. Safari hii ilikuwa zaidi kuhubiri Habari Njema kwa Asia Ndogo. Kwa safari ya pili ya kuhubiri, Habari Njema ilifikia inchi ya Yunani. Safari ya tatu ilikuwa zaidi kwa wilaya ya Asia na mji wa Efeso, lakini wahubiri walifikia tena makanisa katika Asia Ndogo na Yunani vilevile. Safari hizi za kuhubiri ziliendelea kwa muda wa karibu miaka kumi na mitano.

(Wakati tunapoandika juu ya safari za kuhubiri za Paulo, tutaandika na herufi kubwa majina mazima ya miji wakati inapotajwa mara ya kwanza.)

Toka Antiokia katika Suria watumishi hawa wawili wa Kristo **walitelemuka kwenda SELEUKIA**, bandari karibu kilomètres 24 toka Antiokia. Toka pale **walikwenda na chombo** hata kisanga cha **KIPURO**.

**13:5** Nyuma ya kufikia **SALAMI,** kwa pwani ya mashariki ya Kipuro, walifikia **masunagogi** na kuhubiri **Neno la Mungu.** Mgeni mwanamume akifikia sunagogi, ilikuwa desturi kumpa njia kusoma au kueleza Maandiko. **Yoane** Marko alikuwa pamoja nao kwa wakati ule na **aliwatumikia**. Kwa njia ya kufikia sunagogi kwanza, Barnaba na Saulo walitimiza agizo la Mungu kwa Habari Njema kuhubiriwa kwanza kwa Wayuda, kisha kwa Mataifa.

**13:6** Toka Salami walipita kwa urefu mzima wa **kisanga kufika PAFO** kwa pwani wa mangaribi. Salami ulikuwa mji mkubwa wa biashara wa kisanga na **Pafo** ulikuwa mji mkubwa wa serikali.

**13:7, 8** Kwa Pafo walikutana na Myuda aliyekuwa **nabii wa uwongo na mchawi, jina lake Bara-Yesu** (*maana ya jina hili ni Mwana wa Yesu* au *wa Yosua*). Ni kama **mchawi** huyu alifungana na **mtawala** Mroma wa kisanga **Sergio Paulo**, mtu **mwenye akili**. **Mtu huyu aliita Barnaba na Saulo** kufika karibu naye kumfundisha **Neno la Mungu,** lakini **mchawi** alijaribu kuwazuiza; tunafikiri alikuwa akiongozwa na Shetani kuzuiza mahubiri ya Habari Njema.

Ndani ya shairi 8 mchawi aliitwa **Elema**, maana yake "mwenye hekima," ndilo jina lisilofaa hata kidogo.

**13:9, 10** Saulo alifahamu kwamba Sergio Paulo alitaka sana kujua kweli ya Mungu, na ya kwamba mchawi alikuwa adui ya kweli ya Mungu. Basi **Saulo**,

**akijaa Roho Mtakatifu**, akamhamakia na ukali sana. Akikazia mchawi macho, akamshitaki kuwa **mwenye kujaa hila na uovu wote.** Hakudanganywa na jina lake Bara-Yesu, lakini aliita Elema **mwana wa Shetani.** Mchawi alikuwa **adui ya haki yote** asiyeacha kupotoa kweli ya Mungu.

**13:11** Halafu, akiwa mtume na kupewa amri kama mtume, Saulo alitangaza kwamba Elema atakuwa mpofu **kwa wakati**. Kwa sababu alikuwa amejaribu kufunga wengine, kama yule mtawala, katika giza la roho, yeye mwenyewe ataazibiwa na upofu wa mwili. **Mara moja kunguku ilimwangukia na giza**, naye alipapasapapasa akitafuta mtu kushika mkono wake na **kumwongoza**.

Tunaweza kufikiri juu ya Elema kama mfano wa taifa la Israeli wasiotaka kupokea Bwana Yesu wao wenyewe, na waliojaribu vilevile kuzuiza wengine wasimpokee. Kwa sababu hii Mungu aliwapa upofu wa roho, lakini **kwa wakati tu.** Mwishoni baki lao waliotubu watageuka kwa Yesu kama Masiya na kuokolewa.

**13:12** **Mtawala** alishangaa sana wakati alipoona azabu ya ajabu toka Mungu kwa Elema, na alishangaa hata kupita juu ya **maneno** ambayo Barnaba na Saulo **walimfundisha**. Aliamini Bwana Yesu na roho ya kweli, mwamini wa kwanza kwa safari ile ya kwanza ya kuhubiri.

Jina la Mataifa la Saulo lilikuwa Paulo. Ona ya kwamba ndani ya shairi 9 Luka alianza kumwita *Paulo*, kama alama kwamba Habari Njema itaenea katikati ya Mataifa kupita na kupita.

**13:13** Maneno haya **"Paulo na wenzake"** yanaonyesha kwamba Paulo alikuwa amegeuka kiongozi chao. Toka **Pafo** walisafiri kwa kaskazini-mangaribi kwenda **PERGA** katika **PAMFILIA**. **Pamfilia** ilikuwa wilaya ya Waroma kwa pwani ya kusini ya Asia Ndogo. **Perga** ulikuwa mji wake mkubwa. Ulikuwa karibu kilomètres 11 toka pwani kwa mto Kestros.

Wakati walipofikia **Perga, Yoane** Marko aliachana nao, **akarudia Yerusalema.** Labda hakufurahi juu ya kupeleka Habari Njema kwa Mataifa. **Paulo** alifikiri kwamba ilikuwa vibaya sana kwa Marko kuacha hivi utumishi wake kwa Mungu, na hakumruhusu kusafiri pamoja nao kwa safari yao ya pili ya kuhubiri. Kwa sababu ya neno hili **Paulo** na Barnaba walitengana na hawakufanya safari nyingine tena pamoja (ona 15:36-39). Mwishoni Marko alikubaliwa na **Paulo** tena (2 Tim. 4:11).

Hakuna habari nyingine juu ya saa waliyoshinda katika **Perga**.

**13:14, 15** Nyuma yake walifikia **ANTIOKIA katika PISIDIA,** karibu kilomètres 160 toka Perga kwa upande wa kaskazini. Kama ilivyokuwa desturi yao, waliingia **sunagogi siku ya sabato.** Wakati **wakubwa wa sunagogi** walipomaliza kusoma Maandiko, waliona kwamba wageni waliofikia sunagogi walikuwa Wayuda na waliwapa njia **kusema kama wakiwa na neno la kufaa watu** waliokuwa pale. Nyuma ya miaka michache wahubiri wa Habari Njema hawakupewa ruhusa namna hii tena.

**13:16** Haikuwa desturi ya **Paulo** kuacha njia kuhubiri Habari Njema kupita bure, hivi **alisimama** na kusema na watu katika sunagogi. Ilikuwa desturi yake kukumbusha wasikiaji historia ya Wayuda kwanza na halafu kuongeza habari nyingine kufika matukio ya maisha na utumishi wa Kristo, kisha kutangaza habari za ufufuko wa Kristo na ya kwamba zambi zao zinaweza kusamehewa kwa njia ya Mwokozi, na kuonya watu kwamba ni hatari kukataa kumpokea.

**13:17** Alianza hotuba yake na kuwaambia kwamba Mungu alikuwa amechagua **Israeli** kuwa watu wake hapa duniani.

Aliendelea na kuwapasha juu ya wakati walipokuwa **wageni inchini mwa Misri,** na alitukuza neema ya Mungu ambayo iliwaondosha toka utumwa wa Farao kwa **mkono ulionyanyuliwa**.

**13:18** Kwa **miaka makumi ine** Mungu **alivumilia** manunguniko ya Israeli jangwani na aliwalinda.

**13:19-22** Tunafikiri ya kwamba wakati Paulo alipotaja **miaka mia ine na makumi tano** alianza na wakati wa Abrahamu, Isaka na Yakobo, na hata kufika mwanzo wa muda wa waamuzi.

Nyuma ya kuingia kwa Israeli katika inchi ya Kanana Mungu aliwapa **waamuzi kuwaongoza kufika wakati wa Samweli nabii.** Wakati **walipoomba kupewa mfalme** kwa sababu walitaka kuwa sawasawa na mataifa mengine, **Mungu aliwapa Saulo, mwana wa Kisi, mtu wa kabila la Benyamina;** alitawala kwa **miaka makumi ine**. Lakini Saulo **aliondoshwa** kwa kiti cha ufalme kwa sababu ya kuasi kwake, na Mungu **alinyanyua Daudi** kumkomboa. Mungu alisifu Daudi sana na kusema alikuwa **mtu aliyependeza moyo wake, atakayefanya mapenzi yake yote.** Shairi 22 linataja sehemu za Zab. 89:20 na 1 Sam. 13:14.

**13:23** Nyuma ya kupasha juu ya Daudi, haikuwa nguvu kwa Paulo kuendelea na habari za **Yesu, uzao** wa Daudi. Mtu mmoja alisema, "Hotuba zote za Paulo zilifikisha wasikiaji kwa Kristo." Labda ni nguvu kwa sisi kufahamu kipimo cha uhodari kilichohitajiwa kutangaza kwa watu wa **Israeli** kwamba **Yesu** alikuwa **Mwokozi** ambaye **Mungu** aliahidi kuwapa. Mawazo yao juu ya **Yesu** hayakupatana na masemo ya Paulo!

**13:24** Halafu Paulo alipasha tena juu ya utumishi wa **Yoane** Mbatizaji. Mbele ya **kuja** kwa Kristo (maana yake mwanzo wa utumishi wa Kristo katikati ya watu) **Yoane** alikuwa akihubiri habari za **ubatizo wa toba kwa watu wote wa Israeli.** Alikuwa ametangaza **kuja** kwa Masiya na kuwaambia **watu** kutubu kwa kujitayarisha kwa **kuja kwake.** Iliwapasa kuonyesha kwamba **walitubu** kwa njia ya kubatizwa ndani ya mto Yorodani.

**13:25** Yoane hakuruhusu watu kwa hata dakika moja kufikiri kwamba yeye ndiye Masiya ambaye Mungu aliahidi kutuma. **Kufika mwisho wa utumishi wake** alikaa kusema tena na tena kwamba **yeye si Yule** ambaye manabii walisema juu yake, na **hakustahili hata kufungua viatu vya miguu** ya **Yule** ambaye alitangaza kuja kwake.

**13:26** Paulo aliita wasikiaji wake **ndugu** na **wana wa uzao wa Abrahamu,** na aliwakumbusha kwamba **neno la wokovu huu lilitumwa** kwanza kwa taifa la Israeli. Yesu alifikia kondoo wapotevu wa nyumba ya Israeli, nao walikuwa watu wa kwanza waliosikia mahubiri ya Habari Njema toka wanafunzi.

**13:27, 28** Lakini **watu wa Yerusalema na watawala wao** hawakutambua Yesu kuwa Masiya ambaye walingojea kwa muda mrefu. Hawakufahamu kwamba ndiye ambaye **manabii** waliandika habari zake. Wakati waliposikia unabii juu ya Masiya toka Maandiko kila **sabato** hawakutambua kwamba unabii huu ulikuwa juu ya Yesu wa Nazareti, lakini wao wenyewe walitimiza maandiko haya kwa njia ya **kumhukumu**. **Hawakukuta neno lililofaa kufa ndani yake,** lakini hata hivi walimtoa kwa **Pilato auawe.**

**13:29** Sehemu ya kwanza ya shairi hili *'walipokwisha kutimiza'* ndio Wayuda waliotimiza Maandiko Matakatifu kwa njia ya kukataa Masiya. Kwa mwisho wa shairi hili *'wakamshusha toka mti'*, ndio Yosefu wa Arimatea na Nikodemo waliozika mwili wa Bwana Yesu na mapendo.

**13:30, 31** Ufufuko wa Yesu **toka wafu** ulijulikana wazi. **Watu waliopanda pamoja na** Yesu **toka Galilaya hata**

**Yerusalema** walikuwa kwanza hai na haikuwezekana kubisha ushuhuda wao.

**13:32, 33** Halafu mtume alitangaza kwamba **ahadi** ya kuja kwa Masiya **waliyopewa baba zao** katika Agano la Kale **ilikuwa imetimizwa** ndani ya Yesu. **Ilitimizwa** kwanza kwa kuzaliwa kwake katika Betelehemu. Paulo alitaja Zaburi 2:7, pahali Mungu aliposema, **"Wewe ndiwe Mwana wangu, siku hii ya leo nimekuzaa"** kuonyesha neno hili. Maana ya shairi hili haiko ya kwamba Kristo alianza kuwa Mwana wa Mungu wakati alipozaliwa katika Betelehemu. Alikuwa Mwana wa Mungu tangu milele, lakini alionekana kwa dunia kama Mwana wa Mungu kwa njia ya kuzaliwa kama mtu. Zaburi 2:7 halikani kwamba Kristo ni Mwana wa milele wa Mungu.

**13:34** Ndani ya shairi hili tunasoma juu ya ufufuko wa Yesu. Mungu **alimfufua toka wafu, asipate kurudia kuoza.** Halafu Paulo alitaja Isaya 55:3, **"Nitakupa maneno matakatifu ya Daudi."** Shairi hili ni nguvu kwa wasomaji wengine kufahamu. Kwa njia gani shairi hili toka Isaya linasema juu ya ufufuko wa Kristo? Ufufuko wa Mwokozi na agano la Mungu na **Daudi** yanafungana pamoja namna gani?

Mungu aliahidi **Daudi** kiti cha kifalme na ufalme wa milele, na mzao kuketi juu ya kiti kile cha kifalme kwa milele. Lakini **Daudi** alikufa na mwili wake ulioza. Ufalme ulibaki kwa wakati nyuma ya kufa kwa Daudi, lakini taifa la Israeli hawakuwa na mfalme kwa miaka kupita mia ine. Jamaa ya **Daudi** iliendelea kufika Yesu wa Nazareti. Yosefu alikuwa baba ya Yesu kwa njia ya sheria, lakini hakuwa baba yake kabisa, na kwa njia ya Yosefu Yesu aliriti haki ya ufalme wa **Daudi**, lakini Yesu alikuwa mzao wa **Daudi** kwa njia ya jamaa ya Maria.

Paulo alionyesha kwamba **ahadi** ya maneno matakatifu ambayo **Daudi** alipewa ilitimizwa ndani ya Kristo. Yeye ndiye mzao wa **Daudi** atakayeketi juu ya kiti cha kifalme cha **Daudi** kwa wakati wa kuja. **Amefufuliwa toka wafu** na kuishi kwa milele. Hivi agano la milele ambalo Mungu alifanya na **Daudi** linatimia kwa njia ya Kristo.

**13:35** Paulo aliongeza kusema juu ya neno hili kwa njia ya kutaja maneno ya Zaburi 16:10, **"Hutaachia Mtakatifu wako kuona kuoza."** Maana yake ndiyo tangu Bwana Yesu alifufuliwa toka wafu, mauti haina uwezo juu yake. Hatakufa tena kamwe, na mwili wake **hautaoza**.

**13:36, 37** **Daudi** alitaja maneno haya ya Zaburi 16:10, lakini hakuyasema juu yake mwenyewe. **Wakati alipokwisha kutumikia kizazi chake sawasawa na mapenzi ya Mungu,** alikufa na **alizikwa,** na mwili wake ulioza. Lakini Bwana Yesu **alifufuliwa** toka wafu siku ya tatu, mbele ya mwili wake kuweza **kuoza**.

**13:38** Ufufuko wa Kristo ulikuwa muhuri wa ukubali wa Mungu wa kazi ambayo Kristo alikuwa amefanya. Hivi sasa Paulo aliweza kutangaza usamehe **wa zambi**, akasema, **"Kwa huyu munahubiriwa usamehe wa zambi."**

**13:39** Lakini zaidi ya ile Paulo aliweza kutangaza kwamba kwa njia ya Kristo mwamini anahesabiwa haki katika maneno yote. Hili ndilo neno **Torati ya Musa** isiloweza kufanya kamwe.

Kuhesabia haki ndilo tendo la Mungu kwa njia yake anahesabia haki wenye zambi wanaopokea Mwana wake kuwa Bwana na Mwokozi wao. Ni tendo la haki ndani ya nia ya Mungu, na kwa njia yake mwenye zambi anaondolewa hatia yote. Mungu anaweza kuwa haki pamoja na kuondoa hatia ya mwenye zambi, kwa sababu Bwana Yesu Kristo alibeba azabu kwa zambi zake zote wakati alipokufa msalabani kwa ajili yake.

Labda wakati tunaposoma shairi hili

kwanza inaonekana ya kwamba **torati ya Musa** inaweza kutuhesabia haki toka maneno fulani, lakini kwa njia ya Kristo mtu anaweza kuhesabiwa haki toka maneno mengi mengine. Lakini haya si mafundisho ya shairi hili hata kidogo. **Torati** haikuweza kuhesabia mtu haki kamwe; iliweza kumhukumu tu. Paulo alisema hapa kwamba kwa njia ya kuamini Kristo mtu **anaweza kuhesabiwa hak**i toka kila zambi, kila hatia – ndilo neno lisilowezekana kwa njia ya **torati ya Musa.**

**13:40, 41** Mtume alimaliza hotuba yake na maonyo ya nguvu kwa wale ambao waliweza kujaribiwa kukataa kupokea wokovu ambao Mungu kwa rehema yake alitaka kuwapa. Alitaja maneno ya Hab. 1:5 (na labda sehemu za Isa. 29:14 na Mez. 1:24-31) pahali Mungu alipoonya **wenye kubeua** neno lake na kuwajulisha kwamba atawamwangia gazabu kubwa sana **wasiyoamini,** hata kama mtu akiwaambia mbele juu yake. Kwa wakati wa Paulo gazabu hili ni uharibifu wa Yerusalema kwa 70 A.D., lakini inasema vilevile juu ya hukumu ya milele ya Mungu kwa wale wanaokataa Mwana wake.

**13:42, 43** Kwa mwisho wa kusanyiko katika **sunagogi, wengi wa Wayuda na wageuzi** (ndio watu waliokuwa wamegeuka Wayuda) **walifuata Paulo na Barnaba** wakiweka roho sana juu ya maneno waliyokwisha kusikia, nao walikaa kuwatia moyo **kuendelea katika neema ya Mungu.**

**13:44** Nyuma ya juma moja Paulo na Barnaba walirudia sunagogi kuendelea na mafundisho yao pahali walipoacha juma la mbele. Karibu watu wote wa mji walikusanyika kusikia **Neno la Mungu.** Mafundisho ya wahubiri hawa wawili yalikuwa yamegusa roho za watu wengi.

**13:45** Lakini **Wayuda** wasioamini walikuwa na **wivu** na gazabu juu ya mafundisho haya ya namna nyingine ya Paulo, wakabisha maneno yake na matukano.

**13:46, 47** Haikuwa nyepesi kuogopesha Paulo na Barnaba. Walieleza kwamba walilazimishwa kuhubiri Habari Njema kwanza kwa Wayuda. Lakini kwa sababu Wayuda waliikataa na walijihukumu kama watu **wasiostahili kupokea uzima wa milele,** wahubiri walitangaza kwamba watahubiri kwa **Mataifa**. Walitaja Isaya 49:6 kama ruhusa yao kwa kufanya hivi. Ndiyo, Mungu alisema maneno haya kwa Masiya, **"Nimekuweka uwe nuru ya Mataifa, upate kuwa wokovu hata mwisho wa dunia."** Lakini Roho Mtakatifu aliruhusu watumishi wa Masiya kusema maneno haya juu yao wenyewe, kwani walikuwa watumishi wake kuleta **nuru** na **wokovu** kwa Mataifa.

**13:48** Tangazo hili lilikasirisha Wayuda, lakini lilifurahisha sana **Mataifa** waliokuwa pale. **Walitukuza Neno la Bwana** walilokwisha kusikia, na wote **waliokusudiwa kwa uzima wa milele waliamini.** Shairi hili linaonyesha mchaguo wa Mungu mwenye enzi. Inatupasa kuliamini hata kama labda ni nguvu kwa sisi kulifahamu. Biblia inafundisha wazi kwamba Mungu alichagua wengine mbele ya kuumbwa kwa dunia wawe ndani ya Kristo. Na inafundisha vilevile ya kwamba mtu amepewa kutaka kwake, naye ni huru kuchagua, na kama akipokea Yesu Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wake ataokolewa. Hivi Biblia inafundisha kweli hizi mbili: mchaguo wa Mungu, na ya kwamba mtu ni huru kuchagua vilevile. Kwa nia ya Mungu kweli hizi mbili zinapatana. Sisi wenye nia za binadamu tunafazaishwa sana, lakini hata hivi inatupasa kuziamini.

Watu wanalaaniwa kwa milele kwa sababu wao wenyewe wanachagua kutokuamini Mwokozi, si kwa sababu Mungu anachagua kuwalaani. Kama

watu wote wa dunia wangalipokea hukumu ambayo wanastahili kupata, wangalipotea wote. Lakini Mungu kwa neema yake anaokoa wengine. Ni ruhusa yake kufanya hivi? Kabisa. Mafundisho ya uchaguo yanampa Mwenyezi Mungu heshima ambayo anastahili kuwa nayo kutawala ulimwengu na kufanya neno lo lote analochagua, naye hachagui kufanya kamwe neno lo lote linalokosa haki au mapendo. Mwalimu Erdman aliandika:

> Enzi ya Mungu ni kamili; lakini hatumiki nalo kuhukumu watu ambao wanapaswa kuokolewa, lakini zaidi kwa kuokoa watu wanaostahili kupotea.[10]

**13:49, 50** Hata kama Wayuda walishindana sana na kutangazwa kwa Habari Njema, **Neno la Mungu likaenea katika inchi ile yote. Wayuda** walioshindana nalo walijaribu kwa kila njia kulizuiza. Walisukuma **wanawake wenye haki** na heshima waliokuwa wamepokea dini ya Wayuda, na **wakubwa wa mji** kutesa **Paulo na Barnaba** sana na kuwafukuza toka mipaka yao.

**13:51, 52** Kama Bwana Yesu alivyoagiza katika Luka 9:5 na 10:11, wahubiri **waliwakungutia mavumbi ya miguu yao,** wakakwenda **IKONIO**. Lakini Wakristo hawakufikiri juu ya tukio hili kama alama ya kwamba Habari Njema ilishindwa. Tunasoma kwamba **walijazwa furaha na Roho Mtakatifu.**

**14:1, 2** Kama pahali pengine, kulikuwa na **sunagogi** katika **Ikonio**, na Paulo na Barnaba walipewa ruhusa kuhubiri, kama ilivyokuwa desturi ya Wayuda kwa wakati ule. Roho Mtakatifu alitumika na uwezo sana na mahubiri yao hata **Wayuda wengi** na Wayunani waliofuata dini ya Wayuda waliamini Bwana Yesu. Neno hili lilikasirisha **Wayuda** wale waliokataa kutii Habari Njema, na **waliamsha uadui katikati ya Mataifa juu ya waamini.** Ndani ya kitabu cha Matendo Wayuda wasioamini walianzisha mateso mengi juu ya mitume hata kama wao wenyewe hawakuwatendea mabaya. Walikuwa mafundi kabisa ndani ya kazi ya kusukuma Mataifa kutimiza mashauri yao maovu.

**14:3** Hata kama mitume walijua matata ilikuwa karibu, walikaa kuhubiri kwa **uhodari** katika jina la **Bwana**, naye alisimamia mafundisho yao kwa njia ya kuwapa **alama na maajabu** yafanyike kwa mikono yao. **Alama na maajabu ni mbalimbali**. Alama linafundisha neno; ajabu linaamsha kustaajabu, na hata hofu ndani ya roho ya watu.

**14:4-7** Lakini watu katika mji walitengana; **wengine walikuwa kwa upande wa Wayuda** na **wengine kwa upande wa mitume.** Mwishoni **Mataifa na Wayuda** wasioamini walikusudi kurukia **mitume** na kuwatendea jeuri. Wakisikia habari hizi walikimbilia **LISTRA** na **DERBE** wasitupiwe mawe. Listra na Derbe ilikuwa **miji ya LIKAONIA** kwa upande wa katikati ya Asia Ndogo. Walikaa **kuhubiri Habari Njema** na bidii kama mbele katika inchi ile yote.

Wakati Paulo na Barnaba walipotambua walikuwa katika hatari ya kutupiwa mawe, **walikimbilia Likaonia.** Mara nyingine hawakukimbia hata kwa wakati wa hatari. Kwa nini walikimbia mara nyingine, lakini walikaa pahali pa hatari mara nyingine? Neno moja tunaloona wazi sana ndani ya kitabu cha Matendo ndilo maongozi ya Roho Mtakatifu. Watu hawa waliishi na ushirika wa karibu sana na Bwana. Wakikaa ndani yake, Roho Mtakatifu aliweza kuwafunulia nia na mapenzi ya Mungu. Waliweka roho sana juu ya ushirika huu wa karibu na Bwana.

**14:8, 9 Katika Listra** mitume walikutana na mtu aliyekuwa **kiwete** tangu kuzaliwa kwake. Mtu huyu alisikiliza **masemo ya Paulo** sana, na Paulo alitambua kwamba alikuwa na **imani ku-**

**pata kuponyeshwa mwilini.** Hatusomi kama **Paulo** alijua neno hili namna gani, lakini tunaamini mhubiri wa Habari Njema anawezeshwa kufahamu hali ya roho ya watu ambao anajaribu kuleta kwa Bwana. Ni kama anaweza kujua kama mtu fulani anasumbushwa sana na mzigo wa zambi zake au sivyo.

**14:10-12** Mara moja wakati **Paulo** alipoagiza mtu huyu **kusimama wima**, … **alisimama upesi, akatembea.** Ajabu hili lilitokea mbele ya **watu** wengi waliokuwa wakiangalia na kushangaa sana juu ya maneno yaliyotokea, kwa sababu Paulo **alisema kwa sauti kubwa**. Walifikiri miungu yao imewafikia kwa mifano ya Paulo na Barnaba, na walitaka kuwaabudu. Walifikiri **Barnaba** ndiye **Zeu**, mungu mkubwa, na **Paulo** ni **Merkurio**, mjumbe wa Zeu, kwa sababu ndiye msemaji.

**14:13** Hata **kuhani la Zeu** alifikiri mungu wao umewafikia, akatoka **hekaluni mwake mbele ya mji na ngombe na taji za maua** kutoa zabihu kubwa. Maneno haya yalikuwa hatari kwa imani ya Wakristo, hata kupita mateso yote mengine. Mtumishi wa Bwana akibarikiwa ndani ya utumishi wake kwa Bwana, ni hatari kwa watu ambao anajaribu kuwasaidia na maneno ya roho, kuheshimu mtumishi huyu wa Kristo kupita Bwana wake.

**14:14, 15a Barnaba na Paulo** hawakufahamu mara moja maneno watu waliyokusudi kufanya kwa sababu hawakujua lugha yao. Wakati walipotambua kwamba watu walikuwa karibu kuwaabudu kama miungu, **walipasua mavazi yao** mara moja kuonyeshea watu huzuni yao na ya kwamba hawakukubali maneno haya hata kidogo. **Walikwenda mbio kuingia katika makutano** na walipaza sauti zao kuwaonya wasifanye maneno namna hii. Hawakuwa miungu, lakini **watu tu wenye tabia namna moja nao**. Walikuwa wamefika katikati yao kuwaletea habari njema kwamba ilipasa watu **kugeuka toka** maneno haya ya bure, na sanamu zisizo na uzima, na kuanza kufuata **Mungu aliye hai.**

**14:15b-17** Ona ya kwamba Paulo na Barnaba walitaja mashairi toka Agano la Kale kwa Wayuda, lakini hawakufanya hivi kwa Mataifa. Walianza kuwapasha habari za kuumbwa kwa dunia, ndizo habari watu wa mataifa yote wanafurahi kusikia. Wahubiri walieleza ya kwamba **katika siku zilizopita** Mungu **aliacha mataifa yote waende katika njia zao wenyewe.** Lakini hata kwa wakati ule hakujiacha pasipo ushuhuda kwa njia ya vitu ambavyo aliumba na aliwapatia. Ni **yeye** ambaye aliwapa **mvua** … na **mavuno, akishibisha mioyo** yao **na chakula na furaha.**

**14:18** Basi watu walisikiliza masemo yao, wakakubali kuacha **kutoa zabihu** kwa watumishi hawa wa Bwana.

**14:19, 20 Wayuda wasioamini toka Antiokia na Ikonio** walifuata **Paulo** na Barnaba hata Listra, wakaweza kugeuza Mataifa kuwa adui za wahubiri. Watu wale wale ambao walitaka kuwaabudu kama miungu mbele **walitupia Paulo mawe sasa na kumkokota inje ya mji, wakizania** amekwisha kufa.

Paulo **aliuawa kweli** kwa njia ya kutupiwa mawe? Kama alifikiri juu ya tukio hili wakati alipoandika 2 Kor.12:2, yeye mwenyewe hakujua. Tunaweza kusema tu kwamba kupona kwake kulikuwa ajabu. **Wakati wanafunzi walipomzunguka, alisimama na kuingia mji tena** pamoja nao. **Kesho yake yeye na Barnaba walikwenda zao hata DERBE.**

**14:21** Wahubiri hawakuweka roho zaidi juu ya kuepuka hatari, hivi nyuma ya **kuhubiri Habari Njema** kwa Derbe **walirudia LISTRA,** pahali Paulo alipotupiwa mawe.

Hatuoni jina la Timoteo hapa, lakini labda aliokolewa kwa sababu ya kusikia mahubiri ya Paulo wakati huu. Wakati

Paulo alipofikia **Listra** mara ya nyuma Timoteo alikuwa amegeuka mfuata aliyeheshimiwa na waamini wa pale (Mdo. 16:1,2). Kwa wakati wa nyuma Paulo alimwita "mwana wangu wa kweli katika imani" (1 Tim. 1:2), lakini labda alikuwa "mwana wa kweli" kwa njia ya kuiga maisha na utumishi wa Paulo.

Wakati wahubiri walipomaliza kazi yao kwa **Listra** walikwenda tena kwa **IKONIO** na **ANTIOKIA** katika PISIDIA, pahali makanisa yaliposimamishwa mbele. Kwa mawazo yao haikutosha kwa watu kuamini Habari Njema tu, lakini walijaribu kuwapatisha nguvu katika imani, zaidi kwa njia ya kuwafundisha kweli ya kanisa na ya kwamba Mungu anaweka roho sana juu yake.

Mwalimu Eerdman alisema,

> Lilikuwa kusudi la Paulo kwa ndugu za kila kanisa ambalo alianza kuweza kuongoza kanisa wao wenyewe, na kuanza makanisa mengine wakati hesabu ya waamini ilipoongezeka.[6]

**14:22** Hivi **aliwapatisha nguvu katika imani** kwa njia ya kuwafundisha neno la Mungu. Ona masemo yake katika Kol. 1:28, 29, "tukionya kila mtu na kufundisha kila mtu na akili yote, ili tupate kuleta kila mtu mtimilifu katika Kristo Yesu. Kwa sababu hii ninajitaabisha, nikishindana na nguvu kwa kadiri ya kutenda kazi kwake anayetenda kazi ndani yangu kwa nguvu."

Waliwaonya vilevile **wadumu katika imani,** kwa sababu waamini walikuwa wakiteswa sana kwa wakati ule, na kwa sababu **kwa mateso mengi imetupasa kuingia katika ufalme wa Mungu.** Shairi hili linasema juu ya **ufalme wa Mungu** kwa wakati wa kuja wakati waamini watakaposhiriki utukufu wa Kristo. Msiyeamini anaingia **ufalme wa Mungu** wakati anapozaliwa tena. **Mateso** hayawezi kuokoa mtu. Lakini watu **wanaoingia ufalme wa Mungu** kwa njia ya imani kwa wakati wa sasa wajue kwamba watakutana na **mateso** mengi njiani kwendea utukufu ulio mbele. "Tukiteswa pamoja naye, ili tutukuzwe pamoja naye vilevile" (Rom. 8:17b).

**14:23** Kwa wakati huu wahubiri **walichagua wazee katika kila kanisa.** Tuone maneno mengine juu ya neno hili:

1. Wazee katika Agano Jipya walikuwa wanaume wenye kukomea kwa maneno ya Mungu walioongoza maneno ya kanisa. Waliitwa waangalizi vilevile.
2. Ndani ya Matendo wazee hawakuchaguliwa mara moja wakati kanisa jipya liliposimamishwa. Mtume alifanya hivi wakati alipofikia kanisa lile tena nyuma. Ndani ya muda nyuma ya kusimamishwa kwa kanisa jipya na kufika kwa mtume mara ya pili, ilionekana watu gani walikuwa wamechaguliwa na Roho Mtakatifu kuwa wazee.
3. Wazee waliwekwa na mitume au watu waliotumika pamoja nao. Kwa wakati ule Agano Jipya halijaandikwa bado kuleta mafundisho juu ya kazi ya wazee, lakini mitume walijua maneno haya na waliweza kuchagua watu waliostahili kwa kazi hii.
4. Hakuna mitume kwa wakati wa sasa kuchagua wazee lakini kuna mafundisho juu ya kazi yao katika 1 Timoteo 3 na Tito 1. Hivi ingepasa watu wa kila kanisa kuweza kutambua watu gani ndani ya kanisa lao wanaostahili kuwa wachungaji wa kondoo.

Nyuma ya **kuomba pamoja na kufunga**, Paulo na Barnaba waliweka waamini katika **mikono ya Mungu**. Tunashangaa kuona makanisa haya kusimamishwa mbio hivi nyuma ya kupokea mafundisho toka mitume kwa muda mfupi tu, na kwa makanisa haya kuendelea vizuri peke yao kwa Bwana.

Neno hili liliwezekana kwa uwezo mkubwa wa Roho Mtakatifu. Uwezo huu ulionekana ndani ya maisha ya watu kama Paulo na Barnaba. Kila pahali walipokwenda waligusa watu na uwezo kwa Mungu. Watu walitambua kwamba walikuwa watu wa Mungu kabisa. Waliweza kuona kwamba mahubiri yao mbele ya watu yalipatana na mwenendo wao, ndio ushuhuda wa uwezo mkubwa.

Mashairi 21-23 yanaonyesha shauri la mitume kwa kazi yao:

1) kuhubiri Habari Njema;
2) kufundisha waamini wa sasa;
3) kuanza makanisa; na
4) kuyapatisha nguvu.

**14:24-26 Nyuma ya kupita** katikati ya **Pisidia** walisafiri kwa upande wa kusini hata **PAMFILIA**. Wakafikia **PERGA** tena, kisha walitelemuka mpaka **ATALIA**, ndio bandari, wakasafiri toka pale baharini kufika **ANTIOKIA** katika Suria, ndio mwisho wa safari yao ya kwanza ya kuhubiri. Ni toka pale **waliwekwa katika neema ya Mungu kwa kazi waliyokwisha kutimiza.**

**14:27** Bila shaka waamini walifurahi sana wakati **walipokusanyisha kanisa** kwa Antiokia kusikia habari za safari ya kuhubiri ya watumishi hawa wawili wa Mungu. Na unyenyekevu waliwaelezea **yote ambayo Mungu alifanya pamoja nao, na namna alivyofungua mlango wa imani kwa Mataifa.** Hawakupasha juu ya kazi yao kwa **Mungu,** lakini habari za kazi ambayo ilipendeza **Mungu** kufanya kwa njia yao.

**14:28 Walibaki** katika Antiokia kwa **wakati mrefu pamoja na wanafunzi**, labda mwaka mmoja au hata miaka miwili.

## MAFUNDISHO JUU YA UTARATIBU WA KUENEZA HABARI NJEMA

Ni neno la kufurahisha kabisa kusoma juu ya wanafunzi wachache walioishi kwa pahali pasipojulikana duniani, waliopewa kazi ya utukufu ya kueneza Habari Njema, na namna wao wote walivyojitoa na roho moja kuifanya.

Mara nyingi waamini wa mji wao walizungumuza na watu ambao walikaa pamoja nao pamoja na kufanya kazi yao ya kila siku.

Mitume na watu wengine vilevile walisafiri kwa inchi mbalimbali wakihubiri Habari Njema na kuanza makanisa. Walikwenda watu wawili au zaidi pamoja. Mara nyingine kijana alikwenda pamoja na mzee, kama Timoteo na Paulo.

Habari Njema ilienezwa zaidi kwa njia mbili: kwa njia ya mwamini mmoja kusemezana na msiyeamini mmoja, na kwa njia ya mahubiri kwa makusanyiko ya watu. Katika Matendo karibu kila mara wahubiri hawakutayarisha hotuba zao mbele, lakini walihubiri kwa sababu ya neno fulani lililotukia gafula wakati wenyewe.

Mitume na wale waliokuwa pamoja nao waliongozwa na Roho Mtakatifu, na mara nyingi maongozi haya yalihakikishwa na ndugu za kanisa. Hivi tunasoma juu ya manabii na walimu kwa Antiokia wakiwekea Barnaba na Paulo mikono yao na kuwatuma kwa safari yao ya kwanza ya kuhubiri (Mdo. 13:2). Na tunasoma kwamba Timoteo alishuhudiwa vizuri na ndugu waliokuwa katika Listra na Ikonio mbele ya kuanza kusafiri pamoja na Paulo (Mdo. 16:2). Na Paulo na Sila waliombewa tena na ndugu za Antiokia wapewe neema ya Mungu mbele ya kuanza safari yao ya pili ya kuhubiri (Mdo.15:40).

Watu wengine wanafundisha ya kwamba ilikuwa desturi yao kwendea miji mikubwa kwanza kuanza makanisa ili waamini wa makanisa yale waweze kufikisha Habari Njema kwa vijiji kando kando. Tunafikiri ilikuwa desturi yao kutii maongozi ya Roho Mtakatifu na kwenda pahali gani alipowatuma, au kwa mji mkubwa au mdogo. Roho

Mtakatifu aliondosha Filipo kwa Samaria pahali Habari Njema ilipohubiriwa na uwezo na baraka, kusudi akutane na mtu mmoja kwa njia inayokwenda Gaza (Mdo. 8:26-40). Na aliongoza Paulo kwenda Beroya (Mdo. 17:10), ndio mji uliokuwa mbali. Aliongoza watumishi wake, si kwa kawaida ya watu, lakini kufuata mapenzi yake mwenyewe.

Pahali watu walipopokea na kuamini Habari Njema makanisa yalisimamishwa. Waamini ndani ya makanisa haya waliongoza maneno yao ya mali, kazi ya kuhubiri Habari Njema, vivi hivi, wao wenyewe. Mitume waliwafikia tena kupatisha waamini nguvu na kuwatia moyo (Mdo. 14:21, 22; 15:41; 20:1,2), na kuchagua wazee (Mdo. 14:23).

Mara nyingine mitume na wale waliosafiri pamoja nao walitumika kazi na mikono kwa kupata mali kwa mahitaji yao (Mdo. 18:3; 20:34); mara nyingine makanisa na ndugu mmoja mmoja waliwapa zawadi kuwasaidia (Flp. 4:10, 15-18). Paulo alitumika kazi kwa kupata mali kwa mahitaji yake mwenyewe na ya watu ambao walikuwa pamoja naye (Mdo. 20:34).

*Walitumwa* kwa kazi ya Mungu na kanisa lao, na *kusaidiwa na zawadi* toka makanisa mengine vilevile, lakini *hawakutawaliwa* na makanisa haya. Walikuwa watumishi wa Bwana, na walikuwa huru kutangaza Neno zima la Mungu bila kufichia wasikiaji wao neno lo lote ambalo liliweza kuwa na faida kwao (Mdo. 20:20).

Kwa mwisho wa safari zao za kuhubiri Habari Njema walirudia kanisa ambalo liliwatuma kwa kazi ya Bwana, na kutoa habari namna gani Mungu alitumika kwa njia yao (Mdo. 14:26-28; 18:22, 23). Ni vizuri kwa watumishi wa Mungu wa kila muda kuwaiga ndani ya maneno haya. ❖

### E. Baraza kwa Yerusalema (15:1-35)

**15:1** Kuna habari katika Gal. 2:1-10 vilevile juu ya mabishano katika kanisa kwa Antiokia juu ya maneno ya tohara. Tukisoma habari katika Mdo. 15 na Gal. 2 pamoja tunaona ya kwamba watu **wengine** (si waamini wa kweli) walitoka **Yerusalema** kwenda Antiokia, na kuhubiri kule ya kwamba inapasa Mataifa **kutahiriwa** kwa kuweza **kuokolewa**. Haikutosha kuamini Bwana Yesu Kristo tu; lazima watii sheria **ya Musa** vilevile. Mafundisho haya hayapatani na Habari Njema ya neema ya Mungu. Habari Njema ya kweli ya neema inafundisha kwamba Kristo alitimiza msalabani kazi iliyohitajiwa kwa wokovu wa watu. Mwenye zambi anahitaji kumpokea kwa imani tu. Habari Njema si ya neema tena wakati inapochanganywa na matendo mema ya watu. Habari Njema ya neema inategemea Mungu tu, si watu. Tukiongeza matendo ya watu juu yake, wokovu si zawadi tena, lakini inageuka deni. Lakini wokovu *ni* zawadi; hakuna kazi sisi tunayoweza kufanya kwa kupata au kutustahilisha kuupokea.

**15:2, 3 Paulo na Barnaba** walishindana na nguvu na walimu hawa wa sheria, wakijua kwamba walifika kuondolea waamini wa Mataifa uhuru wao katika Kristo.

Hapa kwa Matendo 15 tunaona kwamba ndugu katika Antiokia walituma **Paulo na Barnaba na wengine … kwenda Yerusalema kwa mitume na wazee.** Katika Gal. 2:2 Paulo alisema alikwendea Yerusalema kwa ufunuo. Maneno haya hayabishi habari katika Mdo. 15. Roho Mtakatifu alifunulia Paulo kwamba ilimpasa kwenda, na alifunulia kanisa katika Antiokia kwamba iliwapasa kumtuma. Kwa safari yao kwenda **Yerusalema** walipita kwa **Foiniki na Samaria** na kupasha habari kwamba **watu wa Mataifa wanaokolewa** vilevile, **wakafurahisha** ndugu zote.

**15:4 Wakati** Paulo alipofikia **Yerusalema,** alikwenda kuona **mitume na wazee** kwanza na kuwapasha peke yao

habari zote za Habari Njema aliyohubiri kwa Mataifa. Walikubali kwamba ilikuwa Habari Njema ile waliyohubiri kwa Wayuda.

**15:5** Ni kama ndani ya kusanyiko la kanisa zima **Wafarisayo wengine** waliokuwa waamini **walisimama** na kusema ni lazima kwa waamini Mataifa kutahiriwa na **kutii torati ya Musa** kwa kuweza kuwa wafuata wa kweli.

**15:6** Tukisoma shairi hili tungeweza kufikiri kwamba **mitume na wazee** tu walikuwa pale kuwaza juu ya neno hili, lakini ni kama shairi 12 linaonyesha kwamba watu wote wa kanisa walikuwa pale vilevile.

**15:7-10** Wakati **Petro** aliposimama kusema, labda walimu wa sheria waliwaza mafikiri yake yatapatana na mafikiri yao kwa sababu alikuwa mtume kwa wenye tohara. Sivyo. **Petro** aliwakumbusha kwamba **Mungu** aliamuru mbele **kwa Mataifa kusikia Habari Njema toka** kinywa chake. Neno hili lilifanyikana nyumbani mwa Kornelio. Wakati **Mungu** alipoona kwamba watu wale wa **Mataifa** walikuwa na imani, **aliwapa Roho Mtakatifu, namna alivyofanya** kwa Wayuda siku ya Pentekote. Kwa wakati ule **Mungu** hakulazimisha Mataifa hawa kutahiriwa. Hakuwatendea namna nyingine na waamini Wayuda. Alisafisha **mioyo yao kwa imani**. **Mungu** alikuwa amepokea **Mataifa** hawa kwa sababu ya **imani** yao, si kwa sababu walishika sheria. Hivi **Petro** aliuliza kwa sababu gani wataweka **mzigo** wa torati juu ya shingo zao, – **mzigo** ambao hata **baba zao** wala **wao wenyewe hawakuweza kubeba.** Torati haikuweza kuokoa mtu kamwe. Kazi yake ilikuwa kuhukumu watu, si kuwahesabia haki. Torati inatujulisha zambi, lakini haiokoi mtu toka zambi.

**15:11** Petro alijumlisha maneno haya hivi: Aliamini kabisa ya kwamba **kwa njia ya neema ya Bwana Yesu** (si kwa njia ya kushika torati) **sisi** (Wayuda) **tutaokolewa sawasawa nao** (Mataifa). Tungefikiri kwamba Petro, Myuda, angesema ya kuwa Mataifa wataokolewa namna Wayuda walivyookolewa. Lakini **neema** ilishinda maneno ya kabila, hivi alitaja Mataifa kwanza.

**15:12** Wakati Petro alipomaliza kusema, **Barnaba na Paulo** walipasha namna **Mungu** alivyotumika katikati ya **Mataifa** kwa njia ya **alama na maajabu** wakati walipohubiri Habari Njema.

**15:13, 14** Petro alikuwa amepasha namna **katika siku za kwanza,** Bwana alivyochagua kwa **Mataifa** kusikia Habari Njema kwa njia yake. Paulo na Barnaba walitoa ushuhuda wa namna Bwana alivyotumika kwa njia yao kuwaletea Habari Njema. Halafu **Yakobo** alisema na amri kwamba ilikuwa kusudi la Mungu kwa wakati ule kuchagua **toka Mataifa … watu kwa jina lake.** Masemo yake yalipatana na maneno ambao **Petro** aliyokwisha kusema.

**15:15-19** Halafu Yakobo alitaja sehemu ya Amo. 9:11-12. Ona ya kama hakusema wokovu wa **Mataifa** ulitimiza unabii wa Amosi, lakini *ulipatana* na **maneno ya manabii.** Hivi waamini wasishangae kuona kwamba **Mungu** aliangalia **Mataifa** na kuchagua toka kwao wengine kuokolewa kwani neno hili lilitabiriwa wazi katika Agano la Kale. **Mungu** ametabiri kwamba **Mataifa** watabarikiwa kama Mataifa, si kama waamini Wayuda.

Maneno toka Amosi yanatangulia utawala wa Kristo kwa miaka elfu moja wakati atakapokaa juu ya kiti cha ufalme wa **Daudi** na wakati **Mataifa** watakapotafuta **Bwana**. Yakobo *hakusema* kwamba unabii ule ulikuwa ukitimizwa kwa wakati alipokuwa akisema, lakini kwamba wokovu wa **Mataifa** kwa wakati ule *ulipatana* na maneno ambayo Amosi alisema yatatokea nyuma.

Masemo ya hotuba ya Yakobo yalifuatana hivi: Kwanza **Mungu** ataangalia

**Mataifa kusudi achague kwao watu kwa jina lake.** Hili ndilo neno lililokuwa likitokea wakati Yakobo alipokuwa akisema (na linatokea hata sasa). **Mataifa** waliokwisha kuokolewa walipokewa ndani ya kanisa pamoja na Wayuda waliookolewa. Kwa wakati ule **Mataifa** wengine walikuwa wakiokolewa, lakini kwa wakati wa nyuma Mataifa wengi zaidi wataamini wakati Kristo atakaporudi, na kurudisha taifa la Israeli tena, na **kuokoa Mataifa wote watakaoitwa** na **jina** lake.

Yakobo alifikiri juu ya maneno yaliyotokea kwa wakati ule kama mara ya kwanza Mungu aliyofikia **Mataifa,** na ya kama yalipatana na maneno Amosi aliyotabiri juu ya Kristo kufikia **Mataifa** wakati wa kuja saa atakaporudi tena kama Mfalme. Matukio haya mawili ni mbalimbali lakini *yanapatana*.

Hivi matukio haya yalifuatana hivi:

1. Kuchaguliwa toka **Mataifa watu kwa jina la Mungu** (sh.14) kwa muda huu wa neema.
2. Kurudishwa kwa sehemu ya taifa la Israeli watakaokuwa waamini wakati Kristo atakaporudi (sh.16).
3. Wokovu wa Mataifa nyuma ya kurudishwa kwa Israeli (sh.17). **Mataifa** haya wanaitwa hapa **Mataifa yote walioitwa kwa jina langu.**

Maneno Yakobo aliyotaja toka Amosi 9:11-12 si namna yaliyoandikwa katika Agano la Kale. Labda Yakobo aliyataja kwa Kiyunani, na vilevile Roho Mtakatifu aliyeongoza mwandishi katika Agano la Kale kuchagua maneno ambayo ilimpasa kuandika, aliruhusu Yakobo kutumia maneno mengine kusaidia mahitaji ya wakati ule.

**Nyuma ya maneno haya nitarudi** (sh.16)**.** Yakobo alikuwa amesema mbele kwamba lilikuwa shauri la Mungu kwa muda huu wa sasa kufungua njia kwa **Mataifa** kuokolewa. Hawataokolewa wote, lakini Mungu atakamata **toka kwao watu kwa jina lake.** Sasa Yakobo aliongeza ya kwamba nyuma ya **maneno haya**, ndiyo kuitwa kwa kanisa toka Mataifa, Mungu **atarudi** na **kujenga tena nyumba ya Daudi iliyoanguka. Nyumba ya Daudi** ndiyo jamaa yake. Kwa wakati wa nyuma jamaa ya kifalme itasimama tena na kiti cha kifalme cha **Daudi,** na Kristo ataketi juu yake kama mfalme. Halafu Israeli litakuwa mfereji wa baraka kwa dunia nzima. **Baki la watu watatafuta Bwana, hata Mataifa yote wanaoitwa kwa jina lake.**

Hivi, kwa sababu ni kusudi la Mungu kuita watu **toka Mataifa kuwa watu wake,** Yakobo alisema haifai kusumbusha **Mataifa** na kuwalazimisha kutii sheria ya Musa. Walihitaji imani tu kwa kupata wokovu.

**15:20** Hata hivi alifikiri ilifaa waandike barua kwa kanisa katika Antiokia, vizuri **wajitenge na maneno yaliyochafushwa na sanamu, na uzini, na nyama zilizosongwa, na damu.** Tukisoma maneno haya labda tunafikiri kwamba Yakobo aliwalazimisha tena kushika sheria. Lakini sivyo. Maonyo haya si kwa kuwawezesha kupata wokovu. Ni kusaidia waamini Wayuda na waamini Mataifa *kupatana* vizuri. Haikupasa watii maonyo haya kwa kupata wokovu, lakini kwa kuepuka magomvi katika kanisa kwa mwanzo wake.

Haya ndiyo maneno yaliyokatazwa:

1. **Maneno yaliyochafushwa na sanamu,** kama vyakula vilivyotolewa kwa sanamu (sh. 29). Kama waamini Mataifa wakikaa kula vyakula namna hii, waamini Wayuda wangeweza kuwa na shaka kama waliacha kuabudu sanamu. Hata waamini wa Mataifa walikuwa huru kula chakula namna hii, neno hili lingeweza kuwa kikwazo kwa ndugu zao Wayuda, hivi haifai wafanye hivi.

2. **Uzini**.[11] Hii ilikuwa zambi iliyofunga Mataifa sana na kwa sababu hii ilipasa Yakobo kuitaja hapa pamoja na maneno haya mengine. Agizo la kuepukana na zambi hii halikuondoshwa kamwe ndani ya Biblia. Ni agizo kwa watu wa kila wakati.

3. **Nyama zilizosongwa.** Mungu alitoa agizo hili kwanza kwa wakati wa Noa, nyuma ya garika (Mwa. 9:4). Hivi ni agizo kwa watu wote wa dunia, si kwa taifa la Israeli tu.

4. **Damu.** Agizo hili lilitolewa kwanza kwa Mwanzo 9:4 vile vile, mbele ya Torati ya Musa. Agano hili na Noa halikuondoshwa kamwe, hivi maagizo haya ni kwa wakati wa sasa vilevile.

**15:21** Shairi hili linaonyesha sababu ya maagizo ndani ya shairi 20. Kulikuwa na Wayuda **ndani ya kila mji** waliofundishwa kwamba ni vibaya kufanya maneno haya. Ilikuwa vibaya kutenda uzini na kula vyakula vilivyotolewa kwa sanamu, mnofu ya nyama zilizosongwa, na damu. Haifai Mataifa kuchukiza Mungu kwa njia ya kuzini, na kuchukiza watu kwa njia ya kufanya maneno yale mengine.

**15:22** Hivi lilikusudiwa kwamba si lazima kwa Mataifa kutahiriwa kupata wokovu. **Mitume na wazee** katika Yerusalema, **pamoja na kanisa zima, walituma barua kwa kanisa katika Antiokia kuwajulisha neno hili.** Walichagua **Yuda aliyeitwa Barisaba** vilevile, **na Sila**, **watu wakubwa katika ndugu,** kurudi kwa **Antiokia pamoja na Paulo na Barnaba.** Kwa wakati wa nyuma **Sila** alisafiri pamoja na **Paulo.** Ndani ya barua za Agano Jipya aliitwa Silvano.

**15:23-29** Mashairi haya yanapasha maneno yaliyoandikwa ndani ya barua yao. Ona ya kwamba watu wale waliotoka Yerusalema na kufundisha maneno ya uwongo walifanya hivi bila ukubali wa kanisa katika Yerusalema (sh. 24).

Ona ndani ya shairi 28 namna wanafunzi walivyotegemea maongozi ya **Roho Mtakatifu** kila dakika na kwa kila neno: **Imependeza Roho Mtakatifu na sisi …**

**15:30, 31** Waamini wa kanisa katika **Antiokia walitiwa roho** wakati waliposikia habari za **barua** hii, **wakafurahi kwa maonyo haya**. Na walijua sasa kwamba Mungu aliwaokoa kama Mataifa, si kwa sababu waligeuka Wayuda.

**15:32-34 Yuda na Sila** walibaki katika Antiokia kwa wakati na **walithibitisha** na **kusimamisha ndugu** kwa maneno mengi. Kisha ndugu walirudia Yerusalema na salama ila Sila aliyerudia Yerusalema nyuma, na ndani ya shairi 40 tunamwona akikwenda pamoja na Paulo kwa safari yake ya pili ya kuhubiri.

**15:35 Paulo na Barnaba** walibaki **katika Antiokia** kwa wakati huu, **wakifundisha na kuhubiri Neno la Mungu**. Kulikuwa na watumishi wengine **wengi** wa Bwana waliofundisha kanisa. Tunafikiri habari za Gal. 2:11-14 zilitokea kwa wakati ule.

### F. Safari ya pili ya Paulo kuhubiri: Asia Ndogo na Yunani (15:36 – 18:22)

**15:36-41** Wakati wa kuanza safari ya kuhubiri ya pili ilikuwa imefika. **Paulo** alisema na **Barnaba** ya kwamba ingekuwa vema wafikie tena miji pahali **walipohubiri neno la Mungu mbele. Barnaba** alitaka sana mwana wa ndugu yake, ndiye **Marko**, aende pamoja nao tena, lakini **Paulo** alikataa neno hili kabisa. Alikumbuka namna Marko **alivyowaacha katika Pamfilia,** na bila shaka aliogopa angeweza kufanya hivi tena. **Mabishano** kati ya **Barnaba na Paulo yalikuwa makali sana hata** watumishi hawa wawili wenye heshima **waliachana. Barnaba akachukua Marko, wakakwenda Kipuro na chombo cha maji,** pahali pa kuzaliwa kwake,

na vilevile pahali pa kwanza walipofikia kwa safari yao ya kwanza ya kuhubiri. **Paulo alichagua Sila,** wakasafiri **kupita katika SURIA na KILIKIA, na kupatisha makanisa nguvu.**

Mashairi 36 na 41 yanatufunua roho ya mchungaji wa kweli ya **Paulo** kwa watu wa Mungu.

Basi watu wanauliza kama "nani alitenda vizuri, **Paulo** au **Barnaba**?" Labda wao wawili walikuwa na kosa. Labda **Barnaba** alisukumwa na mapendo yake ya jamaa kwa **Marko.** Shairi 39 linaonyesha kwamba kulikuwa na **mabishano makali** kati ya **Paulo** na **Barnaba**. "Majivuno yanaleta ugomvi" (Mezali 13:10). Basi wote wawili walikuwa na hatia ya kiburi katika jambo hili. Watu ambao wanafikiri **Paulo** alitenda kwa haki wanaonyesha kwamba hakuna habari nyingine ya **Barnaba** ndani ya Agano Jipya nyuma ya wakati ule. Na vilevile, **Paulo** na **Sila waliombewa na wale ndugu, wapewe neema ya Mungu,** lakini hili *halisemwi* juu ya Barnaba na Yoane Marko. Ni asante kukumbuka kwamba mwishoni Marko alikubaliwa tena na Paulo kwa ushirika mzuri (2 Tim. 4:11).

## MAFUNDISHO JUU YA HAKI YA KANISA KUJITAWALA YENYEWE

Kusanyiko kwa Yerusalema ingeweza kuonekana kama baraza kubwa ya dini, lakini neno hili si kweli.

Kila kanisa la pahali fulani katika siku za mwanzo za Ukristo lilikuwa huru kujitawala. Hakuna shirikisho la makanisa na mamlaka kubwa juu yao. Kila kanisa la pahali fulani lilipaswa kusimama mbele ya Bwana peke yake kueleza habari za kazi yake. Hii ni picha katika Ufunuo 1:13 pahali Bwana anapoonekana akisimama katikati ya vinara saba vya zahabu, ndiyo makanisa saba ya Asia. Hakuwa na kiongozi mkubwa aliyesimamia makanisa haya mbele ya Kichwa mkubwa wa kanisa, ndiye Kristo. Kila kanisa moja moja *liliongozwa na Bwana tu.*

Kwa nini hili ni neno kubwa sana? Kwanza, linazuiza kuenea kwa mafundisho ya uwongo. Wakati makanisa yanapoungwa pamoja chini ya mamlaka ya kawaida, ni nyepesi kwa wenye kuleta mafundisho ya uwongo na uasi kulazimisha waamini wote kunyenekea mafundisho yao mabaya kwa njia ya kutawala mamlaka ya kawaida tu. Lakini kila kanisa likiwa huru, inapasa adui kupiga vita na kila kanisa peke yake.

Neno la pili, uhuru wa kanisa la pahali fulani unalisaidia sana wakati inchi inapotawaliwa na serikali walio adui za Wakristo. Wakati kuna shirikisho la makanisa, serikali wanaweza kushindana nao kwa njia ya kutiisha viongozi wao wachache tu. Wakati makanisa yanapokataa kutii shirikisho la mamlaka yo yote, ni nyepesi kwao kukaa kukutana kwa maficho kwa nyakati za taabu.

Serikali za inchi nyingi leo, kama démocratie au wa usultani, wanajaribu kufungamisha makanisa madogo pamoja. Wanasema hawataki kutumika na kanisa moja moja, lakini na comité moja ambayo inayasimamia yote. Serikali za inchi huru wanajaribu kuleta umoja huu kwa njia ya kutoa ahadi ya kusaidia makanisa kwa njia mbalimbali. Serikali nyingine wanajaribu kuyafunga pamoja kwa njia ya amri. Makanisa yote ambayo yananyenyekea maneno haya yanapoteza uhuru wao pamoja na uwezo wao wa kushindana na mafundisho ya sasa yasiyopatana na Biblia, na hawawezi tena kuendelea kukutana kwa siri kwa wakati wa mateso.

Labda wengine wanafikiri kwamba makanisa katika Matendo yalikuwa

chini ya mamlaka kubwa, ndiyo Baraza katika Yerusalema tuliyosoma juu yake sasa tu. Lakini tukisoma mashairi haya tena polepole, tutaona kwamba Baraza hii haikuwa na mamlaka ya kutawala. Ilikuwa kusanyiko la mitume na wazee waliotoa mashauri tu.

Baraza hawakuita watu kuja kutoka Antiokia; ni wao waliochagua kuja kushauriana na wanaume katika Yerusalema. Mashauri ya Baraza hayakuwa sheria kwa makanisa; yalikuwa mawazo ya makusanyiko ya watu wale tu.

Historia ya kanisa inaonyesha wazi kwamba po pote makanisa yalipofunganishwa pamoja na kuwa chini ya shirika kubwa, yalianza kurudi nyuma mbio kupita. Makanisa yenye ushuhuda safi zaidi kwa Mungu ndiyo makanisa ambayo hawatatawaliwi na watu wageni. ❖

**16:1, 2** Bila shaka Paulo alikumbuka maneno ambayo yalimpata mara ya kwanza alipofika kwa **DERBE** na **LISTRA**, na namna alivyotupiwa mawe kwa Listra. Angeweza kuwa na shaka juu ya kurudi tena kule. Lakini mtume alijua kwamba Mungu alikuwa na watu katika pahali pale, na hakuzuizwa na woga wa hatari.

Kama tulivyosema mbele, labda **Timoteo** aliokolewa wakati Paulo alipofikia **Listra** mara ya kwanza (tunafikiri kilikuwa kijiji pahali Timoteo alipopata nguvu). Mama yake Eunike na mama ya mama yake, Loisi, walikuwa wote waamini **Wayuda** (2 Tim. 1:5). **Baba yake alikuwa Myunani** na labda alikuwa amekufa kwa wakati huu.

Paulo alifurahi kusikia kutoka kwa **ndugu wa … Listra na Ikonio** kwamba **Timoteo** alikuwa akiendelea vizuri katika imani ya kikristo. **Paulo** alimwomba kwenda pamoja nao katika safari hii ya kuhubiri. Tuone kwamba ilikuwa desturi kwa mitume wawili kusafiri pamoja, na zaidi ya ile walichukua pamoja nao ndugu vijana (Marko na Timoteo) kuwafundisha namna gani kutumikia Bwana. Ilikuwa baraka kubwa kwa vijana hawa kuweza kushiriki na watumishi hawa wa kukomea katika kazi ya Mungu.

**16:3** Mbele ya kwenda zao, **Paulo alitahiri** Timoteo. Kwa nini alifanya hivi, wakati alipokataa kwa Tito kutahiriwa mbele (Gal. 2:1-5)? Jibu ndilo hili: kwa maneno ya Tito ilikuwa mafundisho ya msingi wa Kikristo, lakini hapa haikuwa hivi. Walimu wa uwongo walisema na nguvu kwamba ni lazima kwa watu wa Mataifa, kama Tito, kutahiriwa ili kuokolewa. Paulo alitambua ya kuwa mafundisho haya yalikana kwamba kazi ya upatanisho ya Kristo inatosha kabisa, na hakuruhusu Tito kutahiriwa. Maneno hapa kwa Listra yalikuwa namna nyingine kabisa. Watu wa pahali pale walijua kwamba Timoteo alikuwa Myuda kwa sababu mama yake alikuwa Myuda. **Paulo**, Sila, na Timoteo walikuwa wakikwenda kuhubiri Habari Njema na watakutana na matata nyingi na Wayuda. Kama **Wayud**a hawa walijua kwamba Timoteo hakutahiriwa, wangeweza kukataa kusikiliza mahubiri yao, lakini kama akitahiriwa, neno la tohara halikuwa angukisho kwao. Kwa sababu hapa halikuwa neno la mafundisho (doctrine) **Paulo** alitahiri Timoteo kupatana na sheria hii ya Wayuda. Alifanya mambo yote kwa watu wote ili kwa njia zote apate kuokoa wengine (1 Kor. 9:19-23).

Ni kama tafsiri kwamba Paulo alitahiri Timoteo kusudi Wayuda waweze kukubali kusikiliza Habari Njema ni tafsiri nzuri kwani tunasoma **akamtahiri kwa sababu ya Wayuda … kwa sababu wote walijua ya kuwa baba yake alikuwa Myunani.**

**16:4-5** Wakati wajumbe hawa watatu wa Mungu waliposafiri **katika miji** ya

Likaonia, **walijulisha** makanisa **amri** ambazo ziliandikwa na **mitume na wazee kule Yerusalema.** Hizi ndizo **amri** zenyewe, kwa ufupi:

1. Kwa maneno ya wokovu, imani peke yake inahitajiwa. Haifai kuongeza tohara au kutii sheria kwa imani kama neno la sharti kwa kupata wokovu.

2. Uasherati ulikatazwa kwa waamini wote na kwa wakati wote, lakini labda zaidi watu wa Mataifa walikumbushwa neno hili kwa sababu hii ilikuwa (na ni hata sasa) zambi ambayo inawafunga sana.

3. Watu walikatazwa kula nyama iliyotolewa kama sadaka kwa sanamu, nyama zilizonyongwa, na damu, si kama lazima kwa wokovu, lakini kwa kuwezesha ushiriki kati ya waamini wa Wayuda na wa Mataifa. Mengine ya maagizo haya yaligeuzwa nyuma (angalia 1 Kor. 8-10; 1 Tim. 4:4, 5).

Kwa sababu ya mafundisho ya watu hawa, **makanisa yalipata nguvu katika imani, na hesabu yao iliongezeka kila siku.**

**16:6-8** Mashairi haya yanaonyesha neno kubwa sana, ndilo ya kwamba Roho Mtakatifu ni juu ya maneno yote na aliongoza wanafunzi katika maneno yote. Nyuma ya kufikia makanisa katika **FURIGIA** na **GALATIA** tena, walikuwa na mawazo ya kwenda kuingia wilaya ya **Asia**, katika mangaribi ya Asia Ndogo, lakini **Roho Mtakatifu** aliwakataza. Hatuambiwi kwa sababu gani walikatazwa; wengine wanafikiri kwamba labda Mungu aliwekea Petro inchi ile (angalia 1 Pet. 1:1). Basi walisafiri kaskazini-mangaribi kwa **MISIA**. Hii ilikuwa sehemu ya wilaya ya **Asia,** lakini ni kama hawakuhubiri pale. Walipojaribu kwenda kaskazini-mashariki na **kuingia Bitinia**, kando ya pwani ya Bahari Nyeusi, **Roho hakuwaruhusu.** Basi, wakakwenda kwa mangaribi kwa mji wa pwani, ndio **TROA**. Kutoka kule waliweza kuangalia ngambo kwa bahari kuelekea Uyunani, pahali pa kuingia Ulaya. Ryrie aliandika:

> Asia ilihitaji Habari Njema, lakini huu haukuwa wakati wa Mungu kwa inchi ile. Hitaji hili halikuwa mwito wa Mungu kwao. Walikuwa wametoka upande wa mashariki; walikatazwa kwenda kusini au kaskazini, lakini hawakujua kwamba Bwana alikuwa akiwaongoza kwenda kwa mangaribi; wakangoja kuongozwa naye. Haifai kutegemea akili yetu tu na kufikiri huu ndio mwito wa Mungu.[12]

**16:9** Wakati wa **ono** usiku, Paulo aliona **mtu wa MAKEDONIA** akimwita **kuvuka na kusaidia**. **Makedonia** ilikuwa sehemu ya kaskazini ya Uyunani, kwa upande wa mangaribi wa Troa. Watu wa **Makedonia** (na wa Ulaya wote!) walihitaji Habari Njema ya neema inayoweza kuokoa watu. Bwana alikuwa amefunga milango ya Asia ili watumishi wake waweze kubeba habari njema kwa Ulaya. Stalker aliandika hivi:

> [Yule mtu wa Makedonia] ni mfano wa Ulaya, na kilio chake kwa kusaidiwa na Kristo. Paulo alitambua kwamba maono haya ni mwito wa Mungu, na waliingia chombo mara moja kwenda Makedonia.[13]

**16:10** Ona ya kwamba hapa mwandishi aligeuka na kwa pahali pa kusema yeye alisema **sisi**. Tunafikiri kwamba Luka, mwandishi wa Matendo, alijiunga na Paulo, Sila, na Timoteo kwa wakati huu. Kutoka saa ile aliandika juu ya maneno aliyoona na macho yake mwenyewe.

### MAFUNDISHO JUU YA MAONGOZI YA MUNGU

Kwa kufanya kazi yao vizuri kanisa la mwanzo walitegemea maongozi ya

Kichwa chake mbinguni. Lakini jinsi gani Bwana Yesu aliwajulisha mapenzi yake?

Aliwajulisha shauri lake kubwa mbele ya kupanda mbinguni, ndilo, "Mutakuwa washuhuda wangu katika Yerusalema, na katika Yudea yote, na Samaria, hata mpaka wa dunia" (Mdo. 1:8).

Nyuma ya kupanda mbinguni aliwajulisha kutaka kwake kwa njia mbalimbali:

Petro na wanafunzi wengine waliongozwa na *Maandiko* katika Agano la Kale (Zab. 69:25) kuchagua mtu kwa pahali pa Yuda (Mdo. 1:15-26).

Mara tano au zaidi Bwana aliongoza watu kwa njia ya *maono* … Anania (Mdo. 9:10-16); Kornelio (Mdo. 10:3); Petro (Mdo. 10:10, 11, 17), Paulo (mara mbili – Mdo. 16:9, 10; 18:9).

Mara mbili aliwaongoza kwa njia ya *manabii* (Mdo. 11:27-30; 21:10-12).

Wakati mwingine Wakristo waliongozwa kwa njia ya *matukio.* Kwa mfano, walisambazwa na kufukuzwa na mateso (Mdo. 8:1-4; 11:19; 13:50, 51; 14:5, 6). Serikali waliomba Paulo na Sila kuondokea Filipi (Mdo. 16:39, 40). Kwa wakati wa nyuma Paulo alichukuliwa na serikali kutoka Yerusalema hata Kaisaria (23:33). Paulo alitaka kuhukumiwa na Kaisari na kwa sababu hii alifanya safari yake kwenda Roma (Mdo. 25:11), na maneno mengine yalitokea kwa sababu ya kuharibika kwa chombo cha maji (Mdo. 27:41; 28:1).

Wakati mwingine uongozi ulikuja kwa njia ya *mashauri na akili ya Wakristo wengine.* Kanisa la Yerusalema walituma Barnaba aende Antiokia (11:22). Agabo alitabiri kwamba kutakuwa na njaa, na habari hizi zilisukuma kanisa la Antiokia kutuma zawadi kwa waamini katika Yudea (11:27-30). Ndugu kwa Antiokia walituma Paulo na Barnaba kwa Yerusalema (15:2). Yuda na Sila walitumwa na kanisa katika Yerusalema kwenda pamoja na Barnaba na Paulo (15:25-27). Paulo na Sila waliombewa na ndugu ili neema ya Mungu iwe pamoja nao wakati walipoanza safari ya pili ya kuhubiri (15:40). Paulo alichukua Timoteo pamoja naye wakati alipoondokea Listra (16:3). Ndugu za Tesalonika walituma Paulo na Sila waende Beroya kwa sababu ya hatari (17:10). Ndugu za Beroya walituma Paulo mbali kwa sababu hii vilevile (17:14, 15). Mwishoni, Paulo alituma Timoteo na Erasto kwa Makedonia (19:22).

Mara nyingine ni kama watu walijulishwa mapenzi ya Mungu mara moja *toka mbingu*. Malaika wa Bwana aliongoza Filipo kufikia towashi wa Etiopia (8:26). Roho Mtakatifu alisema na manabii na walimu katika Antiokia wakati walipokuwa wakifunga na kuomba (13:1, 2). Paulo na Timoteo walikatazwa na Roho Mtakatifu kuhubiri neno katika Asia (16:6). Wakati wa nyuma walijaribu kuingia Bitinia, lakini Roho Mtakatifu hakuwaruhusu kwenda (16:7).

Kwa kufupisha basi, Wakristo wa kwanza waliongozwa:

1. Kwa njia ya Maandiko.
2. Kwa njia ya maono na unabii.
3. Kwa njia ya matukio.
4. Kwa njia ya maonyo na mashauri ya Wakristo wengine.
5. Kwa njia ya maongozi moyoni mwao toka mbinguni. ❖

**16:11,12** Wahubiri hawa wasiochoka walikwenda na **chombo** kwa kaskazini-mangaribi kutoka **Troa,** mpaka **SAMOTIRAKE**. Kesho yake walifika **NEAPOLI**, karibu kilomètres 190 toka **Troa**. Walisafiri kilomètres chache nyingine kuingia inchi kufika **FILIPI**, ndio mji mkubwa wa sehemu ile ya **Makedonia, ndiyo wilaya.**

**16:13-15** Ni kama sunagogi halikuwa katika Filipi, lakini Paulo na wenzake walisikia habari kwamba Wayuda wengine walikusanyika **siku ya Sabato** nje ya mji **kando ya mto**. Wakati walipofika pale, walikuta kundi la **wanawake** wakiomba, pamoja na **mmoja aliyeitwa Ludia.** Tunafikiri alikuwa Mtaifa aliyefuata dini ya Wayuda. **Alitoka mji wa Tuatera**, katika wilaya ya Ludia, upande wa mangaribi wa Asia Ndogo, aliyehama kwa Filipi pahali alipokuwa **mwuzaji wa nguo zilizotiwa rangi ya zambarau**. **Tuatera** ulijulikana kwa rangi zake.

**Moyo** wa Ludia ulikuwa wazi kupokea Habari Njema. Nyuma ya kupokea Bwana Yesu, **yeye na watu wa nyumba yake walibatizwa.** Bila shaka **watu wa nyumba yake** walikuwa wamepokea wokovu vilevile mbele ya **kubatizwa.** Hatusomi ya kwamba Ludia alikuwa na mume; labda **watu wa nyumba yake** walikuwa watumishi.

**Ludia** hakuokolewa kwa sababu ya kutenda mema, lakini aliokolewa kusudi atende mema. Alihakikisha kwamba alikuwa ameokolewa kweli kwa njia ya kufungua nyumba yake kwa Paulo, Sila, Luka, na Timoteo.

**16:16-18** Siku nyingine, wakati **Paulo** na wenzake walipokwenda kwa pahali pa **maombi**, walikutana na **msichana mtumwa mmoja** aliyekuwa na **pepo ya kuagua**. Alikaliwa na pepo mchafu na alikuwa na uwezo wa kutabiri maneno yatakayotokea, na kufunua maneno mengine ya kushangaza. Kwa njia hii **alipatia bwana zake** mali nyingi.

Wakati **alipokutana** na wahubiri, **aliwafuata kwa siku nyingi,** akapaza sauti na kulia, **"Hawa watu ni watumishi wa Mungu aliye juu, wenye kutuhubiri njia ya wokovu."** Neno alilosema lilikuwa *kweli*, lakini **Paulo** hakuweza kukubali ushuhuda wa pepo wachafu. Na vilevile alikuwa na huzuni kwa sababu ya hali mbaya ya msichana huyu mtumwa. Hivi, **katika jina** lenye nguvu zote **la Yesu Kristo**, aliagiza pepo **kutoka**. Msichana alifunguliwa mara moja kutoka utumwa huu mbaya, na aligeuka mtu mwenye akili njema.

### MAFUNDISHO JUU YA MAAJABU

Tunapata habari za maajabu mengi ndani ya kitabu cha Matendo. Tuone mengine ya kujulikana zaidi:

Uwezo wa kusema na lugha nyingine (2:4; 10:46; 19:6).

Kuponyeshwa kwa kiwete kwa mlango wa hekalu (3:7).

Hukumu ya gafla, ndiyo mauti ya Anania na Safira (5:5, 10).

Ukombozi wa mitume toka gereza (5:19).

Kukutana kwa Paulo na Kristo mtukuzwa (9:3-6).

Kuponyeshwa kwa Ainea na Petro (9:34).

Kufufuliwa kwa Dorika (9:40).

Maono ya Petro ya nguo ikishushwa chini kutoka mbinguni (10:11).

Kufunguliwa kwa Petro kutoka gerezani (12:7-10).

Uuaji wa Herode na malaika (12:23).

Hukumu ya upofu juu ya Elima, yule mchawi (13:11).

Kuponyeshwa kwa kiwete katika Listra na Paulo (14:10).

Kutiwa nguvu tena kwa Paulo nyuma ya kutupiwa mawe kwa Listra (14:19, 20).

Ono la Paulo la mtu wa Makedonia akiita kusaidiwa (16:9).

Paulo akitoa roho mbaya toka msichana kwa Filipi (16:18).

Kuponyeshwa kwa Paulo na Sila toka gereza kwa Filipi (16:26).

Paulo akirudishia Eutiko uzima wake (20:10, 11).

Unabii wa Agabo (21:10,11).

Kuponyeshwa kwa Paulo toka sumu ya nyoka katika Melita (28:3-6).

Kuponyeshwa kwa baba yake Publio toka homa (28:8).

Kuponyeshwa kwa wagonjwa wengine (28:9).

Zaidi ya haya, tunasoma kwamba mitume walifanya maajabu na alama nyingi (2:43); Stefano alifanya maajabu na alama mbele ya watu (6:8), Filipo alifanya alama na maajabu (8:6,13); Barnaba na Paulo walifanya alama na maajabu (15:12); na Mungu alifanya maajabu kwa mikono ya Paulo (19:11).

Wakati watu wanaposoma kitabu cha Matendo wanauliza, "Tutaweza kuona maajabu haya wakati wa sasa vilevile?" Inatupasa kuepuka majibu mawili kwa ulizo hili. La kwanza ni ya kwamba Yesu Kristo akiwa sawasawa, jana, leo na kwa milele, ingetupasa kuweza kuona leo maajabu yaliyofanyikana kwa wakati wa mwanzo wa kanisa.

Jibu la pili ambalo inatupasa kuepuka ni ya kwamba maajabu yalikuwa tu kwa wakati wa mwanzo wa kanisa na kwamba haifai kwetu kufikiri tutaona maajabu kwa wakati wa sasa.

Ndiyo, kweli Yesu Kristo ni sawasawa, jana, leo na hata milele (Ebr. 13:8). Lakini neno hili si kusema namna anavyotumika haibadiliki. Kwa mfano, Mungu hakutumika mara ya pili na mapigo ambayo alileta juu ya Misri. Uwezo wake haugeuki. Hata sasa anaweza kutenda ajabu lo lote. Lakini si *lazima* kwake kufanya maajabu namna hii katika kila muda.

Lakini haifai tufikiri maajabu hayawezi kutokea kwa muda wa kanisa.

Maisha yetu si ya dunia hii tu. Ingetupasa kuona mkono wa Mungu akituongoza kwa njia ya ajabu. Ingetupasa kuona matukio ndani ya maisha yetu yasiyotukia ndani ya maisha ya wasioamini, na namna Mungu anavyofungua njia kwa sisi kwa kazi yake na kumshuhudia, na kushinda adui zetu.

Ingetupasa kuona majibu kwa maombi yetu. Ingetupasa kuona Mungu akitumika ndani ya maisha ya watu wengine wakati tunapokutana nao. Inatupasa kutambua mkono wa Mungu wakati wa matata na hasara. Ingetupasa kumwona akituponyesha na kutupa nguvu, uhodari, salama, na akili zinazopita zile za watu wa dunia.

Kama tukiishi maisha yetu katika desturi za dunia tu, kwa njia gani sisi ni namna nyingine na watu wasio Wakristo? Ni mapenzi ya Mungu kwa maisha yetu kujazwa na uwezo wake, kwa uzima wa Yesu Kristo kuonekana ndani yetu na kupita kwa watu wengine. Wakati neno hili linapotokea, maneno *yasiyowezekana* yatafanyika, na milango kwa kazi ya Bwana itafunguliwa kwa sababu ya uwezo wa Roho Mtakatifu. ❖

**16:19-24** Ingalipasa **mabwana** wa msichana kufurahi kwa sababu pepo mchafu aliondoshwa ndani yake, lakini sivyo. Walikasirika sana kwa sababu hawakuweza kupata **mali** tena kwa njia ya kutabiri kwake. Walikokota **Paulo na Sila mbele ya watawala wa mji** na kuwashitaki kuwa **Wayuda** waliofazaisha mji sana, na kufundisha desturi zisizo halali kwa Waroma. Makutano waliwakwendea kwa nguvu, **watawala wakaondosha nguo** za Paulo na Sila na **kuagiza wapigwe kwa fimbo**. Nyuma ya kupigwa sana, wahubiri walitupwa gerezani, na **mlinzi wa gereza** aliagizwa **kuwalinda sana**. Basi **aliwatupa katika chumba cha ndani, akawafunga miguu kwa mikatale.**

Ndani ya mashairi haya tunaona njia mbili ambayo Shetani anatumika nazo kujaribu kuharibu kazi ya Mungu: 1) Urafiki wa uwongo – ushuhuda wa msichana yule mwenye pepo. 2) Wakati njia ile inapokufa bure, analeta mateso. A.J. Pollock aliandika,

> Bila shaka Shetani alifurahi sana akifikiri alikuwa ameharibu kazi ya watumishi hawa wa Mungu kwa gafula. Lakini furaha yake ilikwisha mbio kwani mambo aliyofanya yalisaidia kazi ya Bwana *kwenda mbele*.[14]

**16:25 Katikati ya usiku Paulo na Sila … walikuwa wakiomba kwa Mungu, na kumwimbia sifa.** Furaha yao haikutegemea maneno ya dunia. Yule aliyejaza mioyo yao na **nyimbo za sifa** alikuwa mbinguni. Morgan aliandika,

> Mtu ye yote anaweza kuimba wakati milango ya gereza zinapokwisha kufunguliwa naye ni huru tena. Mkristo anaimba hata ndani ya gereza … Tunaona hapa utukufu wa Roho Mtaka-tifu anayeshinda maneno magumu na maneno yote ambayo yanataka kuzuiza utumishi wetu.[15]

**16:26** Wakati wafungwa wengine walipokuwa wakisikiliza maombi yao na nyimbo zao za sifa kwa Mungu, gereza ilitikiswa na **tetemeko la inchi**. **Milango ya gereza ilifunguka** na mikatale na **minyororo** ya watu wote ililegezwa, lakini halikuharibu nyumba.

**16:27, 28** Wakati mlinzi wa gereza alipoamka toka usingizi na kuona **gereza wazi**, alifikiri bila shaka **wafungwa walikuwa wamekimbia**. Akijua kwamba yeye mwenyewe atauawa kwa sababu hakuwalinda vizuri **alitoa upanga wake** kwa kujiua mwenyewe. **Lakini Paulo** alisema naye na kumkataza na nguvu asifanye hivi kwa sababu wafungwa **wote** walikuwa pale.

**16:29, 30** Sasa mlinzi wa gereza alishikwa na woga namna nyingine. Kwa pahali pa kuogopa kupoteza kazi yake na labda uzima wake, alishikwa na woga mkubwa wa mzigo wa zambi zake. Sasa aliogopa kukutana na Mungu na zambi zake zote. Hivi alipaza sauti na kuuliza, **"Bwana zangu, nifanye nini niokolewe?"**

Hili ndilo neno ambalo inapasa kila mtu kuuliza mbele ya kuokolewa kwelikweli. Mbele ya kuweza *kuokolewa* inapasa mtu kufahamu kwamba yeye ni *mpotevu*. Haifai kumwambia mtu namna gani anaweza kuokolewa wakati mtu huyu asipofahamu kwanza anastahili kwenda Gehena.

**16:31** Watu wa pekee katika Agano Jipya walioambiwa kuamini Bwana Yesu Kristo ndio wale waliokwisha kujua kabisa kwamba wao ni wenye zambi. Sasa wakati mlinzi gereza alipokwisha kuhuzunika sana juu ya zambi zake aliambiwa: **"Amini Bwana Yesu Kristo, nawe utaokolewa, pamoja na nyumba yako."**

Maana yake haiko ya kwamba *yeye* akiokolewa, watu wa nyumba yake wataokolewa vilevile. Maana yake ndiyo ya kwamba yeye **akiamini Bwana Yesu Kristo ataokolewa,** na **watu wa nyumba** yake **wataokolewa** kwa njia ile vilevile. "Amini … na utaokolewa, na watu wa nyumba yako wafanye vivyo hivyo."

Ni kama ni nguvu kwa watu wengi kwa wakati wa sasa kufahamu kama kuamini ni nini. Lakini wakati mwenye zambi anapofahamu yeye ni mpotevu na hawezi kujisaidia mwenyewe, ya kwamba hana tumaini, naye ni kwa njia inayofikisha upotevu, anafahamu maana ya masemo haya vizuri. Hakuna neno lingine *analoweza* kufanya ila kuamini!

**16:32-34** Wakati Paulo na Sila walipokwisha kufundisha Neno la Mungu kwa watu wa nyumba ile, mlinzi alionyesha kwamba alikuwa ameamini kweli kwa njia ya kuosha vidonda vyao, na **kubatizwa** bila kuchelewa. **Aliwaleta nyumbani mwake** vilevile na kuwakulisha, akifurahi saa zote **pamoja na nyumba yake yote** kwa sababu wao wote walikwisha kuamini Mungu.

Tunataka kusema tena kwamba hakuna neno linaloonyesha kwamba kulikuwa na watoto wachanga au watoto wadogo sana ndani ya nyumba ile waliobatizwa. Wao wote walikuwa na umri

wa kutosha kuweza **kuamini Mungu.**

**16:35** Ni kama **watawala** waligeuza mafikiri yao usiku, kwa sababu asubui walituma **wakubwa wa askari** na agizo kwa wafungwa hawa wawili kufunguliwa.

**16:36, 37** Wakati mlinzi wa gereza alipojulisha **Paulo** habari hizi, mtume alikataa kwenda. Ndiyo, yeye na Sila walikuwa Wayuda, lakini walikuwa wenyeji wa Roma vilevile. Walikuwa **wamepigwa** na kuhukumiwa bila haki. Sasa watawala walifikiri watakwenda zao polepole kama wenye hatia? **Sivyo, hata kidogo!** Watawala **waje** wao wenyewe na kufungua wafungwa.

**16:38-40** Basi, **watawala** walifika wao wenyewe na walisihi Paulo na Sila kuondokea mji bila machafuko. Hivi na heshima ya wana wa Mfalme, watumishi wa Bwana **walitoka kifungo,** lakini hawakuondokea mji mara moja. Walikwenda kwanza kwa **nyumba** ya Ludia kuonana na **ndugu na kuwatia moyo nguvu.** Ndiyo, wale waliopaswa kufarijiwa wenyewe walifariji wengine.

Nyuma ya kumaliza kazi yao kwa Filipi, **walikwenda zao** na heshima.

**17:1** Nyuma ya kuondokea Filipi, Paulo na Sila walisafiri kilomètres 48 kwa upande wa kusini-mangaribi kwa **AMFIPOLI**. Wakaendelea na safari yao hata **APOLONIA**. Toka pale walisafiri kilomètres 59 kufikia **TESALONIKA,** mji mzuri kwa wenye kufanya biashara. Roho Mtakatifu alichagua mji huu kuwa msingi toka pahali Habari Njema itakapoenea na kungaa katika pande nyingi. Kwa wakati wa sasa mji huu unaitwa Saloniki.

Labda Luka alibaki kwa Filipi wakati Paulo na Sila walipokwenda kuhubiri Habari Njema pahali pengine, kwani tunasoma *wao* kwa pahali pa *sisi.*

**17:2, 3** Kama ilivyokuwa desturi yao, wahubiri walikwendea sunagogi pahali walipohubiri Habari Njema. **Kwa sabato tatu** Paulo alionyesha wazi toka Agano la Kale kwamba **itapasa Masiya kuteswa na kufufuka tena toka wafu.** Kisha aliendelea na kutangaza kwamba **Yesu** wa Nazareti ndiye Masiya ambaye watu walikuwa wamengoja kufika tangu siku nyingi. Ni yeye aliyeteswa na kufa, na aliyefufuka toka wafu. Maneno haya yanahakikisha kwamba yeye ni **Kristo** wa Mungu.

**17:4-7 Wengine** wa Wayuda **walikubali** maneno haya na walifungana na **Paulo na Sila** kama waamini wa Habari Njema. Wayunani wengi walioogopa Mungu na **wanawake wakubwa si wachache waliamini vilevile. Wayuda** wasioamini hawakufurahi hata kidogo juu ya neno hili, wakakwenda pahali pa **soko** na kukusanya watu waovu bila heshima, wakakutanisha makutano, wakafanya makelele katika mji, wakakwendea nyumba ya Yasoni, pahali **Paulo na Sila** walipopanga kama wageni. **Wakati hawakukuta** Paulo na Sila nyumbani, **walikokota Yasoni na wengine** wa waamini mbele ya **wakubwa wa mji.** Bila kusudi kufanya hivi waliheshimu Paulo na Sila sana wakati waliposema juu yao kwamba **walipindua dunia.** Halafu waliwashitaki ya kwamba walijaribu kuharibu utawala wa **Kaisari** kwa njia ya kuhubiri juu ya **mfalme mwingine, ndiye Yesu.** Ni kitu cha kushangaza kuona **Wayuda** hawa wakisimamia serikali ya **Kaisari** na bidii, kwani walikuwa na mapendo nusu tu kwa ufalme wa Waroma.

Lakini mashitaki yao yalikuwa kweli? Bila shaka walikuwa wamesikia Paulo na Sila wakitangaza habari za kuja kwa pili kwa Yesu kutawala kama mfalme juu ya dunia nzima. Lakini habari hizi hazikuwa hatari kwa Kaisari, kwa sababu Kristo hatarudi kutawala mbele ya kutubu kwa taifa la Israeli.

**17:8, 9** Wakubwa wa mji **walifazaika** wakati waliposikia maneno haya.

Waliagiza **Yasoni** na wenzake kulipa amana waweze kufunguliwa na kwenda zao. Tunafikiri waliagiza wageni wake kuondokea mji vilevile.

**17:10-12 Ndugu** katika Tesalonika walifikiri ingekuwa vizuri kwa wahubiri kwenda zao, hivi **waliwatuma usiku kwenda BEROYA**, nao walikwendea **sunagogi la Wayuda** kule mara moja. Wayuda wa pale walisikiliza na nia tayari, na walitafuta **maandiko** ya Agano la Kale kuona kama maneno waliyohubiri yalikuwa kweli. Wengi wa Wayuda hawa waliamini, pamoja na **wanawake** Mataifa **wengi wenye heshima, na wanaume vilevile.**

**17:13, 14** Wakati habari zilipofika kwa **Tesalonika** kwamba **Paulo** na Sila waliendelea kuhubiri Habari Njema kwa **Beroya**, **wengine wa Wayuda** walisafiri kwenda Beroya **kuamsha machafuko** na uadui katika makutano juu ya Paulo. Kwa sababu hii **ndugu Wakristo** walipeleka Paulo pamoja na ndugu wengine kufikia bahari. Tunafikiri walimsindikiza hata DIUM na toka kule alisafiri katika chombo kufika kwa **ATENE**. **Sila na Timoteo walibaki** kwanza kwa Beroya.

**17:15** Ilikuwa safari ndefu toka Beroya kufika **Atene,** na ilionyesha mapendo ya kweli ya Wakristo, hata wengine katikati yao walikuwa tayari kusindikiza **Paulo** na kumfikisha kule. Wakati walipokuwa tayari kurudi kwao, alituma habari pamoja nao **kwa Sila na Timoteo kufika kwake mbio.**

**17:16** Wakati Paulo **alipowangoja kwa Atene,** alihuzunishwa sana kuona watu wakiabudu sanamu nyingi. **Atene** ulikuwa mji wa elimu na mafunzo, lakini Paulo hakuweka roho juu ya maneno haya.

**17:17, 18 Alibishana na Wayuda na waabudaji wa Mataifa** katika sunagogi, lakini kwa pahali pa **soko** alihubiri kwa mtu ye yote aliyekubali kusikiliza. Kwa njia hii alikutana na **Waepikurio** na **Wastoiko**, wenye elimu na hekima. Waepikurio walikuwa wafuata wa Epikurio, aliyefundisha kwamba anasa, si elimu, ndilo neno kubwa la maisha ya mtu. Wastoiko walifundisha kwamba hekima ndiyo kukaa bila furaha au huzuni, lakini ni kuwa tayari kunyenyekea tu mambo yo yote ambayo yanatupata. Wakati watu hawa waliposikiliza Paulo, waliwaza yeye ni **mtu wa masemo mengi** na **mhubiri wa miungu migeni, kwani alihubiri habari za Yesu na ufufuko.**

**17:19-21 Walimpeleka kwa Areopago,** iliyokuwa kama baraza waliokutana juu ya kilima cha Mars, wakampa Paulo njia kuwapasha, pamoja na watu wote habari za mafundisho yake, ona shairi 21. **Watu wa Atene** walipenda sana kuzungumza na kusikiliza watu wengine. Ni kama walikuwa na saa nyingi kufanya hivi.

**17:22** Akisimama **katikati** ya Baraza, **Paulo** alitoa hotuba. Inatupasa kukumbuka kwamba alikuwa akisema kwa Mataifa, si Wayuda. Hawakujuana na habari za Agano la Kale, hivi ilimpasa kuanza hotuba na neno waliloweza kufahamu. Basi alisema kwamba aliona watu wa Atene walikuwa watu wa **kutafuta maneno ya dini sana.** Na kweli hesabu ya sanamu ilipita hesabu ya watu ndani ya mji ule!

**17:23** Wakati Paulo alipowaza juu ya sanamu alizoona, alikumbuka ya kwamba alikuwa ameona **mazabahu moja na andiko hili: KWA MUNGU YULE ASIYEJULIKANA.** Andiko hili linafundisha maneno makubwa mawili: 1) ya kwamba **Mungu** yuko, na 2) ya kwamba watu wa Atene hawakujuana **naye**. Maneno haya mawili yalimpa **Paulo** njia kuwafundisha juu ya **Mungu wa kweli.**

**17:24, 25** Wahubiri wanasema njia nzuri zaidi kuanza kufundisha wapagano

juu ya Mungu ni kuwafundisha juu ya kuumbwa kwa dunia. Paulo alifanya hivi na watu wa Atene. Alisema juu ya **Mungu** kama yule **aliyefanya ulimwengu na vitu vyote ndani yake.** Wakati alipotazama mahekalu mengi ya sanamu kando kando, alikumbusha wasikiaji wake ya kuwa **Mungu wa kweli hakai ndani ya mahekalu yaliyojengwa kwa mikono ya watu**, wala hategemei utumishi wa **mikono ya watu** kwa mahitaji yake. Mara nyingi ndani ya mahekalu makuhani wanaletea miungu yao vyakula na vitu vingine kwa "mahitaji" yao. Lakini Mungu wa kweli hahitaji kitu toka watu kwa sababu **yeye** mwenyewe anawapa wote **uzima na pumuzi na vitu vyote.**

**17:26-28a** Halafu alionyesha kwamba mataifa yote ya dunia wana mzazi mmoja, ndiye Adamu. Mungu alifanya kila taifa kuwa la damu moja na **alichagua** kwa wakati gani na kwa pahali gani kila taifa litakapokaa. Aliwapa vitu vyote kusudi waweze **kumtafuta** na **kumwona**, hata kama **yeye si mbali na kila mmoja wao.** Tunaishi, na **tunakwenda na tuna uhai wetu ndani** ya Mungu wa kweli**. Yeye** si Mwumba wetu tu, lakini yeye ni kandokando yetu vilevile.

**17:28b** Halafu Paulo alitaja masemo ya mmoja wa **waandishi** wao Wayunani, **aliyesema, "Maana sisi sote tuko wazao wake."** Maana ya semo hili si kufundisha undugu wa watu na ubaba wa Mungu. Tuko **uzao** wa Mungu kwa sababu alituumba, lakini tunageuka *wana* wa Mungu kwa njia ya kuamini Bwana Yesu Kristo tu.

**17:29** Paulo aliendelea kueleza ya kwamba **watu wakiwa wazao wa Mungu,** haiwezekani kufikiri Mungu ni **sanamu ya zahabu au feza au jiwe.** Sanamu hizi zinafanywa na watu walio wakubwa kupita sanamu zenyewe. Ni kama sanamu hizi ni wazao wa watu, lakini kweli ndiyo ya kwamba watu wanaumbwa na Mungu.

**17:30** Nyuma ya kuonyesha upumbavu wa kuabudu sanamu, Paulo aliendelea kusema kwamba kwa mia za miaka **Mungu hakuangalia ujinga** wa Mataifa, lakini sasa Habari Njema ilikuwa imefunuliwa, naye **ameamuru watu wote wa pahali pote kutubu,** na kugeuka.

**17:31** Hizi ni habari za lazima, **kwa sababu** Mungu **ameweka siku wakati atakapohukumu dunia kwa haki** kwa Bwana Yesu Kristo, ndiye **Mtu yule ambaye alimweka kwa kazi hii.** Hukumu hii itatokea wakati Kristo atakaporudia duniani na kushinda adui zake zote na kuanza utawala wake wa miaka elfu moja. Mungu alihakikisha neno hili kwa njia ya kufufua Bwana Yesu **toka wafu.** Ufufuko wa Kristo ndio habari Paulo alizopenda sana kutangaza.

**17:32, 33** Labda Paulo hakumaliza hotuba yake kwa sababu wengine wa wasikiaji **walifanya zihaka** wakati walipo**sikia habari za ufufuko wa watu. Wengine** hawakuzihaki, lakini walikuwa **na shaka, wakasema, "Tutakusikiliza tena juu ya habari hizi."** Hawakukataa kabisa kuamini Kristo, lakini walisema, 'Si sasa'.

**17:34** Haifai kusema kwamba hotuba ya Paulo haikuwa na faida. Kulikuwa na wengine walioamini, kama **Dionisio**, mtu wa Baraza ile, ndiye **Mwareopago**, **mwanamke jina lake Damari, na wengine** vilevile tusiojulishwa majina yao.

**Kisha Paulo alitoka Atene**. Hakuna habari nyingine juu ya Atene. Paulo alirudia pahali alipohubiri na kuteswa mbele, lakini hakuwa na maneno mengine kusema kwa wenye akili walioona masemo yake bure.

Watu wengine wanafikiri hotuba yake ilisifu watu wa Athene kwa sababu ya dini yao, ndiyo kuabudu sanamu. Wanasema mtume Paulo hakuhubiri

Habari Njema wazi pale kama ndani ya hotuba zake nyingine. Lakini mashitaki yao hayakuwa vizuri. Tumeona namna Paulo alitafuta njia kwa watu kusikiliza mafundisho yake juu ya Mungu wa kweli, na aliendelea kuwaelezea kwamba walihitaji kutubu kwa sababu Kristo atakuja kama Mwamuzi. Na watu wengine waliokolewa kwa sababu ya hotuba hii.

### HABARI NJEMA ILIHUBIRIWA KWA PAHALI NAMNA NAMNA

Mahubiri ya Paulo toka Areopago ni mfano wa pahali *namna namna* waamini wa kwanza walipohubiri Neno la Mungu.

Ni kama mara nyingi hawakuwa nyumbani saa walipohubiri. Tunafikiri ilikuwa hivi siku ya Pentekote kwa sababu watu wengi sana waliamini na kuokolewa (Mdo. 2:6, 41). Soma vilevile Mdo. 8:5, 25, 40; 13:44; 14:8-18.

Habari Njema ilihubiriwa mara tatu au zaidi kwa *upande wa hekalu*, ona Mdo. 3:1-11; 5:21, 42. Paulo na wale waliokuwa pamoja naye walihubiri *kando ya mto* kwa Filipi, Mdo. 16:13. Hapa kwa Atene alihubiri *kwa soko* (Mdo. 17:17), na juu ya kilima cha Mars. Katika Yerusalema alihubiri kwa makutano yenye gazabu *toka daraja* ya nyumba kubwa (Mdo. 21:40 – 22:21).

Habari Njema ilihubiriwa mara ine au zaidi *mbele ya watu wa Baraza*: na Petro na Yoane, Mdo. 4:8, 19; na Petro na mitume wengine, Mdo. 5:27-32; na Stefano, Mdo. 7:2-53; na Paulo, 22:30 – 23:10.

Ilikuwa desturi ya Paulo na wale waliokuwa pamoja naye kuhubiri habari njema *ndani ya masunagogi* (Mdo. 9:20; 13:5, 14; 14:1; 17:1, 2, 10, 17; 18:4,19, 26; 19:8).

Habari Njema ilihubiriwa ndani ya *nyumba za watu* vilevile. Petro alihubiri nyumbani mwa Kornelio (Mdo. 10:22, 24). Paulo na Sila walishuhudia Kristo nyumbani mwa mlinzi wa gereza katika Filipi (Mdo. 16:31,32). Kwa Korinto Paulo alihubiri nyumbani mwa Krispo, mtawala wa sunagogi (Mdo. 18:7, 8). Alihubiri kufika saa sita ya usiku ndani ya nyumba ya mtu mmoja kwa Troa (Mdo. 20:7). Katika Efeso alifundisha nyumba kwa nyumba (Mdo. 20:20), na kwa Roma ndani ya nyumba pahali alipopanga na kuilipa (Mdo. 28:30, 31).

Filipo alihubiri kwa towashi ya Etiopia *ndani ya gari* (Mdo. 8:31-35), na Paulo *ndani ya merikebu* (Mdo. 27:21-26). Kwa Efeso alisemezana na watu kila siku ndani ya chumba cha darasa (Mdo. 19:9).

Paulo alihubiri ndani ya *Baraza za serikali* mbele ya Feliki (Mdo. 24:10), Festo (Mdo. 25:8), na Agripa (Mdo. 26:1-29).

Ndani ya Matendo 8:4 tunasoma kwamba waamini waliokuwa wakiteswa walikwenda *pahali po pote* na kuhubiri neno.

Habari hizi zinaonyesha kwamba hawakufikiri walihitaji kuhubiri tu kwa nyumba fulani zilizowekwa mbali kwa kazi ile. Walitangaza habari za Kristo kila pahali walipokuta watu. A.B. Simpson aliandika,

> Wakristo wa kwanza walishuhudia Kristo saa na wakati na pahali gani walipoweza. Hata wakati walipofikishwa mbele ya wafalme na watawala hawakujaribu kamwe kuficha kwamba wao ni Wakristo ili kuepuka hatari. Walifikiri ni njia kuhubiri Habari Njema kwa wafalme na watawala ambao wasiisikia kwa njia yo yote nyingine. Ni kama Mungu anataka sisi kuwa baraka kwa njia yo yote kwa roho na maisha ya kila mtu ambaye tunakutana naye.

Bwana Yesu alikuwa amewaagiza “Kwendeni katika dunia pia, mukahubiri Habari Njema kwa kila mtu” (Mk. 16:15). Ndani ya kitabu cha Matendo tunawaona wakitii agizo hili.

Ni kama wahubiri katika Matendo

hawakutayarisha zaidi ya mafundisho yao mbele ya kuyatoa. Hawakuwa na saa kutayarisha hotuba, lakini mafundisho yao yalitoka ndani ya maisha yao yaliyokwisha kutayarishwa na Roho Mtakatifu. ❖

**18:1** Watu wengine wanafikiri **Paulo alitoka Atene** kwa sababu mahubiri yake yalizaa matunda nusu tu pale. Sisi tunapenda kufikiri ya kwamba aliongozwa na Roho Mtakatifu kusafiri kwa upande wa mangaribi kwa **KORINTO**, mji mkubwa wa AKAYA. Mji huu ulijulikana kwa sababu ya uovu wake. Ilikuwa lazima kwa Habari Njema kuhubiriwa pale na kanisa kusimamishwa.

**18:2, 3** Kwa Korinto Paulo alikutana na **Akila na mke wake Prisila,** nao waligeuka rafiki zake maisha. **Akila** alikuwa **Myuda** toka **Ponto**, ndiyo wilaya kwa kaskazini-mashariki ya Asia Ndogo. Yeye na mke wake walikaa kwa Roma mbele, lakini walifukuzwa toka pale na **Klaudio** Kaisari aliyeagiza Wayuda wote kuondoka. Korinto ulikuwa mji kwa njia kubwa toka Roma kwenda upande wa mashariki, nao walibaki pale na kutumika kazi kama wenye kufanya hema. Paulo alikuwa amefanya kazi ile vilevile, na alikutana nao.

Tunafikiri Akila na Prisila walikuwa waamini mbele ya kufikia Korinto na kukutana na Paulo, lakini neno hili halionekani wazi.

**18:4** Paulo **alibishana katika sunagogi kila sabato na Wayuda na Mataifa** waliokuwa wameshika dini ya Wayuda, na kuwashawishi ya kwamba Yesu ni kweli Kristo wa Mungu.

**18:5** Paulo alikuwa ameacha **Sila na Timoteo** katika Beroya wakati alipokwenda mbele kwa Atene. Toka Atene alituma mtu kuwaita, nao walimfikia kwa Korinto.

Nyuma ya kufika kwao, Paulo aliweka roho yake yote kuhubiri Neno. Alikuwa na mzigo mkubwa rohoni toka Bwana kuhubiri Habari Njema na bidii kabisa na kushuhudia **Wayuda ya kwamba Yesu ni Kristo.** Labda aliacha kufanya hema kwa wakati huu, na alijitoa mzima kwa kazi ya kuhubiri Habari Njema. Aliandika barua ya 1 Tesalonika karibu na saa hii (karibu 52 A.D.)

**18:6** Wayuda wasioamini **walishindana** na Paulo na **kumtukana**. Mtu anayekataa Habari Njema anashindana na *yeye mwenyewe.* Msiyeamini anajiumiza mwenyewe kupita mtu ye yote mwingine.

Halafu Paulo **alikunguta mavazi yake, akasema nao,** "**Damu yenu iwe juu ya vichwa vyenu; mimi ni safi: tangu sasa nitakwenda kwa watu wa Mataifa.**" Kwa njia ya kukunguta mavazi yake alionyesha kwamba alijitenga nao. Lakini neno hili halikumzuiza asikwendee sunagogi katika mji mwingine, ndio Efeso (Mdo. 19:8).

Masemo ya Paulo yanatukumbusha kwamba kila Mkristo ana deni karibu na watu wote. Mungu atamhukumu kama asipolipa deni hii kwa njia ya kuhubiri Habari Njema. Lakini akishuhudia Kristo na uaminifu, na watu wanakataa ushuhuda wake, yeye mwenyewe hana hatia, lakini mwenye kukataa ushuhuda wake atahukumiwa.

Ndani ya shairi hili tunaona tena taifa la Israeli likiwekwa kando kupita, na mahubiri ya Habari Njema yakiendelea mbele. Mungu alikuwa ameagiza Habari Njema ifikie Wayuda kwanza, lakini ndani ya kitabu cha Matendo taifa la Israeli walikataa Habari Njema kupita na kupita, hivi Roho ya Mungu aliwaacha na huzuni.

**18:7, 8** Nyuma ya mashindano na matukano ya Wayuda, Paulo alikwenda kukaa ndani ya nyumba ya **Yusto,** Mtaifa aliyekuwa amepokea dini ya Wayuda. Nyumba yake ilikuwa **mpaka mmoja na sunagogi.** Paulo alikaa kuhubiri toka pale na alifurahishwa kuona

**Krispo, mtawala wa sunagogi … pamoja na nyumba yake yote wakiamini Bwana.** Wakorinto **wengi** wengine waliokolewa na **walibatizwa.** Paulo alibatiza Krispo na waamini wachache wengine (1 Kor. 1:14-16), lakini ilikuwa desturi yake kuacha Mkristo mwingine kubatiza waamini. Aliogopa watu watamheshimu yeye zaidi kwa pahali pa kupenda na kufuata Bwana Yesu na roho moja.

**18:9,10 Bwana alisema na neema na Paulo usiku ndani ya ono** ya kwamba haifai awe **na woga**. Alimwambia Paulo kukaa kuhubiri Habari Njema kwa sababu Mungu alikuwa pamoja naye na atamlinda. Alikuwa na **watu wengi ndani ya mji** ule, maana alikuwa akitumika ndani ya roho zao na mwishoni wataokolewa.

**18:11** Paulo alibaki katika Korinto kwa miezi 18 akifundisha Neno la Mungu. Kuna habari nyingine juu ya muda huu ndani ya 1 na 2 Wakorinto.

**18:12-16** Tunafikiri karibu na mwisho wa muda huu **Galio** aligeuka **liwali la Akaya** (karibu 51 A.D.). **Wayuda** walifikiri **liwali** huyu mpya atakuwa na roho nzuri na walileta Paulo mbele **ya kiti cha hukumu** kwa pahali pa soko katika Korinto. Walishitaki **Paulo** kusema alikuwa akiwashawishi **kuabudu Mungu** kwa njia **isiyopatana na sheria ya Wayuda**. Wakati Paulo asipofungua kinywa chake bado kujisimamia, **Galio** alikataa kabisa kuhukumu shitaki hili. Alisema na Wayuda kwamba hili lilikuwa neno la **sheria yao yenyewe,** si neno ambalo ilimpasa yeye kuhukumu. Kama mtu **akitenda uovu au kwa hila mbaya**, **Galio angewasikiliza na saburi,** lakini yalikuwa mabishano tu juu ya **maneno na majina na sheria ya Wayuda.** Galio **alikataa kuhukumu maneno ya namna hii**, akafukuza washitaki Wayuda**.**

**18:17** Watu wengine wanafikiri kwamba **Wayunani** waliazibu **Sositeni** kwa sababu alileta Paulo mbele ya **Galio** na mashitaki madogo namna hii. Wakati tunaposoma **Galio hakuona mambo yale kuwa kitu,** si kusema aliona Habari Njema bure, lakini kwamba hakutaka kujiingiza ndani ya sheria na desturi za Wayuda.

**18:18** Nyuma ya matukio haya **Paulo alibaki** katika Korinto kwa **siku nyingi**. Labda kwa wakati huu aliandika 2 Watesalonika.

Wakati mwishoni **alipoondokea** Korinto, pamoja na **Prisila na Akila**, aliingia chombo kwenda Suria, na toka kule alikusudi kurudia Antiokia. Walimu hawajui kabisa kama nani **alinyoa kichwa chake kwa Kenkurea,** Paulo au Akila. Kenkurea ulikuwa bandari ya mashariki ya Korinto. Wengine wanafikiri maneno ya **kiapo** ilikuwa desturi ya Wayuda isiyofaa kwa Mkristo kamili kama Paulo.

**18:19, 20** Wakati chombo chao kilipofika **EFESO,** Prisila na Akila walitoka chombo wakikusudi kubaki pale. Paulo alifikia **sunagogi** kwa saa ndogo chombo lilichobaki pale na **alisemezana na Wayuda**. Walimwomba kubaki pale saa kidogo tena, lakini neno hili halikuwezekana.

**18:21** Chombo kilikuwa karibu kuondoka, lakini Paulo **aliahidi kurudia Efeso, Mungu akitaka,** nyuma ya **siku kubwa katika Yerusalema.**

**18:22** Chombo kilisimama tena kwa **KAISARIA.** Toka pale mtume alipanda na **kusalimu kanisa** kwa Yerusalema. Kisha **alishuka kwa ANTIOKIA**. Ilikuwa mara ya mwisho aliyofika pale. Ulikuwa mwisho wa safari ya pili ya Paulo kuhubiri Habari Njema.

### G. Safari ya tatu ya Paulo ya kuhubiri: kwa Asia Ndogo na Yunani (18:23 – 21:26)

**18:23** Nyuma ya kubaki kwa Antiokia siku nyingi, Paulo alikuwa tayari kuanza safari ndefu nyingine kuhubiri

Habari Njema. Habari za safari hii zinaendelea kufika 21:16.

Alifikia kwanza makanisa katika inchi ya **GALATIA** na **FURIGIA**, moja kwa moja, na **kupatisha wanafunzi nguvu katika imani.**

**18:24-26** Mashairi haya yanaturudisha kwa habari zilizotukia kwa **Efeso. Akila na Prisila** walibaki pale**. Mtu wa elimu** alifika pale, **jina lake Apolo, naye alijuana sana na Maandiko ya Agano la Kale.** Alizaliwa **Myuda**, na alitoka kwa Alesanduria, mji mkubwa wa sehemu ya kaskazini ya Misri. Alihubiri na uwezo sana, pamoja na bidii, lakini hakujua maneno yote ya imani ya Wakristo. Alijifunza karibu na **Yoane** Mbatizaji na alijua namna **Yoane** alivyoita taifa la Israeli kutubu na kujitayarisha kwa kuja kwa Masiya. Ni kama hakujua habari za ubatizo wa Wakristo, na alikuwa mjinga kwa maneno mengine ya mafundisho ya Wakristo. Wakati **Akila na Prisila walipomsikia** akihubiri **katika sunagogi,** walifahamu kwamba alihitaji kujifunza maneno mengine. **Walimpeleka kwao, wakamfunulia zaidi njia ya Bwana.** Ni vizuri kuona kwamba mhubiri huyu **mwenye uwezo kwa masemo** alikubali kufundishwa na mfanya hema na mke wake.

**18:27,28** Kwa sababu Apolo alikuwa na roho tayari kupokea mafundisho, **ndugu** za Efeso walimtia moyo kwenda Korinto kuhubiri Neno la Mungu, **wakamwandikia barua** kusudi ndugu wa kule wampokee vizuri. Basi Apolo aliweza kusaidia waamini katika Korinto sana. **Alishindana na Wayuda kabisa kabisa** na kuonyesha **mbele ya watu wote kwamba Yesu ni** kweli **Kristo** wa Mungu.

**19:1** Wakati Paulo alipokuwa katika **Efeso** mbele, aliahidi Wayuda katika sunagogi kwamba atarudi tena, kama Mungu akitaka. Sasa alitaka kutimiza ahadi hii na alisafiri toka Galatia na Furigia kwenda **EFESO** kwa pwani ya mangaribi ya Asia. Pale alikutana na wanaume kumi na wawili waliosema walikuwa wanafunzi. Wakati aliposemezana nao alifahamu kwamba walijua nusu tu juu ya imani ya Wakristo. Alikuwa na shaka kama walikuwa wamepokea Roho Mtakatifu.

**19:2** Hivi aliwauliza, **"Mulipokea Roho Mtakatifu wakati mulipoamini?"** Maana wakati mwenye zambi anapoamini Mwokozi, anapokea Roho Mtakatifu saa ile ile.

Wanafunzi wale walijibu, **"Hapana, hatukusikia ya kama Roho Mtakatifu yuko."** Watu hawa walikuwa wanafunzi wa Yoane Mbatizaji (ona sh. 3) na ingaliwapasa kujua kwa njia ya Agano la Kale kwamba **Roho Mtakatifu** yuko. Na vilevile Yoane alikuwa amefundisha wanafunzi wake kwamba Yule ambaye atamfuata atawabatiza na Roho Mtakatifu. Neno wanafunzi hawa wasilojua ni ya kwamba **Roho Mtakatifu** alikuwa amefika siku ya Pentekote.

**19:3, 4** Wakati Paulo alipowauliza juu ya ubatizo, aliona kwamba watu hawa walijua habari za **ubatizo wa Yoane** tu. Hivi walifahamu kwamba Masiya alikuwa karibu, na walionyesha ya kuwa **walitubu zambi** zao kwa njia ya **kubatizwa**, ndilo neno walilohitaji kujitayarisha kwa kumpokea kama Mfalme. Hawakujua kwamba **Kristo** alikuwa amekufa, alizikwa, alifufuliwa toka wafu, alirudi tena mbinguni, na ya kwamba alikuwa alituma Roho Mtakatifu. **Paulo** aliwaelezea maneno haya yote. Aliwakumbusha kwamba wakati **Yoane** alipowabatiza na **ubatizo wa toba,** aliwaonya **kuamini … Kristo Yesu.**

**19:5 Wakati waliposikia habari hizi, wakabatizwa katika jina la Bwana Yesu.** Ndani ya kitabu cha Matendo tunasoma tena na tena juu ya enzi na mamlaka ya Yesu kama Bwana. Hivi

wanafunzi wa Yoane **walibatizwa** kwa amri ya **Bwana Yesu** na kama ushuhuda mbele ya watu kwamba walikuwa wamepokea Yesu Kristo kama Bwana (Yehova).

**19:6, 7** Kisha **Paulo aliweka mikono** yake **juu yao,** na walipokea **Roho Mtakatifu**. Hii ni mara ya ine **Roho Mtakatifu** aliyotolewa ndani ya Matendo. Mara ya kwanza ilikuwa ndani ya sura 2, siku ya Pentekote wakati alipotolewa zaidi kwa Wayuda. Mara ya pili ilikuwa ndani ya sura 8, wakati Wasamaria walipopewa Roho Mtakatifu saa Petro na Yoane walipowawekea mikono. Mara ya tatu ilikuwa katika Matendo 10, nyumbani mwa Mtaifa, Kornelio, kwa Yopa. Tulionyesha mbele kwamba matukio yaliyofikisha watu kupokea **Roho Mtakatifu** yalifuatana namna nyingine. Hapa katika Matendo 19 yalifuatana hivi:

Imani
Ubatizo mara ya pili
Kuwekewa **mikono** na mtume
Kupokea **Roho Mtakatifu.**

Kwa njia ya kutumika na **mikono** ya Paulo **kutoa Roho Mtakatifu** kwa wanafunzi wa Yoane, Bwana alizuiza watu kusema kwa wakati wa nyuma kwamba Paulo alikuwa chini ya Petro, Yoane, au mitume wengine.

Wakati wanafunzi wa Yoane walipopokea **Roho Mtakatifu walisema kwa lugha na kutabiri.** Mungu aliwezesha watu kufanya hivi mbele ya kuandikwa kwa Agano Jipya. Kwa wakati wa sasa tunajua tunapokea **Roho Mtakatifu** wakati tunapookolewa, si kwa njia ya alama na maajabu, au kwa njia ya kusikia furaha rohoni, lakini kwa njia ya ushuhuda wa Maandiko ya Agano Jipya.

Kwa dakika mtu anapoamini Bwana Yesu Kristo, Roho Mtakatifu anapanga ndani yake; anatiwa mhuri na Roho Mtakatifu; anapokea arabuni ya Roho; anapakaliwa na Roho; na anabatizwa na Roho kuingia Mwili wa Kristo. Lakini mara nyingine Roho anakuja juu ya mwamini fulani na uwezo mkubwa zaidi toka Mungu na kumpa uwezo mkubwa kwa kazi fulani, na uhodari katika imani, na kumjaza na hamu kubwa sana kwa wokovu wa watu.

**19:8** Paulo alifikia sunagogi katika Efeso kwa **miezi mitatu, akibishana na watu, na kuwavuta kuamini maneno ya ufalme wa Mungu.** Habari kubwa ya hotuba hizi ilikuwa **"Maneno ya Ufalme wa Mungu."**

C.E. Stuart alieleza:

> Ona ya kama Paulo angalihubiri *Habari Njema* ya Ufalme, neno hili lisingalikuwa taratibu kwa wakati ule. Bwana Yesu alihubiri juu yake, lakini itatimizwa kwa wakati wa kuja (Mt. 24:14; Ufu. 14:6,7). Lakini Paulo alihubiri juu ya Ufalme wa Mungu ulio kwa wakati wa sasa duniani.

**19:9, 10** Wakati wengine wa Wayuda walipopata **mioyo migumu** (kwa akili yao) na kukataa kutii (na kutaka kwao), wakati walipoamsha uadui katikati ya **makutano** juu ya **Njia**, Paulo aliondokea sunagogi, na **aliondosha wanafunzi** wake toka pale. Aliwapeleka kwa **darasa ya Tirano,** pahali alipokuwa na ruhusa kuwafundisha **kila siku**. Walimu wanafikiri **Tirano** alikuwa Myunani, mwalimu wa usemaji na elimu nyingine. **Kwa miaka miwili** Paulo alifundisha wanafunzi, kisha aliwatuma kufundisha watu wengine vilevile. Kwa njia hii watu wote waliokaa katika wilaya ya **Asia walisikia neno la Bwana Yesu, Wayuda na Wayunani vilevile**. Hivi mlango mkubwa wa kufaa sana ulifunguliwa kwa Paulo, hata kama kulikuwa na adui wengi (1 Kor. 16:9).

**19:11,12** Kwa sababu **Paulo** alikuwa mtume wa Yesu Kristo, alikuwa na uwezo wa kufanya alama na maajabu. Maneno haya yalihakikisha kwamba yeye alikuwa mtume kweli na ma-

fundisho yake yalitoka kweli kwa Mungu. Uwezo ulipita ndani yake hata **vitambaa na nguo** alizogusa zilikuwa na uwezo kuponyesha **wagonjwa** na wenye pepo wachafu. Halafu watu wanauliza kama inawezekana kwa **maajabu** haya kufanywa leo vilevile. Roho Mtakatifu ni mwenye enzi, naye anaweza kufanya neno lo lote analotaka. Tunakubali kwamba mitume na wajumbe wao walipewa enzi. Kwa wakati wa sasa hatuna mitume namna ya mitume ya zamani, hivi haifai kusema maajabu haya yanaweza kufanywa leo.

**19:13, 14** Kila mara Mungu anapotumika na uwezo, Shetani ni karibu kuzuiza na kushindana na kazi yake. Wakati Paulo alipokuwa akihubiri na kufanya maajabu, kulikuwa na Wayuda wengine wenye kutangatanga katika Efeso waliotoa **pepo wachafu.** Waliagiza **pepo wachafu** (wakitaja **jina la Bwana Yesu** kama dawa) kutoka ndani ya wenye kukaliwa nao. Bwana Yesu alikubali kwamba wengine wa Wayuda walikuwa na uwezo wa kutoa pepo wachafu (Lk. 11:19).

Wengine wa wachawi hawa Wayuda walikuwa wana saba wa Sikewa. Sikewa aliwekwa kuwa **kuhani mkubwa**. Siku moja wana wake walijaribu kutoa pepo mchafu ndani ya mtu. Walisema na pepo mchafu, **"Tunakuapiza kwa Yesu yule anayehubiriwa na Paulo."**

**19:15, 16** Walisema maneno haya, lakini walikosa uwezo wenyewe, na pepo mchafu hakutii. Alijibu, **"Yesu ninajua, na Paulo ninafahamu, lakini ninyi ni nani?"**

Ona tofauti Maandiko yanayoweka katika **pepo mchafu** (sh.15) na **mtu mwenye pepo mchafu** (sh.16). Ndani ya shairi 15 pepo alisema, lakini ndani ya shairi 16 mwenye pepo **alirukia** wana wa Sikewa, **akawashinda,** nao walikimbia nyumba ile, wichi na wenye vidonda.

**19:17** Wakati habari za kushindwa kwa pepo za Shetani zilipoenea katikati ya watu kando kando waliogopa sana, lakini **jina la Bwana Yesu likatukuzwa**. Halikuwa jina la Paulo lililotukuzwa, lakini **jina la** Mwokozi wa Paulo.

**19:18, 19** Hivi Roho ya Mungu alitumika na uwezo kabisa katikati ya wale waliotenda uchawi namna namna mbele, na wengi wao waliamini Kristo, **wakakiri … matendo yao.** Nyuma ya kufanya hivi walionyesha imani yao wazi mbele ya watu wote kwa njia ya kuleta **vitabu vyao** vya uchawi na kuviteketeza kwa moto mkubwa. Kwa wakati vitabu hivi vilipoandikwa, bei yao ilikuwa vipande elfu makumi tano vya feza. Ni nguvu kujua kama bei yao ilikuwa ngapi kwa mali ya wakati wa sasa.

**19:20** Habari za kuachana na desturi hizi za wapagano **zilisaidia Neno la Mungu kuzidi sana na kushinda.** Labda kama Wakristo wa sasa wangalichoma vitabu na gazeti zao za bure ya zambi, Neno la Mungu lingaliendelea kupita sana kwa wakati wa sasa.

**19:21** Muda Paulo aliyoshinda katika Efeso ulikuwa karibu kwisha, naye alikusudi **kurudia Yerusalema** kwa njia ya kupita kwa **Makedonia na Akaya**, na nyuma yake alitaka **kuona Roma vilevile**. Roho yake ilijaa mapendo na huruma na hamu kufikia pahali Habari Njema ilipoweza kuhubiriwa, na toka pale Habari Njema ilipoweza kuenea kwa pahali pengine vilevile.

**19:22 Alituma Timoteo na Erasto** mbele yake kwa **Makedonia**, lakini **yeye** mwenyewe alikaa katika **Asia** kwa saa ndogo. Ni kama aliandika 1 Wakorinto kwa wakati ule (karibu 56 A.D.).

**19:23-27** Kwa sababu ya mahubiri ya Paulo Waefeso wengi waliamini Bwana na waliachana na sanamu zao. Neno hili lilipunguza kazi ya wafanyaji sanamu sana. **Demetrio, mwenye kufua**

**feza** alikuwa mmoja wa wale ambao walipata hasara sana. Kazi yake ilikuwa kufanya vihekalu vidogo vya feza vya Diana. Alikutanisha wote wenye kazi hii na alijaribu kuwaamsha kufungana pamoja kuzuiza hatari hii. Aliwakumbusha ya kuwa **Paulo** aliweza kuaminisha **watu wengi** kwamba hakuna **miungu inayofanywa kwa mikono ya watu.** Demetrio alifunua kusudi la kweli la roho yake wakati aliposema ya kwamba kuna **hatari kwa kazi yao**, lakini alijaribu kuheshimu **Diana** na **hekalu** lake sana.

**19:28-31** Kusanyiko la wenye kufua feza liliongezeka kuwa machafuko ya **mji mzima**. Makutano wakilalamika, **"Diana wa Waefeso ni mkubwa"** wakaingia **nyumba ya michezo** kwa mbio na kukamata **Gayo na Aristarko,** wawili wa **watu waliosafiri pamoja na Paulo,** bila shaka na kusudi kuwaua. Paulo yeye mwenyewe **alitaka** kusema na makutano, lakini **wanafunzi** walimzuiza, na watu wengine wa Asia waliokuwa rafiki za **Paulo** walimsihi asijaribu kuingia nyumba ya michezo.

**19:32** Basi makutano walichafuka kabisa. Wengi wao hawakufahamu kwa sababu gani walikuwa pale na walilalamika maneno mbalimbali.

**19:33, 34** Myuda mmoja, jina lake **Alesanduro** alijaribu kusema na makutano. Bila shaka alikusudi kusimamia Wayuda na kuonyesha kwamba machafuko haya si kosa lao. **Lakini wakati** makutano **walipotambua kwamba alikuwa Myuda** walifanya makelele makubwa. Kwa karibu saa mbili walilalamika kwamba **"Diana wa Waefeso ni mkubwa!"**

**19:35** Kwa wakati ule **mkubwa wa mji** aliweza kutuliza **makutano**. Alisema na watu kwamba hawakuhitaji kuogopa neno. Watu wote walijua kwamba Efeso ulichaguliwa kuwa **mlinzi wa hekalu la mungu mke mkubwa Diana**. Hata kama miji karibu kumi na mitatu ya Asia ilishiriki ndani ya kuchunga hekalu, ilikuwa kazi ya heshima ya Waefeso kulilinda. Nao walipewa heshima vilevile kulinda sanamu ya Diana waliyofikiri ilianguka toka mbinguni.

**19:36-41** Akisema kwamba dini yao ilikuwa imara na ya kwamba hakuna neno lililoweza kuzuiza watu wasiabudu Diana, alionyeshea watu upumbavu wao kufanya makelele namna hii. Watu wale ambao walilalamikia hawakuwa **wizi wa hekalu** na **hawakutukana** Diana. **Kama Demetrio na mafundi waliokuwa pamoja naye** walikuwa na mashitaki ya haki, wayalete kwa **baraza** na **wakubwa**. Lakini walikuwa wamekutana na machafuko. Waroma hawakupendezwa na makusanyiko ovyo ya namna hii, na watu wa Efeso **wakisitakiwa kwa ajili ya makelele haya** wasingaliweza kueleza maana yake. Na mkubwa wa mji alijua vilevile ya kwamba alikuwa katika hatari ya kuondoshewa kazi yake, na labda hata uzima wake kama habari za makelele haya zikifikia Roma.

Halafu makutano walitulia na kurudia nyumba zao.

**20:1** Tukisoma shairi 1 tungefikiri kwamba Paulo alisafiri mara moja toka Efeso kwenda **Makedonia**. Lakini tukisoma 2 Wakorinto tunaona kwamba alikwendea TROA kwanza. Njia ilikuwa wazi kwaye kuhubiri Habari Njema pale, lakini alitaka sana kuona Tito na kusikia habari kama Wakorinto walipokea barua yake ya kwanza namna gani. Wakati asipokuta Tito kwa Troa alivuka bahari kwa upande wa kaskazini-mashariki kufika **MAKEDONIA.** Bila shaka alifikia inchi kavu kwa Neapoli, na aliendelea na safari yake kwenda Filipi. Tunafikiri alikutana na Tito kwa Filipi na alifurahi kusikia habari toka Korinto. Labda aliandika barua yake ya pili kwa Wakorinto kwa

wakati ule (56 A.D.?) (Ona 2 Kor. 1:8, 9; 2:12-14; 7:5-7.)

**20:2, 3a** Nyuma ya kuhubiri kwa Makedonia kwa wakati, alisafiri kwa upande wa kusini **kwa YUNANI**. Ni kama alishinda karibu **miezi mitatu** katika KORINTO, na aliandika barua yake kwa Waroma kwa muda ule. Watu wengine wanafikiri aliandika Wagalatia vile vile kwa wakati ule.

**20:3b** Paulo alikusudi kuvuka bahari toka Korinto kwenda Suria. Lakini wakati aliposikia kwamba **Wayuda** walikusudi kumwua njiani, aligeuka na alikwenda kwa upande wa kaskazini na kupita tena kwa **MAKEDONIA.**

**20:4** Sasa tunasoma habari za wengine wa watu waliosafiri pamoja na Paulo. Walikwenda pamoja naye **mpaka Asia**, lakini tunajua kwamba wengine walisafiri hata Roma pamoja naye:

Labda **Sopateri wa Beroya** alikuwa Sosipateri, mtu wa jamaa ya Paulo katika Rom. 16:21.

**Aristarko** wa Tesalonika alikuwa karibu kufa kwa wakati wa machafuko kwa Efeso (Mdo. 19:29). Kwa wakati wa nyuma alikuwa gerezani pamoja na Paulo kwa Roma (Flm. 24; Kol. 4:10).

**Sekundo** alikuwa mtu wa Tesalonika na alisafiri pamoja na Paulo kufika Asia, labda Troa au Mileto.

**Gayo, mtu wa Derbe**, si mtu wa Makedonia ambaye alishikwa na makutano kwa Efeso (Mdo. 19:29). Tunasoma juu ya Gayo mwingine aliyekuwa mwenyeji wa Korinto aliyepokea Paulo nyumbani mwake wakati alipokuwa pale (Rom.16:23). Mtume Yoane aliandika barua yake ya tatu kwa mtu aliyeitwa Gayo. Tunafikiri Gayo huyu aliishi katika mji mwingine karibu na Efeso. Ni kama watu wengi waliitwa Gayo.

**Timoteo alisafiri pamoja na Paulo kwa Asia,** na alikuwa pamoja naye kwa Roma mara ya kwanza alipokuwa gerezani. Nyuma yake alisafiri pamoja na Paulo kwa Asia. Ndani ya barua yake ya pili kwa Timoteo Paulo alimwambia kwamba alitaka sana kumwona tena, lakini hatujui kama neno hili liliwezekana.

Tunafikiri **Tikiko**, mtu wa **Asia Ndogo**, alisafiri pamoja na Paulo kufika Mileto. Nyuma ya wakati alifungana na Paulo tena kwa Roma na alitumika pamoja naye kufika wakati Paulo alipofungwa mara ya pili.

Ni kama **Trofimo** alikuwa Mtaifa wa Efeso, katika Asia Ndogo. Alikwenda pamoja na Paulo kufika Yerusalema. Bila kukusudia Paulo alifungwa kwa sababu yake. Jina lake linatajwa katika 2 Tim. 4:20 vilevile.

**20:5, 6** Ni kama ndugu hawa saba walisafiri mbele kwa **Troa**, lakini Paulo na Luka walifikia **FILIPI** kwanza. (Tunafikiri Luka alikuwa pamoja na Paulo kwa sababu aliandika *ku**tu**ngojea* katika shairi 5 na ***tu**litoka,* vivi hivi ndani ya shairi 6.) **Nyuma ya siku za mikate pasipo chachu**, au Pasaka, Paulo na Luka walitoka Filipi kwenda kwa njia ya bahari toka Makedonia kufika **TROA.** Haikuwa safari ndefu, lakini hatuambiwi kwa sababu gani ilihitaji **siku tano** mara hii.

**20:7-9** Tukisoma mashairi 6 na 7 pamoja, ni kama mtume alingoja na kusudi kwa siku saba katika Troa ili aweze kuwa pale **siku ya Bwana** kwa kusanyiko la wanafunzi kuvunja **mkate.** Shairi 7 linaonyesha wazi kwamba ilikuwa desturi ya Wakristo kwa wakati wa mwanzo wa Kanisa kukutana **siku ya kwanza ya juma** kuvunja mkate.

Haifai tushangae kwa sababu **Paulo** alihubiri **kufika saa sita ya usiku**. Wakati roho ya waamini kanisani inapowaka, Roho Mtakatifu ni huru kutumika na uwezo bila kufungwa na saa. Lakini wakati saa za mangaribi zilipopita, hewa ndani ya chumba cha juu iligeuka nguvu kuvuta kwa sababu ya

taa nyingi zilizokuwa zikiwaka na hesabu kubwa ya watu waliokuwa pale. **Kijana mmoja, jina lake Eutiko,** aliyeketi kwa **dirisha** wazi, alishindwa na usingizi, akaanguka chini hata udongo inje ya nyumba, akauawa.

**20:10** Lakini Paulo alishuka, akajinyolosha juu ya mwili wa kijana, namna manabii walivyofanya zamani. Kisha aliwaambia watu kwamba haifai wakae kufazaika juu ya neno hili kwa sababu Eutiko alikuwa hai. Labda masemo haya ya Paulo yangetufikirisha kwamba watu hawakuhitaji kusumbukia hali ya kijana kwa sababu hakufa; **uzima wake** ungali **ndani yake.** Lakini shairi 9 linaonyesha wazi kwamba alikuwa amekufa kweli. Akitumika na uwezo wake kama mtume **Paulo** alikuwa ametenda ajabu na kumfufua.

**20:11, 12** Wakati Paulo alipopanda tena, walivunja **mkate** (sh.11), maana walikula karamu ya Bwana, ndilo kusudi la kusanyiko lao (sh.7). Nyuma yake walikula chakula pamoja. Karamu hii ya mapendo *(agape* kwa Kiyunani) ilikuwa desturi ya waamini kwa wakati wa mwanzo wa Kanisa, lakini nyuma ya wakati desturi mbaya yaliingia ndani yake (1 Kor. 11:20-22) na polepole Wakristo waliacha kula karamu hii pamoja.

Nyuma ya kusanyiko hili lililoendelea usiku mzima, mtume aliagana na waamini katika Troa.

**20:13-15** Paulo aliondokea Troa, akitembea na mguu kilomètres 32 kufikia Asosi. Watu wale waliosafiri pamoja naye walikwenda ndani ya merikebu na walikutana naye kwa Asosi. Labda alitaka kuwa peke yake kwa wakati kuwaza juu ya Neno la Mungu na maombi.

Walisafiri kwa pwani ya mangaribi ya Asia Ndogo, wakafikia **MITILENE** kwanza, ndio mji mkubwa wa kisanga cha LESBOS. Kesho yake walishusha nanga karibu na kisanga cha **KIO**. Safari ya siku moja nyingine iliwafikisha kwa kisanga cha **SAMOSI na walikaa kwa TROGULIO**. Mwishoni walifikia **MILETO,** bandari moja kwa pwani ya kusini-mangaribi, kilomètres 56 toka Efeso kwa kusini.

**20:16 Paulo** hakufikia **Efeso** na kusudi saa hii kwa sababu alikuwa **akisafiri mbio akijaribu kufikia Yerusalema mbele ya siku ya Pentekote.**

**20:17** Wakati wasafiri walipofikia **Mileto**, Paulo alituma habari kwa wazee katika **Efeso** kuwaomba kufika kukutana naye. Bila shaka saa nyingi kidogo ilihitajiwa kwa habari hizi kuwafikia na kwa kufanya safari kwenda kusini. Hata hivi walipokea zawabu kubwa, ndiyo kuweza kusikia hotuba hii nzuri sana toka mtume yule mheshimiwa. Ndani yake tunaona mfano wa mtumishi mzuri sana wa Bwana Yesu Kristo. Tunaona mtu ambaye alijitoa na mapendo kupita kipimo kwa Mwokozi. Alitumika bila kuacha, bila kuchoka na bila kushindwa. Alikuwa mwenye unyenyekevu wa kweli. Alikuwa tayari kulipa bei gani iliyohitajiwa. Utumishi wake ulikuwa tunda la hamu kubwa rohoni kupendeza Bwana. Alikuwa mwenye uhodari uliotoka kwa Bwana. Halikuwa neno kubwa kwake kama ataishi au kufa; neno lililokuwa kubwa kweli lilikuwa kwa mapenzi ya Mungu kufanyika na kwa watu kusikia Habari Njema. Hakujifikiri mwenyewe wala faida yake mwenyewe ndani ya maneno yote aliyofanya. Alipenda kusaidia watu kupita kusaidiwa mwenyewe. Hakuacha mambo magumu kumzuiza. Alifanya yeye mwenyewe maneno aliyohubiri.

**20:18,19** Paulo alikumbusha wazee wa Efeso **namna alivyoishi katikati yao. Tangu siku ya kwanza** alipofikia **Asia,** na kwa muda zima aliyokaa pale alitumikia **Bwana** na **unyenyekevu** wa kweli, akijikana mwenyewe. Ulikuwa utumishi mgumu kwa roho yake, pamoja na **machozi** ya huzuni na **taabu.**

Alikuwa akiteswa wakati wote kwa sababu ya **hila ya Wayuda**. Hata hivi alitumikia Bwana na uhodari bila woga.

**20:20,21** Paulo **hakufichia** Waefeso neno lo lote lililoweza kuwa na faida kwa roho zao. **Aliwafundisha mbele ya watu, na nyumba kwa nyumba,** akisukumwa na mapendo ya Kristo. Hakuweka saa fulani kwa makusanyiko ya kanisa, lakini alitumika saa yo yote aliyopata njia kusaidia waamini kupata nguvu katika imani. Bila kuweka roho kama wasikiaji walikuwa watu wa taifa gani au dini gani, alihubiri kwamba **iliwapasa kutubu kwa Mungu na kuamini Bwana wetu Yesu Kristo.** Hizi ndizo sehemu kubwa mbili za Habari Njema. Kila mara mtu anapogeuka kwa Bwana kwelikweli, **anatubu kwanza, kisha anaamini Yesu. Toba** ni bure bila **imani** ndani ya Mwana wa Mungu. Mwenye zambi **anatubu** kweli wakati anapogeuka na kukubali kwamba yeye ni mpotevu na ananyenyekea hukumu ya Mungu. **Imani** ni kujitoa mwenyewe kwa Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi.

Ndani ya mashairi mengi katika Agano Jipya tunasoma kwamba **imani** tu inahitajiwa kwa wokovu. Lakini tunajua kwamba **toba** inatangulia **imani**. Namna gani mtu ataweza kweli kweli kupokea Yesu Kristo kama Mwokozi bila kufahamu kwanza kwamba anahitaji Mwokozi? Ni kazi ya Roho Mtakatifu ndani ya roho ya mtu ambayo inamfahamisha hatia yake na kumwongoza **kutubu.**

**20:22,23** Nyuma ya kukumbusha Waefeso juu ya maisha yake katikati yao Paulo alifikiri juu ya mateso ambayo yalimngojea. Alifungwa na **Roho kwenda Yerusalema,** maana yake ni kama Roho Mtakatifu alimsukuma kwenda. Hakujua kabisa mambo gani yatatokea kule, lakini alijua maisha ya **vifungo na mateso** yalimngojea. **Roho Mtakatifu** alimfahamisha neno hili ndani ya **kila mji**, labda kwa njia ya manabii au kumfahamisha rohoni kwa njia nyingine toka juu.

**20:24** Wakati mtume alipofikiri juu ya maneno haya, hakuwaza kwamba **uzima** wake mwenyewe ulikuwa neno kubwa. Neno aliloweka roho juu yake zaidi lilikuwa kutii Mungu na kumpendeza. Alikuwa tayari **kutoa uzima wake** kama ikihitajiwa. Hakuna toleo lililo kubwa zaidi kwa Bwana yule ambaye alimkufia. **Alitaka tu kumaliza mwendo wake** na **kazi aliyopewa na Bwana Yesu**, **kushuhudia Habari Njema ya neema ya Mungu**, habari za kufurahisha zaidi kwa wenye zambi ambao walistahili maumivu katika gehena tu kwa milele. Ni habari za kuja kwa Mwana mpendwa wa Mungu toka utukufu mkubwa zaidi wa mbingu kuvumilia mateso kutoa damu yake, na kufa kwa Kalvari kusudi wale ambao wanamwamini waweze kupokea usamehe kwa zambi zao na uzima wa milele.

**20:25-27** Paulo alijua hataona ndugu zake wapenzi wa Efeso tena, lakini aliwaondokea na zamiri safi. Alikuwa amewatangazia **makusudi yote ya Mungu.** Hakuwafundisha Habari Njema tu, lakini kweli zote ambazo walihitaji kuwawezesha kutukuza Mungu ndani ya maisha yao ya kila siku.

**20:28** Na kwa sababu hatawaona tena, aliwaonya sana **wachunge roho zao wenyewe** safi mbele ya Mungu. Kama wao wasipokuwa na upatano wa karibu na Mungu, hawataweza kuongoza **kanisa** vizuri kwa maneno ya roho.

Kazi yao kama wazee ilikuwa kuangalia **kundi lote … ambalo Roho Mtakatifu aliwapa kuwa wasimamishi ndani yake.** Wasimamishi ndani ya kanisa waliitwa wazee na waangalizi vilevile. Shairi hili linaonyesha kwamba wazee hawachaguliwi na kanisa la pahali fulani. **Roho Mtakatifu aliwaweka kuwa wasimamishi na** inapasa waamini ambao wanatumika katikati yao kuwakubali kuwa wasimamishi wao.

Ilikuwa kazi yao **kulisha kanisa la Mungu.** Hii ilikuwa kazi kubwa kwa sababu **alilinunua kwa damu yake mwenyewe.** Walimu wa Biblia wamefazaika sana juu ya semo hili, kwa sababu linaonyesha **Mungu,** aliye Roho, akimwanga damu yake. Ni Bwana Yesu aliyemwanga damu yake, na hata kama Yesu ni Mungu, hatusomi pahali po pote juu ya **Mungu** akitoa damu yake au akikufa.

J.N. Darby, mtafsiri mmoja wa Biblia alitafsiri semo hili hivi: "Kanisa la Mungu ambalo alinunua na damu ya yule aliye yake." Ni kusema Mungu alinunua Kanisa, lakini alifanya hivi na damu ya Mwana wake mwenyewe, Bwana Yesu Mbarikiwa.

**20:29, 30** Paulo alifahamu kwamba **nyuma ya kuondoka** kwake, adui watashindana na kanisa toka inje na ndani. Walimu wa uwongo, kama imbwa wakali za poli wataingia kundi bila huruma. Watu wengine wa kanisa watajaribu kugeuka viongozi na wenye kuonekana katikati yao, wakifundisha maneno yasiyo kweli, na **kuvuta wanafunzi kuwafuata.**

**20:31** Kwa sababu ya hatari hii ilipasa wazee kukaa na ange kabisa, na kukaa **kukumbuka** ya kwamba **kwa miaka mitatu** mtume aliwaonya **usiku na mchana na machozi.**

**20:32** Ona ya kwamba Paulo aliwaweka **kwa mikono ya Mungu, na katika neno la neema yake**. Hakuwatia kwa mikono ya watu wengine kuwaongoza. **Mungu na** Maandiko tu yaliweza **kuwajenga na kuwapa uriti pamoja nao wote waliotakaswa**.

**20:33-35** Mtume Paulo alimaliza hotuba yake na kukumbusha wazee mfano wa maisha na utumishi wake mwenyewe. Alisema na haki kwamba **hakutamani feza, wala zahabu, wala mavazi** ya mtu. Hakutumikia Bwana kwa sababu alitaka kujipatia mali. Kwa maneno ya dunia alikuwa masikini, lakini kwa maneno ya Mungu alikuwa tajiri. Akiwaonyeshea mikono yake aliweza kuwakumbusha kwamba na **mikono** hii alikuwa ametumika kazi kwa **mahitaji yake na ya wale waliokuwa pamoja naye.** Na zaidi ya ile, alifanya hema kwa kupata mali aweze kusaidia wagonjwa na walio **zaifu** katika mwili au roho. Wazee wakumbuke neno hili na kujaribu kutendea watu wengine mema kwa njia yo yote, na kukumbuka **masemo ya Bwana Yesu kwamba: "Heri ya kutoa inapita heri ya kupokea."** Masemo haya hayakuandikwa pahali pengine ndani ya vitabu vya Habari Njema, lakini yanajumlisha mafundisho ya Bwana, na Roho Mtakatifu aliyaongeza hapa.

**20:36-38** Kwa mwisho wa hotuba yake Paulo **alipiga magoti, akaomba pamoja na** wazee, nao walihuzunishwa sana. Walionyesha mapendo yao kwa mtume wao mpendwa kwa njia ya kumwangukia kwa **shingo na kumbusu.** Neno ambalo liliwahuzunisha zaidi lilikuwa semo yake kwamba **hawataona uso wake tena.** Na roho za huzuni **walimshindikiza hata merikebu** kwa safari yake kwenda Yerusalema.

**21:1-4a** Nyuma ya kuagana na ndugu na mapendo mengi kwa Mileto Paulo na rafiki zake walisafiri ndani ya merikebu hata kisanga **KOSI**, wakalala pale usiku. **Kesho yake** waliendelea na safari yao kwenda kwa kusini kwa kisanga cha **RODO**, na kutoka kule walisafiri kwa upande wa mashariki na kufika **PATARA**, bandari ya Likia kwa upande wa pwani ya kusini ya Asia Ndogo. Kwa **Patara** waliingia **merikebu nyingine iliyovuka hata Foiniki,** ndiyo pwani ya **Suria**. **Tiro** ulikuwa mmoja wa miji mikubwa ya Foiniki. Wakisafiri kwa upande wa kusini-mashariki na kuvuka bahari ya Kati, walipita kisanga cha **Kipuro** kwa kusini

na **kushoto**. Bandari ya kwanza kwa inchi ya Palestina ilikuwa **TIRO. Mizigo ya merikebu** iliondoshwa pale, hivi Paulo na rafiki zake walipata njia kuonana na waamini pale na **kukaa** pamoja nao kwa **siku saba**.

**21:4b** Kwa wakati huu wanafunzi wa pale, **wakiongozwa na Roho walikataza Paulo kwenda Yerusalema.** Tangu miaka mingi wanafunzi wa Biblia wamejiuliza kama **Paulo** aliasi agizo hili na kusudi wakati alipokwenda **Yerusalema**, au kama hakutambua mapenzi ya Mungu wakati alipokwenda Yerusalema, au kwamba yalikuwa kweli kutaka kwa Mungu kwaye kwenda kule. Tukisoma shairi hili mbio bila kuwaza sana, labda tungefikiri mtume alikuwa mkaidi na aliasi uongozi wa Roho na kusudi. Lakini tukilisoma tena polepole, labda tutafahamu kwamba **Paulo** hakutambua ya kuwa wenye kutoa maonyo haya waliongozwa na **Roho**. Luka alipasha wasomaji wake kwamba wanafunzi wa Suria waliongozwa na Roho, lakini hakusema Paulo alifahamu neno hili. Tunafikiri labda Paulo alifikiri rafiki zake walitaka kumponyesha toka maumivu ya mwili, na hata mauti. Akipenda watu wa taifa lake, ndio Wayuda, sana, hakufikiri hali yake ya mwili ilikuwa neno kubwa zaidi.

**21:5, 6** Wakati **siku** saba zilipokwisha waamini *wote* wa Tiro walisindikiza wahubiri kufika pwani, ndio mfano mzuri wa mapendo ya Wakristo. Nyuma ya wakati wa maombi na kuagana na mapendo, **merikebu** iliondokea pwani na watu waliobaki **walirudi kwao.**

**21:7** Paulo na rafiki zake walisafiri hata **TOLEMAI,** bandari karibu 40 kilomètres toka Tiro. Pahali pale panaitwa Akko sasa, karibu na mji wa Haifa. Waliweza kuonana na **ndugu** za pale kwa siku moja.

**21:8** **Kesho yake** walisafiri na merikebu kwa kilomètres 48 kwa upande wa kusini na kumaliza safari yao kufikia **KAISARIA**. Walikaa pale ndani ya **nyumba ya Filipo, mhubiri** wa Habari Njema (si mtume Filipo). Filipo huyu alichaguliwa kuwa mmoja wa watumishi ndani ya kanisa kwa Yerusalema na alifikisha Habari Njema kwa Samaria. Towashi ya Etiopia aliokolewa wakati aliposikia mafundisho yake.

**21:9** Filipo huyu **alikuwa na binti wane, mabikira waliotabiri.** Walipewa zawadi toka Roho Mtakatifu kupokea habari kutoka Mungu na kuzijulisha kwa watu wengine. Watu wengine wamesema kwamba shairi hili linaleta ruhusa kwa wanawake kuhubiri na kufundisha kanisani. Lakini pahali pengine ndani ya Maandiko wanawake *wanakatazwa waziwazi* kufundisha, kusema, au kuwa na amri juu ya wanaume kanisani (1 Kor. 14:34,35; 1 Tim. 2:11,12). Hivi tunafahamu kwamba **binti hawa mabikira wane** walitabiri nyumbani mwao au kwa makusanyiko mengine, lakini si kanisani.

**21:10, 11** Wakati Paulo alipokuwa kwa Kaisaria, **nabii mmoja, jina lake Agabo alishuka toka Yudea.** Alikuwa **nabii** yule aliyefikia Antiokia toka Yerusalema na kutabiri kwamba kutakuwa na wakati wa njaa, ndio unabii uliotimizwa kwa wakati wa utawala wa Klaudio (Mdo. 11:28). **Sasa alikamata mkaba wa Paulo na kufunga mikono na miguu yake mwenyewe** nao. Tendo lake lilikuwa mfano wa neno litakalotokea. Manabii wengi katika Agano la Kale walijulisha watu habari zao namna hii. Halafu Agabo aliendelea kuonyesha maana ya mfano huu. Namna alivyokuwa **amejifungia mikono na miguu, vivyo hivyo Wayuda wa Yerusalema watafunga** mikono na miguu ya Paulo na kumtoa **kwa serikali ya Mataifa**. Kwa sababu ya utumishi wake kwa Wayuda (**mkaba** ndio mfano wake)

atakamatwa na kufungwa nao.

**21:12-14 Wakati** rafiki za Paulo na Wakristo katika Kaisaria waliposikia habari hizi **walimsihi asipande kwenda Yerusalema,** lakini Paulo hakushiriki masikitiko yao. Machozi yao yalivunja **moyo** wake tu. Aache woga wa kufungwa na kuwekwa gerezani kumzuiza asifanye neno aliloamini kuwa mapenzi ya Mungu? Alitaka wafahamu kwamba **alikuwa tayari, si kufungwa tu, lakini kufa katika Yerusalema kwa ajili ya jina la Bwana Yesu.** Maonyo yao yote yalikuwa bure, hivi walisema, **"Mapenzi ya Bwana yafanyike."**

Ni nguvu kuamini kwamba maneno ya kuagana ya Paulo yalisemwa na mtu aliyeasi maongozi ya Roho Mtakatifu na kusudi. Tunajua kwamba wanafunzi kwa Tiro, wakiongozwa na Roho Mtakatifu walimkataza asiendee Yerusalema (sh.4). Lakini Paulo ali*jua* kwamba walisema wakiongozwa na Roho Mtakatifu? Na ni kama kwa wakati wa nyuma Bwana alikubali safari hii kwenda Yerusalema wakati aliposema na Paulo, "Tia moyo kwa sababu sawasawa ulivyonishuhudia katika Yerusalema, hivyo imekupasa kunishuhudia vilevile katika Roma" (Mdo. 23:11). Maneno mawili ni wazi kabisa: 1. *Paulo* hakufikiri kwamba neno kubwa zaidi ambalo ilimpasa kuweka roho juu yake lilikuwa kuepuka hatari ndani ya utumishi wake kwa Bwana. 2. Bwana alitumika na matukio haya yote kwa utukufu wake.

**21:15, 16 Toka Kaisaria** walisafiri kwa inchi kavu kwenda Yerusalema, safari ya kilomètres 80, ndiyo safari ndefu kwa wakati ule. Hesabu ya wale waliosafiri pamoja ilikuwa imeongezeka kwani **wengine wa wanafunzi wa Kaisaria** walikwenda pamoja nao, na vilevile Mkristo mmoja, jina lake Mnasoni toka **Kipuro**, mmoja wa waamini wa kwanza kwa kisanga kile. Alikaa kwa **Yerusalema** sasa, na aliheshimiwa kwa njia ya kuweza kupangisha Paulo na wale waliosafiri pamoja naye nyumbani mwake wakati Paulo alipofikia **Yerusalema** mara ya mwisho.

Kufika kwa Paulo kwa **Yerusalema** kulimaliza safari zake za kuhubiri. Ndani ya baki la kitabu cha Matendo tunasoma juu ya kufungwa kwake, hukumu yake, safari yake kwenda Roma, kuhukumiwa na kuwekwa gerezani pale.

**21:17, 18 Ndugu kwa Yerusalema** walipokea Paulo na rafiki zake vizuri wakati walipofika. Kesho yake **Yakobo na wazee wote** walikusanyika nao. **Hatuwezi** kujua kabisa kama huyu alikuwa **Yakobo** gani. Labda alikuwa ndugu ya Bwana Yesu, au mwana wa Alufayo, au mtu mwingine mwenye jina hili. Tunafikiri alikuwa ndugu ya Bwana Yesu.

**21:19, 20a** Paulo alianza mazungumzo yao kwa njia ya **kuwaambia habari za maneno moja moja Mungu aliyotenda katika Mataifa kwa njia ya kazi yake.** Wasikiaji walifurahi sana kusikia habari hizi.

**21:20b-22** Hata hivi ndugu Wayuda walikuwa na shaka. Habari zilikuwa zimeenea kwamba mafundisho ya mtume Paulo hayakupatana na Musa na sheria. Maneno haya yangeweza kuamsha matata katika Yerusalema.

Watu walishitaki Paulo juu ya kufundisha **Wayuda wote** waliokaa katika inchi za Mataifa **kuacha Musa**, kwa njia ya kuwakataza **wasitahiri watoto wao, wala kufuata desturi za Wayuda.** Basi Paulo alifundisha maneno haya kweli au sivyo?

Ndiyo, alifundisha kwamba Kristo ni mwisho wa sheria kwa maneno ya haki kwa wale wanaoamini (Rom. 10:4). Alifundisha ya kwamba tangu kufika kwa Habari Njema ya Kristo waamini Wayuda hawatawaliwi tena na sheria.

Alifundisha kwamba mtu akitahiriwa kwa kuhesabiwa haki, mtu huyu anajitenga na wokovu katika Kristo Yesu. Alifundisha kwamba kurudi tena kwa mifano na vivuli vya sheria, nyuma ya kufika kwa Kristo kunapunguza heshima ya Kristo. Si nguvu kufahamu mawazo ya Wayuda juu ya Paulo.

**21:23, 24** Lakini waamini Wayuda walikuwa na shauri ambalo walifikiri litatuliza roho za Wayuda wenzao waamini na wasioamini. Walisema vizuri Paulo ashiriki na **watu wane** waliofungwa na naziri, ajisafishe pamoja nao, na kulipa gharama yao. Hili ndilo elezo la F.W. Grant:

> Afungane na waamini wane kama yeye, waliofungwa na kiapo cha wanaziri, na kutokea pamoja nao hekaluni akiwa amejisafisha, na kulipa mbele ya watu mali ambayo iliyohitajiwa kutimiza kiapo chao, kusudi watu waweze kutambua kwamba hakugeukia sheria yeye mwenyewe.[76]

Hatujui maneno mengi juu ya **naziri** hii, ila ya kwamba ilikuwa **kiapo** *kiyuda*, na kama Wayuda wakiona Paulo akitimiza kawaida yake, **watajua** bila shaka kwamba Paulo hakuongoza watu wengine kuacha kushika **sheria** ya Musa, na alishika **sheria** yeye mwenyewe.

Watu wengine wamesema ilikuwa vizuri kwa Paulo kutimiza maneno ya kiapo hiki kiyuda, na wengine wamesema hakutenda vizuri. Tunajua Paulo alitaka sana kufanya maneno haya yote kwa watu wote ili kwa njia zote apate kuokoa wengine (1 Kor. 9:19-23). Watu wengine wanafikiri alijaribu kupita kipimo kupatanishwa na Wayuda, na kwa njia hii alitenda kwamba mtu aliyetawaliwa na sheria. Wanasema matendo yake hayakupatana vizuri na mafundisho yake kwamba mwamini si chini ya sheria kwa kuhesabiwa haki au kwa mwenendo wake (Gal. 1 na 2). Hata kama tukifikiri nini sisi wenyewe, hatuwezi kujua mawazo na makusudi yake.

**21:25** Ndugu katika Yerusalema walijulisha Paulo kwamba **waamini wa Mataif**a hawakulazimishwa kutii maagizo ya sheria **ila kujilinda na vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu, na damu, na kitu kilichosongwa, na uasherati** (Mdo. 15:19, 20).

**21:26** Hatufahamu vizuri kwa wakati wa sasa maneno **Paulo** aliyotenda ndani ya shairi hili. Walimu wengine wanafikiri yalikuwa maneno ya kiapo cha naziri, lakini hata ikiwa hii, hatufahamu vizuri maneno yote yanayoandikwa ndani ya shairi hili.

### H. Paulo anafungwa na kuhukumiwa (21:27 – 26:32)

**21:27-29** **Wakati siku saba** za kiapo zilipokuwa **karibu kwisha**, tendo la Paulo kujaribu kutuliza **Wayuda** lilikufa bure. Wakati wengine wa **Wayuda** wasioamini toka **Asia** walipomwona **hekaluni** walianza makelele na machafuko kwa sababu yake. Walimshitaki kusema alifundisha maneno yasiyopatana na **Wayuda na sheria**. Zaidi ya ile walimshitaki juu ya kuchafua **hekalu** kwa njia ya kuingiza Wayunani ndani yake. Walikuwa wameona **Paulo** pamoja na **Trofimo mjini** mwa Yerusalema. **Trofimo** alikuwa mwamini Mtaifa toka Efeso. Kwa sababu Wayuda waliwaona pamoja, **walizania Paulo** alikuwa amepeleka rafiki yake kwa **kiwanja cha ndani cha hekalu** pamoja naye.

**21:30-35** Ni wazi ya kwamba mashitaki haya hayakuwa kweli, lakini hata hivi yalianza **machafuko makubwa mjini**. Watu **walikamata Paulo na nguvu, wakamkokota inje ya hekalu na kufunga malango ya viwanja vya ndani** nyuma yao. Habari za maneno haya zilifikia mkubwa wa kikosi cha askari wakati Wayuda walipotafuta njia kuua Paulo, akashuka mbio pamoja na askari na kuondosha Paulo katika

mikono ya watu wale walioshindwa na gazabu. Alifunga Paulo na minyororo miwili na kuuliza kama alikuwa nani na amefanya nini. Watu wa makutano walijibu **maneno ovyo yasiyopatana**. Basi mkubwa wa kikosi aliagiza askari kuleta mfungwa wao **ndani ya nyumba kubwa** ili aweze kupata njia kufahamu vizuri nini ilikuwa ikitokea. Makutano walikaa kufanya matata mengi kujaribu kukamata Paulo, hata ilipasa askari kubeba Paulo juu ya madaraja na kumwingiza nyumbani.

**21:36** Wakati walipokuwa wakifanya hivi walisikia watu wakilalamika, **"Ondoa mtu huyu."** Labda wengine wao walisikia maneno haya mbele.

**21:37-39** Wakati walipokuwa karibu kumfikisha ndani ya nyumba kubwa Paulo aliomba mkubwa ruhusa kusema neno. Mkubwa alishituka wakati aliposikia Paulo akisema kwa Kiyunani. Ni kama alifikiri alikuwa amefunga **Mmisri aliyeanza maasi mbele na kuongoza watu elfu ine** walioitwa **Wauaji kwenda jangwani**. Paulo alimjulisha kwamba alikuwa Myuda, mwenyeji wa Tarso, **mji wa Kilikia** usio mji bure. Tarso ulijulikana kwa sababu ya elimu na biashara na uliwekwa kuwa "mji huru" na mfalme Augustino. Kama ilivyokuwa desturi yake, **Paulo,** bila woga, aliomba ruhusa kusema na watu.

**21:40 Akipewa ruhusa, alisimama** pale katikati ya askari na kutuliza watu kwa njia ya kuwapungia mkono, na makelele makubwa ya mbele yalikombolewa na **kimya kubwa**. Halafu Paulo alikuwa tayari kutoa ushuhuda wake mbele ya Wayuda wa Yerusalema.

Tunafikiri **lugha ya Kiebrania** ilikuwa Kiaramaic iliyofanana sana na Kiebrania na iliyotumiwa na Waebrania kwa wakati ule.

**22:1, 2** Ilikuwa akili nzuri kwa Paulo kusema na makutano na Kiaramaic, si na Kiyunani. Watu **walipendezwa** wakati waliposikia lugha yao, wakaacha kulalamika kwa wakati.

**22:3-5** Paulo alianza na kuwapasha kwamba alikuwa **Myuda, alizaliwa katika Tarso, mji wa Kilikia,** akajifunza **kwa miguu** ya **Gamalieli**, mwalimu Myuda aliyejulikana sana kwa mafundisho yake juu ya dini ya Wayuda. Alipasha wasikiaji wake kwamba alikuwa na wivu sana kwa Mungu kama Myuda. Alikuwa **ametesa** Wakristo na kujaza **vifungo** na wale walioamini Yesu. **Kuhani mkubwa** na watu wa Baraza **walikuwa washuhuda** kwamba alifanya kazi hii na bidii sana, maana **walimpa barua** kumruhusu kwenda **Damasiki na kurudia Yerusalema na waamini** toka pale **waweze kuazibiwa.**

**22:6-8** Kufika saa ile Wayuda waliweza kufahamu hotuba ya Paulo vizuri na kukubali kwamba alisema kweli. Halafu sasa mtume atawaambia habari za tukio lililogeuza maisha yake kabisa. Itakuwa kazi yao kukata shauri kama tukio hili lilitoka kwa Mungu au sivyo.

Wakati Paulo alipokuwa **akisafiri** kwenda **Damasiki** … **nuru kubwa toka mbingu ilingaa kando yake**. Hapa ni mara ya kwanza iliyoandikwa kwamba neno hili lilitokea **saa sita azuhuri** na kutufahamisha **nuru** hii ilingaa hata kupita nuru ya jua wakati wa saa sita. Ukali wa **nuru** uliangusha mtesaji chini naye alisikia **sauti** toka mbingu **ikisema, "Saulo, Saulo, kwa sababu gani unanitesa?"** Akiuliza kama ilikuwa sauti ya nani, aliambiwa kwamba alikuwa **Yesu wa Nazareti** aliyekuwa akisema naye toka mbingu. Mnazareti huyu alikuwa amefufuka toka wafu na alitukuzwa mbinguni.

**22:9** Watu waliosafiri pamoja na Paulo **waliona nuru**, na walisikia **sauti bila kuweza kufahamu** maneno sauti iliyosema.

**22:10, 11** Nyuma ya kusikia peke

yake sauti ya Bwana wa uzima na utukufu, Paulo alijitoa mzima kwa roho, nafsi na mwili wake pia. Ulizo lake, **"Nitafanya nini, Bwana?"** linatufahamisha neno hili. Bwana Yesu alimwagiza **kwenda Damasiki. Ataambiwa pale** nini itampasa kufanya. Kungaa sana kwa **nuru ya utukufu** wa Kristo kulikuwa kumefanyiza Paulo mpofu, na **aliongozwa na mkono** wa mmoja wa watu waliosafiri pamoja naye na kufikishwa kwa mji.

**22:12** Kwa Damasiki **Anania** alimfikia. Paulo alisema kwa wasikiaji wake kwamba Anania **alikuwa mwenye kuogopa Mungu kwa kufuata sheria, aliyeshuhudiwa wema na Wayuda wote waliokaa kule. Ushuhuda** huu ulikuwa na faida sana kuhakikisha habari za wokovu wa Paulo.

**22:13** Anania akiita Paulo **"Ndugu Saulo,"** akamwagiza **kupata kuona**. Halafu Paulo **alimwona na macho** mara ya kwanza.

**22:14-16** Ndani ya mashairi 14-16 tunasoma mara ya kwanza maneno Anania aliyosema na Paulo,

> **"Mungu wa baba zetu amekwisha kukuchagua kujua mapenzi yake, na kuona Mwenye Haki, na kusikia sauti iliyotoka kinywa chake. Kwa maana utakuwa mshuhuda wake kwa watu wote, wa maneno yale uliyoona na kusikia. Basi sasa, unakawia nini? Simama ubatizwe, usafishe zambi zako, ukiitia jina la Bwana."**

Tuwaze juu ya maneno makubwa mengine ndani ya mashairi haya: Neno la kwanza Anania alilosema lilikuwa kwamba **Mungu wa baba zetu** aliongoza maneno yaliyotokea kwa njia ya Damasiki. Wayuda wakishindana na maneno haya yaliyotokea, walikuwa wakipigana na **Mungu.** Neno la pili ndilo hili: Anania alimwambia Paulo kwamba atakuwa **mshuhuda** wa Bwana kwa watu *wote.* Maneno haya yangalipasa kutayarisha makutano Wayuda kwa tangazo la Paulo kwamba alitumwa kwa Mataifa. Mwishoni, Paulo aliagizwa: **"Simama ubatizwe, usafishe zambi zako, ukiitia jina la Bwana."**

Wengine wametumika na shairi 16 kufundisha kwamba watu wanaweza kubatizwa kwa kupata wokovu. Labda shairi hili ni kwa Paulo tu kama Myuda aliyehitaji kujitenga na taifa lake waliokataa Kristo, kwa njia ya ubatizo (ona mafundisho juu ya Mdo. 2:38).

Njia nzuri kupita kutafsiri shairi hili ni: "Ukisimama, pata ubatizo, na pata kusafishwa kwa zambi zako kwa njia ya kuitia jina la Bwana kupata ondoleo la zambi." (Ona Yoeli 2:32; Mdo. 2:21; Rom. 10:13.)

**22:17-21** Mashairi haya yanatujulisha, mara ya kwanza, neno lililotokea karibu na mwisho wa mara ya kwanza Paulo **alipofikia Yerusalema** nyuma ya kuokolewa kwake. Wakati **alipokuwa akiomba hekaluni**, alikuwa katika **hali ya kuzimia** na alisikia Bwana akimwagiza **kutoka Yerusalema upesi**, kwa sababu watu **hawatapokea ushuhuda wake juu ya** Kristo. Ilikuwa nguvu kwa mtume kuamini kwamba watu wa taifa lake mwenyewe watakataa kumsikiliza. Wao wote walijua kwamba alikuwa Myuda mwenye bidii kabisa, na namna **alivyofunga** gerezani na kupiga wanafunzi wa Yesu, na kusaidia ndani ya uuaji wa **Stefano.** Lakini Bwana alimwagiza mara ya pili, **"Ondoka, nitakutuma mbali kwa watu wa Mataifa."**

**22:22, 23** Kufika saa hii watu walisikiliza Paulo vizuri, lakini masemo yake juu ya kwendea watu wa Mataifa na Habari Njema yaliamsha wivu na machukio kupita kipimo ndani ya roho zao, wakapaza sauti na kulalamika kwa Paulo kuuawa.

**22:24, 25** Wakati **mkubwa** alipo-

ona gazabu yao, alifikiri kwamba Paulo alikuwa ametenda kosa kubwa sana. Hakufahamu hotuba ya Paulo aliyesema na Kiaramaic, hivi alikusudi kuagiza Paulo apigwe kwa fimbo kumlazimisha kukiri kwa njia gani alikuwa amevunja sheria. Hivi **aliagiza** mfungwa wake **arudishwe kwa nyumba kubwa** na kufungwa na kamba kumtayarisha kupigwa fimbo. Wakati matayarisho haya yalipoendelea kwa kupigwa kwake, **Paulo** aliuliza akida polepole kama wana ruhusa **kupiga mtu aliye Mroma na asiyehukumiwa bado.** Hawakuwa na ruhusa hata kwa kufunga mwenyeji wa **Roma**! Kumpiga na **fimbo** kulikuwa zambi kubwa sana.

**22:26** **Akida alikwenda** mbio **kujulisha mkubwa akae na ange kwa neno** alilokusudi kutendea Paulo, kwa sababu alikuwa mwenyeji wa Roma.

**22:27,28** Habari hizi zilifikisha **mkubwa** karibu na **Paulo** mbio mbio**.** Aliulizana naye na kusikia kwamba alikuwa kweli mwenyeji wa **Roma.** Kwa wakati ule kulikuwa na njia tatu kwa mtu kugeuka mwenyeji wa Roma. 1. Mara nyingine mfalme wa Roma alifanyiza mtu mwenyeji wa Roma kama zawabu kwa utumishi wake kwa serikali. 2. Inawezekana kuwa **Mroma** kwa njia ya kuzaliwa. Ilikuwa hivi na **Paulo; alizaliwa** kwa Tarso, ndio mji huru katika ufalme wa Roma, na baba yake alikuwa mwenyeji wa Roma. 3. Mtu aliweza kununua **wenyeji** huu kwa **mali nyingi. Mkubwa wa askari** alikuwa amefanya hivi.

**22:29** Wakati ilipojulikana kwamba Paulo alikuwa mwenyeji wa **Roma**, agizo la kumpiga fimbo lilifutwa na watu wa serikali waliogopa.

**22:30** Basi mkubwa alitaka sana **kujua kwa sababu gani Paulo alishitakiwa na Wayuda**. Hata hivi alitaka kufanya maneno haya yote kwa utaratibu wa sheria. Hivi kesho yake nyuma ya makelele katika Yerusalema, aliagiza **Paulo** kuondoshwa gerezani na kufikishwa mbele ya **wakubwa wa makuhani na** Baraza.

**23:1, 2** Wakati **Paulo** aliposimama mbele ya wakubwa wa Baraza, alianza na kusema kwamba **aliishi kwa zamiri safi** kwa maisha yake mazima kufika saa ile. Masemo haya yalikasirisha **Anania**, ndiye kuhani mkubwa sana. Bila shaka kwa macho yake Paulo alikuwa mkufuru wa dini ya Wayuda, mhuni. Namna gani mtu aliyeacha dini ya Wayuda na kugeuka Mkristo aliweza kusema neno namna hii? Hivi kuhani mkubwa aliagiza mfungwa apigwe kwa kinywa chake. Halikuwa agizo la haki kwani hukumu ya Paulo lilianza sasa tu.

**23:3** **Paulo** aljibu Anania na kasirani kwamba **Mungu atampiga yeye** kwani alikuwa **ukuta uliopakaliwa makesi!** Kwa macho ya watu kuhani mkubwa alionekana kuwa mtu wa haki, lakini rohoni mwake alikuwa mwovu. Alitenda kama mwenye **kuhukumu** watu kupatana na sheria, lakini alikosea sheria wakati **alipoagiza Paulo kupigwa.**

**23:4** Watu waliokuwa pale walishitushwa sana wakati waliposikia kemeo kali la mtume. Hakufahamu kwamba alikuwa akisema na **kuhani mkubwa?**

**23:5** Hatujui kwa sababu gani **Paulo** hakufahamu kwamba Anania **alikuwa kuhani mkubwa.** Wakubwa wa Baraza walikuwa wamekusanyika kwa haraka, na labda Anania hakuvaa mavazi yake ya ukuhani. Labda hakuketi kwa kiti cha **kuhani mkubwa**. Labda uzaifu wa macho ya Paulo ulimwangusha. Hakusema **na kusudi** maneno haya **mabaya** kwa yule aliyewekwa kuwa **mtawala**. Aliomba mbio kusamehewa kwa masemo yake makali, akitaja Kutoka 22:28, **"Usiseme mabaya juu ya mkubwa wa watu wako."**

**23:6** Ni kama Paulo alifahamu kwa njia ya masemo katika Baraza kwamba

**Wafarisayo** na **Wasadukayo** hawakupatana vizuri, hivi alifikiri vizuri aongeze magawanyiko yao kwa njia ya kutangaza kwamba yeye ni **Mfarisayo** aliyekuwa akihukumiwa kwa sababu ya tumaini la **ufufuko wa wafu**. Wasadukayo hawakuamini kwamba kuna **ufufuko**, wala roho na malaika, lakini **Wafarisayo** waliamini kuna ufufuko, na malaika na roho (ona 23:8).

Walimu wengine wanafikiri haikuwa vizuri kwa Paulo kujaribu kujisaidia mwenyewe kwa njia ya kutenga wasikiaji wake kwa njia hii.

**23:7-9** Masemo yake yalianza **ugomvi katikati ya Wafarisayo na Wasadukayo, na makutano waligawanyika.** Wengine wa waandishi wa upande wa Wafarisayo walisimamia Paulo wakisema hana kosa, na kwamba si neno **kama roho au malaika alisema naye.**

**23:10** Magomvi ya Wafarisayo na Wasadukayo yalizidi kuongezeka hata **mkubwa** aliagiza **askari** kuondosha Paulo toka chumba cha Baraza na kumrudisha kwa **nyumba ya askari.**

**23:11 Usiku ule Bwana** yeye mwenyewe alitokea **Paulo** gerezani, akasema naye, **"Tia moyo, kwa sababu sawasawa ulivyonishuhudia katika Yerusalema, hivyo imekupasa kunishuhudia vilevile katika Roma."** Ona ya kwamba kwa wakati ule watu wengine waliposhitaki Paulo juu ya maneno aliyofanya, **Bwana** yeye mwenyewe alimsifu kwa sababu alimshuhudia na uaminifu **katika Yerusalema.** Mwokozi hakumkemea juu ya neno hata moja. Alimsifu tu. Kazi ya Paulo haiyakwisha bado. Alitumikia Bwana na uaminifu **katika Yerusalema**, na **atashuhudia Kristo vivyo hivyo katika Roma.**

**23:12-15 Kesho yake Wayuda wengine walifungana pamoja** na kupatana kuua mtume Paulo. **Zaidi ya watu makumi ine walijifunga kwa kiapo** ya kwamba **hawatakula vyakula kufika** wakati watakapokwisha kumwua**.** Hili lilikuwa shauri lao: Watafikia **wakubwa wa makuhani na wazee,** na kusema nao vizuri waombe watu wa Baraza kukutana tena kusudi wasikie habari za Paulo vizuri zaidi. Halafu watu wa baraza waombe **mkubwa wa askari** kuleta Paulo kutokea mbele yao tena. Lakini wale wauaji **makumi ine** watajificha njiani inayotoka nyumba ya askari na kufikia nyumba ya Baraza. Wakati **Paulo** atakapofika karibu walikusudi kumrukia na **kumwua.**

**23:16-19** Kwa maongozi ya Mungu, mjomba wa Paulo alisikia habari za shauri lao na alijulisha **Paulo**. Paulo alifikiri ni halali kwaye kujaribu kujichunga kwa njia yo yote iliyo ya sheria na alijulisha **akida mmoja** habari hizi. Yule akida yeye mwenyewe alifikisha **kijana karibu na mkubwa.**

**23:20, 21** Mjomba wa Paulo alijulisha mkubwa habari zote za shauri la **Wayuda** na alimsihi asikubali wakati watakapoomba **Paulo** aletwe chini kwa Baraza.

**23:22** Wakati **mkubwa** alipokwisha kusikia habari aliruhusu **kijana** kwenda zake pamoja na agizo asimwambie mtu ye yote kwamba alikuwa amekutana naye kwa siri. Mkubwa alifahamu kwamba lazima atayarishe njia kwa haraka kuondosha mfungwa wake toka gazabu ya kuwaka ya Wayuda.

**23:23-25** Mkubwa aliita mbio **maakida wawili** na kutayarisha njia kwa **askari mia mbili, wapandaji farasi makumi saba, na wenye mikuki mia mbili kupeleka Paulo kwa Kaisaria.** Aliagiza waanze safari wakati wa giza – saa tatu ya **usiku.**

Mkubwa hakutuma hesabu kubwa hivi ya askari kwa sababu ya heshima yake kwa mjumbe huyu mwaminifu wa Kristo, lakini kwa sababu alitaka wakubwa wake Waroma kufahamu kwamba alikuwa mwongozi mzuri. Kama

Wayuda wangaliweza kuua Paulo, mwenyeji Mroma, mkubwa angalihukumiwa kwa sababu hakufanya kazi yake na uaminifu.

**23:26-28** Ndani ya barua yake kwa **Feliki**, **mtawala** Mroma kwa Kaisaria, mwandishi alijiita **Claudio Lusia.** Kusudi la barua lilikuwa kueleza kwa sababu gani alituma Paulo. Ni neno la kuchekesha kuona **Lusia** akijionyesha kuwa mhodari na mwenye kusimamia haki. Labda aliogopa sana ya kwamba **Feliki** atasikia kwamba Claudio Lusia alikuwa amefunga **Mroma** asiyehukumiwa bado. Paulo hakujulisha Feliki habari hizi.

**23:29, 30** Mkubwa alionyesha ya kwamba Paulo hakufanya neno baya **linalofaa mauti au kufungwa.** Machafuko ya Wayuda yalikuwa **mabishano** juu ya sheria yao. Wakati Claudio alipopata habari za shauri baya la Wayuda juu ya Paulo, alifikiri ni vema atume Paulo kwa Kaisaria ili **wenye kumshitaki** waende pale vilevile, na kupasha habari hizi zote mbele ya Feliki.

**23:31-35** Kwa safari yao kwenda Kaisaria walisimama kwa muda fupi kwa **Antipatiri**, mji ulio karibu km. 64 toka Yerusalema na km. 40 km toka **Kaisaria**. Wakati walipofika pale, hatari haikuwa tena kwamba Wayuda walijificha njiani kuwaangukia, hivi **askari** walirudia Yerusalema, na **wapandaji farasi** tu walifikisha **Paulo** karibu na Feliki kwa Kaisaria pamoja na **barua** ya Lusia. Wakati Feliki alipofahamu kwamba Paulo alikuwa kweli mwenyeji wa Roma, aliahidi kusikiliza **mashitaki ya Wayuda** wakati **watakapofika** toka Yerusalema. Kufika saa ile aliagiza **Paulo kulindwa katika nyumba ya Herode.**

Mtawala wa Waroma, ndiye Feliki, alikuwa mtumwa kwa ujana wake, lakini aligeuka mwongozi na mtu wa kuonekana katika ufalme wa Roma. Alikuwa mwovu kabisa. Wakati alipowekwa kuwa mtawala wa wilaya ya Yuda, alikuwa na wanawake watatu. Nyuma ya kuanza kazi yake ya mtawala alianza kupendana na Durusila, aliyekuwa mke wa Azizus, mfalme wa Emesa. Josephus, mwandishi wa historia, alisema Simoni, mchawi wa Kipuro alitengeneza maneno ya ndoa hii.

Feliki alikuwa mtawala mkali aliyeagiza kuhani mkubwa, jina lake Yonatana, kuuawa kwa sababu alikuwa amemchambua kwa sababu ya utawala wake mbaya.

Ilipasa Paulo kusimama mbele ya Feliki huyu.

**24:1 Siku tano** nyuma ya kuondoka kwa **Paulo** kwa Yerusalema na kwenda Kaisaria, **Anania, kuhani mkubwa** alifikia Kaisaria pamoja na wazee wengine wa Baraza. Walilipa Mroma, jina lake Tertulo, kuwasimamia mbele ya Feliki na kushitaki **Paulo.**

**24:2-4 Tertulo** alianza masemo yake na kubembeleza mtawala na sifa mno kusudi aweze kumsikiliza vizuri. Ndiyo, mengine ya maneno aliyosema yalikuwa kweli. **Feliki** alikuwa ametawala vizuri na kuzuiza fitina na maasi.

**24:5-8** Tertulo aliendelea kushitaki Paulo juu ya maneno mane. Alisema kwamba Paulo:

1) alikuwa **mtu wa matata;**
2) alikuwa **mwenye kuanza** fitina katikati ya **Wayuda wote;**
3) alikuwa **mwongozi wa dini ya Wanazareti;**
4) **alijaribu kuchafusha hekalu**.

**24:9 Wayuda** walikubali maneno Tertulo aliyosema na kusema ni kweli.

**24:10** Halafu **mtawala** alimpa **Paulo** ruhusa kusema kwa njia ya kumpungia mkono, na Paulo alianza kujisimamia. Alianza kwa njia ya kusema alikuwa na asante kwani alipewa ruhusa kusimama mbele ya mtu aliyekuwa mwamuzi wa Wayuda kwa **miaka mingi**, na kujuana

na desturi zao vizuri. Masemo haya hayakuwa mabembelezi, lakini njia ya adabu kusema neno lililo kweli.

Halafu mtume aliendelea kujibu mashitaki haya yote, moja nyuma ya lingine.

**24:11** Juu ya kuwa mtu wa matata na mwenye kuanza fitina, alisema **siku kumi na mbili** zilipita tangu alipofikia **Yerusalema** kwa **kuabudu**, si kwa kuleta matata.

**24:12, 13** Aliendelea na kubisha kwamba kwa saa yo yote alisukuma watu kufanya fujo, au **hekaluni, … ndani ya masunagogi au mjini.** Hakuna mtu aliyeweza kubisha kwamba alisema kweli.

**24:14-17** Paulo hakubisha shitaki lao la tatu, kwamba yeye ni mwongozi wa **dini** wa Wanazareti. Alisema kwa Njia ile wanayoita dini alitumikia **Mungu** wa Wayuda, **akiamini maneno yote yanayoandikwa ndani ya Agano la Kale.** Pamoja na Wayuda wa kweli wote, zaidi Wafarisayo, aliamini kwamba **utakuwa na ufufuko wa wafu, wenye haki na wasio haki pia.** Kwa sababu **hii** alizobelea kuwa na zamiri safi pasipo kosa mbele ya Mungu, na mbele ya watu siku zote. Hakufikia Yerusalema kuanza fitina, lakini **kuleta sadaka na matoleo** kwa Wayuda. Alikuwa akisema juu ya zawadi makanisa kwa Makedonia na Akaya walizotuma kusaidia Wakristo Waebrania katika Yerusalema waliokuwa na mahitaji.

**24:18, 19** Juu ya shitaki la ine, ya kwamba alikuwa amechafua **hekalu**, Paulo alisema alikuwa akileta matoleo kwa **hekalu** kwa kutimiza kiapo cha Wayuda. Pale **Wayuda wengine toka Asia** walipomwona na kumshitaki juu ya kuleta watu wa mataifa wasiosafishwa **hekaluni.** Neno hili halikuwa kweli. Paulo alikuwa peke yake kwa wakati ule, na alikuwa **amesafishwa** kwa maneno ya dini. Ingalipasa **Wayuda hawa toka Asia** ambao walimshitaki kufikia Kaisaria na mashitaki yao **kama walikuwa na neno** juu yake.

**24:20, 21** Halafu Paulo alisema na **Wayuda waliokuwa pale** wataje wazi matendo ya kuvunja sheria aliyohukumiwa kuwa na hatia wakati aliposimama mbele ya Baraza katika Yerusalema, lakini hawakuweza. Wangeweza kusema tu kwamba Paulo **alipaza sauti, "Kwa ajili ya ufufuko wa wafu ninahukumiwa mbele yenu leo."** Hivi mashitaki yao yalikuwa juu ya maneno yasiyovunja sheria.

**24:22** Habari hizi ziliamsha mashaka rohoni mwa **Feliki**. Maneno aliyojua juu ya imani ya Wakristo yalitosha kumfahamisha kwamba Paulo hakukosea sheria ya Waroma. Lakini kama akiachilia Paulo na kusema hana hatia, atakasirisha Wayuda sana. Ilikuwa faida kwa yeye mwenyewe kuwabembeleza. Hivi alisema hatahukumu mashitaki yao siku ile lakini atangojea kufika kwa **Lusia, mkubwa wa askari,** kwa Kaisaria. Lilikuwa njia kuchelewisha hukumu. Hatusomi kwamba **Lusia** alifika kweli kwa wakati wa nyuma.

**24:23** Hivi Feliki **aliagiza** akida ya kwamba **Paulo** alindwe, bila kumfunga kabisa, na kuruhusu **rafiki zake** kumfikia na **kumletea** vyakula na mavazi. Agizo hili linaonyesha kwamba Feliki hakufikiri **Paulo** alikuwa mwasi wa sheria ya Waroma.

**24:24, 25a Siku nyingine** nyuma ya hukumu hii mbele ya watu, **Feliki** na **mke wake Durusila** aliyekuwa Myuda walifikia Paulo peke yao kusikiliza **habari za imani katika Kristo Yesu**. Bila woga Paulo alifundisha mtawala huyu na mke wake, wazinifu, **juu ya haki, na kiasi, na hukumu itakayokuja.** Hawakutembea katika **haki** mbele ya watu au nyumbani mwao. Ndoa yao ovu ilionyesha kwamba hawakujuana na **kiasi.** Walihitaji maonyo haya juu ya **hukumu itakayokuja**

kwani bila kupata usamehe kwa zambi zao kwa njia ya damu ya Kristo, wataangamizwa katika ziwa la moto.

**24:25b,26** Ni kama maonyo ya Paulo yaligusa roho ya **Feliki** kupita ile ya Durusila, lakini hata kama **aliogopa**, hakuamini Mwokozi siku ile. Alichelewa na kusema, **"Kwenda zako kwa sasa, wakati ninapopata nafasi nitakuita tena."** Ni huzuni kwani hatusomi ndani ya Biblia kwamba **"alipata nafasi"** kamwe. Hata hivi Paulo alitoa ushuhuda kwa **Feliki** tena. Ndani ya miaka miwili iliyofuata, mtawala alimwita tena na tena wakati Paulo alipokuwa mfungwa kwa Kaisaria. Alitaraji rafiki za Paulo watamlipa mali (rushwa) ili aweze kuagiza Paulo kufunguliwa.

**24:27** Nyuma ya miaka miwili, **Porkio Festo alifuata Feliki** kwa kazi. **Feliki, akitaka kupendeza Wayuda,** aliacha Paulo katika kifungo kwa Kaisaria.

**25:1** Mfalme Nero alichagua Porkio **Festo** kuwa mtawala Mroma wa Yudea kwa 60 A.D. **Kaisaria** ulikuwa mji mkubwa wa serikali wa Suria, ndiyo wilaya ya Roma, na Yudea ilikuwa sehemu ya Suria. **Nyuma ya siku tatu** Festo **alipanda toka Kaisaria kwenda Yerusalema,** uliokuwa mji mkubwa kwa maneno ya dini wa inchi iliyotawaliwa naye.

**25:2,3** Miaka miwili ilikuwa imepita tangu **Paulo** alipofungwa kwa Kaisaria, lakini **Wayuda** hawakumsahau. Walikaa kumchukia na kutaka kumwua. Wakitaraji **kusaidiwa** na mtawala mpya, **kuhani mkubwa na wakubwa wa Wayuda** walijaza masikio yake na mashitaki **juu ya Paulo** na walimwomba atume Paulo kwa **Yerusalema** kwa kuhukumiwa na Baraza. Lakini kusudi lao lilikuwa **kumwua** kwa safari kwendea Yerusalema.

**25:4,5** Lakini bila shaka **Festo** alijulishwa habari za shauri lao la mbele kuua **Paulo**, na matengenezo yote ya mtawala katika Yerusalema kumwondosha kule na kumfikisha kwa Kaisaria. Hivi hakukubali kutuma **Paulo** kwa Yerusalema, lakini aliruhusu Wayuda kufikia **Kaisaria** kumshitaki.

**25:6-8** Nyuma ya kushinda **zaidi ya siku kumi** katika Yerusalema, Festo alirudia **Kaisaria,** na **kesho yake** aliketi katika kiti cha hukumu. Wayuda walifikia Kaisaria kwa haraka vilevile, wakaleta **mashitaki mengi na mazito juu ya Paulo,** lakini hawakuweza **kuhakikisha** kweli yao. Paulo alifahamu kwamba mashitaki yao yalikuwa zaifu, akasema tu kwamba hakukosa neno **juu ya sheria ya Wayuda, wala juu ya hekalu, wala juu ya Kaisari**.

**25:9-11** Ni kama kwa saa ndogo **Festo** alikuwa tayari kukubali neno **Wayuda** waliloomba, na kutuma **Paulo kwa Yerusalema** ahukumiwe pale mbele ya Baraza, lakini si pasipo ruhusa ya mfungwa. Paulo alifahamu kwamba akikubali kwenda, atauawa njiani. Hivi alikataa akisema Kaisaria ndipo pahali ilipofaa kwa hukumu. Kama **alikosea** ufalme wa Roma, hakukataa kufa. Lakini kama asipokuwa na hatia, kwa sababu gani atatolewa kwa **Wayuda**? Akiwa mwenyeji wa Roma, alijibu, **"Ninataka kuhukumiwa na Kaisari."**

Ilikuwa vizuri kwa **Paulo** kuomba kuhukumiwa na **Kaisari**? Au ingalimpasa kuweka neno hili zima mkononi mwa Mungu bila kutegemea haki yake ya Mroma, ndilo neno la dunia? Hatujui kama alianguka wakati alipofanya hivi. Tunajua tu kwamba **kuomba Kaisari** kumhukumu kulimzuiza asifunguliwe kwa wakati ule, na kama asingaliomba kuhukumia na Kaisari, angalifikia Roma kwa njia nyingine.

**25:12** Nyuma ya **kusemezana** kidogo na watu wa Baraza juu ya utaratibu

wa sheria, **Festo** alisema na Paulo, labda na sauti ya kukasirika kidogo, **"Unataka kuhukumiwa na Kaisari, basi, utakwenda kwa Kaisari."**

**25:13** Nyuma ya kupita kwa siku nyingine, Mfalme Herode **Agripa 2** pamoja na ndugu yake mke Berenike walifika kutakia Festo heri kwa kazi yake mpya kwa Kaisaria. Agripa alikuwa mwana wa Herode Agripa 1, aliyeua Yakobo na kufunga Petro (Matendo 12). Ndugu yake mke alikuwa mwanamke wa kuonekana vizuri sana. Waandishi wengine wa historia waliandika habari mbaya juu ya namna alivyokaa pamoja na ndugu mume wake, lakini hakuna habari namna hii ndani ya Agano Jipya.

**25:14-16** Mfalme Agripa na Berenike walishinda siku nyingi kidogo kwa Kaisaria. Basi **Festo** alifikiri ni njema kwaye kumwambia Agripa habari ambazo zilimsumbusha juu ya mfungwa mmoja, jina lake Paulo. Kwanza alipasha namna **Wayuda** walitaka bila adabu kwa Paulo kuhukumiwa bila kuweza kujisimamia mwenyewe. Basi Festo, akijionyesha kuwa mwenye kusimamia sheria, alisema sharti mfungwa aweze kuonekana na washitaki wake **uso kwa uso** na kujisimamia mwenyewe mbele yao.

**25:17-19** Siku ya hukumu ya maneno haya, Festo alifahamu kwamba mfungwa huyu hakutenda neno baya juu ya ufalme. Wayuda walikuwa na **"maulizo juu yake katika dini yao wenyewe, na juu ya habari za mtu mmoja, Yesu, aliyekuwa amekufa, naye Paulo alisema kwamba yeye ni hai."**

**25:20-22** Halafu Festo alipasha kwamba aliuliza **Paulo** juu ya **kwenda Yerusalema** kwa kuhukumiwa, lakini Paulo aliomba kuhukumiwa na **Augusto** (Augusto hapa ni jina la heshima kwa Kaisari). Halafu Festo alifazaika kama atamtuma kwa Roma na shitaki gani. **Agripa** alikuwa Myuda na alijuana na maneno ya dini ya Wayuda, hivi Festo alitaraji labda atamsaidia kuandika shitaki lililofaa.

**25:23** **Kesho yake** kusanyiko lilitayarishwa, na **Agripa na Berenike** walikuja na **mapambo mengi**. **Maakida na watu wakubwa wa mji** walikuwa pamoja nao**.** Kisha **Paulo aliletwa.**

**25:24-27** Halafu **Festo** alipasha tena habari za **namna Wayuda** waliomba tena na tena Paulo auawe, na ya kwamba **Festo** hakuona kosa ndani ya mwenendo wa Paulo **lililostahili kufa,** na kwamba Paulo aliomba kuhukumiwa na Kaisari. Kwa sababu ya ombi hili la Paulo, ilikuwa lazima kwa Festo kumtuma, lakini hakuwa na shitaki kabisa aliloweza kutuma pamoja naye. Hivi Festo alisema wazi kwamba alitaraji **Agripa** ataweza kumsaidia ndani ya neno hili. **Kwa sababu ni neno pasipo maana kutuma mfungwa, pasipo kuonyesha mashitaki yaliyo juu yake.**

**26:1-3** Kwa maneno ya roho tunaweza kuhurumia **Agripa,** lakini mtume Paulo, mwenye imani, hakuacha mambo magumu kumshinda.

Wakati **Agripa** alipompa ruhusa, **Paulo alinyolosha mkono wake na** alianza kupasha habari za maisha yake kama Mkristo. Kwanza alileta asante kwa sababu alipewa ruhusa kujisimamia mbele ya mtu aliyekuwa Myuda na kujuana na **desturi na maulizo** katikati ya Wayuda. Hakusema hivi kubembeleza Agripa, lakini kwa kuonyesha adabu na kwa sababu ilikuwa kweli.

**26:4, 5** Kwa ujana wake mtume alikuwa mfano mzuri wa mwenye kutii na kufuata sheria zote za Wayuda, na alikuwa **Mfarisayo aliyefuata desturi za dini yao**. Wayuda walijua neno hili na wangaliweza **kulishuhudia kama wangalitaka.**

**26:6** Halafu **sasa** alikuwa akihukumiwa kwa kosa hili tu, ndilo kosa la kushikamana na **tumaini la ahadi**

**Mungu** aliyotoa kwa **baba** Wayuda katika Agano la Kale. Ni kama mawazo ya Paulo yalifuatana hivi: Ndani ya Agano la Kale Mungu alifanya maagano na viongozi vya Israeli, kama Abrahamu, Isaka, Yakobo, Daudi na Solomono. Agano kubwa zaidi lilikuwa juu ya ahadi ya Masiya, kuja kwake kuokoa taifa la Israeli na kutawala dunia. Baba wazee wa Agano la Kale walikufa bila kuona kutimizwa kwa ahadi hii. Halafu Mungu hatatimiza maagano haya? Atayatimiza kabisa! Lakini ataweza kufanya hivi namna gani wakati baba wazee hawa walipokwisha kufa? Jibu kwa ulizo hili ni, "Kwa njia ya kuwafufua toka wafu." Hivi kwa njia hii iliyokuwa wazi kabisa mtume alifunganisha ahadi ambazo watakatifu wa Agano la Kale walipewa na ufufuko wa wafu.

**26:7** Mtume alipasha juu ya **makabila kumi na mawili** ya Israeli **wakitumikia Mungu na bidii sana**, wakitumaini kuona kutimia kwa ahadi hii. Ona ya kwamba Paulo alitaja **makabila kumi na mawili.** Hili ni neno kubwa kwa sababu kwa wakati wa sasa walimu wengine wanafundisha kwamba kumi ya makabila haya "yamepotea" tangu wakati wa uhamisho. Hata kama makabila haya yalisambazwa katikati ya Mataifa, mtume Paulo aliwaona kama taifa moja, mbali na mataifa yote mengine, **wakitumikia Mungu** na kutazamiwa kutimia kwa ahadi ya kuja kwa Mwokozi.

**26:8** Hivi zambi ya Paulo ilikuwa hii: Aliamini **kwamba Mungu** atatimiza ahadi aliyotolea baba wazee kwa njia ya kuwafufua **toka wafu**. Paulo aliuliza Agripa na wote waliokuwa pamoja naye kwa sababu gani itawashinda kuamini neno hili?

**26:9-11** Halafu Paulo aliendelea na habari za maisha yake. Alipasha namna gani, na ukali sana, alipiga vita na wafuata wa Kristo. Alishindana na **jina la Yesu wa Nazareti. Wakubwa wa makuhani** walimpa amri kufunga **wengi** wa Wakristo katika Yerusalema. Hakuwasimamia hata kidogo wakati waliposimama mbele ya Baraza kuhukumiwa. Aliongoza azabu ya wote ambao alikuta ndani ya **masunagogi**, na kujaribu sana kuwalazimisha kukana Bwana wao. (Wakati tunaposoma **"nikawashurutisha kukufuru,"** si kusema kwamba walikufuru kweli, lakini ya kwamba Paulo *alijaribu kuwasukuma* kufanya hivi.) Hakufanya hivi katika Yerusalema na Yudea tu, lakini ndani ya **miji ya inchi nyingine vile vile.**

**26:12-14** Halafu neno lililotokea kwa moja ya safari zake kwa miji ile mingine liligeuza maisha yake kabisa. Alikuwa akisafiri kwenda Damasiki akibeba barua za serikali zikimruhusu kufunga Wakristo na kuwarudisha kwa Yerusalema kuazibiwa. **Kwa azuhuri** (saa sita) alishindwa na ono la utukufu. **Nuru kubwa kupita kungaa kwa jua ilimwangazia toka mbingu**. **Nyuma ya kuanguka chini**, alisikia **sauti** ikimwuliza: **"Saulo! Saulo! kwa sababu gani unanitesa?"** Halafu **sauti** iliongeza maneno mengine, **"Ni nguvu kwako kupiga miiba kwa miguu." Miiba** ile ilikuwa fimbo zenye ncha za chuma zilizotumiwa kusukuma nyama kwenda mbele. Paulo alikuwa akipigana na damiri yake mwenyewe, na zaidi na sauti ya Roho Mtakatifu. Hakuweza kusahau kamwe roho ya utulivu na neema za Stefano saa ya kufa kwake. Alikuwa **amepigana** na Mungu mwenyewe.

**26:15** Paulo aliuliza, **"Wewe ni nani, Bwana?"** Sauti ilijibu, **"Mimi ni Yesu, ambaye unatesa."** *Yesu?* Neno hili liliwezekana namna gani? Yesu hakusulibishwa na kuzikwa? Na wanafunzi wake walikuwa wameiba maiti yake na kuizika kwa pahali pasipojulikana? Basi namna gani Yesu aliweza kusema naye sasa? Paulo alifahamu neno hili mbio. Yesu alizikwa kweli,

lakini *alifufuliwa* toka wafu! Alikuwa amerudia mbingu, na alisema na Paulo toka pale. Wakati Paulo alipokuwa akitesa Wakristo, alikuwa **akitesa** Bwana wao. Na kwa njia ya **kumtesa** yeye, **alitesa** Masiya ya Israeli, ndiye Mwana wa Mungu mwenyewe.

**26:16** Halafu Paulo alijumlisha maagizo aliyopokea toka Bwana Yesu Kristo aliyekwisha kufufuliwa. Bwana alimwagiza **kuamka na kusimama kwa miguu yake.** Alipewa ono hili la Kristo katika utukufu kwa sababu alikuwa amewekwa kuwa mtumishi wa Bwana, **na mshuhuda** wa maneno yote **aliyoona** siku ile na wa kweli kubwa zote za imani ya Wakristo atakazojulishwa kwa wakati wa kuja.

**26:17** Alipewa ahadi vilevile ya kwamba ataokolewa **toka Wayuda na Mataifa** kufika wakati kazi yake itakapokwisha.

**26:18** Paulo atatumwa zaidi kwa Mataifa **kufungua macho yao, wageuke toka giza waingie nuru, watoke katika nguvu za Shetani na kufikia Mungu.** Kwa njia ya kuamini Bwana Yesu, **watapokea usamehe wa zambi na uriti pamoja nao waliotakaswa.** Mwalimu mmoja, jina lake H. K. Downie alionyesha kwamba shairi 18 ni jumlisho zuri la Habari Njema:

1. Inapunguza giza.
2. Inaleta uhuru toka uwezo wa Shetani.
3. Inasamehe zambi.
4. Inarudisha uriti uliopotezwa.

**26:19-23** Halafu Paulo alielezea **Agripa** kwamba nyuma ya kuamriwa hivi na Bwana **hakuasi maono ya mbinguni. Kwa Damasiki na kwa Yerusalema, na katika inchi yote ya Yudea, na kwa Mataifa** alihubiri ya kwamba **inapasa watu kutubu na kugeuka kwa Mungu,** na kufanya **matendo** yanayohakikisha kwamba walikuwa **wametubu kweli.** Alikuwa akifanya hivi **wakati Wayuda walipomkamata hekaluni na kujaribu kumwua.** Lakini **Mungu** alikuwa amemlinda, naye alikaa kutoa ushuhuda kwa watu wote aliokutana nao, akihubiri habari **manabii na Musa** walizohubiri katika Agano la Kale. Zilikuwa habari kwamba Masiya **atateswa**, **ya kwamba atakuwa wa kwanza atakayefufuliwa toka wafu,** ya kwamba **ataonyesha nuru kwa Wayuda na kwa Mataifa vilevile.**

**26:24-26** **Festo** alikuwa Mtaifa, hivi tunafikiri hakufahamu masemo yote ya Paulo. Ilimshinda kufahamu kabisa mtu aliyejazwa na Roho Mtakatifu, hivi alishitaki **Paulo** na sauti kubwa kusema alikuwa na wazimu kwa sababu ya **kujifunza maneno mengi**. Paulo alimjibu na upole, bila kukasirika hata kidogo, kwamba neno hili halikuwa kweli, na ya kwamba **masemo** yake yalikuwa masemo ya **kweli na akili**. Aliongeza kusema ya kuwa bila shaka **mfalme** alijua kwamba yalikuwa masemo ya kweli na ya akili. Mwenendo na ushuhuda wa Paulo hazikuwa kwa siri. Wayuda walijua maneno haya yote, na bila shaka habari hizi zilifikia Agripa vilevile.

**26:27** Halafu Paulo aliuliza mfalme, **"Mfalme Agripa, unaamini manabii?"** Aliendelea kujibu ulizo lake yeye mwenyewe, **"Ninajua ya kama unaamini."** Maana ya masemo yake yalikuwa wazi. Paulo alisema yeye mwenyewe aliamini maneno yote manabii yaliyosema katika Agano la Kale, akaendelea kusema na mfalme, "Nawe unayaamini vilevile, sivyo, **Agripa**? Basi namna gani Wayuda wanaweza kunishitaki mbele yako juu ya kosa linalostahili kufa? Au namna gani unaweza kunihukumu kwa sababu ninaamini maneno ambayo unaamini wewe mwenyewe?"

**26:28** **Agripa** akifahamu kwamba Paulo alisema kweli, akajibu, **"Kwa maneno machache unazani kunishawishi kuwa Mkristo."** Maana ya jibu lake ni kwamba alikuwa karibu kuamini

Kristo? Ni kama jibu la Paulo ndani ya shairi 29 linaonyesha kwamba ilikuwa hivi. Lakini walimu wengine wanafikiri **Agripa** alisema hivi na kuzihaki, “Unafikiri kwamba na maneno machache unaweza kunisukuma kugeuka Mkristo?”

**26:29** Hatujui kama Agripa alisema na roho ya kweli au na kuzarau, lakini **Paulo** hakujibu na kuzarau hata kidogo. Alitaka sana sana kwa **wote** waliokuwa pale kuweza kushiriki ndani ya furaha na baraka za Wakristo, na kwa wote **kugeuka** kuwa kama yeye **ila** kwa maneno ya **vifungo** vyake.

**26:30-32** Halafu **mfalme, mtawala, Berenike,** na wakubwa wengine walitoka chumbani kusemezana peke yao. Iliwapasa wote kukubali kwamba Paulo **hakufanya neno lililostahili azabu ya mauti wala kufungwa**. Labda **Agripa alisema na Festo** na huzuni **ya kwamba Paulo angaliweza kufunguliwa kama asingaliomba kuhukumiwa na Kaisari**.

Tunafazaika kwa sababu gani haikuwezekana kugeuza ombi hili la Paulo kuhukumiwa **na Kaisari**. Tunajua tu kwamba lilikuwa kusudi la Mungu kwa mtume kwa Mataifa kwenda kwa Roma kuhukumiwa na mfalme (Mdo. 23:11), na kupata neno alilotaka, ndilo kufananishwa na kufa kwa Bwana wake.

### I. Safari ya Paulo kwenda Roma; kuharibika kwa merikebu (27:1 – 28:16)

Ndani ya sura 27 tunapata habari za ajabu za safari ya mtume toka Kaisaria kufika Melita, kwa njia ya kwenda Roma.

**27:1** Kwa safari hii **Paulo** aliwekwa kwa mikono ya **akida** aliyeitwa **Yulio.** Alikuwa mtu wa **kikosi cha Augusto,** sehemu yenye heshima ya jeshi la Waroma. Kama maakida yote ambao tunasoma habari zao katika Agano Jipya, alikuwa mtu wa haki, mwema, na mwenye kukumbuka mahitaji ya watu wengine.

**27:2** Kulikuwa na wafungwa wengine vilevile ndani ya merikebu, waliokuwa wakipelekwa kwa Roma kuhukumiwa. **Aristarko** na Luka waliosafiri pamoja na Paulo mbele walikuwa pamoja naye sasa vilevile. **Merikebu** yao ilikuwa ya **Adaramiti**, ndio mji kwa pwani ya Misia kwa upande wa kaskazini-mangaribi wa Asia Ndogo. Lilikuwa shauri kwa merikebu **kusafir**i kwa kaskazini na mangaribi, na kusimama njiani kwa bandari nyingine kwa **pwani** ya wilaya ya mangaribi ya Asia Ndogo.

**27:3** Merikebu ilisafiri kwenda kwa kaskazini, karibu ya pwani ya Palestina, kufikia **Sidona,** km. 112 toka Kaisaria. Akida **Yulio** alitendea **Paulo mema** na **kumruhusu** kuondokea merikebu na **kuonana na rafiki zake na kutunzwa nao.**

**27:4, 5** Toka Sidona walisafiri kwa upande wa kuume wa kisanga **Kipuro,** kilichosaidia kuepuka kuvuma kwa upepo. Nyuma yake, **hata kama walizuizwa na upepo**, walisafiri kwa upande wa mangaribi, **wakapita Kilikia na Pamfulia** na kufikia **Mira,** ndio **mji wa** bandari **wa Likia.**

**27:6** Kwa Mira **akida** alihamisha wafungwa wake kwa **merikebu** nyingine, kwa sababu merikebu yao ya mbele haitawafikisha kwa **Italia,** lakini ilisafiri kwa njia nyingine na kurudia pahali ilipoanza safari yake.

**Merikebu** hii ya pili ilitoka Alesanduria, mji kwa pwani ya kaskazini ya Afrika, na ilibeba watu 276 na mzigo wa ngano, ikasafiri kwenda **Italia.**

**27:7, 8** Walisafiri **na matata** na polepole **kwa siku nyingi** mbele ya kufikia Kinido, bandari kwa pembe ya kusini-mangaribi kabisa ya Asia Ndogo. **Upepo** ulishindana nao, hivi walisafiri kwa kusini karibu na upande wa mashariki wa kisanga cha **Krete.** Wakishindana na upepo, walifika kwa pahali palipoitwa **Bandari Nzuri karibu**

**na mji wa Lasea,** kwa pwani ya kusini ya Krete.

**27:9, 10** Wakati **mrefu** ulikwisha kupita sasa kwa sababu ya ugumu wa safari hii. Wakati wa baridi ulikaribia, saa safari nyingine ingekuwa na **hatari** zaidi. Ni kama ilikuwa karibu na mwisho wa mwezi wa tisa au mwanzo wa mwezi wa kumi, kwa sababu **siku za kufunga** (siku kubwa ya upatanisho) **zilikuwa zimekwisha kupita**. **Paulo** alionya wabaharia juu ya hatari ya kuendelea na safari hii, na ya kwamba watapoteza **merikebu na vitu ilivyobeba,** na labda hata maisha ya wengine wa watu.

**27:11,12** Lakini **kapiteni na mwenye merikebu** walitaka kuendelea na safari. **Akida** na zaidi ya watu wengine walikubali shauri lao. Walifikiri **bandari kwa Foinike ingekuwa pahali pazuri** kupita kwa watu kushinda **wakati wa baridi**. **Foinike** palikuwa karibu km 65 toka Bandari Nzuri, na **bandari** yake ilitazama kwa kusini-mangaribi na kaskazini-mangaribi wa **Krete**.

**27:13-17 Wakati upepo wa kusini ulipoanza kuvuma kidogo**, wabaharia walifikiri wataweza kufikia Foinike. Waliondosha nanga na kusafiri kwenda mangaribi, karibu na pwani. Halafu upepo wa nguvu toka kaskazini-mashariki ulioitwa **Eurakilo** ulipiga merikebu toka pwani. Wabaharia hawakuweza kuongoza **merikebu** tena vizuri na iliwapasa kuacha upepo ule mkubwa kuitembeza. Upepo uliwasukuma kwa upande wa kusini-mangaribi kwa **kisanga kidogo jina lake Kauda** karibu km. 30-50 toka **Krete.** Wakati walipofikia upande wa **kisanga** usiopigwa na upepo, waliweza kwa matata kufunga **mashua** ambayo walikuwa wakikokota. Mwishoni waliweza kuipandisha **juu ya merikebu.** Kisha walifunga **merikebu** kwa njia ya kupitisha **kamba** chini yake kusudi isivunjwe na mawimbi makubwa ya bahari. Waliogopa kwamba watasukumwa kwa kusini na kukwama kwa mchanga wa **Sirti,** pahali maji yalipokuwa nusu karibu na pwani ya Afrika. Kuepuka hatari hii **walishusha matanga, na hivi walichukuliwa** na mawimbi.

**27:18, 19** Nyuma ya kutembezwa bila huruma na uwezo wa tufani, walianza kutupa mizigo baharini. Bila shaka maji mengi yalikuwa yameingia **merikebu**, na ilikuwa lazima kupunguza mizigo ndani ya merikebu kuizuiza isizame.

**27:20 Kwa siku nyingi** merikebu ilisukasuka na wasafiri hawakuweza kuona **jua** wala **nyota,** hivi hawakuweza kutambua pahali walipokuwa. Mwishoni **tumaini** lao kwamba wataweza kupona **ilikwisha pia**.

**27:21-26** Njaa iliongeza taabu yao. Siku nyingi zilikuwa zimepita tangu watu wale walipokula vyakula. Bila shaka walishinda na kazi ya kuondosha maji toka merikebu. Labda njia ya kupiga chakula haikuwa, na walikosa hamu ya kula kwa sababu ya ugonjwa, woga, na kukata tamaa. Walikuwa na vyakula, lakini walikosa hamu kuvikula.

**Halafu Paulo alisimama katikati yao** na habari za kuwasha tumaini lao. Kwanza aliwakumbusha na upole kwamba **isingaliwapasa kutoka Krete.** Kisha aliwajulisha ya kwamba hata **merikebu** yao itaharibika, wao wenyewe **hawatakufa**. Alijua neno hili namna gani? **Malaika** ya Mungu alikuwa ametokea kwake **usiku** na kumjulisha kwamba bila shaka atasimama **mbele ya Kaisari** kwa Roma. Na **Mungu** alikuwa amempa watu **wote waliosafiri pamoja naye,** maana wataponyeshwa vilevile. Basi watie moyo. **Paulo** aliamini kwamba itakuwa sawasawa alivyoambiwa hata kama merikebu yao itaharibiwa nao watatupwa juu ya **kisanga kimoja**.

**27:27-29** Siku kumi na ine zilikuwa zimepita tangu walipoondokea Bandari

Nzuri. Merikebu yao ilichukuliwa na mawimbi ya **bahari** iliyozunguka inchi za Yunani, Italia, na Afrika. **Karibu na saa sita ya usiku wabaharia walifikiri walikuwa wakikaribia inchi kavu;** labda walisikia mawimbi yakipiga pwani. Wakati walipopima urefu kwenda chini wa maji **walikuta ni mapimo makumi mbili** (karibu mètres 37), nyuma kidogo yalikuwa **kumi na tano** (karibu mètres 27). Kuzuiza merikebu isitupwe pahali pa miamba, **walitupa nanga ine toka upande wa nyuma wa merikebu,** wakangoja kufika kwa mchana pamoja na maombi.

**27:30-32 Wabaharia** waliogopa watakufa ndani ya maji, wakafanya shauri kujiponyesha ndani ya chombo kidogo. Walikuwa wakishusha **chombo** toka **merikebu**, wakitenda kama walivyotaka **kutupa nanga** mbele ya merikebu. **Paulo** alijulisha shauri lao **kwa akida,** akimwambia kama wabaharia wasipobaki ndani ya merikebu, watu wengine **hawataweza kuokolewa. Halafu askari walikata kamba** zilizofunga **chombo** na merikebu, **wakaacha chombo kuanguka ndani ya maji.** Hivi **wabaharia** walilazimishwa kujaribu kuokoa maisha yao wenyewe pamoja na maisha ya watu wengine waliokuwa ndani ya merikebu.

**27:33,34** Wakati tunaposoma mashairi haya tukumbuke maogopesho ya tufani baharini na ya kwamba Paulo hakuwa kapiteni ya merikebu hii, lakini msafiri mfungwa tu.

Saa ndogo mbele ya mapambazuko **Paulo alisihi** watu kula chakula, akiwakumbusha kwamba walikuwa wameshinda majuma mawili **bila kula vyakula**. Ilikuwa saa sasa kula chakula kama wakitaka kupona. Mtume aliwajulisha kwamba **hata unyole** wa mmoja katikati yao hautapotea.

**27:35** Kisha mbele yao wote alitwaa **mkate**, **akashukuru Mungu** mbele yao yote, akaanza kula. Mara nyingine tunaogopa kuomba mbele ya watu wengine, lakini mara nyingi maombi namna hii yanagusa roho za watu kupita mahubiri yetu.

**27:36, 37** Halafu watu **walipatishwa nguvu rohoni, wakakula vilevile**. Kulikuwa na **watu mia mbili na makumi saba na sita ndani ya merikebu ile.**

**27:38-41** Wakati walipomaliza kula **walipunguza mzigo wa merikebu** kwa njia ya **kutupa ngano baharini**. **Inch**i **kavu** ilikuwa karibu, **lakini iliwashinda kutambua** kama ilikuwa inchi gani. Wakiona hori kidogo yenye kivuko, walifanya shauri kujaribu kuingiza **merikebu** kule. **Wakatupa nanga** mbali na **kuziacha baharini**, wakalegeza kamba za sukani, wakanyanyua **tanga la mbele** lipate upepo, wakakwendea kivuko. Wakifikia **pahali bahari mbili zilipokutana**, walikwamisha merikebu kwa udongo hata **kipande cha mbele** kilikwama kabisa, lakini **kipande chake cha nyuma** kilianza kuvunjika kwa sababu ya **nguvu ya mawimbi**.

**27:42-44 Askari walikusudi kuua wafungwa** ili wasipate njia **kukimbia,** lakini **akida** hakuwaruhusu kufanya hivi **kwa sababu alitaka kuponyesha Paulo.** Aliagiza wote **walioweza kuogelea** kujaribu kufikia pwani. **Watu wengine,** wakishikamana na **mbao na vitu vingine** vya merikebu, walifikia pwani wakichukuliwa na maji. Kwa njia hii wao wote **walifikia inchi kavu salama.**

**28:1, 2** Wakati watu wa merikebu walipofikia pwani walifahamu kwamba walikuwa kwa **kisanga** kilichoitwa **Melita**. Wengine wa **wenyeji** wa kisanga waliona mavunjiko ya merikebu na wasafiri wakijaribu kufikia inchi kavu. Waliwatendea mema kwa njia ya kuwasha **moto** kusudi wasafiri waweze kukausha mavazi yao na kupata moto kwani **mvua** ilinyesha vilevile.

**28:3** Wakati **Paulo** alipokuwa akisaidia na kuni kwa **moto,** nyoka yenye

sumu ilimwuma. Ni kama nyoka ile alikuwa akilala ndani ya mbao zilizoachwa kwa pwani wakati maji yaliporudi baharini. Wakati kuni zilipowekwa **juu ya moto**, **nyoka** ilifufuka mbio, **ikafungana na mkono** wa mtume na kumwuma.

**28:4-6** Kwanza wenyeji wa kisanga walifikiri bila shaka kwamba Paulo alikuwa **mwuaji**. Alikuwa **amepona** saa ya kuharibika kwa merikebu, lakini **haki** haikumwacha kuishi. Waliwaza mwili wake **utavimba** nyuma kidogo, au kwamba **gafula ataanguka maiti.** Lakini wakati walipoona ya kuwa Paulo hakuumizwa na sumu ya nyoka, **waligeuza mawazo yao**, wakafikiri **yeye ni mungu!** Ni mfano mwingine wa kugeukageuka kwa roho na nia za watu.

**28:7** **Mkubwa wa kisanga** cha Melita kwa wakati ule alikuwa **Publio**. Mtu huyu alikuwa na mashamba mengi kwa upande wa pwani pahali wasafiri walipotoka baharini. Mroma mtajiri huyu **alipokea** Paulo na rafiki zake na **adabu** kama wageni wake **kwa siku tatu,** kufika saa walipoweza kupata pahali pa kupanga kwa wakati wa majira ya baridi.

**28:8** Mtaifa huyu hakukosa kupokea zawabu kwa wema wake. Kwa wakati ule **baba** yake alishikwa na **ugonjwa wa homa na kuhala damu**. **Paulo alimfikia na aliomba, akaweka mikono juu yake, akamponyesha.**

**28:9,10** Habari za ajabu hili ya kuponyeshwa zilienea mbio katika **kisanga**. Kwa miezi mitatu iliyofuata watu walifikisha wagonjwa wao karibu na Paulo, nao wote waliponyeshwa. Watu wa Melita walionyesha asante yao kwa Paulo na Luka[13] wakati walipoendelea na safari yao kwa njia ya kuwaonyeshea heshima nyingi na kuwaletea zawadi za vitu ambavyo vitawasaidia kwa safari yao kwenda Roma.

**28:11** **Nyuma ya miezi mitatu** wakati wa baridi ulipita na haikuwa hatari tena kusafiri baharini. Halafu akida na wafungwa wake waliingia merikebu ya **Alesanduria … iliyoshinda kwa Melita vilevile kwa wakati wa baridi. Alama ya merikebu hii** ilikuwa **Mapasa Wanaume.** Majina ya wapasa haya yalikuwa Kastor na Pollux. Wabaharia wapagano walitegemea miungu hii kuwalinda.

**28:12-14** Toka Melita walisafiri karibu km. 130 kufikia **Sirakuse,** mji mkubwa wa kisanga cha Sicili kwa pwani yake ya mashariki. Walibaki pale kwa **siku tatu,** kisha waliendelea na safari yao kwenda **Regio,** kwa upande wa kusini-mangaribi wa Italia. Kesho yake **upepo** mzuri **toka kusini ulivuma** ambao uliwawezesha kusafiri kwa km. 290 kwenda kaskazini karibu na pwani ya mangaribi ya Italia na kufikia **Puteoli**. Mji huu ulikuwa karibu km. 240 toka **Roma,** kwa upande wake wa kusini-mashariki. Paulo **alikuta ndugu** Wakristo pale, akaweza kushinda pamoja nao kwa **siku saba.**

**28:15** Hatujui namna gani habari za kufika kwa Paulo kwa Puteoli zilifikia Roma, lakini mafungu mawili ya **ndugu** walishika njia **kukutana naye.** Fungu moja walisafiri km. 69 toka Roma kwa upande wa kusini-mashariki na kufikia **Soko la Apio**. Fungu la pili walisafiri km. 53 kwenda kusini-mashariki kwa **Nyumba Tatu za Wageni**. Kufika kwao kukutana naye kulisaidia roho ya **Paulo** sana na alishukuru Mungu kwa mapendo ya waamini wa Roma.

**28:16** Wakati wafungwa walipofikia **Roma**, akida aliyesafiri pamoja nao aliwatia katika mikono ya mkubwa wa walinzi, lakini **Paulo alipewa ruhusa kukaa kwake** nyumbani **pamoja na askari ambaye alimlinda.**

### J. Paulo, akifungwa nyumbani, ana kushuhudia Wayuda katika Roma (28:17-31)

**28:17-19** Ilikuwa desturi ya **Paulo** kutoa ushuhuda kwanza kwa **Wayuda**,

hivi aliomba **viongozi vyao vya dini** kumfikia. **Wakati walipokutana kwake** nyumbani aliyolipia kodi, **aliwaelezea** habari zake. Aliwaambia kwamba **hakutendea** Wayuda **neno baya**, wala **desturi** zao, lakini **Wayuda** katika **Yerusalema walimtoa kwa mikono ya Waroma** wamhukumu. Wenye amri ya Mataifa hawakuona kosa ndani yake, na walitaka kumfungua, **lakini Wayuda waligombana juu ya shauri hili**, hivi mtume **alilazimishwa kuomba Kaisari** kusikia maneno yake. Kusudi lake halikuwa kushitaki **taifa** la Wayuda**,** lakini kujisimamia mwenyewe.

**28:20** Paulo hakutendea Wayuda mabaya yo yote na kwa sababu hii **aliita** wakubwa wa Wayuda wa Roma kukutana kwake. Alikuwa **amefungwa kwa mnyororo kwa sababu ya tumaini la Israeli.** Kama tulivyoeleza mbele, **tumaini la Israeli** ndilo kutimizwa kwa ahadi wazee Wayuda wenye heshima walizopewa, zaidi juu ya Masiya. Sehemu ya ahadi hizi ilikuwa ufufuko wa wafu.

**28:21, 22** Viongozi Wayuda walisema hawakujua habari za mtume Paulo. **Hawakupokea barua toka Yudea na habari zake,** na hata mmoja wa Wayuda wenzao hakurudi kwao na habari mbaya juu yake. Lakini walitaka Paulo kuwaambia habari nyingine, kwa sababu walijua watu kwa **kila pahali walisema maneno mabaya** juu ya dini ya Wakristo.

**28:23** Nyuma ya muda fulani wengi wa Wayuda walifikia pahali **Paulo alipopanga** kusudi waweze kusikia habari nyingine toka kwake. Paulo aliwafundisha na kushuhudia **ufalme wa Mungu,** na kuwaonya **juu ya Yesu**. Alitaja mbele yao mashairi toka **Sheria ya Musa na Manabii, tangu asubui hata mangaribi.**

**28:24** Wengine waliamini habari za Paulo, na wengine **hawakuziamini**, maana walikataa kabisa.

**28:25-28** Wakati **Paulo** alipoona kwamba zaidi ya Wayuda walikataa Habari Njema, alitaja Isa. 6:9-10, pahali nabii alipoagizwa kuhubiri kwa **watu** wenye **mioyo isiyofahamu**, wenye **masikio** mazito, na **macho** yasiyoona. Roho ya mtume ilivunjika tena wakati alipohubiri Habari Njema kwa watu ambao hawakutaka kuisikia. Hivi kwa sababu Wayuda walikataa Habari Njema tena, **Paulo** alitangaza kwamba ataipeleka kwa **Mataifa.** Aliamini kabisa kwamba **Mataifa wataisikia** na kuipokea.

**28:29** Basi **Wayuda** wasioamini **walikwenda zao wakiulizana sana katikati yao.** Mwalimu Calvin alionyesha kwamba walikasirishwa sana wakati Paulo alipowashitaki na kutaja unabii juu ya Masiya. Walikuwa na gazabu kubwa kwa Wayuda wale ambao walipokea.

> Calvin alisema vilevile kwamba haifai kusema Habari Njema inaleta magomvi. Magomvi haya ndiyo tunda la mioyo migumu ya watu. Tukitaka kuwa na salama na Mungu, ni lazima kwa sisi kushindana na wale ambao wanamzarau.

**28:30** Nyuma ya maneno haya **Paulo** alibaki katika Roma kwa **miaka miwili mizima**, akikaa ndani ya nyumba ambayo alilipa. Alikaribisha watu wengi waliofika kusemezana naye. Tunafikiri aliandika barua kwa Waefeso, Wafilipi, Wakolosayi, na Filemono kwa wakati ule.

**28:31** Aliweza **kuhubiri habari za ufalme wa Mungu bila mazuizo, na kufundisha watu maneno ya Bwana Yesu, kwa uhodari wote, na hakuna mtu ambaye alimkataza.**

Tumefikia mwisho wa kitabu cha Matendo. Kama tulivyosoma kwa mwanzo wake, kusudi la Bwana lilitimizwa na Habari Njema ilihubiriwa kwa Yerusalema, Yudea, Samaria, na sasa kwa Mataifa vilevile.

Habari za maisha ya Paulo nyuma ya

mwisho wa Matendo hazikuandikwa waziwazi. Tunaweza kutambua nusu nusu tu kwa njia ya barua alizoandika nyuma ya wakati ule.

Ni kama nyuma ya kushinda miaka miwili kwa Roma, mashitaki yake yaliletwa mbele ya Nero, na Paulo alifunguliwa bila kuhukumiwa.

Kisha alianza safari nyingine ya kuhubiri, ndiyo safari yake ya ine. Tunawaza alifika pahali pale:

1. Kolosayi na Efeso (Flm. 22)
2. Makedonia (1 Tim. 1:3; Flp. 1:25; 2:4)
3. Efeso (1 Tim. 3:14)
4. Spania (Rom. 15:24)
5. Krete (Tit. 1:5)
6. Korinto (2 Tim. 4:20)
7. Mileto (2 Tim. 4:20)
8. Nikopoli kwa wakati wa baridi (Tit. 3:12)
9. Troa (2 Tim. 4:13)

Hatujui kwa sababu gani, wakati gani au pahali gani alipofungwa tena, lakini alipelekwa kwa Roma mara ya pili. Mara ile aliteswa kupita mara ya kwanza (2 Tim. 2:9). Zaidi ya rafiki zake walimwacha (2 Tim. 4:9-11), naye alijua kwamba mauti yake ilikuwa karibu (2 Tim. 4:6-8).

Maandiko mengine ya zamani yanaonyesha kwamba alikatiwa kichwa inje ya Roma kwa A.D. 67 au 68. Paulo alipasha habari za maisha yake kwa 2 Kor. 4:8-10; 6:4-10 na 11:23-28. Soma mashairi haya pamoja na mafundisho ndani ya kitabu hiki.

## MAFUNDISHO JUU YA HABARI ZA MATENDO

Nyuma ya kusoma Kitabu cha Matendo, ni vizuri kuwaza juu ya mafundisho na matendo ya Wakristo wa kwanza. *Maneno gani yanaonekana zaidi ndani ya maisha ya Wakristo mmoja mmoja, na ndani ya makanisa pahali walipokusanyika?*

Neno la kwanza tunaloona ni ya kwamba Wakristo walioishi kwa muda wa miaka mia ya kwanza waliweka maneno ya Bwana Yesu kwanza. Walikumbuka Kristo ndani ya maneno yote waliyofanya. Kusudi kubwa la maisha yao lilikuwa kushuhudia Mwokozi, nao walijitoa na bidii kwa kazi hii. Hata wakizungukwa na watu wa dunia walioweka roho juu ya kujipatia mahitaji yao wenyewe tu, kulikuwa na fungu la Wakristo wenye bidii sana walioweka ufalme wa Mungu na haki yake kwanza. Mwito huu wa utukufu ulikuwa neno kubwa kupita maneno yote mengine ndani ya maisha yao.

Mahubiri yao yalikuwa juu ya ufufuko na utukufu wa Bwana Yesu Kristo. Walishuhudia Mwokozi aliyekwisha kufufuliwa. Watu walikuwa wameua Masiya, lakini Mungu alikuwa amemfufua toka wafu na kumpa pahali pa juu zaidi mbinguni. Itakuwa lazima kwa kila mtu kuinama mbele yake, ndiye Mtu aliyetukuzwa kwa mkono wa kuume wa Mungu. Hakuna njia nyingine kupata wokovu.

Hata walikaa katikati ya wenye chuki, uchungu, na choyo, wanafunzi walionyesha mapendo kwa watu wote. Walitendea mema wale ambao waliwatesa na waliombea wale waliopigana nao. Adui zao waliona mapendo yao kwa Wakristo wenzao, walilazimishwa kusema, “Ona namna Wakristo hawa wanavyopendana!”

Ni kama Wakristo hawa wa kwanza walijinyima vitu vizuri kwa kusaidia Habari Njema kutangazwa. Hawakuhesabu vitu vyao kuwa mali yao wenyewe, lakini kama uwakili toka Mungu. Pahali gani watu walikuwa na hitaji fulani, kulikuwa na mali kuwasaidia.

Silaha zao hazikuwa za mwili, lakini zilikuwa za uwezo katika Mungu kuangusha maboma ya vita. Walifahamu kwamba hawakupigana na viongozi vya dini au serikali, lakini na falme na ma-

mlaka katika pahali pa mbingu. Basi walitoka kupiga vita na silaha ya imani, maombi, na Neno la Mungu. Hesabu ya Wakristo haikuongezeka kwa sababu ya jeuri, kama hesabu ya wafuata wa dini nyingine.

Wakristo hawa walikaa mbali na dunia. Walikaa duniani na kushuhudia wasioamini, lakini hawakushiriki na watu wa dunia ndani ya maisha yao ya zambi na anasa. Kama wasafiri na wageni, walisafiri ndani ya inchi ya kigeni wakijaribu kuwa baraka kwa watu wote bila kuchafuwa nao.

Wakristo hawakushiriki ndani ya kazi ya kutawala inchi kujaribu kutengeneza desturi mbovu za watu. Waliamini kwamba uovu na matendo mabaya yote duniani ni tunda la uovu wa tabia ya zambi ya watu, na ya kwamba Habari Njema tu inaweza kuigeuza. Hivi walikaa kuhubiri Habari Njema saa zote. Pahali pote Habari Njema ilipohubiriwa desturi za zambi za watu zilipunguka au kuondoshwa.

Hawakushangaa wakati walipopata mateso. Bwana aliwafundisha mbele kwamba watateswa. Hawakulipa maovu na maovu au kujaribu kujipigania, lakini walitia maneno haya kwa mikono ya Mungu, anayehukumu kwa haki. Hawakujaribu kuepuka mateso, lakini waliomba Mungu kuwapa uhodari kutangaza Kristo kwa watu wote ambao walikutana nao.

Kusudi la wanafunzi lilikuwa kwa dunia nzima kusikia Habari Njema. Hawakufikiri inchi na taifa lao wenyewe tu, lakini ulimwengu pia. Lakini hawakuhubiri Habari Njema ili watu waokolewe tu, na kuacha waamini wa sasa kuhangaika peke yao. Walikutanisha waamini ndani ya makanisa ya Wakristo waweze kufundishwa Neno la Mungu, na kupatishwa nguvu katika maombi na imani. Nyuma yake ilipasa waamini hawa wa sasa kwenda kuhubiri Habari Njema kwa watu wengine.

Kusimamisha makanisa haya kulipatisha kazi ya Mungu nguvu na kusaidia waamini kuhubiri Habari Njema kwa inchi kando kando. Waamini wa makanisa haya waliyaongoza wao wenyewe na kuyaendelesha kuanza makanisa mengine ndani ya inchi kando kando, wakitumika na mali yao wenyewe. Walikuwa na ushirika na waamini wa makanisa mwengine, lakini chama kubwa haikuwa kuwaongoza na kuwasaidia na mali.

Makanisa yalikuwa pahali Wakristo walipokutana na kusaidiana na kujengana katika roho, si pahali kwa kuhubiri Habari Njema. Ni pahali walipokutana kwa karamu ya ukumbusho, kuabudu, maombi, kujifunza Biblia, na ushirika. Habari Njema ilihubiriwa kila pahali waamini walipopata njia kusema na wasioamini – ndani ya masunagogi, sokoni, njiani, gerezani, na ndani ya nyumba za watu mmoja mmoja.

Makanisa hayakuwa na nyumba zilizojengwa kwa Wakristo kukutana ndani yao. Walikusanyika ndani ya nyumba za waamini. Neno hili liliwasaidia sana wakati wa mateso, na kuwawezesha kufichama upesi.

Kwa mwanzo wa kanisa waamini wote walijulikana kama viungo vya mwili wa Kristo, na kanisa la pahali fulani lilikuwa mfano wa kanisa zima la dunia.

Tofauti haikuwa katikati ya waamini. Hakuna mtu aliyekuwa na ruhusa peke yake kufundisha neno la Mungu kanisani, na kuhubiri, kubatiza watu au kuongoza meza ya Bwana. Walifahamu kwamba kila mwamini alipewa zawadi fulani, na alikuwa na ruhusa kutumikia Mungu na zawadi hii.

Wale waliopewa zawadi ya mtume, nabii, mhubiri wa Habari Njema, mchungaji au mwalimu hawakujitafutia ukubwa na kujaribu kuwa viongozi vya lazima vya kanisa lao. Kazi yao ilikuwa kupatisha waamini nguvu katika imani,

ili wao vilevile waweze kutumikia Bwana kila siku. Wanaume wa wakati wa Agano Jipya walipewa zawadi hizi na Roho Mtakatifu. Kwa sababu hii wanaume wasiokuwa na elimu ya dunia waliweza kufanya kazi kubwa kanisani.

Ndani ya kitabu cha Matendo, Habari Njema ilihubiriwa pamoja na maajabu na maalama ya Roho Mtakatifu mara nyingi. Maneno haya yalionekana kupita kwa mwanzo wa kitabu hiki, lakini yaliendelea hata mwisho wake.

Wakati kanisa lilipokwisha kusimama na kuendelea kwa wakati, mitume au wajumbe wao walichagua waamini wengine kuwa wazee, ndio wasimamizi waliochunga kundi la waamini. Kila kanisa lilikuwa na wazee kupita mmoja.

Ndani ya Matendo tunasoma juu ya watumishi ndani ya makanisa waliotumikia Bwana kwa njia ya kusaidia na kazi namna namna.

Waamini wa kwanza walibatizwa kwa njia ya kuzimishwa mwili mzima ndani ya maji. Ni kama walibatizwa muda mfupi tu nyuma ya kuokolewa. Siku ya kwanza ya juma wanafunzi walikusanyika kukumbuka Bwana kwa njia ya kuvunja mkate. Ni kama walifanya hivi bila kuwa na kawaida namna tuliyo nayo sasa, na ya kama pamoja na kuvunja mkate kukumbuka kufa kwa Bwana wao walikula chakula vilevile, ndiyo karamu ya mapendo.

Waamini walijitoa kabisa kwa maombi, na kupata toka Mungu kuongozwa na uwezo. Waliomba na imani na bidii. Walifunga chakula vilevile ili waweze kuweka mafikiri yao yote juu ya maombi bila kuhangaishwa na mawazo mengine au kushindwa na usingizi.

Nyuma ya wakati wa kukaa na maombi na kufunga, manabii na walimu kwa Antiokia walitenga Barnaba na Saulo kwenda kuhubiri Habari Njema kwa wasioamini pahali pengine. Wao wawili walikuwa wametumikia Bwana kwa wakati mbele ya saa ile. Kwa njia ya kufanya hivi viongozi kwa Antiokia walionyesha ukubali wao kwamba Roho Mtakatifu aliwaita kweli. Lilikuwa vilevile tendo kuonyesha ushirika wa kanisa zima na kazi Barnaba na Saulo waliyokwenda kufanya.

Watu hawa waliokwenda kuhubiri Habari Njema hawakutawaliwa na kanisa lao ndani ya kazi yao. Ni kama waliweza kufanya kazi waliyoongozwa na Roho Mtakatifu kufanya. Lakini walirudia kanisa lao kwa Antiokia na kuwaambia namna Mungu alivyobariki mahubiri yao.

Kanisa halikutengenezwa kuwa na utaratibu fulani kwa maneno yote. Lilikuwa kama kitu chenye uhai kilichofuata maongozi ya Bwana saa zote. Kichwa cha kanisa, Kristo mbinguni, aliongoza watu, nao walijaribu kutii. Hivi hatuoni ndani ya kitabu cha Matendo utaratibu fulani mmoja kwa makusanyiko ya makanisa yote, lakini makusanyiko yalikuwa mbalimbali kidogo. Haikuwa lazima kwa mtume kukaa kwa kanisa fulani kwa muda fulani. Hivi Paulo alishinda miezi mitatu kwa Tesalonika na miaka mitatu kwa Efeso, kupatana na muda uliohitajiwa kutayarisha waamini kuendesha kazi ya kanisa hili wao wenyewe.

Watu wengine wanafikiri mitume waliweka roho zaidi juu ya kazi ya kuhubiri Habari Njema ndani ya miji mikubwa, na kutegemea makanisa ya pahali pale kwenda kutangaza Habari Njema kwa vijiji kando kando. Neno hili ni kweli? Hii ilikuwa kweli desturi yao, au walitii kila siku maagizo na maongozi ya Bwana, au kuhubiri katika miji mikubwa, au kwa watu ndani ya vijiji vidogo?

Neno moja linaloonekana wazi ndani ya kitabu cha Matendo ndilo hili: waamini wa kwanza walitazamia na kutegemea Bwana kuwaongoza. Walikuwa wameacha vyote kwa ajili

ya Kristo. Walibaki na Bwana tu. Hivi walimtazamia yeye tu kuwaongoza kila siku.

Ni kama ilikuwa desturi kwa wakati ule wa mwanzo kwa wahubiri wawili kusafiri pamoja. Mara nyingi mmoja wao alikuwa kijana na alijifunza karibu na mkubwa wake. Mitume walikuwa wakitafuta saa zote vijana ambao waliweza kufundisha.

Mara nyingine watumishi wa Bwana walitumika kazi kwa kujipatia mali kwa mahitaji wao. Mara nyingine waamini au makanisa waliwasaidia na zawadi zao za mapendo.

Waamini wa kanisa walitambua wanani katikati yao walikuwa viongozi kwa maneno ya Mungu. Alikuwa Roho Mtakatifu ambaye aliwawezesha kusema na amri. Na alikuwa Roho Mtakatifu vilevile aliyeweka ndani ya waamini roho kunyenyekea amri yao.

Waamini walitii serikali ila wakati walipokatazwa kuhubiri Habari Njema. Halafu walitii Mungu, si watu. Wakiazibiwa na serikali, walibeba azabu hii bila ukaidi, na bila kufanya shauri kamwe kushindana na serikali.

Habari Njema ilihubiriwa kwanza kwa Wayuda, lakini wakati taifa la Israeli hawakuipokea, ilihubiriwa kwa Mataifa. Kwa wakati wa sasa Wayuda na Mataifa ni sawa mbele ya Mungu – hakuna tofauti, "kwa sababu *wote* wamefanya zambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu."

Uwezo wa Mungu ulionekana wazi ndani ya kanisa kwa wakati wa mwanzo. Watu waliogopa kukasirisha Mungu, hivi hawakukiri kwa haraka kuwa Wakristo. Zambi kanisani ilifunuliwa mbio, na mara nyingine Mungu aliiazibu na ukali sana, kwa mfano zambi ya Anania na Safira.

Kwa kumaliza, nyuma ya kusoma na kujifunza kitabu cha Matendo, tunaamini kwamba:

Kama *sisi* tukiiga mfano wa kanisa la mwanzo, kwa maneno ya imani, kujitoa pia kwa kazi ya Mungu, mapendo, na utumishi bila kuchoka, dunia nzima ingeweza kusikia Habari Njema kwa kizazi chetu. ❖

## Notes

[1] (2:39) Charles H Spurgeon, *The Treasury of the New Testament,* 1:530

[2] (2:44,45) F.W. Grant, "Acts," *The Numerical Bible: Acts to 2 Corinthians,* VI:25,26.

[3] (2:46) Whenever we read of Paul and others going into the temple, it means into the temple *courts*, not into the sanctuary. Only the priests could enter there. Gentiles were permitted to go only into the outer court; to venture further was punishable by death.

[4] (4:13) James A. Stewart, *Evangelism*, p. 95.

[5] (4:14-18) J. H. Jowett, *The Redeemed Family of God,* p. 137.

[6] (7:20-43) Daily Notes of the Scripture Union, May 31, 1969.

[7] (8:27-29) Male servants of female dignitaries were sometimes castrated. Eunuchs were barred from first class citizens in Judaism (Deut. 23:1). They were limited to the status of "proselytes of the gate." But here a eunuch becomes a full-fledged member of the Christian Church.

[8] (8:27-29) *Candace* (or *Kandake*) is probably a title, like Pharaoh, rather than a personal name.

[9] (8:40) Ethiopia is the only country in Africa with a continuous Christian tradition from earliest times to today. Philip's faithfulness was perhaps the key that unlocked the door for the church there.

[10] (13:48) Charles R. Erdman, *The Epistle of Paul to the Romans,* p. 109.

[11] (15:20) Some think that the four for-

bidden practices refer back to Leviticus 17 and 18, as follows: things polluted by idols (17:8,9); sexual immorality – not only adultery and polygamy (18:20), homosexuality (18:22), and bestiality (18:23), but also marrying blood relatives (18:6-14), and even relatives by mariage, that is, relatives by marriage, that is, in-law relatives (18:15,16); eating things strangled or improperly butchered (17:15); eating blood (Lev. 17:10-12). Jewish believers would be offended if they saw Gentile believers violating these codes (Acts 15:21)

[12] (16:6-8) Ryrie, *Acts,* pp. 88, 89.

[13] (16:9) James Stalker, *Life of St. Paul*, p. 78.

[14] (16:19-24) J. Pollock, *The Apostle Paul and His Missionary Labors*, p. 56.

[15] (16:25) G. Campbell Morgan, *The Acts of the Apostles,* pp. 389-390.